# Kitabu cha Mormoni

## Ushuhuda Mwingine wa Yesu Kristo

Study edition © 2017 by Benjamin Crowder. All rights reserved.

Text of the Book of Mormon © 2017 by Intellectual Reserve, Inc. All rights reserved.

*The text of this study edition is licensed from The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints with the following disclaimer: The Product offered by Benjamin Crowder is neither made, provided, approved, nor endorsed by, Intellectual Reserve, Inc. or The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints. Any content or opinions expressed, implied, or included in or with the Product offered by Benjamin Crowder are solely those of Benjamin Crowder and not those of Intellectual Reserve, Inc. or The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints.*

http://bencrowder.net/mormon/book-of-mormon/study-edition/

Version 2.0, published August 2017

# Kitabu cha Mormoni

## Historia Iliyoandikwa kwa Mkono wa Mormoni Kwenye Bamba Zilizochukuliwa kutoka Bamba za Nefi

Kwa hivyo, huu ni ufupisho wa maandishi ya watu wa Nefi, na pia ya Walamani — Iliyoandikiwa Walamani, ambao ni sazo la nyumba ya Israeli; na pia kwa Myahudi na kwa Myunani — Imeandikwa kutokana na amri, na pia kwa roho ya unabii na ufunuo — Imeandikwa na kufungwa, na kufichwa katika Bwana, ili isiharibiwe — Ipate kutolewa kwa karama na uwezo wa Mungu na hata utafsiri wake — Ulifungwa kwa mkono wa Moroni, na kufichwa katika Bwana, ili ije itolewe wakati wa kufaa kupitia Myunani — Na kutafsiriwa kwa karama ya Mungu.

Na pia ufupisho kutoka kitabu cha Etheri pia, ambayo ni maandishi kuhusu watu wa Yaredi, ambao walitawanyishwa wakati Bwana alipochanganyisha lugha za watu, walipokuwa wakijenga mnara ili wafike mbinguni — Ambayo ni kuonyesha sazo la nyumba ya Israeli vitu vikubwa ambavyo Bwana aliwatendea baba zao; na ili wajue maagano ya Bwana, kuwa hawakutupiliwa mbali milele — Na pia kuwathibitishia Myahudi na Myunani kwamba Yesu ndiye Kristo, Mungu wa Milele, anayejidhihirisha kwa mataifa yote — Na sasa, kama kuna makosa ni hitilafu ya wanadamu; kwa hivyo, usilaumu vitu vya Mungu, ili usipatikane na doa kwenye kiti cha hukumu cha Kristo.

Tafsiri asili ya Kiingereza kutoka kwa bamba na Joseph Smith, Mdogo

Nakala ya kwanza ya Kiingereza ilichapishwa Palmyra, New York, USA, katika 1830

# Kitabu cha Kwanza cha Nefi

## Utawala na Huduma Yake

*Historia ya Lehi na mkewe Saria, na wanawe wanne, wanaoitwa, (kuanzia kifungua mimba) Lamani, Lemueli, Samu, na Nefi. Bwana anamwonya Lehi aondoke kutoka nchi ya Yerusalemu, kwa sababu alitoa unabii kuhusu maovu ya watu nao wanatafuta kutoa uhai wake. Anaelekea nyikani na kusafiri kwa siku tatu akiwa na jamii yake. Nefi anawachukua kaka zake na kurejea nchi ya Yerusalemu kuchukua maandishi ya Wayahudi. Historia ya mateso yao. Wanawaoa mabinti za Ishmaeli. Wanachukua jamaa zao na kuelekea nyikani. Mateso na masumbuko yao wakati wakiwa nyikani. Njia zao safarini. Wanafikia maji makubwa. Kaka za Nefi wanamuasi. Anawafadhaisha, na kujenga merikebu. Walipaita pahali pa Neema. Wanavuka bahari na kufika katika nchi ya ahadi, na hali kadhalika. Haya ni kulingana na historia ya Nefi; hii ina maana kwamba, mimi, Nefi, ndiye niliyeandika maandishi haya.*

## 1 Nefi 1

1 Mimi, Nefi, nikiwa nimezaliwa na wazazi wema, kwa hivyo nilikuwa nimefunzwa
karibu yote ambayo baba yangu alijua; na baada ya kushuhudia masumbuko mengi
maisha mwangu, haidhuru, nikiwa nimebarikiwa na Bwana maishani mwangu;
ndio, nikiwa nimepokea ufahamu wa wema na siri za Mungu, kwa hivyo naandika
maandishi juu ya mambo ya maisha yangu.
2 Ndio, naandika maandishi kwa lugha ya baba yangu, ambayo ni pamoja na elimu
ya Wayahudi na lugha ya Wamisri.
3 Na ninajua kwamba maandishi ambayo ninaandika ni ya kweli; na ninayaandika
kwa mkono wangu; na ninayaandika kadiri nijuavyo.
4 Kwani ikawa mwanzoni mwa mwaka wa kwanza wa utawala wa Zedekia, mfalme
wa Yuda, (baba yangu, Lehi, akiwa ameishi katika Yerusalemu maisha yake yote); na
katika mwaka huo walikuja manabii wengi, wakitoa unabii na kuwaambia watu
kwamba lazima watubu, au sivyo mji mkuu wa Yerusalemu lazima uangamizwe.
5 Kwa hivyo ikawa baba yangu, Lehi, aliendelea mbele aliomba dua kwa Bwana,
ndio, hata na moyo wake wote, kwa niaba ya watu wake.
6 Na ikawa alipokuwa akimwomba Bwana, palitokea moto mfano wa nguzo na
ukatua juu ya mwamba uliokuwa mbele yake; na akaona na kusikia mengi; na kwa
sababu ya vitu alivyoona na kusikia alitetemeka na kutapatapa kupita kiasi.
7 Na ikawa kwamba alirejea nyumbani kwake Yerusalemu; na akajitupa kitandani
mwake, akiwa amelemewa na Roho na vitu alivyoviona.
8 Na ikiwa amelemewa na Roho, alichukuliwa kwa ono, hata kwamba aliona
mbingu zikifunguka, na akadhani kuwa alimwona Mungu ameketi kwenye kiti
chake cha enzi, akizingirwa na malaika wasio na idadi wakiwa katika hali ya
kumwimbia na kumsifu Mungu wao.
9 Na ikawa kwamba alimwona Mmoja akishuka kutoka katikati ya mbingu, na

akaona mng'aro wake ulikuwa zaidi ya jua la adhuhuri.
10 Na pia akaona wengine kumi na wawili wakimfuata, na mng'aro wao ulikuwa
zaidi ya ule wa nyota angani.
11 Na wakaja chini na wakatembea usoni mwa dunia; na wa kwanza akaja na
kusimama mbele ya baba yangu, na akampatia kitabu, na akamwamuru asome.
12 Na ikawa alipokuwa akisoma, alijazwa na Roho wa Bwana.
13 Na akasoma, akisema: Ole, ole kwa Yerusalemu, kwani nimeona machukizo
yako! Ndio, na vitu vingi vilisomwa na baba yangu kuhusu Yerusalemu—kwamba
itaangamizwa, na wenyeji wake pia; wengi wangekufa kwa upanga, na wengi
wangetekwa nyara na kupelekwa Babilonia.
14 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu kusoma na kuona vitu vingi vikubwa na
vya ajabu, alipaza sauti kwa Bwana akisema vitu vingi; kama: Kazi zako ni kuu na za
ajabu, Ewe Bwana Mungu Mwenyezi! Kiti chako cha enzi kiko juu mbinguni, na
nguvu zako, na wema wako, na rehema zako ziko juu ya wakazi wote wa dunia; na,
kwa sababu una huruma, hutakubali wale ambao watakuja kwako waangamie!
15 Na baba yangu alitumia maneno kama haya kwa kumsifu Mungu wake; kwani
nafsi yake ilishangilia, na moyo wake wote ulijaa furaha, kwa sababu ya vitu vile
alivyokuwa ameona, ndio, vile Bwana alivyokuwa amemwonyesha.
16 Na sasa mimi, Nefi, siandiki maandishi yote ambayo baba yangu aliandika, kwani
ameandika vitu vingi ambavyo aliona kwa maono na kwa ndoto; na pia ameandika
vitu vingi ambavyo alitoa unabii na kuwaambia watoto wake, ambayo mimi
sitaandika yote.
17 Lakini nitaandika maandishi ya matendo yangu maishani mwangu. Tazama,
ninafupisha maandishi ya baba yangu, na kuyaandika katika bamba ambazo
nilitengeneza kwa mikono yangu mwenyewe; kwa hivyo, baada ya kufupisha
maandishi ya baba yangu ndipo nitaandika maandishi kuhusu maisha yangu.
18 Kwa hivyo, ningetaka mjue, kwamba baada ya Bwana kumwonyesha baba yangu,
Lehi, vitu vingi vya ajabu, ndio, kuhusu kuangamizwa kwa Yerusalemu, tazama
alienda miongoni mwa watu, na akaanza kutoa unabii na kuwatangazia vile vitu
alivyokuwa ameviona na kusikia.
19 Na ikawa kuwa Wayahudi walimfanyia mzaha kwa sababu ya vitu vile
alivyowashuhudia; kwa kweli aliwashuhudia kuhusu uovu wao na machukizo yao;
na akawashuhudia kwamba vitu vile ambavyo alivyokuwa ameviona na kusikia, na
pia vitu ambavyo alikuwa amesoma katika kitabu, vilidhihirisha wazi kuja kwa
Masiya, na pia ukombozi wa ulimwengu.
20 Na wakati Wayahudi waliposikia vitu hivi, walimkasirikia; ndio, jinsi ilivyokuwa
kwa manabii wa kale, ambao walikuwa wamewatupa nje, na kuwapiga kwa mawe, na
kuwaua; na pia walimtafuta ili watoe uhai wake. Lakini tazama, mimi, Nefi,
nitawaonyesha nyinyi kuwa Bwana ana huruma nyororo juu ya wale ambao
amewachagua, kwa sababu ya imani yao, kuwatia nguvu hata kwenye uwezo wa
ukombozi.

## 1 Nefi 2

1 Kwani tazama, ikawa kuwa Bwana alimzungumzia baba yangu, ndio, hata katika
ndoto, na akamwambia: Umebarikiwa ewe Lehi, kwa sababu ya vitu ambavyo
umetenda; na kwa sababu umekuwa mwaminifu na kuwatangazia hawa watu vile

vitu nilivyokuamrisha, tazama, wanakutafuta watoe uhai wako.
2 Na ikawa kuwa Bwana akamwamrisha baba yangu, hata kwenye ndoto, kuwa
aichukue jamii yake na aelekee nyikani.
3 Na ikawa kuwa alikuwa mtiifu kwa neno la Bwana, kwa hivyo alitenda kulingana
na yale Bwana aliyomwamuru.
4 Na ikawa kuwa akatoka na kuelekea nyikani. Na akaacha nyumba yake, na nchi
yake ya urithi, na dhahabu yake, na fedha yake, na vitu vyake vya thamani, na
hakubeba chochote, isipokuwa jamii yake, na maakuli, pamoja na mahema, na
akaelekea nyikani.
5 Na akashuka mipakani karibu na ufuko wa Bahari ya Shamu; na akasafiri nyikani
mipakani ambayo imekaribia Bahari ya Shamu; na akasafiri nyikani na jamii yake,
ambayo ilikuwa ni mama yangu, Saria, na kaka zangu wakubwa ambao walikuwa ni
Lamani, Lemueli, na Samu.
6 Na ikawa kuwa baada ya yeye kusafiri nyikani kwa siku tatu, alipiga hema lake
bondeni kando ya mto wa maji.
7 Na ikawa kwamba alijenga madhabahu ya mawe, na akamtolea Bwana dhabihu,
na kumshukuru Bwana Mungu wetu.
8 Na ikawa kwamba aliuita ule mto, Lamani, na ulitiririka ukielekea Bahari ya
Shamu; na bonde lilikuwa mipakani karibu na kinywa cha huo mto.
9 Na wakati baba yangu alipoona kwamba maji ya ule mto yalitiririka kwenye
chemchemi ya Bahari ya Shamu, alimzungumzia Lamani, na kusema: Ee kwamba
uwe kama mto huu, daima ukitiririka kwenye chemchemi ya haki yote!
10 Na pia akamzungumzia Lemueli: Ee kwamba uwe kama bonde hili, imara na
thabiti, na asiyetingishika kwa kuweka amri za Bwana!
11 Sasa aliyazungumza haya kwa sababu ya ugumu wa Lamani na Lemueli; kwani
tazama walinung'unika kwa vitu vingi dhidi ya baba yao, kwa sababu alikuwa ni mtu
wa maono, na alikuwa amewatoa kutoka nchi ya Yerusalemu, kuacha nchi yao ya
urithi, na dhahabu zao, na fedha zao, na vitu vyao vya thamani, kuangamia nyikani.
Na wakasema alikuwa ametenda haya kwa sababu ya mafikira ya ujinga moyoni
mwake.
12 Na hivyo ndivyo Lamani na Lemueli, wakiwa wakubwa, walivyonung'unika
dhidi ya baba yao. Na walinung'unika kwa sababu hawakujua matendo ya yule
Mungu aliyewaumba.
13 Wala hawakuamini kuwa Yerusalemu, mji ule mkuu, ungeangamizwa kulingana
na maneno ya manabii. Na walikuwa kama Wayahudi waliokuwa Yerusalemu,
ambao walimtafuta baba yangu wakitaka kumtoa uhai wake.
14 Na ikawa kwamba baba yangu akawazungumzia katika bonde la Lemueli, kwa
nguvu, akiwa amejazwa na Roho, hadi miili yao ikatetemeka mbele yake. Na
aliwafadhaisha, kwamba hawakunena lolote kinyume chake; kwa hivyo, wakatenda
alivyowaamrisha.
15 Na baba yangu aliishi kwenye hema.
16 Na ikawa kuwa mimi, Nefi, nikiwa mdogo, ingawa nilikuwa na mwili mkubwa,
na pia nikiwa na hamu ya kujua siri za Mungu, kwa hivyo, nikamlilia Bwana; na
tazama akanijia mimi, na akanigusa moyo wangu kwamba nikaamini maneno yote
ambayo baba yangu alikuwa amezungumza; kwa hivyo, mimi sikumwasi kama kaka
zangu.
17 Na nikazungumza na Samu, nikimjulisha vile vitu ambavyo Bwana alikuwa

amenidhihirishia kwa Roho Mtakatifu. Na ikawa kwamba aliamini maneno yangu.
18 Lakini, tazama, Lamani na Lemueli hawakusikiza maneno yangu; na nikiwa nimehuzunishwa na ugumu wa mioyo yao nikamlilia Bwana kwa niaba yao.
19 Na ikawa kwamba Bwana akanizungumzia, akisema: Umebarikiwa ewe, Nefi, kwa sababu ya imani yako, maana umenitafuta kwa bidii, kwa unyenyekevu wa moyo.
20 Na kadiri utakavyozishika amri zangu, wewe utafanikiwa, na utaongozwa kwa nchi ya ahadi; ndio, hata nchi ambayo nimekutayarishia wewe; ndio nchi ambayo ni bora kuzidi nchi zingine.
21 Na kadiri kaka zako watakavyokuasi wewe, watatengwa mbali na Bwana.
22 Na kadiri utakavyo weka amri zangu, wewe utakuwa mtawala na mwalimu wa kaka zako.
23 Kwani tazama, katika siku ile watakaponiasi, nitawalaani hata na laana kali, na hawatakuwa kwa uwezo juu ya uzao wako ijapokuwa pia nao waniasi.
24 Na kama wataniasi, watakuwa mjeledi kwa uzao wako, kwa kuwavuruga wakumbuke njia zangu.

# 1 Nefi 3

1 Na ikawa kuwa mimi, Nefi, nilirudi kwenye hema la baba yangu, baada ya kusema na Bwana.
2 Na ikawa kuwa akanisemesha, na kuniambia: Tazama nimeota ndoto, ambapo Bwana ameniamrisha kwamba wewe na kaka zako mtarejea Yerusalemu.
3 Kwani tazama, Labani anayo maandishi ya Wayahudi na pia nasaba ya babu zangu, na imechorwa kwenye bamba za shaba nyeupe.
4 Kwa hivyo, Bwana ameniamrisha mimi kwamba wewe na kaka zako mwende nyumbani kwa Labani, mtafute hayo maandishi, na kuyaleta hapa nyikani.
5 Na sasa, tazama kaka zako wananung'unika, wakisema kuwa ni kitu kigumu ninachokihitaji kutoka kwao; lakini, tazama mimi sijahitaji hilo kwao, lakini ni amri ya Bwana.
6 Kwa hivyo nenda, mwana wangu, nawe utapendeka kwa Bwana, kwa sababu wewe hujanung'unika.
7 Na ikawa kuwa mimi, Nefi, nilimwambia baba yangu: Nitaenda na kutenda vitu ambavyo Bwana ameamuru, kwani ninajua kwamba Bwana hatoi amri kwa watoto wa watu, isipokua awatayarishie njia ya kutimiza kitu ambacho amewaamuru.
8 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu kusikia maneno haya alifurahi sana, maana alijua kuwa nimebarikiwa na Bwana.
9 Na mimi, Nefi, na kaka zangu tukachukua safari nyikani, pamoja na mahema yetu, tukielekea nchi ya Yerusalemu.
10 Na ikawa kwamba tulipokuwa tumesafiri hadi nchi ya Yerusalemu, mimi na kaka zangu tulijadiliana.
11 Na tukapiga kura—ni nani kati yetu ataingia nyumbani mwa Labani. Na ikawa kwamba kura ikamwangukia Lamani; na Lamani akaenda nyumbani mwa Labani, na akaongea na yeye alipokuwa ameketi nyumbani mwake.
12 Na akamwomba Labani yale maandishi yaliyokuwa yamechorwa kwenye bamba za shaba, ambayo yalikuwa na nasaba ya baba yangu.
13 Na tazama, ikawa kwamba Labani alikasirika, na akamtoa nje; na asitake

kumpatia yale maandishi. Kwa hivyo, akamwambia: Tazama wewe ni mnyang'anyi, na nitakuua.
14 Lakini Lamani alitoroka kutoka kwake, na akatuelezea vitu ambavyo Labani alitufanyia. Na tulishikwa na huzuni nyingi, na kaka zangu walikuwa karibu kurudi nyikani kwa baba yangu.
15 Lakini tazama nikawaambia kwamba: Kadiri Bwana aishivyo, na tuishivyo sisi, hatutarudi kwa baba yetu nyikani mpaka tukamilishe kile kitu ambacho Bwana alituamrisha sisi.
16 Kwa hivyo, tuwe waaminifu katika kushika amri za Bwana; kwa hivyo tuteremke hadi kwa nchi ya urithi ya baba yetu, kwani tazama aliacha dhahabu na fedha, na kila aina ya utajiri. Na haya yote ametenda kwa sababu ya amri za Bwana.
17 Kwani alijua kwamba lazima Yerusalemu iangamizwe, kwa sababu ya uovu wa watu.
18 Kwani tazama, wamekataa maneno ya manabii. Kwa hivyo, kama baba yangu ataishi katika nchi baada ya kuamriwa atoroke nchi hiyo, tazama, pia yeye ataangamia. Kwa hivyo, inabidi lazima atoroke nchi hiyo.
19 Na tazama, ni hekima katika Mungu tupate kuchukua haya maandishi, ili tuweze kuhifadhia watoto wetu lugha ya baba zetu;
20 Na pia kwamba tuwahifadhie maneno yaliyonenwa kwa vinywa vya manabii watakatifu, ambayo walipewa na Roho na nguvu za Mungu, tangu mwanzo wa ulimwengu, hadi nyakati za sasa.
21 Na ikawa kwamba niliwashawishi kaka zangu kwa maneno haya, ili wawe waaminifu kwa kushika amri za Mungu.
22 Na ikawa kwamba tulishuka na kuenda katika nchi yetu ya urithi, na tukakusanya dhahabu yetu, na fedha yetu, na vitu vyetu vya thamani.
23 Na baada ya kukusanya hivi vitu pamoja, tukaenda tena nyumbani mwa Labani.
24 Na ikawa kwamba tulikutana na Labani, na tukataka atupatie yale maandishi ambayo yalikuwa yamechorwa kwenye bamba za shaba, nasi tungempatia dhahabu yetu, na fedha yetu, na vitu vyetu vyote vya thamani.
25 Na ikawa kwamba wakati Labani alipoona mali yetu, na kwamba ilikuwa nyingi sana, aliitamani, hadi kwamba akatufukuza nje, na akatuma watumishi wake watuue, ili kwamba aweze kupata mali yetu.
26 Na ikawa kwamba tuliwakimbia watumishi wa Labani, na ikatubidi kuacha mali yetu, na ikangukia mikononi mwa Labani.
27 Na ikawa kwamba tulitorokea nyikani, na watumishi wa Labani hawakutupata, na tukajificha kwenye pango la mwamba.
28 Na ikawa kwamba Lamani alinikasirikia mimi, na baba yangu pia; na pia Lemueli, kwani alisikiliza maneno ya Lamani. Kwa hivyo Lamani na Lemueli walituzungumzia kwa maneno mengi ya uchungu, sisi kaka zao wadogo, na wakatupiga sisi hata kwa bakora.
29 Na ikawa kwamba walipokuwa wakitupiga kwa bakora, tazama malaika wa Bwana alikuja na akasimama mbele yao, na akawazungumzia, akisema: Mbona mnampiga kaka yenu mdogo kwa bakora? Hamjui kuwa Bwana amemchagua yeye kuwa kiongozi wenu, na hii ni kwa sababu ya maovu yenu? Tazama mtarudi tena Yerusalemu, na Bwana atamkabidhi Labani mikononi mwenu.
30 Na baada ya malaika kutuzungumzia, akatoweka.
31 Na baada ya malaika kutoweka, Lamani na Lemueli wakaanza kunung'unika

tena, wakisema: Vipi itawezekana kwamba Bwana atamkabidhi Labani mikononi mwetu? Tazama, yeye ni mtu shujaa, na anaweza kuamuru watu hamsini; ndio, hata kuwaua watu hamsini; je, kwa nini asituue sisi?

## 1 Nefi 4

1 Na ikawa kwamba nikawazungumzia kaka zangu, nikisema: Twendeni tena Yerusalemu, na tuwe waaminifu kwa kuzishika amri za Bwana; kwani tazama yeye ni mkuu kupita ulimwengu wote, basi kwa nini asiwe mkuu kupita Labani na watu wake hamsini, ndio, au hata kupita kumi ya maelfu?

2 Kwa hivyo twendeni; tuwe hodari kama Musa; kwani alizungumzia maji ya Bahari ya Shamu na yakagawanyika sehemu mbili, na babu zetu wakapita, katika nchi kavu, kutoka utumwani, na majeshi ya Farao yakafuata na kuzama majini mwa Bahari ya Shamu.

3 Tazama sasa mnajua kwamba hii ni kweli; na pia mnajua kwamba malaika amewazungumzia; je mnaweza kuwa na shaka? Twendeni; Bwana anaweza kutukomboa, kama baba zetu, na kumwangamiza Labani, hata kama Wamisri.

4 Sasa baada ya mimi kunena maneno haya, bado walikuwa na hasira, na wakaendelea kunung'unika; walakini walinifuata hadi tukafika nje ya kuta za Yerusalemu.

5 Na ilikuwa usiku; na nikawaambia wajifiche nje ya kuta. Na baada ya wao kujificha, mimi, Nefi, nilinyemelea hadi ndani ya mji na nikaelekea hadi nyumba ya Labani.

6 Na nikaongozwa na Roho, wala sikujua kimbele vitu ambavyo ningefanya.

7 Walakini niliendelea mbele, na nilipokaribia nyumba ya Labani nilimwona mtu, na alikuwa ameanguka kwenye ardhi mbele yangu, kwani alikuwa amelewa kutokana na mvinyo.

8 Na nilipomkaribia niligundua kwamba alikuwa Labani.

9 Na nikaona upanga wake, na nikautoa kutoka uo wake; na mpini wake ulikuwa wa dhahabu halisi, na uumbaji wake ulikuwa mzuri sana, na nikaona upanga wake ulikuwa wa chuma chenye thamani.

10 Na ikawa kwamba Roho alinishurutisha nimuue Labani; lakini nikasema moyoni mwangu: Sijawahi wakati wowote kumwaga damu ya mtu. Na nikasita na sikutaka kumuua.

11 Na Roho aliniambia tena: Tazama Bwana amemkabidhi mikononi mwako. Ndio, na pia nilijua kwamba alikuwa amenitafuta kunitoa uhai; ndio, na pia hakusikiza amri za Bwana; na alikuwa pia amechukua mali yetu.

12 Na ikawa kwamba Roho aliniambia tena: Muuwe, kwani Bwana amemkabidhi mikononi mwako;

13 Tazama Bwana huwaua waovu ili atimize madhumuni yake ya haki. Yafaa mtu mmoja afe badala ya taifa kufifia na kuangamia katika kutoamini.

14 Na sasa, mimi, Nefi, niliposikia maneno haya, nikakumbuka maneno ya Bwana ambayo alinizungumzia nyikani, akisema kwamba: Kadiri uzao wako utakavyoshika amri zangu, watafanikiwa katika nchi ya ahadi.

15 Ndio, na pia nikafikiria kwamba hawangeshika amri za Bwana kulingana na sheria za Musa, hadi wawe na hizo sheria.

16 Na pia nilijua kwamba sheria hizo zilikuwa zimechorwa katika bamba za shaba.

17 Na tena, nilijua kwamba Bwana alikuwa amemkabidhi Labani mikononi
mwangu kwa sababu hii—kwamba nipate kuchukua yale maandishi kulingana na
amri zake.
18 Kwa hivyo nikatii sauti ya Roho, na nikamshika Labani kwa nywele za kichwa
chake, na nikamkata kichwa chake kwa upanga wake.
19 Na baada ya kukata kichwa chake kwa upanga wake, nilichukua mavazi ya Labani
na nikayavaa; ndio, hata kila chembe; na nikafunga vazi la vita lake kiunoni
mwangu.
20 Na baada ya kutenda hivyo, nilielekea kwenye nyumba ya hazina ya Labani. Na
nilipoelekea kwenye nyumba ya hazina ya Labani, tazama, nilimwona mtumishi wa
Labani ambaye alikuwa na funguo za nyumba ya hazina. Na nikamwamrisha nikiiga
sauti ya Labani, kwamba aandamane na mimi hadi nyumba ya hazina.
21 Na akadhania kwamba mimi ni tajiri wake, Labani, kwani aliona mavazi na pia
upanga nimeufunga kiunoni.
22 Na akanizungumzia kuhusu wazee wa Wayahudi, yeye akijua kwamba tajiri yake,
Labani, alikuwa nje miongoni mwao usiku ule.
23 Nami nikazungumza na yeye kama kwamba nilikuwa Labani.
24 Na pia nikamwambia kwamba inanibidi kuchukua michoro, ambayo ilikuwa
kwenye bamba za shaba, kwa kaka zangu, waliokuwa nje ya kuta.
25 Na pia nikamwamuru anifuate.
26 Na yeye, akidhania kwamba nilikuwa nikizungumza kuhusu ndugu wa kanisa, na
kwamba nilikuwa Labani ambaye nilikuwa nimemwua, kwa hivyo alinifuata.
27 Na akanizungumzia mara nyingi kuhusu wazee wa Wayahudi, nilipokuwa
nikielekea kwa kaka zangu, ambao walikuwa nje za kuta.
28 Na ikawa kwamba wakati Lamani aliponiona alishikwa na woga mwingi, pia
Lemueli na Samu. Na walinikimbia; kwani walidhani kuwa ni Labani, na kwamba
alikuwa ameniua na alikuwa anajaribu kutoa uhai wao pia.
29 Na ikawa kwamba niliwaita, na wakanisikia; kwa hivyo wakaacha kunitoroka.
30 Na ikawa kwamba wakati mtumishi wa Labani aliona kaka zangu alianza
kutetemeka, na alikuwa karibu kutoroka na kurejea katika mji wa Yerusalemu.
31 Na sasa mimi, Nefi, nikiwa mtu mwenye umbo kubwa, na pia nikiwa nimepokea
nguvu nyingi za Bwana, kwa hivyo nikamkamata mtumishi wa Labani, na
nikamzuia, kwamba asitoroke.
32 Na ikawa kwamba nikamzungumzia, kwamba kama angesikiza maneno yangu,
kama Bwana anavyoishi, na kama ninavyoishi, endapo angesikiza maneno yetu, basi
tungehifadhi maisha yake.
33 Na nikamzungumzia, hata kwa kiapo, kwamba asiogope; kwamba atakuwa mtu
huru kama sisi ikiwa atakwenda nyikani pamoja nasi.
34 Na pia nikamzungumzia, nikisema: Kwa kweli Bwana ametuamuru kutenda kitu
hiki; je hatutakuwa wenye juhudi kuweka amri za Bwana? Kwa hivyo, kama utaenda
nyikani kwa baba yangu utapata mahali pa kuishi pamoja nasi.
35 Na ikawa kwamba Zoramu alifarijika na maneno ambayo nilimzungumzia. Sasa
Zoramu lilikuwa jina lake huyo mtumishi; na akaahidi kwamba ataenda huko
nyikani kwa baba yetu. Ndio, na pia aliapa kwamba ataishi pamoja nasi kutoka siku
ile na kuendelea.
36 Sasa tulitaka aishi nasi kwa sababu hii, ili Wayahudi wasijue kuhusu ukimbizi
wetu wa nyikani, na kutufuata ili watuangamize.

37 Na ikawa kwamba wakati Zoramu alitupatia kiapo, hofu yetu kumhusu ikakoma.
38 Na ikawa kwamba tukazichukua bamba za shaba na mtumishi wa Labani, na kuelekea nyikani, na kusafiri hadi kwenye hema la baba yetu.

# 1 Nefi 5

1 Na ikawa kuwa kwamba baada ya sisi kufika nyikani kwa baba yetu, tazama, alijazwa na shangwe, na pia mama yangu, Saria, alifurahi sana, kwani alikuwa ameomboleza kwa sababu yetu.
2 Kwani alikuwa amedhani kwamba tulikuwa tumeangamia nyikani; na pia alikuwa amemlalamikia baba yangu, akimwambia kwamba yeye ni mtu wa maono; na kusema: Tazama wewe umetuongoza kutoka nchi yetu ya urithi, na wana wangu hawapo tena, na tunaangamia nyikani.
3 Na kwa lugha ya aina hii mama yangu alimlalamikia baba yangu.
4 Na ikawa kwamba baba yangu akamzungumzia, na kusema: Najua kwamba mimi ni mtu wa maono; kwani kama nisingeona vitu vya Mungu katika maono nisingejua wema wa Mungu, lakini ningekaa huko Yerusalemu, na kuangamia pamoja na ndugu zangu.
5 Lakini tazama, nimepokea uthibitisho wa nchi ya ahadi, vitu ambavyo kwavyo ninafurahia; ndio, na ninajua kwamba Bwana atawakomboa wana wangu kutoka mikononi mwa Labani, na kuwaleta hapa kwetu nyikani.
6 Na kwa lugha ya aina hii baba yangu, Lehi, alimfariji mama yangu, Saria, kutuhusu, tulipokuwa tukisafiri kutoka nyikani hadi nchi ya Yerusalemu, kuchukua maandishi ya Wayahudi.
7 Na tulipokuwa tumerudi kwenye hema la baba yangu, tazama shangwe yao ilikuwa tele, na mama yangu akafarijika.
8 Na mama yangu akazungumza, akisema: Sasa najua kwa hakika kwamba Bwana amemwamuru mume wangu kutorokea nyikani; ndio, na pia najua kwa hakika kwamba Bwana amewalinda wana wangu, na kuwakomboa kutoka mikononi mwa Labani, na kuwapatia uwezo wa kutimiza kitu ambacho Bwana aliwaamuru. Na hii ndio lugha ambayo mama yangu alitumia.
9 Na ikawa kwamba walishangilia sana, na wakamtolea Bwana dhabihu za kuteketezwa kwa moto pamoja na sadaka; na kumshukuru Mungu wa Israeli.
10 Na baada ya kumshukuru Mungu wa Israeli, baba yangu, Lehi, alichukua yale maandishi ambayo yalikuwa yamechorwa kwenye bamba za shaba, na aliyapekua tangu mwanzo.
11 Na akagundua kwamba yalikuwa na vitabu vitano vya Musa, ambavyo vilieleza historia ya kuumbwa kwa dunia, na pia kwa Adamu na Hawa, ambao ndio wazazi wetu wa kwanza;
12 Na pia maandishi ya Wayahudi kutoka mwanzo, hadi mwanzo wa utawala wa Zedekia, mfalme wa Yuda;
13 Na pia unabii wa manabii watakatifu, tangu mwanzo, hadi mwanzoni mwa utawala wa Zedekia; na pia unabii mwingi ambao ulizungumzwa kutoka kinywa cha Yeremia.
14 Na ikawa kwamba baba yangu, Lehi, pia alipata kwenye bamba za shaba nasaba ya babu zake; kwa hivyo akajua kwamba yeye ni wa kizazi cha Yusufu; ndio, hata yule Yusufu, ambaye alikuwa mwana wa Yakobo, ambaye aliuzwa Misri, na ambaye

alihifadhiwa kwa mkono wa Bwana, ili amhifadhi baba yake, Yakobo, na wote wa
jamii yake wasiangamie kwa njaa.
15 Na waliongozwa pia kutoka utumwani na kutoka nchi ya Misri, na yule Mungu
ambaye alikuwa amewahifadhi.
16 Na hivyo baba yangu, Lehi, aligundua nasaba ya baba zake. Na Labani pia
alikuwa kizazi cha Yusufu, ndipo yeye na baba zake wakaweka yale maandishi.
17 Na sasa baba yangu alipoona vitu hivi vyote, alijawa na Roho, na akaanza kutoa
unabii kuhusu uzao wake—
18 Kwamba hizi bamba za shaba zipelekewe katika mataifa yote, kabila zote, lugha
zote, na watu wote wa uzao wake.
19 Kwa hivyo, alisema kwamba hizi bamba za shaba zisiangamie kamwe; wala
zisichakazwe na wakati. Na akatoa unabii wa vitu vingi kuhusu uzao wake.
20 Na ikawa kwamba mpaka hapo mimi na baba yangu tulikuwa tumeweka amri
ambazo Bwana alikuwa ametuamuru.
21 Na tulikuwa tumepata yale maandishi ambayo Bwana alikuwa ametuamuru, na
kuyachunguza na tukagundua kwamba yalikuwa ya kupendeza; ndio, hata yenye
thamani kubwa kwetu sisi, kwani tungeweza kuhifadhi amri za Bwana na kuwapa
watoto wetu.
22 Kwa hivyo, ilikuwa ni hekima katika Bwana kwamba tuyabebe tulipokuwa,
tukisafiri nyikani tukielekea nchi ya ahadi.

# 1 Nefi 6

1 Na sasa mimi, Nefi, sitaandika nasaba ya baba zangu katika sehemu hii ya maandishi
yangu; wala sitaiandika baadaye wakati wowote katika hizi bamba ambazo
ninaandika; kwani imeandikwa kwenye maandishi ambayo yamewekwa na baba
yangu; kwa hivyo, sitaiandika katika bamba hizi.
2 Kwani inanitosha kusema kuwa sisi ni kizazi cha Yusufu.
3 Na sio muhimu kwangu kutoa taarifa kamili ya vitu vya baba yangu, kwani
haviwezi kuandikwa kwenye bamba hizi, kwani nahitaji nafasi ya kuandika vitu vya
Mungu.
4 Kwani lengo langu kamili ni kuwashawishi watu waje kwa Mungu wa Ibrahimu,
na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo ili waokolewe.
5 Kwa hivyo, sitaandika vitu vile ambavyo vinafurahisha ulimwengu, bali
nitaandika yale ambayo yanamfurahisha Mungu na wale wasio wa ulimwengu.
6 Kwa hivyo, nitatoa amri kwa uzao wangu, kwamba hawataandika vitu visivyo na
thamani kwa watoto wa watu kwenye bamba hizi.

# 1 Nefi 7

1 Na sasa ningetaka mjue, kwamba baada ya baba yangu, Lehi, kumaliza kutoa unabii
kuhusu uzao wake, ikawa kwamba Bwana akamzungumzia tena, akisema kuwa
haifai yeye, Lehi, kuipeleka jamii yake pekee nyikani; lakini kwamba wana wake
waoe mabinti, ili waweze kuendeleza uzao wa Bwana katika nchi ya ahadi.
2 Na ikawa kwamba Bwana akamwamuru kwamba mimi, Nefi, na kaka zangu,
turudi tena katika nchi ya Yerusalemu, na tumlete Ishmaeli na jamii yake nyikani.

3 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, pamoja na kaka zangu, tena, tukaenda nyikani na
kuelekea Yerusalemu.
4 Na ikawa kwamba tuliingia katika nyumba ya Ishmaeli, na Ishmaeli akakubaliana
nasi, hata tukamwelezea maneno ya Bwana.
5 Na ikawa kwamba Bwana aliulainisha moyo wa Ishmaeli, pia na jamii yake, hata
wakasafiri pamoja nasi hadi nyikani kwenye hema la Baba yetu.
6 Na ikawa kwamba tulipokuwa tukisafiri nyikani, tazama Lamani na Lemueli, na
mabinti wawili wa Ishmaeli, na wale wana wawili wa Ishmaeli na jamii zao, waliasi
dhidi yetu; ndio, dhidi yangu, Nefi, na Samu, na baba yao, Ishmaeli, na mke wake,
na mabinti zake wengine watatu.
7 Na ikawa katika kuasi kwao, walitaka kurejea katika nchi ya Yerusalemu.
8 Na sasa mimi, Nefi, nikiwa nimehuzunishwa na ugumu wa mioyo yao, kwa hivyo
nikawazungumzia, nikisema, ndio, hata kwa Lamani na Lemueli: Tazama nyinyi
ndio kaka zangu wakubwa, je, kwa nini mna ugumu mioyoni yenu, na upofu katika
akili zenu, hata mnahitaji kwamba mimi kaka yenu mdogo, niwazungumzie, ndio,
hata kuwa kielelezo kwenu?
9 Je, kwa nini hamjasikiza neno la Bwana?
10 Je, ni vipi mmesahau kwamba mliona malaika wa Bwana?
11 Ndio, na ni vipi kwamba mmesahau vitu vikubwa ambavyo Bwana ametutendea,
katika kutukomboa kutoka mikononi mwa Labani, na pia kwamba tukaweza kupata
yale maandishi?
12 Ndio, na ni vipi kwamba mmesahau kuwa Bwana anaweza kufanya vitu vyote
kulingana na nia yake, kwa watoto wa watu, ikiwa watatekeleza imani kwake? Kwa
hivyo, tuwe waaminifu kwake.
13 Na kama tutakuwa waaminifu kwake, tutapokea nchi ya ahadi; na hapo baadaye
mtajua kwamba neno la Bwana litatimia kuhusu kuangamizwa kwa mji wa
Yerusalemu; kwani vitu vyote ambavyo Bwana amezungumza kuhusu kuangamizwa
kwa Yerusalemu lazima yatimizwe.
14 Kwani tazama, Roho wa Bwana ataacha karibuni kujishughulisha nao; kwani
tazama, wamewakataa manabii, na wamemtia Yeremia gerezani. Na wamemtafuta
baba yangu kumtoa uhai wake, mpaka wamemfukuza kutoka nchini.
15 Tazama sasa, nawaambia kama nyinyi mtarudi Yerusalemu pia nanyi mtaangamia
nao. Na sasa, mkiwa na uwezo wa kuchagua, nendeni kwenye nchi, na kumbukeni
maneno ambayo nawazungumzia, kwamba kama mtaenda pia mtaangamia; kwani
Roho wa Bwana ananishurutisha kuzungumza.
16 Na ikawa kwamba baada ya mimi, Nefi, kuwazungumzia kaka zangu maneno
haya, walinikasirikia. Na ikawa kwamba walinikamata, kwani tazama, walikuwa na
hasira nyingi, na wakanifunga kwa kamba, kwani walitaka kunitoa uhai wangu,
kwamba wangeniacha nyikani niliwe na wanyama wa mwituni.
17 Lakini ikawa kwamba nilimwomba Bwana, nikisema: Ewe Bwana, kulingana na
imani yangu kwako, unikomboe kutoka mikononi mwa kaka zangu; ndio, hata
unipatie nguvu ili nizikate kamba ambazo nimefungwa nazo.
18 Na ikawa kwamba baada ya kusema haya maneno, tazama, kamba kwa mikono
na miguu yangu zililegezwa, na nikasimama mbele za kaka zangu, na
nikawazungumzia tena.
19 Na ikawa kwamba walinikasirikia tena, na wakataka kunishika; lakini tazama,
mmoja wa mabinti za Ishmaeli, ndio, na mama yake pia, na mmoja wa wana wa

Ishmaeli, wakawasihi kaka zangu, hadi wakalainisha mioyo yao; na wakaacha kutaka
kujaribu kutoa uhai wangu.
20 Na ikawa kwamba walihuzunishwa, kwa sababu ya uovu wao, hadi wakaniinamia,
na kunisihi niwasamehe kitu ambacho walikuwa wametenda dhidi yangu.
21 Na ikawa kwamba niliwasamehe kwa ukweli na moyo wangu wote kwa yote
waliyofanya, na nikawahimiza kwamba wamuombe Bwana Mungu wao msamaha.
Na ikawa kwamba walitenda hivyo. Na baada ya wao kumaliza kumwomba Bwana,
tulisafiri tena tukielekea kwenye hema la baba yetu.
22 Na ikawa kwamba tulifika kwenye hema la baba yetu. Na baada ya mimi na kaka
zangu pamoja na nyumba yote ya Ishmaeli kufika kwenye hema la baba yangu,
walitoa shukrani kwa Bwana Mungu wao; na wakamtolea dhabihu na sadaka za
kuteketezwa kwa moto.

## 1 Nefi 8

1 Na ikawa kwamba tulikuwa tumekusanya jinsi zote za mbegu za kila aina, pamoja na
nafaka za kila aina, na pia mbegu za kila aina ya matunda.
2 Na ikawa kuwa wakati baba yangu alipoishi nyikani alituzungumzia, akisema:
Tazama, nimeota ndoto; au kwa maneno mengine, nimeona ono.
3 Na tazama, kwa sababu ya kitu ambacho nilikuwa nimekiona, nina sababu ya
kutoa shukrani kwa Bwana kwa sababu ya Nefi na pia ya Samu; nina sababu ya
kuamini kwamba wao, na pia wengi wa uzao wao, watakombolewa.
4 Lakini tazama, Lamani na Lemueli, ninaogopa sana kwa sababu yenu; kwani
tazama, nilidhania niliona ndotoni mwangu, nyika yenye giza na yenye
kuhuzunisha.
5 Na ikawa kwamba niliona mtu, na alikuwa amevaa joho jeupe; na akaja na
kusimama mbele yangu.
6 Na ikawa kwamba alinizungumzia, na aliniamuru nimfuate.
7 Na ikawa kwamba nilipokuwa namfuata nilijiona kwamba nilikuwa katika
mahali penye giza na ukiwa wa jangwa.
8 Na baada ya kusafiri kwa masaa mengi gizani, nilianza kumwomba Bwana
anihurumie, kulingana na wingi wa rehema na fadhili zake.
9 Na ikawa kuwa baada ya mimi kumwomba Bwana, niliona uwanja mkubwa na
mpana.
10 Na ikawa kwamba niliona mti, ambao matunda yake yalitamanika kumfurahisha
mwanadamu.
11 Na ikawa kwamba nilienda na nikala matunda yake; na nikagundua kwamba
yalikuwa matamu, zaidi ya yote ambayo nilikuwa nimeonja. Ndio, na nikaona
kwamba tunda lake lilikuwa leupe, kushinda weupe wote ambao nilikuwa
nimeuona.
12 Na nilipokula tunda lile lilijaza nafsi yangu na shangwe tele; kwa hivyo, nikaanza
kutaka jamii yangu na wao pia wale; kwani nilijua kwamba lilikuwa tunda la
kupendeza zaidi ya yote.
13 Na nilipotazama hapa na pale, ili pia labda nione jamii yangu, niliona mto wa
maji; na ulitiririka, karibu na mti ule ambao nilikuwa nikila matunda yake.
14 Na nikatazama nione ulitoka wapi; na nikaona chimbuko lake mbali kidogo; na
kwenye chimbuko nikaona mama yenu Saria, na Samu, na Nefi; na walisimama

wakawa kama hawajui wanapoenda.
15 Na ikawa kwamba niliwapungia mkono; na pia kwa sauti kubwa nikawaambia
wanikaribie, na wale tunda, ambalo lilikuwa la kupendeza zaidi kuliko tunda lingine.
16 Na ikawa kwamba walinikaribia na kula tunda pia.
17 Na ikawa kwamba nilitaka pia Lamani na Lemueli waje na kula tunda; kwa
hivyo, nikatazama kwenye chimbuko la mto, kwamba labda niwaone.
18 Na ikawa kwamba niliwaona, lakini hawakunijia na kula tunda.
19 Na nikaona fimbo ya chuma, na ilinyooka kando ya ukingo wa mto, mpaka
kwenye mti niliposimama.
20 Na pia nikaona njia nyembamba imesonga, ambayo iliambatana na fimbo ya
chuma, hata hadi ambapo nilipokuwa nimesimama kwenye mti; na pia ilielekea
kwenye chimbuko la chemchemi, hadi kwenye uwanja mkubwa mpana, kama
kwamba ni ulimwengu.
21 Na nikaona umati mkubwa wa watu usio na idadi, wengi wao ambao walikuwa
wanasogea mbele, ili wapate kufikia njia ambayo ilielekea kwenye mti ambapo
nilikuwa nimesimama.
22 Na ikawa kwamba walifika hapo mbele, na kuipata njia iliyoelekea kwenye mti.
23 Na ikawa kwamba kulitokea ukungu wa giza; ndio, hata ukungu mkubwa wa
giza, hadi wale ambao walikuwa wametangulia njia walipotea njia, kwamba
walizungukazunguka na kupotea.
24 Na ikawa kwamba niliona wengine wakisonga mbele, na wakafika mbele na
wakashika mwisho wa fimbo ya chuma; na wakasonga mbele na kupenya ukungu wa
giza, wakishikilia fimbo ya chuma, hadi wakafika na kula matunda ya mti.
25 Na baada ya kula matunda ya mti wakatupa macho yao hapa na pale wakawa
kama wanaaibika.
26 Na pia nikatupa macho yangu hapa na pale, na nikaona, kwenye ng'ambo
nyingine ya mto wa maji, jengo kubwa na pana; na lilikuwa ni kama linaelea hewani,
juu zaidi ya ardhi.
27 Na lilikuwa limejaa watu, wazee kwa vijana, wanaume kwa wanawake; na mavazi
yao yalikuwa mazuri kupita kiasi; na walikuwa na tabia ya kufanya mzaha na
kuwaonyesha kwa vidole vyao wale ambao walikuwa wanakuja na kula matunda.
28 Na baada ya kuonja matunda waliaibika, kwa sababu ya wale waliokuwa
wakiwadharau; na wakaingia katika njia zilizokataliwa na wakapotea.
29 Na sasa mimi, Nefi, sizungumzi maneno yote ya baba yangu.
30 Lakini, nikifupisha katika kuandika, tazama, aliona umati mwingine ukisonga
mbele; na wakaja na kushika mwisho wa ile fimbo ya chuma; na wakasonga mbele,
daima wameshikilia ile fimbo ya chuma, hadi wakafika na kuinama na kula matunda
ya ule mti.
31 Na pia akaona umati mwingine ukipapasapapasa wakielekea kwa lile jengo
kubwa na pana.
32 Na ikawa kwamba wengi walizama kwenye kilindi cha chemchemi; na wengi
wakapotea asipate kuwaona, wakizururazurura katika njia ngeni.
33 Na umati ule ulioingia kwenye lile jengo geni ulikuwa mkubwa. Na baada ya
kuingia kwenye lile jengo walitufanyia ishara za madharau kwa vidole vyao mimi na
wale ambao walikuwa wakila matunda; lakini hatukuwasikiza.
34 Haya ndio maneno ya baba yangu: Kuwa wengi waliowasikiza, walianguka.
35 Na baba yangu akasema kuwa Lamani na Lemueli hawakula matunda, alisema

baba yangu.
36 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu kuzungumza maneno yote ya ndoto yake
au ono, ambayo yalikuwa mengi, akatuambia sisi, kwa sababu ya vitu hivi vyote
ambavyo alivyoona katika ono, aliwahofia kupita kiasi Lamani na Lemueli; ndio,
alihofia wasije wakatupiliwa mbali kutoka kwenye uwepo wa Bwana.
37 Na aliwasihi kwa huruma zote za mzazi mwenye upendo, kwamba wasikilize
maneno yake, na pengine Bwana angewarehemu, na asiwatupilie mbali; ndio, baba
yangu aliwahubiria.
38 Na baada ya kuwahubiria, na pia kuwatolea unabii wa vitu vingi, aliwaamuru
kuweka amri za Bwana; na akakoma kuwazungumzia.

# 1 Nefi 9

1 Na baba yangu aliona vitu hivi vyote, na kusikia, na kuvizungumza, alipokuwa
kwenye hema, katika bonde la Lemueli, na pia vitu vingi zaidi, ambavyo haviwezi
kuandikwa kwenye bamba hizi.
2 Na sasa, kulingana na yale nimeyosema kuhusu hizi bamba, tazama sio zile
bamba ambazo ninaandika historia kamili ya watu wangu; kwani bamba ambazo
nimeandika historia kamili ya watu wangu nimeziita kwa jina la Nefi; kwa hivyo,
zinaitwa bamba za Nefi, kufuatana na jina langu; na pia hizi bamba zinaitwa bamba
za Nefi.
3 Walakini, nimepokea amri ya Bwana kwamba nizitengeneze hizi bamba, kwa
kusudi muhimu kwamba kuweko na historia iliyochorwa ya huduma ya watu wangu.
4 Kwenye zile bamba nyingine ichorwe historia ya utawala wa wafalme, na vita na
mabishano ya watu wangu; kwa hivyo hizi bamba sehemu kubwa ni ya huduma; na
zile bamba nyingine sehemu kubwa ni ya utawala wa wafalme na vita na pia
mabishano ya watu wangu.
5 Kwa hivyo, Bwana ameniamuru kuandika hizi bamba kwa kusudi lake lenye
hekima, ambalo kusudi mimi silijui.
6 Lakini Bwana anavijua vitu vyote kuanzia mwanzoni; kwa hivyo, anatayarisha
njia ya kutimiza kazi zake zote miongoni mwa watoto wa watu; kwani tazama, ana
uwezo wote wa kutimiza maneno yake yote. Na hivyo ndivyo ilivyo. Amina.

# 1 Nefi 10

1 Na sasa mimi, Nefi, ninaendelea kuandika historia kuhusu matendo yangu kwenye
hizi bamba, pamoja na utawala na huduma yangu; kwa hivyo, ili niendelee na
historia yangu, lazima nizungumze machache kuhusu vitu vya baba yangu, na pia
kaka zangu.
2 Kwani tazama, ikawa kwamba baada ya baba yangu kumaliza kuzungumza
maneno ya ndoto yake, na pia kuwasihi waendelee kwenye jitihada,
aliwazungumuzia kuhusu Wayahudi—
3 Kwamba baada yao kuangamizwa, hata ule mji mkuu Yerusalemu, na wengi
kupelekwa uhamishoni Babilonia, kulingana na nyakati za Bwana, watarejea tena,
ndio, hata kurejeshwa kutoka uhamishoni; na baada ya kutolewa uhamishoni
watamiliki tena nchi yao ya urithi.

4 Ndio, hata baada ya miaka mia sita tangu baba yangu atoke Yerusalemu, Bwana
Mungu atainua nabii miongoni mwa Wayahudi — hata Masiya, au, kwa maneno
mengine, Mwokozi wa ulimwengu.
5 Na pia akazungumzia kuhusu manabii, jinsi wengi wao walivyokuwa
wameshuhudia vitu hivi, kuhusu Masiya ambaye alikuwa amemzungumzia, au huyu
Mkombozi wa ulimwengu.
6 Kwa hivyo, wanadamu wote walikuwa wamepotea na wako katika hali ya
kuanguka, na watakuwa hivyo hata milele wasipomtegemea huyu Mkombozi.
7 Na alizungumza pia kuhusu nabii ambaye angemtangulia Masiya, ili
kumtayarishia Bwana njia yake —
8 Ndio, hata ataondoka mbele na kutangaza nyikani: Itayarisheni njia ya Bwana,
na yanyosheni mapito yake; kwani miongoni mwenu amesimama yeye msiyemjua;
na yeye ni mkuu kunishinda, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya kiatu
chake. Na baba yangu alizungumza mengi kuhusu kitu hiki.
9 Na baba yangu akasema atabatiza katika Bethabara, ng'ambo ya Yordani; na pia
akasema kuwa atabatiza kwa maji; hata kwamba atambatiza Masiya kwa maji.
10 Na baada ya kumbatiza Masiya kwa maji, itambidi kuona na kushuhudia kwamba
alimbatiza Mwanakondoo wa Mungu, ambaye ataondoa dhambi za ulimwengu.
11 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu kuzungumza maneno haya
aliwazungumzia kaka zangu kuhusu injili ambayo itahubiriwa miongoni mwa
Wayahudi, na pia kuhusu kufifia kwa Wayahudi katika kutoamini. Na baada ya
kumuua Masiya, ajaye, na baada ya kuuwawa atafufuka kutoka kwa wafu, na
ajidhihirishe, kupitia nguvu za Roho Mtakatifu, kwa Wayunani.
12 Ndio, baba yangu hata alizungumza mengi kuhusu Wayunani, na pia kuhusu
nyumba ya Israeli, kwamba watalinganishwa na mzeituni, ambao matawi yake
yatakatwa na kutawanywa kote kote usoni mwa dunia.
13 Kwa hivyo, akasema ni lazima sote tuongozwe pamoja hadi kwa nchi ya ahadi, ili
maneno ya Bwana yatimizwe, kuwa tutawanywe kote usoni mwa dunia.
14 Na baada ya nyumba ya Israeli kutawanyika watakusanyika tena pamoja; au, kwa
usemi mwingine, baada ya Wayunani kupokea utimilifu wa Injili, matawi ya asili ya
mzeituni, au masazo ya nyumba ya Israeli, yatapandikizwa, au kumfahamu Masiya
wa ukweli, Bwana wao na Mkombozi wao.
15 Na baba yangu alitumia maneno haya kwa kuwatolea kaka zangu unabii, na
kuwazungumzia na pia vitu vingi mno ambavyo siandiki kwenye kitabu hiki; kwani
nimeandika mengi yaliyonipasa kwa kile kitabu changu kingine.
16 Na vitu hivi vyote, ambavyo nimezungumza, vilifanyika wakati baba yangu
aliishi kwenye hema, katika bonde la Lemueli.
17 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, baada ya kusikia maneno yote ya baba yangu,
kuhusu vile vitu ambavyo alikuwa ameona katika ono, na pia vile vitu
alivyozungumza kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, nguvu alizopokea kwa imani katika
Mwana wa Mungu — na Mwana wa Mungu alikuwa Masiya ajaye — mimi, Nefi,
nikatamani nione pia, na kusikia, na kuvijua vitu hivi, kwa nguvu ya Roho
Mtakatifu, ambayo ni karama ya Mungu kwa wote wale ambao humtafuta kwa bidii,
sio tu katika nyakati zilizopita, lakini pia katika nyakati anajidhihirisha kwa watoto
wa watu.
18 Kwani yeye ni yule yule jana, leo, na milele; na njia imetayarishiwa wanadamu
wote tangu msingi wa ulimwengu, ikiwa itakuwa kwamba watatubu na kuja kwake.

19 Kwani atafutaye kwa bidii atapata; na watafunguliwa siri za Mungu, kwa nguvu
ya Roho Mtakatifu, kama ilivyokuwa katika nyakati hizi na nyakati za kale, na vile
vile hizo nyakati za kale, na pia nyakati zijazo; kwa hivyo, mpangilio wa Bwana ni
mpangilio imara milele.
20 Kwa hivyo kumbuka, Ewe mwanadamu, utahukumiwa kwa yale yote utendayo.
21 Kwa hivyo, kama uliteua kutenda maovu katika nyakati za majaribio yako, basi
utapatwa mchafu mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu; na hakuna kitu kichafu
chaweza kuishi na Mungu; kwa hivyo, lazima utupiliwe mbali milele.
22 Na Roho Mtakatifu ananipatia mamlaka kuzungumza vitu hivi, na nisiyazuie.

## 1 Nefi 11

1 Kwani ikawa baada ya kutamani kujua vitu ambavyo baba yangu aliona, na
nikiamini kwamba Bwana anaweza kunijulisha haya kwangu, nikiwa nimekaa
nikiwaza moyoni mwangu nilinyakuliwa na Roho wa Bwana, ndio, hadi kwenye
mlima mrefu zaidi, ambao sijawahi kuona hapo awali kamwe, na ambao juu wake
sijawahi kukanyagisha mguu wangu hapo awali kamwe.
2 Na Roho akaniambia: Tazama, ni nini unachotamani?
3 Na nilisema: Natamani kuona vitu ambavyo baba yangu aliona.
4 Na Roho akaniambia: Unaamini kwamba baba yako aliuona mti ambao
ameuzungumzia?
5 Na nikasema: Ndio, wewe unajua kwamba ninaamini maneno yote ya baba
yangu.
6 Na baada ya mimi kuzungumza haya maneno, Roho akapaza sauti, na kusema:
Hosana kwa Bwana, Mungu aliye juu sana; kwani yeye ndiye Mungu juu ya ardhi
yote, ndio, hata juu ya yote. Na umebarikiwa ewe, Nefi, kwa sababu unamwamini
Mwana wa Mungu aliye juu sana; kwa hivyo, wewe utaona vitu ulivyotamani.
7 Na tazama utapewa kitu hiki kama ishara, kwamba baada ya kuona mti ambao
ulizaa tunda ambalo baba yako alionja, wewe utaona pia mtu akiteremka kutoka
mbinguni, na wewe utashuhudia; na baada ya kumwona wewe utashuhudia kwamba
yeye ni Mwana wa Mungu.
8 Na ikawa kwamba Roho akaniambia: Tazama! Na nikatazama na kuona mti; na
ulikuwa kama ule mti ambao baba yangu aliuona; na urembo wake ulikuwa hauna
kipimo, ndio, zaidi ya urembo wote; na weupe wake ulizidi weupe wa theluji
ivumayo.
9 Na ikawa baada ya kuona huu mti, nikamwambia Roho: Nimeona kuwa
umenionyesha mti ulioadimika zaidi ya yote.
10 Na akaniambia: Nini unachotamani?
11 Na nikamwambia: Kufahamu maana yake—kwani nilimzungumzia kama
mwanadamu; kwani niliona kuwa alikuwa kwa mfano wa mwanadamu; walakini,
nilijua kwamba ni Roho wa Bwana; na akanizungumzia kama mwanadamu
anavyozungumzia na mwingine.
12 Na ikawa kwamba akaniambia: Tazama! Na nikatazama ili nimwone, na
sikumwona; kwani alikuwa ameenda kutoka machoni mwangu.
13 Na ikawa kwamba nilitazama na nikaona mji mkuu wa Yerusalemu, na pia miji
mingine. Na nikaona mji wa Nazareti; na katika mji wa Nazareti nikamwona bikira,
na alikuwa mrembo na mweupe.

14 Na ikawa kwamba niliona mbingu zikifunguka; na malaika akateremka na
kusimama mbele yangu; na akaniambia: nini unachokiona, Nefi?
15 Na nikamwambia: Ni bikira, ambaye ni mrembo na mtakatifu zaidi ya bikira
wengine wote.
16 Na akaniambia: Je wajua ufadhili wa Mungu?
17 Na nikamwambia: Najua kwamba anawapenda watoto wake; walakini, sijui
maana ya vitu vyote.
18 Na akaniambia: Tazama, bikira unayemwona ni mama wa Mwana wa Mungu,
katika kimwili.
19 Na ikawa kwamba niliona alinyakuliwa na Roho; na baada ya kunyakuliwa na
Roho kwa muda, malaika akanizungumizia, akisema: Tazama!
20 Na nikatazama na kumwona yule bikira tena, akimbeba mtoto mikononi mwake.
21 Na malaika akaniambia: Tazama Mwanakondoo wa Mungu, ndio, hata Mwana
wa Baba wa Milele! Je, unajua maana ya ule mti ambao baba yako aliuona?
22 Na nikamjibu, nikasema: Ndio, ni upendo wa Mungu, ambao umejimimina
mioyoni mwa watoto wa watu, kwa hivyo, ni wa kupendeza zaidi ya vitu vyote.
23 Na akanizungumzia, na kusema: Ndio, na inafurahisha moyo kwa shangwe.
24 Na baada ya kusema maneno haya, akaniambia: Tazama! Na nikatazama, na
nikamwona Mwana wa Mungu akienda miongoni mwa watoto wa watu; na
nikawaona wengi wakiinama mbele ya miguu yake na kumuabudu.
25 Na ikawa kwamba niliona ile fimbo ya chuma, ambayo baba yangu aliiona,
ilikuwa neno la Mungu, na ilielekea hadi kwenye chemchemi ya maji ya uhai, au
kwenye mti wa uzima; maji ambayo ni kielelezo cha upendo wa Mungu; na pia
nikaona kwamba ule mti wa uzima ulikuwa pia kielelezo cha upendo wa Mungu.
26 Na malaika akaniambia tena: Angalia na uone ufadhili wa Mungu!
27 Na nikatazama na kuona Mkombozi wa ulimwengu, ambaye baba yangu alikuwa
amenena kumhusu; na pia nikaona nabii atakayemtayarishia njia mbele yake. Na
Mwanakondoo wa Mungu akamwendea na akabatizwa naye; na baada ya kubatizwa,
nikaona mbingu zikifunguka, na Roho Mtakatifu akishuka kutoka mbinguni na
kutua juu yake kwa mfano wa njiwa.
28 Na nikaona kwamba alienda na kuwahudumia watu, kwa uwezo na utukufu
mkuu; na umati ukakusanyika kumsikiliza; na nikaona kwamba walimfukuza
kutoka miongoni mwao.
29 Na pia nikaona wengine kumi na wawili wakimfuata. Na ikawa kwamba
walichukuliwa na Roho kutoka machoni mwangu, na sikuwaona.
30 Na ikawa kwamba malaika akanizungumzia tena, akisema: Angalia! Na
nikaangalia, na kuona mbingu zikifunguka tena, na nikaona malaika wakiwashukia
watoto wa watu; na kuwahudumia.
31 Na akanizungumzia tena, akasema: Angalia! Na nikaangalia, na nikamwona
Mwanakondoo wa Mungu akienda miongoni mwa watoto wa watu. Na nikaona
umati wa watu waliokuwa wagonjwa, na ambao walikuwa wakiugua kutokana na
aina zote za magonjwa, pamoja na ibilisi na pepo wachafu; na malaika akazungumza
na kunionyesha hivi vitu vyote. Na wakaponywa kwa nguvu za Mwanakondoo wa
Mungu; na ibilisi pamoja na pepo wachafu wakafukuzwa.
32 Na ikawa kwamba malaika akanizungumzia tena, akisema: Angalia! Na
nikaangalia na nikamwona Mwanakondoo wa Mungu, kwamba alikamatwa na
watu; ndio, Mwana wa Mungu asiye na mwisho alihukumiwa na ulimwengu; na

niliona na kuyashuhudia.

33 Na mimi, Nefi, nikaona kwamba aliinuliwa juu ya msalaba na kuuawa kwa dhambi za ulimwengu.

34 Na baada ya yeye kusulubiwa nikaona umati wa dunia, ukiwa umekusanyika pamoja kupigana dhidi ya mitume wa Mwanakondoo; kwani hivi ndivyo wale kumi na wawili waliitwa na malaika wa Bwana.

35 Na umati wa dunia ulikusanyika pamoja; na nikaona kwamba walikuwa kwenye jengo kubwa na pana, kama jengo lile baba yangu aliloliona. Na malaika wa Bwana akanizungumzia tena, akisema: Tazama ulimwengu na hekima yake; ndio, tazama nyumba ya Israeli imekusanyika pamoja kupinga mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo.

36 Na ikawa kwamba niliona na ninashuhudia, kwamba lile jengo kuu na pana lilikuwa ni kiburi cha ulimwengu; na lilianguka, na muanguko wake ulikuwa mkuu zaidi. Na malaika wa Bwana akanizungumizia tena, akisema: Hivyo ndivyo mataifa yote, makabila yote, lugha zote, na watu wote, ambao wanawapinga wale mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo wataangamizwa.

## 1 Nefi 12

1 Na ikawa kwamba malaika akaniambia: Angalia, na uone uzao wako, na pia uzao wa kaka zako. Na nikaangalia na kuona nchi ya ahadi; na nikaona vikundi vya watu, ndio, hata hesabu yao ilikuwa nyingi kama mchanga wa bahari.

2 Na ikawa kwamba niliona vikundi vimekusanyika pamoja kupigana, moja dhidi ya mwingine; na nikaona vita, na uvumi wa vita, na mauaji makuu kwa upanga miongoni mwa watu wangu.

3 Na ikawa kwamba niliona vizazi vingi vikipita, baada ya vita vya namna hii na mabishano katika nchi; na nikaona miji mingi, ndio, hata sikuihesabu.

4 Na ikawa kwamba niliona ukungu mweusi usoni mwa nchi ya ahadi; na nikaona umeme, na nikasikia radi, na mitetemeko ya ardhi, na aina zote za misukosuko na makelele; na nikaona ardhi, na miamba, kwamba ilipasuka; na nikaona milima ikivunjika vipande vipande; na nikaona tambarare za ardhi, kwamba zilipasuka; na nikaona miji mingi imezama; na nikaona mingi iliyochomwa kwa moto; na nikaona mingi iliyoanguka chini, kwa sababu ya ile mitetemeko.

5 Na ikawa baada ya kuona vitu hivi, nikaona ule ukungu wa giza, ukitoweka kutoka usoni mwa ulimwengu; na tazama, nikaona makundi ya wale ambao hawakuanguka kwa sababu ya hukumu kuu ya kuhofisha kwa Bwana.

6 Na nikaona mbingu zikifunguka, na Mwanakondoo wa Mungu akiteremka kutoka mbinguni; na akashuka chini na akajionyesha kwao.

7 Na pia niliona na ninashuhudia kwamba Roho Mtakatifu aliwashukia wengine kumi na wawili; na walichaguliwa na kuteuliwa, na Mungu.

8 Na malaika akanizungumzia, na kusema: Tazama wale wanafunzi kumi na wawili wa Mwanakondoo, ambao wameteuliwa kuhudumia uzao wako.

9 Na akaniambia: Je, unawakumbuka wale mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo? Tazama ni wao watakaohukumu yale makabila kumi na mawili ya Israeli; kwa hivyo, wale wahudumu kumi na wawili wa uzao wako watahukumiwa na wao; kwani nyinyi ni wa nyumba ya Israeli.

10 Na hawa wahudumu kumi na wawili uwaonao watahukumu uzao wako. Na,

tazama, wao ni watakatifu milele; kwa sababu ya imani yao katika Mwanakondoo wa Mungu mavazi yao yanafanywa kuwa meupe kwa damu yake.

11 Na malaika akaniambia: Angalia! Na nikaangalia, na kuona vizazi vitatu vikiishi kwa utakatifu; na mavazi yao yalikuwa meupe kama ya Mwanakondoo wa Mungu. Na malaika akaniambia: Hawa wamefanywa kuwa weupe kwa damu ya Mwanakondoo, kwa sababu ya imani yao kwake.

12 Na mimi, Nefi, pia nikaona wengi katika kizazi cha nne wakiishi katika utakatifu.

13 Na ikawa kwamba niliona vikundi vya dunia vimekusanyika pamoja.

14 Na malaika akaniambia: Tazama uzao wako, na pia uzao wa kaka zako.

15 Na ikawa kwamba niliangalia na kuona watu wa uzao wangu wamekusanyika pamoja katika vikundi kupigana na uzao wa kaka zangu; na walikusanyika pamoja wapigane vita.

16 Na malaika akanizungumzia, akisema: Tazama chemchemi ya maji machafu ambayo baba yako aliiona; ndio, hata mto ambao aliuzungumzia; na kilindi chake ni kilindi cha jahanamu.

17 Na ukungu wa giza ni majaribio ya ibilisi, yanayopofusha macho, na ambayo inashupaza mioyo ya watoto wa watu, na kuwaelekeza kwenye njia pana, ili waangamie na kupotea.

18 Na jengo kubwa na pana, ambalo baba yako aliliona, ni mawazo yasiyofaa na kiburi cha watoto wa watu. Na shimo kubwa la kuhofisha linawagawanya; ndio, hata neno la haki la Mungu wa Milele, na Masiya ambaye ni Mwanakondoo wa Mungu, ambaye anashuhudiwa na Roho Mtakatifu, tangu mwanzo wa ulimwengu hadi sasa, na tangu sasa hadi milele.

19 Na wakati malaika alipokuwa akisema maneno haya, nikatazama na kuona kwamba uzao wa kaka zangu walichokozana na uzao wangu, kulingana na maneno ya malaika; na kwa sababu ya kiburi cha uzao wangu, na majaribio ya ibilisi, nikaona kwamba uzao wa kaka zangu waliwashinda watu wa uzao wangu.

20 Na ikawa kwamba nilitazama, na kuona kwamba watu wa uzao wa kaka zangu waliwashinda uzao wangu; na wakendelea mbele katika vikundi kwenye uso wa nchi.

21 Na nikawaona wamekusanyika pamoja katika vikundi; na nikaona vita na uvumi wa vita miongoni mwao; na nikaona vizazi vingi vikiishi kwenye vita na uvumi wa vita.

22 Na malaika akaniambia: Tazama hawa watafifia katika kutoamini.

23 Na ikawa kwamba niliona, baada ya wao kufifia katika kutoamini wakawa watu wa giza, wenye makuruhu, wenye uchafu, waliojaa uzembe na kila aina ya machukizo.

# 1 Nefi 13

1 Na ikawa kwamba malaika akanizungumzia, akisema: Angalia! Na nikaangalia na kuona mataifa mengi na falme nyingi.

2 Na malaika akaniambia: Nini unachoona? Na nikasema: Naona mataifa mengi na falme nyingi.

3 Na akaniambia: Haya ni mataifa na falme za Wayunani.

4 Na ikawa kwamba niliona miongoni mwa mataifa ya Wayunani mwanzo wa kanisa kuu.

5 Na malaika akaniambia: Tazama mwanzo wa kanisa ambalo lina machukizo
mengi zaidi ya makanisa yote mengine, ambalo linawaua watakatifu wa Mungu,
ndio, na kuwatesa na kuwafunga, na kuwatia nira ya chuma, na kuwapeleka
utumwani.
6 Na ikawa kwamba niliona hili kanisa kuu la machukizo; na nikaona ibilisi,
kwamba ndiye alikuwa mwanzilishi wake.
7 Na pia nikaona dhahabu, na fedha, na hariri, na nguo za rangi nyekundu, na
kitani nzuri, na kila aina ya nguo ya thamani; na nikaona makahaba wengi.
8 Na malaika akanizungumzia, akisema: Tazama, dhahabu, na fedha, na hariri, na
nguo za rangi nyekundu, na kitani nzuri, na nguo ya thamani, na makahaba, ni
tamaa za kanisa hili kuu la machukizo.
9 Na pia kwa sababu ya sifa za ulimwengu wanawaua watakatifu wa Mungu, na
kuwapeleka utumwani.
10 Na ikawa kwamba niliangalia na kuona maji mengi; na yaliwagawanya Wayunani
kutoka kwa uzao wa kaka zangu.
11 Na ikawa kwamba malaika akaniambia: Tazama ghadhabu ya Mungu iko juu ya
uzao wa kaka zako.
12 Na nikaangalia na kuona mtu miongoni mwa Wayunani, ambaye alitenganishwa
kutokana na uzao wa kaka zangu na yale maji mengi; na nikaona Roho ya Mungu,
kwamba ilishuka na kumshawishi mtu huyo; na akasafiri kwa yale maji mengi, hadi
akaufikia uzao wa kaka zangu, kwenye nchi ya ahadi.
13 Na ikawa kwamba niliona Roho ya Mungu, kwamba iliwashawishi Wayunani
wengine, na walitoka utumwani, na kusafiri kwenye maji mengi.
14 Na ikawa kwamba niliona vikundi vingi vya Wayunani katika nchi ya ahadi; na
nikaona ghadhabu ya Mungu, kwamba ilikuwa juu ya uzao wa kaka zangu; na
wakatawanywa na Wayunani na kupigwa.
15 Na nikaona Roho ya Bwana, kwamba ilikuwa juu ya Wayunani, na wakafanikiwa
na kupata nchi kwa urithi wao; na nikaona kwamba walikuwa weupe, na warembo
zaidi, kama watu wangu kabla hawajauawa.
16 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliona kwamba Wayunani waliotoka utumwani
walinyenyekea kwa Bwana; nao walikuwa na nguvu za Bwana.
17 Na nikaona kwamba waasili wa Wayunani walikusanyika pamoja kwenye maji, na
pia kwenye ardhi, ili kupigana dhidi yao.
18 Na nikaona kwamba walikuwa na nguvu za Bwana, na pia kwamba ghadhabu ya
Mungu ilikuwa juu ya wale wote waliokusanyika pamoja kupigana dhidi yao.
19 Na mimi, Nefi, nikaona kwamba wale Wayunani ambao walitoka utumwani
walikombolewa na nguvu za Mungu kutoka mikononi mwa mataifa mengine yote.
20 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliona kwamba walifanikiwa nchini; na nikaona
kitabu, ambacho walikuwa nacho miongoni mwao.
21 Na malaika akaniambia: Je, unajua maana ya hicho kitabu?
22 Na nikamjibu: Sijui.
23 Na akaniambia: Tazama kinatokana na kinywa cha Myahudi. Na mimi, Nefi,
nikakiona; na akaniambia: Kitabu unachokiona ni maandishi ya Wayahudi,
ambacho kina maagano ya Bwana, ambayo aliagana na nyumba ya Israeli; na pia
kina unabii mwingi wa manabii watakatifu; na ni maandishi kama michoro iliyo
katika bamba za shaba nyekundu, ila tu sio nyingi vile; walakini, zina maagano ya
Bwana, ambayo aliagana na nyumba ya Israeli; kwa hivyo, zina thamani kubwa kwa

Wayunani.
24 Na malaika wa Bwana akaniambia: Wewe umeona kwamba hicho kitabu
kilitoka kwenye kinywa cha Myahudi; na wakati kilitoka kwenye kinywa cha
Myahudi kilikuwa na utimilifu wa injili ya Bwana, ambaye anashuhudiwa na
mitume kumi na wawili; na wanashuhudia kulingana na ukweli ambao uko na
Mwanakondoo wa Mungu.
25 Kwa hivyo, vitu hivi vinatoka kwa usafi kutoka kwa Wayahudi na kuwafikia
Wayunani, kulingana na ukweli wa Mungu.
26 Na baada ya kusonga mbele kwa mikono ya wale mitume kumi na wawili wa
Mwanakondoo, kutoka kwa Wayahudi hadi kwa Wayunani, wewe unaona mwanzo
wa lile kanisa kuu la machukizo, ambalo lina machukizo zaidi ya makanisa yote;
kwani tazama, wameondoa kutoka kwa injili ya Mwanakondoo sehemu nyingi
ambazo ni wazi na zenye thamani; na pia wamepunguza maagano mengi ya Bwana.
27 Na haya yote wamefanya kwamba wachafue njia nzuri za Bwana, kwamba
wapofushe macho na kushupaza mioyo ya watoto wa watu kuwa migumu.
28 Kwa hivyo, wewe umeona kwamba baada ya hicho kitabu kusonga mbele kupitia
mikono ya hilo kanisa kuu la machukizo, kwamba vitu vingi vilivyo wazi na vyenye
thamani viliondolewa kutoka kwenye hicho kitabu, ambacho ni kitabu cha
Mwanakondoo wa Mungu.
29 Na baada ya hivi vitu vilivyo wazi na vyenye thamani kutolewa kiliyafikia mataifa
yote ya Wayunani; na baada ya kufikia mataifa yote ya Wayunani, ndio, hata
ng'ambo ya yale maji mengi ambayo uliona wale Wayunani wakitoka utumwani,
wewe unaona — kwa sababu ya kuondolewa kwa vitu vingi vilivyo wazi na vyenye
thamani kutoka hicho kitabu, ambavyo vilikuwa wazi na kueleweka na watoto wa
watu, kulingana na udhahiri ulio katika Mwanakondoo wa Mungu — kwa sababu ya
kuondolewa kwa vitu hivi ambavyo vimetoka kwa injili ya Mwanakondoo, wengi
zaidi wamepotea, ndio, mpaka Shetani ana nguvu juu yao.
30 Walakini, wewe umeona kwamba wale Wayunani waliotoka utumwani, na
wakainuliwa kwa nguvu za Mungu juu ya mataifa mengine yote, usoni mwa nchi
ambayo ni nchi bora zaidi ya nchi zingine, ambayo ndio nchi Bwana Mungu
aliagana na baba yako kwamba uzao wake watapata kuwa nchi yao ya urithi; kwa
hivyo, unaona kwamba Bwana Mungu hatakubali kwamba Wayunani
wawaangamiza kabisa mchanganyiko wa uzao wako, ulio miongoni mwa kaka zako.
31 Wala hatakubali kwamba Wayunani waiangamize uzao wa kaka zako.
32 Wala Bwana Mungu hatakubali kwamba Wayunani wataishi milele katika hali
hiyo mbaya ya upofu, ambayo umeona wanayo, kwa sababu ya sehemu zilizo wazi na
zenye thamani za injili ya Mwanakondoo ambazo zimefichwa na lile kanisa la
machukizo, ambalo umeona uanzilishi wake.
33 Kwa hivyo asema Mwanakondoo wa Mungu: Nitawarehemu Wayunani, kwa
kutembelea sazo la nyumba ya Israeli kwa hukumu kuu.
34 Na ikawa kwamba malaika wa Bwana akanizungumzia, akisema: Tazama, asema
Mwanakondoo wa Mungu, baada ya kuadhibu sazo la nyumba ya Israeli — na haya
sazo hili ambalo nalizungumzia ni uzao wa baba yako — kwa hivyo, baada ya
kuwaadhibu kwa hukumu, na kuwapiga kwa mkono wa Wayunani, na baada ya
Wayunani kupotea zaidi, kwa sababu ya kufichwa kwa sehemu za injili ambazo ni
muhimu na kanisa la machukizo, ambalo ni mama ya makahaba, asema
Mwanakondoo — nitakuwa na huruma kwa Wayunani siku hiyo, hata kwamba

nitawaletea, kwa nguvu zangu, wingi wa injili yangu ambayo itakuwa wazi na yenye
thamani, asema Mwanakondoo.
35 Kwani, tazama, asema Mwanakondoo: Nitajidhirihisha kwa uzao wako, kwamba
wataandika vitu vingi ambavyo nitawahudumia, ambavyo vitakuwa wazi na vyenye
thamani; na baada ya uzao wako kuangamizwa, na kufifia katika kutoamini, pia na
uzao wa kaka zako, tazama, vitu hivi vitafichwa, na kutolewa kwa Wayunani, kwa
karama na nguvu za Mwanakondoo.
36 Na kwa hayo itaandikwa injili yangu, asema Mwanakondoo, na mwamba wangu
na wokovu wangu.
37 Heri wale ambao watatafuta kujenga Sayuni yangu katika siku ile, kwani
watapata karama na nguvu za Roho Mtakatifu; na wakivumilia hadi siku ya mwisho
watainuliwa katika siku ya mwisho, na wataokolewa katika ufalme usio na mwisho
wa Mwanakondoo; na yeyote atakayetangaza amani, ndio, habari za shangwe, jinsi
gani watakavyokuwa warembo milimani.
38 Na ikawa kwamba niliona sazo la uzao wa kaka zangu, na pia kitabu cha
Mwanakondoo wa Mungu, ambacho kilitoka kwenye kinywa cha Myahudi,
kwamba kilitokana na Wayunani na kuwafikia masazo ya uzao wa kaka zangu.
39 Na baada ya kuwafikia nikaona vitabu vingine, ambavyo vilitolewa kwa nguvu za
Mwanakondoo, kutoka kwa Wayunani hadi kwao, ili kuwasadikisha Wayunani na
sazo la uzao wa kaka zangu, na pia Wayahudi waliotawanywa kote usoni mwa dunia,
kwamba maandishi ya manabii na wale mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo
ni kweli.
40 Na malaika akanizungumzia, akisema: Haya maandishi ya mwisho, ambayo
umeona miongoni mwa Wayunani, yatathibitisha juu ya kweli kwa yale ya kwanza,
ambayo ni ya wale mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo, na yatafahamisha
vitu vilivyo wazi na vyenye thamani viliyotolewa kutoka kwao; na yatafahamisha
makabila yote, lugha zote, na watu wote, kwamba Mwanakondoo wa Mungu ndiye
Mwana wa Baba wa Milele, na Mwokozi wa ulimwengu; na kwamba lazima watu
wote wamkubali yeye, kama sio hivyo, hawawezi kuokolewa.
41 Na ni lazima wamkubali kulingana na yale maneno ambayo yatanenwa kwa
kinywa cha Mwanakondoo; na maneno ya Mwanakondoo yatafumbuliwa katika
maandishi ya uzao wako, vile vile katika maandishi ya wale mitume kumi na wawili
wa Mwanakondoo; kwa hivyo zote mbili zitaunganishwa kuwa moja; kwani kuna
Mungu mmoja na Mchungaji mmoja ulimwenguni kote.
42 Na wakati unafika atakapojidhihirisha mwenyewe kwa mataifa yote, kwa
Wayahudi na pia kwa Wayunani; na baada ya kujidhihirisha mwenyewe kwa
Wayahudi na pia kwa Wayunani, ndipo atajidhihirisha mwenyewe kwa Wayunani
na pia kwa Wayahudi, na wa mwisho atakuwa wa kwanza, na wa kwanza atakuwa wa
mwisho.

# 1 Nefi 14

1 Na itakuwa kwamba, ikiwa Wayunani watamsikiliza Mwanakondoo wa Mungu
katika siku hiyo atajidhirishia kwa neno, pia kwa nguvu, na kwa kila kitendo, kwa
kuwaondolea vikwazo vyao—
2 Na wasishupaze mioyo yao dhidi ya Mwanakondoo wa Mungu, watahesabiwa
miongoni mwa uzao wa baba yako; ndio, watahesabiwa miongoni mwa nyumba ya

Israeli; na watakuwa watu wenye baraka za milele katika nchi ya ahadi; hawatatiwa
utumwani tena; na nyumba ya Israeli haitachanganywa tena.
3 Na lile shimo kuu, walilochimbiwa na lile kanisa kuu la machukizo, ambalo
lilianzishwa na ibilisi na wana wake, ili aelekeze nafsi za watu hadi jahanamu — ndio,
lile shimo kuu ambalo limechimbwa kwa maangamizo ya watu, litajazwa na wale
waliolichimba, kwa kuangamizwa kwao kabisa, asema Mwanakondoo wa Mungu;
sio maangamizo ya nafsi, bali ni kutupwa katika jahanamu isiyo na mwisho.
4 Kwani tazama, hii ni kulingana na utumwa wa ibilisi, na pia kulingana na haki ya
Mungu, kwa wale wote watakaotenda uovu na machukizo mbele yake.
5 Na ikawa kwamba malaika alinizungumzia mimi, Nefi, akisema: Wewe umeona
kwamba Wayunani wakitubu itakuwa vyema kao; na pia wewe unajua kuhusu
maagano ya Bwana na nyumba ya Israeli; na pia wewe umesikia kwamba yeyote
asiyetubu lazima aangamie.
6 Kwa hivyo, ole kwa Wayunani ikiwa watashupaza mioyo yao dhidi ya
Mwanakondoo wa Mungu.
7 Kwani wakati unafika, asema Mwanakondoo wa Mungu, kwamba nitatenda kazi
kuu na ya maajabu miongoni mwa watoto wa watu; kazi ambayo haitakuwa na
mwisho, pengine kwa upande mmoja au kwa mwingine — labda kuwasadikisha kwa
amani na uzima wa milele, au kwa kuwakabidhi kwa ugumu wa mioyo yao na upofu
wa fikira zao na kuwatia utumwani, na pia katika maangamizo, ya kimwili na kiroho,
kulingana na utumwa wa ibilisi, ambao nimeuzungumzia.
8 Na ikawa kwamba wakati malaika alipokuwa amenizungumzia maneno haya,
akaniambia: Wewe unakumbuka maagano ya Baba na nyumba ya Israeli?
Nikamwambia, Ndio.
9 Na ikawa kwamba akaniambia: Angalia, na tazama lile kanisa kuu na la
machukizo, ambalo ni mama wa machukizo, ambaye mwanzilishi wake ni ibilisi.
10 Na akaniambia: Tazama kuna ila tu makanisa mawili pekee; moja ni kanisa la
Mwanakondoo wa Mungu, na lingine ni kanisa la ibilisi; kwa hivyo, yule ambaye sio
wa kanisa la Mwanakondoo wa Mungu ni wa kanisa lile kuu, ambalo ni mama wa
machukizo; na yeye ni kahaba wa ulimwengu wote.
11 Na ikawa kwamba niliangalia na kuona kahaba wa ulimwengu wote, na aliketi
kwenye maji mengi; na alikuwa na mamlaka ulimwenguni kote, miongoni mwa
mataifa yote, makabila yote, lugha zote, na watu.
12 Na ikawa kwamba niliona kanisa la Mwanakondoo wa Mungu, na hesabu yake
ilikuwa chache, kwa sababu ya uovu na machukizo ya kahaba aliyeketi kwenye maji
mengi; walakini, nikaona kwamba kanisa la Mwanakondoo, ambao walikuwa ni
watakatifu wa Mungu, pia nao walikuwa kote usoni mwa dunia; na utawala wao
usoni mwa dunia yalikuwa madogo, kwa sababu ya uovu wa yule kahaba mkuu
niliyemuona.
13 Na ikawa kwamba niliona kuwa yule mama mkuu wa machukizo alikusanya
pamoja vikundi usoni mwote mwa dunia, miongoni mwa mataifa yote ya Wayunani,
ili kupigana dhidi ya Mwanakondoo wa Mungu.
14 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliona nguvu za Mwanakondoo wa Mungu,
kwamba ziliwashukia watakatifu wa kanisa la Mwanakondoo, na kwa watu wa
agano wa Bwana, ambao walitawanyika kote usoni mwa dunia; na walikuwa
wamejikinga kwa utakatifu na kwa nguvu za Mungu katika utukufu mkuu.
15 Na ikawa kwamba ghadhabu ya Mungu ililiteremkia lile kanisa kuu la

machukizo, hata kukawa na vita na uvumi wa vita miongoni mwa mataifa yote na makabila yote duniani.

16 Na kulipoanza kuwa na vita na uvumi wa vita miongoni mwa mataifa yote ambayo yalikuwa ya mama wa machukizo, malaika akanizungumzia, akisema: Tazama, ghadhabu ya Mungu imemteremkia mama wa makahaba; na tazama, wewe unaona vitu hivi vyote—

17 Na siku itakapofika wakati ghadhabu ya Mungu itamteremkia mama wa makahaba, ambalo ni lile kanisa kuu la machukizo ulimwenguni mwote, ambaye mwanzilishi wake ni ibilisi, katika siku ile, kazi ya Baba itaanza, katika kutayarisha matimizo ya maagano yake, ambayo ameagana na watu wake ambao ni wa nyumba ya Israeli.

18 Na ikawa kwamba malaika akanizungumzia, akisema: Angalia!

19 Na nikaangalia na kumwona mtu, na alikuwa amevalia joho leupe.

20 Na malaika akaniambia: Tazama mmoja wa wale mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo.

21 Tazama, ataona na kuandika vitu hivi vilivyobaki; ndio, na pia vitu hivi vingi vilivyokuwepo.

22 Na pia ataandika kuhusu mwisho wa ulimwengu.

23 Kwa hivyo, vitu hivyo atakavyoandika ni vya haki na kweli; na tazama vimeandikwa kwenye kitabu ulichoona kikitoka kwenye kinywa cha Myahudi; na wakati kwenye kinywa cha Myahudi, au, wakati kitabu kilitoka kinywani mwa Myahudi, vitu vilivyoandikwa vilikuwa wazi na vitakatifu, na vyenye thamani na rahisi kueleweka na watu wote.

24 Na tazama, vitu ambavyo huyu mtume wa Mwanakondoo ataandika ni vitu vingi ambavyo umeona; na tazama, vilivyosalia wewe utaviona.

25 Lakini vitu utakavyoona baadaye wewe hutaviandika; kwani Bwana Mungu amemchagua mtume wa Mwanakondoo wa Mungu aviandike.

26 Na pia wengine ambao wameishi, kwao amewaonyesha vitu vyote, na wameviandika; na vimefungwa na vitatokea kwa usafi, kulingana na ukweli ulio na Mwanakondoo, na hivi vitakuwa katika wakati wa Bwana, kwa nyumba ya Israeli.

27 Na mimi, Nefi, nilisikia na ninashuhudia, kwamba jina la yule mtume wa Mwanakondoo lilikuwa ni Yohana, kulingana na neno la malaika.

28 Na tazama, mimi, Nefi, nimekatazwa kwamba nisiandike vitu vilivyokuwa vimebaki ambavyo niliviona na kusikia; kwa hivyo vitu ambavyo nimeandika vimenitosha; na nimeandika sehemu ndogo tu ya yale niliyoona.

29 Ninashuhudia kwamba niliona vile vitu ambavyo baba yangu aliviona, na malaika wa Bwana alinifahamisha hayo.

30 Na sasa nakoma kuzungumza kuhusu vile vitu ambavyo niliviona nilipokuwa nimenyakuliwa na Roho; na ikiwa vitu vyote ambavyo niliviona havijaandikwa, vile vitu ambavyo nimeviandika ni vya kweli. Na hivyo ndivyo ilivyo. Amina.

## 1 Nefi 15

1 Na ikawa kwamba baada ya mimi, Nefi, kunyakuliwa katika roho, na kuona vitu hivi vyote, nilirudi kwenye hema la baba yangu.

2 Na ikawa kwamba niliona kaka zangu, na walikuwa wakibishana kuhusu vile vitu ambavyo baba yangu aliwazungumzia.

3 Kwa kweli aliwazungumzia vitu vikubwa, vilivyokuwa vigumu kueleweka, isipokuwa mtu amuulize Bwana; na wao wakiwa wagumu mioyoni mwao, kwa hivyo hawakumtazama Bwana jinsi ilivyowapasa.

4 Na sasa mimi, Nefi, nilihuzunika kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao, na pia, kwa sababu ya vitu ambavyo niliviona, na nilijua lazima vitimizwe kwa sababu ya uovu mkuu wa wanadamu.

5 Na ikawa kwamba nililemewa na masumbuko yangu, kwa maana nilidhani kwamba masumbuko yangu yalizidi yote, kwa sababu ya kuangamia kwa watu wangu, kwani nilikuwa nimeona kuanguka kwao.

6 Na ikawa kwamba baada ya kupokea nguvu nikawazungumzia kaka zangu, nikitaka kujua chanzo cha ugomvi wao.

7 Na wakasema: Tazama, hatuwezi kuelewa maneno ambayo baba yetu amesema kuhusu matawi ya asili ya mti wa mzeituni, na pia kuhusu Wayunani.

8 Na nikawaambia: Je mmemuuliza Bwana?

9 Na wakasema: Hapana; kwani Bwana hatujulishi vitu hivi.

10 Tazama, nikawaambia: Kwa nini hamtii amri za Bwana? Kwa nini mwangamie, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu?

11 Kwani hamkumbuki vitu ambavyo Bwana amesema?—Kama hamtashupaza mioyo yenu, na mniulize kwa imani, mkiamini kwamba mtapokea, kwa bidii katika kutii amri zangu, kwa kweli vitu hivi vitafanywa vijulikane kwenu.

12 Tazama, nawaambia, kuwa nyumba ya Israeli ililinganishwa na mti wa mzeituni, na Roho ya Bwana aliyekuwa ndani ya baba yetu; na tazama si sisi tumetokana na nyumba ya Israeli, na si sisi ni tawi la nyumba ya Israeli?

13 Na sasa, kitu ambacho baba yetu anamaanisha kuhusu kupandikizwa kwa matawi ya asili kwa kupitia utimilifu wa Wayunani, ni, kwamba katika siku za baadaye, wakati uzao wetu utakuwa umefifia katika kutoamini, ndio, kwa muda wa miaka mingi, na vizazi vingi baada ya Masiya kudhihirishwa katika mwili kwa watoto wa watu, ndipo utimilifu wa injili ya Masiya utawafikia Wayunani, na kutoka kwa Wayunani hadi kwa sazo la uzao wetu—

14 Na katika siku ile sazo la uzao wetu litajua kwamba wao ni wa nyumba ya Israeli, na kwamba wao ni watu wa agano la Bwana; na kisha watajua na pia kupata ufahamu wa babu zao, na pia ufahamu wa injili ya Mkombozi wao, ambayo aliwahudumia babu zao; kwa hivyo, watamfahamu Mkombozi wao na mambo halisi ya mafundisho yake, ili waweze kujua jinsi ya kumkaribia na waokolewe.

15 Na basi katika siku ile, si watashangilia na kumsifu Mungu asiye na mwisho, mwamba wao na wokovu wao? Ndio, katika siku ile, si watapokea nguvu na malisho kutoka kwa ule mzabibu wa kweli? Ndio, si wataungana na zizi la kweli la Mungu?

16 Na tazama, nawaambia, Ndio; watakumbukwa tena miongoni mwa nyumba ya Israeli; watapandikizwa ndani, wakiwa tawi la asili la mti wa mzeituni, kwenye mti wa mzeituni wa kweli.

17 Na hii ndio baba yetu anamaanisha; na anamaanisha kwamba haitatimizwa hadi watawanywe na Wayunani; na anamaanisha itatimizwa na Wayunani, ili Bwana awaonyeshe Wayunani nguvu zake, na kwa sababu hii atakataliwa na Wayahudi, au na nyumba ya Israeli.

18 Kwa hivyo, baba yetu hajazungumza juu ya uzao wetu pekee, lakini pia nyumba yote ya Israeli, akilenga agano ambalo litatimizwa katika siku za baadaye; agano ambalo Bwana aliagana na baba yetu Ibrahimu, akisema: Kwa uzao wako makabila

yote ya dunia yatabarikiwa.
19 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwaambia mengi kuhusu vitu hivi; ndio, niliwaambia kuhusu uamsho wa Wayahudi katika siku za baadaye.
20 Na nikawasimulia maneno ya Isaya, ambaye alizungumza kuhusu kurudi kwa Wayahudi, au nyumba ya Israeli; na baada ya wao kuamshwa hawatachanganyika tena, wala kutawanyika tena. Na ikawa kwamba niliwaelezea kaka zangu maneno mengi, hata kwamba waliridhika na wakajinyenyekeza mbele ya Bwana.
21 Na ikawa kwamba walinizungumzia tena, wakisema: Kitu hiki kinamaanisha nini ambacho Baba yetu alikiona ndotoni? Nini maana ya ule mti aliouona?
22 Na nikawaambia: Ni kielelezo cha mti wa uzima.
23 Na wakaniambia: Nini maana ya fimbo ya chuma ambayo baba aliona, ikielekeza kwenye ule mti?
24 Na nikawaambia kwamba ilikuwa neno la Mungu; na yeyote atakayesikiza hilo neno la Mungu, na alizingatie, hataangamia; wala majaribu na mishale ya moto ya adui kuwalemea na kuwapofusha, ili kuwaelekeza kwenye maangamio.
25 Kwa hivyo, mimi, Nefi, niliwasihi wasikize neno la Bwana; ndio, niliwasihi kwa nguvu zote za nafsi yangu, na kwa uwezo wote ambao nilikuwa nao, kwamba wasikilize neno la Mungu na wakumbuke kutii amri zake kila wakati katika vitu vyote.
26 Na wakaniuliza: Nini maana ya ule mto ambao baba yetu aliuona?
27 Na nikawaambia kwamba yale maji ambayo baba aliona ni uchafu; na mawazo yake yalikuwa yamemezwa katika vitu vingine kwamba hakuona uchafu wa yale maji.
28 Nikawaambia kwamba lilikuwa ni shimo la kuogopesha, ambalo liligawanya waovu kutokana na mti wa uzima, na pia kutoka kwa watakatifu wa Mungu.
29 Nikawaambia kwamba ilikuwa kielelezo cha ile jahanamu ya kuogopesha, ambayo yule malaika aliniambia imetayarishwa kwa waovu.
30 Na nikawaambia kwamba baba yetu pia aliona kwamba haki ya Mungu imewatenga waovu kutoka kwa watakatifu; na mng'aro wake ulikuwa ni kama mng'aro wa moto, ambao unapaa kwa Mungu milele na milele, bila mwisho.
31 Na wakaniambia: Je, hii inamaanisha mateso ya mwili wakati wa majaribio, au hali ya mwisho ya nafsi baada ya kifo cha mwili, au inazungumza kuhusu vitu ambavyo ni vya muda?
32 Na ikawa kwamba niliwaambia kuwa ilikuwa ni kielelezo cha vitu ambavyo ni vya muda na kiroho; kwa maana siku itafika watakapohukumiwa kulingana na matendo yao, ndio, hata matendo yaliyotendwa katika mwili wa muda katika siku zao za majaribio.
33 Kwa hivyo, wakifa katika uovu wao lazima watupwe pia, kulingana na vitu vya kiroho, ambavyo vinalingana na utakatifu; kwa hivyo, lazima waletwe kusimama mbele ya Mungu, wahukumiwe kulingana na matendo yao; na kama matendo yao yalikuwa machafu lazima wao wawe wachafu; na kama wao ni wachafu lazima iwe kwamba hawawezi kuishi katika ufalme wa Mungu; au ikiwa hivyo, ufalme wa Mungu lazima uwe mchafu pia.
34 Lakini tazama, nawaambia, ufalme wa Mungu sio mchafu, na hakuna kitu chochote kichafu kiwezacho kuingia katika ufalme wa Mungu; kwa hivyo lazima pawe na mahali pa uchafu ambapo pametayarishiwa yale ambayo ni machafu.
35 Na kuna pahali pametayarishwa, ndio, hata ile jahanamu ya kuogofya ambayo nimeizungumzia, na ibilisi ndiye mtayarishaji; kwa hivyo hali ya mwisho ya nafsi za

wanadamu ni kuishi katika ufalme wa Mungu, au kutupwa nje kwa sababu ya ile
haki ambayo nimezungumzia.
36 Kwa hivyo, waovu wamekataliwa kutoka kwa watakatifu, na pia kutoka kwa mti
wa uzima, ambao matunda yake ni yenye thamani na bora zaidi ya matunda
mengine; ndio, na ni karama ya Mungu ambayo ni kuu zaidi ya karama zote. Na
hivyo ndivyo nilivyowazungumzia kaka zangu. Amina.

# 1 Nefi 16

1 Na sasa ikawa kwamba baada ya mimi, Nefi, kumaliza kuwazungumzia kaka zangu,
tazama wakaniambia: Wewe umetuelezea vitu vigumu, kuliko tunavyoweza
kuvumilia.
2 Na ikawa kwamba niliwaambia kuwa nilijua kwamba nilikuwa nimezungumza
vitu vigumu kinyume cha waovu, kulingana na ukweli; na nilikuwa
nimewathibitisha wenye haki, na kushuhudia kwamba watainuliwa katika siku ya
mwisho; kwa hivyo, wenye hatia huchukua ukweli kuwa mgumu, kwani huwakata
hadi sehemu zao za ndani.
3 Na sasa kaka zangu, kama nyinyi mngekuwa watakatifu na mngetaka kusikiza
ukweli, na kuufuata, ili mtembee imara mbele ya Mungu, basi hamngenung'unika
kwa sababu ya ukweli, mkisema: Unazungumza vitu vigumu dhidi yetu.
4 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwasihi kaka zangu, kwa bidii zote, watii amri
za Bwana.
5 Na ikawa kwamba walijinyenyekesha kwa Bwana; hata kwamba nikawa na
shangwe na matumaini mengi, kwamba watatembea katika njia za utakatifu.
6 Sasa, vitu hivi vyote vilizungumziwa na kufanyika vile baba yangu alipoishi
kwenye hema katika bonde aliloliita Lemueli.
7 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nilimchukua binti mmoja wa Ishmaeli kuwa mke
wangu, na pia kaka zangu wakaoa mabinti za Ishmaeli; na pia Zoramu akamwoa
binti mkubwa wa Ishmaeli.
8 Na hivyo baba yangu alitimiza amri zote ambazo alipewa na Bwana. Na pia,
mimi, Nefi, nilibarikiwa na Bwana zaidi.
9 Na ikawa kwamba sauti ya Bwana ikamzungumzia baba yangu usiku, na
kumwamuru kwamba kesho yake aanze kusafiri nyikani.
10 Na ikawa kwamba wakati baba yangu alipoamka asubuhi, na akaenda mlangoni
mwa hema, kwa mshangao wake mkuu, akaona hapo chini mpira wa ufundi
maalumu; na ulikuwa wa shaba nyeupe ya hali ya juu. Na ndani ya huu mpira
kulikuwa mishale miwili; na moja ilionyesha njia tutakayofuata nyikani.
11 Na ikawa kwamba tulikusanya pamoja vitu ambavyo tungebeba nyikani, na pia
mabaki ya maakuli ambayo Bwana alikuwa ametupatia; na tukachukua mbegu za
kila aina ili tubebe nyikani.
12 Na ikawa kwamba tulichukua hema zetu na kuelekea nyikani, na tukavuka
ng'ambo ya mto Lamani.
13 Na ikawa kwamba tulisafiri kwa muda wa siku nne, tukielekea karibu upande wa
kusini-kusini-mashariki, na tukapiga hema zetu tena; na tukaita mahali pale Shazeri.
14 Na ikawa kwamba tulichukua pinde zetu na mishale yetu, na kuenda nyikani
kuwindia jamii zetu; na baada ya kuwindia jamii zetu chakula tulirejea tena kwa
jamii zetu huko nyikani, mahali palipoitwa Shazeri. Na tulisafiri tena nyikani,

tukielekea upande ule ule, tukifuata sehemu ambazo zilikuwa nzuri nyikani, ambazo
zilikuwa mipakani mwa Bahari ya Shamu.
15 Na ikawa kwamba tulisafiri kwa muda wa siku nyingi, tukiwinda chakula chetu
njiani, kwa pinde zetu na mishale yetu na mawe yetu na kwa kombeo zetu.
16 Na tulifuata majira ya ule mpira, ambayo ilituelekeza katika sehemu zenye rutuba
zaidi nyikani.
17 Na baada ya kusafiri kwa muda wa siku nyingi, tukapiga hema zetu kwa muda
mfupi, ili tujipumzishe tena na tutafutie jamii zetu chakula.
18 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nilipoenda kuwinda, tazama, nikavunja upinde
wangu, ambao ulikuwa umetengenezwa kwa chuma nyororo; na baada ya kuvunja
upinde wangu, tazama, ndugu zangu walinikasirikia kwa kupotelewa na upinde
wangu, kwa sababu hatukupata chakula chochote.
19 Na ikawa kwamba tulirudi kwa jamii zetu bila chakula, na wakiwa wamechoka
zaidi, kwa sababu ya kusafiri, waliteseka sana kwa kutaka chakula.
20 Na ikawa kwamba Lamani na Lemueli na wana wa Ishmaeli walianza
kunung'unika zaidi, kwa sababu ya mateso yao na masumbuko huko nyikani; na pia
baba yangu alianza kumnung'unikia Bwana, Mungu wake; ndio, na wote walikuwa
na huzuni zaidi, hata wakamnung'unikia Bwana.
21 Sasa ikawa kwamba mimi, Nefi, nikiwa nimeumizwa na kaka zangu kwa sababu
ya kupotelewa na upinde wangu, na pinde zao zikiwa zimelegea na zimenyumbuka,
ilianza kuwa shida zaidi, ndio, hata tukakosa chakula.
22 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwazungumzia kaka zangu, kwa sababu
walikuwa wameshupaza mioyo yao tena, hata wakamnung'unikia Bwana Mungu
wao.
23 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nikatengeneza upinde kutoka kwa mbao, na
kutoka kwa kijiti kinyoofu, nikatengeneza mshale; kwa hivyo, nikajiami kwa upinde,
na mshale, kombeo na mawe. Na nikamuuliza baba yangu: Niende kuwinda wapi?
24 Na ikawa kwamba akamuomba Bwana, kwani walijinyenyekeza kwa sababu ya
maneno yangu; kwani niliwaambia vitu vingi kwa nguvu za nafsi yangu.
25 Na ikawa kwamba sauti ya Bwana ikamjia baba yangu; na akakemewa kwa kweli
kwa kumnung'unikia Bwana, hadi akadhilika kwa huzuni mwingi.
26 Na ikawa kwamba sauti ya Bwana ikamwambia: Angalia kwenye ule mpira, na
uone vitu vilivyoandikwa.
27 Na ikawa kwamba wakati baba yangu alipoona vitu vilivyoandikwa kwenye
mpira, aliogopa na kutetemeka sana, pia na kaka zangu, na wana wa Ishmaeli na
wake zetu.
28 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliona kwamba vile vyuma vilivyokuwa kwenye
mpira, vilifanya kazi kulingana na imani na bidii na utiifu, ambao tulivipatia.
29 Na pia paliandikwa juu yao maandishi mengine mapya, ambayo yalikuwa rahisi
kwa kusomwa, ambayo yalitupatia ufahamu kuhusu njia za Bwana; na yaliandikwa
na kubadilishwa mara kwa mara, kulingana na imani na bidii ambayo tuliipatia. Na
hivyo tunaona kwamba kwa njia ndogo Bwana anaweza kuleta vitu vikubwa.
30 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nilienda juu ya mlima, kulingana na maelezo
yaliyokuwa kwenye mpira.
31 Na ikawa kwamba niliwinda wanyama wa mwitu, hata nikapata chakula cha
jamii zetu.
32 Na ikawa kwamba nilirudi kwenye hema zetu, nikibeba wanyama ambao

niliwinda; na sasa walipoona nilikuwa nimepata chakula, walifurahia sana! Na
ikawa kwamba walijinyenyekeza kwa Bwana, na wakamtolea shukrani.
33 Na ikawa kwamba tulianza safari yetu tena, tukisafiri kwa majira karibu kama
mwanzoni, na baada ya kusafiri kwa muda wa siku nyingi tulipiga hema zetu tena, ili
tukae kwa muda.
34 Na ikawa kwamba Ishmaeli alifariki, na akazikwa mahali palipoitwa Nahomu.
35 Na ikawa kwamba mabinti za Ishmaeli waliomboleza zaidi, kwa sababu ya kifo
cha baba yao, na kwa sababu ya masumbuko yao nyikani; na wakamnung'unikia
baba yangu, kwa sababu aliwatoa nchi ya Yerusalemu, wakisema: Baba yetu
amekufa; ndio, na tumezunguka sana nyikani, na tumepata masumbuko mengi,
njaa, kiu, na uchovu; na baada ya haya mateso yote tutaangamia nyikani kwa njaa.
36 Na hivyo wakalalamika dhidi ya baba yangu, na pia dhidi yangu; na wakataka
kurudi tena Yerusalemu.
37 Na Lamani akamwambia Lemueli na pia wana wa Ishmaeli: Tazama, tumuue
baba yetu, na pia kaka yetu Nefi, ambaye amejifanya kuwa mtawala na mwalimu
wetu, sisi ambao ni kaka zake wakubwa.
38 Na sasa, anasema kwamba Bwana amemzungumzia, na pia kwamba malaika
wamemhudumia. Lakini tazama, tunajua kwamba anatudanganya; na anatuambia
vitu hivi, na anatenda vitu vingi kwa ujanja wake, ili atufunike macho yetu,
akidhani, kwamba, labda atatuelekeza kwenye nyika ya ugeni; na baada ya kufanya
hivyo, amepanga kujifanya mfalme na mtawala wetu, ili atutendee kulingana na nia
na mapenzi yake. Na jinsi hii ndivyo kaka yangu Lamani alivyochochea hasira
mioyoni mwao.
39 Na ikawa kwamba Bwana alikuwa pamoja nasi, ndio, hata sauti ya Bwana ikaja na
kuwazungumzia maneno mengi, na ikawakemea zaidi; na baada ya kukemewa na
sauti ya Bwana wakaacha hasira yao, na wakatubu dhambi zao, hata kwamba Bwana
akatubariki tena kwa chakula, kwamba hatukuangamia.

# 1 Nefi 17

1 Na ikawa kwamba tulianza safari yetu tena nyikani; na tulisafiri tukielekea
mashariki tangu ule wakati. Na tulisafiri na kupitia mateso mengi huko nyikani; na
wanawake zetu walizaa watoto nyikani.
2 Na baraka kuu za Bwana zilikuwa nasi, kwamba wakati tulipokula nyama mbichi
huko nyikani, bibi zetu walipata maziwa ya kutosha ya kunyonyesha watoto wao, na
walikuwa na nguvu, ndio, hata kama wanaume; na wakaanza kusafiri bila
kunung'unika.
3 Na hivyo tunaona kwamba lazima amri za Mungu zitimizwe. Na kama watoto
wa watu watatii amri za Mungu atawalisha, na kuwatia nguvu, na kuwapatia uwezo
ili wakamilishe kitu ambacho amewaamuru; kwa hivyo, alitupatia uwezo tulipopitia
nyikani.
4 Na tulipitia nyikani kwa muda wa miaka mingi, ndio, hata miaka minane
nyikani.
5 Na tulifika nchi ambayo tuliita Neema, kwa sababu ya matunda yake mengi na
asali ya mwitu; na vitu hivi vyote vilitayarishwa na Bwana ili tusiangamie. Na
tukaona bahari, ambayo tuliita Ireantumu, ambayo, maana yake, ni maji mengi.
6 Na ikawa kwamba tulipiga hema zetu pwani, ingawaje tulipata mateso na

masumbuko mengi, ndio, hata mengi zaidi kwamba hatuwezi kuandika yote,
tulishangilia sana wakati tulipofika pwani; na tukaita pahali pale Neema, kwa
sababu ya matunda yake mengi.
7 Na ikawa kwamba baada ya mimi, Nefi, kuwa katika nchi ya Neema kwa muda
wa siku nyingi, sauti ya Bwana ikanijia na kuniambia: Ondoka, na uende mlimani.
Na ikawa kwamba niliinuka na kuenda mlimani, na nikamlilia Bwana.
8 Na ikawa kwamba Bwana akanizungumzia, na kusema: Wewe utajenga
merikebu, kulingana na vile nitakavyokuonyesha, ili niwavushe watu wako haya
maji.
9 Na nikasema: Bwana, ni wapi nitakapoenda ili nipate mawe yenye madini ya
kuyeyusha, ili nijenge vifaa vya kutengenezea merikebu jinsi vile umenionyesha?
10 Na ikawa kwamba Bwana akanieleza pa kwenda ili nipate mawe yenye madini, ili
nijenge vifaa.
11 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nilitengeneza mivuo ya kupuliza moto, kwa ngozi
za wanyama; na baada ya kutengeneza mivuo, ya kupuliza moto, niligongesha mawe
mawili pamoja ili nipate moto.
12 Kwani Bwana hakuturuhusu tuwashe moto mwingi, tulipokuwa tukisafiri
nyikani; kwani alisema: Nitafanya chakula chenu kiwe kitamu, hata hamtakipika;
13 Na pia nitakuwa nuru yenu huko nyikani; na nitawatayarishia njia, kama mtatii
amri zangu; kwa hivyo, vile mtakavyotii amri zangu mtaongozwa hadi kwenye nchi
ya ahadi; na mtajua kwamba ni mimi ninayewaongoza.
14 Ndio, na Bwana pia akasema kwamba: Baada ya kuwasili katika nchi ya ahadi,
mtajua kwamba mimi, Bwana, ndiye Mungu; na kwamba mimi, Bwana,
niliwakomboa kutoka maangamizoni; ndio, kwamba niliwatoa kutoka nchi ya
Yerusalemu.
15 Kwa hivyo, mimi, Nefi, nilijaribu kutii amri za Bwana, na nikawasihi kaka zangu
wawe waaminifu na wenye jitihada.
16 Na ikawa kwamba nilitengeneza vifaa kutoka kwa mawe yenye madini ambayo
nilikuwa nimeyayeyusha kutoka kwa mwamba.
17 Na wakati kaka zangu walipoona kwamba niko karibu kujenga merikebu,
walianza kunung'unika dhidi yangu, na kusema: Kaka yetu ni mjinga, kwani
anafikiri kuwa anaweza kujenga merikebu; ndio, na anafikiri pia kwamba anaweza
kuvuka haya maji makuu.
18 Na hivyo ndivyo kaka zangu walilalamika dhidi yangu, na hawakutaka kufanya
kazi, kwani hawakuamini kwamba ningejenga merikebu; wala hawakuamini kuwa
nilifundishwa na Bwana.
19 Na sasa ikawa kwamba mimi, Nefi, nilikuwa na huzuni zaidi kwa sababu ya
ugumu wa mioyo yao, na sasa walipoona kwamba nilianza kuwa na huzuni
walifurahi mioyoni mwao, hata wakanishangilia kwa kusema: Tulijua kwamba
huwezi kujenga merikebu, kwani tulijua ulipungukiwa na mawazo; kwa hivyo, wewe
huwezi kutimiza kazi kubwa hivyo.
20 Nawe uko kama baba yetu, aliyepotoshwa na mawazo ya ujinga moyoni mwake;
ndio, ametutoa kutoka nchi ya Yerusalemu, na tumezunguka nyikani kwa hii miaka
mingi; na wanawake wetu wamefanya kazi ya kuchosha, wakiwa wajawazito; na
wamezaa watoto nyikani na kuteseka kwa vitu vyote, ila kifo tu; na ingekuwa vyema
wafe kabla ya kutoka Yerusalemu badala ya kuteseka na haya masumbuko.
21 Tazama, hii miaka mingi tumeteseka nyikani, na pengine huu wakati

tungefurahia mali yetu na nchi yetu ya urithi; ndio, na pengine tungekuwa na
furaha.
22 Na tunajua kwamba wale watu waliokuwa katika nchi ya Yerusalemu walikuwa
watu watakatifu; kwani walitii masharti na hukumu za Bwana, na amri zake zote,
kulingana na sheria ya Musa; kwa hivyo, tunajua kwamba ni watu watakatifu; na
baba yetu amewahukumu, na ametupotosha kwa sababu tulisikiza maneno yake;
ndio, na kaka yetu ni kama yeye. Na kwa lugha kama hii, kaka zangu
walinung'unika na kulalamika dhidi yetu.
23 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nikawazungumzia nikasema: Je, mnaamini
kwamba baba zetu, ambao walikuwa wana wa Israeli, wangekombolewa kutoka
mikononi mwa Wamisri kama hawakutii maneno ya Bwana?
24 Ndio, mnadhania kwamba wangetolewa utumwani, kama Bwana hakumwamuru
Musa awatoe utumwani?
25 Sasa mnajua kwamba wana wa Israeli walikuwa utumwani; na mnajua kwamba
walikuwa na mizigo mizito, ambayo ilikuwa migumu kuvumilia; kwa hivyo, mnajua
kwamba lazima iwe ilikuwa kitu kizuri kwao, kutolewa utumwani.
26 Sasa mnajua kwamba Musa aliamriwa na Bwana kutenda ile kazi kuu; na mnajua
kwamba kwa maneno yake, maji ya Bahari ya Shamu yaligawanyika huku na kule, na
wakapitia nchi kavu.
27 Lakini mnajua Wamisri walizama katika Bahari ya Shamu, ambao walikuwa
majeshi la Farao.
28 Na pia mnajua kwamba walilishwa kwa mana kutoka mbinguni huko nyikani.
29 Ndio, na pia mnajua kwamba Musa, kwa neno lake kulingana na nguvu za
Mungu ambazo alikuwa nazo, aligonga mwamba, na pakatiririka maji, ili wana wa
Israeli watulize kiu yao.
30 Na ijapokuwa waliongozwa, na Bwana Mungu wao, Mkombozi wao,
akiwatangulia, akiwaongoza mchana na kuwapatia nuru usiku, na kuwafanyia yote
yaliyompasa mwanadamu kupokea, waliposhupaza mioyo yao na kupofusha
mawazo yao, na wakamtusi Musa pamoja na Mungu anayeishi na wa kweli.
31 Na ikawa kwamba aliwaangamiza kulingana na neno lake; na akawaongoza
kulingana na neno lake; na aliwatendea vitu vyote kulingana na neno lake; na
hakuna lolote lililotendwa ila tu kulingana na neno lake.
32 Na baada ya kuvuka mto Yordani aliwatia nguvu za kuwafukuza wana wa nchi
ile, ndio, hata kuwatawanya kwa maangamizo.
33 Na sasa, mnadhani kuwa wana wa nchi hii, waliokuwa kwenye nchi ya ahadi,
waliofukuzwa na babu zetu, mnadhani kuwa walikuwa watakatifu? Tazama,
nawaambia, Hapana.
34 Je, mnadhania kwamba Baba zetu wangekuwa bora zaidi yao, kama wangekuwa
watakatifu? Ninawaambia, Hapana.
35 Tazama, Bwana anawapenda watu wote sawa sawa; yule ambaye ni mtakatifu
anapendelewa na Mungu. Lakini tazama, hawa watu walikataa kila neno la Mungu,
na walikuwa wamekomaa kwenye maovu; na utimilifu wa ghadhabu ya Mungu
ulikuwa juu yao; na Bwana akalaani nchi dhidi yao, na akaibariki kwa babu zetu;
ndio, alitamka laana dhidi yao kwa maangamizo yao, na akaibariki kwa baba zetu ili
wapate mamlaka juu yake.
36 Tazama, Bwana ameumba dunia ili watu waishi ndani yake; na ameumba wana
wake ili wairithi.

37 Na huinua taifa takatifu, na kuangamiza mataifa maovu.
38 Na anawaongoza watakatifu kwenye nchi za thamani, na waovu anawaangamiza,
na kulaani nchi kwa sababu yao.
39 Anatawala juu mbinguni, kwani ndicho kiti chake cha enzi, na dunia ni kiti
chake cha kuegemesha miguu.
40 Na anawapenda wale ambao watamkubali awe Mungu wao. Tazama, aliwapenda
baba zetu na akaagana nao, ndio, hata na Ibrahimu, Isaka, na Yakobo; na
akakumbuka maagano aliyoagana nao; kwa hivyo, akawatoa kutoka nchi ya Misri.
41 Na aliwanyosha kwa fimbo yake huko nyikani; kwani walishupaza mioyo yao,
hata kama nyinyi; na Bwana aliwanyosha kwa sababu ya uovu wao. Aliwatumia
nyoka wakali warukao miongoni mwao; na baada ya wao kuumwa akawatayarishia
njia ya kuponywa; na lile waliopaswa kutenda ni kutazama; na kwa sababu ya wepesi
wa njia, au urahisi wake, kulikuwa na wengi walioangamia.
42 Na walishupaza mioyo yao mara kwa mara, na wakamwasi Musa, na pia Mungu;
walakini, mnajua kuwa waliongozwa kwa nguvu zake zisizoshindikana hadi
wakafika katika nchi ya ahadi.
43 Na sasa, baada ya vitu hivi vyote, wakati umefika kwamba wamekuwa waovu,
ndio, kupita kiasi; na nafikiri inawezekana leo wanakaribia kuangamizwa; kwani
najua siku itafika ambayo lazima waangamizwe, ila tu wachache, ambao
watapelekwa utumwani.
44 Kwa hivyo, Bwana alimwamuru baba yangu kukimbilia nyikani; na Wayahudi
pia wakajaribu kumtoa uhai; ndio, nanyi pia mmejaribu kumtoa uhai wake; kwa
hivyo, nyinyi ni wauaji mioyoni mwenu na nyinyi mnafanana na wao.
45 Nyinyi ni wepesi kwa kutenda maovu lakini wanyonge kumkumbuka Bwana
Mungu wenu. Mmeona malaika, na akawazungumzia; ndio, mmesikia sauti yake
mara kwa mara; na amewazungumzia kwa sauti ndogo tulivu, lakini mlikuwa
mmekufa ganzi, kwamba hamkupata yale maneno yake; kwa hivyo,
amewazungumzia kwa sauti kama radi, ambayo ilisababisha dunia kutetemeka kama
ambayo inapasuka.
46 Na pia mnajua kwamba kwa nguvu za neno lake kuu anaweza kusababisha dunia
imalizike; ndio, na mnajua kwamba kwa neno lake anaweza kusababisha
palipopotoka pawe pamenyooka, na paliponyooka pavunjike. Je, kwa nini, basi,
muwe wagumu mioyoni mwenu?
47 Tazama, nafsi yangu imevunjwa na uchungu kwa sababu yenu, na moyo wangu
unaumwa; nina hofu kwamba mtatupwa milele. Tazama, nimejazwa na Roho
mtakatifu wa Mungu, hata kwamba kiwiliwili changu hakina nguvu.
48 Na sasa ikawa kwamba nilipozungumza maneno haya walinikasirikia, na
walitaka kunitupa katika kilindi cha bahari; na walipokuja kunikamata
nikawazungumzia, nikisema: Katika jina la Mwenyezi Mungu, ninawaamuru
msiniguse, kwani nimejazwa na nguvu za Mungu, hata kwamba kiwiliwili changu
chaweza kuungua; na yeyote atakayenigusa atakauka kama nyasi iliyokauka; na
atakuwa bure mbele ya nguvu za Mungu, kwani Mungu atamwadhibu.
49 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwaambia wasilalamike tena juu ya baba yao;
wala wasikatae kunitumikia, kwani Mungu aliniamuru nijenge merikebu.
50 Na nikawaambia: Kama Mungu aliniamuru kutenda vitu vyote ningevifanya.
Kama ataniamuru niyaambie maji haya, yawe ardhi, yangekuwa ardhi; na kama
nikisema, ingetendeka.

51 Na sasa, ikiwa Bwana anazo nguvu nyingi hivyo, na amefanya miujiza mingi
miongoni mwa watoto wa watu, je, kwa nini hawezi kunishauri, kwamba nijenge
merikebu?
52 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwaambia kaka zangu vitu vingi, mpaka
wakafadhaishwa wasiweze kubishana na mimi; wala hawakuthubutu kunigusa kwa
mikono yao au vidole vyao, kwa muda wa siku nyingi. Sasa hawakuthubutu kufanya
hivyo ili wasikauke mbele yangu, kwani Roho ya Mungu alikuwa na nguvu nyingi;
hata wakaguswa.
53 Na ikawa kwamba Bwana aliniambia: Nyosha mkono wako tena kwa kaka zako,
na hawatakauka mbele yako, lakini nitawashitua, asema Bwana, na nitafanya hivi, ili
wajue kwamba mimi ndimi Bwana Mungu wao.
54 Na ikawa kwamba niliwanyoshea kaka zangu mkono wangu, na hawakukauka
mbele yangu; lakini Bwana aliwashitua, kulingana na neno ambalo alikuwa
amelizungumza.
55 Na sasa, wakasema: Tunajua kwa hakika kwamba Bwana yuko nawe, kwani
tunajua kwamba ni nguvu za Bwana zimetushitua. Na wakainama mbele yangu, na
walikuwa karibu kuniabudu, lakini sikuwaruhusu, nikisema: Mimi ni kaka yenu,
ndio, hata kaka yenu mdogo; kwa hivyo, mwabuduni Bwana Mungu wenu, na
mheshimu baba yenu na mama yenu, ili maisha yenu yawe marefu katika nchi
ambayo Bwana Mungu wenu atawapatia.

## 1 Nefi 18

1 Na ikawa kwamba walimuabudu Bwana, na wakajiunga na mimi; na tukaunda
mbao kwa ufundi maalumu. Na Bwana alinionyesha mara kwa mara namna ya
kuunda zile mbao za merikebu.
2 Sasa mimi, Nefi, sikuunda mbao kulingana na njia zilizofahamiwa na watu, wala
sikujenga merikebu kulingana na njia za watu; lakini niliijenga kulingana na vile
Bwana alivyonionyesha; kwa hivyo, haikuwa kulingana na njia za wanadamu.
3 Na mimi, Nefi, nilienda mlimani mara nyingi, na nilimuomba Bwana mara
nyingi; kwa hivyo Bwana alinionyesha vitu vikubwa.
4 Na ikawa kwamba baada ya mimi kumaliza kujenga merikebu, kulingana na neno
la Bwana, ndugu zangu waliona kwamba ni nzuri, na ufundi wake ulikuwa stadi;
kwa hivyo, wakajinyenyekeza tena kwa Bwana.
5 Na ikawa kwamba sauti ya Bwana ikamjia baba yangu, kwamba tuinuke na
kuingia kwenye merikebu.
6 Na ikawa kwamba kesho yake, baada ya kutayarisha vitu vyote, matunda mengi
na nyama kutoka nyikani, na asali nyingi, na maakuli kulingana na yale Bwana
aliyotuamuru, tuliingia kwenye merikebu, pamoja na mizigo yetu yote na mbegu
zetu, na kitu chochote ambacho tulileta nasi, kila mmoja kulingana na umri wake;
kwa hivyo, tuliingia sote kwenye merikebu, pamoja na wake zetu na watoto wetu.
7 Na sasa, baba yangu alikuwa amepata watoto wawili nyikani; mkubwa aliitwa
Yakobo na mdogo alikuwa ni Yusufu.
8 Na ikawa kwamba baada ya sisi sote kuingia kwenye merikebu, na kuchukua
maakuli yetu na vitu ambavyo tuliamriwa, tulitweka baharini na tukaendeshwa
mbele na upepo tukielekea nchi ya ahadi.
9 Na baada ya sisi kuendeshwa na upepo kwa muda wa siku nyingi, tazama, kaka

zangu na wana wa Ishmaeli pia na wake zao walianza kujifurahisha, hata wakaanza
kucheza ngoma, na kuimba, na kuzungumza kwa ujeuri sana, ndio, hata kwamba
wakasahau kwa nguvu gani waliletwa hapo; ndio, waliinuliwa zaidi kwa ujeuri.
10 Na mimi, Nefi, nikaanza kuogopa zaidi kwamba Bwana atatukasirikia, na atupige
kwa sababu ya uovu wetu, hata tuzame kwenye kilindi cha bahari; kwa hivyo, mimi,
Nefi, nilianza kuwazungumzia kwa makini; lakini tazama walinikasirikia, wakisema:
Hatutakubali kuwa kaka yetu mdogo awe mtawala wetu.
11 Na ikawa kwamba Lamani na Lemueli walinikamata na kunifunga kwa kamba,
na wakawa wakali sana kwangu; walakini, Bwana alikubali haya ili aonyeshe nguvu
zake, kwa kutimiza maneno yake aliyosema kuhusu wale waovu.
12 Na ikawa kwamba waliponifunga hata nisingeweza kutembea, dira, ambayo
Bwana alikuwa ameitayarisha, ilikoma kufanya kazi.
13 Kwa hivyo, hawakujua njia gani ambayo wangeelekeza merikebu, hata mpaka
kukawa na dhoruba kubwa, ndio, dhoruba kuu na kali, na tukarudishwa nyuma
majini kwa muda wa siku tatu; na wakaanza kuogopa kupita kiasi kwamba
watazama baharini; walakini hawakunifungua.
14 Na baada ya kurudishwa nyuma kwa siku nne, dhoruba ilianza kuwa kali zaidi.
15 Na ikawa kwamba tulikuwa karibu kumezwa kilindini mwa bahari. Na baada ya
kurudishwa nyuma katika maji kwa muda wa siku nne, kaka zangu wakaanza kuona
kwamba hukumu za Mungu zilikuwa juu yao, na kwamba lazima wafe kama
hawatatubu maovu yao; kwa hivyo, wakanijia na kunifungua kamba ambazo
zilikuwa kwa viwiko vyangu, na tazama vilikuwa vimefura zaidi; na pia vifundo
vyangu vilivimba sana, na uchungu ulikuwa mwingi.
16 Walakini, nilimtazama Mungu wangu, na nilimsifu siku yote nzima; na
sikumlalamikia Bwana kwa sababu ya masumbuko yangu.
17 Sasa baba yangu, Lehi, alikuwa amewaambia vitu vingi, na pia kwa wana wa
Ishmaeli; lakini, tazama, walitoa vitisho vingi kwa yeyote ambaye alinitetea; na
wazazi wangu wakiwa na umri mkuu, na wakiwa wameteseka kwa hofu kuu kwa
sababu ya wana wao, walilemewa, ndio, hadi wakaugulia vitandani.
18 Kwa sababu ya hofu yao na huzuni nyingi, na maovu ya kaka zangu, walikaribia
kukutana na Mungu wao; ndio, mvi zao zilikaribia kulazwa mavumbini; ndio, hata
karibu watupwe na huzuni katika kaburi la maji.
19 Na Yakobo na Yusufu pia, wakiwa wachanga, na wakihitaji kulishwa sana,
walihuzunishwa na masumbuko ya mama yao; pia na mke wangu na machozi yake
na sala, na pia watoto wangu, hawakulainisha mioyo ya kaka zangu ili wanifungue.
20 Na hapakuwa chochote ila nguvu za Mungu, zilizowatisha na maangamizo,
kingelainisha mioyo yao; kwa hivyo, walipoona kwamba walikuwa karibu kuzama
baharini walitubu kwa kitu kile ambacho walitenda, hata wakanifungua.
21 Na ikawa kwamba baada ya wao kunifungua, tazama, nilichukua dira, na ilitenda
nilivyotaka. Na ikawa kwamba nikamwomba Bwana; na baada ya mimi kusali,
upepo ulikoma, na dhoruba ikaisha, na kukawa na utulivu mkuu.
22 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliendesha merikebu, hata tukasafiri tena
tukielekea nchi ya ahadi.
23 Na ikawa kwamba baada ya kusafiri kwa muda wa siku nyingi tuliwasili katika
nchi ya ahadi; na tukatembea kwenye ardhi, na tukapiga hema zetu; na tukaiita nchi
ya ahadi.
24 Na ikawa kwamba tulianza kulima ardhi, na tukaanza kupanda mbegu; ndio,

tulitia mbegu zetu zote udongoni, tulizokuwa tumebeba kutoka nchi ya
Yerusalemu. Na ikawa kwamba zilimea zaidi; kwa hivyo, tukapata baraka tele.
25 Na ikawa kwamba tuliposafiri nyikani, tulipata katika nchi ya ahadi, wanyama
huko porini wa kila aina, ngombe na dume, na punda na farasi, na mbuzi wa
nyumbani na mbuzi wa kichaka, na kila aina ya wanyama wa mwitu, ambao
walimfaidisha mwanadamu. Na tukapata kila aina ya mawe yenye madini, ya
dhahabu, na ya fedha, na shaba nyekundu.

# 1 Nefi 19

1 Na ikawa kwamba Bwana akaniamuru, kwa hivyo nilitengeneza bamba za mawe
yenye madini ili nichore juu yake maandishi ya watu wangu. Na kwenye zile bamba
ambazo nilitengeneza, niliandika maandishi ya baba yangu, na pia safari zetu
nyikani, na unabii wa baba yangu; na pia unabii wangu mwingi mwenyewe
nimeuandika hapo.
2 Na sikujua ule wakati nilipozitengeneza kwamba nitaamriwa na Bwana
kuzitengeneza hizi bamba; kwa hivyo, maandishi ya baba yangu, na nasaba ya baba
zake, na mengi kuhusu yaliyotupata huko nyikani yamechorwa kwenye zile bamba
za kwanza nilizozizungumzia; kwa hivyo, vitu vilivyotukia kabla ya kutengeneza
hizi bamba, kwa kweli, vimeelezwa zaidi kwenye zile bamba za kwanza.
3 Na baada ya kutengeneza hizi bamba kwa amri, mimi, Nefi, nilipokea amri
kwamba ile huduma na unabii, sehemu zake zilizo wazi zaidi na zenye thamani,
ziandikwe katika hizi bamba; na kwamba vitu vilivyoandikwa vihifadhiwe kwa
kuwashauri watu wangu, ambao watamiliki nchi, na pia kwa sababu zingine zenye
hekima, sababu ambazo zinajulikana na Bwana.
4 Kwa hivyo, mimi, Nefi, niliandika maandishi kwenye zile bamba zingine, ambazo
zinaeleza, au ambazo zinafafanua zaidi kuhusu vita na mabishano na maangamizo ya
watu wangu. Na nimetenda hivi, na kuwaamuru watu wangu kile watakachofanya
baada mimi kuaga dunia; na kwamba hizi bamba zipitishwe kutoka kizazi kimoja
hadi kingine, au kutoka nabii mmoja hadi kwa mwingine, mpaka Bwana
atakapoamuru vingine.
5 Na maelezo ya utengenezaji wa hizi bamba utaelezwa hapo baadaye; na kisha,
tazama, nitaendelea kulingana na yale ambayo nimezungumza; na ninafanya haya ili
yale ambayo ni matakatifu zaidi yahifadhiwe kwa ufahamu wa watu wangu.
6 Walakini, siandiki chochote kwenye hizi bamba, ila tu kile ambacho nafikiri ni
kitakatifu. Na sasa, kama nitakosea, wale nao ambao walinitangulia walikosea; sio
ati kwamba nitajihalalisha mwenyewe kwa sababu ya watu wengine, lakini ni kwa
sababu ya unyonge ulio ndani yangu, kulingana na mwili, nitajihalalisha.
7 Kwani vitu ambavyo watu wengine wanafikiria ni vya thamani kuu, kwa mwili na
kwa roho, wengine wanavidharau na kuvikanyaga miguuni mwao. Ndio, hata yule
Mungu wa Israeli watu humkanyaga miguuni; nasema, kumkanyaga miguuni mwao
lakini ningezungumza kwa maneno mengine — wanamdharau, na hawasikilizi sauti
ya mawaidha yake.
8 Na tazama anakuja, kulingana na maneno ya malaika, baada ya miaka mia sita
tangu baba yangu alipotoka Yerusalemu.
9 Na ulimwengu, kwa sababu ya uovu wao, utamhukumu kuwa jambo la dharau;
kwa hivyo wanampiga kwa mijeledi, na anavumilia; na wanamchapa, na anavumilia.

Ndio, na wanamtemea mate, na anavumilia, kwa sababu ya upendo wake mkarimu
na subira yake kwa watoto wa watu.
10 Na Mungu wa baba zetu, ambao walitolewa Misri, kutoka utumwani, na pia
wakahifadhiwa nyikani na yeye, ndio, Mungu wa Ibrahimu, na wa Isaka, na Mungu
wa Yakobo, kulingana na maneno ya malaika, kama mtu, anajikabidhi mikononi
mwa watu waovu, ili ainuliwe, kulingana na maneno ya Zenoki, na kusulubiwa,
kulingana na maneno ya Neumu, na kuzikwa kaburini, kulingana na maneno ya
Zeno, ambayo alizungumza kuhusu zile siku tatu za giza, ambazo zitakuwa ni ishara
imetolewa ya kifo chake kwa wale watakaoishi katika visiwa vya bahari, muhimu
zaidi itatolewa kwa wale ambao ni wa nyumba ya Israeli.
11 Kwa hivyo alizungumza nabii: Kwa hakika Bwana Mungu atatembelea nyumba
yote ya Israeli katika siku ile, wengine kwa sauti yake, kwa sababu ya utakatifu wao,
kwa shangwe yao kuu na wokovu wao, na wengine kwa radi na umeme wa nguvu
zake, kwa dhoruba, kwa moto, na kwa moshi, na ukungu wa giza, na kwa upasukaji
wa ardhi, na kwa milima ambayo itainuliwa.
12 Na hivi vitu vyote lazima vitimizwe, asema nabii Zeno. Na miamba ya ardhi
lazima ipasuke; na kwa sababu ya mingurumo ya dunia, wafalme wengi wa visiwa vya
bahari watashawishiwa na Roho ya Mungu, kupaza sauti: Mungu wa asili anateseka.
13 Na kwa wale ambao watakuwa Yerusalemu, asema nabii, watapigwa kwa mijeledi
na watu wote, kwa sababu wanamsulubu Mungu wa Israeli, na kugeuza mioyo yao
upande, wakikataa ishara na maajabu, na nguvu na utukufu wa Mungu wa Israeli.
14 Na kwa sababu wanageuza mioyo yao upande, asema nabii, na wamemdharau
yule Mtakatifu wa Israeli, watarandaranda maishani mwao, na kuangamia, na kuwa
wa kufanyiwa mzaha na kutukanwa, na kuchukiwa miongoni mwa mataifa yote.
15 Walakini, wakati siku ile itafika, asema nabii, kwamba hawatageuza tena mioyo
yao upande kinyume cha yule Mtakatifu wa Israeli, ndipo atakumbuka maagano
ambayo aliagana na baba zao.
16 Ndio, ndipo atakumbuka visiwa vya bahari; ndio, na watu wote ambao ni wa
nyumba ya Israeli nitawakusanya, asema Bwana, kutoka pembe nne za ulimwengu,
kulingana na maneno ya nabii Zeno.
17 Ndio, na ulimwengu wote utaona wokovu wa Bwana, asema nabii; kila taifa,
kabila, lugha, na watu watabarikiwa.
18 Na mimi, Nefi, nimewaandikia watu wangu vitu hivi, ili pengine niwashawishi
wamkumbuke Bwana Mkombozi wao.
19 Kwa hivyo, nazungumza kwa nyumba yote ya Israeli, kama watapokea hivi vitu.
20 Kwani tazama, nina jambo rohoni, ambalo limenichosha hata kwamba viungo
vyangu vyote vimenyong'onyea, kwa wote ambao wako Yerusalemu; kwani ikiwa
Bwana hakuwa na huruma, na kunionyesha yaliyowahusu, kama hata wale manabii
wa kale, pia nami ningeangamia.
21 Na kwa hakika aliwaonyesha manabii wa kale vitu vyote vilivyowahusu; na pia
alionyesha wengi yaliyotuhusu; kwa hivyo, ni lazima tujue yaliyowahusu kwani
yameandikwa katika bamba za shaba.
22 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwafunza kaka zangu vitu hivi; na ikawa
kwamba niliwasomea vitu vingi, vilivyochorwa kwenye zile bamba za shaba, ili
wajue kuhusu vitendo vya Bwana katika nchi zingine, miongoni mwa watu wa kale.
23 Na niliwasomea vitu vingi ambavyo viliandikwa kwenye vitabu vya Musa; lakini
ili niwashawishi kabisa wamwamini Bwana Mkombozi wao niliwasomea yale

ambayo yaliandikwa na nabii Isaya; kwani nililinganisha maandiko yote nasi, ili yatufaidishe na kutuelimisha.

24 Kwa hivyo niliwazungumzia, nikisema: Sikizeni maneno ya nabii, nyinyi ambao ni sazo la nyumba ya Israeli, tawi ambalo wamevunjwa; sikilizeni maneno ya nabii, ambayo yaliandikiwa nyumba yote ya Israeli, na myalinganishe nanyi, ili mpate matumaini vile vile na ndugu zenu ambao mlitawanyika kutoka kwao; kwani hivi ndivyo nabii ameandika.

## 1 Nefi 20

1 Sikilizeni na msikie haya, Ee nyumba ya Yakobo, ambao wanajulikana kwa jina la Israeli, na wametoka katika maji ya Yuda, au kutoka kwenye maji ya ubatizo, ambao wanaapa kwa jina la Bwana, na kutaja Mungu wa Israeli, walakini hawaapi kwa ukweli wala kwa utakatifu.

2 Walakini, wanajiita wakazi wa mji mtakatifu, lakini hawamtegemei Mungu wa Israeli, ambaye ni Bwana wa Majeshi; ndio, jina lake ni Bwana wa Majeshi.

3 Tazama, nimetangaza vitu vilivyokuja awali kutoka mwanzoni; na yalitoka kinywani mwangu, na niliyadhihirisha. Niliyadhihirisha kwa ghafla.

4 Na niliitenda kwa sababu nilijua kwamba wewe ni mkaidi, na shingo yako ni ngumu kama chuma, na paji lako kama shaba;

5 Na nimekutangazia hata tangu mwanzo, kabla hayajakuwa niliyaonyesha kwako; na nilikuonyesha usije ukasema — Sanamu yangu imezitenda, na mfano uliochongwa wangu, na mfano ulioyeyushwa wangu ndio imeziamuru.

6 Umeona na kusikia haya yote; na je wewe hutayatangaza? Na kwamba nimekuonyesha vitu vipya tangu wakati huu, hata vitu vilivyofichwa, na wewe hukuvijua.

7 Yameumbwa sasa, na si tangu mwanzo, hata kabla ya ile siku ambayo hukuyasikia yalikuwa yametangazwa kwako, ili usiseme — Tazama niliyajua.

8 Ndio, na wewe hukusikia; ndio, wewe hukujua; ndio, tangu ule wakati sikio lako halikufunguliwa; maana nilijua kwamba ungetenda uhaini, na ulikuwa mvunja sheria kutoka tumboni.

9 Walakini, kwa sababu ya heshima ya jina langu nitazuia ghadhabu yangu, na kwa sababu ya sifa zangu nitajizuia tokana nawe, kwamba nisikuangamize.

10 Kwani, tazama, nimekutakasa, nimekuchagua kutoka kalibu ya masumbuko.

11 Kwa heshima yangu, ndio, kwa heshima yangu nitatenda hii, kwani sitakubali jina langu lichafuliwe, na sitampatia mwingine utukufu wangu.

12 Nisikilize mimi, Ee Yakobo, na Israeli wateule wangu, kwani mimi ndiye yeye; mimi ndiye wa kwanza, na pia mimi ndiye wa mwisho.

13 Mkono wangu pia umejenga msingi wa dunia, na mkono wangu wa kiume umetandaza mbingu. Naziita na zinasimama pamoja.

14 Nyinyi nyote, kusanyikeni, na msikie; ni nani miongoni mwao amewatangazia vitu hivi? Bwana amempenda; ndio, na atatimiza neno lake ambalo amesema kupitia kwao; na atatendea Babilonia nia yake, na mkono wake utanyoshewa Wakaldayo.

15 Pia, Bwana asema; mimi, Bwana, ndio, nimesema; ndio, nimemuita kutangaza, nimemleta, na atafanikiwa katika njia zake.

16 Njooni karibu na mimi; sijazungumza kwa siri; tangu mwanzo, tangu ilipotangazwa nimezungumza; na Bwana Mungu, na Roho yake, amenituma.

17 Na hivi ndivyo Bwana anasema, Mkombozi wenu, Mtakatifu wa Israeli;
nimemtuma, Bwana Mungu wenu anayekufundisha kufaidika, ambaye
anakuongoza katika njia inayokupasa, ameitenda.
18 Ee kwamba ungesikiza amri zangu — basi amani yako ingekuwa kama mto, na
utakatifu wako ungekuwa kama mawimbi ya bahari.
19 Uzao wako ungekuwa pia kama mchanga; na kizazi cha matumbo yenu ingekuwa
kama changarawe yake; jina lake halingetupiliwa mbali wala kuangamizwa kutoka
mbele yangu.
20 Tokeni kutoka Babilonia, waondokeeni Wakaldayo, kwa sauti ya kuimba
tangazeni nyinyi, semeni haya, ambieni hadi mwisho wa ulimwengu; semeni nyinyi;
Bwana amemkomboa mtumishi wake Yakobo.
21 Na hawakuona kiu; aliwaongoza majangwani; akasababisha maji kutiririka
kutoka kwenye mwamba kwa sababu yao; alipasua mwamba pia na maji yakatoka.
22 Ingawa ametenda haya yote, na makuu pia, hakuna amani, asema Bwana, kwa
waovu.

## 1 Nefi 21

1 Na tena: Sikiliza, Ee nyinyi nyumba ya Israeli, nyote ambao mmetenganishwa na
kufukuzwa kwa sababu ya uovu wa wachungaji wa watu wangu; ndio, nyinyi nyote
ambao mmetenganishwa, na kutawanywa ugenini, wale ambao ni wa watu wangu,
Ee nyumba ya Israeli. Sikilizeni, Ee visiwa, nisikilizeni mimi, na watu walio mbali
pia sikilizeni; Bwana ameniita kabla sijazaliwa, kutoka tumboni mwa mama yangu,
ametaja jina langu.
2 Na amefanya kinywa changu kuwa kama upanga mkali; amenificha katika kivuli
cha mkono wake, na akanifanya mshale uliong'aa; amenificha katika podo lake.
3 Na akaniambia: Wewe ndiye mtumishi wangu, Ee Israeli, ambaye nitatukuzwa
ndani yake.
4 Kisha nikasema, nimefanya kazi bure, nimetumia nguvu zangu bure na bila faida;
kwa hakika hukumu yangu iko na Bwana, na vitendo vyangu na Mungu wangu.
5 Na sasa, asema Bwana — ambaye aliniumba kutoka tumboni ili niwe mtumishi
wake, kumrejesha Yakobo kwake tena — ingawa Israeli haijakusanyika, bado
nitakuwa mwenye utukufu machoni mwa Bwana, na Mungu wangu atakuwa nguvu
yangu.
6 Na alisema: Ni kitu rahisi kuwa wewe uwe mtumishi wangu ili uinue makabila
ya Yakobo, na kurudisha waliohifadhiwa kutoka Israeli. Nitakufanya pia uwe nuru
kwa Wayunani, kwamba uwe wokovu wangu hadi mwisho wa ulimwengu.
7 Hivyo asema Bwana, Mkombozi wa Israeli, Mtakatifu wake, kwa yule
anayechukiwa na watu, kwa yule anayedharauliwa na mataifa, kwa mtumishi wa
watawala: Wafalme wataona na kuinuka, wana wa wafalme pia wataabudu, kwa
sababu ya Bwana ambaye ni mwaminifu.
8 Bwana asema hivi: Kwa wakati uliokubalika nimekusikia, Ee visiwa vya bahari,
na kwa siku ya wokovu nilikusaidia; na nitakuhifadhi, na ninakupatia mtumishi
wangu uwe agano la watu, kuimarisha nchi, kuwasababisha kurithi makao
yaliokuwa yenye ukiwa.
9 Ili uwaambie wafungwa: Ondokeni; kwa wale ambao wanaketi gizani:
Jidhihirisheni. Watakula njiani, na malisho yao yatakuwa juu ya majabali.

10 Hawataona njaa wala kiu, wala joto au jua kuwachoma; kwani yule
anayewarehemu atawaongoza, hata kwenye chemchemi za maji atawaongoza.
11 Na nitafanya milima yangu yote iwe njia, na njia zangu zitainuliwa.
12 Na kisha, Ee nyumba ya Israeli, tazama, haya yatatoka mbali; na tazama, haya
kutoka kaskazini na kutoka magharibi; na haya kutoka nchi ya Sinimu.
13 Imbeni, Ee mbingu; na ushangilie, Ee dunia; kwani miguu ya wale ambao wako
mashariki itaimarishwa; na anzeni kuimba, Ee milima; kwani hawatapigwa tena;
kwani Bwana amewafariji watu wake, na atawarehemu wanaosumbuka.
14 Lakini, tazama, Sayuni imesema: Bwana ameniacha, na Bwana wangu
amenisahau — lakini ataonyesha kwamba hajafanya hivyo.
15 Kwani mwanamke anaweza kusahau mtoto wake ambaye anamnyonyesha,
kwamba asiwe na huruma kwa mwana wa tumbo lake? Ndio, wanaweza kusahau,
lakini sitakusahau, Ee nyumba ya Israeli.
16 Tazama, nimekuchora viganjani mwa mikono yangu; kuta zako daima ziko
mbele yangu.
17 Watoto wako wataharakisha dhidi ya waharibifu wako; na wale waliokuharibu
wataondoka kutoka kwako.
18 Inua macho yako pande zote na utazame; hawa wote wanakusanyika pamoja, na
watakuja kwako. Na vile ninavyoishi, Bwana asema, wewe utajivika na wao wote,
kama pambo, na kujifunga kwao kama bibi arusi.
19 Kwani utupu wako na kwenye ukiwa, na nchi yako ya maangamizo, itakuwa hata
sasa nyembamba kwa sababu ya wakazi; na wale ambao walikumeza watakuwa
mbali.
20 Watoto utakaopata, baada ya kupoteza wale wa kwanza, watasema tena
masikioni mwako: Hapa mahali ni padogo sana kwangu; nipe mahali ili niishi.
21 Kisha utasema moyoni mwako: Nani alinizalia hawa, akiona nimepoteza watoto
wangu, na nina ukiwa, mtumwa, na akizurura hapa na pale? Nani amelea hawa?
Tazama, niliachwa pekee yangu; hawa, walikuwa wapi?
22 Bwana Mungu asema hivi: Tazama, nitawanyooshea Wayunani mkono wangu,
na nitapeperusha bendera yangu miongoni mwa watu; na wataleta wana wako kwa
mikono yao, na mabinti zako watabebwa mabegani mwao.
23 Na wafalme watakuwa baba zako walezi, nao malkia wao watakuwa mama zako
walezi; watainama mbele yako nyuso zao zikiielekea ardhi, na kuramba mavumbi ya
miguu yako; na utajua kwamba mimi ni Bwana; kwani hawataaibika
wanaoningojea.
24 Kwani mateka watanyakuliwa kutoka kwa shupavu, au watumwa halali
kukombolewa?
25 Lakini Bwana asema hivi, hata watumwa wa shupavu watachukuliwa, na mateka
wa wale walio wa kutisha watakombolewa; kwani nitashindana na yule
anayeshindana nawe, na nitaokoa watoto wako.
26 Na nitawalisha wanaokudhulumu kwa nyama yao wenyewe; watalewa kwa damu
yao wenyewe kama kwa mvinyo mtamu; na watu wote watajua kwamba mimi,
Bwana, ni Mwokozi wenu na Mkombozi wenu, Mwenyezi Mkuu wa Yakobo.

# 1 Nefi 22

1 Na sasa ikawa kwamba baada ya mimi, Nefi, kusoma vitu hivi vilivyochorwa kwenye
bamba nyeupe, kaka zangu walinijia na kuniambia: Nini maana ya vitu hivi
ambavyo umesoma? Tazama, je, vitafahamiwa kulingana na vitu vya kiroho,
ambavyo vitatimizwa kulingana na roho na sio mwili?
2 Na mimi, Nefi, niliwaambia: Tazama vilidhirihishwa kwa nabii kwa sauti ya
Roho; kwani kwa Roho vitu vyote vinafunuliwa kwa manabii, ambavyo vitawajia
watoto wa watu kulingana na mwili.
3 Kwa hivyo, vitu ambavyo nimesoma ni vitu vinavyolingana na vitu vya muda na
vya kiroho; kwani inaonekana kwamba nyumba ya Israeli, sasa au baadaye,
itatawanyika usoni mwote mwa dunia, na pia miongoni mwa mataifa yote.
4 Na tazama, tayari kuna wengi ambao wamepotea kutokana na ufahamu wa wale
ambao walioko Yerusalemu. Ndio, sehemu kubwa ya makabila yote yamepotoshwa;
na yametawanyika hapa na pale katika visiwa vya bahari; na pale yalipo hakuna
yeyote baina yetu ajuaye, ila tunajua kwamba yamepotoshwa.
5 Na kwa vile wamepotoshwa, vitu hivi vimetabiriwa juu yao, na pia kuhusu wale
wote ambao watatawanywa baadaye na kuchanganyika, kwa sababu ya yule
Mtakatifu wa Israeli; kwani watashupaza mioyo yao dhidi yake; kwa hivyo,
watatawanywa miongoni mwa mataifa yote na watachukiwa na watu wote.
6 Walakini, baada ya wao kulelewa na Wayunani, na Bwana kunyoshea Wayunani
mkono wake na kuwainua kama bendera, na watoto wao wamebebwa mikononi
mwao, na mabinti zao wamebebwa mabegani mwao, tazama vitu hivi ambavyo
vimezungumziwa ni vya muda; kwani hayo ndiyo maagano ya Bwana na baba zetu;
na inatuhusu katika siku zijazo, na pia kaka zetu wote ambao ni wa nyumba ya
Israeli.
7 Na inamaanisha kwamba wakati unafika kwamba baada ya nyumba yote ya Israeli
kutawanywa na kuchanganywa, kwamba Bwana Mungu atainua taifa shupavu
miongoni mwa Wayunani, ndio, hata usoni mwa nchi hii; na kwa wao uzao wetu
utatawanywa.
8 Na baada ya uzao wetu kutawanywa Bwana Mungu ataanza kutenda kazi ya
maajabu miongoni mwa Wayunani, ambayo itakuwa ya thamani kubwa kwa uzao
wetu; kwa hivyo, unalinganishwa na wao wakilishwa na Wayunani na wakibebwa
mikononi mwao na mabegani mwao.
9 Na pia itakuwa yenye thamani kwa Wayunani; na sio tu kwa Wayunani lakini
kwa nyumba yote ya Israeli, kwa kujulisha maagano ya Baba wa Mbingu kwa
Ibrahimu, akisema: Katika uzao wako makabila yote ya dunia yatabarikiwa.
10 Na ningetaka, kaka zangu, kwamba mngejua kwamba makabila yote ya dunia
hayawezi kubarikiwa isipokuwa aweke mkono wake wazi machoni mwa mataifa.
11 Kwa hivyo, Bwana Mungu ataendelea kuweka mkono wake wazi machoni mwa
mataifa yote, katika kutimiza maagano yake na injili yake kwa wale ambao ni wa
nyumba ya Israeli.
12 Kwa hivyo, atawatoa tena utumwani, na watakusanyika pamoja katika nchi yao
ya urithi; na watatolewa kutoka fumboni na kutoka gizani; na watajua kwamba
Bwana ni Mwokozi wao na Mkombozi wao, Mwenyezi Mkuu wa Israeli.
13 Na damu ya lile kanisa kuu na la machukizo, ambalo ni kahaba wa ulimwengu
wote, itakuwa juu ya vichwa vyao wenyewe; kwani watapigana wenyewe kwa
wenyewe, na upanga wa mikono yao utaangukia vichwa vyao vyenyewe, na watalewa

kwa damu yao wenyewe.
14 Na kila taifa ambalo litapigana nawe, Ee nyumba ya Israeli, watageukiana mmoja
dhidi ya mwingine, na wataanguka kwenye shimo walilochimba kutega watu wa
Bwana. Na wote watakaopigana dhidi ya Sayuni wataangamizwa, na yule kahaba
mkuu, ambaye ameharibu njia sahihi za Bwana, ndio, lile kanisa kuu la machukizo,
litaanguka mavumbini na muanguko wake utakuwa mkuu.
15 Kwani tazama, asema nabii, wakati unafika kwa haraka kwamba Shetani
hatakuwa na nguvu yoyote mioyoni mwa watoto wa watu; maana siku inafika
kwamba wote wenye kiburi na wale wanaotenda maovu watakuwa kama kapi; na
siku inafika ambayo lazima wachomwe.
16 Kwani wakati unafika mapema ambapo utimilifu wa ghadhabu ya Mungu
utakuwa juu ya watoto wa watu wote; kwani hatakubali kwamba waovu
wawaangamize walio watakatifu.
17 Kwa hivyo, atawahifadhi walio wa haki kwa nguvu zake, hata kama ghadhabu
yake timilifu ije, na watakatifu wahifadhiwe, hata katika maangamizo ya maadui
wao kwa moto. Kwa hivyo, watakatifu hawafai kuogopa; kwani hivyo asema nabii,
wataokolewa, hata kama ni kwa moto.
18 Tazama, kaka zangu, nawaambia, kwamba vitu hivi lazima vitimizwe karibuni;
ndio, hata damu, na moto, na ukungu wa moshi lazima uje; na ni lazima itendeke
usoni mwa dunia hii; na inawajia binadamu kulingana na mwili ikiwa watashupaza
mioyo yao dhidi ya yule Mtakatifu wa Israeli.
19 Kwani tazama, watakatifu hawataangamia; kwani wakati lazima kwa hakika ufike
kuwa wale ambao wanapinga Sayuni wataondolewa mbali.
20 Na Bwana kwa kweli atatayarishia watu wake njia, kwa kutimiza maneno ya
Musa, ambayo alizungumza, akisema: Bwana Mungu wenu atawainulia nabii, kama
mimi, yeye mtamsikiliza kwa vitu vyote atakavyowaambia. Na itakuwa kwamba
wale wote ambao hawatamsikiliza nabii wataondolewa kutoka miongoni mwa watu.
21 Na sasa mimi, Nefi, ninawatangazia, kwamba huyu nabii aliyetajwa na Musa ni
yule Mtakatifu wa Israeli; kwa hivyo, atapitisha hukumu kwa haki.
22 Na watakatifu hawapaswi kuogopa, kwani wao hawatachanganyika. Lakini ni
ufalme wa ibilisi, ambao utajengwa miongoni mwa watoto wa watu, ambao ni
ufalme ulioimarishwa miongoni mwa wale wanaoishi—
23 Kwani kwa haraka wakati utafika ambapo makanisa yote ambayo yamejengwa
kwa kupata faida, na wote waliojengwa kwa kupata mamlaka juu ya mwili, na wale
ambao walijengwa ili wapate sifa machoni mwa ulimwengu, na wale wanaotafuta
tamaa za mwili na vitu vya ulimwengu, na kutenda kila aina ya uovu; ndio,
mwishowe, wale wote ambao ni wa ufalme wa ibilisi ndio wanafaa kuogopa, na
kutetemeka, na kutapatapa; wao ndio lazima washushwe chini mavumbini; wao
ndio lazima watachomwa kama kapi; na haya ni kulingana na maneno ya nabii.
24 Na wakati unafika kwa haraka kwamba wale watakatifu lazima waongozwe kama
ndama wa zizini, na yule Mtakatifu wa Israeli lazima atawale kwa mamlaka, na
uwezo, na nguvu, na utukufu mkuu.
25 Na anawakusanya watoto wake kutoka pembe nne za ulimwengu; na anahesabu
kondoo wake, na wanamjua; na kutakuwa na zizi moja na mchunganji mmoja; na
atalisha kondoo wake, na kwake watapata malisho.
26 Na kwa sababu ya utakatifu wa watu wake, Shetani hana nguvu; kwa hivyo,
hawezi kufunguliwa kwa muda wa miaka mingi; kwani hana nguvu juu ya mioyo ya

watu, kwani wanaishi katika utakatifu, na yule Mtakatifu wa Israeli anatawala.
27 Na sasa tazama, mimi, Nefi, ninawaambia kwamba lazima vitu hivi vyote vitimizwe kulingana na mwili.
28 Lakini, tazama, mataifa yote, makabila yote, lugha zote, na watu wote wataishi salama katika Yule Mtakatifu wa Israeli ikiwa watatubu.
29 Na sasa mimi, Nefi, ninakoma; kwani sitathubutu kuzungumza zaidi kuhusu vitu hivi.
30 Kwa hivyo, kaka zangu, ningetaka mjue kwamba vile vitu vilivyoandikwa kwenye bamba za shaba ni vya kweli; na vinashuhudia kwamba lazima mtu atii amri za Mungu.
31 Kwa hivyo, msidhani kwamba mimi na baba yangu ndio tumeshuhudia pekee, na kuyafundisha. Kwa hivyo, kama mtatii amri, na kuvumilia hadi mwisho, mtaokolewa katika siku ya mwisho. Na hivyo ndivyo ilivyo. Amina.

# Kitabu cha Pili cha Nefi

*Historia ya kifo cha Lehi. Kaka za Nefi wanamwasi. Bwana anamwonya Nefi akimbilie nyikani. Safari zake nyikani na kadhalika.*

## 2 Nefi 1

1 Na ikawa kwamba baada ya mimi, Nefi, kumaliza kufundisha kaka zangu, baba yetu,
Lehi, naye pia aliwaelezea vitu vingi, na akawaambia, jinsi Bwana alivyowafanyia
vitu vikuu kwa kuwatoa kutoka nchi ya Yerusalemu.
2 Na aliwazungumzia kuhusu maasi yao majini, na huruma za Mungu katika
kuhifadhi maisha yao, kwamba hawakuzama.
3 Na pia aliwaelezea kuhusu nchi ya ahadi, ambayo walipokea — jinsi Bwana
alivyokuwa na huruma katika kutuonya kwamba tukimbie kutoka nchi ya
Yerusalemu.
4 Kwani, tazama, alisema, nimeona ono, ambalo najua kwamba Yerusalemu
imeangamizwa; na kama tungebaki Yerusalemu tungekuwa tumeangamia pia.
5 Lakini, akasema, ingawa tumepata masumbuko, tumepokea nchi ya ahadi, nchi
ambayo ni bora zaidi ya nchi zingine zote; nchi ambayo Bwana Mungu ameagana na
mimi kwamba itakuwa urithi wa uzao wangu. Ndio, Bwana ameagana na mimi
kuhusu nchi hii, na kwa watoto wangu milele, na pia wale wote ambao watatolewa
kutoka nchi zingine kwa mkono wa Bwana.
6 Kwa hivyo, mimi, Lehi, natoa unabii kulingana na mahimizo ya Roho aliye ndani
yangu, kwamba hakuna yeyote atakayekuja katika nchi hii ila tu wale ambao
wataletwa na mkono wa Bwana.
7 Kwa hivyo, nchi hii imewekwa wakfu kwa yule atakayeletwa na yeye. Na ikiwa
kwamba watamtumikia kulingana na amri ambazo amewapatia, itakuwa nchi ya
uhuru kwao; kwa hivyo, hawatatekwa nyara kamwe; au sivyo, itakuwa ni kwa sababu
ya uovu; kwani uovu ukiwepo, nchi italaaniwa kwa sababu yao, lakini kwa wale
watakatifu itabarikiwa milele.
8 Na tazama, ni hekima kwamba hii nchi ifichwe tokana na ufahamu wa mataifa
mengine; kwani tazama, mataifa mengi yangeinyakua hii nchi, hata kwamba pasiwe
na mahali pa kurithiwa.
9 Kwa hivyo, mimi, Lehi, nimepokea ahadi, kwamba kama wale ambao Bwana
Mungu atawatoa kutoka nchi ya Yerusalemu watatii amri zake, watafanikiwa katika
nchi hii; na watafichwa tokana na mataifa mengine, kwamba wapokee nchi hii. Na
kama watatii amri zake watabarikiwa usoni mwa nchi hii, na hakuna yeyote
atakayewaudhi, wala kuwanyang'anya nchi yao ya urithi; na wataishi salama milele.
10 Lakini tazama, wakati ukitimia watakapofifia katika kutoamini, baada ya
kupokea baraka nyingi kutoka mkono wa Bwana — wakiwa na ufahamu wa uumbaji
wa dunia, na watu wote, wakielewa kazi kuu na ya maajabu ya Bwana tangu uumbaji
wa ulimwengu; na wakipewa nguvu za kutenda vitu vyote kwa imani; wakiwa na
amri zote tangu mwanzo, na wakiwa wameletwa kwa wema wake usio na kikomo
katika nchi hii ya ahadi — tazama, nasema, kama siku itafika ambapo watamkataa
yule Mtakatifu wa Israeli, yule Masiya wa kweli, Mkombozi wao na Mungu wao,

tazama, hukumu za yule mwenye haki zitakuwa juu yao.
11 Ndio, atawaletea mataifa mengine, na atayapatia nguvu, na ataondoa kutoka
kwao nchi ile ambayo ni mali yao, na atawasababisha kutawanywa na kupigwa.
12 Ndio, wakati kizazi kitakapopita kwa kingine kutakuwa na umwagaji wa damu,
na mapigo makali miongoni mwao; kwa hivyo, wana wangu, ningetaka mkumbuke;
ndio, ningetaka kwamba msikilize maneno yangu.
13 Ee kwamba nyinyi mngezinduka; zindukeni kutoka usingizi mzito, ndio, hata
kutoka usingizi wa jahanamu, na mjifungue minyororo ambayo mmefungiwa,
ambayo ni minyororo inayowafunga watoto wa watu, kwamba wanachukuliwa
mateka hadi kwenye lile shimo la milele lenye mateso na huzuni.
14 Zindukeni! na muinuke kutoka mavumbini, na msikie maneno ya mzazi dhaifu,
ambaye viungo vyake hivi karibuni lazima mvitie kwenye kaburi kimya lenye baridi,
ambalo hakuna msafiri yeyote anayeweza kurejea kutoka humo; siku chache
zimebaki na nitaenda njia ya ulimwengu wote.
15 Lakini tazama, Bwana ameikomboa nafsi yangu kutoka jahanamu; nimeuona
utukufu wake, na nimezingirwa milele katika mikono ya upendo wake.
16 Na ninatamani kwamba mkumbuke kuchunguza sheria na hukumu za Bwana;
tazama, huu ndio wasiwasi wa nafsi wangu tangu mwanzoni.
17 Moyo wangu umechoshwa na huzuni mara kwa mara, kwani naogopa kwamba
tokana na ugumu wa mioyo yenu Bwana Mungu wenu atawateremkia kwa
ghadhabu yake timilifu, hata kwamba mtengwe na kuangamizwa milele.
18 Au, kwamba laana itawapata kwa muda wa vizazi vingi; na muadhibiwe kwa
upanga, na kwa njaa, na mchukiwe, na kuongozwa kulingana na nia na utumwa wa
ibilisi.
19 Enyi wana wangu, kwamba vitu hivi visiwajie, lakini kwamba muwe watu wateule
na wa kuheshimika na Bwana. Lakini tazama, nia yake itendeke; kwani njia zake ni
takatifu milele.
20 Na amesema kwamba: Kama mtashika amri zangu mtafanikiwa nchini; lakini
kama mtakataa amri zangu mtatengwa tokana na uwepo wangu.
21 Na sasa ili roho yangu iaeshangwe nanyi, na ili moyo wangu uondoke ulimwengu
huu ukifurahishwa nanyi, kwamba nisishushwe chini kaburini kwa hofu na huzuni,
basi, inukeni kutoka mavumbini, wana wangu, na muwe wanaume, na muamue kwa
mawazo na kwa moyo mmoja, mkiungana kwa vitu vyote, ili msiingie utumwani;
22 Ili msilaaniwe kwa laana kali; na pia, ili msijiletee ghadhabu ya Mungu wa haki,
kwa kuangamizwa, ndio, kuangamizwa milele kwa roho na mwili.
23 Zindukeni, wana wangu; jivikeni silaha za utakatifu. Jifungueni minyororo
ambayo imewafunga, na mtoke fumboni, na muinuke kutoka mavumbini.
24 Msimwasi kaka yenu tena, ambaye maono yake yamekuwa matukufu, na ambaye
ametii amri tangu wakati tulipoondoka Yerusalemu; na ambaye amekuwa chombo
mikononi mwa Mungu, katika kutuleta hadi kwenye nchi ya ahadi; kwani kama sio
yeye, lazima tungeangamia kwa njaa huko nyikani; walakini, mlitaka kumtoa uhai
wake; ndio, na ameteseka kwa hofu nyingi kwa sababu yenu.
25 Na ninaogopa na kutetemeka zaidi kwa sababu yenu, kwamba atateseka tena;
kwani tazama, mmemlaumu kwamba alitaka awe na uwezo na mamlaka juu yenu;
lakini najua kwamba hakutaka awe na uwezo wala mamlaka juu yenu, lakini alitaka
kumtukuza Mungu, na ustawi wenu wa milele.
26 Na mmenung'unika kwa sababu amekuwa wazi kwenu. Mmesema kwamba

ametumia ukali; na mnasema kwamba amewakasirikia; lakini tazama, ukali wake
ulikuwa ukali wa nguvu za neno la Mungu, ambalo lilikuwa ndani yake; na lile
mnaloliita hasira lilikuwa ukweli, kulingana na ule ulio ndani ya Mungu, ambao
hangezuia, akidhihirisha kwa ujasiri kuhusu maovu yenu.
27 Na ni lazima kwamba nguvu za Mungu ziwe na yeye, hata kwamba lazima mtii
akiwaamrisha. Lakini tazama, sio yeye, bali ilikuwa Roho ya Bwana iliyokuwa ndani
yake, ambayo ilifungua kinywa chake ili azungumze hata kwamba hangefunga
kinywa chake.
28 Na sasa mwana wangu, Lamani, na pia Lemueli na Samu, na pia wana wangu
ambao ni wana wa Ishmaeli, tazama, kama mtasikiliza sauti ya Nefi hamtaangamia.
Na kama mtamsikiliza nitawaachia baraka, ndio, hata baraka yangu ya kwanza.
29 Lakini ikiwa hamtamsikiza ninaondoa baraka yangu ya kwanza, ndio, hata
baraka yangu, na itakuwa juu yake.
30 Na sasa, Zoramu, nakuzungumzia wewe: Tazama, wewe ni mtumishi wa Labani;
walakini, wewe umetolewa kutoka nchi ya Yerusalemu, na ninajua kwamba wewe ni
rafiki wa kweli wa mwana wangu Nefi, milele.
31 Kwa hivyo, kwa vile umekuwa mwaminifu uzao wako utabarikiwa pamoja na
mbegu yake, hata kwamba wataishi kwa mafanikio kwa muda mrefu katika nchi hii;
na hakuna chochote, ila tu ni uovu miongoni mwao, kitakachowadhulumu au
kusumbua mafanikio yao usoni mwa nchi hii milele.
32 Kwa hivyo, kama utatii amri za Bwana, Bwana ameweka nchi hii wakfu kwa
usalama wa uzao wako na uzao wa mwana wangu.

## 2 Nefi 2

1 Na sasa, Yakobo, nakuzungumzia: Wewe ndiye mzaliwa wa kwanza katika siku
zangu za taabu nyikani. Na tazama, katika utoto wako, umeteseka kwa masumbuko
na huzuni nyingi, kwa sababu ya ujeuri wa kaka zako.
2 Walakini, Yakobo, mzaliwa wangu wa kwanza nyikani, wewe unajua ukuu wa
Mungu; na ataweka wakfu masumbuko yako kwa faida yako.
3 Kwa hivyo, nafsi yako itabarikiwa, na wewe utaishi salama na kaka yako, Nefi; na
utamtumikia Mungu wako maishani mwako. Kwa hivyo, najua kwamba wewe
umekombolewa, kwa sababu ya utakatifu wa Mkombozi wako; kwani wewe umeona
kwamba katika wakati mtimilifu yeye atakuja kuwaletea wanadamu wokovu.
4 Na wewe umeona ujanani mwako utukufu wake; kwa hivyo, wewe umebarikiwa
kama wale atakaowahudumia katika mwili; kwani Roho ni sawa, jana, leo, na milele.
Na njia imetayarishwa tangu kuanguka kwa mwanadamu, na wokovu ni bure.
5 Na wanadamu wanashauriwa kikamilifu kwamba wajue mema na maovu. Na
wanadamu wanapewa sheria. Na hakuna yeyote anayekubalika kwa sheria; au, kwa
sheria wanadamu wanatengwa. Ndio, walitengwa kwa sheria ya muda; na pia, kwa
sheria ya kiroho wanaangamizwa tokana na yale yalio mema, na wanadhoofika
milele.
6 Kwa hivyo, ukombozi unakuja kupitia Masiya Mtakatifu; kwani amejaa neema
na kweli.
7 Tazama, anajitoa kuwa dhabihu ya dhambi, kutimiza masharti ya sheria, kwa
wale wote wenye moyo uliopondeka na roho iliyovunjika; na hakuna mwingine
yeyote anayeweza kutimiza masharti ya sheria.

8 Kwa hivyo, ni muhimu sana kuwajulisha wakazi wa dunia kuhusu vitu hivi, ili wajue hakuna binadamu anayeweza kuishi karibu na Mungu, bila fadhili, na rehema, na neema za Masiya Mtakatifu, ambaye anatoa maisha yake mwilini, na kuichukua tena kwa uwezo wa Roho, ili alete ufufuo wa wafu, akiwa wa kwanza kufufuka.

9 Kwa hivyo, yeye ni malimbuko kwa Mungu, kwani atawaombea watoto wa watu wote; na wale watakaomwamini wataokolewa.

10 Na kwa sababu ya maombi kwa wote, watu wote wanamjia Mungu; kwa hivyo, wanasimama kwenye uwepo wake, na kuhukumiwa na yeye kulingana na ukweli na utakatifu wake. Kwa hivyo, masharti ya sheria ambayo yule Mtakatifu ametoa, yatalingana na maadhibio na mapigo yake, haya maadhibio ni kinyume cha furaha ya kutii amri, hii ni kutimiza masharti ya upatanisho—

11 Kwani lazima, kuwe na upinzani katika vitu vyote. Kama sio hivyo, mzaliwa wangu wa kwanza nyikani, utakatifu haungepatikana, wala uovu, wala utakatifu au hofu, wala uzuri au ubaya. Kwa hivyo, vitu vyote lazima viwe kitu kimoja; kwa hivyo, kama ni kitu kimoja lazima kikae kama mauti, bila uhai wala kifo, wala uharibifu au kutoharibika, furaha wala hofu, wala kufahamu au kutofahamu.

12 Kwa hivyo, itakuwa kwamba kiliumbwa bure; kwa hivyo itakuwa kwamba hakuna kusudi la kuumbwa kwake. Kwa hivyo, kitu hiki kinaangamiza hekima ya Mungu na makusudi yake ya milele, na pia nguvu, na rehema, na haki ya Mungu.

13 Na kama mtasema hakuna sheria, mtasema pia hakuna dhambi. Kama mtasema hakuna dhambi, mtasema pia hakuna utakatifu. Na kama hakuna utakatifu hakuna furaha. Na kama hakuna utakatifu wala furaha basi hakuna adhabu wala huruma. Na kama vitu hivi havipo basi hakuna Mungu. Na kama hakuna Mungu basi sisi hatupo, wala dunia; kwani hakungekuwa na uumbaji wa vitu, wala kutenda au kutendewa; kwa hivyo, vitu vyote lazima vingetokomea.

14 Na sasa, wana wangu, nawaambia vitu hivi kwa faida yenu na elimu; kwani kuna Mungu, na ameumba vitu vyote, mbingu na dunia, na vitu vyote vilivyomo, vitu vya kutenda na vitu vya kutendewa.

15 Na kutimiza makusudio yake ya milele katika kikomo cha mwanadamu, baada ya kuumba wazazi wetu wa kwanza, na wanyama wa porini na ndege wa hewani, na mwishowe, vitu vyote vilivyoumbwa, ilibidi lazima kuwe na upinzani, hata tunda lililokataliwa kinyume cha mti wa uzima; mmoja ukiwa mtamu na mwingine ukiwa chungu.

16 Kwa hivyo, Bwana Mungu amemruhusu mwanadamu kujitendea mwenyewe. Kwa hivyo, mwanadamu hangeweza kujitendea mwenyewe bila kuvutiwa na moja au nyingine.

17 Na mimi, Lehi, kulingana na vitu ambavyo nimesoma, lazima niwaze kwamba malaika wa Mungu, alianguka kutoka mbinguni, kulingana na yale yameandikwa; kwa hivyo, akawa ibilisi, kwani alitaka kutenda maovu machoni mwa Mungu.

18 Na kwa sababu alianguka kutoka mbinguni, na kuhuzunika milele, aliwatakia wanadamu nao pia wahuzunike. Kwa hivyo, akamwambia Hawa, ndio, hata yule nyoka wa zamani, ambaye ni ibilisi, ambaye ni baba wa uwongo wote, kwa hivyo akasema: Kuleni tunda lililokatazwa, na hamtakufa, lakini mtakuwa kama Mungu, mkifahamu mema na maovu.

19 Na baada ya Adamu na Hawa kula tunda lililokatazwa walifukuzwa kutoka bustani ya Edeni, ili walime ardhi.

20 Na wamezaa watoto; ndio, hata jamii ya dunia yote.

21 Na maisha ya watoto wa watu yaliongezewa, kulingana na nia ya Mungu, ili
waweze kutubu wakiwa hai; kwa hivyo, hali yao ikawa hali ya majaribio, na wakati
wao ukaongezewa, kulingana na amri ambazo Bwana Mungu aliwapatia watoto wa
watu. Kwani alitoa amri kwamba lazima wanadamu wote watubu; kwani alionyesha
wanadamu wote kwamba walipotea, kwa sababu wazazi wao walivunja sheria.
22 Na sasa, tazama, kama Adamu hangevunja sheria hangeanguka, lakini angeishi
katika bustani ya Edeni. Na vitu vyote vilivyoumbwa vingebaki katika hali yao ya
kwanza baada ya kuumbwa; na vingebaki vivyo hivyo milele, na kuwa bila mwisho.
23 Na hawangezaa watoto; na hivyo wangeishi katika hali ya kitoto, bila shangwe,
kwani hawakufahamu dhiki; bila kutenda mema, kwani hawakujua dhambi.
24 Lakini tazama, vitu vyote vimetendwa kwa hekima ya yule ajuaye vitu vyote.
25 Adamu alianguka ili wanadamu wawe; na wanadamu wapo, ili wapate shangwe.
26 Na Masiya anakuja katika wakati mtimilifu, ili awakomboe watoto wa watu
tokana na mwanguko. Na kwa sababu wamekombolewa tokana na mwanguko
wamekuwa huru milele, wakielewa mema na maovu; kujitendea wenyewe na sio
kutendewa, ila tu katika kuadhibiwa na sheria katika siku ile kuu ya mwisho,
kulingana na amri ambazo Mungu ametoa.
27 Kwa hivyo, wanadamu wana uhuru wanapoishi; na wamepewa vitu vyote
ambavyo ni muhimu kwa mwanadamu. Na wana haki kuchagua uhuru na uzima wa
milele, kupitia yule Mpatanishi mkuu wa wanadamu wote, au kuchagua utumwa na
kifo, kulingana na utumwa na nguvu za ibilisi; kwani anataka wanadamu wote wawe
na dhiki kama yeye.
28 Na sasa, wana wangu, ningetaka mtazame yule Mpatanishi mkuu, na msikilize
amri zake kuu; na muwe waaminifu kwa maneno yake, na mchague uzima wa milele,
kulingana na mapenzi ya Roho Mtakatifu wake.
29 Na msichague kifo cha milele, ambacho ni kulingana na nia ya mwili na uovo
ulio ndani yake, ambayo inaipatia roho ya ibilisi nguvu za kuteka nyara, na kukuleta
jahanamu, ili awatawale katika ufalme wake.
30 Nimewazungumzia nyinyi nyote, wana wangu, haya maneno machache, katika
siku zangu za mwisho za majaribio; na nimechagua sehemu njema, kulingana na
maneno ya nabii. Na sina lengo lingine lolote ila ustawi wenu usio na mwisho wa
nafsi zenu. Amina.

# 2 Nefi 3

1 Na sasa nakuzungumzia wewe, Yusufu, kitinda mimba wangu. Wewe ulizaliwa huko
nyikani nikisumbuka; ndio, katika siku za msiba wangu mkuu mama yako alikuzaa.
2 Na Bwana akuwekee wakfu nchi hii pia, ambayo ni nchi bora zaidi, kwa urithi
wako na kwa urithi wa uzao wako na kaka zako, kwa usalama wako milele, kama
utatii amri za yule aliye Mtakatifu wa Israeli.
3 Na sasa, Yusufu, kitinda mimba wangu ambaye nimemzaa huko nyikani
nikisumbuka, Bwana akubariki milele, kwani uzao wako hautaangamizwa kabisa.
4 Kwani tazama, wewe ni matunda ya kiuno changu; na mimi ni uzao wa Yusufu
aliyeuzwa Misri. Na makubwa yalikuwa maagano ya Bwana ambayo alimfanyia
Yusufu.
5 Kwa hivyo, Yusufu kwa hakika aliona siku yetu. Na akapokea ahadi kwa Bwana,
kwamba kutoka matunda ya viuno vyake Bwana Mungu angeinulia nyumba ya

Israeli, tawi takatifu; sio Masiya, lakini tawi ambalo lingekatwa, walakini,
kukumbukwa katika maagano ya Bwana kwamba Masiya angethirihishwa kwao
katika siku za baadaye, katika roho ya nguvu, ya kuwatoa gizani hadi kwenye
nuru — ndio, kutoka maficho ya giza na kutoka utumwani hadi kwenye uhuru.
6 Kwani Yusufu alishuhudia kwa hakika, akisema: Bwana Mungu wangu atainua
mwonaji, ambaye atakuwa mwonaji bora kwa uzao wa viuno vyangu.
7 Ndio, Yusufu kwa hakika alisema: Hivi ndivyo Bwana ananiambia: Ni mwonaji
bora nitakayeinua kutoka matunda ya viuno vyako; na ataheshimiwa zaidi
miongoni mwa matunda ya viuno vyako. Naye nitamwamurisha afanyie matunda ya
viuno vyako kazi, ndugu zake, ambayo itakuwa ya thamani kuu kwao, hata kwa
kuwafahamisha ufahamu wa maagano ambayo nimeagana na baba zenu.
8 Na nitampatia amri kwamba asitende kazi nyingine, ila ile kazi
nitakayomwamuru. Na nitamuinua juu machoni mwangu; kwani atafanya kazi
yangu.
9 Na atakuwa mkuu kama Musa, ambaye nimesema nitamuinulia, kukomboa watu
wangu, Enyi nyumba ya Israeli.
10 Na nitamuinua Musa, ili akomboe watu wako kutoka nchi ya Misri.
11 Lakini nitamuinua mwonaji kutoka matunda ya viuno vyako; na nitampatia
nguvu za kuleta neno langu kwa uzao wa viuno vyako — na sio tu kuwaletea neno
langu pekee, asema Bwana, lakini hata kwa kuwathibitishia wao neno langu, ambalo
watakuwa wamelipata awali.
12 Kwa hivyo, uzao wa viuno vyako utaandika; na uzao wa viuno vya Yuda
utaandika; na yale yatakayoandikwa na uzao wa viuno vyako, na pia yale yatakayo
andikwa na uzao wa viuno vya Yuda, yatakua pamoja, kwa kufadhaisha mafundisho
ya uwongo na kutatua mabishano, na kuimarisha amani miongoni mwa uzao wa
viuno vyako, na kuwapatia ufahamu wa baba zao katika siku za mwisho, na pia
kufahamu maagano yangu, asema Bwana.
13 Na kutoka kwa unyonge atapewa nguvu, katika siku ile ambayo kazi yangu
itaanza miongoni mwa watu wangu, kwa kuwarudisha nyinyi, Enyi nyumba ya
Israeli, asema Bwana.
14 Na hivi ndivyo Yusufu alivyotoa unabii, akisema: Tazama, Bwana atambariki
yule mwonaji; na wale ambao wanataka kumwangamiza watateketezwa; kwani
ahadi hii, ambayo nimepokea kutoka kwa Bwana, kuhusu uzao wa viuno vyangu,
itatimizwa. Tazama, nina hakika kwamba ahadi hii itatimizwa;
15 Na jina lake litakuwa kama langu; na litakuwa sawa na jina la baba yake. Na
atakuwa kama mimi; kwani kuwa kitu, ambacho Bwana atakileta kwa mkono wake,
kwa uwezo wa Bwana atawaleta watu wangu kwenye wokovu.
16 Ndio, hivi ndivyo Yusufu alivyotoa unabii: Nina uhakika kwa kitu hiki, hata vile
nilivyo na uhakika wa ahadi ya Musa; kwani Bwana ameniambia, nitaihifadhi uzao
wako milele.
17 Na Bwana amesema: Nitamuinua Musa mmoja; na nitampatia nguvu kwa
fimbo; na nitampatia hukumu katika maandishi. Lakini sitalegeza ulimi wake, ili
aweze kuzungumza mengi, kwani sitamfanya awe hodari kwa mazungumzo. Lakini
nitamuandikia sheria zangu, kwa kidole cha mkono wangu; na nitampatia mnenaji.
18 Na Bwana aliniambia pia: Nitainua uzao wa viuno vyako; na nitampatia
mnenaji. Na mimi, tazama, nitamwezesha kwamba aandike maandishi ya uzao wa
viuno vyako, kwa uzao wa viuno vyako; na mnenaji wa viuno vyako ataitangaza.

19 Na maneno atakayoandika yatakuwa maneno ambayo kwa hekima yangu ni
lazima yafikie mazao ya viuno vyako. Na itakuwa ni kama uzao wa viuno vyako
uliwalilia kutoka mavumbini; kwani ni najua imani yao.
20 Na watalia kutoka mavumbini; ndio, hata toba kwa ndugu zao, hata baada ya
vizazi vingi kuwapitia. Na itakuwa kwamba kilio chao kitapita, hata kulingana na
wepesi wa maneno yao.
21 Kwa sababu ya imani yao maneno yao yatatoka kutoka kinywa changu hadi kwa
ndugu zao ambao ni uzao wa viuno vyako; na katika unyonge wa maneno yao
nitawatia nguvu kwa imani, ya kukumbuka agano langu ambalo niliagana na baba
zako.
22 Na sasa, tazama, mwana wangu Yusufu, hivi ndivyo baba yangu wa kale alitoa
unabii.
23 Kwa hivyo, kwa sababu ya hili agano umebarikiwa; kwani uzao wako
hautaangamizwa, kwani watatii maneno ya hicho kitabu.
24 Na atainuka mmoja miongoni mwao ambaye atakuwa shujaa, ambaye atatenda
mema mengi, kwa maneno na kwa vitendo, akiwa chombo mikononi mwa Mungu,
mwenye imani kuu, kutenda maajabu makuu, na kutenda kile kitu ambacho ni
kikuu machoni mwa Mungu, kwa kutimiza ufufuo wa nyumba ya Israeli, pamoja na
uzao wa kaka zako.
25 Na sasa, Yusufu, umebarikiwa. Tazama, wewe ni mchanga; kwa hivyo sikiliza
maneno ya kaka yako, Nefi, na utatendewa kulingana na yale maneno ambayo
nimezungumza. Kumbuka maneno ya baba yako anayekufa. Amina.

## 2 Nefi 4

1 Na sasa, mimi, Nefi, ninazungumza kuhusu ule unabii ambao baba yangu alitaja,
kuhusu Yusufu, ambaye alipelekwa hadi Misri.
2 Kwani tazama, kwa kweli alitoa unabii kuhusu uzao wake wote. Na hakuna
unabii mwingi mkubwa, zaidi ya yale aliyoandika. Na alitoa unabii kutuhusu sisi, na
vizazi vyetu vya baadaye; na umeandikwa kwenye bamba za shaba.
3 Kwa hivyo, baada ya baba yangu kukoma kuzungumza kuhusu unabii wa Yusufu,
akaita wana wa Lamani, wana wake, na mabinti zake, na akawaambia: Tazameni,
wana wangu, na mabinti zangu, ambao ni wana na mabinti za kifungua mimba
wangu, ningependa kwamba msikilize maneno yangu.
4 Kwani Bwana Mungu amesema kwamba: Kadiri mtakavyo tii amri zangu
mtafanikiwa nchini; na msipotii amri zangu mtatengwa kutokana na uwepo wangu.
5 Lakini tazameni, wana wangu na mabinti zangu, siwezi kufa kabla sijawapatia
baraka; kwani tazameni, ninajua kwamba kama mtalelewa kulingana na njia inayo
wapasa hamtaiacha.
6 Kwa hivyo, kama mmelaaniwa, tazameni, ninawaachia baraka yangu, kwamba ile
laana iondolewe kwenu na iwe juu ya wazazi wenu.
7 Kwa hivyo, kwa sababu ya baraka yangu Bwana Mungu hatakubali kwamba
mwangamie; kwa hivyo, atawarehemu nyinyi na uzao wenu milele.
8 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu kumaliza kuzungumzia wana na mabinti
za Lamani, aliwasababisha wana na mabinti za Lemueli kusimama mbele yake.
9 Na akawazungumzia, akisema: Tazama, wana wangu na mabinti zangu, ambao
ni wana na mabinti za mwana wangu wa pili; tazama ninawapatia baraka kama ile

ambayo niliwapatia wana na mabinti za Lamani; kwa hivyo, nyinyi hamtaangamizwa kabisa; lakini uzao wenu utabarikiwa mwishowe.

10 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu kukoma kuwazungumzia, tazama, aliwazungumzia wana wa Ishmaeli, ndio, na hata nyumba yake yote.

11 Na baada ya kukoma kuwazungumzia, alimwambia Samu, akisema: Heri wewe, na uzao wako; kwani wewe utarithi nchi kama vile kaka yako Nefi. Na uzao wako utahesabiwa na uzao wake; na wewe utakuwa kama kaka yako, na uzao wako kama uzao wake; na wewe utabarikiwa katika siku zako zote.

12 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu, Lehi, kumaliza kuzungumzia jamaa yake yote, kulingana na mawazo ya moyo wake na Roho ya Bwana ambaye alikuwa ndani yake, akawa mzee. Na ikawa kwamba alifariki, na akazikwa.

13 Na ikawa kwamba muda mfupi baada ya kifo chake, Lamani na Lemueli pamoja na wana wa Ishmaeli walinikasirikia kwa sababu walirudiwa na Bwana.

14 Kwani mimi, Nefi, nilishurutishwa kuwazungumzia, kulingana na neno lake; kwani nilikuwa nimewazungumzia vitu vingi, na pia baba yangu, kabla ya kifo chake; maneno mengi ambayo yameandikwa kwenye bamba zangu zingine; kwani sehemu kubwa zaidi ya historia imeandikwa kwenye bamba zangu zingine.

15 Na katika hizi nimeandika mambo ya nafsi yangu, na maandiko mengi ambayo yamechorwa kwenye bamba za shaba. Kwani moyo wangu unafurahia maandiko, na moyo wangu huyatafakari, na kuyaandika kwa elimu na faida ya watoto wangu.

16 Tazama, nafsi yangu hufurahia vitu vya Bwana; na moyo wangu huyatafakari mara kwa mara vitu ambavyo nimeviona na kuvisikia.

17 Walakini, ingawa Bwana ana wema mkubwa, hata kunionyesha kazi yake kuu na ya maajabu, moyo wangu unalia: Ewe mimi mtu mwovu! Ndio, moyo wangu unahuzunishwa kwa sababu ya mwili wangu; moyo wangu unahofishwa na dhambi zangu.

18 Nimezingirwa, kwa sababu ya majaribio na dhambi ambazo zinaninasa kwa urahisi.

19 Na ninapotaka kushangilia, moyo wangu huugua kwa sababu ya dhambi zangu; walakini, ninajua ninayemwamini.

20 Mungu wangu amekuwa tegemeo langu; ameniongoza katika masumbuko yangu nyikani; na amenihifadhi hata kutoka kilindi kikuu cha maji.

21 Amenijaza upendo wake, hata kwa kumaliza mwili wangu.

22 Amewafadhaisha maadui wangu, hata kuwasababisha kutetemeka mbele yangu.

23 Tazama, amesikia kilio changu mchana, na kunipatia ufahamu usiku kwa maono.

24 Na kwa mchana nimesali kwa ujasiri; ndio, nimepaza sauti yangu juu; na malaika wakateremka na kunihudumia.

25 Na kwenye mabawa ya Roho yake mwili wangu umebebwa na kuchukuliwa kwenye milima mirefu zaidi. Na macho yangu yameona vitu vikuu, ndio, hata vikuu sana kwa mwanadamu; kwa hivyo niliamriwa kwamba nisiviandike.

26 Ee basi, kama nimeona mambo makuu hivi, kama Bwana katika ufadhili wake kwa watoto wa watu amewafariji wanadamu kwa huruma kuu hivi, kwa nini moyo wangu ulie na nafsi yangu kusita katika bonde la hofu, na mwili wangu kuwa mnyonge, na nguvu zangu kufifia, kwa sababu ya masumbuko yangu?

27 Na kwa nini nitumikie dhambi, kwa sababu ya mwili wangu? Ndio, kwa nini niyakubali majaribio, hata kwamba yule mwovu apate nafasi moyoni mwangu ya kuangamiza amani na kusumbua nafsi yangu? Kwa nini nikasirishwe na adui yangu?

28 Amka, roho yangu! Usilemewe na dhambi tena. Shangilia, Ewe moyo wangu, na
usimpatie adui wa nafsi yangu mahali.
29 Usikasirike tena kwa sababu ya maadui zangu. Usipungukiwe na nguvu kwa
sababu ya masumbuko yangu.
30 Shangilia, Ewe moyo wangu, na umlilie Bwana, na kusema: Ewe Bwana,
nitakusifu milele; ndio, nafsi yangu itashangilia ndani yako, Mungu wangu, na
mwamba wa wokovu wangu.
31 Ewe Bwana, je, utaikomboa nafsi yangu? Je, utaniopoa kutoka mikononi mwa
maadui zangu? Je, utanifanya kwamba nitetemeke nikiona dhambi?
32 Na milango ya jahanamu ifungwe mbele yangu daima, kwa sababu moyo wangu
umevunjika na nafsi yangu imepondeka! Ewe Bwana, je, usiifunge milango ya haki
yako mbele yangu, ili nitembee katika mapito ya bonde iliyo chini, hata niwe mkali
kwenye njia iliyo wazi!
33 Ewe Bwana, je, utanizingira na joho la haki yako! Ewe Bwana, je, utanitayarishia
njia ya kutorokea maadui wangu! Je, utaninyooshea mapito yangu! Je, utaniwekea
kikwazo kwa njia yangu—lakini kwamba unifanyie njia zangu ziwe wazi, na usizibe
njia yangu, lakini njia za adui yangu.
34 Ewe Bwana, nimekuamini, na nitakuamini milele. Sitaweka tumaini langu
kwenye mkono wa mwanadamu; kwani ninajua amelaaniwa yule anayeweka
tumaini lake kwa mkono wa mwanadamu. Ndio, amelaaniwa yule anayeweka
tumaini lake kwa mwanadamu au amfanyaye kuwa mkono wake.
35 Ndio, ninajua kwamba Mungu humsaidia anayeomba bila kizuizi. Ndio, Mungu
wangu atanipatia, nikiomba bila kasoro; kwa hivyo nitakupazia sauti yangu; ndio,
nitakulilia, Mungu wangu, mwamba wa haki yangu. Tazama, nitakupazia sauti
yangu milele, mwamba wangu na Mungu wangu asiye na mwisho. Amina.

## 2 Nefi 5

1 Tazama, ikawa kwamba mimi, Nefi, nilimlilia Bwana Mungu wangu, kwa sababu ya
hasira ya kaka zangu.
2 Lakini tazama, hasira yao ilinizidia, hata wakataka kunitoa uhai.
3 Ndio, walininung'unikia, wakisema: Kaka yetu mdogo anataka kututawala; na
tumepatwa na majaribu mengi kwa sababu yake; kwa hivyo, tumuue sasa, ili
tusisumbuke tena kwa sababu ya maneno yake. Kwani tazama, hatutakubali awe
mtawala wetu; kwani utawala ni wetu, sisi ambao ni kaka zake wakubwa,
kuwatawala hawa watu.
4 Sasa mimi siandiki kwenye bamba haya maneno yote ambayo walininung'unikia.
Lakini inatosha mimi kusema, kwamba walitaka kunitoa uhai wangu.
5 Na ikawa kwamba Bwana alinionya, mimi, Nefi, kwamba niwaondokee na
nikimbilie huko nyikani, pamoja na wale wote watakaonifuata.
6 Kwa hivyo, ikawa kwamba mimi, Nefi, nilichukua jamaa yangu pia na Zoramu na
jamaa yake, na Samu, kaka yangu mkubwa, na jamaa yake, na Yakobo na Yusufu,
kaka zangu wadogo, pia na dada zangu, na wale wote ambao wangenifuata. Na wale
wote ambao wangenifuata ni wale ambao waliamini maonyo na ufunuo wa Mungu;
kwa hivyo, walitii maneno yangu.
7 Na tukachukua hema zetu na vitu ambavyo viliwezekana kwetu, na tukasafiri
nyikani kwa muda wa siku nyingi. Na baada ya kusafiri kwa muda wa siku nyingi

tulipiga hema zetu.
8 Na watu wangu walitaka tupaite pahali pale Nefi; kwa hivyo, tulipaita Nefi.
9 Na wale wote waliokuwa na mimi waliamua kujiita watu wa Nefi.
10 Na tuliendelea kutii hukumu, maagizo na amri za Bwana katika vitu vyote,
kulingana na sheria ya Musa.
11 Na Bwana alikuwa pamoja nasi; na tulifanikiwa zaidi; kwani tulipanda mbegu,
na tukavuna kwa wingi. Na tukaanza kufuga mifugo, na makundi, na kila aina ya
wanyama.
12 Na mimi, Nefi, nilikuwa nimeleta maandishi yaliyokuwa yamechorwa kwenye
bamba za shaba; pamoja na mpira, au duara, ambayo baba yangu alitengenezewa na
mkono wa Bwana, kulingana na yale yameandikwa.
13 Na ikawa kwamba tulianza kufanikiwa zaidi, na kuongezeka katika nchi.
14 Na mimi, Nefi, nilichukua upanga wa Labani, na nikatengeneza panga nyingi
kwa umbo lake, nikishuku kwamba wale watu ambao sasa walikuwa wanaitwa
Walamani watatushukia na kutuangamiza; kwani nilijua chuki waliyokuwa nayo
kwangu na kwa watoto wangu na kwa wale walioitwa watu wangu.
15 Na niliwafundisha watu wangu kujenga majengo, na kutengeneza vitu vya kila
aina kwa kutumia mbao, na kwa chuma, na kwa shaba nyekundu, na kwa shaba, na
kwa pua, na kwa dhahabu, na kwa fedha, na kwa mawe ya thamani, ambayo
yalikuwa kwa wingi.
16 Na mimi, Nefi, nilijenga hekalu; na nilijenga kwa umbo la hekalu la Sulemani ila
tu halikujengwa na vitu vingi vya thamani; kwani havikupatikana nchini, kwa hivyo,
haingejengeka kikamilifu kama hekalu la Sulemani. Lakini umbo la mjengo ulikuwa
kama hekalu la Sulemani; na ujenzi wake ulikuwa wa hali ya juu.
17 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwasababisha watu wangu kuwa na bidii, na
kutenda kazi kwa mikono yao.
18 Na ikawa kwamba walitaka niwe mfalme wao. Lakini mimi, Nefi, sikutaka
wapate mfalme; walakini, niliwatendea kulingana na yale ambayo yalikuwa kwenye
uwezo wangu.
19 Na tazama, maneno ya Bwana yametimia kwa ndugu zangu ambayo alisema juu
yao, kwamba nitakuwa mtawala wao na mwalimu wao. Kwa hivyo, nilikuwa
mtawala wao na mwalimu wao, kulingana na amri za Bwana, hadi ule wakati ambao
walitaka kunitoa uhai.
20 Kwa hivyo, neno la Bwana lilitimizwa ambalo alinizungumzia, akisema: Kadiri
watakapokataa kusikiliza maneno yako watatolewa kwenye uwepo wa Bwana. Na
tazama, waliondolewa kutoka uwepo wake.
21 Na akasababisha laana iwashukie, ndio, hata laana kali, kwa sababu ya uovu wao.
Kwani tazama, walishupaza mioyo yao kwake, kwamba wakawa kama gumegume;
kwa hivyo, vile walikuwa weupe, na wenye ngozi nyororo na ya kuvutia na
kupendeza, ili wasiwashawishi watu wangu Bwana Mungu alisababisha wawe na
ngozi ya weusi.
22 Na Bwana Mungu akasema hivi: Nitasababisha kwamba wawe chukizo kwa watu
wako, wasipotubu maovu yao.
23 Na italaaniwa uzao wa yule atakayechanganyika na uzao wao; kwani watalaaniwa
kwa laana kama ile. Na Bwana akainena, na ikatendeka.
24 Na kwa sababu ya laana yao ambayo ilikuwa juu yao wakawa watu wavivu,
walijawa na ujanja na udanganyifu, na waliwinda wanyama wa mwituni huko

nyikani.
25 Na Bwana Mungu akaniambia: Watakuwa mjeledi kwa uzao wako, kuwachochea
wao kunikumbuka; na wasiponikumbuka, na kusikiza maneno yangu, watawapiga
hadi kuwaangamiza.
26 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwatenga Yakobo na Yusufu, kwamba wawe
makuhani na walimu katika nchi ya watu wangu.
27 Na ikawa kwamba tuliishi kwa furaha.
28 Na miaka thelathini ilikuwa imepita tangu tutoke Yerusalemu.
29 Na mimi, Nefi, nilikuwa nimeandika maandishi ya watu wangu, hadi ule wakati,
kwenye zile bamba nilizokuwa nimetengeneza.
30 Na ikawa kwamba Bwana Mungu akaniambia: Tengeneza bamba zingine; nawe
utaandika vitu vingi kwenye hizo bamba ambavyo ni vyema machoni mwangu, kwa
manufaa ya watu wako.
31 Kwa hivyo, mimi, Nefi, kwa kuwa ni mtiifu kwa amri za Bwana, nilienda na
kutengeneza hizi bamba ambazo nimeandikia vitu hivi.
32 Na niliandika yale ambayo yalimpendeza Mungu. Na kama watu wangu
watafurahishwa na vitu vya Mungu watafurahishwa na maandishi yangu ambayo
yako kwenye bamba hizi.
33 Na kama watu wangu wanataka kujua kikamilifu historia ya watu wangu lazima
wasome zile bamba zangu zingine.
34 Na inanitosha kusema kwamba miaka arobaini ilikuwa imepita, na tayari
tulikuwa na vita na mabishano dhidi ya kaka zangu.

## 2 Nefi 6

1 Maneno ya Yakobo, kaka yake Nefi, ambayo aliwazungumzia watu wa Nefi:
2 Tazameni, ndugu zangu wapendwa, mimi, Yakobo, nikiwa nimeitwa na Mungu,
na kutawazwa wake mtakatifu, na nikiwa nimetawazwa na kaka yangu Nefi, ambaye
mnamtegemea kama mfalme au mlinzi, na ambaye pia mnamtegemea kwa usalama,
tazameni mnajua kwamba nimewazungumzia vitu vingi zaidi.
3 Walakini, nawazungumzia tena; kwani ninajali ustawi wa nafsi zenu. Ndio,
wasiwasi wangu ni mkubwa kwenu; na nyinyi mnajua imekuwa hivyo tangu
mwanzo. Kwani nimewashauri kwa bidii zote; na nimewafundisha maneno ya baba
yangu; na nimewazungumzia nyinyi kuhusu vitu vyote vilivyoandikwa, tangu
kuumbwa kwa ulimwengu.
4 Na sasa, tazameni, ningewazungumzia kuhusu vitu vilivyo, na vile vitakavyokuja;
kwa hivyo, nitawasomea maneno ya Isaya. Na ni maneno yale ambayo kaka yangu
anataka niwasomee. Na ninawazungumzia kwa manufaa yenu, ili mjifunze na
kulitukuza jina la Mungu wenu.
5 Na sasa, maneno ambayo nitasoma ni yale ambayo Isaya alizungumza kuhusu
nyumba yote ya Israeli; kwa hivyo, yanaweza kulinganishwa nanyi, kwani nyinyi ni
wa nyumba ya Israeli. Na kuna vitu vingi ambavyo vimezungumzwa na Isaya
ambavyo vinaweza kulinganishwa nanyi, kwa sababu nyinyi ni wa nyumba ya Israeli.
6 Na sasa, haya ndiyo maneno: Bwana Mungu asema hivi: Tazama, nitawainulia
Wayunani mkono wangu, na kuwapeperushia watu bendera yangu; na watawaleta
wana wenu mikononi mwao, na kuwabeba mabinti zenu mabegani mwao.
7 Na wafalme watakuwa baba walezi wenu, na malkia wao watakuwa mama walezi

wenu; watainamisha nyuso zao mbele zenu zikielekea udongoni, na kuramba
mavumbi ya miguu yenu; nanyi mtajua kwamba Mimi ni Bwana; kwani wale
wanaonisubiri hawataaibika.
8 Na sasa mimi, Yakobo, nitazungumza kuhusu maneno haya. Kwani tazama,
Bwana amenionyesha kwamba wale waliokuwa Yerusalemu, kule tulipotoka,
wameuawa na kupelekwa utumwani.
9 Walakini, Bwana amenionyesha kwamba watarejea tena. Na pia amenionyesha
kwamba Bwana Mungu, aliye Mtakatifu wa Israeli, atajidhihirisha kwao katika
mwili; na baada ya kujidhihirisha watampiga na kumsulubu, kulingana na maneno
ya malaika aliyenizungumzia.
10 Na baada ya wao kushupaza mioyo yao na kukaza shingo zao kwa yule Mtakatifu
wa Israeli, tazama hukumu za yule aliye Mtakatifu wa Israeli zitawateremkia. Na
siku inakuja kwamba watachapwa na kusumbuliwa.
11 Kwa hivyo, baada ya wao kufukuzwa hapa na pale, kwani malaika asema hivi,
wengi watasumbuka sana mwilini, na hawatakubaliwa kuangamia, kwa sababu ya
sala za walio waaminifu; watatawanywa, na kupigwa, na kuchukiwa; walakini,
Bwana atawarehemu, kwamba wakati watakapomfahamu Mkombozi wao,
watakusanywa pamoja tena katika nchi yao ya urithi.
12 Na heri Wayunani, wale ambao nabii ameandika juu yao; kwani tazama, kama
watatubu na hawapigani na Sayuni, na wasijiunge na lile kanisa kuu la machukizo,
wataokolewa; kwani Bwana Mungu atatimiza maagano yake aliyoagana na watoto
wake; na ni kwa sababu hii nabii ameandika maneno haya.
13 Kwa hivyo, wale wanaopigana dhidi ya Sayuni na watu wa agano la Bwana
wataramba mavumbi ya miguu yao; na watu wa Bwana hawataaibika. Kwani watu
wa Bwana ni wale wanaomsubiri; kwani bado wanangoja kuja kwa Masiya.
14 Na tazama, kulingana na maneno ya nabii, Masiya ataanza tena kwa mara ya pili
kuwakomboa; kwa hivyo, atajidhihirisha kwao kwa uwezo na utukufu mkuu, kwa
kuangamiza maadui wao, wakati siku ile itakapofika ambapo watamwamini; na
hatamuangamiza yeyote yule atakayemwamini.
15 Na wale wasiomwamini yeye wataangamizwa, kwa moto, na kwa dhoruba, na
kwa matetemeko ya ardhi, na kwa vita, na kwa tauni, na kwa njaa. Na watajua
kwamba Bwana ni Mungu, yule Mtakatifu wa Israeli.
16 Kwani mawindo yatanyang'anywa kutoka wale wenye nguvu, au mateka halali
kukombolewa?
17 Lakini Bwana asema hivi: Hata mateka wa shujaa watanyakuliwa, na mawindo ya
waovu kukombolewa; kwani Mwenyezi Mungu atawakomboa watu wake wa agano.
Kwani Bwana asema hivi: Nitashindana na wale wanaoshindana nawe—
18 Na nitawalisha wale wanaowadhulumu, kwa miili yao wenyewe; na watalewa kwa
damu yao wenyewe kama vile kwa mvinyo mtamu; na miili yote itafahamu kwamba
mimi Bwana ndiye Mwokozi wako na Mkombozi wako, yule Mwenye Enzi wa
Yakobo.

# 2 Nefi 7

1 Ndio, kwani Bwana asema hivi: Je, nimekuweka kando, au kukutenga milele?
Kwani Bwana asema hivi: Cheti cha talaka cha mama yako kiko wapi? Kwa nani
nimekuweka, au ni kwa nani anayenidai nimekuuza? Ndio, kwa nani nimekuuza?

Tazama, ni kwa uovu wenu mmejiuza, na ni kwa makosa yenu mama yenu ametengwa.

2 Kwa hivyo, nilipokuja, hakukuwepo mtu yeyote; nilipoita, ndio, hakukuwepo na yeyote wa kujibu. Ee nyumba ya Israeli, je, mkono wangu umefupishwa kwamba siwezi kukomboa, au sina uwezo wa kukomboa? Tazama, kwa kukemea kwangu ninakausha bahari, ninafanya mito yao kuwa nyika na samaki wao kunuka kwa sababu maji yao yamekauka, na wanakufa kwa sababu ya kiu.

3 Ninavisha mbingu na weusi, na kusababisha gunia iwe mavazi yao.

4 Bwana Mungu amenipatia ulimi wa aliyeelimika, kwamba niweze kujua jinsi ya kuwazungumzia katika majira, Ee nyumba ya Israeli. Wakati mmechoka anaamka asubuhi kwa asubuhi. Anaamsha sikio langu kusikia kama yule aliyeelimika.

5 Bwana Mungu amefungua sikio langu, na sikuasi wala kurudi nyuma.

6 Niliwapatia walionipiga mgongo wangu, na mashavu yangu kwa waliong'oa nywele. Sikuuficha uso wangu tokana na aibu na kutemewa mate.

7 Kwani Bwana Mungu atanisaidia, kwa hivyo sitafadhaishwa. Kwa hivyo nimekaza uso wangu kama jiwe, na ninajua kwamba sitaaibishwa.

8 Na Bwana yuko karibu, na ananitetea. Nani atashindana na mimi? Tusimame pamoja. Nani adui yangu? Anikaribie mimi, na nitampiga kwa nguvu za kinywa changu.

9 Kwani Bwana Mungu atanisaidia. Na wale watakaonihukumu, tazama, wote watakuwa wazee kama nguo, na kuliwa na nondo.

10 Ni nani miongoni mwenu anayemwogopa Bwana, anayetii sauti ya mtumishi wake, anayetembea kwa giza bila nuru?

11 Tazameni nyote mnaowasha moto, ambao mnajizingira kwa chembe za moto, tembeeni katika nuru ya moto wenu na kwa chembe za moto mnaowasha. Mtapata haya kutoka mkono wangu — mtalala chini kwa huzuni.

## 2 Nefi 8

1 Nisikizeni mimi, nyinyi ambao mnatafuta utakatifu. Tazameni mwamba kutoka ambapo mlichongwa, na kwenye shimo mlikotolewa.

2 Tazameni Ibrahimu, baba yenu, na Sara, aliyewazaa; kwani nimemwita pekee, na kumbariki.

3 Kwani Bwana atafariji Sayuni, atafariji sehemu zake zote zenye ukiwa; na atasababisha nyika yake kuwa kama Edeni, na jangwa lake kama bustani ya Bwana. Shangwe na furaha itakuwa ndani yake, pia na shukrani na sauti ya uimbaji.

4 Nisikilizeni, watu wangu; na mnipe sikio, Ee taifa langu; kwani sheria itatoka kwangu, na nitafanya hukumu zangu kubaki kama mwangaza kwa watu.

5 Haki yangu iko karibu; wokovu wangu umesonga mbele, na mkono wangu utahukumu watu. Visiwa vitaningoja, na watauamini mkono wangu.

6 Elekezeni macho yenu mbinguni, na mtazame huko chini duniani; kwani mbingu zitatoweka kama moshi, na dunia itazeeka kama vazi; na wale wanaoishi ndani yake watakufa vivyo hivyo. Lakini wokovu wangu utakuwa milele, na haki yangu haitaondolewa.

7 Nisikilizeni mimi, nyinyi ambao mnajua haki, wale watu ambao nimeandika sheria yangu moyoni mwao, msiogope mzaha wa wanadamu, wala msiogope matusi yao.

8 Kwani nondo atawala kama vazi, na mchango kuwala kama manyoya. Lakini
haki yangu itakuwa milele, na wokovu wangu utakuwa kutoka kizazi hadi kizazi.
9 Inuka, inuka! Vaa nguvu, Ee mkono wa Bwana; inuka kama katika siku za kale.
Kwani wewe sio yule aliyemchinja Rahabu, na kuumiza joka?
10 Kwani wewe sio yule ambaye amekausha bahari, maji ya kilindi kikuu; ambaye
amesababisha kilindi cha bahari kuwa njia ya wale waliokombolewa kupitia?
11 Kwa hivyo, wale waliokombolewa na Bwana watarejea, na kuja Sayuni wakiimba;
na shangwe isiyo na mwisho na utakatifu itakuwa juu ya vichwa vyao, na watapokea
furaha na shangwe; huzuni na kuomboleza zitatoweka.
12 Mimi ndiye; ndio, mimi ndimi yule anayekufariji. Tazama, wewe ni nani,
kwamba umwogope mwanadamu, atakayekufa, na mwanadamu, ambaye atafanywa
kuwa kama nyasi?
13 Na kumsahau Bwana muumba wako, ambaye ametandaza mbingu, na kujenga
msingi wa dunia, na ameendelea kuogopa kila siku, kwa sababu ya hasira ya
mdhalimu, kama aliye tayari kukuangamiza? Na hasira ya mdhalimu iko wapi?
14 Mateka mkimbizi anaharakisha, ili afunguliwe, na kwamba asife shimoni, wala
kwamba asikose mkate wake.
15 Lakini mimi ni Bwana Mungu wako, ambaye mawimbi yake yalizuka; Bwana wa
Majeshi ni jina langu.
16 Na nimeweka maneno yangu kinywani mwako, na kukuficha katika kivuli cha
mkono wangu, ili nipande mbingu na kujenga msingi wa dunia, na kuambia Sayuni:
Tazama, nyinyi ni watu wangu.
17 Inuka, inuka, simama wima, Ee Yerusalemu, ambaye amekunywa kutoka mkono
wa Bwana kikombe cha hasira yake — umekunywa mabaki ya kikombe cha
kuogopesha —
18 Na hakuna yeyote miongoni mwa wana wake wote aliozaa anayeweza
kumwongoza; wala yule anayemchukua kwa mkono wake, miongoni mwa wana
wale wote aliolea.
19 Hawa wana wawili wamekujia, ambao watakuhurumia — ukiwa na uangamizo
wako, na njaa na upanga — na ni kwa kupitia nani nitakayekufariji?
20 Wana wako wamezimia, ila tu hawa wawili; wanangoja kwenye njia zote; kama
ndume wa kichakani kwenye wavu, wamejaa hasira ya Bwana, kemeo la Mungu
wako.
21 Kwa hivyo sikiliza haya sasa, wewe uliyesumbuka, na kulewa, na sio kwa mvinyo:
22 Bwana wako asema hivi, Bwana na Mungu wako anatetea maslahi ya watu wake;
tazama, nimeondoa mkononi mwako kikombe cha kuogopesha, mabaki ya kikombe
cha hasira yangu; wewe hutakinywa tena.
23 Lakini Mimi nitakiweka mkononi mwa wale wanaokusumbua; wale ambao
wameiambia nafsi yako: Inama chini, ili tupite juu — na wewe umelaza mwili wako
chini na ukawa kama njia kwa wale waliopita.
24 Inuka, inuka, vaa nguvu zako, Ee Sayuni; vaa mavazi yako maridadi, Ee
Yerusalemu, mji mtakatifu; kwani tangu sasa wasiotahiriwa na walio wachafu
hawatakuingia.
25 Jitingishe kutoka mavumbini; inuka, kaa chini, Ee Yerusalemu; jifungue tokana
na vifungo vya shingo lako, Ee binti mateka wa Sayuni.

# 2 Nefi 9

1 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, nimesoma vitu hivi ili mfahamu kuhusu yale
maagano ya Bwana aliyoagana na nyumba yote ya Israeli—
2 Kwamba amezungumza kwa Wayahudi, kwa kinywa cha manabii wake
watakatifu, hata tangu mwanzo hadi chini, kizazi kwa kizazi, mpaka wakati ufike
watakaporejeshwa kwa lile kanisa la kweli na zizi la Mungu; wakati
watakapokusanywa nyumbani kwenye nchi zao za urithi, na wataimarishwa katika
nchi zao zote za ahadi.
3 Tazameni, ndugu zangu wapendwa, nawazungumzia vitu hivi ili kwamba
mshangilie, na muinue vichwa vyenu juu milele, kwa sababu ya baraka ambazo
Bwana Mungu atawateremshia watoto wenu.
4 Kwani najua kwamba wengi wenu, mmetafuta sana, kujua vitu vijavyo; kwa hivyo
najua kwamba mnajua kuwa miili yetu lazima izeeke na kufa; walakini, katika miili
yetu tutamuona Mungu.
5 Ndio, najua kwamba mnajua kwamba atajidhihirisha kimwili kwa wale walio
Yerusalemu, kule tulikotoka; kwani ni lazima iwe miongoni mwao; kwani ilimpasa
Muumba mkuu akubali kuwa chini ya mwanadamu katika mwili, na afe kwa
wanadamu wote, ili wanadamu wote wawe chini yake.
6 Kwani kifo kimewapata wanadamu wote, ili kutimiza mpango wa huruma wa
Muumba mkuu, inahitajika lazima pawe na nguvu ya ufufuo, na inahitajika lazima
ufufuo umfikie mwanadamu kwa sababu ya mwanguko; na mwanguko ulitokana na
kosa; na kwa sababu mwanadamu alianguka alitengwa tokana na uwepo wa Bwana.
7 Kwa hivyo, unahitajikana iwe upatanisho usio na kipimo—bila huu upatanisho
usio na kipimo huu uharibifu hauwezi kuvaa kutoharibika. Kwa hivyo, hukumu ya
kwanza iliyompata mwanadamu lazima ingekuwa kwa muda usio na mwisho. Na
kama ni hivyo, miili hii lazima ingelala chini kuoza na kurudi mavumbini ilipotoka,
bila kufufuka tena.
8 Ee hekima ya Mungu, huruma zake na neema! Kwani tazama, kama miili
haifufuki tena roho zetu lazima ziwe chini ya yule malaika aliyeanguka kutoka
uwepo wa Mungu wa Milele, na akawa ibilisi, bila kufufuka tena.
9 Na roho zetu lazima zingekuwa kama yeye, na tuwe mashetani, malaika kwa
ibilisi, kutengwa na uwepo wa Mungu wetu, na kuishi na baba wa uwongo, katika
huzuni, kama yeye mwenyewe; ndio, kwa kile kiumbe kilichodanganya wazazi wetu
wa kwanza, ambaye hujigeuza kuwa malaika wa nuru, na huvuruga watoto wa watu
kuwa na makundi maovu ya siri na ya mauaji na kila aina ya kazi za siri za giza.
10 Ee jinsi gani ilivyo kuu wema wa Mungu wetu, anayetutayarishia njia ya kuepuka
kunaswa na huyu mnyama mwovu; ndio, huyo mnyama, kifo na jahanamu, ambayo
naita kifo cha mwili, na pia kifo cha roho.
11 Na kwa sababu ya njia ya ukombozi wa Mungu wetu, Mtakatifu wa Israeli, hiki
kifo, ambacho nimetaja, ambacho ni cha muda, kitaachilia wafu wake; kifo
ambacho ni kaburi.
12 Na kifo hiki ambacho nimetaja, ambacho ni kifo cha kiroho, kitaachilia wafu
wake; kifo cha kiroho ambacho ni jahanamu; kwa hivyo, kifo na jahanamu lazima
ziachilie wafu wao, na jahanamu lazima iachilie roho zake zilizo utumwani, na
kaburi lazima liachilie miili yake iliyo utumwani, na miili na roho za wanadamu
itaunganishwa tena; na ni kwa nguvu za ufufuo za yule Mtakatifu wa Israeli.
13 Ee jinsi gani ulivyo mkuu mpango wa Mungu wetu! Kwani katika njia nyingine,

peponi ya Mungu lazima iachilie roho za walio haki, na kaburi iachilie miili ya walio
haki; na roho na mwili kuunganishwa tena, na wanadamu wote wawe wasioharibika,
na wasiokufa, na wao ni nafsi zinazoishi, wakiwa na ufahamu kamili kama sisi tulio
na miili, ila tu ufahamu wetu utakuwa kamili.
14 Kwa hivyo, tutakuwa na ufahamu kamili wa hatia zetu, na uchafu wetu, na uchi
wetu; na walio haki watakuwa na ufahamu kamili wa furaha yao, na utakatifu wao,
wakiwa wamevishwa usafi, ndio, hata kwa joho la utakatifu.
15 Na itakuwa kwamba baada ya wanadamu wote kupita mauti haya ya kwanza na
kupata uzima, jinsi vile wamekuwa wasiokufa, lazima watasimama mbele ya kiti cha
hukumu cha yule Mtakatifu wa Israeli; na kisha hukumu itafika, na kisha lazima
wahukumiwe kulingana na hukumu takatifu ya Mungu.
16 Na kwa hakika, kama Bwana anavyoishi, kwani Bwana Mungu amelizungumza,
na ni neno lake la milele, ambalo halikosi kutimizwa, kwamba wale walio haki bado
watakuwa haki, na wale walio waovu bado watakuwa waovu; kwa hivyo, wale ambao
ni waovu ni ibilisi na malaika wake; na watatupwa kwenye moto usio na mwisho,
waliotayarishiwa; na mateso yao ni kama ziwa la moto na kiberiti ambacho ndimi
zake zinapanda juu milele na daima bila mwisho.
17 Ee jinsi gani ilivyo kuu haki ya Mungu wetu! Kwani anatimiza maneno yake yote,
na yametoka kinywani mwake, na sheria yake lazima itimizwe.
18 Lakini, tazama, watakatifu, wale wateule wa yule Mtakatifu wa Israeli, wale
ambao wamemwamini yule Mtakatifu wa Israeli, wale ambao wamevumilia
misalaba ya ulimwengu, na kudharau aibu yake, watarithi ufalme wa Mungu, ambao
walitayarishiwa tangu mwanzo wa dunia, na shangwe yao itakuwa tele milele.
19 Ee jinsi gani ilivyo kuu rehema ya Mungu wetu, yule Mtakatifu wa Israeli! Kwani
huwakomboa watakatifu wake tokana na yule mnyama mwovu yaani ibilisi, na kifo,
na jahanamu, na lile ziwa la moto na kiberiti, ambalo ni mateso yasiyo na mwisho.
20 Ee jinsi gani ulivyo mkuu utakatifu wa Mungu wetu! Kwani anafahamu vitu
vyote, na hakuna jambo lolote asilolijua.
21 Na anakuja ulimwenguni ili awaokoe wanadamu wote kama watakubali sauti
yake; kwani tazama, anapokea maumivu ya wanadamu wote, ndio, maumivu ya kila
kiumbe kinachoishi, waume kwa wake, na watoto, ambao ni wa jamii ya Adamu.
22 Na anakubali haya ili ufufuo uwafikie wanadamu wote, ili wote wasimame mbele
yake katika siku ile kuu ya hukumu.
23 Na anawaamuru wanadamu wote kwamba lazima watubu, na wabatizwe katika
jina lake, wakiwa na imani kamili katika yule Mtakatifu wa Israeli, au kama sivyo
hawawezi kuokolewa katika ufalme wa Mungu.
24 Na kama hawatatubu na kuamini katika jina lake, na kubatizwa kwa jina lake, na
kuvumilia hadi mwisho, lazima wapate laana ya milele; kwani Bwana Mungu, yule
Mtakatifu wa Israeli, amezungumza.
25 Kwa hivyo, ametoa sheria; na ambapo hakuna sheria imetolewa hakuna adhabu;
na pasipo adhabu hakuna hukumu; na pasipo hukumu rehema za yule Mtakatifu wa
Israeli zinawadai, kwa sababu ya upatanisho; kwani wanakombolewa kwa nguvu
zake.
26 Kwani upatanisho unatimiza madai yake ya haki kwa wale ambao hawakupatiwa
sheria, kwamba wanakombolewa tokana na yule mnyama mwovu, kifo na
jahanamu, na yule ibilisi, na ziwa la moto na kiberiti, ambalo ni mateso bila mwisho;
na wanarejeshwa kwa yule Mungu aliyewapatia pumzi, ambaye ni yule Mtakatifu wa

Israeli.
27 Lakini ole kwa yule ambaye alipewa sheria, ndio, aliye na sheria zote za Mungu, kama sisi, na huzivunja, na yule anayepoteza siku za majaribio yake, kwani hali yake ni mbovu!
28 Ee ule mpango wa ujanja wa yule mwovu! Ee utupu, na ugoigoi, na upumbavu wa wanadamu! Wanapoelimika wanadhani kwamba wana hekima, na hawasikii mawaidha ya Mungu, kwani wanaiweka kando, wakifikiria kwamba wanajua wenyewe, kwa hivyo, hekima yao ni ujinga na haiwafaidi. Na wataangamia.
29 Lakini kuelimika ni vyema ikiwa watatii mawaidha ya Mungu.
30 Lakini ole kwa matajiri, ambao ni matajiri kwa vitu vya ulimwengu. Kwani kwa sababu wao ni matajiri wanachukia walio masikini, na wanawatesa wale wapole, na mioyo yao iko kwenye hazina yao; kwa hivyo, hazina yao ni mungu wao. Na tazama, hazina yao itaangamia nao pia.
31 Na ole kwa viziwi wale wasiosikia; kwani wataangamia.
32 Ole pia kwa wale walio vipofu wasioona; kwani nao pia wataangamia.
33 Ole kwa wale wasiotairiwa moyoni, kwani ufahamu wa maovu yao utawasonga katika siku ya mwisho.
34 Ole kwa aliye mdanganyifu, kwani atatupwa jahanamu.
35 Ole kwa muuaji anayeua akitaka, kwani atakufa.
36 Ole kwa wale wanaotenda ukahaba, kwani watatupwa jahanamu.
37 Ndio, ole kwa wale wanaoabudu masanamu, kwani ibilisi wa ibilisi wote huwafurahia.
38 Na, mwishowe, ole kwa wale wote wanaokufa katika dhambi zao; kwani watamrejea Mungu, na kuona uso wake, na kubaki katika dhambi zao.
39 Ee, ndugu zangu wapendwa, kumbukeni uovu wa kumkosea yule Mungu Mtakatifu, na pia uovu wa kukubali ushawishaji wa yule mwovu. Kumbukeni, kufikiria kimwili ni kifo, na kufikiria kiroho ni uzima wa milele.
40 Ee, ndugu zangu wapendwa, sikilizeni maneno yangu. Kumbukeni ukuu wa yule Mtakatifu wa Israeli. Msiseme kwamba nimezungumza vitu vigumu dhidi yenu; kwani mkifanya hivyo, mtaasi kinyume cha ukweli; kwani nimenena maneno ya Muumba wenu. Najua kwamba maneno ya kweli ni makali kwa uchafu wote; lakini walio haki hawayaogopi, kwani wanapenda ukweli na hawatingishwi.
41 Kisha, Ee ndugu zangu wapendwa, njooni kwa Bwana, yule Mtakatifu. Kumbuka kwamba mapito yake ni matakatifu. Tazama, njia ya mwanadamu ni nyembamba, lakini imenyooka mbele yake, na mlinzi wa mlango ni yule Mtakatifu wa Israeli; na haajiri mtumishi yeyote pale; na hakuna njia nyingine yoyote isipokuwa kwa mlango; kwani hawezi kudanganywa, kwani Bwana Mungu ndilo jina lake.
42 Na kwa yeyote anayebisha, kwake yeye atamfungulia; na kwa wenye hekima, na walioelimika, na wale walio matajiri, ambao wanajidai kwa sababu ya elimu yao, na hekima yao, na utajiri wao — ndio, hao ndio anaochukia; na wasipoacha vitu hivi, na wajichukue kama wajinga mbele ya Mungu, na kunyenyekea, hatawafungulia.
43 Lakini vitu vya wenye hekima na walio werevu vitafichwa kwao milele — ndio, furaha ile iliyotayarishiwa watakatifu.
44 Ee, ndugu zangu wapendwa, kumbukeni maneno yangu. Tazama, navua mavazi yangu, na kuzisukasuka mbele yenu; Naomba kwamba Mungu wa wokovu wangu anitazame na jicho lake linaloona kila mahali; kwa hivyo, mtajua katika siku ile ya

mwisho, wakati wanadamu wote watakapohukumiwa kulingana na kazi zao, kwamba Mungu wa Israeli alishuhudia kwamba nilijitoa mzigo wa maovu yenu kutoka nafsi yangu, na kwamba nasimama kwa usafi mbele yake, na kwamba damu yenu haiko juu yangu.

45 Ee, ndugu zangu wapendwa, acheni dhambi zenu; jifungueni minyororo ya yule atakayewafunga; njooni kwa yule Mungu aliye mwamba wa wokovu wenu.

46 Tayarisheni nafsi zenu kwa siku ile ya utukufu ambapo wale walio watakatifu watahudumiwa kwa haki, hata siku ile ya hukumu, kwamba msitetemeke kwa woga; na kwamba msikumbuke hatia yenu ya uovu katika ukamilifu, na mlazimishwe kulia: Takatifu, takatifu ni hukumu zako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi—lakini najua hatia yangu; nilivunja sheria yako, na makosa yangu ni yangu; na ibilisi amenipata, na kwamba mimi ni mawindo kwa huzuni yake mbovu.

47 Lakini tazameni, ndugu zangu, je, ni lazima niwafahamishe huu ukweli wa kutisha wa vitu hivi? Je, ningesumbua nafsi zenu kama mawazo yenu yangekuwa mema? Ningekuwa wazi kwenu kulingana na udhahiri wa kweli kama mngepata uhuru wa dhambi?

48 Tazama, kama mngekuwa watakatifu ningewazungumzia kuhusu utakatifu; lakini kwa vile nyinyi sio watakatifu, na mnanitegemea mimi kama mwalimu, lazima niwafunze kuhusu matokeo ya dhambi.

49 Tazama, nafsi yangu inachukia dhambi, na moyo wangu unafurahishwa na utakatifu; na nitalisifu jina takatifu la Mungu wangu.

50 Njooni, ndugu zangu, kila mmoja aliye na kiu, njooni kwenye maji; na yule asiye na pesa, njoo ununue na ule; ndio, njooni mnunue mvinyo na maziwa bila pesa na bei.

51 Kwa hivyo, msitumie pesa zenu kwa yale yasiyo na thamani, wala nguvu zenu kwa yale yasiyotosheleza. Mnisikilize kwa makini, na mkumbuke yale maneno ambayo nimezungumza; na mje kwa yule Mtakatifu wa Israeli, na mle yale yasiyoangamia, wala kuharibiwa, na mruhusu nafsi zenu zifurahie unono.

52 Tazameni, ndugu zangu wapendwa, kumbukeni maneno ya Mungu wenu; muombeni bila kukoma kwa mchana, na mshukuru jina lake takatifu kwa usiku. Acheni mioyo yenu ishangilie.

53 Na tazameni jinsi gani yalivyo makuu maagano ya Bwana, na jinsi gani ilivyo kuu ufadhili wake kwa watoto wa watu; na kwa sababu ya ukuu wake, na neema yake na rehema, ametuahidi kwamba uzao wetu hautaangamizwa kabisa, kimwili, lakini kwamba atawahifadhi; na katika vizazi vya baadaye watakuwa tawi takatifu kwa nyumba ya Israeli.

54 Na sasa, ndugu zangu, ningewazungumzia zaidi; lakini kesho nitawaelezea maneno yangu yaliyosalia. Amina.

## 2 Nefi 10

1 Na sasa mimi, Yakobo, nawazungumzia tena, ndugu zangu wapendwa, kuhusu tawi hili takatifu ambalo nimelitaja.

2 Kwani tazama, ahadi ambazo tumepokea ni ahadi kwetu kuhusu kimwili; kwa hivyo, kwa vile nimeonyeshwa kwamba watoto wetu wengi wataangamia kimwili kwa sababu ya kutoamini, walakini, Mungu atawarehemu wengi; na watoto wetu watarejeshwa, ili wapokee kile ambacho kitawapatia ufahamu wa kweli wa

Mkombozi wao.
3 Kwa hivyo, kama vile nilivyowaambia, lazima inahitajika kwamba
Kristo — kwani usiku uliopita malaika aliniambia kwamba hili litakuwa jina
lake — atakuja miongoni mwa Wayahudi, miongoni mwa wale ambao ni waovu
zaidi ulimwenguni; na watamsulubu — hivyo ndivyo ilimpasa Mungu wetu, na
hakuna taifa lingine duniani ambalo lingemsulubu Mungu wao.
4 Kwani miujiza mikuu ingetendwa miongoni mwa mataifa mengine wangetubu,
na wangejua kwamba yeye ni Mungu wao.
5 Lakini kwa sababu ya ukuhani wa uongo, walio Yerusalemu watamkazia shingo
zao, hata mpaka asulubiwe.
6 Kwa hivyo, kwa sababu ya uovu wao, maangamizo, njaa, tauni, na umwagaji wa
damu zitawapata; na wale ambao hawataangamizwa watatawanywa miongoni mwa
mataifa yote.
7 Lakini tazama, Bwana Mungu anasema hivi: Siku itakapofika watakaponiamini,
kwamba mimi ni Kristo, basi nimeagana na baba zao kwamba watarejeshwa kimwili,
duniani, kwenye nchi za urithi wao.
8 Na itakuwa kwamba watakusanywa kutoka mtawanyiko wao wa muda mrefu,
kutoka visiwa vya bahari, na kutoka sehemu nne za dunia; na mataifa ya Wayunani
yatakuwa makuu machoni mwangu, asema Mungu, kwa kuwapeleka katika nchi zao
za urithi.
9 Ndio, wafalme wa Wayunani watakuwa baba zao walezi, na malkia wao
watakuwa mama walezi; kwa hivyo, ahadi za Bwana ni kuu kwa Wayunani, kwani
ameizungumza, na nani anayeweza kubisha?
10 Lakini tazama, nchi hii, Mungu alisema, itakuwa nchi ya urithi wako, na
Wayunani watabarikiwa katika nchi hii.
11 Na nchi hii itakuwa nchi ya uhuru kwa Wayunani, na hakutakuwa na wafalme
katika nchi hii, ambao watainuka juu ya Wayunani.
12 Na nitaimarisha nchi hii dhidi ya nchi zingine zote.
13 Na yule anayepigana na Sayuni ataangamia, asema Mungu.
14 Kwani yule anayeniinulia mfalme ataangamia, kwani mimi, Bwana, mfalme wa
mbingu, nitakuwa mfalme wao, na nitakuwa nuru kwao milele, kwa wale wanaosikia
maneno yangu.
15 Kwa hivyo, kwa sababu hii, ili maagano yangu niliyoagana na watoto wa watu
yaweze kutimizwa, yale nitakayowatendea kimwili, lazima niangamize kazi za siri za
giza, na za mauaji, na za machukizo.
16 Kwa hivyo, yule anayepigana dhidi ya Sayuni, Myahudi na Myunani, mateka na
walio huru, waume kwa wake, wataangamia; kwani wao ndio makahaba wa dunia
yote; kwani wale wasio wangu wako dhidi yangu, asema Mungu.
17 Kwani nitatimiza ahadi zangu ambazo niliagana na wanadamu, kwamba
nitawatendea kimwili —
18 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, Mungu wetu asema hivi: Nitasumbua uzao
wenu kwa mkono wa Wayunani; walakini, nitalainisha mioyo ya Wayunani,
kwamba watakuwa kama baba kwao; kwa hivyo, Wayunani watabarikiwa na
kuhesabiwa miongoni mwa nyumba ya Israeli.
19 Kwa hivyo, nitaiwekea wakfu uzao wako hii nchi, na wale watakaohesabiwa
miongoni mwa uzao wako, milele, kuwa nchi yao ya urithi; kwani ni nchi bora,
Mungu ananiambia, zaidi ya nchi zingine zote, kwa hivyo nitawataka wanadamu

wote wanaoishi juu yake kwamba wataniabudu, asema Mungu.
20 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, kwa vile Mungu wetu wa huruma ametupatia
ufahamu mkuu hivyo kuhusu vitu hivi, hebu tumkumbuke, na kuacha dhambi zetu,
na tusiinamishe vichwa vyetu, kwani hatujatupwa; walakini, tumefukuzwa kutoka
nchi yetu ya urithi; lakini tumeongozwa hadi nchi ile iliyo bora zaidi, kwani Bwana
amesababisha bahari kuwa njia yetu, na tuko kwenye kisiwa cha bahari.
21 Lakini kubwa ni ahadi za Bwana kwa wale walio kwenye visiwa vya bahari; kwa
hivyo kama vile inavyosema visiwa, lazima pawe na zaidi ya haya, na pia wale
wanaoishi humo ni ndugu zetu.
22 Kwani tazama, Bwana Mungu ametoa kutoka nyumba ya Israeli mara kwa mara,
kulingana na nia na furaha yake. Na sasa tazama, Bwana hukumbuka wale wote
waliotengwa, kwa hivyo anatukumbuka pia sisi.
23 Kwa hivyo, changamsheni mioyo yenu, na kumbukeni kwamba mko huru
kujitendea — kuchagua njia ya kifo kisicho na mwisho au njia ya uzima wa milele.
24 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, jipatanisheni na nia ya Mungu, na sio kwa
nia ya ibilisi na mwili; na kumbukeni, baada ya kupatanishwa na Mungu, kwamba ni
kwa na kupitia neema ya Mungu pekee mnaokolewa.
25 Kwa hivyo, Mungu awafufue kutoka kwa wafu kwa nguvu za ufufuo, na pia
kutoka kifo kisicho na mwisho kwa nguvu za upatanisho, kwamba mpokelewe
katika ufalme wa milele wa Mungu, kwamba mmsifu kwa neema takatifu. Amina.

## 2 Nefi 11

1 Na sasa, Yakobo aliambia watu wangu vitu vingi zaidi katika ule wakati; walakini ni
hivi vitu pekee nimesababisha viandikwe, kwani vitu nilivyoandika vimenitosha.
2 Na sasa mimi, Nefi, naandika maneno zaidi ya Isaya, kwani nafsi yangu
inafurahia maneno yake. Kwani nitalinganisha maneno yake kwa watu wangu, na
nitayatuma kwa watoto wangu wote, kwani kweli alimwona Mkombozi wangu, hata
vile nilivyomwona.
3 Na kaka yangu, Yakobo, pia amemwona vile nilivyomwona; kwa hivyo,
nitayatuma maneno yao kwa watoto wangu kuwathibitishia wao kwamba maneno
yangu ni ya kweli. Kwa hivyo, Mungu amesema, kwa maneno ya watatu,
nitaimarisha neno langu. Walakini, Mungu huwatuma mashahidi wengi, na
anathibitisha maneno yake yote.
4 Tazama, nafsi yangu inafurahia kuwathibitishia watu wangu ukweli wa kuja kwa
Kristo; kwani, ni kwa lengo hili kwamba sheria ya Musa imetolewa; na vitu vyote
vilivyopewa na Mungu tangu mwanzo wa dunia, kwa mwanadamu, ni kielelezo
chake.
5 Na pia moyo wangu unafurahia maagano ya Bwana aliyoagana na baba zetu;
ndio, moyo wangu unafurahia neema yake, na katika haki yake, na nguvu, na
rehema zilizo katika mpango mkuu wa milele wa ukombozi kutoka mauti.
6 Na moyo wangu unafurahia kuwathibitishia watu wangu kwamba ijapokuwa
Kristo aje lazima wanadamu wote waangamie.
7 Kwani kama hakuna Kristo hakuna Mungu; na kama hakuna Mungu basi nasi
hatupo, kwani hakungekuwa na uumbaji. Lakini kuna Mungu, na yeye ni Kristo, na
atakuja katika utimilifu wa wakati wake mwenyewe.
8 Na sasa naandika baadhi ya maneno ya Isaya, ili wowote wa watu wangu

watakaoona maneno haya wangeinua mioyo yao na kufurahia kwa wanadamu wote. Sasa haya ndiyo maneno, na mnaweza kuyalinganisha nanyi na kwa wanadamu wote.

## 2 Nefi 12

1 Neno ambalo Isaya, mwana wa Amozi, aliona kuhusu Yuda na Yerusalemu:

2 Na itakuwa kwamba katika siku za mwisho, wakati mlima wa nyumba ya Bwana itajengwa kileleni mwa milima, na itainuliwa juu ya vilima, na mataifa yote yataitiririkia.

3 Na watu wengi wataenda na kusema, Njooni ninyi, na hebu twende juu ya mlima wa Bwana, kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo; na atatufunza njia zake, na tutatembea katika mapito yake; kwani kutoka Sayuni itatokea sheria, na neno la Bwana kutoka Yerusalemu.

4 Na atahukumu miongoni mwa mataifa, na kukemea watu wengi: na watafua panga zao kuwa majembe, na mikuki yao itakuwa visu vya kupogoa—taifa halitainua upanga kwa taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena.

5 Ee nyumba ya Yakobo, njooni na tutembee katika nuru ya Bwana; ndio, njooni, kwani nyote mmepotea, kila moja katika njia zake mbovu.

6 Kwa hivyo, Ee Bwana, wewe umewaacha watu wako, nyumba ya Yakobo, kwa sababu wamejaa na mila za mashariki, na wanatii wachawi kama Wafilisti, na wanajifurahisha na watoto wa wageni.

7 Nchi yao pia imejaa fedha na dhahabu, wala hakuna mwisho wa hazina zao; nchi yao pia imejaa farasi, wala hakuna mwisho wa magari yao makubwa.

8 Nchi yao pia imejaa sanamu; wanaabudu kazi ya mikono yao yenyewe, yale ambayo vidole vyao vyenyewe vimeunda.

9 Na mtu wa kawaida hainami chini, na yule mtu aliye jasiri hanyenyekei, kwa hivyo, usimsamehe.

10 Ee nyinyi mlio waovu, ingieni kwenye mwamba, na mjifiche wenyewe kwenye mavumbi, kwani woga wa Bwana na utukufu wa nguvu zake utawachapa.

11 Na itakuwa kwamba kiburi cha mwanadamu kitanyenyekeshwa, na maringo ya wanadamu yatashushwa, na Bwana pekee ndiye atainuliwa katika siku ile.

12 Kwani siku ya Bwana wa Majeshi hivi punde itatukia kwa mataifa yote, ndio, katika kila mmoja; ndio, kwa wale walio na kiburi na maringo, na kwa kila mmoja aliyejiinua, na atashushwa chini.

13 Ndio, na siku ya Bwana itateremkia mierezi yote ya Lebanoni, kwani iko juu na kuinuliwa; na juu ya mialoni yote ya Bashani;

14 Na juu ya milima yote mirefu, na juu ya vilima vyote, na juu ya mataifa yote yaliyoinuliwa, na juu ya kila watu;

15 Na juu ya kila mnara mrefu, na juu ya kila ukuta uliozungushwa;

16 Na juu ya meli zote za bahari, na juu ya meli zote za Tarshishi, na juu ya picha zote nzuri.

17 Na kiburi cha mwanadamu kitashushwa, na maringo ya wanadamu kuteremshwa; na Bwana pekee ndiye atayeinuliwa katika siku ile.

18 Na ataangamiza sanamu kabisa.

19 Na zitaingia katika mashimo ya miamba, na mapango ya dunia, kwani woga wa Bwana utawafikia na utukufu wa fahari yake utawapiga, atakapoinuka kusukasuka ulimwengu vikali.

20 Katika siku ile mwanadamu atatupa sanamu zake za fedha, na sanamu zake za
dhahabu, ambazo alijiundia mwenyewe kwa kuabudu, kwa fuko na kwa popo;
21 Kuingia katika mianya ya miamba, na vilele vya miamba iliyopasuka, kwani woga
wa Bwana utawajia na fahari ya utukufu wake utawachapa, atakapoinuka
kusukasuka ulimwengu vikali.
22 Acha mwanadamu, ambaye hupumua katika pua zake; kwani nini anacho?

## 2 Nefi 13

1 Kwani tazama, Bwana, Bwana wa Majeshi, huondoa kutoka Yerusalemu, na Yuda,
kijiti na bakora, bakora yote ya mkate, na kijiti chote cha maji—
2 Mwanadamu aliye shujaa, na mwanadamu aliye wa vita, mwamuzi, na nabii, na
aliye na hekima, na mzee;
3 Kapteni wa wanajeshi hamsini, na yule anayeheshimika, na mshauri, na mganga
mwerevu, na mzungumzaji shujaa.
4 Na nitawapatia watoto kuwa wafalme wao, na watoto wachanga watawatawala.
5 Na watu watadhulumiwa, kila mmoja na mwingine, na kila mmoja na jirani yake;
watoto watajivunia wazee, na mshenzi kwa anayeheshimika.
6 Wakati mtu atamkumbatia kaka yake wa nyumba ya baba yake, na kusema:
Wewe unayo mavazi, kuwa kiongozi wetu, na usikubali haya maangamizo kushukia
kwa mkono wako—
7 Katika siku ile ataapa, akisema: Mimi sitakuwa mponyaji; kwani nyumbani
mwangu hamna mkate wala mavazi; msinifanye kiongozi wa watu.
8 Kwani Yerusalemu imeangamizwa, na Yuda imeanguka, kwa sababu ndimi zao
na matendo yao yamekuwa kinyume cha Bwana, kwa kuchokoza utukufu wa macho
yake.
9 Umbo la nyuso zao linashuhudia dhidi yao, na kutangaza kwamba dhambi yao ni
kama ya Sodoma, na hawawezi kuificha. Ole kwa roho zao, kwani wamejilipiza kwa
uovu!
10 Waambieni walio watakatifu kwamba wako salama; kwani watakula matunda ya
matendo yao.
11 Ole kwa wale walio waovu, kwani wataangamia; kwani malipo ya mikono yao
yatakuwa juu yao!
12 Na watu wangu, wanadhulumiwa na watoto, na kutawaliwa na wanawake. Ee
watu wangu, wale wanaowaongoza wanawasababisha kukosa na kuangamiza njia ya
mapito yenu.
13 Bwana husimama kuwatetea, na husimama kuhukumu watu.
14 Bwana atawahukumu wazee wa watu wake na wana wa wafalme wao; kwani
mmekula mzabibu na mali ya maskini nyumbani mwenu.
15 Mnamaanisha nini? Mnawapiga watu wangu kuwa vipande, na kusaga nyuso za
maskini, asema Bwana Mungu wa Majeshi.
16 Zaidi ya hayo, Bwana asema: Kwa sababu mabinti za Sayuni wanaringa, na
kutembea na shingo mbele na macho ya tamaa, na mwendo wa kiburi, na kuliza
sauti ya njuga kwa miguu yao—
17 Kwa hivyo Bwana atachapa kipaji cha mabinti za Sayuni, kwa kigaga, na Bwana
atagundua sehemu zao za siri.
18 Na katika siku ile Bwana ataondoa urembo wa pambo zao, na kofia zao

zilizoshonwa, na ushanga na duara ya mviringo kama mwezi.
19 Mikufu na bangili, na buibui za vito;
20 Kofia, na mavazi ya miguu, na vitambaa vya kichwa, na marashi, na vipuli vya
masikio;
21 Na pete, na vipuli vya pua;
22 Na mavazi mengi mazuri, na kanzu, na shali, na vibeti;
23 Na vioo, na kitani dhaifu, na shela, na setiri.
24 Na itakuwa kwamba, badala ya kunukia utamu kutakuwa na uvundo; na badala
ya mshipi, kiraka; na badala ya nywele, upara; na badala ya nguo nzuri, mshipi wa
gunia; kuchomeka badala ya urembo.
25 Wanaume wako wataanguka kwa upanga na mashujaa wako kwa vita.
26 Na milango yake italia na kuomboleza; na atakuwa na ukiwa, na atakaa ardhini.

## 2 Nefi 14

1 Na katika siku ile, wanawake saba watamshika mwanaume mmoja, wakisema:
Tutakula mkate wetu wenyewe, na kuvaa mavazi yetu wenyewe; turuhusu tu tuitwe
kwa jina lako ili tuondolewe aibu yetu.
2 Katika siku ile tawi la Bwana litakuwa la urembo na tukufu; matunda ya udongo
yatakuwa mema na ya kupendeza kwa wale waliokimbia kutoka Israeli.
3 Na itakuwa kwamba, wale waliobaki Sayuni na kubaki Yerusalemu wataitwa
watakatifu, kila mmoja aliyeandikwa miongoni mwa wale walio hai Yerusalemu—
4 Wakati Bwana atakapokuwa ameuosha uchafu wa mabinti za Sayuni, na
kuisafisha damu ya Yerusalemu kutoka kati yake kwa roho ya hukumu na kwa roho
ya kuchoma.
5 Na Bwana ataumba juu ya kila makao ya mlima wa Sayuni, na juu ya kila
mkusanyiko wake, wingu na moshi mchana na mng'aro wa miale ya moto usiku;
kwani juu ya utukufu wote wa Sayuni kutakuwa na ulinzi.
6 Na kutakuwa na hekalu la hema kwa kivuli mchana kwa sababu ya joto, na
mahali pa kukimbilia, na kujificha nyakati za dhoruba na mvua.

## 2 Nefi 15

1 Na kisha nitamuimbia mpenzi wangu wimbo wa mpenzi wangu, kuhusu shamba
lake la mizabibu. Mpenzi wangu analo shamba la mizabibu katika kilima kinono
sana.
2 Na alilizingira kwa ua, na akayatoa mawe yake, na akapanda mizabibu iliyo bora,
na akajenga mnara katikati yake, na akajenga pia kishinikizo ndani yake; na
akaonelea kwamba litazaa zabibu, nalo likazaa zabibu-mwitu.
3 Na sasa, Ee wakazi wa Yerusalemu, nanyi watu wa Yuda, nawasihi, amueni, kati
yangu na shamba langu la mizabibu.
4 Ni nini kingefanywa zaidi katika shamba langu la mizabibu ambacho sijafanya
ndani yake? Kwa hivyo, nilipotumaini kwamba itazaa zabibu ikazaa zabibu-mwitu.
5 Na sasa basi; nitawaambia nitakachotenda kwenye shamba langu la
mizabibu—nitaondoa ua hili, nalo litaliwa; na nitabomoa ukuta wake, nao
utakanyagwa;

6 Na nitaliharibu; halitapogolewa wala kulimwa; lakini litamea mbigili na miiba;
mimi nitaamuru pia mawingu kwamba yasinyeshe mvua juu yake.
7 Kwani shamba la mizabibu la Bwana wa Majeshi ni nyumba ya Israeli, na watu wa
Yuda ndio mmea wake wa kupendeza; na alitafuta hukumu, na tazama, dhuluma;
kwa haki, lakini tazama, kilio.
8 Ole kwa wale wanaoungana nyumba kwa nyumba, mpaka pasiwe na mahali,
kwamba wawekwe peke yao katikati ya dunia!
9 Katika masikio yangu, alisema Bwana wa Majeshi, hakika nyumba nyingi
zitakuwa zenye ukiwa, na miji mikuu na mizuri itakuwa haina mtu.
10 Ndio, ekari kumi za shamba la mizabibu zitazaa bathi moja, na mbegu ya homeri
itatoa efa tu.
11 Ole wao waamkao alfajiri, ili watafute pombe kali, wanaoendelea hadi usiku wa
manane, mpaka mvinyo unawachoma kama moto!
12 Na kinubi, na zeze, matari, na filimbi, na mvinyo ziko katika karamu zao; lakini
hawashughuliki na kazi ya Bwana, wala kuyafikiri matendo ya kazi yake.
13 Kwa hivyo, watu wangu wamepelekwa utumwani, kwa sababu hawana ufahamu;
na watu wao wanaoheshimika wana njaa, na wengi wao wamekauka kwa kiu.
14 Kwa hivyo, jahanamu imejipanua, na kufungua kinywa chake bila kipimo; na
utukufu wao, na wingi wao, na fahari yao, na yule anayefurahia, atateremka ndani
yake.
15 Na mtu wa kawaida atashushwa chini, na yule mtu shujaa atanyenyekeshwa, na
macho ya aliye na kiburi yatanyenyekeshwa.
16 Lakini Bwana wa Majeshi atainuliwa katika hukumu, na Mungu aliye mtakatifu
atatakaswa katika haki.
17 Kisha wanakondoo watakula kama kawaida yao, na mahali palipoharibiwa pa
wale wanono pataliwa na wageni.
18 Ole kwa wale wavutao uovu kwa kamba za ubatili, na dhambi kama kwa kamba
ya gari;
19 Wanaosema: Hebu afanye haraka, aihimize kazi yake, ili tuione; na hebu
mawaidha ya yule Mtakatifu wa Israeli yaharakishwe na kutukia, ili tuyafahamu.
20 Ole kwa wale wanaoita uovu wema, na wema uovu, watiao giza badala ya nuru,
na nuru badala ya giza, watiao ukali badala ya utamu, na utamu badala ya ukali!
21 Ole kwa wao walio wenye hekima katika macho yao wenyewe, na wenye busara
katika fikira zao wenyewe!
22 Ole kwa wale hodari wa kunywa mvinyo, na wanaume walio shujaa katika
kuchanganya pombe;
23 Wanaompatia mwovu haki kwa kupokea zawadi, na kumwondolea haki yule aliye
mtakatifu!
24 Kwa hivyo, kama vile moto uchomavyo mabua makavu, na mwali wa moto
humaliza nyasi kavu, mzizi wao utaoza, na maua yao yatapeperushwa kama vumbi;
kwa sababu wameitupa sheria ya Bwana wa Majeshi, na kudharau neno la yule
Mtakatifu wa Israeli.
25 Kwa hivyo, hasira ya Bwana imewawakia watu wake, na amewanyoshea mkono
wake dhidi yao, na kuwachapa; na vilima vilitetemeka, na mizoga yao ilipasuliwa
katikati ya njia. Lakini bado hasira yake haijakoma, bado amenyosha mkono wake.
26 Na atayainulia mataifa kutoka mbali bendera, na atawapigia miunzi tokea
mwisho wa dunia; na tazama, watakuja mbio upesi sana; hakuna yeyote miongoni

mwao atakayechoka wala kujikwaa.
27 Hakuna yeyote atakayesinzia wala kulala; wala mshipi wa viuno vyao kulegea, wala kamba za viatu vyao kukatika;
28 Mishale yao itakuwa mikali, na pinde zao zote kupindika, na kwato za farasi zao zitahesabika kama gumegume, na gurudumu zao kama kimbunga, na ngurumo zao kama simba.
29 Watanguruma kama wana-simba; ndio, watanguruma, na kukamata mawindo, na kuyachukua kwa usalama, na hakuna yeyote atakayeokoa.
30 Na siku ile watawangurumia kama ngurumo ya bahari; na kama watatazama nchini, tazama, giza na huzuni, na nuru itatiwa giza katika mbingu zake.

## 2 Nefi 16

1 Katika mwaka ule mfalme Uzia alifariki, nilimwona Bwana pia akikalia kiti cha enzi, kilicho juu na kuinuliwa, na pindo za vazi lake zilijaza hekalu.
2 Na juu yake walisimama maserafi; kila mmoja alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka.
3 Na mmoja alimwitia mwingine, na akasema: Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana wa Majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake.
4 Na vizingiti vya mlango vilitetemeka kwa sauti ya yule aliyelia, na nyumba ilijaa moshi.
5 Kisha nikasema: Ole wangu! kwani nitaangamizwa; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu; na ninaishi miongoni mwa watu wenye midomo michafu; kwani macho yangu yamemwona Mfalme, Bwana wa Majeshi.
6 Kisha mmoja wa wale maserafi aliruka na akanikaribia, akiwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitoa kwenye madhabahu kwa makoleo;
7 Na akaliweka kwa kinywa changu, na kusema: Tazama, hili limegusa midomo yako; na uovu wako umeondolewa, na dhambi zako kuoshwa.
8 Pia nilisikia sauti ya Bwana, ikisema: Nitamtuma nani, na ni nani atakayeenda kwa niaba yetu? Kisha nikasema: Niko hapa; nitume mimi.
9 Na akasema: Enenda na uwambie watu hawa—Kwa kweli mlisikiliza, lakini hamkufahamu, mliona, lakini hamkuelewa.
10 Kinaisha moyo wa watu hawa uwe mgumu, na fanya masikio yao yawe mazito, na funga macho yao—wasije wakaona kwa macho yao, na kusikia kwa masikio yao, na kufahamu kwa moyo wao, na waongoke na kuponywa.
11 Kisha nikasema: Bwana, hadi lini? Na akasema: Hadi miji hii itakapokuwa na ukiwa bila mkazi, na nyumba bila wanadamu, na nchi itakapokuwa ganjo;
12 Na Bwana amewahamisha watu mbali, kwani kutakuwa na uhamisho mkuu miongoni mwa nchi.
13 Lakini itasalia sehemu ya kumi, na watarejea, na kuliwa, kama mvinje, na kama mwaloni ambao nguvu zake ziko ndani yake wakati majani yanaanguka; kwa hivyo mbegu takatifu itakuwa nguvu yake.

# 2 Nefi 17

1 Na ikawa katika siku za Ahazi mwana wa Yothamu, mwana wa Uzia, mfalme wa
Yuda, kwamba Resini, mfalme wa Shamu, na Peka mwana wa Remalia, mfalme wa
Israeli, walienda kushambulia Yerusalemu, lakini hawakuiweza.
2 Na nyumba ya Daudi, ikaambiwa: Shamu imeungana na Efraimu. Na moyo
wake ukatetemeka, na moyo wa watu wake, jinsi vile miti ya kichaka hupeperushwa
na upepo.
3 Kisha Bwana akamwambia Isaya: Nenda sasa ukamlaki Ahazi, wewe na mwana
wako Shear-yashubu, huko mwisho wa mfereji wa dimbwi la juu katika njia kuu ya
uwanja wa dobi;
4 Na umwambie: Sikiliza, na utulie; usiogope, wala usifadhaike moyoni kwa
sababu ya hii mikia miwili ya mwenge itokayo moshi, kwa sababu ya hasira kali ya
Resini na Shamu, na ya mwana wa Remalia.
5 Kwa sababu Shamu, Efraimu, na mwana wa Remalia, wamekusudia maovu juu
yako, wakisema:
6 Hebu twende dhidi ya Yuda na kuichokoza, na tuigawanye kati yetu, na tuweke
mfalme kati yake, ndio, mwana wa Tabeeli.
7 Bwana Mungu asema hivi: Haitasimama, wala kutimika.
8 Kwani kichwa cha Shamu ni Dameski, na kichwa cha Dameski, Resini; na katika
muda wa miaka sitini na tano Efraimu itaangamizwa isiwe tena kikundi cha watu.
9 Na kichwa cha Efraimu ni Samaria, na kichwa cha Samaria ni mwana wa
Remalia. Kama hamtaamini kwa hakika hamtaimarishwa.
10 Tena, Bwana akazungumza zaidi na Ahazi, akamwambia:
11 Itisha ishara kutoka kwa Bwana Mungu wako; iwe chini kwenye shimo, au juu
kwenye mawingu.
12 Lakini Ahazi akasema: Sitaitisha, wala sitamjaribu Bwana.
13 Na akasema: Sikilizeni sasa, Enyi nyumba ya Daudi; Je, ni kitu kidogo kwenu
kuwachosha wanadamu, hata mkataka kumchosha Mungu wangu pia?
14 Kwa hivyo, Bwana mwenyewe atakupatia ishara — Tazama, Bikira atapata
mimba, na atazaa mwanamume, na atamwita kwa jina Imanueli.
15 Atakula siagi na asali, ili ajue kukataa maovu na kuchagua mema.
16 Kwani kabla huyo mtoto hajajua kukataa maovu na kuchagua mema, nchi ile
ambayo unaichukia itakataliwa na wafalme wake wawili.
17 Bwana atakuteremshia, na juu ya watu wako, na juu ya nyumba ya baba yako,
nyakati ambazo hazijawahi kuoneka tangu siku ile Efraimu alipoondoka kutoka
Yuda, mfalme wa Ashuru.
18 Na itakuwa kwamba katika siku ile Bwana ataipigia miunzi nzi aliye sehemu za
mbali za Misri, na kwa nyuki aliye katika nchi ya Ashuru.
19 Na watakuja, na watapumzikia wote katika mabonde yaliyo na ukiwa, na katika
mashimo ya miamba, na kwenye miiba yote, na juu ya vichaka vyote.
20 Na siku ile ile Bwana atanyoa kwa wembe ulioajiriwa, na hao ng'ambo ya mto, na
mfalme wa Ashuru, kichwa, na malaika ya miguu; na pia itamaliza ndevu.
21 Na itakuwa kwamba katika siku ile, mtu atalisha ng'ombe mmoja na kondoo
wawili;
22 Na itakuwa kwamba, kwa wingi wa maziwa watakayotoa atakula siagi; kwani kila
mmoja aliyesalia katika nchi ile atakula siagi na asali.
23 Na itakuwa kwamba katika siku ile, kila mahali patakuwa, ambapo palikuwa

mizabibu elfu inayo gharama fedha elfu, ambapo patakuwa na mbigili na miiba.
24 Na watu wataenda huko na mishale na pinde, kwa sababu nchi yote itakuwa
mbigili na miiba.
25 Na vilima vyote vitakavyolimwa kwa jembe, hapatafika huko woga wa mbigili na
miiba; lakini hapo patakuwa mahali pa kuelekeza ng'ombe, na mahali pa
kukanyagwa na kondoo.

## 2 Nefi 18

1 Tena, neno la Bwana liliniambia: Chukua hati ndefu, na uandike juu yake kwa
kalamu ya mwanadamu, kuhusu Maher-shalal-hash-bazi.
2 Na nilichukua mashahidi waaminifu ili waandike, Uria yule kuhani, na Zekaria
mwana wa Yeberekia.
3 Na nilimwendea huyo nabii wa kike; na akapata mimba na akazaa mwana wa
kiume. Kisha Bwana akaniambia: Muite jina lake, Maher-shalal-hash-bazi.
4 Kwani tazama, kabla ya huyo mtoto hajajua kulia, baba yangu, na mama yangu,
utajiri wa Dameski na mateka ya Samaria yatachukuliwa na mfalme wa Ashuru.
5 Bwana alinizungumzia tena, akisema:
6 Kwa vile watu hawa wameyakataa maji ya Shiloa yapitayo polepole, na
wanafurahia Resini na mwana wa Remalia;
7 Kwa hivyo sasa, tazama, Bwana ataleta maji ya huo mto juu yao, yenye nguvu, na
mengi, hata mfalme wa Ashuru na utukufu wake wote; atakuja na kupita juu ya
mifereji yake yote, na kingo zake zote.
8 Na atapitia Yuda; atafurika na kuwa zaidi, atafika hata shingoni; na
atakaponyosha mabawa yake yatajaa upana wa nchi, Ee Imanueli.
9 Jiunganishe, Ee nyinyi watu, na mtavunjwa vipande vipande; na sikiliza nyinyi
nyote mtokao nchi za mbali; jiwekeni tayari na silaha, na mtavunjwa vipande
vipande; jiwekeni tayari na silaha, na mtavunjwa vipande vipande.
10 Fanyeni shauri pamoja, na hamtafanikiwa; nena neno, na halitatimia; kwani
Mungu yu pamoja nasi.
11 Kwani Bwana alinizungumzia hivyo kwa kunionya vikali, na akanishauri kuwa
nisitembee katika njia za watu hawa, akisema:
12 Msiseme, Muungano, kwa wale wote ambao hawa watu watasema, Muungano;
wala msiogope woga wao, wala kuogopa.
13 Mtakaseni Bwana wa Majeshi mwenyewe, na mkubali awe hofu yenu, na awe
tisho lenu.
14 Na atakuwa kimbilio; lakini jiwe la kujikwaa, na mwamba wa kuchukiza kwa
nyumba zote mbili za Israeli, na mtego na tanzi kwa wakazi wa Yerusalemu.
15 Na wengi miongoni mwao watajikwaa na kuanguka, na kuvunjwa, na kutegwa,
na kukamatwa.
16 Ufunge huo ushuhuda, na ufunge sheria miongoni mwa wanafunzi wangu.
17 Na nitamngojea Bwana, ambaye huficha uso wake kutoka kwa nyumba ya
Yakobo, na nitamtafuta.
18 Tazama, mimi na watoto ambao Bwana amenipatia ni kwa ishara na maajabu
katika Israeli kutoka kwa Bwana wa Majeshi, yule anayekaa katika Mlima Sayuni.
19 Na watakapokuambia: Tafuta ushauri kwa watu wenye pepo wa utambuzi, na
kwa wachawi wanaochungulia na kunong'ona — je, haiwapasi watu kutafuta ushauri

kutoka kwa Mungu ili wanaoishi wasikie kutoka kwa wafu?
20 Kwa sheria na kwa ushuhuda; na wao wasiponena kulingana na neno hili, ni kwa
sababu hakuna nuru ndani yao.
21 Nao wao watapita katikati yake wamedhikika na wakiwa na njaa; na itakuwa
kwamba watakapopata njaa, watajikasirisha wenyewe, na kumlaani mfalme wao na
Mungu wao na kutazama juu.
22 Na watatazama ardhi na kutazama shida, na giza, kufa moyo, na wataingizwa
gizani.

## 2 Nefi 19

1 Walakini, giza halitakuwa kubwa kama ilipokuwa katika dhiki yake
aliposhambuliwa, wakati hapo mwanzoni alitesa kidogo nchi ya Zabuloni, na nchi
ya Naftali, na baadaye kwa uzito akapitia kwa njia ya Bahari ya Shamu ng'ambo ya
Yordani katika Galilaya ya mataifa.
2 Watu wale waliotembea gizani wameona nuru kuu; wale wanaoishi katika nchi
ya kivuli cha kifo, wameangaziwa na nuru.
3 Umeliongeza taifa, na kuzidisha shangwe — wanajaa shangwe mbele yako
kulingana na shangwe ya mavuno, na kama vile watu wanavyofurahia
wanapogawana nyara.
4 Kwani umevunja nira ya mzigo wake, na gogo la bega lake, fimbo ya yule
anayemdhulumu.
5 Kwani kila vita vya askari shujaa huunganishwa na makelele, na mavazi
yaliyovingirishwa kwenye damu; lakini hii itakuwa ni ya kuchomwa na kuwa makaa
ya moto.
6 Kwani kwetu sisi mtoto amezaliwa, kwetu tumepewa mwana; na serikali itakuwa
kwenye bega lake; nalo jina lake litaitwa, Ajabu, Mshauri, Mwenyezi Mungu, Baba
asiye na mwisho, Mwana Mfalme wa Amani.
7 Na hakuna mwisho wa upanuzi wa serikali na amani, katika kiti cha enzi cha
Daudi, na juu ya utaratibu wa ufalme wake, na kuiimarisha kwa hukumu na kwa
haki tangu sasa, na hata milele. Bidii ya Bwana wa Majeshi itatenda haya.
8 Bwana alimtumia Yakobo neno lake na limemulikia Israeli.
9 Na watu wote watajua, hata Efraimu na wakazi wa Samaria, wanaosema kwa
kiburi na ugumu wa moyo:
10 Matofali yameanguka chini, lakini sisi tutajenga kwa mawe yaliyochongwa;
mikuyu imekatwa, lakini sisi tutaibadilisha iwe mierezi.
11 Kwa hivyo Bwana atawainua maadui wa Resini dhidi yake, na kuwaunganisha
maadui wake pamoja;
12 Waashuri mbele yao na Wafilisti nyuma yao; na watamla Israeli kwa kinywa
kilicho wazi. Lakini hata baada ya haya hasira yake haitapunguka, lakini bado
amenyoosha mkono wake.
13 Kwani watu hawatamrejea aliyewapiga, wala kumtafuta Bwana wa Majeshi.
14 Kwa hivyo Bwana atakata kutoka Israeli kichwa na mkia, tawi na tete katika siku
moja.
15 Mzee, ndiye kichwa; na nabii anayefunza uwongo, ndiye mkia.
16 Kwani viongozi wa watu hawa wanawasabisha wakose; na wale wanaoongozwa
nao wanaangamia.

17 Kwa hivyo Bwana hatakuwa na shangwe katika vijana wao, wala hatawahurumia yatima wao na wajane wao; kwani kila mmoja wao ni mnafiki na mwovu, na kila mdomo unanena upumbavu. Kwa haya yote hasira yake haitapungua, lakini bado amenyoosha mkono wake.

18 Kwani uovu huteketea kama moto; itaila mibigili na miiba, na itawasha vichaka vya mwitu, na yatapaa juu kama kuinuka kwa moshi.

19 Kwa kupitia ghadhabu ya Bwana wa Majeshi nchi inatiwa giza, na watu hao watakuwa kama makaa ya moto; hakuna mtu yeyote atakayemhurumia kaka yake.

20 Na atapokonya upande wa mkono wa kulia na kuwa na njaa; na atakula kwa upande wa mkono wa kushoto na hawatatosheka; kila mtu atakula nyama ya mkono wake mwenyewe—

21 Manase dhidi ya Efraimu; na Efraimu dhidi ya Manase; wao wawili pamoja watamshambulia Yuda. Kwa haya yote hasira yake haitapunguka, lakini bado amenyoosha mkono wake.

## 2 Nefi 20

1 Ole wao ambao huweka maagizo yasiyo ya haki, na wale waandikao sheria ngumu ambazo wameweka;

2 Kuwageuza walio na mahitaji kutokana na haki, na kuwanyang'anya watu wangu maskini haki yao, ili wajane wawe mateka wao, na ili wawaibie mayatima!

3 Nanyi mtafanya nini katika siku ya hukumu, na katika ukiwa utokao mbali? mtamkimbilia nani awasaidie? na mtaacha wapi utukufu wenu?

4 Bila mimi watainamia wafungwa, na watakufa miongoni mwa waliouawa. Lakini kwa haya yote hasira yake haitapunguka, lakini bado amenyoosha mkono wake.

5 Ee Mwashuri, fimbo ya hasira yangu, na bakora iliyo mkononi mwao ni ghadhabu yao.

6 Nitamtuma dhidi ya taifa la wanafiki, na dhidi ya watu wa ghadhabu yangu nitamwamuru kuchukua mateka, na kuchukua mawindo, na kuwakanyaga kama matope ya barabara.

7 Lakini hivyo sivyo akusudiavyo, wala sivyo moyo wake unavyowaza; lakini katika moyo wake akusudia kuangamiza na kutenga mataifa na sio machache tu.

8 Kwani anasema: Si wakuu wangu wote ni wafalme?

9 Je, Kalno si kama Karkemishi? Si Hamathi ni kama Arpadi? Si Samaria ni kama Dameski?

10 Kama vile mkono wangu ulijenga falme za sanamu, ambazo sanamu zake za kuchongwa zilikuwa bora kuliko za Yerusalemu na za Samaria;

11 Je, si nitatendea Samaria na sanamu zake, vile nilitendea Yerusalemu na sanamu zake?

12 Kwa hivyo itakuwa kwamba baada ya Bwana kutenda kazi yake yote kwenye Mlima Sayuni na kwenye Yerusalemu, nitaadhibu matunda ya moyo thabiti wa mfalme wa Ashuru, na utukufu wa majivuno ya macho yake.

13 Kwani yeye anasema: Kwa nguvu za mkono wangu na hekima yangu nimetenda vitu hivi; kwani mimi ni mwerevu; na nimesogesha mipaka ya watu, na kuiba hazina zao, na kuwaangusha wenyeji kama mtu shujaa;

14 Na mkono wangu umegundua kwamba utajiri wa watu ni kama kiota cha ndege; na kama vile mtu hukusanya mayai yalioachwa ndivyo nimekusanya dunia yote; na

hakuna yeyote aliyetikisa bawa, au kufungua kinywa, au kulia.
15 Je, shoka litajisifu dhidi ya yule ambaye hukata nalo? Je, msumeno utajitukuza
dhidi ya yule anayeutingisha? Ni kama fimbo ingejitikisa yenyewe dhidi ya
waiinuayo, au ni kama bakora ingejiinua ni kama sio mbao!
16 Kwa hivyo Bwana, Bwana wa Majeshi, atawatumia walionona, kukonda; na kwa
utukufu wake atawasha uteketeo kama uteketezo wa moto.
17 Na nuru ya Israeli itakuwa kama moto, na Mtakatifu wake atakuwa kama
muwako wa moto, na atachoma na kumaliza miiba yake na mbigili zake katika siku
moja;
18 Na atauteketeza utukufu wa msitu wake, na shamba lake linalostawi, zote mbili
nafsi na mwili; na watakuwa kama vile yule mshika bendera anazimia.
19 Na miti ya msitu wake inayosalia itakuwa michache, hata mtoto ataweza
kuihesabu.
20 Na itakuwa kwamba katika siku ile, kwamba sazo la Israeli, na wale walioepuka
wa nyumba ya Yakobo, hawatamtegemea tena yeye aliyewapiga, lakini
watamtegemea Bwana, yule Mtakatifu wa Israeli, kwa ukweli.
21 Sazo litarejea, ndio, hata sazo la Yakobo, kwa mwenyezi Mungu.
22 Kwani ingawa watu wako Israeli ni wengi kama mchanga wa bahari, lakini bado
sazo lao litarejea; maangamizo yaliyowekwa yatafurika kwa haki.
23 Kwani Bwana Mungu wa Majeshi atafanya maangamizo, kugeuza nchi yote.
24 Kwa hivyo, hivi ndivyo asema Bwana Mungu wa Majeshi: Enyi watu wangu
wanaoishi Sayuni, msiogope Mwashuri; atawapiga kwa fimbo, na kuwainulia gongo
lake, kama jinsi walivyofanya Misri.
25 Kwani bado kwa muda mfupi, na ghadhabu itaisha, na hasira yangu katika
maangamizo yao.
26 Na Bwana wa Majeshi atamsukumia mjeledi kama vile alivyoua Midiani katika
jabali la Orebu; na jinsi fimbo yake ilivyoinuliwa juu ya bahari, hivyo hivyo jinsi
ataiinua jinsi alivyofanyia Misri.
27 Na itakuwa kwamba katika siku ile mzigo wake utaondolewa kutoka bega lako,
na nira yake kutoka shingo yako, na nira itaharibiwa kwa sababu ya kupakwa mafuta.
28 Yeye Amefika Ayathi, amepitia Migroni; na ameweka magari yake huko
Mikmashi.
29 Wamevuka kipito; wamelala Geba; Rama anaogopa; Gibea wa Shauli
amekimbia.
30 Paza sauti, Ewe binti wa Galimu; na ifanye isikike hadi Laisha, Ee Anathothi
maskini.
31 Madmena amehamishwa; wakazi wa Gebimu wamejikusanya ili wakimbie.
32 Lakini bado siku ile atabaki Nobu; atatikisa mkono wake dhidi ya mlima wa binti
wa Sayuni, kilima cha Yerusalemu.
33 Tazama, Bwana, Bwana wa Majeshi atayakata matawi kwa mtisho; na walio na
ukubwa watakatwa; na waliojiinua watanyenyekeshwa.
34 Na atavikata vichaka vya msitu kwa chuma, na Lebanoni itaangushwa na
mwenye nguvu.

## 2 Nefi 21

1 Na patatokea mbele fimbo kutoka Shina la Yese, na tawi litamea kutoka mizizi yake.

2 Na Roho ya Bwana itakuwa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho ya
mashauri na uwezo, roho ya elimu na ya kumcha Bwana;
3 Na atamsababisha aweze kufahamu kwa haraka katika kumcha Bwana; na
hatahukumu kulingana na maono ya macho yake, wala kukemea kulingana na
kusikia kwa masikio yake.
4 Lakini kwa haki atahukumu walio maskini, na akemee kwa adili walio
wanyenyekevu wa dunia; na ataipiga dunia kwa fimbo ya kinywa chake, na kwa
pumzi ya midomo yake atawaua walio waovu.
5 Na haki itakuwa mshipi wa viuno vyake, na uaminifu mshipi wa mafigo yake.
6 Pia mbwa-mwitu ataishi na mwanakondoo, na chui atalala na mwana mbuzi, na
ndama na mwana simba na ng'ombe mnono pamoja; na mtoto mchanga
atawaongoza.
7 Na ng'ombe na dubu watakula pamoja; watoto wao watalala chini pamoja; na
simba atakula majani kama ng'ombe.
8 Na mtoto anayenyonya atacheza kwenye tundu la nyoka, na mtoto aliyeachishwa
kunyonya atatia mkono wake kwenye pango la fira.
9 Hawatadhuru wala kuharibu katika mlima wangu wote mtakatifu, kwani dunia
yote itajaa elimu ya Bwana, kama vile maji yanavyoifunika bahari.
10 Na katika siku ile kutakuwa na mzizi wa Yese, ambao utasimama kama bendera ya
watu; na Wayunani watautafuta; na pumziko lake litakuwa takatifu.
11 Na itakuwa kwamba katika siku ile Bwana atanyoosha mkono wake tena mara ya
pili kurudisha sazo la watu wake litakalobaki, kutoka Ashuru, na kutoka Misri, na
kutoka Pathrosi, na kutoka Kushi, na kutoka Elamu, na kutoka Shinari, na kutoka
Hamathi, na kutoka visiwa vya bahari.
12 Na atawatwekea mataifa bendera, na kuwakusanya watu wa Israeli waliofukuzwa,
na kuwakusanya pamoja wale waliotawanywa wa Yuda kutoka pembe nne za dunia.
13 Na wivu wa Efraimu pia utaondoka, na maadui wa Yuda watatengwa; Efraimu
hatamhusudu Yuda, na Yuda hatamuudhi Efraimu.
14 Lakini wao watashambulia juu ya mabega ya Wafilisti kuelekea upande wa
magharibi; watawapora wale kutoka mashariki pamoja; watainyooshea Edomu na
Moabu mkono wao; na watoto wa Amoni watawatii.
15 Na Bwana atauangamiza ulimi wa bahari ya Misri; na kwa upepo wake mkali
atatingisha mkono wake juu ya mto, na kuugawanya uwe vijito saba, na kuwavusha
watu kwa miguu mikavu.
16 Na kutakuwa barabara kuu kwa sazo la watu wake waliosalia, kutoka Ashuru,
kama vile ilivyokuwa katika Israeli katika siku ile waliyotoka nje ya nchi ya Misri.

## 2 Nefi 22

1 Na katika siku ile utasema: Ee Bwana, nitakusifu; ingawa ulinikasirikia hasira yako
imegeuka, na unanifariji.
2 Tazama, Mungu ni wokovu wangu; nitatumaini, na wala sitaogopa; kwani
Bwana Yehova ndiye nguvu yangu na wimbo wangu; pia amekuwa wokovu wangu.
3 Kwa hivyo, kwa shangwe utateka maji kutoka visima vya wokovu.
4 Na katika siku ile utasema: Msifuni Bwana, liiteni jina lake, tangazeni matendo
yake miongoni mwa watu, taja jina lake ili liinuliwe.
5 Mwimbieni Bwana; kwani ametenda vitu vyema; haya yanajulikana

ulimwenguni kote.
6 Pazeni sauti na mlie, ewe mkazi wa Sayuni; kwani mkuu ni yule Mtakatifu wa
Israeli aliye baina yenu.

## 2 Nefi 23

1 Mzigo wa Babilonia, ambao Isaya mwana wa Amozi aliuona.
2 Inueni bendera juu ya mlima mrefu, wapazieni sauti, wapungieni mkono, ili
waingie milangoni mwa wakuu.
3 Nimewaamuru wale wangu waliotakaswa, pia nimewaita mashujaa wangu,
kwani hasira yangu haipo juu ya wote wanaofurahia ukuu wangu.
4 Kelele za umati huko milimani ni kama za watu wengi, ngurumo na kelele za
falme za mataifa zilizokusanyika, Bwana wa Majeshi anapanga jeshi kwa vita.
5 Wanatoka nchi ya mbali, kutoka mwisho wa mbingu, ndio, Bwana, na silaha za
ghadhabu yake; ili kuangamiza nchi yote.
6 Pigeni yowe, kwani siku ya Bwana iko karibu; itakuja kama maangamizo kutoka
kwa Mwenyezi.
7 Kwa hivyo mikono yote italegea, moyo wa kila mtu utayeyuka;
8 Na wataogopa; watashikwa na kichomi na huzuni; watashangaa mmoja kwa
mwingine; nyuso zao zitakuwa kama ndimi za moto.
9 Tazama, siku ya Bwana inafika, pamoja na ukali na ghadhabu na hasira kuu,
kuifanya nchi iwe na ukiwa; na atawaangamiza wenye dhambi kutoka ndani yake.
10 Kwa maana nyota za mbingu na makundi ya nyota hayatatoa nuru yao; jua
litatiwa giza wakati wa mwendo wake, na mwezi hautasababisha nuru yake
kumulika.
11 Na nitauadhibu ulimwengu kwa sababu ya uovu, na waovu kwa sababu ya maovu
yao; nitakomesha fahari ya wenye kiburi, na nitayalaza chini majivuno ya watishao.
12 Nitamfanya mtu mmoja kuadimika kuliko dhahabu safi; na hata watu kuliko
kabari ya dhahabu ya Ofiri.
13 Kwa hivyo, nitatingisha mbingu, na kuiondoa dunia mahali pake, katika
ghadhabu ya Bwana wa Majeshi, na katika siku ya hasira yake kali.
14 Na itakuwa kama paa anayekimbizwa, na kama kondoo asiyechungwa; na kila
mtu atarudi kwa watu wake wenyewe, na kila mmoja kukimbilia nchi yake.
15 Kila mtu ambaye ana kiburi atadungwa kwa upanga; ndio, na yule ambaye
ameungana na mwovu atauawa kwa upanga.
16 Watoto wao wataaruliwa vipande mbele ya macho yao; nyumba zao zitaporwa na
wake zao watanajisiwa.
17 Tazama, nitawachochea Wamedi dhidi yao, ambao hawatafikiri fedha na
dhahabu, wala hawatazifurahia.
18 Na pinde zao zitawakatakata vijana kwa vipande vipande; na hawatahurumia
matunda ya tumbo; macho yao haitawaacha watoto.
19 Na Babilonia, utukufu wa falme, na urembo wa ubora wa Wakaldayo, itakuwa
kama wakati Mungu alivyopindua Sodoma na Gomora.
20 Hautakaliwa tena, wala watu hawataishi ndani yake tangu kizazi hadi kizazi:
wala Mwarabu kupiga hema hapo; wala wachungaji hawatalaza makundi yao huko.
21 Lakini wanyama wakali wa jangwani watalala huko; na nyumba zao zitajaa
wanyama wa kuhuzunisha; na bundi wataishi huko, na mbuzi wa mwitu watacheza

huko.
22 Na nyumbu wa visiwani watabweka katika nyumba zao zilizo na ukiwa, na majoka katika ngome zao nzuri; na wakati wake unakaribia, na siku yake haitaongezeka. Kwani nitamwangamiza kwa haraka; ndio, kwani nitawarehemu watu wangu, lakini waovu wataangamia.

## 2 Nefi 24

1 Kwani Bwana atamrehemu Yakobo, na hata hivyo atachagua Israeli, na kuwaweka katika nchi yao wenyewe; na wageni wataunganishwa na wao, na kuungana na nyumba ya Yakobo.
2 Na watu watawachukua na kuwapeleka mahali pao; ndio, kutoka mbali hadi sehemu za mwisho za dunia; na watarejea katika nchi zao za ahadi. Na nyumba ya Israeli itawamiliki, na nchi ya Bwana itakuwa ya watumishi na wajakazi; na watawachukua wafungwa wale waliowafunga; na watawatawala wadhalimu wao.
3 Na itakuwa kwamba katika siku ile kwamba Bwana atakupatia pumziko, kutoka kwa huzuni yako, na kutoka woga wako, na kutoka ufungwa mgumu ambao ulifanywa kutumika.
4 Na itakuwa kwamba katika siku ile, kwamba utarudia methali hii dhidi ya mfalme wa Babilonia, na kusema: Jinsi gani mwenye kudhulumu amekoma, na mji wa dhahabu kukoma!
5 Bwana amelivunja gongo la waovu, dalili za enzi za watawala.
6 Yeye aliyewapiga watu katika ghadhabu kwa mapigo yasiyokoma, yeye aliyetawala mataifa kwa hasira, anaadhibiwa, na hakuna yeyote anakayezuia.
7 Ulimwengu wote unapumzika, na umekuwa kimya; wanaanza kuimba.
8 Ndio, misunobari inakusherekea, na pia mierezi ya Lebanoni, ikisema: Tangu ulazwe chini hakuna yeyote amekuja dhidi yetu.
9 Jahanamu imetaharuki kukulaki utakapokuja; inawaamsha wafu kwa sababu yako, hata walio wakuu wote wa dunia; imewainua kutoka viti vyao vya enzi wafalme wote wa mataifa.
10 Wote watanena na kukwambia: Je, nawe pia umekuwa mnyonge kama sisi? Je, nawe umekuwa kama sisi?
11 Fahari yako imeshushwa chini kaburini; na kelele ya mazeze yako haisikiki; funza ametandazwa chini yako, na funza wamekufunika.
12 Jinsi gani umeanguka kutoka mbinguni, Ee Lusiferi, mwana wa asubuhi! Je, umekatwa chini, ambaye alidhoofisha mataifa!
13 Kwani umesema moyoni mwako: Mimi nitapanda mbinguni, nitainua kiti changu cha enzi juu ya nyota za Mungu; nitaketi pia juu ya mlima wa mkutano, katika pande za kaskazini;
14 Nitapanda kupita vimo vya mawingu; nitakuwa kama yeye Aliye Juu Sana.
15 Bado wewe utashushwa chini jahanamu, hadi pande za shimo.
16 Wale watakaokuona watakukazia macho kwa makini, na kukufikiria, na watasema: Je huyu ni yule mtu aliyetetemesha dunia, aliyetingisha falme?
17 Na kufanya ulimwengu kama nyika, na kuangamiza miji iliyomo ndani yake, na hakufungua nyumba za wafungwa wake?
18 Wafalme wote wa mataifa, ndio, wote, wamezikwa kwa utukufu, kila mmoja wao katika nyumba yake mwenyewe.

19 Lakini wewe umetupwa mbali na kaburi lako kama tawi linalochukiza, na sazo la
wanaouawa, wanaodungwa kwa upanga, ambao wanashuka chini hadi kwenye
mawe ya shimo; kama mzoga uliokanyagwa chini miguuni.
20 Wewe hutaunganishwa na wao katika mazishi, kwa sababu umeangamiza nchi
yako na kuwaua watu wako; uzao wa waovu hautaheshimiwa kamwe.
21 Tayarisheni machinjo kwa watoto wao kwa sababu ya maovu ya baba zao, ili
wasije wakainuka, wala kumiliki nchi, wala kujaza uso wa dunia na miji.
22 Kwani nitainuka dhidi yao, asema Bwana wa Majeshi, na kutenga kutoka
Babilonia jina, na sazo, na mwana, na mpwa, asema Bwana.
23 Pia nitaifanya makao ya ngojamaliko, na maziwa ya maji; na nitaifagia kwa
ufagio wa maangamizo, asema Bwana wa Majeshi.
24 Bwana wa Majeshi ameapa, akisema: Kwa kweli vile nimefikiria, hivyo yatatimia;
na yale niliyoamua, ndiyo yatabaki imara—
25 Kwamba nitamleta Mwashuri nchini mwangu, na kwenye milima yangu
nitamkanyaga chini ya miguu; kisha nira yake itawaondokea, na mzigo wake
kuondoka kutoka mabega yao.
26 Hili ndilo kusudi lililonuiwa ulimwenguni mwote; na huu ndio mkono
ulionyoshewa mataifa yote.
27 Kwani Bwana wa Majeshi amenuia, na nani atakayelibatilisha? Na mkono wake
umenyooshwa, na nani atakayeurudisha nyuma?
28 Katika ule mwaka ambao mfalme Ahazi alikufa kulikuwa na mzigo huu.
29 Usifurahi ewe, Ufilisti wote, kwa sababu fimbo ya aliyekupiga imevunjika; kwani
kutoka mzizi wa nyoka atatoka fira, na uzao wake utakuwa nyoka wa moto arukaye.
30 Na kifungua-mimba wa maskini watakula, na walio na shida watalala kwa
usalama; na nitaua mzizi wako kwa njaa, na ataua sazo lako.
31 Pigeni yowe, Ee lango; lia, Ee mji, wewe, Ufilisti wote, umeyeyuka; kwani kutoka
kaskazini kutakuja moshi, na hakuna yeyote atakayekuwa pekee mahali
alipopangiwa.
32 Nini hapo kitakacho wajibu wajumbe wa mataifa? Kwamba Bwana ameimarisha
Sayuni, na walio maskini wa watu wake wataitumaini.

## 2 Nefi 25

1 Sasa mimi, Nefi, nasema machache kuhusu maneno ambayo nimeandika, ambayo
yamenenwa na kinywa cha Isaya. Kwani tazama, Isaya alizungumza vitu vingi
ambavyo vilikuwa vigumu kufahamika na watu wangu; kwani hawajui kuhusu
mtindo wa kutoa unabii miongoni mwa Wayahudi.
2 Kwani mimi, Nefi, sijawafunza vitu vingi kuhusu desturi za Wayahudi; kwani
kazi zao zilikuwa kazi za giza, na matendo yao yalikuwa matendo ya machukizo.
3 Kwa hivyo, ninawaandikia watu wangu, kwa wale wote watakaopokea hapo
baadaye vitu hivi ambavyo ninaandika, ili wajue hukumu za Mungu, kwamba
zinashukia mataifa yote, kulingana na neno ambalo amenena.
4 Kwa hivyo, sikilizeni, Enyi watu wangu, ambao ni wa nyumba ya Israeli, na
msikilize maneno yangu; kwani kwa sababu maneno ya Isaya sio wazi kwenu,
walakini ni wazi kwa wale wote ambao wamejazwa na roho ya unabii. Lakini
nawapatia unabii, kulingana na roho aliye ndani yangu; kwa hivyo nitatoa unabii
kulingana na unyofu uliokuwa na mimi tangu wakati nitoke Yerusalemu na baba

yangu; kwani tazama, nafsi yangu inafurahia unyofu kwa watu wangu, ili wajifunze.
5 Ndio, na nafsi yangu inafurahia maneno ya Isaya, kwani nilitoka Yerusalemu, na
macho yangu yameona vitu vya Wayahudi, na ninajua kwamba Wayahudi
wanafahamu vitu vya manabii, na hakuna watu wengine wanaofahamu vitu
vilivyonenwa Wayahudi kama wao, ila tu kwamba wawe wamefunzwa desturi ya vitu
vya Wayahudi.
6 Lakini tazama, mimi, Nefi, sijafunza watoto wangu desturi za Wayahudi; lakini
tazama, mimi, mwenyewe, nimeishi Yerusalemu, kwa hivyo najua kuhusu eneo
karibu inayoizingira; na nimewatajia watoto wangu kuhusu hukumu za Mungu,
ambazo zimefanyika miongoni mwa Wayahudi, kwa watoto wangu, kulingana na
yale yote ambayo Isaya amezungumza, na siyaandiki.
7 Lakini tazama, ninaendelea na unabii wangu, kulingana na unyofu wangu;
ambamo kwayo najua kwamba hakuna mtu yeyote anayeweza kukosea; walakini,
katika siku ambazo unabii wa Isaya utatimizwa watu watajua kwa hakika, wakati
yatatimizwa.
8 Kwa hivyo, yana thamani kwa watoto wa watu, na kwa yule anayedhani kwamba
hayana, kwa hawa nitawazungumzia zaidi, na kuyatilia mkazo kwa watu wangu;
kwani ninajua kwamba yatawafaidi sana katika siku za mwisho; kwani katika siku
hizo watayafahamu; kwa hivyo, ni kwa faida yao nimeyaandika.
9 Na kama vile kizazi kimoja miongoni mwa Wayahudi kimeangamizwa kwa
sababu ya uovu, hata hivyo wameangamizwa kutoka kizazi hadi kizazi kulingana na
maovu yao; na hakuna aliyeangamizwa bila kuaguliwa na manabii wa Bwana.
10 Kwa hivyo, walikuwa wameelezewa kuhusu maangamizo yatakayowajia, mara tu
baada ya baba yangu alipotoka Yerusalemu; walakini, walishupaza mioyo yao; na
kulingana na unabii wangu wameangamizwa, ijapokuwa wale waliopelekwa
utumwani huko Babilonia.
11 Na sasa haya nazungumza kwa sababu ya roho iliyo ndani yangu. Na ingawaje
wamehamishwa watarejea tena, na kumiliki nchi ya Yerusalemu; kwa hivyo,
watarudishwa tena katika nchi yao ya urithi.
12 Lakini, tazama, watakuwa na vita, na uvumi wa vita; na wakati siku inafika
ambayo Mzaliwa Pekee wa Baba, ndio, hata Baba wa mbingu na dunia,
atajithirihisha mwenyewe kwao katika mwili, tazama, watamkataa, kwa sababu ya
maovu yao, na ugandamizo wa mioyo yao, na ugumu wa shingo zao.
13 Tazama, watamsulubu; na baada ya kulazwa katika ziara kwa muda wa siku tatu
atafufuka kutoka kwa wafu, na uponyaji katika mabawa yake; na wale wote
watakaoamini kwa jina lake wataokolewa katika ufalme wa Mungu. Kwa hivyo,
moyo wangu unafurahia kutoa unabii kumhusu, kwani nimeona siku yake, na moyo
wangu unatukuza jina lake takatifu.
14 Na tazama itakuwa kwamba baada ya Masiya kufufuka kutoka kwa wafu, na
kujithirihisha kwa watu wake, kwa wengi kadiri watakavyoliamini kwa jina lake,
tazama, Yerusalemu itaangamizwa tena; kwani ole kwa wale wanaopigana dhidi ya
Mungu na watu wa kanisa lake.
15 Kwa hivyo, Wayahudi watatawanywa miongoni mwa mataifa yote; ndio, na
Babilonia pia itaangamizwa; kwa hivyo, Wayahudi watatawanywa na mataifa
mengine.
16 Na baada ya wao kutawanywa, na Bwana Mungu kuwapiga kwa mataifa mengine
kwa muda wa vizazi vingi, ndio, hata chini kutoka kizazi hadi kizazi mpaka

watashawishwa kumwamini Kristo, Mwana wa Mungu, na upatanisho, ambao ni
kwa wanadamu wote bila kikomo — na wakati ile siku itakapofika kwamba
watamwamini Kristo, na kumwabudu Baba katika jina lake, na mioyo mieupe na
mikono safi, na wasimtazamie Masiya mwingine, kisha, katika ule wakati, siku
itafika ambapo itakuwa lazima waamini vitu hivi.
17 Na Bwana atanyoosha mkono wake tena mara ya pili kuwarudisha watu wake
kutoka kwa hali yao ya kupotea na kuanguka. Kwa hivyo, ataendelea kutenda kazi
kuu na maajabu miongoni mwa watoto wa watu.
18 Kwa hivyo, atawaletea maneno yake, maneno yale yatakayowahukumu katika siku
ya mwisho, kwani yatapewa kwao kwa lengo la kuwasadikisha kuhusu Masiya wa
kweli, aliyekataliwa nao; na kuwasadikishia kwamba hawana haja tena kumtazamia
Masiya mwingine aje, kwani hakuna mwingine atakayekuja, ila tu awe Masiya wa
bandia atakayewadanganya watu; kwani kuna Masiya mmoja tu anayezungumziwa
na manabii, na huyo Masiya ndiye yule atakayekataliwa na Wayahudi.
19 Kwani kulingana na maneno ya manabii, Masiya atakuja baada ya miaka mia sita
tangu baba yangu atoke Yerusalemu; na kulingana na maneno ya manabii, na pia
neno la malaika wa Mungu, jina lake litakuwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.
20 Na sasa, ndugu zangu, nimezungumza wazi ili msikosee. Na jinsi aishivyo Bwana
Mungu aliyewatoa Israeli kutoka nchi ya Misri, na akampatia Musa uwezo kwamba
aponye mataifa baada ya wao kuumwa na nyoka wenye sumu, kama wangemtazama
nyoka ambaye aliinua mbele yao, na pia akampa uwezo kwamba agonge mwamba na
maji yatokee; ndio, tazama nawaambia, kwamba jinsi vile hivi vitu ni kweli, na jinsi
Bwana Mungu aishivyo, hakuna jina lingine ambalo limetolewa chini ya mbingu ila
tu awe huyu Yesu Kristo, ambalo nimelizungumzia, ambamo kwamba mwanadamu
anaweza kuokolewa.
21 Kwa hivyo, kwa sababu hii Bwana Mungu ameniahidi kwamba hivi vitu ambavyo
ninaandika vitawekwa na kuhifadhiwa, na kutolewa kwa uzao wangu, kutoka kizazi
hadi kizazi, ili ahadi atimiziwe Yusufu, kwamba uzao wake hautaangamia kamwe
kadiri dunia itakavyosimama.
22 Kwa hivyo, hivi vitu vitaendelea kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine kadiri
dunia itakavyokuwepo; na vitaendelea kulingana na njia na mapenzi ya Mungu; na
mataifa yatakayovimiliki yatahukumiwa kwavyo kulingana na maneno ambayo
yameandikwa.
23 Kwani tunajitahidi kuandika, kuwashawishi watoto wetu, na pia ndugu zetu,
kumwamini Kristo, na kupatanishwa na Mungu; kwani tunajua kwamba ni kwa
neema kwamba tunaokolewa, baada ya kutenda yote tunayoweza.
24 Na, ingawa tunamwamini Kristo, tunatii sheria ya Musa, na kutazama mbele kwa
uthabiti kwa Kristo, hadi sheria itakapotimizwa.
25 Kwani, ni kwa kusudi hili sheria ilitolewa; kwa hivyo sheria imekufa kwetu, na
tumefanywa hai katika Kristo kwa sababu ya imani yetu; lakini bado tunatii sheria
kwa sababu ya amri.
26 Na tunazungumza kuhusu Kristo, tunafurahia katika Kristo, tunahubiri kuhusu
Kristo, tunatoa unabii kumhusu Kristo, na tunaandika kulingana na unabii wetu, ili
watoto wetu wajue asili ya kutegemea msamaha wa dhambi zao.
27 Kwa hivyo, tunazungumza kuhusu sheria ili watoto wetu wajue mauti ya sheria;
na wao, kwa kujua mauti ya sheria; watatazama mbele kwa ule uhai ulio katika
Kristo, na wafahamu ni kwa kusudi gani sheria ilitolewa. Na baada ya sheria

kutimizwa katika Kristo, kwamba wasishupaze mioyo yao dhidi yake wakati sheria
itakapotakiwa kuwekwa kando.
28 Na sasa tazama, watu wangu, nyinyi ni watu wa shingo gumu; kwa hivyo,
nimewazungumzia kwa uwazi, ili msielewe vibaya. Na maneno ambayo
nimezungumza yatabaki kama ushuhuda dhidi yenu; kwani yanatosha kumfundisha
mtu yeyote njia iliyo sawa; kwani njia iliyo sawa ni kuamini katika Kristo na
kutomkana kwani kwa kumkana unawakana pia manabii na sheria.
29 Na sasa tazama, nawaambia kwamba njia iliyo sawa ni kuamini katika Kristo, na
kutomkana; na Kristo ndiye Mtakatifu wa Israeli; kwa hivyo lazima msujudu mbele
yake, na mmwabudu kwa uwezo wenu wote, akili, na nguvu, na nafsi zenu zote; na
mkifanya hivi, hamtatengwa kwa njia yoyote.
30 Na, kadiri itakavyohitajika, lazima utii matendo na masharti ya Mungu hadi
sheria aliyopewa Musa itakapotimizwa.

## 2 Nefi 26

1 Na baada ya Kristo kufufuka kutoka kwa wafu atajidhihirisha kwenu nyinyi, watoto
wangu, na ndugu zangu wapendwa; na maneno atakayowazungumzia yatakuwa
sheria mtakayoitii.
2 Kwani tazama, nawaambia kwamba nimeona kwamba vizazi vingi vitapita, na
kutakuwa na vita kuu na mabishano miongoni mwa watu wangu.
3 Na baada ya Masiya kuja watu wangu watapewa ishara kuhusu kuzaliwa kwake,
na pia kuhusu kifo chake na kufufuka kwake; na siku ile itakuwa kuu na mbovu kwa
wale walio waovu, kwani wataangamia; na wanaangamia kwa sababu waliwafukuza
manabii, na watakatifu, na kuwapiga mawe, na kuwaua; kwa hivyo kilio cha damu ya
watakatifu kitapanda kwa Mungu kutoka chini dhidi yao.
4 Kwa hivyo, wale wote walio na kiburi, na watendao maovu, siku itakayofika
itawachoma, asema Bwana wa Majeshi, kwani watakuwa kama makapi.
5 Na wale wanaoua manabii, na watakatifu, watamezwa na kina cha ardhi, asema
Bwana wa Majeshi; na milima itawafunika, na vimbunga vitawabeba, na majengo
kuwaangukia na kuwavunja kwa vipande na kuwasaga kama unga.
6 Na wataadhibiwa kwa radi, na umeme, na matetemeko ya ardhi, na kila aina ya
maangamizo, kwani moto wa hasira ya Bwana utawawakia, na watakuwa kama
makapi, na ile siku inayokuja itawamaliza, asema Bwana wa Majeshi.
7 Ee uchungu, na maumivu ya nafsi yangu kwa sababu ya watu wangu waliopotea
kwa kuuawa! Kwani mimi, Nefi, nimeiona, na inakaribia kunimaliza katika uwepo
wa Bwana; lakini lazima nimlilie Mungu wangu: Njia zako ni za haki.
8 Lakini tazama, wenye haki wanaotii maneno ya manabii, na bila kuwaangamiza,
lakini wanamtazamia Kristo kwa uthabiti na ishara zinazotolewa, ingawa mateso
hayo yote — tazama, wao ndio wao ambao hawataangamia.
9 Lakini Mwana wa Uadilifu atawatokea; na atawaponya, na watakuwa na amani
na yeye, hadi vizazi vitatu vitakuwa vimepita, na wengi wa kizazi cha nne watakuwa
wamepita kwa uadilifu.
10 Na wakati vitu hivi vimepita maangamizo ya haraka yatawajia watu wangu;
kwani ingawa nafsi yangu ina uchungu, nimeiona; kwa hivyo, najua kwamba
itatimia; na wanajiuza bure; kwani, kwa zawadi ya kiburi chao na upumbafu wao
watavuna maangamizo; kwani kwa sababu watajitolea ibilisi na kuchagua kazi za

giza badala ya nuru, kwa hivyo lazima waende chini jahanamu.
11 Kwani Roho ya Bwana daima haitajishughulisha na wanadamu. Na wakati Roho anakoma kujishughulisha na wanadamu basi maangamizo ya haraka yanakuja, na hii inahuzunisha nafsi yangu.
12 Na kama nilivyosema kuhusu kuwasadikisha Wayahudi, kwamba Yesu ndiye yule Kristo, inahitajika lazima kwamba Wayunani pia nao wasadikishiwe kwamba Yesu ndiye Kristo, Mungu wa Milele;
13 Na kwamba anajidhihirisha kwa wale wote wanaomwamini, kwa nguvu za Roho Mtakatifu; ndio, kwa kila taifa, kabila, lugha, na watu, akifanya maajabu makuu, ishara, na miujiza, miongoni mwa watoto wa watu kulingana na imani yao.
14 Lakini tazama, nawatolea unabii kuhusu siku za mwisho; kuhusu siku zile Bwana Mungu atakapowaletea watoto wa watu vitu hivi.
15 Baada ya uzao wangu na uzao wa kaka zangu kufifia katika kutoamini, na watakuwa wamepigwa na Wayunani; ndio, baada ya Bwana Mungu kuwazingira, na kuwahusuru kwa kilima, na kuinua ngome dhidi yao; na baada ya wao kushushwa chini mavumbini, hadi wamalizwe kabisa, bado maneno ya wenye haki yataandikwa, na sala za waumini yatasikika, na wale wote ambao wamefifia katika kutoamini hawatasahaulika.
16 Kwani wale watakaoangamizwa watawazungumzia kutoka ardhini, na sauti yao itakuwa sauti kunjufu kutoka mavumbini, na sauti yao itakuwa kama moja ambayo ina pepo ya utambuzi; kwani Bwana Mungu atampatia uwezo, kwamba anong'one juu yao, hata iwe ni kama kutoka ardhini; na sauti yao itanong'ona kutoka mavumbini.
17 Kwani Bwana Mungu asema hivi: Wataandika vile vitu vitakavyotendwa miongoni mwao, na vitaandikwa na kutiwa muhuri katika kitabu, na wale waliofifia katika kutoamini hawatavipokea, kwani wanajaribu kutafuta kuharibu vitu vya Mungu.
18 Kwa hivyo, kwa kuwa wale walioangamizwa wameangamizwa kwa haraka; na kundi la watu watishao watakuwa kama makapi yapitayo—ndio, hivi ndivyo asema Bwana Mungu: Itakuwa kwa muda, ghafula—
19 Na itakuwa, kwamba wale waliofifia katika kutoamini watapigwa kwa mkono wa Wayunani.
20 Na Wayunani wamejiinua kwa kiburi cha macho yao, na wamejikwaa, kwa sababu ya kikwazo kikuu, kwamba wamejenga makanisa mengi; walakini, wanadharau uwezo na miujiza ya Mungu, na kujihubiria wao wenyewe hekima yao na elimu yao, ili wafaidike na kuseta uso wa maskini.
21 Na kuna makanisa mengi ambayo yamejengwa yanayosababisha wivu, na ubishi, na chuki.
22 Na pia kuna makundi maovu ya siri, hata kama siku za kale, kulingana na makundi ya ibilisi, kwani yeye ndiye chanzo cha vitu hivi vyote; ndio, chanzo cha mauaji, na kazi za giza; ndio, na huwaongoza kwa shingo na mkanda wa kitani, hadi anawafunga kwa mikanda yake milele.
23 Kwani tazama, ndugu zangu wapendwa, nawaambia kwamba Bwana Mungu hatendi kazi yake gizani.
24 Hafanyi chochote ila tu kwa manufaa ya ulimwengu; kwani anapenda ulimwengu, hata kwamba anatoa maisha yake ili awavute wanadamu wote kwake. Kwa hivyo, hamwamuru yeyote asipokee wokovu wake.

25 Tazama, je yeye hulilia yeyote, na kusema: Niondokeeni? Tazama, nawaambia,
Hapana; lakini husema: Njooni kwangu nyote kutoka pande zote za mwisho wa
ulimwengu, nunueni maziwa na asali, bila pesa na bila bei.
26 Tazama, je amemwamuru yeyote kutoka katika masinagogi, au kutoka nyumba
za ibada? Tazama, nawaambia, Hapana.
27 Je, amewaamuru wowote wasipokee wokovu wake? Tazama nawaambia,
Hapana; lakini ameutoa bure kwa wanadamu wote; na amewaamuru watu wake
kwamba wawashawishi wanadamu wote watubu.
28 Tazama, je, Bwana amewaamuru wowote wasipokee wema wake? Tazama
nawaambia, Hapana; lakini wanadamu wote wana haki sawa, na hakuna yeyote
anayekatazwa.
29 Anaamuru kwamba kusiwe na ukuhani wa uongo; kwani, tazama, ukuhani wa
uongo ni kwamba wanadamu wanahubiri na kujiinua wawe nuru ya ulimwengu, ili
wafaidike na wapate sifa za ulimwengu; lakini hawajali ustawi wa Sayuni.
30 Tazama, Bwana amekataza kitu hiki; kwa hivyo, Bwana Mungu ametoa amri
kwamba wanadamu wote wawe na hisani, hisani ambayo ni upendo. Na bila kuwa
na hisani wao sio chochote. Kwa hivyo, kama wangekuwa na hisani hawangekubali
mtumishi wa Sayuni kuangamia.
31 Lakini mtumishi wa Sayuni atatumikia Sayuni; kwani kama watatumikia kwa
sababu ya pesa wataangamia.
32 Na tena, Bwana Mungu ameamuru kwamba wanadamu wasiue; kwamba
wasidanganye; kwamba wasiibe; kwamba wasiape bure kwa jina la Bwana Mungu
wao; kwamba wasiwe na wivu; kwamba wasiwe na chuki; kwamba wasibishane wao;
kwamba kwa wao wasifanye usherati; na kwamba wasitende vyovyote vya vitu hivi;
kwani yeyote atakayevitenda ataangamia.
33 Kwani hakuna yoyote ya haya maovu yatokayo kwa Bwana; kwani anatenda yale
ambayo ni mema miongoni mwa watoto wa watu; na hatendi lolote lisilo wazi kwa
watoto wa watu; na anawakaribisha wote kuja kwake na kupokea wema wake; na
hamkatazi yeyote anayemjia, weusi kwa weupe, wafungwa na walio huru, wake kwa
waume; na anawakumbuka kafiri; na wote ni sawa kwa Mungu, wote wawili,
Myahudi na Myunani.

## 2 Nefi 27

1 Lakini, tazama, katika siku za mwisho, au katika siku za Wayunani—ndio, tazama
mataifa yote ya Wayunani na pia Wayahudi, wote watakaokuja katika nchi hii na
wale watakaokuwa katika nchi zingine, ndio, hata katika nchi zote za dunia, tazama,
watalewa kwa maovu na aina zote za machukizo—
2 Na siku ile itakapofika wataadhibiwa na Bwana wa Majeshi, kwa radi na kwa
mtetemeko wa ardhi, na kwa ngurumo, na kwa dhoruba, na kwa tufani, na kwa
mwali wa moto unaounguza.
3 Na mataifa yote yapiganayo dhidi ya Sayuni, na yale yanayomuudhi, yatakuwa ni
kama ndoto ya maono usiku; ndio, itakuwa kwao, hata kama mtu mwenye njaa
aotaye, na tazama anakula lakini anaamka na nafsi yake ni tupu; au kama mtu aliye
na kiu aotaye, na tazama anakunywa lakini anaamka na tazama anazirai, na nafsi
yake ina hamu; ndio, hata hivyo ndivyo utakavyokuwa umati wa mataifa yote
yapiganayo dhidi ya Mlima Sayuni.

4 Kwani tazama, nyote mnaotenda maovu, kaeni mlipo na mstaajabu, kwani
mtalia, na kulia; ndio, mtalewa lakini sio kwa mvinyo, mtayumbayumba lakini sio
kwa pombe kali.
5 Kwani tazama, Bwana amewamwagia roho ya usingizi. Kwani tazama, mmefunga
macho yenu, na mmewakataa mwonaji; na watawala wenu, na manabii
amewafunika kwa sababu ya uovu wenu.
6 Na itakuwa kwamba Bwana Mungu atawaletea ninyi maneno ya kitabu, na
yatakuwa maneno ya waliokufa.
7 Na tazama, hicho kitabu kitakuwa kimetiwa muhuri; na katika kitabu hicho
patakuwa na ufunuo kutoka kwa Mungu, tangu mwanzo wa dunia hadi mwisho
wake.
8 Kwa hivyo, kwa sababu ya vitu ambavyo vimetiwa muhuri, vitu viliyotiwa muhuri
havitatolewa katika siku za uovu na machukizo ya watu. Kwa hivyo kitabu hicho
kitawekwa mbali nao.
9 Lakini kitabu hicho atapewa mtu, na atapewa maneno ya kitabu hicho, ambayo
ni maneno ya wafu walio mavumbini, na atatoa maneno haya kwa mwingine;
10 Lakini maneno yaliyotiwa muhuri hatatoa, wala hatatoa hicho kitabu. Kwani
kitabu hicho kitatiwa muhuri kwa nguvu za Mungu, na ufunuo uliotiliwa muhuri
utawekwa kitabuni humo hadi wakati mkamilifu wa Bwana utimie, kwamba
yajulikane; kwani tazama, yanafunua vitu vyote tangu msingi wa ulimwengu hadi
mwisho wake.
11 Na siku inafika ambapo yale maneno ya kile kitabu yaliyotiwa muhuri yatasomwa
kutoka juu ya nyumba; na yatasomwa kwa uwezo wa Kristo; na vitu vyote
vitafunuliwa watoto wa watu vile vilivyokuwa miongoni mwa watoto wa watu, na
vile vitakavyokuwa hata hadi mwisho wa dunia.
12 Kwa hivyo, katika siku ile ambayo hicho kitabu kitatolewa kwa yule mtu ambaye
nimemtaja, kitabu hicho kitafichwa tokana na macho ya ulimwengu, kwamba
hakuna macho yoyote yatakayokiona ila tu mashahidi watatu watakiona, kwa nguvu
za Mungu, na kwa yule ambaye atapewa kitabu hicho; na watashuhudia ukweli wa
kitabu hicho na kwa vitu vilivyomo.
13 Na hakuna yeyote atakayekiona, ila tu wachache kulingana na nia ya Mungu,
kushuhudia kuhusu neno lake kwa watoto wa watu; kwani Bwana Mungu amesema
kwamba maneno ya waaminifu yatanena ni kama kutoka kwa wafu.
14 Kwa hivyo, Bwana Mungu ataendelea kutoa maneno ya kitabu hicho; na kwa
vinywa vya mashahidi wengi kama apendavyo ataimarisha neno lake; na ole ni kwa
yule anayekataa neno la Mungu!
15 Lakini tazama, itakuwa kwamba Bwana Mungu atamwambia yule aliyempa
hicho kitabu: Chukua maneno haya ambayo hayajawekwa muhuri na umpatie
mwingine, ili amwonyeshe aliyeelimika, akisema: Soma hii, nakusihi. Na
aliyeelimika atasema: Leta hapa kitabu, na nitayasoma.
16 Na sasa, kwa sababu ya utukufu wa ulimwengu na kupata faida watasema haya,
na sio kwa utukufu wa Mungu.
17 Na yule mtu atasema: Siwezi kuleta hicho kitabu, kwani kimetwa muhuri.
18 Kisha aliyeelimika atasema: Siwezi kukisoma.
19 Kwa hivyo itakuwa kwamba, Bwana Mungu atatoa tena kitabu hicho na maneno
haya kwa yule asiyeelimika; na yule mtu asiyeelimika atasema: Mimi sina elimu.
20 Kisha Bwana Mungu atamwambia: Walioelimika hawatayasoma, kwani

wameyakataa, na ninaweza kufanya kazi yangu mwenyewe; kwa hivyo wewe
utasoma yale maneno nitakayokupatia.
21 Usiguse vitu vilivyotiwa muhuri, kwani nitavitoa katika wakati wangu
mkamilifu; kwani nitawaonyesha watoto wa watu kwamba ninaweza kufanya kazi
yangu mwenyewe.
22 Kwa hivyo, ukishamaliza kusoma maneno yale niliyokuamuru, na kupata wale
mashahidi ambao nilikuahidi, basi utakitia kile kitabu muhuri tena, na kukificha
kwangu, ili niyahifadhi maneno ambayo hujasoma, hadi nitakapotaka katika
hekima yangu kuwafunulia watoto wa watu mambo yote.
23 Kwani tazama, mimi ni Mungu; na mimi ni Mungu wa miujiza; na nitauonyesha
ulimwengu kwamba mimi ndiye yule jana, leo, na milele; na kwamba mimi sitendi
lolote miongoni mwa watoto wa watu ila tu kulingana na imani yao.
24 Na tena itakuwa kwamba Bwana atamwambia yule atakayesoma yale maneno
atakayopewa:
25 Kwa sababu watu hawa wananikaribia kwa kinywa chao, na kwa midomo yao
wananisifu, lakini mioyo yao iko mbali nami, na hofu yao kwangu mimi
inafundishwa kwa njia ya wanadamu—
26 Kwa hivyo, nitaendelea kufanya kazi ya kushangaza miongoni mwa watu hawa,
ndio, kazi ya kushangaza na ya maajabu, kwani hekima ya walio werevu na wenye
elimu itaangamia, na ufahamu wa wapiga ramli wao utafichwa.
27 Na ole kwa wale wanaojaribu kumficha Bwana mashauri yao! Na matendo yao
yako gizani; na wanasema: Nani anayetuona, na nani anayetujua? Na pia wanasema:
Kwa hakika, upinduzi wako wa vitu juu chini utahesabiwa kama udongo wa
mfinyanzi. Lakini tazama, nitawaonyesha, asema Bwana wa Majeshi, kwamba najua
matendo yao yote. Kwani kitu kitamwambia aliyekiunda, kwamba hakuniunda? Au
kitu kilichojengwa kitamwambia mjenzi, hakuwa na ufahamu?
28 Lakini tazama, asema Bwana wa Majeshi: Nitaonyesha watoto wa watu kwamba
ni muda kidogo uliobaki kwamba Lebanoni itageuzwa kuwa shamba lizaalo; na
shamba lizaalo litakuwa kama msitu.
29 Na katika siku ile viziwi watasikia maneno ya kitabu, na macho ya vipofu yataona
kutoka fumboni na giza.
30 Na wapole pia nao wataongezeka, na shangwe yao itakuwa katika Bwana, na
walio masikini miongoni mwa wanadamu watashangilia katika yule Mtakatifu wa
Israeli.
31 Kwa hakika jinsi Bwana aishivyo wataona kwamba yule ambaye hutisha atakuwa
bure, na mwenye kudharau ameangamizwa, na kwamba wale wote wanaotafuta
uovu wanatengwa;
32 Na wale wanaomkosesha mtu kwa neno, na kumtegea mtego yule anayekemea
langoni, na kumkataa mwenye haki kwa kitu kisichofaa.
33 Kwa hivyo, hivi asema Bwana, aliyemkomboa Ibrahimu, kuhusu nyumba ya
Yakobo: Sasa Yakobo hataaibika, wala uso wake kugeuka rangi uwe mweupe.
34 Lakini atakapoona watoto wake, ambao ni kazi ya mikono yangu, kati yake,
watatakasa jina langu, na kumtakasa yule Mtakatifu wa Yakobo, na watamheshimu
Mungu wa Israeli.
35 Wale nao pia waliokosea katika roho watafahamu, na wale walionung'unika
watajifunza mafundisho ya dini.

# 2 Nefi 28

1 Na sasa, tazameni, ndugu zangu, nimewazungumzia, kulingana na vile Roho
ameniongoza; kwa hivyo, najua kwamba kwa kweli lazima yatimizwe.
2 Na vitu ambavyo vitaandikwa kutoka kwenye kitabu hicho vitakuwa vya
dhamana kuu kwa watoto wa watu, na hasa kwa uzao wetu, ambayo ni sazo la
nyumba ya Israeli.
3 Kwani itakuwa kwamba katika siku ile makanisa ambayo yamejengwa, na siyo
kwa Bwana, wakati mmoja italiambia nyingine: Tazama, Mimi, Mimi ni wa Bwana;
na jingine litasema: Mimi, Mimi ni wa Bwana; na kila mmoja aliyejenga makanisa,
yasiyo ya Bwana atasema hivyo—
4 Na watabishana mmoja na mwingine; na makuhani wao watabishana mmoja na
mwingine, na watafunza kulingana na elimu yao, na watamkana Roho Mtakatifu,
anayetoa maneno.
5 Na wanakana nguvu za Mungu, yule Mtakatifu wa Israeli; na kuwaambia watu:
Tusikilizeni sisi, na sikiliza mawaidha yetu; kwani tazama hakuna Mungu leo, kwani
Bwana na Mkombozi ametenda kazi yake, na amewapatia wanadamu uwezo wake;
6 Tazameni, sikilizeni mawaidha yangu; kama watasema kuna muujiza uliotendwa
kwa mkono wa Bwana, msiamini; kwani leo yeye sio Mungu wa miujiza; ametenda
kazi yake.
7 Ndio, na kutakuwa na wengi ambao watasema: Kuleni, kunyweni, na mshangilie,
kwani kesho tutakufa; na sisi tutakuwa salama.
8 Na kutakuwa pia na wengi ambao watasema: Kuleni, kunyweni na mshangilie;
walakini, mwogopeni Mungu—ataturuhusu kutenda dhambi kidogo; ndio,
danganya kidogo, tumieni wengine kwa sababu ya maneno yao, mchimbie jirani
yako shimo; hakuna hatia kwa haya; na mtende vitu hivi vyote, kwani kesho
tutakufa, na kama tutakuwa na hatia, Mungu atatuadhibu kwa mijeledi michache,
na mwishowe tutaokolewa katika ufalme wa Mungu.
9 Ndio, na kutakuwa na wengi watakaofundisha kwa namna hii, uwongo na
yasiyofaa na mafundisho ya kipumbavu, na watajifurisha mioyoni mwao, na
watajitahidi kumfichia Bwana mashauri yao; na matendo yao yatakuwa gizani.
10 Na damu ya watakatifu italia kutoka chini dhidi yao.
11 Ndio, wote wamepotea njia; wameharibika.
12 Kwa sababu ya kiburi, na kwa sababu ya walimu bandia, na mafundisho ya
bandia, makanisa yao yameharibika, na makanisa yao yamejiinua; kwa sababu ya
kiburi yamefura.
13 Wanawapora maskini kwa sababu ya makutaniko yao mazuri; wanawapora
maskini kwa sababu ya mavazi yao mazuri; na kuwatesa walio wapole na maskini
katika moyo, kwa sababu katika kiburi chao wamefura.
14 Wanakaza shingo zao na kufanya vichwa vyao kuwa na kiburi; ndio, na kwa
sababu ya kiburi, na uovu, na machukizo, na usherati, wote wamepotea ila tu
wachache, ambao ni wafuasi wanyenyekevu wa Kristo; walakini, wanaongozwa, na
inakuwa kwamba katika wakati mwingi wanakosea kwa sababu wanafunzwa kwa
mawaidha ya wanadamu.
15 Ee wenye hekima, na walioelimika, na matajiri, ambao wanajivuna kwa kiburi
cha roho zao, na wale wote wanaofunza mafundisho ya bandia, na wale wote
wanaofanya usherati, na kupindua njia zilizo sawa za Bwana, ole, ole, ole ni kwao,
asema Bwana Mungu Mwenyezi, kwani watatupwa jahanamu!

16 Ole kwa wale wanaokataa la haki kwa kitu kisichofaa na kushutumu kilicho
chema, na kusema kwamba hakina thamani! Kwani siku inafika ambapo Bwana
Mungu ataadhibu wakazi wa dunia kwa haraka; na katika siku ile ambayo watakuwa
wameiva kabisa katika maovu wataangamia.
17 Lakini tazama, kama wakazi wa dunia watatubu uovu wao na machukizo
hawataangamizwa, asema Bwana wa Majeshi.
18 Lakini tazama, kanisa lile kuu la machukizo, yule kahaba wa ulimwengu wote,
lazima aporomoke duniani, na kubwa utakuwa muanguko wake.
19 Kwani ufalme wa ibilisi lazima utetemeke, na wale ambao ni wake lazima
wavurugwe hadi watubu, au ibilisi atawafunga kwa minyororo yake isiyo na mwisho,
na wavurugwe, kwa hasira na waangamie.
20 Kwani tazama, katika siku ile atavuma mioyoni mwa watoto wa watu, na
awavuruge wakasirikie yale ambayo ni mema.
21 Na wengine atawapatanisha, na awapatie usalama wa kimwili, kwamba
watasema: Yote yako salama Sayuni; ndio, Sayuni inafanikiwa, yote ni mema—na
hivyo ibilisi anadanganya roho zao, na kuwapeleka kwa makini hadi jahanamu.
22 Na tazama, wengine atawadanganya, na kuwaambia kwamba hakuna jahanamu;
na kuwaambia: Mimi sio ibilisi, kwani hakuna yeyote—na anawanong'onezea hivyo
masikioni mwao, hadi awashike na minyororo yake miovu, kutoka ambapo hakuna
ukombozi.
23 Ndio, wamefungwa na mauti, na jahanamu; na mauti, na jahanamu, na ibilisi, na
wale wote ambao wameshikwa na hao lazima watasimama mbele ya kiti cha enzi cha
Mungu, na wahukumiwe kulingana na matendo yao, na kutoka hapo lazima waende
mahali walipotayarishiwa, hata kwenye ziwa la moto na kiberiti, ambayo ni mateso
yasiyo na mwisho.
24 Kwa hivyo, ole kwa yule anayestarehe Sayuni!
25 Ole kwa yule anayetangaza: Yote yako salama!
26 Ndio, ole kwa yule anayetii mawaidha ya wanadamu, na kukana nguvu za
Mungu, na kipawa cha Roho Mtakatifu!
27 Ndio, ole kwa yule anayesema: Tumepokea, na hatuhitaji zaidi!
28 Na mwishowe, ole kwa wale wote wanaotetemeka, na wanakasirika kwa sababu
ya ukweli wa Mungu! Kwani tazama, yule ambaye amejengwa katika mwamba
huyapokea kwa furaha; na yule aliyejengwa kwenye msingi wa mchanga hutetemeka
asije akaanguka.
29 Ole kwa yule atakayesema: Tumepokea neno la Mungu, na hatuhitaji mengine
zaidi ya maneno ya Mungu, kwani tuna ya kutosha!
30 Kwani tazama, hivi asema Bwana Mungu: Nitawapatia watoto wa watu mstari
juu ya mstari, amri juu ya amri, hapa kidogo na pale kidogo; na heri wale
wanaosikiza kanuni zangu, na kutii mashauri yangu, kwani watasoma hekima;
kwani kwa yule atakayepokea nitampatia zaidi; na kutoka kwa wale watakaosema,
Tuna ya kutosha, watapokonywa hata yale walio nayo.
31 Amelaaniwa yule ambaye anaweka imani yake kwa mwanadamu, au amfanyaye
kuwa mkono wake, au kusikiza kanuni za wanadamu, isipokuwa kanuni zao
zipeanwe na nguvu ya Roho Mtakatifu.
32 Ole kwa Wayunani, asema Bwana Mungu wa Majeshi! Ingawa nitawanyoshea
mkono wangu siku kwa siku, watanikana; walakini, nitawarehemu, asema Bwana
Mungu, kama watatubu na kunijia mimi; kwani mkono wangu umenyooshwa siku

yote, asema Bwana Mungu wa Majeshi.

## 2 Nefi 29

1 Lakini tazama, kutakuwa na wengi—katika siku ile ambayo nitaanza kutenda kazi
ya maajabu miongoni mwao, kwamba nikumbuke maagano yangu ambayo nilifanya
na watoto wa watu, kwamba ninyooshe mkono wangu tena mara ya pili kurudisha
watu wangu, ambao ni wa nyumba ya Israeli.
2 Na pia, ili nikumbuke ahadi nilizokuahidi wewe, Nefi, na pia kwa baba yako,
kwamba nitakumbuka uzao wako; na kwamba maneno ya uzao wako utatoka
kinywani mwangu hadi kwa uzao wako; na maneno yangu yatapigwa miunzi hadi
mwisho wa dunia, kwani itakuwa bendera kwa watu wangu, ambao ni wa nyumba
ya Israeli.
3 Na kwa sababu maneno yangu yatapigwa miunzi mbele—Wayunani wengi
watasema: Biblia! Biblia! Tunayo Biblia, na hakuwezi kuwako na Biblia nyingine.
4 Lakini Bwana Mungu asema hivi: Enyi wajinga, watapata Biblia; na itatoka kwa
Wayahudi, watu wangu wa kale wa maagano. Na wamewashukuru Wayahudi vipi
kwa ile Biblia waliyoipokea kutoka kwao? Ndio, Wayunani wanamaanisha nini? Je,
wanakumbuka shida, mateso, na maumivu ya Wayahudi, na bidii yao kwangu mimi,
katika kuwaletea Wayunani wokovu?
5 Ee nyinyi Wayunani, je, mmekumbuka Wayahudi, watu wangu wa kale wa
maagano? Hapana; lakini mmewalaani, na kuwachukia, na hamkutaka
kuwarudisha. Lakini tazama, nitarudisha vitu hivi vyote juu ya vichwa vyenu
wenyewe; kwani mimi Bwana sijasahau watu wangu.
6 Ewe mjinga, utakayesema: Biblia, tunayo Biblia, na hatuhitaji Biblia ingine. Je,
umepokea Biblia isipokuwa kwa Wayahudi?
7 Je, hujui kwamba kuna mataifa mengi zaidi ya moja? Je, hujui kwamba Mimi,
Bwana Mungu wako, nimeumba wanadamu wote, na kwamba nawakumbuka wale
ambao wako visiwani vya bahari; na kwamba ninatawala juu mbinguni na chini
duniani; na kwamba nitaleta mbele neno langu kwa watoto wa watu, ndio, hata
katika mataifa yote ya ulimwengu?
8 Kwa hivyo unanung'unika, kwa sababu mtapokea maneno yangu zaidi? Je,
hamjui kwamba ushuhuda wa mataifa mawili ni ushahidi kwenu kwamba mimi ni
Mungu, na kwamba nakumbuka taifa moja kama lingine? Kwa hivyo, nazungumzia
taifa moja maneno sawa na lingine. Na wakati mataifa mawili yatakapoishi pamoja
ushuhuda wa hayo mataifa mawili utaenda pia pamoja.
9 Ninafanya haya ili niwathibitishie wengi kwamba mimi ndiye yule yule jana, leo,
na milele; na kwamba ninazungumza maneno yangu nipendavyo. Na ati kwa sababu
nimenena neno moja hamna haja kudhani kwamba siwezi kunena lingine; kwani
kazi yangu bado haijakamilika; wala haitakamilika hadi mwisho wa mwanadamu,
wala kutoka wakati huo hadi milele.
10 Kwa hivyo, kwa sababu mna Biblia msidhani kwamba inayo maneno yangu yote;
wala hamna haja kudhani kwamba sijasababisha mengine kuandikwa.
11 Kwani ninawaamuru wanadamu wote, kutoka mashariki na magharibi, na
kaskazini, na kusini, na katika visiwa vya bahari, kwamba wataandika maneno
ambayo nitawazungumzia; kwani kutoka kwa vitabu ambavyo vitaandikwa
nitahukumu ulimwengu, kila mwanadamu kulingana na matendo yake, kulingana

na yale yaliyoandikwa.
12 Kwani tazama, nitawazungumzia Wayahudi na wataiandika; na pia
nitawazungumzia Wanefi na wataiandika; na pia nitazungumzia makabila mengine
ya nyumba ya Israeli, ambayo nimeyaongoza mbali, na wataiandika; na pia
nitazungumzia mataifa yote ya dunia na wataiandika.
13 Na itakuwa kwamba Wayahudi watapokea maneno ya Wanefi, na Wanefi
watapokea maneno ya Wayahudi; na Wanefi na Wayahudi watapokea maneno ya
makabila ya Israeli yaliyopotea; na makabila ya Israeli yaliyopotea yatapokea
maneno ya Wanefi na Wayahudi.
14 Na itakuwa kwamba watu wangu, ambao ni wa nyumba ya Israeli, watakusanywa
nyumbani katika nchi zao za kumiliki; na pia neno langu litakusanywa pamoja. Na
nitawaonyesha wale ambao wanapigana dhidi ya neno langu na dhidi ya watu
wangu, ambao ni wa nyumba ya Israeli, kwamba mimi ni Mungu, na kwamba
niliagana na Ibrahimu kwamba nitakumbuka uzao wake milele.

## 2 Nefi 30

1 Na sasa tazama, ndugu zangu wapendwa, nitawazungumzia; kwani mimi, Nefi,
sitakubali kwamba nyinyi mdhani kuwa nyinyi ni watakatifu zaidi ya vile Wayunani
watakavyokuwa. Kwani tazameni, msipotii amri za Mungu nyote mtaangamia pia;
na kwa sababu ya maneno ambayo yamezungumzwa msidhani kwamba Wayunani
wameangamizwa kabisa.
2 Kwani tazama, nawaambia kwamba kadiri Wayunani watakavyotubu wao
wanakuwa watu wa maagano wa Bwana; na kadiri wengi Wayahudi wasivyotubu
watatengwa; kwani Bwana haagani na yeyote ila tu wale wanaotubu na kumwamini
Mwana wake, ambaye ndiye Mtakatifu wa Israeli.
3 Na sasa, nitatoa unabii mchache zaidi kuhusu Wayahudi na Wayunani. Kwani
baada ya kitabu kile nilichokizungumzia kutokea, na kuandikiwa Wayunani, na
kutiwa muhuri tena katika Bwana, kutakuwa na wengi ambao wataamini maneno
yaliyoandikwa; na wao watayapelekea sazo la uzao wetu.
4 Na kisha sazo la uzao wetu litajua kutuhusu, vile tulivyotoka Yerusalemu, na
kwamba wao ni ukoo wa Wayahudi.
5 Na injili ya Yesu Kristo itatangazwa miongoni mwao; kwa hivyo, wao
watarejeshwa tena kwa ufahamu wa baba zao, na pia kwa ufahamu wa Yesu Kristo,
ambao ulikuwa miongoni mwa baba zao.
6 Na kisha watashangilia; kwani watajua kwamba ni baraka kwao kutoka mkono
wa Mungu; na magamba yao ya giza yataanza kuanguka kutoka macho yao; na vizazi
vingi havitapita miongoni mwao, ila tu watakuwa safi na watu wema.
7 Na itakuwa kwamba Wayahudi waliotawanyika wataanza kumwamini Kristo; na
wataanza kukusanyika katika uso wa nchi; na kadiri wengi watakavyomwamini
Kristo pia nao watakuwa watu wema.
8 Na itakuwa kwamba Bwana Mungu ataanza kazi yake miongoni mwa mataifa
yote, kabila, lugha, na watu, kuleta marejesho ya watu wake katika dunia.
9 Na kwa utakatifu Bwana Mungu atawahukumu maskini, na kuwakemea kwa
kiasi kwa walio wapole duniani. Na ataipiga dunia kwa fimbo ya kinywa chake; na
kwa pumzi ya midomo yake atawaua walio waovu.
10 Kwani wakati unafika upesi ambapo Bwana Mungu atasababisha mgawanyiko

mkuu miongoni mwa watu, na ataangamiza waovu; na atawahurumia watu wake,
ndio, hata kama lazima aangamize waovu kwa moto.
11 Na haki itakuwa mshipi wa viuno vyake, na uaminifu utakuwa mshipi wa mafigo
yake.
12 Na kisha mbwa mwitu ataaishi na mwanakondoo; na chui atalala na
mwanambuzi, na ndama, na mwana-simba, na kinono, pamoja; na mtoto mdogo
atawaongoza.
13 Na ng'ombe na dubu watakula; na watoto wao watalala pamoja; na simba atakula
majani kama ng'ombe.
14 Na mtoto anayenyonya atachezea katika tundu la nyoka sumu, na mtoto
aliyeachishwa atatia mkono wake kwenye pango la fira.
15 Hawatadhuru wala kuharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; maana dunia
itajawa na ufahamu wa Bwana kama vile maji yanavyofunika baharini.
16 Kwa hivyo, vitu vya mataifa yote vitajulikana; ndio, vitu vyote vitajulikana na
watoto wa watu.
17 Hakuna jambo ambalo ni la siri ambalo halitafunuliwa; hakuna kazi ya giza
ambayo haitafunuliwa katika nuru; na hakuna jambo lolote ambalo limetiwa
muhuri duniani ambalo halitafunguliwa.
18 Kwa hivyo, vitu vyote ambavyo vimewahi kufunuliwa watoto wa watu katika siku
ile vitafunuliwa; na Shetani hatakuwa na nguvu juu ya mioyo ya watoto wa watu
tena, kwa muda mrefu. Na sasa, ndugu zangu wapendwa, namalizia maneno yangu
hapo.

## 2 Nefi 31

1 Na sasa mimi, Nefi, namaliza kuwatolea unabii, ndugu zangu wapendwa. Na siwezi
kuandika isipokuwa tu vitu vichache, ambavyo najua kwa hakika lazima vitatimia;
wala siwezi kuandika isipokuwa tu maneno machache ya kaka yangu Yakobo.
2 Kwa hivyo, vitu ambavyo nimeandika vimenitosha, ila tu maneno machache
ambayo lazima niyazungumze kuhusu mafundisho ya Kristo; kwa hivyo,
nitawazungumzia kwa uwazi, kulingana na unyofu wangu ninapotoa unabii.
3 Kwani nafsi yangu inafurahia unyoofu; kwani kwa namna hii ndivyo Bwana
Mungu anavyotenda kazi miongoni mwa wanadamu. Kwani Bwana Mungu hutoa
nuru kwa ufahamu; kwani huzungumza na wanadamu kulingana na lugha yao, kwa
ufahamu wao.
4 Kwa hivyo, ningependa mkumbuke kwamba nimewahi kuwazungumzia kuhusu
yule nabii ambaye Bwana alinionyesha, kwamba atambatiza Mwanakondoo wa
Mungu, ambaye ataondoa dhambi za ulimwengu.
5 Na sasa, kama Mwanakondoo wa Mungu, akiwa mtakatifu, alihitaji kubatizwa
kwa maji, ili kutimiza utakatifu wote, Ee basi, jinsi gani tunahitaji zaidi sisi, tusio
watakatifu, kubatizwa, ndio, hata kwa maji!
6 Na sasa, ningewauliza nyinyi, ndugu zangu wapendwa, ni vipi Mwanakondoo wa
Mungu alitimiza utakatifu wote alipobatizwa kwa maji?
7 Je, hamjui kwamba alikuwa mtakatifu? Lakini ingawa alikuwa mtakatifu,
anawaonyesha watoto wa watu kwamba, kulingana na mwili anajinyenyekeza mbele
ya Baba, na kumshuhudia Baba kwamba yeye atakuwa mwaminifu kwake katika
kutii amri zake.

8 Kwa hivyo, baada ya kubatizwa kwa maji Roho Mtakatifu alimshukia katika umbo la njiwa.
9 Na tena, inaonyesha watoto wa watu unyofu wa njia, na wembamba wa lango, ambalo wataliingilia, baada ya yeye kuwatolea mfano.
10 Na akawaambia watoto wa watu: Nifuateni mimi. Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, je, tunaweza kumfuata Yesu tusipokubali kushika amri za Baba?
11 Na Baba alisema: Tubuni, tubuni, na mbatizwe katika jina la Mwana wangu Mpendwa.
12 Na pia, sauti ya Mwana ilinijia, ikisema: Yule anayebatizwa katika jina langu, atapewa Roho Mtakatifu na Baba, kama mimi; kwa hivyo, nifuateni, na mfanye vitu ambavyo mmeniona nikifanya.
13 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, najua kwamba kama mtamtii Mwana, kwa moyo wa lengo moja, bila unafiki na udanganyifu mbele yake Mungu, lakini kwa kusudi kamili, na kutubu dhambi zenu, mkishuhudia kwa Baba kwamba mnataka kujivika juu yenu jina la Kristo, kwa ubatizo—ndio, kwa kumfuata Bwana wenu na Mwokozi wenu chini majini, kulingana na neno lake, tazameni, ndipo mtapokea Roho Mtakatifu; ndio, kisha ubatizo wa moto na Roho Mtakatifu unakuja; na kisha mtaweza kuzungumza kwa lugha ya malaika, na kupiga kelele za sifa kwa yule Mtakatifu wa Israeli.
14 Lakini, tazama, ndugu zangu wapendwa, hivyo sauti ya Mwana ilinijia, ikisema: Baada ya kutubu dhambi zenu, na kushuhudia Baba kwamba mko tayari kutii amri zangu, kwa ubatizo wa maji, na kupokea ubatizo wa moto na wa Roho Mtakatifu, na kuzungumza kwa lugha mpya, ndio, hata lugha ya malaika, na baada ya haya mnikane, ingekuwa vyema kama hamkunifahamu.
15 Na nikasikia sauti kutoka kwa Baba, ikisema: Ndio, maneno ya Mpendwa wangu ni ya kweli na maaminifu. Yule atakayevumilia hadi mwisho, huyo ataokolewa.
16 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, najua kwamba bila ya mwanadamu kuvumilia hadi mwisho, kwa kufuata mfano wa Mwana wa Mungu aliye hai, hawezi kuokolewa.
17 Kwa hivyo, fanyeni vitu ambavyo nimewaambia nimeona kwamba Bwana wenu na Mkombozi wenu atatenda; kwani, nimeonyeshwa haya kwa lengo hili, ili mjue ni kwa lango gani mtakaloingilia. Kwani lango ambalo mtaingilia ni toba na ubatizo kwa maji; na kisha unakuja msamaha wa dhambi zenu kwa moto kwa Roho Mtakatifu.
18 Na kisha mnaingia katika njia hii nyembamba iliyosonga ambayo inaelekea uzima wa milele; ndio, mmeingia kwa hilo lango; mmetenda kulingana na amri za Baba na Mwana; na mmempokea Roho Mtakatifu, ambaye anawashuhudia Baba na Mwana, katika kutimiza ahadi ambayo ametoa, kwamba mkiingia kwa njia mtapokea.
19 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, baada yenu kuingia katika njia hii nyembamba na iliyosonga, nauliza je, yote yamekamilishwa? Tazama, nawaambia, Hapana; kwani hamjafika hapa ila tu kwa neno la Kristo na kwa imani isiyotingishika ndani yake, mkitegemea kabisa ustahili wa yule aliye mkuu kuokoa.
20 Kwa hivyo, lazima msonge mbele mkiwa na imani imara katika Kristo, mkiwa na mng'aro mkamilifu wa tumaini, na upendo kwa Mungu na wanadamu wote. Kwa hivyo, kama mtasonga mbele, mkila na kusherekea neno la Kristo, na mvumilie hadi mwisho, tazama, hivi ndivyo asema Baba: Mtapokea uzima wa milele.
21 Na sasa, tazama, ndugu zangu wapendwa, hii ndiyo njia; na hakuna njia nyingine

wala jina lililotolewa chini ya mbingu ambalo mwanadamu anaweza kuokolewa
katika ufalme wa Mungu. Na sasa, tazama, hili ndilo fundisho la Kristo, na
fundisho pekee na la kweli la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, ambao ni
Mungu mmoja, bila mwisho. Amina.

## 2 Nefi 32

1 Na sasa, tazama, ndugu zangu wapendwa, nadhani kwamba mnawaza machache
mioyoni mwenu kuhusu yale mtakayotenda baada ya kuingia kwa njia hiyo. Lakini,
tazama, kwa nini mnawaza vitu hivi mioyoni mwenu?
2 Je, hamkumbuki kwamba niliwaambia kwamba baada ya kupokea Roho
Mtakatifu mngezungumza kwa lugha ya malaika? Na sasa, vipi mngezungumza kwa
lugha ya malaika bila Roho Mtakatifu?
3 Malaika wanazungumza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu; kwa hivyo,
wanazungumza maneno ya Kristo. Kwa hivyo, niliwaambia, shiriki maneno ya
Kristo; kwani tazama, maneno ya Kristo yatawaelezea vitu vyote mnavyostahili
kutenda.
4 Kwa hivyo, na sasa baada ya kuzungumza maneno haya, kama hamwezi
kuyafahamu, ni kwa sababu hamuombi, wala kubisha; kwa hivyo, hamjaletwa
kwenye nuru, lakini lazima mwangamie gizani.
5 Kwani tazama, tena nawaambia kwamba kama mtaingia kwa njia hiyo, na
kupokea Roho Mtakatifu, atawaonyesha vitu vyote ambavyo mnastahili kutenda.
6 Tazameni, haya ndio mafundisho ya Kristo, na hakutakuwa na mafundisho
mengine yatakayotolewa hadi atakapojidhihirisha kwenu katika mwili. Na
atakapojithirihisha kwenu katika mwili, mtachunguza na kufanya vile vitu
atakavyowaambia.
7 Na sasa mimi, Nefi, siwezi kuzungumza zaidi; Roho anayokomesha
mazungumzo yangu, na ninaachwa kuomboleza kwa sababu ya kutoamini, na uovu,
na ujinga, na majivuno ya wanadamu; kwani hawatatafuta ufahamu, wala kuelewa
ufahamu wa juu, wanapoelezewa wazi wazi, hata wazi vile neno linaweza kuwa.
8 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, naona kwamba bado mnatafakari mioyoni
mwenu; na inanihuzunisha kwamba lazima nizungumze kuhusu kitu hiki. Kwani
ikiwa mtasikiliza Roho ambaye anawafunza wanadamu kusali, mtajua kwamba
lazima msali, kwani roho mchafu hawafunzi mwanadamu kusali, lakini humfunza
kwamba lazima asisali.
9 Lakini tazameni, nawaambia kwamba lazima msali kila wakati, na msife moyo;
na kwamba msifanye lolote kwa Bwana bila kumuomba Baba kwa jina la Kristo,
kwamba awatakasie matendo yenu, kwamba matendo yenu yawe ni kwa ajili ya
ustawi wa nafsi yako.

## 2 Nefi 33

1 Na sasa mimi, Nefi, siwezi kuandika vitu vyote ambavyo vilifundishwa miongoni
mwa watu wangu; wala mimi sio shujaa kwa kuandika, kama nilivyo katika
mazungumzo; kwani mwanadamu anapozungumza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu
uwezo wa Roho Mtakatifu huyapeleka katika mioyo ya watoto wa watu.

2 Lakini tazama, kuna wengi wanaoshupaza mioyo yao dhidi ya Roho Mtakatifu,
kwamba hana nafasi ndani yao; kwa hivyo, wanatupa vitu vingi ambavyo
vimeandikwa na kuvichukua kama vitu visivyofaa.
3 Lakini mimi, Nefi, nimeandika yale ambayo nimeandika, na kuyachukua kuwa
yenye thamani kuu, na zaidi kwa watu wangu. Kwani nawaombea siku zote kwa
mchana, na macho yangu huitia mto maji usiku, kwa sababu yao; na ninamlilia
Mungu wangu kwa imani, na ninajua kwamba atasikia kilio changu.
4 Na ninajua kwamba Bwana Mungu ataweka wakfu sala zangu kwa faidha ya watu
wangu. Na maneno ambayo nimeandika kwa unyonge yatatiwa nguvu kwao; kwani
inawashawishi kutenda mema; inawafahamisha wao kuhusu babu zao; na
inazungumza kuhusu Yesu, na kuwashawishi kumwamini, na kuvumilia hadi
mwisho, ambao ni uzima wa milele.
5 Na inazungumza kwa ukali dhidi ya dhambi, kulingana na vile ukweli ulivyo
wazi; kwa hivyo, hakuna mtu yeyote atakayekasirikia maneno ambayo nimeandika
ila tu awe na roho ya ibilisi.
6 Nafurahia kwa uwazi; nafurahia ukweli; namfurahia Yesu wangu, kwani
ameikomboa nafsi yangu kutoka jahanamu.
7 Nina hisani kwa watu wangu, na imani kuu katika Kristo kwamba nitakutana na
nafsi nyingi zisizokuwa na mawaa katika kiti chake cha hukumu.
8 Nina hisani kwa Myahudi — nasema Myahudi, kwa sababu nina maana kwamba
nilitoka huko.
9 Na pia nina hisani kwa Wayunani. Lakini tazama, siwezi kuwatumainia ila tu
wao wapatanishwe na Kristo, na kuingia katika lile lango jembamba, na watembee
katika njia ile iliyosonga inayoelekeza uzima wa milele, na waendelee katika njia
hiyo hadi mwisho wa siku ya majaribio.
10 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, na pia Myahudi, na nyinyi nyote mlio pande
zote za ulimwengu, sikilizeni maneno haya na mwamini katika Kristo; na kama
hamwamini katika maneno haya aminini katika Kristo. Na kama mtamwamini
Kristo mtaamini katika maneno haya, kwani ni maneno ya Kristo, na ameyapatia
kwangu; na yanafunza wanadamu wote kwamba wafanye mema.
11 Na kama sio maneno ya Kristo, amueni nyinyi — kwani Kristo atawaonyesha,
kwa uwezo na utukufu mkuu, kwamba ni maneno yake, katika siku ya mwisho; na
wewe na mimi tutasimama uso kwa uso kwenye baraza lake; na utajua kwamba
nimeamriwa na yeye kuandika vitu hivi, ingawa mimi ni mnyonge.
12 Na ninamuomba Baba kwa jina la Kristo kwamba wengi wetu, kama sio wote,
waokolewe katika ufalme wake siku ile kuu ya mwisho.
13 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, wale wote ambao ni wa nyumba ya Israeli, na
nyote hadi mwisho wa ulimwengu, nawazungumzia kama sauti inayolia kutoka
mavumbini: Kwa herini hadi siku ile kuu itakapofika.
14 Na wewe usiyekubali kupokea wema wa Mungu, na kuheshimu maneno ya
Wayahudi, na pia maneno yangu, na maneno yatakayotoka kutoka kinywa cha
Mwanakondoo wa Mungu, tazama, nakupigia kwaheri isiyo na mwisho, kwani
maneno haya yatakuhukumu siku ya mwisho.
15 Kwani yale ambayo ninayatia muhuri duniani, yataletwa dhidi yako katika baraza
la hukumu; kwani Bwana ameniamuru hivi, na ni lazima nitii. Amina.

# Kitabu cha Yakobo

## Kaka ya Nefi

*Maneno aliyowahubiria ndugu zake. Anamfadhaisha mtu aliyetaka kupindua mafundisho ya Kristo. Maneno machache kuhusu historia ya watu wa Nefi.*

## Yakobo 1

1 Kwani tazama, ikawa kwamba miaka hamsini na mitano ilikuwa imepita tangu Lehi
atoke Yerusalemu; kwa hivyo, Nefi alinipatia mimi, Yakobo, amri kuhusu bamba zile
ndogo, ambako vitu hivi vimechorwa.
2 Na akanipatia mimi, Yakobo, amri kwamba niandike kwenye bamba hizi vitu
vichache ambavyo nilivifikiria kuwa vyenye thamani; na kwamba nisiguse, ila
kidogo tu, kuhusu historia ya hawa watu wanaoitwa watu wa Nefi.
3 Kwani alisema kwamba historia ya watu wake iandikwe kwenye zile bamba zake
zingine, na kwamba nihifadhi bamba hizi na kupokelezea uzao wangu, kutoka
kizazi hadi kizazi.
4 Na kama kulikuwa na mahubiri yaliyo matakatifu, au ufunuo ulio mkuu, au
kutoa unabii, kwamba nichore yaliyo muhimu katika bamba hizi, na niyagusie sana
kama iwezekanavyo, kwa ajili ya Kristo, na kwa faida ya watu wetu.
5 Kwani kwa sababu ya imani na wasiwasi mwingi, kwa hakika tulidhihirishiwa,
kuhusu vile vitu vitakavyowapata watu wetu.
6 Na pia tulikuwa na ufunuo mwingi, na roho ya unabii mwingi; kwa hivyo, tulijua
kuhusu Kristo na ufalme wake, utakaokuja.
7 Kwa hivyo tulifanya kazi kwa bidii miongoni mwa watu wetu, kwamba
tuwashawishi waje kwa Kristo, na waonje wema wa Mungu, ili waingie katika
pumziko lake, na ili kwa njia yoyote asiape katika ghadhabu yake kwamba
hawataingia ndani, kama walivyomtia hasira katika siku za majaribio wakati wana
wa Israeli walipokuwa nyikani.
8 Kwa hivyo, tunatamani kutoka kwa Mungu kama ingewezekana kwamba
tungewashawishi wanadamu wote wasimwasi Mungu, kumtia hasira, lakini kwamba
watu wote wangemwamini Kristo, na kutafakari kuhusu kifo chake, na kubeba
msalaba wake na kuchukua aibu ya ulimwengu; kwa hivyo, mimi, Yakobo,
najichukulia kutimiza amri ya kaka yangu Nefi.
9 Sasa Nefi akaanza kuzeeka, na akajua kwamba anakaribia kufariki; kwa hivyo,
akamtia mtu mafuta awe mfalme na mtawala juu ya watu wake sasa, kulingana na
utawala wa wafalme.
10 Watu walikuwa wamempenda Nefi sana, kwa vile alikuwa mlinzi wao mkuu, na
kuupunga upanga wa Labani kwa ulinzi wao, na alikuwa ametumikia kwa ustawi
wao katika maisha yake yote—
11 Kwa hivyo, watu walitaka kulikumbuka jina lake. Na yeyote atakayetawala baada
yake watu walimwita, Nefi wa pili, Nefi wa tatu, na kadhalika, kulingana na utawala
wa wafalme; na hivyo ndivyo walivyoitwa na watu, haidhuru jina lolote walilokuwa

nalo.
12 Na ikawa kwamba Nefi alifariki.
13 Sasa wale watu ambao hawakuwa Walamani walikuwa Wanefi; walakini, waliitwa
Wanefi, Wayakobo, Wayusufu, Wazoramu, Walamani, Walemueli, na Waishmaeli.
14 Lakini mimi, Yakobo, hapa baadaye sitawapambanua kwa haya majina, lakini
wale wanaotaka kuangamiza watu wa Nefi nitawaita Walamani, na wale ambao ni
marafiki wa Nefi nitawaita Wanefi, au watu wa Nefi, kulingana na utawala wa
wafalme.
15 Na sasa ikawa kwamba watu wa Nefi, chini ya utawala wa mfalme wa pili,
walianza kuwa wagumu mioyoni mwao, na kujihusisha katika matendo maovu,
kama vile Daudi wa kale wakitamani wake wengi na makahaba, na pia mwana wake,
Sulemani.
16 Ndio, na hata pia wakaanza kutafuta dhahabu na fedha nyingi, na wakaanza
kuinuliwa katika kiburi.
17 Kwa hivyo mimi, Yakobo, niliwapatia maneno haya nilipowafundisha katika
hekalu, nikiwa nimepokea kwanza mwito wangu kutoka kwa Bwana.
18 Kwani mimi, Yakobo, na kaka yangu Yusufu tulikuwa tumetengwa tuwe
makuhani na walimu kwa watu hawa, kwa mkono wa Nefi.
19 Na tuliadhimisha ofisi yetu kwa Bwana, tukijichukulia jukumu, na wajibu wa
dhambi za watu vichwani mwetu kama hatungewafunza neno la Mungu kwa bidii
yote; kwa hivyo, tulitumikia kwa uwezo wetu ili damu yao isiwe katika mavazi yetu;
la sivyo, damu yao ingekuwa katika mavazi yetu, na hatungepatikana bila alama
katika siku ile ya mwisho.

## Yakobo 2

1 Maneno ambayo Yakobo, kaka ya Nefi, aliwazungumzia watu wa Nefi, baada ya kifo
cha Nefi:
2 Sasa, ndugu zangu wapendwa, mimi, Yakobo, kulingana na jukumu langu kwa
Mungu, kutukuza ofisi yangu kwa ufahamu, na ili niyaondolee mavazi yangu
dhambi zenu, naja hapa hekaluni siku hii ili niwatangazie neno la Mungu.
3 Na nyinyi mnajua mpaka sasa kwamba nimekuwa na bidii katika ofisi
niliyoitiwa; lakini siku ya leo nimelemewa sana kwa hamu na wasiwasi wa ustawi wa
nafsi zenu zaidi ya vile nilivyokuwa hapo awali.
4 Kwani tazama, hadi sasa, mmekuwa watiifu kwa neno la Bwana, ambalo
nimewapatia.
5 Lakini tazama, nisikilizeni mimi, na mjue kwamba kwa usaidizi wa Muumba wa
mbingu na dunia na aliye na uwezo wote naweza kuwaambia kuhusu mawazo yenu,
jinsi vile mmeanza kutumikia katika dhambi, dhambi ambayo ni ya machukizo zaidi
kwangu, ndio, na ya machukizo kwa Mungu.
6 Ndio, inahuzunisha nafsi yangu na kunisababisha nijitenge kwa aibu mbele ya
uwepo wa Muumbaji wangu, kwamba lazima niwashuhudie kuhusu uovu wa mioyo
yenu.
7 Na pia inanihuzunisha kwamba lazima nitumie maneno makali nikizungumza
kuwahusu, mbele za wake zenu na watoto wenu, ambao wengi wao mawazo yao ni
mepesi sana na yenye unyoofu na ya kuvutia mbele ya Mungu, kitu ambacho ni cha
kupendeza kwa Mungu;

8 Na nimedhania kwamba wamekuja kusikia neno la kupendeza la Mungu, ndio,
neno ambalo linaponya nafsi iliyojeruhiwa.
9 Kwa hivyo, inahuzunisha nafsi yangu kwamba ninashurutishwa, kwa sababu ya
amri kali ambayo nimepokea kutoka kwa Mungu, kuwaonya kulingana na makosa
yenu, kupanua vidonda vya wale ambao wamejeruhiwa, badala ya kuwafariji na
kuponya vidonda vyao; na wale ambao hawajajeruhiwa, badala ya kujiburudisha
kwa neno la kupendeza la Mungu wamewekewa visu vidunge nafsi zao na kujeruhi
mawazo yao mepesi.
10 Lakini, ingawa kazi hii ni kuu, lazima nitende kulingana na amri kali za Mungu,
na niwaambie kuhusu uovu wenu na machukizo yenu, katika uwepo wa walio safi
moyoni, na moyo uliopondeka, na chini ya tazamo la jicho lenye kupenya la
Mwenyezi Mungu.
11 Kwa hivyo, lazima niwaambie ukweli kulingana na udhahiri wa neno la Mungu.
Kwani tazama, nilipokuwa nikimuomba Bwana, neno likanijia hivi, likisema:
Yakobo, kesho uende hekaluni, na uwatangazie watu neno nitakalokupatia.
12 Na sasa tazameni, ndugu zangu, hili ndilo neno ambalo nawatangazia, kwamba
wengi wenu mmeanza kutafuta dhahabu, na fedha, na kila aina ya mawe yenye
madini, ambayo yamejaa tele, katika nchi hii, ambayo ni nchi ya ahadi kwenu na
kwa uzao wenu.
13 Na mkono wa majaliwa umewapendelea sana, hata kwamba mmepata utajiri
mwingi; na kwa sababu wengine wenu mmepata tele zaidi kuliko ndugu zenu
mmejiinua juu kwa kiburi cha mioyo yenu, na kukaza shingo zenu na kuinua vichwa
vyenu kwa sababu ya mavazi yenu yenye gharama, na kuwatesa ndugu zenu kwa
sababu mnadhani kwamba nyinyi ni bora kuliko wao.
14 Na sasa, ndugu zangu, je, mnadhani kwamba Mungu anawakubalia katika kitu
hiki? Tazama, nawaambia, Hapana. Lakini anawahukumu, na mkiendelea katika
vitu hivi lazima hukumu zake ziwateremkie kwa haraka.
15 Ee kwamba angewaonyesha kuwa anaweza kuwadunga, na kwa tazamo moja la
jicho lake anaweza kuwaangusha mchangani!
16 Ee kwamba angewaondolea uovu huu na chukizo. Na, Ee kwamba mngesikiliza
neno la amri zake, na msikubali hiki kiburi cha mioyo yenu kuangamiza nafsi zenu.
17 Fikirieni ndugu zenu jinsi mnavyojifikiria nyinyi wenyewe, na mfanye urafiki na
wote na muwe wakarimu katika utajiri wenu, ili nao wawe matajiri kama nyinyi.
18 Lakini kabla ya kutafuta utajiri, tafuteni ufalme wa Mungu.
19 Na baada ya kupokea tumaini katika Kristo mtapokea utajiri, kama mtautafuta;
na mtautafuta kwa kusudi la kutenda mema — kuvisha walio uchi, na kulisha wenye
njaa, na kuwakomboa wafungwa, na kuwatolea msaada walio wagonjwa na
wanaoteseka.
20 Na sasa, ndugu zangu, nimewazungumzia kuhusu kiburi; na wale wenu ambao
mmetesa jirani yenu, na kumdhulumu kwa sababu mlikuwa na kiburi mioyoni
mwenu, kwa sababu ya vitu vile ambavyo Mungu amewapatia, je, mnasema nini?
21 Je, hamdhani kwamba vitu kama hivi ni vya kuchukiza kwa yule aliyeumba watu
wote? Na mwanadamu mmoja ni mwenye thamani machoni mwake kama
mwingine. Na wanadamu wote wametoka mavumbini; na aliwaumba kwa kusudi
moja, kwamba watii amri zake na kumtukuza milele.
22 Na sasa ninakoma kuwazungumzia kuhusu kiburi hiki. Na kama sio lazima
kwamba niwazungumzie kuhusu makosa makuu zaidi, moyo wangu ungeweza

kushangilia sana kwa sababu yenu.

23 Lakini neno la Mungu linanipatia mzigo kwa sababu ya dhambi zenu kuu: Kwani tazama, Bwana asema hivi: Watu hawa wanaanza kutenda uovu; hawafahamu maandiko, kwani wanatafuta kisingizio cha kutenda usherati, kwa sababu ya vile vitu vilivyoandikwa kuhusu Daudi, na Sulemani mwana wake.

24 Tazama, Daudi na Sulemani kwa hakika walikuwa na wake wengi na makahaba, kitu ambacho kilikuwa cha kuchukiza mbele yangu, asema Bwana.

25 Kwa hivyo, Bwana asema hivi, nimewaongoza watu hawa kutoka nchi ya Yerusalemu, kwa uwezo wa mkono wangu, ili niinue tawi takatifu kutoka kwa matunda ya viuno vya Yusufu.

26 Kwa hivyo, mimi Bwana Mungu sitakubali kwamba watu hawa watende kama wale wa kale.

27 Kwa hivyo, ndugu zangu, nisikilizeni, na mtii neno la Bwana: Kwani hakuna mtu yeyote miongoni mwenu ambaye atakuwa na mke zaidi ya mmoja; wala hatakuwa na masuria;

28 Kwani mimi, Bwana Mungu, nafurahia usafi wa kimwili wa wanawake. Na ukahaba ni chukizo mbele yangu; ndivyo hivi Bwana wa Majeshi anavyosema.

29 Kwa hivyo, watu hawa watatii amri zangu, asema Bwana wa Majeshi, la sivyo nchi italaaniwa kwa sababu yao.

30 Kwani kama, nitainua kizazi kwangu, asema Bwana wa Majeshi, nitawaamuru watu wangu; la sivyo, watatii vitu hivi.

31 Kwani tazama, mimi, Bwana, nimeona huzuni, na kusikia maombolezi ya mabinti za watu wangu katika nchi ya Yerusalemu, ndio, na katika nchi zote za watu wangu, kwa sababu ya uovu na machukizo ya mabwana wao.

32 Na sitakubali, asema Bwana wa Majeshi, kwamba vilio vya mabinti wazuri wa hawa watu, ambao niliwaongoza kutoka nchi ya Yerusalemu, kunifikia mimi kwa sababu ya wanaume wa watu wangu, asema Bwana wa Majeshi.

33 Kwani hawatawapeleka utumwani mabinti za watu wangu kwa sababu ya upole wao, la sivyo nitawaadhibu kwa laana kali, hata kuwaangamiza; kwani hawatatenda usherati, kama wale wa kale, asema Bwana wa Majeshi.

34 Na sasa tazameni, ndugu zangu, mnajua kwamba hizi amri zilitolewa kwa baba yetu, Lehi; kwa hivyo, mlizijua hapo awali; na mmepokea hukumu kuu; kwani mmetenda vitu hivi ambavyo hamkustahili kutenda.

35 Tazama, mmetenda maovu makuu kuliko Walamani, ndugu zetu. Mmevunja mioyo ya wake zenu wapole, na kuvunja tumaini la watoto wenu, kwa sababu ya mifano miovu mbele yao; na vilio vya mioyo yao kwa sababu yenu vinamfikia Mungu. Na kwa sababu ya ukali wa neno la Mungu, unaoshuka dhidi yenu, mioyo mingi ilikufa, ikiwa imedungwa na vidonda vikubwa.

## Yakobo 3

1 Lakini tazama, mimi, Yakobo, nitawazungumzia wale walio safi moyoni. Mtegemeeni Mungu kwa mawazo yenu yote, na mmuombe, kwa imani kuu, na atawafariji katika mateso yenu, na atatetea kesi yenu, na kuwateremshia hukumu wale wanaotaka kuwaangamiza.

2 Ee nyinyi nyote mlio safi moyoni, inueni vichwa vyenu na kupokea neno la kupendeza la Mungu, na kusherekea upendo wake; kwani mnaweza, kama mawazo

yenu yatakuwa imara, daima.
3 Lakini, ole, ole, kwa nyinyi msio safi moyoni, wale ambao ni wachafu mbele ya Mungu leo; kwani msipotubu nchi italaaniwa kwa sababu yenu; na Walamani, ambao sio wachafu kama nyinyi, walakini wamelaaniwa kwa laana kali, watawadhulumu hadi wawaangamize.
4 Na wakati unafika haraka, kwamba msipotubu watamiliki nchi yenu ya urithi, na Bwana Mungu atawaondoa wenye haki miongoni mwenu.
5 Tazameni, Walamani ndugu zenu, ambao mnawachukia kwa sababu ya uchafu wao na laana ambayo imeshika ngozi zao, ni watakatifu zaidi yenu; kwani hawajasahau amri ya Bwana, ambayo ilipewa kwa baba yetu — kwamba waoe mke mmoja pekee, na wasiwe na makahaba, na wasitende usherati miongoni mwao.
6 Na sasa, wanatii amri hii kwa bidii; kwa hivyo, kwa sababu ya huu utiifu, katika kuweka amri hii, Bwana Mungu hatawaangamiza, lakini atawarehemu; na siku moja watakuwa watu wenye baraka.
7 Tazama, mabwana zao wanawapenda wake zao, na wake zao wanawapenda mabwana zao; na mabwana zao na wake zao wanawapenda watoto wao; na kutoamini kwao na chuki yao kwenu ni kwa sababu ya uovu wa baba zao; kwa hivyo, je, nyinyi ni wema zaidi yao, machoni pa Muumba wenu mkuu?
8 Enyi ndugu zangu, nawahofia kwamba msipotubu dhambi zenu ngozi zao zitakuwa nyeupe zaidi yenu, mtakapoletwa pamoja na wao mbele ya kiti cha enzi cha Mungu.
9 Kwa hivyo, nawapatia amri, ambayo ni neno la Mungu, kwamba msiwachukie tena kwa sababu ya weusi wa ngozi zao; wala hamtawachukia kwa sababu ya uchafu wao; lakini mtakumbuka uchafu wenu wenyewe, na kukumbuka kwamba uchafu wao ulitokana na baba zao.
10 Kwa hivyo, mtakumbuka watoto wenu, jinsi mlivyodhulumu mioyo yao kwa sababu ya mfano mliowapatia; na pia, kumbukeni kwamba mnaweza, kwa sababu ya uchafu wenu, kuwatia watoto wenu katika maangamizo, na dhambi zao zitakuwa vichwani vyenu katika siku ya mwisho.
11 Ee ndugu zangu, sikilizeni maneno yangu; amsheni fahamu za nafsi zenu; jitingisheni ili muamke kutoka katika usingizi wa kifo; na mjifungue kutoka katika uchungu wa jahanamu ili msiwe malaika wa ibilisi, na kutupwa katika ziwa la moto na kiberiti ambalo ni mauti ya pili.
12 Na sasa mimi, Yakobo, niliwazungumzia watu wa Nefi vitu vingi zaidi nikiwaonya wasitende uasherati na tamaa, na kila aina ya dhambi, na kuwaelezea matokeo yao.
13 Na haiwezakani kuandika hata asilimia moja ya yale yaliotendwa na watu hawa, ambao waliongezeka kuwa wengi, katika bamba hizi; lakini matendo yao mengi yameandikwa katika zile bamba kubwa, na vita vyao, na mabishano yao, na utawala wa wafalme wao.
14 Bamba hizi zinaitwa bamba za Yakobo, na zilitengenezwa kwa mkono wa Nefi. Na ninakoma kuzungumza maneno haya.

## Yakobo 4

1 Tazama sasa, na ikawa kwamba mimi, Yakobo, nikiwa nimewahudumia watu wangu sana kwa kunena, (na siwezi kuandika ila tu maneno machache, kwa sababu ya

ugumu wa kuchora maneno yetu kwenye bamba) na tunajua kwamba vitu ambavyo tunaandika kwenye bamba hizi lazima vitadumu;

2 Lakini vitu vyovyote tunavyoandika kwenye kitu kingine isipokuwa kwenye bamba lazima viangamie na kutoweka; lakini tunaweza kuandika maneno machache kwenye bamba, ambayo yatawapatia watoto wetu, na pia ndugu zetu wapendwa, kiasi kidogo cha ufahamu kutuhusu sisi, au kuhusu baba zao—

3 Sasa tunafurahia kitu hiki; na tunatumikia kwa bidii kuchora maneno haya kwenye bamba, tukitumai kwamba ndugu zetu wapendwa na watoto wetu watayapokea kwa mioyo ya shukrani, na kuyatazamia ili wajifunze kwa shangwe na sio kwa huzuni, wala kwa dharau, yanayowahusu wazazi wao wa kwanza.

4 Kwani, kwa madhumuni haya tumeandika vitu hivi, ili wajue kwamba tulijua kuhusu Kristo, na tulikuwa na matumaini ya utukufu wake miaka mia mingi kabla ya kuja kwake; na sio tu sisi pekee tuliokuwa na tumaini la utukufu wake, lakini pia manabii wote watakatifu ambao walikuwa mbele yetu.

5 Tazama, walimwamimi Kristo na kumwabudu Baba katika jina lake, na pia sisi tunamwabudu Baba katika jina lake. Na kwa madhumuni haya tunatii sheria ya Musa, ambayo inaelekeza nafsi zetu kwake; na kwa lengo hili imetakaswa kwetu sisi ili tuwe wenye haki, hata kama vile ilivyochukuliwa kwa Ibrahimu huko nyikani awe mtiifu kwa amri za Mungu kwa kumtoa mwana wake Isaka awe sadaka, ambayo ilikuwa ni mfano wa Mungu na Mwana wake wa Pekee.

6 Kwa hivyo, tunawachunguza manabii, na tunao ufunuo mwingi na roho ya unabii; pamoja na mashahidi hawa wote tunapokea tumaini, na imani yetu haiwezi kutingishwa, hadi kwamba kwa kweli tunaweza kuamuru katika jina la Yesu na miti itutii, au milima, au mawimbi ya bahari.

7 Walakini, Bwana Mungu hutuonyesha unyonge wetu ili tujue kwamba ni kwa neema yake, na ufadhili wake mkuu kwa watoto wa watu, kwamba tunao uwezo wa kutenda vitu hivi.

8 Tazama, kazi za Bwana ni kuu na za kushangaza. Jinsi gani zilivyofichika siri zake; na haiwezekani kwamba mwanadamu agundue njia zake zote. Na hakuna mwanadamu yeyote ajuaye njia zake bila kufunuliwa kwake; kwa hivyo, ndugu, msidharau ufunuo wa Mungu.

9 Tazama kwani, kwa nguvu za neno lake mwanadamu alikuja usoni mwa dunia, dunia ambayo iliumbwa kwa nguvu za neno lake. Kwa hivyo, kama Mungu aliweza kuzungumza na ulimwengu ukawepo, na kuzungumza na mwanadamu akaumbwa, Ee basi, kwa nini asiweze kuamuru dunia, au kazi ya mikono yake usoni mwa ulimwengu, kulingana na nia yake na raha yake?

10 Kwa hivyo, ndugu, msijaribu kumshauri Bwana, lakini mpokee ushauri kutoka mkono wake. Kwani tazama, nyinyi wenyewe mnajua kwamba anatoa ushauri juu ya kazi yake yote kwa hekima, na kwa haki, na kwa rehema kuu.

11 Kwa hivyo, ndugu wapendwa, patanishweni na yeye kwa upatanisho wa Kristo, Mwana wake wa Pekee, na mnaweza kupokea ufufuo, kulingana na nguvu za ufufuo ambazo zimo katika Kristo, na mkabidhiwe kama malimbuko ya Kristo kwa Mungu, mkiwa na imani, na kupokea tumaini jema la utukufu kwake kabla hajajidhihirisha katika mwili.

12 Na sasa, wapendwa, msishangae kwamba ninawaambia vitu hivi; kwani kwa nini isizungumziwe upatanisho wa Kristo, na kupata ufahamu kamili kwake, ili kupokea ufahamu wa ufufuo na ulimwengu ujao?

13 Tazameni, ndugu zangu, yule anayetoa unabii, hebu yeye atoe unabii wa
kueleweka na wanadamu; kwani Roho huzungumza ukweli wala sio uwongo. Kwa
hivyo, huzungumza kuhusu vile vitu vilivyo, na vile vitu vitavyokuwa; kwa hivyo,
tunadhihirishiwa vitu hivi wazi wazi, kwa wokovu wa nafsi zetu. Lakini tazama, sisi
sio mashahidi wa pekee katika vitu hivi; kwani Mungu alivizungumza pia kwa
manabii wa kale.
14 Lakini tazama, Wayahudi walikuwa ni watu wenye shingo ngumu; na walidharau
maneno yaliyokuwa wazi, na wakawaua manabii, na wakatafuta vitu ambavyo
hawakuweza kufahamu. Kwa hivyo, kwa sababu ya upofu wao, upofu ambao
ulitokana na kuangalia zaidi ya lengo, lazima waanguke; kwani Mungu ameuondoa
udhahiri wake kutoka kwao, na kuwapatia wao vitu vingi ambavyo hawawezi
kufahamu, kwa sababu walivitamani. Na kwa sababu walivitamani Mungu
alivitenda, ili wajikwaze.
15 Na sasa mimi, Yakobo, naongozwa na Roho kwa kutoa unabii; kwani ninahisi
kwa matendo ya Roho aliye ndani yangu, kwamba kwa kujikwaa kwa Wayahudi
watalikataa jiwe ambalo wangejenga juu yake na kuwa na msingi salama.
16 Lakini tazama, kulingana na maandiko, jiwe hili litakuwa lile kuu, na la mwisho,
na msingi wa kweli ambao ni wa pekee, ambao Wayahudi kuweza kujenga juu yake.
17 Na sasa, wapendwa wangu, itawezekanaje, baada ya hawa kukataa msingi wa
kweli, kuweza kujenga juu yake, kwamba uwe kichwa cha pembe yao?
18 Tazameni, ndungu zangu wapendwa, nitawafunulia siri hii; kama sitatingishwa,
vyovyote, kutokana na msimamo wangu wa Roho, na kujikwaa kwa sababu ya
wasiwasi wangu juu yenu.

## Yakobo 5

1 Tazameni, ndugu zangu, hamkumbuki mliposoma maneno ya nabii Zeno, ambayo
alizungumzia nyumba ya Israeli, akisema.
2 Sikilizeni, Ee nyinyi nyumba ya Israeli, na msikie maneno yangu, nabii wa Bwana.
3 Kwani tazama, hivi ndivyo asema Bwana, nitakulinganisha, Ee nyumba ya Israeli,
na mzeituni uliochukuliwa na mtu na akaulisha shambani mwake; na ukakua, na
kuzeeka, na ukaanza kuoza.
4 Na ikawa kwamba bwana wa shamba akaenda mbele, na akaona kwamba
mzeituni wake ulianza kuoza; na akasema: Nitaupogoa, na kuupalilia, na kuulisha,
ili pengine uchipuke matawi yaliyo mazuri, na usiangamie.
5 Na ikawa kwamba aliupogoa, na kuupalilia, na kuulisha kulingana na neno lake.
6 Na ikawa kwamba baada ya siku nyingi ukaanza kutoa matawi machache,
machanga na yaliyo nyororo; lakini tazama, kilele chake kikaanza kuangamia.
7 Na ikawa kwamba mwenye shamba akaliona, na akamwambia mtumishi wake:
inanihuzunisha kwamba nitaupoteza mti huu; kwa hivyo, nenda ukate matawi
kutoka mchekele, na uyalete hapa kwangu; na tutayagoboa yale matawi yake ya kati
ambayo yameanza kukauka, na tutayatia motoni ili yachomeke.
8 Na tazama, asema Bwana wa shamba, ninaondoa matawi haya mengi yaliyo
machanga na miororo, na nitayapandikiza popote ninapotaka; na haidhuru kama
mzizi wa mti huu utaangamia, Nitajihifadhia matunda yake; kwa hivyo, nitachukua
matawi haya machanga na miororo, na nitayapandikiza popote nitakapo.
9 Chukua ewe matawi mchekele, na uyapandikize, badala yake; na haya ambayo

nimeyagoboa nitayatupa motoni na kuyachoma, ili yasikwaze mchanga wa shamba
langu.
10 Na ikawa kwamba mtumishi wa Bwana wa shamba alitenda kulingana na neno la
Bwana wa shamba, na akapandikiza matawi mchekele.
11 Na Bwana wa shamba akasababisha kwamba ipaliliwe, na ipogolewe, na ilishwe,
akimwambia mtumishi wake: Inanihuzunisha kwamba nitaupoteza mti huu; kwa
hivyo, ili pengine nihifadhi mizizi yake ili isiangamie, na ili nijihifadhie, nimetenda
kitu hiki.
12 Kwa hivyo, fuata njia yako; chunga mti, na uulishe, kulingana na maneno yangu.
13 Na haya nitayaweka katika sehemu ya mbali shambani mwangu, mahali popote
nitakapo, na haikuhusu wewe; na ninaitenda ili nijihifadhie matawi ya asili ya ule
mti; na pia, kwamba nijiwekee, akiba ya matunda wakati wa majira; kwani
inanihuzunisha kwamba nitapotelewa na mti huu na matunda yake.
14 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba akaenda njia zake, na akaficha matawi ya
kiasili ya ule mzeituni sehemu za mbali za shamba, mingine hapa na mingine pale,
kulingana na nia yake na raha yake.
15 Na ikawa kwamba muda mrefu ukapita, na Bwana wa shamba akamwambia
mtumishi wake: Njoo, hebu twende shambani, ili tufanye kazi shambani.
16 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba, na pia yule mtumishi, walienda shambani
kufanya kazi. Na ikawa kwamba yule mtumishi akamwambia bwana wake: Tazama,
angalia hapa; tazama ule mti.
17 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba aliangalia na kuona ule mti ambao yale
matawi ya mchekele yalikuwa yamepandikizwa; na ulikuwa umeanza kuota na
kuanza kuzaa matunda. Na akaona kwamba ni mazuri; na matunda yake yalikuwa
kama matunda ya kawaida.
18 Na akamwambia yule mtumishi: Tazama, matawi ya ule mti wa mwituni
yametoa umande kutoka mzizi wake, kwamba mzizi wake umeleta nguvu nyingi; na
kwa sababu ya nguvu hizo nyingi za mzizi yale matawi ya mwituni yamezaa matunda
ya kinyumbani. Sasa, kama hatungepandikiza haya matawi, ule mti ungeangamia.
Na sasa, tazama, nitaweka matunda mengi, ambayo yamezaliwa na ule mti; na
matunda yake nitajiwekea akiba, kwa wakati wa majira.
19 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba akamwambia mtumishi: Njoo, twende
katika sehemu za mbali za shamba, na tutazame kama matawi ya mti hayajazaa
matunda mengi pia, ili nijiwekee akiba, mimi mwenyewe.
20 Na ikawa kwamba walienda pale pahali ambapo yule bwana alikuwaameficha
matawi ya ule mti wa kawaida, na akamwambia yule mtumishi: Tazama haya; na
akaona ule wa kwanza kwamba ulikuwa umezaa matunda mengi; na akaona pia
kwamba yalikuwa mazuri. Na akamwambia yule mtumishi: Chukua matunda yake,
na uyaweke kama akiba wakati wa majira, ili nijihifadhie, kwani tazama, akasema,
nimeulisha kwa muda huu wote, na umezaa matunda mengi.
21 Na ikawa kwamba yule mtumishi akamwambia bwana wake: Kwa nini ulikuja
kupanda mti huu hapa, au tawi la mti huu? Kwani tazama, palikuwa ndipo pahali
pabovu katika shamba lako lote.
22 Na Bwana wa shamba akamwambia: Usinipatie mawaidha; nilijua kwamba
palikuwa ni pahali pabovu shambani; ndivyo, nikakwambia, nimeulisha huu muda
mrefu, na wewe unaona kwamba umezaa matunda mengi.
23 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba akamwambia mtumishi wake: Tazama

hapa; tazama nimepanda tawi lingine la mti pia; na wewe unajua kwamba pahali
hapa ni pabovu zaidi ya pale pa mwanzo. Lakini, tazama mti. Nimeulisha kwa muda
huu mrefu, na umezaa matunda mengi; kwa hivyo, uyavune, na uyaweke kama
hazina wakati wa majira, ili nijiihifadhie mimi mwenyewe.
24 Na ikawa kwamba yule Bwana wa shamba akamwambia tena mtumishi wake:
Tazama hapa; na uone tawi lingine, ambalo pia nimelipanda; tazama pia
nimelilisha, na limezaa matunda.
25 Na akamwambia mtumishi: Tazama hapa na uone la mwisho. Tazama,
nimepanda hili pahali pema pa shamba; na nimelilisha kwa muda huu mrefu, na
sehemu moja pekee ya mti imezaa matunda ya kinyumbani, na sehemu ingine ya mti
imezaa matunda ya mwituni; tazama, nimeulisha mti huu kama yale mengine.
26 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba akamwambia mtumishi wake: Chuma yale
matawi ambayo hayajazaa matunda mema, na uyatupe motoni.
27 Lakini tazama, yule mtumishi akamwambia: Hebu tuupogoe, na tuupalilie, na
tuulishe kwa muda mwingine mrefu kidogo tena, kwamba pengine utakuzalia
matunda mema, yale ambayo unaweza kujiwekea akiba wakati wa majira.
28 Na ikawa kwamba yule Bwana wa shamba na mtumishi wa Bwana wa shamba
walilisha matunda yote ya shamba.
29 Na ikawa kwamba muda mrefu ulipita, na Bwana wa shamba akamwambia
mtumishi wake: Njoo, twende kule shambani, ili tufanye kazi tena. Kwani tazama,
wakati unakaribia, na mwisho unafika hivi karibuni; kwa hivyo, lazima nijiwekee
akiba, wakati wa majira.
30 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba na mtumishi wake walienda shambani; na
wakafika kwenye ule mti ambao matawi yake ya kawaida yalivunjwa, na matawi ya
mwituni kupandikizwa; na tazama matunda ya kila aina yaliufunika ule mti.
31 Na ikawa kwamba yule Bwana wa shamba alionja yale matunda, kila aina
kulingana na wingi wake: Na yule Bwana wa shamba akasema: Tazama, kwa muda
huu mrefu tumeulisha mti huu, na nimejiwekea akiba kwa wakati wa majira.
32 Lakini tazama, wakati huu umezaa matunda mengi, na hakuna yoyote ambayo ni
mazuri. Na tazama, kuna kila aina ya matunda mabaya; na hainifaidi chochote,
ingawa tumeuchokea sana; na sasa inanihuzunisha kwamba nitapoteza mti huu.
33 Na Bwana wa shamba akamwambia yule mtumishi: Tutaufanya nini mti huu, ili
nijihifadhie mimi mwenyewe matunda mazuri?
34 Na yule mtumishi akamwambia bwana wake: Tazama, kwa sababu wewe
ulipandikiza matawi ya mchekele, yamelisha mizizi, hata iwe hai na isiangamie; kwa
hivyo wewe unaona kwamba bado ni mizuri.
35 Na ikawa kwamba Bwana wa lile shamba akamwambia mtumishi wake: Huu mti
haunifaidi chochote, na mizizi yake hainifaidi chochote ikiwa utazaa matunda
maovu.
36 Walakini, najua kwamba mizizi yake ni mizuri, na kwa shauri langu
nimeihifadhi; na kwa sababu ya nguvu yao imezaa, kutoka kwa matawi ya mwituni,
matunda mazuri.
37 Lakini tazama, yale matawi ya mwituni yamekua zaidi ya mizizi yake; na kwa
sababu matawi ya mwituni yamezidi mizizi yake umezaa matunda mengi maovu; na
kwa sababu umezaa matunda mengi maovu wewe unaona kwamba umeanza
kuangamia; na utaoza hivi karibuni, na kutupwa motoni, tusipotenda jambo ili
kuuhifadhi.

38 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba akamwambia mtumishi wake: Twende
kule sehemu za ndani ya shamba, na tuone kama matawi ya kawaida pia nayo
yamezaa matunda maovu.
39 Na ikawa kwamba walienda katika sehemu za ndani za lile shamba. Na ikawa
kwamba waliona kuwa yale matunda ya matawi ya kiasili pia nayo yalikuwa
yameharibika; ndio ya kwanza na ya pili na ya mwisho pia; na yote yalikuwa
yameharibika.
40 Na matunda ya mwituni ya ule wa mwisho yalizidi sehemu ile ya mti ambayo
ilizaa matunda mema, hata kwamba lile tawi likanyauka na kuangamia.
41 Na ikawa kwamba yule Bwana wa shamba alilia, na akamwambia mtumishi
wake: Je, ningefanya nini zaidi kuhusu shamba langu?
42 Tazama, nilijua kwamba matunda yote ya lile shamba, isipokuwa haya, yalikuwa
yameharibika. Na sasa hii ambayo hapo awali ilizaa matunda mema pia imeharibika;
na sasa miti yote ya shamba langu hainifaidi chochote ila kukatwa na kutiwa motoni.
43 Na tazama huu wa mwisho, ambao tawi lake limekauka, nilikuwa nimeupanda
katika sehemu nzuri; ndio, hata ile ambayo ilikuwa ni bora zaidi ya sehemu zingine
za shamba langu.
44 Na wewe uliona pia kwamba nilikata ile iliyofunika sehemu hii, ili nipande mti
huu pahala pake.
45 Na wewe uliona kwamba sehemu moja ilizaa matunda mema, na sehemu ingine
ikazaa matunda ya mwituni; na kwa sababu sikungo'a matawi yake na kuyatupa
motoni, tazama, yamelemea tawi lile njema hata kwamba likakauka.
46 Na sasa, tazama, ingawa tulilitunza sana shamba langu, miti yake imeharibika,
hata kwamba haizai matunda mema; na nilikuwa nimetarajia kuihifadhi, na
kujiwekea hazina, wakati wa majira. Lakini, tazama, imekuwa kama ule mchekele,
na haina faida ila tu kukatwa na kutupwa motoni; na inanihuzunisha kwamba
nitaipoteza.
47 Lakini ningefanya nini zaidi shambani mwangu? Je nimelegeza mkono wangu,
hata kwamba sikuulisha? Hapana, nimeulisha, na kuupalilia, na kuupogoa, na
nimeutia mbolea; na nimeunyosha mkono wangu karibu siku yote, na mwisho
unakaribia. Na inanihuzunisha kwamba nitakata miti yote ya shamba langu, na
kuitupa motoni ili ichomeke. Ni nani aliyeharibu shamba langu?
48 Na ikawa kwamba yule mtumishi akamwambia bwana wake: Je, sio kiburi cha
shamba lako — kwamba matawi yake yamezidi mizizi ambayo ni mizuri? Na kwa
sababu yale matawi yamezidi mizizi yake, tazama yalikua zaidi ya nguvu ya mizizi,
na kujichukulia nguvu. Tazama, nasema, je, si hii ndio sababu ya uharibifu wa miti
ya shamba lako?
49 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba akamwambia mtumishi wake: Hebu
twende na tukate miti ile ya shamba na tuitupe motoni, ili isifunike ardhi ya shamba
langu, kwani nimeshatenda yote. Je, ni yapi mengine ningeutendea shamba langu?
50 Lakini, tazama, yule mtumishi akamwambia Bwana wa shamba: Liachilie kwa
muda mdogo zaidi.
51 Na Bwana akasema: Ndio, nitaliachilia kwa muda mdogo zaidi, kwani
inanihuzunisha kwamba nitapoteza miti ya shamba langu.
52 Kwa hivyo, hebu tukate matawi mengine ya hii ambayo nimepanda katika
sehemu za ndani za shamba langu, na hebu tuyapandikize katika ule mti ambao
yalitolewa; na hebu tungo'e matawi kutoka ule mti ambao matunda yake ni

machungu zaidi, na badala yake tupandikize matawi ya kawaida.
53 Na nitatenda haya ili ule mti usiangamie, ili, pengine, nijihifadhie mizizi yake
kwa matumizi yangu.
54 Na, tazama, mizizi ya yale matawi ya mti ambao nimeupanda popote nipendapo
bado ingali hai; kwa hivyo, ili nijihifadhie hayo pia kwa matumizi yangu mwenyewe,
nitaondoa matawi ya mti huu, na nitayapandikiza ndani yake. Ndio,
nitayapandikiza katika matawi ya mti mzazi wao, ili nijihifadhie pia hiyo mizizi, ili
itakapopokea nguvu za kutosha pengine itanizalia matunda mema, na ili bado
nitukuzwe na matunda ya shamba langu.
55 Na ikawa kwamba walichukua kutoka mti wa kawaida ambao ulikuwa umegeuka
kuwa wa mwituni, na kupandikiza katika miti ya kawaida, ambayo pia ilikuwa
imegeuka kuwa ya mwituni.
56 Na pia wakachukua kutoka miti ya kawaida ambayo ilikuwa imegeuka kuwa ya
mwituni, na kupandikiza katika ule mti mzazi wao.
57 Na Bwana wa shamba akamwambia mtumishi wake: Using'oe yale matawi ya
mwituni kutoka ile miti, ila tu yale ambayo ni machungu zaidi; na utapandikiza
ndani yao kulingana na yale ambayo nimesema.
58 Na tutalisha tena ile miti ya shamba, na tutachenga matawi yake; na tutang'oa
kutoka hiyo miti yale matawi yaliyooza, ambayo lazima yaangamie, na kuyatupa
motoni.
59 Na nitatenda haya ili, pengine, mizizi yake ipokee nguvu kwa sababu ya ubora
wao; na kwa sababu ya mabadiliko ya matawi, kwamba wema uzidi ubaya.
60 Na kwa sababu kwamba nimehifadhi yale matawi ya kawaida na mizizi yake, na
kwamba nimepandikiza matawi ya kawaida tena katika ule mti mzazi wao, na
nimehifadhi mizizi ya ule mti mzazi wao, ili, pengine, miti ya shamba langu izae
tena matunda mema; na ili nishangilie tena kwa matunda ya shamba langu, na, ili,
nishangilie zaidi kwamba nimehifadhi mizizi na matawi ya malimbuko—
61 Kwa hivyo, nenda, ulete watumishi, ili tufanye kazi shambani kwa bidii na kwa
nguvu zetu, ili tuitayarishe njia, ili nirejeshe tena lile tunda la kawaida, tunda la
kawaida ambalo ni bora zaidi ya matunda mengine yote.
62 Kwa hivyo, hebu twende na tutumike kwa nguvu zetu mara hii ya mwisho, kwani
tazama mwisho unakaribia, na hii ndio mara ya mwisho ambayo nitapogoa shamba
langu.
63 Pandikizeni matawi; anzeni na ya mwisho ili yawe ya kwanza, na kwamba ya
kwanza yawe ya mwisho, na mlime miongoni mwa miti, iliyo mchanga na
iliyokomaa, ya kwanza na ya mwisho; na ya mwisho na ya kwanza, ili yote ilishwe
tena kwa mara ya mwisho.
64 Kwa hivyo, chimbeni miongoni mwao, na muipogoe, na kuitia mbolea mara
nyingine, kwa mara ya mwisho, kwani mwisho unakaribia. Na kama haya
mapandikizo ya mwisho yatakua, na kuzaa matunda ya kawaida, basi
mtayatayarishia njia, ili yakue.
65 Na itakapoanza kukua mtaondoa matawi yanayozaa matunda machungu,
kulingana na nguvu na kipimo cha uzuri wake; na hamtaondoa yaliyo mabaya kwa
ghafla, isiwe kwamba mizizi yake inazidi nguvu ya lile pandikizo, na pandikizo hilo
liangamie, na nipoteze miti ya shamba langu.
66 Kwani inanihuzunisha kwamba nitapoteza miti ya shamba langu; kwa hivyo
mtafyeka iliyo miovu kulingana na vile iliyo mizuri itakavyomea, ili mizizi na kilele

ziwe na nguvu sawa, hadi iliyo nzuri izidi iliyo mbovu, na iliyo mbovu ikatwe na kutiwa motoni, ili isifunike ardhi ya shamba langu; na hivyo ndivyo nitaufagia uovu kutoka shamba langu.

67 Na matawi ya mti wa kawaida nitayapandikiza tena kwenye mti ule wa kawaida;

68 Na matawi ya mti wa kawaida nitayapandikiza katika matawi ya kawaida ya ule mti; na ndivyo nitakavyoiunganisha pamoja tena, ili izae matunda ya kawaida, na iwe kitu kimoja.

69 Na iliyo mbovu itatupwa mbali, ndio, hata kutoka ardhi yote ya shamba langu la mizabibu; kwani tazama, ni kwa hii mara moja tu nitakayopogoa shamba langu la mizabibu.

70 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba la mizabibu alimtuma mtumishi wake; na mtumishi akaenda na kutenda kulingana na vile alivyoamriwa na Bwana, na akaleta watumishi wengine; na walikuwa wachache.

71 Na Bwana wa shamba la mizabibu akawaambia: Nendeni, na mkatumikie shamba la mizabibu, kwa uwezo wenu. Kwani tazama, hii ndiyo mara ya mwisho nitakayolisha shamba langu la mizabibu; kwani mwisho unakaribia, na wakati unafika kwa haraka; na kama mtatumikia na mimi kwa nguvu zenu mtakuwa na shangwe katika matunda nitakayojiwekea kwa wakati unaokaribia.

72 Na ikawa kwamba watumishi walienda na kutumikia kwa nguvu zao; na Bwana wa shamba la mizabibu akatumikia shambani pia nao; na wakatii amri za Bwana wa shamba la mizabibu katika vitu vyote.

73 Na matunda ya kawaida yakaanza kukua tena pale shambani la mizabibu; na matawi ya kawaida yakaanza kukua na kufanikiwa sana; na matawi ya mwituni yakapobolewa na kutupwa mbali; na wakaweka mizizi yake na kilele chake kuwa sawa, kulingana na nguvu zake.

74 Na wakatumikia hivyo, kwa bidii zote, kulingana na amri za Bwana wa shamba la mizabibu, hadi iliyo bovu ikatolewa shambani, na Bwana alikuwa amejihifadhia kwamba ile miti ilikuwa matunda ya kawaida tena; na ikawa kama kitu kimoja; na matunda yalikuwa sawa; na yule Bwana wa shamba la mizabibu alikuwa amejihifadhia mwenyewe matunda ya kawaida, ambayo yalikuwa bora zaidi tangu hapo mwanzoni.

75 Na ikawa kwamba wakati yule Bwana wa shamba la mizabibu alipoona kuwa matunda yake ni mazuri, na kwamba shamba lake la mizabibu halikuwa liharibifu tena, aliwaita watumishi wake, na kuwaambia: Tazama, tumelilisha shamba langu la mizabibu kwa mara hii ya mwisho; na nyinyi mmeona kwamba nimetenda kulingana na nia yangu; na nimehifadhi matunda ya kawaida, na ni mazuri, kama vile yalivyokuwa hapo mwanzoni. Na heri nyinyi; kwani kwa sababu mmekuwa na bidii katika kutumikia na mimi katika shamba langu la mizabibu, na mmetii amri zangu, na kuniletea tena matunda ya kawaida, kwamba shamba langu sio bovu tena, na iliyo bovu imetupwa mbali, tazama mtapokea shangwe na mimi kwa sababu ya matunda ya shamba langu la mizabibu.

76 Kwani tazama, kwa muda mrefu nitajiwekea matunda ya shamba langu kwa wakati wa majira, unaokaribia kwa haraka; na nimelisha shamba langu la mizabibu kwa mara ya mwisho, na kulipogoa, na kulilimia, na kulitia mbolea; kwa hivyo nitajiwekea matunda, kwa muda mrefu, kulingana na yale ambayo nimezungumza.

77 Na wakati ule utakapofika ambao matunda maovu yatakuja tena katika shamba langu la mizabibu, basi nitasababisha yale yaliyo mazuri na mabaya kukusanywa; na

yale mazuri nitajiwekea, na yale mabaya nitayatupa mahali pake. Na kisha wakati wa majira utafika na mwisho; na nitasababisha shamba langu la mizabibu lichomwe kwa moto.

## Yakobo 6

1 Na sasa, tazameni, ndugu zangu, kama vile nilivyowaambia kwamba nitatoa unabii,
tazama, huu ndio unabii wangu — kwamba vile vitu ambavyo huyu nabii Zeno
alizungumza, kuhusu nyumba ya Israeli, ambapo aliwalinganisha na mzeituni,
lazima vitimie.
2 Na siku ambayo atanyoosha mkono wake tena mara ya pili ili kuwaokoa watu
wake, ni siku ile, ndio, hata mara ya mwisho, ambayo watumishi wa Bwana
wataenda mbele kwa nguvu zake, kulisha na kupogoa shamba lake la mizabibu; na
baada ya hayo mwisho utafika.
3 Na heri wale ambao wametumikia shamba lake la mizabibu kwa bidii; na jinsi
gani watakavyolaaniwa wale ambao watatupwa mahala pao! Na ulimwengu
utachomwa kwa moto.
4 Na jinsi gani alivyoturehemu sisi Mungu wetu, kwani anakumbuka nyumba ya
Israeli, mizizi pamoja na matawi; na anawanyoshea mikono yake siku yote na ni
watu wenye shingo ngumu na ubishi; lakini wale wote ambao hawatashupaza mioyo
yao wataokolewa katika ufalme wa Mungu.
5 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, ninawasihi kwa maneno ya kiasi kwamba
mtubu, na mje kwa moyo wa lengo moja, na mjishikilie kwa Mungu kama vile
anavyowashikilia. Na msishupaze mioyo yenu, wakati amewanyoshea mkono wake
wa huruma mchana.
6 Ndio, leo, kama mtasikia sauti yake, msishupaze mioyo yenu; kwani, kwa nini
mfe?
7 Kwani tazama, baada yenu kulishwa kwa neno jema la Mungu kwa siku yote, je,
mtazaa matunda maovu, ili mkatwe na kutupwa motoni?
8 Tazameni, je, mtayakataa maneno haya? Je, mtayakataa maneno ya manabii; na
je, mtayakataa maneno yote ambayo yamezungumzwa kuhusu Kristo, baada ya
wengi sana kuzungumza kumhusu yeye; na kukana neno jema la Kristo, na nguvu ya
Mungu, na kipawa cha Roho Mtakatifu, na kuzimisha Roho Mtakatifu, na kufanyia
mzaha ule mpango mkuu wa ukombozi, ambao mmepangiwa nyinyi?
9 Je, hamjui kwamba mkitenda vitu hivi, kwamba nguvu za ukombozi na ufufuo,
ambazo ziko katika Kristo, zitawaleta kusimama katika kiti cha hukumu cha Mungu
kwa aibu na hatia kuu?
10 Na kulingana na nguvu za haki, kwani haki haiwezi kuzuiwa, lazima mtupwe
kwenye lile ziwa la moto na kiberiti, ambalo ndimi zake za moto hazizimiki, na
ambalo moshi wake unapaa juu milele na milele, ambalo ziwa la moto na kiberiti ni
mateso yasiyo na mwisho.
11 Ee basi, ndugu zangu wapendwa, tubuni nyinyi, na muingie katika mlango
uliosonga, na mwendelee katika njia ambayo ni nyembamba, hadi mtakapopokea
uzima wa milele.
12 Ee pokeeni hekima; niseme nini zaidi?
13 Mwishoni, nawaaga kwa heri, hadi nitakapokutana nanyi kwa furaha katika kiti
cha enzi cha Mungu, kiti ambacho kinawatia walio waovu woga na hofu ya kutisha.

Amina.

## Yakobo 7

1 Na sasa ikawa kwamba baada ya miaka kadhaa kupita, palitokea mtu miongoni mwa
watu wa Nefi, aliyeitwa Sheremu.
2 Na ikawa kwamba alianza kuhubiri miongoni mwa wale watu, na kuwatangazia
kwamba hakutakuwa na Kristo. Na akahubiri vitu vingi ambavyo vilikuwa vya
kupendeza kwa watu; na alifanya hivi ili apindue mafundisho ya Kristo.
3 Na akatumika kwa bidii ili apotoshe mioyo ya watu, hadi akapotosha mioyo
mingi; na yeye akijua kwamba mimi, Yakobo, nilikuwa na imani kwa Kristo
atakayekuja, alitafuta nafasi ili anijie.
4 Na alikuwa ameelimika, hata kwamba alifahamu kikamilifu lugha ya wale watu;
kwa hivyo, angerairai, na alikuwa na uwezo wa kuzungumza sana, kulingana na
nguvu ya ibilisi.
5 Na alikuwa anatumaini kwamba ataniondoa kutoka imani, ingawa nilikuwa na
ufunuo mwingi na vitu vingi ambavyo nilikuwa nimeona kuhusu vitu hivi; kwani
kwa kweli nilikuwa nimewaona malaika, na walikuwa wamenihudumia. Na pia,
nilikuwa nimesikia sauti ya Bwana ikinizungumzia kwa maneno dhahiri, mara kwa
mara; kwa hivyo, singetetemeshwa.
6 Na ikawa kwamba alinijia, na akanizungumzia hivi, akisema: Kaka Yakobo,
nimetafuta nafasi ili nikuzungumzie; kwani nimesikia na pia ninajua kwamba wewe
unasafiri sana, ukihubiri ile ambayo unaiita injili, au mafundisho ya Kristo.
7 Na umepotosha watu hawa wengi kwamba wamegeuza njia ile sawa ya Mungu,
na hawatii amri ya Musa ambayo ndio njia sawa; na kubadili sheria ya Musa kuwa
ibada ya mtu ambaye unasema kwamba atakuja baada ya miaka mia na mia. Na sasa
tazama, mimi, Sheremu, nakutangazia wewe kwamba huu ni ukufuru; kwani
hakuna mtu anayejua vitu hivi; kwani hawezi kuzungumza kuhusu vitu vile
vitakavyokuwepo. Na Sheremu alibishana na mimi katika njia hii.
8 Lakini tazama, Bwana Mungu alinishushia Roho wake katika nafsi yangu, hadi
nikamfadhaisha katika maneno yake yote.
9 Na nikamwambia: Je, wewe unamkana Kristo ambaye atakuja? Na akasema:
kama Kristo atakuwepo, singemkana; lakini najua kwamba hakuna Kristo, wala
hajakuwepo, wala hatakuwepo.
10 Na nikamwambia: Je, wewe unaamini maandiko? Na akasema, Ndio.
11 Na nikamwambia: Basi hauyafahamu; kwani yanashuhudia Kristo kwa kweli.
Tazama, nakuambia kwamba hakuna manabii walioandika, wala kutoa unabii, bila
kuzungumza kuhusu huyu Kristo.
12 Na haya sio yote—imedhihirishwa kwangu mimi, kwani nimesikia na kuona; na
pia imedhihirishwa kwangu kwa nguvu za Roho Mtakatifu; kwa hivyo, najua kama
hakuna upatanisho wanadamu wote watapotea.
13 Na ikawa kwamba aliniambia: Nionyeshe ishara kwa hizi nguvu za Roho
Mtakatifu ambazo zinakuwezesha kujua haya mengi.
14 Na nikamwambia: Mimi ni nani ili nimjaribu Mungu akuonyeshe ishara kwa
kitu unachokijua kwamba ni kweli? Lakini bado wewe unalikana, kwa sababu wewe
ni wa ibilisi. Walakini, nia yangu isitendeke; lakini kama Mungu atakupiga, hebu
hiyo na iwe ishara kwako kwamba ana nguvu, mbinguni na duniani; na pia, kwamba

Kristo atakuja. Na nia yako, Ewe Bwana, itendeke, sio yangu.
15 Na ikawa kwamba wakati mimi, Yakobo, nilizungumza maneno haya, nguvu za
Bwana zikamshukia, hadi akainama kwenye ardhi. Na ikawa kwamba alilishwa kwa
muda wa siku nyingi.
16 Na ikawa kwamba aliwaambia watu: Kusanyikeni pamoja hapo kesho, kwani
nitafariki; kwa hivyo, natamani kuzungumza na watu kabla sijafariki.
17 Na ikawa kwamba umati ulikusanyika pamoja kesho yake; na akazungumza kwao
wazi wazi na akakana vile vitu alivyokuwa amewafundisha, na akamkiri Kristo, na
nguvu za Roho Mtakatifu, na huduma ya malaika.
18 Na akawazungumzia wazi, kwamba alikuwa amedanganywa na nguvu ya ibilisi.
Na akazungumza kuhusu jahanamu, na umilele, na adhabu ya milele.
19 Na akasema: Nahofia kwamba nimetenda dhambi isiyosamehewa, kwani
nimesema uwongo mbele ya Mungu; kwani nilimkana Kristo, na nikasema kwamba
niliamini maandiko; na kwa kweli yanamshuhudia yeye. Na kwa sababu
nimemdanganya Mungu naogopa kwamba hali yangu itakuwa mbaya; lakini
ninatubu kwa Mungu.
20 Na ikawa kwamba baada ya kusema haya maneno hakuweza tena kusema
mengine, na akafariki.
21 Na umati uliposhuhudia kwamba alizungumza vitu hivi akiwa karibu ya kufariki,
walishangazwa sana; hadi nguvu za Mungu zikawashukia, na wakazidiwa na
kuinama ardhini.
22 Sasa, kitu hiki kilinifurahisha mimi, Yakobo, kwani nilikuwa nimemwomba
Baba yangu aliye mbinguni; kwani alisikia kilio changu na kujibu sala yangu.
23 Na ikawa kwamba amani na upendo wa Mungu ulirejeshwa tena miongoni mwa
watu; na wakasoma maandiko, na hawakutii tena maneno ya huyu mtu mwovu.
24 Na ikawa kwamba mbinu nyingi zilitumiwa kuwarejesha Walamani ili wapate
ufahamu wa kweli; lakini yote yalikuwa ni bure, kwani walifurahia vita na umwagaji
wa damu, na walikuwa na chuki ya milele kwetu sisi, ndugu zao. Na wakataka kwa
uwezo wao wa silaha kutuangamiza daima.
25 Kwa hivyo, watu wa Nefi wakajiimarisha dhidi yao kwa silaha zao, na kwa nguvu
zao zote, wakimwamini Mungu na mwamba wa wokovu wao; kwa hivyo, wakawa,
washindi wa maadui zao.
26 Na ikawa kwamba mimi, Yakobo, nilianza kuzeeka; na maandishi ya watu hawa
yakiwa yameandikwa katika zile bamba zingine za Nefi, kwa hivyo, namaliza historia
hii, nikikiri kwamba nimeandika kulingana na ufahamu wangu kamili, na kusema
kwamba wakati ulipita pamoja nasi, na pia maisha yetu yalipita kama ndoto, sisi
tukiwa watu wenye upweke na unadhiri, wahamaji, tuliotupwa nje kutoka
Yerusalemu, tukizaliwa kwenye mateso, kwenye nyika, na kuchukiwa na ndugu zetu,
ambao walisababisha vita na mabishano; kwa hivyo, tuliomboleza maisha yetu.
27 Na mimi, Yakobo, nikafahamu kwamba lazima hivi karibu niende kaburini; kwa
hivyo, nikamwambia mwana wangu Enoshi: Chukua hizi bamba. Na nilimwambia
vile vitu ambavyo kaka yangu Nefi aliniamuru, na akaahidi kutii zile amri. Na
ninamaliza kuandika katika bamba hizi, uandishi ambao umekuwa mfupi; na kwa
msomaji nakuaga kwa heri, nikitumaini kwamba ndugu zangu wengi watasoma
maneno haya. Ndugu, Mungu awe nanyi.

# Kitabu cha Enoshi

1 Tazama, ikawa kwamba mimi, Enoshi, nikijua kwamba Baba yangu alikuwa mtu wa
haki — kwani alinifunza kwa lugha yake, na pia katika malezi na maonyo ya
Bwana — na jina la Mungu wangu libarikiwe kwa hayo —
2 Na nitakuelezea kuhusu mweleka ambao nilikuwa nao mbele ya Mungu, kabla ya
kupokea msamaha wa dhambi zangu.
3 Tazama, nilienda kuwinda wanyama porini; na maneno ambayo nilikuwa
nimezoea kumsikia baba yangu akizungumza kuhusu uzima wa milele, na shangwe
ya watakatifu, yakapenya ndani ya moyo wangu.
4 Na nafsi yangu ikapata njaa; na nikapiga magoti mbele ya Muumba wangu, na
nikamlilia kwa sala kuu na nikamsihi kwa nafsi yangu; na kwa siku nzima nikamlilia;
ndio, na wakati usiku ulipofika bado nilipaza sauti yangu hata ikafika mbinguni.
5 Na sauti ikanijia, ikisema: Enoshi, umesamehewa dhambi zako, na wewe
utabarikiwa.
6 Na mimi, Enoshi, nilijua kwamba Mungu hawezi kusema uwongo; kwa hivyo,
hatia yangu iliondolewa mbali.
7 Na nikasema: Bwana, je, inafanywa vipi?
8 Na akaniambia: Kwa sababu ya imani yako katika Kristo, ambaye wewe
hujamwona kamwe wala kumsikia. Na miaka mingi itapita kabla yeye
hajajidhihirisha katika mwili; kwa hivyo, nenda, imani yako imekufanya mkamilifu.
9 Sasa, ikawa kwamba baada ya kusikia maneno haya nilianza kushughulika na
ustawi wa ndugu zangu, Wanefi; kwa hivyo, nilimlilia Mungu kwa roho yangu yote
kwa niaba yao.
10 Na nilipokuwa nikishindana hivyo rohoni, tazama, sauti ya Bwana ikanijia
mawazoni mwangu tena, ikisema: Nitagawanyia ndugu zako kulingana na bidii yao
katika kutii amri zangu. Nimewapatia nchi hii, na hii ni nchi takatifu; na siwezi
kuilaani ila tu kwa sababu ya dhambi; kwa hivyo, nitagawanyia ndugu zako
kulingana na yale ambayo nimesema; na nitawateremshia juu ya vichwa vyao
wenyewe huzuni ya dhambi zao.
11 Na baada ya mimi, Enoshi, kusikia maneno haya, imani yangu kwa Bwana ikawa
haitikisiki; na nikamwomba kwa vilio vingi kwa niaba ya ndugu zangu, Walamani.
12 Na ikawa kwamba baada ya kuomba na kumtumikia kwa bidii, Bwana
akaniambia: Kwa sababu ya imani yako, nitakutendea kulingana na mahitaji yako.
13 Na sasa tazama, hili ndilo hitaji ambalo nilihitaji kwake — kwamba, kama watu
wangu, Wanefi, wataanguka dhambini, na kwa vyovyote waangamizwe, na,
Walamani wasiangamizwe, kwamba Bwana Mungu angehifadhi maandishi ya watu
wangu, Wanefi; hata kama ni kwa nguvu za mkono wake mtakatifu, ili katika siku za
usoni yafunuliwe kwa Walamani, ili, pengine, waokolewe —
14 Kwani kwa sasa majaribio yetu ya kuwarudisha katika imani ya kweli yalikuwa ni
bure. Na wakaapa katika hasira zao, kwamba, kama itawezekana, wataangamiza
maandishi yetu pamoja nasi, na pia desturi zote za baba zetu.
15 Kwa hivyo, mimi nikijua kwamba Bwana Mungu anaweza kuhifadhi maandishi
yetu, nilimlilia sana bila kukoma, kwani alikuwa ameniambia: Chochote
utakachoomba kwa imani, ukiamini kwamba utapokea kwa jina la Kristo,
utakipokea.
16 Na nilikuwa na imani, na nikamlilia Mungu kwamba angehifadhi yale

maandishi; na akaagana na mimi kwamba atayafunua kwa Walamani katika wakati wake.

17 Na mimi, Enoshi, nilijua kwamba itakuwa kulingana na agano alilofanya; kwa hivyo nafsi yangu ikapumzika.

18 Na Bwana akaniambia: Baba zako nao pia wameniomba kitu hiki; na kitatendwa kulingana na imani yao; kwani imani yao ilikuwa kama yako.

19 Na sasa ikawa kwamba mimi, Enoshi, nilienda miongoni mwa watu wa Nefi, nikitoa unabii kuhusu vitu vitakavyokuja, na nikishuhudia kuhusu vitu ambavyo nilikuwa nimevisikia na kuona.

20 Na ninashuhudia kwamba watu wa Nefi walijaribu kwa bidii kuwarejesha Walamani katika imani ya kweli ya Mungu. Lakini kazi zetu zilikuwa bure; na chuki yao ilikuwa imeimarishwa, na walitawaliwa na maumbile yao maovu na wakawa wachokozi, wakali, na watu wapendao umwagaji wa damu na kuabudu sanamu na uchafu; wakila wanyama wa porini; na kuishi katika mahema, na kuzunguka nyikani, na kuvaa ngozi za wanyama viunoni mwao na kunyoa nywele zao; na ustadi wao ulikuwa ni wa upinde, na upanga, na shoka. Na wengi wao hawakula chochote isipokuwa nyama mbichi, na walijaribu kila mara kutuangamiza.

21 Na ikawa kwamba watu wa Nefi walilima ardhi, na kupanda kila aina ya nafaka, na matunda, na makundi ya wanyama, na makundi yote ya kila aina ya ngombe, na mbuzi, na mbuzi wa mwitu, na pia farasi wengi.

22 Na kulikuwa na manabii wengi sana miongoni mwetu. Na watu walikuwa watu wenye shingo ngumu, wagumu katika kufahamu.

23 Na hakukuwa na chochote ila ukali mwingi, mahubiri na kutoa unabii kuhusu vita, na mabishano, na maangamizo, na kuwakumbusha kila mara kuhusu mauti, na kipindi cha umilele, na hukumu na nguvu za Mungu, na hivi vitu vyote — kuwavuruga kila mara ili wamwogope Bwana. Nasema hapakuwa na mambo chini ya vitu hivi, na mazungumzo dhahiri, ili kuwafanya wasiangamie kwa haraka. Na ninaandika jinsi hii juu yao.

24 Na niliona vita vingi miongoni mwa Wanefi na Walamani maishani mwangu.

25 Na ikawa kwamba nilianza kuzeeka, na miaka mia moja, sabini na tisa ilikuwa imepita tangu baba yetu Lehi aondoke Yerusalemu.

26 Na nikaona kwamba ni lazima ninakaribia kuelekea kaburini, nikiwa nimewezeshwa na nguvu za Mungu ili nihubiri na niwatolee watu hawa unabii, na nitangaze neno kulingana na ukweli ulio katika Kristo. Na nimeutangaza katika maisha yangu yote, na nimeufurahia zaidi ya yote ulimwenguni.

27 Na hivi karibuni naelekea mahala pa pumziko langu, ambapo ni pamoja na Mkombozi wangu; kwani najua kwamba nitapumzika na yeye. Na ninafurahia siku ile ambayo huu mwili wenye kutokufa utajivika, na kusimama mbele yake, kisha nitaona uso wake kwa furaha, na ataniambia: Njoo kwangu, heri wewe, umetayarishiwa mahali katika nyumba za Baba yangu. Amina.

# Kitabu cha Yaromu

1 Sasa tazama, mimi, Yaromu, naandika maneno machache kulingana na amri ya baba
yangu, Enoshi, ili nasaba yetu iwekwe.
2 Na kwa vile hizi bamba ni ndogo, na kwa vile vitu hivi vimeandikwa kwa
madhumuni ya kuwafaidi ndugu zetu Walamani, kwa hivyo, ni lazima niandike
machache; lakini sitaandika vitu kuhusu utoaji wa unabii wangu, wala kuhusu
ufunuo wangu. Kwani naweza kuandika nini zaidi ya yale baba zangu waliyoandika?
Kwani siwamefunua kuhusu mpango wa wokovu? Nawaambia, Ndio; na hii
inanitosheleza.
3 Tazama, ni lazima mengi yatendwe miongoni mwa watu hawa, kwa sababu ya
ugumu wa mioyo yao; na uziwi wa masikio yao, na upofu wa mawazo yao, na ugumu
wa shingo zao; walakini, Mungu anawarehemu sana, na bado hajawaondoa usoni
mwa nchi.
4 Na kuna wengi miongoni mwetu ambao wana ufunuo mwingi, kwani sio wote
wanye shingo ngumu. Na kwa wale wengi ambao hawana ugumu wa shingo na wana
imani, wana ushirika na Roho Mtakatifu, ambaye anawadhihirishia watoto wa watu,
kulingana na imani yao.
5 Na sasa, tazama, miaka mia mbili ilikuwa imepita, na watu wa Nefi walikuwa
wamepata nguvu katika nchi. Walitia bidii kutii sheria ya Musa na pia siku ya Sabato
kuwa takatifu kwa Bwana. Wala hawakutusi; au kukufuru. Na sheria za nchi
zilikuwa kali sana.
6 Na walitawanyika sana usoni mwa nchi, na pia Walamani. Na walikuwa ni wengi
zaidi ya Wanefi; na walipenda mauaji na hata kunywa damu ya wanyama.
7 Na ikawa kwamba walitushambulia mara nyingi sisi, Wanefi, ili tupigane. Lakini
wafalme na viongozi wetu walikuwa ni watu mashujaa kwa imani ya Bwana; na
wakafunza watu njia za Bwana; kwa hivyo, tuliwapiga Walamani na kuwaondoa
kutoka nchi yetu, na tukaanza kujenga nyua miji yetu, au mahali popote pa urithi
wetu.
8 Na tukaongezeka sana, na tukatawanyika usoni mwa nchi, na tukatajirika sana
kwa dhahabu, na kwa fedha, na katika vitu vyenye thamani, na katika kazi nzuri za
mbao, katika majengo, na katika mitambo, na pia katika chuma na shaba nyekundu,
na shaba na chuma, na kutengeneza kila aina ya vyombo vya kulima, na silaha za
vita — ndio, mshale mkali, na podo, na kiparara, na sagai, na matayarisho yote ya
vita.
9 Na hivyo tukiwa tayari kukutana na Walamani, wao hawakufanikiwa kwetu sisi.
Lakini neno la Bwana lilithibitishwa, ambalo aliwazungumzia Baba zetu, akisema
kwamba: Kadiri mtakavyo tii amri zangu ndivyo mtakavyofanikiwa nchini.
10 Na ikawa kwamba manabii wa Bwana waliwatisha watu wa Nefi, kulingana na
neno la Mungu, kwamba kama hawakutii amri, lakini waanguke dhambini,
wangeangamizwa kutoka usoni mwa nchi.
11 Kwa hivyo, manabii, na makuhani, na walimu, walitumikia kwa bidii,
wakiwaonya watu kwa subira watie bidii; wakifunza sheria ya Musa, na kwa
madhumuni gani ilitolewa; kuwashawishi wamtazamie Masiya, na wamwamini yeye
atakayekuja kama vile tayari yuko. Na hivi ndivyo walivyowafundisha.
12 Na ikawa kwamba kwa kufanya hivyo waliwazuia watu wasiangamizwe kutoka
usoni mwa nchi; kwani waliwadunga mioyo yao kwa neno, kila mara na kuwavuruga

ili watubu.
13 Na ikawa kwamba miaka mia mbili, thelathini na minane ilikuwa imepita — kwa
muda mkubwa wa huu wakati kulikuwa na vita, mabishano, na mafarakano.
14 Na mimi, Yaromu, sitaandika mengine, kwani bamba ni ndogo. Lakini tazameni,
ndugu zangu, mnaweza kusoma bamba zile zingine za Nefi; kwani tazama,
maandishi kuhusu vita vyetu yako humo na yameandikwa, kulingana na maandiko
ya wafalme, au yale ambayo waliamuru yaandikwe.
15 Na ninamkabidhi mwana wangu Omni bamba hizi, ili ziwekwe kulingana na
amri za baba zangu.

# Kitabu cha Omni

1 Tazama, ikawa, kwamba mimi, Omni, nikiwa nimeamriwa na baba yangu, Yaromu,
kwamba niandike kwenye bamba hizi, ili nasaba yetu ihifadhiwe—
2 Kwa hivyo, ningetaka mjue kwamba, katika maisha yangu, nilipigana sana kwa
upanga ili kuwahifadhi watu wangu, Wanefi, wasianguke mikononi mwa maadui
wao, Walamani. Lakini tazama, mimi mwenyewe ni mtu mwovu, na sijatii amri za
Bwana na sheria zake kama vile ilivyonipasa.
3 Na ikawa kwamba miaka mia mbili, sabini na sita ilikuwa imepita, na tulikuwa na
vipindi vingi vya amani; na tulikuwa na vipindi vingi vya vita na umwagaji wa damu.
Ndio, na kwa ufupi, miaka mia mbili, themanini na miwili ilikuwa imepita, na
nilikuwa nimeweka bamba hizi kulingana na amri za baba zangu; na nikampatia
mwana wangu Amaroni hizo bamba. Na ninakoma hapa.
4 Na sasa mimi, Amaroni, naandika vitu ambavyo ninaandika, ambavyo ni
vichache, katika kitabu cha baba yangu.
5 Tazama, na ikawa kwamba miaka mia tatu na ishirini ilikuwa imepita, na sehemu
kubwa ya Wanefi waovu ikaangamizwa.
6 Kwani Bwana hangeruhusu, baada ya kuwaongoza kutoka nchi ya Yerusalemu na
kuwahifadhi wasianguke mikononi mwa maadui zao, ndio, hangekubali kwamba
yale maneno ambayo aliwaambia baba zetu, yasithibitishwe, akisema kwamba:
Msipotii amri zangu hamtafanikiwa nchini.
7 Kwa hivyo, Bwana aliwaadhibu kwa hukumu kuu; walakini, aliwaokoa wenye
haki kwamba wasiangamie, lakini aliwakomboa kutoka mikononi mwa maadui zao.
8 Na ikawa kwamba nilimpatia Kemishi kaka yangu zile bamba.
9 Sasa mimi, Kemishi, naandika vitu vichache, katika kitabu sawa na kaka yangu;
kwani tazama, niliona ya mwisho aliyoandika, kwamba aliandika kwa mkono wake
mwenyewe; na aliyaandika siku ile aliyonipatia. Na tunaweka maandishi katika njia
hii, kwani ni kulingana na amri za baba zetu. Na ninakoma hapo.
10 Tazama, mimi, Abinadomu, ni mwana wa Kemishi. Tazama, ikawa kwamba
mimi niliona vita vingi na ubishi kati ya watu wangu, Wanefi, na Walamani; na
mimi, kwa upanga wangu mwenyewe, nimeondoa maisha ya Walamani wengi kwa
ulinzi wa ndugu zangu.
11 Na tazama, maandishi ya watu hawa yameandikwa katika bamba ambazo
zimekuwa na wafalme, kulingana na vizazi; na sijui ufunuo wowote ambao
haujaandikwa, wala unabii; kwa hivyo, yaliyoandikwa yametosha. Na ninakoma
hapo.
12 Tazama, mimi ni Amaleki, mwana wa Abinadomu. Tazama, nitawazungumzia
kuhusu Mosia, ambaye alitawazwa mfalme katika nchi ya Zarahemla; kwani tazama,
yeye akiwa ameonywa na Bwana kwamba atoroke kutoka nchi ya Nefi, na wale wengi
watakaotii sauti ya Bwana pia nao waondoke nchini na yeye, na waelekee nyikani—
13 Na ikawa kwamba alitenda kulingana na vile Bwana alivyomwamuru. Na
walitoka nchi ile na kuelekea nyikani, wote ambao walisikiliza sauti ya Bwana; na
waliongozwa kwa mahubiri mengi na unabii. Na wakaonywa kila mara kwa neno la
Mungu; na waliongozwa kwa nguvu za mkono wake, huko nyikani hadi wakafika
katika nchi inayoitwa nchi ya Zarahemla.
14 Na wakawavumbua watu, walioitwa watu wa Zarahemla. Sasa, kulikuwa na
furaha kuu miongoni mwa watu wa Zarahemla; na pia Zarahemla alifurahi sana,

kwa sababu Bwana alikuwa ametuma watu wa Mosia pamoja na bamba za shaba
ambazo zilikuwa na maandishi ya Wayahudi.
15 Tazama, na ikawa kwamba Mosia alivumbua kuwa watu wa Zarahemla
waliondoka Yerusalemu wakati Zedekia, mfalme wa Yuda, alipohamishwa
Babilonia utumwani.
16 Na wakasafiri nyikani, na wakavushwa kwa mkono wa Bwana katika yale maji
makuu, hadi katika nchi ile ambayo Mosia aliwavumbua, na wakaishi katika nchi ile
tangu wakati huo.
17 Na ule wakati Mosia alipowavumbua, walikuwa wamekuwa wengi sana.
Walakini, walikuwa wamekuwa na vita vingi na mabishano makubwa, na walikuwa
wameanguka kwa upanga mara kwa mara; na lugha yao ilikuwa imechafuka; na
hawakuwa wamebeba maandishi yoyote; na walikana uwepo wa Muumba wao; na
Mosia, wala watu wa Mosia, hawakuweza kuwaelewa.
18 Lakini ikawa kwamba Mosia akasababisha kwamba wafunzwe kwa lugha yake.
Na ikawa kwamba baada ya kufunzwa lugha ya Mosia, Zarahemla akatoa nasaba ya
baba zake, kulingana na ukumbuko wake; na yameandikwa, lakini sio katika bamba
hizi.
19 Na ikawa kwamba watu wa Zarahemla, na watu wa Mosia, waliungana pamoja;
na Mosia akateuliwa kuwa mfalme wao.
20 Na ikawa kwamba katika siku za Mosia, aliletewa jiwe kubwa lililokuwa na
maandishi juu yake; na akatafsiri hayo maandishi kwa karama na nguvu za Mungu.
21 Na yalieleza historia ya mmoja aliyeitwa Koriantumuri, na mauaji ya watu wake.
Na Koriantumuri alivumbuliwa na watu wa Zarahemla; na akaishi nao kwa muda
wa miezi tisa.
22 Na pia ilizungumza maneno machache kuhusu babu zake. Na wazazi wake wa
kwanza walitoka katika ule mnara, wakati Bwana alipochanganya lugha za watu; na
mapigo ya Bwana yaliwashukia kulingana na hukumu zake, ambazo ni za haki; na
mifupa yao ilitawanyika katika nchi za kaskazini.
23 Na tazama, mimi, Amaleki, nilizaliwa katika siku za Mosia; na nimeishi kuona
kifo chake; na mwana wake, Benyamini anatawala mahali pake.
24 Na tazama, nimeona, katika siku za mfalme Benyamini, vita vikali na umwagaji
wa damu miongoni mwa Wanefi na Walamani. Lakini tazama, Wanefi walipata
ushindi juu yao; ndio, hadi mfalme Benyamini akawafukuza kutoka nchi ya
Zarahemla.
25 Na ikawa kwamba nilianza kuzeeka; na nikiwa sina uzao, na nikijua kwamba
Mfalme Benyamini alikuwa mwenye haki kwa Bwana, kwa hivyo, nitamkabidhi
bamba hizi, nikiwasihi wanadamu wote wamjie Mungu, yule Mtakatifu wa Israeli,
na kuamini katika unabii, na katika ufunuo, na kuhudumu kwa malaika, na katika
kipawa cha kunena kwa ndimi, na katika kipawa cha kutafsiri ndimi, na katika vitu
vyote vilivyo vyema; kwani hakuna lolote jema lisilotokana na Bwana: na kwamba
yale yaliyo maovu yanatokana na ibilisi.
26 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, natamani mje kwa Kristo, ambaye ni Mtakatifu
wa Israeli, na mpokee wokovu wake, na nguvu za ukombozi wake. Ndio, njooni
kwake, na mmtolee nafsi zenu kama sadaka kwake, na muendelee katika kufunga na
kusali, na kuvumilia hadi mwisho; na kama vile Bwana anavyoishi mtaokolewa.
27 Na sasa nitazungumza machache kuhusu wengine walioelekea nyikani ili kurejea
katika nchi ya Nefi; kwani kulikuwa na wengi waliotamani kumiliki nchi yao ya

urithi.
28 Kwa hivyo, walielekea nyikani. Na kiongozi wao akiwa mtu mwenye nguvu na shujaa, na mtu mwenye shingo ngumu, kwa hivyo alisababisha ubishi miongoni mwao; na wote wakauawa, huko nyikani, isipokuwa hamsini, na wakarejea katika nchi ya Zarahemla.
29 Na ikawa kwamba waliwachukua wengine pia, na wakaelekea katika safari nyingine huko nyikani.
30 Na mimi, Amaleki, nilikuwa na kaka, ambaye pia alienda pamoja nao; na tokea hapo sijajua lolote juu yao. Na sasa ninakaribia kulala katika kaburi langu; na bamba hizi zimejaa. Na ninamaliza mazungumzo yangu.

# Maneno ya Mormoni

1 Na sasa mimi, Mormoni, nikikaribia kuyakabidhi yale maandishi ambayo
nimeandika mikononi mwa mwana wangu Moroni, tazama nimeshuhudia karibu
maangamizo yote ya watu wangu, Wanefi.
2 Na ni baada ya miaka mia kadha baada ya kuja kwa Kristo ninapompatia mwana
wangu maandishi haya; na ninadhani kwamba atashuhudia maangamizo yote ya
watu wangu. Lakini na Mungu amjalie aweze kuishi, ili aandike juu yao, na kwa
vyovyote kuhusu Kristo, ili pengine wafaidike katika nyakati zingine.
3 Na sasa, ninazungumza kuhusu yale ambayo nimeandika; kwani baada ya
kufanya ufupisho kutoka zile bamba za Nefi, hadi utawala wa huyu mfalme
Benyamini, ambaye alizungumziwa na Amaleki, nilipekua miongoni mwa haya
maandishi niliyopewa, na nikapata hizi bamba, ambazo zilikuwa na hii historia
ndogo ya manabii, kutoka Yakobo hadi utawala huu wa mfalme Benyamini, na pia
maneno mengi ya Nefi.
4 Na vitu ambavyo vimo katika bamba hizi vikinifurahisha, kwa sababu ya unabii
wa kuja kwa Kristo; na baba zangu wakijua kwamba vingi vimetimizwa; ndio, na pia
najua kwamba vingi vilivyobashiriwa kutuhusu sisi hadi siku hii vimetimizwa, na
vingi ambavyo vitazidi leo lazima kwa ukweli vitimizwe—
5 Kwa hivyo, nachagua vitu hivi, ili nimalize maandishi yangu juu yao, maandishi
ambayo nitatoa kutoka bamba za Nefi; na siwezi kuandika hata sehemu moja ya mia
ya vitu vya watu wangu.
6 Lakini tazama, nitachukua bamba hizi, ambazo zina unabii na ufunuo, na
kuziweka pamoja na mabaki ya yale maandishi yangu, kwani ni bora kwangu; na
ninajua kwamba yatakuwa bora kwa ndugu zangu.
7 Na ninatenda haya kwa madhumuni ya busara; kwani ninanong'onezewa,
kulingana na kazi za Roho wa Bwana aliye ndani yangu. Na sasa, sijui mambo yote;
lakini Bwana anajua vitu vyote vitakavyokuja; kwa hivyo, anafanya kazi ndani yangu
ili nitende kulingana na nia yake.
8 Na sala yangu kwa Mungu ni kuhusu ndugu zangu, kwamba wamfahamu Mungu
tena, ndio, ukombozi wa Kristo; ili tena wawe watu wema.
9 Na sasa mimi, Mormoni, namalizia maandishi yangu, ambayo ninayatoa kutoka
bamba za Nefi; na ninayaandika kulingana na maarifa na ufahamu ambao Mungu
amenipatia.
10 Kwa hivyo, ikawa kwamba baada ya Amaleki kumpatia Mfalme Benyamini
bamba hizi, alizichukua na kuziweka pamoja na zile bamba zingine, ambazo
zilikuwa na maandishi ambayo yalitolewa na wafalme, kutoka kizazi hadi kizazi
mpaka siku za Benyamini.
11 Na yalipitishwa chini kutoka mfalme Benyamini, kutoka kizazi hadi kizazi
mpaka zikafika mikononi mwangu. Na mimi, Mormoni, naomba Mungu kwamba
yahifadhiwe tangu sasa. Na ninajua kwamba zitahifadhiwa; kwani kuna mambo
makuu ambayo yameandikwa juu yake, ambayo yatahukumu watu wangu na ndugu
zao katika siku ile kuu ya mwisho, kulingana na neno la Mungu ambalo
limeandikwa.
12 Na sasa, kuhusu huyu mfalme Benyamini—alikuwa na mabishano fulani
miongoni mwa watu wake.
13 Na ikawa kwamba pia majeshi ya Walamani yaliondoka nchi ya Nefi, ili yapigane

na watu wake. Lakini tazama, mfalme Benyamini alikusanya pamoja majeshi yake,
na akawapinga; na alipigana kwa nguvu ya mkono wake mwenyewe, akitumia
upanga wa Labani.

14 Na kwa nguvu za Bwana walipigana dhidi ya maadui wao, hadi wakawaua maelfu
mengi ya Walamani. Na ikawa kwamba walipigana na Walamani hadi wakawaondoa
kutoka nchi yao yote ya urithi wao.

15 Na ikawa kwamba baada ya kuwa na Kristo wengi bandia, na vinywa vyao
vikafungwa, na wakaadhibiwa kulingana na makosa yao;

16 Na baada ya kuwepo na manabii wa bandia, na wahubiri bandia na walimu
bandia miongoni mwa watu, na hawa wote wakiwa wameadhibiwa kulingana na
makosa yao; na baada ya kuwepo na ubishi mwingi na ukengefu mwingi kwa
Walamani, tazama, ikawa kwamba mfalme Benyamini, kwa msaada wa manabii
watakatifu waliokuwa miongoni mwa watu wake—

17 Kwani tazama, mfalme Benyamini alikuwa mtu mtakatifu, na alitawala watu
wake kwa haki; na kulikwa na watu wengi watakatifu nchini ile, na walinena neno la
Mungu kwa nguvu na mamlaka; na walitumia ukali mwingi kwa sababu ya utukutu
wa wale watu—

18 Kwa hivyo, kwa msaada wa hawa, mfalme Benyamini, kwa kutumikia kwa nguvu
zote za mwili wake na uwezo wa nafsi yake yote, na pia manabii, aliimarisha tena
amani katika nchi ile.

# Kitabu cha Mosia

## Mosia 1

1 Na sasa kulikuwa hakuna ubishi katika nchi yote ya Zarahemla, miongoni mwa
watu wote wa mfalme Benyamini, hata kwamba mfalme Benyamini akawa na amani
katika siku zake zote zilizo salia.
2 Na ikawa kwamba alipata wana watatu; na akawaita majina yao, Mosia, na
Helorumu, na Helamani. Na akasababisha kwamba wafunzwe kwa lugha yote ya
babu zake, ili wawe watu wenye ufahamu; na ili wajue kuhusu unabii uliokuwa
umezungumzwa kwa vinywa vya babu zao, ambao ulikuwa umetolewa na mkono wa
Bwana.
3 Na pia akawafunza kuhusu maandishi ambayo yalikuwa yamechorwa kwenye zile
bamba za shaba, akisema: Wana wangu, nataka mkumbuke kwamba kama sio hizi
bamba, ambazo zina maandishi haya na amri hizi, lazima tungeteseka kwa kutojua,
mpaka wakati huu, kwa kutofahamu siri za Mungu.
4 Kwani haingewezekana kwamba baba yetu Lehi, angevikumbuka vitu hivi vyote,
kuvifundisha kwa watoto wake, bila usaidizi wa bamba hizi; kwani yeye alikuwa
amefunzwa kwa lugha ya Wamisri kwa hivyo yeye aliweza kusoma michoro hii, na
kuwafunza watoto wake, ili nao wawafunze watoto wao, na hivyo kutimiza amri za
Mungu, hadi wakati huu.
5 Nawaambia, wana wangu, kama sio kwa sababu ya vitu hivi, ambavyo
vimewekwa na kuhifadhiwa kwa mkono wa Mungu, ili tusome na tufahamu siri
zake, na tuwe na amri zake kila mara machoni mwetu, hata kwamba baba zetu
wangefifia katika kutoamini, na tungekuwa kama ndugu zetu, Walamani, ambao
hawajui lolote kuhusu vitu hivi, au hata kwamba hawaviamini wanapofundishwa,
kwa sababu ya desturi za baba zao, ambazo sio sawa.
6 Enyi wana wangu, ningependa mkumbuke kwamba hii misemo ni ya kweli, na
pia kwamba haya maandishi ni ya kweli. Na tazama, pia bamba za Nefi, ambazo zina
maandishi na misemo ya baba zetu tangu walipotoka Yerusalemu hadi sasa, na ni za
kweli; na tunaweza kujua ukweli wao kwa sababu ziko mbele machoni mwetu.
7 Na sasa, wana wangu, ningependa kwamba myapekue kwa bidii, ili mfaidike; na
ningependa kwamba mtii amri za Mungu, ili mfanikiwe nchini kulingana na ahadi
ambazo Bwana aliwafanyia babu zetu.
8 Na ni vitu vingi zaidi ambavyo mfalme Benyamini aliwafunza wana wake,
ambavyo havijaandikwa kwenye kitabu hiki.
9 Na ikawa kwamba baada ya mfalme Benyamini kumaliza kuwafunza wana wake,
kwamba alizeeka, na akaona kwamba lazima hivi karibuni aelekee katika ile njia ya
ulimwengu wote; kwa hivyo, akadhani kwamba ni muhimu aukabidhi ufalme wake
kwa mmoja wa wana wake.
10 Kwa hivyo, akasababisha Mosia asimamishwe mbele yake; na haya ndiyo maneno
ambayo alimzungumzia, akisema: Mwana wangu, nataka utangaze kote nchini hii
miongoni mwa watu hawa wote, au watu wa Zarahemla, na watu wa Mosia ambao
wanaishi katika nchi hii, kwamba wakusanyike pamoja; kwani kesho nitawatangazia
watu wangu kwa kinywa changu kwamba wewe ni mfalme na mtawala juu ya hawa
watu, ambao Bwana Mungu wetu ametupatia.
11 Na juu ya hayo, nitawapatia watu hawa jina, ili waweze kutofautishwa kutokana

na watu wote ambao Bwana Mungu aliwatoa kutoka nchi ya Yerusalemu; na hivi ninatenda kwa sababu wamekuwa watu wa bidii kwa kutii amri za Bwana.

12 Na ninawapa jina ambalo halitafutwa, ila tu kwa dhambi.

13 Ndio, na zaidi ninakwaambia, kwamba ikiwa watu hawa walioheshimiwa na Bwana zaidi wataanguka kwenye dhambi, na wawe waovu na watu wazinifu, kwamba Bwana atawatoa, ili wawe wanyonge kama ndugu zao; na hatawalinda tena kwa nguvu zake zisizokuwa na kipimo; kama vile alivyowahifadhi babu zetu.

14 Kwani ninakwambia, kwamba kama hangenyosha mkono wake kuwahifadhi babu zetu lazima wangeanguka mikononi mwa Walamani, na waumie kwa sababa ya chuki yao.

15 Na ikawa kwamba baada ya mfalme Benyamini kumaliza kumzungumzia mwana wake, kwamba aliweka mikononi mwake mambo yote ya ufalme.

16 Na zaidi ya hayo, aliweka mikononi mwake yale maandishi yaliyochorwa kwenye bamba za shaba; na pia zile bamba za Nefi; na pia, upanga wa Labani, na dira au kielekezo, ambacho kiliwaelekeza babu zetu kupita nyikani, ambacho kilitayarishwa na mkono wa Bwana ili waelekezwe, kila mmoja kulingana na utiifu na bidii waliompatia.

17 Kwa hivyo, kwa vile hawakuwa waaminifu hawakufanikiwa wala kuendelea katika safari yao, lakini walirudishwa nyuma, na kujiteremshia hasira ya Mungu juu yao; na kwa hivyo walipigwa kwa njaa na maumivu makali, ili kuwavuruga wakumbuke jukumu lao.

18 Na sasa, ikawa kwamba Mosia aliendा na kutenda kulingana na yale baba yake aliyomwamuru, na kuwatangazia watu wote waliokuwa katika nchi ya Zarahemla kwamba wajikusanye pamoja, ili waende kwenye hekalu kusikiza maneno ambayo baba yake atawazungumzia.

## Mosia 2

1 Na ikawa kwamba baada ya Mosia kutenda kulingana na vile baba yake alivyomwamuru, na kutangaza nchini kote, kwamba watu walikusanyika pamoja nchini kote, ili waende kwenye hekalu kusikia maneno ambayo mfalme Benyamini atawaelezea.

2 Na walikuwa idadi kubwa, hata kuwa wengi sana kwamba hawakuhesabika; kwani walikuwa wameongezeka zaidi na kuwa wengi katika nchi.

3 Na pia walichukua malimbuko ya mifugo yao, ili watoe dhabihu na sadaka za kuteketezwa kwa moto kulingana na sheria ya Musa;

4 Na pia kwamba wamtolee Bwana Mungu wao shukrani, ambaye alikuwa amewaleta kutoka nchi ya Yerusalemu, na ambaye alikuwa amewakomboa kutoka mikono ya maadui zao, na kuwachagulia watu wenye haki kuwa walimu wao, na pia mtu mwenye haki kuwa mfalme wao, ambaye alikuwa ameanzisha amani katika nchi ya Zarahemla, na ambaye aliwafunza kutii amri za Mungu, ili washangilie na kujazwa na upendo kwa Mungu na kwa watu wote.

5 Na ikawa kwamba walipowasili kwenye hekalu, walipiga hema zao kando yake, kila mtu kulingana na jamii yake, akiwa na mke wake, na wana wake, na mabinti zake, na wana wao, na mabinti zao, kutoka mkubwa hadi kwa aliye mdogo, kila jamii ikiwa imetengana na nyingine.

6 Na wakapiga hema zao na kuizingira hekalu, kila mtu akielekeza mlango wa

hema lake kwenye hekalu, ili wakae ndani ya hema zao na kusikia maneno ambayo
mfalme Benyamini angewazungumzia;
7 Kwani umati ulikuwa mkubwa sana hata kwamba mfalme Benyamini hangeweza
kuwafunza wote katika kuta za hekalu, kwa hivyo akaamuru mnara ujengwe, ili
watu wake wasikie maneno ambayo angewazungumzia.
8 Na ikawa kwamba alianza kuwazungumzia watu wake kutoka mnarani; na wote
hawangeweza kusikia maneno yake kwa sababu ya wingi wa umati; kwa hivyo
akasababisha kwamba maneno aliyozungumza yaandikwe na kupelekwa miongoni
mwa wale ambao hawakuwa karibu na sauti yake, ili wao pia wapokee maneno yake.
9 Na haya ndiyo maneno aliyozungumza na kusababisha yaandikwe, akisema:
Ndugu zangu, nyote ambao mmekusanyika pamoja, nyinyi ambao mtasikia maneno
yangu ambayo nitawazungumzia leo; kwani sijawaamrisha kuja hapa ili
kuchezacheza na maneno ambayo nitawazungumzia, lakini kwamba mnisikilize, na
mfungue masikio yenu ili msikie, na mioyo yenu ili mfahamu, na akili zenu ili siri za
Mungu zifunguliwe machoni mwenu.
10 Sijawaamuru kuja hapa ili mniogope, au kwamba mnidhanie kwamba mimi
mwenyewe ni zaidi ya binadamu.
11 Lakini mimi niko kama nyinyi, kwa unyonge wa kila aina mwilini na akilini;
walakini nimechaguliwa na watu hawa, na kutakaswa na baba yangu, na
nikaruhusiwa kwa mkono wa Bwana kwamba niwe mtawala na mfalme wa watu
hawa; na nimelindwa na kuhifadhiwa kwa uwezo wake usio na kipimo, ili
niwatumikie kwa uwezo wote, na nguvu ambazo Bwana amenipatia.
12 Ninawaambia kwamba kwa vile nimekubaliwa kuwatumikia nyinyi maishani
mwangu, hata hadi sasa, na sijatazamia kupata faida ya dhahabu au fedha au aina
yoyote ya utajiri kutoka kwenu;
13 Wala sijaruhusu kwamba mfungwe gerezani, wala nyinyi wenyewe kuwafanya
wengine watumwa, wala kuua, au kupora, au kuiba, au kuzini; wala hata mimi
sijawaruhusu kwamba mtende aina yoyote ya uovu, na nimewafunza nyinyi kwamba
mtii amri za Bwana, katika vitu vyote ambavyo amewaamuru—
14 Na hata mimi, mwenyewe, nimefanya kazi kwa mikono yangu mwenyewe ili
niwatumikie nyinyi, na kwamba msilemewe na makodi, na kwamba msipatwe na
chochote ambacho hamuwezi kuvumilia—na nyinyi ni mashahidi leo, kwa vitu
vyote ambavyo nimewazungumzia siku hii.
15 Lakini, ndugu zangu, sijatenda vitu hivi ili nijivune, wala sisemi vitu hivi ili
niwalaumu; lakini nawaambia vitu hivi ili mjue kwamba sina lawama katika
dhamira yangu mbele ya Mungu siku ya leo.
16 Tazama, nawaambia kwamba kwa sababu niliwaambia kuwa nimewatumikia
maishani mwangu, sitamani kujivuna, kwani nimekuwa tu katika utumishi wa
Mungu.
17 Na tazama, nawaambia vitu hivi ili mpate hekima; ili mjifunze kwamba
mnapowatumikia wanadamu wenzenu mnamtumikia tu Mungu wenu.
18 Tazama, mmeniita mfalme wenu; na kama mimi, ambaye mnaniita mfalme
wenu, ninajichosha kuwatumikia, je, haiwapasi nanyi kujichosha kutumikiana?
19 Na tazama pia, kama mimi, ambaye mnaita mfalme wenu, ambaye
amewatumikia siku zake zote nyinyi, na walakini amekuwa katika utumishi wa
Mungu, ninastahili shukrani kutoka kwenu, Je, inawapasa jinsi gani nyinyi
kumshukuru Mfalme wenu wa mbinguni!

20 Ninawaambia, ndugu zangu, kwamba kama mtamtolea shukrani zote na sifa ambazo nafsi zenu zina uwezo wa kuwa nazo, Mungu aliyewaumba, na aliyewaweka na kuwahifadhi, na kuwasababisha nyinyi kufurahi, na kuwezesha kwamba nyinyi muishi kwa amani kati yenu—

21 Ninawaambia kwamba kama mtamtumikia yule ambaye aliwaumba tangu mwanzo, na anawahifadhi siku kwa siku, kwa kuwaazima pumzi, kwamba muishi na mtembee na kutenda kulingana na nia zenu, na hata kuwasaidia muda kwa muda—nasema, kama mtamtumikia kwa nafsi zenu zote kwa jumla bado mtakuwa watumishi wasioleta faida.

22 Na tazama, yote ambayo anahitaji kutoka kwenu ni kutii amri zake; na amewaahidi kwamba kama mtatii amri zake mtafanikiwa nchini; na kamwe hageuki kutoka kwa yale aliyosema; kwa hivyo, kama mtatii amri zake atawabariki na kuwafanikisha.

23 Na sasa, kwanza, amewaumba, na kuwapatia uhai wenu, ambao anawadai.

24 Na cha pili, anahitaji kwamba nyinyi mtende yale ambayo amewaamuru; kwani kama mtatenda hivyo, atawabariki papo hapo; na kwa hivyo amewalipa. Na hivyo basi bado anawadai, na hata sasa, na baadaye hadi milele na milele; kwa hivyo, je, mna nini ambacho mnajivunia?

25 Na sasa nauliza, je mnaweza kujiongezea chochote wenyewe? Ninawajibu, Hapana. Hamwezi kusema mko hata kuzidi mavumbi ya dunia; ingawa mliumbwa kutoka mavumbi ya dunia; lakini tazama, ni yake yule aliyewaumba.

26 Na mimi, hata mimi, ambaye mnaniita mfalme wenu, sio bora zaidi ya vile mlivyo; kwani mimi pia nilitoka katika mavumbi. Na mnaona kwamba mimi ni mzee, na ninakaribia kuupeleka mwili huu kwenye udongo.

27 Kwa hivyo, kama vile nilivyowaambia kwamba niliwatumikia, nikiwa na dhamira iliyo safi kwa Mungu, hata hivyo wakati huu mimi nimesababisha kwamba mkusanyike pamoja, ili nisipatikane na lawama, na kwamba damu yenu isiwe juu yangu, nitakaposimama mbele ya Mungu ili nihukumiwe kwa vile vitu alivyoniamrisha kuwahusu.

28 Nawaambia kwamba nimesababisha mkusanyike pamoja ili nitoe damu yenu kutoka mavazi yangu, wakati huu ambao ninakaribia kaburi langu, ili niende kwa amani, na roho yangu isiyokufa iungane na kwaya za juu katika kuimba sifa za Mungu aliye wa haki.

29 Na zaidi ya hayo, ninawaambia kwamba nimesababisha mkusanyike pamoja, ili niwatangazie kwamba siwezi kuendelea kuwa mwalimu wenu, wala mfalme wenu;

30 Kwani hata sasa, mwili wangu wote unatetemeka ninapojaribu kuwazungumzia; lakini Bwana Mungu ananisaidia, na ameniruhusu niwazungumzie, na ameniamuru kwamba niwatangazie leo, kwamba mwana wangu Mosia ni mfalme na mtawala wenu.

31 Na sasa, ndugu zangu, nataka mtende kama vile tayari mmetenda. Hadi sasa mmetii amri zangu, na pia amri za baba yangu, na mmefanikiwa, na mmelindwa kwamba msiangukie mikono ya maadui wenu, hata hivyo mkitii amri za mwana wangu, au amri za Mungu ambazo mtapewa naye, mtafanikiwa nchini, na maadui wenu hawatapata uwezo juu yenu.

32 Lakini, Enyi watu wangu, jihadharini kwamba pasiwe na mabishano miongoni mwenu, na mchague kutii pepo mchafu, ambaye alizungumziwa na baba yangu Mosia.

33 Kwani tazama, ole kwa yule anayechagua kutii huyo pepo; kwani akichagua
kumtii, na kuishi na afariki katika dhambi zake, yeye anakunywa adhabu kwa nafsi
yake; kwani yeye hupokea kwa mshahara wake adhabu isiyo na mwisho, kwa sababu
ya kuvunja sheria ya Mungu kinyume cha ufahamu wake.
34 Ninawaambia, kwamba hakuna yeyote miongoni mwenu, ila tu watoto wenu
wadogo ambao hawajafunzwa kuhusu vitu hivi, asiyejua kwamba mnadaiwa milele
na Baba wenu wa mbinguni, kumtolea yote mliyo nayo na vile mlivyo; na pia
mmefundishwa kuhusu maandishi ambayo yana unabii ambao umezungumziwa na
manabii watakatifu, hata hadi wakati baba yetu, Lehi, alipotoka Yerusalemu;
35 Na pia, yote ambayo yamezungumzwa na baba zetu hadi sasa. Na tazama, pia,
walizungumza yale ambayo waliamriwa na Bwana; kwa hivyo, ni ya haki na kweli.
36 Na sasa, nawaambia, ndugu zangu, kwamba baada ya kujua na kufunzwa vitu hivi
vyote, kama mtakosa na kutenda kinyume cha yale yaliyozungumzwa, kwamba
mnajitenga na Roho wa Bwana, kwamba hana nafasi ndani yenu ili awaongoze
katika njia za hekima ili mpate baraka, mafanikio, na kuhifadhiwa—
37 Ninawaambia, kwamba, yule mtu anayetenda haya, huyo ndiye ambaye anamuasi
Mungu kiwazi; kwa hivyo anachagua kutii pepo mchafu, na kuwa adui wa haki yote;
kwa hivyo, Bwana hana nafasi ndani yake, kwani yeye haishi katika hekalu zisizo
takatifu.
38 Kwa hivyo kama mtu huyu hatatubu, na aishi na afe akiwa adui wa Mungu,
matakwa ya haki takatifu huzindua nafsi yake isiyokufa kwa hatia yake mwenyewe,
ambayo humsababisha kutetemeka mbele ya Bwana, na hujaza kifua chake na hatia,
na uchungu, na huzuni, ambayo ni kama moto usiozimika, ambao miale yake hupaa
juu milele na milele.
39 Na sasa ninawaambia, kwamba huruma haina dai juu ya mtu huyo; kwa hivyo
hukumu yake ya mwisho ni kuvumilia mateso yasiyo na mwisho.
40 Ee nyinyi, watu wote wazee, na pia nyinyi vijana, na nyinyi watoto wachanga
mnaoweza kuelewa maneno yangu, kwani nimezungumza wazi kwenu ili muweze
kuelewa, naomba kwamba muamke kwa ukumbusho wa mahali pa kuogofya ya wale
walioanguka kwenye dhambi.
41 Na zaidi, ningetamani mtafakari juu ya hali ya baraka na yenye furaha ya wale
wanaotii amri za Mungu. Kwani tazama, wanabarikiwa katika vitu vyote, vya muda
na vya kiroho; na kama watavumilia kwa uaminifu hadi mwisho watapokewa
mbinguni, kwamba hapo waishi na Mungu katika hali ya furaha isiyo na mwisho.
Enyi kumbukeni, kumbukeni kwamba vitu hivi ni vya kweli; kwani Bwana Mungu
ameyazungumza.

## Mosia 3

1 Na tena ndugu zangu, nataka mnisikilize, kwani nina mengine ya kuwazungumzia;
kwani tazama, nina vitu vya kuwaambia kuhusu vile vitakavyokuja.
2 Na vile vitu nitakavyowaambia nimejulishwa hivyo na malaika wa Mungu. Na
aliniambia: Amka; na nikaamka, na tazama alisimama mbele yangu.
3 Na akaniambia: Amka, na usikilize yale maneno nitakayokuambia; kwani
tazama, nimekuja kukutangazia habari njema ya shangwe kuu.
4 Kwani Bwana amesikia sala zako, na ameuhukumu utakatifu wako, na
amenituma kwako nikutangazie kwamba ushangilie; na kwamba wewe uwatangazie

watu wako, kwamba wao wajazwe na shangwe.
5 Kwani tazama, wakati unakuja, na sio mbali sana, kwamba kwa uwezo, Bwana
Mwenyezi ambaye anatawala, ambaye alikuwa, na yuko kutoka milele yote hadi
milele yote, atashuka chini kutoka mbinguni miongoni mwa watoto wa watu, na
ataishi katika hekalu la udongo, na ataenda miongoni mwa watu, akitenda miujiza
mikuu, kama kuponya wagonjwa, kufufua wafu, kusababisha viwete kutembea,
vipofu kupata kuona, na viziwi kusikia, na kuponya kila aina ya magonjwa.
6 Na atatoa mashetani, au pepo wachafu wanaoishi katika mioyo ya watoto wa
watu.
7 Na lo, atavumilia majaribu, na maumivu ya mwili, njaa, kiu, na uchovu, hata zaidi
ya vile mtu anaweza kuteseka, ila tu hadi kifo; kwani tazama, damu inatiririka
kutoka kwa kila kinyweleo, mateso yake yatakuwa makuu kwa sababu ya maovu na
machukizo ya watu wake.
8 Na ataitwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Baba wa mbingu na dunia, Muumba
wa vitu vyote tangu mwanzo; na mama yake ataitwa Mariamu.
9 Na lo, anawajia walio wake, ili wokovu uwafikie watoto wa watu hata kupitia
imani kwa jina lake; na hata baada ya haya yote bado watamdhania kuwa yeye ni
mwanadamu, na kusema kwamba amepagawa na ibilisi, na kumpiga, na kumsulubu.
10 Na atafufuka siku ya tatu kutoka kwa wafu; na tazama, anasimama kuhukumu
ulimwengu; na tazama, vitu hivi vyote vinafanyika ili hukumu takatifu iwashukie
watoto wa watu.
11 Kwani tazama, na pia damu yake inalipiza dhambi za wale ambao wameanguka
kwa sababu ya dhambi ya Adamu, ambao wameaga dunia bila kuelewa nia ya
Mungu juu yao, au ambao wametenda dhambi bila kujua.
12 Lakini ole, ole kwa yule anayefahamu kwamba anamuasi Mungu! Kwani wokovu
haumjii yeyote ila tu kwa kutubu na kwa imani katika Bwana Yesu Kristo.
13 Na Bwana Mungu amewatuma manabii wake watakatifu miongoni mwa watoto
wa watu, kutangaza vitu hivi kwa kila kabila, taifa, na lugha, ili hapo kwamba yeyote
atakayeamini kwamba Kristo atakuja, hao watapokea msamaha wa dhambi, na
kushangilia kwa shangwe kuu zaidi, kama vile tayari amekuja miongoni mwao.
14 Lakini Bwana Mungu aliona kwamba watu wake walikuwa wenye shingo ngumu,
na akawapatia sheria, hata sheria ya Musa.
15 Na ishara nyingi, na maajabu, na mifano, na vivuli aliwaonyesha kwao, kuhusu
kuja kwake; na pia manabii watakatifu waliwazungumzia kuhusu kuja kwake; na
bado walishupaza mioyo yao, na hawakufahamu kuwa sheria ya Musa haifaidi
chochote isipokuwa kupitia upatanisho wa damu yake.
16 Na hata kama ingewezekana kwamba watoto wadogo wangetenda dhambi
hawangeweza kuokolewa; lakini ninakuambia wamebarikiwa; kwani tazama, kama
vile katika Adamu, au kwa maumbile, wanaanguka, hata hivyo damu ya Kristo
inalipiza dhambi zao.
17 Na zaidi ya hayo, ninawaambia, kwamba hakuna jina lingine litatolewa wala njia
ingine wala mbinu yoyote ambayo wokovu utawashukia watoto wa watu, ila katika
na kupitia jina la Kristo pekee, Bwana Mwenyezi.
18 Kwani tazama anahukumu, na hukumu yake ni ya haki; na mtoto mchanga
anayefariki uchangani mwake haangamii; lakini wanadamu hunywa adhabu kwa
nafsi yao isipokuwa wajinyenyekeze na kuwa kama watoto wadogo, na kuamini
kwamba wokovu ulikuwa, na upo, na utakuja, kwa na katika upatanisho wa damu ya

Kristo, Bwana Mwenyezi.
19 Kwani mwanadamu wa kawaida ni adui kwa Mungu, na amekuwa tangu
kuanguka kwa Adamu, na atakuwa, milele na milele, asipokubali ushawishi wa
Roho Mtakatifu, na kumvua mtu wa kawaida na kuwa mtakatifu kupitia upatanisho
wa Kristo aliye Bwana, na kuwa kama mtoto, mtiifu, mpole, mnyenyekevu,
mvumilivu, mwenye upendo tele, aliye tayari kukubali vitu vyote ambavyo Bwana
anampatia, hata kama vile mtoto hunyenyekea kwa baba yake.
20 Na zaidi ya hayo, ninakuambia, kwamba wakati unakaribia ambako ufahamu wa
Mwokozi utapenya kila taifa, kabila, lugha, na watu.
21 Na tazama, wakati huo utakapofika, hakuna yeyote atakayepatikana bila lawama
mbele ya Mungu, isipokuwa watoto wadogo, isipokuwa tu kupitia kwa toba na
imani katika jina la Bwana Mungu Mwenyezi.
22 Na hata wakati huu, wakati utakapokuwa umewafunza watu wako vitu vile
ambavyo Bwana Mungu wako amekuamuru, hata hivyo bado hawatapatikana na
lawama machoni mwa Mungu, tu kulingana na yale maneno ambayo
nimekuzungumzia.
23 Na sasa nimezungumza maneno ambayo Bwana Mungu ameniamuru.
24 Na Bwana asema hivi: Watasimama kama ushuhuda ung'arao kinyume cha watu
hawa, siku ile ya hukumu; ambako watahukumiwa, kila mtu kulingana na matendo
yake, kama ni mema, au kama ni maovu.
25 Na kama ni maovu watatolewa kwa mawazo mabaya ya hatia yao na machukizo,
ambayo inawasababisha kukimbia kutoka uwepo wa Bwana na kuingia katika hali ya
hofu na mateso yasiyo na mwisho, kutoka ambapo hawawezi kurejea tena; kwa
hivyo wanajiletea hukumu ya milele katika nafsi zao.
26 Kwa hivyo, wamekunywa kutoka kikombe cha ghadhabu ya Mungu, haki
ambayo haiwezi kuwazuia kama vile haingezuia Adamu aanguke kwa sababu ya kula
tunda lililokatazwa; kwa hivyo, hawawezi kupokea huruma milele.
27 Na mateso yao ni kama ziwa la moto na kiberiti, ambalo miale yake haiwezi
kuzimika, na moshi wake hupaa juu milele na milele. Na hivi ndivyo Bwana
ameniamuru mimi. Amina.

## Mosia 4

1 Na sasa, ikawa kwamba baada ya mfalme Benyamini kumaliza kuzungumza maneno
ambayo alikuwa amepewa na malaika wa Bwana, kwamba alitupa macho kwenye
umati, na tazama walikuwa wameinama ardhini, kwani woga wa Bwana ulikuwa
umewajia.
2 Na walikuwa wamejiona wenyewe katika hali yao ya kimwili, hata kuwa ndogo
zaidi ya mavumbi ya dunia. Na wote wakalia kwa sauti moja, wakisema: Ewe
tuhurumie, na utumie damu ya upatanisho wa Kristo kwamba tupokee msamaha wa
dhambi zetu, na mioyo yetu isafishwe; kwani tunamwamini Yesu Kristo, Mwana wa
Mungu, aliyeumba mbingu na dunia, na vitu vyote; ambaye atashuka chini
miongoni mwa watoto wa watu.
3 Na ikawa kwamba baada ya wao kuzungumza maneno haya Roho wa Bwana
aliwashukia, na wakajazwa na shangwe, wakiwa wamepokea msamaha wa dhambi
zao, na kupata amani katika dhamira zao, kwa sababu ya imani tele waliyokuwa nayo
katika Yesu Kristo atakayekuja, kulingana na maneno ambayo mfalme Benyamini

aliwazungumzia.
4 Na mfalme Benyamini tena akafungua kinywa chake na kuanza kuwazungumzia, akisema: Marafiki zangu na ndugu zangu, ukoo wangu na watu wangu, naomba tena mnisikilize, kwamba msikie na kufahamu maneno yangu yaliyosalia.
5 Kwani tazama, ikiwa ufahamu wa wema wa Mungu wakati huu umewaamsha kwa kuona udhaifu wenu, na kwamba hamna thamani katika hali yenu ya kuanguka—
6 Ninawaambia, kama mmepokea ufahamu wa wema wa Mungu, na nguvu zake zisizo na kifani, na hekima yake, na subira yake, na uvumilivu wake kwa watoto wa watu; na pia, upatanisho uliotayarishwa tangu msingi wa ulimwengu, ili wokovu umshukie yeyote atakayemwamimi Bwana, na awe mwenye bidii katika kushika amri zake, na kuendelea katika imani hata hadi mwisho wa maisha yake, ninamaanisha maisha ya mwili wa muda—
7 Ninasema, kwamba huyu ndiye yule mtu anayepokea wokovu, kupitia kwa upatanisho ambao ulitayarishwa tangu msingi wa ulimwengu kwa wanadamu wote, ambao walikuwa wakati wowote tangu kuanguka kwa Adamu, au wale walio, au wale watakaokuwepo wakati wowote, hata hadi mwisho wa ulimwengu.
8 Na hii ndiyo njia ambayo kwayo wokovu unakuja. Na hakuna wokovu mwingine ila huu ambao umezungumziwa; wala hakuna masharti mengine ambayo kwayo mwanadamu anaweza kuokolewa ila tu masharti yale ambayo nimewaambia.
9 Mwamini Mungu; amini kwamba yupo, na kwamba aliumba vitu vyote, katika mbingu na katika ardhi, amini kwamba ana hekima yote, na uwezo wote, mbinguni na ardhini; mwamini kwamba mwanadamu hafahamu vitu vyote ambavyo Bwana anavyoweza kufahamu.
10 Na tena, mwamini kwamba lazima mtubu dhambi zenu na kuziacha, na kujinyenyekeza mbele ya Mungu; na muombe kutoka moyo wa kweli ili awasamehe; na sasa, kama mnaamini hivi vitu vyote hakikisheni kwamba mnavitenda.
11 Na tena nawaambia vile nilivyosema awali, kwamba kama vile mmefahamu utukufu wa Mungu, au kama mmejua wema wake na kuonja upendo wake, na kupokea msamaha wa dhambi zenu, ambao unawaletea shangwe tele nafsini mwenu, hata hivyo nataka mkumbuke, na kila wakati mshikilie ukumbusho, wa ukuu wa Mungu, na unyonge wenu, na wema wake na subira yake kwenu nyinyi; viumbe vinyonge, na mjinyenyekee kwa unyenyekevu mwingi, mkililingana jina la Bwana kila siku, na kusimama imara katika imani kwa yale yanayokuja, ambayo yalizungumzwa kwa kinywa cha malaika.
12 Na tazama, ninawaambia kwamba kama mtafanya haya mtapokea furaha daima, na kujazwa na upendo wa Mungu, na daima kuhifadhi msamaha wa dhambi zenu; na mtaendelea mkiwa katika ufahamu wa utukufu wa yule aliyewaumba, au katika ufahamu wa yale yaliyo ya haki na kweli.
13 Na hamtataka kuumizana, lakini mtaishi kwa amani, na kumpatia kila mtu anachostahili.
14 Na hamtakubali watoto wenu kupatwa na njaa, au kukaa uchi; wala hamtakubali kwamba wavunje sheria za Mungu, na kupigana na kutetanisha moja kwa mwingine, na kumtumikia ibilisi, ambaye ni bwana wa dhambi, au aliye pepo mchafu ambaye alizungumziwa na babu zetu, yeye akiwa adui wa utakatifu wote.
15 Lakini nyinyi mtawafunza kutembea katika njia za kweli na za kiasi; mtawafunza kupendana, na kutumikiana.
16 Na pia, wenyewe mtawasaidia wale wanaohitaji usaidizi wenu; mtawatolea

misaada wale wanaohitaji; na hamtakubali kwamba maombi ya mwombaji kuwa bure, na kumfukuza ili aangamie.

17 Pengine wewe utasema: Huyu mtu amejiletea taabu; kwa hivyo nitazuia mkono wangu, na sitampatia chakula changu, wala kumtolea msaada ili asiteseke, kwani maadhibio yake ni ya haki—

18 Lakini nakwambia, Ewe mwanadamu, yeyote anayefanya hivyo basi huyo anayo sababu kuu ya kutubu; na asipotubu hilo ambalo ametenda ataangamia milele, na hana haja na ufalme wa Mungu.

19 Kwani tazama, si sisi wote ni waombaji? Je, si sisi sote tunamtegemea yule Mmoja, aliye Mungu, kwa mali yote tuliyo nayo, kwa chakula na mavazi, na kwa dhahabu, na kwa fedha, na kwa kila utajiri tulio nao?

20 Na tazama, hata sasa hivi, mmekuwa mkililingana jina lake, na mkiomba msamaha wa dhambi zenu. Na je amefanya muombe bure? La; amewashushia roho yake, na kusababisha kwamba mioyo yenu ijae shangwe, na kusababisha vinywa vyenu vifungwe ili msipate kuongea, kwa sababu ya ile shangwe yenu tele.

21 Na sasa, kama Mungu, aliyewaumba, ambaye mnamtegemea kwa mahitaji yenu na kwa yote mlio nayo na vile mlivyo, huwapatia chochote mnacho omba kilicho sahihi, kwa imani, mkiamini kwamba mtapokea, Ee hata, inawapasa nyinyi kusaidiana mmoja kwa mwingine.

22 Na kama unamhukumu mtu yule anayekulilia kwa msaada ili asiangamie, na kumshutumu, jinsi gani hukumu yako itakuwa ya haki kwa sababu ya kuzuia msaada wako, ambao sio wako bali ni wa Mungu, ambaye pia maisha yako ni yake; na walakini humlilii, wala kutubu kwa kile kitu ambacho umetenda.

23 Ninawaambia, ole kwa yule mtu, kwani ataangamia na mali yake; na sasa, ninasema vitu hivi kwa wale walio matajiri kwa vitu vya ulimwengu huu.

24 Na tena, nawaambia walio masikini, nyinyi ambao hamna lakini mnayo ya kutosha, kwamba muishi siku kwa siku; namaanisha nyinyi nyote ambao mnawanyima mwombaji, kwa sababu hamna; ningetaka mseme mioyoni mwenu kwamba: Simpi kwa sababu sina, lakini kama ningekuwa nayo, ningempa.

25 Na sasa, kama mtasema hivi mioyoni mwenu mtakuwa hamna hatia, la sivyo mmehukumiwa; na hukumu yenu ni ya haki kwa sababu mnatamani yale ambayo hamjapokea.

26 Na sasa, kwa sababu ya vitu hivi ambavyo nimewazungumzia—kwamba, ili mhifadhi msamaha wa dhambi zenu siku kwa siku, ili mtembee bila hatia mbele ya Mungu—ningetaka kwamba muwapatie masikini mali yenu, kila mtu kulingana na ile aliyo nayo, kwa mfano kulisha wenye njaa, kuvisha walio uchi, kuwatembelea wagonjwa na kuwahudumia katika haja zao, kiroho na kimwili, kulingana na matakwa yao.

27 Na mhakikishe kwamba vitu hivi vyote vinafanywa kwa hekima na mpango; kwani haimpasi mwanadamu kukimbia zaidi kuliko nguvu zake. Na tena, ni lazima awe na bidii, ili ashinde zawadi; kwa hivyo, vitu vyote lazima vitendeke kwa mpango.

28 Na ningependa mkumbuke, kwamba yeyote miongoni mwenu anayeazima chochote kutoka kwa jirani yake lazima arudishe kile alicho kiazima, kulingana na vile alivyokubali, la sivyo utatenda dhambi; na pengine wewe utamsababisha jirani yako kutenda dhambi pia.

29 Na mwishowe, siwezi kuwaelezea vitu vyote ambavyo vinaweza kuwasababisha kutenda dhambi; kwani kuna njia nyingi na mbinu, nyingi sana hata kwamba siwezi

kuzihesabu.
30 Lakini kwa haya naweza kuwaambia hivi, kwamba msipojichunga wenyewe, na
mawazo yenu, na maneno yenu, na matendo yenu, na kufuata sheria za Mungu, na
kuendelea kwa imani katika mambo yale mmesikia kuhusu kuja kwa Bwana, hadi
mwisho wa maisha yenu, lazima mtaangamia. Na sasa, Ee mwanadamu, kumbuka,
na usiangamie.

## Mosia 5

1 Na sasa, ikawa kwamba wakati mfalme Benyamini alipomaliza kuwazungumzia
watu wake, alituma ujumbe miongoni mwao, akitamani kujua kama watu wake
wameyaamini maneno ambayo alikuwa amewazungumzia.
2 Na wote wakalia kwa sauti moja, wakisema: Ndio, tunaamini maneno yote
ambayo umetuzungumzia; na pia, tunajua uhakika na ukweli wao, kwa sababu ya
Roho wa Bwana Mwenyezi, ambaye ameleta mabadiliko makuu ndani yetu, au
mioyoni yetu, hata kwamba hatuna tamaa ya kutenda maovu tena, lakini kutenda
mema daima.
3 Na sisi, wenyewe, pia, kwa wema mkuu wa Mungu, na madhihirisho ya Roho
wake, tunayo maono makuu ya yale yatakayokuja; na kama ingefaa, tungetoa unabii
wa vitu vyote.
4 Na ni kwa imani katika vitu vile ambavyo mfalme wetu ametuzungumzia
ambavyo vimetuletea ufahamu huu mkuu, ambayo kwayo tunasherekea kwa
shangwe kuu sana.
5 Na tunataka tuagane na Mungu wetu ili tutende nia yake, na tuwe watiifu kwa
amri zake kwa vitu vyote atakavyotuamuru, katika maisha yetu yaliyosalia, kwamba
tusijiletee sisi wenyewe mateso yasiyo na mwisho, kama vile alivyosema malaika,
kwamba tusinywe kutoka kile kikombe cha ghadhabu ya Mungu.
6 Na sasa, haya ndiyo maneno ambayo mfalme Benyamini aliwatakia; na kwa
hivyo akawaambia; Mmezungumza maneno yale ambayo nilitaka; na agano ambalo
mmefanya ni agano takatifu.
7 Na sasa, kwa sababu ya agano lile ambalo mmefanya mtaitwa watoto wa Kristo,
wana wake, na mabinti zake; kwani tazama, siku hii amewazaa kiroho; kwani
mnasema kwamba mioyo yenu inabadilishwa kwa imani katika jina lake; kwa hivyo,
amewazaa na mkawa wana wake na mabinti zake.
8 Na chini ya jina hili mmefanywa huru, na hakuna jina lingine ambalo linaweza
kuwafanya muwe huru. Hakuna jina lingine ambalo kwayo huleta wokovu; kwa
hivyo, ningependa mjivike juu yenu jina la Kristo, nyote ambao mmeingia katika
agano na Mungu kwamba mtakuwa watiifu hadi mwisho wa maisha yenu.
9 Na itakuwa kwamba yeyote atakayefanya hivi atakuwa katika mkono wa kulia wa
Mungu, kwani atajua jina ambalo anaitwa; kwani ataitwa kwa jina la Kristo.
10 Na sasa itakuwa kwamba, yeyote asiyejitundika jina la Kristo lazima aitwe kwa
jina lingine; kwa hivyo, anajikuta kwenye mkono wa kushoto wa Mungu.
11 Na nataka pia mkumbuke, kwamba hili ndilo jina ambalo nilisema kwamba
nitawapatia ambalo kamwe halitafutwa, ila tu kwa dhambi; kwa hivyo, jichungeni
kwamba msianguke dhambini, kwamba jina hilo lisifutwe kutoka mioyo yenu.
12 Ninawaambia, nataka kwamba mkumbuke kudumisha jina ambalo limeandikwa
mioyoni mwenu, kwamba msipatikane kwenye mkono wa kushoto wa Mungu,

lakini kwamba msikie na kujua sauti ambayo itawaita, na pia, lile jina ambalo atawaita.

13 Kwani ni vipi mtu atamjua yule bwana ambaye hajamtumikia, na aliye mgeni kwake, na yuko mbali katika mawazo na nia za moyo wake?

14 Na tena, je mtu huchukua punda wa jirani yake, na kumweka? Ninawambia, La; hatakubali hata ale miongoni mwa mifugo yake, lakini atamfukuza, nakumtupilia mbali. Nawambia, itakuwa hivyo nanyi msipojua ni kwa jina gani mtakaloitwa.

15 Kwa hivyo, nataka muwe imara na msiotingishika, daima mkitenda matendo mema, ili Kristo, Bwana Mungu Mwenyezi, awaweke muhuri wake, ili mletwe mbinguni, ili mpokee wokovu usio na mwisho na uzima wa milele, kwa hekima, na uwezo, na haki na rehema za yule aliyeumba vitu vyote, mbinguni na ardhini, ambaye ni Mungu juu ya yote. Amina.

## Mosia 6

1 Na sasa, mfalme Benyamini alifikiria ni vyema, baada ya kumaliza kuongea kwa watu wake, kwamba achukue majina ya wale wote ambao walikuwa wameingia kwenye agano na Mungu kutii amri zake.

2 Na ikawa kwamba hapakuwa yeyote, ila tu watoto wadogo, ambao hawakuingia kwenye agano na kujitundika jina la Kristo.

3 Na tena, ikawa kwamba wakati mfalme Benyamini alipomaliza vitu hivi vyote, na kumtawaza mwana wake Mosia kuwa mtawala na mfalme wa watu wake, na kumpatia masharti yote kuhusu ule ufalme, na pia kuteua makuhani wafunze watu, ili wasikie na kujua amri za Mungu, na kuwachochea ili wakumbuke kile kiapo walichofanya, akalikiza ule umati, na wakarejea, kila mmoja, kulingana na jamii zao, manyumbani kwao.

4 Na Mosia akaanza kutawala badala ya baba yake. Na alianza kutawala alipokuwa na umri wa miaka thelathini, ikatimia, miaka mia nne, sabini na sita tangu Lehi aondoke Yerusalemu.

5 Na mfalme Benyamini akaishi miaka mitatu na kufariki.

6 Na ikawa kwamba mfalme Mosia alifuata njia za Bwana, na kufuata hukumu zake na maagizo yake, na kutii amri zake katika vitu vyote alivyomwamuru.

7 Na mfalme Mosia akasababisha watu wake kulima ardhi. Na pia yeye, mwenyewe, akalima ardhi, ili asiwe mzigo kwa watu wake, na kwamba atende kulingana na vile baba yake alivyotenda katika vitu vyote. Na hapakuwa na ubishi miongoni mwa watu wake wote kwa kipindi cha miaka mitatu.

## Mosia 7

1 Na sasa, ikawa kwamba baada ya mfalme Mosia kuwa na amani kwa kipindi cha miaka mitatu, alitaka kujua kuhusu wale watu walioenda kuishi katika nchi ya Lehi-Nefi, au katika mji wa Lehi-Nefi; kwani watu wake hawakusikia chochote kutoka kwao tangu waondoke nchi ya Zarahemla; kwa hivyo, walimchokesha kwa maswali yao.

2 Na ikawa kwamba mfalme Mosia akaruhusu vijana wao kumi na sita wenye nguvu waende katika nchi ya Lehi-Nefi, kupeleleza kuhusu ndugu zao.

3 Na ikawa kwamba kesho yake walianza safari yao, wakiwa na mmoja aliyeitwa
Amoni, yeye akiwa mtu mwenye nguvu na shujaa, na uzao wa Zarahemla; na
alikuwa pia kiongozi wao.
4 Na sasa, hawakujua njia watakayosafiria huko nyikani ili wafike nchi ya
Lehi-Nefi; kwa hivyo walizungukazunguka huko nyikani kwa siku nyingi, hata siku
arubaini waliozunguka.
5 Na walipozunguka siku arubaini walifika kwenye kilima, ambacho kiko
kaskazini mwa nchi ya Shilomu, na hapo wakapiga hema zao.
6 Na Amoni akawachukua ndugu zake watatu, na majina yao yalikuwa Amaleki,
Helemu, na Hemu, na wakaelekea katika nchi ya Nefi.
7 Na tazama, wakakutana na mfalme wa watu waliokuwa katika nchi ya Nefi, na
katika nchi ya Shilomu; na wakazingirwa na walinzi wa mfalme, na wakakamatwa,
na kufungwa, na kuwekwa gerezani.
8 Na ikawa kwamba baada ya kuwa gerezani siku mbili waliletwa tena mbele ya
mfalme, na mafungo yao yakafunguliwa; na wakasimama mbele ya mfalme, na
walikubaliwa, kwa usahihi zaidi kuamriwa, kwamba wajibu maswali ambayo
atawauliza.
9 Na akawaambia: Tazama, mimi ni Limhi, mwana wa Nuhu, ambaye alikuwa
mwana wa Zenivu, ambaye alitoka nchi ya Zarahemla kurithi nchi hii, ambayo
ilikuwa nchi ya baba zao, ambaye aliteuliwa kuwa mfalme kwa sauti ya watu.
10 Na sasa, nataka kujua kwa nini mlikuwa jasiri hata mkakaribia kuta za mji, wakati
mimi, mwenyewe, nilikuwa na walinzi wangu huko nje?
11 Na sasa, ni kwa kusudi hili nimeruhusu mhifadhiwe, ili niwaulize, au kama sio
hivyo ningeamuru kwamba walinzi wangu wawaue. Mmeruhusiwa kuongea.
12 Na sasa, wakati Amoni alipofahamu kwamba ameruhusiwa kuongea, alisogea
mbele na kuinama mbele ya mfalme; na akainuka na kusema: Ee mfalme,
ninamshukuru Mungu leo kwamba bado niko hai, na nimeruhusiwa kuongea; na
nitajaribu kuongea kwa ujasiri;
13 Kwani nina hakika kwamba kama ungenijua hungeruhusu kwamba nifungwe
kwa hizi kamba. Kwani mimi ni Amoni, na mimi ni uzao wa Zarahemla, na
nimekuja kutoka nchi ya Zarahemla kupeleleza kuhusu ndugu zetu, ambao Zenivu
aliwatoa kutoka nchi hiyo.
14 Na sasa, ikawa kwamba baada ya Limhi kusikia maneno ya Amoni, alikuwa na
furaha tele, na akasema: Sasa, najua kwa hakika kwamba ndugu zangu ambao
walikuwa katika nchi ya Zarahemla bado wako hai. Na sasa, nitasherehekea; na
kesho nitawasababisha watu wangu washerehekee pia.
15 Kwani tazama, sisi tuko utumwani mwa Walamani, na tunatozwa kodi ambayo ni
ngumu kuvumilia. Na sasa, tazama, ndugu zetu watatukomboa kutoka huu utumwa
wetu, au kutoka mikononi mwa Walamani, na tutakuwa watumwa wao; kwani ni
afadhali tuwe watumwa wa Wanefi badala ya kulipa kodi kwa mfalme wa Walamani.
16 Na sasa, mfalme Limhi akawaamuru walinzi wake kwamba wasimfunge tena
Amoni wala ndugu zake, lakini akawasababisha kuenda katika kilima kile
kilichokuwa kaskazini mwa Shilomu, na kuleta ndugu zake mjini, ili wale, na
kunywa, na wajipumzishe kutoka uchovu wa safari yao; kwani walikuwa
wameteseka katika vitu vingi; walikuwa wamepata mateso ya njaa, kiu, na uchovu.
17 Na sasa, ikawa kwamba kesho yake mfalme Limhi akatuma tangazo miongoni
mwa watu wake, kwamba wakusanyike pamoja kwenye hekalu, ili wasikie maneno

ambayo angewazungumzia.
18 Na ikawa kwamba walipokusanyika pamoja aliwazungumzia hivi, akisema: Ee
nyinyi, watu wangu, inueni vichwa vyenu na mfarijiwe; kwani tazameni, wakati
umewadia, au hauko mbali sana, ambapo hatutakuwa chini ya utawala wa maadui
zetu tena, ijapokuwa jitihada zetu nyingi, ambazo zimekuwa za bure; lakini naamini
kwamba bado tunaweza kupata ushindi.
19 Kwa hivyo, inueni vichwa vyenu, na msherehekee, na muweke imani yenu kwa
Mungu, katika huyo Mungu ambaye alikuwa ni Mungu wa Ibrahimu, na Isaka, na
Yakobo; na pia, yule Mungu aliyewatoa wana wa Israeli kutoka nchi ya Misri, na
kusababisha kwamba watembee katika Bahari ya Shamu kwa nchi kavu, na
kuwalisha mana ili wasiangamie huko nyikani; na aliwatendea vitu vingi zaidi.
20 Na tena, huyo Mungu amewatoa babu zetu kutoka nchi ya Yerusalemu, na
amewaweka na kuwahifadhi watu wake hadi sasa; na tazameni, ni kwa sababu ya
maovu na machukizo yetu kwamba ametuleta utumwani.
21 Na nyote ni mashahidi siku ya leo, kwamba Zenivu, ambaye alifanywa kuwa
mfalme wa watu hawa, yeye akiwa mwenye bidii nyingi kwa kurithi nchi ya babu
zake, kwa hivyo alidaganyika kwa ujanja na hila za mfalme Lamani, ambaye baada ya
kuingia katika mkataba na mfalme Zenivu, na baada ya kumpatia sehemu ya ile
nchi, au hata mji wa Lehi-Nefi, na mji wa Shilomu; na ardhi iliyoizingira—
22 Na alitenda haya yote, kwa kusudi moja, la kuwatia hawa watu chini au
utumwani. Na tazameni, sasa sisi tunalipa ushuru kwa mfalme wa Walamani,
ambayo ni nusu ya mahindi yetu, na shayiri yetu, na hata kila aina ya nafaka yetu, na
nusu ya mazao ya mifugo na wanyama wetu; na hata nusu ya chochote ambacho
tunacho mfalme wa Walamani hutudai, au maisha yetu.
23 Na sasa, si hii ni vigumu kuvumiliwa? Na je, si haya maumivu yetu, ni makuu?
Tazameni sasa, jinsi gani tuna sababu kuu ya kuomboleza.
24 Ndio, nawaambia, sababu za kuomboleza kwetu ni kuu; kwani tazameni, ni
ndugu zetu wangapi wameuawa, na damu yao kumwagwa bure, na yote kwa sababu
ya dhambi.
25 Kwani kama watu hawa hawangeanguka dhambini Bwana hangeruhusu kwamba
ovu hili kubwa liwashukie. Lakini tazameni, hawakusikiza maneno yake; lakini
mabishano yalitokea miongoni mwao, hata kwamba wakamwaga damu miongoni
mwao.
26 Na wamemuua nabii wa Bwana; ndio, mtu aliyeteuliwa na Mungu, ambaye
aliwaelezea kuhusu uovu wao na machukizo yao, na kutoa unabii wa vitu vingi
vitakavyokuja, ndio, hata kuja kwa Kristo.
27 Na kwa sababu aliwaambia kwamba Kristo ndiye Mungu, Baba wa vitu vyote, na
kusema kwamba atajichukulia mfano wa mwanadamu, na utakuwa ni ule mfano
ambao mwanadamu alikuwa ameumbwa nao tangu mwanzo; au kwa maneno
mengine, alisema kwamba mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu, na
kwamba Mungu atashuka chini miongoni mwa watoto wa watu, na atachukua juu
yake mwili na damu, na aende usoni mwa dunia—
28 Na sasa, kwa sababu alisema hivi, walimuua; na walifanya vitu vingi ambavyo
viliwashushia ghadhabu ya Mungu. Kwa hivyo, ni nani anayeshangaa kwamba wako
utumwani, na kwamba wamepigwa kwa mateso makali?
29 Kwani tazameni, Bwana amesema: Mimi sitawafariji watu wangu katika siku ile
ya dhambi zao; lakini mimi nitazuia njia zao kwamba wasifanikiwe; na matendo yao

yatakuwa ni kama kizuizi mbele yao.
30 Na tena, anasema: Kama watu wangu watapanda uchafu watavuna makapi
katika tufani; na matokeo yake ni sumu.
31 Na tena anasema: Kama watu wangu watapanda uchafu watavuna upepo wa
mashariki, ambao huleta maangamizo ya ghafla.
32 Na sasa, tazameni, ahadi ya Bwana imetimizwa, na mmepigwa na kusumbuliwa.
33 Lakini kama mtamrudia Bwana kwa moyo wa lengo moja, na kumwamini, na
kumtumikia kwa bidii yote akilini, kama mtafanya hivi, yeye atawaokoa, kutoka
utumwani, kulingana na nia yake na mapenzi yake.

## Mosia 8

1 Na ikawa kwamba baada ya mfalme Limhi kumaliza kuwazungumzia watu wake,
kwani aliwazungumzia vitu vingi na ni vichache tu nilivyoandika katika kitabu hiki,
aliwaambia watu wake vitu vyote kuhusu ndugu zao waliokuwa katika nchi ya
Zarahemla.
2 Na akasababisha Amoni asimame mbele ya ule umati, na kuwaelezea yale yote
ambayo yaliwapata ndugu zao tangu Zenivu aondoke kutoka nchi ile hadi ule
wakati ambao yeye mwenyewe aliondoka kutoka nchi ile.
3 Na pia akakariri yale maneno ya mwisho ambayo mfalme Benyamini aliwafunza,
na akayafafanua kwa watu wa mfalme Limhi, ili wafahamu yale maneno yote
ambayo alizungumza.
4 Na ikawa kwamba baada ya kufanya haya yote, kwamba mfalme Limhi alilikiza
ule umati, na kusababisha kila mmoja arudi nyumbani kwake.
5 Na ikawa kwamba alisababisha zile bamba ambazo zilikuwa na maandishi ya
watu wake tangu watoke nchi ya Zarahemla, ziletwe mbele ya Amoni, ili azisome.
6 Sasa, baada ya Amoni kusoma yale maandishi, mfalme alimuuliza kama anajua
kutafsiri lugha, na Amoni akamwambia kwamba hangeweza.
7 Na mfalme akamwambia: Nikiwa nimehuzunishwa na masumbuko ya watu
wangu, nilisababisha watu wangu arubaini na watatu wasafiri nyikani, ili pengine
waweze kuipata nchi ya Zarahemla, ili tuwaombe ndugu zetu watukomboe kutoka
utumwani.
8 Na walipotea huko nyikani kwa muda wa siku nyingi, lakini bado walikuwa na
bidii, na hawakuipata ile nchi ya Zarahemla lakini walirejea katika nchi hii, baada ya
kusafiri katika nchi iliyo miongoni mwa maji mengi, wakiwa wamegundua nchi
iliyojaa mifupa ya wanadamu, na ya wanyama, na pia ilijaa mabaki ya majengo ya kila
aina, wakiwa wamegundua nchi iliyomilikiwa na watu waliokuwa wengi kama
Waisraeli.
9 Na ili kuthibitisha kwamba vitu walivyosema ni vya kweli wameleta bamba
ishirini na nne ambazo zimejaa michoro, na ni za dhahabu kamili.
10 Na tazama, pia, wameleta dirii, ambazo ni kubwa, na ni za shaba na shaba
nyekundu, na zingali nzuri.
11 Na tena, wameleta panga, ambazo pini zake zimeharibika, na ndimi zake kupata
kutu; na hakuna yeyote nchini anayeweza kutafsiri ile lugha au michoro iliyo
kwenye bamba. Kwa hivyo nilikuuliza: Je unaweza kutafsiri?
12 Nakuambia tena: Je, unajua yeyote anayeweza kutafsiri? Kwani natamani
kwamba haya maandishi yatafsiriwe katika lugha yetu; kwani, pengine, yatatupatia

ufahamu wa sazo la wale watu walioangamizwa, kule haya maandishi yalikotokea;
au, pengine, yatatupatia ufahamu wa hawa watu ambao wameangamizwa; na
natamani kujua sababu ya kuangamizwa kwao.
13 Sasa Amoni akamwambia: Naweza kukuambia kwa uhakika hivi, Ee mfalme,
kuna mtu ambaye anaweza kutafsiri haya maandishi; kwani kuna kitu ambacho
anaweza kutazama, na kutafsiri maandishi yote ya kale; na ni kipawa kutoka kwa
Mungu. Na hivyo vitu vinaitwa vitafsiri, na hakuna mtu yeyote anayeweza kutazama
ndani yake bila kuamriwa, la sivyo ataona yale asiyostahili na aangamie. Na yeyote
anayeamrishwa kutazama ndani yake, huyo anaitwa mwonaji.
14 Na tazama, mfalme wa watu walio katika nchi ya Zarahemla ndiye yule mtu
ambaye ameamriwa kufanya vitu hivi, na aliye na kipawa hiki cha juu kutoka kwa
Mungu.
15 Na mfalme akasema kwamba mwonaji ni mkuu zaidi ya nabii.
16 Na Amoni akasema kwamba mwonaji ni mfunuzi na nabii pia; na hakuna kipawa
kingine kikuu ambacho mwanadamu anaweza kupata, ila kuwa na uwezo wa
Mungu, na hakuna yeyote anayeweza; walakini mwanadamu anaweza kupokea
uwezo mkuu kutoka kwa Mungu.
17 Lakini mwonaji anaweza kujua vitu vilivyopita, na pia vitu vitakavyokuja, na
kupitia kwao vitu vyote vitafunuliwa, kwa usahihi zaidi, vitu vya siri
vitadhihirishwa, na vitu vilivyofichwa kuletwa katika nuru, na vitu visivyojulikana
vitajulishwa na kwao, na pia vitu ambavyo havingejulikana vitajulishwa na wao.
18 Kwa hivyo Mungu ametoa njia ili mwanadamu, kwa imani, aweze kutenda
miujiza mikuu; kwa hivyo anafaidi zaidi binadamu wenzake.
19 Na sasa, wakati Amoni alipomaliza kuzungumza maneno haya mfalme alifurahia
sana, na akamshukuru Mungu, akisema: Bila shaka kuna siri kuu iliyo katika hizi
bamba, na hivi vitafsiri bila shaka vilitayarishwa kwa madhumani ya kufunua siri
zote za aina hii kwa watoto wa watu.
20 Jinsi gani kazi za Bwana zilivyo za kushangaza, na ni kwa muda gani mrefu
ambao anawasubiri watu wake; ndio, na jinsi gani watoto wa watu walivyopofuka na
hawawezi kupenyeka katika fahamu zao; kwani hawatatafuta hekima, wala hawataki
kwamba awatawale.
21 Ndio, wako kama mifugo wenye kichaa wanaomtoroka mchungaji, na
kutawanyika, na kupotea, na kuliwa na wanyama wa mwituni.

*Maandishi ya Zenivu—Historia ya watu wake, tangu waondoke nchi ya Zarahemla hadi ule wakati waliokombolewa kutoka mikononi mwa Walamani.*

# Mosia 9

1 Mimi, Zenivu, nikiwa nimefunzwa kwa lugha yote ya Wanefi, na nikiwa ninajua
nchi ya Nefi, au nchi ya kwanza ya urithi wa baba zetu, na nikiwa nimetumwa kama
mpelelezi miongoni mwa Walamani kwamba nipeleleze jeshi lao, ili jeshi letu
liwashambulie na kuwaangamiza—lakini nilipoona yale yaliyokuwa mazuri
miongoni mwao sikutaka waangamizwe.
2 Kwa hivyo, nikabishana na ndugu zangu nyikani, kwani nilitaka mtawala wetu
afanye mkataba nao; lakini yeye akiwa mwenye ukali na mtu aliyependa kumwaga

damu aliamuru kwamba niuawe; lakini niliokolewa kwa umwagaji wa damu nyingi; kwani kulikuwa na vita kati ya baba kwa baba, na kaka kwa kaka, hadi sehemu kubwa ya jeshi letu likaangamizwa huko nyikani; na tukarejea, wale kati yetu waliopona, katika nchi ya Zarahemla, kuelezea watoto wao na mabibi zao kuhusu ule mkasa.
3 Na bado, mimi nikiwa na uharara mkuu wa kurithi nchi ya baba zetu,
niliwakusanya wengi waliotaka kuenda na kuimiliki ile nchi, na tukaanza tena safari yetu ya nyikani kuelekea ile nchi; lakini tulipatwa na njaa na mateso makali; kwani hatukumkumbuka Bwana Mungu wetu.
4 Walakini, baada ya kuzunguka huko nyikani siku nyingi tulipiga hema zetu
mahali pale ndugu zetu walipouawa, ambapo palikuwa ni karibu na nchi ya babu zetu.
5 Na ikawa kwamba nilienda tena mjini na watu wangu wanne, kwa mfalme, ili
nijue hali ya yule mfalme, na ili nijue kama nitakubaliwa kuingia nchi ile pamoja na watu wangu na kuimiliki kwa amani.
6 Na nikamwendea mfalme, na akaagana na mimi kwamba niimiliki nchi ya
Lehi-Nefi, na nchi ya Shilomu.
7 Na pia akaamuru kwamba watu wake waondoke kutoka nchi ile, na mimi na
watu wangu tukaingia nchi ile ili tuimiliki.
8 Na tukaanza kujenga majengo, na kurekebisha kuta za mji, ndio, hata kuta za mji
wa Lehi-Nefi, na mji wa Shilomu.
9 Na tukaanza kulima ile ardhi, ndio, kwa kila aina ya mbegu, kwa mbegu za
mahindi, na ngano, na shayiri, na nizi, na sheumu, na mbegu za matunda ya aina zote; na tukaanza kuongezeka na kufanikiwa katika nchi ile.
10 Sasa ilikuwa ni ujanja na werevu wa mfalme Lamani, kuwatia watu wangu
utumwani, ndipo akaacha nchi ile ili tuimiliki.
11 Kwa hivyo ikawa kwamba, baada ya sisi kuishi katika nchi ile kwa kipindi cha
miaka kumi na miwili kwamba mfalme Lamani alianza kuwa na wasiwasi, kwamba watu wangu watakuwa wenye nguvu nyingi katika nchi ile, na kwamba hawangeweza kuwalemea na kuwatia utumwani.
12 Sasa walikuwa watu wavivu na wenye kuabudu sanamu; kwa hivyo walitamani
kutuweka utumwani, ili wajikinaishe na jasho la mikono yetu; ndio, ili wafanye karamu kwa mifugo ya mashamba yetu.
13 Kwa hivyo ikawa kwamba mfalme Lamani alianza kuwachochea watu wake
kwamba wabishane na watu wangu; kwa hivyo kulianza kuwa na vita na mabishano katika nchi ile.
14 Kwani, katika mwaka wa kumi na tatu wa utawala wangu katika nchi ya Nefi,
mbali kusini mwa nchi ya Shilomu, wakati watu wangu walipokuwa wanalisha na kunywesha mifugo yao, na kulima mashamba yao, kikundi kikubwa cha Walamani kiliwashukia na kuanza kuwaua, na kuchukua mifugo yao, na nafaka ya mashamba yao.
15 Ndio, na ikawa kwamba wale wote ambao hawakupatwa, walitoroka, hadi mji wa
Nefi, na wakaniomba ulinzi.
16 Na ikawa kwamba niliwapa silaha kama vile pinde, mishale, panga, na visu, na
rungu, na kombeo, na kila aina ya silaha ambayo tungevumbua, na mimi na watu wangu tukaenda kupigana na Walamani.
17 Ndio, kwa nguvu za Bwana tulienda kupigana na Walamani; kwani mimi na
watu wangu tulimlilia Bwana kwa nguvu ili atukomboe kutoka mikononi mwa

maadui zetu, kwani tulikumbushwa kuhusu ukombozi wa babu zetu.
18 Na Mungu alisikia vilio vyetu na akajibu sala zetu; na tukaendelea kwa nguvu
zake; ndio, tuliwashambulia Walamani, na kwa mchana mmoja na usiku tuliwaua
elfu tatu, arubaini na tatu; tuliwaua hadi tukawafukuza kutoka nchi yetu.
19 Na mimi, mwenyewe, kwa mikono yangu, nilisaidia kuzika wafu wao. Na tazama,
kwa hoi yetu kuu na maombolezo, ndugu zetu mia mbili sabini na tisa waliuawa.

## Mosia 10

1 Na ikawa kwamba tulianza tena kuimarisha ufalme na kumiliki nchi ile kwa amani.
Na nilisababisha kwamba silaha za kila aina zitengenezwe, ili niwe na silaha kwa
watu wangu wakati Walamani wangetushambulia.
2 Na nikaweka walinzi waizingire ile nchi, ili Walamani wasituvamie tena kwa
ghafla na kutuangamiza; na hivyo ndivyo nilivyowalinda watu wangu na mifugo
yangu, na kuwachunga wasianguke mikononi mwa maadui wetu.
3 Na ikawa kwamba tulirithi nchi ya baba zetu kwa miaka mingi, ndio, kwa kipindi
cha miaka ishirini na miwili.
4 Na nikasababisha kwamba wanaume walime ardhi, na kupanda kila aina ya
nafaka na matunda ya kila aina.
5 Na nikasababisha kwamba wanawake wasokote, na kujitahidi, na kufanya kazi,
na kushona kila aina ya kitani bora, ndio, na nguo za kila aina, ili tuvishe uchi wetu;
na hivyo tulifanikiwa nchini — na hivyo tukaendelea kupata amani nchini kwa
kipindi cha miaka ishirini na miwili.
6 Na ikawa kwamba mfalme Lamani alifariki, na mwana wake akaanza kutawala
badala yake. Na akaanza kuwachochea watu wake ili wazushe uasi dhidi ya watu
wangu; kwa hivyo wakaanza kujitayarisha kwa vita, na kuja kuwashambulia watu
wangu.
7 Lakini niliwatuma wapelelezi wangu karibu na nchi ya Shemloni, ili nigundue
mipango yao, na kwamba nijikinge na wao, ili wasiwashambulie watu wangu, na
kuwaangamiza.
8 Na ikawa kwamba walikuja na kufika kaskazini mwa nchi ya Shilomu, na umati
wao mkubwa, wanaume wakiwa wamebeba pinde, na mishale, na panga, na sime, na
mawe, na kombeo; na vichwa vyao vilikuwa vimenyolewa kwamba walikuwa uchi;
na walikuwa wamejifunga mishipi ya ngozi viunoni mwao.
9 Na ikawa kwamba nilisababisha kwamba wake na watoto wa watu wangu
wafichwe nyikani; na pia nikasababisha kwamba wanaume wangu wote wazee
ambao wangeweza kubeba silaha, na pia vijana wangu wote ambao wangeweza
kubeba silaha, wakusanyike pamoja ili wapigane na Walamani; na nikawapanga kwa
mistari, kila mtu kulingana na umri wake.
10 Na ikawa kwamba tulienda kupigana dhidi ya Walamani; na mimi, hata mimi,
katika uzee wangu, nilienda kupigana dhidi ya Walamani. Na ikawa kwamba
tulienda kwa nguvu za Bwana kupigana.
11 Sasa, Walamani hawakujua lolote kuhusu Bwana, wala nguvu za Bwana, kwa
hivyo walitegemea nguvu zao wenyewe. Lakini walikuwa watu wenye nguvu,
kulingana na nguvu za wanadamu.
12 Walikuwa wakaidi, na wakorofi, na watu wapendao kumwaga damu, wakiamini
mila ya baba zao, ambayo ndiyo hii — Kuamini kwamba walifukuzwa kutoka nchi

ya Yerusalemu kwa sababu ya maovu ya baba zao, na kwamba walikosewa huko
nyikani na ndugu zao, na kwamba pia walikosewa walipokuwa wakivuka bahari;
13 Na tena, kwamba walikosewa walipokuwa katika nchi ya urithi wao wa kwanza,
baada ya kuvuka bahari, na haya yote ni kwa sababu Nefi alikuwa mwaminifu katika
kutii amri za Bwana — kwa hivyo, alipendelewa na Bwana, kwani Bwana alisikia sale
zake na kuzijibu, na aliwaongoza kwenye safari yao huko nyikani.
14 Na kaka zake walimkasirikia kwa sababu hawakufahamu njia za Bwana; na pia
walimkasirikia huko majini kwa sababu walishupaza mioyo yao dhidi ya Bwana.
15 Na tena, walimkasirikia walipowasili katika nchi ya ahadi, kwa sababu walisema
kwamba aliondoa utawala wa watu mikononi mwao; na wakajaribu kumuua.
16 Na tena, walimkasirikia kwa sababu alikimbilia nyikani kama vile Bwana
alivyokuwa amemwamuru, na akachukua maandishi yale yaliyokuwa yamechorwa
kwenye bamba za shaba, kwani walisema kwamba aliwaibia.
17 Kwa hivyo wamewafunza wana wao kwamba wawachukie, na kwamba wawaue,
na kwamba wawaibie na kuwapora, na kutenda yale yote waliyoweza ili
wawaangamize; kwa hivyo wana chuki ya milele kwa wana wa Nefi.
18 Ni kwa sababu hii mfalme Lamani, kwa ujanja wake, na werevu wake, na ahadi
zake nzuri, alinidanganya, hata kwamba nikawaleta watu hawa wangu katika nchi
hii, ili wawaangamize; ndio, na tumepata mateso miaka nyingi katika nchi hii.
19 Na sasa mimi, Zenivu, baada ya kuvisema vitu hivi vyote kwa watu wangu
kuhusu Walamani, niliwachechemua waende vitani kwa nguvu zao, wakimwamini
Bwana; kwa hivyo, tulipigana nao, ana kwa ana.
20 Na ikawa kwamba tuliwafukuza tena kutoka nchi yetu; na tuliwauwa wengi, hata
kwamba hatukuweza kuwahesabu.
21 Na ikawa kwamba tulirejea tena kwenye nchi yetu, na watu wangu wakaanza tena
kufuga mifugo yao, na kulima mashamba yao.
22 Na sasa mimi, nikiwa mzee, niliutawaza ufalme wangu juu ya mwana wangu
mmoja; kwa hivyo, sisemi mengine. Na Bwana awabariki watu wangu. Amina.

# Mosia 11

1 Na sasa ikawa kwamba Zenivu aliutawaza ufalme juu ya Nuhu, mmoja wa wana
wake; kwa hivyo Nuhu akaanza kutawala badala yake; na hakutembea katika njia za
baba yake.
2 Kwani tazama, hakutii amri za Mungu, walakini alifuata tamaa za moyo wake.
Na alikuwa na wake wengi na makahaba. Na alisababisha watu wake kutenda
dhambi, na kutenda yale ambayo yalikuwa yanamchukiza Bwana. Ndio, na
walifanya ukahaba na kila aina ya uovu.
3 Na aliwatoza kodi fungu la tano kwa chochote walichokuwa nacho, fungu la
tano kwa dhahabu yao na kwa fedha yao, na fungu la tano la zifu yao, na shaba
nyekundu yao, na shaba nyeupe yao, na chuma yao; na fungu la tano la mifugo yao;
na pia fungu la tano la nafaka yao yote.
4 Na alitenda haya yote ili ajisaidie mwenyewe, na wake zake na makahaba wake;
na makuhani wake, na wake zao na masuria wao; na hivyo alibadilisha mipango ya
ule ufalme.
5 Kwani aliwateremsha makuhani wote ambao walikuwa wameteuliwa na baba
yake, na kuteua wengine wapya mahali pao, na wao walikuwa wamejiinua kwa kiburi

cha mioyo yao.
6 Ndio, na hivi ndivyo walisaidiwa katika uvivu wao, na ukafiri wao, na ukahaba
wao, kwa zile kodi ambazo mfalme Nuhu aliwatoza watu wake; kwa hivyo watu
walijichosha zaidi kusaidia uovu.
7 Ndio, na pia wakawa wanaabudu masanamu, kwa sababu walidanganywa na
maneno ya bure na ya ubembelezaji ya mfalme na makuhani; kwani
waliwazungumzia vitu vya ubembelezaji.
8 Na ikawa kwamba mfalme Nuhu alijenga mijengo mingi mizuri na mikubwa; na
akairembesha kwa vitu vizuri vya mbao, na kila aina ya vitu vyenye thamani, vya
dhahabu, na vya fedha, na vya chuma, na vya shaba, na vya zifu, na vya shaba
nyekundu;
9 Na pia alijijengea ikulu kubwa, na hapo katikati kiti cha enzi, ambayo yote
yalikuwa ya mbao bora na kurembeshwa kwa dhahabu na fedha na vitu vyenye
thamani.
10 Na pia akawaamuru mafundi wake warembeshe kuta za hekalu, kwa mbao nzuri,
shaba nyekundu, na shaba.
11 Na viti ambavyo vilikuwa vimewekewa wale makuhani wakuu, ambavyo vilikuwa
juu ya viti vingine vyote, alivirembesha kwa dhahabu kamili; na akasababisha
vijengewe ua mbele yao, ili wapumzishe miili yao na mikono yao
wanapowazungumzia watu wake maneno ya uwongo na yasiyo na busara.
12 Na ikawa kwamba alijenga mnara karibu na hekalu; ndio, mnara mrefu sana, hata
mrefu sana kwamba angesimama juu yake na kuona nchi ya Shilomu, na pia nchi ya
Shemloni, ambayo ilikuwa imemilikiwa na Walamani; na hata angeona nchi yote
ambayo ilikuwa imewazingira.
13 Na ikawa kwamba alisababisha mijengo mingi ijengwe katika nchi ya Shilomu;
na akasababisha mnara mkubwa ujengwe katika kilima kilichokuwa kaskazini mwa
nchi ya Shilomu, ambayo ilikuwa ni kimbilio kwa watoto wa Nefi walipotoroka
kutoka nchi ile; na haya alitenda kwa utajiri alioupata kwa kuwatoza watu wake
kodi.
14 Na ikawa kwamba aliutia moyo wake katika utajiri wake, na aliutumia wakati
wake katika maisha ya anasa na wake zake na masuria wake; na pia makuhani wake
waliutumia wakati wao kwa makahaba.
15 Na ikawa kwamba alipanda mizabibu kote nchini mle; na akajenga vishinikizo,
na kutegeneza divai kwa wingi; na kwa hivyo akawa mlevi, na pia watu wake.
16 Na ikawa kwamba Walamani walianza kuwashambulia watu wake, kwa vikundi
vidogo, na kuwaua mashambani mwao, na walipokuwa wakilisha mifugo yao.
17 Na mfalme Nuhu akatuma walinzi wake nchini kuwafukuza; lakini hakutuma
hesabu ya kutosha, na Walamani waliwashambulia na kuwaua, na kuwanyang'anya
mifugo yao kutoka nchini; na hivyo Walamani walianza kuwaangamiza, na
kuwafanyia chuki.
18 Na ikawa kwamba mfalme Nuhu aliwatumia jeshi lake; na walisukumwa nyuma,
au waliwasukuma nyuma kwa muda; kwa hivyo, walirejea wakifurahia mateka wao.
19 Na sasa, kwa sababu ya ushindi huu mkuu walijiinua sana kwa kiburi cha mioyo
yao; walijivunia nguvu zao, wakisema kwamba kikosi chao cha wanajeshi hamsini
kiliweza kupigana na wanajeshi maelfu ya Walamani; na hivyo ndivyo walijivuna, na
kufurahia damu, na umwagaji wa damu ya ndugu zao, na hii kwa sababu ya uovu wa
mfalme wao na makuhani wao.

20 Na ikawa kwamba kulikuwa na mtu miongoni mwao aliyeitwa Abinadi; na alienda miongoni mwao, na akaanza kutoa unabii, akisema: Tazama, asema Bwana hivi, na ameniamuru hivi, akisema, Nenda, na uwaambie watu hawa, hivi asema Bwana — Ole kwa watu hawa, kwani nimeona machukizo yao, na maovu yao, na ukahaba wao; na wasipotubu nitawatembelea kwa ghadhabu yangu.

21 Na wasipotubu na kumrejea Bwana Mungu wao, tazama, nitawakabidhi mikononi mwa maadui wao; ndio, na watawekwa utumwani; na watanyanyaswa kwa mkono wa maadui wao.

22 Na itakuwa kwamba watajua kuwa mimi ni Bwana Mungu wao, na mimi ni Mungu mwenye hamasa, na huadhibu maovu ya watu wangu.

23 Na itakuwa kwamba hawa watu wasipotubu na kumrejea Bwana Mungu wao, watawekwa utumwani; na hakuna yeyote atakayewakomboa, ila tu Bwana Mwenyezi Mungu.

24 Ndio, na itakuwa kwamba watakaponililia, nitakawia kusikia vilio vyao; ndio, na nitaruhusu maadui wao wawapige.

25 Na wasipotubu kwa gunia na majivu, na wamlilie kwa nguvu Bwana Mungu wao, sitasikia sala zao, wala sitawakomboa kutoka kwa masumbuko yao; na hivi ndivyo asema Bwana, na ameniamuru hivyo.

26 Na ikawa kwamba wakati Abinadi alipowazungumzia maneno haya walimkasirikia, na walitaka kumtoa uhai wake; lakini Bwana alimkomboa kutoka mikono yao.

27 Sasa wakati mfalme Nuhu aliposikia maneno ambayo Abinadi aliwazungumzia watu wale, na yeye pia alikasirika; na akauliza: Je, Abinadi ni nani, kwamba ahukumu watu wangu na mimi, au Bwana ni nani, hata kwamba ateremshie watu wangu mateso makuu hivi?

28 Nawaamuru kwamba mmlete Abinadi hapa, ili nimuue, kwani amesema vitu hivi ili awachochee watu wangu wakasirikiane mmoja kwa mwingine, na kuzusha mabishano miongoni mwa watu wangu; kwa hivyo nitamuua.

29 Sasa macho ya watu yalikuwa yamepofuka; kwa hivyo walishupaza mioyo yao dhidi ya maneno ya Abinadi, na tangu wakati huo walijaribu kumkamata. Na mfalme Nuhu alishupaza moyo wake dhidi ya neno la Bwana, na hakutubu matendo yake maovu.

## Mosia 12

1 Na ikawa kwamba baada ya kipindi cha miaka miwili kwamba Abinadi alikuja miongoni mwao kwa mwigo, na hawakumjua, na akaanza kutoa unabii miongoni mwao, akisema: Bwana ameniamuru hivi, akisema — Abinadi, enda ukawatolee watu hawa wangu unabii, kwani wameshupaza mioyo yao dhidi ya maneno yangu; hawajatubu matendo yao maovu; kwa hivyo, nitawatembelea kwa ghadhabu yangu, ndio, katika ghadhabu yangu kali nitawaadhibu kwa sababu ya uovu na machukizo yao.

2 Ndio, ole kwa uzao huu! Na Bwana akaniambia: Nyosha mkono wako na utoe unabii, ukisema: Bwana asema hivi, itakuwa kwamba uzao huu, kwa sababu ya uovu wao, watatiwa utumwani, na watapigwa shavuni; ndio, na watafukuzwa na watu, na kuuawa; na koho wa angani, na mbwa, ndio, na wanyama wa mwituni, watakula miili yao.

3 Na itakuwa kwamba maisha ya mfalme Nuhu yatakuwa na thamani kama nguo
iliyo katika tanuu, kwani atajua kwamba Mimi ni Bwana.
4 Na itakuwa kwamba nitawapiga watu wangu hawa kwa mapigo makali, ndio,
kwa njaa na tauni; na nitawasababisha walie siku yote.
5 Ndio, na nitafanya wabebe mizigo migongoni mwao; na wataendeshwa kama
punda bubu.
6 Na itakuwa kwamba nitateremsha mvua ya mawe miongoni mwao, na itawapiga;
na pia watapigwa na upepo wa mashariki; na wadudu watasumbua nchi yao pia, na
kuharibu nafaka yao.
7 Na watapigwa kwa maradhi makuu — na nitatenda haya yote kwa sababu ya
maovu yao na machukizo yao.
8 Na itakuwa kwamba wasipotubu nitawaangamiza kutoka uso wa dunia; walakini
wataacha maandishi yao nyuma, na nitayahifadhi kwa mataifa mengine ambayo
yataimiliki nchi; ndio, nitafanya haya ili niyadhihirishie mataifa mengine
machukizo ya watu hawa. Na Abinadi alitoa unabii wa vitu vingi dhidi ya watu
hawa.
9 Na ikawa kwamba walimkasirikia; na wakamchukua na kumpeleka mbele ya
mfalme akiwa amefungwa, na wakamwambia mfalme: Tazama, tumemleta mtu
mbele yako ambaye ametoa unabii mwovu kuhusu watu wako, na kusema kwamba
Mungu atawaangamiza.
10 Na pia anatoa unabii mwovu kuhusu maisha yako, na kusema kwamba maisha
yako yatakuwa kama nguo iliyo katika tanuu ya moto.
11 Na tena, anasema utakuwa kama ubua, hata kama ubua wa shambani uliokauka,
ambao unakimbiwa na wanyama na kukanyagwa kwa miguu.
12 Na tena, anasema wewe utakuwa kama maua ya mwiba, ambalo, kama limeiva, na
kama upepo ukivuma, linapeperushwa kokote usoni mwa nchi. Na anadai kwamba
Bwana ameyasema. Na anasema kwamba haya yote yatakupata usipotubu, na haya
ni kwa sababu ya maovu yako.
13 Na sasa, Ee mfalme, ni uovu gani mkuu uliotenda, au ni dhambi gani kuu
ambazo watu wako wametenda, hata kwamba tuhukumiwe na Mungu au
tuhukumiwe na mtu huyu?
14 Na sasa, Ee mfalme, tazama, hatuna hatia, na wewe, Ee mfalme, hujatenda
dhambi; kwa hivyo, mtu huyu amesema uwongo kukuhusu, na ametoa unabii wa
bure.
15 Na tazama, tuna nguvu, hatutatiwa utumwani, au kutekwa nyara na maadui
wetu; ndio, na wewe umefanikiwa nchini, na wewe pia utafanikiwa.
16 Tazama, mtu huyo ndiye huyu hapa, tunamkabidhisha mikononi mwako;
unaweza kufanya utakavyo naye.
17 Na ikawa kwamba mfalme Nuhu aliamuru kwamba Abinadi atiwe gerezani; na
akaamuru kwamba makuhani wakusanyike pamoja ili wafanye baraza na yeye
kuhusu kile atakachomtendea.
18 Na ikawa kwamba walimwambia mfalme: Mlete hapa ili tumwulize maswali; na
mfalme akaamuru kwamba aletwe mbele yao.
19 Na wakaanza kumwuliza maswali, ili wamfanye ajikanushe, ili wapate sababu ya
kumlaumu; lakini akawajibu kwa ujasiri, na kujibu maswali yao yote, ndio, kwa
mshangao wao; kwani alivumilia maswali yao yote, na kuwatunduwaza katika
maneno yao yote.

20 Na ikawa kwamba mmoja wao alimuuliza: Je, nini maana ya maneno ambayo yameandikwa, na ambayo yamefunzwa na baba zetu, yakisema:

21 Jinsi gani ilivyo vizuri juu ya milima miguu yake aletaye habari njema; anayeleta amani; anayeleta habari njema ya mambo mema; aletaye wokovu; anayeiambia Sayuni, Mungu wako anatawala;

22 Walinzi wako watapaza sauti; kwa sauti moja wote wataimba; kwani wataona jicho kwa jicho Bwana atakapoleta tena Sayuni;

23 Shangilieni kwa shangwe; imbeni pamoja enyi mahali pa ukiwa pa Yerusalemu; kwani Bwana amefariji watu wake, amekomboa Yerusalemu;

24 Bwana ameuweka mkono wake mtakatifu wazi mbele ya macho ya mataifa yote, na nchi zote za ulimwengu zitauona wokovu wa Mungu?

25 Na sasa Abinadi akawaambia: Je, nyinyi ni makuhani, na mnadai kwamba mnafundisha watu hawa, na kwamba mnafahamu roho ya kutoa unabii, na bado mnataka kujua kutoka kwangu maana ya vitu hivi?

26 Nawaambia, ole kwenu kwa sababu ya kuchafua njia za Bwana! Kwani kama mmefahamu vitu hivi hamjavifunza; kwa hivyo, mmechafua njia za Bwana.

27 Hamjajitolea mioyo yenu kwa ufahamu; kwa hivyo, hamjakuwa wenye hekima. Kwa hivyo, ni kitu gani ambacho mnafunza watu hawa?

28 Na wakasema: Tunafunza sheria ya Musa.

29 Na tena akawaambia: Ikiwa mnafunza sheria ya Musa kwa nini hamuitii? Kwa nini mnaweka mioyo yenu kwa utajiri? Kwa nini mnatenda ukahaba na kupoteza nguvu zenu na makahaba, ndio, na kufanya watu hawa watende dhambi, kwamba Bwana ana sababu ya kunituma nitoe unabii kinyume cha watu hawa, ndio, hata uovu mkuu dhidi ya watu hawa?

30 Je, hamjui kwamba nazungumza ukweli? Ndio, mnajua kwamba nazungumza ukweli; na inawapasa kutetemeka mbele ya Mungu.

31 Na itakuwa kwamba mtapigwa kwa sababu ya maovu yenu, kwani mmesema kwamba mnafunza sheria ya Musa. Na nini mnachoelewa kuhusu sheria ya Musa? Je, wokovu unakuja kwa sheria ya Musa? Mnasema nini?

32 Na wakamjibu kwamba wokovu unakuja kwa sheria ya Musa.

33 Lakini sasa Abinadi akawaambia: Najua kwamba mkitii amri za Mungu mtaokolewa; ndio, kama mtatii amri ambazo Bwana alimpatia Musa katika mlima wa Sinai, akisema:

34 Mimi ndimi Bwana Mungu wako, aliyekutoa kutoka nchi ya Misri, kutoka nyumba ya utumwa.

35 Usiwe na Mungu mwingine mbele yangu.

36 Usijifanyie sanamu ya kuchonga, au mfano wa chochote kilicho juu mbinguni, au vitu vilivyo chini ulimwenguni.

37 Sasa Abinadi akawauliza, Je, mmefanya haya yote? Nawaambia nyinyi, La, hamjafanya. Na mmewafunza hawa watu watende vitu hivi vyote? Nawaambia, La, hamjafanya hivyo.

## Mosia 13

1 Na sasa mfalme alipoisikia maneno haya, aliwaambia makuhani wake: Mwondolee huyu mtu mbali, na mmuue; kwani tutafanya nini na yeye, kwani ana kichaa.

2 Na wakasimama na kumsogelea na kujaribu kumkamata; lakini aliwazuia, na

akawaambia:
3 Msiniguse, kwani Mungu atawapiga mkinishika, kwani sijatoa ujumbe ambao
Bwana alinituma kuutoa; wala sijawaambia yale ambayo mliniuliza niwaambie; kwa
hivyo, Mungu hatakubali kwamba niangamizwe sasa.
4 Lakini lazima nitimize amri ambazo Mungu ameniamuru; na kwa sababu
nimewaambia ukweli mnanikasirikia. Na tena, kwa sababu nimezungumza neno la
Mungu mmenihukumu kuwa mimi nina kichaa.
5 Na sasa ikawa kwamba baada ya Abinadi kuzungumza maneno haya watu wa
mfalme Nuhu hawakumkamata tena, kwani Roho wa Bwana alikuwa na yeye; na
uso wake ulimetameta kwa mng'aro mkuu, hata vile uso wa Musa ulivyong'ara
katika mlima wa Sinai, alipokuwa akizungumza na Bwana.
6 Na alizungumza kwa uwezo na mamlaka kutoka kwa Mungu; na akaendelea na
maneno yake, akisema:
7 Mnaona kwamba hamna uwezo wa kuniua, kwa hivyo namaliza ujumbe wangu.
Ndio, na ninaona kwamba inawakera mioyoni yenu kwa sababu nimewaambia
ukweli kuhusu maovu yenu.
8 Ndio, na maneno yangu inawajaza na mshangao na bumbuazi, na hasira.
9 Lakini namaliza ujumbe wangu; na kisha haijalishi ni wapi nitakapoenda, ikiwa
kama nitaokolewa.
10 Lakini nawaambia haya, yale mtakayonifanyia, baada ya haya, yatakuwa ni kama
mfano au kivuli cha vitu vitakavyokuja.
11 Na sasa nitawasomea amri za Mungu zilizosalia, kwani nahisi kwamba
hazijaandikwa mioyoni yenu; nahisi kwamba mmesoma na kufunza uovu kwa muda
mrefu maishani mwenu.
12 Na sasa, mnakumbuka kwamba niliwaambia: Hamtajitengenezea sanamu ya
kuchonga, au mfano wa vitu vyovyote vilivyo juu mbinguni, au vilivyo chini
ardhini, au vilivyo majini chini ya ardhi.
13 Na tena: Hamtaviinamia, wala kuvitumikia; kwani mimi Bwana Mungu wako ni
Mungu wa hamasa, niteremshiaye watoto maovu ya babu zao, kwa kizazi cha tatu na
cha nne kwa wale wanaonichukia;
14 Na kuonyesha rehema kwa maelfu ya wale wanaonipenda na kutii amri zangu.
15 Usichukue jina la Bwana Mungu wako bure; kwani yule anayeapa bure kwa jina
la Bwana bure atakuwa na hatia.
16 Kumbuka siku ya sabato, kuiweka takatifu.
17 Utafanya kazi kwa siku sita, na kufanya kazi yako yote.
18 Lakini siku ya saba, sabato ya Bwana Mungu wako, usifanye kazi yoyote, wewe,
wala mwana wako, wala binti wako, wala mtumishi wako wa kiume, wala mjakazi
wako, wala mifugo yako, wala mgeni wako anayeishi nawe;
19 Kwani kwa siku sita Bwana aliumba mbingu na dunia, na bahari, na vyote vilivyo
ndani yake; kwa hivyo Bwana aliibariki siku ya sabato, na kuitakasa.
20 Heshimu baba yako na mama yako, ili maisha yako yawe marefu katika ya nchi
ambayo Bwana Mungu wako amekupatia.
21 Usiue.
22 Usizini. Usiibe.
23 Usitoe ushahidi wa uwongo dhidi ya jirani yako.
24 Usitamani nyumba ya jirani yako, usitamani mke wa jirani yako, wala mfanyi kazi
wake, wala mjakazi wake, wala dume wake, wala punda wake, wala chochote cha

jirani yako.
25 Na ikawa kwamba baada ya Abinadi kumaliza kusema haya maneno kwamba
akawaambia: Mmewafunza watu hawa kutii vitu hivi vyote ili watii hizi amri?
26 Nawaambia, La; kwani kama mngekuwa mmefanya hivyo, Bwana
hangenisababisha nije na nitoe unabii wa uovu kuhusu watu hawa.
27 Na sasa mmesema kwamba wokovu huja kwa sheria ya Musa. Nawaambia
kwamba ni muhimu mtii sheria ya Musa sasa; lakini nawaambia, kwamba wakati
utafika ambapo haitakuwa muhimu kutii sheria ya Musa.
28 Na juu ya hayo, nawaambia, kwamba wokovu hauji kwa sheria pekee; na kama sio
kwa sababu ya upatanisho, ambao Mungu atautoa kwa sababu ya dhambi na uovu
wa watu wake, kwamba lazima waangamie, ingawa sheria ya Musa ipo.
29 Na sasa nawaambia kwamba ilikuwa lazima kwamba wana wa Israeli wapewe
sheria, ndio, sheria iliyo ngumu, kwani walikuwa watu wenye shingo ngumu, walio
na haraka ya kutenda maovu, na wavivu kwa kumkumbuka Bwana Mungu wao;
30 Kwa hivyo kulikuwa na sheria ambayo walipewa, ndio, sheria ya sherehe na
masharti, sheria ambayo walitakiwa kuitii siku kwa siku, ili kuwakumbusha Mungu
na jukumu lao kwake.
31 Lakini tazama, nawaambia, kwamba vitu hivi vyote vilikuwa ni mfano wa vile
vitakavyokuja.
32 Na sasa, je, walifahamu sheria? Nawaambia, La, wote hawakufahamu ile sheria;
na hii ni kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao; kwani hawakufahamu kwamba
hakuna yeyote angeokolewa ila tu kwa ukombozi wa Mungu.
33 Kwani tazama, si Musa aliwatolea unabii kuhusu kuja kwa Masiya, na kwamba
Mungu atawakomboa watu wake? Ndio, na hata manabii wote ambao wametoa
unabii tangu mwanzo wa ulimwengu—Je, hawajanena mengi au machache kuhusu
vitu hivi?
34 Je, hawajasema kwamba Mungu mwenyewe atashuka chini miongoni mwa
watoto wa watu, na ajivike hali ya mwanadamu, na atembee usoni mwa dunia kwa
uwezo mkuu?
35 Ndio, na je, hawakusema pia kwamba atawezesha ufufuo wa wafu, na kwamba
yeye, mwenyewe, atanyanyaswa na kusumbuliwa?

## Mosia 14

1 Ndio, si hata Isaya anasema: Ni nani ambaye ameamini ujumbe wetu, na ni kwa
nani mkono wa Bwana umefunuliwa?
2 Kwani atakua mbele yake kama mmea mwororo, na kama mzizi kutoka nchi
kavu; hana umbo nzuri wala urembo; na tutakapomuona hana urembo wa
kutuvutia.
3 Amechukiwa na kukataliwa na watu; mtu wa huzuni, na aliyezoea huzuni; na
tukaficha nyuso zetu kutoka kwake; alichukiwa, na hatukumheshimu.
4 Kwa hakika amechukua ghamu zetu, na kubeba huzuni zetu; na tulimdhania
kuwa amepigwa, na Mungu, na kuteswa.
5 Lakini alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya
amani yetu ilikuwa juu yake; na kwa mapigo yake tunaponywa.
6 Sisi sote, kama kondoo, tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake; na
Bwana amemwekea maovu yetu sisi sote.

7 Alidhulumiwa, na aliteswa, lakini hakufungua kinywa chake; yeye analetwa
kama mwanakondoo machinjoni, na kama vile kondoo ni bubu mbele ya wanaokata
manyoya yake hakufungua kinywa chake.
8 Alichukuliwa kutoka gerezani na kutoka kwenye hukumu; na ni nani atatangaza
uzazi wake? Kwani aliondolewa kutoka nchi ya wanaoishi; kwa makosa ya watu
wangu alipigwa.
9 Na kaburi lake lilikuwa pamoja na waovu, na matajiri kifoni mwake; kwa sababu
hakuwa ametenda uovu wowote, wala hapakuwa na uwongo wowote kinywani
mwake.
10 Lakini Bwana alipendezwa kumchubua; amemhuzunisha; utakapotoa nafsi yake
kuwa dhabihu ya dhambi ataona uzao wake, ataongeza siku zake, na mapenzi ya
Bwana yatafanikiwa mkononi mwake.
11 Ataona taabu ya nafsi yake, na kuridhika; kwa maarifa yake mtumishi wangu
mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki; kwani atayachukua maovu yao.
12 Kwa hivyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu, na atagawanya nyara pamoja
na mashujaa; kwa sababu ametoa roho yake hata kufa; na akahesabiwa na wenye
dhambi; na alibeba dhambi za wengi, na kuwatetea wenye dhambi.

## Mosia 15

1 Na sasa Abinadi akawaambia: Nataka mfahamu kwamba Mungu mwenyewe
atashuka miongoni mwa watoto wa watu, na atawakomboa watu wake.
2 Na kwa sababu anaishi katika mwili ataitwa Mwana wa Mungu, na akiwa
ameweka mwili kuwa chini ya mapenzi ya Baba, akiwa Baba na Mwana—
3 Baba, kwa sababu alizaliwa kwa nguvu za Mungu; na Mwana, kwa sababu ya
mwili; kwa hivyo akawa Baba na Mwana—
4 Na wao ni Mungu mmoja, ndio, yule yule Baba wa Milele wa mbingu na wa
dunia.
5 Na hivyo mwili ukiwa chini ya Roho, au Mwana kwa Baba, wakiwa Mungu
mmoja, anateswa kwa majaribio, na hakubali majaribio, lakini anakubali afanyiwe
mzaha, na kupigwa, na kutupwa nje, na kukataliwa na watu wake.
6 Na baada ya haya yote, baada ya kutenda miujiza mingi mikuu miongoni mwa
watoto wa watu, ataongozwa, ndio, hata kama vile Isaya aliposema, kama vile
kondoo huwa bubu mbele ya yule anayemnyoa, kwa hivyo hakufungua kinywa
chake.
7 Ndio, hata hivyo ataongozwa, asulubiwe, na kuuawa, mwili ule ukinyenyekea
hata hadi mauti, nia ya Mwana ikimezwa na nia ya Baba.
8 Na hivyo ndivyo Mungu anavyokata kamba za kifo, baada ya kushinda mauti;
akimpa Mwana uwezo wa kutetea watoto wa watu—
9 Baada ya kupaa mbinguni, na kuwa na moyo wa rehema; akiwa amejawa na
upendo kwa watoto wa watu; na kusimama kati yao na haki; baada ya kukata kamba
za kifo, na kujitwika mwenyewe maovu yao na makosa yao, baada ya kuwakomboa,
na kutosheleza madai ya haki.
10 Na sasa nawaambia, ni nani atakayetangaza kizazi chake? Tazama, nawaambia,
kwamba baada ya nafsi yake kutolewa kama dhabihu ya dhambi ataona uzao wake.
Na sasa mnasema nini? Na ni nani atakuwa uzao wake?
11 Tazama nawaambia, kwamba yeyote ambaye amesikia maneno ya manabii, ndio,

manabii wote watakatifu ambao wametoa unabii kuhusu kuja kwa Bwana — Nawaambia, kwamba wale wote ambao wamesikia maneno yao, na kuamini kwamba Bwana atawakomboa watu wake, na kuitazamia siku ile kwa msamaha wa dhambi zao, nawaambia, kwamba hawa ni uzao wake, au ndiyo warithi wa ufalme wa Mungu.

12 Kwani hawa ndiyo wale dhambi zao amebeba; hawa ndiyo aliwafia, kuwakomboa kutoka kwa makosa yao. Na sasa, je, wao sio uzao wake?

13 Ndio, je, na sio manabii, kila mmoja aliyefungua kinywa chake kutoa unabii, na hajaanguka kwenye makosa, namaanisha manabii wote watakatifu tangu mwanzo wa ulimwengu? Nawaambia kwamba wao ni uzao wake?

14 Na hawa ndiyo wameitangaza amani, walioleta habari njema ya mambo mazuri, ambao wametangaza wokovu; na kuiambia Sayuni: Mungu wako anatawala!

15 Na Ee jinsi gani miguu yao ilivyo mizuri juu ya milima!

16 Na tena, jinsi gani ilivyo mizuri juu ya milima miguu ya wale ambao bado wanatangaza amani!

17 Na tena, jinsi gani ilivyo mizuri juu ya milima miguu ya wale watakaoitangaza amani baadaye, ndio, kutoka wakati huu hadi milele!

18 Na tazama, nawaambia, hii sio yote. Kwani Ee jinsi gani ilivyo rembo juu ya milima miguu ya yule anayeleta habari njema, ambaye ni mwanzilishi wa amani, ndio, hata Bwana, ambaye amewakomboa watu wake; ndio, yule ambaye amewapatia watu wake wokovu;

19 Kwani kama sio kwa sababu ya ukombozi aliowatolea watu wake, ambao ulitayarishwa tangu msingi wa ulimwengu, nawaambia, kama sio kwa sababu hii, wanadamu wote lazima wangeangamia.

20 Lakini tazama, kamba za kifo zitakatwa, na Mwana anatawala, na ana nguvu juu ya wafu; kwa hivyo, anawezesha ufufuo wa wafu.

21 Na kutakuja ufufuo, hata ufufuo wa kwanza; ndio, hata ufufuo wa wale ambao walikuwa, na ambao wapo, na wale watakaokuwa, hadi hata ufufuo wa Kristo — kwani ataitwa hivyo.

22 Na sasa, ufufuo wa manabii wote, na wale wote ambao wameamini maneno yao, au wale wote ambao wametii amri za Mungu, watakuja mbele wakati wa ufufuo wa kwanza; kwa hivyo, wao ndiyo ufufuo wa kwanza.

23 Wanainuliwa ili waishi na Mungu ambaye amewakomboa; kwa hivyo wanao uzima wa milele kupitia Kristo, ambaye amekata kamba za kifo.

24 Na hawa ndiyo wale ambao wana nafasi katika ufufuo wa kwanza; na hawa ndiyo wale waliokufa mbele ya kuja kwa Kristo, walipokuwa hawajui, na hawakuwa wamehubiriwa wokovu. Na hivi ndivyo Bwana huleta uamsho wa hawa; na wanayo nafasi katika ufufuo wa kwanza, au wanao uzima wa milele, baada ya kukombolewa na Bwana.

25 Na watoto wachanga nao pia wana uzima wa milele.

26 Lakini tazama, na uogope, na utetemeke mbele ya Mungu, kwani inakubidi kutetemeka; kwani Bwana hawakomboi wale wanaomuasi na kufa katika dhambi zao; ndio, hata wale wote ambao wameangamia katika dhambi zao tangu mwanzo wa ulimwengu, wale ambao kwa hiari yao wamemuasi Mungu, wale ambao wamezijua amri za Mungu, na hawazitii; hawa ndiyo wale ambao hawana nafasi katika ufufuo wa kwanza.

27 Kwa hivyo haiwapasi kutetemeka? Kwani wokovu hauji kwa kama hawa; kwani

Bwana hajakomboa kama hawa; ndio, wala Bwana hawezi kukomboa kama hawa; kwani hawezi kujikanusha; kwani hawezi kuzuia haki inapohitajika.
28 Na sasa nawaambia kwamba wakati unafika ambapo wokovu wa Bwana utatangazwa katika kila taifa, kabila, lugha, na watu.
29 Ndio, Bwana, walinzi wako watapaza sauti yao; kwa sauti pamoja wataimba; kwani wataonana ana kwa ana, wakati Bwana atakapoleta tena Sayuni.
30 Shangilieni, imbeni pamoja, enyi mahali pa ukiwa pa Yerusalemu; kwani Bwana amewafariji watu wake, amekomboa Yerusalemu.
31 Bwana ameuweka mkono wake wazi mbele ya macho ya mataifa yote; na nchi zote za ulimwengu zitaona wokovu wa Mungu wetu.

## Mosia 16

1 Na sasa, ikawa kwamba baada ya Abinadi kuzungumza maneno haya alinyosha mkono wake na kusema: Wakati utakuja ambapo wote wataona wokovu wa Bwana; wakati kila taifa, kabila, lugha, na watu wataona ana kwa ana na kutubu kwa Mungu kwamba hukumu zake ni za haki.
2 Na kisha waovu watatupwa nje, na watakuwa na sababu ya kupiga makelele, na kulia, na kuomboleza, na kusaga meno yao; na haya ni kwa sababu hawakutii sauti ya Bwana; kwa hivyo Bwana hawakomboi.
3 Kwani wana tamaa na uibilisi, na ibilisi ana uwezo juu yao; ndio, hata yule nyoka wa kale aliyewadanganya wazazi wetu wa kwanza, ambayo ilikuwa ni sababu ya kuanguka kwao; ambayo ni sababu ya wanadamu wote kuwa na tamaa, tamaa za kimwili, uibilisi, kujua uovu na wema, na kujitolea kwa ibilisi.
4 Hivyo wanadamu wote walipotea; na tazama, wangekuwa wamepotea daima kama sio kwamba Mungu aliwakomboa watu wake kutoka hali yao ya upotevu.
5 Lakini kumbuka kwamba yule anayeendelea na kufuata hali yake ya tamaa, na kuendelea katika njia za dhambi na kumuasi Mungu, hubaki katika hali yake ya kuanguka na ibilisi ana uwezo wote juu yake. Kwa hivyo kwake yeye ni kama ukombozi haukufanywa, akiwa adui kwa Mungu; na pia ibilisi ni adui wa Mungu.
6 Na sasa kama Kristo hangekuja ulimwenguni, akizungumza kuhusu vitu vitakavyokuja kama tayari vimeshakuja, hakungekuwa na ukombozi.
7 Na kama Kristo hangefufuka kutoka kwa wafu, au kuvunja kamba za kifo kwamba kaburi lisiwe na ushindi, na kwamba kifo kisiwe na uchungu, hakungekuwa na ufufuo.
8 Lakini kuna ufufuo, kwa hivyo kaburi halina ushindi, na uchungu wa kifo umemezwa katika Kristo.
9 Yeye ni nuru na uzima wa ulimwengu; ndio, nuru isiyo na mwisho, ambayo haiwezi kuwekwa giza; ndio, na pia uzima usio na mwisho, kwamba hakutakuwa tena na kifo.
10 Hata huu mwili wenye kufa utajivika kutokufa, na hii iharibikayo itavaa isiyoharibika, na italetwa kusimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, kuhukumiwa na yeye kulingana na matendo yao kama ni mema au kama ni maovu—
11 Kama ni wema, watafufuliwa katika maisha na furaha isiyo na mwisho; na kama ni waovu, watafufuliwa katika laana ya milele, na kuwekwa kwa ibilisi, ambaye amewatawala, ambayo ni laana—

12 Kwa vile walienda kulingana na nia zao za tamaa na tamaa za kimwili; wakiwa
wamekosa kumlingana Bwana waliponyoshewa mikono ya rehema; kwani
walinyoshewa mikono ya rehema, na hawakukubali; wao wakiwa wameonywa
kuhusu uovu wao lakini hawakuuacha; na waliamriwa watubu lakini hawakutubu.
13 Na sasa, haiwapasi nyinyi kutetemeka na kutubu dhambi zenu, na kukumbuka
kwamba ni kwa na katika Kristo pekee mnakoweza kuokolewa?
14 Kwa hivyo, kama mnafunza sheria ya Musa, funzeni pia kwamba ni kivuli cha vile
vitu vitakavyokuja—
15 Wafunze kwamba ukombozi huja kwa Kristo aliye Bwana, ambaye ni Baba
kamili hasa wa Milele. Amina.

## Mosia 17

1 Na sasa ikawa kwamba baada ya Abinadi kumaliza mazungumzo haya, kwamba
mfalme aliamuru kwamba makuhani wamkamate na kumuua.
2 Lakini kulikuwa na mmoja miongoni mwao ambaye jina lake lilikuwa Alma, yeye
pia akiwa uzao wa Nefi. Na alikuwa kijana, na aliamini maneno ambayo Abinadi
alizungumza, kwani alijua kuhusu ule uovu ambao Abinadi alikuwa ameshuhudia
dhidi yao; kwa hivyo akaanza kumsihi mfalme kwamba asimkasirikie Abinadi,
lakini kwamba amruhusu aende kwa amani.
3 Lakini mfalme alipandwa na hasira zaidi, na akaamuru kwamba Alma aondolewe
kutoka miongoni mwao, na kuwatuma watumishi wake wamfuate ili wamuue.
4 Lakini alitoroka na kujificha hata kwamba hawakumpata. Na yeye akiwa
amejifichiwa kwa siku nyingi, aliyaandika maneno yote ambayo Abinadi alikuwa
amezungumza.
5 Na ikawa kwamba mfalme alisababisha walinzi wake wamzingire Abinadi na
kumkamata; na wakamfunga na kumtia gerezani.
6 Na baada ya siku tatu, baada ya kushauriana na makuhani wake, aliamuru tena
kwamba aletwe mbele yake.
7 Na akamwambia: Abinadi, tumekupata na lawama, na wewe unastahili kifo.
8 Kwani wewe umesema kwamba Mungu mwenyewe atashuka miongoni mwa
watoto wa watu; na sasa, kwa sababu hii utauliwa usiporudisha yale maneno yote
maovu ambayo umezungumza kunihusu na watu wangu.
9 Sasa Abinadi akamwambia: ninakwambia, sitarudisha maneno ambayo
nimekuzungumzia kuhusu watu hawa, kwani ni ya kweli; na ili ujue uhakika wa
haya maneno nimekubali kuanguka mikononi mwako.
10 Ndio, na nitateseka hadi kifo, na sitarudisha maneno yangu, na yatakuwa
ushahidi dhidi yenu. Na mkiniua mtamwaga damu isiyo na hatia, na hii nayo pia
itakuwa ni ushahidi dhidi yenu siku ya mwisho.
11 Na sasa mfalme Nuhu alikuwa karibu kumwachilia huru, kwani aliogopa
maneno yake; kwani aliogopa kwamba hukumu za Mungu zitamshukia.
12 Lakini makuhani walipiga makelele, na kuanza kumshutumu, wakisema:
Amemtusi mfalme. Kwa hivyo mfalme alimkasirikia, na akamtoa ili auawe.
13 Na ikawa kwamba walimkamata na kumfunga, na kumpiga ngozi yake kwa kuni
za moto, ndio, hata akafariki.
14 Na sasa wakati miale ya moto ilianza kumchoma, aliwalilia, akisema:
15 Tazameni, hata vile mmenifanyia, ndivyo itakavyokuwa kwamba uzao wenu

utawafanya wengi kuteseka kwa uchungu kama ule ambao mmenitesa nao, hata uchungu wa kifo kwa moto; na haya ni kwa sababu wanaamini wokovu wa Bwana Mungu wao.

16 Na itakuwa kwamba mtasumbuliwa na aina zote za magonjwa kwa sababu ya maovu yenu.

17 Ndio, na mtapigwa kutoka kila mkono, na mtafukuzwa na kutawanywa hapa na pale, hata kama vile mifugo ya mwituni hukimbizwa na wanyama katili na wakali.

18 Na katika siku ile mtawindwa, na kukamatwa kwa mikono ya maadui zenu, na kisha mtateseka, kama vile ninavyoteseka, uchungu wa kifo kwa moto.

19 Na hivyo ndivyo Mungu hulipiza kisasi juu ya wale wanaowaangamiza watu wake. Ee Mungu, pokea nafsi yangu.

20 Na sasa, baada ya Abinadi kusema maneno haya, alianguka chini, akiwa amepata mateso ya kifo kwa moto; ndio, akiwa ameuawa kwa sababu alikataa kukana amri za Mungu, akiwa ametilia muhuri ukweli wa maneno yake kwa kifo chake.

## Mosia 18

1 Na sasa, ikawa kwamba Alma, ambaye alikuwa ametoroka kutoka kwa watumishi wa Mfalme Nuhu, alitubu dhambi zake na maovu yake, na akaenda kwa siri miongoni mwa watu, na kuanza kufunza maneno ya Abinadi—

2 Ndio, kuhusu yale ambayo yatakuja, na pia kuhusu ufufuo wa wafu, na ukombozi wa watu, ambao ungewezeshwa kwa uwezo, na mateso, na kifo cha Kristo, na ufufuko wake na kupaa mbinguni.

3 Na kwa wengi waliotaka kusikiliza neno lake aliwafunza. Na aliwafunza kwa siri, ili mfalme asijue. Na wengi waliamini maneno yake.

4 Na ikawa kwamba wengi waliomwamini walienda mahali palipoitwa Mormoni, kwani paliitwa kwa jina la mfalme, pakiwa mpakani mwa nchi ambayo ilikuwa imejaa, wanyama wa mwitu nyakati zote.

5 Sasa, hapo Mormoni palikuwa na chemchemi ya maji safi, na Alma alikimbilia hapo, kwani karibu na maji hayo palikuwa na kichaka cha miti midogo, na alijificha hapo wakati wa mchana ili asipatikane na misako ya mfalme.

6 Na ikawa kwamba wale wengi waliomwamini walienda hapo kusikia maneno yake.

7 Na ikawa kwamba baada ya siku nyingi kulikuwa na kikundi kikubwa kimekusanyika pamoja mahali pa Mormoni, ili kusikia maneno ya Alma. Ndio, wote walioamini neno lake walikusanyika pamoja, kumsikiliza. Na aliwafunza, na akawahubiria toba, na ukombozi, na imani kwa Bwana.

8 Na ikawa kwamba aliwaambia: Tazameni, hapa kuna maji ya Mormoni (kwani hivi ndivyo yaliitwa) na sasa, kwa vile mnatamani kujiunga na zizi la Mungu, na kuitwa watu wake, na mko radhi kubeba mizigo ya mmoja na ya mwingine, ili iwe mepesi;

9 Ndio, na mko tayari kuomboleza na wale wanaoomboleza; ndio, na kufariji wale ambao wanahitaji kufarijiwa, na kusimama kama mashahidi wa Mungu nyakati zote na katika vitu vyote, na katika mahali popote mlipo, hata hadi kifo, ili muweze kukombolewa na Mungu, na kuhesabiwa pamoja na wale wa ufufuko wa kwanza, ili mpokee uzima wa milele—

10 Sasa ninawaambia, ikiwa hili ndilo pendo la mioyo yenu, ni nini mnacho dhidi

ya kubatizwa kwa jina la Bwana, kama ushahidi mbele yake kwamba mmeingia
kwenye agano na yeye, kwamba mtamtumikia na kushika amri zake, ili
awateremshie Roho yake juu yenu zaidi?
11 Na sasa wakati watu waliposikia haya maneno, walipiga makofi kwa shangwe, na
wakasema kwa nguvu: Hili ndilo pendo la mioyo yetu.
12 Na sasa ikawa kwamba Alma alimchukua Helamu, yeye akiwa wa kwanza, na
kuenda na kusimama majini, na kupaza sauti yake, akisema: Ee Bwana, mteremshie
mtumishi wako Roho wako, ili afanye kazi hii kwa utakatifu wa moyo.
13 Na aliposema maneno haya, Roho wa Bwana alishuka juu yake, na akasema:
Helamu, nakubatiza wewe, nikiwa na mamlaka kutoka kwa Mwenyezi Mungu,
kama ushahidi kwamba umeingia kwenye agano kumtumikia hadi utakapofariki
mwilini; na Roho wa Bwana akuteremkie; na akupe uzima wa milele, kupitia kwa
ukombozi wa Kristo, ambaye amemtayarisha tangu msingi wa ulimwengu.
14 Na baada ya Alma kusema maneno haya, Alma pamoja na Helamu walizikwa
majini; na wakainuka na wakatoka majini wakishangilia wakiwa wamejazwa na
Roho.
15 Na tena, Alma akamchukua mwingine, na kuingia majini mara ya pili, na
akambatiza kama yule wa kwanza, lakini hakujizika kwa maji tena.
16 Na hivi ndivyo alivyobatiza kila mmoja aliyeenda mahali pa Mormoni; na
walikuwa watu mia mbili na nne; ndio, na walibatizwa katika maji ya Mormoni, na
wakajazwa na neema ya Mungu.
17 Na waliitwa kanisa la Mungu, au kanisa la Kristo, kutoka siku ile na kuendelea
mbele. Na ikawa kwamba yeyote aliyebatizwa kwa uwezo na mamlaka ya Mungu
aliongezwa katika kanisa lake.
18 Na ikawa kwamba Alma, akiwa na mamlaka kutoka kwa Mungu, aliwateua
makuhani; hata kuhani mmoja kwa kila kikundi cha hamsini aliwatawaza
kuwahubiria, na kuwafunza kuhusu vitu vya ufalme wa Mungu.
19 Na akawaamuru kwamba wasifunze chochote ila tu vitu vile ambavyo alikuwa
amewafunza, na ambavyo vilikuwa vimezungumzwa na manabii watakatifu.
20 Ndio, hata aliwaamuru kwamba wasihubiri chochote ila tu toba na imani kwa
Bwana, ambaye alikuwa amewakomboa watu wake.
21 Na akawaamuru kwamba wasiwe na ubishi wao kwa wao, lakini kwamba
watazame kwa jicho moja, kwa imani moja ubatizo mmoja, na mioyo yao ikiwa
imeunganishwa pamoja kwa umoja na kwa kupendana wao kwa wao.
22 Na hivi ndivyo alivyowaamuru kuhubiri. Na hivyo wakawa watoto wa Mungu.
23 Na akawaamuru kwamba waiheshimu siku ya sabato, na kuiweka iwe takatifu, na
pia kwamba wamshukuru Bwana Mungu wao kila siku.
24 Na pia akawaamuru kwamba makuhani wale ambao alikuwa amewateua wafanye
kazi kwa mikono yao ili wajitegemee.
25 Na kulikuwa na siku moja kwa kila juma ambayo ilitengwa ili wakusanyike
pamoja kuwafunza watu, na kumuabudu Bwana Mungu wao, na pia, mara kwa mara
kama walivyo na uwezo, kukusanyika pamoja.
26 Na makuhani wasitegemee watu kwa chakula chao; lakini watapokea neema ya
Mungu kwa sababu ya utumishi wao, ili wapokee nguvu za Roho, na kumfahamu
Mungu, ili wafunze kwa uwezo na mamlaka kutoka kwa Mungu.
27 Na tena Alma akaamuru kwamba watu wa kanisa watoe mali yao, kila mmoja
kulingana na kile alichokuwa nacho; kama yuko na tele basi na yeye atoe kwa wingi;

na kwa yule ambaye ana chache, basi chache ndizo zitahitajika; na yule ambaye hana basi naye apewe.
28 Na hivyo watoe mali yao kwa hiari yao na nia njema kwa Mungu, na kwa wale makuhani waliohitaji, ndio, na kwa kila mtu aliyehitaji, na aliye uchi.
29 Na hivi aliwaambia, akiwa ameamriwa na Mungu; na walitembea imara mbele ya Mungu, wakisaidiana kimwili na kiroho kulingana na mahitaji yao na matakwa yao.
30 Na sasa ikawa kwamba haya yote yalifanywa katika Mormoni, ndio, karibu na maji ya Mormoni, katika mwitu uliokuwa karibu na maji ya Mormoni; ndio, mahali pa Mormoni, maji ya Mormoni, mwitu wa Mormoni, jinsi gani yalivyo na wema machoni mwa wale ambao walimfahamu Mkombozi wao hapo; ndio, na jinsi gani wamebarikiwa, kwani wataimba sifa zake milele.
31 Na vitu hivi vilifanywa mipakani ya nchi, ili visijulikane na mfalme.
32 Lakini tazama, ikawa kwamba mfalme, akiwa amegundua kuwa kuna njama miongoni mwa watu, alituma watumishi wake kuwachunguza. Kwa hivyo siku ile waliyokuwa wanakusanyika pamoja kusikia neno la Bwana waligunduliwa kwa mfalme.
33 Na sasa mfalme akasema kuwa Alma alikuwa anawachochea watu ili wamuasi; kwa hivyo alituma jeshi lake kuwaangamiza.
34 Na ikawa kwamba Alma na watu wa Bwana walijulishwa kuhusu uvamizi wa jeshi la mfalme; kwa hivyo walichukua hema zao na jamii zao na kukimbilia nyikani.
35 Na walikuwa hesabu ya watu karibu mia nne na hamsini.

# Mosia 19

1 Na ikawa kwamba jeshi, la mfalme lilirejea, baada ya msako wao wa watu wa Bwana kukosa kufua dafu.
2 Na sasa tazama, vikosi vya mfalme vilikuwa vidogo, vikiwa vimepunguzwa, na pakaanza kuwa na mgawanyiko miongoni mwa watu waliosalia.
3 Na ile sehemu ndogo ikaanza kumtolea mfalme vitisho, na kukawa na ubishi mkuu miongoni mwao.
4 Na sasa miongoni mwao kulikuwa na mtu ambaye jina lake lilikuwa Gideoni, na yeye akiwa mtu mwenye nguvu na adui ya mfalme, kwa hivyo alichomoa upanga wake, na kuapa kwa hasira kwamba atamuua mfalme.
5 Na ikawa kwamba alipigana na mfalme; na mfalme alipoona kwamba alikuwa karibu kushindwa, alikimbia na kupanda kwenye mnara uliokuwa karibu na hekalu.
6 Na Gideoni alimkimbiza na alikaribia kupanda ule mnara ili amuue mfalme, na mfalme akatazama nchi ya Shemloni, na tazama, jeshi la Walamani lilikuwa mipakani mwa nchi.
7 Na sasa mfalme alilia kwa maumivu ya nafsi yake, na kusema: Gideoni, nisamehe, kwani Walamani wanatushambulia, na watatuangamiza; ndio, wataangamiza watu wangu.
8 Na sasa mfalme hakujali watu wake kama vile alivyojali maisha yake; walakini, Gideoni aliyaokoa maisha yake.
9 Na mfalme akaamuru watu wake kwamba wawakimbie mbele Walamani, na yeye mwenyewe akawaongoza, na wakakimbilia nyikani, pamoja na wake zao na watoto wao.
10 Na ikawa kwamba Walamani waliwafuata, na kuwafikia, na kuanza kuwaua.

11 Sasa ikawa kwamba mfalme aliamuru wanaume wote kwamba wawaache wake zao na watoto wao, na wawatoroke Walamani.

12 Sasa kulikuwa na wengi ambao hawakuwaacha, lakini waliona vizuri kubaki nao na kuangamia nao. Na wengine waliacha wake zao na watoto wao na kukimbia.

13 Na ikawa kwamba wale waliobaki na wake zao na watoto wao waliwafanya mabinti zao walio warembo kusimama mbele ya Walamani na kuwasihi kwamba wasiwaue.

14 Na ikawa kwamba Walamani waliwaonea huruma, kwani walivutiwa na urembo wa wanawake wao.

15 Kwa hivyo Walamani waliokoa maisha yao, na kuwachukua kama mateka na kuwapeleka katika nchi ya Nefi, na kuwaruhusu kwamba warithi nchi ile, na kuwapatia masharti kwamba watamkabidhi mfalme Nuhu mikononi mwa Walamani, na kutoa mali yao, hata nusu ya yote waliyokuwa nayo; nusu ya dhahabu yao, na fedha yao, na vitu vyao vyote vyenye thamani, na hivyo ndivyo watalipa ushuru kwa mfalme wa Walamani mwaka kwa mwaka.

16 Na sasa kulikuwa na mmoja wa wana wa mfalme miongoni mwa wale waliochukuliwa kama mateka, aliyeitwa kwa jina la Limhi.

17 Na sasa Limhi hakutaka baba yake aangamizwe; walakini, Limhi hakukosa kuona maovu ya baba yake, yeye mwenyewe akiwa mtu mwenye haki.

18 Na ikawa kwamba Gideoni alituma watu nyikani kwa siri, kumsaka mfalme na wale waliokuwa na yeye. Na ikawa kwamba waliwapata watu wote nyikani, ila tu mfalme na makuhani wake.

19 Sasa walikuwa wameapa mioyoni mwao kwamba watarejea katika nchi ya Nefi, na kama wake zao na watoto wao wameuawa, na pia wale waliobaki nao, kwamba wangelipiza kisasi, na pia kuangamia nao.

20 Na mfalme akawaamuru kwamba wasirejee; na walimkasirikia mfalme, na kusababisha kwamba afariki, kwa moto.

21 Na walikuwa karibu ya kuwakamata makuhani pia na kuwaua, na waliwatoroka.

22 Na ikawa kwamba walikuwa karibu ya kurejea katika nchi ya Nefi, na wakakutana na watu wa Gideoni. Na watu wa Gideoni wakawaelezea yale yaliyowapata wake zao na watoto wao; na kwamba Walamani walikuwa wamewaruhusu kumiliki nchi kwa kulipa kodi kwa Walamani kiasi cha nusu ya mali yote waliyokuwa nayo.

23 Na wale watu wakawaambia watu wa Gideoni kwamba walikuwa wamemuua mfalme, na makuhani wake walikuwa wametorokea nyikani.

24 Na ikawa kwamba baada ya wao kumaliza ile sherehe, kwamba walirejea katika nchi ya Nefi, wakishangilia, kwa sababu wake zao na watoto wao hawakuwa wameuawa; na wakamwambia Gideoni yale waliyokuwa wamemfanyia mfalme.

25 Na ikawa kwamba mfalme wa Walamani alikula kiapo na wao, kwamba watu wake hawatawaua.

26 Na pia Limhi, akiwa mwana wa mfalme, akiwa amepewa ufalme na watu, aliapa kwa mfalme wa Walamani kwamba watu wake watamlipa ushuru, kiasi cha nusu ya chochote walicho nacho.

27 Na ikawa kwamba Limhi alianza kuimarisha ufalme na kudumisha amani miongoni mwa watu wake.

28 Na mfalme wa Walamani aliweka walinzi waizingire nchi, ili awaweke watu wa Limhi katika nchi ile, ili wasiondoke na kwenda nyikani; na aliwalisha walinzi wake kwa ushuru aliopokea kutoka kwa Wanefi.

29 Na sasa mfalme Limhi alikuwa na amani katika ufalme wake kwa kipindi cha miaka miwili, kwamba Walamani hawakuwavamia wala kutaka kuwaangamiza.

## Mosia 20

1 Sasa palikuwa na pahali katika Shemloni ambapo mabinti za Walamani walikusanyika pamoja kuimba, na kucheza, na kujifurahisha.

2 Na ikawa kwamba siku moja kikundi chao kidogo kilikusanyika pamoja ili waimbe na wacheze.

3 Na sasa makuhani wa mfalme Nuhu, wakiona aibu ya kurejea katika mji wa Nefi, ndio, na pia wakiogopa kwamba watu watawaua, kwa hivyo hawakuwarudia wake zao na watoto wao.

4 Na baada ya kungoja nyikani, na baada ya kugundua mabinti za Walamani, walijificha na kuwatazama;

5 Na wakati walikuwa ni wachache tu waliokusanyika pamoja kucheza, waliondoka pahali pao pa siri na kuwashika na kuwapeleka nyikani; ndio, mabinti ishirini na nne wa Walamani waliwapeleka nyikani.

6 Na ikawa kwamba Walamani walipogundua kwamba mabinti zao walikuwa wamepotea, walikasirikia watu wa Limhi, kwani walidhani kuwa ni watu wa Limhi.

7 Kwa hivyo walituma majeshi yao; ndio, hata mfalme aliongoza watu wake; na wakaelekea nchi ya Nefi kuwaangamiza watu wa Limhi.

8 Na sasa Limhi alikuwa amewaona kutoka kwa mnara, hata matayarisho yao yote ya vita alikuwa ameyaona; kwa hivyo aliwakusanya watu wake, na akawangoja huko mwituni na vichakani.

9 Na ikawa kwamba Walamani walipokuja, wale watu wa Limhi walianza kuwashambulia kutoka pahali pao pa kujificha, na kuanza kuwaua.

10 Na ikawa kwamba vita vilipamba moto, kwani walipigana kama simba kwa mawindo yao.

11 Na ikawa kwamba watu wa Limhi walianza kuwakimbiza Walamani; ingawa hawakuwa wengi kama Walamani. Lakini walipigania maisha yao, na wake zao, na watoto wao; kwa hivyo walijitahidi na wakapigana kama joka.

12 Na ikawa kwamba walimpata mfalme wa Walamani miongoni mwa wafu wao; walakini hakuwa amefariki, akiwa amejeruhiwa na kuachiliwa chini, kwani watu wake walitoroka kwa haraka.

13 Na wakamchukua na kufunga majeraha yake, na kumpeleka mbele ya Limhi, na kusema: Tazama, hapa kuna mfalme wa Walamani; alijeruhiwa na akawa ameanguka miongoni mwa wafu wao, na wamemuacha; na tazama, tumemleta mbele yako; na sasa hebu tumuue.

14 Lakini Limhi akawaambia: Hamtamuua, lakini mleteni hapa ili nimuone. Na wakamleta. Na Limhi akamwambia: Ni sababu gani iliyokufanya kushambulia watu wangu? Tazama, watu wangu hawajavunja kiapo nilichofanya nawe; kwa hivyo, kwa nini uvunje kiapo ulichofanya na watu wangu?

15 Na sasa mfalme akasema: Nimevunja kiapo kwa sababu watu wako waliwachukua mabinti za watu wangu; kwa hivyo, kwa hasira yangu niliwafanya watu wangu wawashambulie watu wako.

16 Na sasa Limhi hakuwa amesikia lolote kuhusu jambo hili; kwa hivyo akasema: Nitatafuta miongoni mwa watu wangu na yeyote ambaye ametenda kitu hiki

ataangamia. Kwa hivyo akaamuru msako ufanywe miongoni mwa watu wake.
17 Sasa Gideoni aliposikia vitu hivi, yeye akiwa kapteni wa mfalme, alienda na
kumwambia mfalme: Nakuomba usubiri na usiwasake watu hawa, na
usiwashutumu kwa kitu hiki.
18 Kwani hukumbuki makuhani wa baba yako, ambao watu hawa walitaka
kuangamiza? Na je, hawako huko nyikani? Na je, si wao ndio waliowachukua
mabinti za Walamani?
19 Na sasa, tazama, mwambie mfalme kuhusu vitu hivi, ili awaambie watu wake na
ili watulizwe nasi; kwani tazama tayari wanajitayarisha kutuvamia; na tazama sisi ni
wachache.
20 Na tazama, wanakuja na majeshi yao; na ijapokuwa mfalme awasihi kwa niaba
yetu lazima tuangamie.
21 Kwani si maneno ya Abinadi yanatimizwa, yale aliyotoa unabii kinyume
chetu — na haya yote kwa sababu hatukutii maneno ya Bwana, na kuacha maovu
yetu?
22 Na sasa hebu tumtulize mfalme, na tutimize kiapo ambacho tulifanya kwake;
kwani ni afadhali tuwe utumwani badala ya kupoteza maisha yetu; kwa hivyo, hebu
tukomeshe umwagaji wa damu nyingi.
23 Na sasa Limhi akamwambia mfalme vitu vyote kuhusu baba yake, na makuhani
waliokimbilia nyikani, na akawashutumu kwa kuwachukua mabinti zao.
24 Na ikawa kwamba mfalme alitulizwa na watu wake; na akawaambia: Hebu
twende tukalaki watu wangu, bila silaha; na ninaapa kwa kiapo kwamba watu
wangu hawatawaua watu wako.
25 Na ikawa kwamba walimfuata mfalme, na wakaenda kuwalaki Walamani bila
silaha. Na ikawa kwamba walikutana na Walamani; na mfalme wa Walamani
akainama mbele yao, na kuwatetea watu wa Limhi.
26 Na Walamani walipoona watu wa Limhi, kwamba hawakuwa na silaha,
waliwaonea huruma na wakatulizwa na wao, na wakarejea na mfalme wao kwa
amani nchini mwao.

## Mosia 21

1 Na ikawa kwamba Limhi na watu wake walirejea katika mji wa Nefi, na wakaanza
kuishi tena kwa amani katika nchi.
2 Na ikawa kwamba baada ya siku nyingi Walamani walianza tena kuzusha hasira
na Wanefi, na wakaanza kusogea karibu na mipaka iliyozingira nchi.
3 Sasa hawakuthubutu kuwaua, kwa sababu ya kile kiapo ambacho mfalme wao
alikuwa amemuapia Limhi; walakini waliwacharaza makofi kwenye mashavu, na
kuwa na mamlaka juu yao; na kuwabebesha mizigo mizito kwa migongo yao, na
kuwakimbiza kama vile wanavyomfanyia punda bubu —
4 Ndio, haya yote yalifanywa ili neno la Bwana litimizwe.
5 Na sasa mateso ya Wanefi yalikuwa ni makuu, na hapakuwa na njia yoyote ya
kujikomboa kutoka mikononi mwao, kwani Walamani waliwazingira kwa kila
upande.
6 Na ikawa kwamba watu walianza kumnung'unikia mfalme kwa sababu ya mateso
yao; na wakaanza kutamani kupigana nao. Na walimsumbua mfalme kwa
malalamiko yao; kwa hivyo akawaruhusu wafanye kulingana na tamaa yao.

7 Na wakakusanyika pamoja tena, na kuvaa silaha zao, na kuwaendea Walamani ili wawafukuze kutoka nchi yao.
8 Na ikawa kwamba Walamani waliwapiga, na kuwasukuma nyuma, na kuwaua wengi wao.
9 Na sasa kulikuwa na maombolezo makuu na kilio miongoni mwa watu wa Limhi, mjane akiomboleza mume wake, mwana na binti wakiomboleza baba yao, na kaka kwa kaka zao.
10 Sasa kulikuwa na wajane wengi nchini, na walilia sana siku kwa siku, kwani woga mkuu wa Walamani uliwaingia.
11 Na ikawa kwamba vilio vyao viliwachochea wale watu waliobaki wa Limhi kuwakasirikia Walamani; na wakaenda vitani tena, lakini walisukumwa nyuma tena, na wakapata maafa makuu.
12 Ndio, walienda tena mara ya tatu, na wakateseka kama hapo awali; na wale ambao hawakuuawa walirejea tena katika nchi ya Nefi.
13 Na wakanyenyekea mpaka mavumbini, na kujitoa kwa nira ya utumwa, na kukubali kupigwa, na kukimbizwa hapa na pale, na kulemeshwa, kulingana na matakwa ya maadui wao.
14 Na walinyenyekea chini kabisa na hata kuwa chini ya unyenyekevu; na walimlilia Mungu sana; ndio, hata siku yote walimlilia Mungu wao kwamba awakomboe kutokana na mateso yao.
15 Na sasa Bwana alikuwa na upole wa kusikia kilio chao kwa sababu ya maovu yao; haidhuru Bwana alisikia vilio vyao, na akaanza kulainisha mioyo ya Walamani kwamba wakaanza kupunguza mizigo yao; walakini Bwana hakuonelea vyema kuwakomboa kutoka utumwani.
16 Na ikawa kwamba walianza kufanikiwa nchini kiasi kwa kiasi, na wakaanza kupanda nafaka kwa wingi, na mifugo, na wanyama, kwamba hawakuteseka kwa njaa.
17 Sasa kulikuwa na wanawake wengi, zaidi ya wanaume; kwa hivyo mfalme Limhi akaamuru kwamba kila mwanaume atoe ili wajane na watoto wao wapate kusaidiwa, na ili wasiangamie kwa njaa; na walitenda haya kwa sababu wengi wao walikuwa wameuawa.
18 Sasa watu wa Limhi waliishi kwa kikundi kama ilivyowezekana, na kulinda nafaka yao na mifugo yao;
19 Na mfalme mwenyewe alihofia maisha yake nje ya ukuta wa mji, isipokuwa awe na walinzi wake na yeye, akiogopa kwamba ingewezekana aanguke mikononi mwa Walamani.
20 Na akasababisha watu wake washike zamu kila mahali nchini, ili ikiwezekana wawakamate makuhani ambao walikuwa wametorokea nyikani, ambao walikuwa wamewachukua mabinti za Walamani, na ambao walikuwa wamesababisha maangamizi makuu kuwapata.
21 Kwani walitamani kuwakamata na kuwaadhibu; kwa sababu walikuwa wameingia katika nchi ya Nefi wakati wa usiku, na kuiba nafaka yao na vitu vyao vingi vyenye thamani; kwa hivyo walijificha na kuwangoja.
22 Na ikawa kwamba hakukuwa na ghasia yoyote miongoni mwa Walamani na watu wa Limhi, hadi ule wakati ambao Amoni na ndugu zake walipowasili katika nchi.
23 Na mfalme akiwa nje ya lango la mji na walinzi wake, aliwaona Amoni na ndugu zake; na akidhani kwamba wao ni makuhani wa Nuhu, kwa hivyo aliamrisha

kwamba washikwe, na kufungwa, na kuwekwa gerezani. Na kama wangekuwa makuhani wa Nuhu, angeamuru wauawe.

24 Lakini alipofahamu kwamba sio wao, walakini walikuwa ndugu zake, waliotoka nchi ya Zarahemla, alijazwa na shangwe kuu.

25 Sasa mfalme Limhi alikuwa ametuma, kikundi kidogo cha watu kutafuta nchi ya Zarahemla, kabla ya kuwasili kwa Amoni; lakini hawakuipata, na walipotea huko nyikani.

26 Walakini, walipata nchi ambamo watu walikuwa wameishi; ndio, nchi ambayo ilijaa mifupa iliyokauka; ndio, nchi ambayo watu walikuwa wameishi na ambao walikuwa wameangamizwa; na wao, wakidhani kuwa ni nchi ya Zarahemla, walirejea katika nchi ya Nefi, wakiwa wamewasili mipakani mwa nchi siku chache kabla ya kufika kwa Amoni.

27 Na walileta maandishi, hata maandishi ya watu wale ambao walipata mifupa yao; na yalikuwa yamechorwa kwenye bamba za chuma.

28 Na sasa Limhi alijawa shangwe tena alipoambiwa kwa kinywa cha Amoni kwamba mfalme Mosia alikuwa na karama kutoka kwa Mungu, ambayo ingemwezesha kutafsiri michoro kama ile; ndio, na hata Amoni pia alifurahi.

29 Walakini Amoni na ndugu zake walijawa na huzuni kwa sababu ndugu zao wengi walikuwa wameuawa;

30 Na pia kwamba mfalme Nuhu na makuhani wake walikuwa wamewafanya watu kumtendea Mungu dhambi nyingi na maovu; na pia waliomboleza kifo cha Abinadi; na pia kuondoka kwa Alma na watu walioenda na yeye, ambao walikuwa wameanzisha kanisa la Mungu kwa nguvu na uwezo wa Mungu, na kwa imani katika yale maneno yaliozungumzwa na Abinadi.

31 Ndio, waliomboleza kuondoka kwao, kwani hawakujua walikotorokea. Sasa wangeungana nao bila kusita, kwani wao wenyewe walikuwa wameingia kwenye agano na Mungu kwamba watamtumikia na kutii amri zake.

32 Na sasa tangu kuwasili kwa Amoni, mfalme Limhi pia alikuwa ameingia kwenye agano na Mungu, na pia watu wake wengi, kumtumikia na kutii amri zake.

33 Na ikawa kwamba mfalme Limhi na watu wake wengi walitamani kubatizwa; lakini hapakuwa na yeyote katika nchi ile aliyekuwa na mamlaka kutoka kwa Mungu. Na Amoni alikataa kufanya kitu hiki, akijidhania kwamba yeye ni mtumishi asiyestahili.

34 Kwa hivyo wakati ule hawakujiunda pamoja kama kanisa, wakimsubiri Roho wa Bwana. Sasa walitamani kuwa kama Alma na ndugu zake, ambao walikuwa wametorokea nyikani.

35 Walitamani kubatizwa kama ushahidi na ushuhuda kwamba wako tayari kumtumikia Mungu kwa mioyo yao yote; walakini waliongeza wakati; na maelezo ya ubatizo wao yatatolewa hapo baadaye.

36 Na sasa mawazo yote ya Amoni na watu wake, na mfalme Limhi na watu wake, yalikuwa ni jinsi ya kujikomboa kutoka mikono ya Walamani na kutoka utumwa.

## Mosia 22

1 Na sasa ikawa kwamba Amoni na mfalme Limhi walishauriana na watu jinsi ya kujikomboa kutoka utumwani; na hata walisababisha kwamba watu wote wakusanyike pamoja; na walifanya hivi ili wapate sauti ya watu kuhusu jambo hili.

2 Na ikawa kwamba hawakupata njia yoyote ya kujitoa utumwani, ila tu
wawachukue wake zao na watoto wao, na mifugo yao, na wanyama wao, na hema
zao, na kuenda nyikani; kwani Walamani wakiwa wengi mno, ilikuwa haiwezekani
kwa watu wa Limhi kupigana nao, wakifikiria kujikomboa kutoka utumwani kwa
upanga.
3 Na sasa ikawa kwamba Gideoni alienda na kusimama mbele ya mfalme, na
kumwambia: Sasa Ee mfalme, wewe umekuwa ukisikiliza maneno yangu mara
nyingi wakati tulipokuwa tunabishana na ndugu zetu, Walamani.
4 Na sasa Ee mfalme, kama wewe hujaniona kuwa mimi ni mtumishi asiyeleta
faida, au kama wewe umesikiliza maneno yangu kwa kiasi chochote, na yamekuwa
yenye huduma kwako, hata hivyo natamani kwamba usikilize maneno yangu wakati
huu, na nitakuwa mtumishi wako na kuwakomboa watu hawa kutoka utumwani.
5 Na mfalme akamruhusu kwamba azungumze. Na Gideoni akamwambia:
6 Tazama ule mlango wa nyuma, kupitia ukuta wa nyuma ulio upande wa nyuma
wa mji. Walamani, au walinzi wa Walamani, huwa wamelewa usiku; kwa hivyo hebu
tutume tangazo miongoni mwa watu hawa kwamba wakusanye pamoja mifugo yao
na wanyama wao, ili wawapeleke kwa usiku huko nyikani.
7 Na nitaenda kulingana na amri yako ili nilipe ushuru wa mwisho wa mvinyo kwa
Walamani, na watalewa; na tutapitia mlango wa siri ulio kushoto mwa kambi yao
watakapokuwa wamelewa na kulala.
8 Na hivyo tutaondoka na wake zetu na watoto wetu, mifugo yetu, na wanyama
wetu na kuenda nyikani; na tutasafiri kando ya nchi ya Shilomu.
9 Na ikawa kwamba mfalme alisikiliza maneno ya Gideoni.
10 Na mfalme Limhi alisababisha kwamba watu wake wakusanye mifugo yao
pamoja; na akatuma ushuru wa mvinyo kwa Walamani; na pia alituma mvinyo zaidi,
kama zawadi kwao; na walikunywa kwa wingi ule mvinyo uliotumwa kwao na
mfalme Limhi.
11 Na ikawa kwamba watu wa mfalme Limhi waliondoka usiku na kuenda nyikani
pamoja na mifugo yao na wanyama wao, na walizunguka nchi ya Shilomu nyikani,
na wakapinda njia yao na kuelekea nchi ya Zarahemla, wakiongozwa na Amoni na
ndugu zake.
12 Na walikuwa wamechukua dhahabu yao yote, na fedha, na vitu vyao vya thamani,
vile ambavyo waliweza kubeba, na pia maakuli yao, na kuenda nyikani; na
wakaendelea na safari yao.
13 Na baada ya kuwa nyikani kwa siku nyingi walifika katika nchi ya Zarahemla, na
kuungana na watu wa Mosia, na kuwa watu wake.
14 Na ikawa kwamba Mosia aliwapokea kwa shangwe; na pia alipokea maandishi
yao, na pia maandishi ambayo yalipatwa na watu wa Limhi.
15 Na sasa ikawa kwamba wakati Walamani walipogundua kwamba watu wa Limhi
walikuwa wameondoka nchini usiku, walituma jeshi huko nyikani kuwafuata;
16 Na baada ya kuwafuata kwa siku mbili, hawangefuata nyayo zao tena; kwa hivyo
walipotea huko nyikani.

*Historia ya Alma na watu wa Bwana, ambao walikimbizwa nyikani na watu wa Mfalme Nuhu.*

# Mosia 23

1 Sasa Alma, akiwa ameonywa na Bwana kwamba majeshi ya mfalme Nuhu
yatawavamia, na baada ya kujulisha watu wake, kwa hivyo walikusanya pamoja
mifugo yao, na kuchukua nafaka yao, na wakaondoka na kuelekea nyikani mbele ya
majeshi ya mfalme Nuhu.
2 Na Bwana aliwaongezea nguvu, kwamba watu wa mfalme Nuhu wasiwafikie na
kuwaangamiza.
3 Na wakasafiri kwa muda wa siku nane huko nyikani.
4 Na wakaja katika nchi fulani, ndio, nchi iliyo rembo na nzuri, nchi ya maji safi.
5 Na wakapiga hema zao, na wakaanza kulima ardhi, na kuanza kujenga majengo;
ndio, walikuwa wenye bidii, na walifanya kazi sana.
6 Na watu walitaka kwamba Alma awe mfalme wao, kwani alipendwa na watu
wake.
7 Lakini aliwaambia: Tazameni, haistahili kwamba tuwe na mfalme; kwani Bwana
asema hivi: Hamtatukuza mwili mmoja zaidi ya mwingine, au mtu asidhani kwamba
yuko juu zaidi ya mwingine; kwa hivyo nawaambia haistahili muwe na mfalme.
8 Walakini, kama ingewezekana muwe na watu wenye haki nyakati zote wawe
wafalme wenu ingekuwa ni vyema kwenu muwe na mfalme.
9 Lakini kumbukeni maovu ya mfalme Nuhu na makuhani wake; na mimi
mwenyewe nilinaswa katika mtego, na nilifanya vitu vingi ambavyo vilikuwa
vinachukiza machoni mwa Bwana, na vilinisababishia shida kuu ya kutubu;
10 Walakini, baada ya shida nyingi, Bwana alisikia vilio vyangu, na akajibu sala
zangu, na amenifanya kuwa chombo mikononi mwake cha kuwezesha wengi wenu
sana kuwa na ufahamu wa ukweli wake.
11 Walakini, kwa hii mimi sijitukuzi, kwani mimi sistahili kujitukuza mwenyewe.
12 Na sasa nawaambia, mmedhulumiwa na mfalme Nuhu, na mmekuwa utumwani
kwake na kwa makuhani wake, na kuwekwa kwenye uovu nao; kwa hivyo
mlifungwa kwa kanda za maovu.
13 Na sasa kwa vile mmekombolewa kwa nguvu za Mungu kutoka kwa hii
minyororo; ndio, kutoka kwa mikono ya mfalme Nuhu na watu wake, na pia kutoka
kwa minyororo ya maovu, hata hivyo ninataka msimame imara kwenye huo uhuru
ambao kwa hii mmekombolewa, na kwamba msimwamini mtu yeyote kuwa mfalme
juu yenu.
14 Na pia msimwamini yeyote kuwa mwalimu wenu wala mhubiri wenu, ila tu awe
mtu wa Mungu, anayetembea katika njia zake na kutii amri zake.
15 Hivi ndivyo Alma alivyowafunza watu wake, kwamba kila mtu ampende jirani
yake jinsi anavyojipenda mwenyewe, kwamba kusiwe na ubishi miongoni mwao.
16 Na sasa, Alma alikuwa kuhani wao mkuu, yeye akiwa mwanzilishi wa kanisa lao.
17 Na ikawa kwamba hakuna yeyote aliyepokea mamlaka ya kuhubiri au kufundisha
ila tu kwa yule wa kutoka kwa Mungu. Kwa hivyo aliwatakasa makuhani wao wote
na walimu wao wote; na hakuna yeyote aliyetakaswa ila tu wale wanadamu
waliokuwa wenye haki.
18 Kwa hivyo waliwalinda watu wao, na kuwalisha vitu vilivyohusu utakatifu.
19 Na ikawa kwamba walianza kufanikiwa sana nchini; na wakaiita nchi ile Helamu.
20 Na ikawa kwamba waliongezeka na kufanikiwa sana katika nchi ya Helamu; na
wakajenga mji, ambao waliuita mji wa Helamu.
21 Walakini Bwana anaonelea vyema kuwarekebisha watu wake; ndio, anajaribu

subira na imani yao.
22 Walakini — yeyote atakayeweka imani yake kwake, yeye atainuliwa juu siku ya mwisho. Ndio, na hivi ndivyo ilivyokuwa na watu hawa.
23 Kwani tazama, nitakuonyesha kwamba walitiwa utumwani, na hakuna yeyote ambaye angewakomboa ila tu Bwana Mungu wao, ndio, hata Mungu wa Ibrahimu na Isaka na wa Yakobo.
24 Na ikawa kwamba aliwakomboa, na akawaonyesha uwezo wake mkuu, na walifurahi sana.
25 Kwani tazama, ikawa kwamba walipokuwa katika nchi ya Helamu, ndio, katika mji wa Helamu, walipokuwa wakilima ardhi ambayo imeizingira, tazama jeshi la Walamani lilikuwa katika mipaka ya nchi.
26 Sasa ikawa kwamba ndugu za Alma walitoroka kutoka mashamba yao, na kujikusanya pamoja kwenye mji wa Helamu; na walikuwa na woga mwingi kwa sababu ya kuonekana kwa Walamani.
27 Na Alma aliwaendea na kusimama miongoni mwao, na kuwasihi kwamba wasiogope, lakini kwamba wamkumbuke Bwana Mungu wao na atawakomboa.
28 Kwa hivyo wakatuliza woga wao, na kuanza kumlilia Bwana kwamba alainishe mioyo ya Walamani, ili wawahurumie, na wake zao, na watoto wao.
29 Na ikawa kwamba Bwana alilainisha mioyo ya Walamani. Na Alma na ndugu zake wakaenda na kujitoa mikononi mwao; na Walamani wakamiliki nchi ya Helamu.
30 Sasa majeshi ya Walamani, yaliokuwa yamefuata watu wa mfalme Limhi, yalipotea nyikani kwa siku nyingi.
31 Na tazama, waliwapata wale makuhani wa mfalme Nuhu, katika mahali walipoita Amuloni; na walikuwa wameanza kumiliki nchi ya Amuloni na kuanza kulima ardhi.
32 Sasa jina la yule kiongozi wa makuhani lilikuwa Amuloni.
33 Na ikawa kwamba Amuloni aliwasihi Walamani; na pia akawatuma wake zao, ambao walikuwa mabinti za Walamani, kusihi ndugu zao, kwamba wasiwaangamize waume wao.
34 Na Walamani waliwaonea huruma Amuloni na ndugu zake, na hawakuwaangamiza, kwa sababu ya wake zao.
35 Na Amuloni na ndugu zake waliungana na Walamani, na walikuwa wakisafiri nyikani wakitafuta nchi ya Nefi walipoigundua nchi ya Helamu, ambayo ilikuwa imemilikiwa na Alma na ndugu zake.
36 Na ikawa kwamba Walamani wakawaahidi Alma na ndugu zake, kwamba kama wangewaonyesha njia ya kuelekea hadi nchi ya Nefi wangeokoa maisha yao na kuwapatia uhuru wao.
37 Lakini baada ya Alma kuwaonyesha njia iliyoelekea hadi nchi ya Nefi Walamani hawakutimiza ahadi yao; lakini waliwawekea Alma na ndugu zake walinzi, kuizingira nchi ya Helamu.
38 Na waliosalia walienda katika nchi ya Nefi; na wengine wao walirejea katika nchi ya Helamu, na pia kuwaleta wake na watoto wa walinzi walioachwa katika nchi.
39 Na mfalme wa Walamani alikuwa amemruhusu Amuloni kwamba awe mfalme na mtawala wa watu wake, ambao walikuwa katika nchi ya Helamu; walakini hakuwa na uwezo wa kufanya lolote ambalo lilikuwa kinyume cha matakwa ya mfalme wa Walamani.

# Mosia 24

1 Na ikawa kwamba Amuloni alipendelewa na mfalme wa Walamani; kwa hivyo,
mfalme wa Walamani aliwaruhusu yeye na ndugu zake wateuliwe kuwa walimu wa
watu wake, ndio, hata juu ya watu waliokuwa katika nchi ya Shemloni, na katika
nchi ya Shilomu, na katika nchi ya Amuloni.
2 Kwani Walamani walikuwa wamemiliki nchi hizi zote; kwa hivyo, mfalme wa
Walamani alikuwa amewateua wafalme katika nchi hizi.
3 Na sasa jina la mfalme wa Walamani lilikuwa Lamani, akiitwa kwa jina la baba
yake; na kwa hivyo aliitwa mfalme Lamani. Na alikuwa mfalme wa watu wengi.
4 Na aliwateua walimu wa ndugu za Amuloni katika kila nchi iliyomilikiwa na
watu wake; na hivyo lugha ya Nefi ilianza kufunzwa miongoni mwa watu wote wa
Walamani.
5 Na walikuwa watu ambao walipendana wao kwa wao, walakini hawakumjua
Mungu; wala ndugu za Amuloni hawakuwafunza chochote kuhusu Bwana Mungu
wao, wala sheria ya Musa; wala hawakuwafunza maneno ya Abinadi;
6 Lakini waliwafunza kuhifadhi maandishi yao, na kwamba waandikiane wao kwa
wao.
7 Na hivyo Walamani wakaanza kufanikiwa kwa utajiri, na wakaanza kufanya
biashara wao kwa wao na kuwa na nguvu, na wakaanza kuwa wajanja na watu wenye
hekima, kulingana na hekima ya ulimwengu, ndio, watu wenye ujanja mwingi, na
kufurahishwa na kila aina ya uovu na uporaji, ila tu miongoni mwa ndugu zao.
8 Na sasa ikawa kwamba Amuloni alianza kuwanyanyasa Alma na ndugu zake, na
kuanza kumtesa na kuwasababisha watoto wake kuwatesa watoto wao.
9 Kwani Amuloni alikuwa amemjua Alma, kwamba alikuwa mmoja wa makuhani
wa mfalme, na kwamba ni yeye aliyeamini maneno ya Abinadi na kufukuzwa kutoka
mbele ya mfalme, na kwa hivyo alikasirishwa na yeye; kwani alikuwa chini ya
mfalme Lamani, na bado aliwanyanyasa, na kuwafanyisha kazi ngumu, na
kuwawekea manyapara.
10 Na ikawa kwamba mateso yao yalikuwa makuu hata kwamba wakaanza kumlilia
Mungu.
11 Na Amuloni akawaamuru kwamba waache vilio vyao; na aliwawekea walinzi
kuwalinda, kwamba yeyote atakayepatikana akimlingana Mungu auawe.
12 Na Alma na watu wake hawakupaza sauti zao kwa Bwana Mungu wao, lakini
walimfunulia mioyo yao; na alijua mawazo ya mioyo yao.
13 Na ikawa kwamba sauti ya Bwana iliwafikia katika mateso yao, ikisema: Inueni
vichwa vyenu na msherehekee, kwani ninajua agano ambalo mlinifanyia; na
nitaagana na watu wangu na kuwakomboa kutoka utumwani.
14 Na pia nitawapunguzia mizigo ambayo imewekwa mabegani yenu, hata kwamba
hamtaisikia kamwe migongoni mwenu, hata mkiwa utumwani; na nitafanya haya ili
muwe mashahidi wangu hapo baadaye, na kwamba mjue kwa hakika kwamba mimi,
Bwana Mungu, huwatembelea watu wangu katika mateso yao.
15 Na sasa ikawa kwamba mizigo ambayo ilikuwa wamewekewa Alma na ndugu
zake ilipunguzwa; ndio, Bwana aliwapatia nguvu kwamba wabebe mizigo yao kwa
urahisi, na walinyenyekea kwa furaha na subira kwa mapenzi ya Bwana.
16 Na ikawa kwamba imani yao na subira yao ilikuwa kuu sana hata kwamba sauti ya
Bwana ikawajia tena, ikisema: Shangilieni, kwani hapo kesho nitawakomboa kutoka
utumwani.

17 Na akamwambia Alma: Wewe utaenda mbele ya hawa watu, na nitaenda nawe na
kuwakomboa watu hawa kutoka utumwani.
18 Na sasa ikawa kwamba Alma na watu wake walikusanya mifugo yao pamoja
usiku, na pia nafaka yao; ndio, hata usiku wote walikusanya mifugo yao pamoja.
19 Na asubuhi Bwana alisababisha usingizi mzito uwapate Walamani, ndio, na
manyapara wao wote walilala usingizi mzito.
20 Na Alma na watu wake walienda nyikani; na walipokuwa wamesafiri mchana
wote walipiga mahema zao katika bonde, na wakaliita lile bonde Alma, kwa sababu
aliwaongoza njiani wakielekea nyikani.
21 Ndio, na katika bonde la Alma walimpigia Mungu wao shukrani kwa sababu
aliwarehemu, na kupunguza mizigo yao, na kuwakomboa kutoka utumwani, kwani
walikuwa utumwani, na hakuna yeyote ambaye angewakomboa ila tu Bwana Mungu
wao.
22 Na wakamshukuru Mungu, ndio, waume wao wote na wake zao wote na watoto
wao wote ambao waliweza kuzungumza walipaza sauti zao na kumshukuru Mungu
wao.
23 Na sasa Bwana akamwambia Alma: Jiharakishe wewe na utoe watu hawa kutoka
nchi hii, kwani Walamani wameamka na wanakufuata; kwa hivyo jiondoe kutoka
nchi hii, na nitawazuia Walamani katika bonde hili ili wasiwafuate watu hawa.
24 Na ikawa kwamba waliondoka bondeni, na kuelekea nyikani.
25 Na baada ya kuwa nyikani kwa siku kumi na mbili walifika katika nchi ya
Zarahemla; na mfalme Mosia aliwapokea kwa shangwe.

## Mosia 25

1 Na sasa mfalme Mosia alisababisha kwamba watu wote wakusanyike pamoja.
2 Sasa hakukuwa na watoto wa Nefi wengi, au wale wengi waliokuwa uzao wa Nefi,
kama vile wale watu wa Zarahemla, ambaye alikuwa ni wa uzao wa Muleki, na wale
ambao walikuja na yeye nyikani.
3 Na watu wa Nefi na watu wa Zarahemla hawakuwa wengi kama Walamani; ndio,
hata hawakuwa nusu yao.
4 Na sasa watu wote wa Nefi walikuwa wamekusanyika pamoja, na pia watu wote
wa Zarahemla, na walikuwa wamekusanyika pamoja kwa vikundi viwili.
5 Na ikawa kwamba Mosia alisoma, na akasababisha kusomwa, kwa maandishi ya
Zenivu kwa watu wake; ndio, alisoma maandishi ya watu wa Zenivu, tangu ule
wakati walipoondoka kutoka nchi ya Zarahemla hadi ule wakati waliporejea tena.
6 Na pia alisoma historia ya Alma na ndugu zake, na mateso yao yote, tangu
waondoke nchi ya Zarahemla hadi ule wakati ambao walirejea tena.
7 Na sasa, Mosia alipomaliza kusoma yale maandishi, watu wake ambao walikuwa
wamebaki katika nchi ile walijazwa na mshangao na kustaajabu.
8 Kwani hawakujua la kufikiria; kwani walipotazama wale ambao walikuwa
wamekombolewa kutoka utumwani walikuwa wamejazwa na shangwe kuu zaidi.
9 Na tena, walipofikiri kuhusu vile ndugu zao walivyouawa na Walamani walijazwa
na huzuni, na hata kumwaga machozi mengi ya huzuni.
10 Na tena, walipofikiri kuhusu wema wa Mungu ulio kamili, na uwezo wake katika
kuwakomboa Alma na ndugu zake kutoka mikono ya Walamani na utumwa,
walipaza sauti zao na kumshukuru Mungu.

11 Na tena, walipofikiri juu ya Walamani, ambao walikuwa ni ndugu zao, jinsi
walivyokuwa katika hali ya dhambi na iliyochafuka, walijazwa na uchungu na
maumivu kwa sababu ya ustawi wa nafsi zao.
12 Na ikawa kwamba wale ambao walikuwa watoto wa Amuloni na ndugu zake,
ambao walikuwa wamewachukua mabinti za Walamani kuwa wake wao,
hawakufurahishwa na tabia za babu zao, na hawakutaka waitwe tena kwa majina ya
babu zao, kwa hivyo walijichukulia jina la Nefi, ili waitwe watoto wa Nefi na
kuhesabiwa miongoni mwa wale walioitwa Wanefi.
13 Na sasa watu wote wa Zarahemla walihesabiwa pamoja na Wanefi, na hii ni kwa
sababu ufalme haukukabidhiwa yeyote ila tu wale waliokuwa wa uzao wa Nefi.
14 Na sasa ikawa kwamba Mosia alipomaliza kuzungumza na kusomea watu, alitaka
Alma pia azungumzie watu.
15 Na Alma aliwazungumzia, walipokusanyika pamoja kwa vikundi vikubwa, na
alienda kutoka kwa kikundi kimoja hadi kingine, akiwahubiria watu toba na imani
katika Bwana.
16 Na akawasihi watu wa Limhi na ndugu zake, wale wote ambao walikuwa
wamekombolewa kutoka utumwani, kwamba wakumbuke kuwa ni Bwana ambaye
alikuwa amewakomboa.
17 Na ikawa kwamba baada ya Alma kuwafunza watu vitu vingi, na kumaliza
kuwazungumzia, kwamba mfalme Limhi alitaka abatizwe; na watu wake wote pia
walitaka kubatizwa.
18 Kwa hivyo, Alma aliingia katika maji na kuwabatiza; ndio, aliwabatiza jinsi
alivyobatiza ndugu zake katika yale maji ya Mormoni; ndio, na wale wote aliobatiza
waliingia katika kanisa la Mungu; na hii ilikuwa ni kwa sababu yao kuamini maneno
ya Alma.
19 Na ikawa kwamba mfalme Mosia alimruhusu Alma kuanzisha makanisa kote
katika nchi ya Zarahemla; na akampa uwezo wa kuwatawaza makuhani na walimu
katika kila kanisa.
20 Sasa haya yalitendeka kwa sababu kulikuwa na watu wengi hata kwamba
hawangetawaliwa na mwalimu mmoja; wala hawangesikia neno la Mungu wakiwa
katika kikundi kimoja;
21 Kwa hivyo walikusanyika pamoja katika vikundi tofauti, na kuitwa makanisa;
kila kanisa likiwa na makuhani wake na walimu wake, na kila kuhani akihubiri neno
kulingana na vile lilivyotolewa kwa kinywa cha Alma.
22 Na hivyo, licha ya kuwa na makanisa mengi, yote yalikuwa kanisa moja, ndio,
hata kanisa la Mungu; kwani hakuna lingine lolote lililohubiriwa makanisani ila tu
toba na imani katika Mungu.
23 Na sasa kulikuwa na makanisa saba katika nchi ya Zarahemla. Na ikawa kwamba
wowote waliotaka kulichukua jina la Kristo, au la Mungu, walijiunga na makanisa ya
Mungu;
24 Na waliitwa watu wa Mungu. Na Bwana aliwateremshia Roho wake juu yao, na
wakabarikiwa, na kufanikiwa katika nchi.

## Mosia 26

1 Sasa ikawa kwamba kulikuwa na wengi wa uzazi mchanga ambao hawakufahamu
maneno ya mfalme Benyamini, kwani walikuwa watoto wadogo alipowazungumzia

watu wake; na hawakuamini mila za babu zao.
2 Hawakuamini yale ambayo yalikuwa yamezungumzwa kuhusu ufufuo wa wafu, wala hawakuamini kuhusu kuja kwa Kristo.
3 Na sasa kwa sababu ya kutoamini kwao hawakufahamu neno la Mungu; na mioyo yao ilikuwa imeshupazwa.
4 Na hawakubatizwa; wala hawakujiunga na kanisa. Na walikuwa watu tofauti kulingana na imani yao, na waliishi hivyo daima, katika hali yao ya kimwili na yenye dhambi; kwani hawakumkimbilia Bwana Mungu wao.
5 Na sasa katika utawala wa Mosia hawakuwa wengi kiasi nusu kama watu wa Mungu; lakini kwa sababu ya mafarakano miongoni mwa ndugu waliongezeka.
6 Kwani ikawa kwamba waliwadaganya wengi kwa maneno yao ya mzaha, ambao walikuwa kanisani, na kuwasababisha kutenda dhambi nyingi; kwa hivyo ilibidi wale ambao walikuwa kanisani, na kutenda dhambi, waonywe na kanisa.
7 Na ikawa kwamba waliletwa mbele ya makuhani, na kukabidhiwa kwa makuhani na walimu; na makuhani wakawaleta mbele ya Alma, ambaye alikuwa ni kuhani mkuu.
8 Sasa mfalme Mosia alikuwa amempatia Alma mamlaka juu ya kanisa.
9 Na ikawa kwamba Alma hakujua mengi juu yao; lakini kulikuwa na mashahidi wengi kinyume chao; ndio, watu walisimama na kushuhudia sana kuhusu uovu wao.
10 Sasa kulikuwa kitu kama hicho hakijawahi kutendeka kanisani; kwa hivyo Alma alisononeka rohoni mwake, na akasababisha kwamba waletwe mbele ya mfalme.
11 Na akamwaambia mfalme: Tazama, hapa kuna wengi ambao tumewaleta mbele yako, na ambao wameshtakiwa na ndugu zao; ndio, na wamepatikana katika maovu mengi. Na hawatubu maovu yao; kwa hivyo tumewaleta mbele yako, ili uwahukumu kulingana na hatia zao.
12 Lakini mfalme Mosia alimwambia Alma: Tazama, mimi sitawahukumu; kwa hivyo nawakabidhi mikononi mwako ili wahukumiwe.
13 Na sasa roho ya Alma ilisononeka tena; na akaenda na kumwuliza Bwana yale atakayotenda kuhusu jambo hili, kwani aliogopa kwamba atafanya vibaya mbele ya Mungu.
14 Na ikawa kwamba baada ya kumfunulia Mungu roho yake, sauti ya Bwana ilimjia, na kusema:
15 Heri wewe, Alma, na heri wale ambao walibatizwa katika maji ya Mormoni. Wewe umebarikiwa kwa sababu ya imani yako kuu katika maneno pekee ya mtumishi wangu Abinadi.
16 Na wamebarikiwa wao kwa sababu ya imani yao kuu katika yale maneno ambayo umewazungumzia.
17 Na wewe umebarikiwa kwa sababu umeanzisha kanisa miongoni mwa watu hawa; na wataimarishwa, na watakuwa watu wangu.
18 Ndio, heri watu hawa kwa sababu wako tayari kulichukua jina langu; kwani wataitwa kwa jina langu; na watakuwa wangu.
19 Na kwa sababu wewe umeniuliza kuhusu mwenye dhambi, wewe umebarikiwa.
20 Wewe ni mtumishi wangu; na ninaagana na wewe kwamba utapokea uzima wa milele; na utanitumikia na kuendelea mbele kwa jina langu, na utakusanya pamoja kondoo wangu.
21 Na yule atakayesikia sauti yangu atakuwa kondoo wangu; na yeye utampokea kanisani, na pia mimi nitampokea.

22 Kwani tazama, hili ni kanisa langu; yeyote atakayebatizwa atabatizwa ubatizo wa toba. Na yeyote utakayempokea ataliamini jina langu; na yeye nitamsamehe bila sharti.

23 Kwani ni mimi ambaye najichukulia dhambi za ulimwengu juu yangu; kwani ni mimi ambaye niliwaumba; na ni mimi ambaye nampatia yule anayeamini hadi mwisho mahali kwa mkono wangu wa kuume.

24 Kwani tazama, kwa jina langu wanaitwa; na ikiwa wananijua watakuja mbele, na watapata mahali pa milele kwa mkono wangu wa kuume.

25 Na itakuwa kwamba tarumbeta ya pili itakapopigwa, basi wale ambao hawajawahi kunijua watakuja mbele na kusimama mbele yangu.

26 Na ndipo watajua kwamba mimi ni Bwana Mungu wao, na kwamba mimi ni Mkombozi wao; lakini hawakutaka kukombolewa.

27 Na kisha nitakiri kwao kwamba sikuwajua; na wataelekea kwenye moto usio na mwisho ambao umetayarishiwa ibilisi na malaika wake.

28 Kwa hivyo nakwaambia, kwamba yule ambaye hatasikia sauti yangu, huyo hutampokea katika kanisa langu, kwani yeye sitampokea katika siku ya mwisho.

29 Kwa hivyo nakuambia, Nenda; na yeyote ambaye ananikosea, huyo utamhukumu kulingana na dhambi ambazo ametenda; na kama ataungama dhambi zake mbele yako na mimi, na atubu kwa moyo wake kwa kweli, utamsamehe, na pia nitamsamehe.

30 Ndio, na kila mara watu wangu watatubu, nitawasamehe makosa yao dhidi yangu.

31 Na pia nyinyi mtasameheana makosa yenu; kwa kweli nawaambia, yule ambaye hatamsamehe jirani yake makosa anaposema kuwa ametubu, huyu amejiweka chini ya hukumu.

32 Sasa nakwambia, Nenda; na yeyote asiyetubu dhambi zake, huyo hatahesabiwa miongoni mwa watu wangu; na hii itafuatwa kutoka wakati huu na daima.

33 Na ikawa kwamba wakati Alma alipokuwa amesikia maneno haya aliyaandika chini ili awe nayo, na kwamba aweze kuwahukumu watu wa kanisa lile kulingana na amri za Mungu.

34 Na ikawa kwamba Alma alienda na kuwahukumu wale ambao walikuwa wamepatikana na maovu, kulingana na neno la Bwana.

35 Na yeyote ambaye alitubu dhambi zake na kuungama, aliwahesabu wao miongoni mwa watu wa kanisa;

36 Na wale ambao hawakutubu dhambi zao na maovu yao, wao hawakuhesabiwa miongoni mwa watu wa kanisa, na majina yao yalifutwa.

37 Na ikawa kwamba Alma aliongoza mambo yote ya kanisa; na wakaanza tena kupata amani na kufanikiwa sana katika mambo ya kanisa, wakitembea kwa uangalifu mbele ya Mungu, wakipokea wengi, na kubatiza wengi.

38 Na sasa hivi vitu vyote ndivyo vile ambavyo Alma na watumishi wenzake waliokuwa juu ya kanisa walifanya, wakitembea kwa uangalifu, wakifunza neno la Mungu katika vitu vyote, wakiteseka kila aina ya mateso, na kuteswa na wale wote ambao hawakuwa wa kanisa la Mungu.

39 Na waliwaonya ndugu zao; na pia nao walionywa, kila mmoja wao kwa neno la Mungu, kulingana na dhambi zake, au dhambi ambazo alikuwa ametenda, na kuamriwa na Mungu wasali bila kukoma, na kushukuru kwa vitu vyote.

# Mosia 27

1 Na sasa ikawa kwamba yale mateso ambayo yaliwekelewa kanisa na wasioamini
yalikuwa makuu hata kwamba kanisa likaanza kunung'unika, na kulalamikia
viongozi wao kuhusu hilo jambo; na walimlalamikia Alma. Na Alma akamwelezea
mfalme wao, Mosia, hii kesi. Na Mosia alishauriana na makuhani wake.
2 Na ikawa kwamba mfalme Mosia alituma tangazo kote nchini kwamba wale
wasioamini wasiwatese wale ambao walikuwa wa kanisa la Mungu.
3 Na kulikuwa na amri kali katika makanisa yote kwamba kusiwe na mateso
miongoni mwao, na kwamba kuwe na usawa miongoni mwa watu wote;
4 Kwamba wasikubali kiburi au maringo kuharibu amani yao; kwamba kila mtu
amheshimu jirani yake jinsi anavyojiheshimu, na kufanya kazi kwa mikono yao
wenyewe ili waishi.
5 Ndio, na makuhani wao wote na walimu wao wote iliwabidi kufanya kazi kwa
mikono yao ili waweze kuishi, katika kila hali isipokuwa wanapougua, au wakiwa na
taabu nyingi; na kwa kufanya vitu hivi, walipokea neema ya Mungu.
6 Na kukawa na amani kubwa tena katika nchi; na watu wakaanza kuongezeka
sana, na wakaanza kutawanyika huku na kule usoni mwa dunia, ndio, kaskazini na
kusini, mashariki na magharibi, wakijenga miji mikubwa na vijiji katika sehemu zote
za nchi.
7 Na Bwana aliwatembelea na kuwafanikisha, na wakawa watu wengi na matajiri.
8 Sasa wana wa Mosia walihesabiwa miongoni mwa wale makafiri; na pia mwana
mmoja wa Alma alihesabiwa miongoni mwao, yeye akiitwa Alma, kama baba yake;
walakini, akawa mtu mwovu na mwenye kuabudu sanamu. Na alikuwa mtu wa
maneno mengi, na aliwaelezea watu maneno mengi ya mzaha; kwa hivyo
aliwaongoza watu wengi watende maovu kama yake.
9 Na akawa pingamizi kuu kwa mafanikio ya kanisa la Mungu; akiiba mioyo ya
watu; akisababisha mafarakano miongoni mwa watu; na kumpatia adui wa Mungu
nafasi ya kuwatawala kwa uwezo wake.
10 Na ikawa kwamba alipokuwa akienda hivyo ili aangamize kanisa la Mungu,
kwani alienda hivyo kwa kisiri na wana wa Mosia ili waangamize kanisa, na
kuwapotosha watu wa Bwana, kinyume cha amri za Mungu, au hata mfalme—
11 Na kama vile nilivyowaelezea, jinsi vile walivyomuasi Mungu, tazama, malaika
wa Bwana aliowatokea; na alishuka kama kwa wingu; na alizungumza kwa sauti
kama radi, iliyosababisha ardhi kutetemeka pale waliposimama;
12 Na walikuwa na mshangao mkuu, hata kwamba wakainama kwenye ardhi, na
hawakufahamu maneno yale ambayo aliwazungumzia.
13 Walakini alipaza sauti tena, akisema: Alma, inuka na usimame, kwa nini wewe
unalitesa kanisa la Mungu? Kwani Bwana amesema: Hili ni kanisa langu, na
nitalijenga; na hakuna lolote litakalolipinga, ila tu watu wangu watende dhambi.
14 Na tena, malaika akasema: Tazama, Bwana amesikia sala za watu wake, na pia
sala za mtumishi wake, Alma, ambaye ni baba yako; kwani ameomba kwa imani
kubwa kukuhusu ili upate kuelimika kwa ukweli; kwa hivyo, ni kwa sababu hii
nimekuja kukusadikisha kuhusu uwezo na mamlaka ya Mungu, kwamba sala za
watumishi wake zijibiwe kulingana na imani yao.
15 Na sasa tazameni, je unaweza kupinga nguvu za Mungu? Kwani tazama, si sauti
yangu inatingisha ardhi? Na pia hunioni mbele yako? Na nimetumwa kutoka kwa
Mungu.

16 Sasa nakwambia: Nenda, na ukumbuke utumwa wa babu zako katika nchi ya
Helamu, na katika nchi ya Nefi; na kumbuka vile vitu vikuu ambavyo amewatendea;
kwani walikuwa utumwani, na amewakomboa. Na sasa nakuambia wewe, Alma,
enda njia yako, na usijaribu kuangamiza kanisa tena, ili sala zao zijibiwe, na hivi hata
kama wewe mwenyewe utataka kutupiliwa mbali.
17 Na sasa ikawa kwamba haya ndiyo yalikuwa maneno ya mwisho ambayo malaika
alimwambia Alma, na akaondoka.
18 Na sasa Alma na wale wengine aliokuwa nao waliinama tena kwenye ardhi kwani
mshangao wao ulikuwa mkuu; kwani kwa macho yao walikuwa wameona malaika
wa Bwana; na sauti yake ilikuwa kama radi, ambayo ilitingisha ulimwengu; na
walijua kwamba hakuna kingine chochote ila tu nguvu za Mungu ambazo
zingetingisha ulimwengu mpaka ionekane kama itapasuka.
19 Na sasa mshangao wa Alma ulikuwa mkubwa sana kwamba akawa bubu, asiweze
kufungua kinywa chake; ndio, na akawa mnyonge, hata kwamba hakuweza
kunyosha mikono yake; kwa hivyo alibebwa na wale ambao walikuwa na yeye, akiwa
hajiwezi, hata mpaka walipomweka mbele ya baba yake.
20 Na wakamwambia baba yake yote ambayo yaliwatokea; na baba yake alifurahi,
kwani alijua kwamba ulikuwa ni uwezo wa Mungu.
21 Na akasababisha kwamba umati ukusanywe pamoja ili ushuhudie yale ambayo
Bwana alikuwa amemtendea mwana wake, na pia kwa wale ambao walikuwa na yeye.
22 Na akasababisha kwamba makuhani wakusanyike pamoja; na wakaanza kufunga,
na kumwomba Bwana Mungu wao kwamba afungue kinywa cha Alma, ili
azungumze, na pia kwamba viungo vyake vipokee nguvu — kwamba macho ya watu
yafunuliwe ili waone na watambue wema na utukufu wa Mungu.
23 Na ikawa kwamba baada ya wao kufunga na kuomba kwa muda wa siku mbili
kuchwa, kucha, viungo vya Alma vilipokea nguvu, na akasimama na akaanza
kuwazungumzia, na kuwaalika kwamba wawe na faraja:
24 Kwani, alisema, nimetubu dhambi zangu, na kukombolewa na Bwana; tazama
nimezaliwa kwa Roho.
25 Na Bwana akaniambia: Usishangae kwamba wanadamu wote, ndio, wanaume na
wanawake, mataifa yote, lugha, kabila, na watu, lazima wazaliwe mara ya pili; ndio,
wazaliwe na Mungu, wabadilishwe kutoka hali yao ya kimwili na ya kuanguka, kwa
hali ya utakatifu, na kukombolewa na Mungu, na kuwa wana na mabinti zake;
26 Na hivyo wanakuwa viumbe vipya; na wasipofanya hivi, hawawezi kwa vyovyote
kurithi ufalme wa Mungu.
27 Nawaambia, isipokuwa hivi, lazima watengwe; na hii najua, kwa sababu karibu
mimi nitengwe.
28 Walakini, baada ya kupitia mateso mengi, na kukaribia kifo kwa kutubu, Bwana
kwa rehema zake ameonelea kwamba ni vyema kuninyakua ili nisiungue milele, na
nimezaliwa na Mungu.
29 Nafsi yangu imekombolewa kutoka nyongo ya uchungu na vifungo vya uovu.
Nilikuwa katika shimo la giza nyingi; lakini sasa naona mwangaza wa ajabu wa
Mungu. Nafsi yangu ilisononeshwa na uchungu usio na mwisho; lakini
nimenyakuliwa, na nafsi yangu haina maumivu tena.
30 Nilimkataa Mkombozi wangu, na kuyakana yale ambayo yalizungumzwa na
babu zetu; lakini sasa ili waone kuwa atakuja, na kwamba yeye hukumbuka kila
kiumbe ambacho ameumba, atajidhihirisha kwa wote.

31 Ndio, kila goti litainama, na kila ulimi utakiri mbele yake. Ndio, hata katika siku
ya mwisho, ambapo wanadamu wote watasimama kuhukumiwa na yeye, kisha
watakiri kwamba yeye ni Mungu; na kisha watakiri, wale ambao wanaishi
ulimwenguni bila Mungu, kwamba hukumu ya adhibio isiyo na mwisho ambayo iko
juu yao ni ya haki; na watatetemeka, na kutikisika, na kuogopa mbele ya tazamo la
jicho lake ambalo huona kote.
32 Na sasa ikawa kwamba Alma alianza kutoka wakati huu na kwenda mbele
kufunza watu, na wale ambao walikuwa na Alma wakati ambao malaika aliwatokea,
wakisafiri kote nchini, wakiwatangazia watu wote vitu vile ambavyo walikuwa
wameona na kusikia, na kuhubiri neno la Mungu kwa mateso mengi, wakiteswa sana
na wale wasioamini, na wakipigwa na wengi wao.
33 Licha ya haya yote, walilifariji kanisa sana, na kuthibitisha imani yao, na
kuwaonya kwa subira kuu na uchungu wazitii amri za Mungu.
34 Na wanne wao walikuwa ni wana wa Mosia; na majina yao yalikuwa ni Amoni,
na Haruni, na Omneri, na Himni; haya ndiyo yalikuwa majina ya wana wa Mosia.
35 Na walisafiri katika nchi yote ya Zarahemla, na miongoni mwa watu wote ambao
walitawaliwa na mfalme Mosia, wakijibidiisha kuponya majeraha yote ambayo
walikuwa wamelifanyia kanisa, wakitubu dhambi zao zote, na kutangaza vitu vyote
ambavyo walikuwa wameona, na wakieleza unabii na maandiko kwa wote ambao
walitaka kuyasikia.
36 Na hivyo walikuwa vyombo mikononi mwa Mungu kwa kuwezesha wengi
kufahamu ukweli, ndio, kwa ufahamu wa Mkombozi wao.
37 Na jinsi gani walivyobarikiwa! Kwani walitangaza amani; walitangaza habari
njema ya mambo mema; na waliwatangazia watu kwamba Bwana anatawala.

# Mosia 28

1 Sasa ikawa kwamba baada ya wana wa Mosia kufanya vitu hivi vyote, walichukua
kikundi kidogo na kurejea kwa baba yao, mfalme, na wakataka waruhusiwe, wao
pamoja na wale ambao walikuwa wamewateua, kwamba waende hadi katika nchi ya
Nefi ili wahubiri vitu vile ambavyo walikuwa wamesikia, na ili wawapatie ndugu zao,
Walamani, neno la Mungu—
2 Ili pengine wawafahamishe kuhusu Bwana Mungu wao, na kuwasadikisha
kuhusu maovu ya baba zao; na ili pengine waponye chuki yao kwa Wanefi, ili pia
wawezeshwe kumsherehekea Bwana Mungu wao, ili wawe marafiki wao kwa wao,
kwamba kusiwe na mabishano katika nchi yote ambayo Bwana Mungu wao alikuwa
amewapatia.
3 Sasa walitamani kwamba wokovu utangaziwe kila kiumbe, kwani
hawangevumilia kwamba nafsi ya mwanadamu yeyote iangamie; ndio, hata mafikira
kwamba kuna nafsi yoyote itakayopata kuteswa kwa milele iliwafanya kutetemeka
na kutikisika.
4 Na hivyo ndivyo Roho wa Bwana alivyowatendea, kwani wao ndio waliokuwa
wenye dhambi mbovu zaidi. Na Bwana katika rehema yake alionelea kwamba inafaa
awaachilie; walakini waliteseka sana katika nafsi zao kwa sababu ya maovu yao,
wakiteseka sana na kuogopa kwamba watatengwa milele.
5 Na ikawa kwamba walimsihi baba yao kwa siku nyingi ili waende katika nchi ya
Nefi.

6 Na mfalme Mosia akaenda kumwuliza Bwana ili ajue kama atawaruhusu wana
wake waende kuhubiria neno miongoni mwa Walamani.
7 Na Bwana akamwaambia Mosia: Waruhusu waende, kwani wengi wataamini
maneno yao, na watapokea uzima wa milele; na nitawakomboa wana wako kutoka
mikono ya Walamani.
8 Na ikawa kwamba Mosia aliwaruhusu waende na kutenda kulingana na haja yao.
9 Na wakasafiri nyikani ili wahubiri neno miongoni mwa Walamani; na nitatoa
historia ya matendo yao hapo baadaye.
10 Sasa mfalme Mosia hakuwa na yeyote wa kumkabidhi ufalme wake, kwani
hakukuwa na yeyote miongoni mwa wana wake aliyekubali ufalme.
11 Kwa hivyo alichukua maandishi ambayo yalikuwa yamechorwa katika bamba za
shaba, na pia bamba za Nefi, na vitu vyote alivyokuwa ameweka na kuhifadhi
kulingana na amri za Mungu, baada ya kutafsiri na kuandikisha maandishi
yaliyokuwa katika bamba za dhahabu ambazo zilikuwa zimepatwa na watu wa
Limhi, na ambazo alipewa kwa mkono wa Limhi;
12 Na alifanya hivi kwa sababu ya wasiwasi mkuu wa watu wake; kwani walitamani
sana kujua kuhusu wale watu ambao walikuwa wameangamizwa.
13 Na sasa alizitafsiri kwa kuyatumia yale mawe mawili ambayo yalikuwa
yamefungiliwa katika ile mizingo miwili ya pinde.
14 Sasa vitu hivi vilikuwa vimetayarishwa tangu mwanzo, na vilipitishwa kutoka
kizazi hadi kizazi, kwa lengo la kutafsiri lugha;
15 Na vimewekwa na kuhifadhiwa kwa mkono wa Bwana, ili afichulie kila kiumbe
ambacho kitamiliki nchi maovu na machukizo ya watu wake;
16 Na yeyote aliye na vitu hivi anaitwa mwonaji, kama zile nyakati za kale.
17 Sasa baada ya Mosia kumaliza kutafsiri maandishi haya, tazama, yalieleza historia
ya watu ambao waliangamizwa, kutoka ule wakati walioangamizwa hadi ule wakati
ule mnara mkuu uliojengwa, ule wakati ambao Bwana alichanganya lugha ya watu
na wakatawanywa kote usoni mwa ulimwengu, ndio, na hata kutoka wakati huo
kurudi nyuma hadi uumbaji wa Adamu.
18 Sasa historia hii iliwafanya watu wa Mosia kuomboleza sana, ndio, walijazwa na
hofu; walakini iliwapa ufahamu mwingi, ambao uliwafurahisha.
19 Na historia hii itaandikwa hapo baadaye; kwani tazama, ni muhimu watu wote
kujua vitu ambavyo vimeandikwa katika historia hii.
20 Na sasa, kama vile nilivyowaambia, kwamba baada ya mfalme Mosia kutenda
vitu hivi, alichukua zile bamba za shaba, na vitu vyote ambavyo alikuwa ameweka,
na kumkabidhi Alma, ambaye alikuwa ni mwana wa Alma; ndio, maandishi yote, na
pia vitafsiri, na kumpatia yeye, na akamwamuru kwamba aviweke na avihifadhi, na
pia aweke maandishi ya wale watu, na kuvipitisha kutoka kizazi hadi kizazi, hata
kama vile vilikuwa vimepitishwa tangu ule wakati Lehi alipoondoka Yerusalemu.

## Mosia 29

1 Sasa baada ya Mosia kufanya hivi alituma kote nchini, miongoni mwa watu wote,
akitaka kujua walitaka nani awe mfalme wao.
2 Na ikawa kwamba sauti ya watu ilikuja, ikisema: Tunataka mwana wako Haruni
awe mfalme wetu na mtawala wetu.
3 Sasa Haruni alikuwa ameenda katika nchi ya Nefi, kwa hivyo mfalme

hangempatia ufalme; wala Haruni hakukubali ufalme; wala hakuna yeyote
miongoni mwa wana wa Mosia aliyetaka kuchukua ufalme.
4 Kwa hivyo mfalme Mosia alituma tena miongoni mwa watu; ndio, alituma
miongoni mwa watu kwa maandishi. Na haya ndiyo maneno yalioandikwa,
yakisema:
5 Tazameni, Ee nyinyi watu wangu, au ndugu zangu, kwani nawaheshimu hivyo,
nataka mfikirie jambo ambalo mnatakiwa kufikiria—kwani mnatamani kupata
mfalme.
6 Sasa nawatangazia kwamba yule anayestahili kupokea ufalme amekataa, na
hatauchukua ufalme.
7 Na sasa kama kuna mwingine atakayeteuliwa badala yake, tazama naogopa
kwamba kutazuka mabishano miongoni mwenu. Na ni nani ajuaye kama mwana
wangu, ambaye ufalme ni wake, atakasirika na kuchukua sehemu ya watu hawa,
ambayo itasababisha vita na mabishano miongoni mwenu, ambayo itasababisha
umwagaji wa damu nyingi na kuchafua njia za Bwana, ndio, na kuangamiza nafsi za
watu wengi.
8 Sasa nawaambia, hebu tuwe na hekima na tuwaze vitu hivi, kwani hatuna haki ya
kumwangamiza mwana wangu, wala hatuna haki ya kumwangamiza mwingine
kama atachaguliwa badala yake.
9 Na kama mwana wangu atarudia kiburi chake atakumbuka vitu vile alivyokuwa
amesema, na adai haki yake katika ufalme, ambayo itamsababisha yeye na pia watu
hawa kutenda dhambi.
10 Na sasa hebu tuwe na hekima na tutazamie vitu hivi, na tufanye lile ambalo
litawaletea watu hawa amani.
11 Kwa hivyo nitakuwa mfalme wenu katika siku zangu ambazo zimesalia; walakini,
hebu tuchague waamuzi, ili wahukumu watu hawa kulingana na sheria yetu; na
tutapanga upya mambo ya watu hawa, kwani tutachagua watu wenye hekima kuwa
waamuzi, ambao watahukumu watu hawa kulingana na amri za Mungu.
12 Sasa ni afadhali mwanadamu ahukumiwe na Mungu badala ya mwanadamu,
kwani hukumu za Mungu ni za haki daima, lakini hukumu za mwanadamu sio za
haki daima.
13 Kwa hivyo, kama ingewezekana muwe na watu wenye haki wawe wafalme wenu,
ambao wangeimarisha sheria za Mungu, na kuhukumu hawa watu kulingana na amri
zake, ndio, kama mngekuwa na watu wawe wafalme wenu ambao wangetenda kama
baba yangu Benyamini alivyowatendea watu hawa—Nawaambia, kama ingekuwa
hivi daima basi ingekuwa inafaa daima muwe na wafalme wa kuwatawala.
14 Na hata mimi mwenyewe nimetumika kwa nguvu zote na uwezo ambao ninao,
kuwafunza amri za Mungu, na kuimarisha amani kote nchini, kwamba kusiwe na
vita wala mabishano, wala kuiba, wala uporaji, wala uuaji, wala uovu wa aina yoyote;
15 Na yeyote ambaye ametenda maovu, nimemuadhibu kulingana na hatia ile
ambayo ametenda, kulingana na sheria ambayo tumepewa na baba zetu.
16 Sasa nawaambia, kwamba kwa sababu sio wanadamu wote walio wenye haki,
haifai muwe na mfalme au wafalme kuwatawala.
17 Kwani tazama, jinsi vile mfalme mmoja mwovu anavyosababisha uovu mkuu
kutendwa, ndio, na ni mashaka makuu!
18 Ndio, kumbuka mfalme Nuhu, uovu wake na machukizo yake, na pia uovu na
machukizo ya watu wake. Tazama jinsi yale maangamizo makuu yalivyowapata; na

pia kwa sababu ya maovu yao waliwekwa utumwani.

19 Na kama sio kwa sababu ya kuingilia kwa Muumba wao mwenye hekima, na haya kwa sababu ya kutubu kwao kwa kweli, wangekuwa lazima wanaishi utumwani hadi sasa.

20 Lakini tazama, aliwakomboa kwa sababu walijinyenyekea mbele yake; na kwa sababu walimlilia sana aliwakomboa kutoka utumwani; na hivi ndivyo Bwana anavyotenda katika hali zote kwa uwezo wake miongoni mwa watoto wa watu, na kuunyosha mkono wake wa rehema kwa wale wote ambao wanamwamini.

21 Na tazama, sasa nawaambia nyinyi, hamuwezi kumpindua mfalme mwovu ila tu kwa ubishi mwingi, na umwagaji wa damu nyingi.

22 Kwani tazama, ana marafiki wake katika uovu, na anajizingira na walinzi; na anavunja sheria za wale ambao walitawala kwa haki kabla yake; na huzikanyaga chini ya miguu yake amri za Mungu.

23 Na hutoa sheria mpya, na kuzituma miongoni mwa watu wake, ndio, sheria ambazo zinafuata uovu wake; na yeyote ambaye hatii amri zake anasababisha aangamizwe; na yeyote ambaye anamuasi anatumia majeshi yake kumpiga, na kama anaweza, atawaangamiza; na hivyo ndivyo mfalme mwovu huchafua njia za haki.

24 Na sasa tazama nawaambia, haifai kwamba machukizo kama haya yawapate.

25 Kwa hivyo, chagueni kwa sauti ya watu hawa, waamuzi, kwamba mhukumiwe kulingana na sheria ambazo mlipewa na baba zetu, ambazo ni za kweli, na ambazo zilitolewa kwao na mkono wa Bwana.

26 Sasa sio kawaida kwamba sauti ya watu itake lile ambalo ni kinyume cha lile lililo la haki; lakini ni kawaida kwa sehemu ndogo ya watu kutaka lile lisilo la haki; kwa hivyo mtafuata hii na kuifanya iwe sheria yenu — kufanya shughuli zenu kulingana na sauti ya watu.

27 Na kama utafika wakati ambao sauti ya watu itachagua maovu, basi huo ndio wakati ambao hukumu za Mungu zitawashukia; ndio, kisha atawatembelea kwa maangamizo makuu kama vile ameshatembelea nchi hii.

28 Na sasa kama mtakuwa na waamuzi, na hawawahukumu kulingana na sheria ambayo imetolewa, mnaweza kufanya wahukumiwe na waamuzi mkuu.

29 Kama waamuzi wenu wakuu hawahukumu kwa haki, mtawakusanya waamuzi wenu wadogo kwa kikundi, na watawahukumu waamuzi wenu wakuu, kulingana na sauti ya watu.

30 Na ninawaamuru kutenda vitu hivi kwa kumuogopa Bwana; na ninawaamuru mtende vitu hivi, na kwamba msiwe na mfalme; ili kama watu hawa wakitenda dhambi na maovu, yatakuwa juu ya vichwa vyao wenyewe.

31 Kwani tazama nawaambia, dhambi za watu wengi zimesababishwa na maovu ya wafalme wao; kwa hivyo maovu yao yanadaiwa juu ya vichwa vya wafalme wao.

32 Na sasa sitaki ubaguzi huu uwe tena katika nchi hii, hasa miongoni mwa watu hawa wangu; lakini nahitaji kwamba nchi hii iwe nchi ya uhuru, na kila mtu afurahie haki zake na heshima zake kwa usawa, kadiri vile Bwana atakavyoonelea ni vyema tuishi na kurithi nchi hii, ndio, hata kadiri vile uzao wetu utaishi katika nchi hii.

33 Na vitu vingi vingine mfalme Mosia aliwaandikia, na kuwafungulia majaribio na shida zote za mfalme mtakatifu, ndio, mateso yote ya nafsi kwa niaba ya watu wao, na pia malalamiko ya watu kwa mfalme wao; na akawaelezea yote.

34 Na akawaambia kwamba lazima mambo haya hayatakiwi kuweko; lakini kwamba uzito lazima uwe kwa watu wote, na kwamba kila mtu abebe sehemu yake.

35 Na pia akawaelezea kuhusu shida ambazo watakuwa nazo, wakitumikia chini ya
utawala wa mfalme mwovu;
36 Ndio, uovu wake wote na machukizo, na vita vyote, na mabishano, na umwagaji
wa damu, na wizi, na uporaji, na kutenda usherati, na kila aina ya maovu ambayo
hayawezi kuhesabika—akiwaambia kwamba lazima vitu hivi havitakiwi kuwepo, na
kwamba vilikuwa ni kinyume cha amri za Mungu.
37 Na sasa ikawa kwamba, baada ya mfalme Mosia kutuma vitu hivi miongoni mwa
watu walisadiki kuhusu ukweli wa maneno yake.
38 Kwa hivyo waliacha haja yao ya mfalme, na wakataka kila mtu apate nafasi yake
katika nchi yote; ndio, na kila mtu akawa tayari kuchukua wajibu wa dhambi zake.
39 Kwa hivyo, ikawa kwamba walijikusanya kwa vikundi katika nchi, ili wapige kura
na kuchagua waamuzi wao, watakaowahukumu kulingana na sheria ambayo
walipewa; na walifurahi sana kwa sababu ya uhuru ambao walipewa.
40 Na waliendelea kumpenda Mosia sana; ndio, walimheshimu zaidi ya mtu
mwingine yeyote; kwani hawakumchukua kama mkorofi aliyetaka kupata faida,
ndio, kwa mapato ya aibu yanayochafua nafsi; kwani hakuwa amewanyang'anya
utajiri, wala kufurahia umwagaji wa damu; lakini alikuwa ameimarisha amani katika
nchi, na alikuwa amewaruhusu watu wake wakombolewe kutoka kila aina ya
utumwa; kwa hivyo walimheshimu, ndio, kupita kipimo.
41 Na ikawa kwamba walichagua waamuzi wa kuwatawala, au kuwahukumu
kulingana na sheria; na walifanya haya kote katika nchi.
42 Na ikawa kwamba Alma alichaguliwa kuwa mwamuzi mkuu wa kwanza, pia
akiwa kuhani mkuu, baada ya baba yake kumpatia ofisi hio, na baada ya kumpatia
jukumu juu ya shughuli zote za kanisa.
43 Na sasa ikawa kwamba Alma alitembea katika njia za Bwana, na akatii amri zake,
na alitoa hukumu za haki; na amani ikaimarika kote katika nchi.
44 Na hivyo utawala wa waamuzi ukaanza kote katika nchi ya Zarahemla, miongoni
mwa watu wote walioitwa Wanefi; na Alma alikuwa mwamuzi mkuu na wa kwanza.
45 Na sasa ikawa kwamba baba yake alifariki, akiwa na umri wa miaka themanini na
miwili, baada ya kuishi na kutimiza amri za Mungu.
46 Na sasa ikawa kwamba Mosia akafariki pia, katika mwaka wa thelathini na tatu
wa utawala wake, akiwa na umri wa miaka sitini na mitatu; ikiwa miaka mia tano na
tisa tangu Lehi aondoke Yerusalemu.
47 Na hivyo utawala wa wafalme ukaisha kwa watu wa Nefi; na hivyo siku zikaisha
za Alma, ambaye alikuwa mwanzilishi wa kanisa lao.

# Kitabu cha Alma

## Mwana wa Alma

*Historia ya Alma, ambaye alikuwa mwana wa Alma, mwamuzi mkuu wa kwanza juu ya watu wa Nefi, na pia kuhani mkuu wa Kanisa. Historia kuhusu utawala wa waamuzi, na vita na mabishano miongoni mwa wale watu. Na pia historia ya vita miongoni mwa Wanefi na Walamani, kulingana na maandishi ya Alma, mwamuzi mkuu wa kwanza.*

## Alma 1

1 Sasa ikawa kwamba katika mwaka wa kwanza wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, tangu wakati huu na kuendelea mbele, mfalme Mosia akiwa ameelekea njia ya ulimwengu wote, akiwa amepigana vita vyema, akiwa ametembea wima mbele ya Mungu, akiwa hajaacha yeyote kutawala badala yake; walakini alikuwa ameanzisha sheria, na zilikubaliwa na watu; kwa hivyo iliwabidi kuishi kulingana na sheria alizokuwa ameweka.

2 Na ikawa kwamba katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Alma katika kiti cha hukumu, kulikuwa na mtu mmoja ambaye aliletwa mbele yake ili ahukumiwe, mtu aliyekuwa mkubwa, na alifahamika kwa sababu ya nguvu zake nyingi.

3 Na alikuwa ameenda miongoni mwa watu, akiwa amewahubiria yale ambayo aliita neno la Mungu, akipinga kanisa; akiwatangazia watu kwamba inafaa kila kuhani na kila mwalimu awe mashuhuri; na haifai wafanye kazi kwa mikono yao, lakini kwamba inafaa walishwe na watu.

4 Na alishuhudia kwa watu pia kwamba wanadamu wote wataokolewa katika siku ya mwisho, na kwamba haistahili waogope au kubabaika, lakini kwamba wainue vichwa vyao na washangilie; kwani Bwana alikuwa ameumba wanadamu wote, na pia kuwakomboa wanadamu wote; na, mwishowe, wanadamu wote watapokea uzima wa milele.

5 Na ikawa kwamba alifunza vitu hivi sana hata kwamba wengi waliamini maneno yake, wengi sana hata wakaanza kumlisha na kumpatia pesa.

6 Na akaanza kujiinua kwa kiburi cha moyo wake, na kuvaa mavazi ya thamani nyingi, ndio, na hata akaanza kuanzisha kanisa kulingana na mafundisho yake.

7 Na ikawa kwamba alipokuwa akienda, kuhubiria wale walioamini neno lake, alikutana na mtu ambaye alikuwa wa kanisa la Mungu, ndio, hata mmoja wa walimu wao; na akaanza kubishana na yeye kwa ukali, ili awapotoshe watu wa kanisa; lakini yule mtu alimpinga, na kumwonya kwa maneno ya Mungu.

8 Sasa jina la yule mtu lilikuwa Gideoni; na ni yeye ndiye aliyekuwa chombo mikononi mwa Mungu cha kuwakomboa watu wa Limhi kutoka utumwani.

9 Sasa, kwa sababu Gideoni alimpinga kwa maneno ya Mungu alimkasirikia Gideoni, na akauchomoa upanga wake na akaanza kumjeruhi. Sasa Gideoni alikuwa amelemewa kwa umri mkuu, kwa hivyo hakuweza kuvumilia mapigo yake, kwa hivyo aliuawa kwa upanga.

10 Na mtu aliyemuua alichukuliwa na watu wa kanisa, na kuletwa mbele ya Alma, kuhukumiwa kulingana na kosa alilotenda.

11 Na ikawa kwamba alisimama mbele ya Alma na kujitetea kwa ushujaa mwingi.

12 Lakini Alma akamwambia: Tazama, hii ndio mara ya kwanza kwamba ukuhani wa uongo umeletwa miongoni mwa watu hawa. Na tazama, hatia yako sio tu ya ukuhani wa uongo, lakini umejaribu kuulazimisha kwa upanga; na kama ukuhani wa uongo utalazimishwa miongoni mwa watu hawa utathibitisha maangamizo yao kabisa.

13 Na wewe umemwaga damu ya mtu mwenye haki, ndio, mtu ambaye ametenda wema mwingi miongoni mwa watu hawa; na kama tutakuachilia basi damu yake itatujia kulipiza kisasi.

14 Kwa hivyo umehukumiwa kufa, kulingana na sheria ambayo tulipewa na Mosia, mfalme wetu wa mwisho; na imekubaliwa na watu hawa; kwa hivyo lazima watu hawa wafuate sheria hiyo.

15 Na ikawa kwamba walimchukua; na jina lake lilikuwa Nehori; na wakambeba na kumpeleka juu ya kilima Manti, na hapo akalazimishwa, kwa usahihi zaidi akakubali, kati ya mbingu na ardhi, kwamba yale ambayo alikuwa amefunza watu yalikuwa kinyume cha neno la Mungu; na hapo akapata kifo cha aibu.

16 Walakini, hii haikukomesha kuenea kwa ukuhani wa uongo katika nchi; kwani kulikuwa na wengi ambao walipenda vitu vya ulimwengu visivyo na faida, na wakaendelea kuhubiri mafunzo ya uwongo; na walitenda haya ili wapate utajiri na heshima.

17 Walakini, hawakuthubutu kudanganya, kama ingejulikana, kwa kuogopa sheria, kwani waongo waliadhibiwa; kwa hivyo walidai kwamba walikuwa wanahubiri kulingana na imani yao; na sasa sheria haikuwa na uwezo wowote juu ya imani ya mtu yeyote.

18 Na hawakuthubutu kuiba, kwani waliogopa sheria, kwani kama hao waliadhibiwa; wala hawakupora, wala kuua, kwani yule aliyeua alihukumiwa kifo.

19 Lakini ikawa kwamba yeyote ambaye hakuwa wa kanisa la Mungu alianza kuwatesa wale ambao walikuwa wa kanisa la Mungu, na waliokuwa wamejivika jina la Kristo.

20 Ndio, waliwatesa, na kuwasumbua kwa maneno ya kila aina, na haya yalikuwa ni kwa sababu ya unyenyekevu wao; kwa sababu hawakuwa na majivuno katika macho yao wenyewe, na kwa sababu walifunzana neno la Mungu, wao kwa wao, bila kutozana pesa na bila gharama.

21 Sasa kulikuwa na sheria kali miongoni mwa watu wa kanisa, kwamba kusiwe na mtu yeyote, miongoni mwa washiriki wa kanisa, atakayeinuka na kuwatesa wale ambao sio washiriki wa kanisa, na kwamba kusiwe na mateso miongoni mwao.

22 Walakini, kulikuwa na wengi miongoni mwao ambao walianza kuwa na kiburi, na kuanza kubishana vikali na wapinzani wao, hata wakapigana kwa ngumi; ndio, walipigana kwa ngumi wao kwa wao.

23 Sasa hii ilikuwa katika mwaka wa pili wa utawala wa Alma, na ilikuwa ni chanzo cha mateso mengi kwa kanisa; ndio, ilikuwa ni chanzo cha majaribio mengi kwa kanisa.

24 Kwani mioyo ya wengi ilishupazwa na majina yao yalifutwa, hata kwamba hawakukumbukwa tena miongoni mwa watu wa Mungu. Na pia wengi walijiondoa kutoka miongoni mwao.

25 Sasa hili lilikuwa ni jaribio kuu kwa wale ambao walikuwa wamesimama imara katika imani; walakini, walikuwa wameimarishwa na hawangeondolewa katika kutii amri za Mungu, na walivumilia kwa subira mateso yale waliyotundikwa.

26 Na wakati makuhani walipoacha kazi zao ili watoe neno la Mungu kwa watu, watu nao pia waliacha kazi zao ili wasikie neno la Mungu. Na makuhani walipomaliza kuwafunza neno la Mungu wote walirudia kazi zao kwa bidii; na kuhani, hakujiinua zaidi ya wale ambao walimsikiliza, kwani mhubiri hakuwa bora zaidi kuliko wale ambao walimsikiliza, wala mwalimu hakuwa bora kuliko mwanafunzi; na hivyo wote walikuwa sawa, na wote walifanya kazi, kila mtu kulingana na nguvu zake.

27 Na walipeana mali yao, kulingana na uwezo wao, kwa masikini, na waliohitaji, na wagonjwa, na walioteswa; na hawakuvaa mavazi ya thamani kubwa, lakini walikuwa wasafi na wa kuvutia.

28 Na hivyo waliimarisha mambo ya kanisa; na hivyo wakaanza kuwa na amani bila kikomo tena, ingawa walikuwa wamepata mateso mengi.

29 Na sasa, kwa sababu ya uthabiti wa kanisa walianza kutajirika sana, wakipokea kwa utele vitu vyote walivyohitaji—utele katika mifugo na wanyama, na vinono vya kila aina, na pia utele wa nafaka, na wa dhahabu, na wa fedha, na wa vitu vya thamani, na utele wa hariri na kitani nzuri, na kila aina ya nguo ya kuvutia.

30 Na hivyo, hata katika hali yao ya kufanikiwa, hawakumfukuza yeyote aliyekuwa uchi, au walio na njaa, au walio na kiu, au wale ambao walikuwa wagonjwa, au wale ambao hawakuwa wamelishwa; na hawakuweka mioyo yao katika utajiri; kwa hivyo walikuwa wakarimu kwa wote, wote wazee kwa vijana, wote watumwa na walio huru, wote wanaume kwa wanawake, washiriki wa kanisa na wale wasio washiriki wa kanisa, bila kubagua wale wote walio na shida.

31 Na hivyo walifanikiwa na wakawa matajiri zaidi ya wale ambao hawakuwa washiriki wa kanisa.

32 Kwani wale ambao hawakuwa washiriki wa kanisa walijishughulisha na uchawi, na kuabudu sanamu au uvivu, na kusengenyana, na wivu na kuzusha mzozo; wakivaa mavazi yaliyo ghali; wakijiinua kwa kiburi machoni mwao; kutesana, kusema uwongo, kuiba, kupora, kufanya ukahaba, na kuua, na kila aina ya uovu; walakini, sheria ilitimizwa kwa wale wote ambao waliivunja, kwa vyovyote ilivyowezekana.

33 Na ikawa kwamba kwa kutimiza amri juu yao, kila mtu akiteseka kulingana na yale ambayo alitenda, wakawa watulivu zaidi, na hawakutenda uovu wowote ikiwa ungegunduliwa; kwa hivyo, kulikuwa na amani kuu miongoni mwa watu wa Nefi hadi mwaka wa tano wa utawala wa waamuzi.

## Alma 2

1 Na ikawa kwamba katika mwanzo wa mwaka wa tano wa utawala wao kulianza kuwa na ubishi miongoni mwa watu; kwani mtu fulani, aliyekuwa anaitwa Amlisi, yeye akiwa mjanja sana, ndio, mtu mwenye hekima kulingana na hekima ya ulimwengu, yeye akiwa mfano wa yule mtu aliyemuua Gideoni kwa upanga, ambaye aliuawa kulingana na sheria—

2 Sasa huyu Amlisi, kwa ujanja wake, alikuwa amewavutia watu wengi; wengi sana hata kwamba wakaanza kuwa wenye nguvu; na wakaanza kujaribu kumfanya Amlisi awe mfalme wa watu.

3 Sasa hii ilikuwa ni ya kuogofya kwa watu wa kanisa, na pia kwa wote ambao
hawakuwa wamevutiwa na vishawishi vya Amlisi; kwani walijua kwamba kulingana
na sheria yao vitu kama hivi lazima vithibitishwe kwa kura ya watu.
4 Kwa hivyo, kama ingewezekana kwamba Amlisi apate kura za watu, yeye akiwa
mtu mwovu, angewanyang'anya haki zao na heshima za kanisa; kwani ilikuwa nia
yake kuangamiza kanisa la Mungu.
5 Na ikawa kwamba watu walikusanyika pamoja kote nchini, kila mtu kulingana
na mawazo yake, kama ilikuwa wanamtaka au wanampinga Amlisi, katika vikundi
tofauti, wakipingana sana na kuwa na mabishano ya kushangaza wao kwa wao.
6 Na hivyo walikusanyika pamoja ili wapige kura kuhusu jambo hilo; na
wakasimama mbele ya waamuzi.
7 Na ikawa kwamba kura za watu zilikuwa kinyume cha Amlisi, kwamba
hakufanywa mfalme wa watu.
8 Sasa hii ilisababisha wale ambao walimpinga wawe na shangwe tele mioyoni
mwao; lakini Amlisi aliwachochea wale ambao walimtaka wawakasirikie wale
ambao walikuwa wanampinga.
9 Na ikawa kwamba walijikusanya pamoja, na kumteua Amlisi awe mfalme wao.
10 Sasa Amlisi alipofanywa kuwa mfalme wao aliwaamuru kwamba wachukue
silaha dhidi ya ndugu zao; na alifanya hivi ili wawe chini yake.
11 Sasa watu wa Amlisi walijulikana kwa jina la Amlisi, wakiitwa Waamlisi; na
waliobakia waliitwa Wanefi, au watu wa Mungu.
12 Kwa hivyo watu wa Wanefi walitambua nia ya Waamlisi, na kwa hivyo
walijitayarisha kupambana nao; ndio, walijiami kwa mapanga, na kwa vitara, na kwa
pinde na kwa mishale, na kwa mawe, na kwa kombeo, na kwa kila aina ya silaha za
vita, za kila namna.
13 Na hivyo ndivyo walivyojitayarisha kukabiliana na Waamlisi wakati
watakapowasili. Na waliwachagua makapteni, na makapteni wa juu, na makapteni
wakuu, kulingana na wingi wao.
14 Na ikawa kwamba Amlisi aliwaamu wanaume wake kwa kila namna ya silaha za
vita; na pia akawachagua watawala na viongozi juu ya watu wake, kuwaongoza ili
wapigane na ndugu zao.
15 Na ikawa kwamba Waamlisi waliwasili katika kilima cha Amnihu, ambacho
kilikuwa mashariki mwa mto wa Sidoni, ambao ulipita kando ya nchi ya Zarahemla,
na hapo wakaanza kushambuliana na Wanefi.
16 Sasa Alma, akiwa mwamuzi mkuu na mtawala wa watu wa Nefi, kwa hivyo
alienda juu na watu wake, ndio, na makapteni wake, na makapteni wakuu wake,
ndio, mbele ya majeshi yake, kupigana dhidi ya Waamlisi kwa vita.
17 Na walianza kuwaua Waamlisi katika kilima kilichokuwa mashariki mwa Sidoni.
Na Waamlisi walikabiliana na Wanefi kwa uwezo mkuu, hata kwamba Wanefi wengi
wakaanguka mbele ya Waamlisi.
18 Walakini Bwana aliutia nguvu mkono wa Wanefi, kwamba wakawaua Waamlisi
kwa mauaji mengi, hata kwamba wakaanza kutoroka kutoka kwao.
19 Na ikawa kwamba Wanefi waliwafuata Waamlisi siku hiyo yote, na kuwauwa kwa
mauaji makuu, hata kwamba Waamlisi elfu kumi na wawili, mia tano thelathini na
wawili walikufa; na Wanefi elfu sita, mia tano sitini na wawili walikufa.
20 Na ikawa kwamba wakati Alma hangewafuata Waamlisi zaidi, alisababisha watu
wake wapige hema zao katika bonde la Gideoni; bonde hilo likiitwa kwa jina la

Gideoni ambaye aliuawa kwa upanga kwa mkono wa Nehori; na Wanefi walipiga hema zao katika bonde hili usiku ule.

21 Na Alma alituma wapelelezi kufuata sazo la Waamlisi, ili ajue mipango yao na mitego yao, ili ajilinde kutokana nao, na ili awahifadhi watu wake wasiangamizwe.

22 Sasa wale ambao alikuwa amewatuma kwenda katika kambi ya Waamlisi waliitwa Zeramu, na Amnori, na Manti, na Limheri; hawa ndio waliokwenda na watu wao kupeleleza kambi ya Waamlisi.

23 Na ikawa kwamba kesho yake walirejea katika kambi ya Wanefi kwa haraka kuu, wakiwa wameshangaa zaidi, na kujawa na woga mkuu, wakisema:

24 Tazama, tulifuata kambi ya Waamlisi, na kwa mshangao wetu mkuu, katika nchi ya Minoni, ambayo iko juu ya nchi ya Zarahemla, katika njia inayoelekea hadi nchi ya Nefi, tuliona mkusanyiko mkuu wa Walamani; na tazama, Waamlisi wameungana nao;

25 Na wamewashambulia ndugu zetu katika nchi ile; na wanatoroka kutoka mbele yao na mifugo yao, na wake zao, na watoto wao, na wanaelekea katika mji wetu; na tusipoharakisha watanyakua mji wetu, na baba zetu, na wake zetu, na watoto wetu watauawa.

26 Na ikawa kwamba watu wa Nefi walichukua hema zao, na kuondoka katika bonde la Gideoni na kuelekea katika mji wao, ambao ulikuwa ni mji wa Zarahemla.

27 Na tazama, walipokuwa wakivuka mto wa Sidoni, Walamani na Waamlisi, wakiwa wengi, kama changarawe ya bahari, waliwavamia ili wawaangamize.

28 Walakini, Wanefi wakiwa wameongezwa nguvu na mkono wa Bwana, baada ya kumwomba sana kwamba awakomboe kutoka mikononi mwa maadui zao, kwa hivyo Bwana alisikia vilio vyao, na akawapa nguvu, na Walamani na Waamlisi wakaanguka mbele yao.

29 Na ikawa kwamba Alma alipigana na Amlisi kwa upanga, ana kwa ana; na walipigana kwa nguvu sana, mmoja kwa mmoja.

30 Na ikawa kwamba Alma akiwa mtu wa Mungu, aliyekuwa na imani kubwa, alipaza sauti, na kusema: Ee Bwana unirehemu na uokoe maisha yangu, ili niwe chombo mikononi mwako cha kuokoa na kuhifadhi watu hawa.

31 Sasa baada ya Alma kunena maneno haya alipigana tena na Amlisi; na akapewa nguvu, hata kwamba akamuua Amlisi kwa upanga.

32 Na pia alipigana na mfalme wa Walamani; lakini mfalme wa Walamani alitoroka kutoka mbele ya Alma na akatuma walinzi wake kupigana na Alma.

33 Lakini Alma, pamoja na walinzi wake, alipigana na walinzi wa mfalme wa Walamani hadi akawaua na kuwasukuma nyuma.

34 Na hivyo alifagia uwanja, kwa usahihi zaidi ufuo, uliokuwa magharibi mwa mto wa Sidoni, na kutupa maiti za Walamani waliokuwa wameuawa katika maji ya Sidoni, ili watu wake wapate nafasi ya kuvuka na kupigana na Walamani na Waamlisi magharibi mwa mto wa Sidoni.

35 Na ikawa kwamba baada ya wao wote kuvuka mto wa Sidoni kwamba Walamani na Waamlisi walianza kutoroka kutoka mbele yao, ingawa walikuwa wengi hata kwamba hawangehesabika.

36 Na wakakimbia kutoka mbele ya Wanefi na kuelekea nyika ambayo ilikuwa magharibi na kaskazini, mbali na mipaka ya nchi; na Wanefi waliwafuata kwa nguvu yao, na kuwaua.

37 Ndio, walikamatwa kwa kila upande, na kuuawa na kukimbizwa, hadi

wakatawanywa magharibi, na kaskazini, hadi walipoifiki nyika, ambayo iliitwa Hermantsi; na ilikuwa ni sehemu ile ambayo ilikuwa imejaa wanyama wa mwitu ambao ni wakali.

38 Na ikawa kwamba wengi wao walikufa nyikani kutokana na majeraha yao, na wakaliwa na wanyama hao na pia tai wa angani; na mifupa yao imepatikana, na imerundikwa ardhini.

# Alma 3

1 Na ikawa kwamba Wanefi ambao hawakuwa wameuawa kwa silaha za vita, baada ya kuzika wale ambao walikuwa wameuawa — sasa idadi ya wale ambao walikuwa wamekufa haingehesabika, kwa sababu nambari yao ilikuwa kubwa — baada ya kuzika watu wao wote walirejea katika mashamba yao, na kwa nyumba zao, na wake zao, na watoto wao.

2 Sasa wanawake wengi na watoto walikuwa wameuawa kwa upanga, na pia mifugo yao na wanyama wao; na pia mashamba yao mengi ya nafaka yaliangamizwa, kwani yalikanyagwa na majeshi.

3 Na sasa Walamani wengi na Waamlisi waliuawa kando ya mto wa Sidoni na kutupwa katika mto wa Sidoni; na tazama mifupa yao iko katika kilindi cha bahari, na ni mingi.

4 Na Waamlisi walitambulikana kutoka kwa Wanefi, kwani walikuwa wamejiweka alama nyekundu katika vipaji vyao kwa kuiga Walamani; walakini hawakuwa wamenyoa vichwa vyao kama Walamani.

5 Sasa vichwa vya Walamani vilikuwa vimenyolewa; na walikuwa uchi, ila tu ngozi ambayo walikuwa wamejifunga viunoni mwao, na pia silaha zao, ambazo walikuwa wamejizungushia, na pinde zao, na mishale yao, na mawe yao, na kombeo zao, na kadhalika.

6 Na ngozi ya Walamani ilikuwa nyeusi, kulingana na alama iliyowekwa juu ya babu zao, ambayo ilikuwa ni laana juu yao kwa sababu ya makosa yao na maasi yao dhidi ya kaka zao, ambao walikuwa ni Nefi, Yakobo, na Yusufu, na Samu, ambao walikuwa ni watu waadilifu na watakatifu.

7 Na kaka zao walitazamia kuwaua, kwa hivyo walilaaniwa; na Bwana Mungu akawaweka alama, ndio, juu ya Lamani na Lemueli, na pia wana wa Ishmaeli, na wanawake wa Kiishmaeli.

8 Na hii ilifanywa ili uzao wao utambulikane kutokana na uzao wa kaka zao, ili Bwana Mungu angewahifadhi watu wake, kwamba wasichanganyike na kuamini mila zisizokuwa halali na ambazo zingewaangamiza.

9 Na ikawa kwamba yeyote aliyechanganya uzao wake na Walamani aliuteremshia uzao wake laana ile.

10 Kwa hivyo, yeyote aliyekubali kupotoshwa na Walamani alijulikana kwa jina lile, na alama iliwekwa juu yake.

11 Na ikawa kwamba yeyote ambaye hakuamini mila za Walamani, lakini aliamini maandishi yale ambayo yalitolewa kutoka nchi ya Yerusalemu, na pia mila za babu zao, ambazo zilikuwa halali, na ambao waliziamini amri za Mungu na kuzitii, waliitwa Wanefi, au watu wa Nefi, tangu siku ile na kuendelea mbele —

12 Na ni wao ambao wamehifadhi maandishi ya watu wao ambayo ni ya kweli, na pia ya watu wa Walamani.

13 Sasa tutarudi tena kwa Waamlisi, kwani nao pia walikuwa na alama juu yao; ndio,
walijiweka alama wao wenyewe, ndio, hata alama nyekundu katika vipaji vyao.
14 Na hivyo neno la Mungu limetimizwa, kwani haya ndiyo maneno ambayo
alimwambia Nefi: Tazama, nimewalaani Walamani, na nitawaweka alama juu yao ili
wao na uzao wao watengwe kutoka kwako na uzao wako, tangu sasa hadi milele,
isipokuwa watubu uovu wao na wanirudie ili niwarehemu.
15 Na tena: Nitamweka alama yeyote atakayechanganya uzao wake na wa ndugu
yako, ili nao pia walaaniwe.
16 Na tena: Nitaweka alama kwa yeyote atakayepigana na wewe na uzao wako.
17 Na tena, ninasema kwamba yeyote atakayekutoroka hatakuwa tena uzao wako;
na nitakubariki, pamoja na yeyote atakayeitwa uzao wako, tangu sasa hadi milele; na
hizi ndizo zilizokuwa ahadi za Bwana kwa Nefi na uzao wake.
18 Sasa Waamlisi hawakujua kwamba walikuwa wakitimiza maneno ya Mungu
walipoanza kujiweka alama katika vipaji vyao; hata hivyo walikuwa wamemwasi
Mungu waziwazi; kwa hivyo ililazimika kwamba laana iwateremkie.
19 Sasa ningetaka mjue kwamba walijiletea laana wao wenyewe; na hata hivyo kila
mtu anayelaaniwa hujiletea lawama.
20 Na sasa ikawa kwamba baada ya siku chache tangu vita vilivyokuwa katika nchi
ya Zarahemla, na Walamani na Waamlisi, kwamba jeshi lingine la Walamani
liliwashambulia watu wa Nefi, katika mahali pale ambapo jeshi la kwanza lilikutana
na Waamlisi.
21 Na ikawa kwamba kulikuwa na jeshi ambalo lilitumwa kuwakimbiza kutoka nchi
yao.
22 Sasa Alma mwenyewe akiwa amejeruhiwa hakuenda wakati huu kupigana na
Walamani;
23 Lakini alituma jeshi kubwa dhidi yao; na walienda na kuwaua Walamani wengi,
na kuwafukuza waliobaki kutoka mipaka ya nchi yao.
24 Na kisha wakarudi tena na kuanza kuimarisha amani katika nchi, bila
kusumbuliwa tena kwa muda na maadui wao.
25 Sasa hivi vitu vyote vilifanywa, ndio, vita hivi vyote na mabishano yalianza na
kukoma katika mwaka wa tano wa utawala wa waamuzi.
26 Na katika mwaka mmoja, kumi ya maelfu ya nafsi zilitumwa katika ulimwengu
wa milele, kwamba wavune zawadi zao kulingana na kazi zao, kama zilikuwa njema
au kama zilikuwa mbaya, kuvuna furaha ya milele au huzuni ya milele, kulingana na
roho ambayo walichagua kutii, kama ni roho nzuri au mbaya.
27 Kwani kila mtu hupokea mshahara kutoka kwa yule anayemchagua kutii, na haya
ni kulingana na maneno ya roho ya unabii; kwa hivyo hebu na iwe kulingana na
ukweli. Na hivyo ukaisha mwaka wa tano wa utawala wa waamuzi.

# Alma 4

1 Sasa ikawa kwamba katika mwaka wa sita wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa
Nefi, hakukuwa na mabishano wala vita katika nchi ya Zarahemla;
2 Lakini watu walisumbuliwa, ndio, walisumbuliwa sana kwa kupoteza ndugu zao,
na pia hasara ya mifugo yao na wanyama wao, na pia hasara ya mashamba yao ya
nafaka, ambayo ilikanyagwa kwa miguu na kuangamizwa na Walamani.
3 Na masumbuko yao yalikuwa makuu sana hata kwamba kila nafsi ilisababishwa

kuomboleza; na waliamini kwamba ilikuwa ni hukumu ya Mungu juu yao kwa sababu ya uovu wao na machukizo yao; kwa hivyo walikumbushwa jukumu lao.

4 Na wakaanza kuimarisha kanisa sana; ndio, na wengi walibatizwa katika maji ya Sidoni na wakaunganishwa kwa kanisa la Mungu; ndio, walibatizwa kwa mkono wa Alma, ambaye alikuwa ametengwa kuwa kuhani mkuu juu ya watu wa kanisa, kwa mkono wa baba yake Alma.

5 Na ikawa kwamba katika mwaka wa saba wa utawala wa waamuzi nafsi elfu tatu na mia tano zilijiunga na kanisa la Mungu na kubatizwa. Na hivyo mwaka wa saba wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi uliisha; na kulikuwa na amani daima kwa wakati huo wote.

6 Na ikawa kwamba katika mwaka wa nane wa utawala wa waamuzi, kwamba watu wa kanisa walianza kupata kiburi, kwa sababu ya utajiri wao wa kupita kiasi, na hariri zao za kuvutia, na vitani vyao vilivyovutia, na kwa sababu ya mifugo yao na wanyama wao wengi, na dhahabu yao na fedha yao, na kila aina ya vitu vya thamani, ambavyo walikuwa wamepata kwa sababu ya bidii yao; na katika vitu hivi vyote walijivuna kwa macho yao, kwani walianza kuvaa mavazi ya bei ghali.

7 Sasa hii ilimsumbua Alma sana, ndio, na pia watu wengi ambao Alma alikuwa amewatenga wawe walimu, na makuhani, na wazee wa kanisa; ndio, wengi wao walianza kuhuzunishwa na uovu ambao waliona umeanza kuwa miongoni mwa watu wao.

8 Kwani waliona na wakahuzunika sana kwamba watu wa kanisa walianza kujiinua kwa kiburi machoni mwao, na kuweka mioyo yao katika utajiri na vitu vya ulimwengu visivyofaidisha, kwamba walianza kufanyiana madharau, wao kwa wao, na wakaanza kuwatesa wale ambao hawakuamini kulingana na nia yao na mapenzi yao.

9 Na hivyo, katika mwaka huu wa nane wa utawala wa waamuzi, kulianza kuwa na mabishano mengi miongoni mwa watu wa kanisa; ndio, kulikuwa na wivu, na mzozo, na chuki, na mateso, na kiburi, hata kuzidi kiburi cha wale ambao hawakuwa washiriki wa kanisa la Mungu.

10 Na hivyo mwaka wa nane wa utawala wa waamuzi ulikwisha; na uovu wa kanisa ulikuwa ni kikwazo kikuu kwa wale ambao hawakuwa washiriki wa kanisa; na hivyo kanisa likaanza kukosa kuendelea.

11 Na ikawa kwamba katika mwanzo wa mwaka wa tisa, Alma aliona uovu wa kanisa, na pia akaona kwamba mfano wa kanisa ulianza kuwaongoza wale wasioamini kutoka uovu mmoja hadi mwingine, hivyo kuwaletea watu maangamizo.

12 Ndio, aliona ukosefu wa usawa miongoni mwa watu, wengine wakijiinua juu kwa kiburi chao, wakidharau wengine, wakikataa kuwasaidia wale ambao walikuwa na shida na walio uchi na wale ambao walikuwa na njaa, na wale ambao walikuwa na kiu, na wale ambao walikuwa wagonjwa na waliosumbuka.

13 Sasa hii ilikuwa ni sababu kuu ya maombolezi miongoni mwa watu, wakati wengine walikuwa wanajinyenyekeza, wakiwasaidia wale ambao walihitaji msaada, kama vile kupeana mali yao kwa wale ambao walikuwa masikini na wenye shida, wakiwalisha wenye njaa, na kuteseka kwa kila aina ya masumbuko, kwa sababu ya Kristo, ambaye angekuja kulingana na roho ya unabii;

14 Wakitazamia mbele kwenye siku ile, na hivyo wakidumisha msamaha wa dhambi zao; wakijazwa na shangwe kuu kwa sababu ya ufufuo wa wafu, kulingana na nia na uwezo na ukombozi wa Yesu Kristo kutoka kamba za kifo.

15 Na sasa ikawa kwamba Alma, baada ya kuona masumbuko ya wafuasi wanyenyekevu wa Mungu, na mateso ambayo walibandikwa na watu wake waliobaki, na kuona ukosefu wa usawa wao wote, alianza kuhuzunika sana; walakini Roho wa Bwana hakumwacha.

16 Na akamchagua mtu mwenye hekima miongoni mwa wazee wa kanisa, na akampatia nguvu kulingana na kura ya watu, kwamba apate uwezo wa kuandika sheria kulingana na sheria ambazo zilikuwa zimetolewa, na kuzitekeleza kulingana na uovu na uhalifu wa watu.

17 Sasa jina la mtu huyu lilikuwa Nefiha, na alichaguliwa kuwa mwamuzi mkuu; na alikaa katika kiti cha hukumu na kuwahukumu na kuwatawala watu.

18 Sasa Alma hakumkabidhi ofisi ya kuhani mkuu wa kanisa, lakini alijihifadhia ofisi ya kuhani mkuu; lakini akamkabidhi Nefiha kiti cha hukumu.

19 Na hii alifanya ili yeye mwenyewe aende miongoni mwa watu wake, au watu wa Nefi, kwamba awahubirie neno la Mungu, kuwasisimua wakumbuke wajibu wao, na kwamba ashushe chini, kwa neno la Mungu, kiburi chao chote na ujanja na mabishano yaliyokuwa miongoni mwa watu wake, kwani hakuona njia nyingine ya kuwaokoa watu wake isipokuwa kwa kuwashawishi ushuhuda halisi.

20 Na hivyo katika mwanzo wa mwaka wa tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, Alma alimkabidhi Nefiha kiti cha hukumu, na akajitolea mwenyewe kabisa kwa ule ukuhani mkuu ulio mpango mtakatifu wa Mungu, kwa ushuhuda wa neno, kulingana na roho ya ufunuo na unabii.

*Maneno ambayo Alma, Kuhani Mkuu kulingana na mpango mtakatifu wa Mungu, aliwatolea watu katika miji yao na vijiji vyao kote katika nchi.*

# Alma 5

1 Sasa ikawa kwamba Alma alianza kuwatolea watu neno la Mungu, kuanzia katika nchi ya Zarahemla, na kuenea kote katika nchi.

2 Na haya ndiyo maneno aliyowaelezea watu katika kanisa lililokuwa limeanzishwa katika nchi ya Zarahemla, kulingana na maandishi yake mwenyewe, akisema:

3 Mimi, Alma, baada ya kuwekwa wakfu na baba yangu, Alma, kuwa kuhani mkuu wa kanisa la Mungu, yeye akiwa na uwezo na mamlaka kutoka kwa Mungu ya kutenda vitu hivi, tazama, ninawaambia kwamba alianza kuimarisha kanisa katika nchi ambayo ilikuwa mipakani mwa Nefi; ndio, nchi ambayo iliitwa nchi ya Mormoni; ndio, na alibatiza ndugu zake katika maji ya Mormoni.

4 Na tazama, ninawaambia, walikombolewa kutoka mikono mwa mfalme Nuhu, kwa rehema na uwezo wa Mungu.

5 Na tazama, baadaye, walitiwa utumwani na mikono ya Walamani huko nyikani; ndio, ninawaambia, walikuwa katika utumwa, na tena Bwana aliwakomboa kutoka utumwani kwa uwezo wa neno lake; na tukaletwa katika nchi hii, na hapa tulianza kuimarisha kanisa la Mungu kote katika nchi hii pia.

6 Na sasa tazama, ninawaambia, ndugu zangu, nyinyi ambao ni washiriki wa kanisa hili, je, mngali mnakumbuka ya kutosha utumwa wa babu zenu? Ndio, na bado mngali mnakumbuka ya kutosha rehema zake na uvumilivu wake kwao? Na zaidi, je, mngali mnakumbuka ya kutosha kwamba amezikomboa nafsi zao kutoka

jahanamu?

7 Tazama, alibadilisha mioyo yao; ndio, aliwaamsha kutoka usingizi mzito, na wakaamka katika Mungu. Tazama, walikuwa katikati ya giza; walakini, nafsi zao ziliangazwa na nuru ya neno lisilo na mwisho; ndio, walizingirwa na kamba za kifo; na minyororo ya jahanamu, na maangamizo yasiyo na mwisho yaliwangojea.

8 Na sasa ninawauliza, ndugu zangu, je, waliangamizwa? Tazama, ninawaambia, hapana, hawakuangamizwa.

9 Na tena ninauliza, kamba za kifo zilikatwa, na minyororo ya jahanamu ambayo iliwazingira, je, ilifunguliwa? Ninawaambia, Ndio, ilifunguliwa, na nafsi zao zikapanuka, na wakaimba upendo unaokomboa. Na ninawaambia kwamba wameokolewa.

10 Na sasa ninawauliza ni kwa masharti gani wanayookolewa? Ndio, ni masharti gani waliyokuwa nayo kutumaini wokovu? Ni sababu gani ya wao kufanywa huru kutokana na kamba za kifo, ndio, na pia minyororo ya jahanamu?

11 Tazama, ninaweza kuwaambia—si baba yangu Alma aliamini maneno ambayo yalizungumzwa kwa kinywa cha Abinadi? Na si yeye alikuwa nabii mtakatifu? Si yeye alizungumza maneno ya Mungu, na baba yangu Alma kuyaamini?

12 Na kulingana na imani yake badiliko kuu likafanyika katika moyo wake. Tazama ninawaambia kwamba haya yote ni ukweli.

13 Na tazama, aliwahubiria babu zenu neno, na mabadiliko makuu yakafanyika katika mioyo yao, na wakajinyenyekeza na kuweka tumaini lao katika Mungu wa kweli na anayeishi. Na tazama, walikuwa waaminifu hadi mwisho; kwa hivyo waliokolewa.

14 Na sasa tazama, ninawauliza, ndugu zangu wa kanisa, je, mmezaliwa kiroho katika Mungu? Mmepokea mfano wake katika nyuso zenu? Mmeshuhudia mabadiliko haya makuu katika mioyo yenu?

15 Mnaweka imani yenu ya ukombozi kwa yule aliyewaumba? Mnatazamia mbele kwa macho ya imani na kuona mwili huu wenye kufa ukifufuliwa katika kutokufa, na uharibifu huu ukiinuliwa katika kutoharibika, kusimama mbele ya Mungu kuhukumiwa kulingana na vitendo ambavyo vilitendwa katika miili inayokufa?

16 Ninawaambia, mnaweza kuwaza kwamba mnasikia sauti ya Bwana, siku ile, ikiwaambia: Njooni kwangu mliobarikiwa, kwani tazameni, kazi zenu zimekuwa kazi za haki usoni mwa dunia?

17 Au mnawaza kwenu nyinyi kwamba mtamdanganya Bwana katika siku ile, na kusema—Bwana, kazi zetu zimekuwa kazi za haki usoni mwa dunia—na kwamba atawaokoa?

18 Au kwa vingine, mnaweza kuwaza nyinyi wenyewe kwamba mmeletwa mbele ya baraza la hukumu ya Mungu na nafsi zenu zimejaa hatia na majuto, mkikumbuka hatia zenu zote, ndio, ukumbuko ulio kamili wa maovu yenu yote, ndio, ukumbuko kwamba mliziasi amri za Mungu?

19 Ninawaambia, mnaweza kumtazama Mungu siku ile kwa moyo safi na mikono safi? Ninawaambia, mnaweza kutazama juu, mkiwa na mfano wa Mungu umechorwa katika nyuso zenu?

20 Ninawaambia, mnaweza kutumaini wokovu baada ya kujitolea kuwa wafuasi wa ibilisi?

21 Ninawaambia, mtajua katika siku ile kwamba hamwezi kuokolewa; kwani mwanadamu yeyote hawezi kuokolewa bila mavazi yake kuoshwa na kuwa meupe;

ndio, lazima mavazi yake yatakaswe hadi yaoshwe kutokana na mawaa yote, kwa kupitia damu ya yule ambaye alizungumziwa na babu zetu, ambaye atakuja kuwakomboa watu wake kutoka dhambi zao.

22 Na sasa ninawauliza, ndugu zangu, mtahisi vipi, kama mtasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, mavazi yenu yakiwa yamechafuliwa na damu na kila aina ya uchafu? Tazama, vitu hivi vitashuhudia nini dhidi yenu?

23 Tazama si yatawashuhudia kwamba nyinyi ni wauaji, ndio, na pia kwamba nyinyi mna hatia kwa sababu ya uovu wa kila namna?

24 Tazama, ndugu zangu, mnadhani kwamba kama huyo atapata nafasi ya kuketi chini katika ufalme wa Mungu, pamoja na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, na pia manabii wote watakatifu, ambao mavazi yao yameoshwa, na hayana doa, safi na meupe?

25 Ninawaambia, Hapana; isipokuwa mumfanye Muumba wetu mwongo tangu mwanzo, au mdhani kwamba yeye ni mwongo tangu mwanzo, hamwezi kudhani kwamba kama huyo anaweza kupata nafasi katika ufalme wa mbinguni; lakini watatupwa nje kwa sababu wao ni watoto wa ufalme wa ibilisi.

26 Na sasa tazama, ninawambia, ndugu zangu, ikiwa mmepata mabadiliko ya moyo, na ikiwa mmesikia kuimba wimbo wa upendo wa ukombozi, ningeuliza, mnaweza kuhisi hivyo sasa?

27 Mmetembea, na mkijiweka bila lawama mbele ya Mungu? Mngesema, kama mngeitwa kufariki wakati huu, ndani yenu, kwamba mlikuwa wanyenyekevu wa kutosha? Kwamba mavazi yenu yameoshwa na kufanywa meupe kwa damu ya Kristo, ambaye atakuja kuwakomboa watu wake kutoka dhambi zao?

28 Tazama, mmevuliwa kiburi? Ninawaambia, kama bado, hamko tayari kukutana na Mungu. Tazama lazima mjitayarishe haraka; kwani ufalme wa mbinguni u karibu, na kama huyu hana uzima wa milele.

29 Tazama, nawaambia, kuna yeyote miongoni mwenu ambaye hajavuliwa wivu? Ninawaambia kwamba huyu hayuko tayari; na ningetaka kwamba ajitayarishe haraka, kwani wakati u karibu, na hajui ni wakati gani utakapofika; kwani kama huyo hatakosa hatia.

30 Na tena ninawauliza, kuna yeyote miongoni mwenu ambaye humfanyia ndugu yake mzaha, au yule ambaye anambandika mateso?

31 Ole kwa huyo, kwani hayuko tayari, na wakati u karibu ambao lazima atubu au hawezi kuokolewa!

32 Ndio, hata ole nyinyi watendaji wote wa uovu; tubuni, tubuni, kwani Bwana Mungu ameizungumza!

33 Tazama, yeye huwatumia wanadamu wote mwaliko, kwani mikono ya huruma imenyoshwa kwao, na anasema: Tubuni, na nitawapokea.

34 Ndio, anasema: Njooni kwangu na mtakula matunda ya mti wa uzima; ndio, mtakula na kunywa mkate na maji ya uhai bure;

35 Ndio, njooni kwangu na mlete kazi za haki, na hamtakatwa na kutupwa motoni—

36 Kwani tazama, wakati uko mkononi ambao yeyote ambaye haleti matunda mema, au yeyote ambaye hatendi kazi za haki, huyo ana sababu ya kulia na kuomboleza.

37 Ee nyinyi watendaji wa uovu; nyinyi ambao mmejazwa na vitu vya ulimwengu visivyo na maana, nyinyi ambao mnakiri kwamba mnajua njia za haki walakini

mmepotea, kama kondoo ambao hawana mchungaji, ingawa mchungaji aliwaita na
angali anawaita, lakini hamtasikia sauti yake!

38 Tazama, ninawaambia, kwamba mchungaji mwema anawaita, ndio, na kwa jina lake mwenyewe anawaita, ambalo ni jina la Kristo; na kama hamtasikia sauti ya mchungaji mwema, kwa jina ambalo mnaitwa nalo, tazama, nyinyi sio kondoo wa mchungaji mwema.

39 Na sasa kama nyinyi sio kondoo wa mchungaji mwema, nyinyi ni wa zizi gani? Tazama, nawaambia, kwamba ibilisi ndiye mchungaji wenu, na nyinyi ni wa zizi lake; na sasa, nani ambaye anaweza kukana haya? Tazama, nawaambia, yeyote ambaye anakana haya ni mwongo na ni mtoto wa ibilisi.

40 Kwani ninawaambia kwamba chochote ambacho ni kizuri kinatoka kwa Mungu, na chochote ambacho ni kiovu kinatoka kwa ibilisi.

41 Kwa hivyo, kama mtu anatenda kazi njema yeye husikiliza sauti ya mchungaji mwema, na humfuata; lakini yeyote ambaye anatenda kazi mbovu, huyo huwa mtoto wa ibilisi, kwani husikiliza sauti yake, na kumfuata.

42 Na yeyote ambaye anatenda haya lazima apokee mshahara wake kwake; kwa hivyo, kwa mshahara wake hupokea mauti, kulingana na vitu vya haki, kwani huwa amekufa kwa kazi zote nzuri.

43 Na sasa, ndugu zangu, ningetaka kwamba mnisikize, kwani ninazungumza na nguvu za nafsi yangu; kwani tazama, nimewazungumzia waziwazi ili msikosee, au nimenena kulingana na amri za Mungu.

44 Kwani nimeitwa kunena jinsi hii, kulingana na utaratibu mtakatifu wa Mungu, ambao umo katika Kristo Yesu; ndio, nimeamriwa nisimame na kushuhudia kwa watu hawa vitu ambavyo vilisemwa na babu zetu kuhusu vitu vitakavyokuja.

45 Na hii sio yote. Hamfikirii kwamba mimi mwenyewe najua vitu hivi? Tazama, nawashuhudia kwamba mimi najua kuwa vitu hivi ambavyo nimezungumza ni vya kweli. Na mnadhaniaje kwamba ninajua ukweli wao?

46 Tazama, ninawaambia kwamba yamesababishwa kujulikana kwangu na Roho Mtakatifu wa Mungu. Tazama, nimefunga na kusali siku nyingi ili nivijue vitu hivi mimi mwenyewe. Na sasa ninavijua mwenyewe kuwa ni vya kweli; kwani Bwana Mungu amevidhihirisha kwangu kwa Roho wake Mtakatifu; na hii ni roho ya ufunuo ambayo iko ndani yangu.

47 Na zaidi, ninawaambia kwamba imefunuliwa kwangu, kwamba maneno ambayo yalizungumzwa na babu zetu ni ya kweli, hata hivyo kulingana na roho ya unabii iliyo ndani yangu, ambayo pia ni dhihirisho la Roho wa Mungu.

48 Ninawaambia, kwamba ninajua mwenyewe ya kuwa lolote nitakalowaambia, kuhusu yale ambayo yatakayokuja, ni ya kweli; na ninawaambia, kwamba ninajua kuwa Yesu Kristo atakuja, ndio, Mzaliwa Pekee wa Baba, amejaa neema, na rehema, na ukweli. Na tazama, ni yeye ambaye anakuja kuondoa dhambi za ulimwengu, ndio, dhambi za kila mtu ambaye daima analiamini jina lake.

49 Na sasa ninawaambia kwamba huu ndio mpango ambao nimeitiwa, ndio, kuhubiria ndugu zangu wapendwa, ndio, na kila mmoja ambaye anaishi katika nchi; ndio, kuwahubiri kwa wote, wazee na vijana, wafungwa na walio huru; ndio, ninawaambia mliozeeka, na pia wenye umri wa kiasi, na kizazi kinachoinukia; ndio, kuwaambia kwamba lazima watubu na kuzaliwa tena.

50 Ndio, hivi anasema Roho: Tubuni, nyinyi kote ulimwenguni, kwani ufalme wa mbinguni umo mkononi; ndio, Mwana wa Mungu anakuja katika utukufu wake

mkuu, kwa nguvu zake, fahari, uwezo, na utawala. Ndio, ndugu zangu wapendwa,
ninawaambia, kwamba Roho anasema: Tazama utukufu wa Mfalme wa ulimwengu
wote; na pia Mfalme wa mbinguni hivi karibuni utametameta miongoni mwa
wanadamu.
51 Na pia Roho inaniambia, ndio, hulia kwangu na kwa sauti kuu, ikisema: Nenda
na uwaambie watu hawa—Tubuni, kwani msipotubu hamwezi kurithi kwa
vyovyote ufalme wa mbinguni.
52 Na tena ninawaambia, Roho inasema: Tazama, shoka limewekwa kwenye mzizi
wa mti; kwa hivyo kila mti ambao hauzai matunda mema utakatwa na kutupwa
katika moto, ndio, moto ambao hauwezi kuisha, hata moto usiozimika. Tazama, na
mkumbuke, Yule Mtakatifu ameinena.
53 Na sasa ndugu zangu wapendwa, ninawaambia, mnaweza kuvumilia misemo hii;
ndio, mnaweza kuweka vitu hivi kando, na mkanyage Yule Mtakatifu miguuni
mwenu; ndio, mnaweza kujazwa na kiburi cha mioyo yenu; ndio, mtaendelea kuvaa
mavazi ya bei na kuiweka mioyo yenu katika vitu vya ulimwengu visivyo na busara,
na utajiri wenu?
54 Ndio, mtaendelea kujidhania kwamba nyinyi ni bora zaidi ya wengine; ndio,
mtaendelea kuwatesa ndugu zenu, ambao ni wanyenyekevu na hufuata mpango
mtakatifu wa Mungu, ambao umewaleta katika kanisa hili, wakishatakaswa na
Roho Mtakatifu, na hutenda kazi njema ya toba—
55 Ndio, na mtaendelea kuwageukia wale ambao ni masikini, na wenye shida, na
kuwakataza msaada?
56 Na mwishowe, nyote ambao mnaendelea katika uovu wenu, ninawaambia
kwamba hawa ndio wale ambao watakatwa na kutupwa motoni wasipotubu kwa
haraka.
57 Na sasa ninawaambia, nyote ambao mnatamani kufuata sauti ya mchungaji
mwema, ondokeni kutoka kwa waovu, na mjitenge, na msiguse vitu vyao vichafu; na
tazama, majina yao yatafutwa, kwamba majina ya waovu hayatahesabiwa miongoni
mwa majina ya wale wenye haki, ili neno la Mungu litimizwe, ambalo linasema:
Majina ya waovu hayatachanganywa na majina ya watu wangu;
58 Kwani majina ya wale wenye haki yataandikwa katika kitabu cha uzima, na kwao
nitawapatia urithi katika mkono wangu wa kulia. Na sasa, ndugu zangu, nini
mtakachosema kinyume cha hivi? Ninawaambia, mkizungumza kinyume cha hivi,
haijalishi, kwani lazima neno la Mungu litimizwe.
59 Kwani ni mchungaji gani miongoni mwenu ambaye ana kondoo wengi na
hawachungi, ili mbwa mwitu wasiingie na kuwararua mifugo yake? Na tazama,
kama mbwa mwitu anashambulia mifugo yake hamfukuzi nje? Ndio, na mwishowe,
akiweza, atamwangamiza.
60 Na sasa ninawaambia kwamba mchungaji mwema anawaita; na ikiwa mtaisikiliza
sauti yake atawaleta katika zizi lake, na nyinyi ni kondoo wake; na anawaamuru
kwamba msikubali mbwa mwitu aliye na njaa aingie miongoni mwenu, ili
msiangamizwe.
61 Na sasa mimi, Alma, ninawaamuru nyinyi kwa lugha ya yule ambaye
ameniamuru, kwamba mtie bidii katika kutii maneno ambayo nimewazungumzia.
62 Nazungumza kwa njia ya amri kwenu ambao mnashiriki katika kanisa; na kwa
wale wasio washiriki wa kanisa nawazungumzia kwa njia ya kuwaalika, na kusema:
Njooni na mpate kubatizwa ubatizo wa toba, ili pia nanyi mshiriki katika kula tunda

la mti wa uzima.

## Alma 6

1 Na sasa ikawa kwamba baada ya Alma kumaliza kuwazungumzia watu wa kanisa,
ambalo lilikuwa limeanzishwa katika mji wa Zarahemla, aliwatawaza makuhani na
wazee, kwa kuwawekea mikono kulingana na mpango wa Mungu, kusimamia na
kuchunga kanisa.
2 Na ikawa kwamba yeyote ambaye hakuwa mshiriki wa kanisa ambaye alitubu
dhambi zake alibatizwa ubatizo wa toba, na akapokelewa katika kanisa.
3 Na ikawa kwamba wale ambao walikuwa washiriki wa kanisa na hawakutubu
uovu wao na kunyenyekea mbele ya Mungu — ninamaanisha wale ambao walikuwa
wamejiinua kwa kiburi cha mioyo yao — wao walikataliwa, na majina yao kufutwa,
kwamba majina yao yasihesabiwe miongoni mwa wale ambao ni wenye haki.
4 Na hivyo walianza kuimarisha mpango wa kanisa katika mji wa Zarahemla.
5 Sasa ningetaka mfahamu kwamba neno la Mungu lilikuwa huru kwa wote, na
kwamba hakuna yeyote aliyenyimwa nafasi ya kukusanyika pamoja ili kusikia neno
la Mungu.
6 Walakini watoto wa Mungu waliamriwa kwamba wakusanyike pamoja muda kwa
muda, na waungane katika kufunga na sala kuu kwa niaba ya ustawi wa nafsi ambazo
hazikumjua Mungu.
7 Na sasa ikawa kwamba baada ya Alma kutoa masharti haya aliondoka kutoka
kwao, ndio, kutoka kanisa ambalo lilikuwa katika mji wa Zarahemla, na akaenda
mashariki mwa mto Sidoni, katika bonde la Gideoni, palipojengwa mji, ambao
uliitwa mji wa Gideoni, ambao ulikuwa katika bonde lililoitwa Gideoni, kwani
lilitungwa yule mtu ambaye aliuawa kwa mkono wa Nehori kwa upanga.
8 Na Alma aliendа na kuanza kutangaza neno la Mungu katika kanisa ambalo
lilikuwa limeanzishwa katika bonde la Gideoni, kulingana na ufunuo wa ukweli wa
neno ambao ulizungumzwa na babu zake, na kulingana na roho ya unabii ambayo
ilikuwa ndani yake, kulingana na ushuhuda wa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu,
ambaye atakuja kuwakomboa watu wake kutoka dhambi zao, na ule mpango
mtakatifu ambao aliitiwa. Na hivyo imeandikwa. Amina.

*Maneno ya Alma ambayo aliwakabidhi watu wa Gideoni, kulingana na maandishi yake mwenyewe.*

## Alma 7

1 Tazama ndugu zangu wapendwa, kwa kuwa nimeruhusiwa kuja kwenu, kwa hivyo
nitajaribu kuwazungumzia kwa lugha yangu; ndio, kwa kinywa changu mwenyewe,
nikiona kwamba hii ndio mara yangu ya kwanza ya kuwazungumzia kwa maneno ya
kinywa changu, kwani nilikuwa nimefungiwa kwa kiti cha hukumu, nikiwa na
shughuli nyingi kwamba sikuweza kuwatembelea.
2 Na hata singeweza kuja sasa kwa wakati huu, ijapokuwa kiti cha hukumu
kimepewa mwingine, atawale badala yangu; na Bwana katika rehema nyingi
amewezesha kwamba niwatembelee.

3 Na tazama, nimekuja kwa matumaini mengi kwamba niwapate kwamba
mmejinyenyekeza mbele ya Mungu, na kwamba mlikuwa mnaendelea kuomba
neema yake, na kwamba niwapate hamna lawama mbele yake, na kwamba
nisiwapate mkiwa katika hali ya kuhofisha kama ile ndugu zetu waliyokuwa nayo
huko Zarahemla.
4 Lakini jina la Mungu libarikiwe, kwani amenijulisha nijue, ndio, amenipatia
shangwe kuu ya kujua kwamba wamejiimarisha tena katika haki yake.
5 Na ninatumai, kulingana na Roho wa Mungu aliye ndani yangu, kwamba pia
nitakuwa na shangwe juu yenu; walakini sitamani kwamba shangwe yangu kwenu
nyinyi ije kwa mateso mengi na huzuni kama ile niliyokuwa nayo kwa ndugu huko
Zarahemla, kwani tazama, shangwe yangu juu yao inakuja baada ya kupitia mateso
mengi na huzuni.
6 Lakini tazama, ninatumai kwamba hamko katika hali ya kutoamini kama vile
waliyokuwa ndugu zenu; ninatumaini kwamba hamjainuliwa kwa kiburi cha mioyo
yenu; ndio, ninatumaini kwamba hamjaweka mioyo yenu katika utajiri na vitu vya
ulimwengu visivyo na busara; ndio, ninatumaini kwamba hamwabudu sanamu,
lakini mnamwabudu Mungu wa kweli na anayeishi, na kwamba mnatazamia
msamaha wa dhambi zenu, kwa imani isiyo na mwisho, inayokuja.
7 Kwani tazama, ninawaambia kuna vitu vingi vitakavyokuja; na tazama, kuna kitu
kimoja ambacho ni muhimu kuliko vyote — kwani tazama, wakati hauko mbali
ambao Mkombozi ataishi miongoni mwa watu wake.
8 Tazama, sisemi kwamba atakuja kati yetu ule wakati atakaokuwa akiishi katika
hekalu la udongo mwilini; kwani tazama, Roho hajaniambia kwamba itakuwa
hivyo. Sasa kitu hiki sikijui; lakini ninajua haya, kwamba Bwana Mungu ana uwezo
wa kutenda vitu vyote ambavyo vinalingana na neno lake.
9 Lakini tazama, Roho ameniambia haya, akisema: Watangazie watu hawa,
ukisema — Tubuni nyinyi, na mtayarishie Bwana njia, na mfuate njia zake, ambazo
ni nyoofu; kwani tazama, ufalme wa mbinguni u karibu, na Mwana wa Mungu
atakuja usoni mwa dunia.
10 Na tazama, atazaliwa na Mariamu, huko Yerusalemu ambayo ni nchi ya babu
zetu, yeye akiwa bikira, chombo cha thamani na kilichochaguliwa, ambaye
atawezeshwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kupata mimba, na kumzaa mwana,
ndio, hata Mwana wa Mungu.
11 Na atakwenda, na kuteseka maumivu na masumbuko na majaribio ya kila aina;
na hii kwamba neno litimizwe ambalo linasema atabeba maumivu na magonjwa ya
watu wake.
12 Na atajichukulia kifo, ili afungue kamba za kifo ambazo zinafunga watu wake; na
atajichukulia unyonge wao, ili moyo wake ujae rehema, kulingana na mwili, ili ajue
kulingana na mwili jinsi ya kuwasaidia watu wake kulingana na unyonge wao.
13 Sasa Roho anajua vitu vyote; walakini Mwana wa Mungu anateseka katika mwili
ili achukue dhambi za watu wake, kwamba aondoe uvunjaji wao wa sheria kulingana
na nguvu za ukombozi wake; na sasa tazama, huu ndio ushuhuda ulio ndani yangu.
14 Sasa nawaambia kwamba lazima mtubu, na mzaliwe tena; kwani Roho anasema
kuwa msipozaliwa tena hamwezi kurithi ufalme wa mbinguni; kwa hivyo njooni
mbatizwe ubatizo wa toba, ili msafishwe kutoka kwa dhambi zenu, ili muwe na
imani katika Mwanakondoo wa Mungu, anayeondoa dhambi za ulimwengu,
ambaye anaweza kuokoa na kuosha kutokana na uovu wote.

15 Ndio, ninawaambia njooni na msiogope, na muweke kando kila dhambi, ambayo inawasumbua, ambayo inawatia katika maangamizo, ndio, njooni na msonge mbele na mmwonyeshe Mungu wenu kwamba mnatamani kutubu dhambi zenu na kuingia kwenye agano naye kuweka amri zake, na kushuhudia kwake siku hii kwa kuingia kwenye maji ya ubatizo.

16 Na yeyote atakayefanya hivi, na atii amri za Mungu tangu leo, huyu atakumbuka kwamba nilimwambia, ndio, atakumbuka kwamba nimemwambia, atapokea uzima wa milele, kulingana na ushuhuda wa Roho Mtakatifu, ambaye anashuhudia ndani yangu.

17 Na sasa ndugu zangu wapendwa, mnaamini vitu hivi? Tazama, ninawaambia, ndio, ninajua kwamba mnaviamini; na jinsi ile ninayojua kwamba mnaviamini ni kwa dhihirisho la Roho aliye ndani yangu. Na sasa kwa sababu imani yenu ina nguvu kuhusu hayo, ndio, kuhusu vile vitu ambavyo nimezungumza, shangwe yangu ni kuu.

18 Kwani kama vile nilivyosema kwenu hapo mwanzo, kwamba nilitamani msiwe katika hali ile ya dharura kama ndugu zenu, hata hivyo nia yangu imependezwa.

19 Kwani ninahisi kwamba mko katika njia za haki; ninahisi kwamba mko katika njia ile inayoelekea katika ufalme wa Mungu; ndio, ninahisi kwamba mnanyoosha njia zake.

20 Ninahisi kwamba imefanywa kujulikana kwenu, kwa ushuhuda wa neno lake, kwamba yeye hawezi kupita katika njia kombo; wala habadilishi yale ambayo amesema; wala hana kivuli cha kugeukia kushoto au kulia, au kutoka kwa mema na kuingilia yale maovu; kwa hivyo, njia zake ni za milele.

21 Na haishi katika hekalu zilizo chafu; wala uchafu au chochote ambacho kisicho safi hakiwezi kupokewa katika ufalme wa Mungu; kwa hivyo ninawaambia kwamba wakati utafika, ndio, na itakuwa siku ya mwisho, kwamba yule aliye mchafu atabaki katika uchafu wake.

22 Na sasa ndugu zangu wapendwa, nimewaambia vitu hivi ili niwaamshe mjue wajibu wenu kwa Mungu, ili mtembee bila lawama mbele yake, ili mtembee kulingana na mpango mtakatifu wa Mungu, ambayo kwayo mmepokelewa.

23 Na sasa ningetaka kwamba muwe wanyenyekevu, na muwe wapole na waungwana; wepesi kusihiwa; wenye utele wa subira na uvumilivu; wenye kiasi katika vitu vyote, wenye bidii katika kutii amri za Mungu wakati wote; mkiomba kwa vyovyote mnavyohitaji, vya kiroho na vya kimwili; na kila wakati kumshukuru Mungu kwa vyovyote mnavyopokea.

24 Na mhakikishe kwamba mna imani, tumaini, na hisani, na kisha mtadumu katika kazi nzuri.

25 Na Bwana awabariki, na ahifadhi mavazi yenu yasiwe na doa, ili mwishowe mletwe mkae chini na Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, na manabii watakatifu ambao wameishi tangu ulimwengu uumbwe, mkiwa na mavazi yenu yasiyo na doa kama vile mavazi yao hayana doa, katika ufalme wa mbinguni bila kutoka nje tena.

26 Na sasa ndugu zangu wapendwa, nimewazungumzia mambo haya kulingana na Roho anayeshuhudia ndani yangu; na nafsi yangu inafurahi sana, kwa sababu ya bidii nyingi na utiifu ambao mmelipatia neno langu.

27 Na sasa, amani ya Mungu iwe nanyi, na kwa nyumba zenu na mashamba yenu, na mifugo yenu na wanyama wenu, na yote ambayo mnamiliki, wake zenu na watoto wenu, kulingana na imani yenu na kazi njema, tangu sasa hadi milele. Na hivyo

nimesema. Amina.

## Alma 8

1 Na sasa ikawa kwamba Alma alirudi kutoka nchi ya Gideoni, baada ya kufunza watu
wa Gideoni vitu vingi ambavyo haviwezi kuandikwa, baada ya kuimarisha
mpangilio wa kanisa, kulingana na vile alivyokuwa amefanya katika nchi ya
Zarahemla, ndio, alirejea katika nyumba yake Zarahemla kujipumzisha kutokana na
ile kazi aliyokuwa ametenda.
2 Na hivyo mwaka wa tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi ulikwisha.
3 Na ikawa kwamba katika mwanzo wa mwaka wa kumi wa utawala wa waamuzi
juu ya watu wa Nefi, kwamba Alma aliondoka kutoka huko na kusafiri katika nchi ya
Meleki, magharibi kando mwa mto Sidoni, magharibi kando mwa mipaka ya nyika.
4 Na akaanza kuwafunza watu katika nchi ya Meleki kulingana na mpango
mtakatifu wa Mungu, ambao alikuwa ameitwa kwake; na akaanza kufunza watu
kote katika nchi ya Meleki.
5 Na ikawa kwamba watu walimjia kutoka mipaka yote ya nchi ambayo ilikuwa
kando ya nyika. Na wakabatizwa kote katika nchi;
6 Kwa hivyo baada ya kukamilisha kazi yake katika Meleki aliondoka huko, na
akasafiri muda wa siku tatu kaskazini mwa nchi ya Meleki; na akafika katika mji
ulioitwa Amoniha.
7 Sasa ilikuwa ni desturi ya watu wa Nefi kutunga nchi zao, na miji yao, na vijiji
vyao, ndio, na hata vijiji vyao vyote vidogo, kwa jina la yule ambaye aliimiliki
kwanza; na ilikuwa hivyo katika nchi ya Amoniha.
8 Na ikawa kwamba baada ya Alma kuwasili katika mji wa Amoniha alianza
kuwahubiria neno la Mungu.
9 Sasa Shetani alikuwa amekamata mioyo ya watu wa mji wa Amoniha; kwa hivyo
hawakusikiliza maneno ya Alma.
10 Walakini Alma alitia bidii sana katika roho, akipambana na Mungu katika sala
kuu, ili awateremshie watu waliokuwa katika mji Roho wake; kwamba akubali
kwamba awabatize katika toba.
11 Walakini, walishupaza mioyo yao, na kumwaambia: Tazama, tunajua kwamba
wewe ni Alma; na tunajua kwamba wewe ni kuhani mkuu wa kanisa ambalo wewe
umeanzisha katika sehemu nyingi za nchi, kulingana na mila zako; na sisi sio
washirika wa kanisa lako, na hatuamini mila za kishenzi kama hizo.
12 Na sasa tunajua kwamba kwa sababu sisi sio washirika wa kanisa lako tunajua
kwamba huna mamlaka juu yetu; na wewe umemkabidhi Nefiha kiti cha hukumu;
kwa hivyo wewe si mwamuzi mkuu juu yetu.
13 Sasa baada ya watu kunena haya, na kuyapinga maneno yake yote, na kumfanyia
mzaha, na kumtemea mate, na kumsababisha kwamba atupwe nje ya mji wao,
aliondoka hapo na akafunga safari yake akielekea mji ambao uliitwa Haruni.
14 Na ikawa kwamba alipokuwa akisafiri huko, na kuzidiwa sana na huzuni, na
kupambana na mateso mengi na kusononeka sana katika nafsi, kwa sababu ya uovu
wa watu ambao walikuwa katika mji wa Amoniha, ikawa kwamba wakati ambao
Alma alikuwa amezidiwa na huzuni, tazama malaika wa Bwana alimtokea, na
kusema:
15 Heri wewe, Alma; kwa hivyo, inua kichwa chako na ufurahi, kwani una sababu

kubwa ya kufurahi; kwani umekuwa mwaminifu katika kutii amri za Mungu tangu
ule wakati ambao ulipokea ujumbe wako mara ya kwanza kutoka kwake. Tazama,
mimi ndiye yule aliyeikukabidhia.
16 Na tazama, nimetumwa kukuamuru kwamba urudi katika mji wa Amoniha, na
uwahubirie tena watu wa mji huo; ndio, uwahubirie. Ndio, uwaambie, wasipotubu
Bwana Mungu atawaangamiza.
17 Kwani tazama, wanapanga kwa wakati huu jinsi ya kuangamiza uhuru wa watu
wako, (kwani Bwana anasema hivi) ambayo ni kinyume cha maagizo, na hukumu,
na amri ambazo amewapatia watu wake.
18 Sasa ikawa kwamba baada ya Alma kupokea ujumbe wake kutoka kwa malaika
wa Bwana alirudi kwa haraka katika nchi ya Amoniha. Na akaingia katika mji kwa
njia nyingine, ndio, kwa njia iliyo kusini mwa mji wa Amoniha.
19 Na alipoingia mjini alikuwa na njaa, na akamwambia mtu fulani: Waweza
kumpatia mtumishi mnyenyekevu wa Mungu kitu cha kula?
20 Na yule mtu akamwambia: Mimi ni Mnefi, na ninajua kwamba wewe ni nabii
mtakatifu wa Mungu, kwani wewe ndiye yule mtu ambaye malaika alisema katika
ono: Wewe utampokea. Kwa hivyo, njoo na mimi katika nyumba yangu na
nitakupatia chakula changu; na ninajua kwamba wewe utakuwa baraka kwangu
mimi na nyumba yangu.
21 Na ikawa kwamba yule mtu alimkaribisha katika nyumba yake; na yule mtu
aliitwa Amuleki; na akaleta mkate na nyama na kumpakulia Alma.
22 Na ikawa kwamba Alma alikula mkate na kushiba; na akambariki Amuleki na
nyumba yake, na akamshukuru Mungu.
23 Na baada ya kula na kushiba akamwambia Amuleki: Mimi ni Alma, na mimi ni
kuhani mkuu wa kanisa la Mungu kote nchini.
24 Na tazama, nimeitwa kuhubiri neno la Mungu miongoni mwa watu hawa wote,
kulingana na roho ya ufunuo na unabii; na nilikuwa katika nchi hii na
hawakunipokea, lakini walinifukuza na karibu niiache nchi hii milele.
25 Lakini tazama, nimeamuriwa kwamba nirudi tena na niwatolee watu hawa
unabii, ndio, na kuwashuhudia dhidi ya maovu yao.
26 Na sasa, Amuleki, kwa sababu umenilisha na kunipokea, umebarikiwa; kwani
nilikuwa mwenye njaa, kwa kufunga siku nyingi.
27 Na Alma akaishi siku nyingi na Amuleki kabla ya kuanza kuwahubiria watu.
28 Na ikawa kwamba watu waliendelea kuwa wabaya zaidi katika uovu wao.
29 Na neno likamjia Alma, likisema: Nenda; na pia umwambie mtumishi wangu
Amuleki, nenda mbele na uwatolee watu hawa unabii, uwaambie — Tubuni, kwani
Bwana anasema, msipotubu nitawatembelea watu hawa kwa ghadhabu yangu; ndio,
na sitabadilisha ghadhabu yangu kali kutoka kwao.
30 Na Alma akaenda, pamoja na Amuleki, miongoni mwa watu, kuwatangazia neno
la Mungu; na walijazwa na Roho Mtakatifu.
31 Na wakapewa uwezo, hata ikawa kwamba haingewezekana wao kufungiwa katika
jela; wala mtu yeyote kuweza kuwaua; walakini hawakutumia uwezo wao hadi
walipofungwa kwa kamba na kuwekwa katika jela. Sasa, haya yalifanywa ili Bwana
adhihirishe uwezo wake ndani yao.
32 Na ikawa kwamba walienda na wakaanza kuhubiria watu na kuwatolea unabii,
kulingana na roho na uwezo ambao Bwana alikuwa amewapatia.

*Maneno ya Alma, na pia maneno ya Amuleki, ambayo yalitangaziwa watu waliokuwa katika nchi ya Amoniha. Na pia wanatupwa katika jela, na kukombolewa kwa nguvu za miujiza ya Mungu ambayo ilikuwa ndani yao, kulingana na maandishi ya Alma.*

# Alma 9

1 Na tena, mimi, Alma, baada ya kuamriwa na Mungu kwamba nimchukue Amuleki na kwenda tena na kuhubiria watu hawa, au watu waliokuwa katika mji wa Amoniha, ikawa kwamba nilipoanza kuwahubiria, nao wakaanza kubishana na mimi, wakisema:

2 Nani wewe? Unadhani kwamba tutaamini ushuhuda wa mtu mmoja, hata ikiwa atatuhubiria kuwa dunia itakwisha?

3 Sasa hawakufahamu yale ambayo walizungumza; kwani hawakujua kwamba dunia itakwisha.

4 Na wakasema pia: Hatutaamini maneno yako kama utatoa unabii kwamba mji huu mkuu utaangamizwa katika siku moja.

5 Sasa hawakujua kwamba Mungu angeweza kufanya vitendo vya ajabu kama hivyo, kwani walikuwa watu wenye mioyo migumu na shingo ngumu.

6 Na wakasema: Mungu ni nani, ambaye hatumi mamlaka zaidi ya mtu mmoja miongoni mwa watu hawa, kuwatangazia ukweli wa vitu vikuu na vya ajabu kama hivi?

7 Na wakasonga mbele ili wanikamate; lakini tazama, hawakuweza. Na nikasimama kwa ujasiri ili niwatangazie, ndio, niliwashuhudia kwa ujasiri, nikisema:

8 Tazameni, Ee nyinyi kizazi kiovu na kibaya, ni vipi mmesahau mila za babu zenu; ndio, vipi mara moja mmesahau amri za Mungu.

9 Hamkumbuki kwamba baba yetu, Lehi, alitolewa Yerusalemu kwa mkono wa Mungu? Hamkumbuki kwamba wote waliongozwa na yeye kupitia nyikani?

10 Na mmesahau haraka vipi kwamba aliwakomboa babu zetu mara nyingi kutoka mikononi mwa maadui wao, na akawahifadhi kutokana na maangamizo, hata kwa mikono ya ndugu zao wenyewe?

11 Ndio, na kama sio kwa uwezo wake usio na kipimo, na rehema yake, na subira yake kwetu sisi, tungekuwa tumetengwa kutoka usoni mwa dunia kitambo sana kabla ya wakati huu, na pengine tungekuwa tumewekwa kwa hali ya taabu na hofu isiyo na mwisho.

12 Tazama, sasa nawaambia kwamba anawaamuru mtubu; na msipotubu, hamwezi kurithi ufalme wa Mungu. Lakini tazama, haya sio yote—amewaamuru kwamba mtubu, au atawaangamiza kabisa kutoka usoni mwa dunia; ndio; atawatembelea katika ghadhabu yake, na katika ghadhabu yake kali hatawarehemu.

13 Tazama, hamkumbuki maneno ambayo alimzungumzia Lehi, akisema kwamba: Kadiri mtakavyoweka amri zangu, ndivyo mtakavyofanikiwa katika nchi? Na tena imesemwa kwamba: Kadiri vile msiposhika amri zangu ndivyo mtakavyotengwa kutoka uwepo wa Bwana.

14 Sasa ningetaka kwamba mkumbuke, kwamba jinsi Walamani wamekosa kushika amri za Mungu, wamekatwa kutokana na uwepo wa Bwana. Sasa tunaona kwamba neno la Bwana limethibitishwa katika kitu hiki, na Walamani wametengwa kutoka uwepo wake, tangu mwanzo wa uasi wao katika nchi hii.

15 Walakini nawaambia, kwamba itakuwa afadhali kwao katika siku ya hukumu
kuliko nyinyi, ikiwa mtabaki katika dhambi zenu, ndio, na hata ya kuvumilika zaidi
katika maisha haya, msipotubu.
16 Kwani kuna ahadi nyingi ambazo Walamani wamenyooshewa; kwani ni kwa
sababu ya mila za babu zao ambazo ziliwasababisha kuishi katika hali yao ya
kutojua; kwa hivyo Bwana atawahurumia na azidishe maisha yao katika nchi.
17 Na wakati utafika ambao watawezeshwa kuamini neno lake, na kujua kasoro za
mila za babu zao; na wengi wao wataokolewa, kwani Bwana atawarehemu wote
ambao wataliita jina lake.
18 Lakini tazama, nawaambia kwamba mkiendelea katika uovu wenu siku zenu
hazitazidishwa katika nchi, kwani Walamani watatumwa kuwashambulia; na
msipotubu watakuja katika wakati ambao hamjui, na mtatembelewa na
maangamizo makuu; na itakuwa kulingana na ghadhabu kali ya Bwana.
19 Kwani hatakubali kwamba muishi katika maovu yenu, kuangamiza watu wake.
Ninawaambia, Hapana; atawaruhusu Walamani wawaangamize watu wake wote
ambao wanaitwa watu wa Nefi, ikiwa ingewezekana kwamba wangeanguka katika
dhambi na maovu, baada ya kupokea nuru nyingi na ufahamu mwingi kutoka kwa
Bwana Mungu wao;
20 Ndio, baada ya kuwa watu waliopendelewa sana na Bwana; ndio, baada ya
kupendelewa zaidi ya taifa, ukoo, lugha, au watu wengine; baada ya kujulishwa vitu
vyote kulingana na kutaka kwao, na imani yao, na sala, za yale ambayo yamekuwa, na
ambayo yako, na ambayo yatakuja;
21 Baada ya kutembelewa na Roho wa Mungu; baada ya kuzungumza na malaika,
na baada ya kuzungumziwa na sauti ya Bwana; na kuwa na roho ya unabii, na roho
ya ufunuo, na pia vipawa vingi, na kipawa cha kunena kwa lugha, kipawa cha
kuhubiri, na kipawa cha Roho Mtakatifu, na kipawa cha utafsiri;
22 Ndio, na baada ya kukombolewa na Mungu kutoka nchi ya Yerusalemu, kwa
mkono wa Bwana; baada ya kuokolewa kutokana na njaa, na kutoka ugonjwa, na
kila aina ya magonjwa ya aina yote; na baada ya wao kupata nguvu katika vita, ili
wasiangamizwe; baada ya wao kutolewa kutoka utumwa mara kwa mara, na baada
ya kuwekwa na kuhifadhiwa hadi sasa; na wamefanikishwa hadi wakapata utajiri
kwa aina yote ya vitu—
23 Na sasa tazama nawaambia, kwamba kama hawa watu, ambao wamepokea baraka
nyingi kutoka mkono wa Bwana, watakosea kulingana na nuru na ufahamu ambao
wamepokea, ninawaambia kwamba kama itakuwa hivyo, kwamba ikiwa wataanguka
kwenye makosa, itakuwa ni heri kwa Walamani kuliko wao.
24 Kwani tazama, ahadi za Bwana zimenyooshewa Walamani, lakini sio zenu
mkivunja sheria; kwani si Bwana ameahidi waziwazi na kutanganza kwa uthabiti,
kwamba mkimuasi mtaangamizwa kutoka usoni mwa dunia?
25 Na sasa kwa sababu hii, kwamba msiangamizwe, Bwana ametuma malaika wake
kuwatembelea wengi wa watu wake, akiwaambia kwamba lazima waende na
kuwatanganzia watu hawa, wakisema: Tubuni nyinyi, kwani ufalme wa mbinguni
umo mkononi;
26 Na sio baada ya siku nyingi kwamba Mwana wa Mungu atakuja katika utukufu
wake; na utukufu wake utakuwa utukufu wa yule Mzaliwa wa Baba, aliyejaa neema,
haki, na ukweli, mwenye subira, rehema, na uvumilivu, mwepesi kusikia vilio vya
watu wake na kujibu sala zao.

27 Na tazama, anakuja kukomboa wale ambao watabatizwa ubatizo wa toba, kupitia
imani katika jina lake.
28 Kwa hivyo, tayarisheni nyinyi njia ya Bwana, kwani wakati umo mkononi
kwamba watu wote watavuna zawadi za kazi zao, kulingana na vile
walivyokuwa — kama wamekuwa wenye haki watavuna wokovu wa nafsi zao,
kulingana na uwezo na ukombozi wa Yesu Kristo; na kama wamekuwa waovu
watavuna mauti ya nafsi zao, kulingana na uwezo na utumwa wa ibilisi.
29 Sasa tazama, hii ni sauti ya malaika, inayowatangazia watu.
30 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, kwani nyinyi ni ndugu zangu, na inafaa muwe
wapendwa, na inafaa mtende vitendo vya toba, nikiona kwamba mioyo yenu
imeshupazwa kupita kiasi dhidi ya neno la Mungu, na nikiona kwamba nyinyi ni
watu ambao wamepotea na kuanguka.
31 Sasa ikawa kwamba wakati mimi, Alma, nilipozungumza maneno haya, tazama,
watu walinikasirikia kwa sababu niliwaambia kwamba wao walikuwa watu wenye
mioyo migumu na shingo ngumu.
32 Na pia kwa sababu niliwaambia kwamba walikuwa watu waliopotea na
walioanguka, walinikasirikia, na wakatafuta jinsi ya kunikamata, ili wanitie katika
jela.
33 Lakini ikawa kwamba Bwana hakuwaruhusu wanichukue ule wakati na kunitupa
katika jela.
34 Na ikawa kwamba Amuleki aliende, na akaanza kuwahubiria pia. Na sasa
maneno yote ya Amuleki hayajaandikwa, walakini sehemu ya maneno yake
yameandikwa katika kitabu hiki.

## Alma 10

1 Sasa haya ndiyo maneno ambayo Amuleki aliwahubiria watu ambao walikuwa
katika nchi ya Amoniha, akisema:
2 Mimi ni Amuleki; mimi ni mwana wa Gidona, ambaye alikuwa mwana wa
Ishmaeli, ambaye alikuwa uzao wa Aminadi; na alikuwa ni huyo Aminadi ambaye
alitafsiri maandiko ambayo yalikuwa kwenye ukuta wa hekalu, ambayo yaliandikwa
kwa kidole cha Mungu.
3 Na Aminadi alikuwa uzao wa Nefi, ambaye alikuwa ni mwana wa Lehi, ambaye
alitoka nchi ya Yerusalemu, ambaye alikuwa uzao wa Manase, ambaye alikuwa
mwana wa Yusufu aliyeuzwa Misri kwa mikono ya kaka zake.
4 Na tazama, mimi pia sio mtu aliye na heshima ndogo miongoni mwa wote
ambao wananijua; ndio, na tazama, nina jamaa na marafiki wengi, na pia nimepokea
utajiri mwingi kutokana na bidii ya mikono yangu.
5 Walakini, hata baada ya haya yote, sijaelewa sana kuhusu njia za Bwana, na siri
zake na nguvu zake za ajabu. Nilisema kuwa sikuwahi kujua mengi kuhusu vitu hivi;
lakini tazama, nimekosea, kwani nimeona siri zake nyingi na nguvu zake za ajabu;
ndio, hata katika kuhifadhiwa kwa maisha ya watu hawa.
6 Walakini, nilishupaza moyo wangu, kwani niliitwa mara nyingi lakini sikusikia;
kwa hivyo nilijua kuhusu vitu hivi, lakini nisingeweza kuvifahamu; kwa hivyo
nikaendelea kumuasi Mungu, katika uovu wa moyo wangu, hadi siku ya nne ya
mwezi huu wa saba, ambao uko katika mwaka wa kumi wa utawala wa waamuzi.
7 Nilipokuwa nikisafiri kumuona mmoja wa jamaa yangu wa karibu, tazama

malaika wa Bwana alinitokea na kuniambia: Amuleki, rudi nyumbani kwako, kwani
utamlisha nabii wa Bwana; ndio, mtu mtakatifu, ambaye amechaguliwa na Mungu;
kwani amefunga siku nyingi kwa sababu ya dhambi za watu hawa, na ana njaa, na
utamkaribisha katika nyumba yako na utamlisha, na atakubariki wewe na nyumba
yako; na baraka ya Bwana itakuwa juu yako na nyumba yako.
8 Na ikawa kwamba nilitii sauti ya malaika, na nikarudi nyumbani kwangu. Na
nilipokuwa nikienda hapo nilimpata mtu ambaye malaika alikuwa ameniambia:
Wewe utampokea katika nyumba yako — na tazama ni huyu mtu ambaye amekuwa
akiwazungumzia kuhusu vitu vya Mungu.
9 Na malaika aliniambia kuwa yeye ni mtu mtakatifu; kwa hivyo najua kwamba
yeye ni mtu mtakatifu kwa sababu ilisemwa na malaika wa Mungu.
10 Na tena, najua kwamba vitu ambavyo ameshuhudia ni vya kweli; kwani tazama
nawaambia, jinsi vile Bwana anavyoishi, hata hivyo amemtuma malaika wake
kufanya vitu hivi vidhihirishwe kwangu; na amefanya haya wakati huyu Alma
alipoishi katika nyumba yangu.
11 Kwani tazama, ameibariki nyumba yangu, amenibariki, na wanawake wangu, na
watoto wangu, na baba yangu na jamaa yangu; ndio, ameibariki jamaa yangu yote,
na baraka za Bwana zimekaa juu yetu kulingana na maneno ambayo alizungumza.
12 Na sasa, Amuleki alipokuwa amezungumza maneno haya watu walianza
kustaajabu, wakiona kwamba kulikuwa na shahidi zaidi ya mmoja ambaye
alishuhudia kuhusu vitu ambavyo walishutumiwa, na pia kuhusu vitu ambavyo
vitakuja, kulingana na roho ya unabii iliyokuwa ndani yao.
13 Walakini, kulikuwa na wengine miongoni mwao ambao walitaka kuwauliza
maswali, ili wawanase katika maneno yao kwa mitego, ili wapate ushuhuda dhidi
yao, ili wawapeleke mbele ya waamuzi wao ili wahukumiwe kulingana na sheria, na
ili wauawe au kutiwa katika jela, kulingana na makosa ambayo wangewasingizia au
kushuhudia kinyume chao.
14 Sasa ilikuwa ni wale watu ambao walijaribu kuwaangamiza, ambao walikuwa ni
mawakili, ambao waliajiriwa au kuchaguliwa na watu kutekeleza sheria wakati wao
wa hukumu, au katika hukumu ya makosa ya watu mbele ya waamuzi.
15 Sasa hawa mawakili walikuwa na elimu ya udanganyifu na ujanja wa watu; na hii
ni kuwawezesha wawe na ustadi katika kazi yao.
16 Na ikawa kwamba walianza kumuuliza Amuleki maswali, ili wamfanye
achanganye maneno yake, au kukanusha maneno ambayo angezungumza.
17 Sasa hawakujua kwamba Amuleki angeweza kujua mipango yao. Lakini ikawa
kwamba walipoanza kumuuliza maswali, alihisi mawazo yao, na akawaambia: Ee
nyinyi kizazi kiovu na kibaya, nyinyi mawakili na wanafiki, kwani mnajenga msingi
wa ibilisi; kwani mnaweka mitego ya kunasa walio watakatifu wa Mungu.
18 Mnapanga mipango ya kuchafua njia za watakatifu, na kuteremsha ghadhabu ya
Mungu juu ya vichwa vyenu, hata kwa maangamizo ya watu hawa.
19 Ndio, si ni Mosia, ambaye alikuwa mfalme wetu wa mwisho, aliyesema
alipokaribia kutoa ufalme, na hakuwa na yeyote angestahili kupewa, na akasababisha
kwamba watu hawa watawaliwe kwa sauti ya watu — ndio, alisema kwamba kama
wakati utafika ambao sauti ya watu itachagua uovu, yaani, wakati ukifika ambao
watu hawa wataanguka katika dhambi, watakuwa tayari kuangamizwa.
20 Na sasa ninawaambia kwamba Bwana anahukumu maovu yenu vyema; na
anawalilia watu hawa vyema, kwa sauti ya malaika wake: Tubuni nyinyi, tubuni,

kwani ufalme wa mbinguni u karibu.
21 Ndio, kwa wema analia, kwa sauti ya malaika wake kwamba: Mimi nitashuka
chini miongoni mwa watu wangu, na usawa na haki mikononi mwangu.
22 Ndio, na ninawaambia kwamba kama sio sala za wenye haki, walio katika nchi hii
sasa, kwamba mngekuwa mmetembelewa kwa maangamizo kamili; lakini
haingekuwa kwa mafuriko, kama watu katika siku za Nuhu, lakini ingekuwa kwa
njaa, na kwa tauni, na kwa upanga.
23 Lakini ni kwa sala za wale wenye haki kwamba mmeachiliwa; sasa kwa hivyo,
kama mtawafukuza wale wenye haki kutoka miongoni mwenu basi Bwana hatauzuia
mkono wake; lakini katika ghadhabu yake atawateremkia; kisha mtapigwa kwa njaa,
na kwa tauni, na kwa upanga; na wakati u karibu msipotubu.
24 Na sasa ikawa kwamba watu walimkasirikia Amuleki zaidi, na wakalia, na
kusema: Huyu mtu anadharau sheria zetu ambazo ni za haki, na mawakili wetu
wenye busara ambao tumewachagua.
25 Lakini Amuleki aliwanyoshea mkono wake, na kusema kwa nguvu: Ee nyinyi
kizazi kiovu, mbona Shetani ameingia katika mioyo yenu jinsi hii? Kwa nini
mnajitoa kwake na kumruhusu awe na uwezo juu yenu, kufunga macho yenu,
kwamba hamfahamu maneno ambayo yamezungumzwa, kulingana na ukweli wao?
26 Kwani tazama, nimezungumza kinyume cha sheria yenu? Nyinyi hamfahamu;
mnasema kwamba nimezungumza kinyume cha sheria yenu; lakini sikufanya hivyo,
lakini nimeisifu sheria yenu, ambayo inawahukumu.
27 Na sasa tazama, nawaambia, kwamba msingi wa maangamizo ya watu hawa
umeanza kujengwa na mawakili wenu na waamuzi wenu ambao hawana haki.
28 Na sasa ikawa kwamba baada ya Amuleki kuzungumza maneno haya watu
walimpigia makelele, na kusema: Sasa tunajua kwamba huyu mtu ni mtoto wa
ibilisi, kwani ametudanganya; kwani ameishutumu sheria yetu. Na sasa anasema
kwamba hajaishutumu.
29 Na tena, amewashutumu mawakili wetu, na waamuzi wetu.
30 Na ikawa kwamba mawakili waliweka vitu hivi katika mioyo yao ili
wavikumbuke dhidi yake.
31 Na kulikuwa na mmoja miongoni mwao ambaye jina lake lilikuwa Zeezromu.
Sasa yeye alikuwa wa mbele kumshtaki Amuleki na Alma, yeye akiwa mwenye ujuzi
mwingi miongoni mwao, na alikuwa na shughuli nyingi miongoni mwa watu.
32 Sasa lengo la mawakili hawa lilikuwa ni kupata faida; na walipata faida kulingana
na kazi yao.

## Alma 11

1 Sasa ilikuwa kwenye sheria ya Mosia kwamba kila mtu ambaye alikuwa mwamuzi wa
sheria, au wale waliochaguliwa kuwa waamuzi, wapokee mshahara kulingana na
muda ule ambao waliutumia katika kufanya uamuzi kwa wale walioletwa mbele yao
kuhukumiwa.
2 Sasa kama mtu alidaiwa na mwingine, na akakataa kulipa deni ambalo alidaiwa,
alishitakiwa kwa mwamuzi; na mwamuzi alitekeleza uwezo wake, na akawatuma
askari ili yule mtu aletwe mbele yake; na akamhukumu yule mtu kulingana na sheria
na ushahidi uliotolewa dhidi yake, na hivyo mtu huyo alilazimishwa kulipa deni
lake, au avuliwe, au aondolewe miongoni mwa watu kama mwizi na mporaji.

3 Na mwamuzi alipokea kwa mshahara wake kulingana na wakati
aliotumia—senina ya dhahabu kwa siku, au senumu ya fedha, ambayo ni sawa na
senina ya dhahabu; na hii ni kulingana na sheria ambayo ilitolewa.
4 Sasa haya ndio majina ya vipande vyao tofauti vya dhahabu, na fedha zao,
kulingana na thamani yao. Na majina yalitungwa na Wanefi, kwani hawakufuata
mpango wa Wayahudi ambao walikuwa Yerusalemu; wala hawakupima kulingana
na mpango wa Wayahudi; lakini walibadilisha vipimo vyao na mpango wao,
kulingana na mawazo na hali ya watu, katika kila kizazi, hadi utawala wa waamuzi,
ambao waliimarishwa na mfalme Mosia.
5 Sasa mpango huo ulikuwa huu—senina ya dhahabu, seoni ya dhahabu, shumu ya
dhahabu, na limnahi ya dhahabu.
6 Senumu ya fedha, amnori ya fedha, ezromu ya fedha, na onti ya fedha.
7 Senumu ya fedha ilikuwa ni sawa na senina ya dhahabu, na zote zilikuwa ni sawa
na kipimo kimoja cha shayiri, na pia kipimo cha kila aina ya nafaka.
8 Sasa kiasi cha seoni ya dhahabu kilikuwa na thamani mara mbili ya senina.
9 Na shumu ya dhahabu ilikuwa na thamani mara mbili ya seoni.
10 Na limnahi ya dhahabu ilikuwa na thamani ya hizo zote.
11 Na amnori ya fedha ilikuwa kuu kama senumu mbili.
12 Na ezromu ya fedha ilikuwa kuu kama senumu nne.
13 Na onti ilikuwa kuu kama hizo zote.
14 Sasa hivi ndivyo vipimo vya chini vya mpango wao—
15 Shibloni ni nusu ya senumu; kwa hivyo, shibloni moja kwa nusu kipimo cha
shayiri.
16 Na shiblumu ni nusu ya shibloni.
17 Na lea ni nusu ya shiblumu.
18 Sasa hii ndio idadi yao, kulingana na mpango wao.
19 Sasa antioni ya dhahabu ilikuwa ni sawa na shibloni tatu.
20 Sasa, ilikuwa ni kwa lengo la kufaidika, kwa sababu walipokea mshahara wao
kulingana na kazi yao, kwa hivyo, waliwachochea watu kufanya ghasia, na kila aina
ya fujo na uovu, ili wapate kazi nyingi, ili wapate pesa kulingana na kesi ambazo
zililetwa mbele yao; kwa hivyo waliwachochea watu dhidi ya Alma na Amuleki.
21 Na huyu Zeezromu alianza kumhoji Amuleki, akisema: Je, utaweza kunijibu
maswali machache ambayo nitakuuliza? Sasa Zeezromu alikuwa ni mtu aliyekuwa
na ujuzi katika mipango ya ibilisi, ili aangamize yale ambayo yalikuwa mema; kwa
hivyo, akamwambia Amuleki: Utajibu maswali ambayo nitakuuliza?
22 Na Amuleki akamwaambia: Ndio, kama itakuwa kulingana na Roho wa Bwana,
aliye ndani yangu; kwani sitasema chochote ambacho ni kinyume cha roho wa
Bwana. Na Zeezromu akamwambia: Tazama, hapa kuna onti sita za fedha, na
nitakupa hizi zote ukikana uwepo wa Kiumbe Mkuu.
23 Sasa Amuleki alisema: Ewe mtoto wa jahanamu, kwa nini unanijaribu? Hujui
kwamba wale wenye haki hawakubali majaribio kama haya?
24 Unaamini kwamba hakuna Mungu? Nakuambia, La, wewe unajua kwamba
Mungu yupo, lakini unapenda pesa zaidi yake.
25 Na sasa wewe umenidanganya mbele ya Mungu wangu. Unaniambia—Tazama
hizi onti sita ambazo zina thamani kuu, nitakupatia—wakati ulikuwa umepanga
moyoni mwako kuziweka kutoka kwangu; na ilikuwa ni haja yako tu kwamba mimi
nimkane Mungu wa kweli na anayeishi, ili uwe na sababu ya kuniangamiza. Na sasa

tazama, kwa sababu ya huu uovu mkuu utapokea upatanisho wako.

26 Na Zeezromu akamwambia: Wewe unasema kwamba kuna Mungu wa kweli na anaiyeshi?

27 Na Amuleki akasema: Ndio, kuna Mungu wa kweli na anayeishi.

28 Sasa Zeezromu akasema: Kuna zaidi ya Mungu mmoja?

29 Na akajibu, Hapana.

30 Sasa Zeezromu akasema kwake tena: Ni vipi unavyojua vitu hivi?

31 Na akasema: Malaika amenijulisha.

32 Na Zeezromu akasema tena: Ni nani atakayekuja? Ni Mwana wa Mungu?

33 Na akamwambia, Ndio.

34 Na Zeezromu akasema tena: Ataokoa watu wake katika dhambi zao? Na Amuleki akajibu na kumwambia: Nakwambia kwamba hatafanya hivyo, kwani yeye hawezi kukana neno lake.

35 Sasa Zeezromu akawaambia watu: Hakikisha kwamba mnakumbuka hivi vitu; kwani alisema kwamba kuna Mungu mmoja pekee; na bado amesema kwamba Mwana wa Mungu atakuja, lakini kwamba hataokoa watu wake — kama aliye na mamlaka ya kumwamuru Mungu.

36 Sasa Amuleki akamwambia tena: Tazama umesema uwongo, kwani umesema kwamba nilizungumza kama yule aliye na mamlaka ya kumwamuru Mungu kwa sababu nilisema kwamba hataokoa watu wake katika dhambi zao.

37 Na ninakwambia tena kwamba yeye hawezi kuwaokoa katika dhambi zao; kwani siwezi kukanusha neno lake, na amesema kwamba hakuna kitu chochote kichafu kitakachorithi ufalme wa mbinguni; kwa hivyo, vipi mtakavyookolewa, msiporithi ufalme wa mbinguni? Kwa hivyo, hamwezi kuokolewa katika dhambi zenu.

38 Sasa Zeezromu akamwambia tena: Mwana wa Mungu ni yule Baba wa Milele?

39 Na Amuleki akamwambia: Ndio, yeye ndiye Baba wa Milele wa mbingu na dunia, na vitu vyote vilivyo ndani yao; yeye ndiye mwanzo na mwisho, wa kwanza na wa mwisho;

40 Na atakuja ndani ya ulimwengu kuwakomboa watu wake; na atajitwaa dhambi za wale wanaoamini katika jina lake; na hawa ndio watakaopokea uzima wa milele, na wokovu hautamjia mwingine yeyote.

41 Kwa hivyo waovu wataishi kama kwamba hakukuweko na ukombozi, ila tu kufanywa huru kutokana na kamba za kifo; kwani tazama, siku inakuja ambayo wote watafufuka kutoka kwa wafu na kusimama mbele ya Mungu, na watahukumiwa kulingana na kazi zao.

42 Sasa, kuna kifo ambacho kinaitwa kifo cha muda; na kifo cha Kristo kitafungua kanda za kifo hiki cha muda, ili wote wafufuliwe kutoka kifo hiki cha muda.

43 Roho na mwili vitaungwa tena katika hali yake ya ukamilifu; viungo vyote vitarudishwa katika sehemu zao kamili, kama vile tulivyo sasa; na tutaletwa kusimama mbele ya Mungu, tukijua kama vile tujuavyo sasa, na kukumbuka hatia zetu zote.

44 Sasa, huu urejesho utakuwa kwa wote, wote wazee na vijana, wote wafungwa na huru, waume na wake, wote waovu na wenye haki; na hakuna hata unywele wa vichwa vyao utakaopotea; lakini kila kitu kitarejeshwa mahali pake kamili, kama vile ilivyo sasa, au katika mwili, na utaletwa na kusimamishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo Mwana, na Mungu Baba, na Roho Mtakatifu, ambao ni Mungu mmoja wa Milele, kuhukumiwa kulingana na vitendo vyao, kama ni vyema au ni viovu.

45 Sasa, tazama, nimekuzungumzia kuhusu kifo cha mwili huu wa muda, na pia kuhusu ufufuo wa mwili huu wa muda. Ninakwambia kwamba mwili huu wa kufa utafufuliwa na kwa mwili usiokufa, yaani kutoka kifo, hata kufufuka kifo cha kwanza hadi katika uhai, kwamba wasife tena; roho zao zikiungana na miili yao, wala hazitatenganishwa tena; hivyo mtu wote utakuwa wa kiroho na asiyekufa, kwamba hataona uharibifu tena.
46 Sasa, Amuleki alipomaliza kuzungumza maneno haya watu walianza kustaajabia tena, na pia Zeezromu akaanza kutetemeka. Na hivyo maneno ya Amuleki yakamalizika, au haya ndiyo yote ambayo nimeandika.

## Alma 12

1 Sasa Alma, alipoona kwamba maneno ya Amuleki yalimnyamazisha Zeezromu, kwani aliona kwamba Amuleki alimpata katika uwongo wake na ujanja wake ili amwangamize, na alipoona kwamba alianza kutetemeka katika dhamira yake ya hatia, alifungua kinywa chake na akaanza kumzungumzia, na kuimarisha maneno ya Amuleki, na kumwelezea mambo zaidi, au kuyafungua maandiko zaidi ya vile Amuleki alivyokuwa amefanya.
2 Sasa maneno ambayo Alma alimwelezea Zeezromu yalisikika na watu waliokuwa karibu; kwani umati ulikuwa mkuu, na alisema hivi:
3 Sasa Zeezromu, nikiona kwamba wewe umeshikwa katika uwongo na ujanja wako, kwani wewe hukudanganya watu pekee lakini wewe umemdanganya Mungu; kwani tazama, anajua mawazo yako yote, na unaona kwamba mawazo yako yamefanywa kujulikana kwetu na Roho yake;
4 Na wewe unaona kwamba tunajua kuwa mpango wako ulikuwa ni mpango wa hila, kama hila ya ibilisi, kwani ulitaka kudanganya na kulaghai watu hawa ili uwafanye wawe dhidi yetu, na watufanyie dharau na kututupa nje—
5 Sasa huu ulikuwa ni mpango wa adui wako, na ameitumia nguvu yake ndani yako. Sasa nataka ukumbuke kwamba yale ambayo ninakwambia pia nawaambia wote.
6 Na tazama nakwambia kwamba huu ulikuwa ni mtego wa adui, ambao ameutega ili awanase watu hawa, ili akutie katika utumwa wake, ili akuzingire na minyororo yake, ili akufunge chini kwa maangamizo yasiyo na mwisho, kulingana na nguvu za utumwa wake.
7 Sasa Alma alipokuwa amezungumza maneno haya, Zeezromu alianza kutetemeka zaidi, kwani alisadikishwa zaidi kuhusu nguvu za Mungu; na pia alisadikishwa kwamba Alma na Amuleki walimfahamu, kwani alisadikishwa kwamba walijua mawazo na nia za moyo wake; kwani walipewa uwezo kwamba wajue vitu hivi kulingana na roho ya unabii.
8 Na Zeezromu akaanza kuwauliza kwa bidii, ili aweze kujua zaidi kuhusu ufalme wa Mungu. Na akamwambia Alma: Ni nini maana ya haya ambayo Amuleki amesema kuhusu ufufuo wa wafu, kwamba wote watafufuka kutoka kwa wafu, wenye haki na wasio na haki, na kwamba watasimamishwa mbele ya Mungu ili wahukumiwe kulingana na vitendo vyao?
9 Na sasa Alma akaanza kumwelezea vitu hivi, akisema: Imepewa kwa wengi kujua siri za Mungu; walakini wamewekwa chini ya amri kali kwamba hawatatoa zaidi ya yale maneno ambayo amewapatia watoto wa watu, kulingana tu na utiifu na bidii

ambayo wanampatia.

10 Na kwa hivyo, yule ambaye atashupaza moyo wake, huyo atapokea sehemu ndogo ya neno; na yule ambaye hatashupaza moyo wake, huyo anapewa sehemu kubwa ya neno, hadi awezeshwe kufahamu siri za Mungu hadi azielewe kikamilifu.

11 Na wale watakaoshupaza mioyo yao, wao watapewa sehemu ndogo ya neno hadi wasijue lolote kuhusu siri zake; na kisha wanatekwa nyara na ibilisi, na kuongozwa kwa pendekezo lake katika maangamizo. Sasa hii ndio maana ya minyororo ya jahanamu.

12 Na Amuleki amezungumza waziwazi kuhusu mauti, na kufufuliwa kutoka hali hii ya muda hadi katika hali ya mwili usiokufa, na kusimamishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, tuhukumiwe kulingana na vitendo vyetu.

13 Kisha kama mioyo yetu imeshupazwa, ndio, kama tumeshupaza mioyo yetu dhidi ya neno, kadiri kwamba halipo ndani yetu, hapo hali yetu itakuwa mbaya, kwani ndipo tutahukumiwa.

14 Kwani maneno yetu yatatuhukumu, ndio, vitendo vyetu vyote vitatuhukumu; hatutakuwa bila waa; na pia mawazo yetu yatatuhukumu; na hatutaweza kumwangalia Mungu wetu katika hali hii mbaya; na tutakuwa na furaha kama tungeweza kuamuru miamba na milima ituangukie ili itufiche kutoka kwa uwepo wake.

15 Lakini hii haiwezekani; lazima tuje na kusimama mbele yake katika utukufu wake, na katika nguvu zake, na uwezo wake, fahari, na mamlaka, na kukubali kwa aibu yetu isiyo na mwisho kwamba hukumu zake zote ni za haki; kwamba yeye ni wa haki katika kazi zake zote, na kwamba yeye huwarehemu watoto wa watu, na kwamba ana nguvu zote za kumwokoa kila mtu ambaye anaamini kwa jina lake na kuzaa matunda ya toba.

16 Na sasa tazama, nawaambia ndipo mauti yanakuja, hata mauti ya pili, ambayo ni mauti ya kiroho; halafu itakuwa wakati kwamba yeyote atakayefariki katika dhambi zake, kama vile mauti ya muda, atakufa pia mauti ya kiroho; ndio, atafariki kulingana na vitu vya utakatifu.

17 Kisha ndio wakati ambao mateso yao yatakuwa kama ziwa la moto liwakalo kwa kibereti, ambalo ndimi zake hupaa juu milele na milele; na kisha utakuwa wakati ambao watafungwa chini katika maangamizo yasiyo na mwisho, kulingana na nguvu na utumwa wa Shetani, yeye akiwa amewasalimisha kulingana na nia yake.

18 Kisha, nawaambia, watakuwa ni kama hapakuwa na ukombozi uliofanywa; kwani hawawezi kukombolewa kulingana na haki ya Mungu; na hawawezi kufariki; kwani hakutakuwa na uharibifu;

19 Sasa ikawa kwamba baada ya Alma kumaliza kuzungumza maneno haya, watu walianza kustaajabika zaidi;

20 Lakini kulikuwa na mmoja ambaye aliitwa Antiona, ambaye alikuwa ni mtawala mkuu miongoni mwao, alikuja mbele na kumwambia: Ni nini hii ambayo umesema, kwamba mwanadamu atafufuliwa kutoka kwa wafu na kubadilishwa kutoka hii hali ya muda hadi katika hali ya mwili usiokufa, kwamba nafsi haitakufa?

21 Maandiko yanamaanisha nini, ambayo yanasema kwamba Mungu aliweka makerubi na upanga unaowaka moto mashariki mwa bustani ya Edeni, isiwe wazazi wetu wa kwanza waingie na kula tunda la mti wa uzima, na kuishi milele? Na hivyo tunaona kwamba haikuwezekana kwamba wawe na nafasi ya kuishi milele.

22 Sasa Alma akamwambia: Hiki ndicho kitu ambacho nilikaribia kuelezea. Sasa

tunaona kuwa Adamu alianguka kwa kula tunda lililokatazwa, kulingana na neno la
Mungu; na hivyo tunaona, kwamba kwa kuanguka kwake, wanadamu wote wakawa
watu waliopotea na walioanguka.
23 Na sasa tazama, nakuambia kama ingewezekana Adamu kula tunda la mti wa
uzima wakati ule, hakungekuwa na mauti, na neno lingekuwa bure, na kumfanya
Mungu mwongo, kwani alisema: Iwapo bila shaka utakufa.
24 Na tunaona kwamba mauti yanampata mwanadamu, ndio, mauti ambayo
yamezungumziwa na Amuleki, ambayo ni mauti ya muda; walakini mwanadamu
alipewa nafasi ya kutubu; kwa hivyo maisha haya yakawa hali ya kujaribiwa; wakati
wa kujitayarisha kukutana na Mungu; wakati wa kujitayarisha kwa ile hali isiyo na
mwisho ambayo imezungumziwa nasi, ambayo ni baada ya ufufuo wa wafu.
25 Sasa, kama hakungekuwa na mpango wa ukombozi, ambao ulipangwa tangu
msingi wa ulimwengu, hakungekuwa na ufufuo wa wafu; lakini kulikuwa na
mpango wa ukombozi ambao ulipangwa, ambao utawezesha ufufuo wa wafu,
ambao tayari umezungumziwa.
26 Na sasa tazama, kama ingewezekana kwamba wazazi wetu wa kwanza wale
kutoka kwa mti wa uzima wangekuwa wenye taabu milele, bila kuwa na hali ya
matayarisho; na hivyo mpango wa ukombozi ungeangamizwa, na neno la Mungu
lingekuwa bure, bila matokeo.
27 Lakini tazama, haikuwa hivyo; lakini ilipangiwa kwamba lazima wanadamu
wafariki; na baada ya kifo, lazima wahukumiwe, hata hukumu ile ambayo
tumeizungumzia, ambayo ni mwisho.
28 Na baada ya Mungu kupanga kwamba hivi vitu lazima vimpate mwanadamu,
tazama, akaona kwamba ilikuwa inafaa mwanadamu ajue kuhusu vile vitu ambavyo
alikuwa amewapangia;
29 Kwa hivyo aliwatuma malaika wazungumze nao, ambao walisababisha
wanadamu kuona utukufu wake.
30 Na wakaanza tangu wakati ule kulilingana jina lake; kwa hivyo Mungu
alizungumza na wanadamu, na akawafahamisha mpango wa ukombozi, ambao
ulikuwa umetayarishwa tangu msingi wa ulimwengu; na aliwafahamisha haya
kulingana na imani yao na toba na vitendo vyao vitakatifu.
31 Kwa hivyo, akawapa wanadamu amri, baada ya wao kuvunja amri za kwanza
zilizokuwa za vitu vya muda, na kuwa kama miungu, wakifahamu mema na maovu,
na kujiweka katika hali ya kutenda, au kuwekwa katika hali ya kutenda kulingana na
nia zao na furaha yao, kama kutenda maovu au kutenda mema—
32 Kwa hivyo Mungu aliwapa amri, baada ya kuwafahamisha mpango wa ukombozi,
ili wasitende maovu, adhabu yake ikiwa ni mauti ya pili, ambayo ni mauti yasiyo na
mwisho kulingana na vitu vya haki; kwani kama huo mpango wa ukombozi
haungekuwa na nguvu, kwani vitendo vya haki havingeweza kuangamizwa,
kulingana na wema wa juu wa Mungu.
33 Lakini Mungu aliwaita wanadamu, kwa jina la Mwana wake, (huu ukiwa mpango
wa ukombozi ambao ulikuwa umepangwa) akisema: Ikiwa mtatubu na msishupaze
mioyo yenu, nitawarehemu, kwa Mwana wangu wa Pekee;
34 Kwa hivyo, yeyote atakayetubu, na asishupaze moyo wake, atakuwa na haki ya
kupokea rehema kwa Mwana wangu wa Pekee, kwa ondoleo la dhambi zake; na
hawa wataingia katika pumziko langu.
35 Na yeyote atakayeshupaza moyo wake na kutenda maovu, tazama, naapa katika

ghadhabu yangu kwamba hataingia katika pumziko langu.
36 Na sasa, ndugu zangu, tazameni, nawaambia, kwamba ikiwa mtashupaza mioyo
yenu hamtaingia katika pumziko la Bwana; kwa hivyo dhambi zenu zinamchokoza
na kumfanya awateremshie ghadhabu yake kama vile alivyochokozwa mara ya
kwanza, ndio, kulingana na neno lake katika uchokozi wa mwisho na wa kwanza,
kwa maangamizo yasiyo na mwisho ya nafsi zenu; kwa hivyo, kulingana na neno
lake, hadi kifo cha mwisho, na pia kile cha kwanza.
37 Na sasa, ndugu zangu, mkiona tunajua hivi vitu, na ni vya kweli, hebu tutubu, na
tusishupaze mioyo yetu, kwamba tusimkasirishe Bwana Mungu wetu akateremsha
ghadhabu yake juu yetu katika amri zake za pili ambazo ametupatia; lakini hebu
tuingie katika pumziko la Mungu, ambalo limetayarishwa kulingana na neno lake.

# Alma 13

1 Na tena, ndugu zangu, ningetaka nikumbushe fikira zenu kuhusu ule wakati ambao
Bwana Mungu aliwapatia watoto wake amri hizi; na ningetaka mkumbuke kwamba
Bwana Mungu aliwatawaza makuhani, kulingana na mpango wake mtakatifu,
ambao ni ule mpango wa Mwana wake, kufunza watu vitu hivi.
2 Na makuhani hao walitawazwa kulingana na mpango wa Mwana wake, katika
hali ambayo watu wangejua ni vipi watakavyomtumainia Mwana wake kwa
ukombozi.
3 Na hivi ndivyo jinsi walivyotawazwa—wakiitwa na kutayarishwa tangu msingi
wa ulimwengu kulingana na ufahamu wa mbeleni wa Mungu, kwa ajili ya imani yao
kuu na vitendo vyao vyema; mwanzoni wakiruhusiwa kuchagua baina ya mema na
maovu; kwa hivyo wao wakiwa wamechagua mema, na kufanya mazoezi ya imani
kuu, wameitwa kwa mwito mtakatifu, ndio, kwa ule mwito mtakatifu ambao
ulitayarishwa, na kulingana na, matayarisho ya ukombozi wao.
4 Na hivyo wameitwa kwa mwito huu mtakatifu kwa ajili ya imani yao, wakati
wengine wangemkataa Roho wa Mungu kwa ajili ya ugumu wa mioyo yao na upofu
wa fikira zao, wakati, kama isingekuwa kwa sababu hii wangekuwa na mamlaka
makuu kama ndugu zao.
5 Au kwa kifupi, hapo mwanzoni walikuwa katika hali sawa na ndugu zao; hivyo
mwito huu mtakatifu ukiwa umetayarishwa tangu msingi wa ulimwengu kwa wale
ambao hawangeshupaza mioyo yao, kupitia na katika upatanisho wa Mwana wa
Pekee, ambaye alitayarishwa—
6 Na hivyo kuitwa na mwito huu mtakatifu, na kutawazwa ukuhani mkuu wa
mpango mtakatifu wa Mungu, kufunza watoto wa watu amri zake, ili nao pia
waingie katika pumziko lake—
7 Ukuhani huu mkuu ukiwa kwa ule mpango wa Mwana wake, mpango ambao
ulikuwa tangu msingi wa ulimwengu; au kwa maneno mengine, haukuwa na
mwanzo wa siku au mwisho wa miaka, ukiwa ulitayarishwa tangu milele hadi milele,
kulingana na ufahamu wake wa mbele wa vitu vyote—
8 Sasa walitawazwa kwa njia hii—wakiwa wameitwa kwa mwito mtakatifu, na
kutawazwa kwa agizo takatifu, na kuchukua ukuhani mkuu juu yao wa mpango
mtakatifu, ambao ni mwito, na agizo, na ukuhani mkuu, usio na mwanzo au
mwisho—
9 Hivyo wakawa makuhani wakuu milele, kulingana na mpango mtakatifu wa

Mwana wa Pekee wa Baba, ambaye hana mwanzo wa siku au mwisho wa miaka,
ambaye amejaa neema, ukweli, na haki. Na hivyo ndivyo ilivyo. Amina.
10 Sasa, kama vile nilivyosema kuhusu mpango huu mtakatifu, au huu ukuhani
mkuu, kulikuwa na wengi ambao walitawazwa na kuwa makuhani wakuu wa
Mungu; na ilikuwa kwa ajili ya imani yao kuu na toba, na haki yao mbele ya Mungu,
wao wakichagua kutubu na kutenda utakatifu badala ya kuangamia;
11 Kwa hivyo waliitwa kulingana na mpango huu mtakatifu, na wakatakaswa, na
mavazi yao yakaoshwa na kuwa meupe kupitia damu ya Mwanakondoo.
12 Na wao, baada ya kutakaswa na Roho Mtakatifu, na mavazi yao kufanywa
meupe, yakiwa safi na bila doa mbele ya Mungu, hawangetazama dhambi bila
kukerwa; na kulikuwa na wengi, wengi sana, ambao walifanywa safi na kuingia
katika pumziko la Bwana Mungu wao.
13 Na sasa, ndugu zangu, ningetaka kwamba mjinyeyekeze mbele ya Mungu, na
mzae matunda yanayostahili toba, ili nyinyi pia muingie katika hilo pumziko.
14 Ndio, jinyenyekeeni hata kama wale watu waliokuwa katika siku za Melkizedeki,
ambaye pia alikuwa kuhani mkuu kulingana na ule mpango ambao
nimeuzungumzia, ambaye pia aliuchukua ukuhani mkuu milele.
15 Na ilikuwa ni kwa huyu Melkizedeki ambaye Ibrahimu alilipa zaka; ndio, hata
baba yetu Ibrahimu alilipa zaka ya fungu la kumi ya mali yote aliyokuwa nayo.
16 Sasa haya maagizo yalitolewa kwa namna hii, ili watu wamtazamie Mwana wa
Mungu, ambayo ikiwa ni mfano wa mpango wake, au ukiwa mpango wake, na ili
wamtazamie mbele kwake kwa ondoleo la dhambi zao, ili waingie katika pumziko la
Bwana.
17 Sasa huyu Melkizedeki alikuwa mfalme katika nchi ya Salemu; na watu wake
walikuwa wametumbukia katika uovu na machukizo; ndio, wote walikuwa
wamepotea njia; walikuwa wamejaa kila aina ya uovu;
18 Lakini Melkizedeki akiwa na imani kuu, na kuipokea ofisi ya ukuhani mkuu
kulingana na mpango mtakatifu wa Mungu, aliwahubiria watu wake toba. Na
tazama, walitubu; na Melkizedeki aliimarisha amani nchini katika siku zake; kwa
hivyo aliitwa mwana mfalme wa amani, kwani alikuwa mfalme wa Salemu; na
alitawala chini ya baba yake.
19 Sasa, kulikuwa na wengi mbele yake, na pia kulikuwa na wengi baadaye, lakini
hapakuwa na yeyote aliyekuwa mkuu zaidi; kwa hivyo, wamemtaja yeye zaidi.
20 Sasa hakuna haja ya kurudia jambo hili; yale ambayo nimesema yametosha.
Tazama, maandiko yako mbele yenu; mkiyapinga itakuwa ni kwa maangamizo yenu.
21 Na sasa ikawa kwamba baada ya Alma kusema maneno haya kwao, alinyosha
mkono wake kwao na kuongea kwa sauti kuu, akisema: Sasa ndio wakati wa kutubu,
kwani siku ya wokovu inakaribia;
22 Ndio, na sauti ya Bwana, kwa vinywa vya malaika, inatangazia mataifa yote; ndio,
inaitangaza, kwamba wawe na habari njema kuu ya shangwe kuu; ndio, anaitangaza
habari hii njema miongoni mwa watu wake wote, ndio, hata kwa wale ambao
wametawanyika kote usoni mwa dunia kwa hivyo wametujia.
23 Na wametufahamisha kwa misemo iliyo wazi, ili tufahamu, ili tusikose; na hii ni
kwa sababu sisi ni wazururaji katika nchi ngeni; kwa hivyo, tumeheshimiwa zaidi,
kwani tumeelezewa habari hii njema katika pande zote za shamba letu.
24 Kwani tazama, malaika wanawatangazia wengi sasa katika nchi yetu; na hii ni
kwa lengo la kutayarisha mioyo ya watoto wa watu ili wapokee neno lake

atakaporudi katika utukufu wake.
25 Na sasa tunasubiri tu kusikia habari njema tukihubiriwa kwa vinywa vya malaika,
kuhusa kuja kwake; kwani wakati unakuja, na hatujui ni lini. Namwomba Mungu
kwamba iwe katika siku zangu; lakini ikiwa sasa au baadaye, nitaifurahia.
26 Na itafahamishwa kwa watu wenye haki na watakatifu, kwa vinywa vya malaika,
wakati wa kuja kwake, kwamba maneno ya babu zetu yatimizwe, kulingana na yale
ambayo waliyozungumza kumhusu, ambayo yalikuwa ni kulingana na roho ya
unabii iliyokuwa ndani yao.
27 Na sasa, ndugu zangu, natamani kutoka sehemu za ndani kabisa za moyo wangu,
ndio, kwa wasiwasi mwingi na hata kwa uchungu, kwamba msikilize maneno yangu,
na mtupe dhambi zenu, na kwamba msiahirishe siku ya toba yenu;
28 Lakini kwamba mtajinyenyekeza mbele ya Bwana, na mliite jina lake takatifu, na
kukesha na kusali daima, kwamba msijaribiwe zaidi ya yale ambayo mnaweza
kuvumilia, na hivyo mwongozwe na Roho Mtakatifu, katika kuwa wanyenyekevu,
wapole, watiifu, wenye subira, wenye upendo na wenye uvumilivu;
29 Mkimwamini Bwana; mkitumaini kwamba mtapokea uzima wa milele; mkiwa
na upendo wa Mungu daima katika mioyo yenu, kwamba muinuliwe katika siku ya
mwisho na muingie katika pumziko lake.
30 Na ikiwezekana Bwana awape toba, kwamba msijiteremshie ghadhabu yake,
kwamba msifungiwe na minyororo ya jahanamu, kwamba msipate mauti ya pili.
31 Na Alma aliwazungumzia watu maneno mengi, ambayo hayajaandikwa katika
kitabu hiki.

# Alma 14

1 Na ikawa kwamba baada ya kumaliza kuzungumzia watu wengi wao waliamini
maneno yake, na wakaanza kutubu, na kupekua maandiko.
2 Lakini sehemu yao kubwa ilitaka kuwaangamiza Alma na Amuleki; kwani
walimkasirikia Alma, kwa sababu ya vile alivyomzungumzia Zeezromu maneno
waziwazi; na pia walisema kwamba Amuleki alikuwa amewadanganya, na alikuwa
amedharau sheria yao na pia mawakili wao na waamuzi wao.
3 Na pia waliwakasirikia Alma na Amuleki; na kwa sababu waliwashuhudia uovu
wao waziwazi, walitaka kuwaondoa kwa siri.
4 Lakini ikawa kwamba hawakufanya hivyo; lakini waliwachukua na kuwafunga
kwa kamba imara, na kuwapeleka mbele ya mwamuzi mkuu wa nchi.
5 Na watu wakaenda na kushuhudia dhidi yao — wakishuhudia kwamba walikuwa
wameidharau sheria, na mawakili wao na waamuzi wa nchi, na pia watu wote ambao
walikuwa katika nchi; na pia wakashuhudia kwamba kuna Mungu mmoja pekee, na
kwamba atamtuma Mwana wake miongoni mwa watu, lakini kwamba hatawaokoa;
na watu waliwasingizia Alma na Amuleki vitu vingi kama hivi. Sasa haya yalifanywa
mbele ya mwamuzi mkuu wa nchi.
6 Na ikawa kwamba Zeezromu alishangazwa na maneno ambayo yalikuwa
yamezungumzwa; na pia alijua kuhusu upofu wa mawazo, ambao alikuwa
amesababisha miongoni mwa watu kwa maneno yake ya uwongo; na nafsi yake
ikaanza kukerwa na dhamira yake kuhusu hatia zake; ndio, alianza kuzingirwa na
uchungu wa jahanamu.
7 Na ikawa kwamba alianza kuwalilia watu, akisema: Tazameni, mimi nina hatia,

na watu hawa hawana lawama mbele ya Mungu. Na akaanza kuwatetea tangu ule wakati na kuendelea; lakini walimfanyia dharau, wakisema: Je, wewe nawe pia umepagawa na ibilisi? Na wakamtemea mate, na kumtupa nje kutoka miongoni mwao, na pia wale wote ambao walikuwa wameamini maneno ambayo yalikuwa yamezungumzwa na Alma na Amuleki; na wakawatupa nje, na kutuma watu kuwapiga mawe.

8 Na wakawaleta wake na watoto wao pamoja, na yeyote aliyeamini au aliyekuwa amefunzwa kuliamini neno la Mungu walisababisha kwamba atupwe motoni; na pia walileta kumbukumbu zao zilizokuwa na maandiko, na kuyatupa motoni pia, ili yachomwe na kuangamizwa kwa moto.

9 Na ikawa kwamba waliwachukua Alma na Amuleki, na kuwabeba na kuwapeleka mahali pa mateso, ili washuhudie wale ambao waliangamizwa kwa kuchomwa kwa moto.

10 Na Amuleki alipoona wanawake na watoto wakiungua kwenye moto, na yeye pia alipatwa na maumivu; na akamwambia Alma: Kwa nini tunashuhudia mkasa huu mwovu? Kwa hivyo tunyooshe mikono yetu, na tutumie nguvu za Mungu tulizo nazo, na tuwaokoe kutoka ndimi za moto.

11 Lakini Alma akamwambia: Roho inanizuia kwamba nisinyooshe mkono wangu; kwani tazama Bwana mwenyewe anawapokea, kwa utukufu; na anakubali wafanye kitu hiki, au kwamba watu wafanye kitu hiki kwao, kulingana na ugumu wa mioyo yao, ili hukumu ambayo atawateremshia katika ghadhabu yake iwe ya haki; na damu ya wale ambao hawana hatia itakuwa ushahidi dhidi yao, ndio, na italia sana dhidi yao katika siku ya mwisho.

12 Sasa Amuleki akamwambia Alma: Tazama, pengine watatuchoma sisi pia.

13 Na Alma akasema: Hebu na iwe kulingana na nia ya Bwana. Lakini, tazama, kazi yetu haijakwisha; kwa hivyo hawawezi kutuchoma.

14 Sasa ikawa kwamba baada ya miili ya wale ambao walikuwa wametupwa motoni kuchomeka, na pia yale maandishi ambayo yalikuwa yametupwa pamoja nao, mwamuzi mkuu wa nchi alikuja na kusimama mbele ya Alma na Amuleki, wakiwa wamefungwa; na akawapiga makofi katika mashavu yao, na kuwaambia: Baada ya yale ambayo mmeona, bado mtahubiria watu hawa, kwamba watatupwa katika ziwa la moto ambalo linawaka na kiberiti?

15 Tazama, mnaona kwamba hamkuwa na uwezo wa kuwaokoa wale ambao walikuwa wametupwa motoni; wala Mungu hakuwaokoa kwa sababu walikuwa wa imani yenu. Na mwamuzi akawapiga tena katika mashavu yao, na kuwauliza: Je, mna nini cha kujisemea?

16 Sasa huyu mwamuzi alikuwa mfuasi wa dini na imani ya Nehori, ambaye alimuua Gideoni.

17 Na ikawa kwamba Alma na Amuleki hawakumjibu chochote; na akawapiga tena, na akawakabidhi kwa polisi ili watupwe katika gereza.

18 Na walipokuwa wametupwa katika jela kwa siku tatu, kulitokea mawakili wengi, na waamuzi, na makuhani, na walimu, ambao walikuwa waumini wa Nehori; na walikuja katika gereza kuwaona, na kuwauliza maswali kuhusu maneno mengi; lakini hawakuwajibu lolote.

19 Na ikawa kwamba mwamuzi alisimama mbele yao, na kusema: Kwa nini hamjibu maneno ya watu hawa? Hamjui kwamba nina uwezo wa kuwatupa kwenye moto? Na akawaamuru wazungumze; lakini hawakujibu lolote.

20 Na ikawa kwamba waliondoka na kwenda zao, lakini walirudi kesho yake; na
yule mwamuzi pia akawapiga tena katika mashavu yao. Na wengi walikuja pia, na
kuwapiga, wakisema: Je, mtasimama tena na kuhukumu watu hawa, na kushutumu
sheria yetu? Kama mnao uwezo huu mkuu kwa nini hamjiokoi?
21 Na waliwaambia vitu vingi kama hivi, wakiwasagia meno yao, na kuwatemea
mate, na kusema: Tutakuwa vipi tukilaaniwa?
22 Na vitu vingi kama hivi, ndio, kila aina ya vitu hivi waliwaambia; na hivyo
wakawafanyia mzaha kwa siku nyingi. Na waliwanyima chakula ili wapate njaa, na
maji ili wapate kiu; na pia waliwavua nguo zao ili wawe uchi; na hivyo walifungwa
kwa kamba imara, na kuzuiliwa gerezani.
23 Na ikawa kwamba baada ya wao kuteseka siku nyingi, (na iliikuwa ni siku ya
kumi na mbili, mwezi wa kumi, katika mwaka wa kumi wa utawala wa waamuzi juu
ya watu wa Nefi) kwamba mwamuzi mkuu katika nchi ya Amoniha na wengi wa
walimu wao na mawakili wao walikwenda katika gereza ambamo Alma na Amuleki
walikuwa wamefungwa kwa kamba.
24 Na mwamuzi mkuu akasimama mbele yao, na kuwapiga tena, na kuwaambia:
Kama mnazo nguvu za Mungu jikomboeni kutoka kwa kamba hizi, na kisha
tutaamini kwamba Bwana atawaangamiza hawa watu kulingana na maneno yenu.
25 Na ikawa kwamba wote walienda na kuwapiga, na kuyarudia yale maneno, hata
hadi yule wa mwisho; na wakati yule wa mwisho aliwazungumzia nguvu za Mungu
zikawateremkia Alma na Amuleki, na wakainuka na kusimama kwa miguu yao.
26 Na Alma akalia, na akisema: Ni kwa muda gani ambao tutateseka kwa
masumbuko haya makuu, Ee Bwana? Ee Bwana, tupatie nguvu kulingana na imani
yetu katika Kristo, ambayo itatukomboa. Na wakakata kamba ambazo walikuwa
wamefungwa nazo; na wakati watu walipoona haya, walianza kutoroka, kwani woga
wa kuagamizwa uliwajia.
27 Na ikawa kwamba woga wao ulikuwa mwingi hata kwamba wakainama kwenye
ardhi, na hawakuufikia mlango wa nje wa gereza; na ardhi ikatetemeka sana, na kuta
za gereza zikabomolewa na kuwa sehemu mbili, na hivyo zikaanguka kwenye ardhi;
na yule mwamuzi mkuu, na mawakili, na makuhani, na walimu, wale ambao
walikuwa wamewapiga Alma na Amuleki, waliuawa katika ule mwanguko.
28 Na Alma na Amuleki wakaondoka gerezani, na hawakuumizwa; kwani Bwana
alikuwa amewapatia uwezo, kulingana na imani yao katika Kristo. Na wakatoka
gerezani moja kwa moja; na wakafunguliwa kutoka kamba zao; na gereza ilikuwa
imeanguka kwenye ardhi, na kila nafsi ambayo ilikuwa ndani ya zile kuta, ila tu
Alma na Amuleki, waliuawa; na wakaingia moja kwa moja kwenye mji.
29 Sasa baada ya watu kusikia kelele nyingi walikuja mbio kwa makundi ili wajue
chanzo chake; na walipoona Alma na Amuleki wakitoka nje ya gereza, na kwamba
kuta zake zilikuwa zimeanguka kwenye ardhi, walipatwa na woga mwingi, na
wakatoroka kutoka uwepo wa Alma na Amuleki hata kama vile mbuzi na wana
mbuzi wake huwatoroka simba wawili; na hivyo wakatoroka kutoka uwepo wa
Alma na Amuleki.

## Alma 15

1 Na ikawa kwamba Alma na Amuleki waliamriwa waondoke kutoka ule mji; na
wakaondoka, na kufika hata katika nchi ya Sidomu; na tazama, kule waliwapata

watu wote ambao walikuwa wametoka nchi ya Amoniha, na ambao walikuwa wametupwa nje na kupigwa kwa mawe, kwa sababu walikuwa wameamini maneno ya Alma.

2 Na wakawaelezea yale yote ambayo yalikuwa yamefanyika kwa wake na watoto wao, na pia kuwahusu wao wenyewe, na nguvu za ukombozi.

3 Na pia Zeezromu aliuguka huko Sidomu, kwa homa kali, ambayo ilisababishwa na masumbuko mengi akilini mwake kwa sababu ya uovu wake, kwani alidhani kwamba Alma na Amuleki walikuwa hawako tena; na alidhani kwamba walikuwa wameuliwa kwa sababu ya uovu wake. Na dhambi hii kubwa, na dhambi zake zingine nyingi, zilimsumbua katika mawazo yake hadi zikawa kama vidonda vikubwa, kwani hakuwa na ukombozi; kwa hivyo aliaanza kuchomwa kwa joto kali.

4 Sasa, aliposikia kwamba Alma na Amuleki walikuwa katika nchi ya Sidomu, moyo wake ulianza kupata ujasiri; na akawatumia ujumbe mara moja, akihitaji wamtembelee.

5 Na ikawa kwamba walikwenda mara moja, kwani walitii ule ujumbe ambao alikuwa amewatumia; na wakaenda ndani ya nyumba ya Zeezromu; na wakampata kitandani mwake, akiwa mgonjwa, akiwa mnyonge kwa homa kali; na alikuwa na maumivu mengi katika akili yake kwa sababu ya maovu yake; na alipowaona, aliunyosha mkono wake, na kuwasihi kwamba wamponye.

6 Na ikawa kwamba Alma alimwambia, akimchukua kwa mkono wake: Je, unaziamini nguvu za wokovu za Kristo?

7 Na akajibu kwa kusema: Ndio, ninaamini maneno yote ambayo mmefundisha.

8 Na Alma akasema: Kama unaamini katika ukombozi wa Kristo wewe unaweza kuponywa.

9 Na akasema: Ndio, ninaamini kulingana na maneno yako.

10 Na ndipo Alma akamlilia Bwana, na kusema: Ee Bwana Mungu wetu, mrehemu mtu huyu, na umponye kulingana na imani yake ambayo iko katika Kristo.

11 Na Alma aliposema maneno haya, Zeezromu aliinuka kwa miguu yake, na kuanza kutembea; na hii ilifanywa kwa mshangao wa watu wote; na kitendo hiki kilijulikana kote katika nchi ya Sidomu.

12 Na Alma akambatiza Zeezromu katika Bwana; na akaanza tangu ule wakati kuwahubiria watu.

13 Na Alma alianzisha kanisa katika nchi ya Sidomu, na akawaweka makuhani na walimu wakfu katika nchi, wabatize yeyote aliyetaka kubatizwa katika Bwana.

14 Na ikawa kwamba walikuwa wengi; kwani walikusanyika kutoka sehemu zote za Sidomu, na wakabatizwa.

15 Lakini kwa watu waliokuwa katika nchi ya Amoniha, bado walibaki na mioyo migumu na shingo ngumu; na hawakutubu dhambi zao, wakifikiria nguvu za Alma na Amuleki kuwa za ibilisi; kwani walikuwa wafuasi wa dini ya Nehori, na hawakuamini katika kutubu dhambi zao.

16 Na ikawa kwamba Alma na Amuleki, Amuleki akiwa ameiacha dhahabu yake yote, na fedha, na vitu vyake vya thamani, vilivyokuwa katika nchi ya Amoniha, kwa neno la Mungu, yeye akikataliwa na wale ambao walikuwa marafiki zake kitambo, na pia na baba yake na jamaa yake;

17 Kwa hivyo, baada ya Alma kuimarisha kanisa katika Sidomu, na kuona zuio kuu, ndio, akiona kwamba watu walizuiliwa kutokana na kiburi kilichokuwa katika mioyo yao, na wakaanza kunyenyekea mbele ya Mungu, na wakaanza kujikusanya

pamoja katika makao yao matakatifu kumwabudu Mungu mbele ya madhabahu,
wakiwa waangalifu na wakiomba daima, kwamba wakombolewe kutokana na
Shetani, na kutoka kifo, na kutoka maangamizo—
18 Sasa kama nilivyosema, baada ya Alma kuona hivi vitu vyote, kwa hivyo
alimchukua Amuleki na kuvuka katika nchi ya Zarahemla, na akampeleka katika
nyumba yake mwenyewe, na kumhudumia katika mateso yake, na kumtia nguvu
katika Bwana.
19 Na hivyo mwaka wa kumi wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi uliisha.

## Alma 16

1 Na ikawa kwamba katika mwaka wa kumi na moja wa utawala wa waamuzi juu ya
watu wa Nefi, katika siku ya tano mwezi wa pili, baada ya kuwepo na amani nyingi
katika nchi ya Zarahemla, kukiwa hakuna vita au mabishano kwa muda wa miaka
kadhaa, hata hadi siku ya tano ya mwezi wa pili katika mwaka wa kumi na moja,
mlio wa vita ulisikika kote katika nchi.
2 Kwani tazama, majeshi ya Walamani yalikuwa yameingia mipakani mwa nchi,
kutoka upande wa nyika, hata katika mji wa Amoniha, na wakaanza kuwaua watu na
kuangamiza ule mji.
3 Na sasa ikawa kwamba, kabla ya Wanefi kuunda jeshi la kutosha kuwaondoa
katika nchi, walikuwa wameangamiza watu ambao walikuwa katika mji wa
Amoniha, na pia wengine katika mipaka ya Nuhu, na kuwachukua wengine mateka
huko nyikani.
4 Sasa ikawa kwamba Wanefi walitamani kuwakomboa wale ambao walikuwa
wamepelekwa utumwani huko nyikani.
5 Kwa hivyo, yule ambaye alikuwa amechaguliwa kapteni mkuu wa majeshi ya
Wanefi, (na jina lake lilikuwa Zoramu, na alikuwa na wana wawili, Lehi na
Aha)—sasa Zoramu na wana wake wawili, wakijua kwamba Alma alikuwa kuhani
mkuu juu ya kanisa, na wakiwa wamesikia kwamba alikuwa na roho ya unabii, kwa
hivyo walimwendea wakitaka kujua kama Bwana alitaka kwamba waende nyikani
kutafuta ndugu zao, ambao walikuwa wamefanywa watumwa na Walamani.
6 Na ikawa kwamba Alma alimwuliza Bwana kuhusu jambo hilo. Na Alma
akarejea na kuwaambia: Tazama, Walamani watavuka mto Sidoni kusini mwa
nyika, mbali na mipaka ya nchi ya Manti. Na tazama mtakutana nao kule, mashariki
mwa mto Sidoni, na kule ndipo Bwana atawakomboa ndugu zenu waliofanywa
watumwa na Walamani.
7 Na ikawa kwamba Zoramu na wana wake walivuka mto wa Sidoni, na majeshi
yao, na wakasafiri mbali na mipaka ya Manti kusini mwa nyika, ambayo ilikuwa
upande wa mashariki wa mto wa Sidoni.
8 Na wakayafikia majeshi ya Walamani, na Walamani walitawanywa na kupelekwa
nyikani; na wakachukua ndugu zao ambao walikuwa wamewekwa utumwani na
Walamani, na hakukuwa na hata nafsi moja iliyopotea miongoni mwa wale ambao
waliwekwa utumwani. Na wakaletwa na ndugu zao kumiliki nchi zao.
9 Na hivyo mwaka wa kumi na moja wa waamuzi ulikwisha, baada ya Walamani
kuondolewa nchini, na watu wa Amoniha waliangamizwa; ndio, kila nafsi iliyo hai
ya Waamoniha iliangamizwa, na pia mji wao mkuu, ambao walisema Mungu
hangeweza kuuangamiza, kwa sababu ya ukubwa wake.

10 Lakini tazama, katika siku moja ilifanywa kuwa ukiwa; na mizoga ikaliwa na
mbwa na wanyama wa mwitu wa nyika.
11 Walakini, baada ya siku nyingi maiti zao zilirundikwa usoni mwa ardhi, na
zikafunikwa kwa mchanga mdogo. Na mnuko ulikuwa mwingi sana hata kwamba
watu hawangeingia kumiliki nchi ya Amoniha kwa miaka mingi. Na iliitwa Ukiwa
wa Wanehori; kwani walikuwa wafuasi wa Nehori, ambao waliuawa; na nchi zao
zikabaki na ukiwa.
12 Na Walamani hawakuja tena kupigana vita na Wanefi hadi mwaka wa kumi na
nne wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi. Na hivyo kwa miaka mitatu watu
wa Nefi walikuwa na amani katika nchi yote.
13 Na Alma na Amuleki wakaenda na kuhubiri toba kwa watu katika mahekalu yao,
na mahali pao patakatifu, na pia katika masinagogi yao, ambayo yalikuwa
yamejengwa kulingana na desturi za Wayahudi.
14 Na kadiri wengi waliosikiliza maneno yao, kwao walifunza neno la Mungu, bila
ubaguzi wa watu, daima.
15 Na hivyo Alma na Amuleki waliendelea mbele, na pia wengi ambao walikuwa
wamechaguliwa kwa ile kazi, kuhubiri neno kote nchini. Na uwekaji wa kanisa
ukaenea kote nchini, katika sehemu zote za nchi, miongoni mwa watu wote wa
Wanefi.
16 Na hakukuwa na ukosefu wa usawa miongoni mwao; Bwana aliteremsha Roho
wake juu ya uso wa nchi ili kutayarisha mawazo ya watoto wa watu, au kutayarisha
mioyo yao kupokea neno ambalo lingefunzwa miongoni mwao wakati wa kuja
kwake—
17 Ili wasishupazwe dhidi ya neno, ili wasikose kuamini, na kwenda katika
maangamizo, lakini kwamba wapokee neno kwa shangwe, na kama tawi
waunganishwe na ule mzabibu wa kweli, ili waweze kuingia katika pumziko la
Bwana Mungu wao.
18 Sasa wale makuhani ambao walienda miongoni mwa watu walihubiri kinyume
cha uwongo wote, na udanganyifu, na wivu, na vita, na dharau, na matusi, na wizi,
unyang'anyi, uporaji, mauaji, uzinzi, na kila aina ya matusi, wakisema kwamba hivi
vitu havistahili kuwa hivyo—
19 Na kuwaelezea vitu ambavyo vitakuja; ndio, kuwaelezea kuhusu kuja kwa Mwana
wa Mungu, mateso yake na kifo chake, na pia ufufuo wa wafu.
20 Na watu wengi waliuliza kuhusu mahali pale ambapo Mwana wa Mungu atakuja;
na walifunzwa kwamba atawatokea baada ya ufufuo wake; na watu waliyapokea
haya kwa shangwe kuu na furaha.
21 Na sasa baada ya kanisa kuanzishwa kote nchini—baada ya kupata ushindi juu ya
ibilisi, na neno la Mungu likihubiriwa katika usafi wake kote nchini, na Bwana
akiwateremshia watu baraka zake—na hivyo mwaka wa kumi na nne wa utawala wa
waamuzi juu ya watu wa Nefi ulikwisha.

*Historia ya wana wa Mosia, ambao walizikataa haki zao za kumiliki ufalme kwa ajili ya neno la Mungu, na wakaenda mpaka nchi ya Nefi kuwahubiria Walamani; mateso yao na ukombozi wao—kulingana na maandishi ya Alma.*

# Alma 17

1 Na sasa ikawa kwamba wakati Alma alipokuwa anasafiri kutoka nchi ya Gideoni
iliyo kusini, mbali kwa nchi ya Manti, tazama, kwa mshangao wake, alikutana na
wana wa Mosia wakielekea nchi ya Zarahemla.
2 Sasa hawa wana wa Mosia walikuwa na Alma ule wakati ambao malaika
alimtokea mara ya kwanza; kwa hivyo Alma alijawa shangwe alipowaona ndugu
zake; na lile ambalo liliongezea furaha yake, ni kwamba walikuwa bado ndugu zake
katika Bwana; ndio, na walikuwa wameongezwa nguvu kwa ufahamu wa ukweli;
kwani walikuwa watu ambao wana ufahamu mwema na walikuwa wameyapekua
maandiko kwa bidii, ili wajue neno la Mungu.
3 Lakini haya sio yote; kwani walikuwa wamejitoa kwa sala, na kufunga; kwa hivyo
walikuwa na roho ya unabii, na roho ya ufunuo, na walipofunza, walifunza kwa
uwezo na mamlaka ya Mungu.
4 Na walikuwa wamefunza neno la Mungu kwa muda wa miaka kumi na nne
miongoni mwa Walamani, wakiwa wamefanikiwa sana kuwaleta wengi katika
ufahamu wa ukweli; ndio, kwa uwezo wa maneno yao wengi walisimama mbele ya
madhabahu ya Mungu, ili wamlingane na kutubu dhambi zao mbele yake.
5 Sasa hii ndio hali ambayo iliwapata katika safari yao, kwani walipata masumbuko
mengi; waliteseka sana, katika mwili na mawazo, kama vile njaa, kiu na uchovu, na
pia kazi katika roho.
6 Sasa hizi ndizo zilikuwa safari zao: Baada ya kupata ruhusa kwa baba yao, Mosia,
katika mwaka wa kwanza wa waamuzi; baada ya kukataa ufalme ambao baba yao
alitamani kuwakabidhi, na pia hii ndiyo ilikuwa katika mawazo ya watu;
7 Walakini waliondoka kutoka nchi ya Zarahemla, na wakachukua panga zao, na
mikuki yao, na pinde zao, na mishale yao, na kombeo zao; na walifanya haya ili
wajitafutie chakula wakiwa huko nyikani.
8 Na hivyo wakaelekea nyikani pamoja na umati ambao walikuwa wameuchagua,
ili waende katika nchi ya Nefi, kuwahubiria Walamani neno la Mungu.
9 Na ikawa kwamba walisafiri kwa siku nyingi nyikani, na wakafunga sana na
kuomba sana kwamba Bwana angewapatia sehemu ya roho yake ili iende pamoja
nao, na kuishi nao, ili wawe chombo mikononi mwa Mungu kuwaleta kama
ingewezekana, ndugu zao, Walamani, wawafahamishe, kuhusu ufahamu wa ukweli,
na ufahamu wa uovu wa mila za babu zao, ambazo hazikuwa za haki.
10 Na ikawa kwamba Bwana aliwatembelea kwa Roho wake, na kuwaambia: Pateni
faraja. Na wakafarijika.
11 Na Bwana akawaambia pia: Nendeni miongoni mwa Walamani, ndugu zenu, na
muimarishe neno langu; walakini mtakuwa wenye subira kwa uvumilivu na mateso,
kwamba muwatolee mfano mwema ndani yangu, na nitawafanya muwe chombo
katika mikono yangu cha kuokoa nafsi nyingi.
12 Na ikawa kwamba mioyo ya wana wa Mosia, na pia wale ambao walikuwa nao,
ilijipatia ujasiri wa kwenda kwa Walamani na kuwatangazia neno la Mungu.
13 Na ikawa kwamba walipofika katika mipaka ya nchi ya Walamani, walijigawanya
na kuachana, wakimwamini Bwana kwamba watakutana tena baada ya mavuno yao;
kwani walidhani kwamba walikuwa na kazi kubwa sana.
14 Na kwa hakika ilikuwa kubwa, kwani walikuwa wamechukua jukumu la kuhubiri
neno la Mungu kwa watu wakaidi na wagumu na wakali; watu ambao walifurahia
kuwaua Wanefi, na kuwanyang'anya na kuwapora; na mioyo yao ilikuwa katika

utajiri, au katika dhahabu na fedha, na mawe ya thamani; lakini walitafuta kupata
hivi vitu kwa kuua na unyang'anyi, ili wasijichoshe kupata kwa mikono yao.
15 Na hivyo walikuwa watu wavivu, wengi wao wakiabudu sanamu, na laana ya
Mungu iliwateremkia kwa sababu ya mila za babu zao; ingawa walikuwa
wamenyooshewa ahadi za Bwana wakitubu.
16 Kwa hivyo, hili ndilo lilikuwa lengo ambalo wana wa Mosia walikuwa
wamejitakia kazi, ili pengine wawalete kwa toba; ili pengine waweze kuwafahamisha
kuhusu mpango wa ukombozi.
17 Kwa hivyo walijigawanya mmoja kutoka kwa mwingine, na wakaenda miongoni
mwao, kila mtu peke yake, kulingana na nguvu za Mungu ambazo alipewa.
18 Sasa Amoni akiwa kiongozi miongoni mwao, kwa usahihi zaidi aliwahudumia,
na akaondoka kutoka kwao, baada ya kuwabariki kulingana na vyeo vyao tofauti,
baada ya kuwazungumzia neno la Mungu, au kuwabariki kabla ya kuondoka kwake;
na hivyo wakaanza safari zao kadha kote nchini.
19 Na Amoni alikwenda katika nchi ya Ishmaeli, kwani nchi hiyo ilitungwa baada
ya wana wa Ishmaeli, ambao pia nao walibadilika na kuwa Walamani.
20 Na wakati Amoni alipoingia katika nchi ya Ishmaeli, Walamani walimchukua na
kumfunga, kama ilivyokuwa desturi yao ya kuwafunga Wanefi wote walioangukia
mikononi mwao, na kuwapeleka mbele ya mfalme; na hivyo ilikuwa ni juu ya
mfalme kuwaua, au kuwafanya watumwa, au kuwatupa gerezani, au kuwafukuza
kutoka nchi yake, kulingana na nia yake na matakwa yake.
21 Na hivyo Amoni alipelekwa mbele ya mfalme aliyekuwa juu ya nchi ya Ishmaeli;
na jina lake lilikuwa Lamoni; na alikuwa wa uzao wa Ishmaeli.
22 Na mfalme akamwuliza Amoni kama alitaka kuishi katika nchi miongoni mwa
Walamani, au miongoni mwa watu wake.
23 Na Amoni akamwambia: Ndio, natamani kuishi miongoni mwa watu hawa kwa
muda; ndio, na pengine hadi siku ile nitakapoaga dunia.
24 Na ikawa kwamba mfalme Lamoni alifurahishwa sana na Amoni, na akaamuru
kwamba kamba zake zifunguliwe; na akataka kwamba Amoni amchukue mmoja wa
mabinti zake awe mke wake.
25 Lakini Amoni akamwambia: La, lakini nitakuwa mtumishi wako. Kwa hivyo
Amoni akawa mtumishi wa mfalme Lamoni. Na ikawa kwamba alipewa kazi ya
kuchunga mifugo ya Lamoni pamoja na watumishi wengine, kulingana na desturi ya
Walamani.
26 Na baada ya kuwa katika utumishi wa mfalme kwa siku tatu, alipokuwa na
watumishi wa Kilamani wakipeleka mifugo yao mahali pa maji, ambapo paliitwa
maji ya Sebo, na Walamani wote walikuwa wakileta mifugo yao hapa, ili inywe
maji—
27 Kwa hivyo, wakati Amoni na watumishi wa mfalme walipokuwa wakipeleka
mifugo yao mahali hapo pa maji, tazama, kikundi fulani cha Walamani, ambacho
kilikuwa kimeleta mifugo yao kwa maji, kilisimama na kutawanya mifugo ya Amoni
na watumishi wa mfalme, na wakawatawanya hadi wakatorokea njia nyingi.
28 Sasa watumishi wa mfalme wakaanza kunung'unika, wakisema: Sasa mfalme
atatuua, kama alivyowaua ndugu zetu kwa sababu mifugo yao ilitawanywa kwa uovu
wa watu hawa. Na wakaanza kulia sana, wakisema: Tazama, mifugo yetu tayari
imetawanywa.
29 Sasa walilia kwa sababu waliogopa kuuawa. Sasa Amoni alipoona haya moyo

wake ulifura ndani yake kwa sababu ya shangwe; kwani, alisema, nitawafunulia
hawa watumishi wenzangu nguvu zangu, au nguvu iliyo ndani yangu, katika
kumrejeshea mfalme mifugo hii, ili niweze kupendeza mioyo ya hawa watumishi
wenzangu, ili waweze kuamini maneno yangu.
30 Na sasa, haya ndiyo yalikuwa mawazo ya Amoni, alipoona mateso ya wale ambao
aliwaita ndugu zake.
31 Na ikawa kwamba aliwafanyia utani kwa maneno yake, na kusema: Ndugu
zangu, jitieni moyo na twende tukatafute mifugo, na tutaikusanya pamoja na tuilete
katika mahali pa maji; na hivyo tutaihifadhi mifugo ya mfalme na hatatuua.
32 Na ikawa kwamba walienda kutafuta ile mifugo, na wakamfuata Amoni, na
wakaenda kwa kasi nyingi na kuikusanya mifugo ya mfalme, na kuirudisha tena
mahali pa maji.
33 Na watu wale wakataka kuitawanya ile mifugo tena; lakini Amoni akawaambia
ndugu zake: Izingireni mifugo ili isitawanyike; na nitakwenda na kukabiliana na
hawa watu wanaotawanya mifugo yetu.
34 Kwa hivyo, wakafanya vile Amoni alivyowaamuru, na akaenda na kukabiliana na
wale ambao walisimama karibu na maji ya Sebo; na idadi yao haikuwa ndogo.
35 Kwa hivyo hawakumwogopa Amoni, kwani walidhani kwamba mmoja wa watu
wao angemuua kulingana na furaha yao, kwani hawakujua kwamba Bwana alikuwa
amemwahidi Mosia kwamba angewakomboa wana wake kutoka mikononi mwao;
wala hawakujua chochote kumhusu Bwana; kwa hivyo walifurahia maangamizo ya
ndugu zao; na kwa sababu hii walisimama kuitawanya mifugo ya mfalme.
36 Lakini Amoni akasimama na akaanza kuwatupia mawe kwa kombeo yake; ndio,
alitupa mawe kwa nguvu nyingi miongoni mwao; na akawaua wengi wao hadi
wakaanza kustaajabishwa na nguvu yake; walakini walikasirishwa kwa sababu ya
ndugu zao waliokuwa wameuawa, na walikata kauli kwamba lazima aanguke; kwa
hivyo, wakiona kwamba hawakuweza kumgonga kwa mawe, walimjia kwa rungu zao
ili wamuue.
37 Lakini tazama, kila mtu aliyeinua rungu lake kumgonga Amoni, alikata mikono
yao kwa upanga wake; kwani alizuia mapigo yao kwa kukata mikono yao kwa ncha
ya upanga wake, hadi kwamba wakaanza kustaajabia, na wakaanza kumtoroka; ndio,
na idadi yao haikuwa ndogo; na akawasababisha watoroke kwa nguvu za mkono
wake.
38 Sasa sita ya wao waliangushwa kwa kombeo, lakini hakuwaua wengine ijapokuwa
kiongozi wao kwa upanga wake; na alikata mikono ya wengi walioinua mikono yao
kumpiga; na hawakuwa wachache.
39 Na wakati alipokuwa amewakimbiza, alirudi na kunywesha mifugo yao maji na
kuirudisha katika malisho ya mfalme, na kumwendea mfalme, wakibeba mikono ile
ambayo ilikuwa imekatwa kwa upanga wa Amoni, ya wale ambao walijaribu
kumuua; na ikapelekwa mbele ya mfalme kama ushahidi wa vitu ambavyo walikuwa
wamefanya.

## Alma 18

1 Na ikawa kwamba mfalme Lamoni alisababisha kwamba watumishi wake wasimame
na washuhudie kuhusu vitu vyote walivyokuwa wameviona kuhusu jambo lile.
2 Na wote walipokuwa wameshuhudia vitu ambavyo walikuwa wameona, na

alikuwa amejulishwa vile Amoni alivyokuwa mwaminifu katika kuhifadhi mifugo yake, na pia kwa nguvu zake kuu za kukabiliana na wale ambao walitaka kumuua, alistaajabu sana, na kusema: Kwa kweli, huyu ni zaidi ya mwanadamu. Tazama, si huyu ndiye Roho Mkuu anawateremshia watu hawa adhabu kwa sababu ya mauaji yao?

3 Na wakamjibu mfalme, na kusema: Hatujui kama yeye ndiye ile Roho Kuu, au mwanadamu; lakini tunajua haya, kwamba hawezi kuuawa na maadui wa mfalme; wala hawawezi kutawanya mifugo ya mfalme akiwa pamoja na sisi, kwa sababu ya uhodari wake na nguvu zake kuu; kwa hivyo tunajua kwamba yeye ni rafiki wa mfalme. Na sasa, Ee mfalme, hatuamini kwamba mwanadamu anazo nguvu kama hizo, kwani tunajua kwamba hawezi kuuawa.

4 Na sasa, mfalme aliposikia maneno haya, aliwaambia: Sasa ninajua kwamba ni Roho Mkuu; na ameshuka chini wakati huu kuhifadhi maisha yenu, ili nisiwaue vile nilivyowafanya ndugu zenu. Sasa huyu ndiye Roho Mkuu ambaye babu zetu walimzungumzia.

5 Sasa hii ndiyo ilikuwa desturi ya Lamoni, ambayo alikuwa amepokea kutoka kwa baba yake, kwamba kulikuwa na Roho Mkuu. Ingawa waliamini katika Roho Mkuu, bado walidhani kwamba yoyote ambayo walitenda yalikuwa ni sawa; walakini, Lamoni alianza kuogopa sana, na aliogopa kwamba alikuwa ametenda mabaya kwa kuwaua watumishi wake;

6 Kwani alikuwa ameua wengi wao kwa sababu ndugu zao walikuwa wametawanya mifugo yao mahali pa maji; na hivyo, kwa sababu mifugo yao ilitawanywa waliuawa.

7 Sasa ilikuwa ni desturi ya Walamani hawa kusimama karibu na maji ya Sebo kutawanya mifugo ya watu, wafukuze wale wengi ambao walikuwa wametawanywa katika nchi yao, hii ikiwa ni desturi yao ya kupora miongoni mwao.

8 Na ikawa kwamba mfalme Lamoni aliwauliza watumishi wake, akisema: Yuko wapi huyu mtu aliye na uwezo huu mkuu?

9 Na wakamwambia: Tazama, analisha farasi wako. Sasa mfalme alikuwa amewaamuru watumishi wake, kabla ya kupeleka mifugo kunywa maji, kwamba watayarishe farasi wake na magari yale yanayovutwa, na wamsindikize hadi nchi ya Nefi; kwani kulikuwa na sherehe kubwa iliyoandaliwa katika nchi ya Nefi, na baba ya Lamoni, ambaye alikuwa mfalme katika nchi yote.

10 Sasa wakati mfalme Lamoni aliposikia kwamba Amoni alikuwa anatayarisha farasi wake na magari yake yanayovutwa alistaajabu zaidi, kwa sababu ya uaminifu wa Amoni, akisema: Kwa hakika hakuna mtumishi mwingine miongoni mwa watumishi wangu ambaye amekuwa mwaminifu kama mtu huyu; kwani hata anakumbuka kutii amri zangu zote na kuzitekeleza.

11 Sasa kwa hakika najua kwamba huyu ndiye Roho Mkuu, na ninatamani kwamba aje ndani kwangu, lakini sithubutu.

12 Na ikawa kwamba wakati Amoni alipomaliza kutayarisha farasi na magari ya mfalme na watumishi wake, alimwendea mfalme, na akaona kwamba uso wa mfalme ulikuwa umebadilika; kwa hivyo alikaribia kuondoka katika uwepo wake.

13 Na mtumishi mmoja wa mfalme akamwambia, Rabana, ambayo, tafsiri yake, ni mwenye nguvu au mfalme mkuu, wakifikiria wafalme wao kuwa wenye nguvu; na hivyo akamwambia: Rabana, mfalme anataka ukae.

14 Kwa hivyo Amoni akamgeukia mfalme, na kumwambia: Ni nini unachotaka nikufanyie, Ee mfalme? Na mfalme hakumjibu kwa muda wa saa moja, kulingana na

wakati wao, kwani hakujua la kumwambia.

15 Na ikawa kwamba Amoni alimwambia tena: Nini unahitaji kwangu? Lakini mfalme hakumjibu.

16 Na ikawa kwamba Amoni, akiwa amejawa na Roho wa Mungu, kwa hivyo alihisi mawazo ya mfalme. Na akamwambia: Ni kwa sababu umesikia kwamba niliwakinga watumishi wako na mifugo yako, na kuwaua ndugu zao saba kwa kombeo na upanga, na kukata mikono ya wengine, ili kulinda mifugo yako na watumishi wako; tazama, ni haya ndio yanayosababisha kushangaa kwako?

17 Nakwambia, ni nini, ambacho kimefanya mshangao wako uwe mkuu? Tazama, mimi ni mwanadamu, na mimi ni mtumishi wako; kwa hivyo, chochote utakachotaka ambacho ni chema, nitatenda.

18 Sasa wakati mfalme aliposikia maneno haya, alishangaa tena, kwani aliona kwamba Amoni angeweza kupambanua mawazo yake; lakini licha ya haya, mfalme Lamoni alifungua kinywa chake, na kumwambia: Wewe ni nani? Wewe ni yule Roho Mkuu, anayejua vitu vyote?

19 Amoni akamjibu na kumwambia: Mimi siye.

20 Na mfalme akasema: Vipi unavyojua mawazo ya moyo wangu? Zungumza kwa ujasiri, na uniambie kuhusu vitu hivi; na pia uniambie ni kwa nguvu gani ulizowaua na kukata mikono ya ndugu zangu waliotawanya mifugo yangu—

21 Na sasa, kama utanielezea kuhusu vitu hivi, chochote utakachoniuliza nitakupa; na kama itahitajika, nitakulinda na majeshi yangu; lakini najua kwamba wewe una nguvu kuliko hao wote; walakini, chochote utakachotaka kutoka kwangu nitakupa.

22 Sasa Amoni akiwa mwenye hekima, lakini mpole, alimwambia Lamoni: Utasikiliza maneno yangu, nikikuelezea ni kwa nguvu gani ninafanya vitu hivi? Na hiki ndicho kitu ambacho ninataka kutoka kwako.

23 Na mfalme akamjibu, na kusema: Ndio, nitaamini maneno yako yote. Na hivyo akanaswa kwa werevu.

24 Na Amoni akaanza kumzungumzia kwa ujasiri, na akamwambia: Unaamini kwamba Mungu yupo?

25 Na akamjibu, na kusema: Mimi sijui maana ya hayo.

26 Na kisha Amoni akasema: Unaamini kwamba kuna Roho Mkuu?

27 Na akasema, Ndio.

28 Na Amoni akasema: Huyu ndiye Mungu. Na Amoni akamwambia tena: Unaamini kwamba huyu Roho Mkuu, ambaye ni Mungu, aliumba vitu vyote vilivyo mbinguni na duniani?

29 Na akasema: Ndio, naamini kwamba aliumba vitu vyote vilivyo ulimwenguni; lakini sijui mbinguni.

30 Na Amoni akamwambia: Mbinguni ni mahali ambapo Mungu anaishi pamoja na malaika wake wote watakatifu.

31 Na mfalme Lamoni akasema: Iko juu ya ulimwengu?

32 Na Amoni akasema: Ndio, na anatazama chini kwa watoto wa watu wote; na anafahamu mawazo yote na nia zote za moyo; kwani tangu mwanzo wote waliumbwa kwa mkono wake.

33 Na mfalme Lamoni akasema: Naamini vitu hivi vyote ambavyo umezungumza. Wewe umetumwa kutoka kwa Mungu?

34 Amoni akamwambia: Mimi ni mwanadamu; na hapo mwanzo mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu, na nimeitwa na Roho Mtakatifu wake ili

niwafunze watu hawa vitu hivi, ili waweze kujua yale yaliyo ya haki na kweli;
35 Na sehemu ya Roho huyo anaishi ndani yangu, ambaye hunipatia ufahamu, na
pia uwezo kulingana na imani yangu na nia iliyo katika Mungu.
36 Sasa baada ya Amoni kusema maneno haya, alianzia tangu kuumbwa kwa
ulimwengu, na pia kuumbwa kwa Adamu, na kumwambia vitu vyote kuhusu
kuanguka kwa mwanadamu, na kumwelezea na kumfunulia maandishi na maandiko
ya watu, ambayo yalikuwa yamezungumzwa na manabii, hata hadi ule wakati ambao
baba yao, Lehi, alipotoka Yerusalemu.
37 Na pia akawasimulia (kwani ilikuwa kwa mfalme na watumishi wake) safari zote
za babu zao huko nyikani, na mateso yao yote ya njaa na kiu, na mateso yao, na
kadhalika.
38 Na pia akawasimulia kuhusu maasi ya Lamani na Lemueli, na wana wa Ishmaeli,
ndio, aliwaeleza kuhusu maasi yao yote; na akawaelezea maandishi na maandiko
yote tangu ule wakati ambao Lehi aliondoka Yerusalemu hadi ule wakati wa sasa.
39 Lakini haya sio yote; kwani aliwaelezea kuhusu mpango wa ukombozi, ambao
ulitayarishwa tangu msingi wa ulimwengu; na pia akawaelezea kuhusu kuja kwa
Kristo, na aliwajulisha kuhusu matendo yote ya Bwana.
40 Na ikawa kwamba baada yake kusema vitu hivi vyote, na kumwelezea mfalme,
kwamba mfalme aliamini maneno yake yote.
41 Na akaanza kumlilia Bwana, akisema: Ee Bwana, nihurumie; kulingana na
rehema zako tele ambazo umewaonyesha watu wa Nefi, nihurumie mimi, na watu
wangu.
42 Na sasa, baada ya kusema haya, akainama kwenye ardhi, kama yule aliyefariki.
43 Na ikawa kwamba watumishi wake walimchukua na kumpeleka kwa mke wake,
na wakamlaza kitandani; na akalala kama aliyekufa kwa muda wa siku mbili na
kucha mbili; na mke wake, na wana wake, na mabinti zake walimwomboleza, kama
ilivyokuwa desturi ya Walamani, wakiomboleza sana kifo chake.

# Alma 19

1 Na ikawa kwamba baada ya siku mbili na kucha mbili walikaribia kuchukua mwili
wake na kuuzika kaburini, ambalo walikuwa wametayarisha kwa kusudi la kuzika
wafu wao.
2 Sasa malkia akiwa amesikia sifa za Amoni, kwa hivyo alituma na akataka kwamba
aje kwake.
3 Na ikawa kwamba Amoni alifanya vile alivyoamriwa, na akamwendea malkia, na
akahitaji kujua yale aliyotaka atende.
4 Na akamwambia: Watumishi wa bwana wangu wamenijulisha kwamba wewe ni
nabii wa Mungu mtakatifu, na kwamba wewe una uwezo wa kutenda vitendo vikuu
katika jina lake;
5 Kwa hivyo, kama hivi ndivyo ilivyo, ningetaka uende na umwone bwana wangu,
kwani amelazwa kitandani mwake kwa muda wa siku mbili na kucha mbili; na
wengine wanasema kwamba hajafariki, lakini wengine wanasema kwamba amefariki
na kwamba ananuka, na kwamba anastahili kuzikwa kaburini; lakini kwangu mimi,
hanuki.
6 Sasa, hili ndilo Amoni alilotaka, kwani alijua kwamba mfalme Lamoni alikuwa
chini ya nguvu za Mungu; alijua kwamba pazia la giza ya kutoamini ilikuwa

inaondolewa mawazoni mwake, na nuru ile ambayo iliangaza mawazo yake, ambayo
ilikuwa ni nuru ya utukufu wa Mungu, ambayo ilikuwa ni nuru ya ajabu ya wema
wake — ndio, nuru hii ilikuwa imejaza nafsi yake na shangwe, wingu la giza likiwa
limeondolewa, na kwamba nuru ya uzima usio na mwisho ilikuwa imewashwa
katika nafsi yake, ndio, alijua kwamba mwili wake ulikuwa umelemewa na haya, na
alikuwa amebebwa na Mungu —
7 Kwa hivyo, yale malkia aliyohitaji yalikuwa ni matakwa yake. Kwa hivyo, akaenda
ndani kumwona mfalme kama vile malkia alivyomhitajia; na alimwona mfalme, na
alijua kwamba hajafariki.
8 Na akamwambia malkia: Yeye hajafariki, lakini amelala katika Mungu, na kesho
atafufuka tena; kwa hivyo usimzike.
9 Na Amoni akamwambia: Wewe unaamini haya? Na akamwambia: Sijapata
ushahidi mwingine ijapokuwa neno lako, na neno la watumishi wetu; walakini
naamini kwamba itakuwa kulingana na yale ambayo umesema.
10 Na Amoni akamwambia: Wewe umebarikiwa kwa sababu ya imani yako nyingi;
nakwambia wewe, mwanamke, hakujawahi kuwa na imani kuu kama hii miongoni
mwa Wanefi.
11 Na ikawa kwamba alilinda kitanda cha bwana wake, tangu wakati ule hadi kesho
yake ule wakati ambao Amoni alikuwa amepanga kwamba atainuka.
12 Na ikawa kwamba aliinuka, kulingana na maneno ya Amoni; na alipoinuka,
alinyosha mkono wake kwa mwanamke wake, na kusema: Jina la Mungu libarikiwe,
na wewe umebarikiwa.
13 Kwani kwa hakika kama vile unavyoishi, tazama, nimemwona Mkombozi
wangu; na atakuja, na atazaliwa na mwanamke, na atakomboa wanadamu wote
ambao wanaamini jina lake. Sasa, aliposema maneno haya, moyo wake ulifura tena
ndani yake, na akazama tena kwa shangwe; na malkia pia akazama, akiwa
amelemewa na Roho.
14 Sasa Amoni akiona kwamba Roho wa Bwana aliteremshwa kulingana na sala
zake kwa Walamani, ndugu zake, ambao walikuwa wamesababisha maombolezo
makuu miongoni mwa Wanefi, au miongoni mwa watu wote wa Mungu kwa sababu
ya maovu yao na mila zao, alipiga magoti, na akaanza kutoa nafsi yake kwa sala na
kumshukuru Mungu kwa roho yake yote kwa sababu ya yale yote ambayo alikuwa
amewatendea ndugu zake; na pia alilemewa na shangwe; na hivyo wote watatu
walikuwa wameanguka ardhini.
15 Sasa, wakati watumishi wa mfalme walipoona kwamba walikuwa wameinama,
nao pia walianza kumlilia Mungu, kwani woga wa Bwana ulikuwa umewaingia nao
pia, kwani wao ndio walikuwa wamesimama mbele ya mfalme na kumshuhudia
kuhusu nguvu kuu za Amoni.
16 Na ikawa kwamba walilingana jina la Bwana, kwa uwezo wao wote, hadi wote
wakainama kwenye ardhi, isipokuwa tu mwanamke mmoja wa Kilamani, ambaye
jina lake lilikuwa Abishi, ambaye alikuwa amemgeukia Bwana kwa muda wa miaka
mingi, iliyotokana na ono la kushangaza la baba yake —
17 Hivyo, baada ya kumgeukia Bwana, na hakuwa amewahi kumjulisha yeyote, kwa
hivyo, alipoona kwamba watumishi wote wa Lamoni walikuwa wameinama kwenye
ardhi, na pia bibi yake, malkia, na mfalme, na Amoni kwamba walikuwa wamelala
katika ardhi kifudifudi, alijua kwamba ni uwezo wa Mungu; na akidhani kwamba
nafasi hii, kwa kufahamisha watu kuhusu yale yaliyokuwa yametendeka miongoni

mwao, kwamba kwa kuona kisa hiki itawasababishia kuamini kwa nguvu za Mungu, kwa hivyo akakimbia kutoka nyumba kwa nyumba, akiwafahamisha watu.

18 Na wakaanza kukusanyika pamoja katika nyumba ya mfalme. Na kikundi kikubwa kikaja, na kwa mshangao wao wakaona mfalme, na malkia, na watumishi wao wamelala chini ardhini, na wote walikuwa wamelala pale kama waliofariki, na pia wakamwona Amoni, na tazama, alikuwa Mnefi.

19 Na sasa watu wakaanza kunung'unika miongoni mwao; wengine wakisema kwamba ni mkasa mwovu mkuu uliokuwa umewateremkia, au juu ya mfalme na nyumba yake, kwa sababu alikuwa ameruhusu Mnefi kuishi katika nchi ile.

20 Lakini wengine waliwakemea, wakisema: Mfalme ameteremshia nyumba yake uovu huu, kwa sababu aliwaua watumishi wake ambao mifugo yao ilitawanywa katika maji ya Sebo.

21 Na pia walikemewa na wale watu ambao walikuwa wamesimama katika maji ya Sebo na kutawanya mifugo ya mfalme, kwani walimkasirikia Amoni kwa sababu ya idadi ambayo alikuwa ameua ya ndugu zao katika maji ya Sebo, alipokuwa akilinda mifugo ya mfalme.

22 Sasa, mmoja wao, ambaye kaka yake alikuwa ameuawa kwa upanga wa Amoni, akiwa amemkasirikia Amoni sana, alitoa upanga wake ili amwangushie Amoni, amuue; na alipoinua upanga wake ili amkate, tazama, alianguka chini na kufariki.

23 Sasa tunaona kwamba Amoni hangeuawa, kwani Bwana alikuwa amemwambia Mosia, baba yake: Nitamhifadhi, na itakuwa juu yake kulingana na imani yako — kwa hivyo, Mosia alimtumainia Bwana.

24 Na ikawa kwamba ule umati ulipoona kwamba yule mtu alikuwa ameanguka na kufariki, aliyekuwa ameinua upanga kumuua Amoni, woga uliwapata wote, na hawakuthubutu kuweka mikono yao kwake au kwa wale ambao walikuwa wameanguka; na wakaanza tena kustaajabu miongoni mwao ni nini kilichosababisha nguvu hizi kuu, au maana ya vitu hivi vyote.

25 Na ikawa kwamba kulikuwa na wengi miongoni mwao waliosema kwamba Amoni alikuwa ni yule Roho Mkuu, na wengine wakasema kwamba ametumwa na Roho Mkuu;

26 Lakini wengine waliwakemea wote, wakisema kwamba alikuwa ni jitu, ambalo lilikuwa limetumwa na Wanefi kuwatesa.

27 Na kulikuwa na wengine ambao walisema kwamba Amoni alikuwa ametumwa na yule Roho Mkuu kuwatesa kwa sababu ya maovu yao; na kwamba ilikuwa ni yule Roho Mkuu aliyekuwa anawasaidia Wanefi daima, ambaye alikuwa amewakomboa kutoka mikononi mwao; na wakasema kwamba ni huyu Roho Mkuu ambaye alikuwa amewaangamiza ndugu zao wengi, Walamani.

28 Na hivyo ubishi ukazidi kuwa mkali miongoni mwao. Na walipokuwa wakibishana, yule mtumishi mwanamke ambaye alikuwa amesababisha umati ukusanyike pamoja alifika, na alipoona ule ubishi uliokuwa miongoni mwa umati alihuzunika sana, hadi akalia machozi.

29 Na ikawa kwamba alienda na kumchukua malkia kwa mkono wake, ili pengine amuinue kutoka ardhini; na alipougusa mkono wake aliinuka na kusimama kwa miguu yake, na kulia kwa sauti kubwa, akisema: Ee Yesu uliyebarikiwa, uliyeniokoa kutoka jahanamu! Ee Mungu uliyebarikiwa, warehemu watu hawa!

30 Na aliposema haya, alipigisha mikono yake, akiwa amejazwa na shangwe, na kuzungumza maneno mengi ambayo hayakufahamika; na alipofanya haya,

alimchukua mfalme, Lamoni, kwa mkono, na tazama aliinuka na kusimama kwa
miguu yake.
31 Na yeye, papo hapo, akiona ubishi uliokuwa miongoni mwa watu wake, alianza
kuwakemea, na kuwafunza maneno aliyoyasikia kutoka kinywa cha Amoni; na
wengi walisikia maneno yake na kuyaamini, na wakamgeukia Bwana.
32 Lakini kulikuwa na wengi miongoni mwao ambao hawakutaka kuyasikia
maneno yake; kwa hivyo walienda zao.
33 Na ikawa kwamba wakati Amoni alipoinuka, na yeye pia aliwahudumia, na pia
watumishi wote wa Lamoni; na wote waliwatangazia watu kitu sawa—kwamba
mioyo yao ilikuwa imebadilishwa; kwamba hawakutamani tena kutenda maovu.
34 Na tazama, wengi waliwatangazia watu kwamba walikuwa wameona malaika na
kuzungumza nao; na hivyo walikuwa wamewaambia vitu vya Mungu, na haki yake.
35 Na ikawa kwamba kulikuwa na wengi walioamini katika maneno yao; na wengi
walioamini walibatizwa; na wakawa watu wenye haki, na wakaanzisha kanisa
miongoni mwao.
36 Na hivyo kazi ya Bwana ikaanza miongoni mwa Walamani; hivyo Bwana alianza
kuteremsha Roho wake juu yao; na tunaona kwamba mkono wake umenyooshwa
kwa watu wote ambao watatubu na kuamini katika jina lake.

## Alma 20

1 Na ikawa kwamba baada ya wao kuanzisha kanisa katika nchi hiyo, mfalme Lamoni
alimtaka Amoni aende pamoja na yeye katika nchi ya Nefi, ili amwonyeshe kwa
baba yake.
2 Na sauti ya Bwana ikamjia Amoni, ikisema: Hutaenda katika nchi ya Nefi, kwani
tazama, mfalme atataka kukutoa uhai wako; lakini utaenda katika nchi ya Midoni;
kwani tazama, kaka yako Haruni, na pia Muloki na Ama wako gerezani.
3 Sasa ikawa kwamba Amoni aliposikia haya, alimwambia Lamoni: Tazama, kaka
yangu na jamaa zangu wako gerezani huko Midoni, na ninaenda ili niwakomboe.
4 Sasa Lamoni akamwambia Amoni: Najua, kwamba kwa nguvu za Bwana wewe
unaweza kufanya vitu vyote. Lakini tazama, nitaenda na wewe katika nchi ya
Midoni; kwani mfalme wa nchi ya Midoni, ambaye jina lake ni Antiomno, ni rafiki
yangu; kwa hivyo nitaenda katika nchi ya Midoni, ili nimtanie mfalme wa nchi, na
atawatoa ndugu zako kutoka gerezani. Sasa Lamoni akamwambia: Nani
aliyekwambia kwamba ndugu zako wako gerezani?
5 Na Amoni akamwambia: Hakuna yeyote aliyeniambia, ijapokuwa Mungu; na
aliniambia—Nenda ukawakomboe ndugu zako, kwani wako gerezani katika nchi
ya Midoni.
6 Sasa Lamoni aliposikia haya aliamuru kwamba watumishi wake watayarishe
farasi wake na magari yake.
7 Na akamwambia Amoni: Njoo, nitaenda nawe katika nchi ya Midoni, na huko
nitamsihi mfalme ili awatoe ndugu zako gerezani.
8 Na ikawa kwamba Amoni na Lamoni walipokuwa wakisafiri huko, walikutana na
baba ya Lamoni, ambaye alikuwa ni mfalme katika nchi yote.
9 Na tazama, baba ya Lamoni akamwambia: Kwa nini hukuja kwa sherehe siku ile
kuu niliyoandaa kwa wana wangu, na watu wangu?
10 Na pia akasema: Unaenda wapi na huyu Mnefi, ambaye ni mmoja wa wana wa

mwongo?

11 Na ikawa kwamba Lamoni akamwelezea kule alikokuwa akienda, kwani aliogopa kumkasirisha.

12 Na pia akamwelezea sababu zake za kukawia katika ufalme wake, na kwa nini hakwenda kwa sherehe ambayo baba yake alikuwa ameandaa.

13 Na sasa wakati Lamoni alipomwelezea vitu hivi vyote, tazama, kwa mshangao wake, baba yake alimkasirikia, na kusema: Lamoni, wewe unaenda kuwakomboa hawa Wanefi, ambao ni wana wa mwongo. Tazama, aliwaibia babu zetu; na sasa watoto wake nao pia wamekuja kati yetu, ili kwa ujanja wao na uwongo wao, watudanganye, ili watuibie mali yetu tena.

14 Sasa baba ya Lamoni alimwamuru kwamba amuue Amoni kwa upanga. Na pia akamwamuru kwamba asiende katika nchi ya Midoni, lakini kwamba arudi na yeye katika nchi ya Ishmaeli.

15 Lakini Lamoni akamwambia: Mimi sitamuua Amoni, wala sitarudi katika nchi ya Ishmaeli, lakini nitaenda katika nchi ya Midoni ili niwakomboe ndugu za Amoni, kwani najua kwamba wao ni watu wenye haki na manabii watakatifu wa Mungu wa kweli.

16 Sasa wakati baba yake aliposikia maneno haya, alimkasirikia, na akatoa upanga wake ili amwangushe chini.

17 Lakini Amoni akasonga mbele na kumwambia: Tazama, huwezi kumuua mwana wako; walakini, heri yeye aanguke chini badala yako, kwani tazama, ametubu dhambi zake; lakini wewe ukianguka wakati huu, katika hasira yako, nafsi yako haiwezi kuokolewa.

18 Na tena, inafaa ujizuie; kwani ukimuua mwana wako, na yeye ni mtu ambaye hana hatia, damu yake itamlilia Bwana Mungu wake kutoka ardhini, kulipiza kisasi kwake; na pengine wewe utapoteza nafsi yako.

19 Sasa wakati Amoni alipomwambia maneno haya, alimjibu, akisema: Najua kwamba nikimuua mwana wangu, kwamba nitamwaga damu isiyo na hatia; kwani wewe ndiye umetaka kumwangamiza.

20 Na akanyoosha mkono wake ili amuue Amoni. Lakini Amoni alivumilia mapigo yake, na pia akaupiga mkono wake kwamba hakuweza kuutumia tena.

21 Sasa mfalme alipoona kwamba Amoni angemuua, alianza kumlilia Amoni kwamba aokoe maisha yake.

22 Lakini Amoni akainua upanga wake, na kumwambia: Tazama, nitakuua usipokubali ndugu zangu watolewe gerezani.

23 Sasa mfalme, akiogopa kwamba atapoteza uhai wake, alisema: Ukiniokoa nitakupa chochote utakachoniuliza, hata kama ni nusu ya ufalme.

24 Sasa Amoni alipoona kwamba mfalme mzee amekubali matakwa yake, alimwambia: Ukikubali kwamba ndugu zangu watolewe gerezani, na pia kwamba Lamoni amiliki ufalme wake, na kwamba usimkasirikie, lakini kwamba umruhusu atende kulingana na nia yake kwa kitu chochote anachofikiria, ndipo nitakuokoa; la sivyo nitakuangusha chini.

25 Sasa Amoni aliposema maneno haya, mfalme akaanza kufurahi kwa sababu ya maisha yake.

26 Na alipoona kwamba Amoni hakuwa na haja ya kumwangamiza, na pia alipoona jinsi alivyompenda mwana wake Lamoni, alishangaa sana, na kusema: Kwa sababu haya pekee ndiyo umetaka, kwamba niwaachilie ndugu zako, na kwamba

nimruhusu mwana wangu Lamoni amiliki ufalme wake, tazama, nitamruhusu
mwana wangu amiliki ufalme wake kutoka sasa hadi milele; na sitamtawala tena—
27 Na pia nitakubali kwamba ndugu zako waondolewe gerezani, na wewe na ndugu
zako mnaweza kunijia, katika ufalme wangu; kwani nitatamani kukuona. Kwani
mfalme alistaajabia sana kwa yale maneno aliyozungumza, na pia yale maneno
ambayo mwana wake Lamoni alikuwa amezungumza, kwa hivyo alitaka kujifunza.
28 Na ikawa kwamba Amoni na Lamoni waliendelea na safari yao ya kuelekea nchi
ya Midoni. Na Lamoni alipata fadhila za mfalme wa nchi; kwa hivyo ndugu za
Amoni waliondolewa gerezani.
29 Na Amoni alipowaona alikuwa na huzuni sana, kwani tazama walikuwa uchi, na
ngozi zao zilikuwa zimenyauka sana kwa sababu ya kufungwa kwa kamba nzito. Na
pia walikuwa wamepatwa na njaa, kiu, na kila aina ya mateso; walakini walivumilia
mateso yao yote.
30 Na, kama vile ilivyotendeka, ilikuwa ni mkosi wao kuchukuliwa na mikono ya
watu ambao walikuwa ni wagumu zaidi, na wenye shingo ngumu zaidi; kwa hivyo
hawangesikiliza maneno yao, na waliwafukuza, na kuwapiga, na kuwakimbiza
kutoka nyumba hadi nyumba, na kutoka mahali hadi mahali, hadi wakafika katika
nchi ya Midoni; na hapo walichukuliwa na kutupwa gerezani, na kufungwa kwa
kamba nzito, na kuwekwa gerezani kwa siku nyingi, na wakakombolewa na Lamoni
na Amoni.

*Maandishi ya mahubiri ya Haruni, na Muloki, na ndugu zao, kwa Walamani.*

# Alma 21

1 Sasa wakati Amoni na ndugu zake walijigawanya katika mipaka ya nchi ya
Walamani, tazama Haruni alisafiri kuelekea nchi iliyoitwa na Walamani,
Yerusalemu, ambayo iliitwa kulingana na nchi ya kuzaliwa ya babu zao; na ilikuwa
na mipaka ya Mormoni.
2 Sasa Walamani na Waamaleki na watu wa Amuloni walikuwa wamejenga mji
mkubwa, ambao uliitwa Yerusalemu.
3 Sasa Walamani wenyewe walikuwa ni wagumu kabisa, lakini Waamaleki na
Waamuloni walikuwa ni wagumu zaidi; kwa hivyo wakawasababisha Walamani
washupaze mioyo yao, kwamba waendelee na maovu yao na machukizo yao.
4 Na ikawa kwamba Haruni alifika katika mji wa Yerusalemu, na kwanza akaanza
kuwahubiria Waamaleki. Na akaanza kuwahubiria katika masinagogi yao, kwani
walikuwa wamejenga masinagogi kulingana na desturi za Wanehori; kwani wengi
wa Waamaleki na Waamuloni walikuwa wafuasi wa Wanehori.
5 Kwa hivyo, Haruni alipoingia katika moja ya masinagogi yao ili awahubirie watu,
na alipokuwa akiwazungumzia, tazama Mwamaleki mmoja alisimama na akaanza
kubishana na yeye, akisema: Ni nini ambacho wewe umeshuhudia? Wewe umeona
malaika? Kwa nini malaika hawatutokei sisi? Tazama si watu hawa ni wema kama
watu wako?
6 Wewe pia unasema, tusipotubu tutaangamia. Jinsi gani wewe unajua mawazo na
nia ya mioyo yetu? Jinsi gani unavyojua kwamba tunayo sababu ya kutubu? Jinsi
gani unavyojua kwamba sisi sio watu wenye haki? Tazama, tumejenga makao

matakatifu, na sisi huwa tunakusanyika pamoja kumwabudu Mungu. Tunaamini
kwamba Mungu ataokoa wanadamu wote.
7 Sasa Haruni akamwambia: Unaamini kwamba Mwana wa Mungu atakuja
kuwakomboa wanadamu kutoka dhambi zao?
8 Na yule mtu akamwambia: Hatuamini kwamba wewe unajua kitu kama hicho.
Hatuamini katika desturi za kijinga kama hizi. Hatuamini kwamba wewe unajua
vitu vile vitakavyokuja, wala hatuamini kwamba baba zako na pia kwamba baba zetu
walijua kuhusu vitu vile walivyozungumza, yaani vile vitakavyokuja.
9 Sasa Haruni akaanza kuwafungulia maandiko kuhusu kuja kwa Kristo, na pia
kuhusu ufufuo wa wafu, na kwamba hakutakuwa na ukombozi kwa wanadamu ila tu
kwa mauti na mateso ya Kristo, na upatanisho wa damu yake.
10 Na ikawa kwamba alipoanza kuwafafanulia vitu hivi walimkasirikia, na wakaanza
kumfanyia mzaha; na hawakutaka kusikia maneno aliyozungumza.
11 Kwa hivyo, alipoona kwamba hawakutaka kusikia maneno yake, aliondoka katika
sinagogi yao, na akaenda katika kitongoji kilichoitwa Ani-Anti, na hapo akampata
Muloki akiwahubiria neno; na pia Ama na ndugu zake. Na wakabishana na wengi
kuhusu neno.
12 Na ikawa kwamba waliona kuwa watu watashupaza mioyo yao, kwa hivyo
wakaondoka na kufika katika nchi ya Midoni. Na wakahubiri neno kwa wengi, na
wachache wakaamini maneno ambayo walifundisha.
13 Walakini, Haruni na idadi fulani ya ndugu zake walishikwa na kutupwa gerezani,
na waliosalia wakatoroka nchi ya Midoni na kuelekea katika sehemu zile
zilizoizingira.
14 Na wale ambao walitupwa gerezani waliteseka kwa vitu vingi, na walikombolewa
kwa mkono wa Lamoni na Amoni, na wakalishwa na kuvishwa.
15 Na wakaenda tena kutanganza neno, na hivyo walikombolewa mara ya kwanza
kutoka gerezani, na hivyo waliteseka.
16 Na walienda popote walipoongozwa na Roho wa Bwana, wakihubiri neno la
Mungu katika kila sinagogi la Waamaleki, au katika kila kusanyiko la Walamani
lililowakaribisha.
17 Na ikawa kwamba Bwana alianza kuwabariki, hata wakaweza kuleta wengi kwa
ufahamu wa ukweli; ndio, waliwasadikisha wengi kuhusu dhambi zao, na desturi za
babu zao, ambazo hazikuwa sawa.
18 Na ikawa kwamba Amoni na Lamoni walirudi kutoka katika nchi ya Midoni na
kwenda katika nchi ya Ishmaeli, ambayo ilikuwa ni nchi yao ya urithi.
19 Na mfalme Lamoni hangekubali kwamba Amoni amtumikie, au awe mtumishi
wake.
20 Lakini alisababisha kwamba masinagogi yajengwe katika nchi ya Ishmaeli; na
akasababisha kwamba watu wake, au watu wale waliokuwa chini ya utawala wake,
wakusanyike pamoja.
21 Na alifurahi juu yao, na akawafunza vitu vingi. Na pia aliwatangazia kwamba
wao ni watu waliokuwa chini ya utawala wake, na kwamba walikuwa watu huru, na
kwamba walikuwa huru kutokana na udhalimu wa mfalme, baba yake; kwani baba
yake alikuwa amemruhusu atawale watu waliokuwa katika nchi ya Ishmaeli, na
katika sehemu iliyowazingira.
22 Na pia akawaambia kwamba wangekuwa na uhuru wa kumwabudu Bwana
Mungu wao kulingana na mahitaji yao, katika mahali popote walipo, ikiwa ilikuwa

katika nchi ile iliyokuwa chini ya utawala wa mfalme Lamoni.
23 Na Amoni akawahubiria watu wa mfalme Lamoni; na ikawa kwamba aliwafunza
vitu vyote vilivyohusu vitu vya haki. Na akawaonya kila siku, kwa bidii zote; na
wakasikiza neno lake, na walikuwa na bidii ya kushika amri za Mungu.

# Alma 22

1 Sasa, vile Amoni alikuwa hivyo alikuwa anafundisha watu wa Lamoni bila kikomo,
tutarudia historia ya Haruni na ndugu zake; kwani baada ya kuondoka kutoka
kwenye nchi ya Midoni aliongozwa na Roho hadi kwenye nchi ya Nefi, hata kwenye
nyumba ya mfalme ambaye alikuwa anasimamia nchi yote isipokuwa nchi ya
Ishmaeli; na alikuwa baba ya Lamoni.
2 Na ikawa kwamba alimwendea kwenye nyumba ya mfalme, na ndugu zake, na
akasujudu mbele ya mfalme, na kusema kwake: Tazama, Ee mfalme, sisi ni ndugu za
Amoni, ambaye ulimwachilia huru kutoka gerezani.
3 Na sasa, Ee mfalme, ikiwa utasalimisha maisha yetu, tutakuwa watumishi wako.
Na mfalme akawaambia: Amkeni, kwani nitamruhusu muishi, na sitakubali muwe
watumishi wangu; lakini nitasisitiza kwamba mnitumikie, kwani nimesumbuliwa
kidogo rohoni mwangu kwa sababu ya ukarimu mkuu wa maneno ya ndugu yako
Amoni; na ninatamani kujua sababu iliyomfanya asitoke na nyinyi Midoni.
4 Na Haruni akamwambia mfalme: Tazama, Roho wa Bwana amemtuma mahali
pengine; ameenda kwenye nchi ya Ishmaeli, kuwafundisha watu wa Lamoni.
5 Sasa mfalme akamwambia: Ni nini mlimaanisha mliposema Roho ya Bwana?
Tazama, hiki ndicho kinanitaabisha mimi.
6 Na pia, ni nini hii ambayo Amoni alisema — Ikiwa mtatubu mtasamehewa, na
ikiwa hamtatubu, mtatupiliwa mbali siku ya mwisho?
7 Na Haruni akamjibu na kumwambia: Unaamini wewe kwamba kuna Mungu?
Na mfalme akasema: Ninajua kwamba Waamaleki wanasema kwamba kuna Mungu,
na nimewaruhusu kwamba wajenge makanisa, kwamba wangekusanyika pamoja
kumwabudu. Na sasa ikiwa unasema kuna Mungu, tazama, nitaamini.
8 Na sasa Haruni aliposikia hivi, moyo wake ulianza kufurahi, na akasema:
Tazama, kwa hakika vile unavyoishi, Ee mfalme, kuna Mungu.
9 Na mfalme akasema: Mungu ni yule Roho Mkuu aliyewaleta babu zetu kutoka
nchi ya Yerusalemu?
10 Na Haruni akamwambia: Ndio, ni yule Roho Mkuu, na aliumba vitu vyote
mbinguni na ardhini. Unaamini hivi wewe?
11 Na akasema: Ndio, ninaamini kuwa Roho Mkuu aliumba vitu vyote, na ninataka
kwamba uniambie kuhusu hivi vitu vyote, na nitaamini maneno yako.
12 Na ikawa kwamba wakati Haruni alipoona kwamba Mfalme angeamini maneno
yake, alianzia tangu Adamu alivyoumbwa, akisoma maandiko kwa mfalme — vile
Mungu alivyomuumba mwanadamu kwa mfano wake mwenyewe, na kwamba
Mungu alimpatia amri, na kwa sababu ya dhambi, binadamu alikuwa ameanguka.
13 Na Haruni akamwelezea maandiko kuanzia uumbaji wa Adamu, akimwelezea
binadamu alivyoanguka, na hali ya kimwili sasa na pia mpango wa ukombozi,
ambao ulitayarishwa tangu uumbaji wa ulimwengu, kupitia kwa Kristo, kwa wote
ambao wataamini katika jina lake.
14 Na kwa sababu binadamu alikuwa ameanguka hangeweza kustahili chochote

mwenyewe; isipokuwa mateso na kifo cha Kristo hulipia dhambi zao, katika imani
na kutubu, na vingine; na kwamba hukata kamba za kifo, kwamba kaburi
halitakuwa na ushindi, na kwamba uchungu wa kifo utashindwa katika matumaini
ya utukufu; na Haruni alieleza hivi vitu vyote kwa mfalme.
15 Na ikawa kwamba baada ya Haruni kumwelezea hivi vitu, mfalme alisema:
Nitafanya nini ili nipate uzima wa milele ambao umeuzungumzia? Ndio, nitafanya
nini ili nizaliwe kwa Mungu, ili hii roho mbovu ing'olewe nje ya mwili wangu, na
nipokee Roho yake, ili niweze kujazwa na shangwe, ili nisitupiliwe nje siku ya
mwisho? Tazama, alisema, nitatoa umiliki wangu wote, ndio, nitaacha ufalme
wangu, ili nipokee hii shangwe kuu.
16 Lakini Haruni alimwambia: Ikiwa unatamani kitu hiki, ikiwa utamsujudia
Mungu, ndio, ikiwa utatubu dhambi zako zote, na umsujudie Mungu, na umlingane
kwa imani, ukiamini kwamba utapokea, ndipo utakapopokea matumaini ambayo
unatamani.
17 Na ikawa kwamba Haruni aliposema maneno haya, mfalme alisujudu mbele ya
Bwana, kwa magoti yake; ndio, hata akajilaza kifudifudi ardhini, na kulia kwa
nguvu, akisema:
18 Ee Mungu, Haruni ameniambia kwamba kuna Mungu; na ikiwa kuna Mungu, na
ikiwa wewe ni Mungu, unaweza kujitambulisha kwangu, na nitaacha dhambi zangu
zote ili nikujue wewe, na kwamba niinuliwe kutoka kwa wafu, na niokolewe siku ya
mwisho. Na sasa wakati mfalme alipokuwa amesema maneno haya, alianguka akawa
kama amekufa.
19 Na ikawa kwamba wafanyi kazi wake walikimbia na kumwambia malkia yote
ambayo yalikuwa yametendeka kwa mfalme. Na akaja mahali ambapo mfalme
alikuwa; na alipomwona amelala kama aliyekufa, na pia Haruni na ndugu zake
wakisimama kama ndio waliosababisha kuanguka kwake, aliwakasirikia, na
kuamuru kwamba watumishi wake, au watumishi wa mfalme, wawachukue na
kuwaua.
20 Sasa watumishi walikuwa wameona kilichosababisha mfalme kuanguka, kwa
hivyo hawakuthubutu kushika Haruni na ndugu zake; na wakamsihi malkia
wakisema: Kwa nini unatuamrisha tuue watu hawa, ikiwa tazama, mmoja wao yu
mkuu kuliko sisi zote? Kwa hivyo wanaweza kutuua.
21 Sasa wakati malkia aliona woga wa watumishi, yeye pia alianza kuogopa sana,
kwamba maovu yasimjie. Na akawaamrisha watumishi wake kwamba waende na
kuita watu, ili wawaue Haruni na ndugu zake.
22 Sasa Haruni alipoona kusudi la malkia, yeye, pia akijua ugumu wa mioyo ya
watu, aliogopa kwamba umati utakusanyika pamoja, na kuwe na ubishi mwingi na
msukosuko miongoni mwao; kwa hivyo alinyosha mkono wake na kumuinua
mfalme kutoka chini, na akamwambia: Simama. Na akasimama, miguu yake ikipata
nguvu zake.
23 Sasa hii ilifanyika machoni mwa malkia na watumishi wengi. Na walipoiona
walishangaa sana, na kuanza kuogopa. Na mfalme alisimama mbele, na kuanza
kuwahudumia. Na aliwahudumia, jinsi kwamba jamii yake yote ilimgeukia Bwana.
24 Sasa kulikuwa na umati uliokusanyika kwa sababu ya amri ya malkia, na kukawa
na manung'uniko mengi miongoni mwao kwa sababu ya Haruni na ndugu zake.
25 Lakini mfalme alisimama mbele miongoni mwao na kuanza kuwahudumia. Na
walitulizwa juu ya Haruni na wale ambao walikuwa na yeye.

26 Na ikawa kwamba wakati mfalme aliona kwamba watu wametulia, alisababisha
kwamba Haruni na ndugu zake wasimame na kusogea katikati ya umati, na kwamba
wawahubirie neno.
27 Na ikawa kwamba mfalme alitoa tangazo nchini kote, miongoni mwa watu wake
wote ambao walikuwa kwenye nchi yake yote, ambao walikuwa ndani ya mikoa yote
iliyokaribiana, hata karibu na bahari, upande wa mashariki na upande wa magharibi,
na ambayo ilitengwa kutoka nchi ya Zarahemla na kipande chembamba cha nyika,
ambayo ilinyooka kutoka mashariki ya bahari hadi magharibi ya bahari, karibu na
mipaka ya pwani, na mipaka ya nyika ambao ulikuwa kaskazini karibu na nchi ya
Zarahemla, kupitia mipaka ya Manti, kupitia kando ya mto wa Sidoni, kutoka
mashariki hadi magharibi — na hivyo ndivyo Walamani na Wanefi
walivyotenganishwa.
28 Sasa, sehemu kubwa ya Walamani ambao walikuwa wazembe waliishi nyikani, na
kuishi kwenye hema; na walikuwa wametawanyika upande wa magharibi, katika
nchi ya Nefi; ndio, na pia kwenye magharibi ya nchi ya Zarahemla, kwenye sehemu
ya ukingo wa bahari, na magharibi kwenye nchi ya Nefi, mahali ambapo babu zao
walirithi mbeleni, na hivyo ikipakana na ukingo wa bahari.
29 Na pia kulikuwa na Walamani wengi mashariki karibu na ukingo wa bahari,
ambapo Wanefi waliwasukuma. Na hivyo Wanefi walizingirwa na Walamani;
ingawaje Wanefi walikuwa wamemiliki sehemu ya kaskazini mwa nchi inayopakana
na nyika, kwenye chimbuko ya mto Sidoni, kutoka mashariki, hadi magharibi,
ikizunguka upande wa nyika; upande wa kaskazini, hata wakaja kwa nchi ambayo
waliita Neema.
30 Na ilikuwa imepakana na nchi waliyoiita Ukiwa, ikiwa mbali sana kaskazini
kwamba iliingia katika nchi iliyokaliwa na watu na kuharibiwa, ambayo mifupa yake
tumeizungumzia, ambayo iligunduliwa na watu wa Zarahemla, ikawa mahali
ambapo walishukia kwanza.
31 Na walikuja kutokea kule juu hadi kwenye nyika ya kusini. Hivyo nchi ya
kaskazini iliitwa Ukiwa, na nchi ya kusini iliitwa Neema, ikiwa nyika ambayo
imejazwa na wanyama wa kila aina, ambao wengine wao walitoka katika nchi ya
kaskazini kwa ajili ya chakula.
32 Na sasa, ilikuwa tu mwendo wa siku moja na nusu kwa usafiri wa Mnefi, kwenye
mpaka miongoni mwa Neema na nchi ya Ukiwa, kutoka mashariki hadi kwenye
bahari ya magharibi; na hivyo nchi ya Nefi na nchi ya Zarahemla zilikuwa karibu
zimezingirwa na maji, kukiwa na kijisehemu cha nchi katikati ya nchi iliyo kaskazini
na nchi iliyo kusini.
33 Na ikawa kwamba Wanefi walikuwa wameimiliki nchi ya Neema, hata kutokea
mashariki hadi kwenye bahari ya magharibi, na hivyo Wanefi kwa hekima yao, na
walinzi wao na majeshi yao, walikuwa wamewafungia Walamani upande wa kusini,
kwa hivyo wasiwe tena na umiliki kaskazini, ili wasiweze kupita na kuleta vita
kaskazini.
34 Kwa hivyo Walamani hawangemiliki kitu kingine isipokuwa tu nchi ya Nefi, na
nyika iliyokuwa karibu. Sasa hii ilikuwa hekima kwa Wanefi — kwani Walamani
walikuwa maadui kwao, hawangekubali mateso yao yatokee kila upande, na pia ili
wapate nchi ambayo wangekimbilia, kulingana na mahitaji yao.
35 Na sasa mimi baada ya kusema haya, narudia tena historia ya Amoni na Haruni,
Omneri na Himni, na ndugu zao.

# Alma 23

1 Tazama, sasa ikawa kwamba mfalme wa Walamani alituma tangazo miongoni mwa
watu wake wote, kwamba wasimuumize Amoni, au Haruni, au Omneri, au Himni,
wala mmoja wao wa ndugu zao ambao ataenda mbele na kuhubiri neno la Mungu,
mahali popote watakaokuwa, kwenye sehemu yoyote ya nchi yao.
2 Ndio, alitoa amri miongoni mwao, kwamba wasiwashike na kuwafunga mikono
yao, au kuwatupa kwenye gereza; wala wasiwatemee mate, wala kuwapiga, wala
kuwatupa nje ya masinagogi yao, wala kuwaadhibu; wala wasiwatupie mawe, lakini
kwamba waruhusiwe kwenye nyumba zao, na pia kwenye mahekalu yao, na mahali
pao patakatifu.
3 Na hivyo wangeweza kwenda mbele, na kuhubiri neno kulingana na kutaka
kwao, kwani mfalme alikuwa amemgeukia Bwana, na jamii yake yote; kwa hivyo
alitoa tangazo lake nchini kote kwa watu, kuwa neno la Mungu lisizuiliwe, lakini
kwamba lingeenda kote kwenye nchi yote, kwamba watu wake wangesadikishwa
kuhusu mila mbovu za babu zao, na kwamba wangesadikishwa kwamba wote
walikuwa ndugu, na kwamba wanapaswa wasiue, wala kunyang'anya, wala kuiba,
wala wasitende uzinzi, wala kutenda aina yoyote ya maovu.
4 Na sasa ikawa kwamba mfalme alipotuma mbele hili tangazo, kwamba Haruni na
ndugu zake walienda kutoka mji mmoja hadi mwingine, na kutoka kwenye nyumba
moja ya ibada hadi nyingine, wakianzisha makanisa, na wakiweka wakfu makuhani
na walimu kote nchini miongoni mwa Walamani, kuhubiri na kufundisha neno la
Mungu miongoni mwao; na hivyo walianza kufanikiwa kwa wingi.
5 Na maelfu waliletwa kwenye ufahamu wa Bwana, ndio, maelfu waliletwa
kuamini desturi za Wanefi; na walifundishwa maandiko na unabii ambao ulikuwa
umetolewa tangu zamani hadi wakati huu.
6 Na kwa kweli kama vile Bwana anavyoishi, kwa hakika vile wengi walivyoamini,
au vile wengi walielimishwa kwa ukweli, kupitia kwa uhubiri wa Amoni na ndugu
zake, kulingana na roho ya ufunuo na ya unabii, na uwezo wa Mungu ukifanya
miujiza ndani yao — ndio, nawaambia nyinyi, vile Bwana anavyoishi, vile wengi wa
Walamani walivyoamini kuhubiri kwao, na wakamgeukia Bwana, hawakuanguka
kamwe kutoka kanisa.
7 Kwani walipata kuwa watu wenye haki na wakaweka chini silaha zao za uasi,
kwamba hawangeweza kupigana na Mungu tena, wala dhidi ya yeyote wa ndugu zao.
8 Sasa, hawa ndio wale waliomgeukia Bwana:
9 Watu wa Walamani ambao walikuwa kwenye nchi ya Ishmaeli;
10 Na pia watu wa Walamani ambao walikuwa kwenye nchi ya Midoni;
11 Na pia watu wa Walamani ambao walikuwa kwenye mji wa Nefi;
12 Na pia watu wa Walamani ambao walikuwa kwenye nchi ya Shilomu, na katika
nchi ya Shemloni, na katika mji wa Lemueli, na katika mji wa Shimnilomu.
13 Na haya ndiyo majina ya miji ya Walamani ambayo ilimgeukia Bwana; na hii
ndiyo iliweka chini silaha zao za uasi, ndio, silaha zao zote za vita; na wote walikuwa
Walamani.
14 Na Waamaleki hawakugeuka, isipokuwa tu mmoja; wala hakukuweko yeyote kwa
Waamuloni; lakini walishupaza mioyo yao, na pia mioyo ya Walamani kwenye hiyo
sehemu ya nchi popote walipoishi, ndio, na kwenye vijiji vyao vyote na miji yao yote.
15 Kwa hivyo, tumeitaja miji yote ya Walamani ambamo walitubu na kupata
ufahamu wa ukweli, na wakageuka.

16 Na sasa ikawa kwamba mfalme na wote ambao waligeuka walitaka kwamba
wawe na jina, ambalo lingewatofautisha na ndugu zao; kwa hivyo mfalme
akashauriana na Haruni na wengi wa makuhani, kuhusu jina ambalo wangejiita, ili
waweze kujitambulisha.
17 Na ikawa kwamba walijiita Anti-Nefi-Lehi; na waliitwa kwa jina hili na
hawakuitwa tena Walamani.
18 Na walianza kuwa watu wenye kushika kazi sana; ndio, na wakawa marafiki wa
Wanefi; kwa hivyo, wakaanza mawasiliano nao, na lawama ya Mungu haikuwa kwao
tena.

## Alma 24

1 Na ikawa kwamba Waamaleki na Waamuloni na Walamani ambao walikuwa katika
nchi ya Amuloni, na pia kwenye nchi ya Helamu, na waliokuwa kwenye nchi ya
Yerusalemu, na kwa kifupi, kwenye nchi yote karibu, ambao hawakuwa wamegeuka
na hawakuwa wamechukua jina la Anti-Nefi-Lehi, walichochewa na Waamaleki na
Waamuloni kuwakasirikia ndugu zao.
2 Na chuki yao ilikuja kuwa jeraha kubwa juu yao, hata kwa kiasi kwamba walianza
kuasi juu ya mfalme wao, hata ikawa hawataki awe mfalme wao; kwa hivyo,
walichukua silaha na kuwakabili watu wa Anti-Nefi-Lehi.
3 Sasa mfalme alimpa mwana wake ufalme, na akamuita jina la Anti-Nefi-Lehi.
4 Na mfalme akafariki mwaka huo huo ambao Walamani walianza kufanya
matayarisho ya kukabiliana na watu wa Mungu.
5 Sasa Amoni na ndugu zake na wote waliokuja na yeye walipoona matayarisho ya
Walamani kuwaangamiza ndugu zao, walienda mbele kwenye nchi ya Midiani, na
huko Amoni alikutana na ndugu zake wote; na kutokea hapo walienda kwa nchi ya
Ishmaeli ili wawe na baraza na Lamoni na pia kaka yake Anti-Nefi-Lehi, wajue cha
kufanya kujikinga kutokana na Walamani.
6 Sasa hakukuwa hata mtu mmoja miongoni mwa wote waliokuwa wamemgeukia
Bwana ambaye angechukua silaha dhidi ya ndugu zao; hapana, hawangeweza
kufanya matayarisho ya vita; ndio, hata mfalme wao aliwaamuru wasifanye hivyo.
7 Sasa haya ndiyo maneno ambayo aliwaambia watu kuhusu hili tatizo:
Ninamshukuru Mungu wangu, wapendwa wangu, kwamba Mungu wetu mkuu kwa
wema amewatuma hawa ndugu zetu, Wanefi, kwetu kutuhubiria, na kutusadikisha
sisi kwa desturi za babu zetu waovu.
8 Na tazama, ninamshukuru Mungu wangu mkuu kwamba ametushawishi na roho
yake na kulainisha mioyo yetu, kwamba tumeanza mawasiliano na hawa ndugu
Wanefi.
9 Na tazama, pia ninamshukuru Mungu wangu, kwamba kwa kuanzisha
mawasiliano tumesadikishwa dhambi zetu, na mauaji mengi ambayo tumetenda.
10 Na pia ninamshukuru Mungu wangu, ndio, Mungu wangu mkuu, kwamba
ametujalia kwetu sisi kwamba tutubu juu ya vitu hivi, na pia kwamba ametusamehe
sisi kwa hizo dhambi zetu na mauaji mengi ambayo tumetenda, na kututolea mbali
hatia kutoka kwenye mioyo yetu, kupitia kwa matendo mema ya Mwana wake.
11 Na sasa tazama, ndugu zangu, vile imekua yote ambayo tungetenda (kwa vile sisi
tulikuwa wapotevu zaidi miongoni mwa wanadamu wote) kutubu dhambi zetu na
mauaji mengi tuliyotenda, na kupata Mungu kuziondoa kutoka mioyo yetu, kwani

ni hii tu tungefanya kutubu ya kutosha mbele ya Mungu kwamba angeondolea mbali hatia yetu —

12 Sasa, ndugu zangu wapendwa sana, vile Mungu ametuondolea mbali hatia zetu, na panga zetu, zimekuwa safi, basi tusichafue panga zetu tena na damu ya ndugu zetu.

13 Tazama, ninawambia nyinyi, Hapana, acheni tuhifadhi panga zetu ili zisichafuliwe tena na damu ya ndugu zetu; kwani huenda kama tunachafua panga zetu tena hazitaoshwa tena na kuwa safi kupitia kwa damu ya Mwana wa Mungu wetu mkuu, ambayo itatiririka kwa upatanisho wa dhambi zetu.

14 Na Mungu mkuu amekuwa na huruma kwetu, na kusabisha hivi vitu kujulikana kwetu ili tusiangamie; ndio, na amesababisha hivi vitu kujulikana kwetu mbeleni, kwa sababu anapenda nafsi zetu vile anapenda watoto wetu; kwa hivyo, kwa rehema yake hututembelea sisi kupitia malaika wake, ili mpango wa wokovu usababishwe kujulikana kwetu na pia uzazi ujao.

15 Ee, jinsi gani Mungu wetu ana huruma! Na sasa tazameni, vile imekuwa kazi ngumu kutoa dhambi kutoka kwetu, na panga zetu zimefanywa safi, acha tuzifiche mbali ili zibaki ziking'ara, kama ushuhuda kwa Mungu wetu katika siku ya mwisho, ama katika siku ambayo tutaletwa kusimama mbele yake kuhukumiwa, kwamba hatujazichafua panga zetu na damu ya ndugu zetu tangu atoe neno lake kwetu na kwa hivyo kutufanya sisi tuwe safi.

16 Na sasa, ndugu zangu, ikiwa ndugu zetu wanatutafuta kutuangamiza, tazama, tutaficha panga zetu mbali, ndio, hata kuzizika udongoni, ili zihifadhiwe zikiwa safi, kama ushuhuda kwamba hatujazitumia, katika siku ya mwisho; na ikiwa ndugu zetu watatuangamiza, tazama, tutaenda kwa Mungu wetu na tutaokolewa.

17 Na sasa ikawa kwamba mfalme alipokuwa amemaliza kuzungumza hii misemo, na watu wote walikuwa wamekusanyika pamoja, walichukua panga zao, na silaha zote ambazo zilitumiwa kwa kumwaga damu ya wanadamu, na wakazizika chini mchangani.

18 Na hii walifanya, ikiwa kwa maoni yao ushuhuda kwa Mungu, na pia kwa binadamu, kwamba hawatatumia silaha tena kumwaga damu ya binadamu; na walifanya hii, ili kudhibitisha na kuagana na Mungu, kwamba badala ya kumwaga damu ya ndugu zao wangetoa maisha yao; na badala ya kuchukua kutoka kwa ndugu wangepeana kwake na badala ya kukaa bila kufanya kitu wangefanya kazi kwa bidii kwa mikono yao.

19 Na hivyo tunaona kwamba, wakati hawa Walamani walipoelekezwa kujua ukweli, walikuwa imara, na wangeumia hata kwenye kifo kuliko kutenda dhambi; na hivyo tunaona kwamba walizika silaha zao za amani, au walizika silaha za vita, kwa amani.

20 Na ikawa kwamba ndugu zao, Walamani, walijiandaa kwa vita, na wakaja kwenye nchi ya Nefi kwa nia ya kumwangamiza mfalme, na kumweka mwingine badala yake, na pia kumwangamiza watu wa Anti-Nefi-Lehi wasiwe nchini.

21 Sasa wakati walipoona kwamba wanakabiliwa waliondoka na kukutana nao, na kujilaza mchangani mbele yao, na kuanza kulilingana kwa jina la Bwana; na hivyo walikuwa katika hali ile wakati Walamani walipoanza kuwashambulia, na wakaanza kuwachinja kwa upanga.

22 Na hivyo bila kuwa na pingamizi, waliwachinja elfu moja na watano wao; na tunajua kwamba wamebarikiwa, kwani wameenda kuishi na Mungu wao.

23 Sasa wakati Walamani waliona kwamba ndugu zao hawakimbii kutoka kwa

upanga, wala hawageuki upande wa kulia au kushoto, lakini kwamba wangelala chini na kuangamia, na kumsifu Mungu hata wakifa kwa upanga—

24 Sasa Walamani walipoona hivi waliacha kuwachinja; na kulikuwa wengi ambao mioyo yao ilikuwa imevimba ndani yao kwa ajili ya ndugu zao ambao waliangukiwa na upanga, hata wakatubu kwa vitu ambavyo walikuwa wamefanya.

25 Na ikawa kwamba walitupa silaha zao za vita chini, na hawangezichukua tena, kwani walikuwa na uchungu kwa mauaji ambayo walikuwa wamefanya; na walilala chini kama ndugu zao, wakitegemea huruma ya wale silaha zao zilizokuwa zimeinuliwa kuwachinja.

26 Na ikawa kwamba watu wa Mungu waliungwa siku ile na ibada kubwa kuliko ya wale ambao walikuwa wameuawa; na wale ambao waliuawa walikuwa watu wenye haki, kwa hivyo hatuna sababu ya kuwa na shaka kwamba waliokolewa.

27 Na hakukuwa na mtu mwovu aliyechinjwa miongoni mwao; lakini kulikuwa na zaidi ya elfu moja walioelimishwa kwa ukweli; hivyo tunaona kwamba Bwana hutumia njia nyingi ili kuokoa watu wake.

28 Sasa idadi kubwa sana ya wale Walamani ambao waliua ndugu zao wengi walikuwa Waamaleki na Waamuloni, idadi kubwa ambayo ilikuwa kulingana na shirika la Wanehori.

29 Sasa, miongoni mwa wale ambao walijiunga na watu wa Bwana, hakukuwepo na Waamaleki au Waamuloni, au ambao walikuwa na desturi ya Nehori, lakini walikuwa hasa watoto wa Lamani na Lemueli.

30 Na hivyo tunaweza kuona wazi, kwamba baada ya watu kuelimishwa na Roho wa Mungu, na wana ufahamu mkuu wa vitu ambavyo vinahusikana na haki, na tena waingie tena kwenye makosa na dhambi, wanakuwa wagumu zaidi, na hivyo hali yao huwa mbaya zaidi kama kwamba hawakujua vitu hivi.

# Alma 25

1 Na tazama, sasa ikawa kwamba wale Walamani walikuwa na hasira sana kwa sababu walikuwa wamewaua ndugu zao; kwa hivyo waliapa kulipiza kisasi juu ya Wanefi; na hawakujaribu mara nyingine tena kuua watu wa Anti-Nefi-Lehi kwa wakati huo.

2 Lakini walichukua majeshi yao na wakaenda juu kwenye mipaka ya nchi ya Zarahemla, na kuwashambulia watu ambao walikuwa kwenye nchi ya Amoniha na kuwaangamiza.

3 Na baada ya hayo, walikuwa na vita vingi na Wanefi, ambako walikimbizwa na kuuawa.

4 Na miongoni mwa Walamani ambao waliuawa karibu wote walikuwa uzao wa Amuloni na ndugu zake, ambao walikuwa makuhani wa Nuhu, na waliuawa kwa mikono ya Wanefi;

5 Na waliosalia, wakikimbilia kwenye nyika ya mashariki, na wakijitwalia uwezo na mamlaka juu ya Walamani, walisababisha kwamba wengi wa Walamani waangamizwe kwa moto kwa sababu ya imani yao—

6 Kwa sababu wengi wao, baada ya kuumia kwa hasara nyingi na mateso mengi, walianza kuvurugwa na kukumbuka maneno ambayo Haruni na ndugu zake waliwahubiria nchini mwao; kwa hivyo, walianza kutoamini desturi za babu zao, na kuamini katika Bwana, na kwamba aliwapa Wanefi uwezo mwingi; na hivyo kulikuwa na wengi wao ambao waligeuka nyikani.

7 Na ikawa kwamba wale watawala ambao walikuwa sazo la watoto wa Amuloni
walisababisha kwamba wauawe, ndio, wale wote ambao waliamini katika vitu hivi.
8 Sasa haya mauaji yalisababisha kwamba wengi wa ndugu zao wachochewe na
kukasirika; na kukaanza kuwa na ubishi nyikani; na Walamani wakaanza kufuata
uzao wa Amuloni na ndugu zake na kuanza kuwaua; na wakakimbilia upande wa
mashariki ya nyika.
9 Na tazama wanatafutwa hadi siku hii na Walamani. Hivyo maneno ya Abinadi
yalitimizwa, ambayo alisema kuhusu uzao wa makuhani ambao walisababisha
kwamba ateswe na kifo kwa moto.
10 Kwa sababu aliwaambia: Yale mtakayonifanyia yatakuwa mfano wa vitu
vitakavyokuja.
11 Na sasa Abinadi alikuwa wa kwanza aliyeumia kifo kwa moto kwa sababu ya
kuamini kwake katika Mungu; sasa hivi ndivyo alivyomaanisha, kwamba wengi
wataumia kifo kwa moto, kulingana na vile alivyoumia.
12 Na akawaambia makuhani wa Nuhu kwamba uzao wao utasababisha wengi
wauawe, kwa njia sawa vile alivyokuwa, na kwamba watatawanyika nje na kuuawa,
hata vile kondoo huwa kama hawana mlinzi hukimbizwa na kuuawa na wanyama wa
mwitu; na sasa tazama, haya maneno yalithibitishwa, kwani walikimbizwa na
Walamani, na waliwindwa, na kuuawa.
13 Na ikawa kwamba Walamani walipoona kwamba hawangeweza kuwashinda
Wanefi walirudi tena kwenye nchi yao; na wengi wao walienda kuishi kwenye nchi
ya Ishmaeli na nchi ya Nefi, na wakaungana na watu wa Mungu, ambao walikuwa
watu wa Anti-Nefi-Lehi.
14 Na pia walizika silaha zao za vita, vile ndugu zao walivyofanya, na wakaanza
kuwa watu wenye haki; na wakatembea kwa njia za Bwana, na kuchunguza na
kuweka amri zake na sheria zake.
15 Ndio, na walihifadhi sheria ya Musa; kwani ilikuwa ya manufaa kwamba
wahifadhi sheria ya Musa bado, kwani yote ilikuwa haijatimizwa. Lakini ijapokuwa
sheria ya Musa, walitazamia kuja kwa Kristo, wakifikiri kwamba sheria ya Musa
ilikuwa mfano wa kuja kwake, na kuamini kwamba lazima wahifadhi kutenda
mambo mengine hadi wakati ambao atafichuliwa kwao.
16 Sasa hawakufikiria kwamba wokovu ulikuja kwa sheria ya Musa; lakini sheria ya
Musa ilitumika kwa kuweka nguvu imani yao kwa Kristo; na hivyo waliweka
matumaini kupitia imani, kwa wokovu wa milele, wakitegemea roho ya unabii,
ambayo ilizungumzia vitu vinavyokuja.
17 Na sasa tazama, Amoni, na Haruni, na Omneri, na Himni, na ndugu zao
walifurahi sana, kwa ushindi ambao waliupata miongoni mwa Walamani, wakiona
kwamba Bwana alikuwa amewakubalia kulingana na sala zao, na kwamba alikuwa
amethibitisha neno lake kwao kwa jumla.

## Alma 26

1 Na sasa, haya ndiyo maneno ya Amoni kwa ndugu zake, ambayo yanasema hivi:
Ndugu zangu na jamaa zangu, tazama nawambia nyinyi, ni sababu kiasi gani tunayo
ya kutufanya tufurahi; kwani tungejuaje wakati tulipoanza safari yetu kutoka
Zarahemla kwamba Mungu angetubariki sisi hivi kwa wingi?
2 Na sasa, nauliza, ni baraka gani kubwa ambayo ametupatia sisi? Mnaweza

kunena?
3 Tazama, ninajibu kwa niaba yenu; kwani ndugu zetu, Walamani, walikuwa
gizani, ndio, hata kwenye shimo la giza kubwa sana, lakini tazama, ni wangapi
miongoni mwao wameletwa kuona mwangaza wa ajabu wa Mungu! Na hii ndiyo
baraka ambayo tumeteremshiwa, kwamba tumetengenezwa kuwa vyombo
mikononi mwa Mungu kuimarisha kazi hii kubwa.
4 Tazama, maelfu miongoni mwao wanafurahi, na kuletwa kwenye zizi la Mungu.
5 Tazama, shamba lilikuwa bivu, na heri nyinyi, kwani mlisukuma pepeto, na
mkavuna kwa nguvu, ndio, siku yote nzima mlifanya kazi; na tazama idadi ya
miganda yenu! Na itakusanywa kwenye maghala, ili isiharibiwe.
6 Ndio, haitaangushwa na dhoruba ya mvua siku ya mwisho; ndio, wala
haitatawanyishwa na vimbunga; lakini dhoruba itakapokuja itakusanywa pamoja,
kwamba dhoruba isiweze kuipenya; ndio, wala haitasukumwa na upepo mkali
popote adui atakapotaka kuipeleka.
7 Lakini tazama, wamo mikononi mwa Bwana wa mavuno, na ni wake; na
atawainua katika siku ya mwisho.
8 Libarikiwe jina la Mungu wetu; acheni tuimbe kwa sifa yake, ndio, wacha
tulishukuru jina lake takatifu, kwani yeye hufanya kazi ya haki milele.
9 Kwani kama hatungekuja kutoka kwa nchi ya Zarahemla, hawa ndugu zetu
wapendwa, ambao wametupenda sana, wangekuwa bado wanasumbuliwa na chuki
juu yetu, ndio, na wangekuwa pia wageni kwa Mungu.
10 Na ikawa kwamba baada ya Amoni kusema maneno haya, ndugu yake Haruni
alimkemea, akisema: Amoni, ninaogopa kwamba shangwe yako imekusababisha
kuelekea kujisifu.
11 Lakini Amoni alimwambia: Mimi sijisifu kwa nguvu yangu, wala kwa hekima
yangu; lakini tazama, shangwe yangu ni tele, ndio, moyo wangu umejawa na
shangwe, na nitafurahi ndani ya Mungu wangu.
12 Ndio, najua kwamba mimi si kitu; kulingana na nguvu zangu mimi ni mlegevu;
kwa hivyo sitaweza kujivuna mwenyewe, lakini nitajivuna katika Mungu wangu,
kwani kwa nguvu zake naweza kufanya vitu vyote; ndio, tazama, miujiza mingi
mikuu tumetenda kwenye nchi hii, ambayo kwayo tutasifu jina lake milele.
13 Tazama, ni maelfu mangapi ya ndugu zetu ambao amewaachilia kutoka kwa
uchungu wa jahanamu; na wamefanywa kuimba upendo ukomboao, na haya kwa
sababu ya uwezo wa neno lake, ambao uko ndani yetu, kwa hivyo, si tuna sababu
kuu ya kufurahi?
14 Ndio, tuna sababu ya kumsifu milele, kwani yeye ni Mungu Aliye Juu Sana, na
amewafungua ndugu zetu kutoka kwa minyororo ya jahanamu.
15 Ndio, walizungukwa na giza lisilo na mwisho na uharibifu; lakini tazama,
amewaleta kwenye mwangaza usio na mwisho, ndio, kwenye wokovu usio na
mwisho; na wamezungukwa na ukarimu usiolinganishwa wa mapenzi yake; ndio, na
tumekuwa vyombo mikononi mwake vya kufanya kazi hii kuu na ya kushangaza.
16 Kwa hivyo, wacha tusifu, ndio, tutamsifu Bwana; ndio, tutafurahi, kwani
shangwe yetu imejaa; ndio, tutamsifu Mungu wetu milele. Tazama, ni nani
anayeweza kufurahia sana kwa Bwana? Ndio, ni nani anaweza kuongea sana juu ya
uwezo wake mkuu, na huruma yake, na uvumilivu wake kwa watoto wa watu?
Tazama nasema kwenu, siwezi kusema sehemu ndogo ya yale ambayo ninahisi.
17 Ni nani ambaye angefikiria kwamba Mungu wetu angekuwa na huruma nyingi

hivyo ili kutuokoa kutoka kwenye hali yetu chafu, ya kutisha, na yenye dhambi?
18 Tazama, tulienda mbele, kwa hasira na vitisho vingi kuangamiza kanisa lake.
19 Ee basi, kwa nini hakutuweka sisi kwenye maangamizo ya kutisha, ndio, kwa nini hakuachilia panga lake la haki kutuangukia, na kutulaani sisi kwa kutukata tamaa milele?
20 Ee, roho yangu, kama ilivyo, iko karibu kukimbia kutoka kwa wazo hilo. Tazama, hakutumia haki yake kwetu, lakini kwa hekima yake kuu ametuleta sisi nje ya shimo lile lisilo na mwisho la kifo na taabu, hata kwenye wokovu wa roho zetu.
21 Na sasa tazama, ndugu zangu, ni mtu gani wa kawaida ambaye anajua vitu hivi? Nawaambia nyinyi, hakuna yeyote ambaye anaelewa hivi vitu, isipokuwa wenye kutubu.
22 Ndio, yule ambaye anatubu na kutimiza imani, na kutenda kazi nzuri, na kuomba wakati wote bila kikomo—kwa hawa inakubaliwa kujua siri za Mungu; ndio, kwa hawa imepeanwa kwa kufumbua vitu ambavyo havijawahi kufumbuliwa; ndio, na itakubaliwa kwa hawa kuleta watu kutubu, hata vile imekubaliwa kwetu kuleta hawa ndugu zetu kutubu.
23 Sasa mnakumbuka, ndugu zangu, kwamba tuliwaambia ndugu zetu kwenye nchi ya Zarahemla, tunaenda kwenye nchi ya Nefi, tuhubirie ndugu zetu, Walamani, na wakatucheka kwa madharau?
24 Kwani walituambia: Mnafikiri kwamba mnaweza kuwafahahamisha Walamani ukweli? Mnafikiri mnaweza kuwasadikisha Walamani makosa ya desturi za babu zao, wakiwa watu wenye shingo ngumu vile walivyo; ambao mioyo yao hufurahia kwa umwagaji wa damu; ambao siku zao zimetumika kwa maovu mabaya sana; ambao njia zao zimekuwa njia za mhalifu tangu mwanzo? Sasa ndugu zangu, mnakumbuka kwamba hii ndiyo ilikuwa lugha yao.
25 Na tena walisema: Acha tuchukue silaha dhidi yao, ili tuwaangamize na maovu yao kutoka nchini, kwa maana wanaweza kutupita na kutuua.
26 Lakini tazama, ndugu zangu wapendwa, tulikuja nyikani sio na nia ya kuwaangamiza ndugu zetu, lakini nia ilikuwa labda tungeponya wachache wao.
27 Sasa wakati mioyo yetu ilihuzunishwa, na tukawa karibu kurudi, tazama, Bwana alitufariji, na kusema: Nendeni miongoni mwa ndugu zenu, Walamani, na mvumilie mateso yenu kwa subira, na nitawapatia mafanikio.
28 Na sasa tazama, tumekuja, na tumekuwa miongoni mwao; na tumekuwa wavumilivu kwenye maumivu yetu, na tumevumilia aina yote ya masumbuko; ndio, tumesafiri kutoka nyumba hadi nyingine, tukitegemea huruma ya walimwengu—sio huruma ya walimwengu pekee lakini juu ya huruma za Mungu.
29 Na tumeingia kwenye nyumba zao na kuwafundisha, na tumewafundisha kwenye njia za miji yao; ndio, na tumewafundisha kwenye vilima vyao; na pia tumeingia kwenye hekalu zao na masinagogi yao na kuwafundisha; na tumetupwa nje, na kufanyiwa mzaha, na kutemewa mate, na kupigwa kwenye mashavu ya uso; na tumepigwa na mawe, na kuchukuliwa na kufungwa kwa kamba za nguvu, na kutupwa kwenye gereza; na kupitia kwa nguvu na hekima wa Mungu tumekombolewa tena.
30 Na tulivumilia aina yote ya mateso, na tulifanya haya yote, kwamba labda tungepata njia ya kuponya watu; na tulifikiri kwamba shangwe yetu ingejaa ikiwa labda tungekuwa na njia ya kuwaokoa wengine.
31 Sasa tazama, tungeweza kuona mbele na kuona matunda ya kazi zetu, na ni

wachache? Ninawaambia: Hapana, ni wengi; ndio, na tunaweza kushuhudia
uaminifu wao, kwa sababu ya mapenzi yao juu ya ndugu zao na pia sisi.
32 Kwani tazama, wangejitolea dhabihu maisha yao kuliko kuwaua adui wao; na
wamezika silaha zao za vita udongoni, kwa sababu ya mapenzi yao juu ya ndugu zao.
33 Na sasa tazama, nawaambia nyinyi, kumewahi kuwa na mapenzi makuu hivi
nchini kote? Tazama, nawaambia, La, hakujakuwepo, hata miongoni mwa Wanefi.
34 Kwani tazama, wangechukua silaha dhidi ya ndugu zao; hawangevumilia
wenyewe wauawe. Lakini tazameni ni wangapi baina ya hawa ambao wametoa
maisha yao; na tunajua kwamba wameenda kwa Mungu wao, kwa sababu ya
mapenzi yao na kwa sababu ya chuki yao kwa dhambi.
35 Sasa si tunayo sababu ya kufurahi? Ndio, nasema kwenu, hakujakuwa na watu
ambao walikuwa na sababu kubwa hivyo ya kufurahi kama sisi, tangu mwanzo wa
dunia; ndio, na shangwe yangu imenichukua mbali, hata kwa majivuno kwa Mungu
wangu; kwani ana uwezo wote, hekima yote, na akili yote; anaelewa vitu vyote, na ni
Kiumbe cha huruma, hata kwenye wokovu, kwa wale ambao watatubu na kuamini
kwa jina lake.
36 Sasa kama hii ni kujivuna, na hata iwe hivyo nitajivuna; kwani haya ni maisha
yangu na mwangaza wangu, shangwe yangu na wokovu wangu, na ukombozi wangu
kutoka kwa taabu usio na mwisho. Ndio, libarikiwe jina la Mungu wangu, ambaye
amewajali watu hawa, ambao ni tawi la mti wa Israeli, na limepotea kutoka kwenye
kiwiliwili chake kwenye nchi ngeni; ndio, ninasema, heri jina la Mungu wangu,
ambaye amekuwa mwangalifu kwetu, watembezi kwenye nchi geni.
37 Sasa ndugu zangu, tunaona kwamba Mungu ni mwangalifu kwa kila watu, nchi
yoyote ambayo wangekuwa ndani; ndio, huhesabu watu wake, na ana huruma za
kutosha kwa ulimwengu wote. Sasa hii ndiyo shangwe yangu, na shukrani yangu
nyingi; ndio, na nitatoa shukrani kwa Mungu wangu milele. Amina.

## Alma 27

1 Sasa ikawa kwamba wakati wale Walamani ambao walikuwa wameanzisha vita na
Wanefi walipata, baada ya kujaribu mara nyingi kuwaangamiza, kwamba ilikuwa ni
bure kutazamia kuwaangamiza, walirudi tena kwa nchi ya Nefi.
2 Na ikawa kwamba Waamaleki, kwa sababu ya hasara yao, walikasirika kupita
kiasi. Na walipoona kwamba hawangelipiza kisasi kwa Wanefi, walianza
kuwavuruga watu kuwa na hasira dhidi ya ndugu zao, watu wa Anti-Nefi-Lehi; kwa
hivyo walianza tena kuwaangamiza.
3 Sasa hawa watu walikataa tena kutwaa silaha zao, na wakavumilia wenyewe
wauawe vile maadui wao walivyotaka.
4 Sasa Amoni na ndugu zake walipoona hii kazi ya mauaji baina ya wale ambao
waliwapenda sana, na kati ya wale waliowapenda — kwani walikuwa wanatendewa
kama kwamba ni malaika waliotumwa kutoka kwa Mungu kuwaokoa kutoka kwa
maangamizo yasiyo na mwisho — kwa hivyo, Amoni na ndugu zake walipoona kazi
hii kubwa ya mauaji, walivurugwa na huruma, na wakamwambia mfalme:
5 Acha tukusanye pamoja hawa watu wa Bwana, na acha sisi tuteremke kwenye
nchi ya Zarahemla mahali pa ndugu zetu Wanefi, na tutoroke kutoka mikono ya
maadui wetu, ili tusiuawe.
6 Lakini mfalme aliwambia: Tazama, Wanefi watatuangamiza, kwa sababu ya

mauaji mengi na dhambi ambazo tumetenda dhidi yao.
7 Na Amoni akasema: Nitaenda kuuliza kutoka kwa Bwana, na ikiwa atatuambia,
nendeni mahali ndugu zenu wapo, je, utaenda?
8 Na mfalme akamwambia: Ndio, ikiwa Bwana atatuambia twende, tutaenda chini
kwenye ndugu zetu, na tutakuwa watumwa wao hadi tutakapowalipa mauaji mengi
na dhambi ambazo tumetenda dhidi yao.
9 Lakini Amoni aliwaambia: Ni kinyume cha sheria ya ndugu zetu, ambayo
ilianzishwa na baba yangu, kwamba kusiwe na watumwa baina yao; kwa hivyo acha
twende chini na kutegemea juu ya rehema ya ndugu zetu.
10 Lakini mfalme aliwambia: Mwulize Bwana, na ikiwa atatuambia twende,
tutaenda; la sivyo tutaangamia hapa nchini.
11 Na ikawa kwamba Amoni akaenda na kumwuliza Bwana, na Bwana
akamwambia:
12 Toa hawa watu kutoka nchi hii, ili wasiangamie; kwani Shetani ameshikilia
mioyo ya Waamaleki, ambao wanawavuruga Walamani kukasirika dhidi ya ndugu
zao kuwaua; kwa hivyo nendeni nyinyi nje ya nchi hii; na heri kwa watu hawa wa
kizazi hiki, kwani nitawahifadhi.
13 Na sasa ikawa kwamba Amoni aliendа na kumwambia mfalme maneno yote
ambayo Bwana alikuwa amemwambia.
14 Na wakakusanya pamoja watu wao wote, ndio, watu wote wa Bwana, na
walikusanya mifugo yao yote na makundi, na kutoka katika nchi, na kwenda kwenye
nyika ambayo ilitenganisha nchi ya Nefi kutoka kwa nchi ya Zarahemla, na ilikuwa
juu karibu na mpaka wa nchi.
15 Na ikawa kwamba Amoni aliwaambia: Tazama, mimi na ndugu zangu tutaenda
mbele kwenye nchi ya Zarahemla, na mtabaki hapa mpaka tutakaporudi; na
tutajaribu mioyo ya ndugu zetu, kama watakubali mje kwa nchi yao.
16 Na ikawa kwamba wakati Amoni alipokuwa anaenda mbele nchini, ndio yeye na
ndugu zake walikutana na Alma, juu mahali ambapo palikuwa pame zungumzwa;
na tazama, huu ulikuwa mkutano wa furaha.
17 Sasa shangwe ya Amoni ilikuwa nyingi sana hata ikajaa; ndio, alimezwa kwenye
shangwe ya Mungu wake, hata akapungukiwa na nguvu; na akainama tena kwenye
ardhi.
18 Sasa si hii ilikuwa shangwe kuu? Tazama, hii ni shangwe ambayo hakuna yeyote
aipataye isipokuwa tu yule ambaye ametubu na anayetafuta furaha kwa
unyenyekevu.
19 Sasa shangwe ya Alma kukutana na ndugu zake kwa kweli ilikuwa kubwa, na pia
shangwe ya Haruni, ya Omneri, na Himni; lakini tazama shangwe yao haikuwa ya
kushinda nguvu zao.
20 Na sasa ikawa kwamba Alma aliwaongoza ndugu zake kurudi kwa nchi ya
Zarahemla; hata kwenye nyumba yake. Na walienda na kumwambia mwamuzi
mkuu vitu vyote ambavyo vilitendeka kwao kwenye nchi ya Nefi, miongoni mwa
ndugu zao, Walamani.
21 Na ikawa kwamba mwamuzi mkuu alituma tangazo nchini kote, akiuliza maoni
ya watu kuhusu kukubaliwa kwa ndugu zao, ambao walikuwa watu wa
Anti-Nefi-Lehi.
22 Na ikawa kwamba sauti ya watu ilirudi, ikisema: Tazama, tutaitoa nchi ya
Yershoni, ambayo iko mashariki kando ya bahari, ambayo inaungana na nchi ya

Neema, ambayo iko kusini mwa nchi ya Neema; na hii nchi ya Yershoni ndiyo nchi
ambayo tutawapatia ndugu zetu kwa urithi.
23 Na tazama, tutaweka majeshi yetu katikati ya nchi ya Yershoni na nchi ya Nefi, ili
tuwalinde ndugu zetu kwenye nchi ya Yershoni; na hivi tunafanya kwa ajili ya
ndugu zetu, kwa sababu ya woga wao wa kuchukua silaha dhidi ya ndugu zao
wakihofia kutenda dhambi; na huu woga wao mwingi uliwajia kwa kutubu sana,
kwa sababu ya mauaji yao mengi na maovu yao ya kutisha.
24 Na sasa tazama, hivi ndivyo tutawafanyia ndugu zetu, ili warithi nchi ya
Yershoni; na tutawakinga kutoka kwa maadui wao na majeshi yetu, kwa masharti
kwamba watatoa sehemu ya mazao yao kutusaidia sisi ili tudumishe majeshi yetu.
25 Sasa, ikawa kwamba Amoni alipokuwa amesikia hivi, alirejea kwa watu wa
Anti-Nefi-Lehi, na pia akiwa na Alma, kwenye nyika, ambapo walikuwa wamepiga
hema zao, na kuwajulisha hivi vitu vyote. Na Alma pia aliwaambia juu ya kuongoka
kwake, na Amoni na Haruni, na ndugu zake.
26 Na ikawa kwamba ilisababisha shangwe nyingi miongoni mwao. Na wakaelekea
chini kwenye nchi ya Yershoni, na kumiliki nchi ya Yershoni; na wakaitwa na Wanefi
watu wa Amoni; kwa hivyo walitambulika kwa hilo jina siku zote za baadaye.
27 Na walikuwa miongoni mwa watu wa Nefi, na pia wakahesabiwa miongoni mwa
watu ambao walikuwa kwenye kanisa la Mungu. Na pia walitambulika kwa juhudi
yao kwa Mungu, na pia kwa watu; kwani walikuwa wakamilifu na wa kuaminiwa na
wa kusimama wima kwa vitu vyote; na walikuwa imara kwa imani yao ya Kristo,
hadi mwisho.
28 Na waliangalia kumwaga damu ya ndugu zao ni machukizo makuu; na
hawangeweza kushawishiwa kuchukua silaha dhidi ya ndugu zao; na hawakuona
kifo kwa woga wowote, kwa matumaini na maoni yao nikatika Kristo na ufufuo;
kwa hivyo, kifo kilimezwa kwao na ushindi wa Kristo juu yake.
29 Kwa hivyo, wangevumilia kifo kwa njia ya kukasirika na kuudhika ambayo
ndugu zao waliwapasha, mbele ya kuchukua panga au kitara kuwaua.
30 Na hivyo walikuwa watu wa juhudi na wapendwa, watu ambao walipendwa sana
na Bwana.

## Alma 28

1 Na ikawa kwamba baada ya watu wa Amoni kuimarishwa kwenye nchi ya Yershoni,
na kanisa pia kuanzishwa kwenye nchi ya Yershoni, na majeshi ya Wanefi kuwekwa
kila mahali kwenye nchi ya Yershoni, ndio, kwenye mipaka yote kuzunguka nchi ya
Zarahemla; tazama majeshi ya Walamani yalikuwa yamewaandama ndugu zao hadi
kwenye nyika.
2 Na hivyo kulikuwa na vita vya kutisha; ndio, hata vita kama hivyo havikuwa
vimeonekana kamwe miongoni mwa watu wote nchini kutoka Lehi alipotoka
Yerusalemu; ndio, na maelfu na maelfu ya Walamani waliuawa na kutawanywa kila
mahali.
3 Ndio, na pia kulikuwa na mauaji ya ajabu miongoni mwa watu wa Nefi; lakini,
Walamani walifukuzwa na kutawanywa, na watu wa Nefi walirudi tena kwa nchi
yao.
4 Na sasa huu ulikuwa wakati ambao kulikuwa na huzuni na vilio vilivyosikika kote
nchini, miongoni mwa watu wa Nefi—

5 Ndio, vilio vya wajane wakiomboleza mabwana zao, na pia baba wakiomboleza
wana wao; na binti kwa kaka, ndio, kaka kwa baba; na hivyo vilio vya kuombeleza
vilisikika miongoni mwao wote, wakiomboleza jamaa zao ambao waliuawa.
6 Na sasa hii ilikuwa siku ya huzuni; ndio, wakati wa unadhiri, na wakati wa
kufunga na kusali.
7 Na hivyo mwaka wa kumi na tano wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi
ukaisha;
8 Na hii ni historia ya Amoni na ndugu zake, matembezi yao kwenye nchi ya Nefi,
kuumia kwao nchini, masikitiko yao, na mateso yao, na shangwe yao isiyo na
kipimo, na makaribisho na ulinzi kutoka kwa ndugu zao kwenye nchi ya Yershoni.
Na sasa Bwana, Mkombozi wa watu wote, aibariki roho zao milele.
9 Na hii ni historia ya vita na mabishano miongoni mwa Wanefi, na pia vita baina
ya Wanefi na Walamani; na mwaka wa kumi na tano wa utawala wa waamuzi
umeisha.
10 Na kutoka mwaka wa kwanza mpaka wa kumi na tano umeleta maangamizo ya
maelfu ya maisha; ndio, umeleta vitendo vibaya vya umwagaji wa damu.
11 Na miili ya wengi imelazwa ardhini, wakati miili ya maelfu inaoza kwa
chunguchungu juu ya ardhi; ndio, na maelfu wengi wanaomboleza kwa kupoteza
jamii yao, kwa ajili wana sababu ya kuogopa, kulingana na ahadi za Bwana, kwamba
wanadhainiwa masharti ya taabu ya daima.
12 Wakati maelfu wengi wa wengine kwa kweli wanaomboleza jamii yao, lakini
wanafurahi na kushangilia kwa matumaini, na hata wanajua, kulingana na ahadi za
Bwana, kwamba wanainuliwa na kuishi kwa mkono wa kulia wa Mungu, kwa hali ya
furaha daima.
13 Na hivyo tunaona vile kutokuwa sawa kwingi kwa watu kwa sababu ya dhambi na
makosa, na nguvu za ibilisi, ambayo huja kwa mipango ya udanganyifu ambayo
amefikiria kutega mioyo ya watu.
14 Na hivyo tunaona mwito mkuu wa uangalifu kwa watu kufanya kazi kwenye
shamba la mizabibu la Bwana; na hivyo tunaona sababu kuu ya huzuni, na pia ya
kufurahi — huzuni kwa sababu ya vifo na uharibifu miongoni mwa watu, na
shangwe kwa sababu ya mwangaza wa Kristo ambao ni uzima.

# Alma 29

1 Ee vile natamani ningekuwa malaika, na ningekuwa na matarajio ya moyo wangu,
kwamba ningeenda mbele na kuhutubia watu na parapanda ya Mungu, na sauti ya
kutingisha ulimwengu, na kuhubiri toba kwa watu wote!
2 Ndio, ningemtangazia kila mtu, kwa sauti kama ya radi, na mpango wa
ukombozi, kwamba watubu na waje kwa Mungu wetu, kwamba kusije kukawa
huzuni zaidi juu ya dunia.
3 Lakini tazama, mimi ni mtu, na hukosa kwa matakwa yangu; kwani ninahitaji
nitosheke na vitu ambavyo Bwana amenipatia.
4 Sitakiwi kubadilisha katika tamaa yangu amri imara na haki za Mungu, kwani
najua kwamba hutoa kwa watu kulingana na kutaka kwao, kama itakuwa kwenye
kifo ama kwenye uhai; ndio, ninajua kwamba hugawanyia watu, ndio, huamuru
kwao sheria ambazo hazibadiliki, kulingana na kutaka kwao, ikiwa zitakuwa za
wokovu au kwa uharibifu.

5 Ndio, na ninajua kwamba uzuri na uovu ulidhihirishwa mema na maovu
yalidhihirisha mbele ya watu wote; yule asiyejua mema na maovu hana lawama;
lakini yule ajuaye uzuri na uovu, kwake itatolewa kulingana na matakwa yake, kama
anataka uzuri au uovu, uzima au kifo, shangwe au majuto ya moyo.
6 Sasa, nikiona kwamba najua hivi vitu, kwa nini nitamani kuliko vile ninavyoeza
kazi ambayo nimeitiwa kufanya?
7 Kwa nini nitamani kwamba ningekuwa malaika, ili niwazungumzie watu wote
wa ulimwengu?
8 Kwani tazama, Bwana huwakubali mataifa yote, kila taifa na lugha yake,
kufundisha neno lake, ndio, kwa hekima, yote ambayo anaona sawa wawe nayo; kwa
hivyo tunaona kwamba Bwana hushauri kwa hekima, kulingana na yale ambayo ni
ya haki na kweli.
9 Najua ile ambayo Bwana ameniamuru mimi, na ninatukuza ndani yake.
Sijitukuzi mimi mwenyewe, lakini natukuza ile ambayo Bwana ameniamuru; ndio,
na hii ni furaha yangu, kwamba labda niwe chombo kwenye mikono ya Mungu
kuleta roho moja kwa toba; na hii ndiyo shangwe yangu.
10 Na tazama, ninapoona wengi wa ndugu zangu wametubu kweli, na kumkubali
Bwana Mungu wao, ndipo moyo wangu hujaa na shangwe; ndipo ninapokumbuka
yale ambayo Bwana amenifanyia mimi, ndio, hata kwamba amesikia sala yangu;
ndio, ndipo ninapokumbuka mkono wake wa huruma ambao alinyosha kwangu.
11 Ndio, na pia nakumbuka utumwa wa babu zangu; kwani kwa kweli najua
kwamba Bwana aliwakomboa kutoka kwenye utumwa, na kufuatana na hayo
alianzisha kanisa lake; ndio, Bwana Mungu, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka,
na Mungu wa Yakobo, aliwaokoa kutoka kwenye utumwa.
12 Ndio, nimekumbuka kila siku utumwa wa babu zangu; na kwamba yule Mungu
ambaye aliwakomboa kutoka kwa mikono ya Wamisri aliwakomboa kutoka kwa
utumwa.
13 Ndio, na yule yule Mungu alianzisha kanisa lake miongoni mwao; ndio, na yule
yule Mungu ameniita mimi kwa mwito mtakatifu, kuhubiri neno kwa watu wake,
na amenifanikisha sana, matokeo ambayo shangwe yangu imejaa.
14 Lakini mimi sijawi shangwe tu kwa kufanikiwa kwangu pekee, lakini shangwe
yangu imejaa zaidi kwa sababu ya kufanikiwa kwa ndugu zangu, ambao wamekuwa
kwenye nchi ya Nefi.
15 Tazama, wamefanya kazi sana, na wameleta matunda mengi; na zawadi yao
itakuwa kubwa aje!
16 Sasa, ninapofikiria mafanikio ya hawa ndugu zangu roho yangu inabebwa, hata
kama imetenganishwa kutoka kwa mwili, vile ilikuwa, kwani shangwe yangu ni
kubwa sana.
17 Na sasa Mungu angewakubalia hawa, ndugu zangu, kwamba waketi kwenye
ufalme wa Mungu; ndio, na pia wale ambao ni matokeo ya kazi yao kwamba
wasitoke nje tena, lakini kwamba wamtukuze milele. Na afadhali Mungu akubali
kwamba itendeke kulingana na maneno yangu, hata vile nilivyosema. Amina.

## Alma 30

1 Tazama, sasa ikawa kwamba baada ya watu wa Amoni kuimarishwa kwenye nchi ya
Yershoni, ndio, na pia baada ya Walamani kukimbizwa kutoka nchini, na wafu wao

kuzikwa na watu wa nchi hiyo—
2 Sasa wafu wao hawakuhesabiwa kwa sababu ya wingi wa idadi yao; hata wafu wa
Wanefi hawakuhesabiwa—lakini ikawa baada ya kuzika wafu wao, na pia baada ya
siku za kufunga, na kuomboleza, na sala, (na ulikuwa mwaka wa kumi na sita wa
utawala wa waamuzi kwa watu wa Nefi) kulianza kuwa na mfululizo wa amani kote
nchini.
3 Ndio, na watu walijitahidi kuweka amri ya Bwana; na walikuwa wakamilifu kwa
kuweka masharti ya Mungu, kulingana sheria ya Musa; kwani walifunzwa kutii
sheria ya Musa hadi itakapotimizwa.
4 Kwa hivyo watu hawakuwa na msukosuko wowote katika mwaka wa kumi na sita
wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.
5 Na ikawa kwamba katika mwaka wa kumi na saba wa utawala wa waamuzi,
kulikuwa na mfululizo wa amani.
6 Lakini ikawa kwenye mwisho wa mwaka wa kumi na saba, kulikuja mtu kwenye
nchi ya Zarahemla, na alikuwa mpinga Kristo, kwani alianza kuhubiria watu dhidi
ya unabii ambao ulizungumzwa na manabii, kuhusiana na kuja kwa Kristo.
7 Sasa hakukuwa na sheria yeyote dhidi ya imani ya mtu; kwani ilikuwa kinyume
kabisa cha amri za Mungu kwamba kuwe na sheria inayoleta watu kutokuwa sawa.
8 Kwa hivyo maandiko yanasema: Chagua wewe siku ya leo, yule ambaye
utamtumikia.
9 Sasa kama mtu alitaka kumtumikia Mungu, ilikuwa ni haki yake; kwa usahihi
zaidi kama aliamini katika Mungu ilikuwa ni haki yake kumtumikia; lakini kama
hakuamini kwake hakukuwa na sheria ya kumwadhibu.
10 Lakini kama aliua aliadhibiwa kwa kifo; na kama alipora aliadhibiwa pia; na
kama aliiba aliadhibiwa pia; na kama alizini aliadhibiwa pia; ndio, kwa huu uovu
wote waliadhibiwa.
11 Kwani kulikuwa na sheria kwamba watu walihukumiwa kulingana na makosa yao.
Walakini, hakukuwa na sheria dhidi ya imani ya mtu; kwa hivyo, mtu aliadhibiwa tu
kwa makosa ambayo alikuwa amefanya; kwa hivyo watu wote walikuwa sawa.
12 Na huyu mpinga Kristo, ambaye jina lake lilikuwa Korihori, (na sheria
haingemshika) alianza kuhubiria watu kwamba hakutakuwa na Kristo. Na jinsi hii
alihubiri, akisema:
13 Ee nyinyi ambao mmefungiwa chini ya upumbavu na tumaini la bure, kwa nini
mnajiweka mzigo na vitu vya upumbavu kama hivi? Kwa nini mnamtafuta Kristo?
Kwani hakuna yeyote ajuaye chochote kitakachokuja.
14 Tazama, hivi vitu ambavyo mnaita unabii, ambavyo mnasema vinatolewa na
manabii watakatifu, tazama, ni mila za upumbavu za baba zenu.
15 Mnajuaje ukweli wao? Tazama, hamwezi kujua vitu ambavyo hamuoni; kwa
hivyo hamwezi kujua kwamba kutakuwa na Kristo.
16 Mnaona mbele na kusema kwamba mnaona msamaha wa dhambi zenu. Lakini
tazama, ni matokeo ya wenda wazimu wa akili; na hii michafuko ya akili yenu
inawajia kwa sababu ya desturi za babu zenu, ambazo zinawaongoza mbali kwa
kuamini kwa vitu ambavyo havipo.
17 Na vitu vingi vya aina hii aliwazungumzia, akiwaambia kwamba hakutakuwa na
upatanisho utakaofanywa kwa dhambi za watu, lakini kila mtu hufaulu katika
maisha haya kulingana na vile alijiendesha; kwa hivyo kila mtu alifanikiwa
kulingana na akili yake, na kila mtu alishinda kulingana na nguvu yake; na chochote

ambacho mtu alifanya si kosa.
18 Na hivyo aliwahubiria, akipotosha mbali mioyo ya wengi, na kuwafanya kubeba
vichwa vyao kwa uovu, ndio, akidanganya wanawake wengi, na pia wanaume,
kutenda ukahaba—akiwaambia kwamba mtu akifa, huo ndio mwisho wake.
19 Sasa huyu mtu aliendа hadi kwenye nchi ya Yershoni pia, kuhubiri vitu hivi
miongoni mwa watu wa Amoni, ambao walikuwa awali watu wa Walamani.
20 Lakini tazama walikuwa werevu kuliko wengi wa Wanefi; kwani walimchukua,
na kumfunga, na kumbeba na kumpeleka mbele ya Amoni, ambaye alikuwa kuhani
mkuu juu ya watu hao.
21 Na ikawa kwamba alilazimisha kwamba atolewe nje ya nchi. Na akaenda kwenye
nchi ya Gideoni, na akaanza kuwahubiria pia; na pale hakufaulu sana, kwani
alichukuliwa na kufungwa na kupelekwa mbele ya kuhani mkuu, pia mwamuzi
mkuu juu ya nchi.
22 Na ikawa kwamba kuhani mkuu alimwambia: Kwa nini unazunguka ukiharibu
njia za Bwana? Kwa nini unafundisha hawa watu kwamba hakutakuwa na Kristo,
kukatisha furaha yao? Kwa nini unazungumza ubaya dhidi ya unabii wote wa
manabii watakatifu?
23 Sasa jina la kuhani mkuu lilikuwa Gidona. Na Korihori akamwambia: Kwa
sababu sifundishi desturi za upumbavu za babu zenu, na kwa sababu sifundishi hawa
kujizuia wenyewe chini ya masharti na utaratibu ambao uliwekwa na makuhani wa
zamani, kujitwalia nguvu na uwezo kwao, kuwaweka katika ujinga, kwamba
wasiweze kubeba vichwa vyao, lakini wawekwe chini kufuatana na maneno yako.
24 Unasema kwamba hawa watu ni watu huru. Tazama, nasema wako kwenye
utumwa. Unasema kwamba ule unabii wa zamani ni wa kweli. Tazama, nasema
kwamba hujui kwamba ni kweli.
25 Unasema kwamba watu hawa wana makosa na ni watu walioanguka, kwa sababu
ya dhambi ya mzazi. Tazama, nasema kwamba mtoto si mkosaji kwa sababu ya
wazazi wake.
26 Na unasema pia kwamba Kristo atakuja. Lakini tazama, nasema kwamba hujui
kwamba kutakuwa na Kristo. Na unasema kwamba atauawa kwa sababu ya dhambi
za ulimwengu—
27 Na hivyo unawapoteza hawa watu kufuata desturi za upuuzi za babu zenu, na
kulingana na kutaka kwako; na unawaweka chini, hata vile walivyokuwa kwenye
utumwa, kwamba ujishibishe na kazi ya mikono yao, ili wasiangalie juu na ujasiri, na
kwamba wasifurahie haki na mapendeleo yao.
28 Ndio, hawatumii ile ambayo ni yao wasije wakachukiza makuhani wao, ambao
wanawataabisha kufuatana na kutaka kwao, na wamewafanya kuamini, kupitia
desturi zao na ndoto zao na upuzi wao na maono yao na siri za kujifanya, kwamba,
ikiwa hawafanyi kufuatana na maneno yao, watachukiza kiumbe ambacho
hakijulikani, ambaye wanasema ni Mungu—kiumbe ambacho hakijaonekana au
kujulikana, ambacho hakikuwepo wala hakitakuwepo.
29 Sasa kuhani mkuu na mwamuzi mkuu walipoona ugumu wa moyo wake, ndio,
walipoona kwamba atatukana hata Mungu, hawakumjibu lolote kwa maneno yake;
lakini wakasababisha kwamba afungwe; na walimkabidhi katika mikono ya askari,
na wakampeleka katika nchi ya Zarahemla, kwamba angeletwa mbele ya Alma, na
mwamuzi mkuu ambaye alikuwa mtawala juu ya nchi yote.
30 Na ikawa kwamba wakati alipopelekwa mbele ya Alma na mwamuzi mkuu,

aliendelea kusema kwa njia sawa vile alivyofanya kwenye nchi ya Gideoni; ndio,
aliendelea kukufuru.
31 Na aliongea maneno kwa sauti kubwa mbele ya Alma, na kuwatukana makuhani
na walimu, akiwashtaki kwa kuwapoteza watu kwa kufuata desturi za ujinga za babu
zao, kwa nia ya kujishibisha kwa kazi ya watu.
32 Sasa Alma alimwambia: Unajua kwamba hatujishibishi sisi wenyewe kwa kazi ya
watu hawa; kwani tazama nimefanya kazi hata kutokea mwanzo wa utawala wa
waamuzi mpaka sasa, kwa mikono yangu kwa kujitegemea, ingawa nilikuwa na
safari nyingi kuzunguka nchi nikitangaza neno la Mungu kwa watu wangu.
33 Na ingawa nimefanya kazi nyingi kanisani, sijapokea hata zaidi ya senine moja
kwa kazi yangu; wala hata mmoja wa ndugu zangu, isipokuwa wakati tulikuwa
kwenye kiti cha kutoa hukumu; na wakati huo tumepokea tu kulingana na sheria
kwa wakati wetu.
34 Na sasa, kama hatuwezi kupokea chochote kwa kazi yetu kanisani, itatufaidi nini
kufanya kazi kanisani isipokuwa tu kutangaza ukweli, ili tuweze kushangilia kwa
shangwe kwa raha ya ndugu zetu?
35 Basi kwa nini wewe unasema kwamba tunawahubiria hawa kupata faida, wakati
wewe, mwenyewe, unajua kwamba hatupati faida yoyote? Na sasa unaamini
kwamba tunadanganya hawa watu, ili tusababishe shangwe ndani ya mioyo yao?
36 Na Korihori akamjibu, Ndio.
37 Na kisha Alma akasema kwake: Unaamini wewe kwamba kuna Mungu?
38 Na akajibu, La.
39 Sasa Alma akasema kwake: Utakataa kwamba kuna Mungu, na pia kumkana
Kristo? Kwani tazama, nakwambia, najua kuna Mungu, na pia kwamba Kristo
atakuja.
40 Na sasa ni ushahidi gani unao kwamba hakuna Mungu, au kwamba Kristo
hatakuja? Nakwambia wewe kwamba huna lolote, isipokuwa tu maneno yako.
41 Lakini, tazama, nina vitu vyote kama ushahidi kwamba hivi vitu ni kweli; na
wewe pia una vitu vyote kama ushuhuda kwako kwamba ni vya kweli; na utakana
hivi vitu? Unaamini kwamba hivi vitu ni kweli?
42 Tazama, najua kwamba unaamini, lakini unaongozwa na roho wa uwongo, na
umeweka mbali Roho ya Mungu ili isiwe na pahali ndani yako; lakini ibilisi ana
uwezo juu yako, na anakubeba kila mahali, akifanya ujanja ili aangamize watoto wa
Mungu.
43 Na sasa Korihori alimwambia Alma: Ikiwa utanionyesha ishara, kwamba
ningesadikishwa kuwa kuna Mungu, ndio, nionyeshe kwamba ana uwezo, na ndipo
nitakubali ukweli wa maneno yako.
44 Lakini Alma akamwambia: Wewe umepata ishara za kutosha; utamjaribu
Mungu wako? Unaweza kusema, Nionyeshe ishara, wakati una ushuhuda wa hawa
ndugu zako wote, na pia manabii watakatifu? Maandiko yamewekwa mbele yako,
ndio, na vitu vyote vinaonyesha kwamba kuna Mungu; ndio, hata dunia, na vitu
vyote vilivyo juu yake, ndio, na mwendo wake, ndio, na pia sayari zote ambazo
huenda kwa utaratibu wao zinashuhudia kwamba kuna Muumba Mkuu.
45 Na bado unaenda ukizunguka, ukidanganya mioyo ya watu hawa, ukitoa
ushuhuda kwamba hakuna Mungu? Na bado utakana huu ushahidi wote? Na
akasema: Ndio, nitakana isipokuwa unionyeshe ishara.
46 Na ikawa kwamba Alma akamwambia: Tazama, nimesikitika kwa sababu ya

ugumu wa moyo wako, ndio, kwamba utazidi kushindana na roho ya ukweli, kwamba nafsi yako iangamizwe.

47 Lakini tazama, ni afadhali roho yako ipotee kuliko kwamba uwe njia ya kuleta roho nyingi kwenye maangamizo, kwa udanganyifu wako na maneno yako ya kusifu; kwa hivyo kama utakana tena, tazama Mungu atakupiga wewe, kwamba uwe bubu, kwamba hutafungua kinywa chako mara nyingine, kwamba hutaweza kudanganya hawa watu mara nyingine.

48 Sasa Korihori akamwambia: Sikatai kuweko kwa Mungu, lakini siamini kwamba kuna Mungu; na ninasema pia, kwamba hujui kuwa kuna Mungu; na isipokuwa unionyeshe ishara, sitaamini.

49 Sasa Alma akamwambia: Hii nitakupatia kwa ishara, kwamba utapigwa na kuwa bubu, kufuatana na maneno yangu; na ninasema, kwamba kwa jina la Mungu, utafanywa bubu, kwamba hutatamka tena.

50 Sasa wakati Alma alipokuwa amenena maneno haya, Korihori alipigwa na akawa bubu, kwamba hangeweza kunena tena, kufuatana na maneno ya Alma.

51 Na wakati mwamuzi mkuu alipoona hivi, alinyosha mkono wake na kuandika kwa Korihori, akisema: Umesadikishwa kwa nguvu za Mungu? Kwake ambaye ulitaka Alma aonyeshe ishara? Ulitaka kwamba atese wengine, akionyesha ishara? Tazama amekuonyesha ishara; na sasa hutabishana zaidi?

52 Na Korihori alinyoosha mkono wake na kuandika, akisema: Najua kwamba mimi ni bubu, kuwa siwezi kuongea; na ninajua kwamba hakuna kingine isipokuwa nguvu ya Mungu pekee ndiyo iliyoweza kuniletea mimi haya; ndio, na nilikuwa kila siku najua kwamba kuna Mungu.

53 Lakini tazama, ibilisi amenidanganya; kwani alinitokea kwa mfano wa malaika, na akaniambia; Nenda na urudishe hawa watu, kwani wote wamepotea wakifuata Mungu asiyejulikana. Na akaniambia: Hakuna Mungu; ndio, na akanifundisha yale ambayo ninahitaji kusema. Na nimefundisha maneno yake; na niliyafundisha kwa sababu yalikuwa yanapendeza kwa akili ya kimwili; na niliyafundisha, hata ikawa ninafaulu sana, hata kwamba niliamini kwamba yalikuwa ya kweli; hata mpaka nimejiletea hii laana kuu kwangu.

54 Sasa wakati alikuwa amesema haya; alimsihi Alma kwamba amuombee Mungu, kwamba laana itolewe kwake.

55 Lakini Alma alimwambia: Laana hii ikitolewa kwako utapoteza mioyo ya watu tena; kwa hivyo, itakuwa nawe hata vile Bwana atakavyohitaji.

56 Na ikawa kwamba laana haikutolewa kutoka kwa Korihori; lakini alitupwa nje, na akaenda akitembea kutoka nyumba hadi nyingine akiomba chakula.

57 Sasa ufahamu wa yaliyompata Korihori mara moja ilitangazwa kote nchini; ndio, tangazo lilitolewa na mwamuzi mkuu kwa watu wote nchini, ikitangaziwa wale ambao walikuwa wameamini maneno ya Korihori kwamba lazima watubu mara moja, isije hukumu sawa ikaletwa kwao.

58 Na ikawa kwamba wote walisadikishwa kwa uovu wa Korihori; kwa hivyo wote walimgeukia tena Bwana; na hii ikaweka mwisho kwa uovu wa aina ya Korihori. Na Korihori alienda kutoka moja nyumba hadi nyingine, akiomba chakula kwa kujiweka hai.

59 Na ikawa kwamba alienda miongoni mwa watu, ndio, miongoni mwa watu ambao walikuwa wamejitenga kutoka kwa Wanefi na kujiita Wazoramu, wakiongozwa na mtu ambaye jina lake lilikuwa Zoramu — na alipoenda miongoni

mwao, tazama, alishambuliwa na kukanyagwa chini, hadi akafa.
60 Na hivyo tunaona mwisho wa yule ambaye anapotosha njia za Bwana; na hivyo
tunaona kwamba ibilisi hatasaidia watoto wake siku ya mwisho, lakini anawachukua
kwa mbio hadi jahanamu.

## Alma 31

1 Sasa ikawa kwamba baada ya mwisho wa Korihori, Alma baada ya kupata habari
kwamba Wazoramu wanapotosha neno la Bwana, na kwamba Zoramu, ambaye
alikuwa kiongozi wao, alikuwa akiongoza mioyo ya watu kusujudu kwa viumbe
visivyosikia wala kusema, moyo wake tena ulianza kuwa na huzuni kwa sababu ya
ubaya wa watu.
2 Kwani ilikuwa chanzo cha huzuni kuu kwa Alma kujua kuhusu uovu miongoni
mwa watu wake; kwa hivyo moyo wake ulikuwa na huzuni sana kwa sababu ya
kutenganishwa kwa Wazoramu kutoka kwa Wanefi.
3 Sasa Wazoramu walikuwa wamejikusanya pamoja kwenye nchi iliyoitwa
Antionumu ambayo ilikuwa mashariki mwa nchi ya Zarahemla, ambayo ilipakana
karibu na juu ya ukingo wa bahari, ambayo ilikuwa kusini mwa nchi ya Yershoni,
ambayo pia ilipakana na nyika kusini, nyika ambayo ilikuwa imejaa Walamani.
4 Sasa Wanefi waliogopa kwamba Wazoramu wangeanza mawasiliano na
Walamani, na kwamba ingekuwa njia ya hasara kubwa kwa upande wa Wanefi.
5 Na sasa, kwa vile kuhubiri kwa neno kulikuwa na maelekezo makubwa ya
kuongoza watu kufanya yale ambayo ni haki — ndio, ilikuwa na matokeo ya nguvu
zaidi kwa akili za watu kuliko upanga, au kitu chochote kingine, ambacho kiliwahi
kufanyika kwao — kwa hivyo Alma alifikiri ilikuwa bora kwamba wangejaribu
matokeo ya uwezo wa neno la Mungu.
6 Kwa hivyo aliwachukua Amoni, na Haruni, na Omneri; na Himni alimwacha
kanisani Zarahemla; lakini wa kwanza watatu walienda na yeye, na pia Amuleki na
Zeezromu, ambao walikuwa Meleki; na pia aliwachukua wawili wa wana wake.
7 Sasa mkubwa kwa wana wake hakuenda na yeye, na jina lake lilikuwa Helamani;
lakini majina ya wale ambao alienda nao yalikuwa Shibloni na Koriantoni; na haya
ndiyo majina ya wale ambao walienda na yeye miongoni mwa Wazoramu,
kuwahubiria neno.
8 Sasa Wazoramu walikuwa wamekataa mafundisho ya Wanefi; kwa hivyo
walikuwa wamepata neno la Mungu kuhubiriwa kwao.
9 Lakini walianza kufanya makosa makubwa, kwani hawangeweza kuchunga amri
za Mungu, na sheria zake, kulingana na sheria ya Musa.
10 Wala hawangechunga heshima za kanisa, kuendelea kwa sala na maombi Mungu
kila siku, kwamba wasiingie kwenye majaribio.
11 Ndio, kwa ufupi, waliharibu njia za Bwana kwa namna nyingi; kwa hivyo, kwa
sababu hii, Alma na ndugu zake waliondoka kwenda nchini kuhubiri neno kwao.
12 Sasa, walipowasili nchini, tazama, kwa mshangao wao walipata kwamba
Wazoramu walikuwa wamejenga masinagogi, na kwamba walikuwa wakikusanyika
pamoja siku moja ndani ya wiki, siku ambayo waliita siku ya Bwana; na waliabudu
kwa njia ambayo Alma na ndugu zake hawajawahi kuona;
13 Kwani walikuwa na mahali palipojengwa katikati ya sinagogi yao, mahali pa
kusimama, ambapo palikuwa parefu kupita kichwa; na juu yake ingemtosha tu mtu

mmoja.
14 Kwa hivyo, yeyote ambaye alitaka kuabudu alilazimika kwenda na kusimama juu
yake, na kunyosha mikono yake juu kueleka mbinguni, na kupaza sauti kuu, akisema:
15 Mtakatifu, mtakatifu Mungu; tunaamini kwamba wewe ni Mungu, na
tunaamini kwamba wewe u mtakatifu, na kwamba ulikuwa roho, na ungali roho, na
utakuwa roho milele.
16 Mungu Mtakatifu, tunaamini kwamba umetutenganisha sisi kutoka kwa ndugu
zetu; na hatuamini kwa desturi ya ndugu zetu, ambayo ilikabidhiwa kwao kwenye
njia ya utoto wa babu zao; lakini tunaamini kwamba umetuchagua sisi kuwa watoto
wako watakatifu; na pia umetudhihirishia kwamba hakutakuwa na Kristo.
17 Lakini wewe ni yule yule jana, na leo, na milele; na umetuchagua kwamba
tuokolewe, wakati wote ambao wako karibu nasi wamechaguliwa na ghadhabu
kwenye jahanamu; kwa kutufanya watakatifu, Ee Mungu, tunakushukuru; na pia
tunakushukuru kwamba umetuchagua sisi, kwamba tusipotezwe na desturi za
upumbavu za ndugu zetu, ambazo zinawafungia chini kwa kuamini Kristo, ambayo
inaongoza mioyo yao kutangatanga kutoka kwako, Mungu wetu.
18 Na tena tunakushukuru wewe, Ee Mungu, kwamba sisi ni wateule na watu
watakatifu. Amina.
19 Sasa ikawa kwamba Alma na ndugu zake na wana wake waliposikia hizi sala,
walishtuka kupita kiasi.
20 Kwani tazama, kila mtu alienda mbele na kutoa sala zilizokuwa sawa.
21 Sasa mahali pale paliitwa na hawa Rameumtomu, ambayo ikifasiriwa, ni kituo
kitakatifu.
22 Sasa, kutoka kwenye kituo hiki, walitoa, kila mmoja, sala sawa kwa Mungu,
wakimshukuru Mungu wao kwamba walichaguliwa na yeye, na kwamba
hakuwapotezea kwa desturi ya ndugu zao, na kwamba mioyo yao haikudanganywa
kuamini kwa vitu vinavyokuja, ambavyo hawakujua chochote kuvihusu.
23 Sasa, baada ya watu wote kutoa shukrani kwa njia hii, walirejea kwao, bila
kuzungumza maneno ya Mungu wao tena hadi wakati wa kukusanyika tena kwenye
kituo kitakatifu, kutoa shukrani kwa njia yao ya kawaida.
24 Sasa Alma alipoona haya moyo wake ulihuzunika; kwani aliona kwamba watu
walikuwa watu waovu na wakaidi; ndio, aliona kwamba mioyo yao ilitamani
dhahabu, na fedha, na vitu vyote vilivyotengenezwa vizuri.
25 Ndio, na aliona pia kwamba mioyo yao ilikuwa imeinuliwa kwa kujisifu sana,
kwa kiburi chao.
26 Na alipaza sauti yake kuelekea mbinguni, na kulia, akisema: Ee, kwa muda gani,
Ee Bwana, utakubali kwamba watumishi wako waishi hapa chini katika mwili,
kuona uovu mwingi miongoni mwa watoto wa watu?
27 Tazama, Ee Mungu, wanaomba kwako, na bado mioyo yao imezidiwa na kiburi
chao. Tazama, Ee Mungu, wanaomba kwako na midomo yao, wakati wanatamani,
hivi vitu vingine vya ulimwengu, kuliko kitu kingine.
28 Tazama, Ee Mungu wangu, mavazi yao ya bei ya juu, na pete zao, na mikufu yao,
na mapambo yao ya dhahabu, na vitu vyao vyote vya thamani ambavyo
wamejipamba navyo; na tazama, mioyo yao iko kwenye hivi vitu, lakini wanaomba
kwako wakisema — Tunakushukuru, Ee Mungu, kwani sisi ni watu wateule kwako,
wakati wengine wataangamia.
29 Ndio, na wanasema kwamba umewahakikishia kwamba hakutakuwa na Kristo.

30 Ee Bwana Mungu, kwa muda gani utakubali kwamba uovu wa aina hii na ukafiri uwe miongoni mwa watu? Ee Bwana, utanipatia nguvu, ili nivumilie na udhaifu wangu. Kwani mimi ni dhaifu, na uovu aina hii miongoni mwa watu unaumiza roho yangu.

31 Ee Bwana, moyo wangu una huzuni nyingi sana, unaweza kutuliza nafsi yangu ndani ya Kristo. Ee Bwana unaweza kunikubalia niwe na nguvu, kwamba niweze kuvumilia haya mateso ambayo yatanijia mimi, kwa sababu ya maovu ya watu hawa.

32 Ee Bwana, utafariji roho yangu, na unipatie mafanikio, na pia wafanyikazi wenzangu ambao wako na mimi—ndio, Amoni, na Haruni, na Omneri, na pia Amuleki na Zeezromu, na pia wana wangu wawili—ndio, hata hawa wote uwafariji, Ee Bwana. Ndio, ufariji roho zao katika Kristo.

33 Uwakubalie hawa kwamba wawe na nguvu, kwamba waweze kuvumilia mateso yao ambayo yatawajia kwa sababu ya maovu ya watu hawa.

34 Ee Bwana, utukubalie sisi kwamba tuwe na mafanikio kwa kuwaleta kwako tena katika Kristo.

35 Tazama, Ee Bwana, roho zao ni za thamani, na wengi wao ni ndugu zetu; kwa hivyo, tupatie, Ee Bwana, uwezo na hekima kwamba tuwalete hawa, ndugu zetu, tena kwako.

36 Sasa ikawa kwamba Alma aliposema maneno haya, kwamba alipiga mikono yake kwa hao wote ambao walikuwa na yeye. Na tazama, alipoweka mikono yake juu yao, walijazwa na Roho Mtakatifu.

37 Na baada ya hayo walitawanyika wenyewe mmoja kutoka kwa mwingine, bila kujifikiria wenyewe watakula nini, au kile watakachokunywa, au kile watakachovaa.

38 Na Bwana aliwaandalia kwamba wasiwe na njaa, wala wasiwe na kiu; ndio, na pia akawapatia nguvu, kwamba wasiteseke kwa namna yote ya mateso, isipokuwa imezwe kwenye shangwe ya Kristo. Sasa hii ilikuwa kulingana na sala ya Alma; na hii ni kwa sababu aliomba kwa imani.

## Alma 32

1 Na ikawa kwamba waliendelea mbele, na kuanza kuhubiri neno la Mungu kwa watu, wakiingia kwenye masinagogi yao, na kwenye nyumba zao; ndio, na hata walihubiri neno kwenye mitaa yao.

2 Na ikawa kwamba baada ya kazi nyingi miongoni mwao, wakaanza kuwa na mafanikio miongoni mwa watu wa vyeo vya chini; kwani tazama, walitupwa nje ya masinagogi kwa sababu ya nguo zao hafifu—

3 Kwa hivyo hawakuruhusiwa kuingia katika masinagogi yao kumwabudu Mungu, wakichukuliwa kama uchafu; kwa hivyo walikuwa masikini; ndio, walichukuliwa na ndugu zao kama takataka; kwa hivyo walikuwa masikini kulingana na vitu vya ulimwengu; na pia walikuwa masikini katika mioyo yao.

4 Sasa, Alma alipokuwa akifundisha na kuwazungumzia watu kwenye mlima Onida, kulitokea kikundi kikubwa kwake, cha wale ambao tulikuwa tukizungumza juu yao, ambao walikuwa masikini moyoni, kwa sababu ya umasikini wao kulingana na vitu vya ulimwengu.

5 Na wakamjia Alma; na yule ambaye alikuwa anawaongoza akamwambia: Tazama, ni nini hawa ndugu zangu watafanya, kwani wanadharauliwa na watu wote kwa sababu ya umasikini wao, ndio, hata nasa na makuhani wetu; kwani

wametutupa nje ya masinagogi ambayo tuliyafanyia kazi kwa wingi kujenga kwa
mikono yetu; na wametutupa nje kwa sababu ya umasikini wetu mkuu; na hatuna
mahali pa kumuabudia Mungu wetu; na tazama, tutafanya nini?
6 Na sasa Alma aliposikia haya, alipindua uso wake mara moja, na kumwangalia,
kwa shangwe kubwa; kwani aliona kwamba mateso yao yalikuwa yamewafanya kwa
kweli kuwa wanyenyekevu, na kwamba walikuwa wamejiandaa kusikiliza neno.
7 Kwa hivyo hakusema mengi kwa huo umati mwingine; lakini alinyoosha mbele
mkono wake, na kupaza sauti kwa wale ambao aliwaona, ambao walikuwa kwa kweli
wametubu, na akawaambia;
8 Ninaona kwamba mmenyenyekea moyoni; na ikiwa ni hivyo, heri kwenu.
9 Tazama ndugu yenu alisema, Tutafanya nini?—kwani tumetupwa nje ya
masinagogi yetu, kwamba hatuwezi kumuabudu Mungu wetu.
10 Tazama ninawaambia, mnafikiri kwamba hamwezi kumuabudu Mungu
isipokuwa kwenye masinagogi yenu pekee?
11 Na zaidi ya hayo, ningewauliza, mnafikiri kwamba lazima mmuabudu Mungu tu
siku moja kwenye juma?
12 Nawaambia, ni vyema kwamba mmetupwa nje ya masinagogi yenu, ili muwe
wanyenyekevu, na ili mjifunze hekima; kwani ni lazima mjifunze hekima; kwani ni
kwa sababu mmetupwa nje, kwamba mmedharauliwa na ndugu zenu kwa sababu ya
umasikini wenu mkuu, kwamba mioyo yenu imenyenyekea; kwani mnyenyekezwa
kwa lazima.
13 Na sasa, kwa sababu mmelazimishwa kunyenyekea heri nyinyi; kwani mtu wakati
mwingine, akilazimishwa kunyenyekea, hutafuta toba; na sasa kwa kweli, yeyote
anayetubu atapata huruma; na yule ambaye anapata huruma na kuvumilia hadi
mwisho huyo ataokolewa.
14 Na sasa, vile nilivyowaambia nyinyi, kwamba kwa sababu mlilazimishwa
kunyenyekea mlibarikiwa, hamdhani kwamba wale ambao wanajinyenyekeza kwa
ukweli wenyewe kwa sababu ya neno wamebarikiwa zaidi?
15 Ndio, yule ambaye anajinyenyekeza mwenyewe kwa ukweli, na kutubu dhambi
zake, na kuvumilia hadi mwisho, huyo atabarikiwa—ndio, atabarikiwa zaidi ya wale
ambao hulazimishwa kunyenyekea kwa sababu ya umasikini wao mwingi.
16 Kwa hivyo, heri wale ambao hunyenyekea wenyewe bila kulazimishwa
kunyenyekea; kwa usahihi zaidi, heri yule ambaye anaamini katika neno la Mungu,
na anabatizwa bila ukaidi wa moyo, ndio, bila kushurutishwa kujua neno, au hata
kulazimishwa kujua, kabla ya kuamini.
17 Ndio, kuna wengi ambao husema: ikiwa utatuonyesha ishara kutoka mbinguni,
ndipo tutajua kwa hakika; halafu tutaamini.
18 Sasa ninauliza; hii ni imani? Tazama, nawaambia, Hapana; kwani ikiwa mtu
anajua kitu hana sababu ya kuamini, kwani anakijua.
19 Na sasa, hulaaniwaje zaidi ya yule ambaye anajua mapenzi ya Mungu na
hayatimizi, kuliko yule ambaye huamini tu, au ana sababu ya kuamini, na kuanguka
kwenye makosa?
20 Sasa, kwa kitu hiki lazima mhukumu. Tazama, nawaambia, kwamba ni sawa
mkono mmoja hata vile ilivyo kwa mwingine; na itakuwa hivyo kwa kila mtu
kulingana na vitendo vyake.
21 Na sasa nilivyosema kuhusu imani—imani sio kuwa na ufahamu kamili wa vitu;
kwa hivyo mkiwa na imani, mnatumainia vitu ambavyo havionekani, ambavyo ni

vya kweli.
22 Na sasa, tazama, ninawaambia, na ningetaka kwamba mkumbuke, kwamba
Mungu ni mwenye hekima kwa wote wanaoamini katika jina lake; kwa hivyo,
anataka kwa mara ya kwanza, kwamba mwamini, ndio, hata katika neno lake.
23 Na sasa, yeye huwatolea wanadamu neno lake kwa malaika, ndio, sio tu kwa
wanaume peke yao lakini pia kwa wanawake. Sasa hii si yote; watoto wadogo huwa
na maneno wanayopewa mara nyingi, ambayo yanawafadhaisha werevu na wasomi.
24 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, kwa vile mnatamani kujua kutoka kwangu
mtafanya nini kwa sababu mnasumbuliwa na kutupwa nje—sasa sitaki mfikirie
kwamba ninamaanisha kutoa hukumu kwenu isipokuwa kulingana na yale ambayo
ni kweli—
25 Kwani simaanishi kwamba nyinyi nyote mmelazimishwa kujinyenyekeza; kwani
ninaamini kwa ukweli kwamba kuna wengine kati yenu ambao wangenyenyekea
wenyewe, hata wawe kwa hali gani.
26 Sasa, vile nilivyosema kuhusu imani—kwamba haikuwa ufahamu kamili—hata
hivyo ni kama maneno yangu. Hamwezi kujua ukweli wao kwanza, kwa ukamilifu,
vile imani si ufahamu kamili.
27 Lakini tazama, ikiwa mtaamka na kuziwasha akili zenu, hata kwenye kujaribu juu
ya maneno yangu na kutumia sehemu ya imani, ndio, hata ikiwa hamwezi ila
kutamani kuamini, acha hamu hii ifanye kazi ndani yenu, hata mpaka mwamini kwa
njia ambayo mtatoa nafasi kwa sehemu ya maneno yangu.
28 Sasa, tutalinganisha neno kwa mbegu. Sasa ikiwa mtatoa nafasi, ili mbegu
ipandwe ndani ya moyo wako, tazama, ikiwa itakuwa mbegu ya kweli, au mbegu
nzuri, ikiwa hamtaitupa nje kwa kutoamini kwenu, kwamba mtashindana na Roho
ya Bwana, tazama, itaanza kuvimba ndani ya vifua vyenu; na wakati mtakaposikia
huu mwendo wa kuvimba, mtaanza kusema ndani yenu—inawezekana kwamba hii
ni mbegu nzuri, au kwamba neno ni nzuri, kwani linaanza kukua ndani ya nafsi
yangu; ndio, inaanza kuangaza kuelewa kwangu, ndio, inaanza kunipendeza mimi.
29 Sasa tazama, si hii itaongeza imani yenu? Ninawaambia, Ndio; walakini haijakua
kwa ufahamu kamili.
30 Lakini tazama, vile mbegu inavyovimba, na kumea, na kuanza kukua, ndipo
mtasema kwamba mbegu ni nzuri; kwani tazama inavimba, na kumea, na kuanza
kukua. Na sasa, tazama, si hii itaimarisha imani yenu? Ndio, itaimarishaa imani
yenu: kwani mtasema tunajua kwamba hii ni mbegu nzuri; kwani tazama
inachipuka na inaanza kukua.
31 Na sasa, tazama, mna hakika kwamba hii ni mbegu nzuri? Nawaambia, Ndio;
kwani kila mbegu huzaa mfano wake.
32 Kwa hivyo kama mbegu inakua ni nzuri, lakini kama haikui, tazama si nzuri, kwa
hivyo hutupiliwa mbali.
33 Na sasa, tazama, kwa sababu mmejaribu utafiti, na kupanda mbegu, na inavimba
na kumea, na kuanza kukua, lazima mjue kwamba mbegu ni nzuri.
34 Na sasa, tazama, ufahamu wenu ni kamili? Ndio, ufahamu wenu ni kamili kwa
kile kitu, na imani yenu inalala; na hii kwa sababu mnajua, kwani mnajua kwamba
neno limevimbisha nafsi zenu, na pia mnajua kwamba limemea, kwamba ufahamu
wenu umeanza kuelimika, na akili zenu zinaanza kupanuka.
35 Ee basi, si hii ni kweli? Nawaambia, Ndio, kwa sababu ni nuru; na chochote
ambacho ni nuru, ni kizuri, kwa sababu kinaonekana, kwa hivyo lazima mjue

kwamba ni nzuri; na sasa tazama, baada ya nyinyi kuonja nuru hii si ufahamu wenu ni kamili?

36 Tazama nawaambia, Hapana; wala msiweke kando imani yenu, kwani mmejaribu tu imani yenu kupanda mbegu kwamba mngejaribu utafiti kujua kama mbegu ilikuwa nzuri.

37 Na tazama, mti ukianza kukua, mtasema: Acha tuulishe kwa uangalifu mkuu, kwamba uweze kupata mizizi, kwamba upate kukua, na kututolea matunda. Na sasa tazama, ikiwa mtaulisha kwa uangalifu mwingi mtapata mizizi, na kukua, na kuleta matunda.

38 Lakini mkiuachilia mti ule, na msifikirie kuulisha, tazama hautapata mzizi wowote; na wakati joto la jua linawadia na kuuchoma, kwa sababu hauna mzizi hukaukia mbali, na mtaukata na kuutupa nje.

39 Sasa, hii sio kwa sababu mbegu haikuwa nzuri, wala sio kwa sababu tunda lake halingekuwa la kutamanika; lakini ni kwa sababu mchanga wenu ni kame, na hamwezi kuulisha mti, kwa hivyo hamwezi kupata tunda juu yake.

40 Na hivyo, ikiwa hamtalisha neno, mkingojea tu kwa imani kupata tunda juu yake, hamwezi mkachuna tunda la mti wa maisha.

41 Lakini ikiwa mtalisha neno, ndio, lisha mti unapoanza kukua, kwa imani yenu kwa bidii kuu, na uvumilivu, mkitumainia kupata tunda kwake, utamea mizizi; na tazama utakuwa mti utakaokua na kuzaa matunda yasiyo na mwisho.

42 Na kwa sababu ya bidii yenu na imani yenu na uvumilivu wenu kwa neno kwa kulilisha, kwamba limee ndani yenu, tazama, baadaye mtavuna matunda kwake, ambayo ni ya thamani sana, ambayo ni tamu kupita kiasi; na ambayo ni meupe kupita kiasi, ndio, na safi kupita kiasi; na mtakula hili tunda mpaka hata mshibe, kwamba hamtapata njaa, wala kuona kiu.

43 Kisha, ndungu zangu, mtavuna zawadi ya imani yenu, na bidii yenu, na subira, na uvumilivu, mkingojea mti kuwatolea matunda.

## Alma 33

1 Sasa baada ya Alma kumaliza kusema haya maneno, walimtumia mnenaji wakitamani kujua kama wangeweza kumwamini katika Mungu mmoja, ili waweze kupokea hilo tunda ambalo alilizungumzia, au vile wangeweza kupanda ile mbegu, au hilo neno ambalo alilizungumzia, ambalo alisema lazima lipandwe ndani ya mioyo yao; au jinsi gani wangeanza kutumia imani yao.

2 Na Alma akawaambia: Tazama, mmesema kwamba hamuwezi kumwabudu Mungu wenu kwa sababu mmetupwa nje ya masinagogi yenu. Lakini tazama, ninawaambia, ikiwa mnadhani ati hamuwezi kumwabudu Mungu, mnafanya kosa kubwa, na mnahitaji kupekua maandiko; ikiwa mnadhania kwamba maandishi yamewafunza hii, nyinyi hamuelewi maandishi.

3 Je, mnakumbuka mlisoma yale ambayo Zeno, nabii wa kale, aliyosema kuhusu sala au ibada?

4 Kwani alisema: Wewe una rehema, Ee Mungu, kwani umesikia sala yangu, hata nilipokuwa nyikani; ndio, ulikuwa mwenye rehema wakati niliposali kuhusu wale ambao walikuwa maadui wangu, na ukawarudisha kwangu.

5 Ndio, Ee Mungu, na ulikuwa na rehema kwangu wakati nilipokulilia kwenye shamba langu; wakati nilipokulilia kwa sala yangu, na ulinisikiliza.

6 Na tena, Ee Mungu, wakati nilipoingia kwenye nyumba ulinisikia mimi kwenye
sala yangu.
7 Na wakati nilipoingia katika kijumba changu, Ee Bwana, na kuomba kwako, na
ulinisikia.
8 Ndio, una huruma kwa watoto wako, wakati wanakulilia wewe, ili wasikilizwe
nawe na sio watu, na utawasikiliza.
9 Ndio, Ee Mungu, umekuwa na rehema kwangu, na kusikia vilio vyangu
miongoni mwa umati wako.
10 Ndio, na pia umenisikia wakati nimetupwa nje na kudharauliwa na maadui
wangu; ndio, ulisikia vilio vyangu, na uliwakasirikia maadui wangu, na
ukawatembelea kwa ghadhabu yako na maangamizo ya haraka.
11 Na wewe ulinisikia kwa sababu ya mateso yangu na uaminifu wangu; na ni kwa
sababu ya Mwana wako kwamba umekuwa na rehema jinsi hivyo kwangu, kwa hivyo
nitakulilia wewe katika mateso yangu yote, kwani nina shangwe ndani yako; kwani
umeniondolea hukumu zako, kwa sababu ya Mwana wako.
12 Na sasa Alma aliwaambia: Mnaamini hayo maandiko ambayo yaliandikwa na
wale wa kale?
13 Tazama ikiwa mnayaamini, lazima mwamini yaliyosemwa na Zeno; kwani
tazama, alisema: Umeondoa hukumu zako kwa sababu ya Mwana wako.
14 Sasa, tazama, ndugu zangu, ningeuliza kama mmesoma maandiko? Ikiwa
mmeyasoma, jinsi gani mnaweza kutomwamini Mwana wa Mungu?
15 Kwani haikuandikwa kwamba Zeno pekee ndiye alisema vitu hivi, lakini Zenoki
pia alizungumzia vitu hivi—
16 Kwani tazama, alisema: Umewakasirikia, Ee Bwana, watu hawa, kwa sababu
hawataelewa rehema zako ambazo umewapatia kwa sababu ya Mwana wako.
17 Na sasa, ndugu zangu, mnaona kwamba nabii wa pili wa kale ameshuhudia juu ya
Mwana wa Mungu, na kwa sababu ya watu kutoelewa maneno yake walimpiga na
mawe hadi akafa.
18 Lakini tazama, haya si yote; hawa sio pekee ambao wamezungumza kuhusu
Mwana wa Mungu.
19 Tazama, alizungumziwa na Musa; ndio, na tazama mfano uliinuliwa nyikani,
kwamba yeyote atakayeuangalia aweze kuishi. Na wengi waliangalia na wakaishi.
20 Lakini wachache walielewa maana ya vitu hivyo, na hii ni kwa sababu ya ugumu
wa mioyo yao. Lakini kulikuwa na wengi ambao walikuwa wamefanywa wagumu
kwamba hawangeangalia, kwa hivyo waliangamia. Sasa sababu yao ya kukataa
kuangalia ni kwa sababu hawakuamini kwamba ingewaponya.
21 Ee ndugu zangu, ikiwa mngeponywa tu kwa kutupa macho yenu kwamba
mponywe, si mngeangalia upesi, au ni afadhali mshupaze mioyo yenu kwa
kutokuamini, na kuwa wazembe, kwamba hamngetupa macho yenu ili mwangamie?
22 Ikiwa hivyo, taabu itawapata; lakini ikiwa si hivyo, basi zungusha macho yako na
uanze kuamini katika Mwana wa Mungu, kwamba aje kukomboa watu wake, na
kwamba atateseka na kufa ili alipe dhambi zao; na kwamba atafufuka tena kutoka
kwa wafu, na kutimiza ufufuo, kwamba watu wote watasimama mbele yake,
kuhukumiwa katika siku ya mwisho, kulingana na matendo yao.
23 Na sasa, ndugu zangu, natamani kwamba mtapanda hili neno kwenye mioyo
yenu, na itakavyoanza kumea endelea kuilisha na imani yenu. Na tazama, itakuwa
mti, ikimea ndani yako kwa maisha yasiyo na mwisho. Na kisha Mungu akubali

kwamba mizigo yenu iwe miepesi, kupitia kwa shangwe inayotokana na Mwana
wake. Na hata haya yote mnaweza mkafanya mkipenda. Amina.

## Alma 34

1 Na sasa ikawa kwamba baada ya Alma kuwazungumzia maneno haya aliketi chini
juu ya ardhi, na Amuleki aliamka na kuanza kuwafunza, akisema:
2 Ndugu zangu, ninadhani kwamba ni vigumu kwamba msijue vitu ambavyo
vimezungumziwa kuhusu kuja kwa Kristo, ambaye tunafundisha kwamba ni Mwana
wa Mungu; ndio, ninajua kwamba hivi vitu vilifundishwa kwenu kwa wingi kabla ya
mfarakano wenu kutoka miongoni mwetu.
3 Na kwa vile mmetaka kwamba ndugu yangu mpendwa awajulishe yale
mnayostahili kufanya, kwa sababu ya mateso yenu; na amewazungumzia machache
ili kuzitayarisha akili zenu; ndio, na amewasihi muwe na imani na uvumilivu—
4 Ndio, hata kwamba muwe na imani nyingi hata mpande neno ndani ya mioyo
yenu, ili mjaribu kujua uzuri wake.
5 Na tumeona kwamba swali kubwa ambalo liko kwenye akili zenu ni kama neno
liko kwa Mwana wa Mungu, au kama hakutakuweko na Kristo.
6 Na mliona kwamba ndugu yangu amewathibitishia, kwa mifano mingi, kwamba
neno la wokovu liko katika Kristo.
7 Ndugu yangu ametumia maneno ya Zeno, kwamba ukombozi huja kupitia
Mwana wa Mungu, na pia alitumia maneno ya Zenoki; na pia amekata rufani kwa
Musa, kuthibitisha kwamba hivi vitu ni vya kweli.
8 Na sasa, tazama, nitawashuhudia mimi mwenyewe kwamba vitu hivi ni vya
kweli. Tazama, nawaambia, kwamba najua kwamba Kristo atakuja miongoni mwa
watoto wa watu, kujitwalia makosa ya watu, na kwamba atalipia dhambi za
ulimwengu; kwani Bwana Mungu amesema.
9 Kwani ni ya kufaa kwamba upatanisho ufanywe, kwani kulingana na mpango
mkuu wa Mungu wa milele lazima upatanisho ufanywe, la sivyo wanadamu wote ni
lazima bila kuepuka wapotee; ndio, wote wamekuwa wagumu; ndio, wote
wameanguka na wamepotea, na ni lazima wapotee isipokuwa wapitie kwa
upatanisho ambao ni lazima ufanywe.
10 Kwani ni ya kufaa kwamba kuwe na dhabihu kuu na ya mwisho; ndio, sio
dhabihu ya mtu, wala ya mnyama, wala ya aina yoyote ya ndege; kwani haitakuwa
dhabihu ya binadamu; lakini lazima iwe isiyo ya mwisho na dhabihu ya milele.
11 Sasa hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kutoa dhabihu ya damu yake ambayo
italipia dhambi ya mwingine. Sasa, kama mtu anaua, tazama, sheria yetu, ambayo ni
ya haki, itachukua maisha ya kaka yake? Nasema kwenu, Hapana.
12 Lakini sheria inahitaji maisha ya yule ambaye ameua; kwa hivyo hakuwezi kuwa
na chochote ambacho kimepungua kuliko upatanisho usio na mwisho ambao
utatosheleza dhambi za ulimwengu.
13 Kwa hivyo, ni ya kufaa kwamba kuwe na dhabihu kubwa na ya mwisho, na ndipo
kutakuweko, au ni ya kufaa kwamba kuweko kikomo kwa umwagaji wa damu; ndipo
sheria ya Musa itapatwa kutimizwa; ndio, yote itatimizwa, kila tone na chembe, na
hakuna yoyote ambayo itafutiliwa mbali.
14 Na tazama, hii ndiyo maana kamili ya sheria, kila chembe kikielekeza kwa ile
dhabihu kubwa na ya mwisho; na hivyo dhabihu kubwa na ya mwisho itakuwa

Mwana wa Mungu, ndio, isiyo ya mwisho na milele.
15 Na hivyo ataleta wokovu kwa wote ambao wataamini katika jina lake; hii ikiwa kusudi la hii dhabihu ya mwisho, kufungua tumbo la rehema, ambayo hupindua haki, na kuwafungulia wanadamu njia ya kupata imani na toba.
16 Na hivyo rehema inaridhisha mahitaji ya haki, na kuwazingira kwa mikono ya usalama, wakati yule ambaye hatumii imani kwa kutubu anajiweka wazi kwa sheria yote ya madai ya haki; kwa hivyo ni tu yule ambaye ana imani kwa toba atatimiziwa mpango mkuu wa ukombozi.
17 Kwa hivyo Mungu awajalie, ndugu zangu, kwamba mwanze kutumia imani yenu kwa toba, kwamba mwanze kulilingana jina lake takatifu, ili awe na rehema kwenu;
18 Ndio, mlilie kwa rehema; kwani ana uwezo wa kuokoa.
19 Ndio, mjinyenyekeze, na kuendelea kusali.
20 Mlilie mkiwa ndani ya mashamba yenu, ndio, juu ya mifugo yenu yote.
21 Mlilie ndani ya nyumba zenu, ndio, wote wa nyumba yako, asubuhi, mchana, na jioni.
22 Ndio, mlilie dhidi ya uwezo wa maadui wenu.
23 Ndio, mlilie dhidi ya ibilisi, ambaye ni adui wa yote yaliyo haki.
24 Mlilie juu ya mimea yenu ndani ya mashamba, kwamba muweze kufanikiwa.
25 Lieni juu ya kundi la mifugo katika mashamba yenu, kwamba iongezeke.
26 Lakini hii sio yote, lazima mfungue roho zenu ndani ya vijumba vyenu, na mahali penu pa siri, na kwenye nyika zenu.
27 Ndio, na wakati hamummlilii Bwana, hebu mioyo yenu ijae, mdumu katika sala kwake siku zote kwa ustawi wenu, na pia kwa ustawi wa wale ambao wako karibu nanyi.
28 Na sasa tazama, ndugu zangu wapendwa, nawaambia, msidhani kwamba haya ni yote; kwani baada ya kufanya hivi vitu vyote, ikiwa mtawafukuza masikini, na walio uchi, na msiwatembelee wagonjwa na walioteseka, na kuwagawia mali yenu, ikiwa mnayo, wale ambao wanahitaji—Ninawaambia, ikiwa hamfanyi vitu hivi, tazama, sala yenu ni ya bure, kwani hayatakupatia chochote, na wewe ni kama wanafiki ambao wanakana imani.
29 Kwa hivyo kama hamuwezi kukumbuka kuwa wakarimu, ninyi ni kama takataka ambayo wasafishaji hutupa nje, (ikiwa haina faida) na inakanyagwa chini na miguu ya watu.
30 Na sasa, ndugu zangu, ningetaka kwamba baada ya kupokea ushahidi mwingi hivyo, mkiona kwamba maandiko matakatifu yanashuhudia vitu hivi, mje mbele na mwonyeshe matunda ya toba.
31 Ndio, ningependa kwamba mje mbele na msishupaze mioyo yenu mara nyingine; kwani tazama, sasa ndio wakati na siku ya wokovu wenu; na kwa hivyo ikiwa mtatubu, na msishupaze mioyo yenu, mara moja mpango mkuu wa ukombozi utatimizwa kwenu.
32 Kwani tazama, maisha haya ndiyo wakati wa watu kujitayarisha kukutana na Mungu; ndio, tazama, wakati wa maisha haya ndiyo siku ya watu kufanya kazi yao wanayohitaji.
33 Na sasa, nilivyosema kwenu mbeleni, kwa vile mna mashahidi wengi, kwa hivyo, nawaomba msiahirishe siku yenu ya toba hadi mwisho; kwani baada ya siku hii ya maisha, ambayo tumepewa ya kujitayarishia milele, tazama, kama hatuwezi kutenda mema wakati tuko kwa maisha haya, kutakuja usiku wa giza ambapo hakutakuwa

chochote kitakachofanywa.
34 Huwezi kusema, wakati utaletwa kwa ile shida ya kutisha, kwamba nitatubu,
kwamba nitamrudia Mungu wangu. Hapana, hamuwezi kusema hivi; kwani ile
roho ambayo inamiliki miili yenu mkitoka katika maisha haya, roho ile ile itakuwa
na uwezo wa kushika mwili wako katika ule ulimwengu wa milele.
35 Kwani tazama, ikiwa mmeahirisha siku zenu za toba hadi kifo, tazama, mmekuwa
chini ya roho wa ibilisi, na amewatia muhuri kuwa wake, kwa hivyo, Roho ya Bwana
imeandoka kwenu, na hana mahali ndani yenu, na ibilisi ana uwezo wote juu yenu;
na hii ndiyo hali ya mwisho wa waovu.
36 Na ninajua haya, kwa sababu Bwana amesema haishi kwenye mahekalu yasiyo
matakatifu, lakini yeye huishi kwenye mioyo ya wale wenye haki; ndio, na pia
amesema kwamba wenye haki watakaa chini katika ufalme wake, bila kwenda nje
tena; lakini nguo zao sharti zifanywe nyeupe kupitia kwa damu ya mwanakondoo.
37 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, natamani kwamba mkumbuke vitu hivi, na
kwamba mtumikie wokovu wenu kwa woga mbele ya Mungu, na kwamba msikane
tena kuja kwa Kristo;
38 Kwamba msibishane tena dhidi ya Roho Mtakatifu, lakini kwamba muipokee, na
mjichukulie jina la Kristo; kwamba mjinyenyekeze sana hata kwenye mavumbi, na
kumwabudu Mungu, mahali popote mtakapokuwa, ndani ya roho na ndani ya
ukweli, na kwamba muishi katika kushukuru kila siku, kwa rehema nyingi na baraka
ambazo anaweka kwenu.
39 Ndio, na pia nawasihi, ndugu zangu, kwamba muwe waangalifu ndani ya sala bila
kikomo, ili msipotezwe na majaribio ya ibilisi, kwamba asiwashinde nyinyi, kwamba
msije mkawa chini yake siku ya mwisho; kwani tazama, hakupatii zawadi ya kitu
kizuri.
40 Na sasa ndugu zangu wapendwa, ningewasihi muwe na uvumilivu, na kwamba
mvumilie aina yote ya mateso; kwamba msishutumu dhidi ya wale waliowatupa nje
kwa sababu ya umasikini wenu mkuu, msije kuwa wenye dhambi kama wao.
41 Lakini kwamba muwe na uvumilivu, na mvumilie yale mateso, na tumaini thabiti
kwamba siku moja mtapumzika kutoka kwa mateso yenu yote.

## Alma 35

1 Sasa ikawa kwamba Amuleki alipomaliza kuzungumza mambo hayo, waliondoka
kutoka lile kundi na wakaenda kwenye nchi ya Yershoni.
2 Ndio, na ndugu wengine, baada ya kuhubiri neno kwa Wazoramu, pia walikuja
kwenye nchi ya Yershoni.
3 Na ikawa kwamba baada ya Wazoramu wengi waliokuwa mashuhuri kushauriana
pamoja kuhusu maneno ambayo yalikuwa yamehubiriwa kwao, walikasirika juu ya
neno, kwani liliharibu hila yao; kwa hivyo hawangesikiliza maneno.
4 Na wakawatuma na waliwakusanya pamoja kote nchini watu wote, na
kuwashauri kuhusu maneno ambayo yalikuwa yamesemwa.
5 Sasa watawala wao na makuhani wao na walimu wao hawawafahamisha watu
kuhusu nia yao; kwa hivyo waligundua kwa kisiri mawazo ya watu wote.
6 Na ikawa kwamba baada ya kupata mawazo ya watu wote, wale ambao waliunga
mkono yale maneno ambayo yalizungumzwa na Alma na ndugu zake walitupwa nje
ya nchi; na walikuwa wengi; na walikuja pia katika nchi ya Yershoni.

7 Na ikawa kwamba Alma na ndugu zake waliwahudumia.
8 Sasa watu wa Wazoramu waliwakasirikia watu wa Amoni ambao walikuwa Yershoni, na mtawala mkuu wa Wazoramu, akiwa mtu mwovu sana, alituma mjumbe kwa watu wa Amoni akiwataka wawatupe nje ya nchi yao wale wote ambao walitoka katika nchi yao.
9 Na alitoa vitisho vingi dhidi yao. Na sasa watu wa Amoni hawakuogopa maneno yao; kwa hivyo hawakuwatupa nje, lakini walipokea Wazoramu wote waliokuwa masikini ambao walikuja kwao; na waliwalisha, na wakawavisha, na wakawapatia ardhi kwa urithi wao; na wakawahudumia kulingana na mahitaji yao.
10 Sasa hii iliwavuruga Wazoramu kuwakasirikia watu wa Amoni, na wakaanza kuchanganyika na Walamani na wakawavuruga pia kukasirika dhidi yao.
11 Na hivyo Wazoramu na Walamani walianza kujiandaa kwa vita dhidi ya watu wa Amoni, na pia dhidi ya Wanefi.
12 Na hivyo ukaisha mwaka wa kumi na saba wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.
13 Na watu wa Amoni waliondoka kutoka nchi ya Yershoni, na wakaingia katika nchi ya Meleki, na wakawapatia majeshi ya Wanefi mahali katika nchi ya Yershoni, ili wakabiliane na majeshi ya Walamani na majeshi ya Wazoramu; na hivyo vita vikaanza kati ya Walamani na Wanefi, katika mwaka wa kumi na nane wa utawala wa waamuzi; na historia itatolewa kuhusu vita vyao baadaye.
14 Na Alma, na Amoni, na ndugu zao, na pia wana wawili wa Alma walirejea katika nchi ya Zarahemla, baada ya kuwa vyombo mikononi mwa Mungu kuleta wengi wa Wazoramu kutubu; na vile walipoletwa kwa toba, walikimbizwa kutoka katika nchi yao; lakini wana mashamba kwa urithi wao katika nchi ya Yershoni, na wametayarisha silaha zao kwa kujikinga wenyewe, na wake zao, na watoto, na mashamba yao.
15 Sasa Alma, akiwa amehuzunishwa na uovu wa watu wake, ndio, kwa vita, na umwagaji wa damu, na mabishano ambayo yalikuwa miongoni mwao; na akiwa ameenda kutangaza neno, au kwa maneno mengine, kutangaza neno miongoni mwa watu wote katika kila mji; na akiona kwamba mioyo ya watu ilianza kuwa migumu, na kwamba walianza kuudhika kwa sababu ya uhalisi wa neno, moyo wake ulihuzunika sana.
16 Kwa hivyo, alisababisha kwamba wana wake wakusanywe pamoja, ili atoe maagizo tofauti, kwa kila mmoja, kuhusu vitu vinavyohusiana na haki. Na tuna historia ya amri zake, ambazo aliwapatia kulingana na maandishi yake.

*Amri za Alma kwa mwana wake Helamani.*

# Alma 36

1 Mwana wangu, sikiliza maneno yangu; kwani naapa kwako, kwamba kadiri utakavyoweka amri za Mungu ndivyo utafanikiwa katika nchi.
2 Ningetaka kwamba ufanye vile nimevyofanya, kwa kukumbuka utumwa wa babu zetu; kwani walikuwa katika utumwa, na hapakuwa na yeyote ambaye angewaokoa isipokuwa awe Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo; na kwa kweli aliwakomboa katika mateso yao.

3 Na sasa, Ee mwana wangu Helamani, tazama, wewe ni kijana, na kwa hivyo, nakuomba wewe kwamba usikilize maneno yangu na ujifunze kutoka kwangu; kwani najua kwamba wote watakaoweka imani yao katika Mungu watasaidiwa kwa majaribio yao, na taabu zao, na mateso yao, na watainuliwa juu katika siku ya mwisho.
4 Na sitaki kwamba ufikiri kwamba nimejijulia — sio kwa kimwili lakini kwa kiroho, sio kwa mawazo ya kimwili lakini ya Mungu.
5 Sasa, tazama, nakwambia, ikiwa nisingezaliwa kwa Mungu nisingekuwa nimejua vitu hivi; lakini Mungu, kwa mdomo wa malaika wake mtakatifu, amethibitisha hivi vitu kwangu, sio kwa sababu ya wema wangu;
6 Kwani nilienda na wana wa Mosia, nikinuia kuharibu kanisa la Mungu; lakini tazama, Mungu alimtuma malaika wake mtakatifu kutuzuia tulipokuwa njiani.
7 Na tazama, alituzungumzia, kwa sauti kama ya radi, na ardhi yote ilitetemeka chini ya miguu yetu; na sisi sote tuliinama kwenye ardhi, kwani hofu ya Bwana ilitujia.
8 Lakini tazama, sauti iliniambia: Amka. Na niliamka na kusimama wima, na nikaona malaika.
9 Na akaniambia: Ikiwa hutaki kuangamizwa mwenyewe, usijaribu tena kuangamiza kanisa la Mungu.
10 Na ikawa kwamba niliinama kwenye ardhi; na ilikuwa kwa muda wa siku tatu na usiku tatu kwamba nisingefungua kinywa changu, wala kutumia viungo vyangu.
11 Na malaika alinizungumzia vitu vingi zaidi, ambavyo vilisikika na ndugu zangu, lakini mimi sikuvisikia; kwani wakati niliposikia maneno — Ikiwa hutaki kujiangamiza mwenyewe, usijaribu tena kuliangamiza kanisa la Mungu — Nilipigwa na woga mwingi sana na mshangao kwa hofu kwamba ningeangamizwa, kwamba niliinama kwenye ardhi na sikusikia tena.
12 Lakini nilisumbuliwa na adhabu ya milele, kwani roho yangu iliteseka kwa kiasi kikubwa sana na kuadhibiwa kwa dhambi zangu zote.
13 Ndio, nilikumbuka dhambi zangu zote na uovu, kwa ajili hiyo niliadhibiwa na uchungu wa jahanamu; ndio, niliona kwamba nimeasi dhidi ya Mungu wangu, na kwamba sikuwa nimetii amri zake.
14 Ndio, na nilikuwa nimeua watoto wake wengi, au kwa usahihi zaidi niliwaelekeza kwenye maangamizo; ndio, na kwa ufupi uovu wangu ulikuwa mwingi sana kwamba ile fikira ya kukaribia uwepo wa Mungu wangu iliiadhibu nafsi yangu kwa hofu kuu isiyoelezeka.
15 Ee, nilifikiri kwamba, ningehaamishwa na kutokuwepo kwa nafsi wala mwili, kwamba nisingeletwa kusimama kwenye uwepo wa Mungu wangu, kuhukumiwa kwa vitendo vyangu.
16 Na sasa, kwa usiku tatu na kucha tatu niliteseka, hata na uchungu wa nafsi iliyolaaniwa.
17 Na ikawa kwamba wakati nilipoteseka na maumivu mabaya, wakati nilihuzunishwa na ufahamu wa dhambi zangu nyingi, tazama, nilikumbuka pia nikisikia baba yangu akitoa unabii kwa watu kuhusu kuja kwa mmoja aitwaye Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kulipia dhambi za ulimwengu.
18 Sasa, nilipofiikiria wazo hili, nililia ndani ya moyo wangu: Ee Yesu, wewe Mwana wa Mungu, nihurumie, mimi ambaye nina uchungu, na nimezungukwa na minyororo ya kifo kisicho na mwisho.

19 Na sasa, tazama, nilipofikiri hivi, sikukumbuka uchungu wangu tena; ndio,
sikuteseka na ufahamu wa dhambi zangu tena.
20 Na Ee, ni shangwe gani, na ni mwangaza gani wa ajabu niliouona; ndio, nafsi
yangu ilijazwa na shangwe ya ajabu kama vile ulikuwa uchungu wangu!
21 Ndio, nakwambia, mwana wangu, kwamba hakungekuwa na chochote
kilichokuwa kikali vile na kichungu vile ulivyokuwa uchungu wangu. Ndio, na tena
ninakwambia, mwana wangu, kwamba upande mwingine, hapawezi kuwa na kitu
kizuri hivyo na kitamu vile ilivyokuwa shangwe yangu.
22 Ndio, nilidhani niliona; hata vile babu yetu Lehi alivymwoona, Mungu akiketi
kwenye kiti chake cha enzi, akizungukwa na umati usiohesabika wa malaika, kwa
hali ya kuimbia na kumsifu Mungu wao; ndio, na nafsi yangu ilitamani kuwa hapo.
23 Lakini tazama, viungo vyangu vilipata nguvu tena, na nilisimama kwa miguu
yangu, na nikajidhihirisha kwa watu kwamba nimezaliwa kwa Mungu.
24 Ndio, na tangu wakati huo hata hadi sasa, nimefanya kazi bila kukoma, kwamba
nilete nafsi za watu kutubu; kwamba ningewaleta wapate kuonja shangwe kuu
ambayo niliiona; ili nao pia wazaliwe ndani ya Mungu, na wajazwe na Roho
Mtakatifu.
25 Ndio, na sasa tazama, Ee mwana wangu, Bwana hunipa shangwe kuu kwa
matokeo ya kazi yangu;
26 Kwani kwa sababu ya neno ambalo amenipatia, tazama, wengi wamezaliwa kwa
Mungu, na wameonja vile nimevyonja, na wameona macho kwa macho vile
nimevyona; kwa hivyo wanajua kuhusu vitu hivi ambavyo nimezungumzia, vile
ninavyojua; na elimu ambayo ninayo ni ya Mungu.
27 Na nimesaidiwa wakati wa majaribio na taabu za kila aina, ndio, na kwa kila aina
ya mateso; ndio, Mungu amenikomboa kutoka jela, na kutoka kufungwa, na kutoka
kifo; ndio, na ninaweka tumaini langu ndani yake, na atanikomboa.
28 Na ninajua kwamba ataiinua katika siku ya mwisho, kuishi na yeye kwenye
utukufu; ndio, na nitamsifu milele, kwani amewaleta babu zetu nje ya Misri, na
amewameza Wamisri ndani ya Bahari ya Shamu; na aliwaongoza na uwezo wake
hadi kwenye nchi ya ahadi; ndio, na amewakomboa kutoka kifungoni na utumwa
mara kwa mara.
29 Ndio, na amewaleta babu zetu kutoka nchi ya Yerusalemu; na pia kwa uwezo
wake usio na mwisho, amewakomboa kutoka kifungoni na utumwa wao, mara kwa
mara hadi wakati huu; na daima nimehifadhi ukumbusho wa utumwa wao; ndio, na
nyinyi pia inawapasa kuhifadhi ukumbusho wa utumwa wao, kama vile
nimevyofanya.
30 Lakini tazama, mwana wangu, hii si yote; kwani unapaswa kujua vile ninajua
kwamba kadiri utakavyoshika amri za Mungu utafanikiwa nchini; na unapaswa
kujua pia kwamba, kadiri utakavyoacha kutii amri za Mungu utatolewa kwenye
uwepo wake. Sasa hii ni kulingana na neno lake.

# Alma 37

1 Na sasa, mwana wangu Helamani, ninakuamuru kwamba uchukue maandishi
ambayo nilikabidhiwa;
2 Na pia ninakuamuru kwamba uandike maandishi ya hawa watu, kulingana na
vile nimefanya, kwenye bamba za Nefi, na uhifadhi vitu hivi vyote vitakatifu

ambavyo nimehifadhi, hata vile nimevihifadhi; kwani ni kwa sababu ya busara
kwamba zimewekwa.
3 Na hizi bamba za shaba, ambazo zina michoro, ambazo zina maandiko
matakatifu juu yake, ambazo zina nasaba ya babu zetu, hata kutoka mwanzoni—
4 Tazama, unabii umetolewa na babu zetu, kwamba zihifadhiwe na kutolewa
kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine, na ziwekwe na kulindwa na mkono wa
Bwana mpaka ziwafikie kila taifa, ukoo, lugha, na watu, kwamba wafahamu siri
zilizomo.
5 Na sasa tazama, ikiwa zitahifadhiwa lazima ziweke mng'aro wao; ndio, na
zihifadhi mng'aro wao; ndio, na pia bamba zote ambazo zina maandiko matakatifu.
6 Sasa labda unadhani kwamba huu ni upuuzi ndani yangu; lakini tazama
nakwambia, kwamba kupitia kwa vitu vilivyo vidogo na rahisi vitu vikubwa
hutendeka; na njia ndogo mara nyingi hufadhaisha wenye hekima.
7 Na Bwana Mungu hutumia njia zake ili kutimiza kusudi lake kuu na la milele; na
kwa njia ndogo sana Bwana hufawadhaisha wale werevu na kutimiza wokovu wa
roho nyingi.
8 Na sasa, mpaka sasa imekuwa hekima ndani ya Mungu kwamba vitu hivi
vihifadhiwe; kwani tazama, vimeongeza ufahamu wa watu hawa, ndio, na
kuwasadikisha wengi kuhusu makosa ya njia zao, na kuwaleta kwenye ufahamu wa
Mungu wao hadi kwa wokovu wa nafsi zao.
9 Ndio, nakwambia wewe, isingekuwa vitu hivi ambavyo maandishi haya yanayo,
ambavyo viko kwenye bamba hizi, Amoni na ndugu zake hawangesadikisha maelfu
wengi hivyo wa Walamani kuhusu desturi zisizo sawa za baba zao; ndio, haya
mandishi na maneno yao yaliwaleta kwenye toba; yaani, yaliwaleta kwa ufahamu wa
Bwana Mungu wao, na kufurahi katika Yesu Kristo Mkombozi wao.
10 Na nani anajua lakini kwamba watakuwa njia ya kuwaleta maelfu wengi wao,
ndio, na pia maelfu wengi wa ndugu zetu wenye shingo ngumu, Wanefi, ambao sasa
wanashupaza mioyo yao kwenye dhambi na uovu, kwa ufahamu wa Mkombozi wao?
11 Sasa hizi siri hazijafahamishwa kwangu kabisa; kwa hivyo sitaongea tena.
12 Na ingetosha kwangu kusema zimehifadhiwa kwa kusudi la busara, kusudi
ambalo linajulikana na Mungu; kwani yeye hushauri kwa hekima juu ya kazi yake
yote, na njia zake ni nyoofu, na mwenendo wake ni ule usiobadilika.
13 Ee kumbuka, kumbuka, mwana wangu Helamani, vile amri za Mungu ni kali. Na
alisema: Ikiwa utatii amri zangu utafanikiwa nchini—lakini kama huwezi kutii
amri zake utatolewa kutoka uwepo wake.
14 Na sasa kumbuka, mwana wangu, kwamba Mungu amekukabidhii vitu hivi,
ambavyo ni takatifu, ambavyo amezifanya zitakatifu, na pia ambavyo ataweka na
kuhifadhi kwa nia ya busara ambayo anajua, ili aweze kuonyesha uwezo wake kwa
vizazi vijavyo.
15 Na sasa tazama, nakwambia kwa roho ya unabii, kwamba ikiwa utavunja amri za
Mungu, tazama, vitu hivi ambavyo ni wakfu vitatolewa kwako kwa uwezo wa
Mungu, na utatolewa kwa Shetani, kwamba aweze kukuchunga kama kapi mbele ya
upepo.
16 Lakini kama utatii amri za Mungu, na ufanye vitu hivi ambavyo ni vitakatifu
kulingana na yale ambayo Bwana amekuamuru ufanye, (kwani lazima uombe
msaada wa Bwana kwa vitu vyote ambavyo unataka kuvitumia) tazama, hakuna
nguvu za ardhini au jahanamu, zinazoweza kuvichukua kutoka kwako, kwani

Mungu ni mwenye uwezo kwa kutimiza maneno yake yote.
17 Kwani atatimza ahadi zake zote ambazo atakuahidi, kwani ametimiza ahadi zake ambazo amewaahidi babu zetu.
18 Kwani aliwaahidi kwamba atahifadhi vitu hivi kwa kusudi la busara kwake, kwamba angeweza kuonyesha nguvu yake kwa vizazi vijavyo.
19 Na sasa tazama, kusudi moja ametimiza, hata kwa kurudisha maelfu wengi wa Walamani kwa ufahamu wa ukweli; na ameonyesha tena uwezo wake kwao, na pia ataonyesha uwezo wake tena ndani yao kwa vizazi vijavyo; kwa hivyo vitahifadhiwa.
20 Kwa hivyo ninakuamuru, mwana wangu Helamani, kwamba uwe na bidii kwa kutimiza maneno yangu yote, na kwamba uwe na bidii kwa kutii amri za Mungu kama zimeandikwa.
21 Na sasa, nitaongea na wewe kuhusu zile bamba ishirini na nne, kwamba uzihifadhi, ili siri na vitendo viovu, na kazi zao za siri, au kazi za siri za wale watu ambao wemeangamizwa, zingeonyeshwa kwa watu hawa; ndio, mauaji yao yote, na wizi, na utekaji nyara wao, na maovu na machukizo yao yote, yangejulikana kwa hawa watu; ndio, na kwamba uzihifadhi vitafsiri hivi.
22 Kwani tazama, Bwana aliona kwamba watu wake walianza kufanya kazi gizani, ndio, walifanya mauaji ya siri na machukizo; kwa hivyo Bwana alisema, ikiwa hawangetubu wangeamizwa kutoka usoni mwa dunia.
23 Na Bwana akasema: Nitatamyarishia mtumishi wangu Gazelemu, jiwe, ambalo litamulika mwangaza gizani, kwamba niwafahamishe watu wangu ambao wananihudumia, kwamba ningewafahamisha kazi za ndugu zao, ndio, kazi zao za siri, kazi zao za gizani, na uovu wao na machukizo yao.
24 Na sasa mwana wangu, hivi vitafsiri zilitayarishwa kwamba neno la Mungu lingetimizwa, ambalo alizungumza, akisema:
25 Nitatoa nje kutoka gizani hadi kwenye mwanga kazi zao za siri na machukizo yao; na wasipotubu nitawaangamiza kutoka uso wa dunia; na nitaleta kwa mwangaza siri zao zote na machukizo yao, kwa kila taifa ambalo kutoka sasa kuendelea litamiliki nchi.
26 Na sasa, mwana wangu, tunajua kwamba hawakutubu; kwa hivyo wameangamizwa, na hivyo neno la Mungu limetimizwa; ndio, siri zao za machukizo zimetolewa gizani na kujulikana kwetu.
27 Na sasa, mwana wangu, ninakuamuru uweke viapo vyao, na maagano yao, na mapatano yao ya siri zao za machukizo; ndio, na ishara zao zote na miujiza ya hila utaficha kutoka kwa hawa watu, ili wasiyajue, isiwe ikawa waanguke gizani pia na waangamizwe.
28 Kwani tazama, kuna laana juu ya nchi hii yote, kwamba maangamizo yatafika juu ya wale wote wanaofanya kazi gizani, kulingana na uwezo wa Mungu, wakati watakuwa wameiva; kwa hivyo natamani kwamba hawa watu wasiangamizwe.
29 Kwa hivyo utaweka hii mipango yao ya siri za viapo na maagano yao kutoka kwa hawa watu, na tu maovu yao na mauaji yao na machukizo yao yatajulishwa kwao; na utawafundisha kuchukia maovu na machukizo na mauaji kama hayo, na utawafundisha pia kwamba hawa watu waliangamizwa kwa sababu ya uovu wao na machukizo na mauaji yao.
30 Kwani tazama, waliwaua manabii wote wa Bwana ambao walikuja miongoni mwao kutangaza kwao kuhusu uovu; na damu ya wale ambao waliwaua ililia kutoka ardhini kwa Bwana Mungu wao kulipiza kisasi kwa wale ambao waliwaua; na hivi

hukumu ya Mungu iliwajia hawa wafanyikazi wa giza na makundi maovu ya siri.
31 Ndio, na nchi ilaaniwe milele na milele kwa wale wafanyikazi wa gizani na makundi ya siri, hata kwenye maangamizo, isipokuwa watubu kabla ya kuwa waovu kabisa.
32 Na sasa, mwana wangu, kumbuka maneno ambayo nimekuzungumzia; usiamini ile mipango ya siri kwa watu hawa, lakini uwafundishe chuki isiyo na mwisho dhidi ya dhambi na uovu.
33 Wahubirie toba, na imani kwa Bwana Yesu Kristo; wafundishe kujinyenyekea na kuwa wapole, na wanyenyekevu moyoni; wafunze kushindana na kila jaribio la ibilisi, na imani yao kwa Bwana Yesu Kristo.
34 Wafunze wasichoke na kazi nzuri daima, lakini kuwa wapole na wanyenyekevu moyoni; kwani kama hawa watapata mapumziko kwa nafsi zao.
35 Ee, kumbuka, mwana wangu, na ujifunze hekima katika ujana wako; ndio, jifunze katika ujana wako kutii amri za Mungu.
36 Ndio, na mlilie Mungu kwa usaidizi wako wote; ndio, acha vitendo vyako vyote viwe kwa Bwana, na popote uendapo acha iwe kwa Bwana; ndio, acha fikira zako zote zielekezwe kwa Bwana; ndio, acha mapenzi ya moyo wako yaelekezwe kwa Bwana milele.
37 Shauriana na Bwana kwenye matendo yako yote, na atakuongoza kwa yale mema; ndio, unapolala usiku lala katika Bwana, ili akulinde usingizini mwako; na ukiamka asubuhi hebu moyo wako ujazwe na shukrani kwa Mungu; na ukifanya vitu hivi, utainuliwa katika siku ya mwisho.
38 Na sasa, mwana wangu, nina machache ya kuzungumza kuhusu kitu ambacho babu zetu wanaita mpira, au mwelekezi—au baba zetu waliita Liahona, ambayo, inaamanisha dira; na Bwana aliitayarisha.
39 Na tazama, hakungekuwa na mtu ambaye angetengeneza kitu cha mtindo aina hii. Na tazama, ilitayarishwa kuwaonyesha babu zetu njia ambayo wangesafiria katika nyika.
40 Na iliwatumikia kulingana na imani yao kwa Mungu; kwa hivyo, kama walikuwa na imani kuamini kwamba Mungu angesababisha hivyo vijiti vingeonyesha njia ambayo wangefuata, tazama, ilifanyika; kwa hivyo walikuwa na muujiza huu, na pia miujiza mingine mingi iliyofanyika kwa uwezo wa Mungu, siku hadi siku.
41 Walakini, kwa sababu hiyo miujiza ilitendeka kupitia kwa njia rahisi iliwaonyesha kazi ya kushangaza. Walikuwa wavivu na walisahau kutumia imani yao na bidii na baadaye zile kazi za ajabu zilikoma, na hawakuendelea kwenye safari yao;
42 Kwa hivyo, walikaa nyikani, au hawakusafiri kwa njia nyoofu, na waliteswa na njaa na kiu, kwa sababu ya makosa yao.
43 Na sasa, mwana wangu, ningependa uelewe kwamba vitu hivi haviko bila mfano wa maana; kwani vile babu zetu walivyokuwa wavivu kufuata hii duara (sasa vitu hivi vilikuwa vya muda) hawakufanikiwa; hata hivyo ndivyo ilivyo na vitu ambavyo ni vya kiroho.
44 Kwani tazama, ni rahisi kama kutii neno la Kristo, ambalo litakuonyesha njia nyoofu kwa raha ya milele, kama vile ilivyokuwa kwa babu zetu kutii hii dira, ambayo ingewaonyesha njia nyoofu kuelekea nchi ya ahadi.
45 Na sasa nasema, hakuna mfano wa kitu hiki? Kwani kwa hakika vile mwongozo huu ulivyowaleta babu zetu kwa kufuata njia yake, kuelekea nchi ya ahadi, hivyo maneno ya Kristo, ikiwa tutafuata mwelekeo wake, yatatuvukisha hili bonde la

huzuni hadi mbali kwenye nchi bora ya ahadi.
46 Ee mwana wangu, usiache tuwe wavivu kwa sababu ya urahisi wa njia; kwani
hivyo ndivyo ilivyokuwa babu zetu; kwani hivyo ndivyo ilivyotayarishwa kwao,
kwamba ikiwa wangeangalia kwake wangeishi; hata hivyo iko nasi. Njia
imetayarishwa, na ikiwa tutaangalia tutaishi milele.
47 Na sasa, mwana wangu, uwe na hakika kwamba unalinda vitu hivi vitakatifu,
ndio, ona kwamba umeelekeza jicho kwa Mungu na uishi. Waendee hawa watu na
kutangaza neno, na uwe na busara. Mwana wangu, kwaheri.

*Amri za Alma kwa mwana wake Shibloni.*

# Alma 38

1 Mwana wangu, sikiliza maneno yangu, kwani ninakwambia, vile nilimwambia
Helamani, kwamba ikiwa utatii amri za Mungu utafanikiwa katika nchi; na kadiri
hutatii amri za Mungu utaondolewa kwenye uwepo wake.
2 Na sasa, mwana wangu, ninaamini kwamba nitakuwa na shangwe kuu juu yako,
kwa sababu ya uthabiti wako na imani yako kwa Mungu; kwani kwa njia hiyo
umeanza katika ujana wako kumtegemea Bwana Mungu wako, hata hivyo natarajia
kwamba utaendelea kutii amri zake; kwani heri yule atakayevumilia hadi mwisho.
3 Nakwambia wewe, mwana wangu, kwamba tayari nimekuwa na shangwe kwako,
kwa sababu ya uaminifu wako na bidii yako na subira yako na uvumilivu wako
miongoni mwa watu wa Wazoramu.
4 Kwani ninajua kwamba ulikuwa umefungwa; ndio, na pia najua kwamba
ulipigwa kwa mawe kwa ajili ya kuhubiri neno; na ulivumilia hivi vitu vyote kwa
sababu Bwana alikuwa nawe; na sasa unajua kwamba Bwana alikuokoa.
5 Na sasa mwana wangu, Shibloni, ningetaka wewe ukumbuke, kwamba kadiri
utakavyoweka imani yako ndani ya Mungu hata hivyo zaidi utakombolewa kutoka
kwa majaribio yako, na taabu zako, na mateso yako, na utainuliwa juu siku yako ya
mwisho.
6 Sasa, mwana wangu singetaka kwamba ufikirie kwamba ninajua vitu hivi kwa
uwezo wangu, lakini ni Roho ya Bwana iliyo ndani yangu ndiyo inayonijulisha vitu
hivi; kwani kama nisingezaliwa kwa Mungu nisingejua vitu hivi.
7 Lakini tazama, Bwana kwa rehema yake kuu alimtuma malaika wake kutangaza
kwangu kwamba nikome kazi ya kuangamiza miongoni mwa watu wake; ndio, na
nimemwona malaika uso kwa uso, na akazungumza na mimi, na sauti yake ilikuwa
kama radi, na ikatetemesha ardhi yote.
8 Na ikawa kwamba nilikuwa kwa usiku tatu na kucha tatu ndani ya uchungu
mkali na maumivu ya roho; na haikuwa mpaka nilipomlilia Bwana Yesu Kristo kwa
huruma, ndipo nikapata kusamehewa dhambi zangu. Lakini tazama, nilimlilia na
nikapata amani ndani ya roho yangu.
9 Na sasa, mwana wangu, nimekwambia hii ili ujifunze hekima, kwamba
ungejifunza kutoka kwangu kwamba hakuna njia nyingine au kwa vyote ambayo
binadamu anaweza kuokolewa, ila tu kwa na kupitia kwa Kristo. Tazama, yeye ni
uzima na mwangaza wa ulimwengu. Tazama, yeye ni neno la ukweli na haki.

10 Na sasa, vile umeanza kufundisha neno hata hivyo ningetaka kwamba uendelee
kufundisha; na ningetaka kwamba uwe na bidii na kiasi kwa vitu vyote.
11 Hakikisha kwamba hujiinui kwa kiburi; ndio, angalia kwamba hujisifu kwa
hekima yako mwenyewe, wala kwa nguvu yako nyingi.
12 Tumia ujasiri, lakini usiwe mjeuri; na pia uone kwamba ujifunze kuzuia tamaa
zako zote, ili uweze kujazwa na mapenzi; hakikisha kwamba uepuke kutokana na
uvivu—
13 Usiombe vile Wazoramu wanavyofanya, kwani umeona kwamba wanaomba
kuonekana na watu, na kusifiwa kwa hekima yao.
14 Usiseme: Ee Mungu, ninakushukuru kwamba tu wema kuliko ndugu zetu; lakini
afadhali useme: Ee Bwana, unisamehe kwa kutokuwa na haki kwangu, na
ukumbuke ndugu zangu kwa huruma—ndio, kubali kutokuwa na haki kwako
mbele ya Mungu wakati wote.
15 Na Bwana aibariki roho yako, na akupokee katika siku ya mwisho ndani ya
ufalme wake, kuketi chini kwa amani. Sasa nenda, mwana wangu, na ufunze neno
kwa hawa watu. Uwe na busara. Mwana wangu, kwaheri.

*Amri za Alma kwa mwana wake Koriantoni.*

# Alma 39

1 Na sasa, mwana wangu, nina vitu vingi zaidi kukuzungumzia kuliko yale
niliyomzungumzia kaka yako; kwani tazama, hujachunguza unyofu wa kaka yako,
uaminifu wake, na bidii yake kwa kutii amri za Mungu? Tazama, si yeye amekupatia
mfano mzuri?
2 Kwani hukutii maneno yangu vile kaka yako alivyofanya, miongoni mwa watu
wa Wazoramu. Sasa hii ndiyo ninayo dhidi yako; uliendelea kujivuna kwa sababu ya
nguvu yako na hekima yako.
3 Na hii siyo yote, mwana wangu. Ulifanya yale ambayo yalikuwa ya kusikitisha
kwangu; kwani uliacha huduma, na ukaenda kwenye nchi ya Sironi ndani ya mipaka
na nchi ya Walamani, kumtafuta kahaba Isabeli.
4 Ndio, aliiba mioyo ya wengi; lakini hii sio kisingizio kwako, mwana wangu.
Ungeendelea kuhudumu pale ambapo uliaminiwa.
5 Hujui, mwana wangu, kwamba vitu hivi ni machukizo machoni mwa Bwana;
ndio, ni machukizo kuliko dhambi zote isipokuwa ile ya kumwaga damu ya wale
wasio na hatia au kumkana Roho Mtakatifu?
6 Kwani tazama, ikiwa utamkana Roho Mtakatifu wakati imekuwa ndani yako, na
unajua kwamba unaikana, tazama, hii ni dhambi ambayo haiwezi kusamehewa;
ndio, na yeyote auaye dhidi ya mwangaza na taarifa ya Mungu, si rahisi kwake
kupata msamaha; ndio, nasema kwako, mwana wangu, kwamba si rahisi kwake
kupata msamaha.
7 Na sasa, mwana wangu, ningemsihi Mungu kwamba hungekuwa na hatia ya kosa
kubwa hivyo. Singetaka kuendelea kukuzungumzia makosa yako, na kuumiza roho
yako, kama haingekuwa kwa faida yako.
8 Lakini tazama, huwezi kuficha makosa yako kwa Mungu; na isipokuwa utubu
zitakuwa ushahidi dhidi yako katika siku ya mwisho.

9 Sasa mwana wangu, ningetaka kwamba utubu na kusahau dhambi zako, na
usiende tena kupendeza tamaa ya macho yako, lakini ujikataze mwenyewe kwa vitu
hivi vyote; kwani usipofanya hii huwezi kwa vyovyote kurithi ufalme wa Mungu.
Ee, kumbuka, na ujichukulie juu yako, na ujikatishe mwenyewe katika vitu hivi.
10 Na nina kuamuru ujichukulie kushauriana na kaka zako wakubwa katika
shughuli zako; kwani tazama, wewe ungali ndani ya ujana wako, na unahitaji
kulishwa na kaka zako. Na kusikiliza ushauri wao.
11 Usiamini kudanganywa na kitu kilicho bure na cha kipumbavu; usikubali ibilisi
apoteze moyo wako kufuata hao makahaba waovu. Tazama, Ee mwana wangu, ni
jinsi gani uovu mkuu uliwaletea Wazoramu; kwani wakati walipoona mwenendo
wako hawakuamini maneno yangu.
12 Na sasa Roho wa Bwana huniambia mimi: Amuru watoto wako watende mema,
la sivyo wataongoza mioyo ya wengi kwenye maangamizo; kwa hivyo nakuamuru,
wewe mwana wangu, kwa heshima ya Mungu, kwamba ujiepushe kutoka uovu
wako;
13 Kwamba umtazamie Bwana na akili, nguvu, na uwezo wako wote; kwamba
usipoteze mioyo ya watu mara nyingine kwa uovu; lakini urudi kwao, na kukiri
makosa yako na ule ubaya ambao umetenda.
14 Usitafute utajiri wala vitu visivyo vya maana vya ulimwengu huu; kwani tazama,
hutavibeba wakati wa kifo.
15 Na sasa, mwana wangu, ningesema machache kwako kuhusu kuja kwa Kristo.
Tazama, nakwambia, kwamba ni yeye kwa kweli atakayekuja kutoa dhambi za
ulimwengu; ndio, anakuja kutangaza habari njema ya wokovu kwa watu wake.
16 Na sasa, mwana wangu, hii ndiyo huduma ambayo uliitiwa, kutangaza hizi
habari njema kwa watu hawa, kutayarisha akili zao; kwa usahihi zaidi afadhali
kwamba wokovu uwajie, kwamba watayarishe akili za watoto wao kusikiliza neno
wakati wa kuja kwake.
17 Na sasa nitatuliza kidogo akili yako kwa hili jambo. Tazama, unashangaa kwa
nini hivi vitu vijulikane mbele. Tazama, nakwambia, si roho wakati huu ina thamani
kwa Mungu vile roho itakuwa wakati wa kuja kwake?
18 Si ni lazima mpango wa ukombozi ufunuliwe watu hawa na watoto wao pia?
19 Je, si ni rahisi wakati huu kwa Bwana kutuma malaika wake kututangazia habari
hii njema kama vile kwa watoto wetu, au kama vile baada ya kuja kwake?

## Alma 40

1 Sasa mwana wangu, hapa nina mengine mengi ningependa kukwambia; kwani
nafikiria kwamba akili yako ina wasiwasi kuhusu ufufuo wa wafu.
2 Tazama, nakwambia, kwamba hakuna ufufuo — au, ningesema, kwa maneno
mengine kwamba mwili wenye kufa haujiviki kutokufa, ya uharibifu haijiviki
kutoharibika — mpaka baada ya kuja kwa Kristo.
3 Tazama, anawezesha ufufuo wa waliokufa kutendeka. Lakini tazama, mwana
wangu, ufufuo haujatimizwa bado. Sasa, nafichua kwako siri; walakini, kuna siri
nyingi ambazo zimefichwa, ambazo hakuna azijuaye isipokuwa Mungu mwenyewe.
Lakini ninakuonyesha kitu kimoja ambacho nimemwuliza Mungu kwa bidii ili
nipate kujua — ambayo inahusu ufufuo.
4 Tazama, kuna wakati ambao umewekwa kwamba wote watatokea kutoka wafu.

Sasa wakati huu utakapotimia hakuna ajuaye; lakini Mungu anajua wakati ambao
umewekwa.
5 Sasa, kama kutakuwa wakati mmoja, au wakati wa pili, au wakati wa tatu,
kwamba wafu watafufuka kutoka kwa wafu, haijalishi; kwani Mungu anajua hivi
vitu vyote; na ninatosheka kujua kwamba hii ndiyo hali — kwamba kuna wakati
ambao umechaguliwa kwamba wote watafufuka kutoka kwa wafu.
6 Sasa lazima kuwe na nafasi kati ya wakati wa kifo na wakati wa kufufuka.
7 Na sasa nitakuuliza ni nini kitatokea kwa roho za binadamu kutoka wakati huu
wa kifo hadi wakati uliowekwa wa kufufuka?
8 Sasa kama kutakuwa na zaidi ya wakati moja ambao umewekwa kwa watu
kuamka haijalishi; kwani wote hawafi wakati mmoja, na hii haijalishi; wakati wote
ni kama siku moja kwake Mungu, na wakati hupimwa tu na watu.
9 Kwa hivyo, kuna wakati ambao umewekewa watu kwamba wataamka kutoka kwa
wafu; na kuna nafasi kati ya wakati wa kifo na ufufuo. Na sasa, kuhusu nafasi hii ya
muda, kitakachotokea kwa roho za watu ni kitu ambacho nimeuliza kwa bidii kwa
Bwana nijue; ni hiki ndicho kitu ninachojua.
10 Na wakati majira yatapofika wakati wote wataamka, ndipo watakapojua kwamba
Mungu anajua wakati wote ambao amewekewa mtu.
11 Sasa, kuhusu hali ya roho kati ya kifo na ufufuo — Tazama, nimejulishwa na
malaika, kwamba roho za watu wote, mara zinapotoka kwa mwili huu wa muda,
ndio, roho za watu wote, zikiwa njema au ovu, zinachukuliwa nyumbani kwa yule
Mungu ambaye alizipatia uhai.
12 Na ndipo itakuja kuwa kwamba roho za wale walio haki zinapokelewa kwa hali
ambayo ni ya furaha, ambayo inaitwa peponi, hali ya kupumzika, hali ya amani,
ambapo zitapumzikia kutoka kwa taabu zao zote na kutoka kwa mashaka yote, na
masikitiko.
13 Na ndipo itakuwa kwamba, zile roho za waovu, ndio, ambazo ni ovu — kwani
tazama, hazina kipande au sehemu ya Roho wa Bwana; kwani tazama, walichagua
kazi mbovu badala ya nzuri; kwa hivyo roho wa ibilisi aliingia ndani yao, na
akamiliki nyumba yao — na hawa watatupwa nje gizani; kutakuwa na kulia, na
kuomboleza, na kusaga meno, na hii ni kwa sababu ya uovu wao, wakiongozwa
kifungoni kwa nia ya ibilisi.
14 Sasa hii ni hali ya roho ya waovu, ndio, kwenye giza, na kwa hali ya kutisha, na
kuogopesha wakitarajia hasira na uchungu wa ghadhabu ya Mungu juu yao; hivyo
wanabaki kwenye hali hii, na vile vile walio wenye haki huko peponi, hadi wakati
wao wa ufufuko.
15 Sasa, kuna wachache ambao wanaelewa kwamba hii hali ya furaha na hii hali ya
taabu ya roho, kabla ya ufufuo, ilikuwa na ufufuo wa kwanza. Ndio, nakubali
inaweza kuitwa ufufuo, kuamka kwa roho au nafsi na upatanisho kwa furaha au
taabu, kulingana na maneno yaliyozungumzwa.
16 Na tazama, imezungumziwa tena, kwamba kuna ufufuo wa kwanza, au ufufuo
wa wale ambao wamekwisha kuwepo, au ambao wako, au watakaokuwa, hadi ufufuo
wa Kristo kutoka kwa wafu.
17 Sasa, hatuwezi kudhani kwamba huu ufufuo wa kwanza, ambao
umezungumziwa kwa njia hii, unaweza kuwa ufufuo wa roho na upatanisho wao
kwa furaha au taabu. Huwezi kudhani kwamba hii ndiyo inamaanisha.
18 Tazama, nakwambia, Hapana; lakini inaamanisha kuunganisha roho na mwili,

kwa wale kutoka siku za Adamu hadi kwa ufufuo wa Kristo.
19 Sasa, kama roho na miili ya wale ambao wamezungumziwa itaunganishwa yote
mara moja, waovu sawa na wenye haki, sisemi; ni ya kutosha kwangu kusema
kwamba, wote watainuka; au kwa njia nyingine, ufufuko wao utakuja kupita kabla
ya ufufuko wa wale ambao hufa baada ya kufufuka kwa Kristo.
20 Sasa, mwana wangu, sisemi kwamba ufufuko huja wakati wa kufufuka kwa
Kristo; lakini tazama, ninatoa kama maoni yangu, kwamba roho na miili
zitaunganishwa, za wale wenye haki, katika ufufuko wa Kristo, na kupaa kwake
mbinguni.
21 Lakini kama itakuwa wakati wa ufufuko wake au ya baadaye, sisemi; lakini hii
yote nasema, kwamba kuna nafasi kati ya kifo na ufufuko wa mwili, na hali ya roho
ndani ya furaha au shida mpaka wakati ambao umechaguliwa na Mungu kwamba
wafu wataamka, na kuunganishwa, vyote roho na mwili, na kuletwa na kusimama
mbele ya Mungu, na kuhukumiwa kulingana na vitendo vyao.
22 Ndio, hii italeta kurudishwa kwa vitu ambavyo vimezungumziwa na midomo ya
manabii.
23 Roho itarudishwa kwa mwili, na mwili kwa roho; ndio, na kila sehemu na kiungo
kitarudishwa kwa mwili wake; ndio, hata nywele ya kichwa haitapotea; lakini vitu
vyote vitarudishwa kwa umbo lao sahihi na kamilifu.
24 Na sasa, mwana wangu, huku ni kurudisha ambako kumezungumzwa na
midomo ya manabii—
25 Na ndipo wale wenye haki wataang'aa ndani ya ufalme wa Mungu.
26 Lakini tazama, kifo cha kutisha kitawajia waovu; kwani wanakufa kulingana na
vitu vilivyo vya haki; kwani hawako safi, na hakuna kitu kichafu kitakachorithi
ufalme wa Mungu; lakini watatupwa nje, na kutolewa kupokea matunda ya vitendo
vyao au kazi zao, ambazo zimekuwa mbovu; na wanakunywa machicha ya kikombe
kikali.

## Alma 41

1 Na sasa, mwana wangu, nina machache ya kusema kuhusu ufufuko ambao
umezungumziwa; kwani tazama, wengine wamegeuza maandiko, na wamepotelea
mbali kwa sababu ya kitu hiki. Na ninaona kwamba akili yako imekuwa na wasiwasi
kuhusu kitu hiki. Lakini tazama, nitakuelezea.
2 Ninakwambia, mwana wangu, kwamba mpango wa ufufuo ni wa lazima na haki
ya Mungu; kwani ni lazima kwamba vitu vyote virudishwe kwa kanuni zao. Tazama,
ni lazima na haki, kulingana na uwezo wa kufufuka kwa Kristo, kwamba roho ya kila
mtu irudishwe kwa mwili wake, na kila sehemu ya mwili sharti irudishwe vile
ilivyokuwa.
3 Na ni lazima na haki ya Mungu kwamba binadamu wahukumiwe kulingana na
vitendo vyao; na ikiwa vitendo vyao vilikuwa vizuri kwenye maisha haya, na nia za
mioyo yao zilikuwa nzuri, ndipo pia itakuwa kwa siku ya mwisho, itarudishwa kwa
ile ambayo ni nzuri.
4 Na ikiwa vitendo vyao ni viovu watarudishiwa uovu. Kwa hivyo, vitu vyote
vitarudishwa kwa kanuni zao, kila kitu kwa asili ya umbo lake—mwili wenye kufa
utafufuliwa katika kutokufa, vilivyoharibika kwa visivyo haribika—vikiinuliwa
kwenye furaha isiyo na mwisho kurithi ufalme wa Mungu, au taabu isiyo ya mwisho

kurithi ufalme wa ibilisi, moja kwa upande mmoja, na mwingine kwa upande mwingine—

5 Mmoja ameinuliwa kwenye furaha kulingana na nia yake ya furaha, au uzuri kulingana na mahitaji yake ya uzuri; na mwingine kwenye ubaya kulingana na nia yake ya ubaya; kwani vile ametamani kutenda maovu siku yote hata hivyo atapata zawadi yake ya uovu wakati usiku utakapoingia.

6 Na hivyo iko kwenye upande mwingine. Ikiwa ametubu dhambi zake, na kuhitaji haki mpaka mwisho wa siku zake, hata hivyo atapata zawadi kwa haki.

7 Hawa ni watu ambao wamekombolewa na Bwana; ndio, hawa ndio wao ambao wametolewa nje, ambao wameokolewa kutoka kwa ule usiku wa giza la milele; na hivyo wanasimama au kuanguka; kwani tazama, wanajihukumu wenyewe, kama watafanya mazuri au maovu.

8 Sasa, maagizo ya Mungu hayabadiliki; kwa hivyo, njia imeandaliwa kwamba yeyote atakaye angetembea juu yake na kuokolewa.

9 Na sasa tazama, mwana wangu, usijihatarishe na kosa lingine moja zaidi dhidi ya Mungu juu ya yale mambo ya mafundisho, ambayo wewe umejihatarisha sasa kwa kutenda dhambi.

10 Usidhani, kwa sababu imezungumzwa kuhusu ufufuo, kwamba utarudishwa kutoka kwenye dhambi hadi kwenye furaha. Tazama, nakwambia, uovu haujapata kuwa furaha.

11 Na sasa, mwana wangu, watu wote ambao wako kwa hali ya asili, au ningesema, kwenye hali ya kimwili, wako kwenye masumbuko ya uchungu na kwenye kifungo cha uovu; hawako na Mungu duniani, na wameenda kinyume cha asili ya Mungu; kwa hivyo, wako kwa hali ya kinyume cha furaha.

12 Na sasa tazama, je, maana ya neno kurudisha ni kuchukua kitu cha hali ya asili na kukiweka kwenye hali isiyo asili, au kukiweka katika hali kinyume cha asili yake?

13 Ee, mwana wangu, hili silo jambo; lakini maana ya neno kurudisha ni kurejesha tena uovu kwa uovu, au mwili kwa mwili, au uibilisi kwa uibilisi—uzuri kwa lile ambalo ni zuri; haki kwa kile ambacho ni haki; adilifu kwa kile ambacho ni adilifu; rehema kwa lile ambalo lina rehema.

14 Kwa hivyo, mwana wangu, ona kwamba unawarehemu ndugu zako; tenda yaliyo mazuri, toa hukumu kwa haki, na ufanye mema kila mara; na ikiwa utafanya vitu hivi vyote ndipo utakapopokea zawadi yako; ndio, utapata rehema irudishwe kwako tena; utapata haki kurudishwa kwako tena; utapata hukumu ya haki kurudishwa kwako tena; na utapata zawadi nzuri kutolewa kwako tena.

15 Kwani yale ambayo unapeyaleka nje yatarudi kwako tena, na kurudishwa kwenye asili yake tena; kwa hivyo, neno kurudisha humhukumu mwenye dhambi, na haimthibitishi hata kidogo.

## Alma 42

1 Na sasa, mwana wangu, naona kuna kitu kidogo zaidi ambacho kinakusumbua akili yako, ambacho huwezi kuelewa—ambacho kinahusu unyoofu wa Mungu kwa kuadhibu wenye dhambi; kwani unajaribu kudhani kwamba si haki kwamba wenye dhambi watupiliwe kwenye hali ya taabu.

2 Sasa tazama, mwana wangu, nitakuelezea hiki kitu. Kwani tazama, baada ya Bwana Mungu kutuma wazazi wetu wa kwanza kutoka kwenye bustani ya Edeni,

kulima ardhi, kutoka ambapo walipelekwa — ndio, alimfukuza huyo mtu, na
akaweka makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto
uliogeuka huku na huko, kulinda mti wa uzima —
3 Sasa, tunaona kwamba yule mtu alikuwa kama Mungu, akijua wema na uovu; na
ili asinyooshe mkono wake mbele, na achukue pia kwa mti wa uzima, na kula na
kuishi milele, Bwana Mungu aliweka makerubi na upanga wa moto, ili asile tunda —
4 Na hivyo tunaona, kwamba kulikuwa na wakati ambao uliwekewa mwanadamu
kutubu, ndio, wakati wa majaribio, wakati wa kutubu na kumtumikia Mungu.
5 Kwani tazama, kama Adamu angenyoosha mkono wake haraka, na kula kutoka
kwa mti wa uzima, angeishi milele, kulingana na neno la Mungu, kukiwa hakuna
nafasi ya toba; ndio, na pia neno la Mungu lingekuwa bure, na mpango mkuu wa
wokovu ungezuiliwa.
6 Lakini tazama, ilipangiwa mwanadamu kufa — kwa hivyo, vile walitolewa mbali
kutoka kwa mti wa uzima wangetolewa mbali kutoka uso wa dunia — na
mwanadamu alipotea milele, ndio, binadamu wakaanguka.
7 Na sasa, kwa hii unaona kwamba wazazi wetu wa kwanza walitolewa mbali yote
kimwili na kiroho kutoka kwa uwepo wa Bwana; na hivyo tunaona wakawa raia wa
kufuata kusudi lao.
8 Sasa tazama, haikuwa ya kufaa kwamba mwanadamu arudishwe kutoka kwa kifo
chake cha mwili, kwani hiyo ingeangamiza mpango mkuu wa furaha.
9 Kwa hivyo, vile roho haingekufa, na mwanguko ulikuwa umeleta kwa wanadamu
wote kifo cha roho na pia cha mwili, inaamanisha, walitolewa mbali na uwepo wa
Bwana, ilikuwa ni lazima kwamba mwanadamu arudishwe kutoka kwenye kifo cha
roho.
10 Kwa hivyo, tangu walipokuwa wamekuwa na tamaa za kimwili, uasherati, na
uibilisi, kwa asili, hii hali ya majaribio ilikuwa hali ya wao kujitayarisha; ikawa hali ya
matayarisho.
11 Na sasa kumbuka, mwana wangu, kama haungekuwa mpango wa ukombozi,
(kuwekwa kando) upesi vile walikufa roho zao zilikuwa taabuni, ikiwa imetolewa
kutoka kwa uwepo wa Bwana.
12 Na sasa, hapakuwa na njia ya kudai wanadamu kutoka hali hii ya kuanguka,
ambayo mwanadamu alijiletea kwa sababu ya kutotii kwake;
13 Kwa hivyo, kulingana na haki, mpango wa ukombozi haungeletwa, tu kwa tabia
ya toba ya wanadamu katika hali hii ya majaribio, ndio, hali hii ya kujitayarisha;
kwani isingekuwa masharti haya, rehema haingefaa isipokuwa iangamize kazi ya
haki. Sasa kazi ya haki haiengeangamizwa; ikiwa hivyo, Mungu angekoma kuwa
Mungu.
14 Na hivyo tunaona kwamba binadamu wote walianguka, na wakawa wameshikwa
na haki; ndio, haki ya Mungu ambayo amewatolea milele watolewe kwenye uwepo
wake.
15 Na sasa, mpango wa rehema haungetimizwa isipokuwa upatanisho ufanywe; kwa
hivyo Mungu mwenyewe hulipia dhambi za ulimwengu, kutimiza mpango wa
rehema, kuwezesha mahitaji ya haki, kwamba Mungu angekuwa mkamilifu, na
Mungu mwenye haki, na Mungu wa huruma pia.
16 Sasa, toba haingewajia watu isipokuwa kuwe na adhabu, ambayo pia ilikuwa ya
milele vile uhai wa roho ulivyo, umepandikishwa kinyume cha mpango wa furaha,
ambao ulikuwa milele vile uhai wa roho ulivyo.

17 Sasa, mtu anaweza kutubu namna gani isipokuwa atende dhambi? Ni vipi angetenda dhambi ikiwa hakukuweko na sheria? Kungekuwaje sheria kusipokuwa na adhabu?

18 Sasa, kulikuwa na adhabu iliyopandikwa, na sheria ya haki ikatolewa, ambayo ilileta majuto ya dhamiri kwa watu.

19 Sasa, kama sheria haingetolewa—ikiwa mtu ataua sharti auawe—je, angeogopa kwamba angekufa ikiwa angeua?

20 Na pia, kama hakungekuwa sheria kutolewa dhidi ya dhambi watu hawangeogopa kutenda dhambi.

21 Na kama sheria haingetolewa, wakati watu wanatenda dhambi, haki ingefanya nini au rehema, kwani hawangekuwa na madai juu ya kiumbe?

22 Lakini sheria imetolewa, na adhabu kuwekwa, na toba kukubaliwa; toba ambayo, rehema hudai; la sivyo, kazi ya haki ingedai kiumbe na kutimiza sheria, na sheria kutoa adhabu; kama sio hivyo matendo ya haki yangeangamizwa, na Mungu kukoma kuwa Mungu.

23 Lakini Mungu hakomi kuwa Mungu, na rehema hudai wanaotubu, na rehema huja kwa sababu ya upatanisho; na upatanisho huleta ufufuo wa wafu; na ufufuo wa wafu huwarudisha watu kwenye uwepo wa Mungu; na hivyo wanarudishwa kwenye uwepo wake, kuhukumiwa kulingana na matendo yao, kulingana na sheria na haki.

24 Kwani tazama, haki hutekeleza madai yake yote, na pia huruma hudai yote yaliyo yake; na hivyo, hakuna ila tu waliotubu kwa ukweli watakaookolewa.

25 Ni nini, unadhani kwamba rehema inaweza kuibia haki? Ninakwambia, Hapana; hata chembe kimoja. Ikiwa hivyo, Mungu atakoma kuwa Mungu.

26 Na hivyo Mungu hutimiza kusudi lake kubwa na milele, ambalo lilitayarishwa kutokea msingi wa dunia. Na hivyo huja wokovu na ukombozi wa binadamu, na pia maangamizo yao na taabu.

27 Kwa hivyo, Ee mwana wangu, yeyote atakeyekuja angekuja na kunywa maji ya uzima bure; yeyote atakayekataa kuja hivyo hatashurutishwa kuja; lakini katika siku ya mwisho itarudishwa kwake kulingana na vitendo vyake.

28 Ikiwa anatamani kufanya uovu, na hajatubu katika siku zake, tazama, uovu utafanywa kwake, kulingana na kurudishwa kwa Mungu.

29 Na sasa, mwana wangu, nataka kwamba usiache vitu hivi vikusumbue mara nyingine, na ni dhambi zako tu zikusumbue, pamoja na taabu hiyo ambayo itakuleta wewe kwa toba.

30 Ee mwana wangu, nataka kwamba usikane haki ya Mungu mara nyingine. Usijaribu kujisamehe mwenyewe hata kwa njia ndogo kwa sababu ya dhambi zako, kwa kukataa haki ya Mungu; lakini uache haki ya Mungu, na rehema yake, na uvumilivu wake uvume ndani ya moyo wako; na acha ikulete chini kwenye mavumbi ndani ya unyenyekevu.

31 Na sasa, Ee mwana wangu, umeitwa na Mungu kuhubiri neno kwa hawa watu. Na sasa, mwana wangu, nenda njia zako, tangaza neno kwa ukweli na busara, kwamba uzilete roho kwenye toba, kwamba mpango mkuu wa rehema ungekuwa na madai juu yao. Na Mungu akupatie hata kulingana na maneno yangu. Amina.

# Alma 43

1 Na sasa ikawa kwamba wana wa Alma walikwenda miongoni mwa watu, kutangaza
neno kwao. Na Alma, pia, mwenyewe, hangepumzika, na yeye pia alienda mbele.
2 Sasa hatutazungumza mengi kuhusu kuhubiri, kwao isipokuwa kwamba
walihubiri neno, na ukweli, kulingana na roho ya unabii na ufunuo; na walihubiri
kulingana na mpango mtakatifu wa Mungu ambao waliitiwa.
3 Na sasa narudia historia ya vita miongoni mwa Wanefi na Walamani, katika
mwaka wa kumi na nane wa utawala wa waamuzi.
4 Kwani tazama, ikawa kwamba Wazoramu waligeuka na kuwa Walamani; kwa
hivyo, katika mwanzo wa mwaka wa kumi na nane watu wa Wanefi waliona kwamba
Walamani walikuwa wanataka kuwashambulia; kwa hivyo walijiandaa kwa vita;
ndio, walikusanya pamoja majeshi yao katika nchi ya Yershoni.
5 Na ikawa kwamba Walamani walikuja kwa maelfu; na wakaja katika nchi ya
Antionumu, ambayo ni nchi ya Wazoramu; ambamo mtu kwa jina la Zerahemna
alikuwa kiongozi.
6 Na sasa, kwa vile Waamaleki walikuwa watu waovu na wauaji kuliko Walamani
walivyokuwa, kwao wenyewe, kwa hivyo, Zerahemna aliteua makapteni wakuu juu
ya Walamani, na wote walikuwa Waamaleki na Wazoramu.
7 Sasa alifanya hivi ili kuhifadhi chuki yao kwa Wanefi, ili awamiliki na kutimiza
kusudi lake.
8 Kwani tazama, kusudi lake lilikuwa kuwavuruga Walamani wawe na hasira dhidi
ya Wanefi; alifanya hivi ili apate uwezo mwingi juu yao, na pia kwamba ajipatie
uwezo juu ya Wanefi kwa kuwaweka katika utumwa.
9 Na sasa kusudi la Wanefi lilikuwa kulinda nchi yao, na nyumba zao, na wake zao,
na watoto wao, ili wawaokoe kutoka kwa mikono ya maadui wao; na pia kwamba
wahifadhi haki zao na mapendeleo yao, ndio, na pia uhuru wao, kwamba wapate
kumwabudu Mungu kulingana na kutaka kwao.
10 Kwani walijua kwamba ikiwa wangeshikwa mateka na Walamani, kwamba yeyote
atakayemwabudu Mungu kwa roho na kwa ukweli, Mungu wa kweli na anayeishi
Walamani wangemwangamiza.
11 Ndio, na walijua pia ile chuki mbaya iliyokuweko ya Walamani kwa ndugu zao,
ambao walikuwa watu wa Anti-Nefi-Lehi, ambao waliitwa watu wa Amoni — na
hawengechukua silaha, ndio, walikuwa wamefanya agano ambalo
hawangevunja — kwa hivyo, kama wangeanguka kwenye mikono ya Walamani
wangeangamizwa.
12 Na Wanefi hawangekubali kwamba waangamizwe; kwa hivyo waliwakabidhi
nchi kwa kumiliki.
13 Na watu wa Amoni walitoa sehemu kubwa ya mali yao kwa Wanefi kusaidia
majeshi yao; na hivyo Wanefi walilazimishwa, kusimama, pekee yao, dhidi ya
Walamani, ambao walikuwa muungano wa Lamani na Lemueli, na wana wa
Ishmaeli, na wale wote ambao hawakukubaliana na Wanefi, ambao walikuwa ni
Waamaleki na Wazoramu, na uzao wa makuhani wa Nuhu.
14 Sasa vile vizazi vilikuwa vingi, karibu kama vile Wanefi walivyokuwa; na hivyo
Wanefi walilazimishwa kupigana na ndugu zao, hata kwa kumwaga damu.
15 Na ikawa wakati majeshi ya Walamani yalipokuwa yamejikusanya pamoja katika
nchi ya Antionumu, tazama, majeshi ya Wanefi yalikuwa yamejiandaa kukabiliana
nao katika nchi ya Yershoni.

16 Sasa, kiongozi wa Wanefi, au mtu ambaye alichaguliwa kuwa kapteni mkuu juu
ya Wanefi — sasa kapteni mkuu alichukua jukumu la kuamrisha majeshi yote ya
Wanefi — na jina lake lilikuwa Moroni;
17 Na Moroni alijitwalia amri yote, na utawala wa vita vyao. Na alikuwa na umri wa
miaka ishirini na tano tu alipochaguliwa kuwa kapteni mkuu juu ya majeshi ya
Wanefi.
18 Na ikawa kwamba alikabiliana na Walamani kwenye mipaka ya Yershoni, na
watu wake walijihami na panga, na vitara, na kila aina ya silaha za vita.
19 Na wakati majeshi ya Walamani yalipoona kwamba watu wa Nefi, au kwamba
Moroni, ameandaa watu wake kwa dirii na ngao za vita, ndio, na pia ngao za
kujikinga vichwa, na pia kuwa walikuwa wamevaa mavazi mazito —
20 Sasa jeshi la Zerahemna halikuwa limejitayarisha kwa kitu cha aina hii; walikuwa
tu na panga zao na vitara vyao, pinde zao na mishale yao, mawe yao na kombeo zao;
na walikuwa uchi, isipokuwa tu ngozi iliyofunika viuno vyao; ndio, wote walikuwa
uchi, isipokuwa Wazoramu na Waamaleki;
21 Lakini hawakuwa wamejihami dirii, wala ngao — kwa hivyo, waliogopa sana
majeshi ya Wanefi kwa sababu ya silaha zao, ingawaje idadi yao ilikuwa kubwa mno
kuliko ya Wanefi.
22 Tazama, sasa ikawa kwamba hawakuthubutu kuwashambulia Wanefi kwenye
mipaka ya Yershoni; kwa hivyo waliondoka nje ya nchi ya Antionumu hadi kwenye
nyika, na kusafiri wakizingira nyika, mbali na chimbuko la mto Sidoni, ili waingie
katika nchi ya Manti na kuimiliki nchi; kwani hawakutarajia kwamba majeshi ya
Moroni yangejua kule walikokwenda.
23 Lakini ikawa kuwa, walipoondoka kuelekea nyikani Moroni alituma wapelelezi
nyikani kuchunguza kituo chao; na Moroni, pia, akiwa anaelewa unabii wa Alma,
akatuma watu kwake, akitamani kwamba amwulize Bwana wapi majeshi ya Wanefi
yangeenda kujikinga dhidi ya Walamani.
24 Na ikawa kwamba neno la Bwana lilimjia Alma, na Alma akawajulisha wajumbe
wa Moroni, kwamba majeshi ya Walamani yalikuwa yameenda taratibu yakizunguka
nyikani, ili yaingie kwenye nchi ya Manti, ili yaanzishe vita mahali ambapo watu
walipungukiwa na nguvu. Na wale wajumbe walienda na kufikisha ujumbe kwa
Moroni.
25 Sasa Moroni, akiacha sehemu ya jeshi lake katika nchi ya Yershoni, isiwe kwa
vyovyote kwamba sehemu ya Walamani ije katika nchi hiyo na kumiliki mji,
alichukua jeshi lililosalia na akaenda kwenye nchi ya Manti.
26 Na alisababisha kwamba watu wote katika sehemu hiyo wajikusanye wenyewe
pamoja kukabiliana dhidi ya Walamani, kulinda ardhi yao na nchi yao, haki zao na
uhuru wao; kwa hivyo walijiandaa dhidi ya ule wakati ambao Walamani wangekuja.
27 Na ikawa kwamba Moroni alisababisha kwamba jeshi lake lijifiche kwenye bonde
ambalo lilikuwa karibu na ufuko wa mto Sidoni, ambao ulikuwa magharibi mwa
mto Sidoni katika nyika.
28 Na Moroni aliweka wapelelezi kila mahali, ili angejua wakati kituo cha Walamani
kitakuja.
29 Na sasa, kwa vile Moroni alijua nia ya Walamani, kwamba ilikuwa nia yao
kuangamiza ndugu zao, au kuwaweka chini yao na kuwafanya watumwa ili
waanzishe utawala wao nchini kote;
30 Na pia akijua kwamba ilikuwa nia ya pekee ya Wanefi kuhifadhi nchi yao, na

uhuru wao, na kanisa lao, kwa hivyo hakufikiri ni dhambi kuwalinda kwa werevu;
kwa hivyo, aligundua kupitia kwa wapelelezi wake njia ambayo Walamani watafuata.
31 Kwa hivyo, aligawanya jeshi lake na kuleta sehemu moja kwenye bonde, na
akawaficha mashariki, na kusini mwa mlima Ripla;
32 Na waliosalia aliwaficha kwenye bonde la magharibi, magharibi mwa mto Sidoni,
na hivyo chini hadi kwenye mipaka ya nchi ya Manti.
33 Na hivyo akiwa ameweka jeshi lake kulingana na mipango yake, alikuwa tayari
kukabiliana nao.
34 Na ikawa kwamba Walamani walikuja juu kaskazini mwa mlima, ambapo
sehemu ya jeshi la Moroni ilijificha.
35 Na vile Walamani walikuwa wamepita mlima Ripla, na wakaja ndani ya bonde,
na wakaanza kuvuka mto Sidoni, jeshi ambalo lilikuwa limefichwa kusini mwa
mlima, ambalo liliongozwa na mtu ambaye jina lake lilikuwa Lehi, na akaongoza
jeshi lake mbele na kuzingira Walamani mashariki nyuma yao.
36 Na ikawa kwamba Walamani, wakati walipoona Wanefi wakiwajia kutoka nyuma
yao, waligeuka na kuanza kukabiliana na jeshi la Lehi.
37 Na kazi ya mauaji ilianza pande zote mbili, lakini ilikuwa ya kutisha zaidi kwa
upande wa Walamani, kwani uchi wao ulijidhihirisha kwa mapigo makubwa ya
Wanefi kwa panga zao na vitara vyao, ambavyo vilileta vifo karibu kwa kila pigo.
38 Wakati kwa upande mwingine, kulikuwa na mtu mmoja hapa na pale akiuawa
miongoni mwa Wanefi, kwa panga zao na kwa kupoteza damu, hawa wakiwa
wemejikinga sehemu muhimu za mwili, au sehemu muhimu za mwili zikikingwa
kutoka na mapigo ya Walamani, kwa dirii zao, na ngao zao za mikono, na vyapeo
vyao; na hivyo Wanefi waliendelea na kazi ya mauaji miongoni mwa Walamani.
39 Na ikawa kwamba Walamani waliogopa, kwa sababu ya uharibifu mkuu
miongoni mwao, hata mpaka wakaanza kutoroka kuelekea mto Sidoni.
40 Na walifuatwa na Lehi na watu wake; na walikimbizwa na Lehi hadi kwenye maji
ya Sidoni, na wakavuka maji ya Sidoni. Na Lehi aliweka majeshi yake kwenye
ukingo wa mto Sidoni kwamba wasivuke.
41 Na ikawa kwamba Moroni na jeshi lake walikabiliana na Walamani kwenye
bonde, kwa upande mwingine wa mto Sidoni, na wakaanza kuwaangukia na
kuwauwa.
42 Na Walamani wakakimbia kutoka kwao, kuelekea nchi ya Manti; na wakakutana
tena na majeshi ya Moroni.
43 Sasa kwa hali hii Walamani walipigana sana; ndio, hakujakuwa na wakati
Walamani wamejulikana kwa kupigana kwa nguvu kama hii na ujasiri, la, sio hata
kutoka mwanzoni.
44 Na walititiwa moyo na Wazoramu na Waamaleki, ambao walikuwa makapteni wao
wakuu na viongozi, na Zerahemna, ambaye alikuwa kapteni wao mkuu, au kiongozi
wao mkuu na amri jeshi; ndio, walipigana kama majoka yenye, na wengi wa Wanefi
waliuawa kwa mikono yao, ndio, kwani walipasua kwa vipande viwili vyapeo vyao,
na wakatoboa dirii zao nyingi, na wakakata mikono yao; na hivyo Walamani
walikata kwa hasira yao nyingi.
45 Walakini, Wanefi waliongozwa na sababu njema, kwani hawakuwa wanapigania
utawala wala uwezo lakini walipigania maskani yao na uhuru wao, wake zao na
watoto wao, na vyote vyao, ndio, kwa kanuni zao za kuabudu na kanisa lao.
46 Na walifanya hayo ambayo walifikiri ni jukumu ambalo waliwiwa Mungu wao;

kwani Bwana alikuwa amewaambia, na pia kwa babu zao, kwamba: Kwa kuwa
hamna hatia kwa kosa la kwanza, wala la pili, hamtakubali wenyewe kuuawa kwa
mikono ya maadui wenu.
47 Na tena Bwana, amesema kwamba: Mtalinda jamaa zenu hata kwa umwagaji wa
damu. Kwa hivyo kwa sababu hii Wanefi walikuwa wakipigana na Walamani,
kujilinda wenyewe, na jamaa zao, na nchi yao, na haki zao, na dini yao.
48 Na ikawa kwamba watu wa Moroni walipoona ukali na hasira ya Walamani,
walikuwa karibu kurudi nyuma na kutoroka kutoka kwao. Na Moroni akiona
kusudi lao, alituma ujumbe mbele na akavuta mioyo yao kwa mawazo haya — ndio,
mawazo ya nchi yao, uhuru wao, ndio, uhuru wao kutoka utumwani.
49 Na ikawa kwamba waliwashambulia Walamani, na wakapaza sauti pamoja kwa
Bwana Mungu wao, kwa ungwana wao na uhuru wao kutoka utumwani.
50 Na wakaanza kusimama dhidi ya Walamani kwa nguvu; na kwenye ile saa
yenyewe kwamba walimlilia Bwana kwa uhuru wao, Walamani walianza kukimbia
kutoka kwao; na wakakimbia hata kwenye maji ya Sidoni.
51 Sasa Walamani walikuwa wengi zaidi, ndio, zaidi ya mara mbili kuliko idadi ya
Wanefi; walakini, walikimbizwa sana kwamba wakajikusanya kwa kundi moja katika
bonde, kando ya mto Sidoni.
52 Kwa hivyo majeshi ya Moroni yaliwazingira, ndio, hata pande zote mbili za mto,
kwani tazama, kwa upande wa mashariki kulikuwa na watu wa Lehi.
53 Kwa hivyo wakati Zerahemna alipoona watu wa Lehi upande wa mashariki wa
mto Sidoni, na majeshi ya Moroni upande wa magharibi wa mto Sidoni, kwamba
walikuwa wamezingirwa na Wanefi, walishikwa na woga.
54 Sasa Moroni, alipoona woga wao, aliamuru watu wake waache kumwaga damu
yao.

## Alma 44

1 Na ikawa kwamba waliacha na wakarudi nyuma hatua kutoka kwao. Na Moroni
akamwambia Zerahemna: Tazama, Zerahemna, kwamba hatutamani kuwa watu wa
damu. Unajua kwamba mko mikononi mwetu, na bado hatutaki kuwaua.
2 Tazama, hatukuja nje kupigana dhidi yenu ili tumwage damu yenu kwa nguvu;
wala hatutaki kumweka yeyote kwenye nira ya kifungo. Lakini hii ndiyo sababu
ambayo imewasababisha nyinyi kutujia sisi; ndio, na mmekasirika nasi kwa sababu
ya dini yetu.
3 Lakini sasa, unaona kwamba Bwana yuko pamoja nasi; na unaona kwamba
amewakabidhi nyinyi mikononi mwetu. Na sasa nataka wewe ujue kwamba hii
imefanywa kwetu kwa sababu ya dini yetu na imani katika Kristo. Na sasa mnaona
kwamba hamwezi kuiangamiza hii imani yetu.
4 Sasa unaona kwamba hii ni imani ya kweli ya Mungu; ndio, unaona kwamba
Mungu atatusaidia, na kutuweka, na kutuhifadhi, kadiri tuwe waaminifu kwake, na
kwa imani yetu, na dini yetu; na kamwe Bwana hatakubali kwamba tuangamizwe
isipokuwa tuanze kufanya makosa na kukana imani yetu.
5 Na sasa, Zerahemna, nakuamuru, kwa jina la Mungu aliye na uwezo wote,
ambaye ameimarisha mikono yetu kwamba tumepata uwezo juu yenu, kupitia imani
yetu, kwa dini yetu, kwa kanuni zetu za kuabudu, na kwa kanisa letu, na kwa kazi
yetu takatifu ya kusaidia wake zetu na watoto wetu, na kwa ule uhuru ambao

unatuunganisha sisi kwa ardhi zetu na nchi yetu; ndio, na pia kwa kushikilia neno takatifu la Mungu, ambalo kwake tunawiwa furaha yetu; na kwa yote yaliyo muhimu kwetu—

6 Ndio, na haya siyo yote; ninakuamuru kwa tamaa yote ambayo unayo kwa kuishi, kwamba utoe silaha zako za vita kwetu, na hatutataka kumwaga damu yenu, lakini tutaokoa maisha yenu, ikiwa mtaenda zenu na msirudi tena kupigana dhidi yetu.

7 Na sasa, kama hamfanyi hivi, tazama, mko mikononi mwetu, na nitaamuru watu wangu wawaangukie, na kuwapiga vidonda vya kifo miilini mwenu, kwamba mmalizike; na ndipo tutaona ni nani atakuwa na uwezo juu ya hawa watu; ndio, tutaona ni nani atakayewekwa utumwani.

8 Na sasa ikawa kwamba wakati Zerahemna aliposikia misemo hii alikuja mbele na kutoa upanga wake na kitara chake, na pinde yake mikononi mwa Moroni, na akamwambia: Tazama, hapa kuna silaha zetu za vita; tutazikabidhi kwenu, lakini hatutakubali wenyewe kuchukua kiapo kwako, ambacho tunajua kwamba tutavunja, na watoto wetu pia; lakini chukueni silaha zetu za vita, na kubali kwamba tuondoke na kwenda nyikani; la sivyo tutabaki na panga zetu, na tutaangamia au kushinda.

9 Tazama, sisi sio wa imani yenu; hatuamini kwamba ni Mungu ambaye ametukabidhi mikononi mwenu; lakini tunaamini kwamba ni ujanja wenu ambao umewahifadhi kutoka kwa panga zetu. Tazama, ni dirii zenu na ngao zenu ambazo zimewahifadhi.

10 Na sasa wakati Zerahemna alipomaliza kuzungumza maneno haya, Moroni alirejesha upanga na silaha za vita, ambazo alikuwa amepokea, kwa Zerahemna, akisema: Tazama, tutamaliza pambano.

11 Sasa siwezi kukumbuka maneno ambayo nimesema, kwa hivyo vile Bwana anavyoishi, hamtaondoka isipokuwa mwondoke na kiapo kwamba hamtarudi tena kwetu kupigana. Sasa vile mko mikononi mwetu tutamwaga damu yenu mchangani, au mkubaliane na masharti ambayo nimetoa.

12 Na sasa wakati Moroni alikuwa amesema maneno haya, Zerahemna aliweka upanga wake, na akamkasirikia Moroni, na akatimka mbele ili amuue Moroni; lakini alipoinua upanga wake, tazama, mmoja wa askari wa Moroni aliupiga hata kwenye ardhi, na ukavunjika kwenye kipini; na pia akampiga Zerahemna kwamba alitoa ngozi ya kichwa chake na ikaanguka ardhini. Na Zerahemna alijiondoa kutoka kwao kupitia katikati ya askari wake.

13 Na ikawa kwamba yule askari ambaye alikuwa amesimama karibu, yule ambaye alikata na kutoa ngozi ya kichwa cha Zerahemna, alichukua ngozi ya kichwa kutoka ardhini kwa kushika nywele, na kuiwekelea kwenye ncha ya upanga wake, na akaunyoosha mbele yao, akisema kwao kwa sauti kubwa:

14 Hata vile ngozi hii imeanguka ardhini, ambayo ni ngozi ya mkuu wenu, hivyo ndivyo mtaanguka ardhini isipokuwa mtoe silaha zenu za vita na kuondoka na agano la amani.

15 Sasa kulikuwa na wengi, wakati waliposikia haya maneno na kuona ngozi ya kichwa ambayo ilikuwa kwenye upanga, kwamba walishikwa na woga; na wengi walisonga mbele na kutupa chini silaha zao za vita miguuni mwa Moroni, na kufanya agano la amani. Na vile wengi waliingia kwenye agano waliwakubalia waelekee nyikani.

16 Sasa ikawa kwamba Zerahemna alighadhibika sana, na akawavuruga askari wake waliosalia kwa hasira, kukabiliana na nguvu zaidi dhidi ya Wanefi.

17 Na sasa Moroni alikasirika, kwa sababu ya ukaidi wa Walamani; kwa hivyo
aliwaamuru watu wake kwamba wawaangukie na kuwaua. Na ikawa kwamba
walianza kuwaua; ndio, na Walamani walipigana na panga zao na uwezo wao.
18 Lakini tazama, ngozi zao zilizokuwa uchi na vichwa vyao vilivyokuwa bure
vilikuwa wazi kwa panga za Wanefi; ndio, tazama zilitobolewa na kukatwa, ndio, na
walianguka haraka sana mbele ya panga za Wanefi; na wakaanza kufagiliwa chini,
hata vile askari wa Moroni alivyokuwa amebashiri.
19 Sasa Zerahemna, alipoona kwamba walikuwa karibu kuangamizwa wote, alilia
sana kwa Moroni, akiahidi kwamba ataweka maagano na pia watu wake na wao,
ikiwa wataponya maisha ya waliosalia, kwamba hawatarudi tena kupigana dhidi yao.
20 Na ikawa kwamba Moroni alisababisha kwamba kazi ya kifo isimamishwe tena
miongoni mwa watu. Na akachukua silaha za vita kutoka kwa Walamani; na baada
ya kuingia kwenye agano la amani na yeye, walikubaliwa kuondoka kwenda kwenye
nyika.
21 Sasa idadi ya wafu wao haikuhesabika kwa sababu ya wingi wa idadi; ndio, idadi
ya wafu wao ilikuwa kubwa sana, kote kwa Wanefi na Walamani.
22 Na ikawa kwamba walitupa wafu wao ndani ya maji ya Sidoni, na wameenda
mbele na kuzikwa kwenye kilindi cha bahari.
23 Na majeshi ya Wanefi, au ya Moroni, yalirejea na kwenda kwenye nyumba zao na
nchi zao.
24 Na hivyo ukaisha mwaka wa kumi na nane wa utawala wa waamuzi juu ya watu
wa Nefi. Na hivyo yakaisha maandishi ya Alma, ambayo yaliandikwa kwenye bamba
za Nefi.

*Historia ya watu wa Nefi, na vita vyao na mafarakano yao, katika siku za Helamani, kulingana na maandishi ya Helamani, ambayo aliweka katika siku zake.*

# Alma 45

1 Tazama, sasa ikawa kwamba watu wa Nefi walikuwa na furaha sana, kwa sababu
Bwana alikuwa amewaokoa tena kutoka mikono ya maadui wao; kwa hivyo walitoa
shukrani kwa Bwana Mungu wao; ndio, na walifunga sana, na kuomba sana na
wakamwabudu Mungu kwa shangwe kuu.
2 Na ikawa katika mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa
Nefi, kwamba Alma alimjia mwana wake Helamani na kumwambia: Unaamini
wewe maneno ambayo nilikuzungumzia kuhusu yale maandiko ambayo
yamehifadhiwa?
3 Na Helamani akasema kwake: Ndio, naamini.
4 Na Alma akasema tena: Unaamini katika Yesu Kristo, atakayekuja?
5 Na akasema: Ndio, ninaamini maneno yote ambayo umesema.
6 Na Alma akasema kwake tena: Utaweka amri zangu?
7 Na akasema: Ndio, nitatii amri zako kwa moyo wangu wote.
8 Na Alma akamwambia: Umebarikiwa wewe; na Bwana atakufanikisha katika
nchi hii.
9 Lakini tazama, nitakutolea unabii mdogo; lakini yale ambayo nitaagua kwako
yasifanywe kujulikana; ndio, yale nitakayoagua kwako hayatafanywa kujulikana,

hata mpaka uaguzi utakavyotimizwa; kwa hivyo andika maneno ambayo nitasema.
10 Na haya ndiyo maneno: Tazama, ninaona kwamba watu hawa, Wanefi,
kulingana na roho ya ufunuo ambayo iko ndani yangu, katika miaka mia nne kutoka
wakati ambao Yesu Kristo atajidhihirisha kwao, watafifia kwa kutoamini.
11 Ndio, na ndipo wataona vita na maradhi ya kuambukiza, ndio, njaa na umwagaji
wa damu, hata mpaka watu wa Nefi watakapomalizika—
12 Ndio, na itafanyika kwa sababu watafifia katika kutoamini na kuangukia kazi za
gizani, na uzinzi, na aina yote ya uovu; ndio, nakwambia, kwamba kwa sababu
watakosa dhidi ya mwangaza ulio mkubwa na hekima, ndio, nakwambia, kwamba
kutokea siku hiyo, hata kizazi cha nne hakitapita kabla ya huu uovu kutokea.
13 Na wakati ile siku kuu itakapowadia, tazama, wakati unawadia mapema kwamba
wale ambao wako sasa, au uzao wa wale ambao wamehesabiwa miongoni mwa watu
wa Nefi, hawatahesabiwa tena miongoni mwa watu wa Nefi.
14 Lakini yeyote atakayebaki, na haangamizwi katika ile siku kuu na ya kuogopesha,
atahesabiwa miongoni mwa Walamani, na atakuwa kama wao, wote, isipokuwa
wachache ambao wataitwa wanafunzi wa Bwana; na hao Walamani watawawinda
mpaka wakati watakapomalizika. Na sasa, kwa sababu ya uovu, huu unabii
utatimizwa.
15 Na sasa ikawa kwamba baada ya Alma kusema vitu hivi kwa Helamani,
alimbariki, na pia wana wake wengine; na pia akabariki ardhi kwa wale walio haki.
16 Na akasema: Bwana Mungu anasema hivi—Nchi italaaniwa, ndio, nchi hii, kwa
kila taifa, kabila, lugha, na watu, kwa uangamizo, ambao wanafanya uovu, wakati
watakapoiva kabisa kwa uovu; na vile nimesema ndivyo itakavyokuwa; kwani hii ni
laana na baraka ya Mungu juu ya nchi, kwani Bwana hawezi kuangalia dhambi na
kuivumilia hata kidogo.
17 Na sasa, wakati Alma alipokuwa amesema maneno haya alibariki kanisa, ndio,
wale wote ambao watasimama imara katika imani kutokea wakati huo na kuendelea.
18 Na wakati Alma alipofanya haya aliondoka kutoka nchi ya Zarahemla, kama
anayeenda katika nchi ya Meleki. Na ikawa kwamba hakusikika tena; hatujui
kulingana kifo chake au kuzikwa kwake.
19 Tazama, haya tunajua, kwamba alikuwa mtu wenye haki; na msemo ukaenea
kanisani kwamba alichukuliwa na Roho, au kuzikwa kwa mkono wa Bwana, kama
vile Musa. Lakini tazama, maandiko yanasema kuwa Bwana alimchukua Musa
kumrudisha kwake mwenyewe; na tunadhani kwamba pia amempokea Alma katika
roho, kwake mwenyewe; kwa hivyo, kwa sababu hii hatujui chochote kuhusu kifo
chake wala mazishi yake.
20 Na sasa ikawa katika mwanzo wa mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa waamuzi
juu ya watu wa Nefi, kwamba Helamani alienda miongoni mwa watu kuwatangazia
neno.
21 Kwani tazama, kwa sababu ya vita vyao na Walamani na mafarakano mengi
madogo na vurugu ambazo zilikuwa miongoni mwa watu, ilikuwa ni lazima
kwamba neno la Mungu litangazwe kwao, ndio, na kwamba maagizo yafanywe
kokote kanisani.
22 Kwa hivyo, Helamani na ndugu zake walienda mbele na kuanzisha kanisa tena
katika nchi, ndio, katika kila mji kote katika nchi ambao ulikuwa umemilikiwa na
watu wa Nefi. Na ikawa kwamba waliteua makuhani na walimu kote nchini, juu ya
makanisa yote.

23 Na sasa ikawa kwamba baada ya Helamani na ndugu zake kuteua makuhani na
walimu juu ya makanisa kwamba kukatokea farakano miongoni mwao, na
hawakusikiliza maneno ya Helamani na ndugu zake;
24 Bali walianza kuwa na kiburi, wakijiinua kwa mioyo yao, kwa sababu ya utajiri
wao mwingi; kwa hivyo walikuwa matajiri kwenye fikira zao, na hawakusikiliza
maneno yao, kutembea wima mbele ya Mungu.

## Alma 46

1 Na ikawa kwamba kadiri wengi ambao hawangesikiza maneno ya Helamani na
ndugu zake walikusanywa pamoja dhidi ya ndugu zao.
2 Na sasa tazama, walikasirika sana, hata kwamba waliamua kuwaua.
3 Sasa kiongozi wa wale ambao walikasirika dhidi ya ndugu zao alikuwa mtu
mkubwa na mwenye nguvu; na jina lake lilikuwa Amalikia.
4 Na Amalikia alitamani kuwa mfalme; na wale watu waliokasirika walitamani
kwamba awe mfalme wao; na walikuwa wengi baina yao waamuzi wa vyeo vya chini
katika nchi, na waliojitafutia ukubwa.
5 Na walikuwa wameongozwa na udanganyifu wa Amalikia, kwamba ikiwa
watamuunga mkono na kumsimamisha kuwa mfalme wao kwamba angewafanya
kuwa watawala juu ya watu.
6 Hivyo waliongozwa na Amalikia kwa mafarakano, ijapokuwa kuhubiri kwa
Helamani na ndugu zake, ndio, ijapokuwa utunzaji wao mkuu juu ya kanisa, kwani
walikuwa makuhani wakuu juu ya kanisa.
7 Na kulikuwa na wengi kanisani ambao waliamini maneno ya udanganyifu ya
Amalikia, kwa hivyo walikataa hata kanisa; na hivyo ndivyo mambo ya watu wa
Nefi yalikuwa yenye shida nyingi na ya hatari, ijapokuwa ushindi wao mkuu ambao
walipata juu ya Walamani, na furaha yao kubwa ambayo walipata kwa sababu ya
wokovu wao kupitia mkono wa Bwana.
8 Hivyo tunaona vile watoto wa watu humsahau Bwana Mungu wao haraka, ndio,
vile hutenda maovu haraka, na kupotoshwa na yule mwovu.
9 Ndio, na pia tunaona ule uovu mwingi ambao mtu mmoja aliye mwovu anaweza
kusababisha kufanyika miongoni mwa watoto wa watu.
10 Ndio, tunaona kwamba Amalikia, kwa sababu alikuwa mtu mjanja na mtu wa
maneno mengi ya kurai, kwamba aliongoza mioyo ya watu wengi kufanya maovu;
ndio, na kutafuta kuangamiza kanisa la Mungu, na kuangamiza msingi wa uhuru
ambao Mungu alikuwa amewakabidhi, au baraka ambayo Mungu alituma katika
ardhi kwa minajili ya wale walio haki.
11 Na sasa ikawa kwamba wakati Moroni, ambaye alikuwa amiri jeshi mkuu wa
majeshi ya Wanefi, aliposikia mafarakano haya, alimkasirikia Amalikia.
12 Na ikawa kwamba alipasua koti lake; na akachukua kipande kutoka kwalo, na
kuandika juu yake — kwa ukumbuko wa Mungu wetu, dini yetu, na uhuru, na amani
yetu, wake zetu, na watoto wetu — na akaifungia juu ya mwisho wa mti.
13 Na akajifunga chapeo kwenye kichwa chake, na dirii yake, na ngao yake, na
kujifungia silaha yake kiunoni mwake; na akaachukua ule mti, ambako mwisho
wake kulikuwa koti lake lililoraruliwa, (na akaiita bendera ya uhuru) na
akajiinamisha chini, na akaomba sana kwa Mungu kuwa baraka ya uhuru iwe na
ndugu zake, kadiri kundi la Wakristo libaki kumiliki nchi —

14 Kwani ndivyo waumini wa Kweli wa Kristo, waliokuwa ndani ya kanisa la
Mungu, walivyoitwa na wale ambao hawakuwa wafuasi wa kanisa.
15 Na wale ambao walikuwa wa kanisa walikuwa waaminifu; ndio, wale wote ambao
waliokuwa waumini wa kweli katika Kristo walijichukulia, kwa furaha, jina la Kristo,
au Wakristo vile waliitwa, kwa sababu ya imani yao katika Kristo ambaye angekuja.
16 Na kwa hivyo, kwa wakati huu, Moroni aliomba kwamba nia ya Wakristo, na
uhuru wa nchi ungependelewa.
17 Na ikawa kwamba alipokuwa ametoa roho yake yote kwa Mungu, aliita nchi yote
iliyo kusini mwa Ukiwa, ndio, na kwa ufupi, nchi yote, kaskazini na kusini — Nchi
iliyochaguliwa, na nchi ya uhuru.
18 Na akasema: Kwa kweli Mungu hawezi kukubali kwamba sisi, ambao
tumedharauliwa kwa sababu tumejichukulia jina la Kristo, tutakanyagwa chini na
kuangamizwa, mpaka tujiletee wenyewe maangamizi kwa makosa.
19 Na Moroni aliposema haya maneno, alienda mbele miongoni mwa watu,
akipepeza kipande cha vazi lake kilichoraruka hewani, ili wote waone maandishi
ambayo aliandika kwenye sehemu iliyoraruka, na akipaza sauti, akisema:
20 Tazama, wowote watakaohifadhi hii bendera katika nchi, hebu waje mbele kwa
uwezo wa Bwana, na kufanya agano kwamba watahifadhi haki yao, na dini yao,
kwamba Bwana Mungu angewabariki.
21 Na ikawa kwamba wakati Moroni alipokuwa ametangaza haya maneno, tazama,
watu walikuja wakikimbia pamoja na silaha zao zikiwa zimefungwa viunoni mwao,
wakirarua nguo zao kama ishara, au kama agano, kwamba hawatamwacha Bwana
Mungu wao; au, kwa maneno mengine, ikiwa wataasi amri za Mungu, au kuingia
kwenye makosa, na wapate aibu kujichukulia jina la Kristo, Bwana angewararua hata
kama vile walivyorarua nguo zao.
22 Sasa hili ndilo agano ambalo walifanya, na walitupa nguo zao miguuni mwa
Moroni, wakisema: Tunaagana na Mungu wetu, kwamba tutaangamizwa, hata
kama vile ndugu zetu katika nchi ya kaskazini, ikiwa tutaingia kwenye makosa;
ndio, atutupe miguuni mwa maadui zetu, hata vile tumetupa nguo zetu miguuni
mwako zikanyagwe chini ya miguu, ikiwa tutaingia kwenye makosa.
23 Moroni akawaambia: Tazama, sisi ni sazo la uzao wa Yakobo; ndio, ni sazo la
uzao wa Yusufu, ambaye koti lake lilirarulíwa na kaka zake kwa vipande vingi; na
sasa tazama, hebu tukumbuke kutii amri za Mungu, au nguo zetu zitararuliwa na
ndugu zetu, na tutupwe gerezani, au tuuzwe, au tuuawe.
24 Ndio, acha tuhifadhi uhuru wetu kama sazo la Yusufu; ndio, acha tukumbuke
maneno ya Yakobo, kabla ya kifo chake, kwani tazama, aliona kwamba sehemu ya
sazo la koti la Yusufu ilihifadhiwa na haikuwa imeoza. Na akasema — Hata vile sazo
la nguo ya mwana wangu limehifadhiwa hata hivyo sazo la uzao wa mwana wangu
uhifadhiwe kwa mkono wa Mungu, na lirudishwe kwake mwenyewe, wakati mabaki
ya uzao wa Yusufu itaangamia, hata vile mabaki ya nguo yake ilikuwa.
25 Sasa tazama, hii inaipatia nafsi yangu huzuni; walakini, nafsi yangu ina shangwe
katika mwana wangu, kwa sababu ya sehemu ya uzao wake ambayo itachukuliwa
kwa Mungu.
26 Sasa tazama, hii ilikuwa lugha ya Yakobo.
27 Na sasa ni nani anaweza kujua kuwa sazo la uzao wa Yusufu, ambayo itaangamia
kama nguo yake, ni wale ambao wametukataa sisi? Ndio, na hata itakuwa sisi ikiwa
hatuwezi kusimama imara katika imani ya Kristo.

28 Na sasa ikawa kwamba Moroni alipokuwa amesema maneno haya alienda mbele,
na pia akatuma kwenye sehemu zote za nchi ambako kulikuwa na mafarakano, na
akawakusanya watu wote ambao walikuwa wanatamani kuhifadhi uhuru wao
pamoja, kusimama dhidi ya Amalikia na wale waliokataa, ambao waliitwa
Waamalikia.
29 Na ikawa kwamba wakati Amalikia alipoona kwamba watu wa Moroni walikuwa
wengi kuliko Waamalikia — na alipoona pia kwamba watu wake walikuwa na
wasiwasi kuhusu haki ya njia ambayo walikuwa wamechukua — kwa hivyo, akiogopa
kwamba hatafaulu katika mambo yake, alichukua wale wa watu wake ambao
wangekubali na wakaondoka na kwenda kwenye nchi ya Nefi.
30 Sasa Moroni alifikiri haikuwa vyema kwamba Walamani wapate nguvu nyingine;
kwa hivyo alifikiri kuwazuia watu wa Amalikia, au kuwachukua na kuwarudisha, na
amuue Amalikia; ndio, kwani alijua kwamba angewavuruga Walamani kukasirika
dhidi yao, na kuwasababisha kuja kwa vita dhidi yao; na hivi alijua kwamba
Amalikia angefanya ili apate kufikia lengo zake.
31 Kwa hivyo Moroni alifikiri ilikuwa ya lazima kwamba achukue majeshi yake,
ambao walikuwa wamejikusanya wenyewe pamoja, na kujihami wenyewe, na
kuingia kwenye agano kuweka amani — na ikawa kwamba alichukua jeshi lake na
kwenda taratibu na hema zake kwenye nyika, kuzuia mwendo wa Amalikia nyikani.
32 Na ikawa kwamba alifanya kulingana na tamaa yake, na akaenda taratibu hadi
kwenye nyika, na kuuzuia mwendo wa majeshi ya Amalikia.
33 Na ikawa kwamba Amalikia alikimbia na idadi ndogo ya watu wake, na waliosalia
waliwekwa kwenye mikono ya Moroni na wakarudishwa katika nchi ya Zarahemla.
34 Sasa, Moroni akiwa ni mtu aliyechaguliwa na waamuzi wakuu na kwa kura ya
watu, kwa hivyo alikuwa na uwezo kulingana na hiari yake na majeshi ya Wanefi,
kuanzisha na kuwa na uwezo juu yao.
35 Na ikawa kwamba yeyote wa Waamalikia ambaye alikataa kuingia katika agano
kuunga mkono njia ya uhuru, kwamba wangehifadhi serikali huru, alisababisha
auawe; na kulikuwa tu wachache waliokataa agano la amani.
36 Na ikawa pia, kwamba alisababisha bendera ya uhuru ipeperushwe kwenye kila
mnara ambao ulikuwa kote nchini, ambayo ilimilikiwa na Wanefi; na hivyo Moroni
alisimika bendera ya uhuru miongoni mwa Wanefi.
37 Na wakaanza kuwa na amani tena nchini; na hivyo wakadumisha amani nchini
mpaka karibu mwisho wa mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa waamuzi.
38 Na Helamani na makuhani wakuu pia waliimarisha amri ndani ya kanisa; ndio,
hata kwa muda wa miaka minne walikuwa na amani nyingi na furaha ndani ya
kanisa.
39 Na ikawa kwamba kulikuwa na wengi waliokufa, walakini imara wakiamini
kwamba nafsi zao zimekombolewa na Bwana Yesu Kristo; hivyo walitoka duniani
wakifurahi.
40 Na kulikuwa na wengi ambao walifariki kwa homa, ambayo kwa misimu fulani
mwakani ilikuweko mara kwa mara nchini — lakini sio kwa wingi hivyo na homa,
kwa sababu ya ubora wa mimea mingi na mizizi ambayo Mungu alikuwa
ametayarisha kutoa mwanzo wa maradhi, ambayo binadamu walikuwa wakishikwa
nayo kwa ajili ya hali ya hewa ya nchi —
41 Lakini kulikuwa na wengi waliokufa wakiwa wamezeeka; na wale waliokufa
ndani ya imani ya Kristo wanayo furaha ndani yake, vile lazima tuwaze.

# Alma 47

1 Sasa tutarudia kwenye historia yetu kwa Amalikia na wale ambao walitoroka na yeye
kwenda nyikani; kwani, tazama, alikuwa amechukua wale ambao walienda na yeye,
na akaenda katika nchi ya Nefi miongoni mwa Walamani, na akawachochea
Walamani kuwa na hasira dhidi ya watu wa Nefi, hata kuwa mfalme wa Walamani
akatoa tangazo kote nchini mwake, miongoni mwa watu wake wote, kuwa
wajikusanye pamoja tena waanze vita dhidi ya Wanefi.
2 Na ikawa kwamba wakati tangazo lilipokuwa limetolewa miongoni mwao
waliogopa sana; ndio, waliogopa kumkasirisha mfalme, na pia waliogopa kwenda
vitani dhidi ya Wanefi wasije wakapoteza maisha yao. Na ikawa kwamba
hawangeweza, au sehemu yao kubwa haingeweza, kutii amri ya mfalme.
3 Na ikawa kwamba mfalme alikasirika kwa sababu ya maasi yao; kwa hivyo alimpa
Amalikia amri juu ya sehemu ya jeshi lake ambalo lilitii amri zake, na akamwamuru
kwamba aende mbele na kuwalazimisha kuchukua silaha.
4 Sasa tazama, hii ndiyo ilikuwa nia ya Amalikia; kwani yeye alikuwa mtu mjanja
kwa kufanya maovu kwa hivyo aliweka mpango ndani ya moyo wake kumwondoa
mfalme wa Walamani.
5 Na sasa alikuwa amepata amri kwa yale makundi ya Walamani ambao walikuwa
wanapendelea mfalme; na akatazamia kupendelewa na wale ambao hawakuwa
watiifu; kwa hivyo alienda mbele katika mahali palipoitwa Onida, kwani hapa
Walamani wote walikuwa wamekimbilia; kwani waligundua jeshi likija, na
wakidhani kwamba lilikuwa linakuja kuwaangamiza, kwa hivyo walikimbilia Onida,
mahali pa silaha.
6 Na walikuwa wamemchagua mtu kuwa mfalme na kiongozi juu yao, wakiwa
wamekata kauli kuwa hawatakwenda dhidi ya Wanefi.
7 Na ikawa kwamba walikuwa wamejikusanya pamoja juu ya kilele cha mlima
ambao uliitwa Antipa, wakijiandaa kupigana.
8 Sasa halikuwa kusudi la Amalikia kupigana nao kulingana na amri ya mfalme;
lakini tazama, lilikuwa kusudi lake kupata mapendeleo kutoka kwa majeshi ya
Walamani, ili ajiweke mwenyewe juu yao na kumwondoa mfalme na kumiliki
ufalme.
9 Na tazama, ikawa kwamba alisababisha jeshi lake kusimamisha hema zao kwenye
bonde ambalo lilikuwa karibu na mlima Antipa.
10 Na ikawa kwamba wakati usiku ulipowadia alituma wajumbe wa siri kwenye
mlima Antipa, akitaka kwamba kiongozi wa wale ambao walikuwa mlimani, ambaye
jina lake lilikuwa Lehonti, kwamba aje chini ya mlima, kwani alitaka kuongea na
yeye.
11 Na ikawa kwamba wakati Lehonti alipopata ujumbe hakuthubutu kwenda chini
ya mlima. Na ikawa kwamba Amalikia akatuma tena mara ya pili, akitaka yeye aje
chini. Na ikawa kwamba Lehonti hangeenda; na akatuma tena mara ya tatu.
12 Na ikawa kwamba wakati Amalikia alipogundua kwamba hangempata Lehonti
aje chini kutoka mlimani, alipanda mlima, karibu na kituo cha Lehonti; na akatuma
tena mara ya nne ujumbe wake kwa Lehonti, akitaka kwamba aje chini, na kwamba
angeleta walinzi wake pamoja na yeye.
13 Na ikawa kwamba wakati Lehonti alipokuja chini na walinzi kwa Amalikia,
kwamba Amalikia alitaka yeye aje chini na jeshi lake wakati wa usiku, na azingire
wale watu kwenye kituo chao ambao mfalme alimpatia kuongoza, na kwamba

angewasalimisha mikononi mwa Lehonti, ikiwa angemfanya (Amalikia) kiongozi wa pili juu ya jeshi lote.

14 Na ikawa kwamba Lehonti aliteremka chini na watu wake na kuwazingira watu wa Amalikia, kwamba kabla ya hao kuamka kukipambazuka walikuwa wamezingirwa na majeshi ya Lehonti.

15 Na ikawa kwamba walipoona kwamba wamezungukwa, walimwomba Amalikia kwamba awakubalie wawe pamoja na ndugu zao, ili wasiangamizwe. Sasa hiki ndicho kitu ambacho Amalikia alitaka.

16 Na ikawa kwamba aliwasalimisha watu wake, kinyume cha amri ya mfalme. Sasa hiki ndicho Amalikia alitaka, kwamba atimize mipango yake ya kumwondoa mfalme.

17 Sasa ilikuwa desturi miongoni mwa Walamani, ikiwa kiongozi wao mkuu aliuawa, kumchagua kiongozi wao wa pili kuwa kiongozi mkuu.

18 Na ikawa kwamba Amalikia alisababisha mmoja wa watumishi wake aweke sumu kidogo kidogo kwa Lehonti, kwamba alikufa.

19 Sasa, Lehonti alipokufa, Walamani walimchagua Amalikia kuwa kiongozi wao na amiri jeshi mkuu.

20 Na ikawa kwamba Amalikia alitembea taratibu na majeshi yake (kwani alikuwa amefaulu yale aliyoyataka) hadi kwenye nchi ya Nefi, kwenye mji wa Nefi, ambao ulikuwa mji mkuu.

21 Na mfalme akaja nje kukutana na yeye pamoja na walinzi wake, kwani alidhani kwamba Amalikia ametimiza amri zake, na kwamba Amalikia alikuwa amekusanya pamoja jeshi kubwa hivyo kwenda dhidi ya Wanefi vitani.

22 Lakini tazama, vile mfalme alipokuja nje kukutana na yeye Amalikia alisababisha kwamba watumishi wake waende na kumpokea mfalme. Na wakaenda na kujiinamisha mbele ya mfalme, kama kumwonyesha heshima kwa sababu ya ukuu wake.

23 Na ikawa kwamba mfalme aliinua mkono wake juu kuwasimamisha, vile ilivyokuwa desturi ya Walamani, kama ishara ya amani, desturi ambayo waliiga kutoka kwa Wanefi.

24 Na ikawa kwamba wakati alipokuwa amemwinua wa kwanza kutoka ardhini, tazama alimdunga mfalme moyoni; na akaanguka ardhini.

25 Sasa watumishi wa mfalme walitoroka, na watumishi wa Amalikia wakapiga nduru, wakisema:

26 Tazama, watumishi wa mfalme wamemdunga moyoni, na ameanguka na wametoroka; tazama, njoeni mwone.

27 Na ikawa kwamba Amalikia aliamrisha majeshi yake yaende mbele na kuona kile kilichotendeka kwa mfalme; na walipofika hapo mahali, na kumpata mfalme amelala katika damu yake, Amalikia alijifanya kukasirika, na kusema: Yeyote aliyempenda mfalme ebu aende mbele, na kuwafuata watumishi wa mfalme ili wauawe.

28 Na ikawa kwamba wale wote waliompenda mfalme, waliposikia haya maneno, walikuja mbele na kuwafukuza watumishi wa mfalme.

29 Sasa watumishi wa mfalme walipoona jeshi likiwafukuza, waliogopa tena, na wakatorokea nyikani, na wakafikia nchi ya Zarahemla na kuungana na watu wa Amoni.

30 Na jeshi ambalo lilikuwa likiwafukuza lilirudi, wakiwa wamewafukuza bila

kufaulu; na hivyo Amalikia, kwa hila yake, alipata imani ya watu.
31 Na ikawa kesho yake akaingia kwenye mji wa Nefi na majeshi yake, na kumiliki
mji.
32 Na sasa ikawa kwamba malkia, aliposikia kwamba mfalme ameuawa — kwani
Amalikia alikuwa ametuma ujumbe kwa malkia kumjulisha kwamba mfalme
ameuawa na watumishi wake, kwamba aliwafukuza na jeshi lake, lakini
haikuwezekana, na wakatoroka —
33 Kwa hivyo, wakati malkia alipokuwa amepokea taarifa hii alituma taarifa kwa
Amalikia, akimtaka kwamba aachilie watu wa mji; na akataka aende kwake; na
akahitaji kwamba aje na mashahidi kushuhudia kuhusu kifo cha mfalme.
34 Na ikawa kwamba Amalikia alimchukua yule mtumishi ambaye alimuua mfalme,
na wote waliokuwa na yeye, na kumwendea malkia, mahali ambapo aliketi; na wote
walishuhudia kwake kwamba mfalme aliuawa na watumishi wake mwenyewe, na pia
wakasema: Wametoroka; si hii inashuhudia dhidi yao? Na hivyo walimridhisha
malkia kuhusu kifo cha mfalme.
35 Na ikawa kwamba Amalikia alihitaji mapendeleo ya malkia, na akamwoa kuwa
mkewe; na hivyo kwa hila yake, na kwa usaidizi wa watumishi wake werevu, alipata
ufalme; ndio, alitambuliwa mfalme kote nchini, miongoni mwa watu wa Walamani,
ambao walikuwa mkusanyiko wa Walamani na Walemueli na Waishmaeli, na wote
waliokimbia kutoka kwa Wanefi, tangu utawala wa Nefi hadi wakati huu.
36 Sasa hawa wakimbiaji, wakiwa na mafundisho sawa na elimu sawa ya Wanefi,
ndio, wakiwa wamefundishwa kwa elimu ya Bwana, walakini, ni vigumu kusimulia,
sio wakati mrefu baada ya mafarakano yao walikuwa wagumu na wasiotubu, na
mazuzu, waovu na wakatili kuliko Walamani — wakikubali desturi za Walamani;
wakijiingiza kwenye uzembe, na kila aina ya uzinifu; ndio, wakimsahau kabisa
Bwana Mungu wao.

# Alma 48

1 Na sasa ikawa kwamba, Amalikia alipopokea utawala alianza kuvuta mioyo ya
Walamani dhidi ya watu wa Nefi; ndio, alichagua watu kuzungumzia Walamani
kutoka kwa minara yao, dhidi ya Wanefi.
2 Na hivyo akavuta mioyo yao dhidi ya Wanefi, kwa wingi kwamba katika mwisho
wa mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa waamuzi, akiwa ametimiza mipango yake
hivyo, ndio, akishafanywa mfalme juu ya Walamani, alifikiria pia kutawala nchi
yote, ndio, na watu wote waliokuwa nchini, Wanefi na pia Walamani.
3 Kwa hivyo alikuwa ametimiza kusudi lake, kwani alikuwa ameshupaza mioyo ya
Walamani na akawapofusha akilini, na kuwachochea kuwa na hasira, kwa wingi
kwamba waende vitani dhidi ya Wanefi.
4 Kwani alikuwa ameamua, kwa sababu ya wingi wa watu wake, kuwashinda
Wanefi na kuwaweka kifungoni.
5 Na hivyo aliweka makapteni wakuu wa Wazoramu, hawa wakiwa wamezoea
nguvu za Wanefi, na mahali pao pa kawaida, na sehemu dhaifu za miji yao; kwa
hivyo aliwaweka kuwa makapteni wakuu wa majeshi yake.
6 Na ikawa kwamba walichukua kituo chao, na kusonga mbele kuelekea nchi ya
Zarahemla katika nyika.
7 Sasa ikawa kwamba wakati Amalikia alikuwa anapokea uwezo kwa hila na

udanganyifu, Moroni, kwa upande mwingine, alikuwa anatayarisha akili za watu
kwa uaminifu kwa Bwana Mungu wao.
8 Ndio, alikuwa akiimarisha majeshi ya Wanefi, na kujenga ngome ndogo, au
mahali pa usalama; akitupa kuta za ardhi karibu kufunika majeshi yake, na pia
kujenga kuta za mawe kuwazunguka, kuzingira miji yao na mipaka ya nchi yao;
ndio, kila mahali nchini.
9 Na kwa udhaifu wao aliweka idadi kubwa zaidi ya watu; na hivyo aliweka nguvu
na kuimarisha nchi ambayo ilimilikiwa na Wanefi.
10 Na hivyo alikuwa akijitayarisha kulinda uhuru wao, nchi yao, wake zao, na
watoto wao, na amani yao, na kwamba wangeishi kwa Bwana Mungu wao, na
kwamba wangeshikilia ile ambayo iliitwa na maadui wao imani ya Wakristo.
11 Na Moroni alikuwa mtu mwenye nguvu na uwezo; na alikuwa mtu wa kuelewa
kikamilifu; ndio, mtu ambaye hakufurahia umwagaji wa damu; mtu ambaye nafsi
yake ilijawa shangwe kwa ajili ya uungwana na uhuru wa nchi yake, na wa ndugu
zake kutoka kifungo na utumwa;
12 Ndio, mtu ambaye moyo wake ulijaa shukrani kwa Mungu wake, kwa
mapendeleo na baraka ambazo aliwapatia watu wake; mtu ambaye alifanya kazi sana
kwa ustawi na usalama wa watu wake.
13 Ndio, na alikuwa mtu ambaye alikuwa imara katika imani ya Kristo, na aliapa na
kiapo kuwa atawalinda watu wake, haki zake, na nchi yake, na dini yake, hata
kwenye kumwaga damu yake.
14 Sasa Wanefi walifundishwa vile wanavyoweza kujilinda wenyewe dhidi ya
maadui zao, hata kwenye kumwaga damu ikiwa ilihitajika; ndio, na walifundishwa
kutodhuru, ndio, na kutoinua upanga isipokuwa dhidi ya adui, isipokuwa wawe
wanahifadhi maisha yao.
15 Na hii ilikuwa imani yao, kwamba kwa kufanya hivyo Mungu angewafanikisha
nchini, au kwa maneno mengine, wakiwa waaminifu kwa kutii amri za Mungu
kwamba angewafanikisha katika nchi; ndio, kuwaonya watoroke, au kuwaandaa kwa
vita, kulingana na hatari iliyopo;
16 Na pia, kwamba Mungu angewawezesha kujua wangeenda wapi kujilinda dhidi
ya maadui zao, na kwa kufanya hivyo, Bwana angewaokoa; na hii ilikuwa imani ya
Moroni, na moyo wake ulifurahi ndani yake; sio kwa kumwaga damu lakini kwa
kutenda mema, kwa kuhifadhi watu wake, ndio, kwa kutii amri za Mungu, na kuzuia
uovu.
17 Ndio, kweli, kweli ninavyowaambia, ikiwa watu wote walikuwa, na wako, na
ikiwa watakuweko daima, kama Moroni, tazama, hizo nguvu za jahanamu
zingetingizika milele; ndio, ibilisi hangekuwa na uwezo juu ya mioyo ya watoto wa
watu.
18 Tazama, alikuwa mtu kama Amoni, mwana wa Mosia, ndio, na hata wana
wengine wa Mosia, ndio, na pia Alma na wana wake, kwani walikuwa wote watu wa
Mungu.
19 Sasa tazama, Helamani na ndugu zake hawakufanya kazi ndogo kwa watu kuliko
Moroni; kwani walihubiri neno la Mungu, na walibatiza ubatizo wa toba watu wote
ambao wangesikiliza maneno yao.
20 Na hivyo wakaendelea na watu walijinyenyekeza kwa sababu ya maneno yao,
kwamba walipendelewa sana na Bwana, na hivyo wakawa huru kutokana na vita na
mabishano miongoni mwao, ndio, hata kwa muda wa miaka minne.

21 Lakini, vile nimesema, kwenye mwisho wa mwaka wa kumi na tisa, ndio,
ijapokuwa amani yao miongoni mwao, walilazimishwa bila kupenda kupigana na
wenzao, Walamani.
22 Ndio, kwa kifupi, vita vyao havikukoma kamwe kwa muda wa miaka mingi na
Walamani, ijapokuwa kutopendelea kwao.
23 Sasa, walihuzunika kuchukua silaha dhidi ya Walamani, kwa sababu
hawakupendelea umwagaji wa damu; ndio, na hii sio yote—walihuzunika kuwa njia
ya kuondoa wengi wa ndugu zao nje ya ulimwengu huu hadi kwenye ulimwengu wa
milele, kabla ya kujitayarisha kukutana na Mungu wao.
24 Walakini, hawangekubali kuweka chini maisha yao, kwamba wake zao na watoto
wao wachinjwe ovyo kwa ukatili na ujeuri wa wale ambao walikuwa siku moja
ndugu zao, ndio, na walioasi kutoka kanisa lao, na waliwaacha na kujaribu
kuwaangamiza kwa kuungana na Walamani.
25 Ndio, hawangevumilia kwamba ndugu zao wafurahi juu ya damu ya Wanefi,
mradi kuwe na yeyote atakayetii amri za Mungu, kwani ahadi ya Bwana ilikuwa,
kama watatii amri zake watafanikiwa nchini.

# Alma 49

1 Na sasa ikawa katika mwezi wa kumi na moja wa mwaka wa kumi na tisa, siku ya
kumi ya mwezi, majeshi ya Walamani yalionekana yakikaribia kuelekea nchi ya
Amoniha.
2 Na tazama, mji ulikuwa umejengwa upya, na Moroni alikuwa ameweka jeshi
karibu na mipaka ya mji, na walikuwa wametupa udongo kuzunguka kuwakinga
kutokana na mishale na mawe ya Walamani; kwani tazama, walipigana kwa mawe na
mishale.
3 Tazama, nilisema kwamba mji wa Amoniha ulikuwa umejengwa upya.
Nakwambia, ndio, ilikuwa sehemu moja imejengwa upya; na kwa sababu Walamani
walikuwa wameuharibu wakati mmoja kwa sababu ya uovu wa watu, walidhani
kwamba tena itakuwa rahisi kwao.
4 Lakini tazama, vile kulikuwa maudhi kwao; kwani tazama, Wanefi walikuwa
wamechimba tuta la ardhi kuwazunguka, ambalo lilikuwa refu sana kwamba
Walamani hawangetupa mawe yao na mishale yao kwao kwamba ingefanya
chochote, wala hawangewafikia isipokuwa wapitie kwenye lango lao la kupitia.
5 Sasa kwa wakati huu makapteni wakuu wa Walamani walishtushwa sana, kwa
sababu ya hekima ya Wanefi kwa kutayarisha mahali pao pa ulinzi.
6 Sasa viongozi wa Walamani walikuwa wamedhani, kwa sababu ya wingi wa idadi
yao, ndio, walidhani kwamba wangenufaika kuwashambulia vile walikuwa
wamefanya awali; ndio, na walikuwa pia wamejitayarisha kwa ngao, na dirii; na
walikuwa pia wamejitayarisha na nguo za ngozi, ndio, nguo nzito sana kwa kufunika
uchi wao.
7 Na wakiwa wamejitayarisha hivyo walidhani kwamba wangeshinda kwa urahisi
na kuwaweka ndugu zao katika nira ya utumwa, au kuwakata na kuwachinja
kulingana na furaha yao.
8 Lakini tazama, kwa mshangao wao mkuu, walikuwa wamejitayarisha kwa ajili
yao, kwa njia ambayo haijajulikana miongoni mwa watoto wa Lehi. Sasa walikuwa
wamejiandaa kwa ajili ya Walamani, kupigana wakifuata njia ya mafundisho ya

Moroni.
9 Na ikawa kwamba Walamani, au Waamalikia, walistaajabu sana katika namna
yao ya matayarisho ya vita.
10 Sasa, kama mfalme Amalikia angekuja chini kutoka nchi ya Nefi, mbele ya jeshi
lake, labda angesababisha Walamani kuwashambulia Wanefi katika mji wa
Amoniha; kwani tazama, hakujali damu ya watu wake.
11 Lakini tazama, Amalikia hakuja chini mwenyewe kupigana. Na tazama,
makapteni wake wakuu hawakuwashambulia Wanefi katika mji wa Amoniha, kwani
Moroni alikuwa amebadilisha shughuli ya usimamizi miongoni mwa Wanefi, hata
kuwa Walamani hawakupendezwa katika mahali pao pa kurudi nyuma na
hawangewajia.
12 Kwa hivyo walirudi nyuma hadi kwenye nyika, na kuchukua kituo chao na
wakaenda taratibu kuelekea nchi ya Nuhu, wakidhani kuwa pale ni pahali pazuri
kwao kuja dhidi ya Wanefi.
13 Kwani hawakujua kwamba Moroni alikuwa amezuia, au alikuwa amejenga
ngome za ulinzi, kwa kila mji chini kote kuzunguka; kwa hivyo, walitembea mbele
taratibu hadi nchi ya Nuhu kwa juhudi imara; ndio, makapteni wao wakuu walikuja
mbele na kula kiapo kwamba wataangamiza watu wa mji huo.
14 Lakini tazama, kwa mshangao wao, mji wa Nuhu, ambao hapo awali ulikuwa
dhaifu, ulikuwa sasa, kwa juhudi za Moroni, kuwa wenye nguvu, ndio, hata
kushinda nguvu ya mji wa Amoniha.
15 Na sasa, tazama, hii ilikuwa hekima ndani ya Moroni; kwani alidhani kwamba
wangeogopa katika mji wa Amoniha; na vile mji wa Nuhu ulikuwa mpaka sasa
sehemu dhaifu katika nchi, kwa hivyo wangeenda hapo kupigana; na hivyo ilikuwa
kulingana na tamaa zake.
16 Na tazama, Moroni alikuwa amemweka Lehi kuwa kapteni mkuu juu ya watu wa
mji huo; na alikuwa ni huyo Lehi ambaye alipigana na Walamani kwenye bonde la
mashariki mwa mto Sidoni.
17 Na sasa tazama ikawa kwamba wakati Walamani walipogundua kwamba Lehi
alikuwa amiri jeshi wa mji, hawakupendezwa kwani walimwogopa Lehi sana;
walakini makapteni wao wakuu walikuwa wameapa na kiapo kuushambulia mji;
kwa hivyo, walileta majeshi yao.
18 Sasa tazama, Walamani hawangeingia katika ngome zao za ulinzi kwa njia ingine
yoyote isipokuwa kwenye lango, kwa sababu ya urefu wa ukingo ambao ulikuwa
umejengwa, na urefu wa kwenda chini wa handaki ambalo lilikuwa limelimbwa
kuzunguka hapo, isipokuwa tu kupitia kwenye lango.
19 Na hivyo Wanefi walijiandaa kuangamiza jaribio kama hilo la kupanda juu na
kuingia ndani ya ngome kwa njia ingine yoyote, kwa kurusha mawe na mishale kwao.
20 Hivyo walijiandaa, ndio, kundi la watu wao wenye nguvu, na panga zao na
kombeo zao, kuwauwa wote ambao wangejaribu kuja kwa pahali pao pa ulinzi
kupitia mahali pa mlango; na hivyo ndivyo walivyojiandaa kujilinda dhidi ya
Walamani.
21 Na ikawa kwamba makapteni wa Walamani walileta majeshi yao mbele ya mahali
pa kuingilia, na wakaanza kushambuliana na Wanefi, kuingia ndani ya mahali pao
pa ulinzi; lakini tazama, waliwafukuza kila wakati kwa wingi, kwamba walichinjwa
kwa uchinjaji mkuu.
22 Sasa wakati walipogundua ya kwamba hawangepata uwezo juu ya Wanefi kupitia

mlangoni, walianza kuchimba chini kingo zao ili wapate njia ya kufikia majeshi yao, kwamba wapate nafasi sawa kupigana; lakini tazama, kwa haya majaribio walifagiliwa mbali kwa mawe na mishale ambayo walitupiwa; na badala ya kujaza mitaro yao kwa kubomoa kingo za mchanga, zilijazwa kwa kiwango na wafu wao na miili iliyojeruhiwa.

23 Hivyo Wanefi walikuwa na uwezo wote juu ya maadui wao; na hivyo Walamani walijaribu kuwaangamiza Wanefi mpaka makapteni wao wakuu wote wakauawa; ndio, na zaidi ya elfu moja ya Walamani waliuawa; wakati, kwa upande mwingine, hakukuwa hata na nafsi moja ya Wanefi ambayo iliuawa.

24 Kulikuwa na karibu hamsini ambao walijeruhiwa, ambao walikuwa wazi kwa mishale ya Walamani kupitia mlangoni, lakini walijikinga na ngao zao, na dirii zao, na vyapeo vyao, hata kwamba vidonda vyao vilikuwa kwa miguu yao, vingi ambavyo vilikuwa vibaya sana.

25 Na ikawa kwamba wakati Walamani walipoona kwamba makapteni wao wakuu wote wameuawa walikimbilia nyikani. Na ikawa kwamba walirejea kwa nchi ya Nefi, kumjulisha mfalme wao, Amalikia, ambaye alikuwa Mnefi kwa kuzaliwa, kuhusu hasara yao kubwa.

26 Na ikawa kwamba alikasirika sana na watu wake, kwa sababu hakuwa amepata matarajio yake juu ya Wanefi; hakuwa amewaweka kwa nira ya utumwa.

27 Ndio, alikasirika sana, na akamlaani Mungu, na pia Moroni, akiapa kwa kiapo kuwa atakunywa damu yake; na hii ni kwa sababu Moroni alikuwa ametii amri za Mungu kwa kutayarisha usalama wa watu wake.

28 Na ikawa kwamba kwa upande mwingine, watu wa Nefi walimshukuru Bwana Mungu, kwa sababu ya nguvu yake isiyo na kifani kwa kuwakomboa kutoka mikono ya maadui zao.

29 Na hivyo ukaisha mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

30 Ndio, na kulikuwa na amani mfululizo miongoni mwao, na mafanikio makuu katika kanisa kwa sababu ya kusikiliza kwao na bidii ambayo walitoa kwa neno la Mungu, ambalo lilitangazwa kwao na Helamani, na Shibloni, na Koriantoni, na Amoni na ndugu zake, ndio, na wote ambao walikuwa wameitwa kwa amri takatifu ya Mungu, wakibatizwa ubatizo wa toba, na kutumwa mbele kuhubiri miongoni mwa watu.

# Alma 50

1 Na sasa ikawa kwamba Moroni hakuacha kujitayarisha kwa vita, au kulinda watu wake dhidi ya Walamani; kwani alisababisha kwamba majeshi yake yaanze katika mwanzo wa mwaka wa ishirini wa utawala wa waamuzi, kwamba waanze kulima vilima vya udongo kuzunguka miji yote, kote katika nchi ambayo ilimilikiwa na Wanefi.

2 Na juu ya haya magongo ya ardhi alisababisha kwamba kuwe na mbao, ndio, kazi za mbao zijengwe kwa urefu wa mtu, kuzunguka miji.

3 Na akasababisha kwamba juu ya kazi hizo za mbao kuwe na ufito wa miiba ujengewe kwenye mbao kuzunguka; na zilikuwa nzito na ndefu.

4 Na akasabisha minara kujengwa ambayo iliangalia zile kuta za walinzi, na akasababisha mahali pa ulinzi kujengwa kwenye hiyo minara, ili mawe na mishale ya

Walamani haingewaumiza.
5 Na walikuwa wamejitayarisha ili waweze kutupa mawe kutoka juu, kulingana na nia yao na nguvu yao, na kumuua yeyote ambaye angejaribu kuja karibu na kuta za mji.
6 Hivyo Moroni aliandaa ngome dhidi ya kuja kwa maadui wao, kuzunguka kila mji nchini.
7 Na ikawa kwamba Moroni alisababisha kwamba majeshi yake yaende mbele kwenye mashariki ya nyika; ndio, na wakaenda mbele na kuwakimbiza Walamani wote waliokuwa ndani ya nyika ya mashariki hadi kwenye nchi zao, ambazo zilikuwa kusini mwa nchi ya Zarahemla.
8 Na nchi ya Nefi ilienea katika mstari mnyoofu kutokea kwenye bahari ya mashariki hadi magharibi.
9 Na ikawa kwamba Moroni alipokuwa amewafukuza Walamani wote nje ya nyika ya mashariki, ambayo ilikuwa kaskazini mwa nchi za umiliki wao, alisababisha kwamba wakaazi ambao walikuwa kwenye nchi ya Zarahemla na nchi iliyoizunguka lazima waende mbele kwenye nyika ya mashariki, hata kwenye mipaka kando ya bahari, na kumiliki nchi.
10 Na pia akaweka majeshi kusini, katika mipaka ya umiliki wao, na akawasababisha wajenge ngome kwamba wangeweka salama majeshi yao na watu wao kutoka mikono ya maadui zao.
11 Na hivyo akaondoa ngome zote za Walamani kwenye mashariki ya nyika, ndio, na pia kwenye magharibi, akiimarisha mpaka miongoni mwa Wanefi na Walamani, kati ya nchi ya Zarahemla na nchi ya Nefi, kutoka magharibi mwa bahari, kuenea kando ya mwanzo wa mto Sidoni — Wanefi wakimiliki nchi yote upande wa kaskazini, ndio, hata nchi yote ambayo ilikuwa upande wa kaskazini ya nchi ya Neema, kulingana na kupenda kwao.
12 Hivyo Moroni, na majeshi yake, ambayo yaliongezeka kila siku kwa sababu ya kuhakikishiwa na ulinzi ambao kazi yake iliwaletea, walitaka kutoa nguvu na uwezo wa Walamani kutoka nchi zao za umiliki, ili wasiwe na uwezo juu ya nchi zao za umiliki.
13 Na ikawa kwamba Wanefi walianza msingi wa mji, na wakaita jina la mji Moroni; na ulikuwa kando ya bahari ya mashariki; na ulikuwa kusini kando ya mpaka wa umiliki wa Walamani.
14 Na pia walianza msingi wa mji kati ya mji wa Moroni na mji wa Haruni, ukiungana na mipaka ya Haruni na Moroni; na wakaita jina la mji, au nchi, Nefiha.
15 Na pia wakaanza kujenga katika mwaka huo huo miji mingi kaskazini, mmoja kwenye njia fulani ambao waliuita Lehi, ambao ulikuwa kaskazini kando na mipaka ya ukingo wa bahari.
16 Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini.
17 Na kwa hii hali ya kufanikiwa waliishi watu wa Nefi katika mwanzo wa mwaka wa ishirini na moja wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.
18 Na walifanikiwa sana, na wakawa matajiri sana; ndio, na wakaongezeka na wakawa na nguvu nchini.
19 Na hivyo tunaona jinsi gani hekima na haki ni matendo yote ya Bwana, kwa kutimiza maneno yake yote kwa watoto wa watu; ndio, tunaweza kuona kuwa maneno yake yanathibitishwa, hata wakati huu, ambayo alimzungumzia Lehi akisema:

20 Umebarikiwa wewe na watoto wako; na watabarikiwa ikiwa watatii amri zangu
watafanikiwa nchini. Lakini kumbuka, ikiwa hawatatii amri zangu watatolewa
mbali kutoka uwepo wa Bwana.
21 Na tunaona kwamba ahadi hizi zimetimizwa kwa watu wa Nefi; kwani imekuwa
ugomvi wao na mateto yao, ndio, mauaji yao, na uporaji wao, ukafiri wao, ukahaba
wao, na unyang'anyi wao, na machukizo yao, ambayo yalikuwa miongoni mwao,
ambayo yalisababisha vita vyao na maangamizo yao.
22 Na wale ambao walikuwa waaminifu kwa kutii amri za Bwana walikombolewa
wakati wote, wakati maelfu ya ndugu zao waovu wameachwa kwenye kifungo, au
kuangamia kwa upanga, au kufifia kwa kutoamini, na kuingiliana na Walamani.
23 Lakini tazama hakujakuwa wakati wa furaha miongoni mwa watu wa Nefi, tangu
siku za Nefi, kuliko siku za Moroni, ndio, hata wakati huu, katika mwaka wa ishirini
na moja wa utawala wa waamuzi.
24 Na ikawa kwamba mwaka wa ishirini na mbili wa utawala wa waamuzi pia
ukaisha kwa amani; ndio, na pia mwaka wa ishirini na tatu.
25 Na ikawa kwamba katika mwanzo wa mwaka wa ishirini na nne wa utawala wa
waamuzi, kungekuwa pia amani miongoni mwa watu wa Nefi kama hakungekuwa
ubishi ambao ulikuweko miongoni mwao kuhusu nchi ya Lehi, na nchi ya
Moriantoni, ambazo ziliungana katika mipaka ya Lehi; zote mbili ambazo zilikuwa
kwenye mipaka kando ya ukingo wa bahari.
26 Kwani tazama, watu ambao walimiliki nchi ya Moriantoni walidai sehemu ya
nchi ya Lehi; kwa hivyo kulianza kuwa na ubishi mkali miongoni mwao, hata
kwamba watu wa Moriantoni walichukua silaha dhidi ya ndugu zao, na walikata
kauli kuwauwa kwa upanga.
27 Lakini tazama, watu ambao walimiliki nchi ya Lehi walikimbilia kituo cha
Moroni, na kumuomba usaidizi; kwani tazama hawakuwa na makosa.
28 Na ikawa kwamba wakati watu wa Moriantoni, ambao waliongozwa na mtu
ambaye jina lake lilikuwa Moriantoni, waligundua kwamba watu wa Lehi walikuwa
wamekimbilia kituo cha Moroni, waliogopa sana isiwe jeshi la Moroni lingekuja
kwao na kuwaangamiza.
29 Kwa hivyo, Moriantoni alisadikisha mioyo yao kwamba wakimbilie nchi ambayo
ilikuwa kaskazini, ambayo ilikuwa imefunikwa kwa miili mikubwa ya maji, na
kumiliki nchi ambayo ilikuwa upande wa kaskazini.
30 Na tazama, wangetekeleza huu mpango kwa vitendo, (ambao ungekuwa mwanzo
wa masikitiko) lakini tazama, Moriantoni akiwa mtu wa juhudi kuu ya roho, kwa
hivyo alimkasirikia mmoja wa wafanya kazi wake wa kike, na akamwangukia na
kumpiga sana.
31 Na ikawa kwamba alitoroka, na akafikia kituo cha Moroni, na kumwambia
Moroni vitu vyote kuhusu mambo hayo, na pia kuhusu mipango yao ya kukimbilia
nchi ya upande wa kaskazini.
32 Sasa tazama, watu ambao walikuwa katika nchi ya Neema, kwa usahihi zaidi
Moroni, waliogopa kwamba wangesikia na kufuata maneno ya Moriantoni na
kuungana na watu wake, na hivyo angepata urithi wa hizo sehemu za nchi, ambao
ungeweka msingi wa matokeo mabaya miongoni mwa watu wa Nefi, ndio, matokeo
ambayo yangekuwa chanzo cha kuongoza upinduzi wa uhuru wao.
33 Kwa hivyo Moroni alituma jeshi, na kituo chao, kuongoza watu wa Moriantoni,
kuwazuia kukimbilia nchi ya upande wa kaskazini.

34 Na ikawa kwamba hawakuwaongoza mpaka walipofikia mipaka ya nchi ya
Ukiwa; na huko waliwaongoza, kwa njia ndogo ambayo ilielekea kando ya bahari
hadi kwenye nchi upande wa kaskazini, ndio, kando ya bahari, kwenye magharibi na
kwenye mashariki.
35 Na ikawa kwamba jeshi ambalo lilitumwa na Moroni, ambalo liliongozwa na
mtu ambaye jina lake lilikuwa Teankumu, lilikutana na watu wa Moriantoni; na
watu wa Moriantoni walikuwa wakaidi sana, (wakiwa wamevutiwa na uovu wake na
maneno yake ya kujisifu) kwamba vita vilianza kati yao, ambamo Teankumu
alimuua Moriantoni na kushinda jeshi lake, na kuwachukua wafungwa, na kurudi
kwenye kituo cha Moroni. Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini na nne wa utawala
wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.
36 Na hivyo watu wa Moriantoni walirudishwa. Na baada ya maagano ya kuweka
amani walirudishwa kwenye nchi ya Moriantoni, na muungano ukafanyika
miongoni mwao na watu wa Lehi; na wao pia walirudishwa katika nchi yao.
37 Na ikawa kwamba katika mwaka huo huo kwamba imani iliimarishwa kwa watu
wa Nefi, kwamba Nefiha, mwamuzi mkuu wa pili, alifariki, akiwa amekalia kiti cha
hukumu kwa haki kamili mbele ya Mungu.
38 Walakini alikuwa amemkataza Alma kuchukua hayo maandishi na vile vitu
ambavyo viliheshimiwa na Alma na baba zake kuwa vitakatifu; kwa hivyo Alma
alikuwa amevipatia kwa mwana wake, Helamani.
39 Tazama, ikawa kwamba mwana wa Nefiha aliwekwa kwenye kiti cha hukumu,
badala ya baba yake; ndio, alifanywa kuwa mwamuzi mkuu na msimamizi juu ya
watu, kwa kiapo na agizo takatifu kuhukumu kwa haki, na kuweka amani na uhuru
wa watu, na kuwapatia mapendeleo matakatifu ya kumwabudu Bwana Mungu wao,
ndio, kusaidia na kudumisha matendo ya Mungu siku zake zote, na kuwaleta waovu
kwenye hukumu kulingana na makosa yao.
40 Sasa tazama, jina lake lilikuwa Pahorani. Na Pahorani alijaza kiti cha baba yake,
na akaanza utawala wake katika mwisho wa mwaka wa ishirini na nne, juu ya watu
wa Nefi.

## Alma 51

1 Na sasa ikawa katika mwanzo wa mwaka wa ishirini na tano wa utawala wa waamuzi
juu ya watu wa Nefi, hao wakiwa wameanzisha amani miongoni mwa watu wa Lehi
na watu wa Moriantoni kuhusu nchi zao, na wakiwa wameanza mwaka wa ishirini
na tano kwa amani;
2 Walakini, hawakudumisha amani kwa muda mrefu nchini, kwani kulianza kuwa
na ubishi miongoni mwa watu kuhusu mwamuzi mkuu Pahorani; kwani tazama,
kulikuwa na sehemu ya watu ambao walitaka kwamba sehemu fulani za sheria
ibadilishwe.
3 Lakini tazama, Pahorani hakubadilisha wala kukubali sheria ibadilishwe; kwa
hivyo, hakuwasikiliza wale ambao walikuwa wamepeleka mashauri na maombi
kuhusu kubadilishwa kwa sheria.
4 Kwa hivyo, wale ambao walitamani kwamba sheria ibadilishwe walimkasirikia,
na wakataka kwamba asiwe tena mwamuzi mkuu katika nchi; kwa hivyo kulitokea
ugomvi mkali kuhusu jambo hili, lakini damu haikumwagwa.
5 Na ikawa kwamba wale ambao walitaka kwamba Pahorani aondolewe kutoka

kiti cha hukumu walikuwa watu wa ufalme, kwani walihitaji kwamba sheria igeuzwe kwa njia ambayo ingeiondoa serikali huru na kuweka mfalme katika nchi.

6 Na wale ambao walitaka kwamba Pahorani abaki mwamuzi mkuu juu ya nchi walijiita watu huru; na hivyo ndivyo ulikuwa mgawanyiko miongoni mwao, kwani watu huru walikuwa wameapa au kutoa agano kulinda haki yao na heshima yao ya dini kwa serikali huru.

7 Na ikawa kwamba hili jambo lao la ubishi lilitulizwa kwa sauti ya watu. Na ikawa kwamba sauti ya watu ilipendelea watu huru, na Pahorani akabaki kwenye kiti cha hukumu, ambayo ilisababisha furaha nyingi miongoni mwa ndugu za Pahorani na pia watu wengi waliotaka uhuru, ambao pia waliwanyamazisha watu wa mfalme, kwamba hawakupinga lakini walihitajika kulinda mwendo wa uhuru.

8 Sasa wale ambao walipendelea wafalme walikuwa wale ambao ni wa cheo cha juu, na walitaka kuwa wafalme; na walisaidiwa na wale ambao walitaka nguvu na uwezo juu ya watu.

9 Lakini tazama, huu ulikuwa wakati wa hatari wa mabishano kuwa miongoni mwa watu wa Nefi; kwani tazama, Amalikia alikuwa amevuruga tena mioyo ya watu wa Walamani dhidi ya watu wa Wanefi, na alikuwa akikusanya pamoja askari kutoka kila sehemu ya nchi yake, na kuwahami kwa silaha, na kuwatayarisha kwa vita kwa bidii yake yote; kwani alikuwa ameapa kunywa damu ya Moroni.

10 Lakini tazama, tutaona kwamba ahadi yake aliyofanya ilikuwa ni ya upumbavu; walakini, alijitayarisha na majeshi yake kupigana dhidi ya Wanefi.

11 Sasa majeshi yake hayakuwa mengi kama vile yalivyokuwa hapo awali, kwa sababu ya maelfu wengi ambao waliuawa kwa mikono ya Wanefi; lakini ijapokuwa kupotewa kwao kwingi, Amalikia alikuwa amekusanya jeshi kubwa la ajabu, hivyo kwamba hakuogopa kuja chini kwenye nchi ya Zarahemla.

12 Ndio, hata Amalikia alikuja chini mwenyewe, mbele ya Walamani. Na ilikuwa katika mwaka wa ishirini na tano wa utawala wa waamuzi; na ilikuwa wakati huo ambao walikuwa wameanza kutatua mambo ya mabishano yao kuhusu mwamuzi mkuu, Pahorani.

13 Na ikawa kwamba wakati watu ambao waliitwa watu wa mfalme walipokuwa wamesikia kwamba Walamani wanakuja kupigana dhidi yao, walifurahi ndani ya mioyo yao; na wakakataa kuchukua silaha, kwani walimkasirikia sana mwamuzi mkuu, na pia watu wa uhuru, kwamba hawangechukua silaha kulinda nchi yao.

14 Na ikawa kwamba Moroni alipoona hivi, na pia kwamba Walamani walikuwa wanakaribia mipaka ya nchi, alikasirika sana kwa sababu ya ukaidi wa watu wale ambao alikuwa amefanyia kazi kwa bidii nyingi kuwalinda; ndio, alikasirika sana; nafsi yake ilijaa hasira dhidi yao.

15 Na ikawa kwamba alituma ombi, na sauti ya watu, kwa msimamizi wa nchi, akitaka kwamba alisome, na kumpatia (Moroni) uwezo kulazimisha hao waasi kulinda nchi yao au wauawe.

16 Kwani lilikuwa jukumu lake la kwanza kumaliza mabishano kama haya na mafarakano miongoni mwa watu; kwani tazama, hii ilikuwa mpaka sasa sababu ya maangamizo yao. Na ikawa kwamba lilikubaliwa kulingana na sauti ya watu.

17 Na ikawa kwamba Moroni aliamuru kwamba majeshi yake yaende dhidi ya watu wa ufalme, kuweka chini kiburi chao na daraja zao kubwa na kuwalainisha na ardhi, au wachukue silaha na kusaidia njia ya uhuru.

18 Na ikawa kwamba majeshi yalienda mbele dhidi yao; na yaliweka chini kiburi

chao na daraja zao kubwa, hata kwamba wakati walipoinua silaha zao za vita kupigana dhidi ya watu wa Moroni waliangushwa chini na kulainishwa na ardhi.

19 Na ikawa kwamba kulikuwa na elfu nne ya wale waasi ambao walitupwa chini kwa upanga; na wale baina ya viongozi wao ambao hawakuuawa vitani walichukuliwa na kutupwa gerezani, kwani hapakuweko na wakati wa majaribio yao wakati huo.

20 Na waasi waliosalia, badala ya kukatwa chini kwa upanga, walijitolea kwa bendera ya uhuru, na walilazimishwa kuinua jina la uhuru kwenye minara yao, na katika miji yao, na kuchukua silaha kwa kulinda nchi yao.

21 Na hivyo Moroni alikomesha wale watu wa ufalme, kwamba hapakuwa na yeyote aliyejulikana kwa jina la watu wa ufalme; na hivyo akakomesha ukaidi na kiburi cha wale watu ambao walidai damu ya wale walio bora; lakini waliletwa chini kujinyenyekea kama ndugu zao, na kupigana kwa ushujaa kwa uhuru wao kutoka kifungoni.

22 Tazama, ikawa kwamba wakati Moroni alipokuwa akiondoa vita na mabishano miongoni mwa watu wake, na kuwaweka kwa imani na utamaduni, na kutengeneza sheria kwa kujiandaa kwa vita dhidi ya Walamani, tazama, Walamani walikuwa wamekuja kwenye nchi ya Moroni, ambayo ilikuwa mipakani mwa ukingo wa bahari.

23 Na ikawa kwamba Wanefi hawakuwa na nguvu ya kutosha katika mji wa Moroni; kwa hivyo Amalikia aliwafukuza, akiua wengi. Na ikawa kwamba Amalikia alimiliki mji, ndio, alimiliki ngome zao zote.

24 Na wale ambao walikimbia kutoka mji wa Moroni walingia kwenye mji wa Nefiha; na pia watu wa mji wa Lehi walijikusanya pamoja, na wakafanya matayarisho na wakawa tayari kuwapokea Walamani kwa vita.

25 Lakini ikawa kwamba Amalikia hakuwaruhusu Walamani kwenda dhidi ya mji wa Nefiha kupigana, lakini akawaweka chini kando ya ukingo wa bahari, akiwaacha watu katika kila mji kuushika na kuulinda.

26 Na hivyo aliendelea, akimiliki miji mingi, mji wa Nefiha, na mji wa Lehi, na mji wa Moriantoni, na mji wa Omneri, na mji wa Gidi, na mji wa Muleki, yote ambayo ilikuwa mashariki mwa mipaka kando ya ukingo wa bahari.

27 Na hivyo Walamani walikuwa wamepata, kwa ujanja wa Amalikia, miji mingi sana, na wenyeji wasiohesabika, yote ambayo ilikuwa imelindwa kwa nguvu kwa njia ya ulinzi wa Moroni; yote ambayo iliwezesha ulinzi kwa Walamani.

28 Na ikawa kwamba walienda taratibu hadi kwenye mipaka ya nchi ya Neema, wakiwafukuza Wanefi mbele yao na kuua wengi.

29 Lakini ikawa kwamba walikutana na Teankumu, ambaye alikuwa amemuua Moriantoni na kuwaongoza watu wake kwa ukimbizi wake.

30 Na ikawa kwamba alimwongoza Amalikia pia, wakati alipokuwa akienda taratibu na jeshi lake la idadi kubwa kwamba angemiliki nchi ya Neema, na pia nchi upande wa kaskazini.

31 Lakini tazama alikabiliana na uchungu kwa kurudishwa nyuma na Teankumu na watu wake, kwani walikuwa mashujaa wakuu; kwani kila mtu wa Teankumu alikuwa anashinda Walamani kwa nguvu na kwa ustadi wao wa vita, hata kuwa walikuwa bora juu ya Walamani.

32 Na ikawa kwamba waliwaangamiza kwa wingi, hata kwamba waliwauwa hata mpaka kukawa na giza. Na ikawa kwamba Teankumu na watu wake walisimamisha

hema zao kwenye mipaka ya nchi ya Neema; na Amalikia akasimamisha hema zake
kwenye mipaka kwenye pwani kando ya ukingo wa bahari, na kwa njia hii
walifukuzwa.
33 Na ikawa kwamba wakati usiku ulipowadia, Teankumu na mtumishi wake
walienda nje usiku kwa kujificha, na wakaenda kwenye kituo cha Amalikia; na
tazama, usingizi ulikuwa umewalemea kwa sababu ya uchovu wao mwingi, ambao
ulisababishwa na kazi na joto la mchana.
34 Na ikawa kwamba Teankumu aliingia kwa siri hadi kwenye hema la mfalme, na
kumchoma kwa sagai kwenye moyo wake; na akasababisha kifo cha mfalme mara
moja kwamba hakuwaamusha watumishi wake.
35 Na akarudi tena kwa siri hadi kwenye kituo chake, na tazama watu wake
walikuwa wanalala, na akawaamsha na kuwaambia vitu vyote ambavyo alikuwa
amefanya.
36 Na akasababisha kwamba majeshi yake yasimame tayari, isiwe Walamani wawe
wameamka na kuwajia.
37 Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini na tano wa utawala wa waamuzi juu ya watu
wa Nefi; na hivyo zikaisha siku za Amalikia.

# Alma 52

1 Na sasa, ikawa katika mwaka wa ishirini na sita wa utawala wa waamuzi juu ya watu
wa Nefi, tazama, wakati Walamani walipoamka asubuhi ya kwanza ya mwezi wa
kwanza, tazama, walipata Amalikia amekufa katika hema lake mwenyewe; na
wakaona pia kwamba Teankumu alikuwa tayari kupigana nao siku hiyo.
2 Na sasa, wakati Walamani walipoona hivi waliogopa; na wakaacha kusudi lao la
matembezi yao ya taratibu ya kuelekea nchi ya kaskazini, na wakarudi nyuma na
majeshi yao yote katika mji wa Muleki, na wakatafuta ulinzi katika ngome zao.
3 Na ikawa kwamba kaka ya Amalikia aliwekwa kuwa mfalme juu ya watu; na jina
lake lilikuwa Amoroni; kwa hivyo mfalme Amoroni, kaka ya mfalme Amalikia,
aliwekwa kutawala badala yake.
4 Na ikawa kwamba aliamuru kwamba watu wake washikilie hiyo miji, ambayo
waliichukua kwa kumwaga damu; kwani walikuwa hawajachukua miji yoyote
isipokuwa walikuwa wamepoteza damu nyingi.
5 Na sasa, Teankumu aliona kwamba Walamani walikuwa wamekata kauli
kushikilia hiyo miji ambayo walikamata, na hizo sehemu za nchi ambazo walimiliki;
na pia akiona ukubwa wa idadi yao, Teankumu alidhani haikuwa ya kufaa kwamba
ajaribu kuwashambulia kwenye ngome zao.
6 Lakini aliweka watu wake wakazingira, kama wanaojitayarisha kwa vita; ndio, na
kweli alikuwa akijitayarisha kujilinda dhidi yao, kwa kujenga kuta kuzunguka na
kutayarisha mahali pa kukimbilia.
7 Na ikawa kwamba aliendelea hivyo kujitayarisha kwa vita mpaka Moroni
alipotuma idadi kubwa ya watu kuimarisha jeshi lake.
8 Na Moroni pia alituma maagizo kwake kwamba aweke wafungwa wote ambao
aliwakamata; kuwa kama vile Walamani walikuwa wamekamata wafungwa wengi,
kwamba aweke wafungwa wote wa Walamani kama fidia kwa wale ambao Walamani
wamekamata.
9 Na pia alituma maagizo kwake kwamba aweke ulinzi kwa nchi ya Neema, na

achunge sehemu nyembamba ambayo ilitangulia kuelekea katika nchi upande wa
kaskazini, la sivyo, Walamani wangechukua mahali hapo na wawe na uwezo wa
kuwahangaisha kwa kila upande.
10 Na Moroni pia alituma kwake, akitaka kwamba awe mwaminifu kwa kuweka
hiyo sehemu ya nchi, na kwamba atafute kila nafasi kupinga Walamani katika hiyo
sehemu, vile ingewezekana kwa nguvu yake, kwamba labda angechukua tena kwa
werevu au baadhi ya njia zingine hiyo miji ambayo ilikuwa imechukuliwa kutoka
kwa mikono yao; na kwamba pia angeimarisha na kuweka nguvu miji iliyokuwa
karibu, ambayo ilikuwa haijaanguka katika mikono ya Walamani.
11 Na pia akamwambia, ningekuja kwako, lakini tazama, Walamani wako juu yetu
kwenye mipaka ya nchi kando ya magharibi ya bahari; na tazama, ninaenda dhidi
yao, kwa hivyo siwezi kuja kwako.
12 Sasa, mfalme (Amoroni) alikuwa ameondoka nje ya nchi ya Zarahemla, na
alikuwa amemjulisha malkia kuhusu kifo cha kaka yake, na alikuwa amekusanya
idadi kubwa ya watu, na alienda mbele kuwashambulia Wanefi kwenye mipaka
kando ya bahari ya magharibi.
13 Na hivyo alikuwa anajaribu kuwahangaisha Wanefi, na kuteka sehemu ya majeshi
yao hadi sehemu ya ile nchi, wakati alikuwa ameamuru wale ambao alikuwa
amewaacha kumiliki miji ambayo alikuwa ameteka, kwamba wao pia
wawahangaishe Wanefi, kwenye mipaka kando ya bahari ya mashariki, na wamiliki
nchi yao kwa wingi vile uwezo wao ungewakubalia, kulingana na nguvu ya majeshi
yao.
14 Na hivyo ndivyo walivyokuwa Wanefi katika hizo hali za hatari kwenye mwisho
wa mwaka wa ishirini na sita wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.
15 Lakini tazama, ikawa katika mwaka wa ishirini na saba wa utawala wa waamuzi,
kwamba Teankumu, kutokana na amri ya Moroni—ambaye alikuwa ameweka
majeshi kulinda kusini na magharibi mwa mipaka ya nchi, na alikuwa ameanza
mwendo wake kuelekea nchi ya Neema, ili amsaidie Teankumu na watu wake kuteka
miji ambayo walikuwa wameipoteza—
16 Na ikawa kwamba Teankumu alikuwa amepokea amri kushambulia mji wa
Muleki, na kuuteka ikiwezekana.
17 Na ikawa kwamba Teankumu alifanya matayarisho kushambulia mji wa Muleki,
na kwenda mbele na jeshi lake dhidi ya Walamani; lakini aliona kwamba ilikuwa
vigumu kuwashinda kwa nguvu wakati walipokuwa kwa hali ya kujikinga; kwa
hivyo aliachilia mipango yake na akarudi tena kwenye mji wa Neema, kungoja
kurudi kwa Moroni, kwamba angepata nguvu kwa jeshi lake.
18 Na ikawa kwamba Moroni aliwasili na jeshi lake katika nchi ya Neema, katika
mwisho wa mwaka wa ishirini na saba wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.
19 Na katika mwanzo wa mwaka wa ishirini na nane, Moroni na Teankumu na
wengi wa makapteni wao wakuu walikuwa na baraza la vita—kutafakari ni nini
wangefanya kusababisha Walamani kuja dhidi yao kupigana; au kwamba
wawabembeleze kwa njia fulani watoke kwenye ngome zao, ili wapate kunufaika juu
yao na kuteka tena mji wa Muleki.
20 Na ikawa wakatuma wajumbe kwa jeshi la Walamani, ambalo lililinda mji wa
Muleki, kwa kiongozi wao, ambaye jina lake lilikuwa Yakobo, wakimhitaji yeye
atoke nje na majeshi yake kukutana nao kwenye uwanda kati ya hiyo miji miwili.
Lakini tazama, Yakobo, ambaye alikuwa Mzorami, hangekuja na jeshi lake kuwakuta

kwenye uwanda.
21 Na ikawa kwamba Moroni, akiwa hana matumaini ya kukutana nao kwenye hali
iliyo sawa, kwa hivyo, alifikiria mpango ambao ungewashawishi Walamani watoke
nje ya ngome zao.
22 Kwa hivyo alisababisha kwamba Teankumu achukue idadi ndogo ya watu
waende chini karibu na ukingo wa bahari; na Moroni na jeshi lake, usiku,
walitembea katika nyika, magharibi mwa mji wa Muleki; na hivyo, kesho yake,
wakati walinzi wa Walamani walipomgundua Teankumu, walikimbia na
kumwambia Yakobo, kiongozi wao.
23 Na ikawa kwamba majeshi ya Walamani yalienda mbele dhidi ya Teankumu,
yakidhani kwa sababu ya idadi yao yangemshinda Teankumu kwa sababu ya uchache
wa idadi yake. Na Teankumu alipoona majeshi ya Walamani yakija dhidi yake
alianza kurudi nyuma kando ya ukingo wa bahari upande wa kaskazini.
24 Na ikawa kwamba wakati Walamani walipoona kwamba ameanza kutoroka,
walijipa moyo na kuwafuata kwa nguvu. Na wakati Teankumu alikuwa
anawaongoza mbali Walamani ambao walikuwa wakiwafukuza bila kufaulu, tazama,
Moroni aliamuru kwamba sehemu ya jeshi lake ambao walikuwa na yeye waende
kwa utaratibu hadi kwenye mji, na kuumiliki.
25 Na hivyo ndivyo walivyofanya, na wakawachinja wale wote ambao waliachwa
nyuma kuulinda mji, ndio, wale wote ambao hawakutaka kusalimisha silaha zao za
vita.
26 Na hivyo Moroni alipata kuumiliki mji wa Muleki na sehemu ya jeshi lake,
wakati alienda taratibu na waliosalia kukabiliana na Walamani wakiwa wamerudi
kutoka kumfukuza Teankumu.
27 Na ikawa kwamba Walamani walimfukuza Teankumu mpaka wakaja karibu na
mji wa Neema, na pale wakakutana na Lehi na jeshi dogo, ambalo lilikuwa
limeachwa kulinda mji wa Neema.
28 Na sasa tazama, wakati makapteni wakuu wa Walamani walipomwona Lehi na
jeshi lake wakija dhidi yao, walikimbia kwa kuchanganyikiwa kwingi, wakiogopa
labda hawataufikia mji wa Muleki kabla Lehi hajawapata; kwani walichoka kwa
sababu ya mwendo wao, na watu wa Lehi walikuwa na nguvu.
29 Sasa Walamani hawakujua kwamba Moroni alikuwa nyuma yao na jeshi lake; na
wale waliogopa alikuwa Lehi na watu wake.
30 Sasa Lehi hakuwa na tamaa ya kuwapita mpaka wakutane na Moroni na jeshi
lake.
31 Na ikawa kwamba kabla ya Walamani kurudi nyuma mbali walizungukwa na
Wanefi, na watu wa Moroni pande moja, na watu wa Lehi upande mwingine, wote
ambao walikuwa na nguvu; lakini Walamani walikuwa wamechoka kwa sababu ya
matembezi yao marefu.
32 Na Moroni akawaamuru watu wake kwamba wawaangukie mpaka watakapotoa
silaha zao za vita.
33 Na ikawa kwamba Yakobo, akiwa kiongozi wao, pia akiwa Mzorami, na akiwa na
roho isiyoshindika, aliwatangulia Walamani mbele kupigana kwa ukatili mwingi
dhidi ya Moroni.
34 Moroni akiwa kwa njia yao ya matembezi, kwa hivyo Yakobo alikuwa ameamua
kuwaua na kukatiza njia yake hadi katika mji wa Muleki. Lakini tazama, Moroni na
watu wake walikuwa na nguvu zaidi; kwa hivyo hawakujilegeza mbele ya Walamani.

35 Na ikawa kwamba walipigana kwa pande zote mbili na ghadhabu kali sana; na
kulikuwa wengi waliouawa pande zote mbili; ndio, na Moroni alijeruhiwa na
Yakobo akauawa.
36 Na Lehi aliwashambulia kutoka nyuma yao kwa nguvu sana na watu wake wenye
nguvu, kwamba Walamani waliokuwa nyuma walisalimisha silaha zao za vita; na
waliosalia, walichanganyikiwa, na hawakujua mahali pa kwenda au kupiga.
37 Sasa Moroni alipoona kuchanganyikiwa kwao, aliwaambia: Ikiwa mtaleta mbele
silaha zenu za vita na kuzisalimisha, tazama, tutaacha kumwaga damu yenu.
38 Na ikawa kwamba wakati Walamani waliposikia haya maneno, makapteni wao
wakuu, wale wote ambao hawakuuawa, walikuja mbele na kutupa chini silaha zao za
vita miguuni mwa Moroni, na pia wakawaamuru watu wao kwamba wafanye hivyo.
39 Lakini tazama, kulikuwa na wengi ambao hawakufanya hivyo; na wale ambao
hawakutoa panga zao walichukuliwa na kufungwa, na silaha zao za vita
zilichukuliwa kutoka kwao, na walilazimishwa kutembea na ndugu zao hadi kwenye
nchi ya Neema.
40 Na sasa idadi ya wafungwa ambao walikamatwa ilizidi idadi ya wale ambao
waliuawa, ndio, zaidi ya wale ambao waliuawa katika pande zote mbili.

# Alma 53

1 Na ikawa kwamba waliweka walinzi juu ya wafungwa wa Walamani, na
kuwalazimisha kwenda kuzika wafu wao, ndio, na pia wafu wa Wanefi ambao
waliuawa; na Moroni aliweka watu kuwachunga wakati walipokuwa wakifanya kazi
zao.
2 Na Moroni akaenda kwenye mji wa Muleki na Lehi, na akachukua mji na
kuukabidhi kwa Lehi. Sasa tazama, huyu Lehi alikuwa ni mtu ambaye alikuwa
pamoja na Moroni katika sehemu nyingi katika vita vyake vyote; na alikuwa na tabia
kama ya Moroni, na walifurahia usalama wa kila mmoja wao; ndio, walikuwa
wanapendana, na pia kupendwa na watu wote wa Nefi.
3 Na ikawa kwamba baada ya Walamani kumaliza kuzika wafu wao na pia wafu wa
Wanefi, walitembezwa na kurudishwa kwenye nchi ya Neema; na Teankumu, kwa
amri ya Moroni, alisababisha kwamba waanze kufanya kazi ya kuchimba handaki
kuzunguka ile nchi, au mji, wa Neema.
4 Na alisababisha kwamba wajenge ukuta wa mbao ndani ya ukingo wa shimo; na
wakatupa uchafu wa shimo juu ya ukuta wa mbao; na hivyo walisababisha
Walamani kufanya kazi mpaka walipouzunguka mji wa Neema kwa ukuta imara wa
mbao na mchanga, kwa kimo kirefu sana.
5 Na huu mji ukawa imara sana kuanzia pale kuendelea mbele; na ndani ya mji huu
walilinda wafungwa wa Walamani; ndio, hata nyuma ya ukuta ambao
waliwasababisha kujenga kwa mikono yao. Sasa Moroni alilazimishwa kusababisha
Walamani kufanya kazi, kwa sababu ilikuwa rahisi kuwalinda wakiwa kazini mwao;
na alihitaji majeshi yake yote wakati alipotaka kuwashambulia Walamani.
6 Na ikawa kwamba Moroni alikuwa amepata ushindi kwa mojawapo ya jeshi
kubwa la Walamani, na alikuwa amemiliki mji wa Muleki, ambao ulikuwa
mojawapo ya ngome imara za Walamani katika nchi ya Nefi; na hivyo alikuwa
amejenga ngome imara ya kuweka wafungwa wake.
7 Na ikawa kwamba hakujaribu tena kupigana na Walamani katika mwaka huo,

lakini aliweka watu wake kujitayarisha kwa vita, ndio, na kwa kujenga ngome za
kujikinga kutokana na Walamani, ndio, na kwa pia kuwaokoa wake zao na watoto
wao kutokana na njaa na mateso, na kutoa chakula kwa majeshi yao.
8 Na sasa ikawa kwamba majeshi ya Walamani, upande wa bahari ya magharibi,
kusini, wakati Moroni alipokuwa hayuko kwa ajili ya hila fulani miongoni mwa
Wanefi, ambayo ilisababisha mafarakano miongoni mwao, yalikuwa yamepata faida
juu ya Wanefi, ndio, hata kwamba walikuwa wamepata kumiliki kiasi cha miji yao
katika sehemu hio ya nchi.
9 Na hivyo kwa sababu ya uovu miongoni mwao, ndio, kwa sababu ya mafarakano
na hila miongoni mwao, walikuwa wamewekwa kwenye hali mbaya sana.
10 Na sasa tazama, nina machache ya kusema kuhusu watu wa Amoni, ambao,
mwanzoni, walikuwa Walamani; lakini kwa sababu ya Amoni na ndugu zake, kwa
usahihi zaidi kwa uwezo na neno la Mungu, walikuwa wamemgeukia Bwana; na
walikuwa wameletwa chini katika nchi ya Zarahemla, na tangu hapo walikuwa
wamelindwa na Wanefi.
11 Na kwa sababu ya kiapo chao walikuwa wamekatazwa kuchukua silaha dhidi ya
ndugu zao; kwani walikuwa wamekula kiapo kwamba kamwe hawatamwaga damu;
na kulingana na kiapo chao wangekuwa wameangamia; ndio, wangekubali wenyewe
kuanguka mikononi mwa ndugu zao, kama haingekuwa huruma na mapenzi mengi
ambayo Amoni na ndugu zake walikuwa nayo kwao.
12 Na kwa sababu hii waliletwa chini katika nchi ya Zarahemla; na tangu hapo
daima walikuwa wamelindwa na Wanefi.
13 Lakini ikawa kwamba wakati walipoona hatari, na mateso mengi na taabu
ambazo Wanefi walihimili kwao, walijazwa na huruma na wakataka kuchukua silaha
kwa kulinda nchi yao.
14 Lakini tazama, vile walipokuwa karibu kuchukua silaha zao za vita,
walisadikishwa na kushawishiwa na Helamani na ndugu zake, kwani walikuwa
karibu kuvunja kiapo ambacho walikuwa wamefanya.
15 Na Helamani aliogopa isije wapoteze nafsi zao; kwa hivyo wale wote ambao
waliingia kwenye agano hili walilazimishwa kutazama ndugu zao wakipitia kwenye
mateso yao, kwenye hali yao ya hatari wakati huu.
16 Lakini tazama, ikawa kwamba walikuwa na wana wengi, ambao hawakuingia
kwenye hilo agano kwamba hawatachukua silaha za vita kujilinda wenyewe dhidi ya
maadui zao; kwa hivyo walijikusanya pamoja wakati huu, wengi vile wangeweza
kuchukua silaha, na wakajiita Wanefi.
17 Na wakaingia katika agano kupigania uhuru wa Wanefi, ndio, kulinda nchi hata
kwa kutoa maisha yao; ndio, hata waliapa kwamba hawataachilia kamwe uhuru wao,
lakini watapigana kwa njia zote kulinda Wanefi na wenyewe kutokana na kifungo.
18 Sasa tazama, kulikuwa elfu mbili ya hao vijana, ambao walifanya agano hili na
wakachukua silaha zao za vita kulinda nchi yao.
19 Na sasa tazama, kwa vile mbeleni hawakuwa zuio kwa Wanefi, walikuwa sasa
katika wakati huu usaidizi mkuu; kwani walichukua silaha zao za vita, na wakataka
kwamba Helamani awe kiongozi wao.
20 Na wote walikuwa vijana, na walikuwa mashujaa kwa uhodari, na pia kwa nguvu
na vitendo; lakini tazama, hii haikuwa yote — walikuwa watu wa ukweli wakati wote
kwa kitu chochote ambacho walikabidhiwa.
21 Ndio, walikuwa watu wa ukweli na wenye busara, kwani walikuwa

wamefundishwa kutii amri za Mungu na kutembea wima mbele yake.
22 Na sasa ikawa kwamba Helamani alitembea mbele ya askari wake vijana elfu
mbili, kwa kusaidia watu walio kuwa mipakani mwa nchi kusini kando ya bahari ya
magharibi.
23 Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini na nane wa utawala wa waamuzi juu ya watu
wa Nefi.

# Alma 54

1 Na sasa ikawa katika mwanzo wa mwaka wa ishirini na tisa wa waamuzi, kwamba
Amoroni alituma kwa Moroni akitaka kwamba abadilishe wafungwa.
2 Na ikawa kwamba Moroni alifurahi sana kwa ombi hili, kwani alitaka chakula
ambacho kilitolewa kwa kuwasaidia wafungwa Walamani kiwe kwa kuwasaidia
watu wake wenyewe; na pia aliwataka watu wake kwa kuimarisha jeshi lake.
3 Sasa Walamani walikuwa wamechukua wanawake wengi na watoto, na hapakuwa
na mwanamke wala mtoto miongoni mwa wafungwa wa Moroni, au wafungwa
ambao Moroni alikuwa amewakamata; kwa hivyo Moroni alikusudia kupata hila ya
kupokea wafungwa wengi wa Wanefi kutoka kwa Walamani vile ingewezekana.
4 Kwa hivyo aliandika waraka, na ukapelekwa na mtumishi wa Amoroni, yule yule
aliyemletea Moroni waraka. Sasa haya ndiyo maneno ambayo alimwandikia
Amoroni, akisema:
5 Tazama, Amoroni, nimekuandikia wewe maoni yangu kuhusu hivi vita ambavyo
umepigana dhidi ya watu wangu, kwa usahihi zaidi ambavyo kaka yako amepigana
dhidi yao, na ambavyo bado unataka kuendelea navyo baada ya kifo chake.
6 Tazama, ningekwambia kidogo kuhusu haki ya Mungu, na upanga wa ghadhabu
yake kubwa, ambayo inaning'inia juu yako isipokuwa utubu na kuondoa majeshi
yako na kuyapeleka kwa nchi zako, au nchi unayomiliki, ambayo ni nchi ya Nefi.
7 Ndio, ningekwambia vitu hivi ikiwa ungekuwa na uwezo wa kuvitii; ndio,
ningekwambia kuhusu ile jahanamu ya kutisha ambayo inangojea kupokea wauaji
kama wewe na kaka yako, msipotubu na kuondoa kusudi lenu la mauaji, na mrudi
na majeshi yenu kwenye nchi zenu.
8 Lakini vile wakati mmoja umekataa vitu hivi, na umepigana dhidi ya watu wa
Bwana, hata hivyo natazamia utafanya hivyo tena.
9 Na sasa tazama, tuko tayari kukupokea; ndio, na isipokuwa uondoe kusudi lako,
tazama, utavuta chini ghadhabu ya Mungu ambaye umemkataa kwako, hata kwenye
uangamizo wako.
10 Lakini, vile Bwana anaishi, majeshi yetu yatawajia isipokuwa mwondoke, na hivi
karibuni mtatembelewa na kifo, kwani tutahifadhi miji yetu na nchi zetu; ndio, na
tutahifadhi dini yetu na njia ya Mungu wetu.
11 Lakini tazama, mimi nadhani kwamba ninakuzungumzia kuhusu hivi vitu bure;
au nadhani kwamba wewe ni mtoto wa jahanamu; kwa hivyo nitamaliza barua
yangu kwa kukwambia kwamba sitabadilisha wafungwa, isipokuwa iwe kwamba
utarudisha mwanaume na mkewe na watoto wake, kwa mfungwa mmoja; ikiwa hivi
ndivyo itakuwa kwamba utaifanya, nitakubali.
12 Na tazama ikiwa hutafanya hivi, nitakushambulia na majeshi yangu; ndio, hata
nitawahami wanawake wangu kwa silaha na watoto wangu, na nitakuja dhidi yako,
na nitakufuata wewe hadi hata kwenye nchi yako, ambayo ilikuwa nchi ya kwanza ya

urithi wetu; ndio, na itakuwa damu kwa damu, ndio, uzima kwa uzima; na
nitakupiganisha vita hata mpaka wakati utaangamizwa kutoka kwenye uso wa dunia.
13 Tazama, niko kwenye hasira yangu, na pia watu wangu; mmefikiri kutuua sisi, na
sisi tumefikiri tu kujilinda wenyewe. Lakini tazama, kama mnafikiri kutuangamiza
sisi, tutatafuta kuwaangamiza; ndio, na tutatafuta nchi yetu, nchi ya kwanza ya
urithi wetu.
14 Sasa nafunga barua yangu. Mimi ni Moroni; mimi ni kiongozi wa watu wa
Wanefi.
15 Sasa ikawa kwamba Amoroni, alipopata barua hii, alikasirika; na akaandika
barua ingine kwa Moroni, na haya ndiyo maneno ambayo aliandika, akisema:
16 Mimi ni Amoroni, mfalme wa Walamani; mimi ni kaka ya Amalikia ambaye
ulimwua. Tazama, nitalipiza damu yake kwako, ndio, na nitakuja kwako na majeshi
yangu kwani siogopi vitisho vyako.
17 Kwani tazama, babu zenu waliwakosea kaka zao, hata kwamba wakawaibia haki
yao kwa serikali wakati ilikuwa ni yao.
18 Na sasa tazama, ikiwa mtaweka chini silaha zenu, na mkubali wenyewe
kutawaliwa na wale ambao serikali ni yao, ndipo nitasababisha kwamba watu wangu
waweke chini silaha zao na hatutakuwa na vita tena.
19 Tazama, umetoa vitisho vingi sana dhidi yangu na watu wangu; lakini tazama,
hatuogopi vitisho vyako.
20 Walakini, nitakubali kubadilisha wafungwa kulingana na ombi lako, kwa furaha,
kwamba niweke chakula changu kwa watu wangu wa vita; na tutapigana vita
ambavyo vitakuwa vya milele, kuwaweka Wanefi chini ya utawala wetu au kwa
kuangamizwa kwao kwa milele.
21 Na kuhusu yule Mungu ambaye unasema ati tumemkataa, tazama, hatujui
kiumbe kama hicho; wala wewe; lakini kama kuna kiumbe kama hicho, hatujui
lakini ametuumba sisi na wewe pia.
22 Na ikiwa hivyo kwamba kuna ibilisi na jahanamu, tazama si atakupeleka wewe
huko upate kuishi na kaka yangu ambaye ulimuua, ambaye ulidokeza kwamba
ameenda mahali kama hapo? Lakini vitu hivi havijalishi.
23 Mimi ni Amoroni, na kizazi cha Zoramu, ambaye babu zako walimlemea na
kumtoa nje ya Yerusalemu.
24 Na tazama, mimi ni Mlamani jasiri; tazama, hivi vita vimeanzishwa kulipiza
mabaya yao, na kuhifadhi na kuweka haki zao kwa serikali; na ninafunga barua
yangu kwa Moroni.

# Alma 55

1 Sasa ikawa kwamba Moroni alipopokea hii barua alikasirika zaidi, kwa sababu alijua
kwamba Amoroni alikuwa na fahamu kamili ya hila yake; ndio, alijua kwamba
Amoroni alijua kwamba haikuwa sababu ya haki ambayo ilimsababisha kuanzisha
vita dhidi ya watu wa Nefi.
2 Na akasema: Tazama, sitabadilisha wafungwa na Amoroni isipokuwa aondoe
kusudi lake, vile nimeeleza kwenye barua yangu; kwani sitamkubalia kwamba awe
na uwezo kuliko ule anao.
3 Tazama, najua mahali ambapo Walamani wanasimamia watu wangu ambao
wamewachukua wafungwa; na kwa vile Amoroni hataki kukubaliana na barua

yangu, tazama, nitampatia kulingana na maneno yangu; ndio, nitatafuta kifo miongoni mwao mpaka watakapoomba amani.

4 Na sasa ikawa kwamba wakati Moroni alikuwa amesema maneno haya, alisababisha kwamba msako ufanywe miongoni mwa watu wake, kwamba labda angepata mtu ambaye alikuwa wa uzao wa Lamani miongoni mwao.

5 Na ikawa kwamba walimpata mmoja, ambaye jina lake lilikuwa Lamani; na alikuwa mmojawapo wa watumishi wa mfalme ambaye aliuawa na Amalikia.

6 Sasa Moroni alisababisha kwamba Lamani na idadi ndogo ya watu wake waende mbele hadi kwenye walinzi ambao walikuwa wanalinda Wanefi.

7 Sasa Wanefi walisimamiwa kwenye mji wa Gidi; kwa hivyo Moroni alimchagua Lamani na kusababisha kwamba idadi ndogo ya watu iende na yeye.

8 Na kulipokuwa usiku Lamani aliwaendea walinzi waliokuwa juu ya Wanefi, na tazama, walimwona akija na wakamuita; lakini aliwaambia: Msiogope; tazama, mimi ni Mlamani. Tazama, tumetoroka kutoka kwa Wanefi, na wanalala; na tazama tumechukua baadhi ya divai yao na kuja nayo.

9 Sasa wakati Walamani waliposikia haya maneno walimpokea kwa shangwe; na wakamwambia: Tupatie divai yako, ili tunywe; tuna furaha kwamba ulichukua divai ukaja nayo kwani sisi tumechoka.

10 Lakini Lamani aliwaambia: Acha sisi tuweke divai yetu mpaka tutakapoenda dhidi ya Wanefi kupigana. Lakini kusema hivi kuliwafanya kuwa na tamaa zaidi ya kutaka kunywa divai;

11 Kwani, walisema: Tumechoka, kwa hivyo acha tunywe divai, na baadaye tutapata divai kwa posha yetu, ambayo itatuimarisha kwenda dhidi ya Wanefi.

12 Na Lamani akawaambia: Mnaweza kufanya kulingana na vile mnavyotaka.

13 Na ikawa kwamba walikunywa divai bila kuzuiliwa; na ilikuwa nzuri walipoionja, kwa hivyo waliinywa kwa wingi; na ilikuwa kali, ikiwa imetayarishwa na nguvu yake.

14 Na ikawa walikunywa na wakafurahi, na baadaye wote walilewa.

15 Na sasa Lamani na watu wake walipoona kwamba wote wamelewa, na wamelala sana, walimrudia Moroni na kumwelezea vitu vyote vilivyotendeka.

16 Na sasa hii ilikuwa kulingana na mpango wa Moroni. Na Moroni alikuwa ametayarisha watu wake na silaha za vita; na akaenda kwenye mji wa Gidi, wakati Walamani walipokuwa katika usingizi mkubwa na wamelewa, na akawatupia wafungwa silaha za vita, mpaka walikuwa wote wamejihami kwa silaha;

17 Ndio, hata kwa wanawake wao, na kwa wale watoto wao wote, wote ambao wangeweza kutumia silaha ya vita, wakati Moroni alikuwa amewaami kwa silaha wale wafungwa wote; na hivyo vitu vyote vilifanyika kwenye unyamavu mkuu.

18 Lakini kama wangewaamsha Walamani, tazama walikuwa wamelewa na Wanefi wangewachinja.

19 Lakini tazama, hii haikuwa tamaa ya Moroni; hakufurahia mauaji au umwagaji wa damu, lakini alifurahia kuokoa watu wake kutoka maangamizo; na kwa hii sababu hakutaka kujiletea yasiyo ya haki, hakuwashambulia Walamani na kuwaangamiza katika ulevi wao.

20 Lakini alikuwa amepata mahitaji yake; kwani alikuwa amewahami kwa silaha wafungwa wa Wanefi ambao walikuwa ndani ya ukuta wa mji, na alikuwa amewapatia uwezo kupata umiliki wa zile sehemu ambazo zilikuwa ndani ya kuta.

21 Na kisha akasababisha wale watu ambao walikuwa na yeye warudi nyuma kiwango fulani kutoka kwao, na kuzunguka majeshi ya Walamani.

22 Sasa tazama hii ilifanyika wakati wa usiku, ili wakati Walamani walipoamka asubuhi waliona kwamba wamezungukwa na Wanefi nje ya ukuta, na kwamba wafungwa wao walikuwa wamejihami kwa silaha ndani.

23 Na hivyo waliona kwamba Wanefi walikuwa na nguvu juu yao; na kwa hali hii waliona kwamba haikuwa ya manufaa kupigana na Wanefi; kwa hivyo makapteni wao wakuu waliitisha silaha zao za vita, na wakazileta mbele na kuzitupa miguuni mwa Wanefi, wakiomba kuonewa huruma.

24 Sasa tazama, hili lilikuwa pendeleo la Moroni. Aliwachukua kuwa wafungwa wa vita na kuumiliki mji, na kusababisha kwamba wafungwa wote waachiliwe, ambao walikuwa Wanefi; na wakajiunga na jeshi la Moroni, na waliongeza nguvu nyingi katika jeshi lake.

25 Na ikawa kwamba alisababisha Walamani, ambao alikuwa amechukua wafungwa, kwamba waanze kazi ya kuimarisha ulinzi kuzunguka mji wa Gidi.

26 Na ikawa kwamba alipoimarisha mji wa Gidi, kulingana na mahitaji yake, alisababisha kwamba wafungwa wake wapelekwe kwenye mji wa Neema; na pia akalinda huo mji kwa nguvu nyingi.

27 Na ikawa kwamba, licha ya hila za Walamani, waliwaweka na kuwalinda wafungwa wote ambao walikuwa wamewachukua, na pia kudumisha ardhi yote na faida ambayo walikuwa wamechukua tena.

28 Na ikawa kwamba Wanefi walianza tena kuwa washindi, na kudai haki zao na mapendeleo yao.

29 Mara nyingi Walamani walijaribu kuwazunguka usiku, lakini kwa haya majaribio walipoteza wafungwa wengi.

30 Na safari nyingi walijaribu kutoa divai kwa Wanefi, ili wawaangamize na sumu au ulevi.

31 Lakini tazama, Wanefi hawakuwa wapole kumkumbuka Bwana Mungu wao kwa huu wakati wa mateso. Hawakuanguka katika mitego yao; ndio, hawakunywa divai yao, isipokuwa wawe wamewapatia kwanza wafungwa wa Walamani.

32 Na wakawa hivyo waangalifu kwamba sumu yoyote isikatolewe miongoni mwao; kwani divai ikimuua Mlamani kadhalika itamuua Mnefi; na hivyo ndivyo walijaribu pombe yao yote.

33 Na ikawa kwamba ilikuwa ya maana kuwa Moroni afanye mipango kushambulia mji wa Moriantoni; kwani tazama, Walamani walikuwa, kwa kazi yao, wameimarisha mji wa Moriantoni mpaka ukawa wenye nguvu sana.

34 Na walikuwa kila wakati wakileta askari wapya katika mji, na pia ruzuku mpya za vyakula.

35 Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini na tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

# Alma 56

1 Na sasa ikawa katika mwanzo wa mwaka wa thelathini wa utawala wa waamuzi, katika siku ya pili katika mwezi wa kwanza, Moroni alipata barua kutoka kwa Helamani, akieleza hali ya watu kwenye eneo hilo la nchi.

2 Na haya ndiyo maneno ambayo aliandika, akisema: Ndugu yangu mpendwa, Moroni, pamoja katika Bwana vile ilivyo katika taabu ya vita vyetu; tazama, ndugu yangu mpendwa, nina kitu kukwambia kuhusu vita vyetu katika sehemu hii ya nchi.

3 Tazama, elfu mbili ya wana wa wale watu ambao Amoni alileta kutoka nchi ya
Nefi—sasa umejua kwamba hawa walikuwa zao la Lamani, ambaye alikuwa
kifungua mimba wa babu yetu Lehi;
4 Sasa sihitaji kukariri kwako kuhusu desturi au kutoamini kwao, kwani unajua
kuhusu vitu hivi vyote—
5 Kwa hivyo inanitosheleza kwamba nikuambie kuwa elfu mbili ya hawa vijana
wamechukua silaha zao za vita, na wanataka kwamba niwe kiongozi wao; na
tumekuja mbele kulinda nchi yetu.
6 Na sasa unajua pia kuhusu agano ambalo baba zao walifanya, kwamba
hawatachukua silaha zao za vita dhidi ya ndugu zao kumwaga damu.
7 Lakini katika mwaka wa ishirini na sita, wakati walipoona mateso yetu na taabu
zetu kwao, walikuwa karibu kuvunja hilo agano ambalo walikuwa wamefanya na
wachukue silaha zao za vita kwa ulinzi wetu.
8 Lakini singewakubalia kwamba wavunje hili agano ambalo walifanya, nikiamini
kwamba Mungu atatuweka nguvu, hivyo kwamba tusiumie zaidi kwa sababu ya
kutimiza kiapo ambacho walikuwa wamechukua.
9 Lakini tazama, hapa kuna kitu kimoja ambacho kingetupatia shangwe kuu.
Kwani tazama, katika mwaka wa ishirini na sita, mimi, Helamani, nilitembea mbele
nikiwaongoza hawa vijana elfu mbili hadi mji wa Yuda, kumsaidia Antipo, ambaye
ulikuwa umemchagua kiongozi juu ya wale watu wa sehemu ile ya nchi.
10 Na nilijiunga na wana wangu elfu mbili (kwani wanastahili kuitwa wana) kwa
jeshi la Antipo, ambamo kwa nguvu hii Antipo alifurahi sana; kwani tazama, jeshi
lake lilikuwa limepunguzwa na Walamani kwa sababu majeshi yao yalikuwa yameua
idadi kubwa ya watu wetu, ambayo inatupatia sababu ya kuomboleza.
11 Walakini, tunaweza kujituliza kwenye hili jambo, kwamba wamefariki kwa
sababu ya nchi yao na Mungu wao, ndio, na wana furaha.
12 Na Walamani walikuwa pia wameweka wafungwa wengi, wote ambao walikuwa
makapteni wakuu, kwani hakuna yeyote ambaye waliachwa mzima. Na tunadhani
kwamba sasa wakati huu wako kwenye nchi ya Nefi; ni hivyo kama hawajauawa.
13 Na sasa hii ndiyo miji ambayo Walamani wamepata kumiliki kwa kumwaga
damu ya wengi wa mashujaa wa watu wetu:
14 Nchi ya Manti, au mji wa Manti, na mji wa Zeezromu, na mji wa Kumeni, na mji
wa Antipara.
15 Na hii ndiyo miji ambayo walimiliki wakati nilipofika katika mji wa Yuda; na
nilimpata Antipo na watu wake wakifanya kazi kwa bidii kuimarisha mji.
16 Ndio, na walikuwa wamedhoofishwa kwa mwili na roho, kwani walipigana kwa
ushujaa mchana na kufanya kazi usiku kuhifadhi miji yao; na hivyo walivumilia
mateso makubwa ya kila aina.
17 Na sasa walikuwa wamekata kauli washinde mahali hapa au wafe; kwa hivyo
unaweza kudhani kwamba hili jeshi dogo ambalo nilileta, ndio, wale wana wangu,
waliwapatia matumaini makubwa na shangwe nyingi.
18 Na sasa ikawa kwamba Walamani walipoona kwamba Antipo amepata nguvu
nyingi zaidi kwa jeshi lake, walilazimishwa kwa amri za Amoroni kutokuja dhidi ya
mji wa Yuda, au dhidi yetu kupigana.
19 Na hivyo tulibarikiwa na Bwana; kwani kama wangekuja katika wakati wa
udhaifu wetu labda wangeangamiza hili jeshi letu dogo; lakini hivyo tulihifadhiwa.
20 Waliamrishwa na Amoroni kulinda hiyo miji ambayo walikuwa wameikamata.

Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini na sita. Na kwenye mwanzo wa mwaka wa ishirini na saba tulikuwa tumeandaa mji wetu na sisi wenyewe kwa ulinzi.

21 Sasa tulikuwa tunataka kwamba Walamani watujie sisi; kwani hatukutaka kufanya mashambulizi juu yao kwenye ngome zao.

22 Na ikawa kwamba tuliweka wapelelezi nje huku na huko, kuchunguza mwenendo wa Walamani, kwamba wasitupite wakati wa usiku ama mchana kufanya mashambulizi juu ya miji yetu mingine ambayo ilikuwa upande wa kaskazini.

23 Kwani tulijua katika hiyo miji hawakuwa na nguvu ya kutosha kukutana nao; kwa hivyo tulikuwa tunatamani, kama wangepita karibu nasi, tuwavamie kutoka nyuma na hivyo kuwazuia kutoka nyuma, kwa wakati sawa walipokabiliwa kutoka mbele. Tulidhani kwamba tungewashinda; lakini tazama, hatukufanikiwa katika hii tamaa yetu.

24 Hawakuthubutu kutupita na jeshi lao lote, wala sehemu yake, isiwe wasiwe na nguvu ya kutosha na washindwe.

25 Wala hawakuthubutu kwenda chini dhidi ya mji wa Zarahemla; wala kuvuka chimbuko la Sidoni, hadi kwenye mji wa Nefiha.

26 Na hivyo, kwa majeshi yao, walikata kauli kulinda hiyo miji ambayo walikuwa wameikamata.

27 Na sasa ikawa katika mwezi wa pili wa mwaka huu, tuliletewa vyakula vingi kutoka kwa baba za wale vijana wangu elfu mbili.

28 Na pia kulitumwa watu elfu mbili kwetu kutoka Zarahemla. Na hivyo tulijitayarisha na watu elfu kumi, na vyakula kwao, na pia kwa wake zao na watoto wao.

29 Na Walamani, hivyo wakiona majeshi yetu yakiongezeka kila siku, na vyakula vikiletwa kwa usaidizi wetu, walianza kuogopa, na wakaanza kutoka kwa ghafula, kama ikiwezekana watukatize ili tusipokee chakula na kuongezewa nguvu.

30 Sasa wakati tulipoona kwamba Walamani wanaanza kuwa na wasiwasi kwa jinsi hii, tulitaka kutumia hila juu yao; kwa hivyo Antipo aliamuru kwamba niende mbele na wana wangu wachanga kwenye mji jirani, tukijifanya kama tunabeba vyakula hadi kwenye mji jirani.

31 Na tulipaswa kusafiri karibu na mji wa Antipara, kama tulikuwa tunaenda upande wa ng'ambo ya pili, kwenye mipaka karibu na ukingo wa bahari.

32 Na ikawa kwamba tulienda mbele, kama tuliokuwa na vyakula vyetu, kwenda kwenye mji huo.

33 Na ikawa kwamba Antipo alienda mbele na sehemu ya jeshi lake, akiacha waliosalia kulinda mji. Lakini hakuenda mbele mpaka nilipoenda mbele na jeshi langu dogo, na kuja karibu na mji wa Antipara.

34 Na sasa kwenye mji wa Antipara kulikuwa kumewekwa jeshi la Walamani la nguvu kuliko yote; ndio, lile kubwa sana.

35 Na ikawa kwamba walipokuwa wamearifiwa na wapelelezi wao, walikuja nje na jeshi lao kutushambulia.

36 Na ikawa kwamba tulitoroka mbele yao, kuelekea kaskazini. Na hivyo tukaongoza mbali jeshi lenye nguvu la Walamani;

37 Ndio, hata kwa mwendo mrefu sana, mpaka kwamba walipoona jeshi la Antipo likiwafuata kwa nguvu zao, hawakugeuka kulia wala kushoto, lakini waliendelea kutufuata, kwa mwendo mnyoofu; na, vile tunadhani, lilikuwa kusudi lao kutuua sisi kabla ya Antipo kuwapita, na hivi kwamba wasizungukwe na watu wetu.

38 Na sasa Antipo, alipoona hatari yetu, aliongeza mwendo wa jeshi lake. Lakini tazama, kulikuwa ni usiku, kwa hivyo hawakutupata, wala Antipo hakuwafikia; kwa hivyo tulipiga hema wakati wa usiku.

39 Na ikawa kwamba kabla ya kupambazuka asubuhi, tazama, Walamani walikuwa wanatufuata. Sasa hatukuwa na nguvu kadiri ya kutosha kupigana nao; ndio, singekubali kwamba vijana wangu wadogo waanguke mikononi mwao; kwa hivyo tuliendelea na mwendo wetu, na tukachukua mwendo wetu hadi nyikani.

40 Sasa hawangethubutu kugeuka kwa kulia wala kushoto wakiogopa kuzungukwa; wala singegeuka kulia wala kushoto wasije wakanipita, na hatungeshindana nao, lakini tuuawe, na wangetoroka; na hivyo tukakimbia hio siku yote kwenye nyika, mpaka kulipokuwa na giza.

41 Na ikawa kwamba tena, wakati mwangaza wa asubuhi ulipotokea, tuliona Walamani walikuwa wametupata na tukawakimbia.

42 Lakini ikawa kwamba hawakutufuata mbali kabla ya wao kusimama; na ilikuwa ni asubuhi ya siku ya tatu ya mwezi wa saba.

43 Na sasa, kama walipatwa na Antipo hatukujua, lakini nikawaambia watu wangu: Tazama, hatujui lakini wamesimama kwa kusudi kwamba turudi dhidi yao, kwamba watushike kwenye mtego wao;

44 Kwa hivyo mnasema nini, nyinyi wana wangu, mtaenda dhidi yao kupigana?

45 Na sasa nakwambia, ndugu yangu mpendwa Moroni, kwamba kamwe sijaona ujasiri mkubwa hivyo, hapana, sio miongoni mwa Wanefi wote.

46 Kwani vile niliwaita kila siku wana wangu (kwani wote walikuwa wachanga sana) hata hivyo waliniambia: Baba, tazama Mungu wetu yuko pamoja nasi, na hatakubali kwamba tuanguke; basi twende mbele; hatungeua ndugu zetu ikiwa wangetuacha peke yetu; kwa hivyo acha twende, wasije wakashinda jeshi la Antipo.

47 Sasa walikuwa hawajawahi kupigana, na bado hawakuogopa kifo; na walifikiri zaidi juu ya uhuru wa baba zao kuliko maisha yao wenyewe; ndio, walikuwa wamefundishwa na mama zao, kwamba ikiwa hawakuwa na shaka, Mungu angewaokoa.

48 Na walirudia kwangu maneno ya mama zao, wakisema: Hatuna shaka kuwa mama zetu walijua.

49 Na ikawa kwamba nilirudi na elfu mbili wangu dhidi ya Walamani ambao walikuwa wametufukuza. Na sasa tazama, jeshi la Antipo lilikuwa limewapata, na vita vikali vilikuwa vimeanza.

50 Jeshi la Antipo wakiwa wamechoka, kwa sababu ya matembezi yao marefu kwenye huo muda mfupi hivyo, walikuwa karibu kuanguka kwa mikono ya Walamani; na kama singerudi na elfu mbili wangu wangepata madhumuni yao.

51 Kwani Antipo alikuwa ameangushwa kwa upanga, na wengi wa viongozi wake, kwa sababu ya uchovu wao, ambao ulisababishwa na mwendo wao wa kasi — kwa hivyo watu wa Antipo, wakiwa wamechanganyikiwa kwa sababu ya vifo vya viongozi wao, walianza kuanguka mbele ya Walamani.

52 Na ikawa kwamba Walamani walipata ujasiri, na wakaanza kuwafukuza; na hivyo Walamani walikuwa wakiwafukuza kwa nguvu wakati Helamani alipowatokea kwa nyuma na wale elfu mbili wake, na akaanza kuwaua sana, hadi kwamba jeshi lote la Walamani likasimama na kumgeukia Helamani.

53 Sasa wakati watu wa Antipo walipoona kwamba Walamani wamegeuka, walikusanya pamoja watu wao na wakaja kutokea upande wa nyuma wa Walamani.

54 Na sasa ikawa kwamba sisi, watu wa Nefi, watu wa Antipo, na mimi na elfu mbili
wangu, tuliwazingira Walamani, na kuwaua; ndio, mpaka kwamba wakalazimishwa
kusalimisha silaha zao za vita na pia wenyewe kama wafungwa wa vita.
55 Na sasa ikawa kwamba wakati walipokuwa wamejisalamisha kwetu, tazama,
niliwahesabu wale vijana ambao walipigana na mimi, nikiogopa kwamba wengi wao
walikuwa wameuawa.
56 Lakini tazama, kwa shangwe yangu kubwa, hakukuwa na hata mmoja ambaye
alikuwa ameinama kwenye ardhi; ndio, na walikuwa wamepigana kama waliokuwa
na nguvu ya Mungu; ndio, hakujatokea watu kujulikana kupigana na nguvu ya
miujiza kama hii; na kwa uwezo mkubwa sana waliwaangukia Walamani, kwamba
waliwaogofya; na kwa sababu hii Walamani walijisalimisha kama wafungwa wa vita.
57 Na kwa vile hatukuwa na mahali kwa wafungwa wetu, kwamba tungewalinda
kutoka kwa majeshi ya Walamani, kwa hivyo tuliwatuma katika nchi ya Zarahemla,
na sehemu ya wale watu wa Antipo ambao hawakuuawa, nao; na waliosalia
niliwachukua na kuwaunganisha kwa vijana wangu Waamoni, na tukarudi hadi
kwenye mji wa Yuda.

## Alma 57

1 Na sasa ikawa kwamba nilipokea barua kutoka kwa Amoroni, mfalme, ikieleza
kwamba ikiwa nitawaachilia wale wafungwa wa vita ambao tuliwakamata kwamba
angeuachilia mji wa Antipara kwetu.
2 Lakini nilituma barua kwa mfalme, kwamba tulikuwa na hakika majeshi yetu
yalikuwa yanatosha kukamata mji wa Antipara na askari wetu; na kwa kukabidhi
wafungwa wetu kwa mji huo tungejidhania wenyewe kuwa bila hekima, na kwamba
tungeachilia tu wafungwa wetu kwa kubadilishana.
3 Na Amoroni alikataa barua yangu, kwani hakutaka kubadilisha wafungwa; kwa
hivyo tulianza matayarisho kwenda dhidi ya mji wa Antipara.
4 Lakini watu wa Antipara waliacha mji, na wakakimbilia miji yao mingine,
ambayo walisimamia, kuiimarisha; na hivyo mji wa Antipara ulianguka mikononi
mwetu.
5 Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini na nane wa utawala wa waamuzi.
6 Na ikawa kwamba mwanzoni mwa mwaka wa ishirini na tisa, tulipokea ruzuku
ya vyakula, na pia ongezeko kwa jeshi letu, kutoka kwa nchi ya Zarahemla, na
kutoka kwa nchi ya karibu, kwa idadi ya watu elfu sita, kando na sitini ya wana wa
Waamoni ambao walikuja kujiunga na ndugu zao, kundi langu dogo la elfu mbili.
Na sasa tazama, tulikuwa na nguvu, ndio, na pia tulikuwa na vyakula vingi
vilivyoletwa kwetu.
7 Na ikawa kwamba ilikuwa kupenda kwetu kupigana vita na jeshi ambalo
liliwekwa kulinda mji wa Kumeni.
8 Na sasa tazama, nitakuonyesha kwamba tulitekeleza haja yetu; ndio, na jeshi letu
la nguvu, au na sehemu ya jeshi letu la nguvu, tulizunguka, usiku, mji wa Kumeni,
mbele kidogo kabla ya hao kupokea ruzuku ya vyakula.
9 Na ikawa kwamba tulipiga hema karibu na mji kwa kucha nyingi; lakini tulilalia
panga zetu, na kulinda kwamba Walamani hawangetujia wakati wa usiku na kutuua,
ambayo walijaribu wakati mwingi; lakini vile walijaribu mara nyingi damu yao
ilimwagika.

10 Mwishowe vyakula vyao viliwasili, na walikuwa karibu kuingia mjini usiku. Na
sisi, badala ya kuwa Walamani, tulikuwa Wanefi; kwa hivyo, tuliwachukua wao na
vyakula vyao.
11 Na ingawa Walamani wakishazuiliwa kutoka kwa usaidizi wao kwa njia hii,
walikuwa bado wamekata kauli kukalia mji huo; kwa hivyo ilikuwa ni muhimu
kwamba tuchukue vile vyakula na kuvipeleka Yuda, na wafungwa wetu kwenye nchi
ya Zarahemla.
12 Na ikawa kwamba siku nyingi zilikuwa hazijaisha kabla ya Walamani kuanza
kupoteza matumaini kwa usaidizi; kwa hivyo walisalimisha mji mikononi mwetu;
na kwa hivyo tulikuwa tumemaliza kusudi letu kwa kupata mji wa Kumeni.
13 Lakini ikawa kwamba wafungwa wetu walikuwa wengi kwamba, ingawa jeshi
letu lilikuwa kubwa kwa idadi, tulilazimishwa kutumia majeshi yetu yote kuwalinda,
au kuwaua.
14 Kwani tazama, wangetoroka kwa idadi kubwa, na wangepigana kwa mawe, na
kwa rungu, au chochote ambacho wangekamata mikononi mwao, mpaka kwamba
tuliua zaidi ya elfu mbili wao baada ya wao kujitolea kama wafungwa wa vita.
15 Kwa hivyo ilikuwa muhimu kwetu, kwamba tumalize maisha yao, au tuwalinde,
na panga mkononi, hadi tuwafikishe nchi ya Zarahemla; na pia vyakula vyetu
vilikuwa vya kutotosha tu kwa watu wetu, ijapokuwa kwamba tulikuwa tumechukua
kutoka kwa Walamani.
16 Na sasa, kwa hiyo hali ngumu, ilikuwa ni mambo mazito sana kuamua kuhusu
hawa wafungwa wa vita; walakini, tuliamua kuwapeleka chini kwa nchi ya
Zarahemla; kwa hivyo tulichagua sehemu ya watu wetu, na tukawapa uwezo juu ya
wafungwa kuwapeleka chini kwenye nchi ya Zarahemla.
17 Lakini ikawa kwamba kesho yake walirudi. Na sasa tazama, hatukuwauliza
kuhusu wafungwa; kwani tazama, Walamani walikuwa juu yetu, na walirudi kwa
wakati ufaao kutuponya kutoanguka mikononi mwao. Kwani tazama, Amoroni
alikuwa ametuma kwa usaidizi wao ruzuku mpya ya vyakula na pia jeshi kubwa la
watu.
18 Na ikawa kwamba wale watu ambao tuliwatuma na wafungwa waliwasili kwa
wakati ufaao na kuwasimamisha, vile walivyokuwa wako karibu kutushinda.
19 Lakini tazama, kundi langu dogo la elfu mbili na sitini walipigana kwa ukali
sana; ndio, walikuwa imara mbele ya Walamani, na walitoa kifo kwa wote ambao
waliwapinga.
20 Na vile wale waliosalia wa jeshi letu walikuwa karibu kujisalimisha kwa
Walamani, tazama, wale elfu mbili na sitini walikuwa imara na bila hofu.
21 Ndio, na walisikiliza na kuchunguza kufanya kila neno la amri kwa uhalisi; ndio,
kulingana na imani yao walifanyiwa; na nilikumbuka maneno ambayo waliniambia
kwamba mama zao waliwafundisha.
22 Na sasa tazama, ni kwa hawa wana wangu, na wale watu ambao walichaguliwa
kupeleka wafungwa, ndio tunawia huu ushindi; kwani ilikuwa hawa ndio
waliowapiga Walamani; kwa hivyo walifukuzwa na kurudi nyuma kwenye mji wa
Manti.
23 Na tukaweka mji wetu wa Kumeni, na sio wote walioangamizwa kwa upanga;
walakini, tulipata hasara kubwa.
24 Na ikawa kwamba baada ya Walamani kukimbia, nilipeana amri mara moja
kwamba watu wangu ambao walikuwa wamejeruhiwa watolewe miongoni mwa

wafu, na kusababisha majeraha yao yafungwe dawa.
25 Na ikawa kwamba kulikuwa na mia mbili, kutoka kwa elfu mbili na sitini wangu, ambao walikuwa walegevu kwa sababu ya kupoteza damu; walakini, kulingana na wema wa Mungu, na kwa mshangao wetu, na pia shangwe ya jeshi lote, hakukuwa na nafsi moja miongoni mwao ambaye aliangamia; ndio, na wala hakukuwa na mmoja miongoni mwao ambaye hakupata majeraha mengi.
26 Na sasa, ulinzi wao ulikuwa wa kushangaza kwa jeshi letu lote, ndio, kwamba walihifadhiwa wakati kulikuwa na elfu moja wa ndugu zetu ambao waliuawa. Na tuna hakika kwamba walikombolewa kwa uwezo wa miujiza wa Mungu, kwa sababu ya imani yao kubwa kwa yale ambayo walikuwa wamefundishwa kuamini—kwamba kuna Mungu mwenye haki, na yeyote asiyemshuku, kwamba watahifadhiwa na uwezo wake wa ajabu.
27 Sasa hii ilikuwa imani ya wale ambao nimezungumzia; ni wachanga, na akili zao ni imara, na wanaweka matumaini yao kwa Mungu siku zote.
28 Na sasa ikawa kwamba baada ya kushugulikia watu wetu waliojeruhiwa, na kuwazika wafu wetu na wale wa Walamani, ambao walikuwa wengi, tazama, tulimwuliza Gidi kile kilichotendeka kuhusu wafungwa ambao walianza kwenda chini kwenye mji wa Zarahemla nao.
29 Sasa Gidi alikuwa kapteni mkuu juu ya kundi ambalo lilichukuliwa kuwachunga hadi kwenye ile nchi.
30 Na sasa, haya ndiyo maneno ambayo Gidi aliniambia: Tazama, tulianza kuelekea chini kwenye nchi ya Zarahemla na wafungwa wetu. Na ikawa kwamba tulikutana na wapelelezi wa majeshi yetu, ambao walikuwa wametumwa kuchungulia kituo cha Walamani.
31 Na wakapaza sauti kwetu, wakisema—Tazama, majeshi ya Walamani yanatembea taratibu kuelekea mji wa Kumeni; na tazama, watawashambulia, ndio, watawaangamiza watu wetu.
32 Na ikawa kwamba wafungwa wetu walisikia mlio wao, ambao uliwasababisha kuwa na ujasiri; na wakaasi dhidi yetu.
33 Na ikawa kwa sababu ya uasi wao tulisababisha kwamba panga zetu ziwaangukie. Na ikawa kwamba kwa kikundi, walikimbilia panga zetu, ambamo matokeo yake idadi yao kubwa iliuawa; na waliosalia walipenya walinzi na kukimbia kutoka kwetu.
34 Na tazama, wakati walipokuwa wamekimbia na hatukuweza kuwapata, tulichukua matembezi yetu kwa kasi kuelekea mji wa Kumeni; na tazama, tuliwahi kufika kwamba tuwasaidie ndugu zetu kwa kuuhifadhi mji.
35 Na tazama, tumeokolewa tena kutoka mikononi mwa maadui wetu. Na heri ni jina la Mungu wetu; kwani tazama, yeye ndiye ametuokoa; ndio, amefanya hiki kitu kikubwa kwa niaba yetu.
36 Sasa ikawa kwamba mimi, Helamani, niliposikia haya maneno ya Gidi, nilijazwa na shangwe kuu kwa sababu ya wema wa Mungu kutuhifadhi sisi, kwamba tusiangamizwe sote; ndio, na ninaamini kwamba nafsi za wale ambao waliuawa zimeingia kwenye mapumziko ya Mungu wao.

# Alma 58

1 Na tazama, sasa ikawa kwamba lengo letu la pili lilikuwa kushika mji wa Manti; lakini tazama, hakukuwa na njia ambayo tungewaongoza nje ya mji na makundi

yetu madogo. Kwani tazama, walikumbuka yale ambayo tulikuwa tumefanya hapo
awali; kwa hivyo hatungeweza kuwashawishi kutoka kwenye ngome zao.
2 Na walikuwa wengi sana kuliko jeshi letu kwamba hatungeenda mbele na
kuwashambulia ndani ya ngome zao.
3 Ndio, na ilihitajika kwamba tutumie watu wetu kuhifadhi hizo sehemu za nchi
ambazo tulikuwa tumezichukua tena kwa umiliki wetu; kwa hivyo ikawa muhimu
kwamba tungoje, kwamba tupate kuongezewa nguvu kutoka kwa nchi ya Zarahemla
na pia tupate ruzuku mpya ya vyakula.
4 Na ikawa kwamba tulituma ujumbe kwa mtawala wa nchi yetu, kumweleza
kuhusu mambo ya watu wetu. Na ikawa kwamba tulingoja kupokea vyakula na
nguvu kutoka nchi ya Zarahemla.
5 Lakini tazama, hii ilitusaidia tu kidogo; kwani Walamani pia walikuwa pia
wanapokea nguvu nyingi siku kwa siku, na pia vyakula vingi; na hivyo ndivyo
ilikuwa hali yetu kwa wakati huo.
6 Na Walamani walikuwa wanatokea kwa nguvu dhidi yetu mara kwa mara,
wakinuia kutuangamiza kwa hila; walakini hatukuweza kupigana nao, kwa sababu
ya kurudi kwao nyuma na ngome zao.
7 Na ikawa kwamba tulingoja katika hii hali ngumu kwa muda wa miezi mingi,
hata karibu tulipokuwa karibu kuangamia kwa ukosefu wa chakula.
8 Lakini ikawa kwamba tulipokea chakula, ambacho kililindwa kwetu na jeshi la
watu elfu mbili ambalo lilikuja kutusaidia; na huu ndiyo usaidizi wote ambao
tulipata, kujilinda wenyewe na nchi yetu kutoanguka mikononi mwa maadui wetu;
ndio, kupigana na adui ambaye hahesabiki.
9 Na sasa sababu ya haya matatizo yetu, au kwa nini hawakutuletea nguvu zaidi,
hatukujua; kwa hivyo tulihuzunika na pia tulijawa na woga, isiwe kwa njia yoyote
hukumu ya Mungu ije kwa nchi yetu, kwa kutugeuza na kutuharibu kabisa.
10 Kwa hivyo tuliweka roho zetu kwenye sala kwa Mungu, kwamba angetuimarisha
na kutukomboa kutoka kwa mikono ya maadui wetu, ndio, na pia kutupatia nguvu
kwamba tungeweka miji yetu, na nchi zetu, na umiliki wetu, kwa kuwasaidia watu
wetu.
11 Ndio, na ikawa kwamba Bwana Mungu wetu alitubariki na hakikisho kwamba
angetukomboa; ndio, mpaka kwamba akazungumza amani kwa roho zetu, na
kutupatia imani kubwa, na alitusababishia kwamba tuwe na matumaini kwake kwa
ukombozi wetu.
12 Na tukapata ujasiri na jeshi letu dogo ambalo tulikuwa tumepokea, na
tulithibitisha kusudi letu kushinda maadui zetu, na kuhifadhi nchi zetu, na umiliki
wetu, na wake zetu, na watoto wetu, na asili ya uhuru wetu.
13 Na hivyo tulienda mbele kwa nguvu yetu yote dhidi ya Walamani, ambao
walikuwa kwenye mji wa Manti; na tukapiga hema zetu kando ya upande wa nyika,
ambao ulikuwa karibu na mji.
14 Na ikawa kwamba kesho yake, wakati Walamani walipoona kwamba tulikuwa
kwenye mipaka kando ya nyika ambayo ilikuwa karibu na mji, kwamba walituma
wapelelezi wao karibu nasi kwamba wagundue idadi na nguvu ya jeshi letu.
15 Na ikawa kwamba walipoona kwamba hatukuwa na nguvu, kulingana na idadi
yetu, na wakiogopa kwamba tungewakatiza kutoka kwa tegemeo lao isipokuwa waje
nje na kupigana dhidi yetu na watuue, na pia wakidhani kwamba wangetuangamiza
kwa urahisi na jeshi lao kubwa, kwa hivyo walianza kujitayarisha kuja nje dhidi yetu

kupigana.
16 Na wakati tuliona kwamba walikuwa wanajitayarisha kuja dhidi yetu, tazama,
nilisababisha kwamba Gidi na idadi ndogo ya watu, wajifiche nyikani, na pia
kwamba Teomneri na idadi ndogo ya watu wajifiche nyikani.
17 Sasa Gidi na watu wake walikuwa kwa mkono wa kulia na wengine kwa kushoto;
na wakati walipokuwa wamejificha wenyewe, tazama, nilibaki, na jeshi langu
lililosalia, mahali pale ambapo tulikuwa wakati wa kwanza tumepiga hema zetu
tukijitayarisha wakati ule Walamani wangekuja nje kupigana.
18 Na ikawa kwamba Walamani walikuja nje na jeshi lao kubwa dhidi yetu. Na
wakati walikuwa wamekuja na wako karibu kutuangukia kwa upanga, nilisababisha
kwamba watu wangu, wale ambao walikuwa na mimi, warudi nyuma kwenye nyika.
19 Na ikawa kwamba Walamani walitufuata kwa mwendo wa kasi, kwani walitaka
sana kutupata ili watuue; kwa hivyo walitufuata hadi nyikani; na tulipita katikati ya
Gidi na Teomneri, hata kwamba hawakugunduliwa na Walamani.
20 Na ikawa kwamba Walamani walipopita, au wakati jeshi lilipokuwa limepita,
Gidi na Teomneri waliinuka kutoka kwa maficho yao, na wakawazuia wapelelezi wa
Walamani ili wasirejee mjini.
21 Na ikawa kwamba wakati walipokuwa wamewazuia, walikimbia hadi kwenye mji
na kushambulia walinzi ambao waliachwa kulinda mji, mpaka kwamba
wakawaangamiza na wakamiliki mji.
22 Sasa hii ilifanyika kwa sababu Walamani walikuwa wameruhusu jeshi lao lote,
kuongozwa nyikani, isipokuwa walinzi wachache pekee.
23 Na ikawa kwamba Gidi na Teomneri kwa njia hii walipata umiliki wa ngome zao.
Na ikawa kwamba tulichukua njia yetu, baada ya kusafiri sana kwenye nyika
kuelekea nchi ya Zarahemla.
24 Na wakati Walamani waliona kwamba walikuwa wanatembea kuelekea nchi ya
Zarahemla, waliogopa sana, kusiwe kuna mtego umewekwa kuwaongoza kwenye
maangamizo; kwa hivyo walianza kurudi nyuma hadi kwenye nyika tena, ndio, hata
nyuma kutumia ile njia ambayo walikuja nayo.
25 Na tazama, kulikuwa usiku na wakapiga hema zao, kwani makapteni wakuu wa
Walamani walidhani kwamba Wanefi wamechoka kwa sababu ya matembezi yao; na
wakidhani kwamba walipeleka jeshi lao lote kwa hivyo hawakufikiri kuhusu mji wa
Manti.
26 Sasa ikawa kwamba wakati usiku ulipowadia, nilisababisha kwamba watu wangu
wasilale, lakini kwamba watembee mbele kwa njia nyingine kuelekea mji wa Manti.
27 Na kwa sababu ya haya matembezi yetu ya usiku, tazama, kesho yake tulikuwa
mbele ya Walamani, mpaka kwamba tuliwasili kabla yao katika mji wa Manti.
28 Na hivyo ikawa kwamba, kwa werevu huu tulimiliki mji wa Manti bila kumwaga
damu.
29 Na ikawa kwamba wakati majeshi ya Walamani yalipowasili karibu na mji, na
kuona kwamba tulikuwa tayari kupigana nao, walistaajabu sana na wakashikwa na
woga mwingi, mpaka kwamba walikimbilia kwenye nyika.
30 Ndio, na ikawa kwamba majeshi ya Walamani yalikimbia nje kutoka sehemu hii
yote ya nchi. Lakini tazama, wamebeba nao wanawake wengi na watoto na
wamewapeleka nje ya nchi.
31 Na hiyo miji ambayo ilichukuliwa na Walamani, yote kwa wakati huu iko katika
umiliki wetu; na baba zetu na wanawake wetu na watoto wetu wanarejea nyumbani

kwao, wote isipokuwa wale ambao wamechukuliwa wafungwa na kubebwa na Walamani.
32 Lakini tazama, majeshi yetu ni machache kulinda idadi kubwa hiyo ya miji na umiliki mwingi hivyo.
33 Lakini tazama, tunamwamini Mungu wetu ambaye ametupatia ushindi juu ya hizo nchi, mpaka kwamba tumepata hiyo miji na hizo nchi, ambazo zilikuwa zetu.
34 Sasa hatujui kwa nini serikali haitupatii nguvu zaidi; wala watu ambao wamekuja kwetu hawajui kwa nini hatujapokea nguvu nyingi zaidi.
35 Tazama, hatujui lakini kwamba hamjashinda, na mmehitaji majeshi katika sehemu ile ya nchi; ikiwa hivyo, hatuwezi kunung'unika.
36 Na ikiwa si hivyo, tazama, tunaogopa kwamba kuna ugomvi katika serikali, kwamba hawawezi kuleta watu wengi zaidi kwa usaidizi wetu; kwani tunajua kwamba wako wengi kuliko wale ambao wametuma.
37 Lakini, tazama, haitujalishi — tunaamini Mungu atatukomboa, ijapokuwa majeshi yetu ni dhaifu, ndio, na kutukomboa kutoka kwa mikono ya maadui zetu.
38 Tazama, huu ni mwaka wa ishirini na tisa, karibu mwisho wake, na tumemiliki nchi zetu; na Walamani wamekimbia hadi kwenye nchi ya Nefi.
39 Na wale wana wa watu wa Amoni, ambao nimezungumzia kwa uzuri, wako na mimi katika mji wa Manti; na Bwana amewasaidia, ndio, na kuwaweka kutokana na kuuawa kwa upanga, kwa matokeo kwamba hata mtu mmoja hakuuawa.
40 Lakini tazama, wamepata majeraha mengi; lakini wanasimama imara kwa huo uhuru ambamo kwake Mungu amewafanya huru; na wako waangalifu kumkumbuka Bwana Mungu wao siku hadi siku; ndio, wanachunga kutii sheria zake, na hukumu zake, na amri zake siku zote; na imani yao iko na nguvu katika unabii kuhusu yale ambayo yatakuja.
41 Na sasa, ndugu yangu mpendwa, Moroni, naomba Bwana Mungu wetu, ambaye ametukomboa na kutufanya huru, akulinde siku zote katika uwepo wake; ndio, na awabariki hawa watu, hata kwamba ufaulu kwa kupata tena umiliki wa yale yote ambayo Walamani wamechukua kutoka kwetu, ambayo yalikuwa kwa usaidizi wetu. Na sasa tazama, ninamaliza barua yangu. Mimi ni Helamani, mwana wa Alma.

## Alma 59

1 Sasa ikawa katika mwaka wa thelathini wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, baada ya Moroni kupokea na kusoma barua ya Helamani, alifurahi sana kwa sababu ya ustawi, ndio, kufaulu kwingi ambako Helamani alikamata nchi ambazo zilikuwa zimepotea.
2 Ndio, na aliwajulisha watu wake wote, katika nchi yote karibu na ile sehemu ambayo alikuwa, kwamba wafurahi pia.
3 Na ikawa kwamba mara moja alituma barua kwa Pahorani, akitaka kwamba asababishe watu wajikusanye pamoja kumtia Helamani nguvu, au majeshi ya Helamani, ili aweze kulinda kwa urahisi sehemu hio ya nchi ambayo alikuwa ameipata tena kwa miujiza.
4 Na ikawa wakati Moroni alikuwa ametuma hii barua kwa nchi ya Zarahemla, alianza tena kufikiria kuweka mpango kwamba angeweza kupata tena mabaki ya umiliki na miji ambayo Walamani walikuwa wamechukua kutoka kwao.
5 Na ikawa kwamba wakati Moroni alikuwa anafanya mipango kwenda dhidi ya

Walamani kupigana, tazama, watu wa Nefiha, ambao walikusanyika pamoja kutoka
mji wa Moroni na mji wa Lehi na mji wa Moriantoni, walishambuliwa na Walamani.
6 Ndio, hata wale ambao walikuwa wamelazimishwa kukimbia kutoka nchi ya
Manti, na kutoka nchi karibu, walikuwa wamekuja na kujiunga na Walamani katika
sehemu hii ya nchi.
7 Na hivyo wakiwa wengi sana, ndio, na wakipokea nguvu siku hadi siku, kwa amri
ya Amoroni walikuja mbele dhidi ya watu wa Nefiha, na wakaanza kuwaua kwa
wingi.
8 Na majeshi yao yalikuwa mengi sana kwamba watu wa Nefiha waliosalia
walilazimishwa kukimbia mbele yao; na wakaja hata wakaungana na jeshi la Moroni.
9 Na sasa vile Moroni alidhani kwamba kuwe na watu watumwe kwenye mji wa
Nefiha, kwa usaidizi wa wale watu kuulinda mji huo, na akijua kwamba ilikuwa ni
rahisi kulinda mji usianguke kwenye mikono ya Walamani kuliko kuuteka kutoka
kwao, alidhani kwamba wangelinda mji huo kwa urahisi.
10 Kwa hivyo aliweka majeshi yake yote kwa kuhifadhi zile sehemu ambazo alikuwa
ameteka tena.
11 Na sasa, Moroni alipoona kwamba mji wa Nefiha umechukuliwa tena alikuwa na
huzuni nyingi sana, na akaanza kuwa na shaka, kwa sababu ya uovu wa watu, ikiwa
hawataanguka katika mikono ya ndugu zao.
12 Sasa hii ndiyo ilikuwa fikira ya makapteni wake wote wakuu. Walishuku na
kustaajabu pia kwa sababu ya uovu wa watu, na hii ni kwa sababu ya kufaulu kwa
Walamani juu yao.
13 Na ikawa kwamba Moroni alikasirishwa na serikali, kwa sababu ya kutojali kwao
kuhusu uhuru wa nchi yao.

## Alma 60

1 Na ikawa kwamba alimwandikia tena mtawala wa nchi, ambaye alikuwa Pahorani,
na haya ndiyo maneno ambayo aliandika, akisema: Tazama, ninaelekeza barua
yangu kwa Pahorani, katika mji wa Zarahemla, ambaye ni mwamuzi mkuu na
mtawala wa nchi, na pia kwa wale wote ambao wamechaguliwa na hawa watu
kutawala na kuendesha shughuli za vita hivi.
2 Kwani tazama, nina kitu cha kuwaambia kwa njia ya lawama; kwani tazama,
nyinyi wenyewe mnajua kwamba mmewekwa kukusanya watu pamoja, na
kuwahami kwa mapanga, na vitara, na namna zote za silaha za vita za kila aina, na
kutuma na mbele dhidi ya Walamani, kwenye hizo sehemu ambazo wangeingilia
katika nchi yetu.
3 Na sasa tazama, nawaambia nyinyi kwamba mimi, na pia watu wangu, na pia
Helamani na watu wake, tumeumia maumivu makubwa sana; ndio, hata njaa, kiu,
na uchovu, na namna zote za mateso ya kila aina.
4 Lakini tazama, ikiwa haya ndiyo yote tuliyoumia hatungelalamika wala
kunung'unika.
5 Lakini tazama, mauaji yamekuwa makubwa miongoni mwa watu wetu; ndio,
maelfu wameanguka kwa upanga, wakati ingekuwa vingine kama mngeyapa majeshi
yetu nguvu za kutosha na usaidizi kwao. Ndio, kutojali kwenu kumekuwa kwingi
sana kwetu.
6 Na sasa tazama, tunataka kujua chanzo cha huku kutojali sana; ndio, tunataka

kujua sababu ya hii hali ya kutofikiri kwenu.
7 Mnaweza kufikiri kukalia viti vyenu vya enzi kwa hali ya kupotelewa na akili, wakati maadui wenu wanatambaza kazi ya vifo karibu nanyi? Ndio, wakati wanaua maelfu ya ndugu zenu—
8 Ndio, hata wale ambao wamewategemea kwa ulinzi, ndio, wamewaweka kwa nafasi kwamba mngewasaidia, ndio, mngetuma majeshi kwao, ili kuwapatia nguvu, na kuponya maelfu yao kutokana na kuanguka kwa upanga.
9 Lakini tazama, haya sio yote—mmezuia chakula kuwaendea, mpaka kwamba wengi wamepigana na wametokwa na damu na kufa kwa sababu ya mahitaji makubwa ambayo walikuwa nayo kwa sababu ya ustawi wa hawa watu; ndio, na hii wamefanya wakati walikuwa karibu kuangamia kwa njaa, kwa sababu ya kutojali kwenu sana kuwahusu.
10 Na sasa, ndugu zangu wapendwa—kwani mnahitajika kuwa wapendwa; ndio, na mnapaswa kujivuruga wenyewe kwa bidii kwa ustawi na uhuru wa hawa watu; lakini tazama, mmewadharau mpaka kwamba damu ya maelfu itakuwa juu ya vichwa vyenu kwa kisasi; ndio, kwani Mungu anafahamu vilio vyao vyote, na taabu zao—
11 Tazama, mnaweza kudhani kwamba mtaketi kwenye viti vyenu vya enzi, na kwa sababu ya uzuri mwingi wa Mungu hamngefanya chochote na atawakomboa? Tazama, kama mmedhani hivi mmedhani bure.
12 Mnadhani kwamba, kwa sababu ndugu zenu wengi wameuawa ni kwa sababu ya uovu wao? Ninawaambia, ikiwa mmedhani hivyo mmedhani bure; kwani ninawaambia, kuna wengi ambao wameuawa kwa upanga; na tazama ni kwa lawama yenu;
13 Kwani Bwana anakubali wenye haki kuuawa ili haki yake na hukumu ijie wale waovu; kwa hivyo hampaswi kudhani kwamba wenye haki wamepotea kwa sababu wameuawa; lakini tazama, wanaingia kwa pumziko la Bwana Mungu wao.
14 Na sasa tazama, nawaambia, ninaogopa sana kwamba hukumu za Mungu zitawajia watu hawa, kwa sababu ya uvivu wao mkuu, ndio, hata uvivu wa serikali yetu, na dharau zao kubwa kwa ndugu zao, ndio, kuelekea wale ambao wameuawa.
15 Kwani kama haingekuwa kwa uovu ambao ulianzia kwa serikali yetu, tungezuia maadui wetu kwamba hawangekuwa na uwezo juu yetu.
16 Ndio, kama haingekuwa kwa ajili ya vita ambavyo vilianza miongoni mwetu; ndio, kama haingekuwa kwa hawa watu wa mfalme, ambao walisababisha damu nyingi kumwagika miongoni mwetu; ndio, wakati tulikuwa tunakabiliana miongoni mwetu, kama tungeunganisha nguvu zetu vile tulivyofanya awali; ndio, kama haingekuwa tamaa ya uwezo na mamlaka ambayo wale watu wa mfalme walikuwa nayo juu yetu; kama wangekuwa waaminifu katika mwanzo wa uhuru wetu, na kujiunga nasi, na kuenda mbele dhidi ya maadui wetu, badala ya kuchukua panga zao dhidi yetu, ambayo ilisababisha umwagaji wa damu nyingi miongoni mwetu; ndio, kama tungekuwa tumeenda dhidi yao kwa uwezo wa Bwana, tungekuwa tumewatawanya maadui zetu, kwani ingefanyika, kulingana na kutimiza neno lake.
17 Lakini tazama, sasa Walamani wanatushambulia, wakimiliki nchi zetu, na wanawaua watu wetu kwa upanga, ndio, wake zetu na watoto wetu, na pia kuwachukua kama wafungwa, wakisababisha kwamba waumie namna yote ya mateso, na hii ni kwa sababu ya uovu mkuu wa wale ambao wanatafuta uwezo na mamlaka, ndio, hata wale watu wa mfalme.
18 Lakini kwa nini niseme mengi kuhusu hili jambo? Kwani hatujui lakini kuwa

nyinyi wenyewe mnatafuta mamlaka. Hatujui lakini nyinyi pia ni wasaliti kwa nchi
yenu.
19 Au ni kwamba hamtujali kwa sababu mko katikati ya nchi yetu na
mmezungukwa na usalama, kwamba hamsababishi vyakula viletwe kwetu, na pia
watu kuimarisha majeshi yetu?
20 Mmesahau amri za Bwana Mungu wenu? Ndio, mmesahau utumwa wa babu
zetu? Mmesahau ni mara ngapi tumekombolewa kutoka mikono ya maadui zetu?
21 Au mnadhani kwamba Bwana atatukomboa, wakati tunakalia viti vyetu vya enzi
na hatutumii njia ambazo Bwana ametutolea?
22 Ndio, je, mtaketi bila kufanya kitu wakati mnazingirwa na maelfu ya wale, ndio,
na kumi ya maelfu, ambao pia huketi kwenye uvivu, wakati kuna maelfu karibu
katika mipaka ambao wanaanguka kwa upanga, ndio, wamejeruhiwa na kutokwa na
damu?
23 Mnafikiri kwamba Mungu atawaona kama wasio na makosa wakati mnakaa
wima na kutazama vitu hivi? Tazama nawaambia, Hapana. Sasa nataka kwamba
mkumbuke kwamba Mungu amesema kwamba chombo cha ndani kitasafishwa
kwanza, ili nje yake nayo ipate kuwa safi.
24 Na sasa, isipokuwa mtubu kwa yale ambayo mmefanya, na kuanza kuamka na
kufanya, na kutuma mbele vyakula na watu kwetu, na pia kwa Helamani, ili alinde
hizo sehemu za nchi yetu ambazo amekamata tena, na ili tujirudishie tena umiliki
wetu ambao umesalia katika sehemu hizi, tazama itakuwa ya kufaa kwamba
tusipigane tena na Walamani mpaka kwanza tuoshe ndani ya chombo chetu, ndio,
hata uongozi mkuu wa serikali yetu.
25 Na isipokuwa mkubali barua yangu, na mje nje kunionyesha mimi roho ya kweli
ya uhuru, na mjaribu kuimarisha na kuongeza nguvu ya majeshi yetu, na
kuwapelekea chakula kwa usaidizi wao, tazama nitaacha sehemu ya wahuru wangu
kulinda sehemu hii ya nchi yetu, na nitaacha nguvu na baraka za Mungu juu yao,
kwamba nguvu nyingine isiweze kuja dhidi yao—
26 Na hii ni kwa sababu ya imani yao kubwa, na uvumilivu wao katika taabu zao—
27 Na nitakuja kwenu, na ikiwa kutakuwa yeyote miongoni mwenu ambaye ana
mahitaji ya uhuru, ndio, ikiwa kunaweza kuwa na hata cheche ya uhuru ambayo
imebaki, tazama nitavuruga uasi miongoni mwenu, hata mpaka wale ambao
wametaka kuchukua nguvu na mamlaka watamalizika.
28 Ndio, tazama siogopi nguvu zenu wala mamlaka yenu, lakini ni Mungu wangu
ambaye ninamwogopa; na ni kulingana na amri zake kwamba ninachukua upanga
wangu kulinda mwendo wa nchi yangu, na ni kwa sababu ya uovu wenu kwamba
tumeumia kwa kupoteza kwingi.
29 Tazama ni wakati, ndio, wakati sasa uko mkononi, kwamba isipokuwa mwanze
kwenda katika ulinzi wa nchi yenu na watoto wenu, upanga wa haki unaning'inia
juu yenu; ndio, na utawaangukia na kuwaadhibu hata kwenye uangamizo wenu.
30 Tazama, nangojea usaidizi kutoka kwenu; na, msipohudumia mahitaji yetu,
tazama, nakuja kwenu, hata kwa nchi ya Zarahemla, na kuwakata kwa upanga,
mpaka kwamba hamtakuwa na uwezo mwingine wa kuchelewesha maendeleo ya
watu hawa kwa kusudi la uhuru wetu.
31 Kwani tazama, Bwana hatakubali kwamba muishi na mzidi kuwa na nguvu kwa
uovu wenu kuwaangamiza watu hawa wenye haki.
32 Tazama, mnaweza kudhani kwamba Bwana atawaachilia na atoe hukumu kwa

Walamani, wakati ni desturi ya babu zao ambayo imesababisha chuki yao, ndio, na
imeongezwa mara mbili na wale ambao wameasi kutoka kwetu, wakati uovu wenu
ni kwa kusudi la mapenzi yenu ya furaha na vitu vya bure vya dunia?
33 Mnajua kwamba mnakosea sheria za Mungu, na mnajua kwamba mnayakanyagia
chini ya miguu yenu. Tazama, Bwana ananiambia: Ikiwa wale ambao wamepewa
utawala hawatubu dhambi zao na uovu, utaenda na kupigana nao.
34 Na sasa tazama, mimi, Moroni, nimelazimishwa, kulingana na agano ambalo
nimefanya kuweka amri za Mungu; kwa hivyo nataka kwamba mjishikilie kwa neno
la Mungu, na mtume kwa haraka kwangu kutoka kwenu vyakula na watu, na pia kwa
Helamani.
35 Na tazama, kama hamtafanya hivi nitakuja kwenu haraka; kwani tazama, Mungu
hawezi kukubali kwamba tuangamie kwa njaa; kwa hivyo atatupatia sehemu ya
chakula chenu, hata kama ni kwa upanga. Sasa hakikisha kwamba mnatimiza neno
la Mungu.
36 Tazama, mimi ni Moroni, kapteni wenu mkuu. Sihitaji ukubwa, lakini kuuweka
chini. Sitafuti heshima ya ulimwengu, lakini utukufu wa Mungu wangu, na uhuru
na ustawi wa nchi yangu. Na hivyo ninamaliza barua yangu.

## Alma 61

1 Tazama, sasa ikawa kwamba mara baada ya Moroni kutuma barua yake kwa mtawala
mkuu, alipata barua kutoka kwa Pahorani, mtawala mkuu. Na haya ndiyo maneno
ambayo alipokea:
2 Mimi, Pahorani, ambaye ni mtawala mkuu wa nchi hii, natuma maneno haya
kwa Moroni, kapteni mkuu juu ya jeshi. Tazama, nakwambia, Moroni, kwamba
sijawi shangwe na mateso yako makuu, ndio, inaisikitisha roho yangu.
3 Lakini tazama, kuna wale ambao wanajawa shangwe kwa mateso yako, ndio,
mpaka kwamba wameasi kwa uhalifu dhidi yangu, na pia dhidi ya watu wangu
ambao ni watu huru, ndio, na wale ambao wameasi ni wengi sana.
4 Na ni wale ambao wanataka kuchukua kiti cha hukumu kutoka kwangu ambao
wemesababisha huu uovu mkuu; kwani wametumia maneno makubwa ya
udanganyifu, na wameongoza mbali mioyo ya watu wengi, ambayo itakuwa sababu
ya taabu ya kutisha miongoni mwetu; wamesimamisha vyakula vyetu, na
wamewatisha watu wetu wote huru kwamba hawajafika kwako.
5 Na tazama, wamenikimbiza mimi mbele yao, na nimekimbilia nchi ya Gideoni,
na watu wengi vile nilivyoweza kupata.
6 Na tazama, nimetuma tangazo kote katika sehemu hii ya nchi; na tazama,
wanajikusanya kwetu kila siku, na silaha zao, kwa kukinga nchi yao na uhuru wao, na
kulipiza kisasi kwa wale waliotukosea.
7 Na wamekuja kwetu, mpaka kwamba wale ambao wameasi kwa uhalifu dhidi
yetu, ndio, wametudharau, ndio, mpaka kwamba wanatuogopa na hawathubutu
kuja kukabiliana nasi kwa vita.
8 Wanasimamia nchi, au mji, wa Zarahemla; wamejiwekea mfalme, na
amemwandikia mfalme wa Walamani, ambamo kwake amekubali kuunda
muungano na yeye; kwa muungano ambamo amekubali kulinda mji wa Zarahemla,
ulinzi ambao anadhani utawezesha Walamani kushinda nchi iliyosalia, na atawekwa
mfalme juu ya hawa watu wakati watashindwa chini ya Walamani.

9 Na sasa, kwenye barua yako, umenilaumu, lakini hainijalishi; sijakasirika, lakini
nina furaha kwa ujasiri wa moyo wako. Mimi, Pahorani, sitafuti ukubwa, isipokuwa
tu niweke kiti changu cha hukumu ili nihifadhi haki na uhuru wa watu wangu. Nafsi
yangu inasimama imara kwa ule uhuru ambao kwake Mungu ametufanya huru.
10 Na sasa, tazama, tutashindana na uovu hata kwenye umwagaji wa damu.
Hatungemwaga damu ya Walamani ikiwa wangekaa katika nchi yao.
11 Hatungemwaga damu ya ndugu zetu kama hawangeasi kwa uhalifu na kuchukua
upanga dhidi yetu.
12 Tungejitolea wenyewe kwenye nira ya utumwa kama ingekuwa kanuni ya
Mungu, au kama angetuamuru kufanya hivyo.
13 Lakini tazama yeye hatuamuru kwamba tujitolee wenyewe kwa maadui wetu,
lakini kwamba tuweke imani yetu kwake, na atatukomboa.
14 Kwa hivyo, ndugu yangu mpendwa, Moroni, acha tupinge uovu, na uovu wowote
ambao hatuwezi kupinga na maneno yetu, ndio, kama maasi na mafarakano, acha
tupinge kwa panga zetu, ili tuweke uhuru wetu, ili tufurahi kwenye ufanisi mkuu wa
kanisa letu, na kwa njia ya Mkombozi wetu na Mungu wetu.
15 Kwa hivyo, kuja kwangu na wachache wa watu wako, na uwaache waliosalia
waangalie Lehi na Teankumu; wape uwezo kuendesha vita katika sehemu hiyo ya
nchi, kulingana na Roho ya Mungu, ambayo pia ni roho ya uhuru ambayo iko ndani
yao.
16 Tazama nimetuma vyakula vichache kwao, ili wasiangamie kabla hujakuja
kwangu.
17 Kusanya pamoja jeshi lolote unaloweza wakati wa kuja kwako hapa, na tutaenda
haraka dhidi ya wale wasiokubali, katika nguvu za Mungu wetu kulingana na imani
ambayo iko ndani yetu.
18 Na tutautwaa mji wa Zarahemla, ili tupate chakula zaidi kutumia Lehi na
Teankumu; ndio, tutaenda mbele dhidi yao katika nguvu za Bwana, na tutamaliza
huu uovu mkuu.
19 Na sasa, Moroni, nina shangwe kwa kupata barua yako, kwani nilikuwa na
wasiwasi kuhusu kile tutakacho fanya, ikiwa itakuwa haki kwetu kwenda dhidi ya
ndugu zetu.
20 Lakini umesema, isipokuwa watubu Bwana amekuamuru uwashambulie.
21 Hakikisha kwamba umeimarisha Lehi na Teankumu katika Bwana; uwaambie
wasiogope, kwani Mungu atawakomboa, ndio, na pia wale wote wanaosimama
imara kwa ule uhuru ambao kwao Mungu amewafanya huru. Na sasa namaliza
barua yangu kwa ndugu yangu mpendwa, Moroni.

# Alma 62

1 Na sasa ikawa kwamba Moroni alipopata barua hii moyo wake ulipata ujasiri, na
ukajazwa na shangwe kuu kwa sababu ya uaminifu wa Pahorani, kwamba hakuwa
pia msaliti kwa uhuru na asili ya nchi yake.
2 Lakini pia alilia sana kwa sababu ya uovu wa wale ambao walimwondoa Pahorani
kutoka kwa kiti cha hukumu, ndio, kabisa kwa sababu ya wale ambao waliasi dhidi
ya nchi yao na pia Mungu wao.
3 Na ikawa kwamba Moroni alichukua idadi ndogo ya watu, kulingana na kutaka
kwa Pahorani, na kuwapatia Lehi na Teankumu amri juu ya jeshi lake lililosalia, na

akaanza mwendo wake kuelekea nchi ya Gideoni.

4 Na aliinua bendera ya uhuru mahali popote alipoingia, na akafaidika kwa kila jeshi aliloweza kwa matembezi yake yote kuelekea nchi ya Gideoni.

5 Na ikawa kwamba maelfu walifuata uongozi wake, na kuchukua panga zao kwa kulinda uhuru wao, ili wasije utumwani.

6 Na hivyo, Moroni alipokuwa amekusanya pamoja watu wote vile alivyoweza wakati wa mwendo wake, alifika nchi ya Gideoni; na akiunganisha majeshi yake na yale ya Pahorani wakawa na nguvu sana, hata na nguvu kuliko watu wa Pako, ambaye alikuwa mfalme wa wale waasi ambao walikuwa wamewafukuza watu huru nje ya nchi ya Zarahemla na walikuwa wamechukua umiliki wa nchi.

7 Na ikawa kwamba Moroni na Pahorani walienda chini na majeshi yao katika nchi ya Zarahemla, na wakashambulia mji, na wakakutana na watu wa Pako, mpaka kwamba wakaanza vita.

8 Na tazama, Pako aliuawa na watu wake wakachukuliwa wafungwa, na Pahorani akarudishwa kwenye kiti chake cha hukumu.

9 Na watu wa Pako walipata hukumu yao, kulingana na sheria, na pia watu wa mfalme ambao walikuwa wamechukuliwa na kutupwa gerezani; na waliuawa kulingana na sheria; ndio, wale watu wa Pako na wale watu wa mfalme, yeyote ambaye hangechukua silaha kulinda nchi yao, lakini apigane dhidi ya nchi, waliuawa.

10 Na hivyo ikawa ni lazima kwamba hii sheria izingatiwe sana kwa usalama wa nchi yao; ndio, na yeyote aliyepatikana akikana uhuru wao aliuawa kwa haraka kulingana na sheria.

11 Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi; Moroni na Pahorani wakiwa wamerudisha amani katika nchi ya Zarahemla, miongoni mwa watu wao, wakiwa wamesababisha kuuawa kwa wale wote ambao hawakuwa na imani kwa chanzo cha uhuru.

12 Na ikawa katika mwanzo wa mwaka wa thelathini na moja wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, Moroni kwa haraka alisababisha kwamba vyakula vipelekwe, na pia jeshi la watu elfu sita lipelekwe kwa Helamani, kumsaidia kuhifadhi ile sehemu ya nchi.

13 Na pia akasababisha kwamba jeshi la watu elfu sita, na chakula cha kutosha, wapelekwe kwa majeshi ya Lehi na Teankumu. Na ikawa kwamba hii ilifanyika kuimarisha nchi dhidi ya Walamani.

14 Na ikawa kwamba Moroni na Pahorani, baada ya kuacha kundi kubwa la watu katika nchi ya Zarahemla, walishika mwendo wao na kundi kubwa la watu na wakaelekea nchi ya Nefiha, wakiwa wamekata kauli kuwashinda Walamani katika mji huo.

15 Na ikawa kwamba walipokuwa wakitembea kuelekea ile nchi, walichukua kundi kubwa la watu wa Walamani, na wakachinja wengi wao, na kuchukua vyakula vyao na silaha zao za vita.

16 Na ikawa baada ya kuwachukua, waliwasababisha kufanya agano nao kwamba kamwe hawatachukua silaha za vita dhidi ya Wanefi.

17 Na wakati walikuwa wameingia kwenye agano hili waliwatuma kuishi na watu wa Amoni, na walikuwa idadi ya karibu elfu nne ambao walikuwa hawajauawa.

18 Na ikawa kwamba walipowakubalia waondoke waliendelea na matembezi yao kuelekea nchi ya Nefiha. Na ikawa kwamba wakati walikuwa wamefikia mji wa

Nefiha, walipiga hema zao kwenye tambarare ya Nefiha, ambayo iko karibu na mji
wa Nefiha.
19 Sasa Moroni alitaka kwamba Walamani waje nje wapigane dhidi yao, kwenye
tambarare; lakini Walamani, wakijua kuhusu ujasiri wao mkuu, na kuona ukubwa
wa idadi yao, kwa hivyo hawakuthubutu kuja nje dhidi yao; kwa hivyo hawakuja
kupigana siku hio.
20 Na wakati usiku ulipowadia, Moroni alienda mbele katika giza ya usiku, na
kupanda ukuta kupeleleza ni sehemu gani ya mji Walamani waliweka kituo cha jeshi
lao.
21 Na ikawa kwamba walikuwa katika upande wa mashariki, kando ya lango; na
wote walikuwa wamelala. Na sasa Moroni alirudi kwenye jeshi lake, na kuwaagiza
kwamba watayarishe kwa haraka kamba nzito na ngazi, ziteremshwe kutoka juu ya
ukuta hadi sehemu ya ndani ya ukuta.
22 Na ikawa kwamba Moroni alisababisha kwamba watu wake watembee mbele na
waje juu ya ukuta, na wajiteremshe ndani ya sehemu ile ya ule mji, ndio, hata kwenye
magharibi, ambapo Walamani hawakukaa na majeshi yao.
23 Na ikawa kwamba wote waliteremshwa kwenye mji wakati wa usiku, kwa
kutumia kamba zao nzito na ngazi zao; hivyo wakati kulipokucha wote walikuwa
ndani ya kuta za mji.
24 Na sasa, Walamani walipoamka na kuona kwamba majeshi ya Moroni yalikuwa
ndani ya kuta, waliogopa kupita kiasi, mpaka kwamba wakakimbia kupitia kwenye
lango la mji.
25 Na wakati Moroni alipoona kwamba wanatoroka kutoka kwake, agiza kwamba
watu wake wawashambulie, na kuua wengi, na wakawazunguka wengine wengi, na
kuwachukua wafungwa; na waliosalia walikimbilia nchi ya Moroni, ambayo ilikuwa
kwenye mipaka kando ya ukingo wa bahari.
26 Hivyo Moroni na Pahorani walikamata tena mji wa Nefiha bila kupoteza nafsi
moja; na kulikuwepo na Walamani wengi waliouawa.
27 Sasa ikawa kwamba wengi wa Walamani waliokuwa wafungwa walitaka kujiunga
na watu wa Amoni na kuwa watu huru.
28 Na ikawa kwamba kadiri wengi waliotamani, kwao ilikubaliwa kulingana na
mapenzi yao.
29 Kwa hivyo, wafungwa wote wa Walamani walijiunga na watu wa Amoni, na
walianza kufanya kazi sana, kulima ardhi, kukuza kila namna ya nafaka, na makundi
na mifugo ya kila aina; na hivyo Wanefi waliondolewa mzigo mkubwa; ndio, mpaka
kwamba walipumzishwa kutoka kwa wafungwa wote wa Walamani.
30 Sasa ikawa kwamba, baada ya Moroni kukamata mji wa Nefiha, akiwa
amechukua wafungwa wengi, ambao walipunguza majeshi ya Walamani sana, na
akiwa ameokoa Wanefi ambao walikuwa wamechukuliwa wafungwa, ambao
waliimarisha jeshi la Moroni sana; kwa hivyo Moroni alienda mbele kutoka kwa
nchi ya Nefiha hadi nchi ya Lehi.
31 Na ikawa kwamba wakati Walamani walipoona kwamba Moroni alikuwa
anakuja dhidi yao, waliogopa tena na kulitoroka jeshi la Moroni.
32 Na ikawa kwamba Moroni na jeshi lake waliwafuata kutoka mji hadi mji, mpaka
walipokutana na Lehi na Teankumu; na Walamani wakakimbia kutoka kwa Lehi na
Teankumu, hata mpaka chini kwenye mipaka kando ya ukingo wa bahari, mpaka
walipofika nchi ya Moroni.

33 Na majeshi ya Walamani yalijikusanya pamoja, mpaka yalikuwa kikundi kimoja
katika nchi ya Moroni. Sasa Amoroni, mfalme wa Walamani, alikuwa pia nao.
34 Na ikawa kwamba Moroni na Lehi na Teankumu walikaa na majeshi yao karibu
na mipaka ya nchi ya Moroni, mpaka kwamba Walamani walizungukwa karibu na
mipaka kando ya nyika kusini, na kwenye mipaka kando ya nyika mashariki.
35 Na hivyo waliweka kituo usiku. Kwani tazama, Wanefi na Walamani walikuwa
pia wamechoka kwa sababu ya matembezi marefu; kwa hivyo hawakukata kauli ya
kutenda hila yoyote wakati wa usiku, isipokuwa Teankumu; kwani alikuwa
amemkasirikia Amoroni sana, mpaka alifikiria kwamba Amoroni, na Amalikia kaka
yake, walikuwa kiini cha vita hivi virefu kati yao na Walamani, ambavyo vilikuwa
mwanzo wa vita vingi na umwagaji wa damu, ndio, na njaa nyingi.
36 Na ikawa kwamba Teankumu kwa hasira yake alienda kwenye kituo cha
Walamani, na kujiteremsha chini kwenye ukuta wa mji. Na akaenda mbele na
kamba, kutoka mahali hadi pengine, mpaka alipompata mfalme; na akatupa sagai
kwake, ambayo ilimchoma karibu na moyo. Lakini tazama, mfalme aliamsha
watumishi wake kabla ya kufa, mpaka kwamba wakamfuata Teankumu, na kumuua.
37 Sasa ikawa kwamba wakati Lehi na Moroni walipojua kwamba Teankumu
amekufa walihuzunika sana; kwani tazama, alikuwa mtu ambaye alipigana na
ushujaa sana kwa nchi yake, ndio, rafiki wa kweli wa uhuru; na aliumia mateso
mabaya mengi. Lakini tazama, alikuwa amekufa, na alienda njia ya kawaida ya
binadamu.
38 Sasa ikawa kwamba Moroni alienda mbele kesho yake, na kuwashambulia
Walamani, mpaka kwamba waliwaua mauaji makuu; na waliwafukuza kutoka
nchini; na walikimbia, hata kwamba hawakurudi wakati huo dhidi ya Wanefi.
39 Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini na moja wa utawala wa waamuzi juu ya
watu wa Nefi; na hivyo walikuwa wamekuwa na vita, na umwagaji wa damu, na njaa,
na mateso, kwa muda wa miaka mingi.
40 Na kulikuwa na mauaji, na mabishano, na mafarakano, na kila namna yote ya
uovu miongoni mwa watu wa Nefi; walakini kwa faida ya wale walio haki, ndio, kwa
sababu ya sala za walio haki, waliachiliwa.
41 Lakini tazama, kwa sababu ya muda mrefu wa vita miongoni mwa Wanefi na
Walamani wengi walikuwa wamefanywa kuwa na roho ngumu, kwa sababu ya vita
virefu; na wengi walilainishwa kwa sababu ya mateso yao, mpaka kwamba
wakajinyenyekeza mbele ya Mungu, hata unyenyekevu wa ndani.
42 Na ikawa kwamba baada ya Moroni kuimarisha hizo sehemu za nchi ambazo
zilikuwa wazi zaidi kwa Walamani, mpaka walipopata nguvu ya kutosha, alirudi mji
wa Zarahemla; na pia Helamani alirudi mahali pake pa urithi; na kukawa tena
amani miongoni mwa watu wa Nefi.
43 Na Moroni aliweka mamlaka ya majeshi katika mikono ya mwana wake, ambaye
jina lake lilikuwa Moroniha; na akastaafu na kurudi nyumba ni kwake kwamba
atumie siku zake za mwisho kwa amani.
44 Na Pahorani alirudia kiti chake cha hukumu; na Helamani alichukua tena
jukumu la kuwahubiria watu neno la Mungu; kwani kwa sababu ya vita vingi na
mabishano ilikuwa imekuwa muhimu kwamba msimamo uwekwe tena kanisani.
45 Kwa hivyo, Helamani na ndugu zake walienda mbele, na kutangaza neno la
Mungu kwa uwezo mwingi kwa kusadikisha watu wengi juu ya uovu wao, ambayo
iliwafanya wakatubu dhambi zao na kubatizwa kwa Bwana Mungu wao.

46 Na ikawa kwamba walianzisha tena kanisa la Mungu, kote nchini.
47 Ndio, na msimamo uliwekwa kuhusu sheria. Na waamuzi wao, na waamuzi wao
wakuu walichaguliwa.
48 Na watu wa Nefi walianza kufanikiwa tena katika nchi, na wakaanza kuongezeka
na kuwa na nguvu sana nchini. Na wakaanza kutajirika sana.
49 Lakini ijapokuwa utajiri wao, au nguvu yao, au mafanikio yao, hawakujiinua kwa
kiburi machoni mwao; wala hawakuwa wavivu wa kumkumbuka Bwana Mungu
wao; lakini walijinyenyekeza sana mbele yake.
50 Ndio, walikumbuka vitu gani vikubwa ambavyo Bwana aliwafanyia, kwamba
alikuwa amewakomboa kutoka kifo, na kutoka kifungoni, na kutoka magerezani, na
kutoka kila aina ya mateso, na alikuwa amewakomboa kutoka katika mikono ya
maadui zao.
51 Na waliomba kwa Bwana Mungu wao siku zote, mpaka kwamba Bwana
aliwabariki, kulingana na neno lake, kwamba walikuwa na nguvu na kufanikiwa
nchini.
52 Na ikawa kwamba vitu hivi vyote vilifanyika. Na Helamani akafariki, katika
mwaka wa thelathini na tano wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

## Alma 63

1 Na ikawa katika mwanzo wa mwaka wa thelathini na sita wa utawala wa waamuzi
juu ya watu wa Nefi, kwamba Shibloni alijichukulia hivyo vitu vyote vitakatifu
ambavyo vilitolewa kwa Helamani na Alma.
2 Na alikuwa mtu mwenye haki, na alitembea wima mbele ya Mungu; na
alitazamia kutenda mema siku zote, kutii amri za Bwana Mungu wake; na pia kaka
yake alifanya hivyo.
3 Na ikawa kwamba Moroni alifariki pia. Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini
na sita wa utawala wa waamuzi.
4 Na ikawa kwamba katika mwaka wa thelathini na saba wa utawala wa waamuzi,
kulikuwa na kundi kubwa la watu, hata kwa idadi ya elfu tano na mia nne ya watu,
na wake zao na watoto wao, waliondoka nje ya nchi ya Zarahemla hadi kwenye nchi
ambayo ilikuwa upande wa kaskazini.
5 Na ikawa kwamba Hagothi, yeye akiwa mtu mchunguzi sana, kwa hivyo alienda
mbele na akajenga merikebu kubwa sana, kwenye mipaka ya nchi ya Neema, kando
ya nchi ya Ukiwa, na akaishusha ndani ya bahari ya magharibi, kando na mkondo
wa nchi ambao ulielekea nchi iliyokuwa upande wa kaskazini.
6 Na tazama, walikuwepo Wanefi wengi miongoni mwao ambao waliingia ndani
na kusafiri mbele na vyakula vingi, na pia wanawake wengi na watoto; na walisafiri
kuelekea kaskazini. Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini na saba.
7 Na katika mwaka wa thelathini na nane, huyu mtu alijenga merikebu zingine. Na
merikebu ya kwanza pia ilirejea, na watu wengi zaidi waliingia ndani yake; na pia
walichukua vyakula vingi, na kuanza safari tena kuelekea nchi ya kaskazini.
8 Na ikawa kwamba hawakusikika tena. Na tunadhani kwamba walizama ndani ya
kina cha bahari. Na ikawa kwamba merikebu nyingine pia ilisafiri mbele; na mahali
ilipoenda hatujui.
9 Na ikawa kwamba katika mwaka huu kulikuwa na watu wengi walioenda katika
nchi upande wa kaskazini. Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini na nane.

10 Na ikawa katika mwaka wa thelathini na tisa wa utawala wa waamuzi, Shibloni
alikufa pia, na Koriantoni alikuwa ameenda kwenye nchi ya kaskazini ndani ya
merikebu, kupeleka vyakula kwa watu ambao walikuwa wameenda katika nchi ile.
11 Kwa hivyo ilikuwa muhimu kwa Shibloni kupeleka vitu hivyo vitakatifu kabla ya
kifo chake, kumkabidhi mwana wa Helamani, ambaye alikuwa Helamani, akiitwa
baada ya jina la baba yake.
12 Sasa tazama, ile michoro yote ambayo ilikuwa kwa ulinzi wa Helamani
iliandikwa na kupelekwa miongoni mwa watoto wa watu kote nchini, isipokuwa
hizo sehemu ambazo zilikuwa zimeamriwa na Alma zisidhihirishwe.
13 Walakini, hivi vitu vilitakiwa kuwekwa wakfu, na kutolewa kutoka uzao mmoja
hadi mwingine; kwa hivyo, katika mwaka huu, vilikuwa vimekabidhiwa Helamani,
kabla ya kifo cha Shibloni.
14 Na ikawa pia katika mwaka huu kwamba kulikuwa na waasi ambao walikuwa
wamewaendea Walamani; na wakavurugwa tena na kukasirika dhidi ya Wanefi.
15 Na pia katika mwaka huo walikuja na jeshi kubwa kupigana vita dhidi ya watu wa
Moroniha, au dhidi ya jeshi la Moroniha, ambapo walipigwa na kurudishwa nyuma
tena kwa nchi zao, wakipoteza na kuumia sana.
16 Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini na tisa wa utawala wa waamuzi juu ya
watu wa Nefi.
17 Na hivyo ikaisha historia ya Alma, na Helamani mwana wake, na pia Shibloni,
ambaye alikuwa mwana wake.

# Kitabu cha Helamani

*Historia ya Wanefi. Vita vyao na mabishano, na mafarakano yao. Na pia unabii wa manabii wengi watakatifu, kabla ya kuja kwa Kristo, kulingana na maandishi ya Helamani, ambaye alikuwa mwana wa Helamani, na pia kulingana na maandishi ya wana wake, hata mpaka kuja kwa Kristo. Na pia wengi wa Walamani wanageuka. Maelezo ya ugeuzi wao. Maelezo ya uhaki wa Walamani, na uovu na machukizo ya Wanefi, kulingana na maandishi ya Helamani na wana wake, hata mpaka kuja kwa Kristo, ambayo yanaitwa kitabu cha Helamani, na kadhalika.*

## Helamani 1

1 Na sasa tazama, ikawa katika mwanzo wa mwaka wa arubaini wa utawala wa
waamuzi juu ya watu wa Nefi, kulianza kuwa na taabu kubwa miongoni mwa watu
wa Wanefi.
2 Kwani tazama, Pahorani alikuwa amefariki, na kwenda njia ya kawaida ya
ulimwengu; kwa hivyo kulianza kuwa na ubishi kuhusu ni nani atakayechukua kiti
cha hukumu miongoni mwa kaka, ambao walikuwa wana wa Pahorani.
3 Sasa haya ndiyo majina ya wale ambao walishindania kiti cha hukumu, ambao pia
walisababisha watu kugombana: Pahorani, Paanki, na Pakumeni.
4 Sasa hawa sio wana wote wa Pahorani (kwani alikuwa na wengi), lakini hawa
ndio wale ambao walishindania kiti cha hukumu; kwa hivyo, walianzisha
migawanyiko mitatu miongoni mwa watu.
5 Walakini, ikawa kwamba Pahorani alichaguliwa kwa sauti ya watu kuwa
mwamuzi mkuu na mtawala juu ya watu wa Nefi.
6 Na ikawa kwamba wakati Pakumeni alipoona kwamba hangepata kiti cha
hukumu, alikubaliana na sauti ya watu.
7 Lakini tazama, Paanki, na sehemu ya watu ambao walitaka kwamba awe mtawala
wao, walikasirika sana; kwa hivyo, alikuwa karibu kuwachochea hao watu kuasi
dhidi ya ndugu zao.
8 Na ikawa kwamba vile alipokuwa karibu kufanya hivi, tazama, alikamatwa, na
kujaribiwa kulingana na sauti ya watu, na kuhukumiwa kifo; kwani alikuwa ameasi
na alitaka kuangamiza uhuru wa watu.
9 Sasa wakati wale watu ambao walitaka kwamba awe mtawala wao walipoona
kwamba amehukumiwa kifo, kwa hivyo walikasirika, na tazama, walimtuma mtu
mmoja kwa jina la Kishkumeni, kwenda kwa kiti cha hukumu cha Pahorani, na
kumuua Pahorani wakati alipokuwa amekalia kiti cha hukumu.
10 Na akafukuzwa na watumishi wa Pahorani; lakini tazama, mwendo wa
Kishkumeni ulikuwa wa kasi sana kwamba mtu yeyote hangemshika.
11 Na akarudi kwa wale ambao walimtuma, na wote wakaingia katika agano, ndio,
wakiapa kwa Muumba wao asiye na mwisho, kwamba hawatamwambia yeyote
kwamba Kishkumeni alikuwa amemuua Pahorani.
12 Kwa hivyo, Kishkumeni hakujulikana miongoni mwa watu wa Nefi, kwani
alikuwa amejigeuza wakati ambao alimuua Pahorani. Na Kishkumeni na kundi lake,
ambao walikuwa wamefanya agano naye, walijichanganya miongoni mwa watu, kwa

njia kwamba hawangeweza kupatikana; lakini wale waliopatikana walihukumiwa kifo.

13 Na sasa tazama, Pakumeni alichaguliwa, kulingana na sauti ya watu, kuwa mwamuzi mkuu na mtawala juu ya watu, kutawala mahali pa kaka yake Pahorani; na ilikuwa kulingana na haki yake. Na hayo yote yalifanyika katika mwaka wa arubaini wa utawala wa waamuzi; na yalikuwa na mwisho.

14 Na ikawa katika mwaka wa arubaini na moja wa utawala wa waamuzi, kwamba Walamani walikuwa wamekusanya pamoja jeshi kubwa wasiohesabika la watu, na kuwahami kwa panga, na kwa vitara na kwa pinde, na kwa mishale, na kwa vyapeo, na kwa dirii, na kwa kila namna ya ngao ya kila aina.

15 Na walikuja tena ili waanzishe vita dhidi ya Wanefi. Na waliongozwa na mtu ambaye jina lake lilikuwa Koriantumuri; na alikuwa wa uzao wa Zarahemla; na alikuwa mwasi kutoka miongoni mwa Wanefi; na alikuwa mtu mkubwa na mwenye nguvu.

16 Kwa hivyo, mfalme wa Walamani, ambaye jina lake lilikuwa Tubalothi, ambaye alikuwa mwana wa Amoroni, alidhani kwamba Koriantumuri, akiwa na nguvu nyingi, angeweza kusimama dhidi ya Wanefi, na nguvu zake na pia hekima yake kuu, mpaka kwamba kwa kumtuma yeye mbele angepata uwezo juu ya Wanefi —

17 Kwa hivyo aliwachochea kuwa na hasira, na akakusanya pamoja majeshi yake, na kumweka Koriantumuri kuwa kiongozi wao, na kuwasababisha kwenda chini kwenye nchi ya Zarahemla kupigana dhidi ya Wanefi.

18 Na ikawa kwamba kwa sababu ya ubishi mwingi na taabu nyingi serikalini, kwamba hawakuwa wameweka walinzi wa kutosha katika nchi ya Zarahemla; kwani walikuwa wamefikiri kwamba Walamani hawangekuja hadi katikati ya nchi yao kushambulia huo mji mkubwa wa Zarahemla.

19 Lakini ikawa kwamba Koriantumuri alitembea mbele ya jeshi lake kubwa, na kuwafikia wakazi wa mji, na mwendo wao ulikuwa wa kasi sana kwamba hakukuweko na nafasi ya Wanefi kukusanya majeshi yao pamoja.

20 Kwa hivyo Koriantumuri aliua walinzi wa lango la mji, na akaenda mbele na jeshi lake lote hadi kwenye mji, na wakamuua yeyote aliyewapinga, mpaka kwamba wakamiliki mji wote.

21 Na ikawa kwamba Pakumeni, ambaye alikuwa mwamuzi mkuu, alitoroka mbele ya Koriantumuri, hata akafikia kuta za mji. Na ikawa kwamba Koriantumuri alimpiga kwenye ukuta, mpaka akafa. Na hivyo siku za Pakumeni zikaisha.

22 Na sasa wakati Koriantumuri alipoona kwamba amemiliki mji wa Zarahemla, na kuona kwamba Wanefi wamewatoroka, na wameuawa, na wamekamatwa, na wametupwa gerezani, na kwamba amepata uwezo juu ya mji wenye nguvu sana katika nchi yote, moyo wake ulipata ujasiri mpaka kwamba alikuwa karibu kwenda dhidi ya nchi yote.

23 Na sasa hakukawia kwenye nchi ya Zarahemla, lakini alienda na jeshi kubwa, hata na kuelekea kwenye mji wa Neema; kwani nia yake ilikuwa kwenda mbele na kupata njia yake kwa kutumia upanga, ili aweze kupata sehemu za kaskazini ya nchi.

24 Na, akidhani kwamba nguvu zao kubwa zilikuwa katikati ya nchi, kwa hivyo alienda mbele, bila kuwapatia nafasi ya kujikusanya wenyewe pamoja isipokuwa tu kwa vikundi vidogo; na kwa njia hii waliwashukia na kuwatupa chini ardhini.

25 Lakini tazama, huu mwendo wa Koriantumuri kupitia katikati ya nchi ulimpatia Moroniha faida kubwa juu yao, ingawa ni idadi kubwa ya Wanefi waliouawa.

26 Kwani tazama, Moroniha alikuwa amedhani kwamba Walamani
hawangethubutu kuja katikati ya nchi, lakini kwamba wangeshambulia miji iliyo
karibu na mipaka vile walivyokuwa wamefanya hapo awali; kwa hivyo Moroniha
alikuwa ameamuru kwamba majeshi yao yenye nguvu yalinde sehemu hizo karibu
na kando ya mipaka.
27 Lakini tazama, Walamani hawakuogopa kulingana na kusudi lake, lakini
walikuwa wamekuja katikati ya nchi, na walikuwa wamekamata mji mkuu ambao
ulikuwa Zarahemla, na walikuwa wanapitia katika sehemu nyingi kubwa za nchi,
wakiwaua watu na mauaji makubwa, wote wanaume, wanawake, na watoto,
wakimiliki miji mingi na ngome nyingi.
28 Lakini Moroniha alipogundua hii, mara moja alimtuma Lehi na jeshi
kuwazunguka na kuwazuia kabla ya kufika nchi ya Neema.
29 Na hivyo ndivyo alivyofanya; na aliwazuia kabla ya hao kufikia nchi ya Neema,
na akakabiliana nao, mpaka kwamba wakaanza kurudi nyuma kuelekea nchi ya
Zarahemla.
30 Na ikawa kwamba Moroniha aliwazuia kukimbia, na akakabiliana nao, mpaka
kwamba kukawa na vita vya kumwaga damu nyingi; ndio, wengi waliuawa, na
miongoni mwa idadi ya waliouawa Koriantumuri alipatikana miongoni mwao.
31 Na sasa, tazama, Walamani hawakuweza kurudi nyuma upande wowote, upande
wa kaskazini, wala kusini, wala mashariki, wala magharibi, kwani walizungukwa kila
upande na Wanefi.
32 Na hivyo Koriantumuri alikuwa amewatumbukiza Walamani katikati ya Wanefi,
mpaka kwamba walikuwa chini ya uwezo wa Wanefi, na yeye mwenyewe akauawa,
na Walamani wakajisalimisha kwa Wanefi.
33 Na ikawa kwamba Moroniha alichukua tena mji wa Zarahemla, na kuamuru
kwamba Walamani ambao walikuwa wameshikwa mahabusu wakubaliwe kutoka
nchini kwa amani.
34 Na hivyo ukaisha mwaka wa arubaini na moja wa utawala wa waamuzi.

# Helamani 2

1 Na ikawa katika mwaka wa arubaini na mbili wa utawala wa waamuzi, baada ya
Moroniha kuanzisha tena amani miongoni mwa Wanefi na Walamani, tazama
hakukuwa na yeyote wa kuchukua kiti cha hukumu; kwa hivyo kulianza kuwa na
ubishi tena miongoni mwa watu kuhusu ni nani atakayechukua kiti cha hukumu.
2 Na ikawa kwamba Helamani, ambaye alikuwa mwana wa Helamani,
alichaguliwa kuchukua kiti cha hukumu, kwa sauti ya watu.
3 Lakini tazama, Kishkumeni, ambaye alimuua Pahorani, alivizia kumwamgamiza
Helamani pia; na alisaidiwa na kundi lake, ambao walikuwa wameingia katika agano
kwamba uovu wake usijulikane na yeyote.
4 Kwani kulikuwa na mtu mmoja aliyejulikana kama Gadiantoni, ambaye alikuwa
stadi sana kwa maneno mengi, na pia kwa hila yake, kutenda kazi yake ya siri ya
mauaji na unyang'anyi; kwa hivyo, alikuwa kiongozi wa kundi la Kishkumeni.
5 Kwa hivyo aliwadanganya, na pia Kishkumeni, kwamba ikiwa watampatia kiti
cha hukumu angewakubalia wale ambao walikuwa wa kundi lake kwamba
wangewekwa kwenye uwezo na mamlaka miongoni mwa watu; kwa hivyo
Kishkumeni alitafuta kumwangamiza Helamani.

6 Na ikawa kwamba aliposonga mbele kuelekea kwenye kiti cha hukumu
kumwangamiza Helamani, tazama mmoja wa watumishi wa Helamani, ambaye
alikuwa nje usiku, na akiwa amepata, taarifa ya mipango hiyo kwa njia ya
kujibadilisha ambayo ilikuwa imewekwa na hili kundi kumwangamiza Helamani—
7 Na ikawa kwamba alikutana na Kishkumeni, na kumwonyesha ishara; kwa hivyo
Kishkumeni alitambua nia ya mahitaji yake, akitaka kwamba amsaidie kufika
kwenye kiti cha hukumu ili amuue Helamani.
8 Na wakati mtumishi wa Helamani alipojua lengo lote la Kishkumeni, na vile
kusudi lake lilikuwa kuua, na pia kwamba kusudi la wote ambao walikuwa wa kundi
lake lilikuwa ni kuua, na kunyan'ganya, na kupata mamlaka, (na huu ulikuwa
mpango wao wa siri, na shirika lao) mtumishi wa Helamani akamwambia
Kishkumeni: Acha twende kwenye kiti cha hukumu.
9 Sasa hii ilimpendeza Kishkumeni sana, kwani aliona kwamba atatimiza kusudi
lake; lakini tazama, vile walipokuwa wanaenda mbele kwenye kiti cha hukumu,
mtumishi wa Helamani alimchoma kisu Kishkumeni, hata mpaka kwenye moyo,
kwamba alianguka na kufa bila kugumia. Na alikimbia na kumwambia Helamani
vitu vyote ambavyo alikuwa ameona, na kusikia, na kufanya.
10 Na ikawa kwamba Helamani alituma walinzi kushika hili kundi la wezi na wauaji
wa siri, ili wauawe kulingana na sheria.
11 Lakini tazama, wakati Gadiantoni alipogundua kwamba Kishkumeni hakurejea
aliogopa kwamba asije akaangamizwa; kwa hivyo aliamuru kundi lake limfuate. Na
walikimbia kutoka nchini, kwa njia ya siri, hadi kwenye nyika; na hivyo wakati
Helamani alipotuma wachukuliwe hawakupatikana.
12 Na mengine ya huyu Gadiantoni yatazungumzwa baadaye. Na hivyo ukaisha
mwaka wa arubaini na mbili wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.
13 Na tazama, mwishoni mwa kitabu hiki mtaona kwamba Gadiantoni alithibitisha
upinduzi, ndio, karibu kuangamizwa kwote kwa watu wa Nefi.
14 Tazama simaanishi mwisho wa kitabu hiki cha Helamani, lakini mwisho wa
kitabu cha Nefi, ambamo nimepata historia yote ambayo nimeandika.

## Helamani 3

1 Na sasa ikawa katika mwaka wa arubaini na tatu wa utawala wa waamuzi, hakukuwa
na ubishi miongoni mwa watu wa Nefi isipokuwa kiburi kidogo ambacho kilikuwa
kanisani, ambacho kilianzisha mafarakano madogo miongoni mwa watu, mambo
ambayo yalirekebishwa mwishoni mwa mwaka wa arubaini na tatu.
2 Na hakukuweko na ubishi miongoni mwa watu katika mwaka wa arubaini na
nne; wala hakukuweko ubishi mwingi katika mwaka wa arubaini na tano.
3 Na ikawa katika mwaka wa arubaini na sita, ndio, kulikuwa na mafarakano
mengi na ugomvi mwingi; hata kwamba kulikuwa na wengi sana ambao waliondoka
nchi ya Zarahemla, na kwenda kwenye nchi ya upande wa kaskazini kurithi nchi.
4 Na walisafiri kwa mwendo mrefu sana, mpaka kwamba wakafika kwenye maziwa
makubwa na mito mingi.
5 Ndio, na hata walitawanyika katika sehemu zote za nchi, katika sehemu zozote
ambazo hazikuwa zimefanywa kuwa na ukiwa na bila miti, kwa sababu ya wakazi
wengi ambao walikuwa wamerithi ile nchi mbeleni.
6 Na sasa hakukuwa na sehemu yeyote ya nchi ambayo ilikuwa ya ukiwa, isipokuwa

pale pasipokuwa na miti; lakini kwa sababu ya kuangamizwa watu wengi walioishi
nchini mbeleni iliitwa ukiwa.
7 Na kwa vile kulikuwa na miti michache tu nchini, hata hivyo watu walioenda
huko walipata kuwa na ujuzi mwingi kwa kutumia saruji; kwa hivyo walijenga
nyumba za saruji, ambamo waliishi.
8 Na ikawa kwamba waliongezeka na kutawanyika, na wakasonga mbele kutoka
nchi ya upande wa kusini hadi kwa nchi ya upande wa kaskazini, na wakatawanyika
mpaka kwamba wakaanza kuenea usoni mwa ulimwengu wote, kutoka bahari ya
kusini hadi bahari ya kaskazini, kutoka bahari ya magharibi hadi bahari ya mashariki.
9 Na watu waliokuwa katika nchi ya upande wa kaskazini waliishi kwenye hema,
na kwenye nyumba za saruji, na waliachilia mti wa aina yoyote uliomea juu ya ardhi
ya nchi kwamba ukue, ili kwa muda ujao wangepata miti ya kujengea nyumba zao,
ndio, miji yao, na mahekalu yao, na masinagogi yao, na mahali pao patakatifu, na
aina yote ya mijengo yao.
10 Na ikawa kwa vile miti ilikuwa michache katika nchi ya upande wa kaskazini,
walisafirisha mingi kwa kutumia meli.
11 Na hivyo waliwezesha watu waliokuwa kwenye nchi ya upande wa kaskazini
kujenga miji mingi, yote ya miti na saruji.
12 Na ikawa kwamba kulikuwa na watu wengi wa watu wa Amoni, ambao walikuwa
Walamani kwa kuzaliwa, ambao pia walienda kwenye nchi hii.
13 Na sasa kuna maandishi mengi juu yao ambayo yameandikwa ya historia ya watu
hawa ambazo ni halisi na kubwa.
14 Lakini tazama, sehemu moja ya mia ya historia ya watu hawa, ndio, historia ya
Walamani na Wanefi, na vita vyao, na mabishano, na mafarakano, na mahubiri yao,
na unabii wao, na meli zao na uundaji wa meli zao, na ujenzi wao wa mahekalu, na
ya masinagogi yao na mahali pao patakatifu, na haki yao, na uovu wao, na mauaji
yao, na uporaji wao, na unyang'anyi wao, na aina yote ya machukizo na ukahaba,
haiwezi kuwekwa yote kwa maandishi haya.
15 Lakini tazama, kuna vitabu vingi na maandishi mengi ya kila aina, na
yameandikwa zaidi na Wanefi.
16 Na kupeana kutoka kizazi kimoja hadi kingine na Wanefi, hata mpaka wameanza
kutenda dhambi na wameuawa, kuporwa, na kuwindwa, na kufukuzwa, na kuuawa,
na kutawanywa usoni mwa ulimwengu, na kuchanganywa na Walamani mpaka
hawaitwi tena Wanefi, wakiwa waovu, na washenzi, na wakatili, ndio, hata kuwa
Walamani.
17 Na sasa narudia tena historia yangu; kwa hivyo, yale ambavyo nimesema
yalifanyika baada ya kuweko mabishano makuu, na misukosuko, na vita, na
mafarakano, miongoni mwa watu wa Nefi.
18 Mwaka wa arubaini na sita wa utawala wa waamuzi uliisha;
19 Na ikawa kwamba kulikuwa bado na ubishi mkubwa nchini, ndio, hata katika
mwaka wa arubaini na saba, na pia mwaka wa arubaini na nane.
20 Walakini Helamani alichukua kiti cha hukumu kwa haki na uadilifu; ndio,
alichunga na kutii sheria na uamuzi, na amri za Mungu; na alifanya kile kilichokuwa
sawasawa machoni mwa Mungu siku zote; na alikuwa na mwendo sawa na baba
yake, mpaka kwamba alifanikiwa nchini.
21 Na ikawa kwamba alikuwa na wana wawili. Alimwita yule mkubwa kwa jina la
Nefi, na mdogo, kwa jina la Lehi. Na walianza kukua wakimtii Bwana.

22 Na ikawa kwamba vita na mabishano yalianza kupunguka, kidogo, miongoni
mwa watu wa Wanefi, katika mwisho wa mwaka wa arubaini na nane wa utawala wa
waamuzi juu ya watu wa Nefi.
23 Na ikawa katika mwaka wa arubaini na tisa wa utawala wa waamuzi,
kuliimarishwa amani ya kudumu katika nchi, yote isipokuwa makundi maovu ya siri
ambayo Gadiantoni mwizi alikuwa ameanzisha katika sehemu za nchi ambazo
zilikuwa zimekaliwa kwa wingi, ambazo wakati huo hazikuwa zimejulikana kwa
viongozi wa serikali; kwa hivyo hawakuangamizwa kutoka nchini.
24 Na ikawa kwamba katika mwaka huo huo kulikuwa na mafanikio mengi sana
katika kanisa, mpaka kwamba kulikuwa na maelfu waliojiunga na kanisa na
walibatizwa ubatizo wa toba.
25 Na mafanikio ya kanisa yalikuwa mengi sana, na baraka nyingi zilipokelewa na
watu, kwamba hata makuhani wakuu na walimu wenyewe walishangaa kupita kiasi.
26 Na ikawa kwamba kazi ya Bwana ilifanikiwa na watu wengi kubatizwa na
kuunganishwa kwa kanisa la Mungu, ndio, hata makumi ya maelfu.
27 Hivyo tunaweza kuona kwamba Bwana ana huruma kwa wote ambao, kwa
uaminifu wa mioyo yao, wanaolingana kwa jina lake takatifu.
28 Ndio, hivyo tunaona kwamba mlango wa mbinguni umefunguliwa kwa wote,
hata kwa wale ambao wataamini katika jina la Yesu Kristo, ambaye ni Mwana wa
Mungu.
29 Ndio, tunaona kwamba yeyote atakaye angelishikilia neno la Mungu, ambalo ni
jepesi na lenye nguvu, ambalo litaangamiza ujanja wote na mitego na hila za ibilisi,
na kumwongoza mfuasi wa Kristo katika njia iliyosonga na nyembamba mpaka
ng'ambo ya shimo la dhiki isiyo na mwisho ambalo lilitayarishwa kumeza waovu —
30 Na kuangusha roho zao, ndio, roho zao zisizokufa, katika mkono wa kuume wa
Mungu katika ufalme wa mbinguni, kuketi chini na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo,
na babu zetu wote watakatifu, ambako hawataondoka tena milele.
31 Na katika mwaka huu kulikuwa na furaha ya kudumu katika nchi ya Zarahemla,
na katika nchi zote zilizokuwa karibu, hata kwenye nchi yote ambayo ilimilikiwa na
Wanefi.
32 Na ikawa kwamba kulikuwa na amani na shangwe kubwa katika mwisho wa
mwaka wa arubaini na tisa; ndio, na pia kulikuwa na amani ya kudumu na shangwe
nyingi katika mwaka wa hamsini wa utawala wa waamuzi.
33 Na katika mwaka wa hamsini na moja wa utawala wa waamuzi kulikuwa na amani
pia, isipokuwa tu kiburi ambacho kilianza kuingia kanisani — sio katika kanisa la
Mungu, lakini katika mioyo ya watu ambao walidai kuwa wa kanisa la Mungu —
34 Na waliinuka kwa kiburi, hata kwenye kudhulumu ndugu zao wengi. Sasa huu
ulikuwa uovu mkubwa, ambao ulisababisha sehemu kubwa ya walio wanyenyekevu
kuumia udhalimu mkuu, na kuvumilia mateso mengi.
35 Walakini walifunga na kuomba kila wakati, na wakapokea nguvu kwa nguvu
katika unyenyekevu wao, na wakawa imara zaidi na imara katika imani ya Kristo,
hadi nafsi zao jikajazwa na shangwe na faraja, ndio, hata kwenye kusafishwa na
utakaso wa mioyo yao, utakaso ambao huja kwa sababu ya wao kumtolea Mungu
mioyo yao.
36 Na ikawa kwamba mwaka wa hamsini na mbili uliisha kwa amani pia, isipokuwa
kiburi kikubwa ambacho kilikuwa kimeingia katika mioyo ya watu; na ilikuwa kwa
sababu ya utajiri wao mwingi na kufanikiwa kwao nchini; na kiliendelea kukua kwao

kutoka siku hadi siku.
37 Na ikawa katika mwaka wa hamsini na tatu wa utawala wa waamuzi, Helamani
alifariki, na mwana wake wa kwanza Nefi akaanza kutawala badala yake. Na ikawa
kwamba alichukua kiti cha hukumu kwa haki na uadilifu; ndio, alitii amri za
Mungu, na alitembea kwa njia za baba yake.

## Helamani 4

1 Na ikawa katika mwaka wa hamsini na nne kulikuwa na mafarakano mengi
kanisani, na kulikuwa na ubishi pia miongoni mwa watu, mpaka kwamba kukawa
na umwagaji mwingi wa damu.
2 Na sehemu ile ya wahalifu waliuawa na kufukuzwa kutoka nchini, na
wakamwendea mfalme wa Walamani.
3 Na ikawa kwamba walijaribu kuwavuruga Walamani kupigana dhidi ya Wanefi;
lakini tazama, Walamani waliogopa sana, mpaka kwamba hawakusikiliza maneno ya
wale waasi.
4 Lakini ikawa katika mwaka wa hamsini na sita wa utawala wa waamuzi, kulikuwa
na waasi ambao walienda kutoka kwa Wanefi na kujiunga na Walamani; na
walifaulu kwa usaidizi wa wale wengine kuwachochea kuwa na hasira dhidi ya
Wanefi; na walijitayarisha mwaka huo wote kwa vita.
5 Na katika mwaka wa hamsini na saba walikuja chini dhidi ya Wanefi kupigana,
na walianza kazi ya mauaji; ndio, mpaka kwamba katika mwaka wa hamsini na nane
wa utawala wa waamuzi walifaulu kupata umiliki wa nchi ya Zarahemla; ndio, na
pia nchi zote, hata mpaka kwenye nchi iliyokuwa karibu na nchi ya Neema.
6 Na Wanefi na majeshi ya Moroniha walifukuzwa hata mpaka kwa nchi ya Neema;
7 Na huko walijiimarisha dhidi ya Walamani, kutoka bahari ya magharibi, hata
mpaka kwenye mashariki; ikiwa safari ya siku moja kwa Mnefi, kwenye mstari ambao
walikuwa wameimarisha na kuweka majeshi yao kulinda nchi yao ya kaskazini.
8 Na hivyo wale waasi wa Wanefi, kwa usaidizi wa jeshi kubwa la Walamani,
walipata nchi yote ya Wanefi ambayo ilikuwa nchi ya upande wa kusini. Na hayo
yote yalifanywa katika miaka ya hamsini na nane hadi ya tisa ya utawala wa waamuzi.
9 Na ikawa katika mwaka wa sitini wa utawala wa waamuzi, Moroniha alifaulu na
majeshi yake kwa kukamata tena sehemu nyingi za nchi; ndio, walipata tena miji
mingi ambayo ilikuwa imeanguka mikononi mwa Walamani.
10 Na ikawa katika mwaka wa sitini na moja wa utawala wa waamuzi walifaulu
kupata tena hata nusu ya umiliki wao wote.
11 Sasa hii hasara kubwa ya Wanefi, na mauaji makubwa ambayo yalifanyika
miongoni mwao, haingefanyika kama haingekuwa uovu wao na machukizo yao
ambayo yalikuwa miongoni mwao; ndio, na ilikuwa pia miongoni mwa wale ambao
walidai kuwa katika kanisa la Mungu.
12 Na ilikuwa kwa sababu ya kiburi cha mioyo yao, kwa sababu ya utajiri wao
mwingi, ndio, ilikuwa kwa sababu ya udhalimu wao kwa maskini, wakiwanyima
chakula chao wale walio na njaa, wakiwanyima mavazi yao wale walio uchi, na
wakiwapiga ndugu zao wanyenyekevu kwenye shavu, na wakifanyia mzaha yale
yaliyo takatifu, wakikana roho ya unabii na ya ufunuo, wakiua, wakiteka nyara,
wakidanganya, wakiiba, wakitenda zinaa, wakiinuka kwa mabishano makuu, na
kukimbilia mbali hadi kwa nchi ya Nefi, miongoni mwa Walamani—

13 Na kwa sababu ya uovu wao huu mkuu, na majivuno yao kwa nguvu yao, waliachiliwa wategemee nguvu zao; kwa hivyo hawakufanikiwa, lakini waliteswa na kuuawa, na kukimbizwa na Walamani, mpaka walipoteza karibu umiliki wa nchi yao yote.
14 Lakini tazama, Moroniha alihubiri vitu vingi kwa watu kwa sababu ya uovu wao, na pia Nefi na Lehi, ambao walikuwa wana wa Helamani, walihubiri vitu vingi kwa watu, ndio, na walitoa unabii wa vitu vingi kwao kuhusu ubaya wao, na kile ambacho kingefanyika kwao kama hawakutubu dhambi zao.
15 Na ikawa kwamba walitubu, na kadiri vile walipotubu walianza kufanikiwa.
16 Kwani Moroniha alipoona kwamba wametubu alithubutu kuwaongoza mbele kutoka mahali pamoja hadi pengine, na kutoka mji mmoja hadi mwingine, hata mpaka walipopata tena nusu ya mali yao na nusu ya nchi yao yote.
17 Na hivyo ukaisha mwaka wa sitini na moja wa utawala wa waamuzi.
18 Na ikawa katika mwaka wa sitini na mbili wa utawala wa waamuzi, kwamba Moroniha hangeweza kupata tena umiliki juu ya Walamani.
19 Kwa hivyo waliacha kusudi lao la kupata nchi yao iliyobakia, kwani Walamani walikuwa wengi sana kwamba ilikuwa vigumu kwa Wanefi kupata uwezo zaidi juu yao; kwa hivyo Moroniha alitumia majeshi yake yote kwa kulinda hizo sehemu ambazo alikuwa amekamata.
20 Na ikawa kwa sababu ya idadi kubwa ya Walamani Wanefi walikuwa na woga mwingi, wasije wakashindwa, na kukanyagwa chini, na kuuawa, na kuangamizwa.
21 Ndio, walianza kukumbuka unabii wa Alma, na pia maneno ya Mosia; na waliona kwamba walikuwa watu wenye shingo ngumu, na kwamba walifikiri amri za Mungu hazina maana;
22 Na kwamba walikuwa wamegeuza na kuzikanyaga kwa miguu yao sheria za Mosia, au kile ambacho Bwana alimwamuru awape watu; na waliona kwamba sheria zao zilikuwa zimeharibika, na kwamba walikuwa wamekuwa watu waovu, mpaka kwamba walikuwa waovu sawa na Walamani.
23 Na kwa sababu ya uovu wao kanisa lilikuwa limeanza kufifia; na wakaanza kutoamini katika roho ya unabii na katika roho ya ufunuo; na hukumu za Mungu ziliwaangalia machoni.
24 Na waliona kwamba walikuwa wamekuwa walegevu, kama ndugu zao, Walamani, na kwamba Roho ya Bwana haikuwahifadhi; ndio, ilikuwa imejiondoa kutoka kwao kwa sababu Roho ya Bwana haishi kwenye mahekalu yasiyo matakatifu—
25 Kwa hivyo Bwana aliacha kuwahifadhi na miujiza yake na uwezo wake usiolinganishwa, kwani walikuwa wameanguka kwa hali ya kutoamini na uovu wa kutisha; na waliona kwamba Walamani walikuwa wengi sana kuliko wao, na isipokuwa wajishikilie kwa Bwana Mungu wao wataangamia bila kizuizi.
26 Kwani tazama, waliona kwamba nguvu za Walamani zilikuwa nyingi kama zao, hata mtu kwa mtu. Na hivyo walikuwa wameanguka kwenye dhambi hii kuu; ndio, hivyo walikuwa wamekuwa wanyonge, kwa sababu ya makosa yao, kwa muda usio wa miaka mingi.

## Helamani 5

1 Na ikawa kwamba katika mwaka huo huo, tazama, Nefi alitoa kiti cha hukumu kwa mtu ambaye jina lake lilikuwa Sezoramu.

2 Kwani kwa vile sheria zao na serikali yao ilianzishwa kwa sauti ya watu, na
waliochagua uovu walikuwa wengi sana kuliko wale waliochagua mazuri, kwa hivyo
walikuwa wanajitayarisha kwa maangamizo, kwani sheria zilikuwa zimechafuliwa.
3 Ndio, na haya hayakuwa yote; walikuwa watu wa shingo ngumu, mpaka kwamba
hawangetawaliwa na sheria wala haki, isipokuwa tu kwa uharibifu wao.
4 Na ikawa kwamba Nefi alikuwa amechoka kwa sababu ya uovu wao; na akaacha
kiti cha hukumu, na akajichagua mwenyewe kuhubiri neno la Mungu siku zake zote
zilizosalia, na kaka yake Lehi pia, siku zake zote zilizosalia;
5 Kwani walikumbuka maneno ambayo baba yao Helamani aliwazungumzia. Na
haya ndiyo maneno aliyosema:
6 Tazama, wana wangu, ninataka kwamba mtii amri za Mungu; na ningetaka
kwamba mwatangazie watu haya maneno. Tazama, nimewapatia majina ya wazazi
wetu wa kwanza ambao walitoka nchi ya Yerusalemu; na nimefanya hivi ili
mnapokumbuka majina yenu mtaweza kuwakumbuka; na mnapowakumbuka
mngekumbuka kazi zao; na mkikumbuka kazi zao mngejua vile imesemwa, na pia
kuandikwa, kwamba walikuwa wazuri.
7 Kwa hivyo, wana wangu, ninataka kwamba mfanye yale ambayo ni mazuri, ili
izungumzwe juu yenu, na pia iandikwe, hata vile ilivyozungumzwa na kuandikwa
juu yao.
8 Na sasa wana wangu, tazama nina kitu kingine ambacho ningetamani mfanye,
kutamani ambako ni, kwamba msifanye hivi vitu ili mjisifu, lakini kwamba mfanye
hivi vitu kujiwekea wenyewe hazina mbinguni, ndio, ambayo ni ya milele, na
ambayo haitafifia; ndio, ili mpate zawadi ya thamani ya uzima wa milele, ambayo
tuna sababu ya kudhani imepewa kwa babu zetu.
9 Ee kumbukeni, kumbukeni, wana wangu, maneno ambayo mfalme Benyamini
aliwazungumzia watu wake; ndio, kumbukeni kwamba hakuna nyingine njia wala
gharama ambayo kwayo binadamu anaweza kuokolewa, isipokuwa kupitia kwa
upatanisho wa damu ya Yesu Kristo, ambaye atakuja; ndio, kumbuka kwamba
anakuja kuukomboa ulimwengu.
10 Na kumbuka pia maneno ambayo Amuleki alimzungumzia Zeezromu, katika
mji wa Amoniha; kwani alimwambia kwamba Bwana lazima atakuja kuwakomboa
watu wake, lakini kwamba hatakuja kuwakomboa katika dhambi zao, lakini
kuwakomboa kutoka kwa dhambi zao.
11 Na ana uwezo aliopewa kutoka kwa Baba kuwakomboa kutoka kwa dhambi zao
kwa sababu ya toba; kwa hivyo ametuma malaika wake kutangaza habari njema ya
hali ya toba, ambayo inaleta uwezo wa Mkombozi, kuwezesha wokovu wa roho zao.
12 Na sasa, wana wangu, kumbukeni, kumbukeni kwamba ni juu ya mwamba wa
Mkombozi wetu, ambaye ni Kristo, Mwana wa Mungu, kwamba lazima mjenge
msingi wenu; kwamba ibilisi atakapotuma mbele pepo zake kali, ndio, mishale yake
kimbungani, wakati mvua yake ya mawe na dhoruba kali itapiga juu yenu,
hautakuwa na uwezo juu yenu kuwavuta chini kwenye shimo la taabu na msiba
usioisha, kwa sababu ya mwamba ambako kwake mmejengwa, ambao ni msingi
imara, msingi ambako watu wote wakijenga hawataanguka.
13 Na ikawa kwamba haya ndiyo maneno ambayo Helamani aliwafundisha wana
wake; ndio, aliwafundisha vitu vingi ambavyo havijaandikwa, na pia vitu vingi
ambavyo vimeandikwa.
14 Na walikumbuka maneno yake; na kwa hivyo walienda mbele, wakitii amri za

Mungu, kufundisha neno la Mungu miongoni mwa watu wote wa Nefi, kuanzia mji
wa Neema;
15 Na baada ya hapo walienda hadi kwa mji wa Gidi; na kutoka mji wa Gidi hadi
mji wa Muleki;
16 Na hata kutoka mji mmoja hadi mwingine, mpaka walipoenda mbele miongoni
mwa watu wote wa Nefi ambao walikuwa katika nchi upande wa kusini; na kutoka
hapo hadi kwenye nchi ya Zarahemla, miongoni mwa Walamani.
17 Na ikawa kwamba walihubiri kwa uwezo mwingi, mpaka kwamba
waliwafadhaisha wengi wa wale waasi ambao walikuwa wameenda huko kutoka kwa
Wanefi, mpaka kwamba walikuja mbele na kukiri dhambi zao na wakabatizwa
ubatizo wa toba, na mara moja wakarudia Wanefi na kujaribu kurekebisha kwao
mabaya ambayo walikuwa wamefanya.
18 Na ikawa kwamba Nefi na Lehi waliwahubiria Walamani kwa uwezo mkubwa na
mamlaka, kwani walikuwa na uwezo na mamlaka waliyopewa kwamba waweze
kusema, na pia yale ambayo wangezungumza yalipewa kwao—
19 Kwa hivyo waliwazungumzia Walamani kwa maajabu makubwa kuwasadikisha,
mpaka kwamba kukawa na elfu nane ya Walamani ambao walikuwa kwenye nchi ya
Zarahemla na karibu na hapo ambao walibatizwa ubatizo wa toba, na
walisadikishwa kwa uovu wa desturi za babu zao.
20 Na ikawa kwamba Nefi na Lehi walienda kutoka hapo mpaka kwenye nchi ya
Nefi.
21 Na ikawa kwamba walikamatwa na jeshi la Walamani na kutupwa gerezani; ndio,
hata kwenye hilo hilo gereza ambamo Amoni na ndugu zake walitupwa na
watumishi wa Limhi.
22 Na baada ya kutupwa gerezani kwa siku nyingi bila chakula, tazama, walienda
kwenye gereza ili wawakamate na kuwaua.
23 Na ikawa kwamba Nefi na Lehi walizungukwa na kile kilichoonekana kama
moto, mpaka kwamba hawangeweza kuthubutu kuwagusa kwa mikono yao kwa
kuogopa kwamba wangeungua Walakini, Nefi na Lehi hawakuungua; na
walionekana kama wanasimama katikati ya moto na hawaungui.
24 Na walipoona kwamba wamezungukwa na nguzo za moto, na kwamba
hazikuwachoma, mioyo yao ilipata ujasiri.
25 Kwani waliona kwamba Walamani hawakuthubutu kuwagusa; wala
hawangethubutu kuwakaribia, lakini walisimama kama bubu kwa mshangao.
26 Na ikawa kwamba Nefi na Lehi walisimama mbele yao na kuanza
kuwazungumzia, wakisema: Msiogope, kwani tazama, ni Mungu ambaye
amewaonyesha hiki kitu cha ajabu, ambamo kwayo imeonyeshwa kwenu kwamba
hamwezi kutuwekea mikono yenu kutuua.
27 Na tazama, wakati wanasema haya maneno, nchi ilitetemeka sana, na kuta za
gereza zilitikisika kama vile zilikaribia kuanguka ardhini; lakini tazama,
hazikuanguka. Na tazama, wale ambao walikuwa gerezani walikuwa Walamani na
Wanefi ambao walikuwa waasi.
28 Na ikawa kwamba walifunikwa na wingu la giza, na woga wa kutisha mno
uliwajia.
29 Na ikawa kwamba kulisikika sauti kama ilitokea juu ya wingu la giza, ikisema:
Tubuni nyinyi, tubuni nyinyi, na msijaribu tena kuwaangamiza watumishi wangu
ambao nimewatuma kwenu kutangaza habari njema.

30 Na ikawa wakati waliposikia sauti hii, na kuona kwamba haikuwa sauti ya radi,
wala haikuwa sauti kubwa ya kuwachanganya, lakini tazama, ilikuwa sauti tulivu na
kadiri, kama mnong'ono, na ilipenya hata kwenye roho—
31 Na ijapokuwa upole wa sauti, tazama ardhi ilitetemeka sana, na kuta za gereza
zikatingishika tena, kama vile zilikuwa ziko karibu kuanguka ardhini; na tazama
wingu la giza, ambalo lilikuwa limewafunika, halikuondoka—
32 Na tazama sauti ilikuja tena, ikisema: Tubuni nyinyi, tubuni nyinyi, kwani
ufalme wa mbinguni uko karibu; na msijaribu tena kuwaangamiza watumishi
wangu. Na ikawa kwamba nchi ilitetemeka tena, na kuta zikatingisika.
33 Na pia tena safari ya tatu sauti ilisikika, na kuzungumza kwao maneno ya ajabu
ambayo hayawezi kuzungumzwa na binadamu; na kuta zikatingisika tena, na nchi
ikatetemeka kama iko karibu kugawanyika katikati.
34 Na ikawa kwamba Walamani hawangeweza kukimbia kwa sababu ya wingu la
giza ambalo liliwafunika; ndio, na pia hawangetembea kwa sababu ya woga ambao
uliwajia.
35 Sasa kulikuwa mmoja miongoni mwao ambaye alikuwa Mnefi kwa kuzaliwa,
ambaye wakati mmoja alikuwa mtu wa kanisa la Mungu lakini akaasi kutoka kwao.
36 Na ikawa kwamba aligeuka, na tazama, aliona kupitia kwenye wingu la giza na
akaona nyuso za Nefi na Lehi; na tazama, ziling'ara sana, hata kama nyuso za
malaika. Na akaona kwamba waliinua macho yao kuelekea mbinguni; na walikuwa
kwa hali kama walikuwa wanaongea au kupaza sauti kwa kiumbe ambacho
walimwangalia.
37 Na ikawa kwamba huyu mtu alipaza sauti kwa umati, kwamba wageuke na
kuangalia. Na tazama, kulikuwa na uwezo uliopewa kwao kwamba waligeuka na
kutazama; na wakaona nyuso za Nefi na Lehi.
38 Na wakamwambia yule mtu: Tazama, hivi vitu vyote vinaamanisha nini, na ni
nani ambaye hawa watu wanaongea naye?
39 Sasa jina la huyu mtu lilikuwa Aminadabu. Na Aminadabu aliwaambia:
Wanaongea na malaika wa Mungu.
40 Na ikawa kwamba Walamani walimwambia: Tutafanya nini, ili hili wingu la giza
liweze kuondolewa kwamba lisitufunike?
41 Na Aminadabu akawaambia: Lazima mtubu, na mlilie ile sauti, hata mpaka
mtakapopata imani katika Kristo, ambaye mlifundishwa kumhusu na Alma, na
Amuleki, na Zeezromu; na wakati mtakapofanya hivi, wingu la giza litatolewa kwa
kutia kivuli kwenu.
42 Na ikawa kwamba wote walianza kulilia sauti ya yule ambaye alitetemesha nchi;
ndio, walilia hata mpaka wingu la giza lilipoondoka.
43 Na ikawa kwamba wakati walipotupa macho yao karibu kuzunguka, na kuona
kwamba wingu la giza limetoweka kutokana na kuwafunika, tazama, waliona
kwamba wamezingirwa, ndio, kila roho, na nguzo ya moto.
44 Na Nefi na Lehi walikuwa katikati yao; ndio, walizingirwa; ndio, walionekana
kama wako katikati ya ndimi za moto, lakini hazikuwadhuru, wala hazikuchoma
kuta za gereza; na walijazwa na hiyo shangwe ambayo haiwezi kuzungumzwa na
iliyojaa utukufu.
45 Na tazama, Roho Mtakatifu wa Mungu alishuka chini kutoka mbinguni, na
kuingia kwenye mioyo yao, na walijazwa kama na moto, na walizungumza maneno
ya ajabu.

46 Na ikawa kwamba kulisikika sauti kwao, ndio, sauti nzuri, kama mnong'ono,
ikisema:
47 Amani, amani iwe kwenu, kwa sababu ya imani yenu kwa yule Mpendwa Sana
wangu, ambaye alikuwepo tangu msingi wa dunia.
48 Na sasa, wakati waliposikia hivi walitupa macho yao ili waone kule ile sauti
ilikotokea; na tazama, waliona mbingu zikifunguka; na malaika wakaja chini
kutoka mbinguni na kuwahudumia.
49 Na kulikuwa karibu watu mia tatu ambao waliona na kusikia hivi vitu; na
waliambiwa waende na wasistajaabu, wala wasiwe na shaka.
50 Na ikawa kwamba walienda mbele, na kuhudumia watu, wakitangaza kote
nchini mahali hapo vitu vyote ambavyo walisikia na kuona, mpaka kwamba sehemu
kubwa ya Walamani ilisadikishwa juu yao, kwa sababu ya ushahidi mwingi ambao
walikuwa wamepata.
51 Na vile wengi walivyosadikishwa, waliweka chini silaha zao za vita na pia chuki
yao na desturi za babu zao.
52 Na ikawa kwamba waliwapatia Wanefi nchi ya umiliki wao.

# Helamani 6

1 Na ikawa kwamba wakati mwaka wa sitini na mbili wa utawala wa waamuzi
ulipoisha, hivi vitu vyote vilikuwa vimefanyika na wengi wa Walamani walikuwa
sehemu nyingi yao, watu wenye haki, mpaka kwamba uzuri wao ulizidi ule wa
Wanefi, kwa sababu ya uthabiti wao na uadilifu wao kwa imani.
2 Kwani tazama, kulikuwa na Wanefi wengi ambao walikuwa wagumu na wasio
tubu na waovu kupindukia, mpaka kwamba walikataa neno la Mungu na mahubiri
yote na unabii ambao ulikuja miongoni mwao.
3 Walakini, watu wa kanisa walikuwa na shangwe nyingi kwa sababu ya ugeuzi wa
Walamani, ndio, kwa sababu ya kanisa la Mungu, ambalo lilikuwa limeanzishwa
miongoni mwao. Na walishirikiana wao kwa wao, na kufurahiana wao kwa wao, na
wakawa na shangwe kubwa.
4 Na ikawa kwamba wengi wa Walamani walikuja kwenye nchi ya Zarahemla, na
walifundisha Wanefi njia ya ugeuzi wao, na wakawasihi wawe na imani na kutubu.
5 Ndio, na wengi walihubiri kwa uwezo mwingi na mamlaka, kwa kuwaleta chini
wengi wao kwenye kina cha unyenyekevu, kuwa wafuasi wanyenyekevu wa Mungu
na Mwanakondoo.
6 Na ikawa kwamba wengi wa Walamani walienda kwenye nchi iliyokuwa upande
wa kaskazini; na pia Nefi na Lehi walienda katika nchi iliyokuwa upande wa
kaskazini, kuhubiria watu. Na hivyo uliisha mwaka wa sitini na tatu.
7 Na tazama, kulikuwa na amani kote nchini, mpaka kwamba Wanefi walienda
popote nchini walipopenda, kama ni miongoni mwa Wanefi au Walamani.
8 Na ikawa kwamba Walamani pia walienda kokote walipopenda, kama ilikuwa
miongoni mwa Walamani au miongoni mwa Wanefi; na hivyo walikuwa na ushirika
huru miongoni mwao, kununua na kuuza, na kupata faida, kulingana na kutaka
kwao.
9 Na ikawa kwamba walikuwa matajiri sana, wote Walamani na Wanefi; na
walikuwa na kiasi kikubwa cha dhahabu, na cha fedha, na kila namna ya chuma ya
thamani, kote nchini kusini na nchini kaskazini.

10 Sasa nchi ya kusini iliitwa Lehi, na nchi ya kaskazini iliitwa Muleki, ambayo
ilikuwa inaitwa baada ya mwana wa Zedekia; kwani Bwana alimleta Muleki katika
nchi ya kaskazini, na Lehi katika nchi ya kusini.
11 Na tazama, kulikuwa na namna yote ya dhahabu katika hizi nchi zote, na fedha,
na vyuma vya thamani vya kila aina; na kulikuwa pia na mafundi wa ustadi, ambao
walifanya kazi na aina yote ya chuma, na waliisafisha; hivyo wakawa matajiri.
12 Walikuza nafaka kwa wingi, kote kaskazini na kusini; na walifanikiwa sana, kote
kaskazini na kusini. Na waliongezeka na kuwa na nguvu sana nchini. Na walikuza
makundi mengi ya wanyama, ndio, ndama wengi.
13 Tazama wanawake wao walifanya kazi kwa bidii na kushona, na walitengeneza
aina zote za nguo, laini za kitani na nguo za kila aina, kufunika uchi wao. Na hivyo
mwaka wa sitini na nne uliisha kwa amani.
14 Na katika mwaka wa sitini na tano walikuwa pia na shangwe na amani, ndio,
kuhubiri kwingi na unabii mwingi kuhusu yale yatakayokuja mbeleni. Na hivyo
ukaisha mwaka wa sitini na tano.
15 Na ikawa kwamba katika mwaka wa sitini na sita wa utawala wa waamuzi,
tazama, Sezoramu aliuawa na mtu asiyejulikana wakati alipokuwa amekalia kiti cha
hukumu. Na ikawa kwamba katika mwaka huo huo, mwana wake, ambaye, alikuwa
amechaguliwa na watu badala yake, pia aliuawa. Na hivyo ukaisha mwaka wa sitini
na sita.
16 Na katika mwanzo wa mwaka wa sitini na saba watu walianza kuwa waovu sana
tena.
17 Kwani tazama, Bwana alikuwa amewabariki sana na utajiri wa ulimwengu
kwamba hawakuwa wamechochewa kuwa na hasira, kupigana, wala kumwaga
damu; kwa hivyo walianza kuweka mioyo yao katika utajiri wao; ndio, walianza
kutafuta kupata faida kwamba wangeinuliwa mmoja juu ya mwingine; kwa hivyo
walianza kufanya mauaji ya siri, na kunyang'anya na kupora, ili wapate faida.
18 Na sasa tazama, wale wauaji na waporaji walikuwa katika kikundi ambacho
kilianzishwa na Kishkumeni na Gadiantoni. Na sasa ilikuwa kwamba kulikuwa na
wengi sana, hata miongoni mwa Wanefi, kutoka kikundi cha Gadiantoni. Lakini
tazama, walikuwa wengi zaidi katika ile sehemu ovu zaidi ya Walamani. Na waliitwa
waporaji na wauaji wa Gadiantoni.
19 Na hao ndio wale ambao walimuua mwamuzi mkuu Sezoramu, na mwana wake,
wakiwa kwenye kiti cha hukumu; na tazama, hawakupatikana.
20 Na sasa ikawa kwamba wakati Walamani walipogundua kwamba kulikuwa na
wezi miongoni mwao walikuwa na huzuni sana; na walitumia mbinu zote kwa
uwezo wao kuwaangamiza kutoka kwa uso wa dunia.
21 Lakini tazama, Shetani alivuruga mioyo ya sehemu kubwa ya Wanefi, mpaka
kwamba wakaungana na yale makundi ya wezi, na waliungana kwa kufanya
maagano yao na viapo vyao, ili wangejilinda na kujihifadhi wenyewe kwa kila hali
yote ngumu ambayo wangekuwemo, kwamba wasiadhibiwe kwa mauaji yao, na
uporaji wao, na wizi wao.
22 Na ikawa kwamba walikuwa na ishara zao, ndio, ishara zao za siri, na maneno yao
ya siri; na hii ili wapambanue mshiriki wa kundi lao ambaye alikuwa ameingia
kwenye agano, kwamba kwa kila uovu ambao ndugu yake angefanya asiumizwe na
ndugu yake, wala na wale ambao walikuwa washiriki wa kundi lake, ambao
walikuwa wamefanya hili agano.

23 Na hivi wangeua, na kuteka nyara, na kuiba, na kufanya ukahaba na namna yote ya uovu, dhidi ya sheria za nchi yao na pia sheria za Mungu.
24 Na yeyote ambaye alikuwa mshiriki wa kundi lao akifichua kwa watu wengine uovu wao na machukizo yao, angejaribiwa, sio kulingana na sheria za nchi yao, lakini kulingana na sheria za uovu wao, ambazo ziliwekwa na Gadiantoni na Kishkumeni.
25 Sasa tazama, ni hivi viapo vya siri na maagano ambayo Alma alimwamuru mwana wake asifichue kwa ulimwengu, isije zikawa njia ya kuleta watu kwa maangamizo.
26 Sasa tazama, hivyo viapo vya siri na maagano havikumfikia Gadiantoni kutoka kwa maandishi ambayo yalitolewa kwa Helamani; lakini tazama, viliwekwa ndani ya moyo wa Gadiantoni na kile kile kiumbe ambacho kiliwashawishi wazazi wetu wa kwanza kula tunda lililokatazwa—
27 Ndio, kile kile kiumbe ambacho kilimshauri Kaini, kwamba kama atamuua kaka yake Habili haitajulikana katika ulimwengu. Na alishauriana na Kaini na wafuasi wake kutokea wakati ule na kuendelea.
28 Na pia ni kile kile kiumbe ambacho kiliweka mahitaji kwa mioyo ya watu kujenga mnara wa urefu wa kutosha ili waweze kufika mbinguni. Na kilikuwa kile kile kiumbe ambacho kiliongoza wale watu waliotoka kwenye mnara huo kuja katika nchi hii; ambao walisambaza kazi ya giza na machukizo kote usoni mwa nchi, mpaka alipovuta watu chini kwenye maangamizo kamili, na kwenye jahanamu isiyo na mwisho.
29 Ndio, ni kile kile kiumbe ambacho kiliweka katika moyo wa Gadiantoni haja ya kuendelea na kazi ya giza, na mauaji ya siri; na ameidhihirisha kutoka mwanzo wa binadamu hadi sasa.
30 Na tazama, ni yeye ambaye ni mwanzilishi wa dhambi zote. Na tazama, huendesha kazi zake za giza na mauaji ya siri, na hutoa hila zao na viapo vyao, na maagano yao, na mipango ya uovu wa kutisha, kutoka kizazi hadi kingine kulingana na vile anavyoweza kupata mioyo ya watoto wa watu.
31 Na sasa tazama, alikuwa ameshawishi mioyo ya Wanefi; ndio, mpaka kwamba walikuwa wamekuwa waovu sana; ndio, wengi wao walikuwa wametoka kwenye njia ya haki, kuzikanyaga kwa miguu yao amri za Mungu, na wakageukia njia zao wenyewe, na wakajitengenezea sanamu za dhahabu na fedha.
32 Na ikawa kwamba haya maovu yote yaliwajia kwa muda usio wa miaka mingi, mpaka kwamba mengi ya haya yaliwajia katika mwaka wa sitini na saba wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.
33 Na uovu wao uliongezeka katika mwaka wa sitini na nane pia, ambao ulileta huzuni kuu na kulia kwa wale walio wa haki.
34 Na hivyo tunaona kwamba Wanefi walianza kufifia katika kutoamini, na kukua kwenye uovu na machukizo, wakati Walamani nao walianza kukua zaidi katika ujuzi wa Mungu wao; ndio, walianza kutii sheria na amri zake, na kutembea katika ukweli na haki mbele yake.
35 Na hivyo tunaona kwamba Roho ya Bwana ilianza kujiondoa kutoka kwa Wanefi, kwa sababu ya uovu wao na ugumu wa mioyo yao.
36 Na hivyo tunaona kwamba Bwana alianza kuwamwagia Walamani Roho yake, kwa sababu ya wema wao na hiari yao ya kuamini maneno yake.
37 Na ikawa kwamba Walamani walisaka lile kundi la wezi la Gadiantoni; na walihubiri neno la Mungu miongoni mwa wengi wao waliokuwa waovu, mpaka kwamba wezi hao waliangamizwa kabisa kutoka miongoni mwa Walamani.

38 Na ikawa kwa upande mwingine, kwamba Wanefi waliwajenga na kuwasaidia,
kuanzia sehemu kubwa ya waliokuwa waovu sana, mpaka walipoenea kote katika
nchi ya Wanefi, na walikuwa wameishawishi sehemu kubwa ya walio haki mpaka
waliposhushwa na kuamini katika kazi zao na kugawana vilivyoibiwa, na kuungana
nao katika mauaji yao ya siri na makundi yao.
39 Na hivyo walipata uwezo wa kuendesha serikali, mpaka kwamba waliikanyagia
chini ya miguu yao na kupiga na kukataa kusaidia masikini na walio watiifu, na
wafuasi wanyenyekevu wa Mungu.
40 Na hivyo tunaona kwamba walikuwa katika hali ya kutisha, na wakijitayarisha
kwa angamizo lisilo na mwisho.
41 Na ikawa kwamba hivyo ukaisha mwaka wa sitini na nane wa utawala wa
waamuzi juu ya watu wa Nefi.

*Unabii wa Nefi, mwana wa Helamani — Mungu anawatisha watu wa Nefi kwamba atawaadhibu kwa hasira yake, kwa maangamizo yao isipokuwa watubu kutokana na uovu wao. Mungu anawapiga watu wa Nefi kwa maradhi ya kuambukiza; wanatubu na kumrudia. Samweli, Mlamani, anatabiria Wanefi.*

# Helamani 7

1 Tazama, sasa ikawa kwamba katika mwaka wa sitini na tisa wa utawala wa waamuzi
juu ya watu wa Wanefi, kwamba Nefi, mwana wa Helamani, alirejea katika nchi ya
Zarahemla kutoka nchi ya kaskazini.
2 Kwani alikuwa anatembea miongoni mwa watu ambao walikuwa katika nchi ya
upande wa kaskazini, na akahubiri neno la Mungu kwao, na alitabiri vitu vingi sana
kwao;
3 Na walikataa maneno yake yote, mpaka kwamba hangeweza kuishi miongoni
mwao, lakini alirejea tena kwenye nchi yake ya kuzaliwa.
4 Na alipoona watu wakiwa kwa hali ya uovu wa kutisha, na wale wezi wa
Gadiantoni wakichukua viti vya hukumu — wakiwa wamejitwalia uwezo na
mamlaka ya nchi; wakiweka amri za Mungu kando, na bila kutenda hata haki ndogo
mbele yake; bila kufanya haki kwa watoto wa watu;
5 Kuhukumu wale wenye haki kwa sababu ya haki yao; kuachilia walio na hatia na
waovu kuenda bila kuadhibiwa kwa sababu ya pesa yao; na juu ya hayo kupewa
nafasi kubwa kwenye ofisi za serikali, kutawala na kufanya kulingana na nia zao, ili
wapate faida na utukufu wa ulimwengu, na juu ya hayo, kwamba wangefanya
uzinifu kwa urahisi, na kuiba, na kuua, na kufanya kulingana na nia zao wenyewe —
6 Sasa huu ubaya uliwajia Wanefi, katika muda wa miaka isiyo mingi; na wakati
Nefi alipoona haya, moyo wake ulifura kwa huzuni ndani ya kifua chake; na alipaza
sauti kwa maumivu ya nafsi yake:
7 Ee, kwamba ningeishi katika siku ambazo babu yangu Nefi alipotoka mara ya
kwanza kutoka Yerusalemu, kwamba ningefurahi na yeye katika ile nchi ya ahadi;
hapo watu wake walikuwa rahisi kufundishwa, imara kutii amri za Mungu, na sio
rahisi kwa wao kuongozwa kufanya ubaya; na walikuwa wepesi kusikiliza neno la
Bwana —
8 Ndio, kama siku zangu zingekuwa kwenye hizo siku, ndipo roho yangu ingejawa

shangwe wa kwa ajili ya haki ya ndugu zangu.
9 Lakini tazama, nimewekewa kwamba hizi ndizo siku zangu, na kwamba roho
yangu itajazwa na huzuni kwa sababu ya huu uovu wa ndugu zangu.
10 Na tazama, sasa ikawa kwamba ilikuwa juu ya mnara, ambao ulikuwa katika
bustani ya Nefi, ambayo ilikuwa kando ya barabara kuu ambayo ilielekea soko kuu,
ambalo ilikuwa katika mji wa Zarahemla; kwa hivyo, Nefi alikuwa amejisujudia
mwenyewe juu ya mnara ambao ulikuwa kwenye bustani yake, mnara ambao pia
ulikuwa karibu na mlango wa bustani, na kando yake kulikuwa na barabara kuu.
11 Na ikawa kwamba kulikuwa baadhi ya watu waliokuwa wakipita kando na
kumwona Nefi akimimina roho yake kwa Mungu juu ya mnara; na walikimbia na
kuwaambia watu kile ambacho walikuwa wameona, na walikuja pamoja kwa wingi
ili wajue sababu ya maombolezi makubwa kwa uovu miongoni mwa watu.
12 Na sasa, wakati Nefi alipoinuka aliona umati wa watu ambao walijikusanya
pamoja.
13 Na ikawa kwamba alifungua kinywa chake na kuwaambia: Tazama, kwa nini
mmejikusanya wenyewe pamoja? Ili niwaambie kuhusu ubaya wenu?
14 Ndio, kwa sababu nimekuja juu ya mnara wangu ili niminine nafsi yangu kwa
Mungu, kwa sababu ya huzuni nyingi ya moyo wangu, ambayo ni kwa sababu ya
maovu yenu!
15 Na kwa sababu ya kuomboleza kwangu na kulia mmejikusanya pamoja, na
mnashangaa; ndio, na mna uhitaji mwingi wa kushangaa; ndio, mnapaswa
kushangaa kwa sababu mmetolewa ili ibilisi ameshikilia sana mioyo yenu.
16 Ndio, mngewezaje kujitolea kwa ushawishi wa yule ambaye anataka kutupa roho
zenu chini kwenye taabu isiyo na mwisho na msiba bila mwisho?
17 Ee tubuni nyinyi, tubuni nyinyi! Kwa nini mnataka kufa? Geukeni nyinyi,
Mgeukieni Bwana Mungu wenu. Kwa nini amewaacha nyinyi?
18 Ni kwa sababu mmeshupaza mioyo yenu; ndio, hamtatii sauti ya mchungaji
mwema; ndio, mmemchokoza kukasirika dhidi yenu.
19 Na tazama, badala ya kuwakusanya, kama hamtatubu, tazama, atawatawanya kila
mahali kwamba mtakuwa chakula kwa mbwa na wanyama wa mwitu.
20 Ee, jinsi gani mmemsahau Mungu wenu katika ile siku ambayo amewaokoa?
21 Lakini tazama, ni kwa sababu ya kupata faida, kusifiwa na watu, ndio, na kwamba
mngepata dhahabu na fedha. Na mmeweka mioyo yenu juu ya utajiri na vitu visivyo
na maana vya ulimwengu huu, kwani kwa ajili yake mnaua, na kuteka nyara, na
kuiba, na kutoa ushahidi wa uwongo dhidi ya majirani zenu, na kufanya aina yote ya
uovu.
22 Na kwa sababu hii ubaya utawapata isipokuwa mtubu. Kwani kama hamtatubu,
tazama, huu mji mkuu, na pia hiyo miji yote mikubwa ambayo iko karibu, ambayo
iko katika nchi ya umiliki wetu, itachukuliwa mbali kwamba hamtakuwa na mahali
penu ndani yao; kwani tazama, Bwana hatawapatia nguvu, vile alifanya hapo awali,
kuwashinda maadui zenu.
23 Kwani tazama, hivi asema Bwana: Sitaonyesha nguvu zangu kwa wale waovu,
wala kwa mmoja zaidi ya mwingine, isipokuwa kwa wale wanaotubu dhambi zao, na
kusikiliza maneno yangu. Sasa kwa hivyo, ningetaka kwamba muelewe, ndugu
zangu, kwamba itakuwa bora kwa Walamani kuliko nyinyi isipokuwa mtubu.
24 Kwani tazama, wao ni wenye haki kuwazidi, kwani hawajatenda dhambi dhidi ya
ile elimu kubwa ambayo mmepokea; kwa hivyo, Bwana atawahurumia; ndio,

ataongeza siku zao na kuongeza uzao wao, hata baada yenu kuangamizwa kabisa
isipokuwa mtubu.
25 Ndio, msiba uwe kwenu kwa sababu ya yale machukizo ambayo yamekuja
miongoni mwenu; na mmejiunga kwake, ndio, kwa lile kundi la siri ambalo
lilianzishwa na Gadiantoni!
26 Ndio, msiba utawajia kwa sababu ya kile kiburi ambacho mmekubali kiingie
kwenye mioyo yenu, ambacho kimewainua juu kupita yale yaliyo mema kwa sababu
ya utajiri wenu mwingi!
27 Ndio, taabu iwe kwenu kwa sababu ya uovu wenu na machukizo!
28 Na msipotubu mtaangamia; ndio, hata nchi zenu zitachukuliwa kutoka kwenu,
na mtaangamizwa kutoka uso wa dunia.
29 Tazama sasa, mimi, binafsi sisemi kwamba vitu hivi vitakuwa, kwa sababu sio
kwa ajili yangu kwamba najua vitu hivi; lakini tazama, najua kwamba vitu hivi ni vya
kweli kwa sababu Bwana Mungu amevidhihirisha kwangu, kwa hivyo nadhibitisha
kwamba vitakuwa.

# Helamani 8

1 Na sasa ikawa kwamba wakati Nefi alipokuwa amesema haya maneno, tazama,
kulikuwa na watu ambao walikuwa waamuzi, ambao pia walikuwa wa kundi la siri la
Gadiantoni, na walikasirika, na waliongea kwa sauti dhidi yake, wakiwaambia watu:
Kwa nini hamwezi kumkamata huyu mtu na kumleta mbele, ili ahukumiwe
kulingana na kosa ambalo ametenda?
2 Kwa nini mnamwangalia mtu huyu, na kumsikiliza akitukana hawa watu na
sheria zetu?
3 Kwani tazama, Nefi alikuwa amewazungumzia kuhusu sheria yao chafu; ndio,
Nefi alisema vitu vingi ambavyo haviwezi kuandikwa; na hakusema kitu chochote
ambacho kilikuwa kinyume kwa amri za Mungu.
4 Na wale waamuzi walimkasirikia kwa sababu aliongea wazi kwao kuhusu kazi zao
za siri za giza; walakini, hawakuthubutu kuweka mikono yao kwake, kwani
waliogopa watu wasipaze sauti dhidi yao.
5 Kwa hivyo, walilia kwa watu, wakisema: Kwa nini nyinyi mvumilie huyu mtu
kututukana? Kwani tazama anahukumu hawa watu wote, hata kwenye
maangamizo; na pia kwamba hii miji yetu mikubwa itachukuliwa kutoka kwetu,
kwamba hatutakuwa na nafasi ndani yao.
6 Na sasa tunajua kwamba hii haiwezekani, kwani tazama, tuna nguvu, na miji yetu
ni mikubwa, kwa hivyo maadui zetu hawawezi kuwa na nguvu juu yetu.
7 Na ikawa kwamba waliwavuruga watu kumkasirikia Nefi, na wakaanzisha
mabishano miongoni mwao; kwani kulikuwa na wengine waliopaza sauti: Acha
huyu mtu pekee, kwani ni mtu mzuri, na vitu vile ambavyo amesema vitafanyika bila
shaka isipokuwa tutubu;
8 Ndio, tazama, hukumu zote zitatujia ambazo ameshuhudia kwetu; kwani tunajua
kwamba ameshuhudia sawa kwetu kuhusu uovu wetu. Na tazama ziko nyingi, na pia
anajua vitu vyote ambavyo vitafanyika kwetu vile anavyojua uovu wetu wote.
9 Ndio, na tazama, kama hangekuwa nabii hangeweza kushuhudia kuhusu hivyo
vitu.
10 Na ikawa kwamba watu ambao walitaka kumwangamiza Nefi walilazimishwa

kwa sababu ya woga wao, kwamba hawakuweka mikono yao kwake; kwa hivyo
alianza tena kuwazungumzia, akiona kwamba amepata mapendeleo ndani ya fikira
za wengine wao, mpaka kwamba waliosalia waliogopa.
11 Kwa hivyo alilazimishwa kuzungumza zaidi kwao akisema: Tazama, ndugu
zangu, hamjasoma kwamba Mungu aliupatia uwezo kwa mtu mmoja, hata Musa,
kupiga juu ya maji ya Bahari ya Shamu, na yakagawanyika hapa na pale, mpaka
kwamba Waisraeli, ambao walikuwa babu zetu, walipita nchi kavu, na maji yakaja
tena pamoja juu ya majeshi ya Wamisri na kuwazamisha?
12 Na sasa tazama, ikiwa Mungu alimpa huyu mtu uwezo kama huo, basi kwa nini
nyinyi mnashindana miongoni mwenu, na kusema kwamba hajanipatia mimi uwezo
ambamo kwake ningejua kuhusu hukumu ambazo zitatolewa kwenu isipokuwa
mtubu?
13 Lakini, tazama, hamkatai tu maneno yangu, lakini pia mnakataa maneno yote
ambayo yalizungumzwa na babu zetu, na pia maneno ambayo yamezungumzwa na
huyu mtu, Musa, ambaye alipewa nguvu nyingi hivyo kwake, ndio, maneno ambayo
alizungumza kuhusu kuja kwa Masiya.
14 Ndio, sio yeye aliyeshuhudia kwamba Mwana wa Mungu atakuja? Na vile aliinua
nyoka wa shaba nyikani, hata hivyo atainuliwa yule atakayekuja.
15 Na vile wengi wangemtazama yule nyoka wangeishi, hata hivyo jinsi vile wengi
wataangalia juu kwa Mwana wa Mungu na imani, wakiwa na roho iliyovunjika,
wataishi, hata kwenye maisha ambayo ni ya milele.
16 Na sasa tazama, Musa hakushuhudia tu hivi vitu peke yake, lakini pia manabii
wote watakatifu, tangu siku zake hata mpaka siku za Ibrahimu.
17 Ndio, na tazama, Ibrahimu aliona kuja kwake, na akajazwa na uchangamfu na
alifurahi.
18 Ndio, na tazama nawaambia, kwamba Ibrahimu hakujua tu hivi vitu, lakini
kulikuwa na wengi kabla ya siku za Ibrahimu ambao waliitwa kwa amri ya Mungu;
ndio, hata baada ya amri ya Mwana wake; na hivi ili ionyeshwe kwa watu, miaka elfu
nyingi kabla ya kuja kwake, kwamba hata ukombozi utawajia.
19 Na sasa ningetaka kwamba mjue, kwamba hata tangu siku za Ibrahimu
kumekuwa na manabii wengi ambao wameshuhudia hivi vitu; ndio, tazama, nabii
Zeno alishuhudia kwa ujasiri; na kwa kufanya hivyo aliuawa.
20 Na tazama, pia Zenoki, na pia Ezia, na pia Isaya, na Yeremia, (Yeremia akiwa yule
yule nabii ambaye alishuhudia kuharibiwa kwa Yerusalemu) na sasa tunajua kwamba
Yerusalemu iliangamizwa kulingana na maneno ya Yeremia. Ee basi kwa nini
Mwana wa Mungu asije, kulingana na unabii wake?
21 Na sasa mtakataa kukubali kwamba Yerusalemu iliharibiwa? Mtasema kwamba
wana wa Zedekia hawakuuawa, wote isipokuwa tu Muleki? Ndio, na hamwoni
kwamba wana wa Zedekia wako pamoja nasi, na walifukuzwa kutoka nchi ya
Yerusalemu? Lakini tazama, haya sio yote—
22 Babu yetu Lehi alikimbizwa kutoka Yerusalemu kwa sababu alishuhudia hivi
vitu. Nefi pia alishuhudia hivi vitu, na pia karibu babu zetu wote, hata kuja chini
kwa wakati huu; ndio, wameshuhudia kuja kwa Kristo, na wamengojea, na
wamefurahia siku yake ambayo itakuja.
23 Na tazama, yeye ni Mungu, na yuko pamoja nao, na alijidhihirisha kwao, kwamba
walikombolewa na yeye; na wakamtukuza, kwa sababu ya yale ambayo yatakuja.
24 Na sasa, ni wazi kuwa mnajua hivi vitu na hamwezi kuvikana isipokuwa

mdanganye, kwa hivyo katika haya mmetenda dhambi, kwani mmekataa hivi vitu
vyote ingawa mmepata ushuhuda mwingi; ndio, hata mmepokea vitu vyote, vyote
vitu vya mbinguni, na vitu vyote vilivyo ardhini, kama ushahidi kwamba viko kweli.
25 Lakini tazama, mmekataa ukweli, na mmeasi dhidi ya Mungu wenu mtakatifu;
na hata wakati huu, badala ya kujiwekea hazina mbinguni, mahali ambapo hakuna
chochote kitakachochafua, na ambapo hakuna kile kitakachokuja ambacho si safi,
mnajirundikia ghadhabu dhidi ya siku ya hukumu.
26 Ndio, hata wakati huu mnajiweka tayari, kwa sababu ya mauaji yenu, na uasherati
na uovu, kwenye uangamizo usio na mwisho; ndio, na isipokuwa mtubu utawajia
upesi.
27 Ndio, tazama uko sasa hata kwenye milango yenu; ndio, nendeni kwenye kiti cha
hukumu, na mpeleleze; na tazama, mwamuzi wenu ameuawa, na analalia damu
yake; na ameuawa na kaka yake, ambaye anatazamia kiti cha hukumu.
28 Na tazama, wote ni washiriki wa kundi lenu la siri, ambalo mwanzilishi wake ni
Gadiantoni na mwovu ambaye anataka kuangamiza roho za wanadamu.

## Helamani 9

1 Tazama, sasa ikawa kwamba wakati Nefi alipokuwa amezungumza haya maneno,
baadhi ya watu ambao walikuwa miongoni mwao walikimbilia kwenye kiti cha
hukumu; ndio, hata kulikuwa na watano ambao walienda, na wakasema baina yao,
wakienda:
2 Tazama, sasa tutajua kwa kweli kama huyu mtu ni nabii na ameamriwa na
Mungu kutabiri vitu vya maajabu kama hivi kwetu. Tazama, hatuamini kwamba
amemwamuru; ndio, hatuamini kwamba yeye ni nabii; lakini, ikiwa hiki kitu
ambacho amesema kuhusu mwamuzi mkuu kitakuwa cha kweli, kwamba amekufa,
ndipo tutaamini kwamba yale maneno mengine ambayo amesema ni ya kweli.
3 Na ikawa kwamba walikimbia kwa nguvu vile wawezavyo, na kufikia kiti cha
hukumu; na tazama, mwamuzi mkuu alikuwa ameanguka ardhini, na alikuwa
amelalia damu yake.
4 Na sasa tazama, wakati walipoona hivi walishangaa sana, mpaka kwamba
waliinama kwenye ardhi; kwani walikuwa hawajaamini maneno ambayo Nefi
alisema kuhusu mwamuzi mkuu.
5 Lakini sasa, wakati walipoona waliamini, na woga ukawajia isiwe hukumu zote
ambazo Nefi alizungumzia ziwajie watu; kwa hivyo walitetemeka, na waliinama
kwenye ardhi.
6 Sasa, mara mwamuzi alikuwa ameuawa—yeye akiwa amechomwa na kaka yake
kwa mpango wa siri, na alitoroka, na watumishi walikimbia na kuwaambia watu,
wakipasa kilio cha mauaji miongoni mwao;
7 Na tazama watu walijikusanya pamoja katika pahali pa kiti cha hukumu—na
tazama, kwa kustaajabu kwao waliona wale watu watano ambao walikuwa
wameinama kwenye ardhi.
8 Na sasa tazama, watu hawakuwa wamejua kuhusu umati ambao ulijikusanya
pamoja kwenye bustani ya Nefi; kwa hivyo walisema miongoni mwao: Hawa ndio
watu ambao wamemuua mwamuzi, na Mungu amewalaani kwamba hawangeweza
kutoroka kutoka kwetu.
9 Na ikawa kwamba waliwashika kwa ghafla, na kuwafunga na kuwatupa gerezani.

Na matangazo yakatumwa kote kwamba mwamuzi ameuawa, na kwamba wauaji
wamekamatwa na wametupwa gerezani.
10 Na ikawa kwamba kesho yake watu walijikusanya pamoja kuomboleza na
kufunga, katika mazishi ya mwamuzi mkuu ambaye aliuawa.
11 Na hivyo pia wale waamuzi ambao walikuwa kwenye bustani ya Nefi, na walisikia
maneno yake, pia walikusanyika pamoja kwenye mazishi.
12 Na ikawa kwamba walipeleleza miongoni mwa watu, wakisema: Wako wapi wale
watano ambao walitumwa kupeleleza kuhusu mwamuzi mkuu kama amekufa? Na
walijibu wakisema: Kuhusu hawa watano ambao mnasema mliwatuma, hatujui;
lakini kunao watano ambao ni wauaji, ambao tumetupa gerezani.
13 Na ikawa kwamba waamuzi walitaka kwamba waletwe mbele yao; na waliletwa,
na tazama walikuwa wale watu watano ambao walitumwa; na tazama waamuzi
waliwahoji kujua kuhusu lile jambo, na waliwaambia yote ambayo walifanya,
wakisema:
14 Tulikimbia na kuja mahali pa kiti cha hukumu, na tulipoona vitu vyote vile Nefi
aliposhuhudia, tulishangaa mpaka kwamba tuliinama kwenye ardhi; na wakati
tulipopata nguvu kutokana na mshangao wetu, tazama walitutupa gerezani.
15 Sasa, kuhusu mauaji ya huyu mtu, hatujui ni nani aliyeifanya; na hivi tu ndivyo
tunajua, tulikimbia na kuja vile mlivyotaka, na tazama alikuwa amekufa, kulingana
na maneno ya Nefi.
16 Na sasa ikawa kwamba waamuzi walielezea watu mambo haya, na walizungumza
kwa sauti dhidi ya Nefi, wakisema: Tazama, tunajua kwamba huyu Nefi lazima
alikuwa amekubaliana na mtu kumuua mwamuzi, na ili atutangazie, ili atubadilishe
kwa imani yake, ili ajiweke kuwa mtu mkubwa, aliyechaguliwa na Mungu, na pia
nabii.
17 Na sasa tazama, tutamgundua huyu mtu, na ataungama makosa yake na
kutuambia muuaji wa kweli wa huyu mwamuzi.
18 Na ikawa kwamba wale watano waliachiliwa kwenye siku ya mazishi. Walakini,
waliwakemea waamuzi kwa sababu ya maneno ambayo walisema dhidi ya Nefi, na
wakapingana nao mmoja mmoja, mpaka kwamba wakawatunduwaza.
19 Walakini, walisababisha kwamba Nefi achukuliwe na kufungwa na aletwe mbele
ya umati, na wakaanza kumhoji kwa njia mbali mbali ili wamchanganyishe, ili
wamshtaki kwa makosa ya kifo—
20 Wakimwambia: Wewe ni mshiriki; ni nani huyu mtu ambaye amefanya haya
mauaji? Sasa tuambie, na ukubali makosa yako, ukisema: Tazama hapa kuna pesa;
na pia tutakuachia maisha yako ikiwa utatuambia, na ukiri makubaliano ambayo
ulifanya na yeye.
21 Lakini Nefi aliwaambia: Ee nyinyi wajinga, nyinyi msiotahiriwa moyoni, nyinyi
vipofu, nyinyi watu wenye shingo ngumu, mnajua ni muda gani Bwana Mungu
atawakubalia kwamba mwendelee na hizi njia zenu za dhambi?
22 Ee mnapaswa kuanza kulia na kuomboleza, kwa sababu ya maangamizo
makubwa ambayo yanawangojea wakati huu, isipokuwa mtubu.
23 Tazama mnasema kwamba nilikubaliana na mtu kumuua Seezoramu, mwamuzi
wetu mkuu. Lakini tazama, ninawaambia, hii ni kwa sababu nimeshuhudia kwenu
kwamba mngejua kuhusu hiki kitu; ndio, hata kwa ushuhuda kwenu, kwamba
nilijua uovu na machukizo ambayo yapo miongoni mwenu.
24 Na kwa sababu nimefanya hivi, mnasema kwamba nilikubaliana na mtu kwamba

afanye hiki kitu; ndio, kwa sababu niliwaonyesha ishara hii mnanikasirikia, na mnataka kuangamiza maisha yangu.

25 Na sasa tazama, nitawaonyesha ishara nyingine, na nione ikiwa kwa hiki kitu mtataka kuniangamiza.

26 Tazama nawaambia: Nendeni kwa nyumba ya Seantumu, ambaye ni kaka ya Seezoramu, na mmwambie—

27 Nefi, ambaye ni nabii wa kujifanya, ambaye anatoa unabii kuhusu uovu mwingi wa hawa watu, alikubaliana nawe, ili umuue Seezoramu, ambaye ni kaka yako?

28 Na tazama, atawaambia, Hapana.

29 Na mtasema kwake: Wewe umemuua kaka yako?

30 Na atasimama na woga, na hatajua la kusema. Na tazama, atakana kwenu; na atajifanya kama amestaajabu; walakini, atawaelezea kwamba hana hatia.

31 Lakini tazama, mtamjaribu, na mtapata damu upande wa chini wa kanzu yake.

32 Na wakati mtaona hivi, mtasema: Hii damu inatoka wapi? Unafikiri hatujui kama hii ni damu ya kaka yako?

33 Na ndipo atatetemeka, na kunyauka, hata kama aliyekufa.

34 Na hapo mtasema: Kwa sababu ya huu woga wako na huu ugeukaji wa rangi yako ambao umekuja kwa uso wako, tazama, tunajua kwamba una hatia.

35 Na pale woga zaidi utamjia; na hapo atakiri kwenu, na hatakana tena kwamba amefanya haya mauaji.

36 Na hapo atawaambia, kwamba mimi, Nefi, sijui chochote kuhusu hili jambo isipokuwa iwe imetolewa kwangu na uwezo wa Mungu. Na ndipo mtajua kwamba mimi ni mtu mwaminifu, na kwamba nimetumwa kwenu kutoka kwa Mungu.

37 Na ikawa kwamba walienda na kufanya, hata kulingana na vile Nefi alivyokuwa amewaambia. Na tazama, yale maneno ambayo alikuwa amesema yalikuwa kweli; kwani kulingana na maneno alikana; na pia kulingana na maneno alikiri.

38 Na alifanywa kukiri kwamba yeye mwenyewe alikuwa muuaji, mpaka kwamba wale watano waliachiliwa huru, na pia Nefi.

39 Na kulikuwa baadhi ya Wanefi ambao waliamini maneno ya Nefi; na kulikuwa na baadhi ya wengine, walioamini kwa sababu ya ushuhuda wa wale watano, kwani walikuwa wamegeuka walipokuwa gerezani.

40 Na sasa kulikuwa na wengine miongoni mwa watu, ambao walisema kwamba Nefi alikuwa nabii.

41 Na kulikuwa na wengine ambao walisema: Tazama, yeye ni aina ya mungu, kwani kama hangekuwa mungu hangejua hivi vitu. Kwani tazama, ametuambia fikira za mioyo yetu, na pia ametuambia vitu; na hata ameleta kwenye elimu yetu muuaji wa kweli wa mwamuzi wetu mkuu.

## Helamani 10

1 Na ikawa kwamba kulitokea mgawanyiko miongoni mwa watu, mpaka kwamba walijigawa hapa na pale na kuenda njia zao, wakimwacha Nefi peke yake, mahali alipokuwa amesimama katikati yao.

2 Na ikawa kwamba Nefi alijiendea njia yake kuelekea nyumba yake, akitafakari juu ya vitu ambavyo Bwana alikuwa amemfichulia.

3 Na ikawa vile alipokuwa akitafakari—akiwa amehuzunishwa kwa sababu ya uovu wa watu wa Wanefi, kazi zao za siri na za giza, na mauaji yao, na utekaji nyara

wao, na aina yote ya ubaya — na ikawa vile alikuwa anatafakari kwenye moyo wake,
tazama, sauti ilikuja kwake ikisema:
4 Umebarikiwa ewe, Nefi, kwa hivyo vitu ambavyo umefanya; kwani nimeona vile
umetangaza neno bila kusita, neno ambalo nimekupatia, kwa hawa watu. Na
hujawaogopa, na hujatazamia maisha yako, lakini umetazamia kusudi langu, na kutii
amri zangu.
5 Na sasa, kwa sababu umefanya hivi bila kusita, tazama, nitakubariki milele; na
nitakufanya mwenye nguvu kwa neno na vitendo, katika imani na vitendo; ndio,
hata kwamba vitu vyote vitafanyika kwako kulingana na neno lako, kwani hutauliza
kile ambacho ni kinyume cha kusudi langu.
6 Tazama, wewe ni Nefi, na mimi ni Mungu. Tazama, ninatangaza kwako katika
uwepo wa malaika wangu, kwamba utakuwa na uwezo juu ya hawa watu, na utalaani
ardhi na njaa, na ugonjwa wa kuambukiza, na uangamizo, kulingana na uovu wa
hawa watu.
7 Tazama, ninakupatia uwezo, kwamba lolote utakalofunga duniani litafungwa
mbinguni; na lolote utakalofungua duniani litafunguliwa mbinguni; na hivyo
utakuwa na uwezo miongoni mwa watu hawa.
8 Na hivyo, ikiwa utaliambia hekalu hili ligawanyike mara mbili, itafanyika.
9 Na ikiwa utauambia huu mlima, Rudi chini na uwe laini, itafanyika.
10 Na tazama, ikiwa utasema kwamba Mungu atalaani hawa watu, itakuwa hivyo.
11 Na sasa, tazama, ninakuamuru, kwamba utaenda na kuwatangazia watu hawa,
kwamba hivi asema Bwana Mungu, ambaye ni Mwenyezi: Msipotubu mtapigwa,
hata mpaka mtakapoangamizwa.
12 Na tazama, sasa ikawa kwamba wakati Bwana alipokuwa amesema haya maneno
kwa Nefi, alisimama na hakuenda kwa nyumba yake, lakini alirejea kwenye makundi
ambayo yalikuwa yametawanyika nchini, na akaanza kuwatangazia neno la Bwana
ambalo lilisemwa kwake, kuhusu kuangamizwa kwao kama hawakutubu.
13 Sasa tazama, ijapokuwa ule muujiza mkuu ambao Nefi alikuwa amefanya kwa
kuwaambia kuhusu kifo cha mwamuzi mkuu, walishupaza mioyo yao na hawakutii
maneno ya Bwana.
14 Kwa hivyo Nefi alitangaza kwao neno la Bwana, akisema: Isipokuwa mtubu, hivi
asema Bwana, mtapigwa hata mpaka mtakapoangamizwa.
15 Na ikawa kwamba wakati Nefi alipowatangazia neno, tazama, bado walishupaza
mioyo yao na hawakusikiliza maneno yake; kwa hivyo walitoa mashutumu dhidi
yake, na walitaka kujaribu kumshika ili wamtupe gerezani.
16 Lakini tazama, nguvu za Mungu zilikuwa na yeye, na hawangemkamata na
kumtupa gerezani, kwani alichukuliwa na Roho kutoka miongoni mwao na
kubebwa kutoka kwao.
17 Na ikawa kwamba hivyo ndivyo aliendа katika Roho, kutoka kwa umati hadi
mwingine, akitangaza neno la Mungu, hata mpaka alipokuwa amewatangazia wote,
au kutuma ujumbe miongoni mwa watu wote.
18 Na ikawa kwamba hawakusikiliza maneno yake, na kukaanza kuwa na
mabishano, mpaka kwamba waligawanyika dhidi yao wenyewe na wakaanza kuuana
kwa upanga.
19 Na hivyo ukaisha mwaka wa sabini na moja wa utawala wa waamuzi juu ya watu
wa Nefi.

# Helamani 11

1 Na ikawa katika mwaka wa sabini na mbili wa utawala wa waamuzi kwamba
mabishano yaliongezeka, mpaka kwamba kukawa na vita kote nchini miongoni
mwa watu wa Nefi.
2 Na lilikuwa hili kundi la siri la wezi ambalo liliendelea na hii kazi ya uharibifu na
uovu. Na hivi vita viliendelea huo mwaka wote; na katika mwaka wa sabini na tatu
pia viliendelea.
3 Na ikawa kwamba katika huu mwaka Nefi alimlilia Bwana, akisema:
4 Ee Bwana, usikubali kwamba hawa watu waangamizwe kwa upanga; lakini Ee
Bwana, afadhali kuwe na njaa nchini, iwavuruge wakumbuke Bwana Mungu wao,
na labda watatubu na kugeuka kwako.
5 Na hivyo ilifanyika, kulingana na maneno ya Nefi. Na kulikuwa na njaa kubwa
sana katika nchi, miongoni mwa watu wote wa Nefi. Na hivyo katika mwaka wa
sabini na nne njaa iliendelea, na kazi ya kuangamiza kwa upanga ilikwisha lakini
ikawa nyingi kwa njaa.
6 Na hii kazi ya uangamizo pia iliendelea katika mwaka wa sabini na tano. Kwani
nchi ililaaniwa kwamba ilikauka, na haikuzalisha nafaka wakati wa nafaka; na nchi
yote ililaaniwa, hata miongoni mwa Walamani na pia miongoni mwa Wanefi, hata
kwamba walipigwa kwamba waliangamia kwa maelfu katika sehemu zilizokuwa
mbovu zaidi ya nchi.
7 Na ikawa kwamba watu waliona kwamba walikuwa karibu kuangamia kwa
sababu ya njaa, na wakaanza kumkumbuka Bwana Mungu wao; na walianza
kukumbuka maneno ya Nefi.
8 Na watu walianza kupeleka hoja kwa waamuzi wakuu na viongozi wao, ili
waseme kwa Nefi: Tazama, tunajua kwamba wewe ni mtu wa Mungu, kwa hivyo
mlilie Bwana Mungu wetu kwamba amalize hii njaa, isiwe maneno yote ambayo
umesema kuhusu uangamizo wetu yaje yakafanyika.
9 Na ikawa kwamba waamuzi walimwambia Nefi, kulingana na maneno ambayo
yalikuwa yanatakwa. Na ikawa kwamba wakati Nefi alipoona kwamba watu
wametubu na kujinyenyekeza ndani ya nguo za gunia, alimlilia tena Bwana, akisema:
10 Ee Bwana, tazama hawa watu wametubu; na wamefutilia mbali kundi la
Gadiantoni kutoka miongoni mwao mpaka kwamba wamemalizika, na wameficha
mipango yao ya siri ardhini.
11 Sasa, Ee Bwana, kwa sababu ya huu unyenyekevu ambao wanao nakuomba
uondoe hasira yako, na uache hasira yako itulizwe katika uangamizo wa wale waovu
ambao kitambo umeangamiza.
12 Ee Bwana, je, utabadilisha hasira yako, ndio, hasira yako kali, na usababishe
kwamba hii njaa iishe katika nchi hii.
13 Ee Bwana, je, utanisikiliza, na kusababisha kwamba ifanyike kulingana na
maneno yangu, na utume mvua juu ya dunia, kwamba izalishe matunda yake, na
nafaka yake katika wakati wa nafaka.
14 Ee Bwana, ulisikiliza maneno yangu, wakati nilisema, Acha kuwe na njaa, ili
maradhi ya upanga ipate kuisha; na ninajua kwamba wewe; hata wakati huu,
utasikiza maneno yangu, kwani ulisema kwamba: Ikiwa hawa watu watatubu
nitawasamehe.
15 Ndio, Ee Bwana, na umeona kwamba wametubu, kwa sababu ya njaa na ugonjwa
wa kuambukiza na maangamizo ambayo yamewajia.

16 Na sasa, Ee Bwana, utaacha hasira yako, na uwajaribu tena kama watakutumikia?
Na ikiwa hivyo, Ee Bwana, unaweza kuwabariki kulingana na maneno yako ambayo
ulisema.
17 Na ikawa kwamba katika mwaka wa sabini na sita Bwana aliondoa hasira yake
kwa watu, na kusababisha mvua kunyesha juu ya nchi, mpaka kwamba ikazalisha
matunda yake katika majira ya matunda. Na ikawa kwamba ardhi ilileta nafaka
katika majira ya nafaka.
18 Na tazama, watu walifurahi na kumtukuza Mungu, na nchi yote ilijaa na furaha;
na hawakutaka tena kumwangamiza Nefi, lakini walimheshimu kama nabii mkuu,
na mtu wa Mungu, ambaye alikuwa na uwezo mwingi na mamlaka ambayo ilitolewa
kwake kutoka kwa Mungu.
19 Na tazama, Lehi, kaka yake, hakuwa nyuma hata chembe moja kwa vitu
vilivyohusika na haki.
20 Na hivyo ikawa kwamba watu wa Nefi walianza kufanikiwa tena nchini, na
wakaanza kujenga mahala pao palipokuwa ukiwa, na wakaanza kuongezeka na
kutawanyika, hata kwamba wakawa kote nchini, kote kaskazini na kusini, kutoka
kwa bahari ya magharibi hadi kwenye bahari ya mashariki.
21 Na ikawa kwamba mwaka wa sabini na sita uliisha kwa amani. Na mwaka wa
sabini na saba ukaanza kwa amani; na kanisa lilienea kote nchini; na sehemu kubwa
ya watu, wote Wanefi na Walamani, walikuwa ndani ya kanisa, na walikuwa na
amani kubwa sana nchini; na hivyo mwaka wa sabini na saba uliisha.
22 Na pia walikuwa na amani katika mwaka wa sabini na nane, isipokuwa tu
mabishano machache kuhusu mafundisho ya dini ambayo yalikuwa yameandikwa
chini na manabii.
23 Na katika mwaka wa sabini na tisa kulianza kuwa na mzozo mkuu. Lakini ikawa
kwamba Nefi na Lehi, na wengi wa ndugu zao ambao walijua kuhusu ukweli wa
mafundisho ya dini, wakiwa na mafunuo mengi kila siku, kwa hivyo waliwahubiria
watu, mpaka kwamba wakaweka kikomo kwa mzozo wao katika mwaka huo huo.
24 Na ikawa kwamba katika mwaka wa themanini wa utawala wa waamuzi juu ya
watu wa Nefi, kulikuwa na idadi fulani ya waasi kutoka kwa watu wa Nefi, ambao
miaka kadhaa iliyopita walikuwa wameenda kuishi na Walamani, na kujiita
wenyewe Walamani, na pia idadi fulani ambao walikuwa kizazi halisi cha Walamani,
ambao walivurugwa kukasirika na hawa, au na wale waasi, kwa hivyo walianza vita
na ndugu zao.
25 Na wakafanya mauaji, na uporaji; na kisha wangerudi nyuma kwenye milima, na
kwenye nyika na mahali pa siri, wakijificha ili wasipatikane, wakipokea kila siku
idadi ya waasi, waliojiunga nao.
26 Na hivyo baada ya muda, ndio, hata kwa muhula usio wa miaka mingi, walipata
kuwa kundi kubwa sana la wezi; na waligundua mipango yote ya siri ya Gadiantoni;
na hivyo wakawa wezi wa Gadiantoni.
27 Sasa tazama, hawa wezi walifanya hasara kubwa sana, ndio, hata uharibifu mkuu
miongoni mwa watu wa Nefi, na pia miongoni mwa watu wa Walamani.
28 Na ikawa kwamba ilikuwa ni muhimu kwamba kuweko na kikomo cha kazi hii ya
uharibifu; kwa hivyo walituma jeshi la watu wenye nguvu katika nyika na juu ya
milima kutafuta hili kundi la wezi, na kuwaangamiza.
29 Lakini tazama, ikawa kwamba katika mwaka huo huo walirudishwa nyuma hata
mpaka kwenye nchi zao. Na hivyo ukaisha mwaka wa themanini wa utawala wa

waamuzi juu ya watu wa Nefi.
30 Na ikawa katika mwanzo wa mwaka wa themanini na moja walipigana tena na
kundi hili la wezi, na kuangamiza wengi; na wengi wao pia waliangamizwa.
31 Na walilazimishwa tena kuondoka kwenye nyika na kuondoka kwenye milima
hadi kwenye nchi zao, kwa sababu ya ukubwa wa idadi ya wale wanyang'anyi ambao
walitapakaa kwenye nyika na milimani.
32 Na ikawa kwamba hivyo ukaisha mwaka huu. Na wezi walizidi kuongezeka na
kuwa na nguvu, mpaka kwamba wakadharau majeshi yote ya Wanefi, na pia ya
Walamani; na walisababisha woga mwingi sana kwa watu nchini kote.
33 Ndio, kwani walishambulia sehemu nyingi za nchi, na kufanya uharibifu mwingi
kwao; ndio, waliua wengi, na kuchukua wengine kama mateka hadi kwenye nyika,
ndio, na hasa zaidi wanawake na watoto wao.
34 Sasa huu ubaya mkuu, ambao uliwajia watu kwa sababu ya uovu wao,
uliwavuruga tena kwa kumkumbuka Bwana Mungu wao.
35 Na hivyo ukaisha mwaka wa themanini na moja wa utawala wa waamuzi.
36 Na katika mwaka wa themanini na mbili walianza kumsahau tena Bwana Mungu
wao. Na katika mwaka wa themanini na tatu walianza kuwa na nguvu katika uovu.
Na katika mwaka wa themanini na nne hawakurekebisha njia zao.
37 Na ikawa katika mwaka wa themanini na tano walizidi kuwa na nguvu katika
kiburi chao, na katika uovu wao; na hivyo walikuwa wanajitayarisha tena kwa
maangamizo.
38 Na hivyo ukaisha mwaka wa themanini na tano.

## Helamani 12

1 Na hivyo tunaweza kuona vile uwongo, na pia kutoaminika kwa mioyo ya watoto wa
binadamu; ndio, tunaweza kuona kwamba Bwana katika uzuri wake usio na mwisho
hubariki na kufanikisha wale ambao huweka imani yao kwake.
2 Ndio, na tunaweza kuona kwa ule wakati anaofanikisha watu wake, ndio, kwa
kuongeza mavuno yao, na wanyama wao na mifugo yao, na kwa dhahabu, na kwa
fedha, na katika kila aina ya vitu vya thamani vya kila aina na umbo; kuachilia
maisha yao, na kuwaokoa kutoka kwa mikono ya maadui wao; kugusa mioyo ya
maadui wao ili wasitangaze vita dhidi yao; ndio, na kwa kifupi, akifanya vitu vyote
kwa ustawi na furaha ya watu wake; ndio, na hapo ni wakati ambao wanashupaza
mioyo yao, na humsahau Bwana Mungu wao, na kumkanyaga chini ya miguu yao
yule Mtakatifu — ndio, na wanafanya hivi kwa sababu ya utulivu wao, na mafanikio
yao makubwa sana.
3 Na hivyo tunaona kwamba Bwana asipowaadhibu watu wake kwa mateso mengi,
ndio, isipokuwa awaadhibishe kwa kifo na kwa vitisho, na kwa njaa na kwa namna
yote ya magonjwa, hawatamkumbuka.
4 Ee jinsi gani wapumbavu, na jinsi gani bure, na waovu, na wenye uibilisi, na jinsi
gani hufanya mabaya kwa urahisi, na jinsi gani watoto wa watu, hufanya mema
polepole, ndio, huwa wepesi kuyasikia maneno ya mwovu, na kuweka mioyo yao
kwenye vitu vilivyo bure vya ulimwengu!
5 Ndio, jinsi gani kwa haraka wanainuliwa kwa kiburi; ndio, jinsi gani ni wepesi
kwa kujisifu, na kufanya kila aina ya yale ambayo ni ya uovu; na jinsi gani wana
upole kumkumbuka Bwana Mungu wao, na kusikiza amri zake, ndio, na jinsi gani ni

wapole kutembea kwenye njia za hekima!

6 Tazama, hawataki kwamba Bwana Mungu wao, ambaye amewaumba, aongoze na kutawala juu yao; ijapokuwa uzuri wake na rehema yake kuwaelekea, wanachukua kama bure mawaidha yake, na hawataki awe kiongozi wao.

7 Ee ni kubwa jinsi gani hali ya kutokuwa na kitu ya watoto wa watu; ndio, hata wako hafifu kuliko mavumbi ya dunia.

8 Kwani tazama, mavumbi ya dunia huvuma hapa na pale, na hata kugawanyika mbali, wakati inavyoamrishwa kufanya hivyo na Mungu wetu mkuu na asiye na mwisho.

9 Ndio, tazama kwa sauti yake vilima na milima hutetemeka na kutapatapa.

10 Na kwa uwezo wa sauti yake inavunjika, na kuwa laini, ndio, hata kama bonde.

11 Ndio, kwa uwezo wa sauti yake dunia yote hutetemeka;

12 Ndio, kwa uwezo wa sauti yake, misingi ya miamba, hutikisika hata mpaka katikati.

13 Ndio, na ikiwa ataambia dunia — Songa — itasonga.

14 Ndio, na ikiwa ataambia dunia — Utarudi nyuma, ili iongeze siku kwa masaa mengi — itafanyika;

15 Na hivyo, kulingana na neno lake dunia hurudi nyuma, na huonekana kwa binadamu kwamba jua linasimama mahali pamoja; ndio, na tazama, hivyo ndivyo ilivyo; kwani kwa kweli ni dunia ndiyo husogea na sio jua.

16 Na tazama, pia, ikiwa ataambia kilindi cha maji ya bahari — Kauka — inafanyika.

17 Tazama, ikiwa atauambia huu mlima — Inuka juu, na uangukie mji huo, ili uzikwe — tazama inafanyika.

18 Na tazama, ikiwa mtu anaficha hazina ndani ya ardhi, na Bwana aseme — Ebu ilaaniwe, kwa sababu ya ubaya wa yule aliyeificha — tazama, italaaniwa.

19 Na ikiwa Bwana atasema — Wewe ulaaniwe, kwamba hakuna mtu yeyote atakayekupata sasa hadi milele — tazama, hakuna mtu atakayeipata kutokea hiyo siku hadi milele.

20 Na tazama, ikiwa Bwana atamwambia mtu — Kwa sababu ya uovu wako, utalaaniwa milele — itafanyika.

21 Na ikiwa Bwana atasema — Kwa sababu ya uovu wako utatolewa kutoka kwenye uwepo wangu — atasababisha kwamba itakuwa hivyo.

22 Na ole kwake yeye ambaye atamwambia hivi, kwani itakuwa kwake ambaye atafanya maovu, na hataweza kuokolewa; kwa hivyo, kwa sababu hii, kwamba binadamu wangeokolewa, toba imetangazwa.

23 Kwa hivyo, heri wale ambao watatubu na kusikiza sauti ya Bwana Mungu wao; kwani hawa ndio wale ambao wataokolewa.

24 Na Mungu akubali, kwa utimilifu wake mkuu, kwamba watu waonyeshe nia ya kutubu na kufanya matendo mazuri, kwamba wangerudishwa kwenye neema kwa neema, kulingana na vitendo vyao.

25 Na ningetaka kwamba watu wote waokolewe. Lakini tunasoma kwamba katika ile siku kuu ya mwisho kuna wengine ambao watatupwa nje, ndio, ambao watatolewa kwenye uwepo wa Bwana;

26 Ndio, ambao watawekwa kwa hali yenye taabu isiyo na mwisho, kwa kutimiza maneno ambayo yanasema: Wale ambao wametenda mema watakuwa na maisha yasiyo na mwisho; na wale ambao wametenda maovu watapata laana isiyo na mwisho. Na hivyo ndivyo ilivyo. Amina.

*Unabii wa Samweli, Mlamani, kwa Wanefi.*

# Helamani 13

1 Na ikawa katika mwaka wa themanini na sita, Wanefi walibaki kwenye uovu, ndio,
katika uovu mwingi, wakati Walamani walitii amri za Mungu, kulingana na sheria
ya Musa.
2 Na ikawa kwamba katika mwaka huu kulikuwa na mmoja aliyeitwa Samweli,
Mlamani ambaye alikuja kwenye nchi ya Zarahemla, na akaanza kuhuwabiria watu.
Na ikawa kwamba alihubiri, siku nyingi, toba kwa watu, na wakamtupa nje, na
alikuwa karibu kurudi kwa nchi yake.
3 Lakini tazama, sauti ya Bwana ilimjia, kwamba arejee tena, na kuwatabiria hawa
watu vitu vyote vitakavyomjia kwa moyo wake.
4 Na ikawa kwamba hawangemkubalia kwamba aingie kwenye mji; kwa hivyo
aliendа na kupanda juu ya ukuta wa mji, na kunyosha mkono wake mbele na kupaza
sauti, na kutabiria watu vitu vyote ambavyo Bwana aliweka moyoni mwake.
5 Na akawaambia: Tazama, mimi, Samweli, Mlamani, ninaongea maneno ya
Bwana ambayo ameweka kwenye moyo wangu; na tazama ameiweka kwenye moyo
wangu kuwaambia hawa watu kwamba upanga wa haki unaning'inia juu ya hawa
watu; na miaka mia nne haitapita kabla ya upanga wa haki kuwaangukia hawa watu.
6 Ndio, uangamizo mzito unawangojea watu hawa, na kwa kweli utawajia watu
hawa, na hakuna kitakachowaokoa watu hawa isipokuwa toba na imani kwa Bwana
Yesu Kristo, ambaye kwa kweli atakuja duniani, na atavumilia vitu vingi na atauawa
kwa ajili ya watu wake.
7 Na tazama, malaika wa Bwana amenitangazia, na alileta habari njema kwa roho
yangu. Na tazama, nilitumwa kwenu niwatangazie pia, ili mpate habari njema;
lakini tazama mmekataa kunisikiliza.
8 Kwa hivyo, hivi asema Bwana: Kwa sababu ya ugumu wa mioyo ya watu hawa wa
Wanefi, wasipotubu nitachukua ahadi yangu yote kutoka kwao, na nitaondoa Roho
yangu kutoka kwao, na sitawavumilia tena, na nitageuza mioyo ya ndugu zao dhidi
yao.
9 Na miaka mia nne haitapita kabla ya mimi kusababisha kwamba wauawe; ndio,
nitawaadhibu kwa upanga na njaa na maradhi ya kuambukiza.
10 Ndio, nitawatembelea katika hasira yangu kali, na kutakuwa na wengine wa
kizazi cha nne ambao wataishi, baina ya maadui wenu, kuona kuangamizwa kwenu
kabisa; na hii kwa kweli itakuja isipokuwa mtubu, Bwana anasema; na wale wa
kizazi cha nne watawatembelea kwa maaangamizo.
11 Lakini ikiwa mtatubu na kumrudia Bwana Mungu wenu nitabadilisha hasira
yangu, asema Bwana; ndio, hivi asema Bwana, wale watakaotubu na kurudi kwangu
watabarikiwa, lakini ole kwa yule ambaye hatatubu.
12 Ndio, ole kwa huu mji mkuu wa Zarahemla; kwani tazama, ni kwa sababu ya
wale wenye haki kwamba umeokolewa; ndio, ole kwa mji huu mkuu, kwani
ninaona, asema Bwana, kwamba kuna wengi, ndio, hata sehemu kubwa ya huu mji
mkuu ambao watashupaza mioyo yao dhidi yangu, asema Bwana.
13 Lakini heri wale ambao watatubu, kwani hao ndio nitakaowasamehe. Lakini
tazama, kama haingekuwa kwa wale wenye haki ambao wako kwenye mji huu mkuu,
tazama, ningesababisha kwamba moto uje chini kutoka mbinguni na kuuangamiza.

14 Lakini tazama, ni kwa ajili ya wale wenye haki kwamba umesamehewa. Lakini
tazama, wakati unawadia, asema Bwana, kwamba wakati mtatupa walio wenye haki
kutoka miongoni mwenu, ndipo mtakapokuwa tayari kwa uangamizo; ndio, ole
kwa huu mji mkuu, kwa sababu ya uovu na machukizo ambayo yamo ndani yake.
15 Ndio, na ole kwa mji wa Gideoni, kwa uovu na machukizo ambayo yamo ndani
yake.
16 Ndio, na ole kwa miji yote ambayo iko katika nchi karibu na hapa, ambayo
imemilikiwa na Wanefi, kwa sababu ya uovu na machukizo ambayo yamo ndani yao.
17 Na tazama, laana itakujia nchi, asema Bwana wa Majeshi, kwa sababu ya watu
ambao wako nchini, ndio, kwa sababu ya uovu wao na machukizo yao.
18 Na itakuwa, asema Bwana wa Majeshi, ndio, ambaye ni Mungu wetu mkuu na wa
kweli, kwamba yeyote ambaye ataficha hazina ardhini hataipata tena, kwa sababu ya
laana kuu ya nchi, isipokuwa awe mtu mwenye haki na aifiche kwenye Bwana.
19 Kwani ninawataka, asema Bwana, kwamba wafiche hazina zao kwangu; na laana
iwe kwa wale wasioficha hazina zao kwangu; kwani hakuna yeyote ambaye huficha
hazina zake kwangu isipokuwa awe mwenye haki; na yule ambaye hafichi hazina
zake kwangu, amelaaniwa, na pia ile hazina, na hakuna atakayeikomboa kwa sababu
ya laana ya nchi.
20 Na siku itawadia kwamba wataficha hazina zao, kwa sababu wameweka mioyo
yao kwenye utajiri; na kwa sababu wameweka mioyo yao kwenye utajiri wao, na
wataficha hazina zao wakati watakimbia kutoka kwa maadui wao; kwa sababu
hawatazificha kwangu, walaaniwe na pia hazina zao; na katika siku hio ndipo
watakapouawa, asema Bwana.
21 Tazama nyinyi, watu wa huu mji mkuu, na sikilizeni maneno yangu; ndio,
sikilizeni maneno ambayo Bwana anasema; kwani tazama, anasema kwamba
mmelaaniwa kwa sababu ya utajiri wenu, na pia utajiri wenu umelaaniwa kwa
sababu mmeweka mioyo yenu juu yake, na hamjasikiliza maneno ya yule
aliyewapatia huo utajiri.
22 Hammkumbuki Bwana Mungu wenu kwa vitu ambavyo amewabariki navyo,
lakini kila siku mnakumbuka utajiri wenu, bila kumshukuru Bwana Mungu wenu
kwa hivyo vitu; ndio, mioyo yenu haimkaribii Bwana, lakini inavimba kwa kiburi
kikuu, kwa kujisifu, na kwa uvimbe mkuu, mashindano, ukorofi, uovu, mateso, na
mauaji, na kila aina ya uovu.
23 Kwa sababu hii Bwana Mungu amesababisha kwamba laana ije kwa nchi, na pia
kwa utajiri wenu, na hii ni kwa sababu ya maovu yenu.
24 Ndio, ole kwa watu hawa, kwa sababu ya huu muda ambao umewadia, wakati
mnatupa nje manabii, na kuwacheka, na kuwatupia mawe, na kuwaua, na kufanya
kila aina ya uovu kwao, hata vile walioishi zamani walivyofanya.
25 Na sasa mkizungumza, mnanena: Ikiwa siku zetu zingekuwa katika siku za babu
zetu wa zamani, hatungewaua manabii; hatungewapiga kwa mawe, na kuwatupa nje.
26 Tazama nyinyi ni wabaya kuliko hao; kadiri Bwana anavyoishi, ikiwa nabii
anaweza kuja miongoni mwenu na kuwatangazia neno la Bwana, ambalo
linashuhudia dhambi zenu na uovu, mnamkasirikia, na kumtupa nje na kutafuta
njia za namna zote kumwangamiza; ndio, mtasema kwamba ni nabii wa uwongo, na
kwamba ni mwenye dhambi, na mwenye kutoka kwa ibilisi, kwa sababu
anashuhudia kwamba vitendo vyenu ni viovu.
27 Lakini tazama, ikiwa mtu atatokea miongoni mwenu na kusema: Fanya hivi, na

hakutakuweko na ubaya; fanya vile na hamtaumia; ndio, atasema: Tembeeni katika kiburi cha mioyo yenu yenyewe; ndio, tembeeni katika kiburi cha macho yenu, na fanya chochote ambacho moyo wako unapenda—na ikiwa mtu atatokea miongoni mwenu na kusema hivi, hapo mtamkubali, na kusema ni nabii.

28 Ndio, mtamheshimu, na mtampatia mali yenu; mtampatia dhahabu yenu, na fedha yenu, na mtamvalisha mavazi ya thamani; na kwa sababu anazungumza maneno ya udanganyifu kwenu, na anasema kwamba yote ni mema, kwa hivyo hamtampata na makosa.

29 Ee nyinyi kizazi kilichopotea; nyinyi watu wagumu na wenye shingo ngumu, kwa muda gani mnadhani Bwana atawavumilia? Ndio, kwa muda gani mtakubali kuongozwa na wapumbavu na vipofu? Ndio, kwa muda gani mtachagua giza juu ya mwangaza?

30 Ndio, tazama, ghadhabu ya Bwana imewashwa dhidi yenu; tazama, amelaani nchi kwa sababu ya uovu wenu.

31 Na tazama, wakati unawadia kwamba atalaani utajiri wenu, kwamba utateleza, kwamba hamtaweza kuushika; na katika siku za umasikini wenu hamtazishika.

32 Na katika siku za umasikini wenu mtamlilia Bwana; na mtalia bure, kwani ukiwa wenu utakuwa umewajia kitambo, na uharibifu wenu umekamilishwa; na hapo mtatoa machozi na kulia wakati huo, asema Bwana wa Majeshi. Na hapo mtaomboleza, na kusema:

33 Ee kwamba nilikuwa nimetubu, na sikuwaua manabii, na kuwapiga kwa mawe, na kuwatupa nje. Ndio, katika siku hiyo mtasema: Ee kwamba tungemkumbuka Bwana Mungu wetu wakati ambapo alitupatia utajiri wetu, na hapo haungeteleza, kwamba tuupoteze; kwani tazama, utajiri wetu umetuwacha.

34 Tazama, tunaweka hapa chombo na kesho yake kimeenda; na tazama, panga zetu zinachukuliwa kutoka kwetu wakati tunapozitafuta kwa vita.

35 Ndio, tumeficha hazina zetu na zimeponyokea mbali kutoka kwetu, kwa sababu ya laana ya nchi.

36 Ee kwamba tulitubu wakati ambao neno la Bwana lilitujia; kwani tazama nchi imelaaniwa, na vitu vyote vimekuwa vya kuteleza, na hatuwezi kuvishika.

37 Tazama, tumezingirwa na pepo mbaya, ndio, tumezungukwa na malaika wa yule ambaye anataka kuangamiza roho zetu. Tazama, uovu wetu ni mkuu. Ee Bwana, huwezi kugeuza hasira yako kutoka kwetu? Na hii itakuwa lugha yenu wakati huo.

38 Lakini tazama, siku zenu za majaribio zimepita; mmechelewesha siku yenu ya wokovu mpaka imechelewa milele, na maangamizo yenu yamehakikishwa; ndio, kwani mmetafuta siku zote za maisha yenu yale ambayo hamwezi kupata; na mmetafuta furaha kwa kufanya uovu, kitu ambacho ni kinyume cha asili ya haki ambayo huja kutoka kwa mkuu na Kiongozi wetu wa Milele.

39 Ee nyinyi watu wa nchi, ningetaka kwamba msikilize maneno yangu! Na ninaomba kwamba hasira ya Bwana itolewe kutoka kwenu, na kwamba mtatubu na kukombolewa.

# Helamani 14

1 Na sasa ikawa kwamba Samweli, Mlamani, alitabiri vitu vingi zaidi ambavyo haviwezi kuandikwa.

2 Na tazama, aliwaambia: Tazama, ninawapatia ishara; kwani miaka mitano zaidi

inakuja, na tazama, ndipo atakuja Mwana wa Mungu kuwakomboa wale wote ambao wataamini kwa jina lake.

3 Na tazama, hii nitawapatia kama ishara wakati wa kuja kwake; kwani tazama, kutakuwa na mwangaza mwingi mbinguni, mpaka kwamba usiku kabla ya kuja kwake hakutakuwa na giza, mpaka kwamba itaonekana kwa binadamu kama ni mchana.

4 Kwa hivyo, kutakuwa na siku moja na usiku mmoja na siku, kama kwamba ni siku moja bila usiku; na hii itakuwa ishara kwenu kutazamia; kwani mtafahamu kutokea kwa jua na pia kutua kwake; kwa hivyo watajua kwa hakika kwamba kutakuwa na siku mbili na usiku mmoja; walakini usiku hautakuwa na giza; na itakuwa usiku kabla yeye azaliwe.

5 Na tazama, nyota mpya itatokea, aina moja ambayo hamjawahi kuona kamwe; na hii pia itakuwa ishara kwenu.

6 Na tazama haya si yote, kutakuwa na ishara nyingi na vituko mbinguni.

7 Na itakuwa kwamba nyinyi nyote mtashangaa, na kustaajabu, mpaka kwamba mtainama kwenye ardhi.

8 Na itakuwa kwamba yeyote atakayeamini kwa Mwana wa Mungu, yeye atakuwa na maisha yasiyo na mwisho.

9 Na tazama, hivyo ndivyo Bwanaameniamuru, kupitia kwa malaika wake, kwamba nije na kusema hiki kitu kwenu; ndio, ameamuru kwamba nitabiri hivi vitu kwenu; ndio, amesema kwangu: Paza sauti kwa hawa watu, tubuni na mtayarishe njia ya Bwana.

10 Na sasa, kwa sababu mimi ni Mlamani, na nimewazungumzia maneno ambayo Bwana ameniamuru, na kwa sababu yalikuwa magumu dhidi yenu, mmenikasirikia na mnataka kuniangamiza, na mmenitupa nje kutoka miongoni mwenu.

11 Na mtasikia maneno yangu, kwani, ni kwa sababu ya hili kusudi nimepanda ukuta wa mji huu, ili muweze kusikia na kujua hukumu ya Mungu ambayo inawangojea kwa sababu ya uovu wenu, na pia kwamba mngejua hali ya toba;

12 Na pia kwamba mngejua kuhusu kuja kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Baba wa mbingu na dunia, Muumba wa vitu vyote tangu mwanzo; na kwamba mjue ishara za kuja kwake, na tumaini kwamba mngeamini katika jina lake.

13 Na ikiwa mtaamini katika jina lake mtatubu dhambi zenu, kwamba kwa kufanya hivyo mngepata kusamehewa kupitia kwa uzuri wake.

14 Na tazama, tena, ishara nyingine ninawapatia, ndio, ishara ya kifo chake.

15 Kwani tazama, lazima kwa kweli afe kwamba wokovu uje; ndio, inampasa yeye kwa lazima kwamba afe, ili kutimiza ufufuo wa wafu, kwamba kwa hiyo sababu binadamu waletwe kwenye uwepo wa Bwana.

16 Ndio, tazama, hiki kifo huleta kutimiza ufufuo, na hukomboa binadamu wote kutokana na kifo cha kwanza—hicho kifo cha roho; kwani binadamu wote, kwa sababu ya kuanguka kwa Adamu wakitolewa kutoka uwepo wa Bwana, wanafikiriwa kama waliokufa, kwa vitu vya kimwili na vitu vya kiroho.

17 Lakini tazama, ufufuko wa Kristo unakomboa binadamu, ndio, hata binadamu wote, na huwarejesha kwenye uwepo wa Bwana.

18 Ndio, na inasababisha kutimiza hali ya toba, kwamba yeyote anayetubu yeye hatatupwa chini na kuwekwa kwenye moto; lakini yeyote ambaye hatatubu atawekwa chini na kutupwa kwenye moto; na hapo kinawajia kifo cha roho, ndio, kifo cha pili, kwani wametolewa tena kwa vitu vinavyohusika na haki.

19 Kwa hivyo tubuni nyinyi, tubuni nyinyi, isiwe kwamba kwa kuvijua hivi vitu na
kutovifanya mtalaaniwa, na mtaletwa chini kwenye kifo cha pili.
20 Lakini tazama, vile niliwaambia kuhusu ishara nyingine, ishara ya kifo chake,
tazama, katika siku hiyo ambayo atapatwa na kifo jua litawekwa giza na kukataa
kutoa mwangaza wake kwenu; na pia mwezi na nyota; na hakutakuwa na mwangaza
juu ya hii nchi, hata kutokea wakati atakapokufa, kwa muda wa siku tatu, hadi
kwenye siku atakayofufuka tena kutoka kwa wafu.
21 Ndio, wakati atakapokata roho kutakuwa na vishindo vya ngurumo na radi kwa
muda wa masaa mengi, na ardhi itatingishika na kutetemeka; na miamba ambayo
iko juu ya hii dunia, ambayo yote iko juu ya dunia na chini, ambayo mnajua wakati
huu kama ni nzima, au sehemu yake kwa jumla ni nzima, itavunjika;
22 Ndio, yatagawanyika mara mbili, na kutokea hapo itapatikana kwenye pindo na
kwenye nyufa, na kwa vipande vilivyovunjika juu ya dunia yote, ndio, juu ya nchi na
chini yake.
23 Na tazama, kutakuwa na dhoruba kubwa, na kutakuwa na milima mingi
itakayolainishwa, kama bonde, na kutakuwa na mahali pengi ambapo sasa hivi
panaitwa mabonde ambayo itakuwa milima, ambayo urefu wake ni mkubwa.
24 Na barabara nyingi zitaharibiwa, na miji mingi itakuwa jangwa.
25 Na makaburi mengi yatafunguka, na yataachilia wengi wa wafu wao; na
watakatifu wengi watajidhihirisha kwa wengi.
26 Na tazama, hivyo ndivyo malaika ameniambia; kwani aliniambia kwamba
kutakuwa na vishindo vya ngurumo na radi kwa muda wa masaa mengi.
27 Na aliniambia kwamba wakati vishindo vya ngurumo na radi vitakuwa
vikiendelea, na dhoruba, kwamba hivi vitu vitafanyika, na kwamba giza litafunika
dunia yote kwa muda wa siku tatu.
28 Na malaika aliniambia kwamba wengi wataona vitu vingi kuliko hivi, kwa kusudi
kwamba wapate kuamini hizi ishara na haya maajabu yapate kutimizwa juu ya nchi
yote, kwa kusudi kwamba kusiwe na sababu ya kutoamini miongoni mwa watoto wa
watu —
29 Na hili kwa kusudi kwamba yeyote atakayeamini ataokolewa, na kwamba yeyote
ambaye hataamini, hukumu ya haki ingewajia; na pia wakihukumiwa hapo
watajiletea wenyewe hukumu yao.
30 Na sasa kumbukeni, kumbukeni, ndugu zangu, kwamba yeyote anayeangamia,
anaangamia kwa kupenda kwake; na yeyote afanyaye dhambi, anaifanya kwake
mwenyewe; kwani tazama, mko huru; mmekubaliwa kujichagulia; kwani tazama,
Mungu amewapatia elimu na amewafanya huru.
31 Amewapatia nafasi kwamba mjue mema na maovu, na amewapatia kwamba
mchague uzima au kifo; na mnaweza kutenda mazuri na mrejeshwe kwa yale yaliyo
mema, au kupata yale yaliyo mema kurudishwa kwenu; au mnaweza kutenda
maovu, na mpate yale yaliyo maovu yarudishwe kwenu.

## Helamani 15

1 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, tazama, ninawatangazia kwamba msipotubu
nyumba zenu zitaachwa ziwe na ukiwa.
2 Ndio, msipotubu, wanawake wenu watakuwa na sababu ya kuomboleza wakati
watakapokuwa wakinyonyesha; kwani mtajaribu kukimbia lakini hakutakuwa na

mahali pa kimbilio; ndio, na ole kwa wale ambao wana mimba, kwani watakuwa
wazito na hawataweza kukimbia; kwa hivyo, watakanyagwa chini na kuachwa
kuangamia.
3 Ndio, ole kwa watu hawa ambao wanaitwa watu wa Nefi isipokuwa watubu,
wakati wataona ishara hizi zote na maajabu ambayo yataonyeshwa kwao; kwani
tazama, wamekuwa watu waliochaguliwa na Bwana; ndio, aliwapenda watu wa Nefi,
na pia amewakemea; ndio, katika siku zao za dhambi amewakemea kwa sababu
anawapenda.
4 Lakini tazama ndugu zangu, amewachukia Walamani kwa sababu vitendo vyao
vimekuwa viovu wakati wote, na wanafanya hivyo kwa sababu ya uovu wa desturi ya
babu zao. Lakini tazama, wokovu umekuja kwao kupitia kwa mahubiri ya Wanefi;
na kwa kusudi hili Bwana amewaongezea siku zao.
5 Na ningetaka kwamba mwone kwamba sehemu yao kubwa wako kwenye kazi
yao, na wanatembea kwa uangalifu mbele ya Mungu, na wanatii amri zake na sheria
zake na maamuzi yake kulingana na sheria ya Musa.
6 Ndio, ninawaambia, kwamba sehemu yao kubwa wanafanya hivi, na wanajaribu
kwa bidii bila kuchoka ili walete ndugu zao waliosalia kwa elimu ya ukweli; kwa
hivyo, kuna wengi ambao wanaongeza idadi yao kila siku.
7 Na tazama, mnajua wenyewe, kwani mmejionea, kwamba vile wengi wao
wanaletwa kuelimishwa ukweli, na kujua uovu na desturi za machukizo za babu zao,
na wameongozwa kuamini maandiko matakatifu, ndio, utabiri wa manabii
watakatifu, ambao umeandikwa, ambao unawaongoza kuwa na imani kwa Bwana,
na kwenye toba, imani na toba ambavyo huwaletea mabadiliko katika mioyo yao—
8 Kwa hivyo, vile wengi wamekuja kwa ukweli huu, mnajua wenyewe kwamba
wako imara na thabiti katika imani, na pia kitu ambamo kwayo wamefanywa huru.
9 Na mnajua pia kwamba wamezika silaha zao za vita, na wanaogopa kuzichukua
wasije kwa njia yoyote wafanye dhambi; ndio, mnaona kwamba wanaogopa kutenda
dhambi—kwani tazama wanakubali wenyewe kwamba wakanyagwe chini na
kuuawa na maadui wao, na hawatainua panga zao dhidi yao, na hivyo kwa sababu ya
imani yao kwa Kristo.
10 Na sasa, kwa sababu ya uthabiti wao wakati wanaamini kwenye hicho kitu
ambacho wanaamini, kwani kwa sababu ya uthabiti wao mara wakielimishwa,
tazama, Bwana atawabariki na kuongeza siku zao, ijapokuwa ubaya wao—
11 Ndio, hata kama wanafifia kwa kutoamini Bwana ataongeza siku zao, mpaka
wakati utatimia ambao umezungumzwa na babu zetu, na pia nabii Zeno, na manabii
wengine wengi, kuhusu kurudishwa kwa ndugu zetu, Walamani, tena kwa ufahamu
wa ukweli—
12 Ndio, nawaambia, kwamba katika siku za baadaye ahadi za Bwana zimeelekezwa
kwa ndugu zetu, Walamani; na ijapokuwa mateso mengi ambayo watakuwa nayo, na
ingawa watafukuzwa huku na kule duniani, na kuwindwa, na kushambuliwa na
kutawanywa ugenini, wakiwa hawana mahali pa kimbilio, Bwana atawarehemu.
13 Na hii ni kulingana na unabii, kwamba watarejeshwa kwenye ufahamu wa
ukweli, ambao ni ufahamu wa Mkombozi wao, na mchungaji wao mkuu na wa
kweli, na kuhesabiwa miongoni mwa kondoo wake.
14 Kwa hivyo nawaambia, itakuwa bora kwao kuliko kwenu isipokuwa mtubu.
15 Kwani tazama, kama kazi kuu zingeonyeshwa kwao ambazo zimeonyeshwa
kwenu, ndio, kwao ambao wamefifia kwa kutoamini kwa sababu ya desturi za babu

zao, mnaweza kuona wenyewe kwamba hawangeweza tena kufifia kwa kutoamini.
16 Kwa hivyo, Bwana asema: Sitawaangamiza kabisa, lakini nitasababisha kwamba
wakati nitaona ni hekima kwangu watanirudia, asema Bwana.
17 Na sasa tazama, asema Bwana, kuhusu watu wa Wanefi: Kama hawatatubu, na
kujaribu kufanya yale ninayotaka, nitawaangamiza kabisa, asema Bwana, kwa sababu
ya kutoamini kwao ijapokuwa kazi nyingi kubwa ambayo nimefanya miongoni
mwao; na kwa ukweli vile Bwana anavyoishi vitu hivi vitafanyika, asema Bwana.

# Helamani 16

1 Na sasa, ikawa kwamba kulikuwa na wengi ambao walisikia maneno ya Samweli,
Mlamani, ambayo alizungumzia kwenye ukuta wa mji. Na kadiri walivyoamini
neno alilosema walienda na kumtafuta Nefi; na walipoenda na kumpata waliungama
dhambi zao kwake bila kuacha dhambi yoyote nyuma, wakitaka kwamba
wangebatizwa kwa Bwana.
2 Lakini kadiri ambao hawakuyaamini maneno ya Samweli walimkasirikia; na
walimtupia mawe akiwa kwenye ukuta, na wengi pia walimpiga mishale wakati
alipokuwa anasimama kwenye ukuta; lakini Roho wa Bwana alikuwa naye, mpaka
kwamba hawangeweza kumpiga na mawe yao wala mishale yao.
3 Sasa wakati walipoona kwamba hawangeweza kumpiga, kulikuwa na wengi zaidi
ambao waliamini maneno yake, mpaka kwamba walimwendea Nefi kubatizwa.
4 Kwani tazama, Nefi alikuwa anabatiza, na kutabiri, na kuhubiri, na kuwaambia
kwamba watubu, akiwaonyesha ishara na maajabu, akifanya miujiza miongoni mwa
watu, ili wajue kwamba Kristo atazaliwa hivi karibuni—
5 Akiwaambia vitu ambavyo lazima vifanyike, ili wajue na wakumbuke wakati wa
kufanyika kwao kwamba imefanywa kujulikana kwao mbeleni, kwamba
wangeamini; kwa hivyo jinsi vile wengi waliyaamini maneno ya Samweli walienda
mbele kwake kubatizwa, kwani walikuja kutubu na kuungama dhambi zao.
6 Lakini sehemu kubwa yao hawakuyaamini maneno ya Samweli; kwa hivyo
walipoona kwamba hawangeweza kumpiga kwa mawe yao na mishale yao, walipigia
makapteni wao makelele, wakisema: Chukueni huyu mtu na mmfunge, kwani
tazama ana ibilisi; na kwa sababu ya uwezo wa ibilisi ambao uko ndani yake
hatuwezi kumpiga kwa mawe yetu na mishale yetu; kwa hivyo mkamateni na
mmfunge, na kumpeleka mbali.
7 Na walipoenda mbele kumkamata, tazama, alijitupa kutoka kwenye ukuta, na
kutoroka kutoka nchi yao, ndio, hadi kwenye nchi yake, na akaanza kuhubiri na
kutoa unabii miongoni mwa watu wake.
8 Na tazama, hakusikika tena miongoni mwa Wanefi; na hivyo ndivyo zilikuwa
shughuli za watu.
9 Na hivyo ukaisha mwaka wa themanini na sita wa utawala wa waamuzi juu ya
watu wa Nefi.
10 Na hivyo pia ukaisha mwaka wa themanini na saba wa utawala wa waamuzi,
sehemu kubwa ya watu wakibaki katika kiburi chao na uovu, na sehemu ndogo
ikitembea kwa uangalifu mbele ya Mungu.
11 Na hii ilikuwa hali pia, katika mwaka wa themanini na nane wa utawala wa
waamuzi.
12 Na kulikuwa tu na mabadiliko machache katika shughuli za watu, isipokuwa

watu walianza kujiimarisha katika uovu, na kufanya mengi ya yale yaliyo kinyume
cha amri za Mungu, katika mwaka wa themanini na tisa wa utawala wa waamuzi.
13 Lakini ikawa katika mwaka wa tisini wa utawala wa waamuzi, kulikuwa na ishara
kubwa zilizoonyeshwa kwa watu, na maajabu; na maneno ya manabii yalianza
kutimizwa.
14 Na malaika walionekana kwa watu, watu wenye hekima, na kuwatangazia habari
njema ya shangwe kuu; hivyo katika mwaka huu maandiko yalianza kutimizwa.
15 Walakini, watu walianza kushupaza mioyo yao, wote isipokuwa sehemu yao
iliyoamini zaidi, wote Wanefi na Walamani, na wakaanza kutegemea nguvu zao
wenyewe na katika hekima yao wenyewe, wakisema:
16 Baadhi ya vitu walibahatisha vyema, miongoni mwa vingi; lakini tazama, tunajua
kwamba hizi kazi zote kubwa na za ajabu haziwezi kutimizwa, ambazo
zimezungumziwa.
17 Na walianza kubishana na kushindana miongoni mwao, wakisema:
18 Kwamba sio ya maana kwamba kiumbe kama Kristo kitakuja; ikiwa hivyo, na
awe Mwana wa Mungu, Baba wa mbingu na dunia, vile ilizungumziwa, kwa nini
asijidhihirishe kwetu kama kwa wale walio Yerusalemu?
19 Ndio, kwa nini hatajidhihirisha kwa nchi hii kama vile nchi ya Yerusalemu?
20 Lakini tazama, tunajua kwamba hii ni desturi iliyo mbovu, ambayo imetolewa
chini kwetu na babu zetu, kutusababisha kwamba tuamini kwa kitu kikubwa na cha
ajabu ambacho kitakuja kutimizwa, lakini sio miongoni mwetu, lakini katika nchi
iliyo mbali, nchi ambayo hatujui; kwa hivyo wanaweza kutuweka kwenye ujinga,
kwani hatuwezi kushuhudia kwa macho yetu kwamba ni ya kweli.
21 Na wataweza, kwa njia ya werevu na siri ya ustadi wa mwovu, kufanya siri kubwa
ambayo hatuwezi kuielewa, ambayo itatuweka chini kuwa watumwa kwa maneno
yao, na pia watumishi kwao, kwani tunawategemea kutufundisha neno; na hivyo
watatuweka kwenye ujinga ikiwa tutakubali kuongozwa na hao, siku zote za maisha
yetu.
22 Na watu waliwaza mioyoni mwao vitu vingi sana, ambavyo vilikuwa vya
upumbavu na bure; na walisumbuliwa sana, kwani Shetani aliwavuruga kwa
kutenda maovu siku zote; ndio, alizunguka akisambaza uvumi na mabishano
nchini, ili ashupaze mioyo ya watu dhidi ya vile vitu ambavyo vilikuwa vizuri na
dhidi ya vile ambavyo vitakuja.
23 Na ijapokuwa ishara na maajabu ambayo yalifanyika miongoni mwa watu wa
Bwana, na miujiza mingi ambayo walifanya, Shetani alishikilia mioyo ya watu
nchini kote.
24 Na hivyo ukaisha mwaka wa tisini wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.
25 Na hivyo kikamalizika kitabu cha Helamani, kulingana na maandiko ya
Helamani na wana wake.

# Nefi wa Tatu

## Kitabu cha Nefi

Mwana wa Nefi, Ambaye Alikuwa Mwana wa Helamani

*Na Helamani alikuwa mwana wa Helamani, ambaye alikuwa mwana wa Alma, ambaye alikuwa mwana wa Alma, ambaye alikuwa wa uzao wa Nefi ambaye alikuwa mwana wa Lehi, ambaye alitoka Yerusalemu katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Zedekia, mfalme wa Yuda.*

## 3 Nefi 1

1 Sasa ikawa kwamba mwaka wa tisini na moja ulikuwa umepita na ilikuwa miaka mia sita tangu wakati ambao Lehi aliondoka Yerusalemu; na ilikuwa katika mwaka ambao Lakoneyo alikuwa mwamuzi mkuu na msimamizi juu ya nchi.

2 Na Nefi, mwana wa Helamani, alikuwa ameondoka kutoka kwa nchi ya Zarahemla, na kutoa amri kwa mwana wake Nefi, ambaye alikuwa mwana wake mkubwa, kuhusu bamba za shaba, na maandishi yote ambayo yalikuwa yameandikwa, na hivyo vitu vyote ambavyo vilichukuliwa kama vitakatifu kuanzia kuondoka kwa Lehi kutoka Yerusalemu.

3 Kisha aliondoka nje ya nchi, na alikoenda, hakuna mtu yeyote ajuaye; na mwana wake Nefi alihifadhi maandishi badala yake, ndio, maandishi ya hawa watu.

4 Na ikawa kwamba katika mwanzo wa mwaka wa tisini na mbili, tazama, utabiri wa manabii ulianza kutimizwa zaidi kabisa; kwani kulianza kuwa na ishara kubwa na miujiza mikubwa kutokea miongoni mwa watu.

5 Lakini kulikuwa na wengine walioanza kusema kwamba wakati umepita kwa yale maneno kutimizwa, ambayo yalizungumzwa na Samweli, Mlamani.

6 Na walianza kufurahia ndugu zao, wakisema: Tazama wakati umepita, na maneno ya Samweli hayajatimizwa; kwa hivyo, shangwe yenu na imani yenu katika hiki kitu imekuwa bure.

7 Na ikawa kwamba walifanya makelele mengi kote nchini; na watu walioamini walianza kuwa na huzuni sana, wakiogopa kwamba hivyo vitu ambavyo vilizungumzwa havingetimizwa.

8 Lakini tazama, walichunguza wakati wote ule mchana na ule usiku na ule mchana siku ile ambayo itakuwa ni kama siku moja kama vile hakuna usiku, kwamba wangejua kuwa imani yao haikuwa bure.

9 Sasa ikawa kwamba kulikuwa na siku ambayo iliwekwa kando na wasioamini, kwamba wale wote ambao waliamini kwenye desturi hizo wangeuawa isipokuwa ishara zipate kutimizwa, ambazo zilitolewa na nabii Samweli.

10 Sasa ikawa kwamba wakati Nefi, mwana wa Nefi, aliona huu uovu wa watu hawa, moyo wake ulikuwa na huzuni sana.

11 Na ikawa kwamba alienda nje na kujiinamisha ardhini, na kuomba kwa Mungu wake kwa niaba ya watu wake, ndio, wale ambao walikuwa karibu kuangamizwa kwa sababu ya imani yao kwenye desturi za babu zao.

12 Na ikawa kwamba aliomba kwa nguvu kwa Bwana ile siku yote; na tazama, sauti
ya Bwana ilikuja kwake, ikisema:
13 Inua kichwa chako na uchangamke; kwani tazama, wakati umefika, na kwa usiku
wa leo ishara itatolewa, na kesho nitakuja ulimwenguni, kuonyesha dunia kwamba
nitatimiza yote ambayo nimesababisha kuzungumzwa kwa midomo ya manabii
wangu watakatifu.
14 Tazama, naja kwa watu wangu, kutimiza vitu vyote ambavyo nimefanya
kujulikana kwa watoto wa watu tangu msingi wa dunia, na kufanya mapenzi, yote ya
Baba na Mwana — ya Baba kwa sababu yangu, na ya Mwana kwa sababu ya mwili
wangu. Na tazama, wakati umefika, na usiku huu ishara itadhihirishwa.
15 Na ikawa kwamba maneno ambayo yalimjia Nefi yalivyotimizwa, kulingana na
vile yalizungumzwa; kwani tazama, wakati jua lilipotua hakukuwa na giza; na watu
walianza kustaajabu kwa sababu hakukuwa na giza wakati usiku ulipofika.
16 Na kulikuwa na wengi, ambao hawakuwa wameamini maneno ya manabii, ambao
walijilaza kwenye ardhi na wakawa kama waliokufa, kwani walijua kwamba mpango
mkubwa wa uangamizo ambao walikuwa wamewawekea wale ambao waliamini
maneno ya manabii umezuiliwa; kwani ishara ambayo ilitolewa ilikuwa ipo.
17 Na wakaanza kujua kwamba Mwana wa Mungu lazima aonekane karibuni; ndio,
kwa kifupi, watu wote usoni mwa ulimwengu kutoka magharibi hadi mashariki,
kote katika nchi ya kaskazini na katika nchi ya kusini, walistaajabu sana kwamba
walianguka ardhini.
18 Kwani walijua kwamba manabii walikuwa wameshuhudia vitu hivi kwa miaka
mingi, na kwamba ishara ambayo ilitolewa ilikuwa ipo kitambo; na walianza
kuogopa kwa sababu ya uovu wao na kutoamini kwao.
19 Na ikawa kwamba hakukuweko na giza usiku ule wote, lakini kulikuwa na
mwangaza kama kwamba ilikuwa adhuhuri. Na ikawa kwamba jua lilitokea asubuhi
tena, kulingana na utaratibu wake; na walijua kwamba ilikuwa ni siku ambayo
Bwana angezaliwa, kwa sababu ya ishara ambayo ilitolewa.
20 Na ikawa imekuwa, ndio, vitu vyote, kila chembe, kulingana na maneno ya
manabii.
21 Na ikawa pia kwamba nyota mpya ilitokea, kulingana na neno.
22 Na ikawa kwamba kutoka wakati huu kuendelea kulianza kuwa na udanganyifu
ulioletwa na Shetani, miongoni mwa watu, kushupaza mioyo yao, kwa kusudi
kwamba wasiamini kwenye hizo ishara na miujiza ambayo walikuwa wameona;
lakini ingawaje kulikuwa na huu udanganyifu na uwongo sehemu kubwa ya watu
iliamini, na wakamgeukia Bwana.
23 Na ikawa kwamba Nefi alienda mbele miongoni mwa watu, na pia wengine
wengi, akiwabatiza ubatizo wa toba, ambamo kwake kulikuwa na kusamehewa
kwingi kwa dhambi. Na hivyo watu wakaanza tena kuwa na amani nchini.
24 Na hakukuweko na mabishano, isipokuwa wachache ambao walianza kuhubiri,
wakijaribu kuthibitisha kutumia maandiko kwamba haikuwa tena muhimu kutii
sheria ya Musa. Sasa kwa kitu hiki walikosa, wakiwa hawajaelewa maandiko.
25 Lakini ikawa kwamba mara moja waligeuka, na walisadikishwa kwa makosa
ambayo walikuwa nayo, kwani walifahamishwa kwamba sheria haijatimizwa, na
kwamba lazima itimizwe kwa kila chembe; ndio, neno lilikuja kwao kwamba lazima
itimizwe; ndio, kwamba nukta moja wala chembe moja haitapita mpaka yote
yatimie; kwa hivyo kwenye huu mwaka walielemishwa kwa makosa yao na

wakaungama makosa yao.
26 Na hivyo mwaka wa tisini na mbili ulipita, ukileta habari njema kwa watu kwa
sababu ya ishara ambazo zilitimizwa, kulingana na maneno ya uaguzi wa manabii
wote watakatifu.
27 Na ikawa kwamba mwaka wa tisini na tatu pia ulipita katika amani, isipokuwa
wezi wa Gadiantoni, ambao waliishi juu ya milima, ambao waliingilia nchi; kwani
ngome zao zilikuwa na nguvu sana na mahali pao pa siri kwamba watu
hawangewashinda; kwa hivyo walitenda mauaji mengi sana, na kuua wengi
miongoni mwa watu.
28 Na ikawa kwamba katika mwaka wa tisini na nne walianza kuongezeka kwa idadi
kubwa, kwa sababu kulikuwa na wengi wasiokubaliana na Wanefi ambao
walikimbilia kwao, ambao walisababisha huzuni nyingi kwa Wanefi ambao walibaki
nchini.
29 Na pia kulikuwa na sababu ya huzuni nyingi miongoni mwa Walamani; kwani
tazama, walikuwa na watoto wengi ambao walikuwa na kuanza kuwa wazee katika
miaka, kwamba walijitegemea wenyewe, na waliongozwa vibaya na wengine ambao
walikuwa Wazoramu, kwa udanganyifu wao na maneno yao ya kujisifu, kujiunga na
wale wezi wa Gadiantoni.
30 Na hivyo Walamani walihuzunishwa pia, na walianza kupungukiwa kwenye
imani na haki yao, kwa sababu ya uovu wa vijana wa kizazi hiki.

## 3 Nefi 2

1 Na ikawa kwamba hivyo uliisha mwaka wa tisini na tano pia, na watu wakaanza
kusahau hizo ishara na maajabu ambayo walikuwa wamesikia, na wakaanza
kuendelea kupungukiwa zaidi kwa mshangao katika ishara au maajabu kutoka
mbinguni, mpaka kwamba walianza kugandamiza mioyo yao, na kuwa vipofu ndani
ya akili zao, na walianza kutoamini yote ambayo walisikia na kuona—
2 Wakikisia juu ya kitu cha bure ndani ya mioyo yao, kwamba ililetwa na watu na
nguvu za ibilisi, kupoteza na kudanganya mioyo ya watu; na hivyo Shetani
alishawishi mioyo ya watu tena, mpaka kwamba akafunika macho yao na
kuwaongoza mbali kuamini kwamba mafundisho ya Kristo yalikuwa ni upumbavu
na kitu cha bure.
3 Na ikawa kwamba watu walianza kukua ndani ya uovu na machukizo; na
hawakuamini kwamba kutakuwa na ishara zingine au maajabu ambayo yangetolewa;
na Shetani alikuwa akizunguka, akiopotosha mbali mioyo ya watu, akiwajaribu na
kuwasababisha kufanya uovu mkuu ndani ya nchi.
4 Na hivyo ukaisha mwaka wa tisini na sita; na pia mwaka wa tisini na saba; na pia
mwaka wa tisini na nane; na pia mwaka wa tisini na tisa;
5 Na pia miaka mia moja ilikuwa imepita tangu siku za Mosia, ambaye alikuwa
mfalme juu ya watu wa Wanefi.
6 Na miaka mia sita na tisa ilikuwa imepita tangu Lehi aondoke Yerusalemu.
7 Na miaka tisa ilikuwa imepita kutoka wakati ambao ishara ilitolewa, ambayo
ilizungumziwa na manabii, kwamba Kristo atakuja katika ulimwengu.
8 Sasa Wanefi walianza kupima wakati wao kutoka muda huu wakati ishara
ilitolewa, au kutoka kwa kuja kwa Kristo; kwa hivyo, miaka tisa ilikuwa imepita.
9 Na Nefi, ambaye alikuwa baba ya Nefi, ambaye alikuwa ameaminiwa maandiko,

hakurudi katika nchi ya Zarahemla, na hakuonekana katika nchi yote.
10 Na ikawa kwamba watu bado walibaki kwenye uovu, ingawaje kulikuwa na kuhubiri kwingi na uaguzi ambao ulipelekwa miongoni mwao; na hivyo mwaka wa kumi ulipita pia; na mwaka wa kumi na moja pia ulipita katika uovu.
11 Na ikawa katika mwaka wa kumi na tatu kukaanza kuwa na vita na mabishano kote nchini; kwani wezi wa Gadiantoni walikuwa wengi sana, na waliwaua watu wengi, na kuharibu miji mingi, na walisambaza vifo vingi na uchinjaji kote nchini, kwamba ilikuwa muhimu kwamba watu wote, Wanefi na Walamani, wachukue silaha dhidi yao.
12 Kwa hivyo, Walamani wote ambao walikuwa wamemgeukia Bwana waliungana na ndugu zao, Wanefi, na walilazimishwa, kwa usalama wa maisha yao na wanawake wao na watoto wao, kuchukua silaha dhidi ya wezi wa Gadiantoni, ndio, na pia kulinda haki zao, na faida ya kanisa lao na kuabudu kwao, na kwa uhuru wao na uungwana wao.
13 Na ikawa kwamba kabla ya mwaka wa kumi na tatu kupita Wanefi walitishwa na maangamizo makubwa kwa sababu ya vita hivi, ambavyo vilikuwa vikali sana.
14 Na ikawa kwamba wale Walamani ambao walijiunga na Wanefi walihesabiwa miongoni mwa Wanefi;
15 Na laana yao ilitolewa kwao, na ngozi yao ikawa nyeupe kama ya Wanefi;
16 Na vijana wao na mabinti zao wakawa warembo sana; na wakahesabiwa miongoni mwa Wanefi, na kuitwa Wanefi. Na hivyo ukaisha mwaka wa kumi na tatu.
17 Na ikawa katika mwaka wa kumi na nne, vita miongoni mwa wezi na watu wa Nefi viliendelea na vikawa vikali sana; walakini, watu wa Nefi walipata faida juu ya wezi, mpaka kwamba wakawarudisha nyuma kutoka nchi yao hadi kwenye milima na kwenye mahali pao pa siri.
18 Na hivyo ukaisha mwaka wa kumi na nne. Na katika mwaka wa kumi na tano wezi walikuja dhidi ya watu wa Nefi; na kwa sababu ya uovu wa watu wa Nefi, na mabishano yao mengi na mafarakano yao, wezi wa Gadiantoni walipata faida nyingi juu yao.
19 Na hivyo ukaisha mwaka wa kumi na tano, na hivyo ndivyo watu walivyokuwa kwenye hali ya mateso mengi; na upanga wa maangamizo ulining'inia juu yao, mpaka kwamba walikuwa karibu kupigwa chini nao, na hii ni kwa sababu ya uovu wao.

## 3 Nefi 3

1 Na sasa ikawa kwamba katika mwaka wa kumi na sita tangu kuja kwa Kristo, Lakoneyo, msimamizi wa nchi, alipokea barua kutoka kwa kiongozi na msimamizi wa hili kundi la wezi; na haya ndiyo yalikuwa maneno ambayo yaliandikwa, yakisema:
2 Lakoneyo, mkuu sana na msimamizi mkuu wa nchi, tazama, ninakuandikia hii barua, na ninakupatia sifa nyingi sana kwa sababu ya uthabiti wako, na pia uthabiti wa watu wako, katika kulinda kile ambacho mnadhani kuwa ni haki yenu na uhuru wenu; ndio, mnasimama vizuri, kama mnaosaidiwa na mungu, kwenye kulinda uhuru wenu, na mali yenu, na nchi yenu, au kile mnachoita chenu.
3 Na inaonekana kama jambo la huruma kwangu, Lakoneyo mwenye cheo

kikubwa, kwamba ungekuwa mpumbavu na bure kudhani kwamba unaweza
kusimama dhidi ya watu walio shujaa ambao wako chini ya amri yangu, ambao
wakati huu wako tayari na silaha zao, na wanangojea kwa hamu kuu wasikie
neno — Nenda chini kwa Wanefi na muwaangamize.
4 Na mimi, nikijua roho yao ya kutoshindwa, nimewajaribu kwenye uwanja wa
vita, na nikijua chuki yao isiyo na mwisho dhidi yenu kwa sababu ya vitu vingi
vibaya ambavyo mmewafanyia, kwa hivyo ikiwa watashuka dhidi yenu
watawaangamiza kabisa.
5 Kwa hivyo nimeandika hii barua, nikiweka muhuri kwa mkono wangu,
nikifikiria ustawi wenu, kwa sababu ya uthabiti wenu kwenye kile ambacho
mnaamini ni haki, na kwa sababu ya roho yenu kuu katika uwanja wa vita.
6 Kwa hivyo ninakuandikia, nikitaka kwamba usalimishe kwa hawa watu wangu,
miji yenu, nchi zenu, na mali yenu, kuliko kwamba wawashambulie kwa upanga na
kuwaangamiza.
7 Au kwa maneno mengine, mjitolee wenyewe kwetu, na mjiunge nasi na mzoeane
na kazi zetu za siri, na muwe ndugu zetu kwamba muwe kama sisi — sio watumwa
wetu, lakini ndugu zetu na washiriki wa mali yetu yote.
8 Na tazama, naapa kwako, ikiwa mtafanya hivi, kwa kiapo, hamtaangamizwa;
lakini kama hamtafanya hivi, ninaapa na kiapo, kwamba mwezi ujao nitaamuru
kwamba majeshi yangu yatashuka dhidi yenu, na hawatajizuia na hawatawahurumia,
lakini watawachinja, na kuachilia upanga uwaangukie hata mpaka mwangamie.
9 Na tazama, mimi ni Gidianhi; na mimi ni mtawala wa hili shirika la siri la
Gadiantoni; shirika ambalo na kazi ambazo najua ni nzuri; na ni za zamani na
zimepitishwa kwetu.
10 Na ninaandika hii barua kwako wewe, Lakoneyo, na ninatumaini kwamba
mtasalimisha mashamba yenu na mali yenu, bila kumwaga damu, kwamba watu
wangu hawa wangepata tena haki zao na serikali yao, ambao wamewaasi kwa sababu
ya uovu wenu wa kuwakataza wapokee haki za serikali, na msipofanya hivi,
nitalipiza mateso yao. Ni mimi Gidianhi.
11 Na sasa ikawa Lakoneyo alipopata hii barua alistaajabu sana, kwa sababu ya
ujasiri wa Gidianhi kudai umiliki wa nchi ya Wanefi, na pia kwa sababu ya kutisha
watu na kulipiza mabaya ya wale ambao hawakuwa wamefanyiwa makosa, isipokuwa
walijikosea wenyewe kwa kuasi hadi kwenye hawa wezi waovu na wa kuchukiza.
12 Sasa tazama, huyu Lakoneyo, msimamizi, alikuwa mtu wenye haki, na hangeweza
kutishwa na mwizi; kwa hivyo hakutii barua ya Gidianhi, msimamizi wa wezi, lakini
alisababisha kwamba watu wake wamwombe Bwana awapatie nguvu dhidi ya wezi
wakati wangekuja chini dhidi yao.
13 Ndio, alipeleka tangazo miongoni mwa watu wote, kwamba wakusanye pamoja
wanawake wao, na watoto wao, wanyama wao, na mifugo yao, na mali yao yote,
isipokuwa nchi yao, mahali pamoja.
14 Na akasababisha kwamba ngome zijengwe kuwazunguka, na ziimarishwe ndani
sana. Na akasababisha kwamba majeshi, yote ya Wanefi na ya Walamani, au ya hao
wote waliohesabiwa miongoni mwa Wanefi, yawekwe kama walinzi hapo karibu
kuwalinda, na kuwalinda kutokana na waporaji usiku na mchana.
15 Ndio, aliwaambia: Kadiri Bwana anavyoishi, msipotubu maovu yenu yote, na
kumwomba Bwana kwa ukweli, hamtakombolewa kwa njia yoyote kutoka mikono
ya wale wezi wa Gadiantoni.

16 Na maneno na unabii wa Lakoneyo ulikuwa mkubwa na wa ajabu kwamba
yalisababisha woga kuwajia watu wote; na walijaribu kwa uwezo wao wote kufanya
kulingana na maneno ya Lakoneyo.
17 Na ikawa kwamba Lakoneyo aliwateua makaptani wakuu wa majeshi yote ya
Wanefi, kuwaamuru wakati wezi watakapokuja chini kutoka nyikani dhidi yao.
18 Sasa aliyekuwa mkuu wa wote miongoni mwa makapteni wote na amri jeshi
mkuu wa majeshi yote ya Wanefi aliteuliwa, na jina lake lilikuwa Gidgidoni.
19 Sasa ilikuwa ni desturi miongoni mwa Wanefi wote kuwateua kama makapteni
wakuu, (isipokuwa wakati ambao wao walikuwa na uovu mwingi), mtu ambaye
alikuwa na roho ya ufunuo na pia ya unabii; kwa hivyo, huyu Gidgidoni alikuwa
nabii mkuu miongoni mwao, kama vile pia alivyokuwa mwamuzi mkuu.
20 Sasa watu walimwambia Gidgidoni: Omba kwa Bwana, na acha twende juu ya
milima na kwenye nyika, ili tuwashambulie wezi na tuwaangamize kwenye nchi zao.
21 Lakini Gidgidoni aliwaambia: Bwana anakataza; kwani ikiwa tutaenda juu dhidi
yao Bwana atatukabidhi mikononi mwao; kwa hivyo tutajitayarisha katikati ya nchi
zetu, na tutakusanya majeshi yetu yote pamoja, na hatutaenda dhidi yao, lakini
tutangoja mpaka watakapokuja dhidi yetu; kwa hivyo kadiri vile Bwana anavyoishi,
ikiwa tutafanya hivi atawaweka mikononi mwetu.
22 Na ikawa katika mwaka wa kumi na saba, kuelekea mwisho wa mwaka, tangazo la
Lakoneyo lilikuwa limeenezwa kote nchini, na walikuwa wamechukua farasi wao,
na magari yao, na ng'ombe wao, na wanyama wao wote, na mifugo yao, na nafaka
yao, na mali yao yote, na walisonga mbele wakiwa maelfu na maelfu, mpaka
walipokuwa wameenda katika mahali ambapo palikuwa pamechaguliwa kwamba
wajikusanye pamoja, kujilinda dhidi ya maadui zao.
23 Na nchi ambayo ilichaguliwa ilikuwa nchi ya Zarahemla, na nchi ambayo ilikuwa
kati ya nchi ya Zarahemla na nchi ya Neema, ndio, kwenye mpaka ambao ulikuwa
miongoni mwa nchi ya Neema na nchi ya Ukiwa.
24 Na kulikuwa na maelfu ya watu ambao waliitwa Wanefi, ambao walijikusanya
pamoja katika nchi hii. Sasa Lakoneyo alisababisha kwamba wajikusanye pamoja
katika nchi iliyo upande wa kusini, kwa sababu ya laana kubwa ambayo ilikuwa
katika nchi ya upande wa kaskazini.
25 Na walijiimarisha dhidi ya maadui zao; na wakaishi katika nchi moja, na kwenye
kundi moja, na waliogopa maneno ambayo yalizungumzwa na Lakoneyo, mpaka
kwamba wakatubu dhambi zao zote; na wakatoa sala zao kwa Bwana Mungu wao,
kwamba angewakomboa wakati ambao maadui wao watakuja chini dhidi yao
kupigana.
26 Na walikuwa na huzuni sana kwa sababu ya maadui wao. Na Gidgidoni
alisababisha kwamba watengeneze silaha za vita za kila aina, na waimarishwe na
silaha, na ngao, na vigao, kufuata maelezo ya namna yake.

## 3 Nefi 4

1 Na ikawa kwamba mwishoni mwa mwaka wa kumi na nane yale majeshi ya wezi
yalikuwa yamejiandaa kwa vita, na walianza kuja chini na kushambulia kutokea
kwenye vilima, na nje ya milima, na nyikani, na ngome zao, na pahali pao pa siri, na
wakaanza kumiliki nchi, zote ambazo zilikuwa katika nchi, iliyokuwa kusini na
ambazo zilikuwa katika nchi iliyokuwa kaskazini, na wakaanza kumiliki nchi zote

zilizokuwa zimeachwa na Wanefi, na miji ambayo ilikuwa imeachwa kwa hali ya
ukiwa.
2 Lakini tazama, hakukuweko na wanyama wa mwitu wala mawindo katika nchi
hizo ambazo ziliachwa na Wanefi, na hakukuwa na mawindo kwa wezi isipokuwa
kwenye nyika.
3 Na wezi waliweza tu kuishi kwenye nyika, kwa uhitaji wa chakula; kwani Wanefi
waliacha nchi zao zikiwa hazina kitu, na walikusanya wanyama wao na mifugo yao
na mali yao yote, na walikuwa kwenye kikundi kimoja.
4 Kwa hivyo, hakukuwa na nafasi ya wezi kupora na kupata chakula, isipokuwa
wangekuja kwa vita vya wazi kupigana dhidi ya Wanefi; na Wanefi wakiwa katika
kikundi kimoja, na wakiwa na idadi kubwa, na wakiwa wamejiwekea akiba ya
vyakula, na farasi na ng'ombe, na wanyama wa kila aina, kwamba wangejilisha kwa
muda wa miaka saba, wakati ambao walitumainia kuangamiza wezi kutoka nchini;
na hivyo mwaka wa kumi na nane ulipita.
5 Na ikawa kwamba katika mwaka wa kumi na tisa Gidianhi alipata kwamba
ilikuwa muhimu kwake kwamba afanye vita dhidi ya Wanefi, kwani hakukuwa na
njia ambayo wangeishi isipokuwa kupora, kuiba, na kuua.
6 Na hawangethubutu kujitapanya usoni mwa nchi ili wakuze nafaka, wasije
Wanefi wakawaua; kwa hivyo Gidianhi alitoa amri kwa majeshi yake kwamba,
mwaka huu waende kupigana dhidi ya Wanefi.
7 Na ikawa kwamba walikuja kupigana; na ilikuwa katika mwezi wa sita; na
tazama, ile siku ambayo walikuja kupigana ilikuwa kubwa na ya kutisha; na
walikuwa wamevaa kwa njia ya wezi; na walikuwa na ngozi ya mwanakondoo
viunoni mwao, na walijipaka rangi ya damu, na vichwa vyao vilinyolewa, na
walikuwa na vyapeo juu yao; na majeshi ya Gidianhi yalionekana mengi na ya
kuogofya, kwa sababu ya silaha zao, na kwa sababu ya kujipaka damu.
8 Na ikawa kwamba majeshi ya Wanefi, walipoona majeshi ya Gidianhi
yalivyoonekana, wote walijilaza kwenye ardhi, na kumwomba Bwana Mungu wao,
kwamba awahurumie na kuwakomboa kutoka mikono ya maadui wao.
9 Na ikawa kwamba majeshi ya Gidianhi yalipoona hivi walianza kupaza sauti, kwa
sababu ya shangwe yao, kwani walidhani kwamba Wanefi walianguka kwa woga kwa
sababu ya kuonekana kwa vitisho vya majeshi yao.
10 Lakini kwa hiki kitu walisikitika, kwani Wanefi hawakuwaogopa; lakini
walimwogopa Mungu wao na walimwomba awalinde; kwa hivyo, wakati majeshi ya
Gidianhi yalipowavamia walikuwa tayari kukabiliana nao; ndio, kwa nguvu za
Bwana walikabiliana nao.
11 Na vita vilianza kwenye huu mwezi wa sita; na vilikuwa vikubwa na vya kutisha,
ndio, uchinjaji ulikuwa mwingi na wa kutisha, mpaka kwamba hakujakuweko
uchinjaji mkuu kama huo unaojulikana miongoni mwa watu wa Lehi tangu
aondoke Yerusalemu.
12 Na ingawa kulikuwa na vitisho na viapo ambavyo Gidianhi alikuwa amefanya,
tazama, Wanefi waliwashinda mpaka kwamba wakarudi nyuma kutoka kwao.
13 Na ikawa kwamba Gidgidoni aliamuru kwamba majeshi yake yawafukuze hadi
kwenye mipaka ya nyika, na kwamba wasimhurumie yeyote ambaye ataanguka
mikononi mwao njiani; na hivyo waliwafukuza na kuwaua, kwenye mipaka ya
nyika, hata mpaka walipotimiza amri ya Gidgidoni.
14 Na ikawa kwamba Gidianhi, ambaye alisimama na kupigana kwa ujasiri,

alifukuzwa wakati alipokuwa anakimbia; na akiwa amechoka kwa sababu ya
kupigana kwingi alipitwa na kuuawa. Na hivyo maisha ya Gidianhi mwizi yaliisha.
15 Na ikawa kwamba majeshi ya Wanefi yalirejea tena mahali pao pa usalama. Na
ikawa kwamba mwaka wa kumi na tisa ulipita, na wezi hawakuja tena kupigana;
wala hawakuja tena katika mwaka wa ishirini.
16 Na katika mwaka wa ishirini na moja hawakuja kupigana, lakini walikuja kutoka
pande zote na kuwazunguka watu wa Nefi; kwani walidhani kwamba wangewazuilia
mbali watu wa Nefi kutoka katika nchi zao, na kuwafungia ndani kila upande, na
ikiwa wangewazuilia kutoingia kwa haki zao zote za nje, kwamba wangewasababisha
wajitolee wenyewe kulingana na matakwa yao.
17 Sasa walikuwa wamejiteulia kiongozi mwingine, ambaye jina lake lilikuwa
Zemnariha; kwa hivyo alikuwa Zemnariha ndiye aliyeamuru kwamba kuzingirwa
kufanyike.
18 Lakini tazama, hii ilikuwa faida kwa Wanefi; kwani haingewezekana kwa wezi
kuwazingira kwa muda wa kutosha ili kuwe na matokeo kwa Wanefi, kwa sababu ya
vyakula vyao vingi, ambavyo walikuwa wameweka kwenye ghala.
19 Na kwa sababu ya ukosefu wa vyakula miongoni mwa wezi; kwani tazama,
hawakuwa na chochote isipokuwa nyama kwa chakula chao, nyama ambayo
walipata nyikani;
20 Na ikawa kwamba wanyama wa mwitu walikuwa wachache kwenye nyika mpaka
kwamba wezi walikuwa karibu kuangamia kwa njaa.
21 Na Wanefi siku zote walikuwa wakitoka nje mchana na usiku, na kuwashambulia
maadui wao, na kuwaangamiza kwa maelfu na maelfu.
22 Na hivyo ikawa kupenda kwa watu wa Zemnariha kuachilia kusudi lao, kwa
sababu ya uharibifu mkuu ambao uliwajia usiku na mchana.
23 Na ikawa kwamba Zemnariha aliwaamuru watu wake kwamba warudi nyuma
wenyewe kutoka kwa mazingira, na waende kwenye sehemu ya mbali nchi ya
upande wa kaskazini.
24 Na sasa, Gidgidoni akijua kusudi lao, na akijua udhaifu wao kwa sababu ya
ukosefu wa chakula, na mauaji mengi ambayo yalifanywa miongoni mwao, kwa
hivyo alituma nje majeshi yake wakati wa usiku, na akazuia njia yao ya kurudi
nyuma, na akaweka majeshi yake kwenye njia yao ya kurudi nyuma.
25 Na hii ilifanywa wakati wa usiku, na walisonga na kupita mbele ya wezi, kwamba
kesho yake, wakati wezi walipoanza kusonga, walisimamishwa na majeshi ya Wanefi
kote mbele yao na nyuma yao.
26 Na wezi ambao walikuwa kusini walizuiliwa pia kwenye sehemu zao ambazo
wangefuata kwa kurudi nyuma. Na hivi vitu vyote vilifanywa kwa amri ya
Gidgidoni.
27 Na kulikuwa na maelfu wengi ambao walijitoa kama wafungwa kwa Wanefi, na
waliosalia waliuawa.
28 Na kiongozi wao, Zemnariha, alichukuliwa na kunyongwa kwenye mti, ndio,
hata juu ya mti mpaka akafa. Na wakati walipomnyonga mpaka kufa, waliangusha
mti ardhini, na wakapaza sauti, wakisema:
29 Bwana awahifadhi watu wake katika haki na utakatifu wa moyo, ili wasababishe
kuangushwa chini wale wote ambao watataka kuwaua kwa kutumia nguvu na
mashirika ya siri, kwa njia sawa kama vile huyu mtu alivyoangushwa ardhini.
30 Na walifurahi na kupiga makelele tena kwa sauti moja, wakisema: Mungu wa

Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo, awalinde hawa watu kwa haki, kadiri vile watakavyo lilingana jina la Mungu wao kwa kinga.
31 Na ikawa kwamba kwa ghafla, wote pamoja waliimba, na kumsifu Mungu wao kwa kitu kikubwa ambacho aliwafanyia, kwa kuwahifadhi kutoka kwa mikono ya maadui wao.
32 Ndio, walipiga kelele: Hosana kwa Mungu Aliye Juu Sana. Na wakapiga kilele: Heri liwe jina la Bwana Mungu Mwenyezi, Mungu Aliye Juu Sana.
33 Na mioyo yao ilifura kwa shangwe, mpaka kwenye kutoa machozi mengi, kwa sababu ya uzuri mwingi wa Mungu kuwakomboa kutoka mikono ya maadui wao; na walijua ni kwa sababu ya kutubu kwao na unyenyekevu wao kwamba walikuwa wamekombolewa kutoka kwa maangamizo yasiyo na mwisho.

## 3 Nefi 5

1 Na sasa tazama, hakukuwa hata nafsi moja miongoni mwa watu wote wa Wanefi ambayo ilikuwa na shaka hata kidogo katika maneno ya manabii watakatifu ambao walizungumza; kwani walijua kwamba ilikuwa muhimu kwamba yatimizwe.
2 Na walijua kwamba ni muhimu kwamba Kristo alikuwa amekuja, kwa sababu ya ishara nyingi ambazo zilikuwa zimetolewa kulingana na maneno ya manabii; na kwa sababu ya vitu ambavyo vilikuwa vimetimizwa kitambo walijua kwamba ilikuwa muhimu kwamba vitu vyote vitimizwe kulingana na yale ambayo yalikuwa yamezungumzwa.
3 Kwa hivyo waliacha dhambi zao zote, na machukizo yao, na ukahaba wao, na walimtumikia Mungu kwa bidii yote mchana na usiku.
4 Na sasa ikawa kwamba wakati walikuwa wamechukua wezi wote kama wafungwa, mpaka kwamba hakuna aliyetoroka ambaye hakuuawa, waliwatupa wafungwa wao gerezani, na wakasababisha neno la Mungu kuhubiriwa kwao; na kadiri wengi walipotubu dhambi zao na kufanya agano kwamba hawataua tena waliachiliwa huru.
5 Lakini kadiri kulipokuwa na wengi ambao hawakufanya agano, na ambao waliendelea na mauaji ya siri mioyoni mwao, ndio, vile wengi walipatikana wakitoa vitisho kwa ndugu zao walihukumiwa na kuadhibiwa kulingana na sheria.
6 Na hivyo walimaliza yale maovu yote, na siri, na mashirika ya machukizo, ambamo kwake kulikuwa na maovu mengi sana, na kutendeka kwa mauaji mengi.
7 Na hivyo mwaka wa ishirini na mbili ulikuwa umepita, na mwaka wa ishirini na tatu pia, na wa ishirini na nne, na wa ishirini na tano; na hivyo miaka ishirini na tano ilipita.
8 Na vitu vingi vilikuwa vimetendeka ambavyo, kwa maoni ya watu kadhaa, vilikuwa vikubwa na vya kushangaza; walakini, vyote haviwezi kuandikwa kwenye kitabu hiki; ndio, kitabu hiki hakiwezi kutosha hata sehemu moja ya mia ya yale yaliyofanyika miongoni mwa watu wengi hivyo kwa muda wa miaka ishirini na tano.
9 Lakini tazama kuna maandishi ambayo yana mambo yote ya hawa watu; na taarifa fupi zaidi na ya kweli ilitolewa na Nefi.
10 Kwa hivyo nimetengeneza maandishi yangu ya vitu hivi kulingana na kumbukumbu ya Nefi, ambayo ilichorwa kwenye bamba ambazo ziliitwa bamba za Nefi.
11 Na tazama, ninatengeneza maandishi kwenye bamba ambazo nimeunda kwa

mikono yangu mwenyewe.
12 Na tazama, ninaitwa Mormoni, nikiitwa kufuatana na nchi ya Mormoni, nchi ambamo Alma alianzisha kanisa miongoni mwa watu, ndio, kanisa la kwanza ambalo lilianzishwa miongoni mwao baada ya uhalifu wao.
13 Tazama, mimi ni mwanafunzi wa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Nimeitwa na yeye kutangaza neno lake miongoni mwa watu wake, ili wawe na maisha yasiyo na mwisho.
14 Na imekuwa muhimu kwamba mimi, kwa kutii mapenzi ya Mungu, kwamba sala za wale ambao wameenda mbele, ambao walikuwa watakatifu, sharti itatimizwa kulingana na imani yao, niandike maandishi ya vitu hivi ambavyo vimefanywa—
15 Ndio, maandishi madogo ya yale mambo ambayo yamefanyika kutoka wakati ambao Lehi aliondoka Yerusalemu, hata chini mpaka wakati huu.
16 Kwa hivyo nitatengeneza maandishi yangu kutoka kwa kumbukumbu ambazo zilitolewa na wale ambao walikuwa mbele yangu, hadi mwanzo wa maisha yangu;
17 Na ndipo nafanya haya maandishi ya vitu ambavyo nimeona kwa macho yangu.
18 Na ninajua maandishi ninayoandika kuwa ya haki na ya kweli; walakini kuna vitu vingi ambavyo, kwa sababu ya lugha yetu, hatuwezi kuviandika.
19 Na sasa ninamaliza kuzungumza, juu yangu mwenyewe, na nitaendelea kutoa historia yangu ya vitu ambavyo vimefanyika mbele yangu.
20 Mimi ni Mormoni, na ni wa kizazi cha Lehi kamili. Ninayo sababu ya kumsifu Mungu wangu na Mwokozi wangu Yesu Kristo, kwamba aliwaleta babu zetu kutoka nchi ya Yerusalemu, (na hakuna yeyote aliyeijua isipokuwa yeye tu na wale ambao aliwaleta kutoka nchi hiyo) na kwamba amenipatia mimi na watu wangu elimu nyingi katika wokovu wa nafsi zetu.
21 Kwa kweli ameibariki nyumba ya Yakobo, na amekuwa na huruma kwa uzao wa Yusufu.
22 Na ikiwa vile uzao wa Lehi umetii amri zake amewabariki na kuwasaidia kufanikiwa kulingana na neno lake.
23 Ndio, na kwa kweli ataleta sazo la uzao wa Yusufu kuwaelemisha kuhusu Bwana Mungu wao.
24 Na kwa kweli kadiri Bwana anavyoishi, atakusanya ndani kutoka katika pembe nne za dunia sazo lote la uzao wa Yakobo, ambao wametawanyika ugenini kote usoni mwa nchi.
25 Na vile amefanya agano na nyumba yote ya Yakobo, hivyo hivyo agano ambalo amefanya na nyumba ya Yakobo litatimizwa kwa wakati wake mwenyewe, kwa kurudisha nyumba yote ya Yakobo kwenye ujuzi wa agano ambalo amefanya nao.
26 Na hapo ndipo watajua Mkombozi wao, ambaye ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu; na ndipo watakusanywa kutoka pembe nne za dunia hadi kwenye nchi zao, kutoka ambapo walitawanywa; ndio, kadiri Bwana aishivyo ndivyo itakavyokuwa. Amina.

## 3 Nefi 6

1 Na sasa ikawa kwamba watu wa Wanefi wote walirudi kwenye nchi zao katika mwaka wa ishirini na sita, kila mtu na jamaa yake, wanyama wake, na mifugo yake, farasi wake na ngombe wake, na vitu vyote vilivyokuwa vyao.
2 Na ikawa kwamba walikuwa hawajamaliza vyakula vyao vyote; kwa hivyo

walichukua hivyo vyote ambavyo walikuwa hawajala, nafaka yao yote ya kila aina, na dhahabu yao, na fedha yao, na vitu vyao vyote vya thamani, na wakarudi kwenye nchi zao na umiliki wao, kote kaskazini na kusini, kote katika nchi upande wa kaskazini na nchi ya upande wa kusini.

3 Na waliwapatia ardhi wale wezi ambao walishiriki ndani ya agano la kuweka amani ya nchi, ambao walikuwa wamependelea kubaki Walamani, kulingana na wingi wao ili kwa bidii yao wangeweza kujilisha; na hivyo wakaimarisha amani kote nchini.

4 Na walianza tena kufanikiwa na kuwa wakubwa; na miaka ya ishirini na sita na ya saba ilipita, na kukawa na amri nchini; na wakawa wametengeneza sheria zao kulingana na usawa na haki.

5 Na sasa hakukuwa na kitu chochote kote nchini cha kuwazui watu kufanikiwa siku zote, isipokuwa kama wangefanya kosa.

6 Na sasa ikawa ni Gidgidoni, na yule mwamuzi, Lakoneyo, na wale ambao walikuwa wameanzisha hii imani kuu katika nchi.

7 Na ikawa kwamba kulikuwa na miji mingi iliyojengwa upya, na kulikuwa na miji mingi ya kale iliyorekebishwa.

8 Na kulikuwa njia kuu nyingi zilizojengwa, na barabara nyingi zilizotengenezwa, ambazo zilielekea kutoka mji hadi mwingine, na kutoka nchi hadi nyingine, na kutoka mahali hadi pengine.

9 Na hivyo mwaka wa ishirini na nane ulipita, na watu walikuwa na amani siku zote.

10 Lakini ikawa katika mwaka wa ishirini na tisa, kukaanza kuwa na mabishano miongoni mwa watu; na wengine walijiinua kwa kiburi na majivuno kwa sababu ya utajiri wao mkuu, ndio, hata kwenye kutesa wale ambao walikuwa masikini na wanyenyekevu.

11 Kwani kulikuwa na wafanyibiashara wengi katika nchi, na pia mawakili wengi, na wakuu wengi.

12 Na watu walianza kutambuliwa kwa vyeo, kulingana na utajiri wao, na nafasi za kusoma; ndio, wengine walikuwa hawajui kwa sababu ya umasikini wao, na wengine walipata elimu nyingi kwa sababu ya utajiri wao.

13 Wengine walijiinua kwa kiburi na wengine walikuwa wanyenyekevu sana; na wengine walimtukana yeyote aliyewatusi, wakati wengine wangepata matusi na udhalimu na kila aina ya mateso, na hawangegeuka na kutoa matusi, lakini walikuwa wanyenyekevu na wenye kutubu mbele ya Mungu.

14 Na hivyo kulikuwa na kutokuwa na usawa ndani ya nchi yote, mpaka kwamba kanisa lilianza kugawanywa kwenye vikundi; ndio, mpaka kwamba katika mwaka wa thelathini, kanisa liligawanyika ndani ya nchi yote isipokuwa miongoni mwa Walamani wachache ambao waliogeukia imani ya kweli; na hawangeiacha, kwani walikuwa imara, na thabiti na wasiotingishika, na wanaotamani kwa bidii yote kutii amri za Bwana.

15 Sasa kiini cha huu uovu wa watu kilikuwa hiki — Shetani alikuwa na nguvu nyingi kwa kuchochea watu kufanya aina yote ya uovu, na kujaza watu na kiburi, akiwashawishi kutafuta uwezo na mamlaka, na utajiri, na vitu vilivyo bure vya ulimwengu.

16 Na kwa hivyo Shetani aliipotosha mbali mioyo ya watu kufanya aina yote ya uovu; kwa hivyo walifurahishwa na amani lakini kwa miaka michache tu.

17 Na hivyo katika mwanzo wa mwaka wa thelathini — watu wakiwa wameachiliwa kwa muda mrefu kuhangaishwa na majaribio ya ibilisi mahali pote alipotaka kuwapeleka, na kufanya aina yote ya maovu aliyotaka wafanye — na hivyo mwanzoni mwa mwaka huu wa thelathini, walikuwa kwenye hali ya uovu wa kuogopesha.

18 Sasa hawakufanya dhambi bila kujua, kwani walijua kile Mungu alichotaka wafanye, kwani ilikuwa imefundishwa kwao; kwa hivyo waliasi kwa makusudi dhidi ya Mungu.

19 Na sasa ilikuwa katika siku za Lakoneyo, mwana wa Lakoneyo, kwani Lakoneyo alitwaa kiti cha baba yake na akasimamia watu mwaka huo.

20 Na kulianza kuwa na watu waliotumwa mbele na kuongozwa kutoka mbinguni, ambao walisimama miongoni mwa watu katika nchi yote, wakihubiri na kushuhudia kwa ujasiri kwa ajili ya dhambi na uovu wa watu, na kushuhudia kwao kuhusu ukombozi ambao Bwana angewafanyia watu wake, au kwa maneno mengine, ufufuo wa Kristo; na walishuhudia kwa ujasiri kifo chake na maumivu yake.

21 Sasa kulikuwa na watu wengi ambao walikasirika sana kwa sababu ya wale ambao walishuhudia vitu hivi; na wale ambao walikasirika walikuwa kwa wingi waamuzi wakuu na wale waliokuwa makuhani wakuu, na mawakili hapo mbeleni; ndio, wale wote ambao walikuwa mawakili waliwakasirikia wale ambao walishuhudia vitu hivi.

22 Sasa hakukuwa na wakili wala mwamuzi wala kuhani mkuu ambaye alikuwa na uwezo wa kuhukumu mtu yeyote kufa isipokuwa hukumu yao iwekwe muhuri na mlinzi wa nchi.

23 Sasa kulikuwa na wengi ambao walishuhudia vitu hivi kuhusu Kristo, ambao walishuhudia kwa ujasiri, ambao walichukuliwa kisiri na kuuawa na waamuzi, kwamba vifo vyao havikujulikana na mtawala wa nchi mpaka baada ya vifo vyao.

24 Sasa tazama, hii ilikuwa kinyume cha sheria za nchi, kwamba mtu yeyote auawe isipokuwa wapate uwezo kutoka kwa msimamizi wa nchi —

25 Kwa hivyo nung'uniko lilitokea katika nchi ya Zarahemla, kwa msimamizi wa nchi, dhidi ya hawa waamuzi ambao walihukumu kufa kwa manabii wa Bwana, sio kulingana na sheria.

26 Sasa ikawa kwamba walichukuliwa na kuletwa mbele ya mwamuzi, kuhukumiwa kwa kosa ambalo walikuwa wamefanya, kulingana na sheria ambayo ilikuwa imetolewa na watu.

27 Na ikawa kwamba hawa waamuzi walikuwa na marafiki wengi na jamaa; na waliosalia, ndio, hata karibu mawakili wote na makuhani wakuu, walijikusanya pamoja na kujiunga na jamaa za waamuzi ambao walikuwa wajaribiwe kulingana na sheria.

28 Na walifanya agano kila mmoja na mwingine, ndio, hata kwenye lile agano ambalo lilitolewa na wale wa kale, agano ambalo lilitolewa na kusimamiwa na ibilisi, kuungana dhidi ya wote walio haki.

29 Kwa hivyo waliungana dhidi ya watu wa Bwana, na kufanya agano kuwaangamiza, na kuokoa wale ambao walikuwa na hatia ya kuua kutokana na kufahamu haki, ambayo ilikuwa karibu kutekelezwa kulingana na sheria.

30 Na walidharau sheria na haki za nchi yao; na wakafanya agano wao wenyewe kwa wenyewe kumwangamiza msimamizi, na kumweka mfalme juu ya nchi, ili nchi isiwe na uhuru lakini iwe chini ya wafalme.

# 3 Nefi 7

1 Sasa tazama nitawaonyesha nyinyi kwamba hawakumweka mfalme juu ya nchi,
lakini katika mwaka huu huu, ndio, mwaka wa thelathini, walimwangamiza na
kumuua mwamuzi mkuu akiwa kwenye kiti chake cha hukumu.
2 Na watu waligawanyika mmoja dhidi ya mwingine; na walijitenga mmoja kutoka
kwa mwingine kwa makabila, kila mtu kulingana na jamaa yake na ukoo wake na
marafiki; na hivyo wakaharibu serikali ya nchi.
3 Na kila kabila lilichagua chifu au kiongozi juu yao; na hivyo wakapata kuwa
makabila na viongozi wa makabila.
4 Sasa tazama, kila mtu miongoni mwao alikuwa na wengi katika jamaa yake, na
ndugu wengi na marafiki; kwa hivyo makabila yao yalikuwa makubwa sana.
5 Sasa hii yote ilifanyika, na bado hakukuwa na vita miongoni mwao; na huu uovu
wote ulikuwa umewajia watu kwa sababu walijisalimisha kwa nguvu ya Shetani.
6 Na sheria za serikali ziliharibiwa, kwa sababu ya shirika la siri la marafiki na ukoo
wa wale ambao waliwaua manabii.
7 Na walisababisha ubishi mwingi nchini, mpaka kwamba sehemu kubwa ya wenye
haki ilikuwa karibu yote imekuwa mbaya; ndio, kulikuwa tu watu wachache wenye
haki miongoni mwao.
8 Na hivyo miaka sita ilikuwa haijapita tangu sehemu kubwa ya watu igeuke
kutoka kwa haki, kama mbwa akiyarudia matapiko yake mwenyewe au kama
nguruwe aliyeoshwa akirudi kugaagaa matopeni.
9 Sasa hili shirika ovu la siri ambalo lilileta uovu mwingi juu ya watu, walijikusanya
pamoja, na wakamweka mtu waliyemwita Yakobo kuwa kiongozi wao;
10 Na walimwita mfalme wao; kwa hivyo alipata kuwa mfalme wa hili kundi ovu;
na alikuwa mmoja wa watu mashuhuri, ambaye alitoa sauti yake dhidi ya manabii
ambao walishuhudia kuhusu Yesu.
11 Na ikawa kwamba hawakuwa wengi kama makabila ya watu, ambao waliungana
pamoja isipokuwa viongozi wao waliweka sheria kila mmoja kwa kabila lake; hata
hivyo walikuwa maadui; ingawa hawakuwa watu wa haki, lakini waliunganishwa
katika chuki ya wale ambao walikuwa wamefanya agano kuangamiza serikali.
12 Kwa hivyo, Yakobo akiona kwamba maadui wao walikuwa wengi kuliko wao,
kwa sababu alikuwa mfalme wa lile kundi, kwa hivyo aliamuru watu wake kwamba
wakimbilie upande wa kaskazini kabisa ya nchi, na huko waanzishe dola yao, mpaka
waasi watakapojiunga nao, (kwani aliwabembeleza kwamba kutakuwa na waasi
wengi) na mpaka wawe na nguvu ya kutosha kukabiliana na makabila ya watu; na
walifanya hivyo.
13 Na mwendo wao ulikuwa wa kasi sana kwamba hawangesimamishwa mpaka
walipokuwa wameenda mbali kupita ambapo watu wangewafikia. Na hivyo ukaisha
mwaka wa thelathini; na hivyo ndivyo shughuli za watu wa Nefi zilivyokuwa.
14 Na ikawa katika mwaka wa thelathini na moja kwamba walijigawa katika
makabila, kila mtu kulingana na jamaa yake, ukoo na marafiki; lakini walikuwa
wamefikia mkataba kwamba hawangeanza vita tena mmoja na mwingine; lakini
hawakujiunga katika sheria zao, na kila kabila lilikuwa na aina yake ya serikali, kwani
zilianzishwa kufuatana na fikira za wale ambao walikuwa wakuu wao. Lakini
walianzisha sheria kali sana kwamba kabila moja lisichukize lingine, mpaka kwamba
kwa kiasi fulani walikuwa na amani nchini; lakini, mioyo yao iligeuka kutoka kwa
Bwana Mungu wao, na wakawapiga kwa mawe, manabii na kuwatupa nje kutoka

miongoni mwao.
15 Na ikawa kwamba Nefi—akishatembelewa na malaika, na pia sauti ya Bwana,
kwa hivyo akiwa ameona malaika, na akiwa shahidi aliyeona na macho, na akiwa
amepewa uwezo ili ajue kuhusu huduma ya Kristo, na pia akiwa shahidi aliyeona na
macho kurudi kwao kwa haraka kutoka kwa haki hadi kwenye uovu wao na
machukizo;
16 Kwa hivyo, kwa sababu ya kuhuzunishwa kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao na
kutofahamu kwa akili zao—aliendelea miongoni mwao katika huo huo mwaka na
kuanza kushuhudia kwa ujasiri, toba na msamaha wa dhambi kupitia imani katika
Bwana Yesu Kristo.
17 Na aliwafundisha vitu vingi; na vyote haviwezi kuandikwa, na sehemu yao
haiwezi kutosheleza, na kwa hivyo havijaandikwa kwenye kitabu hiki. Na Nefi
alifundisha kwa uwezo na mamlaka.
18 Na ikawa kwamba walimkasirikia, hata kwa sababu alikuwa na uwezo kuwaliko,
kwani haikuwezekana kwamba washuku neno lake, kwani imani yake kwa Bwana
Yesu Kristo ilikuwa kubwa kwamba malaika walimhudumia kila siku.
19 Na katika jina la Yesu alitupa nje mashetani na pepo mbaya; na hata alimfufua
kaka yake kutoka kwa wafu, baada ya watu kumpiga kwa mawe na kumuua.
20 Na watu waliona, na kushuhudia kuwa ilitendeka, na walimkasirikia kwa sababu
ya uwezo wake; na pia alifanya miujiza mingi, machoni mwa watu, katika jina la
Yesu.
21 Na ikawa kwamba mwaka wa thelathini na moja uliisha, na kulikuwa tu
wachache ambao walimgeukia Bwana; lakini kadiri wengi waliogeuka walionyesha
watu kwamba walitembelewa na uwezo na Roho wa Mungu, ambaye alikuwa katika
Yesu Kristo, ambamo kwake waliamini.
22 Na jinsi kwa wengi mashetani yalikuwa yametupwa nje yao, na magonjwa yao
kuponywa, na udhaifu wao, walishuhudia kwa ukweli kwa watu kwamba waliguswa
na Roho ya Mungu, na walikuwa wameponywa; na waliendelea kuonyesha ishara
pia na kufanya miujiza miongoni mwa watu.
23 Hivyo mwaka wa thelathini na mbili uliisha pia. Na Nefi aliwazungumzia watu
kwa sauti kubwa katika mwanzo wa mwaka wa thelathini na tatu; na aliwahubiria
toba na msamaha wa dhambi.
24 Sasa nataka wewe ukumbuke pia, kwamba hakukuwa na mmoja ambaye aliletwa
kwenye toba ambaye hakubatizwa kwa maji.
25 Kwa hivyo walitawazwa na Nefi, watu kwa huduma hii, kwamba yeyote
atakayekuja kwao wangembatiza kwa maji, na walifanya hii kama ushahidi na
ushuhuda mbele ya Mungu, na kwa watu, kwamba wametubu na kusamehewa
dhambi zao.
26 Na kulikuwa na wengi katika mwanzo wa mwaka huu ambao walibatizwa
ubatizo wa toba, na hivyo sehemu kubwa ya mwaka ilipita.

# 3 Nefi 8

1 Na sasa ikawa kwamba kulingana na maandishi yetu, na tunajua maandishi yetu
kuwa ya kweli, kwani tazama, alikuwa mtu wa haki ambaye aliandika haya
maandishi—kwani kweli alifanya miujiza mingi katika jina la Yesu; na hakukuweko
na mtu yeyote ambaye angefanya miujiza katika jina la Yesu isipokuwa awe

ameoshwa kila chembe kutokana na uovu wake.
2 Na sasa ikawa, kama hakukuwa na kosa lililotendwa na huyu mtu katika
kuhesabu majira yetu, mwaka wa thelathini na tatu ulikuwa umepita.
3 Na watu walianza kuangalia kwa bidii kwa ishara ambayo ilitolewa na nabii
Samweli, Mlamani, ndio, kwa wakati ambao kungekuwa na giza kwa muda wa siku
tatu usoni mwa nchi.
4 Na kulianza kuwa na mashaka makuu na ugomvi miongoni mwa watu, ingawaje
ishara nyingi zilikuwa zimetolewa.
5 Na ikawa katika mwaka wa thelathini na nne, katika mwezi wa kwanza siku ya
nne ya mwezi, kulitokea dhoruba kubwa, ambayo haijawahi kujulikana katika nchi
yote.
6 Na kulikuwa pia tufani kubwa na ya kutisha; na kukawa na radi ya kutisha,
mpaka kwamba ilitingisha dunia yote kama karibu kupasuka mbalimbali.
7 Na kulikuwa na umeme wa nguvu sana, ambao haujajulikana katika nchi yote.
8 Na mji wa Zarahemla ulianza kuchomeka.
9 Na mji wa Moroni ulizama kwenye kilindi cha bahari, na wakazi wake walitota.
10 Na ardhi ilifunika mji wa Moroniha, kwamba katika mahali pa mji kulitokea
mlima mkubwa.
11 Na kulikuwa na uharibifu mkuu na wa kutisha katika nchi ya upande wa kusini.
12 Lakini tazama, kulikuwa na uharibifu mkubwa zaidi na wa kutisha katika nchi ya
upande wa kaskazini; kwani tazama, sura ya nchi yote ilibadilika, kwa sababu ya
tufani na kimbunga, na radi na umeme, na tetemeko kubwa la nchi yote.
13 Na barabara kuu zilibomoka, na barabara laini ziliharibika, na mahali pengi laini
palikwaruzwa.
14 Na miji mingi iliyojulikana ilizama, na mingi ikachomwa, na mingi ilitingishwa
mpaka majengo yao yakaanguka ardhini, na wakazi wa miji waliuawa, na mahali
paliwachwa penye ukiwa.
15 Na kulikuwa na miji ambayo ilibaki; lakini uharibifu kwayo ulikuwa mkubwa
sana, na kulikuwa na wengi ndani ya miji ambao waliuawa.
16 Na kulikuwa na wengine ambao walichukuliwa na vimbunga; na mahali
walipoenda hakuna mtu anayejua, isipokuwa wanajua kwamba walipelekwa mbali.
17 Na hivyo uso wa ardhi yote uligeuzwa, kwa sababu ya tufani, na radi, na umeme,
na kutingishika kwa nchi.
18 Na tazama, miamba ilipasuka punde mbili; ilivunjika juu ya uso wa ardhi yote,
mpaka kwamba ilipatikana katika vipande, kwa nyufa na mianya, juu ya uso wa nchi
yote.
19 Na ikawa kwamba wakati radi, na umeme, na vimbunga, na tufani, na tetemeko
la nchi vilipokwisha — kwani tazama, ulidumu muda wa masaa matatu; na watu
wengine walisema kwamba muda ulikuwa mrefu kuliko huo; walakini vitu hivi
vyote vikubwa na vya kutisha vilifanyika katika muda wa masaa matatu — na kisha
tazama, kulikuwa na giza juu ya nchi.
20 Na ikawa kwamba kulikuwa na giza jeusi juu ya uso wa nchi, mpaka kwamba
wakazi wake ambao walikuwa hawajakufa waliweza kuhisi ukungu wa giza;
21 Na hakungekuwa na mwanga kwa sababu ya giza, wala mshumaa, wala mienge;
wala hakungewashwa moto na miti yao mizuri na iliyokauka sana, kwamba
hakungekuwa mwanga wowote;
22 Na hakukuonekana mwanga wowote, wala moto, wala mwanga kidogo, wala jua,

wala mwezi, wala nyota, kwani ukungu wa giza ulikuwa mwingi sana ambao ulikuwa
juu ya uso wa nchi.
23 Na ikawa kwamba ulidumu kwa muda wa siku tatu kwamba hakukuwa na
mwanga ambao ulionekana; na kulikuwa na maombolezo makubwa na kulia kwa
hasira na kilio miongoni mwa watu wote bila kikomo; ndio, kulikuwa na kugumia
kwingi kwa watu, kwa sababu ya giza na uharibifu mkubwa ambao uliwajia.
24 Na mahali pamoja walisikika wakilia wakisema: Ee kwamba kama tulikuwa
tumetubu mbele ya siku hii kubwa ya kutisha, na basi ndugu zetu wangehurumiwa,
na hawangechomwa katika ule mji mkuu wa Zarahemla.
25 Na mahali pengine walisikika wakilia wakisema: Ee tunatamani kama
tungekuwa tumetubu mbele ya hii siku kubwa ya kutisha, na kuwa hatungeua na
kupiga manabii kwa mawe, na kuwatupa nje; hapo mama zetu na mabinti zetu
warembo, na watoto wetu wangehurumiwa, na hawangezikwa katika mji wa
Moroniha. Na hivyo vilio vya watu vilikuwa vikubwa na vya kuhofisha.

# 3 Nefi 9

1 Na ikawa kwamba kulikuwa na sauti iliyosikika miongoni mwa wakazi wa nchi, juu
ya uso wa nchi hii, wakisema kwa sauti:
2 Ole, ole, ole kwa watu hawa; ole kwa wakazi wa dunia nzima isipokuwa watubu;
kwani ibilisi hucheka, na malaika wake hufurahi, kwa sababu ya mauaji ya vijana
wazuri na mabinti za watu wangu; na imefanyika kwa sababu ya uovu wao na
machukizo kwamba wamekufa.
3 Tazama, nimeuchoma mji mkuu wa Zarahemla na wakazi wake kwa moto.
4 Na tazama ule mji mkuu Moroni nimeuzamisha kwenye kilindi cha bahari, na
wakazi wake wamekufa maji.
5 Na tazama huo mji mkuu Moroniha nimeufunika kwa udongo, pamoja na
wakazi wake, kuficha uovu wao na machukizo yao kutoka usoni mwangu, kwamba
damu ya manabii na watakatifu haitarudi mara nyingine kwangu tena dhidi yao.
6 Na tazama, mji wa Gilgali nimeusababisha kuzama na wakazi wake kuzikwa
kwenye kina cha ardhi.
7 Ndio, na mji wa Oniha na wakazi wake, na mji wa Mokumu na wakazi wake, na
mji wa Yerusalemu na wakazi wake; na nimesababisha maji kuja mahali ambapo
walikuwa, kuficha uovu wao na machukizo kutoka mbele ya uso wangu, ili damu ya
manabii na ya watakatifu haitakuja mara nyingine kwangu dhidi yao.
8 Na tazama, mji wa Gadiandi, na mji wa Gadiomna, na mji wa Yakobo, na mji wa
Gimgimno, nimesababisha hiyo yote kuzamishwa, na kubunisha vilima na mabonde
katika mahali pao; na wakazi wake nimewazika kwenye kina cha ardhi, ili kuficha
uovu wao na machukizo kutoka mbele ya uso wangu, kwamba damu ya manabii na
ya watakatifu isije mara nyingine kwangu dhidi yao.
9 Na tazama, ule mji mkuu Yakobugathi, ambao ulikuwa na watu wa Yakobo,
nimesababisha kuchomwa kwa moto kwa sababu ya dhambi zao, na uovu wao,
ambao ulikuwa mwingi kuliko uovu wa dunia nzima, kwa sababu ya wauaji wao wa
siri na mashirika; kwani ni hao ambao waliharibu amani ya watu wangu na serikali
ya nchi; kwa hivyo nilisababisha wachomwe, kuwaangamiza kutoka uso wangu,
kwamba damu ya manabii na ya watakatifu isije kwangu mara nyingine dhidi yao.
10 Na tazama, mji wa Lamani, na mji wa Yoshi, na mji wa Gadi, na mji wa

Kishkumeni, nimesababisha kuchomwa kwa moto, na wakazi wake, kwa sababu ya
uovu wao kwa kuwatupa nje manabii, na kuwapiga kwa mawe wale ambao
niliwatuma kuwatangazia kuhusu uovu wao na machukizo yao.
11 Na kwa sababu waliwatupa wote nje, kwamba hakukuwa na yeyote aliyekuwa wa
haki miongoni mwao, nilituma chini moto na kuwaangamiza, kwamba uovu wao na
machukizo yao yaweze kufichwa kutoka mbele ya uso wangu kwamba damu ya
manabii na ya watakatifu ambao niliwatuma miongoni mwao isilie kwangu kutoka
chini dhidi yao.
12 Na nimesababisha maangamizo mengi juu ya nchi hii, na juu ya hawa watu, kwa
sababu ya uovu wao na machukizo yao.
13 Ee nyinyi nyote ambao mmeachiliwa kwa sababu mlikuwa wenye haki kuliko
hao, je mtarudi kwangu sasa, na kutubu dhambi zenu, na kugeuka ili niwaponye?
14 Ndio, kwa kweli nawaambia, ikiwa mtakuja kwangu, mtapata uzima wa milele.
Tazama, mkono wangu wa rehema umenyoshwa kwenu, na yeyote atakayekuja,
nitampokea; na heri ni wao ambao huja kwangu.
15 Tazama mimi ni Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Niliumba mbingu na dunia, na
vitu vyote vilivyomo. Nilikuwa na Baba kutoka mwanzo. Niko ndani ya Baba na
Baba ndani yangu; na ndani yangu Baba ametukuza jina lake.
16 Nilikuja kwangu na walio wangu hawakunipokea. Na maandiko kuhusu kuja
kwangu yametimizwa.
17 Na vile wengi ambao wamenipokea, kwao nimewapatia kufanyika wana wa
Mungu; na hata hivyo nitawafanya kuwa wengi vile vile wataamini kwa jina langu,
kwani tazama, kupitia kwangu, ukombozi huja, na ndani yangu na kupitia kwangu
sheria ya Musa imetimizwa.
18 Mimi ndimi nuru na uzima wa ulimwengu. Mimi ndimi Alfa na Omega,
mwanzo na mwisho.
19 Na hamtatoa kwangu tena kumwagwa kwa damu; ndio, dhabihu na sadaka zenu
za kuteketezwa zitakomeshwa, kwani sitakubali dhabihu na sadaku zenu zozote za
kuteketezwa.
20 Na mtatoa kwangu dhabihu ya moyo uliopondeka na roho iliyovunjika. Na
yeyote atakayekuja kwangu na moyo uliopondeka na roho iliyovunjika, na huyo
nitambatiza kwa moto na Roho Mtakatifu, hata kwa njia sawa kama Walamani, kwa
sababu ya imani yao kwangu wakati wa kuokoka kwao, walibatizwa kwa moto na
Roho Mtakatifu, na hawakujua.
21 Tazama, nimekuja duniani kuleta ukombozi ili kuokoa dunia kutoka dhambini.
22 Kwa hivyo yeyote anayetubu na kuja kwangu kama mtoto mdogo yeye,
nitampokea, kwani hivyo ndivyo ulivyo ufalme wa Mungu. Tazama, kwa ajili ya
kama hawa, nimetoa maisha yangu, na nimeyachukua tena; kwa hivyo tubu, na mje
kwangu nyinyi nyote mlio duniani na muokolewe.

## 3 Nefi 10

1 Na sasa tazama, ikawa kwamba watu wote nchini walisikia semi hizi, na
walizishuhudia. Na baada ya semi hizi, kulikuwa na unyamavu nchini kwa masaa
mengi;
2 Kwani mshangao wa watu ulikuwa mkubwa sana kwamba wakakoma
kuomboleza na kulilia upotevu wa jamaa zao ambao walikuwa wameuawa; kwa

hivyo kulikuwa na unyamavu katika nchi yote kwa muda wa masaa mengi.
3 Na ikawa kwamba kulitokea sauti tena kwa watu, na watu wote waliisikia, na
wakaishuhudia ikisema:
4 Ee nyinyi watu wa miji mikubwa ambayo imeanguka, ambao ni vizazi vya
Yakobo, ndio, ambao ni wa nyumba ya Israeli, ni mara ngapi nimewakusanya kama
vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake chini ya mbawa, na nimewalisha.
5 Na tena, mara ngapi ningemkusanya kama vile kuku hukusanya vifaranga wake
chini ya mabawa yake, ndio, Ee nyinyi watu wa nyumba ya Israeli, ambao
mmeanguka; ndio, Ee nyinyi watu wa nyumba ya Israeli, nyinyi mnaoishi
Yerusalemu, kama vile wale ambao wameangamizwa; mara ngapi ningekuwa
nimewakusanya kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake chini ya mabawa na
hamnikubalii.
6 Ee nyinyi nyumba ya Israeli ambao nimewahurumia, ni mara ngapi
nitawakusanya kama vile kuku hukusanya vifaranga wake chini ya mabawa yake,
ikiwa mtatubu na kunirudia kwa lengo moja la moyo.
7 Lakini kama sivyo, Ee nyumba ya Israeli, mahali penu pa makao patakuwa tupu
mpaka wakati wa kutimiza agano nililofanya na babu zenu.
8 Na sasa ikawa kwamba baada ya watu kusikia haya maneno, tazama walianza
kulia na kuzomea tena kwa sababu ya vifo vya jamaa zao.
9 Na ikawa kwamba hivyo siku tatu zilipita. Na ilikuwa asubuhi, na giza
likatoweka kutoka uso wa nchi, na ardhi ikakoma kutetemeka, na miamba ikakoma
kupasuka, na kuzomea kwa kutisha kulikoma, na makelele yote ya ghasia yalikoma.
10 Na nchi ilishikamana tena pamoja kwamba ikaimarika; na kuomboleza, na kulia,
na kulia kwa huzuni kwa watu walioachwa wazima kulikoma; na maombolezi yao
yaligeuka kuwa shangwe, na kulia kwao kwa hasira kwa kusifu na kumshukuru
Bwana Yesu Kristo Mkombozi wao.
11 Na hivyo kwa kiwango maandiko yalitimia ambayo yalizungumzwa na manabii.
12 Na ikawa sehemu ya walio haki zaidi ambao waliokolewa, na walikuwa hao
ambao walipokea manabii na hawakuwapiga kwa mawe; na walikuwa hao ambao
hawakumwaga damu ya watakatifu, ambao waliachwa—
13 Na walihurumiwa na hawakuzamishwa na kuzikwa ardhini; na hawakuzamishwa
kwenye kina cha bahari; na hawakuchomwa kwa moto, wala hawakuangukiwa na
kuvunjwa vipande hadi kufa; na hawakubebwa na tufani; wala hawakunyongwa na
mvuke wa moshi na giza.
14 Na sasa yeyote asomaye, acha aelewe; yule ambaye ana maandiko, acha ayapekue,
na aone na kutazama ikiwa hivi vifo na maangamizo kwa moto, na kwa moshi na
kwa dhoruba, na kwa tufani na kwa kufunguliwa kwa ardhi kuwameza, na hivi vitu
vyote havitimizi unabii wa manabii wengi watakatifu.
15 Tazama, ninawaambia, Ndio, wengi wameshuhudia vitu hivi wakati wa kuja kwa
Kristo, na waliuawa kwa sababu walishuhudia vitu hivi.
16 Ndio, nabii Zeno pia alishuhudia vitu hivi, na pia Zenoki alizungumza kuhusu
vitu hivi, kwa sababu vilishuhudia zaidi kutuhusu, ambao ni sazo la uzao wao.
17 Tazama, baba yetu Yakobo pia alishuhudia kuhusu sazo la uzao wa Yusufu. Na
tazama, sisi sio sazo la uzao wa Yusufu? Na hivi vitu ambavyo vinashuhudia juu yao
vimeandikwa kwenye bamba za shaba ambazo babu yetu Lehi alileta kutoka
Yerusalemu?
18 Na ikawa kwamba mwishoni mwa mwaka wa thelathini na nne, tazama,

nitawawonyesha kwamba watu wa Nefi ambao walihurumiwa, na pia wale ambao
waliitwa Walamani, ambao walihurumiwa, upendeleo mwingi ulionyeshwa kwao,
na baraka nyingi zilimwagwa vichwani mwao, mpaka kwamba mara baada ya
kupanda kwa Kristo mbinguni kwa kweli alijidhihirisha kwao—
19 Akiwaonyesha mwili wake, na kuwahudumia; na historia ya huduma yake
itatolewa baadaye. Kwa hivyo kwa wakati huu ninaweka kikomo kwa maneno
yangu.

*Yesu Kristo alijidhihirisha kwa watu wa Nefi, wakati umati ulipokuwa umejikusanya pamoja katika nchi ya Neema, na akawahubiria; na hivi ndivyo alivyojidhihirisha kwao.*

# 3 Nefi 11

1 Na sasa ikawa kwamba kulikuwa na umati mkubwa uliokusanyika pamoja, wa watu
wa Nefi, karibu na hekalu ambalo lilikuwa katika nchi ya Neema; na walistaajabu na
kushangaa mmoja na mwingine, na walionyeshana mabadiliko makubwa na ya ajabu
ambayo yalikuwa yamefanyika.
2 Na walikuwa wanamzungumzia huyu Yesu Kristo, ambaye ishara zilikuwa
zimetolewa kuhusu kifo chake.
3 Na ikawa kwamba wakati walipokuwa huko wakizungumza mmoja na
mwingine, walisikia sauti kama iliyotokea mbinguni; na wakaelekeza macho yao kila
upande, kwani hawakutambua hiyo sauti ambayo walisikia; na haikuwa sauti kali,
wala ya makelele; walakini, na ingawa ilikuwa sauti ndogo tulivu, iliwapenya wale
walioisikia hadi moyoni, mpaka kwamba hakukuweko na sehemu ya miili yao
ambayo haikutetemeka; ndio, iliwatoboa mpaka kwenye roho yenyewe, na
ikasababisha mioyo yao kuchomeka.
4 Na ikawa tena kwamba walisikia ile sauti, na hawakuitambua.
5 Na tena mara ya tatu wakasikia hiyo sauti, na wakafungua masikio yao
kuisikiliza; na macho yao yakaelekea kule kulikotokea sauti; na walitazama kwa
uthabiti kuelekea mbinguni, kule ambako sauti ilitokea.
6 Na tazama, mara ya tatu walielewa ile sauti ambayo walisikia; na ikawaambia:
7 Tazama Mwana wangu Mpendwa ninayependezwa na yeye, ambaye ndani yake
nimetukuza jina langu—msikilizeni yeye.
8 Na ikawa walipofahamu, walielekeza macho yao tena mbinguni; na tazama,
walimwona mtu akiteremka kutoka mbinguni, na alikuwa amevaa joho refu leupe;
na akaja chini na kusimama katikati yao; na macho ya umati wote yaligeuka
kumwangalia, na hawakufungua vinywa vyao, hata mmoja kwa mwingine, na
hawakujua kilichomaanishwa, kwani walidhani ni malaika ambaye alionekana kwao.
9 Na ikawa kwamba alinyosha mkono wake mbele na kuzungumza kwa watu
akisema:
10 Tazama, Mimi ni Yesu Kristo ambaye manabii walishuhudia atakuja ndani ya
ulimwengu.
11 Na tazama mimi ni nuru na uzima wa ulimwengu; na nimekunywa kutoka kwa
kikombe kichungu ambacho Baba amenipatia, na nimemtukuza Bwana kwa
kujivika dhambi za ulimwengu ambamo ndani yake nimevumilia mapenzi ya Baba

katika vitu vyote kutoka mwanzo.
12 Na ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amesema haya maneno, umati wote
uliinama kwenye ardhi; kwani walikumbuka kwamba ilikuwa imetabiriwa miongoni
mwao kwamba Kristo atajidhihirisha kwao baada ya kupaa kwake mbinguni.
13 Na ikawa kwamba Bwana aliwazungumzia akisema:
14 Inukeni na mje kwangu, ili msukume mikono yenu na muitie kwenye ubavu
wangu, na pia kwamba mguse alama za misumari katika mikono yangu na katika
miguu yangu, ili mjue mimi ni Mungu wa Israeli, na Mungu wa ulimwengu wote, na
nimeuawa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu.
15 Na ikawa kwamba umati ulienda mbele, na kusukuma mikono yao ubavuni
mwake, na wakaona alama za misumari katika mikono yake na katika miguu yake;
na hivi walifanya wakienda mbele mmoja mmoja, mpaka walipoenda wote, na
waliona na macho yao na kupapasa kwa mikono yao, na walijua ukweli na
walishuhudia wenyewe kwamba ni yeye, ambaye manabii waliandika kwamba
atakuja.
16 Na wakati walipokuwa wameenda wote na kujishuhudia wenyewe, walipaza sauti
kwa toleo moja wakisema:
17 Hosana! Heri liwe jina la Mungu Aliye Juu Sana! Na waliinama chini miguuni
mwa Yesu na kumwabudu.
18 Na ikawa kwamba alimzungumzia Nefi (kwani Nefi alikuwa miongoni mwa
umati) na kumwamuru kwamba aje mbele.
19 Na Nefi akainuka na kwenda mbele na kusujudu mbele ya Bwana na kubusu
miguu yake.
20 Na Bwana alimwamrisha kwamba ainuke. Na aliinuka na kusimama mbele yake.
21 Na Bwana akamwambia: Ninakupatia uwezo kwamba utabatiza hawa watu
nikiwa nimeenda tena mbinguni.
22 Na tena Bwana aliita wengine, na akawaambia vile vile; na akawapatia uwezo wa
kubatiza. Na akawaambia: Kwa njia hii mtabatiza; na hakutakuwa na ugomvi
miongoni mwenu.
23 Kweli nawaambia, kwamba yeyote atakayetubu dhambi zake kupitia maneno
yenu, na kutaka kubatizwa katika jina langu, kwa njia hii mtawabatiza — Tazama,
mtaenda chini na kusimama majini, na katika jina langu mtawabatiza.
24 Na sasa tazama, haya ndiyo maneno ambayo mtasema, mkiwaita kwa jina,
mkisema:
25 Nikiwa nimepewa mamlaka na Yesu Kristo, ninakubatiza wewe katika jina la
Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.
26 Na hapo mtawatumbukiza katika maji, na kutoka tena nje ya maji.
27 Na kwa kufuata njia hii, mtabatiza katika jina langu; kwani tazama, kweli
nawaambia kwamba, Baba, na Mwana wake, na Roho Mtakatifu wana umoja; na
niko ndani ya Baba, na Baba ndani yangu, na Baba na mimi tuna umoja.
28 Na kulingana na vile nimemwamuru hivyo ndivyo mtabatiza. Na hakutakuwa na
ugomvi miongoni mwenu, kama vile ilivyo hapa sasa; wala hakutakuwa na ugomvi
miongoni mwenu kuhusu nukta za mafundisho yangu, kama vile ilivyokuwa.
29 Kwani amin, amin, nawaambia, yule ambaye ana roho ya ubishi siye wangu,
lakini ni wa ibilisi, ambaye ni baba wa ubishi, na huchochea mioyo ya watu
kubishana na hasira mmoja kwa mwingine.
30 Tazama, hili sio fundisho langu, kuchochea mioyo ya wanadamu kwa hasira,

moja dhidi ya mwingine; lakini hili ndilo fundisho langu, kwamba vitu kama hivi viondolewe mbali.

31 Tazama, amin, amin, ninawaambia, nitatangaza kwenu mafundisho yangu.

32 Na haya ni mafundisho yangu, na ni mafundisho ambayo Baba amenipatia; na ninashuhudia mwenyewe kwa Baba, na Baba anashuhudia mwenyewe kwangu, na Roho Mtakatifu anashuhudia kwa Baba na kwa Mimi, na ninashuhudia kwamba Baba huamuru watu wote, kila mahali, kutubu na kuniamini.

33 Na yeyote aaminiye ndani yangu na kubatizwa, ataokolewa; na hawa ndio watakaorithi ufalme wa Mungu.

34 Na yeyote asiyeamini ndani yangu na hajabatizwa, atahukumiwa.

35 Amin, amin, nawaambia, kwamba, hili ni fundisho langu, na ninashuhudia kutoka kwa Baba; na yeyote anayeamini ndani yangu anaamini kwa Baba pia, na kwake Baba atanishuhudia, kwani atamtembelea na moto na Roho Mtakatifu.

36 Na hivyo ndivyo Baba atakavyoshuhudia kunihusu, na Roho Mtakatifu atashuhudia kwake Baba na Mimi, kwani Baba na Mimi na Roho Mtakatifu tu wamoja.

37 Na tena nawaambia, lazima mtubu na muwe kama mtoto mchanga, na mbatizwe katika jina langu, au hamtapokea vitu hivi kwa njia yoyote.

38 Na tena nawaambia, lazima mtubu na mbatizwe katika jina langu na muwe kama mtoto mchanga au hamtarithi ufalme wa Mungu kwa vyovyote.

39 Amin, amin, nawaambia, kwamba haya ni mafundisho yangu, na yeyote atakayejenga juu ya mwamba wangu, na milango ya jahanamu haitamshinda.

40 Na yeyote atakayetangaza mengi au madogo kuliko haya, na kuyaimarisha kuwa mafundisho yangu, yeye anatokana na uovu, na hajajenga kwenye mwamba wangu; lakini hujenga kwenye msingi wa mchanga, na milango ya jahanamu husimama kupokea mtu kama huyu wakati mafuriko yakija na upepo hujipigisha juu yake.

41 Kwa hivyo muwaendee watu hawa, na mtangaze yale maneno ambayo nimezungumza, hadi mwisho wa dunia.

# 3 Nefi 12

1 Na ikawa kwamba wakati Yesu alikuwa amesema haya maneno kwa Nefi, na kwa wale ambao walipokuwa wameitwa, (sasa idadi ya wale ambao walikuwa wameitwa na kupokea uwezo na mamlaka ya kubatiza, ilikuwa kumi na wawili) na tazama, alinyoosha mkono wake mbele kwa umati, na kuwaambia kwa sauti kubwa akisema: Heri nyinyi ikiwa mtasikiliza maneno ya hawa kumi na wawili ambao nimewachagua kutoka miongoni mwenu kuwahudumia, na kuwa watumishi wenu; na kwao nimewatolea uwezo kwamba wangewabatiza na maji; na baada ya hayo kwamba mmebatizwa na maji, tazama nitawabatiza kwa moto na Roho Mtakatifu; kwa hivyo heri nyinyi ikiwa mtaamini katika mimi na mbatizwe, baada ya kuniona na kujua kwamba ni mimi.

2 Na tena wana heri nyingi wale ambao wataamini kwa haya maneno yenu kwa sababu mtashuhudia kwamba mmeniona, na kwamba mnajua kwamba ni mimi. Ndio, heri kwa wale ambao wataamini katika maneno yenu, na kujileta chini kwenye unyenyekevu na kubatizwa, kwani watatembelewa na moto na Roho Mtakatifu na watasamehewa dhambi zao.

3 Ndio, heri wale walio maskini rohoni, ambao wanakuja kwangu, kwani ufalme

wa mbinguni ni wao.

4 Na tena heri wote walio na huzuni kwani watafarijika.

5 Na heri walio wapole kwani watarithi dunia.

6 Na heri wale wote walio na njaa na kuwa na kiu kwa ajili ya haki, kwani watashibishwa na Roho Mtakatifu.

7 Na heri walio na rehema kwani watapata rehema.

8 Na heri wote walio na moyo mweupe, kwani watamwona Mungu.

9 Na heri wote walio wapatanishi, kwani wataitwa watoto wa Mungu.

10 Na heri wale wote wanaodhulumiwa kwa ajili ya jina langu kwani ufalme wa mbinguni ni wao.

11 Na heri nyinyi, wakati watu watawatukana na kuwadhulumu, na watasema aina yoyote ya uovu dhidi yenu bila ukweli kwa ajili yangu;

12 Kwani mtakuwa na shangwe kubwa na mtakuwa wachangamfu kupita kiasi, kwani thawabu yenu itakuwa kubwa mbinguni; kwani hivyo ndivyo walidhulumu hao manabii ambao walikuweko mbele yenu.

13 Amin, amin, nawaambia, ninawapatia muwe chumvi ya dunia; lakini ikiwa chumvi itapoteza ladha yake, dunia itatiwa chumvi na nini? Chumvi kutokea hapo haitakuwa na uzuri wowote lakini itatupwa na kukanyagwa na miguu ya watu.

14 Amin, amin, ninawaambia, ninawapatia muwe nuru ya watu hawa. Mji uliojengwa kwenye kilima hauwezi kufichwa.

15 Tazama, je, watu huwasha mshumaa na kuuweka chini ya pishi? La, lakini kwenye kinara cha mshumaa na humulika mwanga kwa wote walio ndani ya nyumba;

16 Kwa hivyo acha nuru yenu iangae mbele ya hawa watu, ili wapate kuyaona matendo yenu, na kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni.

17 Msifikirie kwamba nimekuja kuharibu sheria au manabii. Sikuja kuharibu bali kutimiza;

18 Kwani amin ninawaambia, nukta moja wala chembe moja haijaondoka kutoka kwa sheria, lakini ndani yangu yote imetimizwa.

19 Na tazama, nimewapatia sheria na amri za Baba yangu, kwamba mtaamini ndani yangu, na kwamba mtatubu dhambi zenu, na mje kwangu na moyo uliopondeka na roho iliyovunjika. Tazama, mnazo amri mbele yenu, na sheria imetimizwa.

20 Kwa hivyo njooni kwangu na mwokolewe; kwani amin nawaambia kwamba isipokuwa mtii amri zangu ambazo nimewaamuru wakati huu, kwa njia yoyote hamtaingia katika ufalme wa mbinguni.

21 Mmesikia kwamba ilisemekana na wale wa wakati wa kale, na pia imeandikwa mbele yenu, kwamba usiue, na yeyote atakayeua atakuwa hatarini mwa hukumu ya Mungu;

22 Lakini ninawaambia kwamba, yeyote aliye na hasira na ndugu yake atakuwa hatarini ya hukumu yake. Na yeyote atakayesema kwa ndugu yake, Raka, atakuwa hatarini na baraza; na yeyote atakayesema, Wewe mjinga, atakuwa hatarini na moto wa jahanamu.

23 Kwa hivyo ikiwa utakuja kwangu, au utatamani kuja kwangu, na ukumbuke kwamba ndugu yako anacho kitu dhidi yako—

24 Nenda njia yako kwa ndugu yako, na kwanza ondoa tofauti na ndugu yako, na hapo uje kwangu, na moyo wa lengo moja na nitakupokea.

25 Kubaliana na adui yako haraka, wakati uko katika njia moja na yeye, asije akupate

wakati wowote na kukutupa gerezani.
26 Amin, amin, nakwambia hutatoka humo kamwe mpaka utakapolipa senti ya
mwisho. Na wakati ungali upo gerezani unaweza kulipa hata senti moja? Amin,
amin, nakwambia, La.
27 Tazama, imeandikwa na wale wa kale, kwamba usifanye uzinzi.
28 Lakini ninawaambia kwamba, yeyote ambaye anamchungulia mwanamke
kumtamani, huwa tayari amezini moyoni mwake.
29 Tazama, ninakupatia amri ili usikubali vitu hivi kuingia moyoni mwako.
30 Kwani inawafaa kwamba mjizuie wenyewe hivi vitu, ambapo mtajitwika msalaba
wenu, kuliko kwamba mtupwe jahanamu.
31 Imeandikwa kwamba yeyote atakayempatia mke wake talaka, ampe cheti cha
talaka.
32 Amin, amin, nawaambia, kwamba yeyote atakayempatia mke wake talaka,
isipokuwa kwa sababu ya uasherati, humsababisha kutenda uasherati; na yeyote
atakayemwoa yule ambaye amepewa talaka anatenda usherati.
33 Na tena imeandikwa, na wale wa kale kwamba hutaapa uwongo mwenyewe,
lakini utadhihirisha kwa Bwana viapo vyako;
34 Lakini amin, amin ninawaambia, usiape kabisa; wala kwa mbingu, kwani ni kiti
cha enzi cha Mungu;
35 Wala kwa dunia, kwani ndipo mahali pa kuweka miguu yake;
36 Wala hutaapa kwa kichwa chako, kwani huwezi kutengeneza unywele wako
mmoja kuwa mweusi au mweupe;
37 Lakini acha maongezi yenu yawe Ndio, ndio; La, la; kwani chochote kilicho
zaidi ya haya ni ovu.
38 Na tazama, imeandikwa, jicho kwa jicho, na jino kwa jino;
39 Lakini ninawaambia kwamba hamtashindana na uovu, lakini yeyote
atakayekupiga katika shavu la kulia, mgeuzie upande mwingine pia;
40 Na ikiwa mtu yeyote atakushtaki mahakamani na achukue koti lako, mwachie
achukue joho lako pia;
41 Na yeyote atakayekulazimisha kwenda maili moja, nenda na yeye mbili.
42 Mpatie akuombaye, na atakayekukopa kwako usimfukuze.
43 Na tazama, imeandikwa pia na wale wa kale kwamba, utampenda jirani yako na
umchukie adui wako;
44 Lakini tazama ninawaambia, wapendeni maadui zenu, wabariki wanao walaani,
wafanyie mazuri wale ambao wanawachukia, na muwaombee wale ambao
wanawatumia kwa madharau na kuwadhulumu;
45 Ili muwe watoto wa Baba yenu aliye mbinguni; kwani yeye husababisha jua
kung'aa kwa waovu na kwa wenye haki.
46 Kwa hivyo vitu ambavyo vilikuwa vya kale, ambavyo vilikuwa chini ya sheria,
vyote vimetimia.
47 Vitu vya kale vimeachwa na vitu vyote vimekuwa vipya.
48 Kwa hivyo ningependa kwamba mngekuwa wakamilifu hata vile nilivyo, au Baba
yenu ambaye yuko mbinguni ni mkamilifu.

# 3 Nefi 13

1 Amin, amin, nawaambia kwamba toeni sadaka zenu kwa masikini; lakini chungeni kwamba msitoe sadaka zenu mbele ya watu kwa kuonekana nao; la sivyo hamna thawabu ya Baba yenu ambaye yuko mbinguni.
2 Kwa hivyo, wakati mtakapotoa sadaka zenu msivumishe tarumbeta mbele yenu, vile wanafiki hufanya kwenye masinagogi na katika barabara, ili wapate kutukuzwa na watu. Amin nawaambia, wana thawabu yao.
3 Lakini unapotoa sadaka acha mkono wako wa kushoto usijue vile mkono wa kulia unafanya;
4 Ili sadaka zenu ziwe katika siri; na Baba yenu ambaye huona kwa siri, mwenyewe atawalipa wazi.
5 Na wakati mnaomba hamtafanya kama wanafiki wanavyofanya, kwani wanapenda kuomba, wakisimama ndani ya masinagogi na kwenye pembe za barabara, ili waonekane na watu. Amin ninawaambia, wanayo thawabu yao.
6 Lakini wewe, unaposali, ingia kwenye chumba chako kidogo, na wakati umefunga mlango wako, sali kwa Baba yako ambaye yuko mafichoni; na Baba yako, ambaye huona kisiri, atakulipa wazi.
7 Lakini wakati unasali, usitumie marudio ya bure, kama walimwengu, kwani wanadhani kwamba watasikika kwa kutumia maneno mengi.
8 Kwa hivyo usiwe kama hao, kwani Baba yako anajua ni vitu gani unavyohitaji kabla ya wewe kumwuliza.
9 Kwa hivyo msali kwa njia hii: Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe.
10 Mapenzi yako yatimizwe duniani vile yalivyo mbinguni.
11 Na utusamehe deni zetu, kama tunavyowasamehe wadeni wetu.
12 Na usituongoze kwenye majaribu, lakini utuokoe kutoka kwa maovu.
13 Kwani ufalme ni wako, na uwezo, na utukufu, milele. Amina.
14 Kwani, ikiwa mtasamehe watu makosa yao Baba yenu wa mbinguni atawasamehe pia.
15 Lakini kama hamtawasamehe watu makosa yao Baba yenu hatawasamehe makosa yenu.
16 Tena mnapofunga msiwe kama wanafiki, wenye nyuso za kuhuzunika, kwani hukunja nyuso zao ili waonekane wanafunga. Amin ninawaambia, wanayo thawabu yao.
17 Lakini wewe, unapofunga, paka mafuta kwa kichwa chako, na unawe uso wako;
18 Ili usionekane na watu kama unafunga, lakini kwa Baba yako, aliye sirini; na Baba yako, ambaye huona sirini, atakupatia zawadi wazi.
19 Msijiwekee hazina duniani, ambapo nondo na kutu huozesha, na wezi wanavunja na kuiba;
20 Lakini mjiwekee hazina zenu mbinguni, ambapo nondo wala kutu haziozeshi, na ambapo wezi hawawezi kuvunja na kuingia wala kuiba.
21 Kwani mahali ambapo hazina yako ipo, pale pia moyo wako utakuwa.
22 Nuru ya mwili ni jicho; kwa hivyo, ikiwa jicho lako liko moja, mwili wako wote utajaa nuru.
23 Lakini kama jicho lako ni ovu, mwili wako wote utajaa giza. Kwa hivyo, ikiwa nuru iliyopo ndani yako itakuwa giza, sio hio ni giza kuu!
24 Hakuna mtu ambaye anaweza kutumikia mabwana wawili; kwani labda atamchukia mmoja na kumpenda mwingine, au kama sivyo atampenda mmoja na

kumdhulumu mwingine. Huwezi kumtumikia Mungu na Mali.
25 Na sasa ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amezungumza haya maneno alielekeza macho juu ya wale kumi na wawili ambao alikuwa amewachagua, na akawaambia: Kumbukeni maneno ambayo nimezungumza. Kwani tazama, ni nyinyi ambao nimechagua kuwahudumia hawa watu. Kwa hivyo ninawaambia, msisumbukie maisha yenu, ni nini mtakula, au ni nini mtakunywa; wala mtavaa nini, kwenye miili yenu. Je, si maisha yako zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi?
26 Tazama ndege wa angani, kwani hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi kwenye maghala; lakini Baba yenu wa mbinguni huwalisha. Je, si nyinyi ni bora kuliko wewe?
27 Ni nani kati yenu kwa kufikiria anaweza kuongeza mkono mmoja kwa urefu wake?
28 Na kwa nini msumbuke kwa vazi? Fikiria maua ya mwituni vile yanakua; hayataabiki, wala hayasokoti;
29 Na bado ninawaambia, kwamba hata Sulemani, kwa enzi yake yote, hakupambwa kama moja ya hawa.
30 Kwa hivyo, ikiwa Mungu anavika nyasi ya shambani, ambayo ipo leo, na kesho itatupwa kwenye jiko, hata hivyo atakuvisha, ikiwa huna imani ndogo.
31 Kwa hivyo msisumbuke, mkisema, Tutakula nini? au, Tutakunywa nini? au, Tutavaa nini?
32 Kwani Baba yenu wa mbinguni anajua kwamba mna mahitaji ya hivi vitu vyote.
33 Lakini tafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake, na hivi vitu vyote vitaongezwa kwenu.
34 Kwa hivyo msisumbuke kwa kesho, kwani kesho itajishugulisha na vitu vyake yenyewe. Kila siku ina maovu yake ya kutoshana nayo.

# 3 Nefi 14

1 Na sasa ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amezungumza haya maneno aligeuka tena akaelekea umati, na kufungua kinywa chake kwao, na kusema: Kweli, kweli, ninawaambia, Msihukumu, kwamba msije mkahukumiwa.
2 Kwani kwa hukumu mnayo hukumia, mtahukumiwa nayo; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakapopimiwa tena.
3 Na mbona wakitazama kibanzi ambacho kiko ndani ya jicho la ndugu yako, lakini hufikirii kiboriti ambacho kiko kwenye jicho lako?
4 Au utasemaje kwa ndugu yako: Acha nitoe kibanzi ndani ya jicho lako — na tazama, kiboriti kiko ndani ya jicho lako?
5 Wewe mnafiki, kwanza ondoa kiboriti kutoka kwenye jicho lako; na ndipo utaona vema kukitoa kibanzi kutoka ndani ya jicho la ndugu yako.
6 Msitoe kile kilicho kitakatifu kwa mbwa, wala msitupe lulu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, na kugeuka tena na kuwararua.
7 Ombeni, na mtapewa; tafuteni na mtapata, bisheni, na mtafunguliwa.
8 Kwani kila mmoja ambaye huuliza, hupata; na yule anayetafuta, huvumbua; na yule ambaye hubisha, hufunguliwa.
9 Au kuna mtu gani kwenu, ambaye, ikiwa mwana wake anamwomba mkate, atampatia jiwe?

10 Au kama anamwomba samaki, atampatia nyoka?
11 Ikiwa nyinyi, mkiwa waovu, mnajua kuwapatia watoto wenu zawadi nzuri, je, ni
vipi Baba yenu aliye mbinguni atawapa vitu vizuri wale ambao humwomba?
12 Kwa hivyo, vitu vyote ambavyo mngetaka kwamba watu wawafanyie, wafanyie
pia wengine, kwani hii ni sheria na manabii.
13 Ingieni kwa kupitia mlango mwembamba; kwani mlango ni wazi, na pana ndiyo
njia iongozayo kwenye uharibifu, na waiendayo ni wengi;
14 Kwa sababu mlango umesonga, na njia ni nyembamba, iendayo uzimani, nao
waipatao ni wachache.
15 Jihadharini na manabii wa uwongo, ambao huwajia wakiwa wamevaa mavazi ya
kondoo, lakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali.
16 Mtawatambua kwa matunda yao. Je, watu huchuma zabibu katika miiba, au tini
katika mibaruti?
17 Hata hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; lakini mti mwovu huzaa
matunda mabaya.
18 Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya wala mti mbaya kuzaa matunda
mema.
19 Kila mti ambao hauzai matunda mazuri hukatwa, na kutupwa motoni.
20 Kwa hivyo, kwa matunda yao mtawajua.
21 Sio kila anayesema kwangu, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa
mbinguni; lakini yule anayefanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.
22 Wengi watasema kwangu siku ile: Bwana, Bwana, si tulifanya unabii kwa jina
lako, na kwa jina lako si tumetoa pepo chafu, na katika jina lako kufanya miujiza
mingi?
23 Na ndipo nitawaambia dhahiri: Sikuwajua nyinyi kamwe; ondokeni kwangu,
nyinyi mtendao maovu.
24 Kwa hivyo, yeyote asikiaye haya maneno yangu na kuyafanya, nitamfananisha na
mtu mwenye hekima, ambaye alijenga nyumba yake juu ya mwamba—
25 Na mvua ilinyesha, na mafuriko yakaja, na pepo zikavuma, na zikapiga ile
nyumba; na haikuanguka, kwani iliwekwa kwenye mwamba.
26 Na yeyote asikiaye haya maneno yangu na hayafanyi atalinganishwa na mtu
mpumbavu aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga—
27 Na mvua ilinyesha, na mafuriko yakaja, na pepo zikavuma, na zikaipiga ile
nyumba; na ilianguka, na mwanguko wake ulikuwa mkubwa.

## 3 Nefi 15

1 Na sasa ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amemaliza haya maneno alizungusha
macho yake karibu hapo kwa umati, na akawaambia: Tazameni, mmesikia vitu
ambavyo nilifundisha kabla ya kupaa juu kwa Baba yangu; kwa hivyo, yeyote
akumbukaye haya maneno yangu na kuyafanya, yeye nitamwinua juu katika siku ya
mwisho.
2 Na ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amesema haya maneno aliona kwamba
kulikuwa na wengine miongoni mwao ambao walistaajabu, na kushangaa kile
alichotaka kufanya na sheria ya Musa; kwani hawakuelewa msemo uliosema kwamba
vitu vya kale vilikuwa vimepita, na kwamba vitu vyote vilikuwa vimekuwa vipya.
3 Na akawaambia: Msistaajabu kwamba nilisema vitu vya kale vilikuwa vimepita,

na kwamba vyote vilikuwa vimekuwa vipya.
4 Tazama, ninawaambia kwamba sheria imetimizwa ambayo alipewa Musa.
5 Tazama, ni mimi niliyempa ile sheria, na ni mimi niliyeagana na watu wangu
Israeli; kwa hivyo, sheria imetimizwa ndani yangu, kwani nimekuja kutimiza sheria;
kwa hivyo imefika mwisho.
6 Tazama, siharibu maandishi ya manabii, kwani kadiri mengi ambayo
hayajatimizwa ndani yangu, kweli nawaambia, yote yatatimizwa.
7 Na kwa sababu niliwaambia kwamba vitu vya kale vimepita, siharibu ile ambayo
imezungumzwa kuhusu vitu ambavyo vinakuja.
8 Kwani tazama, agano ambalo nimefanya na watu wangu lote halijatimizwa;
lakini sheria ambayo ilipewa Musa imemalizika kwa sababu yangu.
9 Tazama, mimi ndiye sheria, na nuru. Nitazameni mimi, na mvumilie hadi
mwisho, na mtaishi; kwani kwa yule ambaye huvumilia hadi mwisho nitampatia
uzima wa milele.
10 Tazama, nimewapatia amri; kwa hivyo tiini amri zangu. Na hii ni sheria na
maandishi ya manabii, kwani walinishuhudia kwa ukweli.
11 Na sasa ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amezungumza haya maneno,
aliwaambia wale kumi na wawili ambao alikuwa amewachagua:
12 Nyinyi ni wanafunzi wangu; na nyinyi ni nuru kwa hawa watu, ambao ni sazo la
nyumba ya Yusufu.
13 Na tazama, hii ni nchi ya urithi wenu; na Baba amewapatia.
14 Na kamwe hakuna wakati wowote ambao Baba amenipatia amri kwamba
niwaambie ndugu zenu katika Yerusalemu.
15 Wala katika muda wowote Baba hajanipa amri kwamba niwaambie kuhusu
makabila mengine ya nyumba ya Israeli, ambao Baba amewaongoza mbali kutoka
nje ya nchi.
16 Hiki kiasi Baba aliniamuru, kwamba ningewaambia:
17 Kwamba kondoo wengine ninao ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa
kuwaleta, na watasikia sauti yangu; na kutakuwa na kundi moja, na mchungaji
mmoja.
18 Na sasa, kwa sababu ya shingo ngumu na kutoamini, hawakuelewa maneno
yangu; kwa hivyo, niliamrishwa na Baba nisiwaambie zaidi kuhusu kitu hiki.
19 Lakini kweli, nawaambia kwamba Baba ameniamuru, na nawaambia kwamba
mlitenganishwa kutoka miongoni mwao kwa sababu ya uovu wao; kwa hivyo ni
sababu ya uovu wao kwamba hawajui chochote kuwahusu.
20 Na kweli, nawaambia tena kwamba makabila mengine yametengwa na Baba
kutoka kwao; na ni kwa sababu ya uovu wao kwamba hawajui chochote kuwahusu.
21 Na kweli nawaambia, kwamba ni nyinyi ambao nilisema: Kondoo wengine
ninao ambao sio wa zizi hili; hao nao ninapaswa kuwaleta, na watasikia sauti yangu;
na kutakuwa na kundi moja, na mchungaji mmoja.
22 Na hawakunielewa, kwani walidhani kwamba nilizungumza kuhusu Wayunani;
kwani hawakuelewa kwamba Wayunani watageuka kupitia mahubiri yao.
23 Na hawakunielewa kwamba nilisema wataelewa sauti yangu; na hawakunielewa
kwamba Wayunani hawataisikia sauti yangu wakati wowote — kwamba
sitajidhihirisha kwao isipokuwa kupitia kwa Roho Mtakatifu.
24 Lakini tazama, nyote mmesikia sauti yangu, na kuniona; na nyinyi ni kondoo
wangu, na mmehesabiwa miongoni mwa wale ambao Baba amenipatia.

# 3 Nefi 16

1 Na kweli, kweli, nawaambia kwamba ninao kondoo wengine, ambao si wa nchi hii,
wala ya Yerusalemu, wala mahali popote katika nchi ya karibu niliyotoa huduma.
2 Kwani wale ambao ninawazungumzia ni wale ambao bado hawajasikia sauti
yangu; wala sijajidhihirisha kwao.
3 Lakini nimepokea amri kutoka kwa Baba kwamba niwaendee, na kwamba
watasikia sauti yangu, na watahesabiwa miongoni mwa kondoo wangu, ili kuwe na
kundi moja na mchungaji mmoja; kwa hivyo nitaenda kujidhihirisha kwao.
4 Na ninawaamuru kwamba mtaandika maneno haya baada ya mimi kuondoka, ili
ikiwa watu wangu katika Yerusalemu, hao ambao wameniona na kuwa na mimi
katika huduma yangu, hawamwulizi Baba katika jina langu, kwamba
wangeelemishwa kuwahusu kupitia Roho Mtakatifu, na pia kuhusu makabila
mengine ambayo hawajui, kwamba haya maneno ambayo mtaandika yatahifadhiwa
na yatadhihirishwa kwa Wayunani, ili kupitia utimilifu wa Wayunani, sazo la uzao
wao, ambao utatawanyishwa kila mahali kwa uso wa dunia kwa sababu ya kutoamini
kwao, wangeletwa ndani, au wangeletwa kujua kunihusu mimi, Mkombozi wao.
5 Na ndipo nitawakusanya kutoka sehemu nne za ulimwengu; na ndipo nitatimiza
agano ambalo Baba amefanya kwa watu wote wa nyumba ya Israeli.
6 Na heri Wayunani, kwa sababu ya imani yao kwangu, imani ambayo inatokana na
Roho Mtakatifu, ambaye anashuhudia kwao juu yangu na juu ya Baba.
7 Tazama, kwa sababu ya imani yao kwangu, Baba asema, na kwa sababu ya
kutoamini kwenu, Ee nyumba ya Israeli, katika siku ya mwisho, ukweli utawajia
Wayunani, kwamba utimilifu wa hivi vitu utajulikana kwao.
8 Lakini ole, asema Baba, kwa wale Wayunani wasioamini — kwani hata ingawa
wamefika juu ya nchi hii, na wamewatawanya watu wangu ambao ni wa nyumba ya
Israeli; na watu wangu ambao ni wa nyumba ya Israeli wametupwa nje kutoka
miongoni mwao, na wamekanyangwa chini ya miguu na hao;
9 Na kwa sababu ya rehema za Baba kwa Wayunani, na pia hukumu za Baba juu ya
watu wangu ambao ni wa nyumba ya Israeli, kweli, kweli, nawaambia, kwamba
baada ya haya yote, na nimesababisha watu wangu ambao ni wa nyumba ya Israeli
kuuawa, na kuteswa, na kuchinjwa, na kutupwa nje kutoka miongoni mwao, na
kuchukiwa nao, na kuwa wa kufyonya na mithali miongoni mwao —
10 Na hivyo Baba anaamuru kwamba inanibidi niseme kwenu: Katika siku ile
wakati Wayunani watafanya dhambi dhidi ya injili yangu, na watakataa utimilifu wa
injili yangu, na watainuliwa juu katika kiburi cha mioyo yao juu ya mataifa yote, na
juu ya watu wote wa dunia, na wajazwe na kila aina ya udanganyifu, na uwongo, na
madhara, na aina yote ya unafiki, na mauaji, na ukuhani wa uongo, na ukahaba, na
machukizo ya siri; na ikiwa watafanya vitu vile vyote, na wakatae utimilifu wa injili
yangu, tazama, Baba anasema, nitachukua utimilifu wa injili yangu kutoka
miongoni mwao.
11 Na ndipo nitakumbuka agano ambalo nimefanya kwa watu wangu, Ee nyumba
ya Israeli, na nitaleta injili yangu kwao.
12 Na nitawaonyesha, Ee nyumba ya Israeli, kwamba Wayunani hawatakuwa na
uwezo juu yenu; lakini nitakumbuka agano langu na nyinyi, Ee nyumba ya Israeli, na
mtakuja kuwa na ufahamu wa utimilifu wa injili yangu.
13 Lakini ikiwa Wayunani watatubu, na kunirudia, asema Baba, tazama
watahesabika miongoni mwa watu wangu, Ee nyumba ya Israeli.

14 Na sitakubali watu wangu, ambao ni wa nyumba ya Israeli, kupitia miongoni
mwao, na kuwakanyaga chini, anasema Baba.
15 Lakini kama hawatageuka kwangu, na kusikiliza sauti yangu, nitawakubalia,
ndio, nitakubali watu wangu, Ee nyumba ya Israeli, kwamba watapita miongoni
mwao, na watawakanyaga chini, na watakuwa kama chumvi ambayo imepoteza
ladha yake, ambayo kutoka hapo haiwi nzuri kwa chochote lakini ni ya kutupwa nje,
na kukanyagwa na miguu ya watu wangu, Ee nyumba ya Israeli.
16 Kweli, kweli, ninawaambia, hivi ndivyo Baba ameniamuru — kwamba niwape
hawa watu hii nchi kwa urithi wao.
17 Na ndipo maneno ya nabii Isaya yatatimizwa, ambayo yanasema:
18 Walinzi wenu watapaza sauti; na pamoja na sauti wataimba, kwani wataonana
macho kwa macho wakati Bwana atakaporejesha tena Sayuni.
19 Pigeni kelele za shangwe, imbeni pamoja, enyi mahali pa Yerusalemu palipokuwa
ukiwa; kwani Bwana amewafariji watu wake, ameikomboa Yerusalemu.
20 Bwana ameweka wazi mkono wake mtakatifu machoni mwa mataifa yote; na
nchi zote za dunia zitaona wokovu wa Mungu.

# 3 Nefi 17

1 Tazama, sasa ikawa kwamba baada ya Yesu kuzungumza haya maneno alitazama
tena kwa umati, na akasema kwao: Tazama, muda wangu umewadia.
2 Ninahisi kwamba nyinyi ni wadhaifu, kwamba hamwezi kufahamu maneno
yangu yote ambayo nimeamrishwa na Baba kuwazungumzia wakati huu.
3 Kwa hivyo, nendeni nyumbani kwenu, na mfikirie vitu ambavyo nimesema, na
mwulize kutoka kwa Baba, katika jina langu, ili muweze kufahamu, na kutayarisha
akili zenu kwa kesho, na nitakuja kwenu tena.
4 Lakini sasa ninaenda kwa Baba, na pia kujidhihirisha kwa makabila yaliyopotea
ya Israeli, kwani hawajapotea kwa Baba, kwani anajua mahali ambapo aliwapeleka.
5 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kusema hivyo, alielekeza macho yake tena kwa
umati, na akaona kuwa wanalia, na walikuwa wanamwangalia kwa uthabiti kama
wanaotaka kumwomba akae nao kwa muda mrefu zaidi.
6 Na akawaambia: Tazama, matumbo yangu yamejawa na huruma juu yenu.
7 Mnao wowote ambao ni wagonjwa miongoni mwenu? Waleteni hapa. Mnao
wowote ambao ni viwete, au vipofu, au wa kupooza, au vilema, au ukoma, au
walionyauka au ni viziwi, au ambao wanateseka kwa njia yoyote? Waleteni hapa na
nitawaponya, kwani ninayo huruma juu yenu; matumbo yangu yamejaa na huruma.
8 Kwani ninaona kwamba mnataka kwamba niwaonyeshe kile ambacho nilifanya
kwa ndugu zenu wa Yerusalemu, kwani naona kwamba imani yenu ni ya kutosha
kwamba ningewaponya.
9 Na ikawa kwamba wakati alipokuwa amesema hivyo, umati wote, kwa lengo
moja, ulisonga mbele na wagonjwa wao na wote wao waliosumbuka, na vilema wao,
na vipofu wao, na bubu wao, na wote waliosumbuka kwa jinsi yoyote; na
akawaponya kila mmoja vile walileletwa kwake.
10 Na wote, wote ambao walikuwa wameponywa, na wale ambao walikuwa wazima,
waliinama chini miguuni mwake, na kumwabudu; na kadiri wengi walivyoweza
walikuja kutoka miongoni mwa umati walibusu miguu yake, mpaka kwamba
waliosha miguu yake na machozi yao.

11 Na ikawa kwamba aliamuru kwamba watoto wao wachanga waletwe.
12 Kwa hivyo walileta watoto wao wachanga na kuwapanga chini juu ya ardhi
kumzunguka, na Yesu alisimama katikati; na umati ulitoa nafasi mpaka wote
walipoletwa kwake.
13 Na ikawa kwamba baada ya wote kuletwa, na Yesu kusimama katikati, aliamuru
umati kwamba wapige magoti chini.
14 Na ikawa kwamba baada ya hao kupiga magoti chini, Yesu alisononeka moyoni
mwake, na kusema: Baba, ninasumbuliwa kwa sababu ya uovu wa nyumba ya Israeli.
15 Na baada ya kusema haya maneno, yeye mwenyewe pia alipiga magoti ardhini; na
tazama aliomba kwa Baba, na vitu ambavyo aliomba haviwezi kuandikwa, na umati
uliomsikiliza ulishuhudia.
16 Na kwa maneno haya walishuhudia: Jicho halijaona, wala sikio kusikia, hapo
mbeleni, vitu vikubwa na vya ajabu vile tuliona na kusikia Yesu akisema kwa Baba;
17 Na hakuna ulimi unaoweza kusema, wala haiwezi kuandikwa na mtu yeyote, wala
mioyo ya watu haiwezi kufikiria vitu vikubwa na vya ajabu kama tulivyoona na
kusikia Yesu akisema; na hakuna yeyote ambaye anaweza kuona shangwe iliyojaza
nafsi zetu wakati tulipomsikia akituombea kwa Baba.
18 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kumaliza kuomba kwa Baba, aliinuka; lakini
umati ulikuwa na shangwe iliyokuwa kubwa sana kwamba walishindwa.
19 Na ikawa kwamba Yesu aliwazungumzia, na kuwaambia wasimame.
20 Na waliinuka kutoka ardhini, na akawaambia: Heri kwenu kwa sababu ya imani
yenu. Na sasa tazama, shangwe yangu imetimia.
21 Na baada ya kusema haya maneno, alilia, na umati ulishuhudia hii, na akachukua
watoto wao wachanga, mmoja mmoja, na kuwabariki, na kuomba kwa Baba juu yao.
22 Na baada ya kufanya hivi alilia tena;
23 Na alizungumza kwa umati, na kuwaambia: Tazama wachanga wenu.
24 Na walipotazama kuona walielekeza macho yao mbinguni, na wakaona mbingu
zikifunguka, na wakaona malaika wakiteremka kutoka mbinguni kama wakiwa
katikati ya moto; na walikuja chini na kuzunguka wale wachanga, na walizungukwa
na moto; na malaika waliwahudumia.
25 Na umati uliona na kusikia na wanashuhudia; na wanajua kwamba maandishi
yao ni ya kweli kwani wote waliona na kusikia, kila mtu binafsi; na idadi yao ilikuwa
karibu watu elfu mbili na mia tano; na walikuwa wanaume, wanawake, na watoto.

## 3 Nefi 18

1 Na ikawa kwamba Yesu aliamuru wanafunzi kwamba walete mkate na divai kwake.
2 Na walipokuwa wameenda kuleta mkate na divai, aliamuru umati kwamba ukae
ardhini.
3 Na baada ya wanafunzi kurejea na mkate na divai, alichukua mkate na kuumega
kwa vipande na kuutakasa; na akawapatia wanafunzi na kuwaamuru kwamba wale.
4 Na baada ya kula na kushiba, aliwaamuru kwamba watoe kwa umati.
5 Na baada ya umati kula na kushiba, aliwaambia wanafunzi: Tazama kutakuwa na
mmoja atakayetawazwa miongoni mwenu, na kwake nitatolea uwezo kwamba
atamega mkate na kuubariki na kuwapatia watu wa kanisa langu, kwa wote ambao
wataamini na kubatizwa katika jina langu.
6 Na hii mtakumbuka kufanya daima, hata vile nimefanya, hata vile nimemega

mkate na kuubariki na kuwapatia.
7 Na hii mtafanya kwa ukumbusho wa mwili wangu, ambao nimewaonyesha. Na
itakuwa ushuhuda kwa Baba kwamba daima mnanikumbuka. Na ikiwa
mtanikumbuka daima Roho yangu itakuwa na nyinyi.
8 Na ikawa kwamba baada ya kusema haya maneno, aliwaamuru wanafunzi wake
kwamba wachukue divai ndani ya kikombe na wainywe, na kwamba wawapatie
umati ili wanywe.
9 Na ikawa kwamba walifanya hivyo, na wakainywa na kushiba; na kuupatia umati,
na wakanywa, na wakashiba.
10 Na baada ya wanafunzi kufanya hivyo, Yesu aliwaambia: Mna heri kwa hiki kitu
ambacho mmefanya, kwani hii ni kutimiza amri zangu, na hii inashuhudia kwa Baba
kwamba mko tayari kufanya yale ambayo nimewaamuru.
11 Na daima mtafanya hivi kwa wale wanaotubu na kubatizwa katika jina langu; na
mtafanya hivi kwa ukumbusho wa damu yangu, ambayo nilimwaga kwa ajili yenu, ili
mshuhudie kwa Baba kwamba daima mnanikumbuka. Na ikiwa mnanikumbuka
daima Roho yangu itukuwa na nyinyi.
12 Na ninawapatia amri kwamba mtafanya hivi vitu. Na ikiwa mtafanya hivi vitu
daima mna baraka, kwani mmejengwa juu ya mwamba wangu.
13 Lakini yeyote miongoni mwenu ambaye atafanya zaidi au ndogo kuliko haya
hajajengwa juu ya mwamba wangu, lakini wamejengwa kwenye msingi wa mchanga;
na wakati mvua inateremka, na mafuriko kuja, na pepo kuvuma, na kujipigisha juu
yao, wataanguka, na milango ya jahanamu iko tayari kuwapokea.
14 Kwa hivyo mnabaraka nyinyi kama mtatii amri zangu, ambazo Baba ameniamuru
kwamba nitoe kwenu.
15 Kweli, kweli, ninawaambia, lazima mjihadhari na kuomba siku zote, msije
mkajaribiwa na ibilisi, na mwongozwe mbali kama mateka wake.
16 Na kama vile nimeomba miongoni mwenu, basi nanyi muombe hivyo katika
kanisa langu, miongoni mwa watu wangu wanaotubu na kubatizwa katika jina
langu. Tazama, mimi ndimi nuru; nimewapatia mfano.
17 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kuzungumza haya maneno kwa wanafunzi
wake, aliugeukia tena umati na kuwaambia:
18 Tazama, kweli, kweli, nawaambia: lazima mjihadhari na kusali siku zote, msije
mkaingia majaribuni; kwani Shetani amewataka nyinyi, ili apate kuwapepeta kama
vile ngano.
19 Kwa hivyo lazima msali siku zote kwa Baba katika jina langu;
20 Na chochote mtakachomwomba Baba katika jina langu, ambacho ni haki,
mkiamini kwamba mtapata, tazama, kitapewa kwenu.
21 Ombeni katika ukoo wenu kwa Baba, daima katika jina langu, kwamba wake
zenu na watoto wenu wabarikiwe.
22 Na tazama mtakutana pamoja mara kwa mara; na hamtamzuia mtu yeyote kuja
kwenu wakati mnakutana pamoja, lakini wakubalie kwamba waje kwenu na
msiwazuie;
23 Lakini mtawaombea, na hamtawatupa nje; na ikiwa kwamba watakuja kwenu
mara kwa mara, mtawaombea kwa Baba, katika jina langu.
24 Kwa hivyo, inueni juu nuru yenu kwamba iangae juu ya dunia. Tazama mimi ni
mwangaza ambao mtainua—kwamba mfanye yale ambayo mmeniona nikifanya.
Tazama mnaona kwamba nimeomba kwa Baba, na nyote mmeshuhudia.

25 Na mnaona kwamba nimeamuru kwamba yeyote miongoni mwenu asiende,
lakini nimeamuru kwamba mje kwangu, kwamba mngenipapasa na kuniona; hata
hivyo mtafanya kwa ulimwengu; na yeyote anayeasi hii amri anakubali mwenyewe
kuongozwa majaribuni.
26 Na sasa ikawa kwamba baada ya Yesu kusema haya maneno, aligeuza macho yake
tena kuwaelekea wanafunzi ambao alikuwa amewachagua, na kuwaambia:
27 Tazameni kweli, kweli, ninawaambia, ninawapa amri ingine, na ndipo niteanda
kwa Baba yangu ili nitimize amri zingine ambazo amenipatia.
28 Na sasa tazama, hii ndiyo amri ninayowapatia, kwamba msikubali yeyote kuonja
mwili wangu na damu bila kustahili, wakati mtahudumu;
29 Kwani yeyote alaye na anywaye mwili wangu na damu asipostahili hula na
kunywa lawama kwa nafsi yake; kwa hivyo kama mnajua kwamba mtu hastahili kula
na kunywa mwili wangu na damu, mtamzuia.
30 Walakini, hamtamtupa nje kutoka miongoni mwenu, lakini mtamhudumia na
mtamwombea kwa Baba, katika jina langu; na ikiwa kwamba atatubu na kubatizwa
katika jina langu, ndipo mtampokea, na mtamhudumia mwili wangu na damu
yangu.
31 Lakini asipotubu hatahesabiwa miongoni mwa watu wangu, ili asiharibu watu
wangu, kwani tazama najua kondoo wangu, na wamehesabiwa.
32 Walakini, hamtamtupa nje ya masinagogi yenu, au mahali penu pa kuabudu,
kwani kwa hawa mtaendelea kuwahudumia; kwani hamjui lakini watarudi na
kutubu, na kuja kwangu kwa moyo wa lengo moja, na nitawaponya; na ndipo
mtakuwa njia ya kuwaletea wokovu.
33 Kwa hivyo, tii haya maneno ambayo nimewaamuru kwamba msije mkawa chini
ya hukumu; kwani ole kwa yule ambaye Baba anamhukumu.
34 Na ninawapatia hizi amri kwa sababu ya ugomvi ambao umekuwa miongoni
mwenu. Na heri nyinyi kama hamna ugomvi miongoni mwenu.
35 Na sasa nitaenda kwa Baba, kwa sababu ni muhimu kwamba niende kwa Baba
kwa ajili yenu.
36 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kumaliza maneno haya, aliwagusa wanafunzi
ambao alikuwa amewachagua kwa mkono wake mmoja mmoja mpaka alipowagusa
wote, na aliwazungumzia akiwagusa.
37 Na umati haukusikia maneno ambayo alisema, kwa hivyo hawakushuhudia;
lakini wanafunzi wanashuhudia kwamba aliwapatia uwezo kutoa Roho Mtakatifu.
Na nitawaonyesha baadaye kwamba huu ushahidi ni wa kweli.
38 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kuwagusa wote, kulitokea wingu na likafunika
umati kwamba haungemwona Yesu.
39 Na wakati walipokuwa wamefunikwa aliondoka kutoka kwao, na kupaa
mbinguni. Na wanafunzi waliona na wanashudia kwamba alipaa tena mbinguni.

# 3 Nefi 19

1 Na sasa ikawa kwamba baada ya Yesu kupaa mbinguni, umati ulitawanyika, na kila
mtu alimchukua mke wake na watoto wake na kurejea kwa nyumba yake.
2 Na uvumi ulienda nje miongoni mwa watu mara moja, kabla ya giza kushika,
kwamba ule umati ulikuwa umemwona Yesu, na kwamba alikuwa amewahudumia,
na kwamba pia atajidhihirisha kwao kesho.

3 Ndio, na hata usiku kucha ukavumishwa kuhusu Yesu; na kwa ukamilifu mwingi walisambaza kwa watu kwamba kulikuwa na wengi, ndio, idadi kubwa sana ilitembea sana usiku, ili wawe mahali ambapo Yesu atajionyesha mwenyewe kwa umati.

4 Na ikawa kwamba kesho yake baada ya umati kukusanyika pamoja, tazama Nefi na kaka yake ambaye alikuwa amefufuliwa kutoka kwa wafu, ambaye jina lilikuwa Timotheo, na pia mwana wake ambaye jina lake lilikuwa Yona, na pia Mathoni, na Mathoniha, kaka yake, na Kumeni, na Kumenonhi, na Yeremia, na Shemnoni, na Yona, na Zedekia, na Isaya — Sasa haya yalikuwa majina ya wanafunzi ambao Yesu alikuwa amewachagua — na ikawa kwamba walienda mbele na kusimama katikati ya umati.

5 Na tazama, umati ulikuwa mkubwa sana kwamba walisababisha kwamba wagawanywe kwenye vikundi kumi na viwili.

6 Na wale kumi na wawili walifundisha umati; na tazama, walisababisha kwamba umati upige magoti chini juu ya ardhi, na waombe kwa Baba katika jina la Yesu.

7 Na wanafunzi pia waliomba kwa Baba pia katika jina la Yesu. Na ikawa kwamba waliinuka na kuwahudumia watu.

8 Na baada ya kufundisha maneno yale yale ambayo Yesu alizungumza — bila tofauti yoyote na yale Yesu aliyazungumza — tazama, walipiga magoti tena na kuomba kwa Baba katika jina la Yesu.

9 Na waliomba wapate kile ambacho walitaka zaidi; na walitaka kwamba Roho Mtakatifu apewe kwao.

10 Na baada ya kuomba hivyo, walienda chini kwenye ukingo wa maji, na umati ukawafuata.

11 Na ikawa kwamba Nefi alienda chini ndani ya maji na akabatizwa.

12 Na alitoka nje kutoka ndani ya maji na kuanza kubatiza. Na alibatiza wale wote ambao Yesu aliwachagua.

13 Na ikawa baada ya wote kubatizwa na kutoka nje ya maji, Roho Mtakatifu aliteremka kwao, na walijazwa na Roho Mtakatifu na moto.

14 Na tazama, walionekana kama waliozingirwa na moto; na ulikuja chini kutoka mbinguni, na umati ulishuhudia, na kutoa ushahidi; na malaika walikuja chini kutoka mbinguni na kuwahudumia.

15 Na ikawa kwamba malaika walipokuwa wanawahudumia wanafunzi, tazama, Yesu alikuja na kusimama miongoni mwao na kuwahudumia.

16 Na ikawa kwamba alizungumza kwa umati, na kuwaamuru kwamba wapige magoti chini ardhini tena, na pia kwamba wanafunzi wake wapige magoti chini ardhini.

17 Na ikawa kwamba walipopiga magoti chini, aliwaamuru wafuasi wake waombe.

18 Na tazama, walianza kuomba; na waliomba kwa Yesu, wakimwita Bwana wao na Mungu wao.

19 Na ikawa kwamba Yesu alitembea kutoka miongoni mwao, na kuenda pembeni kidogo kutoka kwao na kujiinamisha mwenyewe na kusema:

20 Baba, ninakushukuru kwamba umewapatia hawa watu ambao nimewachagua Roho Mtakatifu; na ni kwa sababu ya imani yao kwangu, kwamba nimewachagua kutoka miongoni mwa watu wa dunia.

21 Baba, nakuomba kwamba utawapatia Roho Mtakatifu wote ambao wataamini kwa maneno yao.

22 Baba, umewapatia Roho Mtakatifu kwa sababu wanaamini ndani yangu; na
unaona kwamba wanaamini kwangu kwa sababu unawasikia, na wanaomba
kwangu; na wanaomba kwangu kwa sababu niko nao.
23 Na sasa Baba, ninaomba kwako kwa ajili yao, na pia wale wote ambao wataamini
maneno yao, kwamba wangeamini ndani yangu, kwamba niwe ndani yao vile uko,
Baba, ndani yangu, ili tuwe kitu kimoja.
24 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kuomba hivyo kwa Baba, aliwajia wanafunzi
wake, na tazama, walikuwa bado wanaendelea, bila kukoma, kuomba kwake; na
hawakuzidisha maneno, kwani walipewa yale ambayo wangeomba, na utashi
uliwajaa.
25 Na ikawa kwamba Yesu aliwabariki wakati walipokuwa wanaomba kwake;
alikunjua uso kwao, na nuru ya uso wake iling'aa kwao, na tazama, walikuwa weupe
kama uso na pia nguo ya Yesu; na tazama, weupe wake ulizidi weupe wote, ndio,
hata hakungekuwa na kitu duniani cheupe kama weupe wake.
26 Na Yesu akasema kwao: Endeleeni kuomba; walakini, hawakukoma kuomba.
27 Na akageuka kutoka kwao tena, na akaenda kando kidogo na akainama
mwenyewe ardhini; na akaomba tena kwa Baba, akisema:
28 Baba, ninakushukuru kwamba umewatakasa wale ambao nimewachagua, kwa
sababu ya imani yao, na ninawaombea, na pia wale ambao wataamini kwa yale
wanayosema, ili watakaswe kupitia kwangu, kwa imani katika maneno yao, kama
vile wanatakaswa ndani yangu.
29 Baba siombei dunia, lakini wale ambao umenipatia kutoka dunia, kwa sababu ya
imani yao, kwamba wangetakaswa kupitia kwangu, kwamba niwe ndani yao vile
wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, ili tuwe kitu kimoja, kwamba nipate kutukuzwa
ndani yao.
30 Na baada ya Yesu kusema haya maneno, alirudi tena kwa wanafunzi wake; na
tazama waliomba kwa uthabiti, bila kukoma, kwake; na akakunjua uso kwao tena;
na tazama, walikuwa weupe, hata kama Yesu.
31 Na ikawa kwamba alienda tena kando kidogo na kuomba kwa Baba;
32 Na ulimi hauwezi kusema yale maneno ambayo aliomba wala hayawezi
kuandikwa na mwanadamu maneno ambayo aliomba.
33 Na umati ulisikia na walitoa ushuhuda; na mioyo yao ilifunguka na walisikia
katika mioyo yao, maneno ambayo aliomba.
34 Walakini, maneno aliyoyatumia kwa kuomba yalikuwa makubwa sana na ya
ajabu, kwamba hayawezi kuandikwa, wala kuongelewa na mtu.
35 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kumaliza kuomba alirudi tena kwa wanafunzi,
na kuwaambia: Sijaona imani kubwa kama hii miongoni mwa Wayahudi; kwa
hivyo, sikuonyesha miujiza mikubwa kwa sababu ya kutoamini kwao.
36 Kweli, ninawaambia, hakuna mmoja wao ambaye ameona vitu vikubwa sana
kama vile nyinyi wala hawajasikia vitu vikubwa kama vile mmesikia.

## 3 Nefi 20

1 Na ikawa kwamba aliamuru umati kwamba wakome kusali na pia wanafunzi wake.
Na akawaamuru kwamba wasikome kusali kwenye mioyo yao.
2 Na akawaamuru kwamba wainuke na wasimame kwa miguu yao. Na waliinuka
na kusimama kwa miguu yao.

3 Na ikawa kwamba alimega mkate tena na kuubariki, na kuwapa wanafunzi waule.
4 Na baada ya wao kula, aliwaamuru wamege mkate na kuwapatia umati.
5 Na baada ya wao kuwapatia umati, aliwapa divai pia kunywa na kuwaamuru
kuwapatia umati.
6 Sasa hakukuweko na mkate wala divai iliyoletwa na wanafunzi, wala na umati.
7 Lakini kwa kweli aliwapatia mkate wale, na pia divai wanywe.
8 Na akawaambia: Yule ambaye anaula huu mkate anakula mwili wangu kwa nafsi
yake; na yule ainywaye hii divai, anakunywa damu yangu kwa nafsi yake; na nafsi
yake haitaona njaa wala kiu, lakini itajazwa.
9 Sasa baada ya umati kunywa na kula, tazama, walijazwa na Roho; na walipiga
yowe kwa sauti moja, na kumtukuza Yesu, ambaye walimwona na kumsikiza.
10 Na ikawa kwamba wakati wote walikuwa wamemtukuza Yesu, aliwaambia:
Tazama sasa ninamaliza amri ambayo Baba aliniamuru kuhusu watu hawa, ambao ni
sazo la nyumba ya Israeli.
11 Mnakumbuka kwamba niliwazungumzia, na kusema kwamba wakati maneno ya
Isaya yangetimizwa — tazama, yameandikwa, mnayo mbele yenu, kwa hivyo
myachunguze —
12 Na kweli, kweli, ninasema kwenu; kwamba wakati yatakavyotimizwa ndipo
kutatimizwa agano ambalo Baba alifanya na watu wake Ee nyumba ya Israeli.
13 Na ndipo masazo ambayo yatatawanywa juu ya dunia, yatakusanywa ndani
kutoka mashariki na kutoka magharibi, na kutoka kusini na kutoka kaskazini; na
wataletwa kwa ufahamu wa Bwana Mungu wao, ambaye amewakomboa.
14 Na Baba ameniamuru kwamba niwapatie hii nchi kwa urithi wenu.
15 Na ninawaambia kwamba kama Wayunani hawatatubu baada ya baraka ambazo
watapata, baada ya wao kutawanya watu wangu —
16 Ndipo nyinyi ambao ni sazo la nyumba ya Yakobo, mtaenda miongoni mwao; na
mtakuwa miongoni mwao ambao ni wengi; na mtakuwa miongoni mwao kama
simba miongoni mwa wanyama wa msitu, na kama mwana simba miongoni mwa
makundi ya kondoo, ambaye, ikiwa atapitia miongoni mwao atawakanyagia chini na
kuwararua katika vipande vipande na hakuna atakayewaokoa.
17 Mikono yenu itainuliwa dhidi ya maadui wenu, na maadui wenu wote
watakatiliwa mbali.
18 Na nitakusanya watu wangu vile mtu hukusanya miganda sakafuni.
19 Kwani nitachagua watu wangu ambao Baba amefanya agano nao, ndio, nifanye
pembe yako kuwa chuma, na kwato zako kuwa shaba. Na utaponda kwenye vipande
vipande watu wengi; na nitaweka wakfu faida yako kwa Bwana, na mali zao kwa
Bwana wa dunia yote. Na tazama mimi ndimi, nitaifanya.
20 Na itakuwa, asema Baba, kwamba upanga wa haki yangu utaning'inia juu yao
siku ile; na wasipotubu, itawaangukia, anasema Baba, ndio, hata kwa mataifa yote ya
Wayunani.
21 Na itakuwa kwamba nitaimarisha watu wangu, Ee nyumba ya Israeli.
22 Na tazama, hawa watu nitawaimarisha katika nchi hii, kwa kutimiza agano
ambalo nilifanya na babu yenu Yakobo; na itakuwa Yerusalemu mpya. Na uwezo wa
mbinguni utakuwa katikati ya hawa watu; ndio, hata mimi nitakuwa katikati yenu.
23 Tazama, ni mimi ambaye Musa alimzungumzia akisema: Bwana Mungu wenu
atainua nabii huyo kutoka miongoni mwa ndugu zenu kama mimi; yeye ndiye
mtamsikiliza kwa vitu vyote atakavyowaambia. Na itakuwa kwamba kila nafsi

ambayo haitamsikiliza nabii itakatiwa mbali kutoka miongoni mwa watu.
24 Kweli, nawaambia, ndio, na manabii wote kutokea Samweli na wale ambao
wanafuata baadaye, kadiri vile wengi wamezungumza, wamenishuhudia.
25 Na tazama, nyinyi ni watoto wa manabii; na nyinyi ni wa nyumba ya Israeli; na ni
wa agano ambalo Baba alifanya na babu zenu akisema kwa Ibrahimu: Na kupitia
uzao wako, makabila yote ya dunia yatabarikiwa.
26 Baba alinitayarisha mimi kwanza, na kunituma niwabariki nyinyi kwa kugeuza
kila mmoja wenu kutoka kwa uovu wake; na hivyo ni kwa sababu nyinyi ni watoto
wa agano—
27 Na baada ya hivyo mlibarikiwa ndipo kutimiza agano ambalo Baba alifanya na
Ibrahimu, akisema: Katika uzao wako, jamaa yote ya dunia itabarikiwa—kwa njia
ya kumwaga nje Roho Mtakatifu kupitia kwangu juu ya Wayunani, baraka ambazo
kwa Wayunani, zitawafanya kuwa na nguvu kuliko wote, kwa kutawanya watu
wangu, Ee nyumba ya Israeli.
28 Na watakuwa mjeledi kwa watu wa nchi hii. Walakini, baada ya hao kupata
utimilifu wa injili yangu, hapo ikiwa watashupaza mioyo yao dhidi yangu,
nitarudishia uovu wao juu ya vichwa vyao, anasema Baba.
29 Na nitakumbuka agano ambalo nimefanya na watu wangu; na nimeagana nao
kwamba nitawakusanya pamoja, katika wakati wangu mwenyewe, kwamba
ningewapa tena nchi ya babu zao kwa urithi, ambayo ni nchi ya Yerusalemu, ambayo
ni nchi ya ahadi kwao milele, anasema Baba.
30 Na itakuwa kwamba wakati utakuja ambapo utimilifu wa injili yangu
utahubiriwa kwao;
31 Na wataamini ndani yangu, kwamba mimi ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, na
kuomba kwa Baba katika jina langu.
32 Ndipo walinzi wao watapaza sauti zao, na kwa sauti, pamoja wataimba; kwani
wataonana jicho kwa jicho.
33 Ndipo Baba atawakusanya pamoja tena na kuwapatia Yerusalemu kuwa nchi ya
urithi wao.
34 Ndipo watapiga kelele za shangwe—Imbeni pamoja enyi mahali pa Yerusalemu
palipo na ukiwa; kwani Baba amefariji watu wake, na ameikomboa Yerusalemu.
35 Baba amefanya mkono wake mtakatifu wazi katika macho ya mataifa yote; na
nchi zote za dunia zitauona wokovu wa Baba; na Baba na Mimi tu wamoja.
36 Na ndipo itakuja kutimia ile ambayo iliandikwa: Amka, amka tena, na jivike
nguvu yako, Ee Sayuni; jivike mavazi yako mazuri, Ee Yerusalemu, mji mtakatifu,
kwani kutokea sasa hawataingia ndani yako, wasiotahiriwa na wasio safi.
37 Jikung'ute mavumbi; inuka uketi chini, Ee Yerusalemu, jifungulie kandaza za
shingo, Ee binti mfungwa wa Sayuni.
38 Kwani Bwana anasema hivi; Mmejiuza bure, na mtakombolewa bila fedha.
39 Kweli, kweli, nawaambia, kwamba watu wangu watajua jina langu; ndio, katika
siku hiyo watajua kwamba ni mimi ndiye husema.
40 Na hapo watasema: Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima, miguu yake, aletaye habari
njema kwao, yeye atangazaye amani; aletaye habari njema ya mambo mema kwao,
yeye atangazaye wokovu, aiambiaye Sayuni: Mungu wako anatawala!
41 Na hapo mlio utatokea: Nendeni nyinyi, nendeni nyinyi, tokeni hapo, msiguse
kile ambacho ni kichafu; tokeni kati yake, muwe safi nyinyi mnaochukua vyombo
vya Bwana.

42 Kwani hamtatoka kwa haraka wala hamtakwenda kwa kukimbia; kwa sababu Bwana atawatangulia, na Mungu wa Israeli atakuwa nyuma yenu kuwalinda.

43 Tazama mtumishi wangu atatenda kwa busara; atatukuzwa na kuinuliwa juu, na kuwa juu sana.

44 Na vile wengi walikustaajabia—uso wake ulikuwa uliharibiwa sana zaidi ya mtu yeyote, na umbo lake zaidi ya wana wa watu—

45 Ndivyo atakavyowanyunyizia mataifa mengi; wafalme watamfungia vinywa vyao, kwani maneno ambayo hawakuambiwa watayaona; na yale ambayo hawakusikia watayafahamu.

46 Kweli, kweli, ninawaambia, hivi vitu vyote vitafanyika, hata vile Baba ameniamrisha. Ndipo hili agano ambalo Baba ameagana na watu wake litatimizwa; na hapo Yerusalemu itakaliwa tena na watu wangu, na itakuwa nchi yao ya urithi.

## 3 Nefi 21

1 Na kweli, ninawaambia, ninawapatia ishara ili mjue muda ambao vitu hivi vitakuwa karibu kufanyika—kwamba nitawakusanya ndani, baada ya kutawanyika kwa muda mrefu, watu wangu, Ee nyumba ya Israeli, na nitaanzisha tena miongoni mwao Sayuni yangu.

2 Na tazama, hiki ndicho kitu ambacho nitawapatia kwa ishara—kwa kweli, ninawaambia kwamba wakati hivi vitu ambavyo nimetangaza kwenu, na ambavyo nitawatangazia baadaye mwenyewe, na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu ambaye atatolewa kwenu na Baba, vitafanywa kujulikana kwa Wayunani ili wajue kuhusu hawa watu ambao ni sazo la nyumba ya Yakobo, na kuhusu hawa watu wangu ambao watatenganishwa na hao;

3 Kweli, kweli, ninawaambia, baada ya hivi vitu kujulikana kwao, kutoka kwa Baba, na vitatokea kutoka kwa Baba kupitia kwao hadi kwenu.

4 Kwani ni hekima katika Baba kwamba waimarishwe katika nchi hii, na wapangwe kama watu huru kwa uwezo wa Baba, kwamba hivi vitu vingekuja mbele kutoka kwao hadi kwa sazo la uzao wenu, kwamba agano la Baba lingetimizwa ambalo ameagana na watu wake, Ee nyumba ya Israeli.

5 Kwa hivyo, baada ya vitu hivi na vitu ambavyo vitafanywa miongoni mwenu baada ya muda huu vitakuja kutoka kwa Wayunani, hadi kwa uzao wenu ambao utafifia katika kutoamini kwa sababu ya uovu;

6 Kwa hivyo ndivyo Baba amepanga kwamba ije kutokea kwa Wayunani, kwamba angeonyesha mbele uwezo wake kwa Wayunani, kwa sababu hii kwamba Wayunani kama hawatashupaza mioyo yao, kwamba watubu na waje kwangu na wabatizwe katika jina langu na wajue habari kamili ya mafundisho yangu, ili wahesabiwe miongoni mwa watu wangu, Ee nyumba ya Israeli.

7 Na wakati vitu hivi vitakapokuja kutimizwa, kwamba uzao wenu utaanza kujua vitu hivi—itakuwa ishara kwao, ili wajue kwamba kazi ya Baba imeanza kitambo kwa kutimizwa kwa agano ambalo amefanya kwa watu ambao ni wa nyumba ya Israeli.

8 Na wakati hiyo siku itakapofika, itakuwa kwamba wafalme watafunga vinywa vyao; kwani yale ambayo hawajaambiwa watayaona; na yale ambayo hawajasikia watayafikiria.

9 Kwani katika siku hiyo, kwa ajili yangu, Baba atafanya kazi ambayo itakuwa

kubwa na kazi ya ajabu miongoni mwao; na kutakuwa miongoni mwao wale ambao
hawataiamini ingawa mtu atawatangazia.
10 Lakini tazama maisha ya mtumishi wangu yatakuwa mkononi mwangu; kwa
hivyo, hawatamdhuru, ingawa ataumizwa kwa sababu yao. Bado nitamponya, kwani
nitawaonyesha kwamba hekima yangu inazidi werevu wa ibilisi.
11 Kwa hivyo itakuwa kwamba yeyote ambaye hataamini katika maneno yangu,
mimi ambaye ni Yesu Kristo, ambaye Baba atamsababisha yeye kuleta mbele kwa
Wayunani, na atampatia uwezo kwamba atayaleta mbele kwa Wayunani, (itafanyika
hata kama Musa alivyosema) watatolewa kutoka kwa watu wangu ambao ni wa
agano.
12 Na watu wangu ambao ni sazo la Yakobo watakuwa miongoni mwa Wayunani,
ndio, miongoni mwao kama simba miongoni mwa wanyama wa msituni, kama
mwana simba miongoni mwa makundi ya kondoo, ambaye akiwa anapita katikati,
hukanyagakanyaga na kuraruararua, kwa vipande vipande, na hakuna wa kuokoa.
13 Mkono wao utainuliwa juu ya maadui zao, na maadui wao wote watakatiliwa
mbali.
14 Ndio, ole kwa Wayunani isipokuwa watubu; kwani itakuwa kwamba katika siku
hiyo, asema Baba, kwamba nitatilia mbali farasi wenu, kutoka kati yenu, na
nitaharibu magari yenu ya vita;
15 Na nitakatilia mbali miji ya nchi yenu, na nitaangusha ngome zenu zote;
16 Na nitakatilia mbali uchawi nje ya nchi yenu, na hamtakuwa tena na wapiga
ramli;
17 Nitaziharibu sanamu zenu, na nguzo zenu za ibada, na hamtaabudu tena kazi ya
mikono yenu;
18 Na nitaving'oa vijisitu vyenu visiwe kati yenu; hivyo nitaangamiza miji yenu.
19 Na itakuwa kwamba uwongo wote na udanganyifu, na wivu, na mashindano, na
ukuhani wa uongo, na ukahaba utaondelewa.
20 Kwani itakuwa, anasema Baba, kwamba katika siku ile, wote ambao hawatatubu
na kuja kwa Mwana wangu Mpendwa, hao nitawakatilia mbali kutoka miongoni
mwa watu wangu, Ee nyumba ya Israeli.
21 Na nitamaliza ghadhabu yangu kali na kisasi juu yao, hata kama kwa wale wasio
na dini, ile mbaya ambayo hawajasikia.
22 Lakini ikiwa watatubu na kutii maneno yangu, na wasishupaze mioyo yao,
nitaimarisha kanisa langu miongoni mwao, na wataingia kwenye agano na
kuhesabiwa miongoni mwa hili sazo la Yakobo, kwa hao ambao nimepeana nchi hii
kwa urithi wao.
23 Na watawasaidia watu wangu, lile sazo la Yakobo, na pia wengi wa nyumba ya
Israeli kama watakuja ili waweze kujenga mji, ambao utaitwa Yerusalemu Mpya.
24 Na ndipo watasaidia watu wangu ili wakusanywe ndani, ambao wametawanyika
kote juu ya nchi, ndani ya Yerusalemu Mpya.
25 Na ndipo uwezo wa mbinguni utakuja chini miongoni mwao; na pia nitakuwa
katikati.
26 Na ndipo kazi ya Baba itaanza katika siku ile, hata wakati ambapo injili
itahubiriwa miongoni mwa sazo la watu hawa. Kweli, nawaambia, katika siku ile,
ndipo kazi ya Baba itaanza miongoni mwa watu wangu waliotawanywa, ndio, hata
makabila ambayo yamepotea, ambayo Baba ameyaongozea mbali kutoka nje ya
Yerusalemu.

27 Ndio, kazi itaanza miongoni mwa wale wote wa watu wangu waliotawanywa,
Baba akiwapo kutayarisha njia ambayo kwayo wangekuja kwangu, ili wamuite katika
jina langu.
28 Ndio, ndipo kazi itakapoanza, na Baba miongoni mwa mataifa yote katika
kutayarisha njia ambayo kwayo watu wake wangekusanywa nyumbani katika nchi
yao ya urithi.
29 Na wataenda nje kutoka kwa mataifa yote; na hawataenda nje kwa haraka, wala
kwenda kwa woga, kwani nitaenda mbele yao, asema Baba, na nitakuwa wao wa
nyuma.

# 3 Nefi 22

1 Na ndipo ile ambayo imeandikwa itatimizwa: Imba, ewe tasa; wewe usiyepata
kujifungua mtoto; anza kuimba na ulie kwa sauti, wewe ambaye hukujifungua
mtoto; kwani wengi ni watoto wa tasa, kuliko watoto wa mke aliyeolewa, asema
Bwana.
2 Panua mahali pa hema lako, na acha watandaze mapazia ya maskani yako; tumia
nafasi yote, ongeza urefu wa kamba zako, na vikaze vigingi vyako;
3 Kwani utaenea kwenye upande wa kulia na kwenye upande wa kushoto na uzao
wako utawamiliki Wayunani na kufanya miji ya ukiwa kumilikiwa.
4 Usiogope, kwani hutaaibika; wala kuteketezwa, kwani hutawekwa aibu; kwani
utasahau aibu ya ujana wako, na hutakumbuka aibu ya ujana wako, na hutaweza
kukumbuka mashtumu ya ujane wako tena.
5 Kwani muumba wako, mume wako, Bwana wa Majeshi ndilo jina lake; na
Mkombozi wako, Mtakatifu wa Israeli—ataitwa Mungu wa dunia yote.
6 Kwani Bwana amekuita kama mke aliyeachwa na kuhuzunishwa rohoni, na mke
wa ujana, wakati ulikataliwa, asema Mungu wako.
7 Kwa muda midogo nimekuacha, lakini kwa rehema nyingi nitakurejesha.
8 Kwa ghadhabu ndogo, nilificha uso wangu kutoka kwako kwa muda mfupi,
lakini kwa wema usio na mwisho nitakuwa na huruma kwako, asema Bwana
Mkombozi wako.
9 Kwani jambo hili limekuwa kama maji ya Nuhu kwangu, kwani vile nilivyoapa
kwamba maji ya Nuhu hayatafunika dunia tena, kadhalika nimeapa kwamba
sitakuwa na hasira nawe.
10 Kwani milima itaondoka, na vilima vitaondelewa, lakini wema wangu
hautaondoka kutoka kwako, wala agano langu la amani liondolewe, asema Bwana
ambaye ana rehema nawe.
11 Ee uliyeteseka, uliyerushwa na tufani, bila kutulizwa! Tazama, nitaweka mawe
yako na rangi nzuri, na kuweka msingi wako na johari ya thamani.
12 Na nitafanya madirisha yako ya akiki, na milango yako ya kito nyekundu, na
mipaka yako yote ya mawe yapendezayo.
13 Na watoto wako wote watafundishwa na Bwana; na amani ya watoto wako
itakuwa kubwa.
14 Utathibitika katika haki; utakuwa mbali na kuonewa, kwani hutaogopa, na
mbali na hofu, kwani haitakuja karibu nawe.
15 Tazama, yamkini watakusanyika pamoja dhidi yako, sio kwa shauri langu; wote
watakaokusanyika pamoja dhidi yako wataanguka kwa ajili yako.

16 Tazama, nimemuumba mhunzi afukutaye moto wa makaa, na ambaye huleta
chombo kwa kazi yake; na nimemuumba mharibifu kuangamiza.
17 Hakuna silaha yoyote itakayotengenezwa dhidi yako ambayo itafaulu; na kila
ulimi ambao utatukana dhidi yako, utahukumu. Huu ndio urithi wa watumishi wa
Bwana, na haki yao inatoka kwangu, asema Bwana.

## 3 Nefi 23

1 Na sasa, tazama, nawaambia kwamba mnapaswa kupekua vitu hivi. Ndio,
ninawapatia amri kwamba mpekue hivi vitu kwa bidii; kwani maneno ya Isaya ni
makuu.
2 Kwani alizungumza akitaja vitu vyote kuhusu watu wangu ambao ni wa nyumba
ya Israeli; kwa hivyo ni muhimu kwake kwamba lazima awazungumzie Wayunani
pia.
3 Na vitu vyote ambavyo alizungumza vimekuwa na vitakuwa, hata kulingana na
maneno ambayo alisema.
4 Kwa hivyo sikilizeni maneno yangu; andikeni vitu ambavyo niliwaambia; na
kulingana na muda na mapenzi ya Baba, vitawaendea Wayunani.
5 Na yeyote atakayetii maneno yangu na kutubu na kubatizwa, yule
atakombolewa. Pekua manabii, kwani wengi wameshuhudia hivi vitu.
6 Na sasa ikawa kwamba baada ya Yesu kusema haya maneno, aliwaambia tena,
baada ya kuwaelezea maandiko ambayo walikuwa wamepokea, aliwaambia: Tazama,
maandiko mengine ningetaka muandike ambayo hamjaandika.
7 Na ikawa kwamba alimwambia Nefi: Leta hapa maandishi ambayo umeweka.
8 Na baada ya Nefi kumletea hayo maandishi, na kuyaweka mbele yake, alielekeza
macho yake kwayo na kusema:
9 Kweli, nawaambia, nilimwamuru mtumishi wangu Samweli, yule Mlamani,
kwamba ashuhudie hawa watu, kwamba katika siku ambayo Baba atatukuza jina lake
ndani yangu kwamba kulikuwa watakatifu wengi ambao wangeinuka kutoka kwa
wafu, na kuonekana na wengi, na kuwahudumia. Na akawaambia: Si ilikuwa hivyo?
10 Na wanafunzi wake walimjibu na kusema: Ndio, Bwana, Samweli alitabiri
kulingana na maneno yako, na yote yalitimizwa.
11 Na Yesu akawaambia: Imekuwaje kwamba hamjaandika kitu hiki, kwamba
watakatifu wengi walifufuka na kuonekana na wengi na kuwahudumia?
12 Na ikawa kwamba Nefi alikumbuka kwamba hiki kitu hakikuwa kimeandikwa.
13 Na ikawa kwamba Yesu aliamuru kwamba iandikwe; kwa hivyo iliandikwa vile
alivyoamuru.
14 Na sasa ikawa kwamba baada ya Yesu kueleza maandiko yote pamoja, ambayo
waliandika, aliwaamuru kwamba wafundishe vitu ambavyo alikuwa amewaeleza.

## 3 Nefi 24

1 Na ikawa kwamba aliwaamuru kwamba waandike maneno ambayo Baba
alimkabidhi Malaki, ambayo angewaambia. Na ikawa kwamba baada ya kuandikwa,
aliyaeleza. Na haya ndiyo maneno aliyowaambia akisema: Baba alimwambia Malaki
hivi—Tazama, nitamtuma mjumbe wangu, na atatayarisha njia kabla yangu, na

Bwana mnayemgojea atakuja kwa ghafla kwenye hekalu lake, hata yule mjumbe wa agano ambaye mnafurahia ndani; tazama atakuja, asema Bwana wa Majeshi.
2 Lakini ni nani atakayestahili siku ya kuja kwake, na ni nani atakayesimama
atakapotokea? Kwani yeye yuko kama moto usafishao fedha, na kama sabuni ya dobi.
3 Na ataketi kama asafishaye fedha na kuitakasa, na atawatakasa wana wa Lawi,
atawasafisha kama dhahabu na fedha, ili dhabihu kwa Bwana liwe toleo kwa haki.
4 Ndipo dhabihu ya Yuda na Yerusalemu zitapendeza mbele ya Bwana, kama
katika siku za kale, na kama katika miaka ya zamani.
5 Na nitawakaribia kwa hukumu; na nitakuwa shahidi mwepesi dhidi ya wachawi,
na dhidi ya wazinzi, na dhidi ya waapao uwongo, na dhidi ya wale wamwoneao mwenye kuajiriwa kwa ajili ya mshahara wake, mjane na yatima, na wale wanaompoteza mgeni, na hawaniogopi, asema Bwana wa Majeshi.
6 Kwa kuwa mimi ni Bwana, sibadiliki; kwa hivyo enyi wana wa Yakobo
hamwangamizwi.
7 Hata kutoka siku za babu zenu, mmegeuka upande kutoka kwa maagizo yangu,
na hamjayashika. Nirudieni na nitarudi kwenu, asema Bwana wa Majeshi. Lakini nyinyi mwasema: Tutarudi kwa namna gani?
8 Je, mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini mmeniibia. Lakini mnasema:
Tumekuibia kwa namna gani? Katika zaka na madhabihu.
9 Mmelaaniwa na laana, kwani mmeniibia, hata hili taifa lote.
10 Leteni zaka kamili ghalani, ili kuweko chakula katika nyumba yangu; na
mnijaribu sasa hivi, asema Bwana wa Majeshi, kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagia baraka, kwamba kusiwe na nafasi ya kutosha ya kuipokea.
11 Na nitamkemea mlaji kwa ajili yenu, na hataharibu matunda ya ardhi yenu; wala
mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake katika ardhi kabla ya wakati wake huko shambani, asema Bwana wa Majeshi.
12 Na mataifa yote yatawaita heri, kwani mtakuwa nchi ya kupendeza, asema Bwana
wa Majeshi.
13 Maneno yenu yamekuwa magumu juu yangu, asema Bwana. Lakini mnasema:
Tumesema nini dhidi yako?
14 Mmesema ni bure kumtumikia Mungu, na tumepata faida gani kwa kuzishika
ibada zake, na kwamba tumetembea kwa huzuni mbele ya Bwana wa Majeshi.
15 Na sasa tunawaita wenye kiburi ndiyo walio heri; ndio, wale wanaotenda maovu
na kunufaika; ndio, wanaomjaribu Mungu ndio wanaookolewa.
16 Ndipo wale wanaomcha Bwana, walisemezana wao kwa wao, na Bwana
akasikiliza na kusikia; na kitabu cha ukumbusho kikaandikwa mbele yake kwa wao wanaomcha Bwana, na kulitafakari jina lake.
17 Na watakuwa wangu, asema Bwana wa Majeshi, katika siku ile nitakapofanya
vito vyangu; na nitawaachilia vile mtu huachilia mwana wake amtumikiaye.
18 Ndipo mtakaporudi, na kupambanua miongoni mwa wenye haki na waovu, na
miongoni mwa yule amtumikiaye Mungu na yule asiyemtumikia.

## 3 Nefi 25

1 Kwani tazama, ile siku inakuja ambayo itawaka kama tanuu; na wote wenye kiburi,
ndio, na wote wanaotenda maovu, watakuwa makapi; na ile siku inayokuja
itawateketeza, asema Bwana wa Majeshi, kwamba haitawaachia shina wala tawi.
2 Lakini kwenu mnaolicha jina langu, yule Mwana wa Haki atawashukia na
uponyaji katika mabawa yake; na nyinyi mtaenda mbele na kukua kama ndama
zizini.
3 Na mtakanyaga waovu; kwani watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu
katika siku nitakayofanya hivi, asema Bwana wa Majeshi.
4 Kumbukeni nyinyi sheria ya Musa, mtumishi wangu, niliyemwamuru huko
Horebu kwa ajili ya Waisraeli wote, na amri za hukumu.
5 Tazama, nitawatumia Eliya nabii kabla ya kuja kwa ile siku kubwa na ya kutisha
ya Bwana.
6 Na atageuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na mioyo ya watoto iwaelekee baba
zao, nisije na kupiga dunia na laana.

## 3 Nefi 26

1 Na sasa ikawa kwamba baada ya Yesu kuwaambia hivi vitu, na alivieleza kwa umati;
na alieleza vitu vyote kwao, vyote vikuu na vidogo.
2 Na alisema: Haya maandiko ambayo hamkuwa nayo, Baba aliamuru kwamba
niwapatie; kwani ilikuwa hekima kwake kwamba yatolewe kwa vizazi vijavyo.
3 Na alieleza vitu vyote, hata kutoka mwanzo mpaka wakati ambao angekuja
katika utukufu wake—ndio, hata vitu vyote ambavyo vingekuja juu ya uso wa
dunia, hata mpaka vitu vya asili vitakapoyeyuka kwa joto lenye nguvu sana, na dunia
itakunjamana pamoja kama karatasi, na mbingu na dunia vitakwisha;
4 Na hata kwenye ile siku kuu, wakati watu wote, na makabila yote, na mataifa
yote, na ndimi watasimama mbele ya Mungu, kuhukumiwa kwa vitendo vyao, kama
ni vizuri au ni viovu—
5 Ikiwa ni vizuri, kwa ufufuo wa uzima usio na mwisho; na vikiwa viovu, kwa
ufufuko wa laana; vikiwa sambamba, moja kwa mkono mmoja na ingine kwa
mkono mwingine, kulingana na hekima, na haki, na utukufu ulio ndani ya Kristo,
ambaye alikuweko kabla ya ulimwengu kuanza.
6 Na sasa hakuwezi kuandikwa kwenye kitabu hiki hata sehemu moja kwa mia ya
vitu ambavyo Yesu aliwafundisha watu kwa ukweli;
7 Lakini tazama, bamba za Nefi zinayo sehemu kubwa ya vitu ambavyo
aliwafundisha watu.
8 Na hivi vitu nimeandika, ambavyo ni sehemu ndogo ya vitu ambavyo
aliwafundisha watu; na nimeviandika kwa kusudi kwamba vingeletwa tena kwa
watu hawa, kutoka kwa Wayunani, kulingana na maneno ambayo Yesu ameongea.
9 Na wakati watakapokuwa wamepokea hii, ambayo ni muhimu kwamba wapate
kwanza, kujaribu imani yao, na ikiwa itakuwa hivyo kwamba wataamini vitu hivi,
ndipo vitu vikubwa zaidi vitadhihirishwa kwao.
10 Na ikiwa itakuwa hivyo kwamba hawataamini vitu hivi, ndipo vile vikubwa zaidi
vitazuiliwa kwao kusababisha lawama kwao.
11 Tazama, nilikuwa karibu kuyaandika, yote ambayo yalikuwa yamechorwa kwenye

bamba za Nefi, lakini Bwana akakataza akisema: Nitajaribu imani ya watu wangu.

12 Kwa hivyo mimi, Mormoni, naandika vitu ambavyo nimeamriwa na Bwana. Na sasa mimi, Mormoni, nafikia mwisho wa kusema kwangu, na ninaendelea kuandika vitu ambavyo nimeamriwa.

13 Kwa hivyo, ningetaka kwamba muelewe kwamba Bwana kweli aliwafundisha watu, kwa muda wa siku tatu; na baada ya hapo alijidhihirisha kwao mara kwa mara, na alimega mkate mara kwa mara na kuubariki na kuwapatia.

14 Na ikawa kwamba aliwafundisha na kuwahudumia watoto wa umati ambao umezungumziwa, na aliwapatia uwezo wa kuongea, na waliwazungumzia baba zao vitu vikubwa na vya ajabu, hata vikubwa kuliko alivyokuwa amewatambulia watu; na alifungua ndimi zao kwamba wangezungumza.

15 Na ikawa kwamba baada ya kupaa mbinguni—baada ya mara ya pili kwamba alijidhihirisha mwenyewe kwao, na alikuwa ameenda kwa Baba, baada ya kuponya wagonjwa wao wote, na vipofu wao, na kufungua masikio ya viziwi, na baada ya kufanya aina yote ya kuponya miongoni mwao, na kufufua mtu kutoka kwa wafu, na alikuwa ameonyesha uwezo wake kwao, na alikuwa amepaa juu kwa Baba—

16 Tazama, ikawa kesho yake kwamba umati ulikusanyika pamoja, na waliona na kusikia watoto hawa; ndio, hata watoto wachanga walifungua vinywa vyao, na kuongea vitu vya kustaajabisha; na vitu ambavyo waliongea vilikatazwa kwamba kusiwe na mtu yeyote wa kuviandika.

17 Na ikawa kwamba wanafunzi ambao Yesu alikuwa amewachagua walianza kutokea wakati huo kubatiza na kufundisha wengi jinsi walivyokuja kwao; na vile wengi walibatizwa katika jina la Yesu, walijazwa na Roho Mtakatifu.

18 Na wengi wao waliona na kusikia vitu visivyosemekana ambavyo havikubaliwi kuandikwa.

19 Na walifundishanana kuhudumiana; na walikuwa na vitu vyote sawasawa miongoni mwao, kila mtu akifanya haki mmoja kwa mwingine.

20 Na ikawa kwamba walifanya vitu vyote hata kama vile Yesu alivyowaamuru.

21 Na wale ambao walibatizwa katika jina la Yesu waliitwa kanisa la Kristo.

# 3 Nefi 27

1 Na ikawa kwamba vile wanafunzi wa Yesu walipokuwa wakisafiri na kuhubiri vitu ambavyo walikuwa wamesikia na kuona, na walikuwa wakibatiza katika jina la Yesu, ikawa kwamba wanafunzi walijikusanya pamoja na kushirikiana kwa sala kuu na kufunga.

2 Na Yesu tena alijidhihirisha kwao, kwani walikuwa wanaomba kwa Baba katika jina lake; na Yesu alikuja na kusimama miongoni mwao, na kuwaambia: Ni kitu gani mnachohitaji kwamba niwapatie?

3 Na wakamwambia: Bwana tunataka kwamba utuambie jina ambalo tutaita hili kanisa; kwani kuna ugomvi miongoni mwa watu kuhusu hili jambo.

4 Na Bwana akawaambia: Amin, amin, nawaambia, kwa nini watu wananung'unika na kubishana kwa sababu ya kitu hiki?

5 Je, hawajasoma maandiko, ambayo yanasema, lazima mjivike juu yenu jina la Kristo, ambalo ni jina langu? Kwani, kwa jina hili ndilo mtaitwa nalo katika siku ya mwisho;

6 Na yeyote atakayechukua jina langu na kuvumilia hadi mwisho, huyo huyo ndiye

atakayeokolewa katika siku ya mwisho.
7 Kwa hivyo chochote mtakachofanya, mfanye katika jina langu; kwa hivyo
mtaliita kanisa katika jina langu; na mtalingana Baba katika jina langu ili aweze
kubariki kanisa kwa ajili yangu.
8 Na linawezaje kuwa kanisa langu isipokuwa liitwe kwa jina langu? Kwani kanisa
likiitwa kwa jina la Musa, hapo litakuwa kanisa la Musa; au likiitwa kwa jina la mtu,
basi litakuwa kanisa la yule mtu; lakini likiitwa katika jina langu, hapo basi litakuwa
kanisa langu, ikiwa kwamba watajengwa juu ya injili yangu.
9 Kweli, nawaambia kwamba mmejengwa juu ya injili yangu; kwa hivyo mtaita vitu
vyovyote mtakavyoita katika jina langu; kwa hivyo ikiwa mnalingana kwa Baba, kwa
kanisa, ikiwa katika jina langu, Baba atawasikia.
10 Na ikiwa itakuwa hivyo kwamba kanisa limejengwa juu ya injili yangu hapo Baba
atafichua kazi yake ndani yake.
11 Lakini ikiwa haitajengwa juu ya injili yangu, na imejengwa kwa vitendo vya watu,
au juu ya vitendo vya ibilisi, amin, nawaambia wana shangwe katika vitendo vyao
kwa muda, na karibuni mwisho unakuja, na wataangushwa chini na kutupwa
kwenye moto, kutoka mahali ambapo hakuna kurudi nyuma.
12 Kwani vitendo vyao huwafuata, kwani ni kwa sababu ya vitendo vyao kwamba
wanaangushwa chini; kwa hivyo kumbuka vitu ambavyo nimewaambia.
13 Tazama, nimewapatia injili yangu, na hii ndiyo injili ambayo
nimewapatia—kwamba nilikuja kwenye ulimwengu kufanya mapenzi ya Baba, kwa
sababu alinituma.
14 Na Baba yangu alinituma ili nipate kuinuliwa juu kwenye msalaba; na baada ya
kuinuliwa juu kwenye msalaba, kwamba ningeleta watu wote kwangu, kwamba
kama nilivyoinuliwa juu na watu, hata hivyo watu wainuliwe juu na Baba, kusimama
mbele yangu, na kuhukumiwa kwa vitendo vyao, ikiwa vitakuwa vizuri au ikiwa
vitakuwa viovu.
15 Na kwa sababu hii nimeinuliwa juu; kwa hivyo, kulingana na uwezo wa Baba,
nitawaleta watu wote kwangu, ili wapate kuhukumiwa kulingana na vitendo vyao.
16 Na itakuwa kwamba yeyote atakayetubu na kubatizwa katika jina langu atajazwa;
na ikiwa atavumilia hadi mwisho, tazama, yeye hatahukumiwa kuwa na hatia mbele
ya Baba yangu kwenye ile siku wakati nitakaposimama kuhukumu ulimwengu.
17 Na yule ambaye hatavumilia hadi mwisho, mtu huyo huyo ndiye ataangushwa
chini na kutupwa kwenye moto, mahali ambapo hawawezi kurudi nyuma, kwa
sababu ya haki ya Baba.
18 Na hili ndilo neno ambalo amewapatia watoto wa watu. Na kwa sababu hii yeye
hutimiza maneno ambayo ameyatoa, na hasemi uwongo bali hutimiza maneno yake
yote.
19 Na hakuna kitu kichafu kinachoweza kuingia kwenye ufalme wake; kwa hivyo
hakuna chochote ambacho huingia kwenye pumziko lake isipokuwa wale ambao
wameosha nguo zao ndani ya damu yangu kwa sababu ya imani yao, na kutubu kwa
dhambi zao zote, na uaminifu wao hadi mwisho.
20 Sasa hii ndiyo amri: Tubuni nyinyi nyote katika sehemu zote za dunia, na mje
kwangu na mbatizwe katika jina langu kwamba muweze kutakaswa kwa kupokea
Roho Mtakatifu, ili msimame mbele yangu bila mawaa katika siku ya mwisho.
21 Kweli, kweli, nawaambia, hii ni injili yangu; na mnajua vitu ambavyo mnahitajika
kufanya katika Kanisa langu; kwani vitendo ambavyo mmeniona nikifanya, hivyo

pia mtafanya; kwani yale ambayo mmeniona nikifanya hata hivyo nyinyi mtafanya;
22 Kwa hivyo mkifanya hivi vitu heri kwenu, kwani mtainuliwa juu katika ile siku ya
mwisho.
23 Andikeni vitu ambavyo mmeona na kusikia, isipokuwa vile ambavyo
vimekatazwa.
24 Andikeni vitendo vya hawa watu, ambavyo vitakuwa, hata kama vilivyoandikwa,
ya yale ambayo yamekuwepo.
25 Kwani tazama, kutoka kwenye vitabu ambavyo vimeandikwa, na ambavyo
vitaandikwa, hawa watu watahukumiwa, kwani kutoka kwa hivyo vitabu vitendo
vyao vitajulikana kwa wanadamu.
26 Na tazama, vitu vyote vimeandikwa na Baba; kwa hivyo kutoka kwenye hivyo
vitabu ambavyo vitaandikwa, dunia itahukumiwa.
27 Na mjue kwamba nyinyi mtakuwa waamuzi wa watu hawa, kulingana na hukumu
ambayo nitawapatia ambayo itakuwa haki. Kwa hivyo mnapaswa kuwa watu wa aina
gani? Amin, nawaambia, hata vile nilivyo.
28 Na sasa naenda kwa Baba. Na amin, nawaambia, vitu vyovyote mtakavyomuuliza
Baba katika jina langu, vitatolewa kwenu.
29 Kwa hivyo, ombeni na mtapokea; bisheni na mtafunguliwa; kwani yule ambaye
huuliza hupokea; na kwa yule ambaye hubisha, itafunguliwa.
30 Na sasa tazama, shangwe yangu ni kubwa, hata kwenye utimilifu, kwa sababu
yenu, na pia kwa sababu ya kizazi hiki; ndio, na hata Baba hufurahi, na pia malaika
watakatifu, kwa sababu yenu na hiki kizazi; kwani hakuna mmoja wao aliyepotea.
31 Tazama, ningetaka kwamba muelewe; kwani ninaamanisha hao ambao sasa ni
wazima wa hiki kizazi; na hakuna hata ambaye amepotea; na kwa sababu yao, nina
utimilifu wa shangwe.
32 Lakini tazama, inanihuzunisha kwa sababu ya kizazi cha nne kutoka kwa hiki
kizazi, kwani wameongozwa mbali kama mateka na yeye, hata kama vile mwana wa
upotevu; kwani wataniuza kwa fedha, na dhahabu, na kwa hiyo ambayo nondo
huharibu na ambayo wezi huvunja na kuingia na kuiba. Na katika ile siku,
nitawaadhibu, hata katika kugeuza vitendo vyao juu ya vichwa vyao.
33 Na ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amemaliza haya maneno, aliwaambia
wanafunzi wake: Ingieni ndani nyinyi kupitia mlango uliosonga; kwani mlango
umesonga na njia ni nyembamba, ambayo inaenda kwa maisha, na kuna wachache
ambao huipata; lakini mpana ni mlango, na pana ni njia iendayo kwenye kifo, na
kuna wengi ambao huisafiria, mpaka usiku unakuja ambapo hakuna mtu
atakayeweza kufanya kazi.

# 3 Nefi 28

1 Na ikawa kwamba Yesu alipokuwa amesema haya maneno, aliwazungumzia
wanafunzi wake mmoja mmoja, akiwaambia: Ni kitu gani ambacho mnahitaji
kutoka kwangu baada ya mimi kwenda kwa Baba?
2 Na wote walisema, isipokuwa watatu, wakisema: Tunataka kwamba baada ya
kuishi umri wa binadamu, kwamba huduma yetu ambayo umetuitia, iishe, kwamba
tuje kwako haraka kwenye ufalme wako.
3 Na akawaambia: Heri kwenu kwa sababu mnataka kitu hiki kutoka kwangu; kwa
hivyo baada ya kuhitimu miaka sabini na miwili, mtakuja kwangu katika ufalme

wangu; na mimi mtapata mapumziko.
4 Na baada ya kuwazungumzia, alijigeuza kuelekea wale watatu, na kuwaambia: Ni
kitu gani ambacho mnataka niwafanyie, wakati nitakapokwenda kwa Baba?
5 Na walihuzunika mioyoni mwao, kwani hawakuthubutu kuzungumza na yeye
kitu ambacho walitaka.
6 Na akawaambia: Tazama, najua mawazo yenu, na mmetaka kitu ambacho
Yohana, mpendwa wangu, ambaye alikuwa na mimi katika huduma yangu kabla ya
mimi kuinuliwa juu na Wayahudi, alichotaka kwangu.
7 Kwa hivyo heri zaidi kwenu kwani kamwe hamtaonja kifo; lakini mtaishi kuona
vitendo vyote vya Baba kwa watoto wa watu, hata mpaka vitu vyote vitatimizwa
kulingana na mapenzi ya Baba, wakati nitakapokuja kwa utukufu wangu na uwezo
wa mbinguni.
8 Na hamtaumia uchungu wa kifo; lakini nitakapokuja katika utukufu wangu
mtabadilishwa kwa nukta moja kutoka hali ya kufa hadi kwa hali ya kutokufa; na
ndipo mtabarikiwa katika ufalme wa Baba yangu.
9 Na tena, hamtapata maumivu wakati mtakapoishi kimwili; wala huzuni
isipokuwa kwa dhambi za ulimwengu; na haya yote nitafanya kwa sababu ya kitu
ambacho mmetaka kutoka kwangu, kwani mmetaka kwamba mlete roho za watu
kwangu, wakati dunia itakaposimama.
10 Na kwa sababu hii mtapata utimilifu wa shangwe; na mtaketi chini katika ufalme
wa Baba yangu; ndio, shangwe yenu itajaa, hata vile Baba amenipatia utimilifu wa
shangwe; na mtakuwa hata kama nilivyo, nami niko hata vile Baba alivyo, na Baba
nami tuko mmoja.
11 Na Roho Mtakatifu hushuhudia mambo ya Baba na Mimi; na Baba huwapa
watoto wa watu Roho Mtakatifu kwa sababu yangu.
12 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kuzungumza haya maneno, alimgusa kila
mmoja wao kwa kidole chake isipokuwa wale watatu ambao walikuwa wa kukawia,
na hapo akaondoka.
13 Na tazama, mbingu zilifunguka, na walichukuliwa juu katika mbingu, na
waliona na kusikiliza vitu visivyosikika.
14 Na walikatazwa kwamba wasiongee; wala hawakupewa uwezo kwamba waongee
juu ya vitu ambavyo waliona na kusikia;
15 Na kama walikuwa katika miili au walikuwa nje ya miili, hawakuja; kwani
ilionekana kwao kama kugeuka sura, kwamba waligeuzwa kutoka kwa huu mwili wa
nyama hadi kwenye kutokufa, kwamba wangeweza kuona vitu vya Mungu.
16 Lakini ikawa kwamba walihubiri tena juu ya dunia; lakini hawakuhubiri juu ya
vitu ambavyo walisikia na kuona kwa sababu ya amri ambayo walipewa mbinguni.
17 Na sasa, kama walikuwa mwili wenye kufa au wa kutokufa kutoka siku ya
kugeuka kwao sura, sijui;
18 Lakini hiki kiasi najua, kulingana na maandishi ambayo yametolewa — walienda
kote juu ya ulimwengu, na kuhubiri kwa watu wote, wakileta kwenye kanisa jinsi vile
wengi walivyoamini katika mahubiri yao; wakiwabatiza, na vile wengi walibatizwa,
walipokea Roho Mtakatifu.
19 Na walitupwa kwenye gereza na wale ambao hawakuwa wa kanisa. Na magereza
hayangewashikilia, kwani yalipasuka katikati.
20 Na walitupwa chini ndani ya ardhi; lakini walipiga ardhi kwa neno la Mungu,
mpaka kwamba kwa uwezo wake walikombolewa kutoka kina cha ardhi; na kwa

hivyo hawangechimba mashimo ya kutosha ya kuwazuia.
21 Na mara tatu walitupwa kwenye tanuu na hawakupata majeraha.
22 Na mara mbili walitupwa kwenye tundu la wanyama wa mwitu; na tazama,
walicheza na hao wanyama kama mtoto na mwanakondoo, na hawakujeruhiwa.
23 Na ikawa kwamba walienda hivyo miongoni mwa watu wote wa Nefi, na
walihubiri injili ya Kristo kwa watu wote usoni mwa nchi; na waliomgeukia Bwana,
na waliunganishwa kwa kanisa la Kristo, na hivyo ndivyo watu wa kizazi hicho
walivyobarikiwa, kulingana na neno la Yesu.
24 Na sasa mimi Mormoni, namaliza kuzungumza kuhusu vitu hivi kwa muda.
25 Tazama, nilikuwa karibu kuandika majina ya wale ambao hawatakufa, lakini
Bwana alinikataza; kwa hivyo siyaandiki, kwani yamefichwa kutoka kwa ulimwengu.
26 Lakini tazama, nimewaona na wamenihubiria.
27 Na tazama, watakuwa miongoni mwa Wayunani, na Wayunani hawatawafahamu.
28 Watakuwa pia miongoni mwa Wayahudi na Wayahudi hawatawafahamu.
29 Na itakuwa, wakati Bwana atakapoona ni vizuri kwa hekima yake, kwamba
watahubiri kwa makabila yote ya Israeli yaliyotawanywa, na kwa mataifa yote,
makabila, ndimi na watu, na kuokoa nafsi nyingi miongoni mwao kwa Yesu, ili
matakwa yao yatimizwe, na pia kwa sababu ya uwezo wa Mungu wa kusadikisha
ambao umo ndani yao.
30 Na wao ni kama malaika wa Mungu, na ikiwa wataomba kwa Baba katika jina la
Yesu, wanaweza kujidhihirisha kwa mtu yeyote ambaye wanaona ni vyema.
31 Kwa hivyo vitendo vikubwa na vya ajabu vitafanywa nao, kabla ya siku kubwa
inayokuja wakati watu wote lazima kwa kweli wasimame mbele ya kiti cha hukumu
cha Kristo.
32 Ndio, hata miongoni mwa Wayunani kutafanyika kazi kubwa na ya ajabu na wao,
kabla ya ile siku ya hukumu.
33 Na kama mngekuwa na maandiko yote ambayo yanatoa historia ya kazi zote za
ajabu za Kristo, mngejua, kulingana na maneno ya Kristo, kwamba hivi vitu lazima
vije kwa kweli.
34 Na ole kwake ambaye hatasikia maneno ya Yesu, na pia kwa wao ambao
amechagua na kutuma miongoni mwao; kwani yeyote ambaye hatapokea haya
maneno ya Yesu na maneno ya wale ambao amewatuma, hatampokea; na kwa hivyo
hatawapokea katika ile siku ya mwisho;
35 Na ingelikuwa afadhali kwao kama hawangezaliwa. Kwani mnadhani kwamba
mnaweza kukwepa haki ya Mungu aliyekosewa, ambaye amekanyagwa chini ya
miguu ya watu, ili wokovu ungekuja?
36 Na sasa tazama, vile nilisema kuhusu wale ambao Bwana amewachagua, ndio,
hata wale watatu waliochukuliwa juu katika mbingu, kwamba sikujua kama
waligeuzwa kutoka mwili wa kufa hadi mwili usiokufa—
37 Lakini tazama, tangu niandike, nimemwuliza, Bwana, na ameifanya kujulikana
kwangu kwamba lazima mabadiliko yaletwe kwenye miili yao, au sivyo, inahitajika
kwamba lazima wapate kufa;
38 Kwa hivyo, ili wasipate kufa, kulikuwa na mabadiliko yaliyofanywa kwenye miili
yao, ili wasiumie na uchungu wala huzuni isipokuwa kwa ajili ya dhambi za
ulimwengu.
39 Sasa hili badiliko halikuwa sawa na lile ambalo litatendeka katika ile siku ya
mwisho; lakini kulikuwa na badiliko lililofanywa kwao, mpaka kwamba Shetani

hangekuwa na uwezo juu yao, kwamba hangewajaribu; na walitakaswa kimwili,
kwamba walikuwa watakatifu, na kwamba nguvu za dunia hazingewashika.
40 Na wangekaa kwa hali hii mpaka siku ya hukumu ya Kristo; na katika ile siku
wangepokea mabadiliko makubwa kuliko mbeleni na kupokewa katika ufalme wa
Baba kutotoka tena, lakini kuishi na Mungu milele mbinguni.

# 3 Nefi 29

1 Na sasa tazama, nawaambia kwamba wakati Bwana atakapoona sawa katika hekima
yake, kwamba haya maneno yatawajia Wayunani kulingana na neno lake, ndipo
mtajua kwamba agano ambalo Baba amefanya na watoto wa Israeli, kuhusu kurudi
kwao kwenye nchi zao za urithi, kitambo imeanza kutimizwa.
2 Na mtajua kwamba maneno ya Bwana, ambayo yamezungumzwa na manabii
watakatifu, yote yatatimizwa; na hamtahitajika kusema kwamba Bwana
anachelewesha kuja kwake kwa watoto wa Israeli.
3 Na hamtakikani kuwaza katika mioyo yenu kwamba maneno ambayo
yamezungumzwa ni ya bure, kwani tazama, Bwana atakumbuka agano lake ambalo
amefanya kwa watu wake wa nyumba ya Israeli.
4 Na wakati mtakapoona haya maneno yakitokea miongoni mwenu, hamtahitaji
tena kudharau mwenendo wa Bwana, kwani upanga wake wa haki uko ndani ya
mkono wake wa kulia; na tazama, katika siku ile, ikiwa mtakataa kwa madharau,
vitendo vyake, ndipo atasababisha kwamba haraka mtapitwa.
5 Ole kwake ambaye hukataa vitendo vya Bwana; ndio, ole kwake ambaye atakataa
Kristo na matendo yake!
6 Ndio, ole kwa yule ambaye atakataa mafunuo ya Bwana, na ambaye atasema
kuwa Bwana hafanyi kazi tena kwa kufunua au unabii, au kwa karama, au kwa lugha
au kwa kuponya, au kwa uwezo wa Roho Mtakatifu!
7 Ndio, na ole kwa yule atakayesema katika ile siku, kupata faida, kwamba
hakuwezi kufanyika miujiza na Yesu Kristo; kwani yule atakayefanya hivi atakuwa
mwana wa upotevu, ambaye kwake hakukuwa na huruma kulingana na neno la
Kristo!
8 Ndio, na hamhitaji tena kufyonya, wala kudharau, wala kuchezea Wayahudi,
wala sazo lolote la nyumba ya Israeli; kwani tazama, Bwana hukumbuka agano lake
kwao, na atawafanyia kulingana na yale ambayo ameapa.
9 Kwa hivyo hampaswi kudhani kwamba mnaweza kugeuza mkono wa kulia wa
Bwana hadi kushoto, ili asifanye hukumu yake kwa kutimiza lile agano ambalo
amefanya kwa nyumba ya Israeli.

# 3 Nefi 30

1 Sikizeni, Ee nyinyi Wayunani, na msikie maneno ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu
anayeishi, ambaye ameniamuru kwamba nisizungumze kuwahusu kwani tazama,
ameniamuru kwamba niandike nikisema:
2 Geukeni nyinyi Wayunani wote, kutoka kwa njia zenu za uovu; na mtubu kutoka
matendo yenu maovu, kutoka kwa uwongo wenu na udanganyifu, na ukahaba wenu,
na makundi yenu ya machukizo na ya siri, na sanamu zenu, na mauaji yenu, na
ukuhani wa uongo, na wivu wenu, na mashindano yenu ya machukizo ya siri, na

kutokana kwa uovu wenu na maovu, na mje kwangu, na mpate kubatizwa kwa jina langu, ili mpate kusamehewa dhambi zenu, na mjazwe na Roho Mtakatifu, ili mhesabiwe na watu wangu ambao ni wa nyumba ya Israeli.

# Nefi wa Nne

## Kitabu cha Nefi

Ambaye ni Mwana wa Nefi — Mmojawapo wa Wafuasi wa Yesu Kristo

*Historia ya watu wa Nefi, kulingana na maandishi yake.*

1 Na ikawa kwamba mwaka wa thelathini na nne ulipita, na pia mwaka wa thelathini
na tano, na tazama wafuasi wa Yesu walikuwa wameanzisha kanisa la Kristo katika
eneo lote karibu. Na kadiri wengi walivyokuja kwao, na kutubu dhambi zao kwa
ukweli, walibatizwa kwa jina la Yesu; na pia walipokea Roho Mtakatifu.
2 Na ikawa katika mwaka wa thelathini na sita, watu wote walimgeukia Bwana,
nchini kote, wote Wanefi na Walamani, na hakukuweko na mabishano na ugomvi
miongoni mwao, na kila mtu alimtendea mwingine haki.
3 Na vitu vyao vyote vilitumiwa kwa usawa miongoni mwao; kwa hivyo hakukuwa
na tajiri na masikini, wafungwa na walio huru, lakini wote walifanywa huru, na
washiriki wa karama ya mbinguni.
4 Na ikawa kwamba mwaka wa thelathini na saba ulipita pia, na bado kukaendelea
kuwa na amani katika nchi.
5 Na kulikuwa na kazi kubwa na ya ajabu iliyofanywa na wafuasi wa Yesu, mpaka
kwamba waliponya wagonjwa, na kufufua wafu, na kusababisha vilema kutembea,
na vipofu kupokea uwezo wa kuona, na viziwi kusikia; na walifanya kila aina ya
miujiza miongoni mwa watoto wa watu; na hawakufanyia kwa njia ingine miujiza
isipokuwa katika jina la Yesu.
6 Na hivyo ndivyo mwaka wa thelathini na nane ulivyopita, na pia wa thelathini na
tisa, na wa arubaini na moja, na wa arubaini na mbili, ndio, hata miaka arubaini na
tisa ilipita, na pia wa hamsini na moja, na wa hamsini na mbili; ndio, na hata miaka
hamsini na tisa ilipita.
7 Na Bwana aliwafanikisha sana katika nchi; ndio, mpaka kwamba walijenga miji
tena ambako miji ilichomwa.
8 Ndio, hata huo mji mkubwa Zarahemla, walisababisha kujengwa tena.
9 Lakini kulikuwa na miji mingi ambayo ilikuwa imezama, na maji kuja mahali
pao; kwa hivyo, hii miji haingefanywa upya.
10 Na sasa, tazama, ikawa kwamba watu wa Nefi walipata nguvu, na wakaongezeka
kwa haraka sana, na wakawa weupe sana na watu wa kupendeza.
11 Na walioa, na kuolewa, na walibarikiwa kulingana na wingi wa ahadi ambazo
Bwana alikuwa amefanya kwao.
12 Na hawakutembea tena kulingana na vitendo na sheria ya Musa; lakini
walitembea kulingana na amri ambazo walipokea kutoka kwa Bwana wao na Mungu
wao, wakiendelea katika kufunga na sala, na kwa kukutana pamoja siku zote
kuomba na kusikia neno la Bwana.
13 Na ikawa kwamba hakukuwepo na ubishi miongoni mwa watu wote, katika ile
nchi yote; lakini kulikuwa na miujiza mikuu iliyofanywa na wafuasi wa Yesu.
14 Na ikawa kwamba mwaka wa sabini na moja ulipita, na pia mwaka wa sabini na
mbili, ndio, na kwa kifupi, mpaka mwaka wa sabini na tisa ulipopita; ndio, hata

miaka mia moja ilikuwa imepita, na wafuasi wa Yesu ambao alichagua, wote
walikuwa wameenda peponi kwa Mungu, isipokuwa wale watatu ambao ni wa
kungoja; na kulikuwa na wafuasi wengine ambao walisimikwa mahali pao; na pia
wengi wa kizazi hicho walikuwa wamekufa.
15 Na ikawa kwamba hakukuwa na ubishi katika nchi, kwa sababu ya mapenzi ya
Mungu ambayo yaliishi katika mioyo ya watu.
16 Na hakukuwa na wivu, wala ubishi, wala misukosuko, wala ukahaba, wala
uwongo, wala mauaji, wala uzinifu wa aina yoyote; na kwa kweli hakujakuwa na
watu ambao wangekuwa na furaha zaidi miongoni mwa watu wote ambao
waliumbwa na mkono wa Mungu.
17 Hakukuwa na wanyang'anyi, wala wauaji, wala hakukuwa na Walamani, wala aina
yoyote ya vikundi; lakini walikuwa kitu kimoja, watoto wa Kristo, na warithi wa
ufalme wa Mungu.
18 Na jinsi gani walibarikiwa! Kwani Bwana aliwabariki kwa matendo yao yote;
ndio, hata walibarikiwa na kufanikiwa mpaka miaka mia moja na kumi ikapita; na
kizazi cha kwanza kutoka Kristo kilikuwa kimepita, na hakukuwa na ubishi katika
nchi yote.
19 Na ikawa kwamba Nefi, yule ambaye aliandika haya maandishi ya mwisho, (na
aliyaandika kwenye bamba za Nefi) alikufa, na mwana wake Amosi aliandika badala
yake; na aliyaandika kwenye bamba za Nefi pia.
20 Na aliandika kwa miaka themanini na minne, na kulikuwa bado na amani
nchini, isipokuwa sehemu ndogo ya watu ambao walikuwa wameasi kutoka kanisa
na kujiita Walamani; kwa hivyo kulianza kuwa tena na Walamani katika nchi.
21 Na ikawa kwamba Amosi alifariki pia, (na ilikuwa miaka mia moja tisini nne
kutoka kuja kwa Kristo) na mwana wake Amosi aliandika maandishi badala yake; na
yeye pia aliandika kwenye bamba za Nefi; na ikaandikwa pia kwenye kitabu cha
Nefi, ambacho ni kitabu hiki.
22 Na ikawa kwamba miaka mia mbili ilikwa imepita; na kizazi cha pili chote
kilikuwa kimepita isipokuwa wachache.
23 Na sasa mimi, Mormoni, ningetaka kwamba mjue kwamba watu walikuwa
wameongezeka, mpaka kwamba walitapakaa kote usoni mwa nchi, na kwamba
walikuwa wametajirika sana, kwa sababu ya kufanikiwa kwao katika Kristo.
24 Na sasa, katika mwaka huu wa mia mbili na moja kulianza kuwa miongoni mwao
wale ambao waliinuliwa katika kiburi, kwa kuvaa nguo za thamani, na kila aina ya
lulu nzuri, na vitu vizuri vya dunia.
25 Na kutokea wakati huo na kuendelea, walikuwa na mali yao na utajiri wao, na
vitu vyao havikuwa sawa miongoni mwao.
26 Na walianza kujigawanya kwenye vyeo; na wakaanza kujenga makanisa yao kwa
kujipatia faida, na wakaanza kukataa kanisa la kweli la Kristo.
27 Na ikawa kwamba wakati miaka mia mbili na kumi ilipokuwa imepita kulikuwa
na makanisa mengi katika nchi; ndio, kulikuwa na makanisa mengi ambayo yalidai
kumjua Kristo, na bado yalikataa sehemu kubwa ya injili yake, mpaka kwamba
yalikubali aina yote ya uovu, na yalitoa kila kilicho kitakatifu kwa yule ambaye
alikuwa amekataliwa kwa sababu ya kutostahili.
28 Na hili kanisa liliongezeka sana kwa sababu ya uovu, na kwa sababu ya nguvu ya
Shetani ambaye alishikilia mioyo yao.
29 Na tena, kulikuwa na kanisa lingine ambalo lilimkana Kristo; na walidhulumu

kanisa la kweli la Kristo, kwa sababu ya uvumilivu wao na kuamini kwao katika
Kristo; na waliwadharau kwa sababu ya miujiza mingi ambayo walifanya miongoni
mwao.
30 Kwa hivyo walionyesha uwezo na mamlaka juu ya wafuasi wa Yesu ambao
walibaki nao, na waliwatupa kwenye gereza; lakini kwa uwezo wa neno la Mungu,
ambao ulikuwa ndani yao, magereza yalipasuka katikati, na wakaenda mbele
wakifanya miujiza mikuu miongoni mwao.
31 Walakini, na ijapokuwa hii miujiza yote, watu walishupaza mioyo yao, na
walitaka kuwaua, hata kama vile Wayahudi wa Yerusalemu walitafuta kumuua Yesu,
kulingana na neno lake.
32 Na waliwatupa kwenye majiko ya moto, na wakatoka nje bila majeraha.
33 Na waliwatupa pia kwenye pango za wanyama wa mwitu, na walicheza na wale
wanyama wa mwitu hata vile mtoto na mwanakondoo; na walitoka na kuja mbele
kutoka miongoni mwao, bila kupata majeraha.
34 Walakini, watu walishupaza mioyo yao, kwani waliongozwa na makuhani wengi
na manabii wa uwongo kuanzisha makanisa mengi, na kufanya aina yote ya uovu.
Na waliwapiga watu wa Yesu; lakini watu wa Yesu hawakulipiza kisasi. Na hivyo
walififia katika kutoamini na uovu, kutoka mwaka mmoja hadi mwingine, hata hadi
miaka mia mbili na thelathini ikapita.
35 Na sasa ikawa katika mwaka huu, ndio, katika mwaka wa mia mbili na thelathini
na moja, kulikuwa na mgawanyiko mkubwa miongoni mwa watu.
36 Na ikawa kwamba katika mwaka huu kulitokea watu ambao waliitwa Wanefi, na
walikuwa waumini wa kweli wa Kristo; na miongoni mwao kulikuwa na wale ambao
waliitwa na Walamani — Wayakobo, na Wayusufu, na Wazoramu;
37 Kwa hivyo waumini wa kweli katika Kristo, na waabudu wa kweli wa Kristo,
(miongoni mwao ambao walikuwa wale wafuasi watatu wa Yesu ambao watakaa)
waliitwa Wanefi, na Wayakobo, na Wayusufu, na Wazoramu.
38 Na ikawa kwamba wale ambao walikataa injili waliitwa Walamani, na Walemueli,
na Waishmaeli; na hawakufifia kwa kutoamini, lakini waliasi makusudi dhidi ya
injili ya Kristo; na waliwafundisha watoto wao kwamba wasiamini, hata vile babu
zao, kutoka mwanzoni, walivyofifia.
39 Na ilikuwa kwa sababu ya uovu na machukizo ya babu zao, hata kama vile
ilivyokuwa mwanzoni. Na walifundishwa kuchukia watoto wa Mungu, hata vile
Walamani walifundishwa kuwachukia watoto wa Nefi kutoka mwanzo.
40 Na ikawa kwamba miaka mia mbili na arubaini na nne ilikuwa imekwisha, na
hivyo ndivyo yalikuwa mambo ya watu. Na sehemu kubwa ya watu waovu ilipata
nguvu, na walikuwa wengi sana kuliko watu wa Mungu.
41 Na bado waliendelea na kujenga makanisa yao, na kuyapamba na aina yote ya
vitu vya thamani. Na hivyo miaka mia mbili na hamsini ilikwisha, na pia miaka mia
mbili na sitini.
42 Na ikawa kwamba sehemu ya watu waovu walianza tena kuanzisha viapo vya siri
na makundi maovu ya siri ya Gadiantoni.
43 Na pia watu ambao waliitwa watu wa Nefi walianza kujisifu katika mioyo yao,
kwa sababu ya utajiri wao mwingi, na kuwa bure kama ndugu zao, Walamani.
44 Na kutoka wakati huu wanafunzi walianza kuhuzunika kwa ajili ya dhambi za
dunia.
45 Na ikawa kwamba wakati miaka mia tatu ilipokwisha, watu wote wa Nefi na

Walamani walikuwa wamepata kuwa waovu sana mmoja akiwa kama mwingine.
46 Na ikawa kwamba wanyang'anyi wa Gadiantoni walitawanyika kote usoni mwa
nchi; na hakukuwa wowote waliokuwa wa haki isipokuwa wanafunzi wa Yesu. Na
waliweka dhahabu na fedha kwa wingi, na walifanya biashara na aina yote ya bidhaa.
47 Na ikawa kwamba baada ya miaka mia tatu na tano kupita, (na watu walibaki
bado kwenye uovu) Amosi alifariki; na kaka yake, Amaroni, aliandika maandishi
badala yake.
48 Na ikawa kwamba baada ya miaka mia tatu na ishirini kupita, Amaroni,
akilazimishwa na Roho Mtakatifu, alificha maandishi yote matakatifu — ndio, hata
maandishi yote matakatifu yaliyotolewa kutoka kizazi hadi kizazi, ambayo yalikuwa
matakatifu — hata mpaka mwaka wa mia tatu na ishirini tangu kuja kwa Kristo.
49 Na aliyaficha kwa Bwana, kwamba yangekuja tena kwa sazo la nyumba ya
Yakobo, kulingana na unabii na ahadi za Bwana. Na huo ndio mwisho wa
maandishi ya Amaroni.

# Kitabu cha Mormoni

## Mormoni 1

1 Na sasa mimi, Mormoni, ninaandika maandishi ya vitu ambavyo nimeona na kusikia, na kuyaita Kitabu cha Mormoni.

2 Na karibu wakati ambao Amaroni alipoficha maandishi kwa Bwana, alikuja kwangu, (mimi nikiwa na umri wa karibu miaka kumi, na nilianza kujifunza kidogo kulingana na namna ya kujifunza kwa watu wangu) na Amaroni akaniambia: Ninaona kwamba wewe ni mtoto mwenye heshima, na ni mwepesi kwa kusoma;

3 Kwa hivyo, wakati utakuwa karibu na umri wa miaka ishirini na nne ninataka kwamba ukumbuke vitu ambavyo umevichunguza kuhusu hawa watu; na wakati utakuwa na huo umri uende kwa nchi ya Antumu, kwenye kilima ambacho kitaitwa Shimu; na hapo nimeweka kwa ulinzi wa Bwana maandishi yote matakatifu kuhusu hawa watu.

4 Na tazama, utajichukulia bamba za Nefi, na zitakazosalia utaacha mahali hapo; na utaandika kwenye bamba za Nefi vitu vyote ambavyo utakuwa umeviona kuhusu hawa watu.

5 Na mimi, Mormoni, nikiwa wa kizazi cha Nefi, (na jina la baba yangu lilikuwa Mormoni) nilikumbuka vitu ambavyo Amaroni aliniamuru nifanye.

6 Na ikawa kwamba mimi, nikiwa na miaka kumi na moja, nilibebwa na baba yangu hadi kwenye nchi iliyokuwa kusini, hata kwenye nchi ya Zarahemla.

7 Uso wa nchi yote ulikuwa umefunikwa na majengo, na watu walikuwa wengi, hata kama mchanga wa bahari.

8 Na ikawa katika mwaka huu kukaanza kuwa na vita miongoni mwa Wanefi, ambao walikuwa mkusanyiko wa Wanefi na Wayakobo na Wayusufu na Wazoramu; na hivi vita vilikuwa miongoni mwa Wanefi, na Walamani na Walemueli na Waishmaeli.

9 Sasa Walamani na Walemueli na Waishmaeli waliitwa Walamani, na yale makundi mawili yalikuwa Wanefi na Walamani.

10 Na ikawa kwamba vita vilianza kuwa miongoni mwao kwenye mipaka ya Zarahemla, kando ya maji ya Sidoni.

11 Na ikawa kwamba Wanefi walikuwa wamekusanya pamoja idadi kubwa ya watu, hata kupita idadi ya elfu thelathini. na ikawa kwamba kwenye huu mwaka walikuwa na vita kadhaa, ambamo Wanefi walishinda Walamani na kuchinja wengi wao.

12 Na ikawa kwamba Walamani waliondoa kusudi lao, na masikilizano ya amani yakaimarishwa nchini; na amani ikadumu kwa muda wa karibu miaka minne, kwamba hakukuwepo na umwagaji wa damu.

13 Lakini uovu ulienea juu ya uso wa nchi yote, mpaka kwamba Bwana akaondoa wanafunzi wake wapendwa, na kazi ya miujiza na ya uponyaji iliisha kwa sababu ya uovu wa watu.

14 Na hakukuwa na vipawa kutoka kwa Bwana, na Roho Mtakatifu hakumjia yeyote, kwa sababu ya uovu wao na kutoamini kwao.

15 Na mimi, nikiwa na umri wa miaka kumi na mitano na nikiwa kidogo na akili timamu, kwa hivyo nilitembelewa na Bwana, na kuonja na kujua uzuri wa Yesu.

16 Na nilijaribu kuwahubiria watu hawa, lakini mdomo wangu ulifungwa, na nikakatazwa kwamba nisihubiri kwao; kwani tazama walikuwa wameasi makusudi

dhidi ya Mungu wao; na wale wanafunzi wapendwa waliondolewa nje ya nchi, kwa sababu ya uovu wao.
17 Lakini nilibaki miongoni mwao, lakini nilikatazwa kuhubiri kwao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo; na kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao nchi ililaaniwa kwa sababu yao.
18 Na hawa wanyang'anyi wa Gadiantoni, ambao walikuwa miongoni mwa Walamani, waliingilia nchi, mpaka kwamba wakazi wa pale walianza kuficha hazina zao udongoni; na zikawa zenye kuteleza, kwa sababu Bwana alikuwa amelaani nchi, kwamba hawangeweza kuzishikilia, wala kuziweka tena.
19 Na ikawa kwamba kulikuwa na uchawi, na ulozi, na uganga; na nguvu za yule mwovu zilitumiwa kote usoni mwa nchi, hata kwa kutimiza maneno yote ya Abinadi, na pia Samweli yule Mlamani.

## Mormoni 2

1 Na ikawa kwamba katika mwaka huo huo kulianza kuwa na vita tena miongoni mwa Wanefi na Walamani. Na ingawaje mimi nikiwa kijana mdogo, nilikuwa mkubwa kwa kimo; kwa hivyo watu wa Nefi walinichagua kwamba niwe kiongozi wao, au kingozi wa majeshi yao.
2 Kwa hivyo ikawa kwamba katika mwaka wangu wa kumi na sita nilienda mbele kuliongoza jeshi la Wanefi, dhidi ya Walamani; kwa hivyo miaka mia tatu na ishirini na sita ilikuwa imepita.
3 Na ikawa kwamba katika mwaka wa mia tatu na ishirini na saba Walamani walitushambulia kwa nguvu nyingi sana, mpaka kwamba wakayatisha majeshi yangu; kwa hivyo hawangepigana, na walianza kurudi nyuma kuelekea nchi za kaskazini.
4 Na ikawa kwamba tulifikia mji wa Angola, na tukaumiliki mji huo, na kufanya matayarisho kujilinda dhidi ya Walamani. Na ikawa kwamba tuliimarisha mji kwa nguvu zetu; lakini injapokuwa kuimarika kwetu Walamani walitushambulia na wakatufukuza hadi nje ya nchi.
5 Na walitukimbiza pia kutoka nchi ya Daudi.
6 Na tulienda mbele na tukafikia nchi ya Yoshua, ambayo ilikuwa kwenye mipaka ya magharibi kando ya bahari.
7 Na ikawa kwamba tulikusanya watu wetu kwa haraka iwezekanavyo, ili tungewakusanya pamoja katika kundi moja.
8 Lakini tazama, nchi ilikuwa imejaa wanyang'anyi na Walamani; na ingawaje kulikuwa na uharibifu mwingi ambao ulining'inia juu ya watu wangu, hawakutubu vitendo vyao viovu; kwa hivyo kulikuwa na usambazaji wa mauaji na maangamizo kote usoni mwa nchi, kote kwenye sehemu ya Wanefi na pia kwenye sehemu ya Walamani; na ulikuwa upinduzi mmoja mkuu kote usoni mwa nchi.
9 Na sasa, Walamani walikuwa na mfalme, na jina lake lilikuwa Haruni; na alitushambulia na jeshi la elfu arubaini na nne. Na tazama, nilimzuia na watu elfu arubaini na mbili. Na ikawa kwamba nilimpiga na jeshi langu kwamba alitoroka mbele yangu. Na tazama, haya yote yalifanyika, na miaka mia tatu na thelathini ikawa imekwisha.
10 Na ikawa kwamba Wanefi walianza kutubu dhambi zao, na wakaanza kulalamika hata kama ilivyotabiriwa na nabii Samweli; kwani tazama hakuna mtu ambaye

aliweza kuweka ile ambayo ilikuwa yake, kwa sababu ya wezi, na wanyang'anyi, na
wauaji, na ustadi wa uganga, na uchawi ambao ulikuwa katika nchi.
11 Hivyo kulianza kuwa na maombolezi na kulia katika nchi kwa sababu ya vitu
hivi, na hasa zaidi miongoni mwa watu wa Nefi.
12 Na ikawa kwamba baada ya mimi, Mormoni, kuona kilio chao na maombolezi
yao na huzuni yao mbele ya Bwana, moyo wangu ulianza kufurahi ndani yangu, kwa
sababu nilijua huruma na uvumilivu wa Bwana, kwa hivyo nikidhani kwamba
atakuwa na huruma kwao kwamba wangekuwa watu wa haki tena.
13 Lakini tazama hii shangwe yangu ilikuwa bure, kwani hii huzuni yao haikuwa ya
toba, kwa sababu ya uzuri wa Mungu; lakini ilikuwa sana huzuni ya waliolaaniwa,
kwa sababu Bwana hakuwaruhusu kufurahi katika dhambi.
14 Na hawakuja kwa Yesu na mioyo iliyovunjika na roho zilizopondeka, lakini
walimlaani Mungu, na wakataka kufa. Hata hivyo wangepigana wakitumia upanga
kwa maisha yao.
15 Na ikawa kwamba huzuni yangu ilinirudia tena, na niliona kwamba siku ya
neema ilikuwa imepita na wao, kimwili pamoja na kiroho; kwani niliona maelfu
wakiangushwa chini kwenye uasi wa wazi dhidi ya Mungu wao, na kurundikwa
kama fungu la mbolea juu ya uso wa nchi. Na hivyo miaka mia tatu na arobaini na
minne ilikuwa imepita.
16 Na ikawa kwamba katika mwaka wa mia tatu na hamsini na tano Wanefi
walianza kutoroka mbele ya Walamani; na walifuatwa mpaka walipofika hata
kwenye nchi ya Yashoni, kabla ya kuwezekana kuwazuia katika kukimbia kwao.
17 Na sasa, mji wa Yashoni ulikuwa karibu na nchi ambayo Amaroni alikuwa
ameficha maandishi kwa Bwana, ili yasiharibiwe. Na tazama nilikuwa nimeenda
kulingana na neno la Amaroni, na kuchukua bamba za Nefi, na niliandika kulingana
na maneno ya Amaroni.
18 Na niliandika juu ya bamba za Nefi nakili kamili ya uovu na machukizo yote;
lakini kwenye hizi bamba nilijizuia kuweka nakili kamili ya uovu wao na
machukizo, kwani tazama, mfululizo wa kuonekana kwa uovu na machukizo
umekuwa mbele ya macho yangu tangu nitoshee kuona mwenendo wa binadamu.
19 Na ole kwangu kwa sababu ya uovu wao; kwani moyo wangu umejawa na huzuni
kwa sababu ya uovu wao, maisha yangu yote; walakini, ninajua kwamba nitainuliwa
juu katika siku ya mwisho.
20 Na ikawa kwamba katika mwaka huu watu wa Nefi waliwindwa na kukimbizwa.
Na ikawa kwamba tulikimbizwa mbele mpaka tulipofikia kaskazini kwa nchi
ambayo iliitwa Shemu.
21 Na ikawa kwamba tuliimarisha mji wa Shemu, na tuliwakusanya humo watu
wetu vile ilivyowezekana, kwamba labda tungewaokoa kutoka kwa maangamizo.
22 Na ikawa katika mwaka wa mia tatu na arubaini na sita walianza kutushambulia
tena.
23 Na ikawa kwamba niliwazungumzia watu wangu, nikiwasihi kwa juhudi kuu,
kwamba wasimame kwa ujasiri mbele ya Walamani na kupigana kwa ajili ya wake
zao, na watoto wao, na nyumba zao, na miji yao.
24 Na maneno yangu yaliwaamsha kidogo kuwa na nguvu, mpaka kwamba
hawakukimbia kutoka mbele ya Walamani, lakini walisimama kwa usajiri dhidi yao.
25 Na ikawa kwamba tulikabiliana na jeshi la elfu thelathini dhidi ya jeshi la elfu
hamsini. Na ikawa kwamba tuliwazuia na uthabiti hivyo kwamba walikimbia

kutoka mbele yetu.
26 Na ikawa kwamba baada ya kukimbia tuliwafuata na majeshi yetu, na tulipigana
na wao tena, na tukawashinda; walakini nguvu za Bwana hazikuwa nasi; ndio,
tuliachwa peke yetu, kwamba Roho ya Bwana haikuwa nasi; kwa hivyo tulikuwa
tumekuwa wanyonge kama ndugu zetu.
27 Na moyo wangu ulihuzunika kwa sababu ya huu msiba mkubwa wa watu wangu,
kwa sababu ya uovu wao na machukizo yao. Lakini tazama, tulienda mbele dhidi ya
Walamani na wale wanyang'anyi wa Gadiantoni, mpaka, tulipokuwa tena
tumeimiliki nchi ya urithi wetu.
28 Na mwaka wa mia tatu na arubaini na tisa ukawa umepita. Na katika mwaka wa
mia tatu na hamsini tuliweka mkataba na Walamani na wanyang'anyi wa
Gadiantoni, ambamo tulipata nchi zetu za urithi kugawanywa.
29 Na Walamani walitupatia nchi ya upande wa kaskazini, ndio, hata njia
nyembamba iliyoelekea nchi ya kusini. Na tukawapatia Walamani nchi yote ya
kusini.

## Mormoni 3

1 Na ikawa kwamba Walamani hawakutushambulia tena hadi miaka kumi ilipopita.
Na tazama, nilikuwa nimeweka watu wangu, Wanefi, kwenye kazi, katika
kutayarisha nchi yao na silaha zao dhidi ya wakati wa vita.
2 Na ikawa kwamba Bwana alisema kwangu: Walilie watu hawa — Tubuni ninyi,
na mje kwangu, na mbatizwe, na mjenge tena kanisa langu, na mtasamehewa.
3 Na niliwahubiria hawa watu, lakini ilikuwa bure; na hawakufahamu kwamba
Bwana ndiye aliyewarehemu, na kuwapatia nafasi ya kutubu. Na tazama
walishupaza mioyo yao dhidi ya Bwana Mungu wao.
4 Na ikawa kwamba baada ya huu mwaka wa kumi kuisha, ikiwa, jumla ya miaka
yote pamoja, mia tatu na sitini kutoka kuja kwa Kristo, mfalme wa Walamani
alinitumia barua, ambayo ilinieleza kwamba walikuwa wanajitayarisha kuja
kupigana dhidi yetu tena.
5 Na ikawa kwamba nilisababisha kwamba watu wangu wajikusanye pamoja katika
nchi ya Ukiwa, kwa mji uliokuwa mipakani, kando ya njia nyembamba ambayo
ilielekea katika nchi iliyokuwa upande wa kusini.
6 Na hapo tuliweka majeshi yetu, ili tuyazuie majeshi ya Walamani, kwamba
wasimiliki yoyote ya nchi zetu; kwa hivyo tulijiimarisha dhidi yao na majeshi yetu
yote.
7 Na ikawa kwamba katika mwaka wa mia tatu na sitini na moja Walamani
walikuja chini kwenye mji wa Ukiwa kupigana nasi; na ikawa kwamba katika mwaka
huo tuliwashinda, mpaka kwamba walirejea kwenye nchi zao tena.
8 Na katika mwaka wa mia tatu na sitini na mbili walikuja chini tena kupigana. Na
tuliwashinda tena, na kuchinja idadi yao kubwa, na wafu wao walitupwa baharini.
9 Na sasa, kwa sababu ya kitu hiki kikubwa ambacho watu wangu, Wanefi,
walikuwa wamefanya, walianza kujisifu kwa nguvu zao, na walianza kuapa kwa
mbingu kwamba watajilipizia kisasi kwa damu ya ndugu zao ambao walikuwa
wameuawa na maadui zao.
10 Na waliapa kwa mbingu, na pia kwa kiti cha enzi cha Mungu, kwamba wataenda
juu kupigana dhidi ya maadui zao, na kuwaangamiza kabisa kutoka uso wa nchi.

11 Na ikawa kwamba mimi, Mormoni, nilikataa kabisa kutokea wakati huu kwenda mbele kuwa amiri jeshi na kiongozi wa hawa watu, kwa sababu ya uovu wao na machukizo yao.
12 Tazama, nilikuwa nimewaongoza, ijapokuwa uovu wao, nilikuwa nimewaongoza mara nyingi vitani, na niliwapenda, kulingana na upendo wa Mungu ambao ulikuwa ndani yangu, na moyo wangu wote; na nafsi yangu ilikuwa imewekwa kwa sala kwa Mungu wangu siku yote nzima kwa ajili yao; walakini, ilikuwa bila imani, kwa sababu ya kushupaza mioyo yao.
13 Na mara tatu nimewaokoa kutoka mikononi mwa maadui zao, na hawajatubu dhambi zao.
14 Na baada ya kuapa na yote ambayo walikatazwa na Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo, kwamba wangeenda kwenye maadui wao ili wapigane, na kujilipizia kisasi kwa damu ya ndugu zao, tazama sauti ya Bwana ilinijia, ikisema:
15 Kulipiza kisasi ni kwangu, na nitalipa; na kwa sababu hawa watu hawakutubu baada ya mimi kuwakomboa, tazama, wataangamizwa kutoka kwa uso wa dunia.
16 Na ikawa kwamba nilikataa kabisa kwenda juu dhidi ya maadui zangu; na nilifanya hata vile Bwana alivyoniamuru; na nilisimama kama shahidi mzembe kushuhudia kwa ulimwengu vitu ambavyo niliona na kusikia, kulingana na ushuhuda wa Roho ambayo ilikuwa imeshuhudia kwa vitu vijavyo.
17 Kwa hivyo naandika kwenu, Wayunani, na pia kwenu, nyumba ya Israeli, wakati kazi itakapoanza, kwamba mtakuwa karibu kujitayarisha kurudi kwenye nchi ya urithi wenu;
18 Ndio, tazama, nawaandikia wote wanaoishi ulimwenguni; ndio, kwenu, makabila kumi na mawili ya Israeli, ambao mtahukumiwa kwa vitendo vyenu na wale kumi na wawili ambao Yesu aliwachagua kuwa wanafunzi wake katika nchi ya Yerusalemu.
19 Na pia nawaandikia sazo la watu hawa, ambao pia watahukumiwa na wale kumi na wawili ambao Yesu aliwachagua katika nchi hii; na watahukumiwa na wale kumi na wawili ambao Yesu aliwachagua katika nchi ya Yerusalemu.
20 Na vitu hivi Roho inanifichulia; kwa hivyo ninawaandikia nyinyi nyote. Na kwa sababu hii ninaandika kwenu, ili mjue kwamba lazima nyote msimame mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ndio, kila nafsi ambayo ni ya ukoo wa mwanadamu ya Adamu; na lazima msimame kuhukumiwa kwa yale mmetenda, ikiwa yatakuwa mazuri au maovu;
21 Na pia kwamba mngeamini injili ya Yesu Kristo, ambayo mtapata miongoni mwenu; na pia kwamba Wayahudi, watu wa agano la Bwana, watakuwa na ushahidi mwingine juu ya yule ambaye wamemwona na kumsikiliza, kwamba Yesu, ambaye walimuua, alikuwa ni Kristo yule yule na Mungu yule yule.
22 Na ningetaka kwamba ningeshawishi kila mtu aishiye duniani atubu na ajitayarishe kusimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.

## Mormoni 4

1 Na sasa ikawa kwamba katika mwaka wa mia tatu na sitini na tatu Wanefi walienda na majeshi yao kupigana dhidi ya Walamani, kutoka nchi ya Ukiwa.
2 Na ikawa kwamba majeshi ya Wanefi yalilazimishwa kurudi nyuma hadi kwenye nchi ya Ukiwa. Na wakati walikuwa bado wamechoka, jeshi lenye nguvu la Walamani liliwashambulia; na walikuwa na vita vibaya, mpaka kwamba Walamani

walimiliki mji wa Ukiwa, na waliwachinja Wanefi wengi, na walichukua wengi wao
kuwa wafungwa.
3 Na waliosalia walikimbia na kujiunga na wakazi wa mji wa Teankumu. Sasa mji
wa Teankumu ulikuwa kwenye mipaka ya ukingo wa bahari; na ulikuwa pia karibu
na mji wa Ukiwa.
4 Na ilikuwa kwa sababu jeshi la Wanefi lilishambulia Walamani kwamba walianza
kuuawa; kwani kama hawangefanya hivyo, Walamani hawangekuwa na uwezo juu
yao.
5 Lakini, tazama, hukumu za Mungu zitashinda uovu; na ni kwa kupitia kwa
waovu kwamba waovu huadhibiwa; kwani ni waovu ambao huchochea mioyo ya
watoto wa watu hadi kwenye umwagaji wa damu.
6 Na ikawa kwamba Walamani walifanya mipango ya kushambulia mji wa
Teankumu.
7 Na ikawa katika mwaka wa mia tatu na sitini na nne Walamani walishambulia
mji wa Teankumu, ili wamiliki mji wa Teankumu pia.
8 Na ikawa kwamba walisukumwa na kurudishwa nyuma na Wanefi. Na baada ya
Wanefi kuona kwamba wamewakimbiza Walamani walijisifu tena kwa nguvu zao;
na wakaenda mbele na uwezo wao wenyewe, na kukamata tena mji wa Ukiwa.
9 Na sasa vitu hivi vyote vilikuwa vimefanyika, na kulikuwa na maelfu waliouawa
kwa pande zote mbili, miongoni mwa Wanefi na miongoni mwa Walamani.
10 Na ikawa kwamba mwaka wa mia tatu na ishirini na sita ukawa umepita, na
Walamani walikuja tena kwa Wanefi ili wapigane; na bado Wanefi hawakutubu kwa
maovu waliyotenda, lakini waliendelea na maovu yao siku zote.
11 Na ni vigumu kwa ulimi kueleza, au kwa mtu kuandika maelezo kamili ya hofu
iliyoonekana ya damu na mauaji ambayo yalikuwa miongoni mwa watu, upande wa
Wanefi na upande wa Walamani, na kila moyo ulishupazwa, kwamba walifurahia
umwagaji wa damu siku zote.
12 Na kulikuwa hakujakuwa na uovu mkuu kama huu miongoni mwa kizazi cha
Lehi, wala hata miongoni mwa nyumba ya Israeli, kulingana na maneno ya Bwana,
vile ilipokuwa miongoni mwa watu hawa.
13 Na ikawa kwamba Walamani walimiliki mji wa Ukiwa, na hii ni kwa sababu
idadi yao ilizidi ya Wanefi.
14 Na walisonga mbele pia dhidi ya mji wa Teankumu, na kulazimisha wakazi wake
kuondoka nje, na wakachukua wafungwa wengi wanawake pamoja na watoto, na
kuwaua kama kafara kwa sanamu zao za kuabudu.
15 Na ikawa kwamba katika mwaka wa mia tatu na sitini na saba, Wanefi wakiwa
wamekasirika kwa sababu ya Walamani kutoa kafara wake zao na watoto wao,
kwamba walienda dhidi ya Walamani kwa hasira kubwa sana, hadi kwamba
waliwapiga Walamani tena, na kuwafukuza kutoka nchi zao.
16 Na Walamani hawakuwashambulia Wanefi mpaka mwaka wa mia tatu na sabini
na tano.
17 Na katika mwaka huu walikuja chini dhidi ya Wanefi kwa uwezo wao wote; na
hawangehesabika kwa sababu ya ukubwa wa idadi yao.
18 Na kutokea wakati huu kwenda mbele Wanefi hawakuwa na uwezo wowote juu
ya Walamani, lakini walianza kuangamizwa na hao vile umande huwa mbele ya jua.
19 Na ikawa kwamba Walamani walishambulia mji wa Ukiwa; na kukawa na vita
vikali sana vilivyopiganwa katika nchi ya Ukiwa, ambamo walishinda Wanefi.

20 Na walitoroka tena kutoka kwao, na kufikia mji wa Boazi; na hapo walizuia
Walamani kwa ujasiri mkubwa, mpaka kwamba Walamani hawakushinda mpaka
waliporudi tena mara ya pili.
21 Na baada ya kurudi mara ya pili, Wanefi walikimbizwa na kuchinjwa na mauaji
makuu; wanawake wao na watoto wao walitolewa kafara tena kwa sanamu.
22 Na ikawa kwamba Wanefi walikimbia tena kutoka kwao, na wakasababisha
wakazi wote kuandamana nao kote, mijini na vijijini.
23 Na sasa mimi, Mormoni, nilipoona kwamba Walamani wako karibu kuchukua
nchi, kwa hivyo nilienda kwenye kilima cha Shimu, na kuyachukua maandishi yote
ambayo Amaroni alikuwa ameyaficha kwa Bwana.

## Mormoni 5

1 Na ikawa kwamba nilienda mbele miongoni mwa Wanefi, na kugeuza kile kiapo
ambacho nilikuwa nimefanya kwamba sitawasaidia; na wakanifanya amiri jeshi tena
wa majeshi yao, kwani walinitazamia kama ningewakomboa kutoka kwa mateso yao.
2 Lakini tazama, sikuwa na tumaini, kwani nilijua hukumu ya Bwana ambayo
ingewajia; kwani hawakutubu uovu wao, lakini walipigania maisha yao bila
kumlingana yule ambaye kiliwaumba.
3 Na ikawa kwamba Walamani walitushambulia vile tulivyokuwa tumekimbilia
mji wa Yordani; lakini tazama, walifukuzwa na kurudishwa nyuma kwamba
hawakukamata ule mji wakati huo.
4 Na ikawa kwamba walitushambulia tena, na tulihifadhi mji. Na kulikuwa na miji
mingine pia ambayo ilihifadhiwa na Wanefi, ambayo ngome zao ziliwazuilia mbali
kwamba hawangeingia nchi ambayo ilikuwa mbele yetu, ili wawaangamize wakazi
wa nchi yetu.
5 Lakini ikawa kwamba nchi yoyote ambayo tulipitia karibu, ambayo wakazi
hawakuwa wamejiunga nasi, waliangamizwa na Walamani, na miji yao, na vijiji vyao,
na miji yao mikuu ilichomwa kwa moto; na hivyo miaka mia tatu na sabini na tisa
ilipita mbali.
6 Na ikawa kwamba katika mwaka wa mia tatu na themanini Walamani walikuja
tena dhidi yetu ili kupigana, na tuliwazuia kwa ujasiri; lakini yote ilikuwa bure,
kwani idadi yao ilikuwa kubwa sana kwamba waliwakanyaga watu wa Wanefi chini
ya miguu yao.
7 Na ikawa kwamba tulikimbia tena, na wale ambao ukimbizi wao ulikuwa wa
upesi kuliko Walamani waliokoka, na wale ambao ukimbizi wao haukushinda
Walamani walikatiwa chini na kuangamizwa.
8 Na sasa tazama, mimi, Mormoni, sitaki kuharibu roho za watu kwa kuwaelezea
mambo ya kutisha ya damu na mauaji kama ilivyoonekana machoni mwangu; lakini
mimi, nikijua kwamba vitu hivi lazima vidhihirishwe kujulikana, na kwamba vitu
vyote ambavyo vimefichwa lazima vifichuliwe wazi—
9 Na pia kwamba ufahamu wa vitu hivi lazima ujie sazo la watu hawa, na pia kwa
Wayunani, ambao Bwana amesema watawatawanya hawa watu, na watu hawa
wahesabiwe kama bure miongoni mwao—kwa hivyo naandika ufupisho mdogo,
bila ya kuthubutu kutoa historia ya vitu ambavyo nimeona, kwa sababu ya amri
ambayo nimepokea, na pia kwamba msiwe na huzuni nyingi sana kwa sababu ya
uovu wa watu hawa.

10 Na sasa tazama, haya ninaizungumzia uzao wao, na pia kwa Wayunani ambao watakuwa na utunzaji kwa nyumba ya Israeli, ambao wanafahamu na kujua ni wapi baraka zao hutoka.
11 Kwani ninajua kwamba hao watahuzunika kwa msiba wa nyumba ya Israeli; ndio, watahuzunika kwa uharibifu wa hawa watu; watahuzunika kwamba watu hawa walikuwa hawajatubu ili wangekumbatiwa katika mikono ya Yesu.
12 Sasa vitu hivi vimeandikiwa sazo la nyumba ya Yakobo; na vimeandikwa kwa njia hii, kwa sababu inafichuliwa kutoka kwa Mungu kwamba hawatajua kupitia kwa maovu; na sharti zifichwe kwa Bwana ili zije mbele katika muda wao.
13 Na hii ni amri ambayo nimepokea; na tazama, vitakuja mbele kulingana na amri ya Bwana, wakati ataona inafaa, katika hekima yake.
14 Na tazama, vitaenda kwa wale Wayahudi wasioamini; na kwa kusudi hili wataenda — ili washawishwe kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu aishiye; kwamba Baba angetimiza, kupitia kwa Mpendwa wake, mpango wake mkuu na wa milele, kwa kuwarudisha Wayahudi, au nyumba yote ya Israeli, kwa nchi yao ya urithi, ambayo Bwana Mungu wao amewapatia, kwa kutimiza agano lake;
15 Na pia kwamba uzao wa watu hawa ungeamini kabisa injili yake, ambayo itaenda mbele yao kutoka kwa Wayunani; kwani hawa watu watatawanywa, na watakuwa weusi, wachafu, na watu wa kuchukiza, nje ya mipaka ya maelezo ambayo yamewahi kuweko miongoni mwetu, ndio, hata ile ambayo imekuweko miongoni mwa Walamani, na hii ni kwa sababu ya kutoamini kwao na ibada ya sanamu.
16 Kwani tazama, Roho ya Bwana imekoma kuwasaidia babu zao; na wako bila Kristo na Mungu katika ulimwengu; na wanapeperushwa kama vumbi litimuliwalo mbele ya kibunga.
17 Walikuwa wakati mmoja watu wa kupendeza, na walikuwa na Kristo kama mchungaji wao; ndio, walikuwa wanaongozwa hata na Mungu Baba.
18 Lakini sasa, tazama, wanaongozwa na Shetani, hata vile vumbi litimuliwalo mbele ya kimbunga, au vile jahazi linavyorushwarushwa juu ya mawimbi, bila tanga wala nanga, au bila kitu chochote cha kuiendesha; na vile ilivyo, ndivyo walivyo.
19 Na tazama Bwana amewawekea baraka, ambazo wangepokea katika nchi, kwa Wayunani ndio watakaoimiliki nchi.
20 Lakini tazama, itakuwa kwamba watakimbizwa na kutawanywa na Wayunani; na baada ya kukimbizwa na kutawanywa na Wayunani, tazama, ndipo Bwana atakumbuka agano ambalo alifanya kwa Ibrahimu na kwenye nyumba yote ya Israeli.
21 Na pia Bwana atakumbuka sala za wenye haki, ambazo zimetolewa kwake kwa minajili yao.
22 Na ikiwa hivyo, Ee nyinyi Wayunani, mtawezaje kusimama mbele ya uwezo wa Mungu, isipokuwa mtubu na kugeuka kutoka njia zenu mbovu?
23 Je, hamjui kwamba mko mikononi mwa Mungu? Je, hamjui kwamba anao uwezo wote, na kwa amri yake kuu dunia itakunjwa pamoja kama karatasi?
24 Kwa hivyo, tubuni nyinyi, na mjinyenyekeze mbele yake, isije, atakuja nje katika haki dhidi yenu — isije sazo la uzao wa Yakobo itaenda mbele miongoni mwenu kama simba, na kuwararua vipande vipande, na hakuna atakayewaokoa.

# Mormoni 6

1 Na sasa ninamaliza maandishi yangu kuhusu kuangamizwa kwa watu wangu,
Wanefi. Na ikawa kwamba tulienda kutoka mbele ya Walamani.
2 Na mimi, Mormoni, niliandika barua kwa mfalme wa Walamani, na kumwuliza
kwamba angetukubalia kwamba tukusanye watu wetu pamoja kwenye nchi ya
Kumora, kando na kilima kilichoitwa Kumora, na hapo tungepigana nao.
3 Na ikawa kwamba mfalme wa Walamani alinikubalia kitu ambacho nilitaka.
4 Na ikawa kwamba tulienda mbele hadi kwenye nchi ya Kumora, na tukapiga
hema zetu kuzunguka karibu na kilima Kumora; na ilikuwa katika nchi ya maji
mengi, mito, na visima; na hapa tulikuwa na tumaini la kufaidika juu ya Walamani.
5 Na baada ya miaka mia tatu na themanini na nne kupita, tulikuwa tumekusanya
watu wote waliosalia kwenye nchi ya Kumora.
6 Na ikawa kwamba baada ya kuwakusanya watu wetu wote pamoja katika nchi ya
Kumora, tazama mimi, Mormoni, nilianza kuzeeka; na nikijua kwamba ni juhudi ya
mwisho ya watu wangu, na nikiwa nimeamriwa na Bwana kwamba nisiyaache
maandishi ambayo yametolewa kutoka zamani na babu zetu, ambayo ni matakatifu,
kuchukuliwa na Walamani, (kwani Walamani wangeyaharibu) kwa hivyo
nilitengeneza haya maandishi kutoka kwenye bamba za Nefi, na nikayaficha katika
kilima cha Kumora maandishi yote ambayo yalikuwa yamekabidhiwa kwangu na
mkono wa Bwana, isipokuwa hizi bamba chache ambazo nilimpatia mwana wangu
Moroni.
7 Na ikawa kwamba watu wangu, na wake zao na watoto wao, sasa waliona majeshi
ya Walamani yakisonga kuwaelekea; na kwa ule woga wa kutisha wa kifo ambao
unajaa vifua vya waovu wote, walingoja washambuliwe.
8 Na ikawa kwamba walikuja kupigana dhidi yetu, na kila nafsi ilijawa na hofu kwa
sababu ya wingi wa idadi yao.
9 Na ikawa kwamba walishambulia watu wangu kwa panga, na kwa pinde, na kwa
mshale, na kwa shoka, na kwa kila aina ya silaha za vita.
10 Na ikawa kwamba watu wangu waliangushwa chini, ndio, hata elfu wangu kumi
ambao walikuwa na mimi, na nilijeruhiwa nikaanguka katikati; na walipita kando
yangu kwamba hawakumaliza maisha yangu.
11 Na baada ya kupita na kuangusha chini watu wangu wote isipokuwa sisi ishirini
na wanne, (miongoni ambamo kulikuwa na mwana wangu Moroni) na sisi tukiwa
tumenusurika kifo cha watu wetu, tulitazamia kesho yake baada ya Walamani
kurudi kwenye vituo vyao, kutoka juu ya kilima Kumora, wale watu wangu elfu
kumi ambao waliangushwa chini, wakiwa wameongozwa mbele na mimi.
12 Na pia tuliona wale elfu kumi ambao waliongozwa na mwana wangu Moroni.
13 Na tazama, elfu kumi wa Gidgidona walikuwa wameanguka, na yeye pia akiwa
katikati.
14 Na Lama alikuwa ameanguka na wale wake elfu kumi; na Gilgali alikuwa
ameanguka na wale wake elfu kumi; na Limha alikuwa ameanguka na wale wake
elfu kumi; na Yeneumu alikuwa ameanguka na wale wake elfu kumi; na Kumeniha,
na Moroniha, na Antionumu, na Shiblomu, na Shemu, na Yoshi, walikuwa
wameanguka kila mmoja na wale wao elfu kumi.
15 Na ikawa kwamba kulikuwa na kumi zaidi walioanguka kwa upanga, kila mmoja
na elfu kumi wao; ndio, hata watu wangu wote, isipokuwa wale ishirini na wanne
waliokuwa na mimi, na pia wachache waliotorokea nchi za kusini, na wachache

ambao walikimbia hadi kwa Walamani, walikuwa wameanguka; na miili yao, na
mifupa, na damu vilitapakaa juu ya uso wa nchi, wakiwa wameachwa na wale ambao
waliwachinja kuozea juu ya udongo, na kugeuka mavumbi na kurudi kwenye
udongo walikotoka.
16 Na nafsi yangu ilipasuka kwa uchungu, kwa sababu ya mauaji ya watu wangu, na
nililia:
17 Ee nyinyi wenye umbo nzuri, ilikuwaje mkatoka kwenye njia ya Bwana! Ee
nyinyi wenye umbo nzuri, ilikuwaje mkamkataa Yesu, ambaye aliwangojea na
mikono wazi kuwapokea!
18 Tazama, kama hamngefanya hivi, hamngekufa. Lakini tazama, mmekufa, na
ninaomboleza kupotea kwenu.
19 Ee nyinyi wana wa umbo nzuri, nyinyi baba na mama, nyinyi mabwana na wake,
nyinyi walio wazuri, vipi kwamba mmekufa!
20 Lakini tazama, mmetokomea, na huzuni yangu haiwezi kuwarejesha.
21 Na wakati unakuja upesi kwamba miili yenu yenye kufa itajivika kutokufa, na
miili hii ambayo sasa inaoza kimwili lazima upesi itakuwa isiyooza; na hapo lazima
mtasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, kuhukumiwa kulingana na
vitendo vyenu; na ikiwa kwamba nyinyi ni wenye haki, hasi mmebarikiwa na babu
zenu ambao wamekufa mbele yenu.
22 Ee ingekuwa kwamba mlitubu kabla ya hili angamizo kuja kwenu. Lakini
tazama, mmekufa, na Baba, ndio, Baba wa Milele wa mbinguni, anajua hali zenu; na
anawafanyia kulingana na haki na rehema yake.

# Mormoni 7

1 Na sasa, tazama, nataka kuzungumza machache kwa sazo la watu hawa ambao
wameachiliwa, ikiwa Mungu atawapatia maneno yangu, ili wajue kuhusu vitu vya
baba zao; ndio, ninawazungumzia, nyinyi sazo la nyumba ya Israeli; na haya ndiyo
maneno ambayo ninasema:
2 Nataka mjue kwamba nyinyi ni wa nyumba ya Israeli.
3 Nataka mjue kwamba lazima mtubu, au hamtaokolewa.
4 Nataka mjue kwamba lazima muweke chini silaha za vita, na msifurahie tena
katika umwagaji wa damu, na msizichukue tena, isipokuwa kama Mungu
atawaamuru.
5 Nataka mjue kwamba lazima muelimike kuhusu babu zenu, na mtubu dhambi
zenu zote na maovu, na kuamini katika Yesu Kristo, kwamba yeye ni Mwana wa
Mungu, na kwamba aliuawa na Wayahudi, na kwa uwezo wa Baba amefufuka tena,
kwa kufanya hivyo amepata ushindi juu ya mauti; na pia kupitia kwake uchungu wa
kifo umetolewa.
6 Na anatimiza ufufuo wa wafu, ambako binadamu lazima atainuliwa kusimama
mbele ya kiti cha hukumu.
7 Na ameleta kutimizwa ukombozi wa ulimwengu, ambako yule ambaye
atapatikana bila makosa mbele yake katika siku ya hukumu atakubaliwa kuishi
kwenye uwepo wa Mungu katika ufalme wake, kuimba sifa zisizo na mwisho na
jamii ya waimbaji wa juu, kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu,
ambao ni Mungu mmoja, katika hali ya furaha ambayo haina mwisho.
8 Kwa hivyo tubuni, na mbatizwe katika jina la Yesu, na mkubali injili ya Kristo,

ambayo itawekwa mbele yenu, sio tu kwa maandishi haya lakini pia kwa maandishi
ambayo yatawajia Wayunani kutoka kwa Wayahudi, maandishi ambayo yatatoka
kwa Wayunani hadi kwenu.
9 Kwani tazama, haya yameandikwa kwa kusudi kwamba mngeamini hayo; na
mkiyaamini hayo mtaamini haya pia; na ikiwa mtaamini haya mtajua kuhusu babu
zenu, na pia kazi za ajabu ambazo zimesababishwa na uwezo wa Mungu miongoni
mwao.
10 Na mtajua pia kwamba nyinyi ni sazo la uzao wa Yakobo; kwa hivyo
mmehesabiwa miongoni mwa watu wa agano la kwanza; na ikiwa itakuwa hivyo
kwamba mtaamini katika Kristo, na mnabatizwa, kwanza kwa maji, halafu kwa
moto na Roho Mtakatifu, mkifuata mfano wa Mwokozi wetu, kulingana na
alivyotuamuru, itakuwa vema nanyi katika ile siku ya hukumu. Amina.

## Mormoni 8

1 Tazama mimi, Moroni, ninamaliza maandishi ya baba yangu, Mormoni. Tazama,
nina vitu vichache tu vya kuandika, vitu ambavyo nimeamriwa na baba yangu.
2 Na sasa ikawa kwamba baada ya vita kubwa na vya kutisha katika Kumora,
tazama, Wanefi ambao walitorokea katika nchi ya kusini waliwindwa na Walamani,
mpaka wote walipoangamizwa.
3 Na baba yangu pia aliuawa na hao, na ni mimi tu nimebaki peke yangu kuandika
kisa cha kuhuzunisha cha kuangamizwa kwa watu wangu. Lakini tazama,
wameenda, na ninatimiza amri ya baba yangu. Na ikiwa wataniua, sijui.
4 Kwa hivyo nitaandika na kuficha maandiko katika ardhi; na haijalishi popote
nitakapoenda.
5 Tazama, baba yangu alibuni haya maandishi, na ameandika kusudi la kufanya
hivyo. Na tazama, ningeyaandika pia ikiwa ningekuwa na nafasi kwenye bamba,
lakini sina; na mawe ya madini sina hata moja, kwani niko peke yangu. Baba yangu
ameuawa vitani, na ukoo wangu wote, na sina marafiki wala popote pa kwenda; na
kwa muda gani Bwana atanikubalia kwamba niishi sijui.
6 Tazama, miaka mia nne imepita tangu kuja kwa Bwana na Mwokozi wetu.
7 Na tazama, Walamani wamewawinda watu wangu, Wanefi, kutoka mji hadi mji
na kutoka mahali hadi pengine, mpaka kwamba hawako tena; na mwanguko wao
umekuwa mkubwa; ndio, mkubwa na wa kustaajabisha ni kuangamizwa kwa watu
wangu, Wanefi.
8 Na tazama, ni mkono wa Bwana ambao umeifanya. Na tazama pia, Walamani
wako vitani wenyewe kwa wenyewe; na uso wote wa nchi hii daima ni mviringo wa
mauaji na umwagaji wa damu; na hakuna yeyote ajuaye mwisho wa vita.
9 Na sasa tazama, sisemi mengi kuhusu hao, kwani hakuna yeyote isipokuwa
Walamani na wanyang'anyi ambao wako kote usoni mwa nchi.
10 Na hakuna yeyote anayemjua Mungu wa kweli isipokuwa wanafunzi wa Yesu,
ambao walibaki katika nchi mpaka uovu wa watu ulipokuwa mwingi sana kwamba
Bwana hakukubalia wabaki na watu; na ikiwa wako juu ya uso wa dunia hakuna mtu
ajuaye.
11 Lakini tazama, baba yangu na mimi tumewaona, na wametuhubiria.
12 Na yeyote atakayepokea haya maandiko, na akose kuyalaumu kwa sababu ya
makosa yaliyomo, basi huyo huyo atajua vitu vikubwa kuliko hivi. Tazama, mimi ni

Moroni; na kama ingewezekana, ningefanya vitu vyote kujulikana kwenu.
13 Tazama, namaliza kuongea kuhusu watu hawa. Mimi ni mwana wa Mormoni, na
baba yangu alikuwa uzao wa Nefi.
14 Na mimi ni yule anayeficha haya maandishi kwa ulinzi wa Bwana; bamba
zilizoko hazina thamani, kwa sababu ya amri ya Bwana. Kwani alisema hakuna
atakayeyapokea kwa faida; lakini maandiko yaliyoko ni ya thamani kubwa; na
yeyote atakayeyadhihirisha, yeye Bwana atambariki.
15 Kwani hakuna aliye na uwezo wa kuyadhihirisha isipokuwa akabidhiwe na
Mungu; kwani Mungu hupendelea kwamba itafanyika jicho likiwa kwa utukufu
wake, au kwa ustawi wa wale wa kale na watu wa agano la Bwana waliotawanywa.
16 Na atabarikiwa yule ambaye atadhihirisha kitu hiki; kwani kitaletwa kutoka
gizani hadi kwenye mwangaza, kulingana na neno la Mungu; ndio, kitaletwa kutoka
udongoni, na kitatoa nuru kutoka gizani, na ije kwa ufahamu wa watu; na itafanyika
kwa uwezo wa Mungu.
17 Na ikiwa kutakuwa na makosa, yatakuwa ni makosa ya binadamu. Lakini tazama,
hatujui kosa lolote; walakini Mungu anajua vitu vyote; kwa hivyo, yeyote ambaye
analaumu, acha ajihadhari asije akawa kwenye hatari ya moto wa jahanamu.
18 Na yule anayesema: Nionyeshe, au utauawa — acha ajihadhari asije akaamrisha
ile ambayo imekatazwa na Bwana.
19 Kwani tazama, yule anayetoa hukumu kwa haraka atahukumiwa kwa haraka
tena; kwani kulingana na vitendo vyake, mshahara wake utakuwa hivyo; kwa hivyo
yule ambaye huua atauawa tena, na Bwana.
20 Tazama maandiko husema nini — mtu hataua, wala hatahukumu; kwani hukumu
ni yangu, asema Bwana, na kisasi ni changu pia, na nitalipiza.
21 Na yule atakayetoa nje ghadhabu na ugomvi dhidi ya kazi ya Bwana, na dhidi ya
watu wa agano wa Bwana ambao ni wa nyumba ya Israeli, ambaye atasema:
Tutaangamiza kazi ya Bwana, na Bwana hatakumbuka agano lake ambalo amefanya
kwa nyumba ya Israeli — yule yule yuko hatarini kukatiwa chini na kutupwa motoni;
22 Kwani kusudi la milele la Bwana litaendelea, mpaka ahadi zake zote
zitakapotimizwa.
23 Pekua unabii wa Isaya. Tazama, siwezi kuyaandika. Ndio, tazama ninawaambia,
kwamba wale watakatifu ambao wameenda kabla yangu, ambao walimiliki hii nchi,
watalia, ndio, hata kutoka kwenye mavumbi watamlilia Bwana; na vile Bwana
anavyoishi atakumbuka agano ambalo amefanya nao.
24 Na hujua sala zao, kwamba zilikuwa kwa niaba ya ndugu zao. Na hujua imani
yao, kwani katika jina lake wangeondoa milima, na katika jina lake wangesababisha
ardhi kutetemeka; na kwa uwezo wa neno lake walisababisha magereza kuanguka
ardhini; ndio, hata kalibu ya moto mkali haingewaumiza, wala wanyama wa mwitu,
wala nyoka wa sumu, kwa sababu ya uwezo wa neno lake.
25 Na tazama, sala zao pia zilikuwa kwa niaba ya yule ambaye Bwana atakubalia
kuleta vitu hivi mbele.
26 Na hakuna yeyote aliye na sababu ya kusema havitakuja, kwani kwa kweli
vitakuja, kwani Bwana ameinena; kwani vitatoka kutoka kwa ardhi, kwa uwezo wa
Bwana, na hakuna atakayeizuia; na itakuja katika ile siku wakati itasemekana
kwamba miujiza imeondolewa; na itatendeka hata kama vile mmoja
anayezungumza kutoka kwa wafu.
27 Na itakuja katika siku ile ambayo damu ya watakatifu itakapolia kwa Bwana, kwa

sababu ya makundi maovu ya siri na kazi za gizani.
28 Ndio, itakuja katika siku wakati uwezo wa Mungu utakataliwa, na makanisa
yatakuwa yamechafuliwa na kujiinua kwa kiburi cha mioyo yao; ndio, hata katika
siku ambayo viongozi wa makanisa na walimu watajiinua kwa kiburi cha mioyo yao,
hata kuwaonea wivu wale ambao wako kwa makanisa yao.
29 Ndio, itakuja katika ile siku wakati kutasikika moto, na tufani, na mivuke ya
moshi katika nchi za kigeni;
30 Na pia kutasikika mambo ya vita, uvumi wa vita na mitetemeko mahali mbali
mbali.
31 Ndio, itakuja katika ile siku wakati kutakuweko uchafu mwingi juu ya uso wa
dunia; kutakuwa na mauaji, na unyang'anyi, na udanganyifu, na ulaghai, na ukahaba,
na kila aina ya machukizo; wakati kutakuwa na wengi ambao watasema, Fanya hivi,
au fanye vile, na haijalishi, kwani Bwana ataokoa hawa katika siku ya mwisho. Lakini
ole kwa hao, kwani wako kwenye nyongo ya uchungu na katika kifungo cha uovu.
32 Ndio, itakuja wakati kutakuwa na makanisa yatakayojengwa ambayo yatasema:
Kuja kwangu, na kwa pesa yako utasamehewa dhambi zako.
33 Ee nyinyi walio waovu na wapotevu na watu wenye shingo ngumu, kwa nini
mmejijengea makanisa kwa kupata faida? Kwa nini mmegeuza neno takatifu la
Mungu, kwamba kwa kufanya hivyo mjiletee lawama kwenye nafsi zenu? Tazama,
tegemeeni unabii wa Mungu; kwani tazameni, wakati unawadia katika siku hiyo
wakati vitu hivi vyote lazima vitimizwe.
34 Tazama, Bwana amenionyesha vitu vikubwa na vya ajabu kuhusu ile ambayo
lazima itokee hivi karibuni, katika siku ile ambayo vitu hivi vitatokea mbele
miongoni mwenu.
35 Tazama, ninawazungumzia kama vile mko hapa, lakini hamko. Lakini tazama,
Yesu Kristo amenionyesha nyinyi kwangu, na ninajua yale mnayofanya.
36 Na ninajua kwamba mnaishi kwa kiburi cha mioyo yenu; na hakuna mmoja
isipokuwa wachache ambao hawajiinui katika kiburi cha mioyo yao, kwa kuvaa nguo
nzuri sana, kusababisha wivu, na ugomvi, na mabishano, na dhuluma, na aina yote
ya maovu; na makanisa yenu, ndio, hata kila moja, yamechafuliwa kwa sababu ya
kiburi cha mioyo yenu.
37 Kwani tazama, mnapenda pesa, na vitu vyenu, na mavazi yenu mazuri, na
kupambwa kwa makanisa yenu, kuliko mnavyowapenda maskini, na wanaohitaji
msaada, wagonjwa na wanaoteseka.
38 Ee nyinyi wachafu, nyinyi wanafiki, nyinyi walimu, ambao mnajiuza kwa kile
ambacho kitaoza, kwa nini mmechafua kanisa takakatifu la Mungu? Kwa nini
mnaaibika kujivika jina la Kristo? Kwa nini hamfikirii kwamba kubwa zaidi ni
thamani ya furaha ya milele isiyo na kikomo kuliko ile taabu ambayo haiishi
kamwe—kwa sababu ya sifa ya ulimwengu?
39 Kwa nini mnajipamba na vitu visivyo na uhai, na bado mnawaachilia wenye njaa,
na wanaohitaji, na walio uchi, na wagonjwa na wanaoteseka kupita kando yenu, na
mnajifanya hamuwaoni?
40 Ndio, kwa nini mnaanzisha makundi mabaya ya siri kwa kupata faida, na
kusababisha wajane kuomboleza mbele ya Bwana, na pia mayatima kuombeleza
mbele ya Bwana, na pia damu ya babu zao na bwana zao kulia kwa Bwana kutoka
chini, kwa kisasi juu ya vichwa vyenu?
41 Tazama, upanga wa kisasi unaning'inia juu yenu; na wakati unatimia mapema

kwamba atalipiza kisasi cha damu ya wale watakatifu juu yenu, kwani hatavumilia kulia kwao tena.

## Mormoni 9

1 Na sasa, ninazungumza pia kuhusu wale ambao hawaamini katika Kristo.
2 Tazama, mtaamini katika siku ya hukumu yenu — tazama, wakati Bwana
atakapokuja, ndio, hata ile siku kuu wakati dunia itakunjwa pamoja kama karatasi,
na vitu vya asili vitayeyuka kwa joto kubwa, ndio, katika siku ile kuu wakati
mtaletwa kusimama mbele ya Mwanakondoo wa Mungu — ndipo mtasema kwamba
hakuna Mungu?
3 Ndipo mtaendelea kumkana Kristo, au mnaweza kumtazama Mwanakondoo wa
Mungu? Mnadhani kwamba mtaishi na yeye chini ya ufahamu wa makosa yenu?
Mnadhani ya kwamba mngekuwa na furaha kuishi na kile Kiumbe kitakatifu,
wakati nafsi zenu zina msukosuko na ufahamu wa makosa kwamba daima mmetusi
sheria zake?
4 Tazama, ninawaambia kwamba mtakuwa na taabu sana kuishi na Mungu aliye
mtakatifu na wa haki, chini ya ufahamu wa uchafu wenu mbele yake, kuliko kuishi
na nafsi zilizolaaniwa katika jahanamu.
5 Kwani tazama, wakati mtaletwa kuona uchi wenu mbele ya Mungu, na pia
utukufu wa Mungu, na utakatifu wa Yesu Kristo, itawasha ulimi wa moto
usiozimika juu yenu.
6 Ee basi nyinyi msioamini, mgeukieni Bwana; lieni kwa Baba kwa nguvu katika
jina la Yesu, kwamba pengine mpatikane bila waa, safi, warembo, na weupe, mkiwa
mmeoshwa na damu ya Mwanakondoo, katika ile siku kuu na ya mwisho.
7 Na tena ninawazungumzia nyinyi ambao hukataa unabii wa Mungu, na kusema
kwamba haifanyiki tena, kwamba hakuna ufunuo, wala unabii, wala vipawa, wala
uponyaji, wala kuzungumza kwenye lugha za kigeni, na kutafsiri lugha;
8 Tazama nawaambia, yule anayekana vitu hivi hajui injili ya Kristo; ndio,
hajasoma maandiko; na ikiwa ameyasoma, hayaelewi.
9 Kwani si tunasoma kwamba Mungu ni yule yule jana, na leo, na hata milele, na
kwake hakuna kubadilika wala kivuli cha kugeukageuka?
10 Na sasa, kama mmejiwazia, mungu anayebadilika, na ambaye ana kivuli cha
kugeukageuka, aidha mmejidhania mungu ambaye si Mungu wa miujiza.
11 Lakini tazama, nitawaelezea Mungu wa miujiza, hata Mungu wa Ibrahimu, na
Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo; na yule yule Mungu aliyeumba mbingu na
dunia, na vitu vyote vilivyomo.
12 Tazama, alimuumba Adamu, na kupitia kwa Adamu kukatokea mwanguko wa
binadamu. Na kwa sababu ya mwanguko wa binadamu Yesu Kristo alikuja, ambaye
ni Baba na Mwana; na kwa sababu ya Yesu Kristo ukombozi wa binadamu ulitokea.
13 Na kwa sababu ya ukombozi wa binadamu, ambao ulifika kupitia kwa Yesu
Kristo, wanarudishwa kwenye uwepo wa Bwana; ndio, hii ndiyo njia ambayo kwake
watu wote wanakombolewa, kwa sababu kifo cha Kristo husababisha kutimizwa
kwa ufufuko, ambao husababisha kutimizwa kwa ukombozi kutoka kwa usingizi wa
milele, usingizi ambamo watu wote wataamshwa kwa uwezo wa Mungu wakati
tarumbeta itakapolia; na watatoka nje, wote wadogo na wakubwa, na wote
watasimama mbele ya hukumu yake, wakikombolewa na kufunguliwa kutoka

kwenye kamba hii ya kifo cha milele, kifo ambacho ni kifo cha mwili.
14 Na ndipo kutatukia hukumu ya Yule Mtakatifu juu yao; na ndipo kutatokea
wakati ambao yule ambaye ni mchafu ataendelea kuwa mchafu; na yule ambaye ni
mwenye haki ataendelea kuwa mwenye haki; yule ambaye ana furaha ataendelea
kuwa na furaha; na yule asiye na furaha ataendelea kuwa bila furaha.
15 Na sasa, Ee nyinyi nyote ambao mmejiwazia mungu ambaye hawezi kufanya
miujiza, ningewauliza, je, vitu hivi vyote ambavyo nimezungumzia, vimefanyika? Je,
mwisho umefika? Tazama nawaambia, Hapana; na Mungu hajakoma kuwa Mungu
wa miujiza.
16 Tazama, si vitu ambavyo Mungu amefanya ni vya ajabu machoni mwetu? Ndio,
na ni nani anayeweza kufahamu kazi za ajabu za Mungu?
17 Ni nani atasema kwamba haikuwa miujiza ambayo kwa neno lake mbingu na
dunia vipo; na kwa uwezo wa neno lake mtu aliumbwa kutoka kwa mavumbi ya
dunia; na kwa uwezo wa neno lake miujiza imefanyika?
18 Na ni nani atasema kwamba Yesu Kristo hakufanya miujiza mingi mikubwa? Na
kulikuwa na miujiza mingi mikubwa iliyofanywa na mitume.
19 Na ikiwa miujiza ilifanyika wakati huo, kwa nini Mungu amekoma kuwa Mungu
wa miujiza na bado awe kiumbe kisichobadilika? Na tazama, nawaambia habadiliki;
ikiwa hivyo angekoma kuwa Mungu; na hakomi kuwa Mungu, na ni Mungu wa
miujiza.
20 Na sababu ambayo inamfanya kukoma kufanya miujiza miongoni mwa watoto
wa watu ni kwa sababu kwamba wamefifia katika kutoamini, na kutoka kwa njia ya
kweli, na hawamjui Mungu ambaye wanapaswa kumwamini.
21 Tazama, ninawaambia kwamba yeyote aaminiye katika Kristo bila tashwishi,
chochote atakachomwomba Baba katika jina la Kristo kitatolewa kwake; na hii
ahadi iko kwa wote, hata mpaka mwisho wa dunia.
22 Kwani tazama, hivi anasema Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kwa wanafunzi
wake ambao watakawia, ndio, na pia kwa wanafunzi wake wote, kundi lilipokuwa
likisikiliza: Nendeni nyinyi katika ulimwengu wote, na mhubiri injili kwa kila mtu;
23 Na yule anayeamini na kubatizwa ataokolewa, lakini yule ambaye haamini
atalaaniwa;
24 Na hizi ishara zitafuatana nao ambao huamini — katika jina langu watawatupa
nje mashetani; watazungumza kwa lugha ngeni; watainua nyoka; na ikiwa
watakunywa kitu cha kuhatarisha hakitawadhuru; wataweka mikono yao kwa
wagonjwa na watapona;
25 Na yeyote atakayeamini katika jina langu, bila kuwa na shaka, kwake
nitamhakikishia maneno yangu yote, hata kwa sehemu zote za dunia.
26 Na sasa, tazama, ni nani anaweza kuzuia kazi ya Bwana? Ni nani anayeweza
kukana misemo yake? Ni nani atakayesimama dhidi ya uwezo usio na kipimo wa
Bwana? Ni nani atachukia kazi za Bwana? Ni nani atachukia watoto wa Kristo?
Tazama, nyote ambao mnachukia kazi za Bwana, kwani mtatangatanga na
kuangamia.
27 Ee basi msidharau, na msishangae, lakini sikilizeni maneno ya Bwana, na
mmwuombe Baba katika jina la Yesu kwa vitu vyote mtakavyohitaji. Msiwe na
shaka, lakini muwe mkiamini, na muanze kama wakati wa kale, na mje kwa Bwana
na mioyo yenu yote, na mtimize wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na
kutetemeka mbele yake.

28 Muwe na hekima katika siku zenu za majaribio; jiondoeni kutoka kwenye
uchafu; msiulize, ili mle kwa tamaa yenu, lakini ulizeni kwa uthabiti usiotingishika,
kwamba msilegee kwa majaribu yoyote, lakini kwamba mheshimu Mungu wa kweli
na aishiye.
29 Oneni kwamba hambatizwi bila kustahili; oneni kwamba msile sakaramenti ya
Kristo bila kustahili; lakini mhakikishe kwamba mnafanya vitu vyote katika
ustahilifu, na mvifanye katika jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aishiye; na
mkifanya hivi, na mvumilie hadi mwisho, hamtatupwa nje kamwe.
30 Tazama, ninawazungumzia kama ninayezungumza kutoka kwa wafu; kwani
najua kwamba mtapokea maneno yangu.
31 Msinilaani kwa sababu ya upungufu wangu, wala baba yangu, kwa sababu ya
upungufu wake, wala wale ambao wameandika mbele yake; walakini mshukuruni
Mungu kwa sababu amewaonyesha upungufu wetu, ili mjifunze kuwa na hekima
zaidi yetu.
32 Na sasa, tazama, tumeandika haya maandiko kulingana na kujua kwetu, katika
herufi ambazo zinaitwa miongoni mwetu Kimisri kilichogeuzwa, ambacho
kilitolewa na kugeuzwa nasi, kulingana na njia yetu ya kuongea.
33 Na ikiwa bamba zetu zingekuwa kubwa za kutosha tungeandika katika
Kihebrania, lakini Kihebrania kimegeuzwa nasi pia; na ikiwa tungeandika katika
Kihebrania; tazama, hamngekuwa na upungufu katika maandishi yetu.
34 Lakini Bwana anajua vitu ambavyo tumeandika, na pia kwamba watu wengine
hawajui lugha yetu; na kwa sababu hakuna watu wengine wajuao lugha yetu, kwa
ajili hii ametayarisha njia ya kutafsiri.
35 Na vitu hivi vimeandikwa ili tuwe huru kutoka kwa jukumu la dhambi
zilizofanywa na ndugu zetu, ambao wamefifia kwa kutoamini.
36 Na tazama, vitu hivi ambavyo tumetaka kuhusu ndugu zetu, ndio, hata
kurudishwa kwao kwa ufahamu wa Kristo, vipo kulingana na sala za watakatifu
ambao waliishi katika nchi.
37 Na ninaomba Bwana Yesu Kristo awakubalie kwamba sala zao zijibiwe kulingana
na imani yao; na namwomba Mungu Baba akumbuke lile agano ambalo amefanya
na nyumba ya Israeli; na ninaomba awabariki milele, kupitia kwa imani kwa jina la
Yesu Kristo. Amina.

# Kitabu cha Etheri

## Etheri 1

1 Na sasa mimi, Moroni, naendelea kutoa historia ya wakazi wa zamani ambao
waliangamizwa na mkono wa Bwana juu ya uso wa nchi hii ya kaskazini.
2 Na ninachukua historia yangu kutoka kwenye zile bamba ishirini na nne ambazo
zilipatwa na watu wa Limhi, ambayo inaitwa Kitabu cha Etheri.
3 Na kwa vile ninadhani kwamba sehemu ya kwanza ya maandishi haya, ambayo
inazungumza kuhusu uumbaji wa dunia, na pia wa Adamu, na historia kutoka
wakati ule hata kwenye mnara mkubwa, na vitu vyovyote vilivyojulikana miongoni
mwa watoto wa watu hadi wakati huo, iko miongoni mwa Wayahudi—
4 Kwa hivyo siandiki vitu hivyo ambavyo vilijulikana kutokea siku za Adamu
mpaka wakati huo; lakini vinaweza kujulikana kwenye bamba; na yeyote
atakayevipata, huyo huyo atakuwa na uwezo kwamba apate historia kamilifu.
5 Lakini tazama, sitatoa historia kamilifu, lakini nitatoa tu sehemu ya historia,
kutokea wakati wa mnara mpaka wakati walipoangamizwa.
6 Na kwa njia hii ninatoa historia. Yule ambaye aliandika ni Etheri, na alikuwa
mzao wa Koriantori.
7 Koriantori alikuwa mwana wa Moroni.
8 Na Moroni alikuwa mwana wa Ethemu.
9 Na Ethemu alikuwa mwana wa Aha.
10 Na Aha alikuwa mwana wa Sethi.
11 Na Sethi alikuwa mwana wa Shibloni.
12 Na Shibloni alikuwa mwana wa Komu.
13 Na Komu alikuwa mwana wa Koriantumu.
14 Na Koriantumu alikuwa mwana wa Amnigada.
15 Na Amnigada alikuwa mwana wa Haruni.
16 Na Haruni alikuwa mzao wa Hethi, ambaye alikuwa mwana wa Hearthomu.
17 Na Hearthomu alikuwa mwana wa Libu.
18 Na Libu alikuwa mwana wa Kishi.
19 Na Kishi alikuwa mwana wa Koromu.
20 Na Koromu alikuwa mwana wa Lawi.
21 Na Lawi alikuwa mwana Kimu.
22 Na Kimu alikuwa mwana wa Moriantoni.
23 Na Moriantoni alikuwa mzao wa Riplakishi.
24 Na Riplakishi alikuwa mwana wa Shezi.
25 Na Shezi alikuwa mwana wa Hethi.
26 Na Hethi alikuwa mwana wa Komu.
27 Na Komu alikuwa mwana wa Koriantumu.
28 Na Koriantumu alikuwa mwana wa Emeri.
29 Na Emeri alikuwa mwana wa Omeri.
30 Na Omeri alikuwa mwana wa Shule.
31 Na Shule alikuwa mwana wa Kibu.
32 Na Kibu alikuwa mwana wa Oriha, ambaye alikuwa mwana wa Yaredi;
33 Yaredi ambaye alitoka na kaka yake na jamaa zao, na wengine na jamaa zao,
kutoka kwa mnara mkubwa, wakati Bwana alipochanganya lugha za watu, na kuapa

katika ghadhabu yake kwamba atawatawanya juu ya uso wa dunia; na kulingana na neno la Bwana watu walitawanywa.

34 Na kaka ya Yaredi akiwa mkubwa na mwenye nguvu, na mtu aliyependelewa sana na Bwana, Yaredi, kaka yake, alimwambia; msihi Bwana, kwamba asituchanganyie lugha ili tusielewane maneno yetu.

35 Na ikawa kwamba kaka ya Yaredi aliomba kwa Bwana, na Bwana alimhurumia Yaredi; kwa hivyo hakuchanganya lugha ya Yaredi, na Yaredi na kaka yake hawakuchafuliwa.

36 Halafu Yaredi akamwambia kaka yake: Omba tena kwa Bwana, na iwe kwamba asiwe na hasira kwa wale ambao ni marafiki zetu, ili asichafue lugha yao.

37 Na ikawa kwamba kaka ya Yaredi alimwomba Bwana, na Bwana akawa na huruma kwa marafiki zao na jamaa zao pia, kwamba hawakuchafuliwa.

38 Na ikawa kwamba Yaredi alimzungumzia kaka yake tena, akisema: Nenda na ukamwulize Bwana kama atatufukuza kutoka nchini, na ikiwa atatufukuza kutoka nchini, mwulize kule ambako tutaenda. Na labda Bwana atatuchukua kwenye nchi ambayo ni nchi iliyochaguliwa kuliko zote duniani kote? Na ikiwa itakuwa hivyo, acha tuwe waaminifu kwa Bwana, ili tuweze kuipokea kwa urithi wetu.

39 Na ikawa kwamba kaka ya Yaredi alimwomba Bwana kulingana na yale ambayo yalizungumzwa na mdomo wa Yaredi.

40 Na ikawa kwamba Bwana alimsikiliza kaka ya Yaredi, na akawa na huruma juu yake, na kusema kwake:

41 Nenda na ukakusanye pamoja wanyama wako, wote wa kiume na wa kike wa kila namna; na pia mbegu ya udongoni ya kila namna; na jamaa yako; na pia Yaredi kaka yako na jamaa yake; na pia marafiki zako na jamaa zao, na marafiki za Yaredi na jamaa zao.

42 Na baada ya kufanya hivi utawaongoza chini hadi kwenye bonde ambalo liko upande wa kaskazini. Na huko nitakukuta, na nitakuongoza kwenye nchi ambayo ni bora kuliko nchi zote duniani.

43 Na huko nitawabariki na uzao wenu, na nitauinua uzao wako kwa yangu, na uzao wa kaka yako, na wale ambao wataenda nawe, taifa kubwa. Na hakutakuwa taifa kubwa kuliko taifa ambalo nitakalolipa uzao wako, juu ya uso wa dunia yote. Na hii nitakufanyia kwa sababu ya muda huu mrefu ambao umeomba kwangu.

## Etheri 2

1 Na ikawa kwamba Yaredi na kaka yake, na jamaa zao, na pia marafiki za Yaredi na kaka yake na jamaa zao, walienda chini kwenye bonde ambalo lilikuwa upande wa kaskazini, (na jina la lile bonde lilikuwa Nimrodi, ikiwa liliitwa baada ya yule mwindaji mashuhuri) na wanyama wao ambao walikuwa wamewakusanya pamoja, wa kiume na wa kike, wa kila namna.

2 Na waliweka mitego na kushika ndege wa hewani; na pia walitayarisha chombo, ambamo ndani yake wangebebea samaki wa majini.

3 Na pia walijibebea desereti, ambayo, kwa tafsiri, ni nyuki wa asali; na hivyo walibeba vikundi vya nyuki, na kila aina ya kile kilichokuwako juu ya uso wa nchi, mbegu za kila aina.

4 Na ikawa kwamba baada ya hao kuja chini kwenye bonde la Nimrodi Bwana alikuja chini na kuongea na kaka ya Yaredi; na alikuwa kwenye wingu, na kaka ya

Yaredi hakumwona.
5 Na ikawa kwamba Bwana aliwaamuru waende mbele nyikani, ndio, katika ile
sehemu ambako mtu hajawai kuwa. Na ikawa kwamba Bwana aliwaongoza, na
alizungumza nao akiwa katika wingu, na akawaonyesha njia ya kusafiri.
6 Na ikawa kwamba walisafiri nyikani, na walijenga mashua, ambamo walivuka
maji mengi, wakiongozwa wakati wote na mkono wa Bwana.
7 Na Bwana hangekubali kwamba wasimame mbele ya bahari nyikani, lakini
alitaka kwamba waje mbele hata mpaka kwenye nchi ya ahadi, ambayo ilikuwa nzuri
kuliko nchi zingine zote, ambayo Bwana Mungu alikuwa amehifadhi kwa watu
wenye haki.
8 Na alikuwa ameapa kwenye ghadhabu yake kwa kaka ya Yaredi, kwamba yeyote
atakayemiliki nchi hii ya ahadi, kutokea wakati huo na kuendelea milele, lazima
amtumikie, yule Mungu wa kweli na wa pekee, au waangamizwe utimilifu wa
ghadhabu ya Mungu ukiwajia.
9 Na sasa, tunaweza kuona amri za Mungu kuhusu nchi hii, kwamba ni nchi ya
ahadi; na taifa lolote litakaloimiliki litamtumikia Mungu, au wataangamizwa wakati
utimilifu wa ghadhabu yake, utakuja juu yao. Na utimilifu wa ghadhabu yake huja
juu yao baada ya wao kuwa waovu sana.
10 Kwani tazama, hii ni nchi ambayo ni nzuri kuliko nchi zingine zote; kwa hivyo
yule atakayeimiliki atamtumikia Mungu au ataangamizwa; kwani ni amri isiyo na
mwisho ya Mungu. Na haitakuwako mpaka utimilifu wa uovu miongoni mwa watu
wa nchi hii, ndipo wataangamizwa.
11 Na hii itakuja kwenu, Ee nyinyi Wayunani, ili mjue amri za Mungu—kwamba
mpate kutubu, na msiendelee mpaka utimilifu wa uovu wenu utakavyotimia,
kwamba msilete utimilifu wa ghadhabu ya Mungu juu yenu kama wakazi wa nchi
hii walivyofanya.
12 Tazama, hii ni nchi nzuri, na taifa lolote litakaloimiliki litakuwa huru kutoka
utumwa, na kutoka kifungo, na kutoka kwa mataifa mengine yote chini ya mbingu,
ikiwa watamtumikia Mungu wa pekee katika nchi, ambaye ni Yesu Kristo, ambaye
amedhihirishwa na vitu ambavyo tumeviandika.
13 Na sasa ninaendelea na maandishi yangu; kwani tazama, ikawa kwamba Bwana
alimleta Yaredi na ndugu zake mbele hata kwenye hiyo bahari kubwa ambayo
inagawanya nchi. Na walipokaribia bahari walipiga hema zao; na waliita mahala
pale Moriankumeri; na waliishi kwenye hema, na wakaishi katika hema kwenye
ukingo wa bahari kwa muda wa miaka minne.
14 Na ikawa katika mwisho wa miaka minne kwamba Bwana alikuja tena kwa kaka
ya Yaredi, na akasimama katika wingu na kuongea na yeye. Na kwa muda wa masaa
matatu, Bwana aliongea na kaka ya Yaredi, na kumkemea kwa sababu hakukumbuka
kulilingana jina la Bwana.
15 Na kaka ya Yaredi alitubu uovu aliofanya, na akalilingana jina la Bwana kwa
niaba ya ndugu zake aliokuwa nao. Na Bwana akamwambia: Nitakusamehe na
ndugu zako kutoka kwa dhambi zao; lakini hutafanya dhambi mara nyingine, kwani
utakumbuka kwamba Roho yangu haitajishughulisha na mwanadamu kila mara;
kwa hivyo, kama utafanya dhambi mpaka ufike mwisho, utakatiliwa mbali kutoka
kwenye uwepo wa Bwana. Na hizi ndizo fikira zangu juu ya nchi ambayo
nitakupatia kwa urithi; kwani itakuwa nchi nzuri kuliko nchi zote.
16 Na Bwana alisema: Nenda ufanye kazi na ujenge, aina ya mashua ambayo

mmejenga hadi sasa. Na ikawa kwamba kaka ya Yaredi alienda kazini, na pia ndugu zake, na kujenga mashua kama aina ambayo walikuwa wamejenga, kulingana na mafundisho ya Bwana. Na yalikuwa madogo, na yalikuwa mepesi juu ya maji, hata kama wepesi wa ndege arukaye juu ya maji.

17 Na yalijengwa kwa aina moja kwamba yalikuwa yamekazwa sana, kwamba yangeshikilia maji kama vile sahani inavyofanya; na chini yake ilikuwa ya kukazwa sana kama sahani; na pande zilikuwa zimekazwa kama sahani; na ncha zilichungoka; na juu yake ilikuwa imekazwa kama sahani; na urefu wake ulikuwa urefu wa mti; na mlango wake, baada ya kufungwa, ulikazika kama sahani.

18 Na ikawa kwamba kaka ya Yaredi aliomba kwa Bwana, akisema: Ee Bwana, nimefanya kazi ambayo uliniamuru, na nimetengeneza mashua kama vile ulivyoniongoza.

19 Na tazama, Ee Bwana, ndani zao hamna mwangaza; tutaielekeza wapi? Na pia tutaangamia, kwani ndani yao hatuwezi kupumua, isipokuwa tu hewa iliyomo ndani yao; kwa hivyo tutaangamia.

20 Na Bwana akamwambia kaka ya Yaredi: Tazama, utatoboa tundu upande wa juu, na pia upande wa chini; na wakati mtakapokosa hewa mtafungua tundu na mpokee hewa. Na ikiwa itakuwa kwamba maji yataingia ndani kwenu, tazama, mtafunga tundu, ili msife katika mafuriko.

21 Na ikawa kwamba kaka ya Yaredi alifanya vile, kulingana na Bwana alivyomwamuru.

22 Na akaomba tena kwa Bwana akisema: Ee Bwana, tazama nimefanya hata vile ulivyoniamuru; na nimetayarisha vyombo kwa watu wangu, na tazama hakuna mwangaza ndani yao. Tazama, Ee Bwana, utakubali tuvuke haya maji mengi kwenye giza?

23 Na Bwana akamwambia kaka ya Yaredi: Ungetaka nifanye nini ili muwe na mwangaza kwenye mashua yenu? Kwani tazama, hamwezi kuwa na madirisha, kwani yatavunjwa vipande vipande; wala hamwezi kubeba moto, kwani hamtaenda kwa mwanga wa moto.

24 Kwani tazama, mtakuwa kama nyangumi katikati ya bahari; kwani milima ya mawimbi yatawaangukia. Hata hivyo, nitawarudisha juu tena kutoka kwenye kilindi cha bahari; kwani pepo hutoka katika mdomo wangu, na pia mvua na mafuriko hutolewa na mimi.

25 Na tazama, ninawatayarisha dhidi ya vitu hivi; kwani hamwezi kuvuka hiki kilindi kikubwa isipokuwa niwatayarishe dhidi ya mawimbi ya bahari, na pepo ambazo zimevuma, na mafuriko ambayo yatakuja. Kwa hivyo unataka nikutayarishie nini ili muwe na mwangaza ndani ya kilindi cha bahari?

## Etheri 3

1 Na ikawa kwamba kaka ya Yaredi, (sasa idadi ya mashua ambazo zilikuwa zimetayarishwa zilikuwa nane) alienda mbele kwenye mlima, ambao waliuita mlima Shelemu, kwa sababu ya urefu wake mwingi, na akachonga mawe madogo kumi na sita kutoka kwenye mwamba; na yalikuwa meupe na safi, hata kama kioo kilicho wazi; na aliyabeba katika mikono yake hadi juu ya kilele cha mlima, na akaomba tena kwa Bwana, akisema:

2 Ee Bwana, umesema kwamba lazima tuzungukwe na mafuriko. Sasa tazama, Ee

Bwana, na usiwe na hasira na mtumishi wako kwa sababu ya udhaifu wake mbele
yako; kwani tunajua kwamba wewe ni mtakatifu na unaishi mbinguni, na sisi
hatufai mbele yako; kwa sababu ya mwanguko maumbile yetu yamekuwa maovu
siku zote; walakini, Ee Bwana, umetupatia amri kwamba tukulingane, kwamba
kutoka kwako tungepokea mahitaji yetu.
3 Tazama, Ee Bwana, umetuadhibu kwa sababu ya uovu wetu, na umetusukuma
mbele, na katika hii miaka mingi tumekuwa katika nyika; walakini, umekuwa
mwenye huruma kwetu. Ee Bwana, nitazame na huruma, na ugeuze hasira yako
kutoka kwa watu hawa, na usikubali kwamba wavuke hii bahari katika giza; lakini
tazama vitu hivi ambavyo nimechonga kutoka katika mwamba.
4 Na ninajua, Ee Bwana, kwamba una uwezo wote, na unaweza kufanya chochote
upendacho kwa faida ya binadamu; kwa hivyo gusa haya mawe, Ee Bwana, na kidole
chako, na uyatayarishe kwamba yaangaze kwenye giza; na yatang'aa kwetu ndani ya
mashua ambayo tumetayarisha, ili tuweze kuwa na mwangaza tutakapovuka bahari.
5 Tazama, Ee Bwana, unaweza kufanya hivi. Tunajua kwamba unaweza kuonyesha
mbele uwezo wako mkuu, ambao unaonekana mdogo katika macho ya watu.
6 Na ikawa kwamba baada ya kaka ya Yaredi kusema maneno haya, tazama, Bwana
alinyoosha mbele mkono wake na kugusa yale mawe moja moja kwa kidole chake.
Na pazia lilitolewa machoni mwa kaka ya Yaredi, na akaona kidole cha Bwana; na
kilikuwa kama kidole cha mtu, sawa kama mwili na damu; na kaka ya Yaredi
alianguka chini mbele ya Bwana, kwani alikumbwa na woga.
7 Na Bwana aliona kwamba kaka ya Yaredi alikuwa ameanguka chini; na Bwana
akasema kwake: Amka, kwa nini umeanguka?
8 Na akamwambia Bwana: Niliona kidole cha Bwana, na nikaogopa asije
akanipiga; kwani sikujua kama Bwana anao mwili na damu.
9 Na Bwana akamwambia: Kwa sababu ya imani yako umeona kwamba
nitachukua juu yangu mwili na damu; na hakujakuwa na mtu aliyekuja kwangu
mbeleni na imani kubwa vile umefanya; kwani kama hungekuwa hivyo hungeona
kidole changu. Je, uliona zaidi ya hii?
10 Na akajibu: Hapana; Bwana, jidhihirishe kwangu.
11 Na Bwana akamwambia: utaamini maneno ambayo nitasema?
12 Na akajibu: Ndio, Bwana, najua kwamba wewe husema ukweli, kwani wewe u
Mungu wa ukweli, na huwezi kudanganya.
13 Na baada ya kusema haya maneno, tazama, Bwana alijionyesha kwake, na
kusema: Kwa sababu unajua vitu hivi umekombolewa kutoka kwenye mwanguko;
kwa hivyo umerudishwa kwenye uwepo wangu; kwa hivyo ninajionyesha kwako.
14 Tazama, ni mimi yule aliyetayarishwa kutoka mwanzo wa dunia kuokoa watu
wangu. Tazama, mimi ni Yesu Kristo. Mimi ni Baba na Mwana. Ndani yangu
binadamu wote watapata maisha, na kwamba milele, hata wale watakaoamini kwa
jina langu; na watakuwa wana wangu na mabinti zangu.
15 Na kamwe sijajionyesha kwa binadamu ambaye nilimuumba, kwani binadamu
hajaamini kwangu vile umefanya. Je, unaona kwamba uliumbwa kwa mfano wangu?
Ndio, hata watu wote waliumbwa katika mwanzo kwa jinsi ya kama maumbile
yangu.
16 Tazama, huu mwili, ambao unauona sasa, ni mwili wa roho yangu; na
nimemuumba mtu jinsi ya mwili wangu wa roho; na hata ninavyoonekana kwako
kuwa katika roho ndivyo nitakavyoonekana kwa watu wangu katika mwili.

17 Na sasa, kwa vile mimi, Moroni, nilisema siwezi kuandika historia kamili ya vitu
hivi ambavyo vimeandikwa, kwa hivyo, ninatosheka kusema kwamba Yesu
alijionyesha kwa mtu huyu katika roho, hata jinsi alivyojionyesha kwa Wanefi.
18 Na alimhudumia kama alivyowahudumia Wanefi; na alifanya haya yote, ili huyu
mtu ajue kwamba alikuwa Mungu, kwa sababu ya matendo mengi makubwa
ambayo Bwana alikuwa amemwonyesha.
19 Na kwa sababu ya ufahamu wa huyu mtu hangeweza kuzuiwa kuona ndani ya
pazia; na aliona kidole cha Yesu, ambacho, baada ya kukiona, alianguka kwa woga;
kwani alijua kwamba kilikuwa kidole cha Bwana; na hakuwa na imani tena, kwani
alijua, bila tashwishi.
20 Kwa hivyo, akiwa na hii elimu kamilifu ya Mungu, hangeweza kuwekwa kwenye
pazia; kwa hivyo alimwona Yesu; na akamhudumia.
21 Na ikawa kwamba Bwana alimwambia kaka ya Yaredi: Tazama, hutaruhusu
lolote la vitu hivi ambavyo umeona na kusikia kufunuliwa kwa ulimwengu, mpaka
wakati utakapotimia nitakapolitukuza jina langu katika mwili; kwa hivyo, utaweka
vitu hivi ambavyo umeviona na kusikia kwako, na usimwonyeshe mtu yeyote.
22 Na tazama, utakapokuja kwangu, utaviandika na kufunga, ili mtu yeyote asiweze
kuvitafsiri; kwani utaviandika kwa lugha ambayo haiwezi kusomeka.
23 Na tazama, haya mawe mawili nitakukabidhi, nawe utayafunga pia pamoja na
vitu utakavyoandika.
24 Kwani tazama, lugha ambayo utaandika nimeichanganya; kwa hivyo
nitasababisha kwa wakati wangu unaonifaa kwamba haya mawe yatakuza macho ni
pa binadamu vitu hivi ambavyo utaandika.
25 Na baada ya Bwana kusema haya maneno, alimwonyesha kaka ya Yaredi wakazi
wote wa dunia ambao walikuwepo, na pia wote watakaokuwepo; na hakuwaficha
kutoka kwenye uwezo wake wa kuona, hata hadi kwenye mwisho wa dunia.
26 Kwani alikuwa amemwambia mbeleni, ikiwa atamwamini kwamba
angemwonyesha vitu vyote — kwamba ataonyeshwa; kwa hivyo Bwana hakuweza
kumzuia lolote, kwani alijua kwamba Bwana angemwonyesha vitu vyote.
27 Na Bwana akamwambia: Andika vitu hivi na uvitie muhuri; na nitavidhihirisha
kwa watoto wa watu katika muda wangu unaonifaa.
28 Na ikawa kwamba Bwana alimwamuru kwamba kuyafungia yale mawe mawili
ambayo alikuwa amepokea, na asiyaonyeshe kwa yeyote, mpaka Bwana
atakapoyadhihirisha kwa watoto wa watu.

# Etheri 4

1 Na Bwana alimwamuru kaka ya Yaredi aende chini kutoka mlimani kutoka kwenye
uwepo wa Bwana, na aviandike vitu alivyokuwa ameviona; na vilikatazwa
kuonekana na watoto wa watu mpaka atakapoinuliwa juu ya msalaba; na kwa
sababu hii mfalme Mosia alivificha, kwamba visijulikane duniani mpaka Kristo
atakapojidhihirisha kwa watu wake.
2 Na baada ya Kristo kujidhihirisha kwa ukweli kwa watu wake aliamrisha kwamba
vijulikane.
3 Na sasa, baada ya hayo, wote wamefifia katika kutoamini; na hakuna yeyote
isipokuwa Walamani, na wamekataa injili ya Kristo; kwa hivyo nimeamriwa
kwamba nivifiche tena ardhini.

4 Tazama, nimeandika juu ya bamba hizi vitu vivyo hivyo ambavyo kaka ya Yaredi aliviona; na hakujakuwa vitu vikubwa vilivyoonyeshwa kuliko hivyo ambavyo vilionyeshwa kwa kaka ya Yaredi.

5 Kwa hivyo Bwana ameniamuru niviandike; na nimeviandika. Na aliniamuru kwamba nivifunge; na pia ameniamuru kwamba nifungie tafsiri yake; kwa hivyo nimeifungia tafsiri, kulingana na amri ya Bwana.

6 Kwani Bwana aliniambia: Havitawaendea Wayunani mpaka siku watakapotubu uovu wao, na kuwa safi mbele ya Bwana.

7 Na katika siku hiyo watakapofanya imani kwangu, asema Bwana, hata kama kaka ya Yaredi alivyofanya, kwamba watakaswe kupitia kwangu, ndipo nitawaonyesha vitu ambavyo kaka ya Yaredi aliviona, hata kwa kuwakunjulia ufunuo wangu wote, anasema Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Baba wa mbingu na wa dunia, na vitu vyote vilivyomo.

8 Na yule ambaye atapingana na neno la Bwana, acha alaaniwe; na yule ambaye atakana vitu hivi, acha alaaniwe; kwani kwao, sitaonyesha vitu vikubwa zaidi, anasema Yesu Kristo; kwani ni mimi ninayezungumza.

9 Na kwa amri yangu mbingu hufunguliwa na kufungwa; na kwa neno langu dunia itatetemeka; na kwa amri yangu wakazi wake watakufa, kama waliochomwa na moto.

10 Na yule ambaye haamini maneno yangu, haamini wanafunzi wangu; na ikiwa hivyo kwamba sisemi, hukumu wewe; kwani utajua kwamba ni mimi ninayezungumza, katika siku ya mwisho.

11 Lakini yule aaminiye maneno haya ambayo nimesema, yeye nitamtembelea na ufunuo wa Roho yangu, na atajua na kushuhudia. Kwani kwa sababu ya Roho yangu atafahamu kwamba vitu hivi ni vya kweli; kwani huwashawishi watu kutenda mema.

12 Na kitu chochote ambacho hushawishi watu kutenda mema ni changu; kwani mema hayatoki kwa yeyote isipokuwa kwangu. Mimi ni yule yule ambaye huongoza watu kwa wema wote; yule ambaye hataamini maneno yangu hataniamini—kwamba ni mimi; na yule ambaye hataniamini hatamwamini Baba ambaye alinituma. Kwani tazama, mimi ni Baba, mimi ni mwangaza, na maisha, na ukweli wa dunia.

13 Njooni kwangu, Ee nyinyi Wayunani, na nitawaonyesha vitu vikuu zaidi, ufahamu ambao umefichwa kwa sababu ya kutoamini.

14 Njooni kwangu, Ee nyinyi nyumba ya Israeli, na itafanywa kujulikana kwenu jinsi Baba alivyoweka vitu kwenu, kutokea msingi wa dunia; na haijawafikia, kwa sababu ya kutoamini.

15 Tazama, wakati mtakapopasua lile pazia la kutoamini ambalo linawasababisha kubaki katika hali yenu ya kutisha ya uovu, na ugumu wa moyo, na upofu wa akili, ndipo vitu vikubwa na vya kustaajabisha ambavyo vilifichwa kutokea mwanzo wa dunia kutoka kwenu—ndio, wakati mtakapomlingana Baba katika jina langu, na moyo uliopondeka na roho iliyovunjika, ndipo mtajua kwamba Baba amekumbuka agano ambalo alifanya na babu zenu, Ee nyumba ya Israeli.

16 Na ndipo ufunuo wangu ambao nimesababisha kuandikwa na mtumishi wangu Yohana utakunjuliwa machoni mwa watu wote. Kumbuka, wakati mtakapoona vitu hivi, mtajua kwamba wakati uko karibu kwamba vitafanywa kuwa wazi kabisa.

17 Kwa hivyo, mtakapopokea haya maandishi mjue kwamba kazi ya Baba imeanza juu ya uso wa nchi.

18 Kwa hivyo, tubuni enyi miisho ya dunia, na mje kwangu, na mwamini katika
injili yangu, na mbatizwe katika jina langu; kwani yule ambaye anaamini na
kubatizwa atakombolewa; lakini yule ambaye haamini atalaaniwa; na ishara
zitaonyeshwa kwa wale ambao wanaamini katika jina langu.
19 Na ana baraka yule atakayepatikana akiwa mwaminifu kwa jina langu katika siku
ya mwisho, kwani atainuliwa kuishi katika ufalme uliotayarishwa kutokea mwanzo
wa dunia. Na tazama ni mimi ambaye nimezungumza. Amina.

# Etheri 5

1 Na sasa mimi, Moroni, nimeandika maneno ambayo niliamriwa, kulingana na
uwezo wangu wa kukumbuka; na nimekwambia vitu ambavyo nimeifungia; kwa
hivyo usiviguse ili uvitafsiri; kwani kitu kile kimekatazwa kwako, isipokuwa baadaye
itakuwa hekima kwa Mungu.
2 Na tazama, ungekubaliwa kwamba ungeonyesha bamba kwa wale ambao
watasaidia kwa kuileta mbele hii kazi;
3 Na kwa watatu zitaonyeshwa kwa uwezo wa Mungu; kwa hivyo watajua kwa
hakika kwamba vitu hivi ni vya kweli.
4 Na kwa vinywa vya mashahidi watatu vitu hivi vitadhihirishwa; na ushuhuda wa
watatu, na kazi hii, ambamo kwake kutaonyeshwa uwezo wa Mungu na pia neno
lake, ambalo Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu wanashuhudia — na haya yote
yatasimama kama ushuhuda dhidi ya dunia katika siku ya mwisho.
5 Na ikiwa itakuwa kwamba watatubu na kurudi kwa Baba katika jina la Yesu,
watapokelewa kwenye ufalme wa Mungu.
6 Na sasa, ikiwa sina mamlaka kwa vitu hivi, hukumuni nyinyi; kwani mtajua
kwamba ninayo mamlaka mtakaponiona, na tutasimama mbele ya Mungu katika
siku ya mwisho. Amina.

# Etheri 6

1 Na sasa mimi, Moroni, ninaendelea kutoa maandishi ya Yaredi na kaka yake.
2 Kwani ikawa baada ya Bwana kutayarisha mawe ambayo kaka ya Yaredi alikuwa
amebeba juu ya mlima, kaka ya Yaredi alishuka chini kutoka kwenye mlima, na
kuweka mawe katika mashua ambayo ilitayarishwa, moja kwa kila mashua; na
tazama, yalitoa mwangaza ndani ya mashua.
3 Na hivyo Bwana alisababisha mawe kutoa nuru gizani, kutoa mwangaza kwa
wanaume, wanawake, na watoto, ili wasivuke maji mengi gizani.
4 Na ikawa kwamba baada ya kutayarisha namna yote ya vyakula, kwamba
wangeishi kwenye maji, na pia vyakula kwa wanyama wao na mifugo yao, na kila
mnyama au ndege waliokuwa wamewabeba — na ikawa kwamba baada ya kufanya
vitu hivi vyote walijipakia kwenye vyombo au mashua, na kuanza mwendo kuelekea
baharini, wakimtegemea Bwana Mungu wao awalinde.
5 Na ikawa kwamba Bwana Mungu alisababisha kwamba kuweko na upepo mkali
utakaovuma juu ya maji kuelekea ile nchi ya ahadi; na hivyo walitupwa juu ya
mawimbi ya bahari mbele ya upepo.
6 Na ikawa kwamba mara nyingi walizikwa kwenye kilindi cha bahari, kwa sababu
ya milima ya mawimbi ambayo iliwaangukia, na pia tufani kubwa za kuogofya

ambazo zilisababishwa na ukali wa upepo.
7 Na ikawa kwamba walipozikwa katika kilindi hakukuwa na maji ambayo
yangewaumiza, jinsi mashua yao ilivyokuwa imekazwa kama bakuli, na pia ilikazwa
kama safina ya Nuhu; kwa hivyo wakati walizingirwa na maji mengi walimwomba
Bwana, na aliwaleta tena nje juu ya maji.
8 Na ikawa kwamba upepo haukukoma kamwe kuvuma kuelekea ile nchi ya ahadi
wakati walikuwa juu ya maji; na hivyo walipelekwa mbele ya upepo.
9 Na waliimba nyimbo za sifa kwa Bwana; ndio, kaka ya Yaredi aliimba sifa kwa
Bwana, na alimshukuru na kumsifu Bwana siku yote nzima; na usiku ulipofika,
hawakukoma kumsifu Bwana.
10 Na hivyo walisukumwa mbele; na hakuna mnyama mkubwa wa baharini ambaye
angewavunja, wala nyangumi ambaye angewaharibu; na walikuwa na mwangaza
daima, hata wakiwa chini ya maji au juu ya maji.
11 Na hivyo ndivyo walivyopelekwa mbele, kwa siku mia tatu arubaini na nne juu ya
maji.
12 Na walitua kwenye ukingo wa nchi ya ahadi. Na baada ya kuweka miguu yao juu
ya ukingo wa nchi ya ahadi walisujudu chini juu ya nchi, na wakajinyenyekeza mbele
ya Bwana, na machozi ya shangwe yakatiririka mbele ya Bwana, kwa sababu ya wingi
wa wororo wa rehema yake juu yao.
13 Na ikawa kwamba walienda juu ya uso wa nchi, na wakaanza kulima ardhi.
14 Na Yaredi alikuwa na wana wanne; na waliitwa Yakomu, na Gilga, na Maha, na
Oriha.
15 Na kaka ya Yaredi pia alizaa wana na mabinti.
16 Na marafiki za Yaredi na kaka yake walikuwa idadi ya karibu watu ishirini na
wawili; na pia walizaa wana na mabinti kabla ya kuja kwenye nchi ya ahadi; na kwa
sababu hiyo walianza kuwa wengi.
17 Na walifundishwa kujinyenyekea mbele ya Bwana; na pia walifundishwa kutoka
juu.
18 Na ikawa kwamba walianza kuenea juu ya nchi, na kuongezeka na kulima ardhi;
na walikuwa na nguvu katika nchi.
19 Na kaka ya Yaredi alianza kuzeeka, na akaona kwamba karibu ataenda chini
kwenye kaburi; kwa hivyo alisema kwa Yaredi: Acheni tukusanye pamoja watu wetu
ili tuweze kuwahesabu; ili tuwaulize ni kitu gani watakachohitaji kutoka kwetu
kabla hatujaenda kwenye makaburi yetu.
20 Na kwa hivyo watu walikusanywa pamoja. Sasa idadi ya wana na mabinti wa
kaka ya Yaredi walikuwa watu ishirini na wawili; na idadi ya wana na mabinti wa
Yaredi walikuwa kumi na wawili, yeye akiwa na wana wanne.
21 Na ikawa kwamba walihesabu watu wao; na baada ya kuwahesabu, waliwauliza
vitu ambavyo wangependa wafanyiwe kabla ya kwenda kwao kwenye makaburi yao.
22 Na ikawa kwamba watu walitaka waweke wakfu mmoja wa wana wao kuwa
mfalme juu yao.
23 Na sasa tazama, hii ilikuwa ngumu kwao. Na kaka ya Yaredi akasema kwao: Kwa
kweli kitu hiki kitawaongoza kwenye utumwa.
24 Lakini Yaredi alisema kwa kaka yake: Wakubalie kwamba wawe na mfalme. Na
kwa hivyo akawaambia: Chagueni kutoka miongoni mwa wana wetu mfalme,
yeyote mtakayemtaka.
25 Na ikawa kwamba walimchagua hata mwana wa kwanza wa kaka ya Yaredi; na

jina lake lilikuwa Pagagi. Na ikawa kwamba alikataa na hakutaka kuwa mfalme wao. Na watu walitaka kwamba baba yake amlazimishe, lakini baba yake hakumlazimisha; na akawaamuru kwamba wasimlazimishe mtu yeyote kuwa mfalme wao.

26 Na ikawa kwamba waliwachagua kaka wote wa Pagagi, na hawakukubali.

27 Na ikawa kwamba hata wana wa Yaredi, nao wote walikataa isipokuwa tu mmoja; na Oriha alitawaza kuwa mfalme juu ya watu.

28 Na alianza kutawala, na watu walianza kufanikiwa; na wakawa matajiri sana.

29 Na ikawa kwamba Yaredi alifariki, na kaka yake pia.

30 Na ikawa kwamba Oriha alijinyenyekea mbele ya Bwana, na alikumbuka vitu gani vikubwa Bwana alikuwa amemfanyia baba yake, na pia aliwafunza watu wake vitu gani vikubwa Bwana alikuwa amewafanyia babu zao.

# Etheri 7

1 Na ikawa kwamba Oriha alitoa hukumu kwenye nchi kwa haki siku zake zote, ambaye siku zake zilikuwa nyingi sana.

2 Na alizaa wana na mabinti; ndio, alizaa thelathini na mmoja, miongoni mwao walikuwa wana ishirini na watatu.

3 Na ikawa kwamba pia alimzaa Kibu katika umri wake wa uzee. Na ikawa kwamba Kibu alitawala badala yake; na Kibu akamzaa Korihori.

4 Na wakati Korihori alipokuwa na miaka thelathini na miwili aliasi dhidi ya baba yake, na akaenda kuishi katika nchi ya Nehori; na alizaa wana na mabinti, na wakawa warembo sana; kwa hivyo Korihori aliwavutia wengi kumfuata.

5 Na baada ya kukusanya pamoja jeshi alikuja kwenye nchi ya Moroni ambapo mfalme aliishi, na kumchukua mateka, ambako kulileta kutimia msemo wa kaka ya Yaredi kwamba watawekwa kwenye utumwa.

6 Sasa nchi ya Moroni, ambako mfalme aliishi, ilikuwa karibu na nchi inayoitwa Ukiwa na Wanefi.

7 Na ikawa kwamba Kibu aliishi utumwani, na watu wake chini ya Korihori mwana wake, mpaka alipokuwa mzee sana; walakini Kibu alimzaa Shule katika umri wake wa uzee, wakati alipokuwa bado utumwani.

8 Na ikawa kwamba Shule alimkasirikia kaka yake; na Shule akaongezeka nguvu, na akawa mwenye nguvu kulingana na nguvu ya mwanaume; na pia alikuwa mkuu kwa kuhukumu.

9 Kwa hivyo, aliendа kwenye kilima cha Efraimu, na akayeyusha chuma kutoka kwa kile kilima, na kutengeneza mapanga kutoka kwa chuma cha pua kwa wale ambao alikuwa amekuja nao; na baada ya kuwahami kwa panga alirejea kwenye mji wa Nehori, na kupigana vita na kaka yake Korihori, kwa njia ambayo alijipatia ufalme na kuurudisha kwa baba yake Kibu.

10 Na sasa kwa sababu ya kitu ambacho Shule alifanya, baba yake alimpa ufalme; kwa hivyo alianza kutawala badala ya baba yake.

11 Na ikawa kwamba alitoa hukumu kwa haki; na alisambaza ufalme wake juu ya nchi yote, kwani watu walikuwa wameongezeka sana.

12 Na ikawa kwamba Shule pia alizaa wana na mabinti wengi.

13 Na Korihori alitubu kutoka kwa maovu mengi ambayo alikuwa ameyafanya; kwa hivyo Shule alimpatia uwezo katika ufalme wake.

14 Na ikawa kwamba Korihori alikuwa na wana wengi na mabinti wengi. Na miongoni mwa wana wa Korihori kulikuwa na mmoja ambaye jina lake lilikuwa Nuhu.

15 Na ikawa kwamba Nuhu aliasi dhidi ya Shule, mfalme, na pia baba yake Korihori, na kumvuta kaka yake Kohori kumfuata, na pia ndugu zake wote na wengi wa watu wengine.

16 Na alifanya vita na Shule, mfalme, ambamo kwake alipata nchi ya urithi wa kwanza; na akawa mfalme juu ya sehemu hiyo ya nchi.

17 Na ikawa kwamba alifanya vita tena na Shule, mfalme; na akamshika Shule, mfalme, na kumchukua mbali hadi Moroni kama mateka.

18 Na ikawa wakati alipokuwa karibu kumuua, wana wa Shule walienda polepole hadi kwenye nyumba ya Nuhu usiku na kumuua, na walivunja mlango wa gereza na kumtoa nje baba yao, na kumweka kwenye kiti cha enzi cha ufalme wake.

19 Kwa hivyo, mwana wa Nuhu aliimarisha ufalme wake badala yake; walakini hawakupata uwezo tena juu ya Shule, mfalme, na watu waliokuwa chini ya utawala wa Shule, mfalme, walifanikiwa sana na walikuwa na nguvu.

20 Na nchi iligawanywa; na kukawa na falme mbili, falme ya Shule, na falme ya Kohori, mwana wa Nuhu.

21 Na Kohori, mwana wa Nuhu, alisababisha kwamba watu wake wapigane na Shule, ambapo Shule aliwashinda na kumuua Kohori.

22 Na sasa Kohori alikuwa na mwana aliyeitwa Nimrodi; na Nimrodi alisalimisha ufalme wa Kohori kwa Shule, na alipata fadhila za Shule; kwa hivyo Shule alimpatia mapendeleo mengi, na alifanya chochote kulingana na kutaka kwake katika ufalme wa Shule.

23 Na pia katika utawala wa Shule kulikuwa na manabii miongoni mwa watu, ambao walitumwa kutoka kwa Bwana, wakitabiri kwamba uovu na kuabudu sanamu kwa watu kulikuwa kumeleta laana juu ya nchi, na wangeangamizwa kama hawangetubu.

24 Na ikawa kwamba watu walitoa matusi dhidi ya manabii, na kuwafanyia mzaha. Na ikawa kwamba mfalme Shule aliwaadhibu wale wote waliotoa matusi dhidi ya manabii.

25 Na aliweka sheria kote nchini, ambayo iliwapatia manabii uwezo kwamba wangeenda popote walipotaka; na katika njia hii watu waliletwa kwenye toba.

26 Na kwa sababu watu walitubu kutoka kwa uovu wao na kuabudu sanamu kwao Bwana aliwasamehe, na wakaanza kufanikiwa tena nchini. Na ikawa kwamba Shule alizaa wana na mabinti katika umri wake wa uzee.

27 Na hapakuwepo na vita tena katika siku za Shule; na alikumbuka vitu vikubwa ambavyo Bwana alikuwa amewafanyia babu zake katika kuwaleta kuvuka kilindi kikubwa hadi kwenye nchi ya ahadi; kwa hivyo alitoa hukumu katika haki siku zake zote.

## Etheri 8

1 Na ikawa kwamba alimzaa Omeri, na Omeri alitawala badala yake. Na Omeri akamzaa Yaredi; na Yaredi akazaa wana na mabinti.

2 Na Yaredi aliasi dhidi ya baba yake, na akaenda kuishi katika nchi ya Hethi. Na ikawa kwamba aliwadanganya watu wengi, kwa sababu ya ujanja wa maneno yake, mpaka alipopata nusu ya ule ufalme.

3 Na baada ya kupata nusu ya ufalme alifanya vita na baba yake, na akamweka baba yake kwenye utumwa, na akamfanya kutumika katika utumwa;

4 Na sasa, katika siku za utawala wa Omeri alikuwa katika utumwa nusu ya maisha yake. Na ikawa kwamba alizaa wana na mabinti, miongoni mwao ambamo walikuwa Esromu na Koriantumuri;

5 Na walikasirika sana kwa sababu ya vitendo vya Yaredi kaka yao, mpaka kwamba waliunda jeshi na kufanya vita na Yaredi. Na ikawa kwamba walifanya vita na yeye wakati wa usiku.

6 Na ikawa kwamba baada ya kuua jeshi la Yaredi walikuwa karibu kumuua yeye pia; na aliwasihi kwamba wasimuue, na angetoa ufalme kwa baba yake. Na ikawa kwamba walimwachia maisha yake.

7 Na sasa Yaredi alihuzunika sana kwa sababu ya kupoteza utawala, kwani alikuwa ameweka moyo wake kwa ufalme na utukufu wa ulimwengu.

8 Sasa binti wa Yaredi akiwa mrembo sana, na akiona huzuni wa baba yake, alifikiria kutafuta mpango ambamo kwake angerudisha utawala kwa baba yake.

9 Sasa binti wa Yaredi alikuwa mrembo sana. Na ikawa kwamba aliongea na baba yake, na kusema kwake: Kwa nini baba yangu una huzuni sana? Hujasoma maandishi ambayo babu zetu walileta kutoka ng'ambo ya kilindi kikubwa? Tazama, hakuna historia kuhusu wale wa kale, kwamba wao kwa mipango yao ya siri walipata falme na utukufu mkuu?

10 Na sasa, kwa hivyo, acha baba yangu amtumainie Akishi, mwana wa Kimnori; na tazama, mimi ni mrembo, na nitacheza mbele yake, na nitampendeza, kwamba atatamani kwamba niwe mke wake; kwa hivyo ikiwa atataka kwamba umpatie mimi kama mke wake, ndipo utasema: Nitakupatia tu ikiwa utaniletea kichwa cha baba yangu, mfalme.

11 Na sasa Omeri alikuwa rafiki ya Akishi; kwa hivyo, wakati Yaredi alipokuwa amemtumainia Akishi, binti wa Yaredi alicheza mbele yake kwamba akampendeza, mpaka kwamba alimtaka awe mke wake. Na ikawa kwamba alisema kwa Yaredi: Nipatie mimi awe mke wangu.

12 Na Yaredi akamwambia: Nitamkabidhi kwako, ikiwa utaniletea kichwa cha baba yangu, mfalme.

13 Na ikawa kwamba Akishi alikusanya kwenye nyumba ya Yaredi jamaa zake wote, na kuwaambia: Mtaapa kwangu kwamba mtakuwa waaminifu kwangu kwa kitu ambacho nitataka kutoka kwenu?

14 Na ikawa kwamba wote waliapa kwake, katika yule Mungu wa mbinguni, na pia na mbingu, pia na dunia, na vichwa vyao, kwamba yeyote atakayetofautiana na usaidizi ambao Akishi alitaka atapoteza kichwa chake; na yeyote atakayetoa wazi kitu chochote ambacho Akishi amewafahamisha, huyo huyo atapoteza maisha yake.

15 Na ikawa kwamba hivyo ndivyo walikubaliana na Akishi. Na Akishi alitoa kiapo kwao ambacho kilitolewa na wale wa kale ambao pia walitaka uwezo, ambao ulitolewa hata kutoka kwa Kaini, ambaye alikuwa muuaji kutoka mwanzo.

16 Na yalihifadhiwa kwa uwezo wa ibilisi kutoa hivi viapo kwa watu, kuwaweka gizani, kuwasaidia wale wanaotafuta nguvu kupata uwezo, na kuua, na kupora, na kudanganya, na kutenda aina yote ya maovu na ukahaba.

17 Na alikuwa binti wa Yaredi aliyemwekea moyo wa kutafuta hivi vitu vya zamani; na Yaredi akaiweka kwenye moyo wa Akishi; kwa hivyo, Akishi aliwaambia jamaa zake na marafiki akiwapotosha mbali na ahadi zisizo za haki kufanya kitu chochote

alichotaka.
18 Na ikawa kwamba waliunda kundi ovu la siri, hata kama vile watu wa zamani
walivyofanya; kundi ambalo lilikuwa la kuchukiza sana na ovu kushinda yote, katika
fikira za Mungu;
19 Kwani Bwana hafanyi kazi katika makundi maovu ya siri, wala hataki kwamba
mtu amwage damu, lakini katika vitu vyote amevikataza tangu mwanzo wa
binadamu.
20 Na sasa mimi, Moroni, siandiki aina ya viapo na makundi, kwani imefanywa
kujulikana kwangu kwamba viko miongoni mwa watu wote, na viko miongoni mwa
Walamani.
21 Na vimesababisha kuangamizwa kwa watu hawa ambao ninawazungumzia sasa,
na pia kuangamia kwa watu wa Nefi.
22 Na taifa lolote litakalokubali makundi maovu ya siri kama haya, kupata uwezo na
utajiri, hadi kuenea juu ya taifa, tazama, wataangamizwa; kwani Bwana hatakubali
kwamba damu ya watakatifu wake, ambayo itamwagwa na hao, ilie siku zote kutoka
mchangani kwa kulipiza kisasi juu yao na bado halipizi kisasi.
23 Kwa hivyo, Ee nyinyi Wayunani, ni hekima kwa Mungu kwamba vitu hivi
vionyeshwe kwenu, kwamba kwa sababu hiyo mngetubu kutoka kwa dhambi zenu,
na msikubali kwamba haya makundi maovu ya siri yawe juu yenu, ambayo
yamejengwa kupata uwezo na utajiri — na kazi, ndio, hata kazi ya uharibifu, ije
kwenu, ndio, hata upanga wa haki wa Mungu wa milele utawaangukia, kwa
upinduaji wenu na uharibifu ikiwa mtakubali vitu hivi kuweko.
24 Kwa hivyo, Bwana anawaamrisha, wakati mtakapoona vitu hivi vikija miongoni
mwenu kwamba mtaamka kwa ufahamu wa hali yenu ya kutisha, kwa sababu ya
kundi hili la siri ambalo litakuwa miongoni mwenu; au ole kwake, kwa sababu ya
damu ya wale ambao wameuawa; kwani hulia kutoka mavumbini kwa kisasi juu
yake, na pia juu ya walioliunda.
25 Kwani inakuwa kwamba yeyote anayeijenga hutaka kuangusha uhuru wa ardhi,
mataifa na nchi zote; na huleta kutimizwa uangamizo wa watu wote, kwani
inaanzishwa na ibilisi, ambaye ni baba wa uwongo wote; hata yule yule
mdanganyifu aliyedanganya wazazi wetu wa kwanza, ndio, hata ndiye yule yule
mdanganyifu ambaye alisababisha binadamu kutenda mauaji tangu mwanzo;
ambaye ameshupaza mioyo ya watu kwamba wamewaua manabii, na kuwapiga kwa
mawe, na kuwatupa nje tangu mwanzo.
26 Kwa hivyo, mimi, Moroni, nimeamriwa kuandika vitu hivi ili uovu
ungeondolewa mbali, na ili wakati ungekuja ambapo Shetani hawezi kuwa na uwezo
kwa mioyo ya watoto wa watu, lakini kwamba wangeshawishiwa kutenda mema siku
zote, kwamba wangekuja kwenye chemichemi ya ukweli wote na kuokolewa.

# Etheri 9

1 Na sasa mimi, Moroni, naendelea na maandishi yangu. Kwa hivyo, tazama, ikawa
kwamba kwa sababu ya makundi maovu ya siri ya Akishi na marafiki zake, tazama,
walipindua utawala wa Omeri.
2 Walakini, Bwana alikuwa na huruma kwa Omeri, na pia kwa wana wake na
mabinti zake ambao hawakutaka kuangamizwa kwake.
3 Na Bwana alimwonya Omeri kwenye ndoto kwamba aondoke nje ya nchi; kwa

hivyo Omeri aliondoka nje ya nchi na jamaa zake, na kusafiri siku nyingi, na akaja juu na kupita kando ya kilima cha Shimu, na akaja juu kando ya mahali ambapo Wanefi waliangamizwa, na kutoka hapo akaenda upande wa mashariki, na akaja mahali palipoitwa Ablomu, kando ya ukingo wa bahari, na hapo akapiga hema lake, na pia wana wake na mabinti zake, na jamaa yake yote, isipokuwa Yaredi na jamaa zake.

4 Na ikawa kwamba Yaredi alitawazwa kuwa mfalme juu ya watu, na wale walio waovu; na akampatia Akishi binti wake kuwa mke wake.

5 Na ikawa kwamba Akishi alitaka kutoa maisha ya baba ya mke wake; na akauliza usaidizi kutoka kwa wale ambao alikuwa amewaapisha kwa kiapo cha watu wa kale, na walikata kichwa cha baba ya mke wake, wakati alipokuwa akikalia kiti cha enzi, akikutana na watu wake.

6 Kwani uenezaji wa hiki chama kiovu na cha siri ulikuwa mkuu kwamba kilikuwa kimebadilisha mioyo ya watu wote; kwa hivyo Yaredi aliuawa akiwa juu ya kiti chake cha enzi, na Akishi akatawala badala yake.

7 Na ikawa kwamba Akishi alianza kuwa na wivu kwa mwana wake, kwa hivyo alimfunga gerezani, na kumpatia chakula kidogo au bila mpaka aliposhindwa na kufariki.

8 Na sasa kaka ya yule aliyeumia hadi kifo, (jina lake lilikuwa Nimra) alikasirika na baba yake kwa sababu ya yale ambayo baba yake alimfanyia kaka yake.

9 Na ikawa kwamba Nimra alikusanya idadi ndogo ya watu, na wakatoroka kutoka nchini, na wakaja kuishi na Omeri.

10 Na ikawa kwamba Akishi alizaa wana wengine, na walipendelewa na watu, ingawaje walikuwa wameapa kwake kufanya aina yote ya uovu kulingana na yale aliyokuwa anataka.

11 Sasa watu wa Akishi walitaka utajiri, hata vile Akishi alivyotaka uwezo; kwa hivyo, wana wa Akishi waliwapatia pesa, kwa njia ambayo ilishawishi sehemu kubwa ya watu kuwafuata.

12 Na kulianza kuwa na vita baina ya watoto wa Akishi na Akishi, ambavyo vilidumu kwa muda wa miaka mingi, ndio, hadi kwenye maangamizo ya watu karibu wote wa ufalme, ndio, hata wote isipokuwa watu thelathini, na wale waliotoroka na nyumba ya Omeri.

13 Kwa hivyo, Omeri alirudishwa tena kwenye nchi ya urithi wake.

14 Na ikawa kwamba Omeri alianza kuzeeka; walakini, katika umri wake wa uzee alimzaa Emeri; na alimtawaza Emeri kuwa mfalme kutawala badala yake.

15 Na baada ya kumtawaza Emeri kuwa mfalme aliona amani nchini kwa muda wa miaka miwili, na akafariki, akiwa ameona siku nyingi, ambazo zilikuwa na huzuni mwingi. Na ikawa kwamba Emeri alitawala mahala pake, na akachukua nafasi ya baba yake.

16 Na Bwana akaanza tena kutoa laana kutoka kwa nchi, na nyumba ya Emeri ilifanikiwa sana wakati wa utawala wa Emeri; na kwa muda wa miaka sitini na mbili walikuwa na nguvu sana, hadi wakawa matajiri kupita kiasi—

17 Wakiwa na kila aina ya matunda, na nafaka, na hariri, na kitani nzuri, na dhahabu, na fedha, na vitu vya thamani;

18 Na pia kila aina ya mifugo, ya ng'ombe wa kiume, na ng'ombe wa kike, na kondoo, na nguruwe, na mbuzi, na pia aina nyingi za wanyama ambao walikuwa wa kufaa kwa chakula cha binadamu.

19 Na pia walikuwa na farasi, na punda, na kulikuwa na ndovu na kurelomu na kumomu; wote ambao walikuwa wa kufaa kwa binadamu, na zaidi ndovu na kurelomu na kumomu.

20 Na hivyo Bwana alitoa baraka zake kwa nchi hii, ambayo ilikuwa nzuri kuliko nchi zote; na aliamuru kwamba yeyote atakayeimiliki ile nchi aimiliki kwa kusudi la Bwana, au wangeangamia baada ya kuwa waovu wa kutosha; kwani juu ya watu kama hawa, asema Bwana: Nitatoa utimilifu wa ghadhabu yangu.

21 Na Emeri alitoa uamuzi wake kwa haki siku zake zote, na alizaa wana na mabinti wengi; na alimzaa Koriantumu, na akamtawaza Koriantumu kutawala badala yake.

22 Na baada ya kumtawaza Koriantumu kutawala badala yake aliishi miaka minne, na aliona amani katika nchi; ndio, na hata alimwona Mwana wa Ukweli, na alifurahi na kusifu katika maisha yake; na alikufa katika hali ya amani.

23 Na ikawa kwamba Koriantumu aliishi kama baba yake, na alijenga miji mingi mikubwa, na alitoa kile ambacho kilikuwa kizuri kwa watu wake katika siku zake zote. Na ikawa kwamba hakupata watoto hadi akawa mzee kabisa.

24 Na ikawa kwamba mke wake alifariki akiwa na miaka mia moja na miwili. Na ikawa kwamba Koriantumu, katika miaka yake ya uzee, alioa mwanamwali, na akazaa wana na mabinti; kwa hivyo aliishi mpaka alipokuwa na miaka mia moja na arubaini na miwili.

25 Na ikawa kwamba alimzaa Komu, na Komu akatawala badala yake; na alitawala kwa miaka arubaini na tisa, na akamzaa Hethi; na pia alizaa wana na mabinti wengine.

26 Na watu walikuwa wameenea tena juu ya uso wa nchi, na kukaanza tena kuwa na uovu mkuu sana juu ya uso wa nchi, na Hethi alianza kujiingiza kwenye mipango ya siri tena ya zamani, kumwangamiza baba yake.

27 Na ikawa kwamba alimwondoa baba yake, kwani alimchinja kwa upanga wake mwenyewe; na akatawala badala yake.

28 Na kukatokea manabii nchini tena, wakihubiri toba kwao — kwamba watayarishe njia ya Bwana au kungetokea laana juu ya uso wa nchi; ndio, hata kungekuwa na njaa kuu, ambamo kwake wangeangamizwa kama hawakutubu.

29 Lakini watu hawakuamini maneno ya manabii, lakini waliwatupa nje; na wengine wao waliwatupa kwenye mashimo na kuwaacha waangamie. Na ikawa kwamba walifanya vitu hivi vyote kufuatana na amri ya mfalme, Hethi.

30 Na ikawa kwamba kulianza kuwa na upungufu mkuu juu ya nchi, na wakazi wakaanza kuangamizwa kwa haraka sana kwa sababu ya upungufu huo, kwani haikuwepo mvua juu ya uso wa ardhi.

31 Na kukatokea nyoka wa sumu pia juu ya uso wa nchi, na waliwauma watu wengi. Na ikawa kwamba mifugo yao ilikimbilia mbele ya nyoka wenye sumu, kuelekea nchi iliyokuwa upande wa kusini, ambayo iliitwa na Wanefi Zarahemla.

32 Na ikawa kwamba kulikuwa na wengi wao waliokufa njiani; walakini, kulikuwa na baadhi yao waliotorokea kwenye nchi ya kusini.

33 Na ikawa kwamba Bwana alisababisha nyoka wasiwafuate tena, lakini wafunge njia ili watu wasiweze kupita, kwamba yeyote atakayejaribu kupita angeuawa na nyoka wa sumu.

34 Na ikawa kwamba watu walifuata njia ya mifugo, na walikula mizoga ya wale waliokufa njiani, mpaka walipokula wote. Sasa wakati watu walipoona kwamba lazima wafe walianza kutubu uovu wao na kumwomba Bwana.

35 Na ikawa kwamba baada ya kujinyenyekeza ya kutosha mbele ya Bwana alileta
mvua juu ya uso wa ardhi; na watu wakaanza kufanikiwa tena, na kukaanza kuwa na
matunda katika upande wa nchi za kaskazini, na katika nchi zote zilizokuwa karibu.
Na Bwana alionyesha uwezo wake kwao katika kuwaokoa kutoka kwenye njaa.

## Etheri 10

1 Na ikawa kwamba Shezi, ambaye alikuwa ukoo wa Hethi—kwani Hethi aliangamia
kwa njaa, na jamaa yake yote isipokuwa Shezi—kwa hivyo Shezi alianza tena
kuwaleta wale watu ambao walikuwa wamegawanyika pamoja.
2 Na ikawa kwamba Shezi alikumbuka kuangamizwa kwa babu zake, na akaweka
utawala wa haki; kwani alikumbuka kile Bwana alichofanya kuwaleta Yaredi na kaka
yake kuwavusha kilindi; na alitembea katika njia za Bwana; na alizaa wana na
mabinti.
3 Na mwana wake mkubwa, ambaye jina lake lilikuwa Shezi, aliasi dhidi yake; hata
hivyo, Shezi aliuawa na mwizi, kwa sababu ya utajiri wake mwingi, ambao ulileta
tena amani kwa baba yake.
4 Na ikawa kwamba baba yake alijenga miji mingi juu ya uso wa nchi, na watu
walianza tena kuenea kwenye uso wa nchi. Na Shezi aliishi na kuwa na umri
mkubwa sana; na alimzaa Riplakishi. Na alikufa, na Riplakishi alitawala badala yake.
5 Na ikawa kwamba Riplakishi hakufanya yale yaliyo mema machoni mwa Bwana,
kwani alikuwa na wake wengi na wanawake wengi wa kinyumba, na aliwawekea
watu mizigo mizito ambayo ilikuwa migumu kuhimili; ndio, aliwatoza kodi kubwa;
na kwa ile kodi alijenga nyumba nyingi kubwa.
6 Na alijitengenezea enzi maridadi sana; na alijenga magereza mengi, na yeyote
ambaye alikataa kulipa ushuru alitiwa gerezani; na yeyote ambaye hakuweza kulipa
ushuru alitiwa gerezani; na alisababisha kwamba wafanye kazi siku zote kwa
mategemeo yao; na yeyote aliyekataa kufanya kazi alisababisha auawe.
7 Kwa hivyo alipata kazi yake nzuri, ndio, hata dhahabu yake laini alisababisha
kusafishwa gerezani; na kila aina ya kazi alisababisha kutengenezwa katika gereza.
Na ikawa kwamba aliwatesa watu kwa ukahaba wake na machukizo yake.
8 Na baada ya kutawala kwa muda wa miaka arubaini na miwili watu waliasi dhidi
yake; na kulianza kuwa na vita tena nchini, mpaka kwamba Riplakishi aliuawa, na
ukoo wake ulifukuzwa kutoka nchini.
9 Na ikawa baada ya muda wa miaka mingi, Moriantoni, (ambaye alikuwa wa ukoo
wa Riplakishi) alikusanya pamoja jeshi la wasiofukuzwa, na akaenda mbele na
kupigana na watu; na akapata uwezo juu ya miji mingi; na vita vilikuwa vikali sana,
na vilikuwako kwa muda wa miaka mingi; na akachukua nchi yote, na akajiweka
mfalme wa nchi yote.
10 Na baada ya kujiweka kuwa mfalme alirahisisha mizigo ya watu, ambako alipata
mapendeleo ya watu, na walimtawaza kuwa mfalme wao.
11 Na aliwafanyia watu haki, lakini sio kwake mwenyewe kwa sababu ya ukahaba
wake mwingi; kwa hivyo alikatwa kutoka kwenye uwepo wa Bwana.
12 Na ikawa kwamba Moriantoni alijenga miji mingi, na watu walitajirika sana chini
ya utawala wake, katika majengo, na katika dhahabu na fedha, na katika kukuza
nafaka, na katika mifugo, na wanyama, na vitu kama hivyo vilivyorudishwa kwao.
13 Na Moriantoni aliishi akawa na umri mkubwa sana, na ndipo akamzaa Kimu; na

Kimu akatawala badala ya baba yake; na alitawala kwa miaka minane, na baba yake akafariki. Na ikawa kwamba Kimu hakutawala kwa haki, kwa hivyo hakupendelewa na Bwana.

14 Na kaka yake aliasi dhidi yake, ambako alimweka kifungoni; na alibaki kifungoni siku zake zote; na alizaa wana na mabinti katika utumwa, na katika umri wake wa uzee alimzaa Lawi; na akafa.

15 Na ikawa kwamba Lawi alitumika kwenye utumwa baada ya kifo cha baba yake, kwa muda wa miaka arubaini na miwili. Na alifanya vita dhidi ya mfalme wa nchi, ambayo kwayo alishinda na kujipatia utawala.

16 Na baada ya kujipatia utawala alifanya yale yaliyokuwa sawa kwa maoni ya Bwana; na watu walifanikiwa katika nchi; na aliishi kwa umri mzuri wa uzee, na alizaa wana na mabinti; na pia alimzaa Koromu, ambaye alimtawaza mfalme badala yake.

17 Na ikawa kwamba Koromu alifanya yale yaliyokuwa mema kwa maoni ya Bwana siku zake zote; na alizaa wana na mabinti wengi; na baada ya kuishi siku nyingi alifariki, kama vile kila kitu ambacho huwa duniani, na Kishi alitawala badala yake.

18 Na ikawa kwamba Kishi alikufa pia, na Libu alitawala badala yake.

19 Na ikawa kwamba Libu pia alifanya yale yaliyokuwa mema katika macho ya Bwana. Na katika siku za Libu nyoka wenye sumu waliangamizwa. Kwa hivyo walienda katika nchi iliyokuwa upande wa kusini, kuwinda chakula kwa watu wa nchi, kwani nchi ilifunikwa na wanyama wa misitu. Na Libu pia alikuwa mwindaji mkuu.

20 Na walijenga mji mkubwa kando ya shingo nyembamba ya nchi, kando ambapo bahari hutenga nchi.

21 Na walihifadhi nchi upande wa kusini kwa jangwa, kupata mawindo. Na uso wote wa nchi upande wa kaskazini ulifunikwa na wakazi.

22 Na walikuwa wenye bidii sana, na walinunua na kuuziana biashara wao kwa wao, ili wapate faida.

23 Na walifanya kazi katika kila aina ya madini, na walitengeneza dhahabu, na fedha, na chuma, na shaba, na kila aina ya madini; na waliichimba kutoka udongoni; kwa hivyo, walitupa rundo kubwa za mchanga ili wapate madini, ya dhahabu, na ya fedha, na ya chuma, na ya shaba nyekundu. Na walifanya kazi yote iliyo laini.

24 Na walikuwa na hariri, na vitani vilivyoshonwa vizuri; na walishona aina yote ya nguo, ili wajivike kutokana na uchi wao.

25 Na walitengeneza kila aina ya vyombo kulimia mashamba, pia vya kulimia na kupanda, kuvuna na kupalilia, na pia kupura.

26 Na walitengeneza kila aina ya vyombo ambavyo wanyama wao walifanyia kazi.

27 Na walitengeneza kila aina ya silaha za vita. Na walifanya aina yote ya ufundi wa hali ya juu.

28 Na hakungekuwa na watu waliobarikiwa kuliko hao, na kufanikishwa zaidi kwa mkono wa Bwana. Na walikuwa katika nchi iliyokuwa nzuri kuliko nchi zote, kwani Bwana alikuwa ameizungumza.

29 Na ikawa kwamba Libu aliishi miaka mingi, na alizaa wana na mabinti; na pia alimzaa Hearthomu.

30 Na ikawa kwamba Hearthomu alitawala badala ya baba yake. Na baada ya Hearthomu kutawala kwa miaka ishirini na minne, tazama, ufalme ulitolewa kutoka kwake. Na alitumikia miaka mingi kwenye utumwa, ndio, hata siku zake zote

zilizosalia.
31 Na alimzaa Hethi, na Hethi aliishi kwenye utumwa maisha yake yote. Na Hethi
alimzaa Haruni, na Haruni aliishi utumwani maisha yake yote; na alimzaa
Amnigada, na Amnigada pia aliishi kwenye utumwa siku zake zote; na alimzaa
Koriantumu, na Koriantumu aliishi kwenye utumwa siku zake zote; na alimzaa
Komu.
32 Na ikawa kwamba Komu alivuta nusu ya ule utawala kumfuata. Na alitawala juu
ya nusu ya ufalme kwa miaka arubaini na miwili; na akapigana na mfalme, Amgidi,
na walipigana kwa muda wa miaka mingi, wakati ambao Komu alimshinda Amgidi,
na akawa na uwezo juu ya utawala uliosalia.
33 Na katika siku za Komu, kulianza kuwa na wanyang'anyi katika nchi; na walianza
kutumia mipango ya zamani, na kupeana viapo kwa njia ya wale wa kale, na kutaka
tena kuharibu ufalme.
34 Sasa Komu alipigana sana dhidi yao; walakini, hakuwashinda.

# Etheri 11

1 Na kulitokea pia katika siku za Komu manabii wengi, na walitoa unabii wa
uharibifu wa wale watu wakuu isipokuwa watubu, na kumgeukia Bwana, na kuacha
mauaji yao na uovu.
2 Na ikawa kwamba manabii walikataliwa na watu, na walimkimbilia Komu kwa
ulinzi, kwani watu walitaka kuwaangamiza.
3 Na walitoa unabii wa vitu vingi kwa Komu; na alibarikiwa kwa siku zake zote
zilizosalia.
4 Na aliishi kwa umri mzuri wa uzee, na alimzaa Shiblomu; na Shiblomu akatawala
badala yake. Na kaka ya Shiblomu aliasi dhidi yake, na kukaanza kuwa na vita
vikubwa katika nchi yote.
5 Na ikawa kwamba kaka ya Shiblomu alisababisha kwamba manabii wote
waliotoa unabii wa uharibifu wa watu wauawe;
6 Na kulikuwa na msiba mkubwa katika nchi yote, kwani walikuwa wameshuhudia
kwamba laana kubwa ingekuja kwenye nchi, na pia juu ya watu, na kwamba
kungekuwa na uharibifu mkuu miongoni mwao, mkubwa kuliko yote iliyowahi
kuwa usoni mwa dunia, na mifupa yao ingekuwa kama mafungu ya mchanga usoni
mwa nchi isipokuwa watubu uovu wao.
7 Na hawakusikiliza sauti ya Bwana, kwa sababu ya makundi yao maovu; kwa
hivyo, kulianza kuwa na vita na mabishano katika nchi yote, na pia njaa nyingi na
maradhi ya kuambukiza, mpaka kwamba kukawa na uharibifu mkuu, ambao
haujawahi kujulikana usoni mwa dunia; na haya yote yalikuja kutimia katika siku za
Shiblomu.
8 Na watu walianza kutubu kutoka kwa uovu wao; na kadiri walivyofanya hivyo,
Bwana alikuwa na huruma kwao.
9 Na ikawa kwamba Shiblomu aliuawa, na Sethi akaletwa kwenye utumwa, na
aliishi kwenye utumwa siku zake zote.
10 Na ikawa kwamba Aha, mwana wake, alichukua ufalme; na akawatawala watu
siku zake zote. Na alifanya aina yote ya uovu katika siku zake, ambamo kwake
alisababisha umwagaji wa damu nyingi; na siku zake zilikuwa chache.
11 Na Ethemu, akiwa wa ukoo wa Aha, alichukua ufalme; na pia alifanya yale

yaliyokuwa maovu katika siku zake.
12 Na ikawa kwamba katika siku za Ethemu kulitokea manabii wengi, na wakatoa
unabii tena kwa watu; ndio, walitabiri kwamba Bwana angewaharibu kabisa kutoka
kwa uso wa dunia isipokuwa watubu uovu wao.
13 Na ikawa kwamba watu walishupaza mioyo yao, na hawangesikiliza maneno yao;
na manabii waliomboleza na kujitoa miongoni mwa watu.
14 Na ikawa kwamba Ethemu alitoa hukumu katika uovu siku zake zote; na alimzaa
Moroni. Na ikawa kwamba Moroni alitawala badala yake; na Moroni alifanya yale
ambayo yalikuwa maovu mbele ya Bwana.
15 Na ikawa kwamba kulitokea uasi miongoni mwa watu, kwa sababu ya lile kundi
ovu la siri ambalo lilianzishwa kupata uwezo na faida; na kulitokea mtu mkubwa wa
uovu miongoni mwao, na akapigana na Moroni, ambamo kwake alipindua nusu ya
ufalme; na akashika nusu ya ule ufalme kwa miaka mingi.
16 Na ikawa kwamba Moroni alimpindua, na kupata ufalme tena.
17 Na ikawa kwamba kulitokea mtu mwingine mwenye nguvu; na alikuwa uzao wa
kaka ya Yaredi.
18 Na ikawa kwamba alimwondoa Moroni na kuchukua ufalme; kwa hivyo, Moroni
aliishi katika utumwa siku zake zote zilizosalia; na alimzaa Koriantori.
19 Na ikawa kwamba Koriantori aliishi katika utumwa siku zake zote.
20 Na katika siku za Koriantori kulitokea manabii wengi, na wakaagua vitu vikubwa
na vya ajabu, na kuhubiri toba kwa watu, na isipokuwa watubu Bwana Mungu
angetoa hukumu dhidi yao hadi watakapoharibiwa kabisa.
21 Na kwamba Bwana Mungu angewatuma au kuwaleta mbele watu wengine
kumiliki nchi, kwa uwezo wake, kwa njia sawa ambayo aliwaleta babu zao.
22 Na walikataa maneno yote ya manabii, kwa sababu ya kundi lao la siri na
machukizo yao maovu.
23 Na ikawa kwamba Koriantori alimzaa Etheri, na akafariki, akiwa ameishi katika
utumwa siku zake zote.

# Etheri 12

1 Na ikawa kwamba siku za Etheri zilikuwa katika siku za utawala wa Koriantumuri;
na Koriantumuri alikuwa mfalme wa nchi yote.
2 Na Etheri alikuwa nabii wa Bwana; kwa hivyo Etheri alijitokeza katika siku za
Koriantumuri, na akaanza kuagua kwa watu, kwani hangeweza kuzuiliwa kwa
sababu ya Roho ya Bwana ambayo ilikuwa ndani yake.
3 Kwani alihubiri kutoka asubuhi, hata mpaka kwenda chini kwa jua, akihimiza
watu kuamini katika Mungu kwenye toba wasije wakaharibiwa, na akiwaambia
kwamba kwa imani vitu vyote hutimizwa—
4 Kwa hivyo, yeyote aaminiye katika Mungu angeweza kwa hakika kutumaini
ulimwengu bora, ndio, hata mahali katika mkono wa kulia wa Mungu, tumaini
ambalo huja kutokana na imani, hutengeneza nanga kwa roho za watu, ambayo
ingewafanya kuwa imara na thabiti, wakizidi sana kutenda kazi njema, wakiongozwa
kumtukuza Mungu.
5 Na ikawa kwamba Etheri aliagua vitu vikubwa vya ajabu kwa watu, ambavyo
hawakuamini, kwa sababu hawakuviona.
6 Na sasa, mimi, Moroni, nitazungumza machache kuhusu vitu hivi; ninataka

kuonyesha ulimwengu kwamba imani ni vitu ambavyo vinatumainiwa na
havionekani; kwa hivyo, msishindane kwa sababu hamwoni, kwani hamtapata
ushahidi wowote mpaka baada ya majaribu ya imani yenu.
7 Kwani ilikuwa kwa imani kwamba Kristo alijionyesha kwa babu zetu, baada ya
kuamka kutoka kwa wafu; na hakujionyesha kwao mpaka walipokuwa na imani
ndani yake; kwa hivyo, lazima iwe kwamba wengine walikuwa na imani ndani yake,
kwani hakujionyesha kwa ulimwengu.
8 Lakini kwa sababu ya imani ya watu amejionyesha kwa watu wa ulimwengu, na
kulitukuza jina la Baba, na alitayarisha njia ambayo kwake wengine wangeshiriki
kwa mwito wa zawadi ya mbinguni, kwamba wangetumainia vitu hivyo ambavyo
hawajaviona.
9 Kwa hivyo, mnaweza kuwa pia na tumaini, na muwe washiriki wa zawadi, ikiwa
mtakuwa tu na imani.
10 Tazama ilikuwa kwa imani kwamba wale wa kale waliitwa kama washiriki wa
agizo takatifu la Mungu.
11 Kwa hivyo, kwa imani, sheria ya Musa ilitolewa. Lakini katika kipawa cha Mwana
wake Mungu ametayarisha njia bora zaidi; na ni kwa imani kwamba imetimizwa.
12 Kwani kama hakuna imani miongoni mwa watoto wa watu, Mungu hawezi
kufanya miujiza miongoni mwao; kwa hivyo, hakujionyesha mpaka baada ya imani
yao.
13 Tazama, ilikuwa imani ya Alma na Amuleki ambayo ilisababisha gereza
kuanguka chini.
14 Tazama, ilikuwa imani ya Nefi na Lehi ambayo ilileta mabadiliko juu ya
Walamani, kwamba walibatizwa kwa moto na kwa Roho Mtakatifu.
15 Tazama, ilikuwa imani ya Amoni na ndugu zake ambayo ilileta muujiza mkuu
miongoni mwa Walamani.
16 Ndio, na hata wote waliofanya miujiza waliifanya kwa sababu ya imani, hata wale
walioishi kabla ya Kristo na pia wale waliokuwako baadaye.
17 Na ilikuwa kwa imani kwamba wale wanafunzi watatu walipata ahadi kwamba
hawangeona kifo; na hawakupokea ahadi hiyo mpaka baada ya wao kuwa na imani.
18 Na wala kwa muda wowote hakujawa na yeyote ambaye amefanya miujiza mpaka
awe na imani; kwa hivyo waliamini kwanza katika Mwana wa Mungu.
19 Na kulikuwa na wengi ambao imani yao ilikuwa na nguvu sana, hata kabla ya
Kristo kuja, ambao hawangeweza kuwekwa nyuma ya pazia, lakini kwa ukweli
waliona kwa macho yao vitu ambavyo walikuwa wameona kwa jicho la imani, na
walifurahi.
20 Na tazama, tumeona katika maandishi haya kwamba mmoja wa hao alikuwa kaka
ya Yaredi; kwani imani yake ilikuwa kubwa sana katika Mungu, kwamba Mungu
alipoweka kidole chake mbele hakuweza kukificha kutoka kwa uwezo wa kuona wa
kaka ya Yaredi, kwa sababu ya neno lake ambalo alikuwa amemzungumzia, neno
ambalo alikuwa amepokea kwa imani.
21 Na baada ya kaka ya Yaredi kuona kidole cha Bwana, kwa sababu ya ahadi
ambayo kaka ya Yaredi alikuwa amepata kwa imani, Bwana hangeweza kumzuia
kuona chochote; kwa hivyo alimwonyesha vitu vyote, kwani hangeweza tena
kuwekwa nje ya pazia.
22 Na ni kwa imani kwamba babu zangu wamepata ahadi kwamba vitu hivi vitakuja
kwa ndugu zao kupitia kwa Wayunani; kwa hivyo Bwana ameniamuru, ndio, hata

Yesu Kristo.
23 Na nikasema kwake: Bwana, Wayunani watachekelea vitu hivi, kwa sababu ya
unyonge wetu katika maandishi; kwani Bwana umetufanya wakubwa katika neno
kwa imani, lakini hujatufanya wakubwa kwenye maandishi; kwani umefanya watu
hawa wote kwamba wanaweza kusema sana, kwa sababu ya Roho Mtakatifu ambaye
umewapatia.
24 Na umetufanya kwamba tuweze kuandika tu machache, kwa sababu ya mikono
yetu kutokuwa miepesi. Tazama, hujatufanya mabingwa kwa uandishi kama kaka ya
Yaredi, kwani ulimfanya ili vitu ambavyo aliandika viwe vikubwa hata vile wewe
ulivyo, kwa kushinda mtu kuvisoma.
25 Umefanya pia maneno yetu yawe yenye nguvu na makubwa, hata kwamba
hatuwezi kuyaandika; kwa hivyo, tunapoandika tunaona udhaifu wetu, na
kuanguka kwa sababu ya upangaji wa maneno yetu; na ninaogopa Wayunani wasije
wakacheka maneno yetu.
26 Na nilipokuwa nimesema hivi, Bwana alinizungumzia, akisema: Wajinga
hucheka, lakini wataomboleza; na uzuri wangu unatosha kwa walio wanyenyekevu,
kwamba hawatafaidika kwa udhaifu wenu;
27 Na ikiwa watu watakuja kwangu nitawaonyesha udhaifu wao. Ninawapatia watu
udhaifu ili katika udhaifu wao wawe wanyenyekevu; na neema yangu inatosha watu
wote ambao hujinyenyekeza mbele yangu; kwani wakijinyenyekeza mbele yangu, na
kuwa na imani ndani yangu, ndipo nitafanya vitu dhaifu kuwa vya nguvu kwao.
28 Tazama, nitawaonyesha Wayunani udhaifu wao, na nitawaonyesha kwamba
imani, tumaini na hisani huwaleta kwangu — chimbuko la haki yote.
29 Na mimi, Moroni, baada ya kusikia maneno haya, nilifarijika, na kusema: Ee
Bwana, haki yako itafanyika, kwani najua kwamba unafanya miujiza kwa watoto wa
watu kufuatana na imani yao;
30 Kwani kaka ya Yaredi alisema kwa mlima Zerini, Nenda — na ulisonga. Na ikiwa
hangekuwa na imani haungesonga; kwa hivyo unafanya miujiza baada ya watu kuwa
na imani.
31 Kwa njia hii ulijionyesha kwa wanafunzi wako; kwani baada ya wao kuwa na
imani, na kuzungumza katika jina lako, ulijidhihirisha kwao kwa uwezo mkuu.
32 Na ninakumbuka kwamba umesema kwamba umetayarisha nyumba kwa watu,
ndio, hata miongoni mwa nyumba za Baba yako, ambamo kwake binadamu
angekuwa na tumaini kamili; kwa hivyo lazima binadamu atumaini, au hatapokea
urithi mahali ambapo umetayarisha.
33 Na tena, ninakumbuka kwamba umesema kwamba unawapenda watu wote
duniani, hata kwenye kuweka maisha yako chini kwa ajili ya walimwengu, ili
ungeyachukua tena kutayarisha mahali kwa watoto wa watu.
34 Na sasa najua kwamba huu upendo ambao umekuwa nao kwa watoto wa watu ni
hisani; kwa hivyo, isipokuwa watu wawe na hisani hawawezi kurithi pale mahali
ambapo umetayarisha nyumbani kwa Baba yako.
35 Kwa hivyo, ninajua kwa kitu hiki ambacho umesema, kwamba ikiwa Wayunani
hawana hisani, kwa sababu ya unyonge wetu, kwamba utawahukumu, na kuchukua
kutoka kwao talanta zao, ndio, hata ile ambayo wamepokea, na uwapatie wale
ambao watakuwa na nyingi zaidi.
36 Na ikawa kwamba niliomba kwa Bwana kwamba awapewe neema Wayunani, ili
wapate kuwa na hisani.

37 Na ikawa kwamba Bwana akasema nami: Kama hawana hisani haikuhusu wewe, umekuwa mwaminifu; kwa hivyo, nguo zako zitafanywa safi. Na kwa sababu umeuona udhaifu wako utafanywa kuwa mwenye nguvu, hata kwa kukaa mahali ambapo nimepatayarisha katika nyumba ya Baba yangu.
38 Na sasa mimi, Moroni, ninaaga kwa Wayunani, ndio, na pia kwa ndugu zangu ambao ninawapenda, mpaka tutakapokutana mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ambapo watu wote watajua kwamba mavazi yangu hayajawekwa mawaa na damu yenu.
39 Na ndipo mtakapojua kwamba nimemwona Yesu, na kwamba amenizungumzia uso kwa uso, na kwamba aliniambia katika unyenyekevu ulio wazi, hata vile mtu humwambia mwenzake kwa lugha yangu, kuhusu vitu hivi;
40 Na ni vichache tu ambavyo nimeandika, kwa sababu ya udhaifu wangu kwa kuandika.
41 Na sasa, nimekupendekeza kumtafuta huyu Yesu ambaye manabii na mitume wameandika kumhusu, kwamba neema ya Mungu Baba, na pia Bwana Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu, ambaye anashuhudia kwao, iwe na kuishi ndani yenu milele. Amina.

## Etheri 13

1 Na sasa mimi, Moroni, naendelea kumaliza maandishi yangu kuhusu uharibifu wa watu ambao nimekuwa nikiandika juu yao.
2 Kwani tazama, walikataa maneno yote ya Etheri; kwani aliwaambia kwa kweli vitu vyote, kutokea mwanzoni mwa binadamu; na kwamba wakati maji yalipokuwa yamepungua kutoka juu ya uso wa nchi ilikuwa nchi iliyochaguliwa kuliko zingine zote, nchi iliyochaguliwa na Bwana; kwa hivyo Bwana alitaka kwamba watu wote wangemtumikia, wale ambao wanaishi juu yake;
3 Na kwamba ilikuwa mahali pa Yerusalemu Mpya, ambayo ingekuja chini kutoka mbinguni, na utakatifu wa wakfu wa Bwana.
4 Tazama, Etheri aliona siku za Kristo, na alizungumza kuhusu Yerusalemu Mpya juu ya nchi hii.
5 Na alizungumza pia kuhusu nyumba ya Israeli, na Yerusalemu ambako Lehi angetokea — baada ya kuharibiwa kwake itajengwa tena, mji mtakatifu wa Bwana; kwa hivyo, haingekuwa Yerusalemu mpya kwani ilikuwa wakati wa kale; lakini ingejengwa tena, na uwe mji mtakatifu wa Bwana; na ingejengwa kwa ajili ya nyumba ya Israeli —
6 Na kwamba Yerusalemu Mpya ingejengwa juu ya nchi hii, kwa ajili ya sazo la uzao wa Yusufu, kwa vitu ambavyo kumekuwa na mfano.
7 Kwani vile Yusufu alimleta baba yake chini katika nchi ya Misri, hata hivyo alikufa huko; kwa hivyo, Bwana alileta sazo la uzao wa Yusufu kutoka nchi ya Yerusalemu, kwamba angekuwa na huruma kwa uzao wa Yusufu kwamba wasiangamie, hata vile alikuwa na huruma kwa baba ya Yusufu ili asiangamie.
8 Kwa hivyo, sazo la nyumba ya Yusufu litajengwa juu ya nchi hii; na itakuwa nchi ya urithi wao; na watajenga mji mtakatifu kwa Bwana, kama Yerusalemu ya kale; na hawatachanganywa tena, mpaka mwisho utakapofika wakati dunia itakapoisha.
9 Na kutakuwa na mbingu mpya na dunia mpya; na zitakuwa kama za kale ijapokuwa ya kale imepita mbali, na vitu vyote vimekuwa vipya.

10 Na ndipo kutatokea Yerusalemu Mpya; na heri wanaoishi ndani yake, kwani ni
hao ambao mavazi yao ni safi kupitia kwa damu ya Mwanakondoo; na ni hao hao
ambao wamehesabiwa miongoni mwa sazo la uzao wa Yusufu, ambao walikuwa wa
nyumba ya Israeli.
11 Na hapo pia kutatokea Yerusalemu ya kale; na wakazi wake, wamebarikiwa,
kwani wameoshwa kwenye damu ya Mwanakondoo; ni hawa ambao walitawanywa
na kukusanywa kutoka pande nne za dunia, na kutoka katika nchi za kaskazini, na
ni washiriki wa lile agano ambalo Mungu alifanya na baba yao, Ibrahimu.
12 Na wakati vitu hivi vitakapokuja, huletwa kutimizwa andiko ambalo linasema,
wako wale walio wa kwanza, watakaokuwa wa mwisho; na wako wale waliokuwa wa
mwisho, ambao watakuwa wa kwanza.
13 Na nilikuwa karibu kuandika zaidi, lakini nimekatazwa; lakini kuu na wa ajabu
ulikuwa unabii wa Etheri; lakini walimdhania kuwa bure, na wakamtupa nje; na
alijificha kwenye pango la mwamba wakati wa mchana, na wakati wa usiku aliendа
akiangalia vitu ambavyo vitawajia watu.
14 Na vile alivyoishi kwenye pango la mwamba aliandika haya maandishi
yaliyosalia, akitazama uharibifu ambao uliwajia watu, wakati wa usiku.
15 Na ikawa kwamba katika mwaka huo huo ambamo alitupwa nje kutoka
miongoni mwa watu vita vikubwa vilianza miongoni mwa watu, kwani kulikuwa na
wengi walioasi, ambao walikuwa watu wenye nguvu, na walitafuta kumwangamiza
Koriantumuri kwa mipango yao ya siri na maovu, ambayo yamezungumziwa.
16 Na sasa Koriantumuri, akiwa amesoma, mwenyewe, katika ustadi wote wa vita na
ujanja wote wa ulimwengu, kwa hivyo alifanya vita na wale waliotaka
kumwangamiza.
17 Lakini hakutubu, wala wana wake wenye sura nzuri na mabinti zake; wala wana
na mabinti za Kohori waliokuwa na sura nzuri; wala wana na mabinti za Korihori
ambao walikuwa na sura nzuri; na kwa kifupi, hakukuwa na wana na mabinti
waliokuwa na sura nzuri juu ya uso wa dunia nzima ambao walitubu dhambi zao.
18 Kwa hivyo, ikawa kwamba katika mwaka wa kwanza ambamo Etheri aliishi
kwenye pango la mwamba, kulikuwa na watu wengi waliouawa kwa upanga wa wale
wa kundi ovu la siri, likipigana dhidi ya Koriantumuri ili wangepata ufalme.
19 Na ikawa kwamba wana wa Koriantumuri walipigana sana na walitokwa na
damu sana.
20 Na katika mwaka wa pili neno la Bwana lilimjia Etheri, kwamba aende na
amtabirie Koriantumuri kwamba, ikiwa angetubu, na nyumba yake yote, Bwana
angempatia ufalme wake na kuwaachilia watu—
21 La sivyo wangeangamizwa, na nyumba yake yote isipokuwa yeye. Na angeishi tu
kushuhudia utimizaji wa unabii ambao umezungumziwa kuhusu watu wengine
kupokea nchi kwa urithi wao; na Koriantumuri angezikwa na hao; na kila mtu
angeangamizwa isipokuwa Koriantumuri.
22 Na ikawa kwamba Koriantumuri hakutubu, wala nyumba yake, wala watu; na
vita havikuisha; na walitaka kumuua Etheri, lakini alitoroka kutoka kwao na
kujificha tena kwenye pango la ule mwamba.
23 Na ikawa kwamba kulitokea mtu ambaye aliitwa Sharedi, na alifanya vita na
Koriantumuri; na alimshinda, mpaka kwamba katika mwaka wa tatu alimweka
kwenye utumwa.
24 Na wana wa Koriantumuri, katika mwaka wa nne, walimshinda Sharedi, na

kumrudisha baba yao kwenye ufalme.
25 Sasa kulianza kuwa na vita juu ya uso wa nchi yote, kila mtu na kundi lake
akipigania kile alichotaka.
26 Na kulikuwa na wanyang'anyi, na kwa kifupi, kila aina ya uovu juu ya uso wa nchi
yote.
27 Na ikawa kwamba Koriantumuri alimkasirikia sana Sharedi, na akamwendea na
jeshi lake kupigana; na walikutana kwa hasira kubwa, na walikutania kwenye bonde
la Gilgali; na vita vikawa vikali sana.
28 Na ikawa kwamba Sharedi alipigana dhidi yake kwa muda wa siku tatu. Na ikawa
kwamba Koriantumuri alimshinda, na kumfukuza mpaka alipofikia mahali
tambarare pa Heshloni.
29 Na ikawa kwamba Sharedi alimfanyia vita tena juu ya tambarare; na tazama,
alimshinda Koriantumuri, na kumrudisha nyuma tena hadi kwenye bonde la Gilgali.
30 Na Koriantumuri alifanya vita na Sharedi tena kwenye bonde la Gilgali, ambamo
kwake alimshinda Sharedi na kumuua.
31 Na Sharedi alimjeruhi Koriantumuri katika paja lake, kwamba hangepigana tena
kwa muda wa miaka miwili, wakati ambamo watu wote juu ya uso wa nchi walikuwa
wanamwaga damu, na hakukuwa na yeyote ambaye angewazuia.

# Etheri 14

1 Na sasa kulianza kuwa na laana kuu juu ya nchi yote kwa sababu ya uovu wa watu,
ambamo kwake, ikiwa mtu angeweka chombo chake au upanga wake juu ya rafu
yake, au mahali ambapo angeiweka, tazama, kufikia kesho yake, hangeipata, kubwa
hivyo ilikuwa laana juu ya nchi.
2 Kwa hivyo kila mtu alishikilia kile kilichokuwa chake, kwa mikono yake, na
hangeomba wala kuazima; na kila mtu aliweka kipini cha upanga wake kwenye
mkono wa kulia, katika kulinda mali yake na maisha yake, na ya mabibi zake na
watoto wake.
3 Na sasa, baada ya muda wa miaka miwili, na baada ya kifo cha Sharedi, tazama,
kulitokea kaka ya Sharedi na akafanya vita na Koriantumuri, ambamo Koriantumuri
alimshinda na kumfukuza hadi kwenye jangwa la Akishi.
4 Na ikawa kwamba kaka ya Sharedi alifanya vita dhidi yake katika jangwa la
Akishi; na vita vilikuwa vikubwa sana, na maelfu wengi walianguka kwa upanga.
5 Na ikawa kwamba Koriantumuri alizingira jangwa; na kaka ya Sharedi alitoka
nje ya jangwa wakati wa usiku, na kuua sehemu ya jeshi la Koriantumuri, wakati
walipokuwa wamelewa.
6 Na akaja mbele hadi kwenye nchi ya Moroni, na kujiweka kwenye kiti cha enzi
cha Koriantumuri.
7 Na ikawa kwamba Koriantumuri aliishi na jeshi lake katika jangwa kwa muda wa
miaka miwili, wakati ambapo alipata nguvu nyingi kwa jeshi lake.
8 Sasa kaka ya Sharedi, ambaye jina lake lilikuwa Gileadi, pia alipata nguvu nyingi
kwa jeshi lake, kwa sababu ya vikundi vyake vya siri.
9 Na ikawa kwamba kuhani mkuu wake alimuua wakati alipokuwa amekalia kiti
chake cha enzi.
10 Na ikawa kwamba mmoja wa wale wa kundi ovu la siri alimuua katika njia ya siri,
na akajipatia ufalme; na jina lake lilikuwa Libu; na Libu alikuwa mtu mnene, kuliko

mtu yeyote miongoni mwa watu wote.
11 Na ikawa kwamba katika mwaka wa kwanza wa Libu, Koriantumuri alikuja
kwenye nchi ya Moroni, na kufanya vita na Libu.
12 Na ikawa kwamba alipigana na Libu, ambamo kwake Libu alimpiga mkono wake
kwamba alimjeruhi; walakini, jeshi la Koriantumuri lilimshambulia Libu, kwamba
alikimbia hadi kwenye mipaka juu ya ukingo wa bahari.
13 Na ikawa kwamba Koriantumuri alimfuata; na Libu akafanya vita na yeye juu ya
ukingo wa bahari.
14 Na ikawa kwamba Libu alishinda jeshi la Koriantumuri, kwamba walikimbia
tena hadi kwenye nyika ya Akishi.
15 Na ikawa kwamba Libu alimfuata mpaka akafikia nchi wazi ya Agoshi. Na
Koriantumuri alikuwa amechukua watu wote na yeye wakati alikimbia mbele ya
Libu katika ile sehemu ya nchi ambapo alikimbilia.
16 Na baada ya kuja kwenye tambarare za Agoshi alifanya vita na Libu, na kumpiga
mpaka akafa; walakini, kaka ya Libu alimshambulia Koriantumuri badala yake, na
vita vikawa vikali sana, ambapo Koriantumuri alikimbia mbele ya jeshi la kaka ya
Libu.
17 Sasa jina la kaka ya Libu lilikuwa Shizi. Na ikawa kwamba Shizi alimfukuza
Koriantumuri, na kuangamiza miji mingi, na aliua wote wanawake na watoto, na
alichoma miji hiyo.
18 Na kukaenea woga juu ya Shizi katika nchi nzima; ndio, mlio ulienda kote
nchini — Ni nani anaweza kushindana na jeshi la Shizi? Tazama, husafisha dunia
mbele yake!
19 Na ikawa kwamba watu walianza kujikusanya pamoja kwa majeshi, kote kwenye
uso wa nchi.
20 Na waligawanyika; na sehemu yao moja ilikimbilia jeshi la Shizi, na sehemu
nyingine ikakimbilia jeshi la Koriantumuri.
21 Na vita vilikuwa vikubwa na vya kudumu, na kuonekana kwa damu kuliendelea
kwa muda mrefu na mauaji, kwamba uso wa nchi ulifunikwa na miili ya waliokufa.
22 Na vita vilikuwa vya upesi sana na haraka kwamba hakukuwa na aliyebaki kuzika
waliokufa, lakini walienda mbele kutoka kwa umwagaji wa damu hadi kwa
umwagaji wa damu mwingine, wakiacha miili ya wote wanaume, wanawake, na
watoto imetawanywa juu ya uso wa nchi, kuwa mawindo ya minyoo ya mwili.
23 Na uvundo kutoka hapo ulienea juu ya uso wa nchi, hata juu ya uso wote wa nchi;
kwa hivyo watu walisumbuliwa mchana na usiku, kwa sababu ya uvundo wa wafu.
24 Walakini, Shizi hakuacha kumkimbiza Koriantumuri; kwani alikuwa ameapa
kujilipiza kisasi juu ya Koriantumuri kwa damu ya kaka yake, ambaye alikuwa
amemuua, na neno la Bwana ambalo lilimjia Etheri kwamba Koriantumuri
hangeuawa kwa upanga.
25 Na hivyo tunaona kwamba Bwana aliwatembelea katika utimilifu wa ghadhabu
yake, na uovu wao na machukizo yao yalitayarisha njia kwa maangamizo yao yasiyo
na mwisho.
26 Na ikawa kwamba Shizi alimfuata Koriantumuri kwa upande wa mashariki,
mpaka kufika kwenye mipaka kando ya ukingo wa bahari, na kule alifanya vita na
Shizi kwa muda wa siku tatu.
27 Na uharibifu ulikuwa wa kutisha sana miongoni mwa majeshi ya Shizi kwamba
watu walianza kuogopa, na kuanza kukimbia mbele ya majeshi ya Koriantumuri; na

walikimbia hadi kwa nchi ya Korihori, na kuangamiza wakazi mbele yao, wale wote
ambao hawakujiunga nao.
28 Na walipiga hema zao katika bonde la Korihori; na Koriantumuri akapiga hema
zake katika bonde la Shuri. Sasa bonde la Shuri lilikuwa karibu na kilima Komnori;
kwa hivyo, Koriantumuri alikusanya majeshi yake juu ya kilima Komnori, na
akapiga tarumbeta kuelekea kwa majeshi ya Shizi kuwakaribisha kupigana.
29 Na ikawa kwamba walikuja mbele, lakini walikimbizwa tena; na wakaja tena
safari ya pili, na wakakimbizwa tena safari ya pili. Na ikawa kwamba walikuja tena
safari ya tatu, na vita vikawa vikali sana.
30 Na ikawa kwamba Shizi alimpiga Koriantumuri kwamba alimpatia majeraha
mengi ya vidonda vikubwa; na Koriantumuri, kwa sababu ya kupoteza damu yake,
alizirai, na alibebwa na kupelekwa mbali kama aliyekufa.
31 Sasa mauaji ya wanaume, wanawake na watoto pande zote mbili yalikuwa
makubwa sana kwamba Shizi aliamuru watu wake wasiyafuatilie majeshi ya
Koriantumuri; kwa hivyo, walirudi kwenye kituo chao.

## Etheri 15

1 Na ikawa baada ya Koriantumuri kupona kutokana na majeraha yake, alianza
kukumbuka maneno ambayo Etheri alikuwa amemzungumzia.
2 Aliona kwamba walikuwa wameuawa kwa upanga kitambo karibu milioni mbili
ya watu wake, na alianza kuhuzunika moyoni mwake; ndio, walikuwa wameuawa
milion mbili ya watu wakuu, na pia wake zao na watoto wao.
3 Alianza kutubu kwa uovu ambao alikuwa amefanya; alianza kukumbuka maneno
ambayo yalizungumzwa kwa midomo ya manabii wote, na aliona kwamba
yametimizwa hadi sasa, kila chembe; na nafsi yake iliomboleza na kukataa
kutulizwa.
4 Na ikawa kwamba aliandika barua kwa Shizi, akimwuliza awasamehe watu, na
angeacha ufalme kwa ajili ya maisha ya watu.
5 Na ikawa kwamba baada ya Shizi kupokea barua yake aliandika barua kwa
Koriantumuri, kwamba kama angejisalamisha, ili amuue kwa upanga wake
mwenyewe, kwamba angeachilia maisha ya watu.
6 Na ikawa kwamba watu hawakutubu kutoka kwa maovu yao; na watu wa
Koriantumuri walichochewa kuwa na hasira dhidi ya watu wa Shizi; na watu wa
Shizi walichochewa kuwa na hasira dhidi ya watu wa Koriantumuri; kwa hivyo,
watu wa Shizi walifanya vita na watu wa Koriantumuri.
7 Na wakati Koriantumuri alipoona kwamba alikuwa karibu kushindwa alikimbia
tena mbele ya watu wa Shizi.
8 Na ikawa kwamba alifikia maji ya Ripliankumu, ambayo, kwa tafsiri, ni kubwa,
au kushinda yote; kwa hivyo, walipofikia haya maji walipiga hema zao; na Shizi pia
akapiga hema zake karibu na wao; na kwa hivyo kesho yake walipigana.
9 Na ikawa kwamba walipigana vita vikali sana, ambamo kwake Koriantumuri
alijeruhiwa tena, na akazirai kwa kupoteza damu.
10 Na ikawa kwamba majeshi ya Koriantumuri yalizidi kushambulia majeshi ya
Shizi kwamba waliwashinda, kwamba waliwasababisha kukimbia kutoka mbele yao;
na walikimbilia upande wa kusini, na kupiga hema zao mahali palipoitwa Ogathi.
11 Na ikawa kwamba jeshi la Koriantumuri lilipiga hema zao kando ya kilima

Rama; na kilikuwa kile kile kilima ambapo baba yangu Mormoni alificha maandishi
kwa ulinzi wa Bwana, ambayo yalikuwa matakatifu.
12 Na ikawa kwamba waliwakusanya watu wote pamoja juu ya uso wa nchi, wale
ambao walikuwa hawajauawa, isipokuwa Etheri.
13 Na ikawa kwamba Etheri aliona matendo yote ya watu; na aliona kwamba watu
ambao walikuwa wafuasi wa Koriantumuri walikusanywa pamoja kuwa jeshi la
Koriantumuri; na watu waliokuwa wafuasi wa Shizi walikusanyika pamoja kwenye
jeshi la Shizi.
14 Basi, walikusanya watu pamoja kwa muda wa miaka minne, kwamba wangepata
wale wote ambao walikuwa juu ya uso wa nchi, na ili wapate nguvu yote ambayo
iliwezekana kupata.
15 Na ikawa kwamba baada ya wote kukusanyika pamoja, kila mtu kwenye jeshi
ambalo alitaka, na wake zao na watoto wao—wote wanaume, wanawake na watoto
wakijihami na silaha za vita, wakiwa na ngao, na dirii, na vyapeo, na wakiwa
wamevalia kwa njia ya vita—walisonga mbele mmoja dhidi ya mwingine kupigana;
na walipigana ile siku yote, na hakuna aliyeshinda.
16 Na ikawa kwamba wakati ilipokuwa usiku walikuwa wamechoka, na wakarudi
kwenye vituo vyao; na baada ya kurudi kwenye vituo vyao walianza kulia na
kuomboleza kwa sababu ya watu wao ambao walikuwa wameuawa; na vilio vyao
vilikuwa vikuu sana, pamoja na maombolezo yao na makelele, kwamba vilipenya
anga kwa wingi.
17 Na ikawa kwamba kesho yake walienda tena kupigana, na siku hiyo ilikuwa
kubwa na ya kutisha; walakini, hawakushinda, na wakati usiku ulipowadia tena
walipenya anga na vilio vyao, na kulia kwao, na maombolezo yao, kwa vifo vya watu
wao.
18 Na ikawa kwamba Koriantumuri aliandika tena barua kwa Shizi, akitaka
kwamba asije tena kwa vita, lakini akubali ufalme, na kuhurumia maisha ya watu.
19 Lakini tazama, Roho ya Bwana ilikuwa imekoma kuwaongoza, na Shetani
alikuwa na uwezo kamili juu ya mioyo ya watu; kwani walikuwa wamejisalimisha
kwa ugumu wa mioyo yao, na upofu wa akili zao kwamba waharibiwe; kwa hivyo
walienda tena vitani.
20 Na ikawa kwamba walipigana ile siku yote, na usiku ulipowadia walilalia panga
zao.
21 Na kesho yake walipigana mpaka hata usiku ukafika.
22 Na usiku ulipofika walikuwa na hasira, kama vile mtu aleweshwavyo na divai; na
walilalia tena panga zao.
23 Na kesho yake walipigana tena; na usiku ulipofika wote walikuwa wameuawa
isipokuwa watu wa Koriantumuri hamsini na wawili, na watu wa Shizi sitini na tisa.
24 Na ikawa kwamba walilalia panga zao usiku huo, na kesho yake wakapigana tena,
na walipigana kwa nguvu yao yote kwa panga na ngao zao, siku hio yote.
25 Na wakati usiku ulipofika kulikuwa na watu wa Shizi thelathini na wawili, na
watu wa Koriantumuri ishirini na saba.
26 Na ikawa kwamba walikula na kulala, na kujitayarishia kifo kesho yake. Na
walikuwa wanene na wenye nguvu wakilinganishwa na watu wa kawaida.
27 Na ikawa kwamba walipigana kwa muda wa masaa matatu, na walizirai kwa
kupoteza damu.
28 Na ikawa kwamba baada ya watu wa Koriantumuri kupata nguvu ya kutosha tena

kwamba wangeweza kutembea, walikuwa karibu kukimbia kwa maisha yao; lakini tazama, Shizi aliamka, na pia watu wake, na akaapa kwa ghadhabu yake kwamba angemuua Koriantumuri au sivyo angeuawa kwa upanga.

29 Kwa hivyo, aliwafuata, na kesho yake akawapata; na wakapigana tena kwa upanga. Na ikawa kwamba wote walipokuwa wamekufa, isipokuwa Koriantumuri na Shizi, tazama Shizi alikuwa amezirai kwa kupoteza damu.

30 Na ikawa kwamba wakati Koriantumuri alikuwa amelalia upanga wake, ili apumzike kidogo, alikata kichwa cha Shizi.

31 Na ikawa kwamba baada ya kukata kichwa cha Shizi, kwamba Shizi alijiinua kwa mikono yake na kisha akaanguka; na baada ya kujitahidi kuvuta pumzi, akafa.

32 Na ikawa kwamba Koriantumuri alianguka ardhini, na kuwa kama hana uhai.

33 Na Bwana akamzungumzia Etheri, na kumwambia: Nenda mbele. Na akaenda mbele, na aliona kwamba maneno ya Bwana yalikuwa yote yametimizwa; na akamaliza maandishi yake; (na ile sehemu moja kwa mia sijaandika) na akayaficha kwa njia ambayo watu wa Limhi waliyapata.

34 Sasa maneno ya mwisho ambayo yameandikwa na Etheri ni haya: Kama Bwana anataka kunichukua nikiwa hai, au kama nitavumilia mapenzi ya Bwana kimwili, haijalishi, ikiwa nitaokolewa katika ufalme wa Mungu. Amina.

# Kitabu cha Moroni

## Moroni 1

1 Sasa mimi, Moroni, baada ya kumaliza kufupisha historia ya watu wa Yaredi,
sikudhania kama ningeandika zaidi, lakini bado sijakufa; na sitaki kujionyesha kwa
Walamani wasije wakaniangamiza.
2 Kwani tazama, vita vyao ni vikali sana miongoni mwao wenyewe; na kwa sababu
ya chuki yao wanaua kila Mnefi ambaye hatamkana Kristo.
3 Na mimi, Moroni, sitamkana Kristo; kwa hivyo, ninarandaranda popote
niwezapo kwa usalama wa maisha yangu.
4 Kwa hivyo, ninaandika vitu vingine vichache, kinyume cha kile nilichotarajia;
kwani nilidhani kuwa sitaandika zaidi ya hayo; lakini ninaandika vitu vichache
zaidi, kwamba vingekuwa vya manufaa kwa ndugu zangu, Walamani, katika siku
zijazo, kulingana na mapenzi ya Bwana.

## Moroni 2

1 Maneno ya Kristo, aliyowazungumzia wanafunzi wake, kumi na wawili ambao
alikuwa amewateua, wakati alipowaweka mikono yake juu yao—
2 Na aliwaita kwa majina, akisema: Mtalingana Baba katika jina langu, katika sala
ya nguvu; na baada ya kufanya hivi mtakuwa na uwezo kwamba kwa yule ambaye
mtamwekea mikono yenu, mtampatia Roho Mtakatifu; na katika jina langu mtatoa,
kwani hivyo ndivyo mitume wangu hufanya.
3 Sasa Kristo alisema maneno haya kwao wakati wa kwanza wa kuonekana kwake;
na umati haukusikia, lakini wanafunzi walisikia; na kwa wengi ambao waliwawekea
mikono yao, Roho Mtakatifu aliwashukia.

## Moroni 3

1 Njia ambayo wanafunzi, ambao waliitwa wazee wa kanisa, waliwatawaza makuhani
na walimu—
2 Baada ya wao kuomba kwa Baba katika jina la Kristo, waliwawekea mikono, na
kusema:
3 Katika jina la Yesu Kristo ninakutawaza uwe kuhani (au kama atakuwa mwalimu,
ninakutawaza uwe mwalimu) kuhubiri toba na msamaha wa dhambi kupitia kwa
Yesu Kristo, kwa kuvumilia kwa imani kwa jina lake hadi mwisho. Amina.
4 Na katika njia hii waliwatawaza makuhani na walimu, kulingana na karama na
wito wa Mungu kwa watu; na waliwatawaza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu,
ambaye alikuwa ndani yao.

## Moroni 4

1 Njia ya wazee wao na makuhani wakibariki mwili na damu ya Kristo kwa washiriki;
na waliubariki kulingana na amri za Kristo; kwa hivyo tunajua njia ni ya kweli; na
mzee au kuhani aliibariki—

2 Na walipiga magoti chini na washiriki, na kuomba kwa Baba katika jina la Kristo, wakisema:
3 Ee Mungu, Baba wa Milele, tunakuomba katika jina la Mwanao, Yesu Kristo, ubariki na utakase mkate huu kwa roho za wale wote watakaoula, ili waweze kuula kwa ukumbusho wa mwili wa Mwanao, na wakushuhudie, Ee Mungu, Baba wa Milele, kwamba wako radhi kujichukulia juu yao jina la Mwanao, na daima kumkumbuka, na kushika amri zake ambazo amewapa, ili daima Roho wake apate kuwa pamoja nao. Amina.

## Moroni 5

1 Njia ya kubariki divai — Tazama, walichukua kikombe, na kusema:
2 Ee Mungu, Baba wa Milele, tunakuomba katika jina la Mwanao, Yesu Kristo, ubariki na utakase divai hii kwa roho za wale wote watakaoinywa, ili waweze kufanya kwa ukumbusho wa damu ya Mwanao, ambayo ilimwagwa kwa ajili yao; kwamba washuhudie kwako, Ee Mungu, Baba wa Milele, kwamba wamkumbuke, ili Roho wake apate kuwa pamoja nao. Amina.

## Moroni 6

1 Na sasa ninazungumza kuhusu ubatizo. Tazama, wazee, makuhani, na walimu walibatizwa; na hawangebatizwa kama hawangezaa matunda yapasayo toba.
2 Wala hawakumpokea yeyote kwenye ubatizo kama hangekuja na moyo uliopondeka na roho iliyovunjika, na kushuhudia kwa kanisa kwamba ametubu kwa kweli kutoka kwenye dhambi zao.
3 Na hakuna waliopokewa kwenye batizo isipokuwa wajivike juu yao jina la Kristo na kukata kauli kumtumikia hadi mwisho.
4 Na baada ya hao kupokewa kwenye ubatizo, na kupokelewa na kusafishwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, walihesabiwa miongoni mwa watu wa kanisa la Kristo; na majina yao yalichukuliwa ili wakumbukwe na kulishwa na neno nzuri la Mungu, kuwaweka kwa njia nzuri, kuwaweka waangalifu siku zote kwenye sala, wakitegemea tu katika nguvu ya wokovu wa Kristo, ambaye alikuwa mwanzilishi na mtimizaji wa imani yao.
5 Na washiriki wa kanisa walikutana pamoja mara kwa mara, kufunga na kuomba, na kuzungumza mmoja na mwingine kuhusu ustawi wa nafsi zao.
6 Na walikutana pamoja mara kwa mara kushiriki kwa mkate na divai, katika kumkumbuka Bwana Yesu.
7 Na walikuwa waangalifu kwamba kusiwe na uovu miongoni mwao; na yeyote aliyepatikana akitenda uovu, na mashahidi watatu wa kanisa waliwahukumu mbele ya wazee, na kama hawakutubu, na hawakukiri, majina yao yalitolewa nje, na hawakuhesabiwa miongoni mwa watu wa Kristo.
8 Lakini mara walipotubu na kuuliza msamaha, na kusudi halisi, walisamehewa.
9 Na mikutano yao iliendeshwa na kanisa kulingana na njia ambayo Roho aliwaongoza, na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu; kwani vile uwezo wa Roho Mtakatifu ulivyowaongoza kuhubiri, au kuhimiza, au kuomba, hata hivyo ndivyo ilivyofanywa.

# Moroni 7

1 Na sasa mimi, Moroni, naandika machache ya maneno ya baba yangu Mormoni,
ambayo alisema kuhusu imani, tumaini, na hisani; kwani hii ndiyo njia
aliyozungumza kwa watu, wakati alipowafundisha katika sinagogi ambayo walikuwa
wamejenga kama mahali pa kuabudu.
2 Na sasa mimi, Mormoni, nazumgumza kwenu ndugu zangu wapendwa; na ni
kwa neema ya Mungu Baba, na Bwana wetu Yesu Kristo, na mapenzi yake
matakatifu, kwa sababu ya karama yake kuniita, kwamba nimekubaliwa
kuzungumza kwenu wakati huu.
3 Kwa hivyo, ningewazungumzia wale ambao ni wa kanisa, ambao ni wafuasi wa
imani ya Kristo, ambao wamepata tumaini la kutosha ambalo kwalo mnaweza
kuingia kwenye makao ya Bwana, kutoka wakati huu kwenda mbele mpaka
mtakapopumzika na yeye mbinguni.
4 Na sasa ndugu zangu, nahukumu vitu hivi kwenu kwa sababu ya matembezi yenu
matulivu na watoto wa watu.
5 Kwani nakumbuka neno la Mungu ambalo linasema kwa matunda yao
mtawatambua; kwani kama matunda yao ni mema, basi ni wema pia.
6 Kwani tazama, Mungu amesema mtu akiwa mwovu hawezi kufanya yale ambayo
ni mema; kwani ikiwa atatoa karama, au kuomba kwa Mungu, isipokuwa aifanye
kwa kusudi jema haimfaidii chochote.
7 Kwani tazama, haihesabiwi kwake kwa haki.
8 Kwani tazama, ikiwa mtu mwovu anatoa zawadi, huifanya bila kupenda; kwa
hivyo inahesabiwa kwake sawa kama angeiweka ile zawadi; kwa hivyo anadhaniwa
mwovu mbele ya Mungu.
9 Na kadhalika husahesibiwa pia uovu kwa mtu, ikiwa ataomba bila nia kamili ya
moyo; ndio, na haimfaidii chochote, kwani Mungu hampokei yeyote wa aina hii.
10 Kwa hivyo, mtu akiwa mwovu hawezi kufanya kile ambacho ni chema; wala
hawezi kutoa karama nzuri.
11 Kwani tazama, chimbuko chungu haliwezi kutoa maji mazuri; wala chimbuko
zuri haliwezi kutoa maji chungu; kwa hivyo, mtu akiwa mtumishi wa ibilisi hawezi
akamfuata Kristo; na akiwa anamfuata Kristo hapo hawezi akawa mtumishi wa
ibilisi.
12 Kwa hivyo, vitu vyote vilivyo vizuri vinatoka kwa Mungu; na kile kilicho kiovu
hutoka kwa ibilisi; kwani ibilisi ni adui wa Mungu, na hupigana dhidi yake siku
zote, na hukaribisha na hushawishi kufanya dhambi, na kufanya kile kilicho kiovu
siku zote.
13 Lakini tazama, kile kilicho cha Mungu hukaribisha na hushawishi kufanya mema
siku zote; kwa hivyo, kila kitu kinachokaribisha na kushawishi kufanya mema, na
kumpenda Mungu, na kumtumikia, kinaongozwa na Mungu.
14 Kwa hivyo, muwe waangalifu, ndugu zangu wapendwa, kwamba msione kile
ambacho ni kiovu kuwa cha Mungu, au kile ambacho ni kizuri na cha Mungu kuwa
cha ibilisi.
15 Kwani tazama, ndugu zangu, mmepewa uhuru kuhukumu, kwamba mjue mema
na maovu; na njia ya kuhukumu ni wazi, kwamba mjue na ufahamu kamili, kama
mwangaza wa mchana kutoka kwa giza la usiku.
16 Kwani tazama, Roho ya Kristo imetolewa kwa kila mtu, ili ajue mema na maovu;
kwa hivyo, ninawaonyesha njia ya kuhukumu; kwani kila kitu kinachokaribisha

kufanya mema, na kushawishi kuamini katika Kristo, kinasababishwa na uwezo na
thawabu ya Kristo; kwa hivyo mngejua na ufahamu kamili kwamba ni cha Mungu.
17 Lakini kitu chochote ambacho hushawishi watu kufanya maovu, na kutoamini
katika Kristo, na kumkana, na kutomtumikia Mungu, hapo mtajua na ufahamu
kamili kwamba ni cha ibilisi; kwani kwa njia hii ndiyo ibilisi hufanya kazi, kwani
hamshawishi mtu yeyote kufanya mema, la, sio mmoja; wala malaika wake; wala
wale ambao hujiweka chini yake.
18 Na sasa, ndugu zangu, nikiona kwamba mnajua nuru ambayo kwake mnaweza
kuhukumu, nuru ambayo ni nuru ya Kristo, mhakikishe kwamba hamhukumu kwa
makosa; kwani hukumu ile mnayohukumu nayo ndiyo mtakayohukumiwa.
19 Kwa hivyo, ninawasihi nyinyi, ndugu, kwamba mtafute kwa bidii katika nuru ya
Kristo kwamba mngejua mema na maovu; na ikiwa utashikilia kila kitu kizuri, na
usilaumu, hapo utakuwa bila shaka mtoto wa Kristo.
20 Na sasa, ndugu zangu, inawezekanaje kwamba mshikilie kila kitu kizuri?
21 Na sasa naja kwa ile imani, ambayo nilisema nitaizungumzia; na nitawaambia
njia ambayo kwake mnaweza kushikilia kwa kila kitu kizuri.
22 Kwani tazama, Mungu akijua vitu vyote, akiwa amekuwepo kutoka milele hadi
milele, tazama, alimtuma malaika kuhudumu kwa watoto wa watu, kuwajulisha
kuhusu kuja kwa Kristo; na katika Kristo kutatokea kila kitu kizuri.
23 Na Mungu pia aliwatangazia manabii, kwa mdomo wake mwenyewe, kwamba
Kristo sharti aje.
24 Na tazama, kulikuwa na njia tofauti ambamo kwake alijulisha vitu kwa watoto
wa watu, ambavyo vilikuwa vyema; na vitu vyote ambavyo ni vyema hutoka kwa
Kristo; la sivyo watu wangebaki kwenye hali ya kuanguka, na hakuna kitu chochote
kizuri ambacho kingewajia.
25 Na kwa hivyo, kwa huduma ya malaika, na kwa kila neno litokalo katika kinywa
cha Mungu, watu walianza kutenda imani katika Kristo; na hivyo kwa imani,
walishikilia kila kitu kizuri; na hivi ndivyo ilivyokuwa mpaka kuja kwa Kristo.
26 Na baada ya yeye kuja watu pia waliokolewa kwa imani katika jina lake; na kwa
kupitia kwa imani, wakawa wana wa Mungu. Na kwa kweli kadiri Kristo aishivyo
alisema haya maneno kwa babu zetu, akisema: Kitu chochote mtakachomwuliza
Baba katika jina langu, ambacho ni kizuri, kwa imani mkiamini kwamba mtapata,
tazama, mtakipokea.
27 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, je, miujiza imekoma kwa sababu Kristo
amepanda mbinguni, na ameketi mkono wa kulia wa Mungu, kudai kutoka kwa
Baba haki zake za huruma ambazo anazo juu ya watoto wa watu?
28 Kwani amejibu mwisho wa sheria, na hudai wale wote ambao wana imani ndani
yake; na wale ambao wana imani ndani yake watajishikilia kwa kila kitu kizuri; kwa
hivyo huzungumza akipendelea watoto wa watu; na huishi mbinguni milele.
29 Na kwa sababu amefanya hivi, ndugu zangu wapendwa, je, miujiza imekoma?
Tazama ninawaambia, La; wala malaika hawajakoma kuwahudumia watoto wa
watu.
30 Kwani tazama, wako chini yake, kuhudumu kulingana na neno la amri yake,
wakijidhihirisha kwa wale walio na imani ya nguvu na akili imara katika kila kitu
cha uchamungu.
31 Na kazi ya huduma yao ni kuita watu kwa toba, na kutimiza na kufanya kazi ya
agano la Baba, ambalo amefanya kwa watoto wa watu, kutayarisha njia miongoni

mwa watoto wa watu, kwa kutangaza neno la Kristo kwa vyombo viteule vya Bwana, kwamba wangekuwa na ushahidi kumhusu.

32 Na kwa kufanya hivyo, Bwana Mungu hutayarisha njia kwamba watu wengine wangekuwa na imani katika Kristo, kwamba Roho Mtakatifu angekuwa na mahali katika mioyo yao, kulingana na uwezo alio nao; na kwa njia hii ndiyo Baba hutimiza, maagano ambayo amefanya kwa watoto wa watu.

33 Na Kristo amesema: Ikiwa mtakuwa na imani ndani yangu mtakuwa na uwezo wa kufanya kitu chochote ambacho ni cha kufaa kwangu.

34 Na amesema: Tubuni enyi miisho ya dunia, na mje kwangu, na mbatizwe katika jina langu, na muwe na imani ndani yangu, ili muokolewe.

35 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, ikiwa hivi ndivyo itakuwa kwamba vitu hivi ni kweli ambavyo nimewazungumzia, na Mungu atawaonyesha, kwa uwezo na fahari kuu katika siku ya mwisho, kwamba ni kweli, na ikiwa ni kweli, je, wakati wa miujiza umekoma?

36 Au malaika wamekoma kuonekana kwa watoto wa watu? Au amesimamisha uwezo wa Roho Mtakatifu kutoka kwao? Au atasimamisha, kadiri muda utakapokuwepo au dunia itakapokuwepo, au kutakuwa na mtu mmoja juu ya uso wake kuokolewa?

37 Tazama ninawaambia, La; kwani ni kwa imani kwamba miujiza hufanyika; na ni kwa imani kwamba malaika huonekana na kuhudumia watu; kwa hivyo, kama vitu hivi vimekoma msiba uwe kwa watoto wa watu, kwani ni kwa sababu ya kutoamini, na yote ni bure.

38 Kwani hakuna atakayeokoka, kulingana na maneno ya Kristo, isipokuwa awe na imani katika jina lake; kwani, ikiwa hivi vitu vimekoma, basi imani imekoma pia; na kutisha ni hali ya mtu, kwani ni kama hakujakuwepo na ukombozi uliofanywa.

39 Lakini tazama, ndugu zangu wapendwa, ninaweza kuona vitu vyema zaidi kwenu, kwani ninaona kwamba mna imani katika Kristo kwa sababu ya uvumilivu wenu; kwani kama hamna imani ndani yake hamfai kuhesabiwa miongoni mwa watu wa kanisa lake.

40 Na tena, ndugu zangu wapendwa, ninataka kuwazungumzia kuhusu tumaini. Inawezekanaje kwamba mtafikia imani, isipokuwa muwe na tumaini?

41 Na ni kitu gani mtakachotumainia? Tazama nawaambia kwamba mtakuwa na tumaini kupitia upatanisho wa Kristo na uwezo wa kufufuka kwake, kuinuliwa kwa maisha ya milele, na hii kwa sababu ya imani yenu kwake kulingana na ile ahadi.

42 Kwa hivyo, ikiwa mtu ana imani lazima ahitaji kuwa na tumaini; kwani bila imani hakuwezi kuwepo na tumaini lolote.

43 Na tena, tazama ninawaambia kwamba hawezi kuwa na imani na tumaini, isipokuwa awe mnyenyekevu, na mpole katika moyo.

44 Ikiwa hivyo, imani na tumaini lake ni bure, kwani hakuna yeyote anayekubaliwa mbele ya Mungu, isipokuwa yule aliye myenyekevu na mpole katika moyo; na mtu akiwa myenyekevu na mpole katika moyo, na kukiri kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kwamba Yesu ni Kristo, lazima awe na ahisani; kwani kama hana hisani yeye si kitu; kwa hivyo lazima awe na hisani.

45 Na hisani huvumilia, na ni karimu, na haina wivu, na haijivuni, haitafuti mambo yake, haifutuki kwa upesi, haifikirii mabaya, na haifurahii uovu lakini hufurahi katika ukweli, huvumilia vitu vyote, huamini vitu vyote, hutumaini vitu vyote, hustahamili vitu vyote.

46 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, kama hamna hisani, nyinyi si kitu, kwani
hisani haikosi kufaulu kamwe. Kwa hivyo, ambatana na hisani, ambayo ni kubwa
kuliko yote, kwani vitu vyote lazima vishindwe—
47 Lakini hisani ni upendo msafi wa Kristo, na inavumilia milele; na yeyote
atakayepatikana nayo katika siku ya mwisho, itakuwa vyema kwake.
48 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, ombeni kwa Baba kwa nguvu zote za moyo,
kwamba mjazwe na upendo huu, ambao ametoa kwa wote ambao ni wafuasi wa
kweli wa Mwana wake, Yesu Kristo; ili muwe wana wa Mungu; kwamba wakati
atakapoonekana tutakuwa kama yeye, kwani tutamwona vile alivyo; ili tuwe na
tumaini hili; ili tutakaswe hata vile alivyo mtakatifu. Amina.

## Moroni 8

1 Barua ya baba yangu Mormoni, iliyoandikwa kwangu, Moroni; na iliandikwa
kwangu mara baada nilipoitwa kwa huduma. Na kwa njia hii aliniandikia, akisema:
2 Mwana wangu mpendwa, Moroni, ninafurahi sana kwamba Bwana wako Yesu
Kristo amekuwa mwangalifu kwako, na amekuita kwa huduma yake, na kwa kazi
yake takatifu.
3 Ninakukumbuka wewe kila siku katika sala zangu, siku zote nikisali kwa Mungu
Baba katika jina la Mtoto wake Mtakatifu, Yesu, kwamba yeye, kupitia kwa uzuri
wake na wema usio na mwisho, atakulinda kupitia uvumilivu wa imani kwa jina lake
milele.
4 Na sasa, mwana wangu, ninakuzungumzia kuhusu lile ambalo linanisikitisha
sana; kwani ninasikitishwa kwamba ugomvi unaweza kutokea miongoni mwenu.
5 Kwani, ikiwa nimejulishwa ukweli, kumekuwa na ugomvi miongoni mwenu
kuhusu ubatizo wa watoto wenu wachanga.
6 Na sasa, mwana wangu, ninataka ufanye kazi kwa bidii, ili hili kosa kubwa
litolewe miongoni mwenu; kwani, kwa kusudi hili nimeandika hii barua.
7 Kwani mara moja nilipojua vitu hivi kuwahusu nilimwuliza Bwana kuhusu hili
jambo. Na neno la Bwana lilinijia kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, likisema:
8 Sikiliza maneno ya Kristo, Mkombozi wako, Bwana wako na Mungu wako.
Tazama, nilikuja duniani sio kuwaita walio wa haki bali wenye dhambi kwenye toba;
wenye afya hawahitaji tabibu, bali wale walio wagonjwa; kwa hivyo, watoto
wachanga ni wazima, kwani hawana uwezo wa kutenda dhambi; kwa hivyo laana ya
Adamu imetolewa kwao ndani yangu, kwamba haina uwezo juu yao; na sheria ya
kutahiriwa imeisha kwa ajili yangu.
9 Na katika njia hii Roho Mtakatifu alidhihirisha neno la Mungu kwangu; kwa
hivyo, mwana wangu mpendwa, ninajua kwamba ni mzaha wa unadhiri mbele ya
Mungu, kwamba mbatize watoto wachanga.
10 Tazama ninakwambia kwamba kitu hiki utafundisha—toba na ubatizo kwa wale
ambao wanawajibika wenye uwezo wa kutenda dhambi; ndio, fundisha wazazi
kwamba lazima watubu na wabatizwe, na wajinyenyeze kama watoto wao wachanga.
11 Na watoto wao wachanga hawahitaji toba yoyote, wala ubatizo. Tazama, ubatizo
upo katika toba ili kutimiza amri kwa msamaha wa dhambi.
12 Lakini watoto wachanga ni wazima katika Kristo, hata kutokea mwanzo wa
dunia; ikiwa si hivyo, Mungu ni Mungu wa upendeleo, na pia Mungu wa kugeuka,
na mwenye kupendelea watu; kwani ni watoto wangapi wachanga wamekufa bila

kubatizwa!
13 Kwa hivyo, ikiwa watoto wachanga hawangeweza kuokolewa bila ubatizo, hao
lazima wameenda kwenye jahanamu ya milele.
14 Tazama ninawaambia, yule ambaye anadhani kwamba watoto wachanga
wanahitaji ubatizo yuko kwenye nyongo chungu na katika kifungo cha uovu; kwani
hana imani, wala tumaini, wala hisani; kwa hivyo, ikiwa atakufa kama bado
anafikiria hivyo, ataenda jahanamu.
15 Kwani kutisha ni uovu kudhani kwamba Mungu huokoa mtoto mmoja kwa
sababu ya ubatizo, na mwingine lazima aangamie kwa sababu hakubatizwa.
16 Laana iwe kwa wale ambao wataharibu njia za Bwana kwa utaratibu huu, kwani
wataangamia wasipotubu. Tazama, naongea kwa ujasiri, nikiwa na uwezo kutoka
kwa Mungu; na siogopi kile watu wanachoweza kufanya; kwani upendo ulio kamili
hutupa nje hofu.
17 Na nimejaa na hisani, ambayo ni upendo usio na mwisho; kwa hivyo, watoto
wote ni kama mimi; kwa hivyo, ninapenda watoto wachanga na upendo ulio kamili;
na wote wako sawa na washiriki wa wokovu.
18 Kwani najua kwamba Mungu si Mungu wa kupendelea, wala kiumbe
kinachobadilika; lakini habadiliki kutoka milele hadi milele yote.
19 Watoto wachanga hawawezi kutubu; kwa hivyo, ni uovu wa kutisha kukana
rehema safi ya Mungu kwao, kwani wote ni wazima ndani yake kwa sababu ya
rehema yake.
20 Na yule anayesema kwamba watoto wachanga wanahitaji ubatizo anakana
huruma za Kristo, na huweka bure upatanisho wake na nguvu ya ukombozi wake.
21 Ole kwa hawa, kwani wako katika hatari ya kifo, jahanamu, na maumivu ya
milele. Ninazungumza kwa ujasiri; Mungu ameniamrisha. Yasikilize na uyafuate, au
yatatumiwa kwako kwa kiti cha hukumu cha Kristo.
22 Kwani tazama kwamba watoto wote wachanga ni wazima katika Kristo; na pia
wale wote ambao hawana sheria. Kwani nguvu ya ukombozi huja kwa wote ambao
hawana sheria; kwa hivyo, yule ambaye hahukumiwi, au yule ambaye hayuko chini
ya hukumu yoyote, hawezi kutubu; na kwa hao ubatizo hauleti chochote—
23 Lakini ni mzaha mbele ya Mungu, kukana huruma za Kristo, na nguvu za Roho
Mtakatifu wake, na kuweka tumaini katika kazi zisizo na uhai.
24 Tazama, mwana wangu, kitu hiki kisifanyike; kwani toba ni kwa wale ambao
wako chini ya hukumu na chini ya laana ya sheria iliyovunjwa.
25 Na matokeo ya kwanza ya toba ni ubatizo; na ubatizo huja na imani kwa
kutimiza amri; na kule kutimiza amri huleta kusamehewa kwa dhambi;
26 Na kusamehewa kwa dhambi huleta unyenyekevu, na upole wa moyo; na kwa
sababu ya unyeyekevu na upole wa moyo huja Roho Mtakatifu, Mfariji ambaye
hujaza tumaini na upendo kamili, upendo ambao huvumilia kwa sala ya bidii,
mpaka mwisho utakapokuja, wakati watakatifu wote watakapoishi na Mungu.
27 Tazama, mwana wangu, nitakuandikia tena ikiwa sitaenda nje tena mapema
dhidi ya Walamani. Tazama, kiburi cha taifa hili, au watu wa Wanefi, kimeleta
uangamizo wao isipokuwa watubu.
28 Waombee, mwana wangu, kwamba toba ije kwao. Lakini tazama, ninaogopa
isiwe Roho amekoma kujitahidi nao; na katika sehemu hii ya nchi wanataka kuweka
chini nguvu zote na mamlaka ambayo inatoka kwa Mungu; na wanamkana Roho
Mtakatifu.

29 Na baada ya kukataa elimu kubwa hivyo, mwana wangu, lazima waangamie
karibuni, kwa kutimiza unabii ambao ulizungumzwa na manabii, na pia maneno ya
Mwokozi wetu mwenyewe.
30 Kwaheri, mwana wangu, mpaka nitakapokuandikia, au nitakapokutana nawe
tena. Amina.

*Barua ya pili ya Mormoni kwa mwana wake Moroni.*

# Moroni 9

1 Mwana wangu mpendwa, ninakuandikia tena ili ujue kwamba bado ni mzima;
lakini ninaandika kidogo kwa yale ambayo ni mazito.
2 Kwani tazama, nimekuwa na vita vikali na Walamani, ambavyo hatukushinda; na
Arkeanto ameuawa kwa upanga, na pia Luramu na Emroni; ndio, na tumepoteza
idadi kubwa ya watu wetu wazuri.
3 Na sasa tazama, mwana wangu, ninaogopa kwamba Walamani watawaangamiza
hawa watu; kwani hawatubu, na Shetani anawachochea siku zote kukasirikiana wao
kwa wao.
4 Tazama, ninajaribu kuwafundisha siku zote; na ninaposema neno la Mungu kwa
ukali wanatetemeka na kukasirika dhidi yangu; na nisipotumia ukali wanashupaza
mioyo yao dhidi yake; kwa hivyo, ninaogopa isiwe Roho wa Bwana amekoma
kujitahidi nao.
5 Kwani wamekuwa na hasira sana kwamba inaonekana kwangu kwamba
hawaogopi kifo; na wamepoteza mapenzi yao, mmoja kwa mwingine; na wana kiu
cha damu na kulipiza kisasi siku zote.
6 Na sasa, mwana wangu mpendwa, hata kwa ugumu wao, acha tuwafundishe kwa
bidii; kwani tukikoma kufanya kazi, tungewekwa kwenye laana; kwani tuna kazi ya
kufanya kama tungali kwenye hekalu hili la udongo, kwamba tuweze kumshinda
adui wa haki yote, na kupumzisha nafsi zetu katika ufalme wa Mungu.
7 Na sasa naandika kidogo kuhusu mateso ya hawa watu. Kwani kulingana na
elimu ambayo nimepokea kutoka kwa Amoroni, tazama, Walamani wanao
wafungwa wengi sana, ambao walikamatwa kutoka kwa mnara wa Sheriza; na
kulikuwa na wanaume, wanawake, na watoto.
8 Na waume na baba za wale wanawake na watoto ambao wamewaua; na
wanawalisha wanawake nyama za waume zao, na watoto nyama za baba zao; na
hakuna maji, isipokuwa machache tu, wanayowapatia.
9 Na ijapokuwa haya machukizo makubwa ya Walamani, hayawezi kuzidi yale ya
watu wetu walio Moriantumu. Kwani tazama, wengi wa mabinti za Walamani
wamechukuliwa wafungwa na hao; na baada ya kuwanyang'anya kile ambacho
kilikuwa cha thamani sana kuliko vitu vyote, ambacho ni usafi wa kimwili na
wema—
10 Na baada ya hao kufanya kitu hiki, waliwauwa kwa njia ya kikatili sana, wakitesa
miili yao hata hadi kifo; na baada ya kufanya haya, wanakula miili yao kama
wanyama wa mwitu, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao; na wanaifanya kama
ishara ya ushujaa.

11 Ee mwana wangu mpendwa, inawezekanaje watu kama hawa, ambao hawana ustaarabu—

12 (Na miaka michache tu imepita, tangu wawe wastaarabu na watu wazuri)

13 Lakini Ee mwana wangu, inawezekanaje watu kama hawa, ambao hupendezwa sana na machukizo mengi—

14 Tunawezaje kutumaini kwamba Mungu atajizuia kutoa hukumu yake dhidi yetu?

15 Tazama, moyo wangu unalia: Ole kwa watu hawa. Njoo nje na uwahukumu, Ee Mungu, na ufiche dhambi zao, na uovu, na machukizo kutoka mbele ya uso wako!

16 Na tena, mwana wangu, kuna wajane wengi na mabinti zao ambao wamebaki katika Sheriza; na sehemu ile ya vyakula ambayo Walamani hawakubeba, tazama, jeshi la Zenefi limebeba, na limewaacha kuzunguka kote ambapo wangepata chakula; na wanawake wengi wazee wanazirai na kufia njiani.

17 Na jeshi ambalo liko na mimi ni dhaifu; na majeshi ya Walamani yako katikati ya Sheriza na mimi; na kwa vile wengi walikimbilia jeshi la Haruni wamekuwa madhabuha kwa ukorofi wao wa kutisha.

18 Ee upotovu wa watu wangu! Hawana msimamo na hawana huruma. Tazama, mimi ni mtu tu, na ninazo nguvu tu za mtu, na siwezi tena kulazimisha amri zangu.

19 Na wamejiimarisha kwa upotovu wao; na ni wakorofi sawasawa, bila kuachilia yeyote, si wazee wala vijana; na wanafurahia kila kitu isipokuwa kile ambacho ni kizuri; na kuumia kwa wanawake wetu na watoto wetu juu ya uso wote wa nchi hii kunazidi kila kitu; ndio, ulimi hauwezi kusema, wala haiwezekani kuandikwa.

20 Na sasa, mwana wangu, sitaendelea kueleza hii tamasha ya kuogofya. Tazama, unajua uovu wa hawa watu; unajua kwamba hawana msimamo, na wamekufa ganzi, na uovu wao unazidi ule wa Walamani.

21 Tazama, mwana wangu, siwezi kuwapendekeza kwa Mungu asije akaniua.

22 Lakini tazama, mwana wangu, ninakupendekeza kwa Mungu, na ninaamini katika Kristo kwamba utaokolewa; na ninamwomba Mungu kwamba atakuhurumia maisha yako, kushuhudia kurudi kwa watu wake kwake, au uharibifu wao halisi; kwani najua kwamba lazima waangamie isipokuwa watubu na wamrudie.

23 Na ikiwa wataangamia itakuwa kama ilivyotendeka kwa Wayaredi, kwa sababu ya ukaidi wa mioyo yao, wakitazamia kuua na kulipiza kisasi.

24 Na ikiwa kwamba wataangamia, tunajua kwamba wengi wa ndugu zetu wametoroka na kujiunga na Walamani, na wengi zaidi pia watatorokea kwao; kwa hivyo, uandike vitu vidogo zaidi, ikiwa utaachwa na nife bila kukuona; lakini ninaamini kwamba nitakuona hivi karibuni; kwani ninayo maandishi matakatifu ambayo nitakupatia.

25 Mwana wangu, uwe mwaminifu katika Kristo; na vitu ambavyo nimeandika visikusikitishe, na kukuwekea mzigo wa kukuua; lakini Kristo akuinue juu, na kuumia kwake na kifo chake, na kudhihirisha kwa mwili wake kwa babu zetu, na rehema yake na uvumilivu, na matumaini ya utukufu wake na uzima wa milele, yawe katika akili yako milele.

26 Na ninaomba neema ya Mungu Baba, ambaye kiti chake cha enzi kiko juu mbinguni, na Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye huketi kwenye mkono wake wa kulia wa uwezo wake, mpaka vitu vyote vitakapokuwa chini yake, iwe, na kiishi nawe milele. Amina.

# Moroni 10

1 Sasa mimi, Moroni, naandika machache ambayo naona ni ya kufaa; na ninaandika
kwa ndugu zangu, Walamani; na ningependa kwamba wajue kwamba zaidi ya miaka
mia nne na ishirini imepita tangu ishara ilipotolewa ya kuja kwa Kristo.
2 Na ninaweka muhuri haya maandishi, baada ya kuzungumza maneno machache
kwa njia ya ushauri kwenu.
3 Tazama, ningewashauri kwamba mtakaposoma vitu hivi, ikiwa itakuwa hekima
katika Mungu kwamba myasome, kwamba mngekumbuka jinsi vile Bwana
amekuwa na huruma kwa watoto wa watu, kutokea kuumbwa kwa Adamu hadi
chini mpaka wakati ambapo mtapokea vitu hivi, na kuitafakari katika mioyo yenu.
4 Na mtakapopokea vitu hivi, ningewashauri kwamba mngemwuliza Mungu, Baba
wa Milele, katika jina la Kristo, ikiwa vitu hivi si vya kweli; na ikiwa mtauliza na
moyo wa kweli, na kusudi halisi, mkiwa na imani katika Kristo, atawaonyesha
ukweli wake kwenu, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
5 Na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu mtajua ukweli wa vitu vyote.
6 Na kitu chochote kilicho kizuri ni haki na kweli; kwa hivyo, hakuna chochote
ambacho ni kizuri ambacho humkana Kristo, lakini hukubali kwamba yuko.
7 Na mngejua kwamba yuko, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu; kwa hivyo
ningewashauri kwamba msikatae uwezo wa Mungu; kwani hufanya kazi kwa uwezo,
kulingana na imani ya binadamu, sawa leo na kesho, na milele.
8 Na tena, ninawashauri, ndugu zangu, kwamba msikatae karama za Mungu,
kwani ni nyingi; na zinatoka kwa yule yule Mungu. Na kuna njia tofauti ambazo
hizi karama hutolewa; lakini ni yule yule Mungu azitendaye kazi zote katika wote;
na hupewa kwa ufunuo wa Roho wa Mungu kwa watu, kuwafaidi.
9 Kwani tazama, kwa mmoja inatolewa kwa Roho wa Mungu, kwamba afundishe
neno la hekima;
10 Na kwa mwingine, kwamba afundishe neno la elimu na Roho yule yule;
11 Na kwa mwingine, imani kubwa sana; na kwa mwingine, karama za kuponya na
Roho yule yule;
12 Na tena, kwa mwingine, kwamba aweze kufanya miujiza mikuu;
13 Na tena, kwa mwingine, kwamba aweze kutoa unabii kuhusu vitu vyote;
14 Na tena, kwa mwingine; kuona kwa malaika na kutumikia roho;
15 Na tena, kwa mwingine, lugha za aina zote;
16 Na tena, kwa mwingine, kutafsiri kwa lugha na ndimi za aina tofauti.
17 Na hizi karama zote huja kwa Roho ya Kristo; na huja kwa kila mtu moja kwa
moja, kulingana na vile anavyotaka.
18 Na ningewashauri nyinyi, ndugu zangu wapendwa, kwamba mkumbuke kwamba
kila karama nzuri hutoka kwa Kristo.
19 Na ningewashauri nyinyi, ndugu zangu wapendwa, kwamba mkumbuke kwamba
yeye ndiye yule yule jana, leo, na milele, na kwamba karama hizi zote ambazo
nimezungumzia, ambazo ni za kiroho, hazitatolewa mbali, kadiri dunia
itakavyokuwepo, kulingana tu na kutoamini kwa watoto wa watu.
20 Kwa hivyo, lazima kuwe na imani; na ikiwa kutakuwa na imani lazima kuwe pia
na tumaini; na ikiwa kutakuwa na tumaini lazima kuwe na pia hisani.
21 Na msipokuwa na hisani hamwezi kwa vyovyote kuokolewa katika ufalme wa
Mungu; wala hamwezi kuokolewa katika ufalme wa Mungu kama hamna imani;
wala hamwezi ikiwa hamna tumaini.

22 Na kama hamna tumaini lazima iwe ni kwa kukata tamaa; na kukata tamaa huja kwa sababu ya uovu.

23 Na Kristo kwa kweli alisema kwa babu zetu: Mkiwa na imani mnaweza kufanya vitu vyote ambavyo vinatakikana kwangu.

24 Na sasa ninazungumzia watu wote waliomo duniani—kwamba ikiwa siku itakuja kwamba uwezo na karama za Mungu zitaondolewa kutoka miongoni mwenu, itakuwa ni kwa sababu ya kutoamini.

25 Na ole kwa watoto wa watu ikiwa itakuwa hivyo; kwani hakutakuwa yeyote ambaye hufanya mema miongoni mwenu, la hata mmoja. Kwani ikiwa kuna mmoja miongoni mwenu ambaye hufanya mema, atafanya kwa uwezo na karama za Mungu.

26 Na ole kwa hao ambao watatoa vitu hivi na kufa, kwani wanakufa katika dhambi zao, na hawawezi kuokolewa katika ufalme wa Mungu; na ninaizungumzia kulingana na maneno ya Kristo; na sidanganyi.

27 Na ninawashauri mkumbuke vitu hivi; kwani wakati unafika haraka kwamba mtajua kwamba sidanganyi, kwani mtaniona katika kiti cha hukumu cha Mungu; na Bwana Mungu atasema kwenu: Je, si mimi nilitangaza maneno yangu kwenu, ambayo yaliandikwa na mtu huyu, kama mmoja anayelia kutoka kwa wafu, ndio, hata kama mmoja asemaye kutoka mavumbini?

28 Ninatangaza vitu hivi kwa kutimiza unabii. Na tazama, yatatoka nje ya mdomo wa Mungu asiye na mwisho; na neno lake litaenda mbele kutoka kwa kizazi hadi kingine.

29 Na Mungu atawaonyesha, kwamba yale ambayo nimeandika ni ya kweli.

30 Na tena ninawashauri kwamba mngekuja kwa Kristo, na kushikilia juu ya kila karama nzuri, na msiguse ile karama mbovu, wala kitu kichafu.

31 Na amka, na kutoka kwenye mavumbi, Ee Yerusalemu; ndio, na ujivike mavazi ya kurembesha, Ee binti wa Sayuni; na imarisha vigingi vyako na ongeza mipaka yako milele, kwamba hutachanganywa tena, kwamba agano la Baba wa milele ambalo amefanya kwako, Ee nyumba ya Israeli, liwezekane kutimizwa.

32 Ndio, mje kwa Kristo na mkamilishwe ndani yake, na mjinyime ubaya wote; na ikiwa mtajinyima ubaya wote, na kumpenda Mungu na mioyo yenu, akili na nguvu zenu zote, basi neema yake inawatosha, kwamba kwa neema yake mngekamilishwa katika Kristo; na ikiwa kwa neema ya Mungu mnakamilika katika Kristo, hamwezi kwa njia yoyote kukana uwezo wa Mungu.

33 Na tena, ikiwa nyinyi kwa neema ya Mungu ni kamili katika Kristo, na hamkani uwezo wake, ndipo mmetakaswa katika Kristo kwa neema ya Mungu, kupitia kwa upatanisho wa Kristo, ambayo ni agano la Baba kwa kusamehewa kwa dhambi zenu, kwamba muwe watakatifu, bila waa.

34 Na sasa ninasema kwenu nyote, kwa herini. Hivi karibuni nitaenda kupumzika katika pepoy ya Mungu, mpaka roho yangu na mwili vitakapounganishwa tena, na niinuliwe juu kwa ushindi kupitia angani, kukutana na nyinyi mbele ya kiti cha enzi cha kupendeza cha yule Yehova mkuu, Mwamuzi wa Milele wa wanaoishi na waliokufa. Amina.

Mwisho